# Tumaini la Vizazi Vyote

**Pambano la Vizazi kama Lilivyodhihirishwa katika Maisha ya Kristo**

Mwandishi: Ellen Gould White

Tafsiri ya Kiswahili ya *The Desire of Ages (DA)*

ya mwaka 1898

2016

**Maneno ya Mtafsiri**

Tafsiri hii ya Kiswahili inayoitwa *Tumaini la Vizazi Vyote* imepatikana kutoka katika toleo la Kingereza linaloitwa *The Desire of Ages* ili kuweza kuwapatia wasomaji wa Kiswahili ujumbe unaofanana au kukaribiana sana na ule uliomo katika toleo la Kingereza. Imekuwa vigumu kutumia maneno sahihi ya Kiswahili ili kumaanisha Desire of Ages, ambayo yanaleta maana kama vile “Tamanio la Vizazi” au “Hamu ya Vizazi” au “Hitaji la Vizazi” au “Takwa la Vizazi”. Hata maneno yenyewe ya Dibaji ya mtunzi wa kitabu yanaonyesha jambo hilo. Hata hivyo, mtafiri ametumia jina *Tumaini la Vizazi Vyote* kwa sababu ndilo lililozoeleka kwa muda mrefu na tena linabeba ujumbe mzuri vile vile na unaofaa.

Kusudi lenyewe la kufanya kazi hii ya kutafsiri lilikuwa ni kupata toleo la Kiswahili ambalo lingefaa kwa matumizi ya familia. Lakini, kwa sababu ya uzuri na ukamilifu wake kwa kulinganishwa na toleo la Kiswahili lililopo, toleo hili linawafaa wasomaji wengine wowote ambao wanapenda kupata ujumbe ule unaopatikana kwa wasomaji wa lugha ya Kingereza.

Katika toleo hili, kurasa rasmi zinazotumika kwa ajili ya rejea za kitabu cha *The Desire of Ages* zimeonyeshwa kwa tarakimu zilizo katika mabano na kukolezwa wino. Kwa hiyo mtumiaji wa toleo hili anaweza kufuatilia nukuu yoyote kwa kuzingatia kurasa hizo.

Namshukuru sana Mungu kwa kuniwezesha kukamilisha kazi hii. Ni matumaini yangu kwamba tafsiri hii itawafaa na kuwabariki watu.

Onesmo Emmanuel

# Yaliyomo


| | |
|---|---|
| DIBAJI | 7 |
| Sura ya 1 | 9 |
| "Mungu Pamoja Nasi" | 9 |
| Sura ya 2 | 13 |
| Watu Waliochaguliwa | 13 |
| Sura ya 3 | 15 |
| "Utimilifu wa Wakati" | 15 |
| Sura ya 4 | 18 |
| Mwokozi kwa Ajili Yenu | 18 |
| Sura ya 5 | 21 |
| Kuwekwa Wakfu | 21 |
| Sura ya 6 | 25 |
| "Tumeiona Nyota Yake" | 25 |
| Sura ya 7 | 29 |
| Akiwa Mtoto | 29 |
| Sura ya 8 | 33 |
| Kuhudhuria Pasaka | 33 |
| Sura ya 9 | 37 |
| Siku za Mgongano | 37 |
| Sura ya 10 | 41 |
| Sauti Nyikani | 41 |
| Sura ya 11 | 47 |
| Ubatizo | 47 |
| Sura ya 12 | 50 |
| Kujaribiwa | 50 |
| Sura ya 13 | 56 |
| Ushindi | 56 |
| Sura ya 14 | 59 |
| "Tumemwona Masihi" | 59 |
| Sura ya 15 | 65 |
| Kwenye Sherehe ya Arusi | 65 |
| Sura ya 16 | 70 |
| Katika Hekalu Lake | 70 |
| Sura ya 17 | 76 |
| Nikodemo | 76 |
| Sura ya 18 | 81 |
| "Yeye Hana Budi Kuzidi" | 81 |
| Sura ya 19 | 84 |
| Penye Kisima cha Yakobo | 84 |
| Sura ya 20 | 90 |
| "Msipoona Ishara na Maajabu" | 90 |
| Sura ya 21 | 93 |
| Bethzatha na Sanhedrin | 93 |
| Sura ya 22 | 101 |
| Kifungo na Kifo cha Yohana | 101 |
| Sura ya 23 | 108 |
| "Ufalme wa Mungu Umekaribia" | 108 |
| Sura ya 24 | 111 |
| "Huyu Si Mwana wa Seremala?" | 111 |
| Sura ya 25 | 115 |

Wito Kando ya Bahari 115
Sura ya 26 119
Kule Kapernaumu 119
Sura ya 27 125
"Waweza Kunitakasa" 125
Sura ya 28 131
Lawi - Mathayo 131
Sura ya 29 136
Sabato 136
Sura ya 30 141
"Akaweka Watu Kumi Na Wawili" 141
Sura ya 31 145
Hotuba ya Mlimani 145
Sura ya 32 154
Akida 154
Sura ya 33 157
Ndugu Zangu ni Akina Nani? 157
Sura ya 34 161
Mwaliko 161
Sura ya 35 164
"Nyamaza, Utulie" 164
Sura ya 36 169
Mguso wa Imani 169
Wainjilisti wa Kwanza 172
Sura ya 38 178
Njoni Mkapumzike Kidogo 178
Sura ya 39 181
"Wapeni Ninyi Chakula" 181
Sura ya 40 185
Usiku Ziwani 185
Sura ya 41 189
Wakati Mgumu Kule Galilaya 189
Sura ya 42 196
Mapokeo 196
Sura ya 43 199
Vikwazo Viletavyo Ubaguzi Vyavunjwa 199
Sura ya 44 202
Ishara ya Kweli 202
Sura ya 45 206
Kuonyesha Kivuli cha Msalaba 206
Sura ya 46 211
Alibadilika Sura 211
Sura ya 47 214
Huduma 214
Sura ya 48 217
Nani Aliye Mkuu? 217
Sura ya 49 223
Kwenye Sikukuu ya Vibanda 223
Sura ya 50 227
Katikati ya Mitego 227
Sura ya 51 232
"Nuru ya Uzima" 232

| | |
|---|---|
| Sura ya 52 | 239 |
| Mchungaji wa Kimbingu | 239 |
| Sura ya 53 | 243 |
| Safari ya Mwisho Kutoka Galilaya | 243 |
| Sura ya 54 | 249 |
| Msamaria Mwema | 249 |
| Sura ya 55 | 253 |
| Si kwa Mwonekano wa Nje | 253 |
| Sura ya 56 | 256 |
| Kuwabariki Watoto | 256 |
| Sura ya 57 | 259 |
| "Umepungukiwa na Neno Moja" | 259 |
| Sura ya 58 | 262 |
| "Lazaro, Njoo Huku Nje" | 262 |
| Sura ya 59 | 269 |
| Njama za Makuhani | 269 |
| Sura ya 60 | 272 |
| Sheria ya Ufalme Mpya | 272 |
| Sura ya 61 | 275 |
| Zakayo | 275 |
| Sura ya 62 | 278 |
| Karamu Nyumbani kwa Simoni | 278 |
| Sura ya 63 | 284 |
| "Mfalme Wako Anakuja" | 284 |
| Watu Walio katika Hukumu ya Kuangamia | 289 |
| Sura ya 65 | 293 |
| Hekalu Latakaswa Tena | 293 |
| Sura ya 66 | 300 |
| Makabiliano | 300 |
| Sura ya 67 | 305 |
| Ole kwa Mafarisayo | 305 |
| Sura ya 68 | 311 |
| Katika Uwanja wa Nje | 311 |
| Sura ya 69 | 315 |
| Kwenye Mlima wa Mizeituni | 315 |
| Sura ya 70 | 320 |
| "Hao Ndugu Zangu Walio Wadogo" | 320 |
| Sura ya 71 | 323 |
| Mtumishi wa Watumishi | 323 |
| Sura ya 72 | 328 |
| "Kwa Ukumbusho Wangu" | 328 |
| Sura ya 73 | 333 |
| "Msifadhaike Mioyoni Mwenu" | 333 |
| Sura ya 74 | 343 |
| Gethsemane | 343 |
| Sura ya 75 | 349 |
| Mbele ya Anasi na Behewani kwa Kayafa | 349 |
| Sura ya 76 | 357 |
| Yuda | 357 |
| Sura ya 77 | 361 |
| Katika Ukumbi wa Hukumu wa Pilato | 361 |
| Sura ya 78 | 371 |

Kalvari 371
Sura ya 79 380
"Imekwisha" 380
Sura ya 80 384
Katika Kaburi la Yusufu 384
Sura ya 81 390
"Bwana Amefufuka" 390
Sura ya 82 394
"Unalilia Nini?" 394
Sura ya 83 397
Njiani Kwenda Emau 397
Sura ya 84 400
"Amani Iwe Kwenu" 400
Sura 85 403
Kando ya Bahari Tena 403
Sura ya 86 407
Mkawafanye Mataifa Yote Kuwa Wanafunzi 407
Sura ya 87 414
"Kwa Baba Yangu, Naye Ni Baba Yenu" 414

# DIBAJI

Katika mioyo ya wanadamu wote, wa jamii yoyote ile au wa mahali popote, kuna hali isiyo bayana ya kutamani kitu fulani ambacho hawana kwa wakati huo. Mungu mwenye rehema ameipandikiza hali hiyo ndani ya mwanadamu, ili kwamba mwanadamu asitoshelezwe na hali iliyopo sasa au na vile alivyokwisha kupata, viwe vyema, vibaya, au vizuri zaidi. Mungu anatarajia kwamba mwanadamu atafute kilicho kizuri zaidi, na kukipata katika vina vya baraka iliyo ndani yake.

Shetani, kwa mbinu mbaya na ustadi, amepindisha hali hiyo ya moyo wa mwanadamu. Anawafanya watu waamini kwamba hamu hiyo ya moyo inaweza kukidhiwa kwa anasa, na utajiri, na starehe, na umaarufu, na uwezo; lakini wale ambao wamedanganywa naye hivyo (na ni wengi kwa idadi yao) hujikuta kwamba hivi vyote vinaelekea katika kukidhi hisia, vikimwacha mtu akiwa mtupu pasipo kutosheka kama vile vile alivyokuwa kabla.

Ni mpango wa Mungu kwamba hamu hii ya moyo wa mwanadamu imwelekeze kwake Yeye ambaye peke yake aweza kutosheleza. Hamu hiyo ya ndani ni yake Yeye ili ielekeze watu kwake Yeye, aliye utimilizaji na utoshelezo wa hamu hiyo. Utimilizaji huo unapatikana katika Yesu Kristo, Mwana wa Mungu wa Milele. "Kwa kuwa katika Yeye ilimpendeza Baba kwamba utimilifu wote ukae;" "maana katika Yeye unakaa utimilifu wote wa Mungu, kwa jinsi ya kimwili." Na ni kweli pia kwamba "na ninyi mmetimilika katika Yeye" mkiwa katika kila hamu ambayo ilipandikizwa na Mungu na kwa kawaida hufuatwa.

Hagai anamwita Huyo kuwa ni tamanio la mataifa yote, na tunaweza tukamwita "Tumaini la vizazi vyote," na kama alivyo "Mfalme wa vizazi."

Ni kusudi la kitabu hiki kumweka wazi Yesu Kristo kama Yeye ambaye ndani yake kila hamu inaweza kutoshelezwa. "Maisha ya Kristo" mengi yameandikwa, vitabu vizuri sana, habari nyingi, maandishi mengi kuhusu nasaba na historia, desturi, na matukio, pamoja na mengi ya mafundisho na mitazamo tofauti ya maisha ya Yesu wa Nazareti. Lakini inaweza kusemwa kwa kweli kwamba hata "nusu haijatangazwa."

Hata hivyo, si kusudi la kitabu hiki kuleta ulinganifu wa Injili, au hata kuonyesha mpangilio wa kufuatana kwa matukio muhimu na masomo ya ajabu ya maisha ya Kristo; lengo lake ni kuuonyesha upendo wa Mungu kama ulivyofunuliwa katika Mwana wake, uzuri wa kiungu wa maisha ya Kristo, ambayo wote wanaweza kushiriki, na siyo kutimiza hamu tu ya kutaka kujua au ya kuhoji na kukosoa. Lakini hata kwa mvuto wa wema wake wa tabia, Yesu aliwavuta wanafunzi kwake, na kwa uwepo wake halisi, kwa hisia zake na mguso wa huruma katika mahitaji na unyonge wao wote, na kwa kujihusianisha nao kwa muda wote, alibadilisha tabia zao kutoka zile za kidunia na kuwa za kimbingu, kutoka kuwa za kibinafsi na kuwa za kujitoa, kutoka kuwa na ujinga wa hofu na mambo ya uongo na kuwa ufahamu wenye ujasiri na upendo wa kina kwa watu wa kabila na lugha zote, ambapo kusudi la kitabu hiki ndilo hilo la kumdhihirisha Mkombozi mbarikiwa na kumsaidia msomaji kuja kwake uso kwa uso, moyo kwa moyo, na kumpata ndani yake, kama ilivyokuwa kwa wanafunzi wale, Yesu Mwenye Nguvu, aokoaye mpaka ndani, na kuwabadilisha wale wote wanaokuja kwa Mungu kupitia kwake kuwafanya kuwa na sura yake ya kimbingu. Lakini ni kiasi gani bado haiwezekani kufunua maisha yake! Ni kama kujaribu kuweka upinde hai wa mvua kwenye hema; kwa tabia zake za weusi na weupe ni muziki mtamu kuliko yote.

Katika kurasa zifuatazo, mwandishi, mwanamke mwenye uzoefu mpana, wa kina na wa muda mrefu katika mambo ya Mungu, ameweka wazi uzuri mpya utokanao na maisha ya Yesu. Ameleta tunu mpya nyingi kutoka katika sanduku la thamani. Anafungua machoni pa msomaji utajiri asioota mtu bado kutoka katika nyumba hii ya hazina isiyo kikomo. Nuru mpya na tukufu inamlikia njia ya wengi, kwa kina ambacho msomaji anaona kama hakijawahi kupimika kabla. Kusema kwa ufupi, Yesu Kristo anafunuliwa kama utimilifu wa Uungu, Mwokozi wa wadhambi mwenye rehema asiye na kikomo, Jua la Haki, Kuhani Mkuu mwenye rehema, Mponyaji wa maradhi na magonjwa yote ya wanadamu, Rafiki mpole na mwenye huruma, Rafiki mwenye msaada aliyepo wakati wote, Mfalme wa Nyumba ya Daudi, Kinga ya watu wake, Mfalme wa Amani, Mfalme Ajaye, Baba wa Milele, aletaye vileleni na kukamilisha hamu na matumaini ya vizazi vyote.

Chini ya baraka za Mungu kitabu hiki kimetolewa kwa ulimwengu kwa kuomba kwamba Bwana kwa Roho wake atayafanya maneno ya kitabu hiki kuwa maneno ya uzima kwa watu wengi ambao hamu yao na hitaji lao halijakidhiwa bado; ya kwamba wapate kumjua "Yeye, na uweza wa kufufuka kwake, na ushirika wa mateso yake," na hatimaye, katika baraka ile ya milele zote, katika mkono wake wa kuume, washiriki katika "ule utimilifu wa furaha," na "raha ya milele na milele," ambavyo vitakuwa matunda yaliyoiva ya wale wote wanaotafuta ndani yake mambo yote katika yote, "aliye Mkuu wa maelfu kumi," na "Yeye mwenye upendo wote."

## Sura ya 1

# "Mungu Pamoja Nasi"

"Nao watamwita jina lake Imanueli, . . . Mungu pamoja nasi." "Nuru ya kujua utukufu wa Mungu" inaonekana "katika uso wake Yesu Kristo." Tangu milele na milele Bwana Yesu Kristo alikuwa katika umoja na Baba; alikuwa "sura yake Mungu," sura ya ukuu na uweza wake, "mng'ao wa utukufu wake." Alikuja katika ulimwengu wetu ili kudhihirisha utukufu huo. Alikuja katika dunia hii ya giza kuifunua nuru ya upendo wa Mungu, - alikuja kuwa "Mungu pamoja nasi." Kwa hiyo kuhusu Yeye ilitabiriwa kwamba, "Atamwita Jina lake Imanueli."

Kwa kule kuja kuishi kati yetu, Yesu alikuwa amfunue Mungu kwa wanadamu na kwa malaika. Alikuwa Neno la Mungu – ni mawazo ya Mungu yaliyofanywa yawe ya kusikika. Katika sala yake kwa ajili ya wanafunzi wake alisema, "Nimewadhihirishia jina lako," - "mwingi wa huruma, mwenye fadhili, si mwepesi wa hasira, mwingi wa rehema na kweli," - "ili pendo lile ulilonipenda mimi liwe ndani yao, nami niwe ndani yao." Lakini ufunuo huu haukutolewa kwa ajili ya watoto wake waliozaliwa katika dunia hii tu. Ulimwengu wetu mdogo ni kitabu cha malimwengu mengine kujifunzia. Kusudi la Mungu la kushangaza la neema, siri ya upendo wa ukombozi, ni mada ambayo kwayo "malaika wanatamani kuyachungulia," na itakuwa mada ya wao kujifunza katika vizazi visivyokoma. Waliokombolewa **(20)** na viumbe ambavyo havikuanguka watapata sayansi yao na wimbo wao katika msalaba. Itadhihirika kwamba utukufu unaong'aa usoni pa Yesu ni utukufu wa upendo wa kujitoa. Katika nuru itokayo Kalvari itaonekana kwamba sheria ya upendo wa kujikana ni sheria ya maisha ya duniani na mbinguni; kwamba asili ya upendo ule ambao "hautafuti mambo yake" iko katika moyo wa Mungu; na ya kwamba katika Yeye aliye mpole na mnyenyekevu inadhihirishwa tabia yake Yeye akaaye katika nuru ambayo hakuna mtu awezaye kuikaribia.

Hapo mwanzo, Mungu alifunuliwa katika kazi zote za uumbaji. Ni Kristo aliyetandaza mbingu hizi, na aliweka msingi wa dunia. Ni mkono wake ulioning'iza malimwengu angani, na kuyapamba maua ya kondeni. "Milima aliiweka imara kwa nguvu zake." Zaburi 65:6; 95:5. Ni Yeye aliyeijaza dunia kwa uzuri, na anga kwa wimbo. Na akaandika ujumbe wa pendo la Baba kwenye vitu vyote vilivyo duniani, hewani, na angani.

Sasa dhambi imeharibu kazi kamilifu ya Mungu, lakini hayo maandishi yake bado yapo. Mpaka sasa vyote vilivyoumbwa vinatangaza uzuri wake. Hakuna hata kimoja kinachoishi kwa ajili ya chenyewe, isipokuwa moyo wa ubinafsi wa mwanadamu. Hakuna ndege arukaye hewani, au mnyama atembeaye kwenye nchi, bila kuwa mhudumu kwa maisha ya vitu vingine. Hakuna jani la mti msituni, au jani la chini la unyasi, ambalo halina huduma kwa vitu vingine. Kila mti na kichaka na jani linaleta hali hiyo ya maisha ambayo pasipo hiyo hakuna mwanadamu au mnyama ambaye angeishi; na mtu na mnyama, kwa upande mwingine, wanahudumia maisha ya mti, kichaka na jani. Maua yanapumua harufu nzuri na yanachanua uzuri wake kama baraka **(21)** kwa ulimwengu. Jua linaangaza mwanga wake na kufurahisha maelfu ya malimwengu. Bahari, yenyewe ikiwa chanzo cha chemchemi zote na bubujiko la maji, inapokea mito kutoka kote katika nchi, lakini inapokea ili kutoa. Mvuke upandao juu kutoka humo hushuka kama matone ya maji na kuinywesha nchi, ili iweze kuchipusha na kuzaa.

Malaika wa utukufu hupata furaha yao katika kutoa – wakitoa upendo na ulinzi usiochoka kwa nafsi ambazo zilianguka na zisizokuwa takatifu. Viumbe hawa wa mbinguni wanaibembeleza mioyo ya watu; wanauletea ulimwengu huu wa giza nuru kutoka juu; kwa huduma ya upole na uvumilivu wanatembelea roho ya mwanadamu, kumleta aliyepotea katika ushirika wa pamoja na Kristo ambao uko karibu kuliko hata wanavyoweza kujua.

Tukiacha viwakilishi hivyo vyote vidogo, tunamwona Mungu ndani ya Yesu. Tukimwangalia Yesu tunaona kwamba Yeye ni utukufu wa Mungu wa kutoa. "Sifanyi neno kwa nafsi yangu;" ndivyo alivyosema Yesu, "Baba aliye hai alivyonituma mimi, nami ni hai kwa Baba." "Siutafuti utukufu wangu," bali wake Yeye aliyenituma. Yohana 8:28; 6:57; 8:50; 7:18. Katika maneno haya kumeonyeshwa kanuni kuu ambayo ni sheria ya maisha katika malimwengu yote. Kristo alipokea vitu vyote kutoka kwa Mungu, lakini alipokea ili kutoa. Kwa hiyo katika makao ya mbinguni, katika huduma yake kwa viumbe vyote; kupitia Mwana mpendwa, maisha ya Baba yanatiririka kwenda kwa wote; kupitia kwa Mwana yanarudi, yakiwa katika sifa na utumishi wa raha, kama

wimbi la upendo, yakirudi kwake Yeye aliye Chanzo cha yote. Na kwa hiyo kupitia Kristo mzunguko wa wema umekamilika, ukiwakilisha tabia ya Mtoaji mkuu, ndiyo sheria ya maisha.

Kule mbinguni ndiko sheria hii ilikovunjiwa. Dhambi iliibuka katika kutafuta ubinafsi. Lusifa, kerubi afunikaye, alitamani kuwa wa kwanza mbinguni. Alitafuta kupata kutawala viumbe wa mbinguni, kuwapeleka mbali na Muumba wao, na kutafuta kupata heshima yao. Kwa hiyo alimwonyesha Mungu kwao isivyo sahihi, **(22)** akimhusisha na tamaa ya kujiinua binafsi. Alitafuta kuzihamishia tabia zake ovu kwa Muumba mwenye upendo. Hivyo akawadanganya malaika. Hivyo ndivyo alivyowadanganya wanadamu. Aliwaongoza kutilia shaka neno la Mungu, na kuacha kuamini wema wake. Kwa kuwa Mungu ni Mungu wa haki na uweza wa kutisha, Shetani aliwasababisha kumwona Mungu kama katili na asiyesamehe. Hivyo akawavuta watu kuungana naye katika uasi wa kumpinga Mungu, na usiku wa ole ukaufunika ulimwengu.

Dunia ilikuwa gizani kwa sababu ya kutomwelewa Mungu. Ili kivuli cha huzuni kiangaziwe nuru, ili ulimwengu urudishwe kwa Mungu, nguvu ya Shetani ya madanganyo ilikuwa haina budi kuvunjwa. Jambo hili lisingefanyika kwa mabavu. Matumizi ya mabavu ni kinyume na kanuni ya serikali ya Mungu; anatamani huduma ya upendo; na upendo hauwezi kuamrishwa; hauwezi kupatikana kwa kulazimisha au kwa kutumia mabavu. Upendo huamshwa na upendo tu. Kumjua Mungu ni kumpenda; lazima tabia yake idhihirike kwa kuonekana ikiwa tofauti na tabia ile ya Shetani. Kazi hii ingewezekana kufanywa na Mmoja tu katika malimwengu yote. Ni Yule tu anayejua kimo na kina cha upendo wa Mungu ambaye angeufanya upendo huo ujulikane. Lazima juu ya usiku wa giza wa ulimwengu Jua la Haki litokeze, likiwa "lenye kuponya katika mbawa zake." Malaki 4:2.

Mpango wa ukombozi wetu si wazo lililokuja tu baadaye, eti ukiwa mpango uliowekwa baada ya anguko la Adamu. Ulikuwa ni ufunuo wa “ile siri iliyositirika tangu zamani za milele." Warumi 16:25. Ulikuwa ni ufunuo wa kanuni ambayo imekuwa msingi wa kiti cha enzi cha Mungu milele zote. Tangu mwanzo, Mungu na Kristo walijua kuhusu kuasi kutakakotokea kwa Shetani, na anguko la mwanadamu kwa sababu ya nguvu ya madanganyo ya mwasi huyo. Mungu hakukubali kwamba dhambi iwepo, lakini aliona kwa mbali kwamba itakuwepo, na akaweka utaratibu wa namna ya kukabiliana na tishio la kuibuka kwa dhambi hiyo. Upendo wake kwa ulimwengu ulikuwa mkubwa sana, kiasi kwamba aliweka agano la kumtoa Mwana wake wa pekee, "ili kwamba kila amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele." Yohana 3:16.

Lusifa alikuwa amesema, "Nitakiinua kiti changu cha enzi juu ya nyota za Mungu; . . . Nitakuwa kama Aliye Juu." Isaya 14:13, 14. Lakini Kristo, "ambaye yeye mwanzo alikuwa yuna namna ya Mungu, naye hakuona kule kuwa sawa na Mungu kuwa ni kitu cha kushikamana nacho; bali alijifanya kuwa hana utukufu, akatwaa namna ya mtumwa, akawa ana mfano wa wanadamu." Wafilipi 2:6, 7.

Hii ilikuwa dhabihu ya hiari. Yesu angeweza kubaki karibu na Baba. Angeweza kubaki na utukufu wake wa mbinguni, na heshima kutoka kwa malaika. Lakini alichagua kuirudisha fimbo ya kifalme **(23)** mkononi mwa Baba, na kushuka chini kutoka katika kiti cha enzi kitawalacho malimwengu yote, kusudi alete nuru kwa walio gizani, na uzima kwa wanaoangamia.

Kadiri ya miaka elfu mbili iliyopita, sauti muhimu ya ajabu ilisikika mbinguni, kutoka katika kiti cha enzi cha Mungu, ikisema, "Tazama nakuja.” “Dhabihu na toleo hukutaka, Lakini mwili uliniwekea tayari;. . . Tazama, nimekuja (katika gombo la chuo nimeandikiwa) Niyafanye mapenzi yako, Mungu." Waebrania 10:5-7. Katika maneno haya unatangazwa utimilifu wa kusudi lililokuwa limefichwa tangu milele na milele. Kristo alikuwa anataka kuutembelea ulimwengu wetu, na kuwa katika mwili. Anasema, "Mwili uliniwekea tayari." Ikiwa angejitokeza akiwa katika utukufu ule uliokuwa wake alipokuwa na Baba kabla ya ulimwengu kuweko, tusingeistahimili nuru ya uwepo wake. Ili tuweze kuuona na kubaki bila kuangamizwa, mwonekano wa utukufu wake ulifunikwa. Uungu wake ulifunikwa na pazia la ubinadamu, - utukufu usioonekana katika umbo la mwanadamu linaloonekana.

Mpango huu ulikuwa umeonyeshwa katika vivuli vya vielelezo na ishara. Kichaka kiwakacho moto, ambamo Kristo alimtokea Musa, kilimfunua Mungu. Alama iliyochaguliwa kuwakilisha Uungu ilikuwa kichaka hafifu, kilichoonekana kama hakivutii. Hiki kilimzunguka Mwenye Uwezo wote. Mungu mwenye rehema zote aliuficha utukufu wake katika kielelezo cha hali ya chini mno, kiasi kwamba Musa aliweza kukiangalia na akaishi. Vivyo hivyo katika nguzo ya wingu wakati wa mchana na nguzo ya moto wakati wa usiku, Mungu alifanya mawasiliano

na Israeli, akifunua mapenzi yake kwa wanadamu, na akiwafundisha neema yake. Utukufu wa Mungu ulishushwa, na ukuu wake ukafunikwa, kusudi macho ya wanadamu wa kufa yaweze kuutazama. Kwa hiyo Kristo alikuwa aje katika "mwili wa unyonge" (Wafilipi 3:21), "akawa ana mfano wa wanadamu." Katika macho ya ulimwengu hakuwa na uzuri hata atamanike; lakini alikuwa Mungu katika mwili, nuru ya mbingu na dunia. Utukufu wake ulifunikwa, ukuu na uweza wake vilifichwa, kusudi aweze kusogea karibu na wanadamu wenye majonzi walioanguka.

Mungu alimwamuru Musa kwa ajili ya Israeli kwamba, "Na wanifanyie patakatifu; nipate kukaa kati yao" (Kutoka 25:8), na alikaa katika patakatifu, katikati ya watu wake. Katika kuhangaika kote jangwani, alama ya uwepo wake ilikuwa pamoja nao. Kwa hiyo Kristo aliweka makao yake katikati ya makazi yetu wanadamu. Alisimika hema lake pembeni tu mwa mahema ya wanadamu, ili akae miongoni mwetu, na kutufanya tupambanue tabia na maisha yake ya kiungu. "Neno alifanyika mwili, na akakaa kwetu (nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa **(24)** Mwana pekee wa Baba), amejaa neema na kweli." Yohana 1:14.

Kwa kuwa Yesu alikuja kukaa nasi, tunajua kwamba Mungu anafahamu majaribu yetu, na anatuonea huruma katika shida zetu. Kila mwana na binti wa Adamu ajue kwamba Muumba wetu ni rafiki wa wenye dhambi. Maana katika kila fundisho la neema, kila ahadi ya raha, kila tendo la upendo, kila mvuto wa kimbingu ulioonyeshwa katika maisha ya Mwokozi alipokuwa duniani, tunamwona "Mungu pamoja nasi."

Shetani huionyesha sheria ya Mungu ya upendo kama sheria ya ubinafsi. Anadai kwamba ni jambo lisilowezekana kwetu kuzitii. Anasukumia kwa Muumba lawama ya anguko la wazazi wetu wa kwanza, pamoja na ole ambazo zimetokana na anguko hilo, akiwafanya watu wamwone Mungu kama mwasisi wa dhambi, na masumbuko, na kifo. Yesu alikuwa afunue uongo huo. Kama mmoja wetu alikuwa atupatie kielelezo cha utii. Kwa ajili ya hili alichukua asili yetu, na kupitia katika uzoefu wetu. "Ilimpasa kufananishwa na ndugu zake." Waebrania 2:17. Ikiwa tungepaswa kukabili chochote ambacho Yesu hakupitia, basi hapo ndipo Shetani angeueleza uwezo wa Mungu kama kitu kisichokidhi mahitaji. Kwa hiyo Yesu "alijaribiwa katika mambo yote kama sisi.” Waebrania 4:15. Alipitia kila jaribu ambalo linatuhusu. Na hakutumia kwa ajili yake uwezo ambao hautolewi bure kwetu. Kama mwanadamu, alikutana na jaribu, na akashinda kwa nguvu alizopewa kutoka kwa Mungu. Anasema, "Kuyafanya mapenzi yako, Ee Mungu wangu, ndiyo furaha yangu; Naam, sheria yako imo moyoni mwangu." Zaburi 40:8. Kadiri alivyotembea akitenda mema, na kuwaponya wote waliokuwa wameathiriwa na Shetani, aliwafunulia wazi wanadamu tabia ya sheria ya Mungu na awaonyesha asili ya utumishi wake. Maisha yake yanashuhudia kwamba inawezekana kwetu kuitii sheria ya Mungu.

Kwa uanadamu wake, Kristo aliugusa uanadamu; kwa uungu wake, anakifikia kiti cha enzi cha Mungu. Kama Mwana wa Adamu, alitupatia kielelezo cha utii; kama Mwana wa Mungu, anatupatia nguvu ya kutii. Alikuwa ni Kristo ambaye aliongea na Musa kutoka katika kichaka katika Mlima Horebu akisema, "Mimi Niko Ambaye Niko. . . . Hivyo ndivyo utakavyowaambia wana wa Israeli, Mimi Niko amenituma kwenu."Kutoka 3:14. Hii ilikuwa ahadi ya kuikomboa Israeli. Kwa hiyo alipokuja "katika mwonekano wa wanadamu," alijitangaza kwamba Yeye ni Mimi Niko. Mtoto wa Bethlehemu, Mwokozi aliye mnyenyekevu na aliyejishusha, ni Mungu “aliyejidhihirisha katika mwili." 1 Tim. 3:16. Na kwetu anasema: "Mimi ndimi mchungaji mwema." "Mimi ni mkate wa uzima." "Mimi ndimi njia, kweli, na uzima." "Nimepewa mamlaka yote **(25)** mbinguni na duniani." Yohana 10:11; 6:51; 14:6; Matt. 28:18. Mimi ndimi uhakika wa kila ahadi. Mimi Niko; msiogope. "Mungu pamoja nasi" ni uhakika wa wokovu wetu kutoka dhambini, uhakika wa nguvu zetu za kutuwezesha kutii sheria ya mbinguni.

Katika kujishusha kuuchukua ubinadamu, Kristo anafunua tabia iliyo kinyume cha tabia ya Shetani. Lakini bado alitembea katika njia ya hali ya chini zaidi, njia ya kujinyenyekeza. "Alipoonekana ana umbo kama mwanadamu, alijinyenyekeza akawa mtii hata mauti, naam, mauti ya msalaba." Wafilipi 2:8. Kama kuhani mkuu awekaye kando mavazi ya ukuu, na kuvaa nguo ya kawaida ya kuhani wa kawaida, ndivyo Kristo alivyochukua namna ya mtumwa, akaitoa dhabihu, Yeye mwenyewe akiwa kuhani, na Yeye mwenyewe akiwa kafara ya dhabihu. "Alijeruhiwa kwa makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu: adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake." Isaya 53:5.

Kristo alitendewa vile tulivyostahili kutendewa sisi, ili ya kwamba tutendewe vile anavyostahili kutendewa Yeye. Alihukumiwa kwa dhambi zetu, ambazo hakuwa na sehemu katika hizo, ili tupate kuhesabiwa haki kwa haki

yake, ambayo hatukuwa na sehemu ndani yake. Alikufa kifo kilichokuwa chetu, kusudi tupokee uzima uliokuwa wake. "Kwa kupigwa kwake tumepona."

Kwa maisha yake na kifo chake, Kristo amepata hata zaidi ya kule kuturejesha kutoka katika maangamizi ya dhambi. Kusudi la Shetani lilikuwa ni kuleta utengano wa milele kati ya Mungu na mwanadamu; lakini katika Kristo tunaunganishwa kwa karibu zaidi na Mungu kuliko vile ambavyo tungekuwa hata kama tusingelianguka. Kwa kuchukua utu wetu, Mwokozi amejifungamanisha na ubinadamu kwa kifungo ambacho hakitavunjwa kamwe. Ameunganishwa nasi milele na milele. "Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwana wake wa pekee." Yohana 3:16. Alimtoa si tu ili kubeba dhambi zetu, na kufa kama dhabihu yetu; alimtoa kwa jamii iliyoanguka. Kutuhakikishia shauri lake la amani lisilofutika, Mungu alimtoa Mwana wake wa pekee ili awe miongoni mwa jamaa ya wanadamu, adumu kuwa na asili ya ubinadamu milele. Hii ni ahadi ya kwamba Mungu ataitimiza ahadi yake. "Kwa ajili yetu mtoto amezaliwa, Tumepewa mtoto mwanaume; Na uweza wa kifalme utakuwa begani mwake." Mungu ameitwaa asili ya mwanadamu katika nafsi ya Mwana wake, na ameipeleka mahali pa juu mbinguni. Ni "Mwana wa Adamu" anayeshiriki katika kiti cha enzi cha malimwengu yote. Ni "Mwana wa Adamu" ambaye jina lake ataitwa, "Mshauri wa ajabu, Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele, Mfalme wa amani." Isaya 9:6. Mimi Niko yuko katikati ya Mungu na mwanadamu, akinyoosha mkono wake kwa wote wawili. Yeye "aliye mtakatifu, asiyekuwa na uovu, asiyekuwa na waa lolote, aliyetengwa na wakosaji, aliyekuwa juu kuliko mbingu," haoni haya kuwaita ndugu zake. Waebrania 7:26; 2:11. Katika Kristo jamaa ya duniani na jamaa ya mbinguni **(26)** zinafungamanishwa pamoja. Kristo aliyetukuzwa ni kaka yetu. Mbinguni kunang’arishwa katika ubinadamu, na ubinadamu umefunuliwa kifuani mwake Yeye aliye Pendo Lisilokoma.

Kuhusu watu wake Mungu asema, "Watakuwa kama vito vya taji, Vikimeta-meta juu ya nchi yake. Maana wema wake, jinsi ulivyo mwingi! Na uzuri wake, jinsi ulivyo mwingi!" Zekaria 9:16, 17. Kuinuliwa juu kwa waliokombolewa kutakuwa ushuhuda wa milele wa rehema za Mungu. "Katika zamani zinazokuja” ataudhihirisha “wingi wa neema yake upitao kiasi kwa wema wake kwetu sisi katika Kristo Yesu." "Ili sasa . . . ijulikane na falme na mamlaka katika ulimwengu wa roho; kwa kadiri ya kusudi la milele alilolikusudia katika Kristo Yesu Bwana wetu." Waefeso 2:7; 3:10, 11.

Kupitia kazi ya Kristo ya ukombozi serikali ya Mungu inasimama katika haki. Yeye Mwenye Nguvu Zote anafanywa kujulikana kama Mungu wa upendo. Lawama za Shetani zinafutwa, na tabia yake inafunuliwa. Uasi hauwezi kuinuka tena. Dhambi haiwezi kuingia katika malimwengu tena. Katika zamani zote wote wako huru mbali na uasi. Kupitia kujitoa dhabihu kwa upendo, wakazi wa dunia na wa mbinguni wanafungamanishwa kwa Muumba wao katika mfungamano wa muungano usiotenganishika.

Kazi ya ukombozi itakuwa kamilifu. Mahali ambapo dhambi ilishamiri, neema ya Mungu inashamiri zaidi na zaidi. Dunia yenyewe, ambayo ndiyo uwanja ambao Shetani anadai kuwa wake, si tu kwamba itakombolewa, bali pia itainuliwa. Ulimwengu wetu mdogo, ulio chini ya laana ya dhambi ukiwa kama nukta yenye giza katika uumbaji wake mtukufu, utainuliwa juu kuliko malimwengu mengine yote ya Mungu. Mahali hapa, ambapo Mwana wa Mungu alikaa akiwa katika mwili; mahali ambapo Mfalme wa utukufu aliishi na kuteseka na kufa, - hapa ndipo makao ya Mungu yatakuwa pamoja na wanadamu, wakati atakapofanya mambo yote kuwa mapya, "naye atafanya maskani yake pamoja nao, nao watakuwa watu wake. Naye Mungu mwenyewe atakuwa pamoja nao." Na kwa zama zisizokoma kadiri waliokombolewa watakavyotembea katika nuru ya Mungu, watamsifu kwa ajili ya Zawadi isiyotamkika, **- Imanueli, "Mungu pamoja nasi."**

## Sura ya 2

# Watu Waliochaguliwa

Kwa zaidi ya miaka elfu moja Wayahudi walikuwa wamengoja kuja kwa Mwokozi. Matumaini yao makubwa yalikuwa yameelekezwa kwenye tukio hili. Katika wimbo na unabii, katika maadhimisho na kaida za kidini hekaluni na ibada za nyumbani, walikuwa wameliangazia jina lake. Lakini wakati alipokuja hawakumjua. Aliye Mpendwa wa mbinguni alikuwa kwao "kama mzizi katika nchi kavu;" Alikuwa "hana umbo wala uzuri;" na waliona ndani yake hakuna uzuri hata wamtamani. "Alikuja kwa walio wake, nao walio wake hawakumpokea." Isaya 53:2; Yohana 1:11.

Lakini Mungu alikuwa amechagua Israeli. Alikuwa amewaita ili wahifadhi miongoni mwa wanadamu ufahamu wa sheria yake, na wa alama na unabii ulioelekeza kwa Mwokozi. Alitamani wawe kama visima vya wokovu kwa ulimwengu. Vile alivyokuwa Ibrahimu katika nchi ya ugeni, Yusufu katika nchi ya Misri, na Danieli katika ufalme wa Babeli, ndivyo Waebrania walivyotakiwa kuwa katikati ya mataifa. Walikuwa wamfunue Mungu kwa watu.

Katika kuitwa kwa Ibrahimu Bwana alikuwa amesema, "Nami nitakufanya wewe kuwa taifa kubwa, na kukubariki, na kulikuza jina lako; nawe uwe baraka; . . . na katika wewe jamaa zote za dunia watabarikiwa." Mwanzo 12:2, 3. Fundisho hilo hilo lilirudiwa kupitia manabii. Hata baada ya Israeli kuwa imeharibiwa na vita na kuchukuliwa mateka, ahadi hiyo ilikuwa yao, "Na hayo mabaki ya Yakobo yatakuwa kati ya kabila nyingi mfano wa umande utokao kwa Bwana, mfano wa manyunyu katika manyasi; yasiyomngojea mtu, wala kuwakawilia." Mika 5:7. Kuhusu hekalu kule Yerusalemu, Bwana alitangaza kupitia kwa Isaya, "Nyumba yangu itaitwa nyumba ya sala kwa mataifa yote." Isaya 56:7.

**(28)** Lakini Waisraeli waliweka matumaini yao katika ukuu wa ulimwengu. Tangu wakati walipoingia Kanaani, walienda mbali na amri za Mungu, na kufuata njia za wapagani. Hata pale Mungu alipowapelekea maonyo kwa kutumia manabii ilikuwa kazi bure. Walipata maonyo ya maumivu ya ukandamizaji wa wapagani lakini ikawa kazi bure. Kila matengenezo yalifuatwa na uasi mkubwa.

Laiti Waisraeli wangekuwa waaminifu kwa Mungu, angekuwa amekamilisha kusudi lake katika kuwainua na kuwatukuza. Laiti wangekuwa wametembea katika njia za utii, angekuwa "amewatukuza juu ya mataifa yote aliyoyafanya, kwa sifa, na jina, na heshima." "Na mataifa yote ya duniani," alisema Musa, "watakuona umeitwa kwa jina la Bwana, nao watakuwa na hofu kwako." "Mataifa watakaozisikia amri hizi zote, nao watasema, Hakika taifa hili kubwa ni watu wenye hekima na akili." Kumbukumbu 26:19; 28:10; 4:6. Lakini kwa sababu ya kutoamini kwao, kusudi la Mungu liliendelea kupita kwao katika nyakati ngumu na mateso.

Waliletwa utumwani Babeli, na wakatawanyika katika nchi za wapagani. Katika hali ngumu hii wengi waliamsha uaminifu wao kwa agano la Mungu. Wakati walipotundika vinubi kwenye miti ya kando ya mto, na kuomboleza kwa ajili ya hekalu takatifu lililoachwa katika uharibifu, nuru ya ukweli iliangaza kutoka kwao, na hali ya kumjua Mungu ilisambazwa kwa wamataifa. Mifumo ya dhabihu za kipagani ilikuwa uigaji potofu wa mfumo ambao Mungu alitoa; na watu wa imani za kipagani wenye nia njema walijifunza kwa Waebrania maana ya huduma ile iliyowekwa na Mungu, na kwa imani waliielewa ahadi ya Mkombozi.

Wengi wa walioishi uhamishoni walipata mateso. Si wachache ambao walipoteza maisha kwa sababu ya kukataa kuacha kuijali Sabato ili kuadhimisha sikukuu za wapagani. Kadiri waabudu wa sanamu walivyoinuka kuushambulia ukweli, Bwana aliwakutanisha watumishi wake uso kwa uso na wafalme na watawala, ili kwamba wao na watu wao waipokee nuru. Mara kwa mara wafalme wakubwa waliongozwa kuutangaza ukuu wa Mungu yule aliyeabudiwa na mateka wa Kiebrania.

Kwa kule kuwa watumwa wa Babeli Waisraeli waliponywa na tabia ya kuabudu sanamu. Mnamo karne zilizofuata, walisumbuliwa na ukandamizaji waliofanyiwa na maadui wapagani, mpaka walipokubali kwa dhati kwamba mafanikio yao yalitegemea utii wao wa sheria ya Mungu. Lakini kwa wengi wao utii haukusukumwa na upendo. Msukumo ulikuwa wa ubinafsi. Walionyesha huduma ya nje kwa Mungu **(29)** kama njia ya kupata ukuu wa taifa lao. Hawakuwa nuru ya ulimwengu, bali walijifungia mbali na ulimwengu ili kukwepa kujaribiwa kuabudu miungu. Katika maelekezo yaliyotolewa kupitia Musa, Mungu alikuwa ameweka vizuizi kuzuia

kushirikiana na waabudu miungu; lakini mafundisho haya yalikuwa yametafsiriwa vibaya. Yalikuwa yamekusudiwa kuwazuia wasiafikiane na matendo ya wapagani. Lakini kwao yalitumika kujenga ukuta unaotenganisha kati ya Israeli na mataifa mengine. Wayahudi waliiona Yerusalemu kama mbinguni, na walikuwa na wivu kwamba Mungu asiwape rehema Mataifa.

Baada ya kurejea kutoka Babeli, hamu kubwa ilielekezwa katika mafundisho ya kidini. Masinagogi yaliinuliwa kote katika nchi, mahali ambako sheria ilifafanuliwa na makuhani na waandishi. Na shule zilianzishwa, ambazo, pamoja na sanaa na sayansi, zilisemekana kufundisha misingi ya haki. Lakini vyombo hivi vilichafuliwa. Mnamo wakati wa kuishi uhamishoni kama mateka, watu wengi walikuwa wamepokea mawazo na desturi za kipagani, na hayo yaliletwa katika taratibu za dini zao. Katika mambo mengi walifanana na matendo ya watu wanaoabudu miungu.

Kadiri walivyoenda mbali na Mungu, Wayahudi walipoteza kwa kiasi kikubwa kuona mafundisho ya ibada ya kweli. Huduma za ibada zilikuwa zimewekwa na Kristo mwenyewe. Katika kila sehemu zilimwashiria Yeye; na zilikuwa zimejaa umuhimu na uzuri wa kiroho. Lakini Wayahudi walipoteza maisha ya kiroho katika maadhimisho yao, na kung'ang'ania taratibu zao wenyewe. Waliamini dhabihu zile na maadhimisho yenyewe, badala ya kumwelekea Yeye ambaye kwake yale yalielekeza. Ili kutoa nafasi kwa ajili ya yale ambayo walikuwa wamepoteza, waandishi na marabi walizidisha matakwa ya mambo yao wenyewe; na kadiri walivyoongezeka katika kusimamia hayo, ndivyo walivyopungua katika kudhihirisha upendo wa Mungu. Walipima utakatifu wao kwa wingi wa maadhimisho na sikukuu, wakati mioyo yao ilikuwa imejazwa na kiburi na unafiki.

Katika kuwa na miongozo yao iliyokuwa mizigo isiyo maana, ilikuwa haiwezekani kuitunza sheria. Wale waliotamani kumtumikia Mungu, na wakajaribu kuyashika maagizo ya marabi, walikuwa katika taabu ya mzigo mzito. Hawakupata pumziko kwa sababu ya kushtakiwa na dhamiri inayosumbuka. Hivyo ndivyo Shetani alivyowakatisha watu tamaa, kushusha ufahamu wao kuhusu tabia ya Mungu, na kuileta imani ya Israeli katika hali ya kuchukiwa. Alitaka kuanzisha dai alilotoa wakati ule alipoasi mbinguni – kwamba matakwa ya Mungu hayakuwa ya haki, na yasingewezekana kutiiwa. Akasema, Hata Israeli hakuishika sheria.

Wakati Wayahudi walikutamani kuja kwa Masihi, hawakuwa na **(30)** uelewa sahihi wa utume wake. Hawakutafuta ukombozi kutoka dhambini, bali ukombozi kutoka kwa Warumi. Walimtazamia Masihi ajaye kama mshindi, kuvunja nguvu za wakandamizaji, na kuikweza Israeli katika mamlaka ya juu. Hivyo ndivyo njia ilivyoandaliwa ya kumkataa Mwokozi.

Wakati wa kuzaliwa kwa Kristo taifa hili lilikuwa katika msuguano likiwa chini ya utawala wa mabwana wa kigeni, na lilikuwa limegubikwa na migogoro ya ndani. Wayahudi walikuwa wameruhusiwa kuwa na namna ya serikali yao iliyo tofauti; lakini hakuna ambacho kingeondoa ile hali ya kwamba walikuwa chini ya kongwa la Warumi, au kuwapatanisha na ubabe wa mamlaka ile. Warumi walijipa haki ya kumchagua na kumwondoa kuhani mkuu, na kazi hiyo mara nyingi ilifanyika kwa njia ya hila, rushwa, na hata mauaji. Kwa hiyo ukuhani ulizidi kuchafuka zaidi na zaidi. Lakini bado makuhani walizidi kuwa na mamlaka makubwa, na waliyatumia kwa ubinafsi na kutafuta fedha. Watu walikuwa wakidaiwa mambo mengi bila huruma, na walikuwa wakitozwa na Warumi kodi kubwa. Hali hii ilisababisha upinzani mkubwa. Matukio ya vurugu yalikuwa ya kawaida. Uchoyo, matumizi ya nguvu, mashaka na kupoa kiroho vilikuwa vikikitafuna kiini chenyewe cha taifa.

Chuki kwa Warumi, na kiburi cha utaifa na cha kiroho, viliwafanya Wayahudi waendelee kufuata mfumo wao wa ibada. Makuhani walijaribu kuhifadhi heshima yao ya utakatifu kwa kutumia maadhimisho ya kidini. Katika giza lao na kukandamizwa, watu wa kawaida na watawala, wakiwa na kiu ya madaraka, walisubiri kuja kwake Yeye ambaye angewaondosha maadui zao na kurudisha ufalme kwa Israeli. Walikuwa wamejifunza unabii, lakini pasipo mtazamo wa kiroho. Kwa hiyo waliangalia kwa juu juu tu maandiko yale yanayoelekeza katika kujishusha kwa ujio wa kwanza wa Kristo, na wakatumia pasipofaa yale yanayoongelea utukufu wa kuja kwake mara ya pili. Kiburi kiliwazuia wasione. Walitafsiri unabii kutegemea na tamaa zao binafsi.

## Sura ya 3

# "Utimilifu wa Wakati"

"Hata ulipowadia utimilifu wa wakati, Mungu alimtuma Mwana wake, . . . kusudi awakomboe hao waliokuwa chini ya sheria, ili sisi tupate kupokea hali ya kuwa wana." Wagalatia. 4:4, 5.

Kuja kwa Mwokozi kulitabiriwa Edeni. Wakati Adamu na Hawa waliposikia ahadi hiyo kwa mara ya kwanza, walitazamia kutimizwa kwake kwa haraka. Walimkaribisha mzaliwa wao wa kwanza kwa furaha, wakitumaini kwamba angeweza kuwa Mwokozi. Lakini utimizo wa ahadi ulichelewa. Wale waliokuwa wa kwanza kuipokea walikufa bila kuiona. Tangu katika siku za Henoko ahadi hiyo ilirudiwa kupitia wazee na manabii, wakihifadhi tumaini la kuja kwake, na bado hakuja. Unabii wa Daniel ulifunua wakati wa kuja kwake, lakini si wote waliotafsiri ujumbe huo kwa usahihi. Karne na karne zilipita; sauti za manabii zilikoma. Mkono wa mkandamizaji ulikuwa mzito juu ya Israeli, na wengi walikuwa tayari kusema, "Siku hizo zinakawia na maono yote hayatimizwi." Ezekieli 12:22.

**(32)** Lakini kama zilivyo nyota katika mzunguko wa njia zake zilizoamuriwa, makusudi ya Mungu hayajui kuwahi wala kuchelewa. Kupitia alama za giza kuu na tanuru la moshi, Mungu alikuwa amefunua kwa Ibrahimu utumwa wa Israeli kule Misri, na alikuwa ametangaza kwamba muda wa wao kukaa ugenini itakuwa miaka mia nne. "Baadaye," alisema, "watatoka na mali mengi." Mwanzo 15:14. Nguvu zote za himaya yenye kiburi ya Farao zilipambana na neno hilo lakini ilikuwa kazi bure. "Ilikuwa siku ile ile" iliyoamriwa katika ahadi ya kimbingu, "ya kwamba majeshi yote ya Bwana yalitoka nchi ya Misri." Kutoka 12:41. Kwa hiyo katika mashauri ya mbinguni saa ya kuja kwa Kristo ilikuwa imepangwa. Wakati mshale wa saa kuu ulipoonyesha kwenye saa hiyo iliyoamuriwa, Yesu alizaliwa Bethlehemu.

"Hata ulipowadia utimilifu wa wakati, Mungu alimtuma Mwana wake." Uongozi wa Mungu ulizielekeza harakati za mataifa, na wimbi la mamlaka na misukumo ya wanadamu, mpaka wakati ulimwengu ulipokuwa umeiva kwa ajili ya ujio wa Mwokozi. Mataifa yalikuwa yameungana chini ya serikali moja. Lugha moja ndiyo iliyokuwa ikitumika kwa sehemu kubwa, na ilitambulika kila mahali kama lugha ya vitabu. Kutoka katika nchi zote Wayahudi waliokuwa katika utawanyiko walikusanyika Yerusalemu katika sikukuu za mwaka. Kwa kadiri ambavyo hawa wangerudi katika nchi zao za ugeni, wangesambaza ulimwenguni kote habari za kuja kwa Masihi.

Mnamo wakati huu mifumo ya kipagani ilikuwa inapoteza nguvu kwa watu. Watu walikuwa na wasiwasi na dini ya matamasha na uongo. Walitamani kupata dini ya kukidhi haja ya moyo. Wakati ambapo ilionekana kama nuru imetoweka miongoni mwa watu, zilikuwepo roho zilizokuwa zinatafuta nuru, na ambazo zilijawa na wasiwasi na huzuni. Walikuwa na kiu ya kumjua Mungu aliye hai, kwa ajili ya uhakika wa maisha ng'ambo ya kaburi.

Kwa kadiri ambavyo Wayahudi walikuwa wameenda mbali na Mungu wao, imani ilikuwa imefifia, na tumaini ilikuwa karibu limekoma kuangazia siku za usoni. Maneno ya manabii yalikuwa hayaeleweki. Kwa watu wengi sana, kifo kilikuwa ni siri ya kutisha; ng'ambo ya hapo kulikuwa na wasiwasi na giza. Kilichobebeshwa kwa nabii kupitia karne nyingi hakikuwa tu maombolezo ya akina mama wa Bethlehemu, bali pia kilio kutoka kwa moyo mkuu wa ubinadamu, - sauti yasikiwa Rama, "Kilio, na maombolezo mengi, Raheli akiwalilia watoto wake, Asikubali kufarijiwa, kwa kuwa hawako." Mathayo 2:18. Katika eneo na uvuli wa mauti, watu walikaa pasipo kufarijika. Kwa macho yenye hamu walikutafuta kule **(33)** kuja kwa Mwokozi, wakati giza litakapofukuzwa, na fumbo la siku za uzoni litakapowekwa wazi.

Nje ya taifa la Kiyahudi kulikuwa na watu waliotabiri kuja kwa mfundishaji wa kimbingu. Watu hawa walikuwa wanautafuta ukweli, na kwao roho ya uvuvio iliwekwa. Mmoja baada ya mwingine, kama vile nyota katika mbingu zenye giza, walimu hao walikuwa wameinuka. Maneno yao ya unabii yalikuwa yamewasha tumaini katika mioyo ya watu maelfu wa ulimwengu wa Mataifa.

Kwa mamia ya miaka maandiko yalikuwa yameshatafsiriwa katika lugha ya Kiyunani, ambayo ilikuwa inazungumzwa sana katika himaya yote ya Kirumi. Wayahudi walikuwa wametawanyika kila mahali, na matarajio yao ya kuja kwa Masihi yalishirikishwa hata kwa Wamataifa kwa kiasi fulani. Miongoni mwa wale ambao waliitwa na Wayahudi wapagani walikuwemo watu waliokuwa na ufahamu bora zaidi wa unabii wa

maandiko kuhusu kuja kwa Masihi kuliko hata ufahamu uliokuwa kwa walimu wa Israeli. Walikuwemo baadhi waliotarajia kuja kwake kama mwokozi aokoaye kutoka dhambini. Wanafalsafa walijitahidi kutafiti siri ya mfumo wa kafara wa Waebrania. Lakini nguvu za utengo za Wayahudi zilizuia kusambaa kwa nuru. Wakiwa na dhamira ya kudumisha utengano kati yao na mataifa mengine, hawakupenda kuwapa ufahamu ambao walikuwa bado wanao kuhusu huduma zile za kivuli. Lazima **(34)** Mtafsiri wa kweli aje. Lazima Yeye ambaye aliwakilishwa na mifano-vivuli hii yote afafanue maana yake.

Kupitia vitu vya asili, kupitia ishara na alama, kupitia wazee na manabii, Mungu amezungumza na ulimwengu. Lazima masomo yatolewe kwa wanadamu kwa lugha ya kibinadamu. Lazima Mjumbe wa agano azungumze. Lazima sauti yake isikike katika hekalu lake. Lazima Kristo aje atamke maneno ambayo yataeleweka kwa uwazi. Akiwa mwasisi wa ukweli, lazima atenganishe ukweli kutoka katika hali ya kufunikwa na maneno ya mwanadamu, ambayo yameufunika na kuufanya usiwe na matokeo yake. Lazima misingi ya serikali ya Mungu na mpango wa ukombozi vielezwe bayana. Lazima masomo ya Agano Jipya yawekwe wazi mbele za watu.

Miongoni mwa Wayahudi kulikuwa bado na watu waliosimama imara, watu wa mtiririko wa ukoo wa watu watakatifu ambao ufahamu wa Mungu ulikuwa umehifadhiwa kupitia kwao. Hawa waliendelea kutazamia tumaini la ahadi iliyofanywa kwa mababa. Waliimarisha imani yao kwa kushikilia ushuhuda uliotolewa kupitia Musa, "Bwana Mungu wenu atawainulieni nabii, katika ndugu zenu, kama mimi; msikieni yeye katika mambo yote atakayonena nanyi." Matendo 3:22. Tena, walisoma jinsi ambavyo Bwana angempaka mafuta Yeye asemaye "niwahubiri wanyenyekevu habari njema," "kuwaganga waliovunjika moyo, kuwatangazia mateka uhuru wao," na kutangaza mwaka wa Bwana uliokubaliwa." Isaya 61:1, 2. Walisoma jinsi ambavyo angeweka "hukumu duniani," namna ambavyo visiwa vingesubiri sheria yake, namna ambavyo Mataifa wangekuja katika nuru yake, na wafalme katika mwangaza wa kuinuka kwake. Isaya 42:4; 60:3.

Maneno ya Yakobo wakati wa kufa kwake yaliwajaza matumaini: "Fimbo ya enzi haitaondoka katika Yuda, Wala mfanya sheria kati ya miguu yake, Hata atakapokuja Yeye, mwenye milki, Ambaye mataifa watamtii." Mwanzo 49:10. Nguvu ya maonyo ya Israeli inashuhudia kwamba kuja kwa Masihi ku karibu. Unabii wa Danieli uliupiga picha utukufu wa enzi ya ufalme wake ambao utafuata baada ya falme za kidunia; na anasema nabii, "Nao utasimama milele na milele." Danieli 2:44. Wakati ambapo wachache waliielewa hali ya utume wa Kristo, miongoni mwa wengi kulikuwa na matarajio kwamba atakuwa mfalme mkuu ambaye angeweka ufalme katika Israeli, na atakayekuja kama mwokozi kwa mataifa.

Utimilifu wa wakati ulikuwa umekuja. Ubinadamu, ukiwa unashuka viwango kwa sababu ya uovu kadiri vizazi vya uasi vilivyoendelea, ulimhitaji Mkombozi. Shetani alikuwa amefanya kazi ya kufanya shimo lililotenganisha dunia na mbingu kuwa la kina kirefu na lisilovukika. Kwa uongo wake alikuwa amewapa moyo mgumu **(35)** watu katika dhambi. Lengo lake lilikuwa ni kuondosha uvumilivu wa Mungu, na kuzima upendo wake kwa mwanadamu, ili auache ulimwengu katika utawala wa kishetani.

Shetani alikuwa anatafuta kuwafungia nje watu wasimjue Mungu, kugeuzia mbali mawazo yao kuhusu hekalu la Mungu, na kuweka ufalme wake. Jitihada zake za kutafuta mamlaka zilionekana kufanikiwa kabisa. Ni kweli kwamba katika kila kizazi Mungu anavyo vyombo vyake. Hata miongoni mwa wapagani, kulikuwa na watu ambao Kristo alifanya kazi kupitia kwao kuwainua watu kutoka katika dhambi zao. Watu hawa walidharauliwa na kuchukiwa. Wengi wao waliuawa. Kivuli cha giza ambacho Shetani aliweka juu ya ulimwengu kiliongezeka zaidi na zaidi.

Kupitia upagani, Shetani amewageuza watu kwa vizazi vingi kuwapeleka mbali na Mungu; lakini alipata ushindi zaidi katika kugeuza imani ya Israeli. Kwa kuamini na kuabudu vitu vyao wenyewe, wapagani walikuwa wamepoteza kumjua Mungu, na walikuwa wameendelea kupotoka zaidi na zaidi. Hivyo ndivyo ilivyokuwa kwa Israeli pia. Kanuni ya kwamba mtu anaweza kujiokoa mwenyewe kwa matendo yake ilikuwa katika msingi wa kila dini ya kipagani; sasa ilikuwa **(36)** imekuwa msingi wa imani ya dini ya Kiyahudi. Shetani alikuwa ameipandikiza kanuni hii kwao. Popote iliposhikiliwa, watu hawana kinga ya dhambi.

Ujumbe wa wokovu hupelekwa kwa watu kupitia mawakala wa kibinadamu. Lakini Wayahudi walihodhi ukweli ambao ni uzima wa milele. Walikuwa wamejihifadhia mana ya uzima, sasa ilikuwa imegeuzwa kuwa upotofu. Dini ambayo walifungia ili wabaki nayo peke yao ilikuwa uhalifu. Walimwibia Mungu utukufu wake; na

kuuchafua ulimwengu kwa injili feki. Walikuwa wamekataa kujisalimisha kwa Mungu kwa ajili ya wokovu wa ulimwengu, na walikuwa wamegeuka kuwa mawakala wa Shetani kwa ajili ya uharibifu wa dunia.

Watu wale ambao walikuwa wameitwa na Mungu kusudi wawe nguzo na uwanja wa ukweli walikuwa wamekuwa wawakilishi wa Shetani. Walikuwa wanafanya kazi ambayo Shetani alitamani wafanye, wakifuata njia ya kuonyesha tabia ya Mungu kwa namna isivyo sahihi, na kuufanya ulimwengu umwone Mungu kama mtawala wa mabavu. Makuhani wale wale ambao walihudumu hekaluni walikuwa wamepoteza uwezo wa kuona umuhimu wa huduma walizokuwa wakifanya. Walikuwa wamekoma kuangalia ili waone kitu halisi kilichokuwa mbele zaidi ya huduma zile zilizokuwa wakilishi. Katika kufanya huduma ya kutoa sadaka za kafara walikuwa kama waigizaji tu katika mchezo wa kuigiza. Kaida za dini ambazo ziliwekwa na Mungu mwenyewe zilifanywa kuwa njia za kutia upofu akili za watu na kuifanya mioyo ya watu kuwa migumu. Mungu asingeweza kufanya jambo zaidi kwa ajili ya mwanadamu kupitia mifereji hii. Lazima mfumo wote ufutiliwe mbali.

Udanganyifu wa dhambi ulikuwa umefikia kilele chake. Mbinu zote za kupotosha roho za watu zilikuwa zimewekwa kazini. Alipouangalia ulimwengu, Mwana wa Mungu aliona mateso na huzuni. Aliona jinsi ambavyo watu walikuwa wamekuwa wahanga wa ukatili wa Shetani. Aliwaangalia kwa huruma wale waliokuwa wamedanganyika, kuuawa na kupotea. Walikuwa wamemchagua mtawala ambaye aliwafunga kwenye gari lake wakiwa mateka. Wakiwa wamechanganywa mawazo na kudanganywa, walikuwa katika msafara wa huzuni kuelekea katika uharibifu wa milele, - katika kifo ambacho hakina tumaini la maisha, kuelekea katika usiku ambao haufuatiwi na asubuhi. Mbinu za Shetani ziliwekwa ndani ya watu, miili ya watu, ambayo ilifanywa iwe makao ya Mungu, ilikuwa imekuwa makao ya pepo waovu. Fahamu, hisia, huruma, na viungo vya wanadamu, vilitumiwa na nguvu ovu zisizo za kawaida kukidhi tamaa binafsi. Muhuri wenyewe wa mapepo ulionekana katika nyuso za watu. Sura za wanadamu zilionyesha mwonekano wa pepo waovu waliowapagaa. Huo ndio mwonekano ambao ulionwa na Mkombozi wa ulimwengu. Je! Huu ndio mwonekano gani wa kuonwa na Yeye Mwenye Usafi Wote!

**(37)** Dhambi ilikuwa imekuwa sayansi, na ufisadi ulikuwa umetawazwa kuwa sehemu ya dini. Uasi ulikuwa umekita mizizi yake kwa kina katika moyo, na uhasama wa mwanadamu ulikuwa mkubwa zaidi dhidi ya mbingu. Ilidhihirishwa mbele ya malimwengu yote kwamba, nje ya Mungu, mwanadamu asingeweza kuinuliwa. Lazima chembe mpya ya maisha na nguvu iwekwe na Yeye aliyeuumba ulimwengu.

Malimwengu ambayo hayakuanguka yamekuwa yakisubiri kwa hamu kubwa kuona Yehova akisimama na kuwafutilia mbali wakazi wa dunia. Na kama Mungu akifanya hivyo, Shetani alikuwa tayari kuendeleza mpango wake wa kutafuta kukubaliwa na viumbe wa mbinguni. Alikuwa ametangaza kwamba misingi ya serikali ya Mungu inafanya msamaha iwe kitu kisichowezekana. Ikiwa dunia ingeharibiwa, angedai kwamba madai yake yamethibitishwa kuwa ya kweli. Alikuwa tayari kumlaumu Mungu, na kusambaza uasi wake kwa malimwengu mengine yaliyo huko juu. Lakini badala ya kuuharibu ulimwengu, Mungu alimtuma Mwana wake kuuokoa. Ingawa upotofu na uharibifu unaonekana katika kila sehemu mahali pote, njia ya kufanya urejeshaji ilikuwa imetolewa. Katika wakati wenyewe, wakati ambapo Shetani alionekana kushinda, Mwana wa Mungu alikuja akileta neema ya mbinguni. Katika kila zama, katika kila saa, upendo wa Mungu umefanywa kwa kila jamii ya watu. Pamoja na kuwepo kwa upinzani wa watu, ishara za neema zimeendelea kuonyeshwa. Na pindi utimilifu wa wakati ulipowadia, Uungu ulitukuzwa kwa kumwaga ulimwenguni mafuriko ya neema iponyayo ambayo kamwe isingezuiwa wala kuondolewa mpaka mpango wa wokovu utimie.

Shetani alikuwa anajigamba kwamba amefanikiwa kuharibu sura ya Mungu ndani ya mwanadamu. Ndipo Yesu akaja kurejesha ndani ya mtu sura ya **(38)** Muumba wake. Mbali na Yesu, hakuna mwingine awezaye kutengeneza upya tabia ambayo imeharibiwa na dhambi. Alikuja kufukuza mapepo ambayo yanatawala utashi. Alikuja kutuinua juu kutoka mavumbini, kuumba tena tabia iliyopotoshwa ili ifanane na ile ya kimbingu, na kuifanya kuwa njema kwa utukufu wake.

## Sura ya 4

# Mwokozi kwa Ajili Yenu

[Sura hii imejengwa katika Luka 2:1-20.]

Mfalme wa utukufu alishuka chini akachukua ubinadamu. Mazingira yake ya duniani yalikuwa ya mabaya na yenye vizuizi. Utukufu wake ulifunikwa, kusudi ukuu wa mwonekano wake wa nje usiwe kitu cha kuvutia watu. Aliondoa hali yote ya kuvutia kwa mwonekano wa nje. Utajiri, heshima ya ulimwengu, na ukuu wa kibinadamu hauwezi kumwokoa mtu na kifo; Yesu alikusudia kwamba kusiwe na kivutio cha asili ya kidunia ambacho kitawaita watu kuja upande wake. Lazima uzuri wa kimbingu ndio uwavute wale ambao wangemfuata. Sifa za Masihi zilikuwa zimeshatabiriwa muda mrefu katika unabii, na alitamani watu wampokee kwa sababu ya ushuhuda wa neno la Mungu.

Malaika walikuwa wameustaajibia mpango wa ukombozi wenye utukufu. Walitazama ili waone jinsi ambavyo watu wa Mungu wangempokea Mwana wake, akiwa amevaa mwili. Walikuja katika nchi ya wale waliochaguliwa. Mataifa mengine yalikuwa yanashughulika na uongo na kuabudu miungu. Malaika walikuja katika nchi ile ambapo utukufu wa Mungu ulikuwa umefunuliwa, na nuru ya unabii ilikuwa imeangaza. Pasipo kuonekana, malaika walikuja Yerusalemu, kwa wale waliochaguliwa kuhifadhi mausia matakatifu ya Mungu, na waliokuwa wahudumu katika nyumba ya **(44)** Mungu. Kukaribia kwa Kristo kulikuwa tayari kumeshatangazwa kwa Zakaria kuhani, wakati alipokuwa akihudumu madhabahuni. Mtangulizi wake alikuwa amezaliwa tayari, utume wake huyo ukithibitishwa na muujiza na unabii. Habari za kuzaliwa kwa mtangulizi huyo na umuhimu wa ajabu wa huduma yale zilikuwa zimesambaa hadi nchi za mbali. Lakini Yerusalemu haikuwa ikijitayarisha kumpokea Mkombozi wake.

Wale wajumbe wa kimbingu walishangaa kuona hali ya kutojali kabisa kwa watu walioitwa na Mungu ili waupelekee ulimwengu nuru ya ukweli mtakatifu. Taifa la Wayahudi lilikuwa limehifadhiwa kama shuhuda kwamba Kristo alikuwa azaliwe katika mbegu ya Ibrahimu na ya Daudi; lakini hawakujua kwamba kuja kwake kulikuwa kumekaribia. Kafara za asubuhi na jioni hekaluni zilikuwa zimeelekeza kila siku kwake aliye Mwana-kondoo wa Mungu; lakini hata hapa hakukuwa na maandalizi ya kumpokea. Makuhani na walimu wa taifa hili hawakujua kwamba tukio kubwa la vizazi lilikuwa linataka kutokea. Walikariri kufanya sala zisizo na maana, na walifanya matendo ya ibada ili kuonekana kwa watu, lakini walikuwa katika kutafuta utajiri na heshima za kidunia wakiwa hawako tayari kwa ajili ya kufunuliwa kwa Masihi. Hali hiyo ya kutojali ilipotosha nchi yote ya Israeli. Mioyo yenye ubinafsi na iliyozungukwa na mambo ya ulimwengu haikuguswa na raha iliyoijaza mbingu furaha. Ni wachache tu waliotafuta kumwona Yeye Asiyeonekana. Kwao hao ndiko ubalozi wa mbinguni ulikotumwa.

Malaika wanamwongoza Yusufu na Mariamu wakati wakisafiri kutoka nyumbani kwao Nazareti kwenda katika mji wa Daudi. Tamko la mtawala wa Kirumi kuhusu kuandikishwa kwa watu walio katika utawala wake lilikuwa limefika hadi kwa wakazi wa vilima vya Galilaya. Kama ilivyokuwa zamani kwa Koreshi aliyeitwa kukalia kiti cha enzi cha himaya ya ulimwengu ili awaweke huru mateka wa Bwana, Kaisari Augusto naye anafanywa wakala kwa ajili ya utimilifu wa kusudi la Mungu kwa kumleta mama wa Yesu Bethlehemu. Huyo mama ni wa ukoo wa Daudi, na lazima Mwana wa Daudi azaliwe katika mji wa Daudi. Kutoka Bethlehemu, alisema nabii, "atanitokea mmoja atakayekuwa mtawala katika Israeli; ambaye matokeo yake yamekuwa tangu zamani za kale, tangu milele." Mika 5:2. Lakini katika mji wa asili yao halisi, Yusufu na Mariamu hawatambuliki wala kuheshimika. Wakiwa wamechoka na bila kupata makao, walitembea umbali wote wa barabara nyembamba, kutoka katika lango la mji hadi mashariki kabisa mwa mji, wakitafuta mahali pa kupumzikia usiku pasipo mafanikio. Katika nyumba ya wageni iliyojaa watu, hakuna nafasi kwa ajili yao. Hatimaye wanapata hifadhi katika nyumba ya hali ya chini inayotumika kuhifadhia wanyama, na hapa ndipo Mkombozi wa ulimwengu anapozaliliwa.

**(47)** Watu hawajui, lakini habari hizo zinaijaza mbingu furaha. Viumbe watakatifu kutoka katika ulimwengu wa nuru wanakuja duniani wakiwa na hamu kubwa sana yenye mguso. Ulimwengu wote unaangazwa kwa sababu ya uwepo wake aliyezaliwa. Kundi la malaika wasiohesabika wamekusanyika juu ya vilima vya Bethlehemu.

Wanasubiri ishara ya kutangaza habari njema kwa ulimwengu. Ikiwa viongozi katika Isareli wangekuwa wakweli katika tumaini lao, huenda wangeshiriki furaha ya kushuhudia kuzaliwa kwa Yesu. Lakini sasa wamepitwa.

Mungu anasema, "Kwa maana nitamimina maji juu yake aliye na kiu, na vijito vya maji juu ya mahali pakavu." "Nuru huwazukia wenye adili gizani." Isaya 44:3; Zaburi 112:4. Miale ya nuru kutoka katika kiti cha enzi cha Mungu itaangaza kuelekea kwa wale ambao wanaitafuta nuru, na wanaoipokea kwa furaha.

Katika mbuga mahali ambapo kijana Daudi alipata kuchunga kondoo, wachungaji walikuwa bado wakikesha katika kulinda usiku. Katika saa za ukimya usiku walikuwa wakiongea pamoja kuhusu Mwokozi aliyeahidiwa, na waliomba kwa ajili ya Mfalme ajaye katika kiti cha enzi cha Daudi. "Malaika wa Bwana akawatokea ghafla, utukufu wa Bwana ukawang'aria pande zote, wakaingiwa na hofu kuu. Malaika akawaambia, Msiogope; kwa kuwa mimi ninawaletea habari njema ya furaha kuu itakayokuwa kwa watu wote; maana leo katika mji wa Daudi amezaliwa, kwa ajili yenu, Mwokozi, ndiye Kristo Bwana."

Kwa maneno haya, maono ya utukufu yanajaza mawazo ya wachungaji hawa walioyasikia. Mwokozi amekuja kwa Israeli! Nguvu, utukufu, ushindi, vinaambatana na ujio wake. Lakini lazima malaika awaandae kumtambua Mwokozi wao katika umaskini na hali ya chini. "Na hii ndiyo ishara kwenu," aliwaambia; "mtamkuta mtoto mchanga amevikwa nguo za kitoto, amelala katika hori ya kulia ng'ombe.

Mjumbe kutoka mbinguni alikuwa amenyamazisha hofu zao. Alikuwa amewaelekeza namna ya kumwona Yesu. Kwa huruma ya kutambua udhaifu wao wa kibinadamu, alikuwa **(48)** amewapa muda wa kuzoea nuru ya kimbingu. Sasa furaha na utukufu haukuweza kufichwa tena. Uwanda wote uliangazwa na mwangaza wa majeshi ya Mungu. Dunia yote ilinyamazishwa, na mbingu iliinama kusikiliza wimbo huu:
"Atukuzwe Mungu juu mbinguni,
Na duniani iwe amani kwa watu aliowaridhia."

Laiti kama jamaa ya wanadamu leo ingetambua wimbo ule! Tangazo lililotolewa wakati ule, ujumbe iliotolewa, vitatanuka hadi mwisho wa wakati, na kusikika hadi katika miisho ya dunia. Wakati Jua la Haki lizukapo, likiwa na uponyaji mbawani mwake, mwangwi wa wimbo ule utatoka katika sauti za mkutano mkuu, kama sauti ya maji mengi, ikisema, "Haleluya; kwa kuwa Bwana Mungu wetu, Mwenyezi, amemiliki." Ufunuo 19:6.

Wakati malaika walipotoweka, nuru ilitoweka, na vivuli vya usiku vikaanguka tena juu ya vilima vya Bethlehemu. Lakini picha ile ya mwanga mkuu usiopata bado kuonwa na macho ya kibinadamu ilibaki katika kumbukumbu za wachungaji wale. "Ikawa, malaika hao walipoondoka kwenda zao mbinguni, wale wachungaji waliambiana, Haya, na twendeni mpaka Bethlehemu, tukalione hilo lililofanyika, alilotujulisha Bwana. Wakaenda kwa haraka wakamkuta Mariamu na Yusufu, na yule mtoto mchanga amelala horini."

Wakiwa wametawanyika kwa furaha kubwa, walitangaza mambo ambayo walikuwa wameona na kusikia. "Wote waliosikia wakastaajabu kwa hayo waliyoambiwa na wachungaji. Lakini Mariamu akayaweka maneno hayo yote, akiyafikiri moyoni mwake. Wale wachungaji wakarudi, huku wanamtukuza Mungu."

Mbingu na dunia haziko mbalimbali sasa zaidi ya vile ilivyokuwa wakati wachungaji waliposikiliza wimbo wa malaika wale. Bado wanadamu ni walengwa wa faraja ya mbingu sasa kama ilivyokuwa wakati ule watu wa kawaida waliokuwa na kazi za kawaida walipokutana na malaika wakati wa mchana, na kuzungumza na wajumbe kutoka mbinguni katika uwanda na katika mashamba ya mizabibu. Katika mapito ya maisha ya kawaida kwetu, mbingu inaweza kuwa karibu sana. Malaika kutoka katika viwanja vya mbinguni watakuwepo katika hatua za wale wanaotembea kwa amri ya Mungu.

Kisa cha Bethlehem ni mada isiyoweza kuelezwa ikaisha yote. Ndani yake kumefichwa "utajiri na hekima na maarifa ya Mungu!" Rom. 11:33. Tunashangazwa na kafara ya Mwokozi ya kufanya mbadilishano kwa kuchukua hori la ng'ombe badala ya kiti cha enzi cha mbinguni, na badala ya wingi wa malaika wamzungukao akawa na **(49)** wanyama katika kibanda. Kiburi cha mwanadamu na kutaka kujitosheleza vinakemewa na uwepo wa Mwokozi. Lakini huu ulikuwa ni mwanzo tu wa Yeye kujidhili. Ingekuwa ni hatua ya kujishusha ya hali ya juu sana kwa Mwana wa Mungu kuchukua ubinadamu, hata kama Adamu asingekuwa alianguka kule Eden. Lakini Yesu alikubali ubinadamu wakati ambapo jamii ya wanadamu ilikuwa imedhoofishwa kwa miaka elfu nne ya kuwepo kwa dhambi. Kama ilivyo kwa kila mtoto wa Adamu Yeye pia alikubali matokeo ya utendaji wa sheria

kuu ya kurithisha. Matokeo haya yalivyokuwa ni kama inavyoonekana katika historia ya wazazi wake waliopita wa kidunia. Alikuja akiwa na urithi huo ili ashiriki huzuni na majaribu, na kutupatia kielelezo cha maisha yasiyo ya dhambi.

Kule mbinguni Shetani alikuwa amemchukia Kristo kwa sababu ya nafasi yake katika mpangilio wa mbinguni. Alimchukia zaidi pale yeye aliposhushwa nafasi. Alimchukia Yeye aliyejitoa kuikomboa jamii ya wadhambi. Lakini Mungu alimruhusu Mwana wake kuja ulimwenguni mahali ambapo Shetani alidai kuwa na utawala, akiwa mtoto asiyejiweza, ambaye anapatikana na udhaifu wa kibinadamu. Alimruhusu akutane na shida za maisha yanayompata kila mtu, kupigana vita ambayo lazima kila mwanadamu aipige, katika hatari ya kushindwa na kupoteza milele.

Moyo wa baba wa kibinadamu una upendo kwa mwanaye. Huuangalia uso wa mtoto wake mdogo, na kutetemeka afikiripo shida za maisha. Anatafuta kumkinga mpendwa wake dhidi ya nguvu za Shetani, akimuepusha na majaribu na misukosuko. Mungu alimtoa Mwana wake wa pekee, kukutana na msukosuko mchungu na hatari kubwa ya kutisha, ili kwamba njia ya maisha iwe ya uhakika kwa ajili ya walio wadogo. "Hili ndilo pendo." Shangaa, Ee mbingu! Shangazwa, Ee dunia!

## Sura ya 5

# Kuwekwa Wakfu

[Sura hii imejengwa katika Luka 2:21-38.]

Kadiri ya siku arobaini baada ya Yesu kuzaliwa, Yusufu na Mariamu walimpeleka Yerusalemu, kumkabidhi kwa Bwana, na kutoa kafara. Jambo hili lilikuwa ni kwa mujibu wa sheria ya Kiyahudi, na kama mbadala wa mwanadamu, lazima Yesu aende sawa na sheria katika kila hali. Alikuwa ameshapitishwa katika desturi ya kutahiriwa, kama ahadi ya utiifu wake kwa sheria.

Kama sadaka ya mama, sheria ilihitaji mwana-kondoo wa umri wa mwaka mmoja kwa ajili ya sadaka ya kuteketezwa, na njiwa au hua kwa ajili ya sadaka ya dhambi. Lakini sheria iliruhusu kwamba ikiwa wazazi ni maskini kiasi cha kutoweza kuleta mwana-kondoo, hua wawili au njiwa wawili walikubalika, mmoja kwa ajili ya sadaka ya kuteketezwa, na mmoja kwa ajili ya sadaka ya dhambi.

Sadaka zilizotolewa mbele za Bwana zilitakiwa zisiwe na mapungufu. Sadaka hizi zilimwakilisha Kristo, na kutokana na hili inathibitika kwamba Yesu mwenyewe hakuwa na mapungufu. Alikuwa "mwana-kondoo asiye na ila, asiye na waa." 1 Petro 1:19. Umbile lake la kimwili halikuwa na ulemavu wowote; mwili wake ulikuwa wenye nguvu na afya njema. Na katika maisha yake yote aliishi sawasawa na sheria za asili. Kimwili **(51)** pamoja na kiroho, alikuwa mfano wa kile ambacho Mungu alipanga kwamba wanadamu wote wawe kwa njia ya kutii sheria zake.

Kutolewa wakfu kwa mzaliwa wa kwanza kulianza nyakati za kale. Mungu alikuwa ameahidi kumtoa Mzaliwa wa kwanza wa mbinguni ili kumponya mwenye dhambi. Zawadi hii ingetambuliwa katika kila nyumba kwa kumtoa wakfu mzaliwa wa kwanza wa kiume. Alikuwa anatakiwa atumike katika kazi ya ukuhani, kama mwakilishi wa Kristo miongoni mwa wanadamu.

Wakati wa kuwaokoa Israeli kutoka Misri, habari ya kumtoa mzaliwa wa kwanza iliamuriwa tena. Wakati wana wa Israeli walipokuwa utumwani Misri, Mungu alimwelekeza Musa kwenda kwa Farao, mfalme wa Misri, na amwambie, “Bwana asema hivi, Israeli ni mwanangu mimi, mzaliwa wa kwanza wangu; nami nimekuambia, Mpe mwanangu ruhusa aende, ili apate kunitumikia, nawe umekataa kumpa ruhusa aende; angalia basi, mimi nitamwua mwanao, mzaliwa wa kwanza wako." Kutoka 4:22, 23.

Musa alipeleka ujumbe ule; lakini jibu la kiburi la mfalme lilikuwa, "Bwana ni nani, hata niisikilize sauti yake, na kuwapa Israeli ruhusa waende zao? Mimi simjui Bwana, wala sitawapa Israeli ruhusa waende zao." Kutoka 5:2. Mungu akatenda ishara na maajabu kwa ajili ya watu wake, kwa kupeleka mapigo ya kutisha juu ya farao. Malaika mwenye kuharibu aliagizwa kuua wazaliwa wa kwanza wa wanadamu na wanyama katika nchi yote ya Misri. Ili Waisraeli wapone na pigo hili walielekezwa kupaka damu ya mwana-kondoo aliyechinjwa kwenye miimo ya milango yao. Kila nyumba ilipaswa kuwekewa alama hiyo, ili ya kwamba wakati malaika alipokuja kwa ajili ya kazi yake ya kuua, apite juu ya nyumba za Waisraeli.

Baada ya kupeleka hukumu hizi juu ya Misri, Mungu alimwambia Musa, "Nitakasie mimi wazaliwa wa kwanza wote, . . . wa binadamu na wa mnyama; ni wangu huyo;” "kwa kuwa hao wazaliwa wa kwanza wote ni wangu; katika siku ile niliyowapiga wazaliwa wa kwanza wote katika nchi ya Misri nikajiwekea wakfu wazaliwa wa kwanza wote wa Israeli, wa wanadamu na wa wanyama; watakuwa wangu; mimi ndimi Bwana." Kutoka 13:2; Hesabu 3:13. Baada ya kuanzisha huduma za patakatifu, Bwana alichagua kabila la Lawi kuhudumu hekaluni mahali pa wazaliwa wa kwanza wa Israeli. Lakini bado wazaliwa wa kwanza walikuwa waendelee kutambuliwa kwamba ni wa Bwana, na walipaswa kurejeshwa nyumbani kwa kukombolewa.

Hivyo ndivyo sheria ya kumtoa mzaliwa wa kwanza ilivyofanywa kuwa na umuhimu mahsusi. Wakati ilikuwa ni kwa kumbukumbu ya Bwana kuwaokoa wana wa Israeli kwa kuwatoa Misri kwa maajabu, iliwakilisha wokovu mkuu, wa kufanywa na Mwana pekee wa Mungu. Kama vile ambavyo damu ilinyunyiziwa kwenye miimo ya milango na kuwaokoa wazaliwa wa kwanza wa Israeli, ndivyo ambavyo damu ya Kristo ina uwezo wa kuuokoa ulimwengu.

**(52)** Basi kule kupelekwa hekaluni kwa Kristo kulikuwa na maana kubwa kiasi gani! Lakini kuhani hakuona kupitia katika pazia lile; hakusoma siri iliyokuwa ng'ambo zaidi ya pale. Kupelekwa hekaluni kwa watoto wachanga lilikuwa tukio la kawaida. Siku baada ya siku kuhani alipokea pesa ya kukomboa watoto kadiri walivyoletwa kwa Bwana. Siku baada ya siku aliingia katika kazi yake ya kila siku, bila kuzingatia sana wazazi au watoto walioletwa, isipokuwa pale alipoona viashiria vya wazazi kuwa matajiri au kuwa na cheo cha juu. Yusufu na Mariamu walikuwa maskini; na pindi walipokuja na mtoto wao, makuhani waliona tu mwanaume na mwanamke wakiwa wamevaa kama watu wa Galilaya, na katika mavazi ya hali ya chini mno. Katika mwonekano wao hakukuwa na kitu chochote cha kuvutia watu, walitoa tu sadaka ambayo hutolewa na watu wa daraja la kimaskini.

Kuhani alifanya utaratibu wa huduma yake rasmi. Alimchukua mtoto mikononi mwake na kumwinua juu mbele ya madhabahu. Baada ya kumrudisha kwa mama yake aliandika jina "Yesu" katika gombo la wazaliwa wa kwanza. Hata kidogo hakufikiri kwamba mtoto aliyekuwa mikononi mwake ni Mkuu wa mbinguni, Mfalme wa utukufu. Kuhani hakufikiria kwamba mtoto huyu alikuwa Yeye ambaye Musa aliandika habari zake, "Bwana Mungu wenu atawainulieni nabii, katika ndugu zenu, kama mimi; msikieni yeye katika mambo yote atakayonena nanyi." Matendo 3:22. Hakufikiria kwamba mtoto huyu alikuwa Yeye mwenye utukufu ambao Musa aliomba kuona. Lakini sasa Yeye aliye mkuu kuliko Musa yuko katika mikono ya kuhani; na wakati alipokuwa akiorodhesha jina la mtoto huyu, alikuwa akiorodhesha jina la Yeye aliyekuwa msingi wa mfumo wote wa kafara wa Kiyahudi. Jina lile lilikuwa ndilo waranti ya kifo chake; maana ule mfumo wa kafara na sadaka ulikuwa unapitwa na wakati; mfano ulikuwa unakuwa uhalisia, kivuli kilikuwa kinakuwa kitu halisi.

Shekina ilikuwa imeondoka hekaluni, lakini ndani ya mtoto wa Bethlehemu kulikuwa kumefichwa utukufu ambao mbele ya huo malaika husujudu. Mtoto huyu ambaye hajitambui alikuwa ndiye mzao wa mwanamke aliyeahidiwa, ambaye madhabahu ya kwanza katika lango la Edeni ilielekeza kwake. Huyu alikuwa ndiye Mwenye miliki, mtoaji wa amani. Alikuwa ndiye yule aliyejitamka kwa Musa kwamba ni Mimi Niko. Alikuwa ni yule ambaye alikuwa kiongozi wa Israeli akiwa katika nguzo ya wingu na ya moto. Huyu ndiye yule ambaye ametabiriwa na watabiri. Alikuwa ni Tumaini la mataifa yote, Mzizi na Mzao wa Daudi, na Nyota ya Asubuhi iang'aayo. Jina lile la mtoto mchanga asiyejiwezea lolote, lililoandikwa katika gombo la Israeli, likimtangaza kama ndugu yetu, lilikuwa tumaini la mwanadamu aliyeanguka. Mtoto ambaye amelipiwa pesa ya ukombozi alikuwa ndiye Yeye ambaye angelipa fidia kwa ajili ya dhambi za ulimwengu wote. Alikuwa kwa kweli "kuhani mkuu juu ya nyumba ya Mungu," mkuu wa "ukuhani usioondoka," mpatanishi **(55)** katika "mkono wa kuume wa Ukuu huko juu." Waebrania 10:21; 7:24; 1:3.

Mambo ya rohoni yanatambuliwa rohoni. Katika hekalu Mwana wa Mungu aliwekwa wakfu kwa ajili ya kazi aliyokuwa amekuja kufanya. Kuhani alimwangalia kama ambavyo angemwangalia mtoto mwingine yeyote. Lakini ingawa hakuona wala kuhisi jambo lolote lisilo la kawaida, tendo la Mungu la kuupatia ulimwengu Mwana wake lilitambuliwa. Tukio hili halikupita bila hali fulani ya kumtambua Kristo. "Na tazama, pale Yerusalemu palikuwa na mtu, jina lake Simeoni, naye ni mtu mwenye haki, mcha Mungu, akiitarajia faraja ya Israeli; na Roho Mtakatifu alikuwa juu yake. Naye alikuwa ameonywa na Roho Mtakatifu ya kwamba hataona mauti kabla ya kumwona Kristo wa Bwana."

Wakati Simeoni anapoingia hekaluni, anaiona familia ikimtoa mwana aliye mzaliwa wa kwanza kwa kuhani. Mwonekano wao unaashiria umaskini; lakini Simeoni anaelewa onyo la Roho, na anashawishika kwa kina kwamba mtoto mchanga ambaye yuko anatolewa kwa Bwana ni Faraja ya Israeli, Yeye yule ambaye amekuwa akitamani kumwona. Kwa kuhani aliyeshtushwa, Simeoni anaonekana kama mtu aliyefurahishwa. Mtoto amerudishwa kwa Maria, naye Simeoni anamchukua na kumshika mikononi mwake na kumkabidhi kwa Mungu, wakati furaha ambayo hajapata kuwa nayo ikimjaa nafsini mwake. Akiwa amemwinua juu mtoto mchanga aliye Mwokozi, anasema, "Sasa, Bwana, wamruhusu mtumishi wako, Kwa amani, kama ulivyosema; Kwa kuwa macho yangu yameuona wokovu wako, Uliouweka tayari machoni pa watu wote; Nuru ya kuwa mwangaza wa Mataifa, Na kuwa utukufu wa watu wako Israeli."

Roho ya unabii ilikuwa juu ya mtu wa Mungu huyu, na wakati Yusufu na Mariamu walipokuwa wamesimama pale, wakishangaa maneno yake, aliwabariki, na kumwambia Mariamu, "Tazama, huyu amewekwa kwa

kuanguka na kuinuka wengi walio katika Israeli, na kuwa ishara itakayonenewa. Nawe mwenyewe, upanga utaingia moyoni mwako, ili yafunuliwe mawazo ya mioyo mingi."

Naye Ana, nabii wa kike, aliingilia na kuthibitisha ushuhuda wa Simeoni kuhusu Kristo. Wakati Simeoni alipoongea, uso wa mwanamke huyu uling'aa kwa utukufu wa Mungu, na alimimina shukrani zake kutoka ndani ya moyo wake kwamba alikuwa ameruhusiwa kumwona Kristo Bwana.

Waabudu hawa wanyenyekevu hawakuwa wamejifunza unabii bure. Lakini waliokuwa na vyeo kama wakuu na makuhani katika Israeli, ingawa hata wao walikuwa na maneno ya unabii ya thamani, hawakuwa wanatembea katika njia ya Bwana, na macho yao hayakuwa wazi kuiona Nuru ya uzima.

**(56)** Hivyo ndivyo ilivyo hata sasa. Matukio ambayo yanathaminiwa na mbingu yote hayazingatiwi, matukio hayo yanatukia pasipo viongozi wa dini na waabudu katika nyumba ya Mungu kujali. Watu wanamkiri Kristo aliye katika historia, huku wakigeukia mbali kutoka kwa Kristo aliye hai. Kristo katika neno lake la wito wa kujikana, katika njia ya umaskini na kuteseka kunakotafuta ahueni, katika njia ya haki inayoendana na umaskini na shida na kejeli, hapokelewi kwa utayari mkubwa sasa zaidi ya vile alivyopokelewa miaka elfu moja na mia nane iliyopita.

Mariamu aliutafakari kwa mapana unabii mrefu uliotolewa na Simeoni. Kadiri alivyomwangalia mtoto aliyekuwa mikononi mwake, na kukumbuka maneno yaliyosemwa na wachungaji wa kondoo wa Bethlehem, alijawa na furaha kuu na mng'ao wa tumaini. Maneno ya Simeoni yalimkumbusha maneno ya unabii ya Isaya: "Basi litatoka chipukizi katika shina la Yese, na tawi litakalotoka katika mizizi yake litazaa matunda. Na roho ya Bwana atakaa juu yake, roho ya hekima na ufahamu, roho ya shauri na uweza, roho ya maarifa na ya kumcha Bwana . . . Na haki itakuwa mshipi wa viuno vyake, na uaminifu mshipi wa kujifungia." "Watu wale waliokwenda katika giza Wameona nuru kuu; Wale waliokaa katika nchi ya uvuli wa mauti, Nuru imewaa ngaza . . . Maana kwa ajili yetu mtoto amezaliwa, Tumepewa mtoto mwanamume; Na uweza wa kifalme utakuwa begani mwake; Naye ataitwa jina lake, Mshauri wa ajabu, Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele, Mfalme wa amani." Isaya 11:1-5; 9:2-6.

Lakini bado Mariamu hakufahamu kazi ambayo Kristo amekuja kufanya. Simeoni alikuwa ametoa unabii kumhusu huyo kama nuru ya kuangazia Wamataifa, na kuwa utukufu wa Israeli. Hivyo ndivyo malaika walivyokutangaza kuzaliwa kwa Mwokozi kama habari njema kwa watu wote. Mungu alikuwa anatafuta kusahihisha ufinyu wa ufahamu wa Wayahudi kuhusu kazi ya Masihi. Alitaka watu wamwone, si tu kama mwokozi wa Israeli, bali kama Mkombozi wa ulimwengu wote. Lakini lazima miaka mingi ipite kabla hata ya mama wa Yesu mwenyewe kuelewa kazi yake hiyo.

Mariamu alitarajia kuwa Masihi atatawala katika kiti cha enzi cha Daudi, lakini hakuona njia ya ubatizo wa maumivu ambayo ingepitwa ili kukipata. Kupitia maneno ya Simeoni imefunuliwa kwamba Masihi hatakuwa na njia isiyo na vizuizi katika ulimwengu. Katika maneno yake kwa Mariamu, "Upanga utaingia moyoni mwako," Mungu katika rehema yake anampa mama wa Yesu kidokezo cha maumivu ambayo kwa ajili ya Yesu tayari alikuwa ameanza kuyabeba.

Simeoni alikuwa amesema, "Tazama, huyu amewekwa kwa kuanguka na kuinuka wengi walio katika Israeli, na kuwa ishara itakayonenewa."

**(57)** Lazima wale ambao wangeinuka tena waanguke. Lazima tuanguke kwenye Mwamba na kuvunjika kabla ya kuinuliwa katika Kristo. Lazima ubinafsi upinduliwe, lazima kiburi kishushwe, ikiwa tunataka kuujua utukufu wa ufalme wa kiroho. Wayahudi wasingepokea heshima ile ambayo inafikiwa kwa njia ya fedheha. Kwa hiyo wasingempokea Mkombozi. Alikuwa ndiye ile ishara ambayo ingenenewa kinyume.

"Ili yafunuliwe mawazo ya mioyo mingi." Katika nuru ya maisha ya Mwokozi, mioyo ya wote, tangu Muumba mpaka mfalme wa giza, inafunuliwa. Shetani amemwasilisha Mungu kwa namna inayoonyesha kuwa ni mbinafsi na mkandamizaji, kama anayedai vyote, na kama asiyetoa chochote, kama anayehitaji kutumikiwa na viumbe wake kwa ajili ya utukufu wake binafsi, na pasipo kutoa chochote kwa ajili ya mema yao. Lakini zawadi ya Kristo inaufunua moyo wa Mungu. Inathibitisha kwamba mawazo ya Mungu kwetu ni "mawazo ya amani, wala si mabaya." Yeremia 29:11. Inatangaza kwamba wakati chuki ya Mungu dhidi ya dhambi ina nguvu kama kifo, upendo wake kwa mdhambi una nguvu zaidi ya kifo. Akiwa ameanzisha ukombozi wetu, hataacha lolote, hata

liwe la gharama kubwa kiasi gani, ambalo ni la lazima katika kukamilisha kazi yake. Hakuna ukweli muhimu kwa wokovu wetu ambao unafichwa, hakuna mwujiza wa rehema ambao unapuuzwa, hakuna nyenzo ya kimbingu ambayo imeachwa bila kutumiwa. Fadhila zimelundikwa juu ya fadhila, zawadi juu ya zawadi. Hazina yote ya mbinguni imefunguliwa kwa wale ambao anatafuta kuwaokoa. Akiwa amekusanya utajiri wote wa malimwengu, na kuweka wazi rasilimali za uwezo usio mwisho, anaviweka vyote mikononi mwa Kristo, na kumwambia, Vyote hivi ni kwa ajili ya mwanadamu. Tumia zawadi hizi kumshawishi aone kwamba hakuna upendo mkubwa kuliko wangu Mimi duniani au mbinguni. Furaha yake kuu kuliko zote itapatikana katika kunipenda Mimi.

Kwenye msalaba wa Kalvari, upendo na ubinafsi vinakabiliana uso kwa uso. Hapa ndipo kulikuwa udhihirisho wa hayo mawili kwa kiwango cha juu. Kristo alikuwa ameishi akifariji na kubariki, na katika kumfikisha katika kifo, Shetani alidhihirisha nia yake mbaya ya chuki dhidi ya Mungu. Alithibitisha kwamba lengo la uasi wake hasa lilikuwa ni kumpindua Mungu, na kumharibu Yeye ambaye kupitia kwake upendo wa Mungu ungeonyeshwa.

Kwa maisha na kifo cha Kristo, mawazo ya watu yanaletwa pia katika kuona. Kutoka katika hori la mifugo mpaka msalabani, maisha ya Yesu yalikuwa ni wito wa kujisalimisha kikamilifu, na kushiriki katika mateso. Yalifunua makusudi ya wanadamu. Yesu alikuja na ukweli wa mbinguni, na wote waliokuwa wanaisikiliza sauti ya Roho Mtakatifu walivutwa kwake. Wale wanaoabudu ubinafsi walikuwa wa ufalme wa Shetani. Katika mtazamo wao kwa Yesu, wote walionyesha kwamba wamesimama upande wa nani. Na hivyo ndivyo kila mmoja anavyopitisha hukumu juu yake mwenyewe.

**(58)** Katika siku ya hukumu ya mwisho, kila nafsi iliyopotea itaelewa namna ilivyoukataa ukweli. Msalaba utaonyeshwa, na uzito wake halisi utaonwa na kila akili ambayo ilikuwa imepofushwa na uovu. Katika kule kuiona Kalvari pamoja na Kafara ya ajabu, wadhambi watakuwa wamesimama katika hali ya kuhukumiwa. Kila uongo wa kusingizia utaondoshwa. Uasi wa mwanadamu utaonekana katika ubaya wake. Watu wataona kile ambacho walikichagua. Kila suala la ukweli na makosa katika pambano la muda mrefu litakuwa limewekwa wazi. Katika hukumu ya malimwengu, Mungu atakuwa wazi pasipo lawama kuhusiana na kuwepo na kuendelea kwa uovu. Itaonyeshwa wazi kwamba maagizo ya kimbingu hayapatani na dhambi. Hakukuwa na mapungufu katika serikali ya Mungu, hakuna sababu ya kutoridhika. Wakati mawazo ya wote yatakapofunuliwa, makundi yote mawili ya watiifu na waasi wataungana katika kutangaza kwamba, "Ni za haki, na za kweli, njia zako, Ee Mfalme wa mataifa. Ni nani asiyekucha, Ee Bwana, na kulitukuza jina lako? . . . kwa kuwa matendo yako ya haki yamekwisha kufunuliwa." Ufunuo 15:3, 4.

# Sura ya 6

## "Tumeiona Nyota Yake"

[Sura hii imejengwa katika Mathayo 2]

"Yesu alipozaliwa katika Bethlehemu ya Uyahudi zamani za mfalme Herode, tazama, mamajusi wa mashariki walifika Yerusalemu, wakisema, Yuko wapi yeye aliyezaliwa mfalme wa Wayahudi? Kwa maana tuliiona nyota yake mashariki, nasi tumekuja kumsujudia."

Mamajusi kutoka Mashariki walikuwa wanafalsafa. Walikuwa watu wa tabaka kubwa na lenye ushawishi lililokuwa na watu wa uzao wa kifalme, na lilikuwa na watu wengi wenye mali na walio na elimu katika taifa lao. Miongoni mwa hawa walikuwemo wengi waliokuwa wanaaminisha watu uongo. Wengine walikuwa watu wanyoofu waliojifunza ishara za Mungu katika maumbile ya asili, na ambao walikuwa wanaheshimiwa kwa uadilifu wao na hekima yao. Wenye hekima hawa waliokuja kwa Yesu walikuwa wenye tabia hii.

Nuru ya Mungu inadumu kuangaza katika giza la upagani. Kadiri mamajusi hawa walivyosoma mbingu zenye nyota, na kutafuta kuelewa siri iliyofichika ya njia zake, waliona utukufu wa Muumba. Wakitafuta kujua kwa uwazi zaidi, waligeukia Maandiko ya Waebrania. Katika nchi yao wenyewe kulikuwa na hazina ya maandiko ya manabii yaliyotabiri kuja kwa mwalimu kutoka mbinguni. Balaamu alikuwa mtu wa jamii ya mamajusi, aliyefikirika wakati fulani kuwa nabii wa Mungu; kwa Roho Mtakatifu alikuwa ametabiri kuhusu kushamiri kwa Israeli na kuja kwa Masihi; na unabii wake **(60)** ulikuwa umerithishwa katika mila zao kutoka karne hata karne. Lakini katika Agano la Kale kuja kwa Mwokozi kulikuwa kumefunuliwa kwa uwazi zaidi. Mamajusi walijifunza kwa furaha kwamba kuja kwake kulikuwa karibu, na ya kwamba ulimwengu wote ulikuwa ujazwe na ufahamu wa utukufu wa Bwana.

Wenye hekima hawa walikuwa wameona nuru ya ajabu katika mbingu katika usiku ule ambao utukufu wa Mungu ulijaza milima ya Bethlehemu. Pindi nuru ilipotoweka, nyota inayowaka ilitokea, na ikaendelea kuwepo angani. Haikuwa nyota iliyosimama wala haikuwa sayari, hali ile iliibua udadisi wa mtu aliye makini. Nyota ile ilikuwa ni kundi la malaika waliokuwa mbali, lakini wale wenye hekima walikuwa hawajui nyota ya namna hii. Hata hivyo walishawishika kuamini kwamba nyota ile ilikuwa na umuhimu kwao. Waliwauliza makuhani na wanafalsafa, na walitafuta katika maandishi yaliyo katika magombo ya kale. Unabii wa Balaamu ulikuwa umesema, "Nyota itatokea katika Yakobo Na fimbo ya enzi itainuka katika Israeli." Hesabu 24:17. Je, hii nyota ngeni haiwezi kuwa imetumwa kama kiashiria cha Yeye Aliyeahidiwa? Mamajusi walikuwa wamekaribisha nuru ya ukweli uliotumwa na mbingu; sasa ilimwagwa juu yao kwa miale inayoangaza zaidi. Katika ndoto waliagizwa kwenda kutafuta habari za Mfalme aliyezaliwa.

Kama vile Ibrahimu alivyotoka kwenda kwa wito wa Mungu, "asijue aendako" (Waebrania 11:8); kama Israeli kwa imani walivyofuata nguzo ya wingu kwenda katika nchi ya ahadi, ndivyo hawa Wamataifa walivyotoka kwenda kumtafuta Mwokozi aliyeahidiwa. Nchi ya Mashariki ilijaliwa kuwa na vitu vya thamani, na mamajusi hawakutoka mikono mitupu. Ilikuwa desturi kutoa zawadi kama tendo la kuonyesha heshima kwa wana wa kifalme au watu wengine wenye hadhi kubwa na zawadi kubwa kabisa zilizowezekana kutoka katika nchi zilibebwa kama sadaka ya kutoa kwake Yeye ambaye katika yeye jamaa zote za dunia zingebarikiwa. Ilikuwa lazima kusafiri usiku ili kuendelea kuiona nyota ile; lakini wasafiri hawa walijiliwaza kwa kurudiarudia misemo ya desturi zao na maneno ya manabii kumhusu Yeye ambaye walikuwa wakimtafuta. Kila walipofanya kituo ili kupumzika, walijifunza maneno ya unabii; na walishawishika sana kuamini kwamba walikuwa wanaongozwa na mbingu. Wakati walikuwa na nyota mbele yao kama ishara ya nje, walikuwa na uthibitisho wa ndani pia wa Roho Mtakatifu, uliokuwa ukisukuma mioyo yao, na kuwapa tumaini. Ingawa ilikuwa ndefu, safari yao ilikuwa ya furaha kwao.

Sasa wamefika katika nchi ya Israeli, na wako wanashuka Mlima wa Mizeituni, Yerusalemu ikiwa machoni pao, na, tazama, nyota ile ambayo imewaongoza katika njia yote ya kuchosha inatulia juu usawa wa hekalu, na baada ya kitambo inatoweka wasiione. Kwa hatua za wenye hamu wanasonga mbele, kwa ujasiri wakitarajia kwamba kuzaliwa kwa Masihi ni mzigo wa furaha kwa kila lugha. Lakini **(61)** matarajio yao ni kazi bure. Wanapoingia

katika mji mtakatifu, wanakwenda hekaluni. Kwa mshangao wanakuta hakuna mtu yeyote anayeonekana kujua lolote kuhusu mfalme aliyezaliwa. Maswali yao hayavuti mwitikio wowote wa furaha kwa watu, bali wanaona mwitikio wa kupigwa butwaa na hofu, ambayo imechanganyika na chuki.

Makuhani wanaendelea kurudia-rudia mapokeo. Wanasifia dini yao na wema wao wenyewe, huku wakiwahukumu Wayunani na Warumi kwamba ni wapagani, na wadhambi wakubwa kuliko wengine. Wale wenye hekima si waabudu sanamu, na mbele za Mungu wanasimama katika viwango vya juu sana kuliko hawa wanaosemwa kuwa watu wanaomwabudu Mungu; lakini bado wanaangaliwa na Wayahudi kama wapagani. Maulizo ya hamu ya wenye hekima hawa hayagusi mawazo hata ya miongoni mwa wale walioamuriwa kuwa walinzi wa Mafundisho Matakatifu.

Kufika kwa mamajusi kulisikika katika Yerusalemu yote. Ujio wao wa kigeni uliamsha msisimko miongoni mwa watu, ambao ulipenya mpaka katika jumba la Mfalme Herode. Muedomu huyu mwenye hila alishtushwa na kile ambacho kingekuwa upinzani kwake. Mauaji yasiyohesabika yalitia alama njia yake ya kukifikia kiti chake cha enzi. Akiwa mwenye asili ya kigeni, alikuwa akichukiwa na watu aliokuwa akiwatawala. Usalama wake pekee ulikuwa unatoka Rumi. Lakini Mfalme huyu mpya anayetajwa alikuwa juu. Alizaliwa ili awe Mfalme.

Herode aliwashuku makuhani kwamba wamekula njama na wageni wale kutaharakisha watu wafanye fujo na kumwondoa katika kiti cha enzi. Hata hivyo aliificha hofu yake hiyo akiazimia kuharibu mpango wao huo kwa mbinu ya hali ya juu. Akiwahutubia wakuu wa makuhani na waandishi, aliwauliza **(62)** mafundisho ya vitabu vyao vitakatifu yasemavyo kuhusu mahali pa kuzaliwa Masihi.

Hali hii ya kiti cha enzi kisicho halali kwao kuuliza, tena kulikofanywa kwa ombi la wageni, kuliking'ata kiburi cha walimu wa Kiyahudi. Hali waliyoonyesha katika kufuatilia magombo ya unabii bila kuonyesha kuwa ni muhimu kulimghadhibisha mtawala huyu mwenye wivu. Aliona kama vile wanajaribu kuficha kile wanachojua kuhusu habari ile. Hawakudiriki kuacha kutekeleza agizo la mamlaka, ambayo iliwaamuru wafanye uchunguzi wa kina, na watangaze mahali Mfalme anayetarajiwa atakapozaliwa. "Nao wakamwambia, Katika Bethlehemu ya Uyahudi; kwa maana ndivyo ilivyoandikwa na nabii,

" Nawe Bethlehemu, katika nchi ya Yuda, Hu mdogo kamwe katika majumbe wa Yuda;

Kwa kuwa kwako atatoka mtawala Atakayewachunga watu wangu Israeli."

Sasa Herode aliwakaribisha mamajusi kwenda kwa mahojiano ya faragha. Hofu na ghadhabu ilikuwa katika moyo wake, lakini alijionyesha kwa nje kama mtulivu, na aliwapokea wageni wale kwa kuwajali. Aliwauliza kuhusu muda ambapo nyota ile ilikuwa imewatokea, na akajifanya kupokea kwa furaha habari ya kuzaliwa kwa Kristo. Aliwaambia wageni wake, "Shikeni njia, mkaulize sana mambo ya mtoto; na mkiisha kumwona, nileteeni habari, ili mimi nami niende nimsujudie." Akisha kusema hivyo, aliwaruhusu washike njia kuelekea Bethlehemu.

Makuhani na wazee wa Yerusalemu hawakuwa watu wasiojua kuhusu kuzaliwa kwa Yesu kiasi kile walichojifanya kuwa. Taarifa ya ujio wa malaika kwa wachungaji wa kondeni zilikuwa zimeshaletwa Yerusalem, lakini marabi walikuwa wameichukulia taarifa hiyo kama kitu kisichostahili kuzingatiwa. Huenda wao wenyewe wangekuwa wameshamwona Yesu, na huenda wangeweza hata kuwaongoza mamajusi hadi mahali Yesu alipozaliwa; lakini badala ya hilo, wenye hekima ndio walikuja kuwaamsha kuhusu kuzaliwa kwa Masihi. Walisema, "Yuko wapi yeye aliyezaliwa mfalme wa Wayahudi? Kwa maana tuliiona nyota yake mashariki, nasi tumekuja kumsujudia."

Wakati huo kiburi na husuda vilifunga mlango dhidi ya nuru. Ikiwa taarifa zilizoletwa na wachungaji na wenye hekima hawa zingethaminiwa, zingeweka nafasi ya makuhani na marabi katika wakati mgumu sana, zikiondoa uhalali wa madai yao ya kuwa wafasiri wa ukweli wa Mungu. Walimu hawa waliosoma hawakuwa tayari kushuka na kuelekezwa na watu walioonekana kwao kama wapagani. Walisema kwamba haiwezekani iwe kama vile Mungu amewapita wao, na kuwasiliana **(63)** na wachungaji wa makondeni na Wamataifa wasiotahiriwa ambapo wote hawa walionekana kuwa wasiojua kitu. Waliazimia kutokukubaliana na taarifa zilizokuwa zinamsumbua Mfalme Herode na watu wote wa Yerusalemu. Wala wasingeenda hata Bethlehemu kuona kama mambo hayo yalikuwa hivyo. Na waliwaongoza watu kuchukulia kuwa mambo hayo yanayohusu Yesu ni hisia za ushupavu. Hapa ndipo makuhani na marabi walipoanzia kumkataa Kristo. Kiburi chao na usumbufu vilianzia

hapa na kukomaa hadi kuwa chuki dhidi ya Mwokozi. Wakati huu ambapo Mungu alikuwa anafungua mlango kwa ajili ya Wamataifa, viongozi wa Wayahudi walikuwa wanajifungia mlango wao wenyewe.

Wenye hekima wa mashariki waliondoka zao kutoka Yerusalemu. Vivuli vya usiku vilikuwa vinakuja wakati walipoyapita malango, lakini kwa furaha kubwa waliiona ile nyota, na walielekezwa kwenda Bethlehemu. Hawakuwa wamepata habari kama zile walizopewa wachungaji kuhusu mahali pa hali ya chini alipokuwa Yesu. Baada ya safari ndefu walikuwa wamefadhaishwa na hali ya kutojali ya viongozi wa Wayahudi, walikuwa wameondoka Yerusalemu wakiwa wamepungukiwa ujasiri kuliko wakati walipoingia katika mji huo. Kule Bethlehemu walikuta hakuna ulinzi wa kifalme ambao umewekwa ili kumlinda Mfalme aliyezaliwa. Hakuna hata mmoja miongoni mwa watu wenye heshima wa ulimwengu waliokuwepo. Yesu alikuwa amelazwa katika hori. Wazazi wake, waliokuwa wakulima ambao si wasomi, walikuwa pekee ndio waangalizi wake. Je, Inawezekana kwamba huyu ndiye Yeye ambaye kwa ajili yake imeandikwa, kwamba angeweza “kuziinua kabila za Yakobo, na kuwarejeza watu wa Israeli waliohifadhiwa;” ili kwamba aweze kuwa “nuru ya mataifa,” na kwa ajili ya “wokovu . . . hata miisho ya dunia"? Isa. 49:6.

"Wakaingia nyumbani, wakamwona mtoto pamoja na Mariamu mamaye, wakaanguka wakamsujudia." Waligundua kwamba ule mwonekano wa nje na wa hali ya chini wa Yesu ulikuwa umefunika ndani yake uwepo wa Uungu. Walimpatia mioyo yao kama Mwokozi wao, halafu wakamtolea tunu zao, - "dhahabu na uvumba na manemane.” Imani yao ya ajabu kiasi gani! **(64)** Wenye hekima hawa kutoka Mashariki wangestahili kuambiwa hivi, kama ilivyokuwa baadaye kwa akida wa Kirumi, "Sijaona imani kubwa namna hii, kwa yeyote katika Israeli." Mathayo 8:10.

Wenye hekima walikuwa hawajatekeleza mpango wa Herode kuhusu Yesu. Wakati makusudi ya safari yao yalipokamilika, walijiandaa kurudi Yerusalemu, wakidhamiria kumjulisha kuhusu mafanikio yao. Lakini walipata ujumbe kutoka mbinguni katika ndoto wakitakiwa wasifanye mawasiliano zaidi na yeye. Walirudi katika nchi yao kwa kupita njia nyingine isiyopita Yerusalemu.

Kwa namna hiyo hiyo Yusufu alipata onyo kwamba akimbilie Misri pamoja na Mariamu na mtoto. Na malaika alisema, "Ukae huko hata nikuambie; kwa maana Herode anataka kumtafuta mtoto amwangamize." Yusufu alitii bila kukawia, akaanza safari usiku kwa ajili ya usalama zaidi.

Kupitia kwa wale wenye hekima, Mungu alikuwa analiamsha taifa la Wayahudi kuhusu kuzaliwa kwa Mwana wake. Kuulizauliza kwao mle Yerusalemu, hisia za watu zilizoibuka, na hata wivu wa Herode, ambao ulilazimisha hata usikivu wa makuhani na marabi, vilielekeza mawazo ya watu katika unabii unaomhusu Masihi, na kwa tukio kuu ambalo lilikuwa limetokea.

**(65)** Shetani alijielekeza katika kuifungia nuru ya mbinguni isionekane ulimwenguni, na alitumia hila zilizopitiliza ili kumharibu Mwokozi. Lakini Yeye ambaye kamwe halali wala hasinzii alikuwa anamlinda Mwana wake mpendwa. Yeye ambaye aliwanyeshea Israeli mana kutoka mbinguni na kumlisha Eliya mnamo wakati wa njaa alipata hifadhi katika nchi ya kipagani kwa ajili ya Mariamu na mtoto Yesu. Na kwa kutumia zawadi za mamajusi kutoka katika nchi ya kipagani, Bwana aliwapatia mahitaji muhimu kwa ajili ya safari ya kwenda Misri na mahitaji ya kuishi katika nchi ya ugeni.

Mamajusi walikuwa miongoni mwa watu wa kwanza kumkaribisha Mkombozi. Zawadi zao ndizo zilizokuwa za kwanza kuwekwa miguuni pake. Na kupitia tunu zile, walipata heshima kiasi gani kwa huduma! Mungu anapenda kuheshimu sadaka itokayo katika moyo wa kupenda, akiipatia uwezo wa hali ya juu wa kutenda katika utumishi kwa ajili yake. Ikiwa tumempatia Yesu mioyo yetu, sisi pia tutamletea zawadi. Dhahabu zetu na fedha, mali zetu za dunia zenye thamani ya juu, vipaji vyetu vya kiakili na kiroho vya hali juu, vitatolewa bure kwake Yeye atupendaye, na aliyejitoa kwa ajili yetu.

Kule Yerusalemu Herode alisubiri kurudi kwa wenye hekima. Na muda ulipopita, bila wao kuonekana, alipatwa na wasiwasi. Ile hali ya marabi kukosa hiari ya kuonyesha mahali azaliwapo Masihi ilimwonyesha kwamba wameshagundua mpango wake, na ya kwamba mamajusi wale walikuwa wamemkwepa kwa makusudi. Alipatwa na wazimu kuhusu wazo hili. Mbinu ilikuwa imeshindwa, lakini alikuwa amesaliwa na azimio la kutumia nguvu. Angemfanya huyu mfalme mtoto kuwa kama hadithi tu. Wale Wayahudi wenye kiburi lazima waone kile ambacho wangetarajia katika azima yao ya kumweka mtawala wao kwenye kiti cha enzi.

Ghafla askari walipelekwa Bethlehemu. Nyumba zilizokuwa na amani za mji wa Daudi zikashuhudia matukio yale ya kutisha ambayo, miaka mia sita kabla yalikuwa yamefunuliwa kwa nabii. "Sauti ilisikiwa Rama, Kilio, na maombolezo mengi, Raheli akiwalilia watoto wake, Asikubali kufarijiwa, kwa kuwa hawako."

Wayahudi walikuwa wamejiletea janga hili juu yao wenyewe. Ikiwa wangekuwa wametembea kwa uaminifu na unyoofu mbele za Mungu, angeweza kutumia namna ya viashirio vya kuifanya ghadhabu ya mfalme isiwe na madhara kwao. Lakini walikuwa wamejitenga na Mungu kwa dhambi zao, na walikuwa wamemkataa Roho Mtakatifu, ambaye ndiye alikuwa kinga yao. Hawakuwa wamejifunza Maandiko ili kuendana na mapenzi ya Mungu. Walikuwa wamechunguza unabii ili ufasiriwe kwa lengo la kujitukuza wao, na kuonyesha jinsi Mungu alivyoyadharau mataifa mengine. Ilikuwa ni kwa sababu ya kujiona kiburi ya kwamba **(66)** Masihi ilikuwa aje kama mfalme, akishinda maadui zake, na kuwapondaponda wapagani katika ghadhabu yake. Hivyo ndivyo walivyokuwa wamejenga chuki ya watawala wao. Katika kutafsiri utume wa Kristo isivyo sahihi, Shetani alikuwa amelenga kutimiza uharibifu wa Mwokozi; lakini badala ya hili, yaligeuka juu ya vichwa vyao wenyewe.

Kitendo hiki cha ukatili kilikuwa moja ya vitendo vya mwisho vilivyotia giza utawala wa Herode. Muda mfupi baada ya mauaji ya wasio na hatia, yeye mwenyewe alilazimishwa kujisalimisha katika hatima ile ambayo haiwezekani kwa mtu yeyote kuisukumia kando. Alikufa kifo cha kuogofya.

Yusufu ambaye alikuwa bado yuko Misri, alielekezwa sasa na malaika wa Mungu kurudi katika nchi ya Israeli. Akichukulia kwamba Yesu atakuwa mrithi wa kiti cha Yakobo, Yusufu alitaka kupafanya Bethlehemu kuwa nyumbani pake pa kuishi; lakini baada ya kujua kuwa Arkelao alikuwa anamiliki Uyahudi mahali pa baba yake Herode, aliogopa kwamba mpango wa baba yake kuhusu Yesu ungetekelezwa na mwanaye huyo. Miongoni mwa wana wote wa Herode, Arkelao ndiye aliyefanana zaidi na baba yake katika tabia. Kurithi kwake utawala wa serikali kulikuwa tayari kumeleta ghasia Yerusalemu, na kwa mauaji ya maelfu ya Wayahudi yaliyofanywa na walinzi wa Kirumi.

Kwa mara nyingine Yusufu alielekezwa kwenda mahali salama. Alirudi Nazareti, nyumbani pake pa kabla, na hapa ndipo mahali ambapo Yesu aliishi kwa karibu miaka thelathini, "ili litimie neno lililonenwa na manabii, Ataitwa Mnazorayo." Galilaya ilikuwa chini ya utawala wa yule mwana wa Herode, lakini ilikuwa na mchanganyiko mkubwa zaidi wa wakazi wageni kuliko Uyahudi. **(67)** Kwa hiyo shauku ya watu katika mambo yanayohusiana na Wayahudi ilikuwa ndogo zaidi, na madai ya Yesu yangekuwa na uwezo mdogo wa kuamsha wivu wa wale waliokuwa madarakani.

Huo ndio uliokuwa ukaribisho wa Mwokozi pindi alipokuja duniani. Ilionekana kama hakukuwa na mahali pa kupumzika au pa salama kwa ajili ya mtoto mchanga aliye Mkombozi. Mungu hakumtegemeza Mwana wake mpendwa kwa wanadamu, hata wakati alipokuwa akiifanya kazi yake kwa ajili ya wokovu wao. Aliwapa malaika kazi ya kumchunga Yesu na kumlinda mpaka akamilishapo kazi yake duniani, na kufa akiuawa na mikononi ya wale aliokuja kuwaokoa.

## Sura ya 7

# Akiwa Mtoto

[Sura hii imejengwa katika Luka 2:39, 40.]

Utoto na ujana wa Yesu ulikuwa katika kijiji kidogo cha milimani. Kusingekuwa na sehemu yoyote duniani ambayo ingeacha kupenda kuheshimiwa kwa ule uwepo wake Yeye. Majumba ya wafalme yangekuwa yamependelewa katika kumpokea mgeni huyu. Lakini alizipita nyumba za wenye utajiri, majumba ya kifalme, na makazi maarufu ya wasomi, na kwenda kufanya makazi yake Nazareti mahali palipofichika na kudharauliwa.

Jambo la ajabu kwa umuhimu ni kumbukumbu fupi ya maisha yake ya awali: "Yule mtoto akakua, akaongezeka nguvu, amejaa hekima, na neema ya Mungu ilikuwa juu yake." Chini ya nuru ya jua ya uso wa Baba yake, Yesu "akazidi kuendelea katika hekima na kimo, akimpendeza Mungu na wanadamu." Luka 2:52. Akili yake ilifanya kazi sawasawa, akiwa na uwezo wa kufikiri na hekima iliyo zaidi ya umri wake. Lakini tabia yake ilikuwa nzuri katika usahihi wake. Uwezo wa akili na mwili uliendelea taratibu, kulingana na sheria za utoto.

Akiwa mtoto, Yesu alidhihirisha upendo usio wa kawaida wa namna yake. Mikono yake ya hiari ilikuwa tayari daima kuwatumikia wengine. Alidhihirisha uvumilivu **(69)** ambao usingeyumbishwa na kitu chochote, na ukweli ambao usingeweza kupoteza uadilifu. Kwenye msingi imara kama mwamba, maisha yake yalifunua neema ya upole usio na ubinafsi.

Kwa umakini mkubwa mama wa Yesu aliangalia maendeleo ya kufunguka kwa uwezo wa Yesu, na kuona ukamilifu wa tabia yake. Kwa furaha alijitahidi kuendeleza ile akili angavu na ijifunzayo haraka. Kwa njia ya Roho Mtakatifu alipata hekima ya kushirikiana na utendaji wa mbingu katika maendeleo ya mtoto huyu, ambaye alidai tu kwamba Mungu ndiye Baba yake.

Tangu nyakati za zamani waaminifu katika Israeli walijali sana elimu kwa vijana. Mungu alikuwa ameamuru kwamba watoto tangu hatua ya uchanga wafundishwe wema wa Mungu na ukuu wake, hasa kama yanavyofunuliwa katika sheria yake, na kuonyeshwa katika historia ya Israeli. Nyimbo na sala na masomo kutoka katika Maandiko yalipaswa yaingizwe katika akili zinazofunguka. Wababa na wamama walipaswa wafundishe watoto wao kwamba sheria ya Mungu ni udhihirisho wa tabia yake, na kwamba kadiri walivyopokea misingi ya sheria katika mioyo yao, sura ya Mungu ilionekana katika akili na nafsi. Mafundisho mengi yalikuwa ni kwa simulizi; lakini vijana pia walijifunza kusoma maandishi ya Waebrania; na Maandiko yaliyokuwa katika magombo ya Agano la Kale yalikuwa wazi kwa ajili yao kujifunza.

Mnamo zama za Kristo, mji mdogo au mkubwa ambao haukuwa na mahali pa kufundishia vijana mafunzo ya kidini ulichukuliwa kwamba una laana ya Mungu. Lakini mafundisho hayo yalikuwa yamekuwa rasmi. Kwa kiasi kikubwa mapokeo yalikuwa yamechukua nafasi ya Maandiko. Elimu ya kweli ingeweza kuwaongoza vijana "wamtafute Mungu, ingawa ni kwa kupapasa-papasa, wakamwone." Matendo 17:27. Lakini walimu wa Kiyahudi walijikita katika mambo ya maadhimisho. Mawazo yalijawa na vitu ambavyo havikuwa na thamani kwa wanaofundishwa, na vile ambavyo visingetambuliwa katika shule ya juu ya mbinguni. Uzoefu ambao unapatikana kupitia hali ya mtu kulipokea neno la Mungu haukuwa na sehemu katika mfumo ule wa elimu. Wakiwa wamemezwa katika mzunguko wa mambo ya pembeni tu, wanafunzi hawakupata muda wa utulivu wa kuwa na Mungu. Hawakusikia sauti ya Mungu ikizungumza na moyo. Katika kutafuta maarifa, waligeuka na kumwacha Yeye aliye Chanzo cha maarifa. Mambo muhimu ya huduma ya Mungu yalipuuzwa. Misingi ya sheria ilifunikwa. Kile kilichoangaliwa kama elimu bora ya hali ya juu ilikuwa ndicho kikwazo kikubwa cha maendeleo. Chini ya mafunzo ya marabi uwezo wa vijana ulikandamizwa. Mawazo yaliminywa na kuwa finyu.

**(70)** Mtoto Yesu hakupata mafunzo katika shule za masinagogi. Mama yake alikuwa mwalimu wake wa kwanza wa kibinadamu. Yesu alijifunza mambo ya kimbingu kutoka katika midomo ya mama yake na magombo ya maandishi ya manabii. Alikuwa sasa anafundishwa katika magoti ya mama yake maneno yale yale ambayo Yeye mwenyewe alikuwa ameyatamka kwa Musa. Kadiri alivyoendelea kutoka utoto kwenda ujana, hakutafuta kwenda katika shule za marabi. Hakuhitaji elimu ambayo ingepatikana kutoka katika vyanzo hivyo; maana Mungu ndiye aliyekuwa mkufunzi wake.

Swali lililoulizwa wakati wa huduma ya Yesu, "Amepataje huyu kujua elimu, ambaye hakusoma?" halina maana kwamba Yesu hakuwa na uwezo wa kusoma, bali kwamba hakupata elimu ya marabi. Yohana 7:15. Kwa kuwa uelewa wake uliendelea kuongeza kama tulivyo, ufahamu wake mkubwa wa Maandiko unaonyesha jinsi alivyotumia kwa bidii miaka yake ya awali katika kujifunza neno la Mungu. Na kile kilichokuwa kimetanda pande zake zote ilikuwa ni maktaba ya kazi zilizofanywa na Mungu. Yeye aliyekuwa ameumba vyote alikuwa anasoma masomo ambayo mikono yake mwenyewe ilikuwa imeandika katika dunia na bahari na anga. Mbali na njia za ulimwengu ambazo si takatifu, Yeye alikusanya mkusanyiko wa ujuzi wa kisayansi kutokana na maumbile ya asili. Alisoma kuhusu maisha ya mimea na wanyama, na maisha ya mwanadamu. Tangu miaka yake ya awali alikuwa na kusudi moja; aliishi kwa kuwabariki wengine. Kwa ajili ya hili alipata rasilimali katika vitu vya asili; mawazo mapya ya njia na mbinu yalimulika katika akili zake wakati alipokuwa akijifunza maisha ya mimea na wanyama. Muda wote alitafuta kupata vielelezo kutokana na vitu vilivyokuwa vinaonekana ili kuwasilisha maagizo ya Mungu yaliyo hai. Mifano aliyoitumia, wakati wa huduma yake, alipenda kuitumia kufundisha masomo ya kweli kuonyesha jinsi roho yake ilivyokuwa wazi kwa ushawishi wa asili, na jinsi alivyokuwa amekusanya mafundisho ya kiroho kutokana na mazingira yanayomzunguka.

Hivyo ndivyo umuhimu wa neno na kazi za Mungu zilivyofunuliwa kwa Yesu kadiri alivyojaribu kuelewa sababu ya vitu. Viumbe wa mbinguni walikuwa naye, na utamaduni wa kuwa na mawazo matakatifu na ushirika vilikuwa vyake. Tangu akili ilipoanza kutua kwake aliendelea kukua katika neema ya roho na ujuzi wa ukweli.

Kila mtoto anaweza kuongeza ufahamu kama ilivyokuwa kwa Yesu. Kadiri tunavyojaribu kumfahamu Baba yetu wa mbinguni kupitia neno lake, malaika watasogea karibu, akili zetu zitatiwa nguvu, tabia zetu zitainuliwa juu na kusafishwa. Tutakuwa kama Mwokozi wetu zaidi. Na kadiri tunavyotazama uzuri wa asili, hisia zetu za upendo zinamtafuta Mungu. Wakati roho inaposhangazwa, nafsi inajazwa nguvu kwa kukutana na Mwenyezi kupitia kazi zake. Ushirika na Mungu kupitia **(71)** maombi huendeleza uwezo wa kiakili na kimaadili, na uwezo wa kiroho huimarika kadiri tunavyopalilia mawazo katika mambo ya kiroho.

Maisha ya Yesu yalikuwa yanapatana na Mungu. Wakati alipokuwa mtoto, alifikiri na kuongea kama mtoto; lakini hakuna chembe ya dhambi iliyochafua sura ya Mungu ndani yake. Lakini hakuachwa huru dhidi ya majaribu. Wakazi wa Nazareti walikuwa mashuhuri kwa uovu. Makadirio ya chini ya hali waliyokuwa nayo yanaonyeshwa na swali la Nathanaeli, "Laweza neno jema kutoka Nazareti?" Yohana 1:46. Yesu aliwekwa mahali ambapo tabia yake ingejaribiwa. Ilikuwa muhimu kwake kuendelea kujichunga ili ahifadhi usafi wake. Hakuwa huru na migogoro ambayo tunapaswa kukutana nayo, kusudi awe kielelezo kwetu katika utoto, ujana na utu uzima.

Shetani hakuchoka katika jitihada zake za kutafuta kumshinda yule Mtoto wa Nazareti. Tangu katika miaka yake ya awali Yesu alilindwa na malaika wa mbinguni, lakini bado maisha yake yalikuwa ya mapambano dhidi ya nguvu za giza wakati wote. Kwamba ni lazima duniani kuwe na maisha ya mmoja ambayo hayana uchafu wa uovu ilikuwa ni kosa na mfadhaiko kwa mfalme wa giza. Hakuna mbinu yoyote aliyoacha bila kuijaribu ili kumnasa Yesu. Hakuna mtoto wa kibinadamu ambaye ataitwa kuishi maisha matakatifu katikati ya misukosuko mikali na majaribu kama ilivyokuwa kwa Mwokozi wetu.

**(72)** Wazazi wa Yesu walikuwa maskini, na waliishi kwa kutegemea kazi ngumu za kila siku. Alikuwa mtu ajuaye umaskini, kujikana, na ufukara. Uzoefu huu ulikuwa kinga yake. Katika maisha ya kazi za uzalishaji hakukuwa na muda wa kukaa bila kazi ambao ungekaribisha majaribu. Hakuna wakati usio na makusudi ambao ungefungulia mlango wa kujihusisha na mambo mabaya. Kwa kiasi kikubwa iwezekanavyo, alifunga mlango wa mjaribu kuingilia. Kutafuta faida au raha, kusifiwa kwa kupigiwa makofi au kupongezwa, havikuweza kumvuta kukubaliana na kitendo chochote kibaya. Alikuwa na busara ya kubaini uovu, na alikuwa na nguvu ya kuupinga.

Kristo ndiye pekee aliyepata kuishi duniani bila dhambi; lakini bado aliishi miongoni mwa wakazi wenye dhambi kule Nazareti. Hali hii ni kemeo kwa wale wanaojidhania kwamba wataishi maisha yasiyolaumika kutegemeana na mahali wanapoishi, mafanikio ya mali, au ustawi. Majaribu, umaskini, maisha ya shida ndiyo nidhamu inayohitajika kwa ajili ya kuendeleza usafi wa maisha na uimara.

Yesu aliishi nyumbani kwa mkulima, na kwa uaminifu na furaha alifanya iliyo sehemu yake katika kubeba mzigo wa familia. Alikuwa amekuwa amiri jeshi mkuu wa mbinguni, na malaika walikuwa wamefurahia kutekeleza maagizo yake; sasa alikuwa kijana mtumishi, mwenye kupenda, na mtii kwa hiari. Alijifunza ufundi, na kwa

mikono yake alifanya kazi katika karakana ya fundi seremala akiwa pamoja na Yusufu. Akiwa katika mavazi ya kawaida ya mtu afanyaye kazi ngumu alitembea katika mitaa ya mji ule mdogo, akienda kufanya kazi yake ile ya hali ya chini na kurudi. Hakutumia nguvu zake za kimbingu kupunguza uzito wa mizigo yake au kurahisisha ugumu wa kazi yake.

Kadiri Yesu alivyofanya kazi wakati wa utoto wake, mwili na akili viliendelezwa. Hakutumia nguvu zake za mwili kizembe, bali katika namna inayomfanya awe na afya, ili kwamba apate kufanya kazi njema zaidi katika kila njia. Hakupenda kuwa na mapungufu, hata katika kutunza vitendea-kazi. Alikuwa mkamilifu katika kazi, kama alivyokuwa mkamilifu katika tabia. Kwa kielelezo chake alitufundisha kwamba tuna wajibu wa kujishughulisha, kwamba kazi yetu inapaswa ifanywe kwa usahihi na ukamilifu, na ya kwamba utumishi kama huo ni wa kuheshimika. Mazoezi yanayoifundisha mikono kutumika na kuwafundisha vijana kubeba sehemu yao ya mizigo ya maisha yanaleta nguvu za mwili, na yanakuza kila uwezo. Wote wanapaswa kutafuta kitu cha kufanya ambacho kitakuwa na manufaa kwao na kuwa na msaada kwa wengine. Mungu aliamuru kufanya kazi kama mbaraka, na yule tu afanyaye kazi kwa bidii ndiye anayepata utukufu na furaha ya kweli katika maisha. Ukubali wa Mungu uko katika kuwapenda watoto na vijana ambao kwa furaha wanashiriki katika majukumu ya nyumbani, wakishiriki kubeba mzigo wa baba na mama. Watoto kama hao watatoka nyumbani kwenda kuwa watu wenye msaada katika jamii.

**(73)** Katika maisha yake yote duniani, Yesu alikuwa mtu wa kufanya kazi kwa bidii. Alitarajia mengi; na kwa hiyo alijaribu kufanya mengi. Baada ya kuingia katika huduma yake, alisema, "Imetupasa kuzifanya kazi zake yeye aliyenipeleka maadamu ni mchana, usiku waja asipoweza mtu kufanya kazi." Yohana 9:4. Yesu hakukwepa kutunza na wajibu, kama wanavyofanya wengi wanaodai kuwa wafuasi wake. Wengi ni wadhaifu na wazembe kwa sababu wanatafuta kukwepa utaratibu huu. Wanaweza kuwa na vipaji vya thamani na vinavyofaa, lakini wanakosa ujasiri na kutokuwa na msaada wakati mambo magumu yanapopaswa kufanywa au pale vikwazo vinapoibuka. Mwelekeo chanya na uwezo, uimara na nguvu ya tabia, vilivyodhihirishwa katika Kristo vinapaswa vikuzwe ndani yetu, kupitia nidhamu ile ile aliyostahimili. Na neema ile aliyopata ni kwa ajili yetu.

Maadamu aliishi miongoni mwa wanadamu, Mwokozi wetu alishiriki sehemu kubwa ya maskini. Alijua kwa uzoefu kujali kwao na ugumu wa maisha, na aliwafariji na kuwatia moyo wote waliofanya kazi kwa unyenyekevu. Wale ambao wana uelewa wa kweli wa mafundisho yaliyo katika maisha yake hawatahisi kamwe kwamba lazima kuwe na utenganisho baina ya matabaka ya watu, kwamba matajiri wanapaswa kuheshimiwa kuliko maskini wastahimilivu.

Yesu alifanya kazi yake kwa furaha na pasipo makosa. Ilihitaji ustahimilivu na hali ya kiroho ya kiwango cha juu kuileta dini ya Biblia katika maisha ya nyumbani na kazini katika karakana, kukabiliana na shida za shughuli za kidunia, na bado kukaza macho kuelekea kwenye utukufu wa Mungu. Hapa ndipo mahali ambapo Kristo alikuwa msaada. Kamwe hakuwa mtu aliyejawa na huruma za kujali kwa mambo ya ulimwengu tu kiasi cha kutokuwa na muda au mawazo kwa ajili ya mambo ya mbinguni. Mara nyingi alidhihirisha furaha ya moyo wake kwa kuimba zaburi na nyimbo za kimbingu. Mara nyingi wakazi wa Nazareti walisikia sauti za kusifu na za shukrani kwa Mungu. Alikuwa na ushirika na mbingu katika wimbo; na pindi wafanya-kazi wenzake walipolalamika kuchoka katika kazi, waliburudishwa na sauti tamu ya muziki uliotoka midomoni mwake. Nyimbo zake za sifa zilionekana kuwaondosha malaika waovu, na, kama uvumba uliofukizwa, zilijaza mahali pale harufu nzuri. Mawazo ya watu waliomsikia yalipandishwa kutoka katika mambo ya kidunia, na kupelekwa nyumbani pa juu mbinguni.

**(74)** Yesu alikuwa chemchemi ya neema iponyayo kwa ajili ya ulimwengu; na katika miaka yote ile iliyofichika kule Nazareti, maisha yake yalitiririka katika mikondo ya huruma na wema. Walio vikongwe, wenye huzuni, na waliolemewa na dhambi, watoto wanaocheza katika hali ya furaha isiyo na hatia, viumbe wadogo mstuni, wanyama wavumilivu wabebao mizigo, - wote walikuwa na furaha kubwa kwa uwepo wake. Yeye ambaye neno lake lenye uwezo linayashikilia malimwengu angeinama ili kutuliza maumivu ya ndege aliyejeruhiwa. Hakukuwa na kitu chochote ambacho kilikuwa chini kupita mahali anapoweza kukijali, hakuna kitu ambacho aliacha kukihudumia.

Kwa hiyo kadiri alivyokua katika hekima na umbo, Yesu aliongezeka katika kumpendeza Mungu na mwanadamu. Alivuta huruma za mioyo yote kwa kuonyesha kwamba Yeye mwenyewe aliweza kuwahurumia wote. Mazingira ya tumaini na kutia moyo yaliyomzunguka yalimfanya kuwa baraka katika kila nyumba. Na mara kwa mara

katika sinagogi siku ya Sabato aliitwa ili kusoma somo kutoka kwa manabii, na mioyo ya wasikilizaji ilisisimshwa kadiri nuru mpya ilivyoangaza katika maneno yaliyokuwa yanajulikana ya maandiko yaliyotukuka.

Lakini bado Yesu alijiepusha na hali ya kufanya maonyesho. Katika miaka yote ya kukaa kwake Nazareti, hakufanya maonyesho yoyote ya uwezo wake wa miujiza. Hakutafuta nafasi ya hadhi ya juu wala hakukalia cheo chochote. Maisha yake ya kimya na mepesi, hata na ukimya wa Maandiko kuhusu miaka yake ya awali, vinatufundisha somo muhimu. Kwa kadiri maisha ya mtoto yanavyokuwa yaliyotulia na mepesi, - kwa kadiri yanavyokuwa mbali na misisimko ya bandia, na kwa kadiri yanavyoendana zaidi na hali ya asili, - ndivyo yanavyofaa kuleta nguvu za mwili na akili na kwa ajili ya uimara kiroho.

Yesu ni kielelezo chetu. Wapo wengi ambao wanajikita kwa hamu katika kipindi cha huduma yake ya hadhara, wakati wanayapita mafundisho ya miaka yake ya awali pasipo kuyazingatia. Lakini ni maisha yake ya nyumbani ambayo yanatoa kielelezo kwa ajili ya watoto na vijana wote. Mwokozi alijishusha katika umaskini, ili kwamba afundishe namna tunavyoweza kwa karibu kutembea na Mungu kwa unyenyekevu mkubwa. Aliishi akimpendeza, akimheshimu, na kumtukuza Baba yake katika mambo ya kawaida ya maisha. Kazi yake ilianza kwa kutukuza fani ya hali duni ya mafundistadi ambao wanafanya kazi ngumu kwa ajili ya mkate wao wa kila siku. Alipokuwa akifanya kazi ngumu kwenye benchi la fundi seremala alikuwa anafanya kazi ya Mungu kama vile alivyokuwa akitenda miujiza kwa makutano. Na kila kijana anayefuata mfano wa Yesu wa uaminifu na utiifu mahali pa nyumbani kwake pa hali duni anaweza kudai atamkiwe maneno yale ambayo Yesu alitamkiwa na Baba kwa njia ya Roho Mtakatifu, kwamba "Tazama mtumishi wangu nimtegemezaye; mteule wangu, ambaye nafsi yangu imependezwa naye." Isaya 42:1.

## Sura ya 8

# Kuhudhuria Pasaka

[Sura hii imejengwa katika Luka 2:41-51.]

Katika jamii ya Wayahudi mwaka wa kumi na mbili ulikuwa ndio umri unaoweka mpaka kati ya kipindi cha utoto na cha ujana. Akishakamilisha mwaka huu mvulana wa Kiebrania aliitwa mwana wa sheria, na pia mwana wa Mungu. Alipewa fursa maalum kwa ajili ya mafundisho ya dini, na alitarajiwa kushiriki katika sikukuu takatifu na maadhimisho. Kwa mujibu wa desturi hizi Yesu katika uvulana wake aliienda kwenye Pasaka kule Yerusalemu. Kama ilivyokuwa kwa Waisraeli wote wenye kuzingatia mambo, Yusufu na Mariamu walienda kule kila mwaka kuhudhuria Pasaka; na wakati Yesu alipotimiza umri uliotakiwa, walimchukua wakaenda naye.

Kulikuwa na sikukuu tatu, Pasaka, Pentekoste, na Sikukuu ya Makambi, ambazo kwa hizo wanaume wote wa Israeli waliamriwa kujihudhurisha mbele za Bwana kule Yerusalemu. Miongoni mwa sikukuu hizi, Pasaka ndiyo iliyohudhuriwa zaidi. Walikuwepo watu wengi kutoka maeneo mbalimbali ya nchi ambako Wayahudi walitawanyika. Waabudu walikusanyika kutoka kila sehemu ya Palestina. Safari ya kutoka Galilaya ilichukua siku kadhaa, na wasafiri waliungana katika makundi makubwa kwa ajili ya kushirikiana kwa safari na usalama. Wanawake na wanaume wazee walipanda farasi katika barabara zile zenye **(76)** mitelemko mikali na miamba. Wanaume wenye nguvu na vijana walisafiri kwa mguu. Wakati wa pasaka ulikuwa sawa na mwishoni mwa Mwezi Machi au mwanzoni mwa Mwezi Aprili, na nchi yote iling'aa kwa maua, na ilifurahisha kwa nyimbo za ndege. Katika njia yote kulikuwa na alama za kukumbukwa katika historia ya Israeli, na wababa na wamama waliwasimulia watoto wao maajabu amabayo Mungu alikuwa amefanya kwa watu wake wa vizazi vilivyopita. Walijiliwaza safarini mwao kwa nyimbo na muziki, na hatimaye mnara wa Yerusalemu ulipoonekana kwao, kila sauti ilijiunga katika wimbo wa ushindi, -

"Miguu yetu imesimama Ndani ya malango yako, Ee Yerusalemu. . . .
Amani na ikae ndani ya kuta zako, Na kufanikiwa ndani ya majumba yako."
Zaburi 122: 2-7.

Maadhimisho ya Pasaka yalianza na kuzaliwa kwa taifa la Waebrania. Katika usiku wa mwisho wa utumwa wao nchini Misri, wakati ambapo hakukutokea **(77)** dalili ya kuokolewa, Mungu aliwaamuru wajiandae kwa ukombozi haraka. Alikuwa amemwonya Farao kuhusu hukumu ya mwisho juu ya Wamisri, na aliwaelekeza Waebrania wakusanye jamaa zao katika makazi yao. Wakiwa wamenyunyizia damu ya mwana-kondoo aliyechijwa katika miimo ya milango, walitakiwa wamle yule kondoo, akiwa ametokoswa, pamoja na mikate isiyotiwa chachu na mimea michungu. Alisema, "Tena mtamla hivi, mtakuwa mmefungwa viuno vyenu, mmevaa viatu vyenu miguuni, na fimbo zenu mikononi mwenu; nanyi mtamla kwa haraka; ni pasaka ya Bwana." Kutoka 12:11. Wakati wa usiku wa manane wazaliwa wa kwanza wote wa Misri waliuawa. Ndipo mfalme akawapelekea Waisraeli ujumbe, "Ondokeni tokeni katika watu wangu, . . . enendeni, kamtumikieni Bwana kama mlivyosema." Kutoka 12:31. Waebrania walitoka Misri wakiwa taifa huru. Bwana alikuwa ameamuru kwamba Pasaka iadhimishwe kila mwaka. Alisema, "Kisha itakuwa hapo watoto wenu watakapowauliza, N'nini maana yake utumishi huu kwenu? Ndipo mtawaambia, Ni dhabihu ya pasaka ya Bwana, kwa kuwa alipita juu ya nyumba za wana wa Israeli huko Misri, hapo alipowapiga Wamisri." Hivyo kutoka kizazi hata kizazi kisa cha ukombozi huu wa ajabu kingerudiwa.

Pasaka ilifuatiwa na siku saba za sikukuu ya mikate isiyotiwa chachu. Mnamo siku ya pili ya sikukuu, malimbuko ya mavuno ya mwaka, mganda wa shayiri, ulitolewa mbele za Bwana. Maadhimisho yote haya yalikuwa mfano wa kazi za Yesu. Kutolewa kwa Israeli kutoka Misri kulikuwa ni somo la kielelezo la ukombozi, ambalo lingewekwa katika kumbukumbu kwa njia ya Pasaka. Mwana-kondoo aliyechinjwa, mikate isiyotiwa chachu, mganda wa malimbuko, vilimwakilisha Mwokozi.

Miongoni mwa wengi mnamo siku zile za Kristo, maadhimisho ya sikukuu hii yalikuwa yamegeuka kuwa mazoea. Lakini sikukuu hii ilikuwa na maana gani kwa Mwana wa Mungu!

**(78)** Kwa mara ya kwanza mtoto Yesu aliliangalia hekalu. Aliwaona makuhani waliovalia kanzu nyeupe wakihudumu kwa dhati. Alimtazama mnyama wa kafara aliyekuwa akichuruzika damu juu ya madhabahu. Aliinama na kusali pamoja na waliokuwa wanaabudu, wakati wingu la moshi lililotoka kwenye uvumba lilipopanda mbele za Mungu. Alishuhudia kaida za kidini zenye mguso zilizofanyika katika huduma ya pasaka. Siku kwa siku aliona maana yake kwa uwazi zaidi. Kila tendo lilionekana kufungamanishwa na maisha yake. Msukumo mpya ulikuwa unaamshwa ndani yake. Akiwa kimya na mwenye kuzama katika mawazo, alionekana kujifunza tatizo kuu. Siri ya kazi yake iliyomleta ilikuwa inamfungukia Mwokozi.

Akiwa amegubikwa na fikira za matukio haya, hakuendelea kuwa karibu na wazazi wake. Alitafuta kuwa peke yake. Wakati huduma ya pasaka ilipoisha, aliendelea kuwa katika viwanja vya hekalu; na wakati waabudu walipotawanyika kutoka Yerusalemu, aliachwa pale.

Katika kwenda Yerusalemu, wazazi wa Yesu walitamani kumwunganisha na walimu wakuu katika Israeli. Wakati alikuwa mtiifu kwa kila namna kwa neno la Mungu, hakufungamana na desturi na tabia za marabi. Yusufu na Mariamu walidhani kwamba huenda angeongozwa kuwaheshimu marabi wasomi, na kusikiliza matakwa yao. Lakini kule hekaluni Yesu alikuwa anafundishwa na Mungu. Kile ambacho alikuwa amekipata, alianza mara moja kukifundisha.

Wakati ule chumba kimoja ambacho kimeungana na hekalu kilikuwa kimefanywa rasmi kuwa shule ya kidini, ikifuata utaratibu wa shule za manabii. Hapa ndipo marabi viongozi na wanafunzi wao walipokusanyikia, na hapa ndipo Yesu alipokuja. Akikaa miguuni pa hawa wasomi waliobobea, alisikiliza mafundisho yao. Kama mtu anayeitafuta hekima, aliwahoji walimu hawa kuhusu manabii, na kwa matukio yaliyokuwa yanatokea yakielekeza kwa ujio wa Masihi.

Yesu alijiweka kama mtu mwenye kiu ya maarifa ya Mungu. Maswali yake yalikuwa yanapendekeza ukweli wa kina ambao ulikuwa umefunikwa, lakini ambayo ilikuwa muhimu kwa wokovu wa roho. Wakati akionyesha jinsi hekima ya wenye hekima wale ilivyokuwa finyu na juu juu tu, kila swali liliwaletea fundisho la kimbingu, na liliweka ukweli katika mtazamo mpya. Marabi waliongelea ufunuo wa ajabu ambao ungeletwa na kuja kwa Masihi kwa taifa la Wayahudi; lakini Yesu aliwasilisha unabii wa Isaya, na aliwauliza maana ya maandiko yale yanayoelekeza katika mateso na kifo cha Mwana-kondoo wa Mungu.

Wale madaktari wasomi walimgeukia kwa kumwuliza maswali, na walishangazwa na majibu yake. Akiwa na unyenyekevu wa mtoto alirudia maneno **(79)** ya Maandiko, akiyapa maana ya kina ambayo ilikuwa haijapata kueleweka kwa wenye hekima wale. Kama ungefuatwa, mnyororo wa ukweli ule ulioonyeshwa naye ungeyaongoza matengenezo katika dini ya wakati ule. Hamu ya kina katika mambo ya kiroho ingeamshwa; na wakati ambapo Yesu angeanza huduma yake, wengi wangekuwa wameandaliwa kumpokea.

**(80)** Marabi walijua kwamba Yesu hakuwa amefundishwa katika shule zao; lakini uelewa wake wa unabii ulizidi ule wa kwao kwa mbali. Ndani ya mvulana huyu wa Galilaya walibaini ahadi kuu. Walitamani kumpata awe mwanafunzi wao, ili ya kwamba baadaye awe mwalimu katika Israeli. Walitaka kuwa na mamlaka juu ya elimu yake, wakihisi kwamba ni lazima elimu iletwe chini ya malezi yao.

Maneno ya Yesu yaliwapa msukumo ambao haujawahi kusababishwa na maneno yaliyotoka midomoni mwa mtu yeyote. Mungu alikuwa anatafuta kuwapa nuru wale viongozi wa Israeli, na alitumia mbinu pekee ambayo ingewezesha kuwafikia. Kwa kiburi chao wangekataa kukubali kupokea mafundisho kutoka kwa mtu yeyote. Ikiwa Yesu angeonekana kama anawafundisha, wangekataa kumsikiliza. Walijisifu kwamba wao ndio waliokuwa wanamfundisha Yeye, au lau kwamba walikuwa wakijaribu waone ufahamu wake wa Maandiko. Unyenyekevu wa ujana na neema ya Yesu uliyashinda mafikirio yao. Bila kutarajia mawazo yao yalifunguka katika neno la Mungu, na Roho Mtakatifu aliongea na mioyo yao.

Hakuna walichoona isipokuwa kwamba matarajio yao kuhusu Masihi hayakuungwa mkono na unabii; lakini hawakuweza kuachana na nadharia ambazo zilikuwa katika dhamira zao. Hawakuweza kukiri kwamba walikuwa hawaelewi mambo ambayo walidai kufundisha. Waliuzana wao kwa wao kwamba, Huyu kijana amepataje ufahamu huu, wakati hakusoma? Nuru ilikuwa inaangaza gizani; lakini "giza halikuiweza." Yohana 1:5.

Baada ya muda mfupi tu Yusufu na Mariamu walikuwa katika maumivu na kuchanganyikiwa. Wakati walipoondoka Yerusalemu hawakumwona Yesu, na hawakujua kwamba amebaki nyuma. Wakati ule mahali pale kulikuwa na watu wengi sana, na msafara kutoka Galilaya ulikuwa mkubwa. Kulikuwa na kuchanganyikiwa kwingi wakati walipokuwa wakiondoka mjini. Raha ya kutembea na marafiki huko njiani na mwitikio wa kufahamu mambo vilizamisha mawazo yao, na hawakugundua kutokuwepo kwake mpaka usiku ulipoingia. Sasa walipofanya kituo ili kupumzika, walikosa mkono wa msaada wa mtoto wao. Wakidhani kwamba yuko katikati ya watu pale, hawakufadhaishwa na kitu. Akiwa mdogo kama alivyokuwa, walikuwa wamemwamini kabisa, wakitarajia kwamba akihitajika, angekuwa tayari kuwasaidia, akikidhi matakwa yao kama ambavyo alikuwa akifanya. Lakini sasa hofu uliingia kwao. Walimtafuta kote katika kundi lililokuwepo, lakini hawakufanikiwa. Kwa kutetemeka walikumbuka jinsi ambavyo Herode alikuwa amejaribu kumwua wakati akiwa bado mtoto mchanga. Giza lilijaza mioyo yao. Kwa uchungu walijilaumu wao wenyewe.

**(81)** Walirudi Yerusalemu na kuanza kumtafuta. Siku iliyofuata, walipojichanganya na wanaoabudu hekaluni, walivutwa na sauti wanayoifahamu. Wasingeikosea; hakuna sauti nyingine iliyokuwa kama ya Yesu, iliyokuwa nzito na makini, ikiwa sauti ya kuvutia.

Walimkuta Yesu katika shule ya marabi. Wakiwa na furaha sana, hawakusahau majonzi na shida waliyopata. Alipokuwa nao tena, mama alisema, kwa maneno yaliyoonyesha kukemea, "Mwanangu, mbona umetutenda hivi? Tazama, baba yako na mimi tulikuwa tukikutafuta kwa huzuni."

"Kwani kunitafuta?" Yesu alijibu. "Hamkujua ya kuwa imenipasa kuwamo katika nyumba ya Baba yangu?" Na kadiri walivyoonekana kutokuelewa maneno yake, alielekeza kidole chake juu. Usoni mwake kulikuwa na nuru iliyowashangaza. Uungu ulikuwa ukiwaka ndani ya ubinadamu. Wakati walipomkuta hekaluni, walikuwa wamesikia maneno yaliyokuwa yakibadilishanwa kati yake na marabi, na walishangazwa na maswali yake na majibu yake. Maneno yake yalianzisha mtiririko wa mawazo ambao usingesahaulika kamwe.

Na swali lake kwao lilikuwa na somo. "Hamkujua ya kuwa imenipasa kuwamo katika nyumba ya Baba yangu?" alisema. Yesu alikuwa katika kazi ile ambayo amekuja ulimwenguni kuifanya; lakini Yusufu na Mariamu walikuwa wamepuuza kazi yao. Mungu alikuwa amewaonyesha heshima ya juu kwa kuwakabidhi Mwana wake. Malaika watakatifu walikuwa wameongoza njia ya Yusufu ili kuhifadhi maisha ya Yesu. Lakini kwa siku nzima walikuwa wamekosa kumwona Yeye ambaye hawakupaswa kumsahau hata kwa muda mfupi. Na wakati huzuni yao ilipoondoshwa, hawakuwa wamejirudi, bali walikuwa wameelekeza lawama kwake.

Lilikuwa jambo la kawaida kwa wazazi wa Yesu kumtafuta kama mtoto wao. Alikuwa nao kila siku, maisha yake yalikuwa kama ya watoto wengine katika mambo mengi, na ilikuwa ngumu kwao kumwona kama Mwana wa Mungu. Walikuwa katika hatari ya kushindwa kutambua mbaraka waliopewa katika uwepo wa Mkombozi. Huzuni ya kutengwa kwao mbali naye, na kemeo la upole ambalo lilikuwa katika maneno yake, vilipangwa ili kuwasukumia katika tumaini lao takatifu.

Katika jibu lililotolewa kwa mama yake, Yesu alionyesha kwa mara ya kwanza kwamba alijua uhusiano wake na Mungu. Kabla ya kuzaliwa kwake malaika alikuwa amemwambia Mariamu, "Huyo atakuwa mkuu, ataitwa Mwana wa Aliye juu, na Bwana Mungu atampa kiti cha enzi cha **(82)** Daudi, baba yake. Ataimiliki nyumba ya Yakobo hata milele." Luka 1:32, 33. Mariamu alikuwa ametafakari maneno haya moyoni mwake; lakini wakati aliamini kwamba mtoto wake angekuwa Masihi wa Israeli, hakuelewa utume wake. Sasa hakuelewa maneno yake; lakini alijua kwamba Yesu alikuwa amekana kuwa wa uzao wa Yusufu, na alikuwa ametangaza jinsi alivyo Mwana wa Mungu.

Yesu hakupuuza uhusiano wake na wazazi wake wa kidunia. Kutoka Yerusalemu alirudi nao, na aliwasaidia katika maisha yao ya masumbufu. Alificha moyoni mwake siri ya utume wake, akisubiri kwa unyenyekevu wakati ulioamuriwa wa Yeye kuingia katika kazi yake. Kwa miaka kumi na minane baada ya Yeye kutambua kwamba ni Mwana wa Mungu, alitambua kifungo kilichomfunga na nyumbani kule Nazareti, na alifanya majukumu ya mwana, kaka, rafiki, na raia.

Kadiri utume wa Yesu ulivyofunguka kwake kule hekaluni, aliacha kuwa pamoja na makutano. Alitamani kurudi kutoka Yerusalemu kimya kimya, pamoja na wale waliojua siri ya maisha yake. Kwa kutumia huduma ya pasaka, Mungu alitaka kuwaita watu wake wakae mbali na kuhangaikia mambo ya kidunia, na kuwakumbusha kuhusu

kazi yake ya ajabu katika kuwakomboa kutoka Misri. Katika kazi hii alitaka waone ahadi ya ukombozi kutoka dhambini. Kama vile damu ya mwana-kondoo aliyechinjwa ilivyokinga nyumba za Waisraeli, ndivyo ambavyo damu ya Kristo ingeokoa nafsi zao; lakini wangeokolewa na Kristo ikiwa tu kwa imani watayafanya maisha yake kuwa yao. Kulikuwa na uzuri katika huduma ile ya kivuli pale tu ilipowaelekeza waamini kwa Kristo kama mwokozi wao. Mungu alipenda kwamba waongozwe katika kujifunza kwa maombi na kicho kuhusu utume wa Kristo. Lakini kadiri makutano walivyoondoka Yerusalemu, hamasa ya safari na mahusiano ya kijamii vilizamisha utayari wao, na huduma waliyokuwa wameshuhudia ikasahauliwa. Mwaokozi hakuvutiwa kwenda nao.

Kadiri ambavyo Yusufu na Mariamu wangekuwa wanarudi kutoka Yerusalemu peke yao wakiwa na Yesu, alitarajia kuelekeza mawazo yao kwa Mwokozi anayepatwa na mateso. Alitafuta kumlika huzuni za mama yake kuelekea Kalvari. Alikuwa akimfikiria sasa. Mariamu alikuwa ashuhudie mateso ya Yesu ya mwisho, na Yesu alitaka mama huyu ajue utume wake, ili ya kwamba atiwe nguvu kustahimili, wakati upanga utakapopenya moyo wa mama huyu. Kama vile ambavyo Yesu alikuwa ametengwa naye, na alikuwa amemtafuta akiwa na huzuni kwa siku tatu, ndivyo ambavyo angempotea tena kwa siku tatu, wakati atakapotolewa kwa ajili ya dhambi za ulimwengu. Na vile ambavyo angefufuka kutoka kaburini, huzuni yake ingegeuka tena kuwa furaha. Lakini angeweza vizuri zaidi **(83)** kustahimili fadhaa ya kifo cha Yesu ikiwa angekuwa ameelewa Maandiko ambayo Yeye alikuwa anajaribu kuelekeza mawazo ya mama yake kwayo!

Ikiwa Yusufu na Mariamu wangeweka mawazo yao kwa Mungu kwa kujitoa na maombi, wangeelewa utakatifu wa tumaini lao, na wasingepotelewa na Yesu. Kwa upuuzi wa siku moja tu walimpoteza Yesu; lakini iliwagharimu siku tatu za huzuni wakimtafuta. Hivyo ndivyo ilivyo kwetu; kwa mazungumzo yasiyo maana, kuongea maovu, au kupuuza maombi, tunaweza tukapoteza uwepo wa Mwokozi ndani ya siku moja, na inaweza kuchukua siku nyingi za huzuni za kumtafuta, ili kupata tena amani ambayo tunakuwa tumepoteza.

Kwa mashirikiano yetu miongoni mwetu, tunapaswa tujihadhari tusimsahau Yesu, na kwenda bila kuzingatia mawazoni kwamba hayuko nasi. Wakati tunapokuwa tumemezwa katika mambo ya dunia mpaka tunakosa kufikiri kuhusu Yeye ambaye ndani yake kuna tumaini letu la milele, tunajitenga na Yesu na malaika wa mbinguni. Viumbe hawa watakatifu hawawezi kubaki mahali ambapo Mwokozi hatakiwi, au ambapo hapana dalili za kuwepo kwake. Hii ndiyo sababu kukata tamaa mara nyingi kuko miongoni mwa wale wanaodaiwa kuwa wafuasi wa Kristo.

Wengi huhudhuria ibada za kidini, na wanafurahishwa na kufarijiwa na neno la Mungu; lakini kwa kupuuza kuzingatia, kukesha, na maombi, wanapoteza mbaraka, na kujikuta wamepungua zaidi kuliko kabla. Mara nyingi wanahisi kwamba Mungu amewatendea vibaya. Hawaoni kwamba makosa ni yao. Kwa kujitenga na Yesu, wamefungia mbali nuru ya uwepo wake.

Ingekuwa vema kwetu kutumia saa moja kila siku kutafakari maisha ya Kristo. Lazima tuyaangalie hatua kwa hatua, na hebu mawazo yetu yaangalie kila tukio, hasa yale ya mwisho-mwisho. Kadiri tunavyojikita kwenye kafara yake kuu kwa ajili yetu, ujasiri wetu ndani yake utadumishwa, upendo wetu utaharakishwa, na tutazamishwa katika kina cha roho yake. Ikiwa tunahitaji kuokolewa hatimaye, lazima tujifunze somo la toba na unyenyekevu chini ya msalaba.

Kadiri tunavyoshiriki pamoja, tunaweza kuwa baraka kwa mtu na mwingine. Ikiwa ni wa Kristo, mawazo yetu matamu zaidi yatakuwa yanayomhusu Yeye. Lazima tupende kuongea habari zake; na kadiri tunavyozungumza kuhusu upendo wake, mioyo yetu italainishwa na ushawishi wa kimbingu. Kwa kuangalia uzuri wa tabia yake, tutabadilishwa tufanane na mfano uo huo, toka utukufu hata utukufu." 2 Wakorintho 3:18.

**Sura ya 9**

# Siku za Mgongano

Tangu miaka yake ya mapema mtoto wa Kiyahudi alizungukwa na maagizo ya marabi. Taratibu ngumu ziliwekwa kwa ajili ya kila tendo, hata lile lililo dogo kabisa maishani. Chini ya walimu wa sinagogi vijana walifundishwa kanuni zisizohesabika amabazo walipaswa kufuata kama Waisraeli wanaoshikilia utamaduni wao. Lakini Yesu hakujihusisha na mambo hayo. Tangu utoto wake alifanya mambo akiwa huru bila kuongozwa na sheria za marabi. Maandiko ya Agano la Kale yalikuwa kitu chake cha kujifunza wakati wote, na maneno, "Hivi ndivyo asemavyo Bwana," yalikuwa midomoni mwake.

Kadiri hali ya watu ilivyoanza kufunguka katika fahamu zake, aliona kwamba matakwa ya jamii na yale ya Mungu yalikuwa katika mgongano wakati wote. Watu walikuwa wanaenda mbali na neno la Mungu, na walikuwa wakishikilia nadharia walizoibua wenyewe. Waliadhimisha desturi za mapokeo ambazo hazikuwa na uadilifu ndani yake. Ibada zao zilikuwa ni mlolongo tu wa kufuata utaratibu; ukweli mtakatifu ambao ilipangwa kwamba ufundishwe kupitia ibada ulifichwa usionekane kwa wanaoabudu. Aliona kwamba hawakupata amani katika ibada zao zisizo za imani. Hawakujua uhuru wa roho ambao ungekuja kwao kwa kumtumikia Mungu katika kweli. Yesu alikuwa amekuja kufundisha maana ya kumwabudu Mungu, na asingeruhusu hali ya kuchanganya matakwa ya mwanadamu katika maagizo ya kimbingu. Hakupinga maagizo au **(85)** vitendo vya walimu wale wasomi; lakini alipolaumiwa kwa tabia yake ile iliyo nyepesi, alilitumia neno la Mungu katika kuhalalisha mwenendo wake.

Katika kila njia ya upole na unyenyekevu, Yesu alijaribu kuwafurahisha wale aliopata kukutana nao. Kwa kuwa alikuwa mpole na asiyejitanguliza, waandishi na wazee walidhani kwamba angweza kushawishiwa na mafundisho yao kwa urahisi. Walimtaka apokee kanuni na mapokeo ambayo yalikuwa yamerithishwa kutoka kwa marabi wa kale, lakini alitaka waonyeshe mamlaka ya hayo katika Maandiko Matakatifu. Angesikiliza kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu; lakini hakuweza kutii mavumbuzi ya wanadamu. Ilionekana kama Yesu alijua Maandika kuanzia mwanzo mpaka mwisho, na aliyasema katika umuhimu wake wa kweli. Marabi waliaibika kwa kufundishwa na mtoto. Waliadai kwamba ofisi yao ndiyo inayotafsiri Maandiko, na kwamba Yeye alistahili kupokea tafsiri yao. Walichukizwa na hali ya Yeye kuwa kinyume na neno lao.

Walijua kwamba hakuna mamlaka yanayoweza kupatikana katika Maandiko kuunga mkono mapokeo yao. Walitambua kwamba Yesu alikuwa mbali sana juu ya wao katika uelewa wa kiroho. Lakini bado walikuwa na hasira kwa sababu Yeye hakutii maelekezo **86)** yao. Wakiwa wameshindwa kumshawishi, walimtafuta Yusufu na Mariamu, wakiwaonyesha njia yake ya kutoheshimu. Kwa hiyo alikemewa na kupingwa.

Katika umri wake wa mapema, Yesu alikuwa ameanza kutenda kwa kujitegemea katika kutengeneza tabia yake, na hata heshima na upendo kwa wazazi wake havikuweza kumgeuza aache kutii neno la Mungu. "Imeandikwa" ilikuwa ndiyo sababu ya kila tendo ambalo lilitofautiana na desturi za familia. Lakini nguvu ya ushawishi ya marabi iliyafanya maisha yake yawe machungu. Hata wakati wa ujana wake ilikuwa lazima ajifunze somo gumu la kuwa kimya na mvumilivu.

Kaka zake, walioitwa wana wa Yusufu, walikuwa upande wa msimamo wa marabi. Walisisitiza kwamba lazima mapokeo yazingatiwe, kwa kiwango kwamba yalikuwa matakwa ya Mungu. Hata walifikia hatua ya kuyaona mafundisho ya wanadamu kama vile yako juu sana kuliko neno la Mungu, na walichukizwa na maelezo ya wazi ya Yesu katika kutofautisha kati ya uongo na ukweli. Waliuhesabu utii wake kwa sheria ya Mungu kama ukaidi. Walishangazwa na ufahamu wake na hekima aliyoonyesha katika kujibu maswali ya marabi. Walijua kwamba hakufundishwa elimu kutoka kwa wenye hekima, lakini hawakuona kingine bali kama vile alikuwa mwalimu wao. Waligundua kwamba elimu yake ilikuwa ya juu zaidi kuliko yao. Lakini hawakukiri kwamba alikuwa na uwezo wa kuufikia mti wa uzima, chanzo cha ufahamu ambao hawakuujua.

Kristo hakuwa mtu wa kuheshimiwa, na alikuwa amefanya kosa mahsusi kwa Mafarisayo kwa kule kuachana na taratibu zao zisizobadilika. Aliona uwanja wa dini ukiwa umezungushiwa wigo kwa kuta zenye kimo kirefu. Alipindua huu ukuta unaotenganisha. Alipokutana na watu hakuuliza, Itikadi yako ya imani ni ipi? Wewe ni wa

kanisa gani? Alitumia nguvu zake za kusaidia kwa ajili ya wote waliohitaji kusaidiwa. Badala ya Yeye kujifungia katika chumba cha upweke ili kuonyesha tabia yake ya kimbingu, alitenda kazi kwa ajili ya wanadamu. Alisisitiza kanuni ya kwamba dini ya Biblia haiko katika kujitesa mwili. Alifundisha kwamba dini safi isiyo na najisi si ile ya kufuata mida iliyopangwa rasmi kwa ajili ya matukio. Alionyesha hamu ya kuwapenda watu wakati wote na mahali pote, na alijivika nuru ya upendo wa kutenda wema. Haya yote yalikuwa ni kemeo kwa Mafarisayo. Ilionekana kwake kwamba dini haikuwa katika ubinafsi, na kwamba kuangalia matakwa binafsi ilikuwa ni kuwa mbali na uchaji wa Mungu wa kweli. Hali hii ilikuwa imeibua uadui wao dhidi ya Yesu, wakajaribu kumlazimisha atii kanuni zao.

**(87)** Yesu alifanya kazi ya kuondoa kila namna ya maumivu aliyoona kwa watu. Alikuwa na kiasi kidogo sana cha pesa za kutoa, lakini alijinyima chakula ili kuwapatia wale walioonekana kuhitaji chakula zaidi ya vile alivyokihitaji. Kaka zake waliona kwamba nguvu ya ushawishi wake ilifika mbali na kupita ushawishi wao. Alikuwa na uelekevu ambao hakuna mwingine aliyekuwa nao, wala aliyetamani kuwa nao. Wakati walipoongea na maskini kwa ukali, walipowadhalilisha viumbe, Yesu aliwatafuta hawa hawa, na aliwaambia maneno ya kutia moyo. Kwa wale waliokuwa katika uhitaji aliwapa japo kikombe cha maji baridi, na kimya-kimya aliweka chakula chake mikononi mwao. Kadiri ambavyo alituliza maumivu yao, ukweli ule aliofundisha uliendana na matendo yake ya huruma, na kwa hiyo ulihifadhiwa katika kumbukumbu.

Haya yote hayakuwafurahisha kaka zake. Wao wakiwa na umri mkubwa kuliko Yesu, walidhani kwamba alipaswa awe chini ya maelekezo yao. Walimlaumu kwa kujifanya kuwa juu yao, na walimkemea kwa kujiweka juu ya walimu na waandishi na wakuu wa watu. Mara nyingi walimtishia na kujaribu kumshinikiza; lakini alisonga mbele, akiyafanya Maandiko kuwa mwongozo wake.

Yesu aliwapenda kaka zake, na aliwatendea kwa wema mkubwa; lakini walikuwa na wivu kwake, na walidhihirisha chuki na kutokuamini kwa wazi mno. Wasingeelewa mwenendo wake. Mgogoro mkubwa uliletwa kati yao na Yesu. Alikuwa Mwana wa Mungu wa asili ya kimbingu, **(88)** lakini hapa alikuwa mtoto asiye na wa kumsaidia. Muumba wa malimwengu, dunia ilikuwa mali yake, lakini umaskini ulikuwa katika kila hatua ya uzoefu wa maisha yake. Alikuwa na hadhi na hali ambayo kwa ujumla ilikuwa mbali na fahari ya kidunia na kutaka madaraka; hakutafuta ukuu wa duniani, na aliridhika hata katika nafasi ya chini kabisa. Hali hii iliwakasirisha kaka zake. Walishindwa kueleza upole wake wa wakati wote hata katika hali ya kujaribiwa na kuonewa. Hawakujua kwamba amekuwa maskini kwa ajili yetu, ili ya kwamba tupate “kuwa matajiri kwa umaskini wake." 2 Wakorintho 8:9. Wangeelewa siri ya utume wake kwa kiasi ambacho si zaidi ya vile ambavyo wale rafiki wa Ayubu waliweza kuelewa unyenyekevu na mateso ya Ayubu.

Yesu hakueleweka vema kwa kaka zake kwa sababu hakuwa kama wao. Kiwango chake hakikuwa kiwango chao. Kwa kuwaangalia wanadamu walikuwa wamegeukia mbali na Mungu, na hawakuwa na nguvu zake maishani mwao. Kawaida za dini walizoshika hazikuweza kubadili tabia zao. Walilipa "zaka za mnanaa na bizari na jira,” lakini waliacha “mambo makuu ya sheria, yaani, adili, na rehema, na imani." Mathayo 23:23. Kielelezo cha Yesu kilikuwa kwao jambo la kuchukiza. Alichukia kitu kimoja tu duniani, nacho ni dhambi. Hakuweza kushuhudia tendo baya bila kuonyesha maumivu yasiyofichika. Tofauti ilionekana wazi kati ya watu walioshikilia dini ya mazoea, ambao utakatifu wa kujionyesha ulificha ndani yao kupenda dhambi, na tabia ambayo ilitawaliwa na ari ya utukufu wa Mungu. Kwa kuwa maisha ya Yesu yalihukumu uovu, alipingwa na makundi yote mawili, la nyumbani na la nje ya nyumbani. Uaminifu wake na kutokuwa kwake na ubinafsi vilibezwa. Ustahimilivu na wema wake vilichukuliwa kama woga.

Katika sehemu zote za machungu yanayowaangukia wanadamu walio wengi, hakuna ambayo haikuonjwa na Yesu. Kulikuwa na wale waliojaribu kumtupia lawama kwa misingi ya kuzaliwa kwake, na hata mnamo wakati wa utoto wake bado angekutana na kejeli zao na mivumo ya uovu. Kama angekabiliana na hayo kwa mtazamo au maneno yasiyo na subira, kama angekubaliana na kaka zake hata katika tendo lisilo sahihi, angekuwa ameshindwa kuwa kielelezo. Hivyo angekuwa ameshindwa kusonga mbele katika mpango wa ukombozi. Angekuwa hata amekubali kuwa na kisingizio cha kukubaliana na dhambi, Shetani angeshinda, na ulimwengu ungepotea. Hii ndiyo sababu mjaribu aliyafanya maisha yake kuwa ya majaribu kwa kiasi kikubwa iwezekanavyo, ili ya kwamba aweze kuanguka.

Lakini katika kila jaribu alikuwa na jibu moja, "Imeandikwa." Alikemea matendo mabaya ya ndugu zake kwa nadra sana, lakini alikuwa na neno **(89)** la kuwaambia kutoka kwa Mungu. Mara nyingi alilaumiwa kuwa mwoga kwa kukataa kuungana nao katika kufanya kitendo kilichokatazwa; lakini jibu lake lilikuwa, Imeandikwa, "Kumcha Bwana ndiyo hekima, Na kujitenga na uovu ndio ufahamu." Ayubu 28:28.

Kulikuwa na baadhi ya watu walioitafuta kushikamana naye, wakihisi kuwa na amani kwa kuwa mahali alipo; lakini wengi walimkwepa, kwa sababu walikemewa na maisha yake yasiyo na uchafu. Vijana wenzake walimtaka afanye yale waliyokuwa wanafanya. Alikuwa na uelewa mkubwa na mwenye furaha; walifurahia kuwepo kwake, na walikaribisha mawazo yake; lakini walikosa uvumilivu katika uadilifu wake hata katika mambo madogo sana, na wakamwita mtu mwenye msimamo mkali. Yesu alijibu hivi, Imeandikwa, "Jinsi gani kijana aisafishe njia yake? Kwa kutii, akilifuata neno lako." "Moyoni mwangu nimeliweka neno lako, Nisije nikakutenda dhambi." Zaburi 119:9, 11.

Mara kwa mara aliulizwa, Kwa nini unaonekana kuwa na mambo ya peke yako hivyo, kuwa tofauti na sisi sote namna hiyo? Alijibu, Imeandikwa, "Heri walio kamili njia zao, Waendao katika sheria ya Bwana. Heri wazitiio shuhuda zake, Wamtafutao kwa moyo wote. Naam, hawakutenda ubatili, Wamekwenda katika njia zake." Zaburi 119:1-3.

Alipoulizwa kwamba ni kwa nini hakuungana na vijana wa Nazareti katika mizaha, alisema, Imeandikwa, "Nimeifurahia njia ya shuhuda zako Kana kwamba ni mali mengi. Nitayatafakari mausia yako, Nami nitaziangalia njia zako. Nitajifurahisha sana kwa amri zako, Sitalisahau neno lako." Zaburi 119:14-16.

Yesu hakupigania haki zake. Mara nyingi kazi yake ilifanywa kuwa chungu bila sababu kwa sababu alikuwa radhi na hakuwa mlalamishi. Lakini hakushindwa wala hakukata tamaa. Aliishi maisha yaliyo juu kuliko magumu haya, kama aliyekuwa katika nuru ya uwepo wa Mungu. Hakulipiza wakati alipofanyiwa baya, bali alivumilia kufanyiwa mabaya.

Tena na tena aliulizwa, Kwa nini unajiweka katika hali kama hiyo ya kudharaulika, hata kwa ndugu zako? Alijibu, Imeandikwa, "Mwanangu, usiisahau sheria yangu, Bali moyo wako uzishike amri zangu. Maana zitakuongezea wingi wa siku. Na miaka ya uzima, na amani. Rehema na kweli zisifarakane nawe; Zifunge shingoni mwako; Ziandike juu ya kibao cha moyo wako. Ndivyo utakavyopata kibali na akili nzuri, Mbele za Mungu na mbele ya mwanadamu." Mithali 3:1-4.

Tangu wakati ule wazazi wa Yesu walipomkuta hekaluni, mwenendo wake ulikuwa fumbo kwao. Hakuwa mtu wa kuingia katika mabishano, lakini kielelezo cha maisha yake kilikuwa somo la wakati wote. Alionekana kama mtu **(90)** aliyewekwa rasmi. Nyakati zake za furaha ni zile ambazo alikuwa peke yake akizungukwa na vitu vya asili na Mungu. Kila wakati nafasi ilipopatikana, aliacha shughuli za kazini kwake, na kwenda mashambani, kutafakari katika mabonde ya kijani, kufanya ushirika na Mungu katika pande za milima au katikati ya miti ya msituni. Mara nyingi asubuhi na mapema ilimkuta katika sehemu zilizojificha, akitafakari, akichunguza Maandiko, au akiomba. Akitoka katika saa hizi za ukimya alikuwa akirudi nyumbani kufanya majukumu yake tena, na kuonyesha kielelezo cha kuhimili ugumu wa kazi kwa uvumilivu.

Maisha ya Yesu yamejaa heshima na upendo kwa mama yake. Mariamu aliamini moyoni mwake kwamba mtoto mtakatifu aliyezaliwa naye alikuwa Masihi aliyeahidiwa muda mrefu, lakini hakuthubutu kuonyesha imani yake hiyo. Katika maisha yake yote duniani alishiriki maumivu ya Yesu. Alishuhudia kwa huzuni majaribu yaliyoletwa kwake wakati wa utoto na ujana wake. Kwa kule kuthibitisha kile alichojua kuwa ni sahihi kuhusu mwenendo wa Yesu, yeye mwenyewe aliletwa katika nafasi ya kujaribiwa. Aliona kwamba utengamano wa nyumbani, na uangalizi wa mama kwa mtoto, ni mambo ya muhimu sana katika kujenga tabia. Wana na binti za Yusufu walilijua jambo hili, na kwa njia ya kumfanya mama awe na wasiwasi, walikosoa mwenendo wa Yesu ili uendane na viwango vyao.

Mara kwa mara Mariamu alimkanya Yesu, na kumtaka aenende kulingana na kawaida za marabi. Lakini hakuweza kushawishika kubadili tabia yake ya kuzitafakari kazi za Mungu na kutafuta kuondosha machungu ya watu au hata ya wanyama wasioweza kuongea. Wakati makuhani na walimu walipotaka msaada wa Mariamu katika kumdhibiti Yesu, mama yule alisumbuka sana; lakini amani ilikuja moyoni mwake pindi Yesu alipomwambia maneno ya Maandiko yaliyounga mkono tabia yake.

Wakati fulani Mariamu aliyumba kati ya upande wa Yesu na ule wa ndugu zake, ambao hawakuamini kwamba Yesu alikuwa ametumwa na Mungu; lakini viashirio vilikuwepo vingi kuonyesha kwamba tabia zake zilikuwa za kimbingu. Alimwona akijitoa kwa ajili ya mema ya watu wengine. Kuwepo kwake kulileta mazingira mazuri nyumbani, na maisha yake yalikuwa kama chachu ifanyavyo kazi katika jamii. Akiwa mtu asiyedhuru wala asiye na uchafu, aliishi miongoni mwa watu wasio na fikira njema, mafidhuli, wakali; miongoni mwa watoza ushuru wasiotenda haki, wabadhirifu wasiojali, Wasamaria wasio haki, askari wapagani, wakulima wakorofi, na makutano ya watu mchanganyiko. Aliongea maneno ya huruma hapa na pale, alipoona watu waliochoka, ambao bado wamelazimika kubeba mizigo mizito. Alishiriki mizigo yao, na kurudia kwao masomo ya upendo, huruma, wema wa Mungu ulioonekana katika maumbile ya asili.

**(91)** Aliwafundisha watu wote kujiona kwamba wamejaliwa talanta za thamani, ambazo zikitumika kwa usahihi zitawapatia utajiri wa milele. Aling'oa na kuondoa majivuno yote kutoka katika maisha, na kwa kielelezo chake mwenyewe alionyesha kwamba kila wakati ulio katika muda umesheheni matokeo ya milele; kwamba unapaswa utambuliwe kama hazina, na utumiwe kwa makusudi matakatifu. Hakumpita mtu yeyote kwamba hana thamani, bali alitafuta kutumia dawa iokoayo kwa kila nafsi. Katika kundi lolote alilojikuta ndani yake, alitoa somo lililofaa kwa wakati na mazingira yale. Alitafuta kuwawekea tumaini wale waliokuwa na vurugu na bila matumaini, akiwapa uhakika kwamba wanaweza kuishi pasipo lawama wala kudhuru mtu, na kupata tabia ile ambayo ingewafanya waonekane kama wana wa Mungu. Mara nyingi alikutana na watu ambao wameogelea katika uongozi wa Shetani, na ambao hawakuwa na uwezo wa kuvunja na kuitoroka mitengo yake Shetani. Kwa watu kama hao, waliokata tamaa, wagonjwa, walioanguka, Yesu alisema maneno ya huruma sana, maneno yale ambayo yalihitajika na ambayo yangeeleweka. Alikutana na wengine **(92)** pia ambao walikuwa wakipambana na adui wa roho ana kwa ana. Aliwahimiza kwamba wajipe moyo, akiwahakikishia kwamba wangeshinda; maana malaika wa Mungu walikuwa upande wao, na wangewapa ushindi. Wale ambao aliwasaidia hivyo walishawishika kwamba huyu alikuwa Yeye ambaye wangemwamini kwa ujasiri kamili. Asingezisaliti zile siri walizomwaga katika masikio yake ya huruma.

Yesu alikuwa mponyaji wa mwili na roho. Aliguswa na kila hatua ya mateso iliyokuja kufahamika kwake, na alileta ahueni kwa kila aliyekuwa anateseka, maneno yake ya kutuliza yakiwa na faraja. Hakuna aliyesema kwamba Yesu alikuwa amefanya mwujiza; bali wema – nguvu ya uponyaji ya wema – ulitoka ndani yake na kwenda kwa wagonjwa na wenye masumbufu. Hivyo ndivyo alivyotenda katika njia isiyozuilika kwa ajili ya watu wengine tangu utotoni mwake. Na hii ndiyo iliyokuwa sababu ya watu wengi kumsikiliza kwa furaha baada ya kuanza huduma yake ya hadhara.

Lakini katika utoto, ujana, na utu uzima wake, Yesu alienenda peke yake. Katika usafi na uaminifu wake, alitembea katika shinikizo la zabibu akiwa peke yake, na miongoni mwa watu hakukuwa na aliyekuwa naye. Alibeba uzito wa kutisha wa majukumu kwa ajili ya wokovu wa watu. Alijua kwamba kusipokuwepo na badiliko la kweli katika misingi na makusudi ya wanadamu, wote wangepotea. Huu ulikuwa mzigo wa roho yake, na hakuna mtu ambaye angetambua uzito uliokuwa juu yake. Akiwa amejawa na makusudi mazito, aliendelea na mpango wa maisha yake ili kwamba Yeye mwenyewe awe nuru ya ulimwengu.

## Sura ya 10

# Sauti Nyikani

[Sura hii imejengwa katika Luka 1:5-23, 57-80; 3:1-18; Mathayo.3:1-12; Marko 1:1-8.]

Kutoka miongoni mwa waaminifu katika Israeli, mtangulizi wa Masihi, aliyesubiriwa kwa muda mrefu, aliinuka. Kuhani mzee Zakaria na mkewe Elisabeti "wote wawili walikuwa wenye haki mbele za Mungu;" na katika maisha yao ya ukimya na matakatifu nuru ya imani iliangaza kama nyota katikati ya giza la uovu wa siku hizo. Kwa watu hawa ahadi ya mtoto ilitolewa, ambaye aliambiwa “utatangulia mbele za uso wa Bwana umtengenezee njia zake.”

Zakaria aliishi katika "milima milima ya Uyahudi," lakini alikuwa ameenda Yerusalemu kuhudumu katika hekalu kwa juma moja, huduma ambayo ilitakiwa kufanywa na makuhani mara mbii kwa kila mwaka. "Basi ikawa, alipokuwa akifanya kazi ya ukuhani katika taratibu ya zamu yake mbele za Mungu, kama ilivyokuwa desturi ya ukuhani, kura ilimwangukia kuingia katika hekalu la Bwana ili kufukiza uvumba."

Alikuwa amesimama mbele ya madhabahu ya dhahabu katika mahali patakatifu pa hekaluni. Wingu la uvumba pamoja na maombi ya Waisraeli vilikuwa vikipanda mbele za Mungu. Ghafla akaona uwepo wa hali ya kimbingu. Malaika wa Mungu alikuwa "amesimama upande wa kuume wa madhabahu ya kufukizia." Uwepo wa malaika yule ilikuwa ishara ya kupendelewa, lakini Zakaria **(98)** hakuzingatia hili. Kwa miaka mingi alikuwa ameomba kuhusu ujio wa Mkombozi; sasa mbingu ilikuwa imemtuma mjumbe wake kutangaza kwamba maombi yalikuwa sasa yajibiwe; lakini rehema ya Mungu ilionekana kuwa kubwa sana kiasi kwamba hakuweza kuithamini. Alijawa na hofu na kujihukumu.

Lakini alisalimiwa kwa namna ya kuhakikishiwa furaha: "Usiogope, Zakaria, maana dua yako imesikiwa, na mkeo Elisabeti atakuzalia mtoto mwanamume, na jina lake utamwita Yohana. Nawe utakuwa na furaha na shangwe, na watu wengi watakufurahia kuzaliwa kwake. Kwa sababu atakuwa mkuu mbele za Bwana; hatakunywa divai wala kileo; naye atajazwa Roho Mtakatifu. . . . Na wengi katika Waisraeli atawarejeza kwa Bwana Mungu wao. Naye atatangulia mbele zake katika roho ya Eliya, na nguvu zake, ili kuigeuza mioyo ya baba iwaelekee watoto, na kuwatilia waasi akili za wenye haki, na kumwekea Bwana tayari watu waliotengenezwa. Zakaria akamwambia malaika, Nitajuaje neno hilo? Maana mimi ni mzee, na mke wangu ni mkongwe wa siku nyingi."

Zakaria alijua vema jinsi Ibrahimu alivyopewa mtoto katika uzee wake kwa sababu aliamini na alikuwa mwaminifu kwake Yeye aliyetoa ahadi. Lakini kwa muda kuhani huyu mzee aligeuza mawazo yake kuyapeleka katika udhaifu wa kibinadamu. Anasahau kwamba Mungu ana uwezo wa kufanya kitu ambacho ameahidi. Ni tofauti kiasi gani kati ya kutokuamini huku na imani tamu, kama ya mtoto, ya mwanamwali wa Nazareti, ambaye jibu lake kwa tangazo la malaika lilikuwa, "Tazama, mimi ni mjakazi wa Bwana; na iwe kwangu kama ulivyosema"! Luka 1:38.

Kuzaliwa kwa mwana wa Zakaria, kama kulivyokuwa kuzaliwa kwa mtoto wa Ibrahimu, na kwa yule wa Mariamu, kulikuwa kwa ajili ya kufundisha ukweli mkuu wa kiroho, ukweli ambao tunajifunza kwa kasi ndogo na kuwa tayari kuusahau. Kwa upande wetu wenyewe hatuna uwezo wa kufanya lolote jema; lakini kile ambacho hatuwezi kufanya kitatengenezwa kwa uwezo wa Mungu katika kila nafsi iaminiyo na kujinyenyekeza. Mtoto wa ahadi alitolewa kwa njia ya imani. Maisha ya kiroho yanapatikana kwa imani, na tunawezeshwa kuzifanya kazi za haki kwa imani.

Kwa swali la Zakaria, malaika alisema hivi, "Mimi ni Gabrieli, nisimamaye mbele za Mungu; nami nimetumwa niseme nawe, na kukupasha habari hizi njema." Miaka mia tano kabla, Gabrieli alikuwa amemfahamisha Danieli kipindi cha unabii ambacho kingeenda hadi kwa ujio wa Masihi. Kule kujua kwamba kipindi hiki kilikuwa kimekaribia kulimfanya Zakaria kuomba kwa ajili ya ujio wa Masihi. Sasa mjumbe yule yule ambaye kupitia kwake unabii ule ulitolewa alikuwa amekuja kutangaza kutimizwa kwake.

**(99)** Maneno ya malaika kwamba, "Mimi ni Gabrieli, nisimamaye mbele za Mungu," yanaonyesha kwamba anakalia nafasi ya heshima ya juu mbinguni. Alipokuja na ujumbe kwa Danieli, alisema, "Wala hapana anisaidiaye juu ya hao ila huyo Mikaeli, mkuu wenu." Danieli 10:21. Kuhusu Gabrieli Mwokozi anasema katika Ufunuo,

akisema kwamba "Naye akatuma kwa mkono wa malaika akamwonyesha mtumwa wake Yohana." Ufunuo 1:1. Na kwa Yohana malaika huyo alisema, "Mimi ni mjoli wako, na wa ndugu zako manabii." Ufunuo 22:9. Ni jambo la ajabu – kwamba malaika anayesimama kwa kuheshimiwa zaidi baada tu ya Mwana wa Mungu ndiye aliyechaguliwa kufungua makusudi ya Mungu kwa mwanadamu mwenye dhambi.

Zakaria alikuwa ameonyesha shaka kwa maneno ya malaika. Asingeongea tena mpaka yatimie. Malaiaka akasema, "Na tazama! Utakuwa bubu, usiweze kusema, mpaka siku ile yatakapotukia hayo, kwa sababu hukuyasadiki maneno yangu; nayo yatatimizwa kwa wakati wake." Katika huduma hii, ilikuwa ni zamu ya kuhani huyu kuomba kwa ajili ya msamaha wa umma wote na kwa dhambi ya taifa, na kwa ajili ya kuja kwa Masihi; lakini pindi Zakaria alipojaribu kufanya hivyo, hakuweza kutamka neno tena.

Wakati alipokuja nje ili kuwabariki watu, "aliendelea kuwaashiria akakaa bubu." Walikuwa wamesubiri sana, na walikuwa wameanza kuogopa, kwamba asije akawa amepigwa na hukumu. Lakini alipokuja kutoka katika mahali patakatifu, uso wake ulikuwa unang’aa kwa utukufu wa Mungu, "nao, walitambua ya kuwa ameona maono." Zakaria aliwasiliana nao kuwajulisha alichoona na kusikia; na "siku za huduma yake zilipokuwa zimetimia akaenda nyumbani kwake."

Muda mfupi baada ya kuzaliwa kwa mtoto aliyeahidiwa, ulimi wa baba ulifunguliwa, “akaanza kunena akimsifu Mungu. Wakaingiwa na hofu wote waliokuwa wakikaa karibu nao; na mambo hayo yote yakatangazwa katika nchi yote ya milima milima ya Uyahudi. Na wote walioyasikia wakayaweka **(100)** mioyoni mwao, wakisema, Mtoto huyu atakuwa wa namna gani?" Yote haya yalikuwa yanavuta usikivu katika ujio wa Masihi, ambako Yohana angetayarisha njia kwa ajili ya huo.

Roho Mtakatifu alikuwa juu ya Zakaria, na katika maneno haya ya kupendeza alitabiri kuhusu kazi ya mwana wake:

“Nawe, mtoto, utaitwa nabii wake Aliye juu,
Kwa maana utatangulia mbele za uso wa Bwana umtengenezee njia zake;
Uwajulishe watu wake wokovu, Katika kusamehewa dhambi zao.
Kwa njia ya rehema za Mungu wetu,
Ambazo kwa hizo mwangaza utokao juu umetufikia,
Kuwaangaza wakaao katika giza na uvuli wa mauti,
Na kuiongoza miguu yetu kwenye njia ya amani.”

"Yule mtoto akakua, akaongezeka nguvu rohoni, akakaa majangwani hata siku ya kutokea kwake kwa Israeli." Kabla ya kuzaliwa Yohana, malaika alikuwa amesema, "Atakuwa mkuu mbele za Bwana; hatakunywa divai wala kileo; naye atajazwa Roho Mtakatifu." Mungu alikuwa amemwita mwana wa Zakaria kwa ajili ya kazi kuu, kazi kubwa mno kuliko yoyote ambayo imepata kutolewa kwa wanadamu. Ili kuifanya kazi hii lazima awe pamoja na Bwana afanye kazi pamoja naye. Na Roho wa Mungu angekuwa pamoja naye ikiwa angesikiliza maelekezo ya malaika.

Yohana angeenda kama mjumbe wa Yehova, kuwaletea wanadamu nuru ya Mungu. Lazima ayapatie mawazo yao mwelekeo mpya. Lazima awashawishi kwa utakatifu wa matakwa ya Mungu, na uhitaji wao wa haki yake kamilifu. Lazima mjumbe wa namna hiyo awe mtakatifu. Lazima awe hekalu kwa ajili ya makazi ya Roho wa Mungu. Ili kukamilisha kazi hii lazima awe na afya njema ya mwili, na nguvu ya akili na roho. Kwa hiyo ilikuwa muhimu aweze kutawala hamu ya kula na kunywa na hisia ya mwili. Lazima aweze kudhibiti namna hiyo nguvu zake zote ili aweze kusimama katikati ya watu bila kuyumbishwa na hali zinazomzunguka kama vile miamba na milima ya nyikani ilivyo.

Katika sika za Yohana Mbatizaji, uchu wa utajiri, na kupenda anasa na kujionyesha vilikuwa vimeenea sana. Starehe, karamu na vinywaji, vilikuwa vinasababisha magonjwa na uovu, vikidhoofisha utambuzi wa kiroho, na kupunguza uwezo wa kugundua dhambi. Yohana alikuwa asimame kama mwanamatengenezo. Kwa maisha yake ya kujizuia na mavazi yake mepesi alikuwa **(101)** akemee kutokuwa na kiasi kwa wakati wake. Hayo ndiyo maagizo yaliyotolewa kwa wazazi wa Yohana, **-** somo la kiasi lililotolewa na malaika kutoka katika kiti cha enzi cha mbinguni.

Wakati wa utoto na ujana tabia ina msukumo mkubwa. Lazima kuwe na uwezo wa kujitawala. Wakati wa kuota moto na katika vikao vya familia ushawishi hufanywa ambao matokeo yake yanadumu hata milele. Zaidi ya kipaji cha asili, mazoea yaliyojengwa mnamo siku za awali yanaamua kama mtu huyo atakuwa mshindi au atashindwa katika vita ya maisha. Ujana ndio muda wa kupanda. Ndio unaoamua tabia ya mavuno, kwa maisha haya na yale yajayo.

Kama nabii, Yohana alikuwa wa "kuigeuza mioyo ya baba iwaelekee watoto, na kuwatilia waasi akili za wenye haki, na kumwekea Bwana tayari watu waliotengenezwa." Katika kuandaa njia kwa ajili ya kuja kwa Kristo kwa mara ya kwanza, alikuwa mwakilishi wa wale ambao watawaandaa watu kwa ajili ya ujio wa Bwana mara ya pili. Ulimwengu umezoea kujifurahisha. Makosa na uongo vimekithiri. Mitego ya Shetani ili kuzinasa roho za watu inazidishwa. Lazima wote ambao wangependa ukamilifu wa utakatifu katika kumcha Bwana wajifunze somo la kiasi na kujitawala. Lazima hamu ya vyakula na vinywaji na hisia za mwili viongozwe na uwezo wa juu wa akili. Hii nidhamu binafsi ni muhimu kwa ajili ya nguvu hizo za akili na uwezo wa kiroho ambavyo vitatuwezesha kuelewa na kufanya ukweli mtakatifu wa neno la Mungu. Kwa sababu hii kuwa na kiasi kuna nafasi katika kazi ya maandalizi kwa ajili ya kuja kwa Kristo mara ya pili.

Katika mpango wa vitu vya asili, mwana wa Zakaria angekuwa ameelimishwa kwa ajili ya ukuhani. Lakini mafunzo ya shule za marabi yasingefaa kwa kazi ya Mungu. Mungu hakumpeleka kwa walimu wa thiolojia kujifunza namna ya kufafanua Maandiko. Alimwita kwenda jangwani, ili kwamba ajifunze kuhusu vitu vya asili na Mungu wa vitu vya asili.

Mahali pa nyumbani kwake palikuwa katika eneo la upweke, katikati ya vilima visivyo na uoto, katika makorongo ya mwitu, na katika mapango ya miamba. Lakini lilikuwa ni chaguo lake kuacha raha na starehe za maisha kwa ajili ya kupata nidhamu ya mazingira magumu ya jangwani. Mazingira yake ya hapa yalihitaji tabia ya maisha mepesi na kujikana. Pasipo kuingiliwa na makelele ya matakwa ya ulimwengu, hapa angejifunza masomo ya maumbile ya asili, ya ufunuo, na ya Mungu. Maneno ya malaika kwa Zakaria yalikuwa yamerudiwa-rudiwa kwa Yohana na wazazi wake hawa wamchao Mungu. Tangu utoto wake kazi yake ilikuwa imewekwa mbele yake, na alikuwa amekubali heshima hiyo takatifu. Kwake upweke wa jangwani ulipokelewa kama njia ya kukwepa jamii ambayo ilikuwa na mashaka, kutokuamini na uchafu. Aliacha kujiamini **(102)** uwezo wake mwenyewe ili astahimili majaribu, na aliacha kukutana na dhambi wakati wote, asije akawa na hali ya kuzoea zaidi maisha ya dhambi.

Akiwa ametolewa kwa Mungu kama mnadhiri tangu kuzaliwa, aliifanya nadhiri hiyo kuwa yake katika maisha yote. Nguo zake zilikuwa zile za manabii wa kale, vazi la singa za ngamia, lililoshikiliwa na mshipi wa ngozi. Alikula "nzige asali ya mwitu" vilivyopatikana jangwani, na alikunywa maji safi kutoka vilimani.

Lakini maisha ya Yohana hayakuachwa pasipo kazi katika upweke ule, au katika kujitenga kule. Nyakati fulani alienda kujichanganya na watu; na muda wote alivutiwa kuchunguza kile kilichokuwa kikiendelea ulimwenguni. Kutokea katika sehemu hiyo alikojitenga, aliangalia kwa mbali matukio yaliyokuwa yakifunguka. Akiwa na maono yaliyomlikiwa na Roho wa kimbingu alichunguza tabia za wanadamu, ili kwamba aelewe namna ya kuifikia mioyo yao akiwa na ujumbe wa mbinguni. Mzigo wa utume wake ulikuwa juu yake. Kwa kutafakari na kuomba, kule alikojificha, alitafuta kujifunga nafsi yake kwa ajili ya kazi ya maisha yake iliyokuwa mbele yake.

Ingawa alikuwa jangwani hakuwa huru pasipo majaribu. Kwa kiasi kiwezekanacho alifunga kila mlango ambao Shetani angeingilia, lakini alikuwa bado ananyemelewa na mjaribu. Hata hivyo fahamu zake za kiroho zilikuwa wazi, alikuwa ameendeleza nguvu na maamuzi ya tabia, na kwa msaada wa Roho Mtakatifu aliweza kugundua njia za Shetani, na kuzipinga nguvu zake.

Yohana aliipata shule yake na mahali pake pa faragha kule jangwani. Kama ilivyokuwa kwa Musa kule katika milima ya Midiani, yeye pia alifungiwa katika uwepo wa Mungu, na kuzungukwa na viashiria vya uweza wake. Yeye hakupata nafasi ya kukaa katika makazi yaliyojitenga kwenye ile milima mikuu, kama ilivyokuwa kwa yule kiongozi mkuu wa Israeli; bali mbele yake yeye vilisimama vilele vya milima ya Moabu, ng'ambo ya Yordani, vikimtangaza Yeye aliyeisimamisha milima mahali pake, na kuifunga kwa nguvu. Ukimya na mwonekano wa kutisha wa asili kule nyumbani kwake pa jangwani ulionyesha kwa uwazi picha ya hali ya Israeli. Shamba la mzabibu la Bwana lenye kuzaa lilikuwa limekuwa ukiwa. Lakini juu ya jangwa lile, mbingu zilipinda katika

mwanga na uzuri wake. Mawingu yaliyokusanyika, na giza nene, vilipenywa na upinde wa mvua. Kwa hiyo juu ya kuharibika kwa Israeli utukufu wa miliki ya Masihi uliangaza. Mawingu ya ghadhabu yalipitwa na upinde wa mvua wa agano la rehema.

Akiwa peke yake katika usiku mtulivu alisoma ahadi ya Mungu kwa Ibrahimu kuhusu uzao wake usiohesabika kama zilivyo nyota. Nuru ya kupambazuka, inayozuka katika milima ya Moabu, ilimweleza kuhusu Yeye atakayekuwa "kama nuru ya asubuhi jua lichapo, Asubuhi isiyo na mawingu." 2 Samweli 23:4. Na katika mwanga wa mchana aliona uzuri wa udhihirisho wa wakati ambapo "utukufu wa Bwana utafunuliwa, Na wote wenye mwili watauona pamoja." Isa. 40:5.

Kwa mshangao lakini wa roho ya kuchangamka kwa furaha alitafuta katika magombo ya unabii ufunuo wa kuja kwa Masihi, - mzao aliyeahidiwa atakayeponda kichwa cha nyoka; Shilo, "mtoaji wa amani," ambaye alikuwa atokee kabla mfalme hajakoma katika kiti cha enzi cha Daudi. Sasa muda ulikuwa umekuja. Mtawala wa Kirumi alikuwa amekaa katika jumba la kifalme la Mlima Sayuni. Kwa neno la hakika la Mungu, Kristo alikuwa amezaliwa tayari.

Maelezo ya Isaya kuhusu utukufu wa Masihi yalikuwa ndiyo masomo ya Yohana mchana na usiku, - Tawi litakalotoka katika mizizi ya Yese; Mfalme atakayetawala katika haki, atatawala "wanyenyekevu wa dunia kwa adili;" "kama mito ya maji mahali pakavu, kama kivuli cha mwamba mkubwa katika nchi yenye uchovu." Israeli hataitwa tena "Aliyeachwa, wala nchi yako haitaitwa tena, Ukiwa;" bali utaitwa wa Bwana." Isaya 11:4; 32:2; 62:4. Moyo wa aliye katika upweke ugenini ulijawa na maono matukufu.

Alimtazama Mfalme katika uzuri wake, na ubinafsi ukasahaulika. Alimtazama mkuu wa utakatifu, na akajiona kuwa yeye mwenyewe hawezi na hastahili. Alikuwa tayari kusonga mbele kama mjumbe wa Mbinguni pasipo kutishwa na mwanadamu, kwa sababu alikuwa amemwangalia Mungu. Angesimama imara na bila hofu mbele ya watawala wa kidunia, kwa kuwa alikuwa amejisalimisha chini ya Mfalme wa wafalme.

Yohana hakuelewa kwa ukamilifu undani wa ufalme wa Masihi. Alitazamia ukombozi wa Israeli kuondokana na maadui wa kitaifa; lakini kuja kwa Mfalme katika haki, na kuisimamisha Israeli kama taifa takatifu, ilikuwa kiini cha tumaini lake. Aliamini kwamba hivyo ndivyo ungetimia unabii uliotolewa kuhusu kuzaliwa kwake:

“Na kulikumbuka agano lake takatifu; . . .
Ya kwamba atatujalia sisi, Tuokoke mikononi mwa adui zetu,
Na kumwabudu pasipo hofu,
Kwa utakatifu na kwa haki Mbele zake siku zetu zote."

Aliwaona watu wake wakiwa katika madanganyo, wakijipenda wenyewe, na wakiwa wamelala katika dhambi zao. Aliazimu kuwaamsha ili kwenda katika maisha matakatifu. Ujumbe ambao Mungu alikuwa amempatia kuubeba ulipangwa kuwagutua kutoka katika udhaifu wao, na **(104)** kuwafanya watetemeke kwa sababu ya uovu wao mkubwa. Kabla ya mbegu ya injili kupata mahali pake, lazima udongo wa moyoni uvunjwe-vunjwe. Kabla ya kutafuta uponyaji kwa Yesu, lazima waamshwe kutoka katika hatari yao ya majeraha ya dhambi.

Mungu hatumi wajumbe ili kumsifia mdhambi. Hapeleki ujumbe wa amani kumliwaza katika usalama wa hatari ya kifo mtu asiyetakasika. Anaweka mizigo mizito juu ya dhamiri ya mtenda-maovu, na kuichoma roho kwa mishale ya kujiona hatia. Malaika wahudumuo humwonyesha hukumu za Mungu za kutisha ili kumfanya awe na uhitaji wa kina, na kumhimiza kulia akisema, "Nifanye nini ili nipate kuokoka?" halafu mkono ule uliojishusha hata mavumbini, unamwinua anayejutia dhambi. Sauti ambayo imekemea dhambi, na kuaibisha kiburi na dhamira ya mafanikio, inauliza kwa upole, "Wataka nikufanyie nini?"

Wakati huduma ya Yohana ilipoanza, taifa lilikuwa katika hali ya taharuki na kutoridhika likielekea katika mapinduzi. Kwa kuondolewa kwa Arkelao, Yuda ilikuwa imewekwa katika utawala wa moja kwa moja wa Rumi. Utawala wa mabavu wa magavana wa Kirumi, na juhudi zao za dhati za kuingiza desturi na alama za kipagani, viliwasha moto wa upinzani, ambao ulikuwa umezimwa kwa damu ya maelfu ya wenye akili sana wa Israeli. Mambo yote haya yaliongeza chuki ya kitaifa dhidi ya Rumi, na yaliongeza hali ya kutafuta kuwa huru mbali na utawala huu.

Katikati ya hali hii ya kutoelewana na mzozo, sauti ilisikika kutoka nyikani, sauti kali na ya kuamsha, lakini ikiwa imejaa matumaini: "Tubuni; kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia." Kwa nguvu mpya na ya ajabu sauti hiyo iliwabadilisha watu. Manabii walikuwa wametabiri kuhusu kuja kwa Kristo kama tukio ambalo liko mbali mbele; lakini sasa hili lilikuwa tangazo kwamba tukio hilo lilikuwa limekaribia. Kuonekana kwa Yohana katika hali isiyo ya kawaida kulirudisha mawazo ya wasikilizaji wake kwa watabiri wa kale. Katika mwonekano wake na mavazi yake alifanana na nabii Eliya. Akiwa na roho na nguvu ya Eliya alipinga vitendo viovu vya taifa, na alikemea dhambi iliyokuwepo. Maneno yake yalikuwa wazi, yenye ufasaha, na yanayogusa. Wengi waliamini kuwa ni mmoja wa manabii aliyefufuka kutoka kwa wafu. Taifa zima lilitikisika. Makundi ya watu yalitiririka kuelekea nyikani.

Yohana alitangaza kuja kwa Masihi, na aliwaita watu watubu. Kama ishara ya kuoshwa dhambi, aliwabatiza katika maji ya mto Yordani. Kwa njia hiyo alitoa somo muhimu la kutumia kielelezo kuwaonyesha kwamba wale waliodai kuwa wateule wa Mungu walikuwa wamenajisiwa na dhambi, na ya kwamba pasipo kusafishwa kwa moyo na maisha wasingekuwa na nafasi katika ufalme wa Masihi.

**(105)** Wana wa kifalme na marabi, askari, watoza ushuru, na wakulima walikuja kumsikiliza nabii huyu. Kwa muda onyo lile la dhati kutoka kwa Mungu liliwashtua. Wengi walifikishwa katika toba, wakabatizwa. Watu wa hadhi zote walijisalimisha katika matakwa ya Mbatizaji, ili waweze kushiriki katika ufalme alioutangaza.

Wengi miongoni mwa waandishi na Mafarisayo walikuja wakikiri dhambi zao, na wakiomba wabatizwe. Walikuwa wamejikweza kwamba wao ni zaidi ya wengine, na walikuwa wamewafanya watu waamini kwamba wao ndio wema; sasa siri za hatia ya maisha yao zilifunuliwa. Lakini Yohana alisukumwa na Roho Mtakatifu kwamba wengi wa watu hawakuwa na toba ya kweli. Wakijifanya kuwa marafiki wa nabii walitumaini kupata upendeleo wa Mfalme ajaye. Na kwa kupata ubatizo mbele ya huyu mwalimu kijana maarufu, walifikiri kwamba wataimarisha ushawishi wao kwa watu.

Yohana alikutana nao kwa swali lenye kuumiza, "Enyi wazao wa nyoka, ni nani aliyewaonya ninyi kuikimbia hasira itakayokuja? Basi zaeni matunda yapasayo toba; wala msiwaze mioyoni mwenu kwamba, **(106)** Tunaye baba, ndiye Ibrahimu; kwa maana nawaambia ya kwamba Mungu aweza katika mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto."

Wayahudi walikuwa wametafsiri vibaya ahadi ya Mungu ya upendeleo wa milele kwa Israeli: "Bwana asema hivi, awapaye watu jua, ili kuwa nuru wakati wa mchana, na amri za mwezi na nyota, ili kuwa nuru wakati wa usiku, aichafuaye bahari, hata mawimbi yake yakavuma; Bwana wa majeshi, ndilo jina lake; Amri hizi zikiondoka, zisiwe mbele zangu, asema Bwana, ndipo wazao wa Israeli nao wataacha kuwa taifa mbele zangu milele. Bwana asema hivi, Kama mbingu zikiweza kupimwa, na misingi ya dunia ikiweza kugunduliwa huko chini, ndipo wazao wa Israeli pia nitawatupilia mbali, kwa ajili ya hayo yote waliyoyatenda, asema Bwana." Yeremia 31:35-37. Wayahudi walichukulia mtiririko wao wa ukoo kutoka kwa Ibrahimu kwamba unawapa haki ya ahadi hiyo. Lakini hawakuzingatia masharti ambayo Mungu alikuwa ameyaweka. Kabla ya kutoa ahadi hiyo, alikuwa amesema, "Bali agano hili ndilo nitakalofanya na nyumba ya Israeli, baada ya siku zile, asema Bwana; Nitatia sheria yangu ndani yao, na katika mioyo yao nitaiandika; nami nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu wangu. Wala hawatamfundisha kila mtu jirani yake, na kila mtu ndugu yake, wakisema, Mjue Bwana; kwa maana watanijua wote, tangu mtu aliye mdogo miongoni mwao hata aliye mkubwa miongoni mwao, asema Bwana; maana nitausamehe uovu wao, wala dhambi yao sitaikumbuka tena." Yeremia 31:33, 34.

Kwa watu wote ambao sheria yake imeandikwa mioyoni mwao, upendeleo wa Mungu ni wa hakika. Wanakuwa kitu kimoja na Yeye. Lakini Wayahudi walikuwa wamejitenga naye. Kwa sababu ya dhambi zao walikuwa wanaumia katika hukumu zake. Hii ilikuwa ndiyo sababu ya kuchukuliwa utumwani katika taifa la kipagani. Mawazo yao yalitiwa giza kwa uovu, na kwa kuwa Bwana alikuwa amewapa upendeleo mkubwa siku za nyuma, walipata kisingizio cha dhambi zao. Walijisifia kwamba walikuwa na heri kuliko watu wengine, kwamba ndio wanaostahili baraka zake.

Mambo haya yameandikwa "ili kutuonya sisi, tuliofikiliwa na miisho ya zamani." 1 Wakorintho 10:11. Ni mara ngapi tunatafsiri vibaya baraka za Mungu, na kujisifia kwamba sisi tumependelewa kwa kuangalia wema wetu!

Mungu hawezi kufanya kwa ajili yetu kile ambacho anatafuta kutufanyia. Vipawa vyake vinatumika kuongeza matakwa yetu wenyewe, na kuifanya migumu mioyo yetu katika kutokuamini na dhambi.

Yohana aliwatangazia walimu wa Israeli kwamba kiburi chao, ubinafsi wao, na ukatili wao vilionyesha kwamba wao ni uzao wa nyoka wenye sumu, laana ya mauti kwa watu, badala ya kuwa watoto wa Ibrahimu mwenye haki na mtiifu. Kulingana na mtazamo wa nuru waliyokuwa wamepokea kutoka kwa Mungu, walikuwa wabaya kuliko hata wapagani, wale ambao waliwadhania kwamba wao wako juu kuliko wao. Walikuwa wameusahau mwamba ambao kutoka kwa huo walimegwa, na nafasi katika shimo mahali ambapo walikuwa wamechimbwa. Mungu alikuwa hategemewi nao kwa ajili ya kutimiza **(107)** kusudi lake. Kama alivyokuwa amemwita Ibrahimu kuondokana na watu wapagani, ndivyo ambavyo angewaita wengine katika huduma yake. Mioyo yao ingeonekana sasa isiyo na uhai kama mawe ya jangwani, lakini Roho wake angewabidisha kufanya mapenzi yake, na wangepokea utimilifu wa ahadi yake.

"Na sasa hivi," alisema nabii, "shoka limekwisha kuwekwa penye mashina ya miti; basi kila mti usiozaa matunda mazuri hukatwa na kutupwa motoni." Thamani ya mti haiamuliwi kwa kuangalia jina lake, bali kwa matunda yake. Ikiwa matendo hayafai, jina haliwezi kuuokoa mti kutokana na kuharibiwa. Yohana aliwaambia Wayahudi kwamba mwonekano wao mbele za Mungu ungetegemea tabia yao na maisha. Kujidai tu hakukufaa kitu. Ikiwa maisha yao na tabia zao havikukubaliana na sheria ya Mungu, hawakuwa watu wake.

Katika maneno ya Yohana yanayopeleleza moyo, wasikilizaji wake walijiona kuwa na hatia. Walikuja kwake wakiuliza, "Tufanye nini basi?" akawajibu, "Mwenye kanzu mbili na ampe asiye na kanzu; na mwenye vyakula na afanye vivyo hivyo." Na aliwaonya watoza ushuru dhidi ya kutotenda haki, askari dhidi ya kutumia mabavu.

Alisema kwamba wote waliokuwa raia wa ufalme wa Kristo wangedhihirisha imani na toba. Huruma, uaminifu, na wema vingeonekana katika maisha yao. Wangetoa huduma kwa wahitaji, na kuleta sadaka zao kwa Mungu. Wangewakinga wasio na kinga, na kuwa kielelezo cha wema na upendo. Hivyo ndivyo ambavyo wafuasi wa Kristo watadhihirisha nguvu ya Roho Mtakatifu ibadilishayo. Katika maisha ya kila siku, haki, rehema, na upendo vitaonekana. La sivyo wako kama makapi ya kutupwa motoni.

"Kweli mimi nawabatiza kwa maji;" alisema Yohana, "lakini yuaja mtu mwenye nguvu kuliko mimi, ambaye mimi sistahili kuilegeza gidamu ya viatu vyake; yeye atawabatiza kwa Roho Mtakatifu na kwa moto." Mathayo 3:11. Nabii Isaya alikuwa ametangaza kwamba Bwana angewasafisha watu wake kutokana na machafu yao "kwa roho ya hukumu na kwa roho ya kuteketeza." Neno la Bwana kwa Israeli lilikuwa, "Nitakuelekezea wewe mkono wangu, na kukutakasa takataka zako kabisa, na kukuondolea bati lako lote." Isaya 4:4; 1:25. Kwa dhambi, kila inapoonekana, "Mungu wetu ni moto ulao." Waebrania 12:29. Roho wa Mungu anakula dhambi kwa wote wanaojisalimisha kwake. Lakini ikiwa watu wanang'ang'ania dhambi, hatimaye wanakuwa watu wanaotambulishwa pamoja nayo. Hapo ndipo lazima utukufu wa Mungu, unaoharibu dhambi, utawaharibu nao. Baada ya usiku wa kushindana na Malaika, Yakobo alihamaki, "Nimeonana na Mungu uso kwa uso, na nafsi yangu imeokoka." Mwanzo 32: 30.

**(108)** Yakobo alikuwa na hatia ya dhambi kubwa iliyotokana na kibaya alichomtendea Esau; lakini alikuwa ametubu. Uovu wake ulikuwa umesamehewa, na alikuwa ameoshwa dhambi yake; kwa hiyo angestahimili ufunuo wa kuwepo kwa Mungu. Lakini kila mahali ambapo watu walikuja mbele za Mungu wakiwa na uovu kwa makusudi, waliangamizwa. Wakati wa kuja kwa Kristo mara ya pili waovu watateketezwa "kwa pumzi ya kinywa chake," na kuangamizwa kwa "ufunuo wa kuwapo kwake." 2 Wathesalonike 2:8. Nuru ya utukufu wa Mungu, ambayo inaleta uzima kwa wenye haki, itawaua waovu.

Mnamo wakati wa Yohana Mbatizaji, Kristo alikuwa atokee kama mfunuaji wa tabia ya Mungu. Uwepo wake tu ungewadhihirishia watu dhambi yao. Ni pale tu ambapo wangekuwa tayari kuoshwa dhambi zao ndipo wangeweza kuingia katika mjumuiko pamoja naye. Ni wenye moyo safi tu ambao wangekuwa naye katika uwepo wake.

Hivyo ndivyo Mbatizaji alivyoutangaza ujumbe ujumbe wa Mungu kwa Israeli. Wengi walizingatia mafundisho yake. Wengi walitoa vyote ili kutii. Makutano walimfuata mwalimu huyu mpya kutoka sehemu moja hadi nyingine, na si wachache waliolishikilia tumaini kwamba yawezekana ndiye Masihi. Lakini pindi Yohana alipoona watu wakimgeukia yeye, alitafuta kila fursa ya kuelekeza imani yao kwake Yeye aliyekuwa anakuja.

# Sura ya 11

## Ubatizo

[Sura hii imejengwa katika Mathayo 3:13-17; Marko 1:9-11; Luka 3:21, 22.]

Habari za nabii wa nyikani na matangazo yake ya ajabu zilisambaa katika Galilaya yote. Ujumbe wake uliwafikia hata wakulima walio katika maeneo ya ndani sana katika miji ya vilimani, na kwa makundi ya wavuvi kando ya bahari, na katika mioyo hii rahisi na ya dhati ujumbe ulipata mwitikio wa kweli. Kule Nazareti habari hizo zilisimuliwa katika karakana iliyokuwa ya Yusufu, na Mmoja aliutambua wito ule. Wakati wake ulikuwa umewadia. Akiondoka katika kazi yake ngumu ya siku, alimuaga mama yake, na akafuata nyayo za watu wa nchi yake waliokuwa wakifurika kwenda Yordani.

Yesu na Johana Mbatizaji walikuwa mtu na binamu yake, na walikuwa na uhusiano wa karibu katika kuzaliwa kwao; lakini hawakuwa wamefahamiana moja kwa moja. Yesu alikuwa ameishi maisha yake Nazareti ya Galilaya; na Yohana alikuwa ameishi katika nyika ya Uyahudi. Katika mazingira yanayotofautiana sana walikuwa wameishi kwa utengano, na hawakuwa wamekuwa na mawasiliano yoyote baina yao. Mungu alikuwa amepanga hivyo. Hakukuwa na uwezekano wa kudai kwamba walikuwa wamekula njama ya kuonyesha kukubaliana katika madai ya kila mmoja wao.

Yohana alikuwa anajua matukio yaliyoonyesha kuzaliwa kwa Yesu. Alikuwa amesikia habari ya kwenda kwake Yerusalemu wakati wa uvulana wake, na kile kilichotokea katika shule ya marabi. Alijua habari ya maisha yake yasiyo na dhambi, na alimwamini kuwa ni Masihi; lakini kuhusu hili hakuwa na uhakika kabisa. Ile hali ya kwamba Yesu alikuwa amebaki katika kujitenga kwa miaka mingi, pasipo kutoa uthibitisho wowote maalum wa utume wake, ilitoa mwanya wa **(110)** mashaka kama kweli angekuwa Yeye Aliyeahidiwa. Mbatizaji, hata hivyo, alisubiri kwa imani, akiamini kwamba katika muda muafaka wa Mungu yote yatawekwa wazi. Ilikuwa imefunuliwa kwake kwamba Masihi angetafuta kubatizwa katika mikono yake, na ya kwamba ishara ya tabia yake ya kimbingu ingetolewa. Hivyo angewezeshwa kumtangaza kwa watu.

Wakati Yesu alipokuja kubatizwa, Yohana aliona ndani yake usafi wa tabia ambao hajapata kuona ndani ya mtu yeyote. Mazingira yaliyomzunguka yalikuwa matakatifu na ya kushangaza. Miongoni mwa makutano waliokuwa wanamzunguka pale Yordani, Yohana alikuwa amesikia visa vibaya vya uhalifu, na alikuwa amekutana na roho ambazo zimelewa na mzigo wa dhambi zisizohesabika; lakini alikuwa hajapata kukutana na mwanadamu ambaye alitoa pumzi ya kiungu kiasi hicho. Yote haya yalikubaliana na vile Yohana alivyokuwa amefunuliwa kuhusu Masihi. Lakini alisita kukubali ombi la Yesu. Ingekuwaje yeye, mdhambi, ambatize Yeye Asiye na dhambi? Na kwa nini Yeye ambaye hakuhitaji kufanya toba ajisalimishe katika kaida iliyoashiria kukiri hatia inayotakiwa kuoshwa?

**(111)** Pindi Yesu alipoomba kubatizwa, Yohana alisita, akahamaki, "Mimi nahitaji kubatizwa na wewe, nawe waja kwangu?" Kwa mamlaka imara lakini kwa upole, Yesu alijibu, "Kubali hivi sasa; kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote." Na Yohana, akikubaliana, alimpeleka Yesu ndani ya Yordani, na kumtosa ndani ya maji. "Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini; na tazama, mbingu zikamfunukia, akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua, akija juu yake."

Yesu hakupata ubatizo kama kukiri dhambi zake mwenyewe. Alijihesabu miongoni mwa wenye dhambi, akipiga hatua ambazo tunapaswa kupiga, na akifanya kazi ambayo tunapaswa kufanya. Maisha yake ya maumivu na ustahimilivu baada ya kubatizwa kwake yalikuwa pia ni kielelezo kwetu.

Wakati akipanda kutoka majini, Yesu alipiga magoti penye ukingo wa mto akaomba. Zama mpya na ya muhimu ilikuwa inafunguka kwake. Sasa alikuwa katika jukwaa pana zaidi, akiingia katika pambano la maisha yake. Ingawa alikuwa Mfalme wa Amani, lazima kuja kwake kuwe kama kufutwa kwa upanga kutoka alani. Ufalme ambao alikuja kusimika ulikuwa kinyuma na ule ambao Wayahudi walitarajia. Yeye aliyekuwa msingi wa kaida na mfumo wa kafara wa Israeli angeonekana kama adui na mharibifu wa Israeli. Yeye aliyeitamka sheria juu ya mlima Sinai angehukumiwa kama mvunja sheria. Yeye aliyekuwa amekuja ili kuvunja nguvu za Shetani angedhihakiwa kwa kuitwa Beelzebuli. Hakuna hata mmoja duniani ambaye alikuwa amemwelewa, na wakati

wa huduma yake lazima aenende peke yake. Katika maisha yake yote mama yake na ndugu zake hawakuelewa utume wake. Hata wanafunzi wake hawakumwelewa. Alikuwa yuko katika nuru ya milele, kama mmoja na Mungu, lakini lazima maisha yake duniani yawe ya upweke.

Kama mmoja wetu, ni lazima abebe mzigo wa hatia na shida zetu. Lazima Yeye Asiye na dhambi aone aibu ya dhambi. Lazima Yeye apendaye amani akae katikati ya vurugu, Aliye mkweli akae pamoja na uongo, msafi awe pamoja na uchafu. Kila dhambi, kila tofauti, kila dhara la unajisi vilivyoletwa na uasi, vilikuwa mateso katika roho yake.

Lazima atembee katika njia peke yake; lazima abebe mzigo akiwa peke yake. Lazima ukombozi wa ulimwengu uwe juu yake Yeye aliyeacha utukufu na kukubali kuwa katika udhaifu wa mwanadamu. Aliona na kuhisi mzigo wote, lakini kusudi lake lilisimama imara. Wokovu wa jamii ya wanadamu walioanguka ulitegemea mkono wake, na aliunyosha mkono wake kuupata mkono wa Upendo wa Mungu.

Mwonekano wa Mwokozi ulionekana kama kuzipenya mbingu pindi alipoimwaga nafsi yake katika maombi. Anajua vema jinsi dhambi ilivyoifanya mioyo ya watu kuwa migumu, **(112)** na jinsi itakavyokuwa vigumu kwao kuijali kazi yake, kukubali zawadi ya wokovu. Anamwomba Baba kwa ajili ya kupata nguvu ya kushinda kutokuamini kwao, kuivunja minyororo ambayo Shetani amewafunga, na kwa niaba yao kumshinda mwenye kuharibu. Anaomba ushuda kwamba Mungu akubali ubinadamu ulio ndani ya Mwana wake.

Kamwe malaika walikuwa hawajapata kusikia ombi kama lile. Wana hamu ya kumpelekea jemadari wao mpendwa ujumbe wa uhakikisho na faraja. Lakini sivyo; Baba mwenyewe atajibu ombi la Mwana wake. Miale ya utukufu wake inatoka katika kiti cha enzi. Mbingu zinafunguka, na kwenye kichwa cha Mwokozi inashuka nuru angavu katika umbo kama hua, - nembo yake sahihi, Yeye aliye mnyenyekevu na mpole.

Miongoni mwa makutano pale Yordani, wachache sana ukiacha Yohana walibaini maono yale ya mbinguni. Lakini mazingira ya uwepo wa hali ya kimbingu yalikuwepo kwa makutano wale. Watu walikaa kimya wakimwangalia Kristo. Umbo lake liliogeshwa katika nuru ile inayozunguka daima kiti cha enzi. Uso wake wa hali ya chini ulitukuzwa kwa namna ambayo uso wa mwanadamu haujapata kuonekana. Kutoka katika mbingu zilizofunguka sauti ilisikika ikisema, "Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye."

Maneno haya ya uthibitisho yalitolewa ili kukaza imani ndani ya wale walioshuhudia tukio hilo, na kumtia nguvu Mwokozi kwa ajili ya kazi yake. Licha ya kuwa dhambi za ulimwengu wenye hatia zilikuwa zimewekwa juu ya Kristo, licha ya kujishusha na kujitwisha hali yetu ya dhambi, sauti kutoka mbinguni ilimtangaza kuwa Mwana wa Yeye Aliye wa milele.

Yohana aliguswa sana alipomwona Yesu amepiga magoti akiomba, akibembeleza kwa machozi ili kupata kibali cha Baba. Wakati utukufu wa Mungu ulipomzunguka, na sauti kutoka mbinguni kusikika, Yohana alikumbuka jambo ambalo Mungu alikuwa ameahidi. Alijua kwamba aliyebatizwa naye alikuwa Mkombozi wa ulimwengu. Roho Mtakatifu alimjilia, na kwa mkono ulionyooshwa kuelekeza kwa Yesu, alisema kwa sauti kuu, Tazama Mwana-kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu."

Hakuna hata mmoja wa watu waliosikia maneno hayo, hata yeye mwenyewe aliyeyasema, aliyeelewa umuhimu wa maneno haya, "Mwana-kondoo wa Mungu." Kwenye Mlima Moria, Ibrahimu alikuwa amesikia swali la mwanae, "Babangu! . . . yuko wapi mwana-kondoo kwa sadaka ya kuteketezwa? Baba yake alijibu, "Mungu atajipatia mwana-kondoo kwa hiyo sadaka, mwanangu." Mwanzo 22:7, 8. Na katika kondoo mume aliyetolewa na mbingu mahali pa Isaka, Ibrahimu aliona ishara ya Yeye ambaye angekufa kwa ajili ya dhambi za wanadamu. Roho Mtakatifu kupitia Isaya, akichukua kielelezo hicho, alitabiri kuhusu Mwokozi, Aletwa **(113)** "Kama mwana-kondoo apelekwaye machinjoni" "na Bwana ameweka juu yake maovu yetu sisi sote" (Isaya 53:7, 6); lakini watu wa Israeli hawakuwa wameelewa somo hilo. Wengi wao walichukulia sadaka za kuteketezwa sana kama vile wapagani walivyochukulia kafara zao, - kama matoleo ambayo kwayo wao wenyewe wangemshawishi Mungu. Mungu alitaka kuwafundisha kwamba katika pendo lake kunatoka matoleo ambayo yanawapatanisha wao na Yeye.

Na neno lililosemwa kwa Yesu pale Yordani kwamba, "Huyu ni Mwanangu mpendwa, ninayependezwa naye," linakumbatia ubinadamu. Mungu aliongea na Yesu kama mwakilishi wetu. Pamoja na dhambi zetu na udhaifu

wetu wote, hatujatupwa kando kama wasiostahili. "Ametuneemesha katika huyo Mpendwa." Waefeso 1:6. Utukufu ambao ulikuja kwa Kristo ni ahadi ya upendo wa Mungu kwetu. Unatujulisha kuhusu nguvu ya maombi, - jinsi ambavyo sauti ya mwanadamu inaweza kulifikia sikio la Mungu, na mahitaji yetu kuzifikia mbingu. Kwa sababu ya dhambi, dunia ilitengwa na mbingu, na kutengwa na ushirika wake; lakini Yesu alikuwa ameiunganisha tena na utukufu ule. Pendo lake limemzunguka mwanadamu, na limefika mbinguni juu. Nuru ile iliyomshukia kutoka katika milango iliyo wazi itatushukia kadiri tunavyoomba kusaidiwa kuyapinga majaribu. Sauti ile iliyotolewa kwa Yesu inasema kwa kila nafsi iaminiyo, Huyu ni mtoto wangu mpendwa, ninayependezwa naye.

"Wapenzi, sasa tu wana wa Mungu, wala haijadhihirika bado tutakavyokuwa; lakini twajua ya kuwa atakapodhihirishwa, tutafanana naye; kwa maana tutamwona kama alivyo." 1 Yohana 3:2. Mwokozi amefungua njia ili kwamba hata aliye mdhambi kuliko wote, mhitaji kuliko wote, aliyekandamizwa na kudharauliwa kuliko wote, apate kumfikia Baba. Ili wote wapate mahali pao katika makao ambayo Yesu amekwenda kuandaa. "Haya ndiyo anenayo yeye aliye mtakatifu, aliye wa kweli, aliye na ufunguo wa Daudi, yeye mwenye kufungua wala hapana afungaye, naye afunga wala hapana afunguaye. . . . Tazama, nimekupa mlango uliofunguliwa mbele yako, ambao hapana awezaye kuufunga." Ufunuo 3:7, 8.

## Sura ya 12

# Kujaribiwa

[Sura hii imejengwa katika Mathayo 4:1-11; Marko 1:12, 13; Luka 4:1-13.]

Na Yesu akiwa amejawa na Roho Mtakatifu alirudi kutoka Yordani, na aliongozwa na Roho kwenda nyikani. Maneno ya Marko bado yana umuhimu zaidi. Anasema, "Mara Roho akamtoa aende nyikani. Akawako huko jangwani siku arobaini, hali akijaribiwa na Shetani; naye alikuwa pamoja na wanyama wa mwitu." "Na siku hizo alikuwa hali kitu."

Wakati Yesu alipoongozwa kwenda jangwani kujaribiwa, aliongozwa na Roho wa Mungu. Hakukaribisha majaribu. Alienda jangwani kukaa peke yake, kutafakari utume wake na kazi yake. Kwa kule kufunga na kuomba alikuwa ajiimarishe mwenyewe kwa ajili ya njia yenye alama ya damu ambayo angeipita. Lakini Shetani alijua kwamba Mwokozi ameenda jangwani, na aliona kwamba huu ndio wakati muafaka wa kumkabili.

Masuala makuu kwa ajili ya ulimwengu yalikuwa hatarini katika pambano kati ya Mfalme wa nuru na kiongozi wa ufalme wa giza. Baada ya kumjaribu mwanadamu na kumwangusha dhambini, Shetani alidai kwamba dunia ni yake, na alijiita mfalme wa ulimwengu. Akiisha kuwaweka baba na mama wa wanadamu katika hali yake, alifikiria kusimamisha himaya yake hapa. Alitangaza kwamba wanadamu wamemchagua yeye kuwa mtawala wao. Kupitia **(115)** udhibiti wake kwa wanadamu, alishikilia umiliki wa ulimwengu wote. Kristo alikuja kuondoa madai hayo ya Shetani. Kama Mwana wa Adamu, Kristo angesimama kumtii Mungu. Hivyo ingeonyeshwa kwamba Shetani hakupata umiliki kamili wa wanadamu, na ya kwamba madai yake kuhusu ulimwengu yalikuwa ya uongo. Wote ambao wangehitaji kukombolewa kutoka katika utawala wake wangewekwa huru. Utawala ule ambao Adamu alipoteza kwa sababu ya dhambi ungerejeshwa.

Tangu tangazo lile lililotolewa kwa nyoka kule Edeni, "Nitaweka uadui kati yako na mwanamke, na kati ya uzao wako na uzao wake" (Mwanzo 3:15), Shetani alikuwa amejua kwamba hakuwa na mamlaka kamili juu ya ulimwengu. Ndani ya watu kulionekana kuwepo kwa nguvu za kupingana na utawala wake. Kwa umakini mkubwa aliziangalia kafara zilizotolewa na Adamu na wana wake. Katika maadhimisho haya aliona alama ya ushirikiano kati ya dunia na mbingu. Alijipanga kukata mawasiliano haya. Alimtangaza Mungu vile asivyo, na akatafsiri isivyo kaida zile zilizoelekeza kwa Mwokozi. Wanadamu waliongozwa kumwogopa Mungu kwamba ndiye anayewaangamiza. Kafara ambazo zingeonyesha upendo wake zilitolewa kama namna ya kutuliza hasira yake. Shetani aliamsha hisia za uovu ndani ya wanadamu, ili kuimarisha utawala wake kwao. Wakati neno la Mungu lililoandikwa lilipotolewa, Shetani alichunguza unabii wa kuja kwa Mwokozi. Kutoka kizazi hata kizazi alifanya kazi ya kuwapofusha watu kuhusu unabii huu, ili kwamba wamkatae Kristo ajapo.

Wakati wa kuzaliwa kwa Yesu, Shetani alijua kuwa Yesu amekuja na utume wa kimbingu kuharibu utawala wake. Alitetemeshwa na ujumbe wa malaika waliotoa ushuhuda wa mamlaka ya Mfalme aliyezaliwa. Shetani alijua vema nafasi ambayo Yesu alikuwa amekalia kule mbinguni kama Mpendwa wa Baba. Kwamba Mwana wa Mungu angekuja katika dunia hii kama mwanadamu lilimjaza mshangao na kutokutulia. Hakuweza kuelewa siri ya kafara hii. Roho yake ya ubinafsi haikuweza kuelewa upendo wa jinsi hiyo kwa ajili ya jamii iliyodanganywa. Utukufu na amani ya mbinguni, na raha ya kuwa pamoja na Mungu, vilikuwa vinaeleweka kwa wanadamu katika uhafifu tu; lakini **(116)** vilikuwa vinajulikana vema kwa Lusifa, kerubi afunikaye. Kwa kuwa alikuwa amepoteza mbingu, aliazimu kutafuta kulipiza kwa kuwafanya wengine pia washiriki anguko lake. Angefanya hili kwa kuwafanya washushe thamani ya vitu vya mbinguni, na kuelekeza mioyo katika vitu vya duniani.

Jemadari wa mbinguni hakuzileta roho za watu katika ufalme wake pasipo upinzani. Tangu wakati alipokuwa mtoto mchanga kule Bethlehemu, alikuwa anawindwa na mwovu muda wote. Sura ya Mungu ilidhihirika ndani ya Kristo, na katika mashauri ya Shetani iliazimiwa kwamba lazima ashindwe. Hakuna mwanadamu aliyekuja duniani akakwepa nguvu za mdanganyaji huyu. Nguvu za majeshi ya mwovu zilipangwa kumfuatilia na kufanya vita dhidi yake, na ikiwezekana kupata ushindi dhidi yake.

Wakati wa kubatizwa Mwokozi, Shetani alikuwa miongoni mwa mashuhuda wale. Aliona utukufu wa Baba ukimfunika Mwana wake. Alisikia sauti ya Yehova ikishuhudia uungu wa Yesu. Daima tangu dhambi ya Adamu,

wanadamu wametengwa na mawasiliano ya moja kwa moja na Mungu; mahusiano kati ya dunia na mbingu yalikuwa yamefanyika kupitia Kristo; lakini sasa Baba mwenyewe alisema kwamba Yesu alikuwa amekuja "katika mfano wa mwili ulio wa dhambi" (Warumi 8:3). Kabla ya hapo alikuwa amewasiliana na wanadamu *kupitia* Kristo; lakini sasa aliwasiliana na wanadamu *katika* Kristo. Shetani alitaraji kwamba hali ya Mungu kukataa uovu ingeleta utengano wa milele kati ya mbingu na dunia. Lakini sasa ilikuwa dhahiri kwamba mwunganiko kati ya Mungu na mwanadamu ulikuwa umerejeshwa.

Shetani aliona kwamba ni lazima ama ashinde au ashindwe. Mambo ya mapambano haya kwa kawaida huhusisha zaidi malaika zake wa karibu. Sasa lazima yeye mwenyewe ahusike katika vita hii. Nguvu zote za uasi zilihusika dhidi ya Mwana wa Mungu. Kristo alikuwa mlengwa wa kila silaha ya kuzimu.

Wengi wanaiangalia vita hii kati ya Kristo na Shetani kama vile haina uhusiano maalum na maisha yao; na kwao wanaona kama hawana jambo la kufanya nayo. Lakini katika kila eneo la moyo wa mwanadamu pambano hili linarudiwa. Kamwe hakuna mtu anayeondoka katika himaya ya Shetani kwenda kumtumikia Mungu pasipo kukutana na mashambulizi ya Shetani. Vishawishi ambavyo Yesu alipinga vilikuwa vile ambavyo tunakutana navyo vikiwa vigumu kuvistahimili. Vililetwa kwake kwa uzito mkubwa kulingana na vile tabia yake ilivyo juu sana kuliko yetu. Akiwa amebeba uzito wa kutisha wa dhambi ya ulimwengu, Kristo alistahimili jaribu kuhusu hamu ya kula, jaribu la kuupenda ulimwengu, na jaribu la kupenda kujionyesha. Haya ni **(117)** majaribu yaliyomshinda Adamu na Hawa, na ambayo kwa haraka hutushinda.

Shetani alielekeza kwa dhambi ya Adamu kama uthibitisho kwamba sheria ya Mungu ilikuwa isiyo ya haki, na ya kwamba haiwezekani kuitii. Katika ubinadamu wetu, Kristo alikuwa afidie kuanguka kwa Adamu. Lakini Adamu aliposhindwa na mjaribu, hakuna chochote kati ya madhara ya dhambi kilichokuwa kwake. Alikuwa katika nguvu za utu mkamilifu, akiwa na nguvu, mwili na akili. Alikuwa amezungukwa na utukufu wa Edeni, na alikuwa katika ushirika na viumbe wa mbinguni. Haikuwa hivyo pale Yesu alipoingia jangwani kukutana na Shetani. Kwa miaka elfu nne wanadamu walikuwa wameendelea kupungua nguvu za mwili, uwezo wa akili, uwezo wa kimaadili; na Kristo alichukua madhaifu haya ya mwanadamu. Ili tu amwokoe mwanadamu kutoka katika vina vya chini kabisa vya uharibifu.

Wengi wanadai kwamba ilikuwa haiwezekani kwa Kristo kushindwa na majaribu. Kama ndivyo basi alipowekwa katika nafasi ya Adamu; asingepata ushindi ambao Adamu alishindwa kuupata. Kama tuna pambano la aina yoyote lenye majaribu zaidi ya lile la Yesu, basi angekuwa na uwezo wa kutusaidia. Lakini Mwokozi wetu alichukua ubinadamu, pamoja na mapungufu yake yote. Alichukua hali ya mwanadamu, akiwa na uwezekano wa kushindwa na majaribu. Hatuna kitu cha kustahimili ambacho Yeye hakustahimili.

Kwa Kristo, kama ilivyokuwa kwa wale wawili katika Edeni, uchu wa chakula ndio msingi wa kwanza wa jaribu kuu. Pale pale uharibifu ulipoanzia, lazima kazi ya ukombozi wetu ianzie hapo. Kama vile ambavyo tamaa ya hamu ya chakula ilivyomwangusha Adamu, vivyo hivyo kwa kuikana hamu ya chakula lazima Kristo ashinde. "Akafunga siku arobaini mchana na usiku, mwisho akaona njaa. Mjaribu akamjia akamwambia, Ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu, amuru kwamba mawe haya yawe mikate. Naye akajibu akasema, Imeandikwa, Mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu."

Tangu wakati wa Adamu hadi Kristo, kutafuta kukidhi matakwa ya mwili kumeongeza nguvu za uchu na hisia za kujifurahisha, mpaka kulipokuwa karibu na kutokuwa na kikomo cha kudhibitiwa. Hivyo watu walikuwa wameshuka viwango na kuwa wagonjwa, na kwao wenyewe ilishakuwa haiwezekani kushinda hilo. Kwa niaba ya mwanadamu, Yesu alishinda kwa kustahimili jaribu kali sana. Kwa ajili yetu alionyesha uwezo wa kujitawala kwa nguvu ya kushinda njaa na kifo. Na katika ushindi huu wa kwanza yalihusishwa mambo mengine ambayo yanaingia katika pambano dhidi ya nguvu za giza.

**(118)** Wakati Yesu alipoingia jangwani, alifungiwa katika utukufu wa Mungu. Akiwa amezama katika ushirika na Mungu, aliinuliwa juu zaidi ya udhaifu wa mwanadamu. Lakini utukufu ulitoweka, na akaachwa apambane na majaribu. Yalikuwa yanamsukuma kila wakati. Hali yake ya ubinadamu iliogopa pambano lililokuwa linamsubiri. Alifunga na kuomba kwa siku arobaini. Akiwa amedhoofu na kuchoshwa na njaa, akiwa amechoshwa na mateso ya akili, "uso wake ulikuwa umeharibiwa sana zaidi ya mtu yeyote, na umbo lake zaidi ya wanadamu." Isaya 52:14. Hii ndiyo ilikuwa fursa ya Shetani. Sasa alijua angemshinda Kristo.

Kwa Mwokozi, kilikuja kitu kama jibu la maombi yake, akija mmoja aliyejifanya kuwa malaika kutoka mbinguni. Alidai kuwa na ujumbe kutoka kwa Mungu kutangaza kwamba mfungo wa Kristo ulikuwa umekwisha. Kama vile Mungu alivyomtuma malaika kuzuia mkono wa Ibrahimu asimtoe Isaka, vivyo hivyo, akiwa ameridhishwa na uhiari wa Kristo kuipita njia yenye alama ya damu, Baba amemtuma malaika kumwokoa. Huu ni ujumbe ulioletwa kwa Yesu. Mwokozi alikuwa amenyong'onyea kwa njaa, alikuwa na shida ya chakula, wakati Shetani alipomjia ghafla. Akielekeza kidole kwenye mawe yaliyotawanyika jangwani, na ambayo yalikuwa na mwonekano kama wa mikate, mjaribu alisema, "Ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu, amuru kwamba mawe haya yawe mikate."

Ingawa anaonekana kama malaika wa nuru, haya maneno ya kwanza kabisa yanasaliti tabia yake. "Ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu." Hapa kuna kiashiria cha kutoamini. Ikiwa Yesu angefanya mapendekezo ya Shetani, ingekuwa ni kukubali mashaka. Mjaribu anapanga kumpindua Kristo kwa mbinu zile zile alizotumia kwa mwanadamu hapo mwanzo. Ni kwa ustadi jinsi gani Shetani alivyoingia kwa Hawa mle Edeni! "Ati! Hivi ndivyo alivyosema Mungu, Msile matunda ya miti yote ya bustani?" Mwanzo 3:1. Mpaka hapo maneno ya mjaribu yalikuwa ya kweli; lakini kwa jinsi alivyoyaongea kulikuwa na hali ya kuficha maneno ya Mungu. Kulikuwa na namna ya kuyakataa iliyojificha, mashaka ya kuhusu ukweli wa maneno ya Mungu. Shetani alitafuta kuingiza katika akili ya Hawa mawazo kwamba Mungu asingeweza kufanya kile alichokuwa amesema; kwamba kuuzuia ule mti mzuri vile kulikuwa kunapingana na na upendo na huruma yake kwa mwanadamu. Vivyo hivyo mjaribu anatafuta kumshawishi Kristo kwa hisia zake mwenyewe. "Ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu." Maneno hayo yana uchungu katika mawazo ya Shetani. Katika namna sauti ilivyotolewa kuna jinsi ya kuonyesha ukakasi. Je, Mungu angemtendea Mwana wake hivi? Angemwacha jangwani akiwa na wanyama wa mwitu; bila ya chakula, bila marafiki, bila faraja? Anadhani kwamba Mungu hakumaanisha kamwe kwamba Mwana wake awe katika hali kama hii. "Ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu," onyesha nguvu zako kwa **(119)** kujiokoa na njaa hii inayokusumbua. Amuru kwamba jiwe hili lifanyike kuwa mkate.

Maneno yaliyotoka mbinguni, "Huyu ni Mwanangu mpendwa wangu, ninayependezwa naye" (Mathayo 3:17), yalikuwa bado yanasikika katika masikio ya Shetani. Lakini alikuwa ameazimia kumfanya Kristo asiamini ushuhuda huu. Neno la Mungu lilikuwa ni hakikisho la utume wa Yesu wa kimbingu. Alikuwa amekuja kuishi kama mwanadamu miongoni mwa wanadamu, na ilikuwa ni neno lile lililotangaza muunganiko wa Yesu na mbingu. Kusudi la Shetani ilikuwa ni kusababisha Yesu atilie mashaka lile neno. Shetani alijua kwamba ikiwa ujasiri wa Kristo katika Mungu ungetikisika, ushindi katika pambano lote ungekuwa wake. Angemshinda Yesu. Alitumaini kwamba katika madhila ya njaa na kukosa tumaini, Kristo angepoteza imani kwa Baba yake, na kutenda mwujiza kwa ajili yake mwenyewe. Ikiwa angefanya hili, mpango wa wokovu ungekuwa umevunjwa.

Wakati Shetani na Mwana wa Mungu walipokutana mara ya kwanza katika pambano, Kristo alikuwa jemedari wa majeshi ya mbinguni; na Shetani, akiwa kiongozi wa uasi mbinguni, alitupwa nje. Sasa hali zao zimekuwa kinyume, na Shetani anajitahidi kuitumia vizuri iwezekanavyo hali hii aliyofikiri ni nafasi yake. Anasema, Mmoja wa malaika wenye nguvu sana amefukuzwa mbinguni. Kuonekana kwa Yesu kunaonyesha kwamba ndiye huyo malaika aliyefukuzwa, akiwa amekataliwa na Mungu, na akiwa ameachwa na wanadamu. Hali ya uungu ingeweza kumsaidia Shetani kuthibitisha madai yake kwa kufanya mwujiza; "Ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu, amuru mawe haya yawe mkate." Shetani alisisitiza kwamba kitendo hicho cha uwezo wa kuumba, kingethibitisha uungu wake. Kwamba kingelifikisha mwisho pambano lile.

Kitendo cha Yesu kumsikiliza mwongo mkuu huku akiwa kimya hakikufanyika pasipo pambano ndani yake. Lakini Mwana wa Mungu asingethibitisha uungu wake kwa Shetani, au kufafanua sababu ya madhila yale. Kwa kutekeleza matakwa ya muasi, hakuna jema ambalo lingepatikana kwa ajili ya mwanadamu au kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Ikiwa Kristo angekubali mapendekezo ya adui, bado Shetani angesema hivi, Nionyeshe ishara nipate kujua kwamba wewe ni Mwana wa Mungu. Ushahidi usingefaa katika kuvunja nguvu za uasi uliokuwa moyoni mwa Shetani. Na Kristo asingeonyesha nguvu za uungu kwa manufaa yake mwenyewe. Alikuwa amekuja kukabili majaribu kama ambavyo lazima tufanye, akituachia kielelezo cha imani na kunyenyekea. Iwe ni wakati huu au wakati mwingine baadaye hakufanya mwujiza kwa ajili yake mwenyewe. Miujiza yake ya ajabu ilikuwa kwa ajili ya mafanikio ya wengine. Ingawa Yesu alimgundua Shetani tangu mwanzo, hakusukumwa kuingia katika pambano dhidi yake. Akipata nguvu kutokana na kumbukumbu ya sauti **(120)** kutoka mbinguni, alitulia katika pendo la Baba yake. Asingejikutanisha na majaribu.

Yesu alikabiliana na Shetani kwa maneno ya Maandiko. Alisema "Imeandikwa." Katika kila jaribu silaha yake ilikuwa neno la Mungu. Shetani alidai apate kwa Kristo mwujiza kama ishara ya uungu wake. Lakini kile ambacho ni zaidi ya mwujiza, kutegemea kabisa maneno kwamba "Bwana asema hivi," kilikuwa ishara ambayo haikuwezekana kupingwa. Kwa kuwa Kristo alishikilia mahali hapo, mjaribu hakupata mafanikio.

Wakati Kristo alipokuwa amedhoofu sana ndipo alipokabiliwa na majaribu makali mno. Hapo Shetani alijua kwamba anashinda. Amepata kuwashinda wanadamu kwa njia hii. Wakati nguvu zinapopungua, na uwezo wa utashi unapodhoofika, na imani inapokoma kuelekea kwa Mungu, ndipo waliposhindwa wale waliokuwa wamesimama imara kwa muda mrefu. Wakati Musa alipokuwa amechoshwa na miaka arobaini ya Waisraeli kuzunguka jangwani ndipo alipopoteza imani yake kwa muda na kuacha kumshikilia mwenye uwezo wa milele. Alianguka karibu na mipaka ya Nchi ya Ahadi. Hivyo ndivyo ilivyokuwa pia kwa Eliya, aliyekuwa amesimama kwa ujasiri mbele ya mfalme Ahabu, ambaye alikuwa amekabiliana na taifa lote la Israeli, wakiwa na manabii mia nne na hamsini wa Baali mbele yao. Baada siku ile ya kutisha kwenye mlima Karmeli, wakati manabii wa uongo walipokuwa wameuawa, na watu walikuwa wametangaza kumwabudu Mungu, Eliya alikimbia kuponya maisha yake kutokana na vitisho vya mwanamke mzinzi Yezebeli. Hivyo ndivyo ambavyo Shetani amekuwa akinufaika na udhaifu wa mwanadamu. Na ataendelea kufanya kazi kwa njia hiyo hiyo. Popote ambapo mtu anazungukwa na mawingu, anapochanganywa na hali iliyopo, anaposumbuliwa na umaskini na maumivu, Shetani yupo karibu yake ili kumjaribu na kumkatisha tamaa. Anatushambulia katika tabia zile ambazo tu dhaifu. Anatafuta kutikisa ujasiri wetu kwa Mungu, anayeruhusu hali ya mambo kama hiyo iwepo. Tunashawishiwa tusimwamini Mungu, na kuhoji kuhusu huo upendo wake. Mara nyingi mjaribu anakuja kwetu kama vile alivyokuja kwa Kristo, akionyesha mbele yetu **(121)** udahifu wetu na maradhi yetu. Anatamani kufadhaisha roho, na kuvunja uwezo wetu wa kumshikilia Mungu. Hapo anakuwa na uhakika wa mawindo yake. Ikiwa tungemkabili vile Yesu alivyomkabili, tungekwepa kushindwa kwingi. Kwa kucheza na adui, tunampa manufaa.

Wakati Kristo alipomwambia mjaribu kwamba, "Mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu," alirudia maneno ambayo alikuwa amemwambia Israeli zaidi ya miaka elfu moja na mia nne kabla: "Bwana, Mungu wako aliyokuongoza miaka hii arobaini katika jangwa. . . . Akakutweza, akakuacha uone njaa, akakulisha kwa mana, usiyoijua wewe wala baba zako hawakuijua; apate kukujulisha ya kuwa mwanadamu haishi kwa mkate tu, bali huishi kwa kila litokalo katika kinywa cha Bwana." Kumbukumbu 8:2, 3. Kule jangwani, wakati njia zote za kuwawezesha ziliposhindwa, Mungu aliwapelekea watu wake mana kutoka mbinguni; na mahitaji ya kutosha na ya wakati wote yalitolewa. Utoaji huu ulikuwa uwafundishe kwamba wakati walipomwamini Mungu na kutembea katika njia zake asingewaacha. Sasa Mwokozi aliweka katika vitendo somo lile alilotoa kwa Israeli. Kwa neno la Mungu msaada ulikuwa umetolewa kwa Waebrania, na kwa neno lile lile ungetolewa kwa Yesu. Alisubiri wakati wa Mungu kuleta msaada. Alikuwa jangwani kwa ajili ya kumtii Mungu, na asingepata chakula kwa kufuata mapendekezo ya Shetani. Mbele ya uwepo malimwengu yaliyokuwa yanashuhudia, Yesu alithibitisha kwamba ni bora kupata maumivu yawayo yoyote kuliko kuachana na mapenzi ya Mungu kwa namna yoyote.

"Mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu." Mara nyingi mfuasi wa Kristo huletwa mahali ambapo hawezi kumtumikia Mungu na kuweza kuendelea kufanya shughuli zake za misha ya duniani. Labda huonekana kama vile kutii baadhi ya matakwa ya Mungu vile yalivyo kutasababisha kukatika kwa njia za yeye kujikimu. Shetani humfanya mtu aamini kwamba ni lazima aitoe kafara imani yake. Lakini kitu kimoja pekee tunachohitaji katika ulimwengu huu ni kutegemea neno la Mungu. "Utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa." Mathayo 6:33. Hata katika maisha haya si salama kwetu kuachana na mapenzi ya Baba yetu wa mbinguni. Tunapojifunza nguvu ya neno lake, hatutafuata mapendekezo ya Shetani ili kupata chakula au kuyaokoa maisha. Maswali yetu pekee yatakuwa, Ipi ni amri ya Mungu? Na ahadi yake ni nini? Tukiyajua haya, tutalitii hilo moja, na kuamini hilo jingine.

Katika upinzani mkuu wa mwisho wa pambano dhidi ya Shetani, wale walio watii kwa Mungu wataona kwamba wametengwa na kila namna ya kujikimu katika maisha ya duniani. Kwa kuwa wanakataa **(122)** kuvunja sheria ya Mungu ili kutii mamlaka za kidunia, watazuiwa kununua au kuuza. Hatimaye itatangazwa kwamba yawapasa wauawe. Angalia Ufunuo 13:11-17. Lakini kwao wanaomtii Mungu ahadi inatolewa, "Huyu ndiye atakayekaa juu; majabali ni ngome yake; atapewa chakula chake; maji yake hayatakoma." Isaya 33:16. Watoto wa Mungu wataishi kwa ahadi hii. Wakati dunia itakapoangukiwa na njaa, wao watashibishwa. "Hawataaibika wakati wa

ubaya, Na siku za njaa watashiba." Ps. 37:19. Nabii Habakuki alitazamia wakati huo wa kufadhaisha, na maneno yake yanadhihirisha imani ya kanisa: "Maana mtini hautachanua maua, Wala mizabibuni hamtakuwa na matunda; Taabu ya mzeituni itakuwa bure, Na mashamba hayatatoa chakula; Zizini hamtakuwa na kundi, Wala vibandani hamtakuwa na kundi la ng'ombe; Walakini nitamfurahia Bwana Nitamshangilia Mungu wa wokovu wangu." Habakuki 3:17, 18.

Katika masomo yote ambayo tunaweza kujifunza kutokana na jaribu la kwanza la Bwana wetu hakuna ambalo ni muhimu zaidi kama lile linalohusu kudhibiti hamu ya kula na kunywa na mivuto ya tamaa. Katika zama zote, majaribu yanayohusisha vitu vionekanavyo yamefanikiwa mno kumpotosha na kumharibu mwanadamu. Kwa kukosa kiasi, Shetani anatafuta kuharibu uwezo wa kiakili na kimaadili ambao Mungu amemjalia mwanadamu ukiwa zawadi isiyoweza kukadiriwa kwa bei. Kwa sababu hiyo inakuwa haiwezekani kwa wanadamu kuthamini vitu vya umilele. Kwa kutafuta kutimiza haja za mwili, Shetani anatafuta kufuta kila alama ya kufanana na Mungu iliyo katika moyo wa mwanadamu.

Hali ya kujifurahisha pasipo kudhibitiwa na matokeo yake ya magonjwa na uharibifu vilivyokuwepo wakati wa kuja kwa Yesu mara ya kwanza vitakuwepo tena kabla ya kuja kwake mara ya pili, vikiwa na uovu mkali. Kristo alisema kwamba hali ya ulimwengu itakuwa kama ilivyokuwa wakati ule wa kabla ya Gharika, na kama ilivyokuwa Sodoma na Gomora. Kila ubunifu wa mawazo ya moyo utakuwa na uovu. Tunaishi sasa katika wakati huo wa kuogopesha, na kwetu lazima somo la Mwokozi la kufunga kula lituingie. Ni kwa kutumia tu shida ile kubwa isiyoelezeka iliyostahimiliwa na Kristo ndipo tunaweza kukadiria uovu wa tabia ya kujifurahisha nafsi. Kielelezo chake kinatangaza kwamba tumaini letu pekee la uzima wa milele ni kusalimisha hamu zetu za vyakula na vinywaji katika mapenzi ya Mungu.

Kwa nguvu zetu wenyewe haiwezekeni kukana matakwa ya hali yetu iliyoanguka. Kwa mfereji huu Shetani ataleta majaribu kwetu. Kristo alijua kwamba adui atakuja kwa kila mwanadamu, kutumia nafasi iliyopo ya udhaifu wa kurithi alio nao, na kwa ushawishi wake wa uongo atawanasa wote ambao hawamwamini Mungu. Na kwa kupitia mahali ambapo **(123)** lazima mwanadamu apite, Bwana wetu ameandaa njia kwa ajili ya sisi kushinda. Si mapenzi ya Bwana kwamba tuwekwe katika hali ngumu katika mapambano na Shetani. Asingependa kutuona tukitishwa na kukatishwa tamaa na mashambulizi ya yule joka. Alisema, "Jipeni moyo; mimi nimeushinda ulimwengu." Yohana 16:33.

Hebu mtu yeyote anayekabiliana na ugumu wa kudhibiti hamu ya kula na kunywa amwangalie Mwokozi katika jangwa la majaribu. Mtazame akiwa katika maumivu kwenye msalaba, pindi anapolia, "Naona kiu." Amestahimili yote yanayowezekana kwetu kustahimili. Ushindi wake ni wetu.

Yesu alitegemea hekima na nguvu za Baba yake wa mbinguni. Alisema, "Maana Bwana MUNGU atanisaidia; kwa sababu hiyo sikutahayari: . . . nami najua ya kuwa sitaona haya. . . . Tazama, Bwana MUNGU atanisaidia." Akielekeza katika kielelezo chake mwenyewe, anatwambia, "Ni nani miongoni mwenu amchaye Bwana, . . . Yeye aendaye katika giza, wala hana nuru, naye alitumainia jina la Bwana, na kumtegemea Mungu wake." Isaya 50:7-10.

"Yuaja mkuu wa ulimwengu huu," Yesu alisema, "wala hana kitu kwangu." Yohana 14:30. Hakukuwa na kitu ndani ya Yesu ambacho kiliweka mwitikio kuelekea kwa uongo wa Shetani. Hakukubaliana na dhambi. Hakukubaliana na jaribu hata kwa wazo tu. Hivyo ndivyo ambavyo ingepaswa kuwa kwetu pia. Uanadamu wa Yesu uliungana na uungu; alifanywa kufaa kwa mapambano kwa njia ya Roho Mtakatifu aliyekaa ndani yake. Na alikuja kutufanya kuwa washirika wa asili hiyo ya uungu. Kwa jinsi ambavyo tunakuwa tumeunganishwa kwake kwa imani, dhambi haitawali tena juu yetu. Mungu hutufikia kuuelekeza mkono wa imani ndani yetu ushikilie uungu wa Kristo, kusudi tuweze kupata ukamilifu wa tabia.

Na Kristo ametuonyesha jinsi hili linavyofanyika. Ni kwa njia gani Yeye alishinda katika vita yake dhidi ya Shetani? Ni kwa neno la Mungu. Aliyapinga majaribu kwa neno tu. Alisema, "Imeandikwa." Na kwetu zinatolewa: "ahadi kubwa mno, za thamani, ili kwamba kwa hizo mpate kuwa washirika wa tabia ya Uungu, mkiokolewa na uharibifu uliomo duniani kwa sababu ya tamaa." 2 Petro 1:4. Kila ahadi iliyo katika neno la Mungu ni yetu. Tutaishi "kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu." Unapokabiliwa na majaribu, usitazame hali ya mambo au udhaifu binafsi, bali tazama nguvu ya neno. Nguvu zote za neno ni zako. Mwimba zaburi anasema,

"Moyoni mwangu nimeliweka neno lako, Nisije nikakutenda dhambi." "Kwa neno la midomo yako Nimejiepusha na njia za wenye jeuri." Zaburi 119:11; 17:4.

# Sura ya 13

## Ushindi

[Sura hii imejengwa katika Mathayo 4:5-11; Marko 1:12, 13; Luka 4:5-13.]

Kisha mwovu alimchukua Yesu na kumpeleka katika mji mtakatifu, akamweka juu ya kinara cha hekalu, na akamwambia, Ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu, jitupe chini: maana imeandikwa:

"Atakuagizia malaika zake;
Na mikononi mwao watakuchukua;
Usije ukajikwaa mguu wako katika jiwe."

Sasa Shetani anajifanya kama amekutana na Yesu katika viwanja vya Yesu mwenyewe. Adui mjanja huyu anasema maneno yaliyotoka katika kinywa cha Mungu. Bado anajitokeza kama malaika wa nuru, na anaweka viashiria kwamba anayajua vema Maandiko, na anaelewa umuhimu wa kile ambacho kimeandikwa. Kama vile Yesu alivyotumia neno la Mungu kabla kuimarisha imani yake, Shetani naye sasa anatumia neno la Mungu kuleta madanganyo yake. Anadai kwamba alikuwa tu anajaribu msimamo wa Yesu, na sasa anapongeza msimamao wake ulio imara. Kwa kuwa Mwokozi amedhihirisha imani yake kwa Mungu, bado Shetani anamhimiza kutoa ushahidi zaidi wa imani yake.

Lakini kwa mara nyingine jaribu hili linatanguliwa na kiashiria cha kutoamini, *"Ukiwa* ndiwe Mwana wa Mungu." Kristo alikuwa anajaribiwa kujibu hiyo "ukiwa;" lakini alikwepa hata jambo dogo tu la kukubali mashaka. Asingehatarisha maisha yake kwa kumpa Shetani uthibitisho.

**(125)** Mjaribu alitaka kutumia nafasi ya ubinadamu wa Yesu, na kumwelekeza katika hali ya kiburi. Lakini wakati Shetani anaweza kushawishi, hawezi kulazimisha mtu kutenda dhambi. Alimwambia Yesu, "Jitupe chini," akijua kwamba yeye asingemtupa chini; maana Mungu angeingilia kati na kumwokoa. Wala Shetani asingeweza kumlazimisha Yesu kujitupa chini. Kristo mwenyewe asipokubaliana na jaribu, asingeweza kushindwa. Hata nguvu zote za dunia na za kuzimu zisingeweza kumlazimisha hata kwa kiasi kidogo kujitenga na mapenzi ya Baba yake.

Kamwe mjaribu hawezi kutulazimisha kufanya maovu. Hawezi kuongoza mawazo isipokuwa kama mawazo yamekubali kuongozwa naye. Lazima kuwepo na uhiari kwanza, lazima imani iwe imeacha kumshikilia Kristo kwanza, ndipo Shetani anaweza kututawala. Lakini kila nia ya dhambi tunayokuwa nayo inampatia Shetani mahali pa kusimama mahali petu. Kila eneo ambalo linatushinda kufikia viwango vya kimbingu ndilo mlango wake ulio wazi wa kuingilia ili kutujaribu na kutuharibu. Na kila kuanguka au kushindwa kwetu kunampatia nafasi ya kumsuta Kristo.

Wakati Shetani aliponukuu ahadi hii, "Atakuagizia malaika zake; Na mikononi mwao watakuchukua," aliondoa maneno haya, "wakulinde katika njia zako zote;" yaani, katika njia zote zinazotakiwa na Mungu. Yesu alikataa kwenda nje ya njia ya utii. Wakati akidhihirisha utegemezi kamili kwa Baba yake, hakujiweka katika nafasi ya kumfanya Baba alazimike kuingilia kati kumponya na kifo, kama hakutakiwa kufanya hivyo. Asingeulazimisha Ukuu wa Mungu kuja kumwokoa, na kwa njia hiyo akawa ameshindwa kuwa kielelezo cha mwanadamu kutumaini na kujisalimisha.

Yesu alimwambia Shetani, "Imeandikwa, Usimjaribu Bwana Mungu wako." Maneno haya yalisemwa na Musa akiwaambia wana wa Israeli wakati walipokuwa na kiu jangwani, na kudai kwamba Musa awape maji wanywe, wakilalama hivi, "Je! Bwana yu kati **(126)** yetu au sivyo?" Kutoka 17:7. Mungu alikuwa amewatendea mema kupita kiasi; lakini bado walipokuwa katika shida waliona mashaka juu yake, na wakadai ushahidi kuonyesha kama yuko nao. Katika kutokuamini kwao, walitafuta kumjaribu Mungu. Na Shetani alikuwa anamtaka Kristo afanye hivyo hivyo. Mungu alikuwa ameshathibitisha kwamba Yesu ni Mwana wake; na sasa kutaka uthibitisho kwamba alikuwa Mwana wa Mungu ingekuwa ni kulijaribu neno la Mungu, - ni kumtia katika majaribu. Na hali ingekuwa hivyo pia kwa kuomba kile ambacho Mungu hakuwa ameahidi. Ingeonyesha hali ya kutoamini, na kwa kweli ingekuwa ni kutaka kupata uhakika, au kumjaribu. Tusipeleke dua zetu kwa Mungu ili kuhakikisha kama atatimiza neno lake, bali tuzipeleke kwa kuwa atatimiza; si kwa ajili ya kuthibitisha kwamba anatupenda, bali ni

kwa sababu anatupenda. "Pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao." Waebrania 11:6.

Lakini imani haifungamani kwa vyovyote na imani ya bandia. Ni yule tu ambaye ana imani ya kweli ndiye yuko huru dhidi ya imani ya bandia. Maana imani ya bandia ni imani ya hisia ya kudhani ambayo inaletwa na Shetani. Imani halisi inadai ahadi za Mungu, na inazaa tunda katika utii. Imani ya bandia pia inadai ahadi, lakini inatumia ahadi hizo vile Shetani alivyofanya, kuhalalisha makosa. Imani ingewaongoza wazazi wetu wa kwanza kutumaini pendo la Mungu, na kutii amri zake. Imani ya kudhania iliwaelekeza katika uasi wa sheria yake, wakiamini kwamba pendo lake kuu lingewaokoa na matokeo ya dhambi yao. Imani haidai upendeleo wa Mungu bila kutii masharti ya kutoa neema hiyo. Imani ya dhati ina msingi wake katika ahadi na maelekezo ya Maandiko.

Mara nyingi Shetani anaposhindwa kuamsha hali ya kutoamini, anafuatisha kutuongoza katika imani ya bandia. Ikiwa anaweza kutufanya tujiweke katika njia ya majaribu bila ulazima, anajua kwamba ushindi utakuwa wake. Mungu atawahifadhi wote wanaotembea katika njia ya utii; lakini kuachana na njia hiyo ni kucheza-cheza katika viwanja vya Shetani. Tukiwa humo kudondoka ni hakika. Mwokozi ametuhimiza, "Kesheni mwombe, msije mkaingia majaribuni." Marko 14:38. Kutafakari na kuomba kungetukinga dhidi ya kwenda katika njia ya hatari pasipo ulazima wa kufanya hivyo, na kwa namna hiyo tutaepuka kushindwa.

Lakini tusipoteze ujasiri tunapokumbwa na majaribu. Mara nyingi tunapojikuta katika hali ya kutujaribu tunapata mashaka kama kweli Roho wa Mungu amekuwa akituongoza. Lakini ni Roho aliyemwongoza Yesu kwenda jangwani ili kujaribiwa na Shetani. Wakati Mungu anapotuleta katika majaribu, huwa ana kusudi la kukamilisha kwa ajili ya mambo mema kwetu. Yesu hakutafuta kujihakikishia imani kuhusu ahadi za Mungu eti ajipeleke katika majaribu bila ulazima, wala hakusalimu **(129)** amri wakati majaribu yalipomjia. Hata sisi tuwe hivyo kama Yeye. "Mungu ni mwaminifu; ambaye hatawaacha mjaribiwe kupita mwezavyo; lakini pamoja na lile jaribu atafanya na mlango wa kutokea, ili mweze kustahimili." Anasema, "Mtolee Mungu dhabihu za kushukuru; Mtimizie Aliye juu nadhiri zako. Ukaniite siku ya mateso; Nitakuokoa, na wewe utanitukuza." 1 Wakorintho 10:13; Zaburi 50:14, 15.

Yesu alikuwa mshindi katika jaribu la pili, na sasa Shetani anajidhihirisha katika tabia yake halisi. Lakini hajitokezi kama jitu baya la kutisha, lenye miguu iliyopasuka-pasuka na mabawa kama ya popo. Ni malaika mkubwa, ingawa alianguka. Anajitambulisha kama kiongozi wa uasi na mungu wa ulimwengu huu.

Akiwa amemweka Yesu kwenye mlima mrefu, Shetani alifanya kwamba enzi zote za dunia, katika utukufu wake wote, zipite mbele ya Yesu zikionyesha mandhari zake zote kwake. Nuru ya jua ilipiga katika miji yenye mahekalu, majumba makubwa ya marumaru, mashamba yenye rutuba, na mashamba ya mizabibu yaliyopamba. Vitu vinavyoonyesha ubaya vilifichwa. Macho ya Yesu, ambayo muda mfupi tu yalikuwa yametoka kukutana na utusitusi na ukiwa, sasa yalikuwa yanaona mandhari ya upendo na ustawi uliokithiri. Halafu sauti ya mjaribu ilisikika: "Nitakupa wewe enzi hii yote, na fahari yake, kwa kuwa imo mikononi mwangu, nami humpa yeyote kama nipendavyo. Basi, wewe ukisujudu mbele yangu yote yatakuwa yako."

Kazi ya Kristo ingetimizwa kwa njia ya mateso tu. Mbele yake kulikuwa na maisha ya huzuni, ugumu wa maisha, na upinzani, na kifo cha aibu. Lazima abebe dhambi za ulimwengu wote. Lazima astahimili kutengwa na pendo la Baba yake. Sasa mjaribu alitoa mamlaka yote aliyokuwa ameteka. Kristo angejiokoa na hali yake ya kutisha ya siku za mbele kwa kutambua ukuu wa Shetani. Lakini kufanya hivyo, ilikuwa ni kusalimisha ushindi katika pambano kuu. Shetani alitenda dhambi mbinguni kwa kutafuta kujiinua juu kuliko Mwana wa Mungu. Ikiwa angeshinda sasa, ingekuwa ni ushindi wa uasi.

Wakati Shetani alipomwambia Kristo, Ufalme na utukufu wa ulimwengu nimepewa mimi, na nampa yeyote ninayependa kumpa, alikuwa amesema ukweli kwa sehemu tu, na alisema hivyo ili kukidhi kusudi lake mwenyewe la kudanganya. Miliki ya Shetani ni ile iliyonyang'anywa kutoka kwa Adamu, lakini Adamu ndiye aliyekuwa ameteuliwa na Muumbaji kutawala mahali pake. Ule haukuwa utawala huru. Dunia ni ya Mungu, na ameviweka vitu vyote kwa Mwana wake. Adamu alikuwa atawale chini ya Kristo. Pindi Adamu aliposaliti utawala wake na kuuweka mikononi mwa Shetani, bado Kristo alibaki kuwa Mfalme halali. Mungu alimwambia mfalme Nebukadneza hivi, "Aliye juu anatawala katika **(130)** ufalme wa wanadamu, naye humpa amtakaye." Dan. 4:17. Shetani anaweza kuendesha tu mamlaka aliyonyakua kwa kadiri Mungu anavyoruhusu.

Wakati mjaribu alimpoonyesha nia ya kumpatia Kristo miliki na utukufu wa ulimwengu, alikuwa anapendekeza kwamba Kristo asalimishe ufalme wake halisi wa ulimwengu, na awe na miliki chini ya Shetani. Hii ndio miliki iliyo kama ile ambayo ilikuwa katika matarajio ya Wayahudi juu yake. Walitarajia ufalme wa ulimwengu huu. Ikiwa Kristo angekubali kuwapa ufalme huo, wangempokea kwa furaha. Lakini laana ya dhambi, na shida zake zote, ilikuwa juu ya huo. Kristo alimwambia mjaribu, "Imeandikwa, Msujudie Bwana Mungu wako, umwabudu yeye peke yake."

Yule aliyeasi mbinguni alimpa Yesu ufalme wa ulimwengu huu, ili kununua heshima ya Yesu katika kanuni za uovu; lakini Yesu hakuweza kununulika; alikuwa amekuja kusimika ufalme wa haki, na asingeachana na kusudi lake. Kwa jaribu kama lile lile Shetani anawaendea wanadamu, na kwao anapata mafanikio kuliko alivyopata kwa Kristo. Anawapa watu ufalme wa dunia hii kwa sharti la kutambua ukuu wake. Anawataka watoe kafara uaminifu, wasijali maadili, watafute tamaa za kibinafsi. Kristo anawahimiza wautafute kwanza ufalme wa mbinguni, na haki yake; lakini Shetani anatembea akiwa kando kando yao akisema: Vyovyote inavyokuwa kweli kuhusu uzima wa milele, ili mfanikiwe katika ulimwengu huu lazima mnitumikie. Ustawi wenu uko mikononi mwangu. Naweza kuwapatia utajiri, raha, heshima, na furaha. Shikeni mashauri yangu. Msikubali kuchukuliwa na dhana zisizo za kawaida za uaminifu na kujikana. Nitawaandalia njia. Hivyo makutano hudanganywa. Wanakubali kuishi wakitumika kwa ajili ya nafsi zao, na Shetani anaridhika. Wakati akiwatamanisha kwa matarajio ya miliki ya ulimwengu, anapata miliki ya roho zao. Lakini anawapatia kile ambacho si haki yake kukitoa, na ambacho muda si mrefu kitanyang'anywa kutoka kwake. Anawaghilibu kuhusu stahili yao ya urithi wa wana wa Mungu.

Shetani alikuwa amehoji kama Yesu alikuwa Mwana wa Mungu. Katika kukataliwa kwake alikuwa amepata uhakika kwamba asingeweza kupinga hilo. Uungu ulimlika ndani ya ubinadamu unaoteseka. Shetani hakuwa na nguvu za kushindana na amri. Akitapatapa kwa kushindwa na kwa ghadhabu, alilazimika kuondoka mbele ya uwepo wa Mkombozi wa ulimwengu. Ushindi wa Yesu ulikuwa mkamilifu sawa sawa na ukamilifu wa lile anguko la Adamu.

Hata sisi tunaweza kupinga majaribu, na kumlazimisha Shetani kutukimbia. Yesu alishinda kwa imani na kujikabidhi kwa Mungu, na kupitia **(131)** mtume anatwambia, "Basi mtiini Mungu. Mpingeni Shetani, naye atawakimbia. Mkaribieni Mungu, naye atawakaribia ninyi." Yakobo 4:7, 8. Hatuwezi kujiokoa wenyewe kutoka katika nguvu ya mjaribu; yeye ameshamshinda mwanadamu, kwa hiyo tunapojaribu kusimama kwa nguvu zetu wenyewe, tutakuwa mawindo katika mitego yake; lakini "Jina la Bwana ni ngome imara; Mwenye haki huikimbilia, akawa salama." Mithali 18:10. Shetani hutetemeka na kumkimbia hata mtu dhaifu sana anayetafuta kimbilio lake katika jina hilo kuu.

Baada ya kuwa adui amekimbia, Yesu alianguka hata nchi akiwa amechoka, akiwa amenyong'onyezwa na kifo kilichokuwa kinamkabili. Malaika wa mbinguni walikuwa wametazama lile pambano, wakimwangalia Jemadari wao mpendwa alivyokuwa akipita katika mateso yasiyoelezeka ili kupata njia kwa ajili ya kupona kwetu. Alikuwa amestahimili jaribio, kubwa kuliko ambalo tutapata kustahimili. Sasa malaika walimhudumia Mwana wa Mungu wakati akiwa amelala kama anayekufa. Alitiwa nguvu kwa chakula, akitiwa moyo na ujumbe wa upendo wa Baba yake na hakikisho alilopata kwamba mbingu yote ilikuwa imeshinda katika ule ushindi wake. Akirejea katika hali ya uhai wa kawaida, moyo wake mkuu unamhurumia mwanadamu, na sasa anaondoka kwenda kukamilisha kazi amabayo alikuwa ameianza; kutokupumzika mpaka pale adui awe ameshindwa, na jamii ya wanadamu iwe imekombolewa.

Gharama ya ukombozi haitaeleweka kamwe mpaka waliokombolewa watakaposimama mbele ya kiti cha enzi. Pindi utukufu wa nyumbani pa milele utakapolipuka katika hisia zetu za furaha wakati huo tutakumbuka kwamba Yesu aliacha vyote hivi kwa ajili yetu, kwamba si tu kwamba aliienda katika nchi ya ugeni mbali na mbinguni, bali pia kwamba kwa ajili yetu aliingia katika hatari ya uwezekano wa kushindwa na kupoteza nafasi milele. Ndipo tutakapozitupa taji zetu miguuni pake, na kuimba wimbo, "Astahili Mwana-Kondoo aliyechinjwa, kuupokea uweza na utajiri na hekima na nguvu na heshima na utukufu na baraka." Ufunuo 5:12.

# Sura ya 14

## "Tumemwona Masihi"

[Sura hii imejengwa katika Yohana 1:19-51.]

Yohana Mbatizaji alikuwa anahubiri huko Bethania, ng'ambo ya Yordani. Mahali hapa si mbali na pale ambapo Mungu alisimamisha mto usitiririke mpaka Waisraeli walipovuka. Umbali kidogo tu kutoka hapa ndipo palipokuwa na ngome ya Yeriko ambayo iliangushwa na majeshi ya Bwana. Kumbukumbu ya matukio haya ilikuwa imerejeshwa sasa, na iliamsha hamu ya kuusikiliza ujumbe wake Mbatizaji. Je, Yeye aliyefanya maajabu kiasi hicho mnamo zama zile zilizopita angedhihirisha nguvu zake tena katika kuwakomboa Israeli? Hayo ndiyo yaliyokuwa mawazo katika mioyo ya watu ambao walifurika katika kingo za Yordani kila siku.

Kuhubiri kwa Yohana kuligusa vina vya taifa lile kiasi cha kuvuta hata mamlaka za dini. Hatari ya uasi kuibuka ilisababisha kila mkusanyiko wa hadhara kuangaliwa na Warumi kwa tahadhari, na chochote kilichoashiria kuhamasisha upinzani wa watu kilileta hofu kwa wakuu wa Wayahudi. Yohana hakuwa ametambua mamlaka ya baraza (Sanhedrin) kwa kutafuta baraka zao kwanza kwa kazi yake; na **(133)** alikuwa amewakemea wakuu na watu, Mafarisayo na Masadukayo kwa namna iliyo sawa. Na bado watu walimfuata kwa hamu. Hamu ya watu katika kazi yake ilionekana kuendelea kuongezeka. Ingawa hakuwa amejali mamlaka yake, baraza (Sanhedrin) lilichukulia kwamba, kama mwalimu wa hadhara, alikuwa chini ya mamlaka yao.

Chombo hiki kiliundwa na wajumbe waliochaguliwa kutoka miongoni mwa makuhani, wakuu na walimu katika taifa lile. Kwa kawaida, kuhani mkuu alikuwa ndiye mwenyekiti. Wajumbe wake wote walikuwa watu wa umri mkubwa sana, ingawa si wazee vikongwe; watu waliosoma, si tu katika dini na historia ya Wayahudi, bali elimu kwa ujumla. Hawakupaswa kuwa wenye hitilafu kimwili, lazima wawe wanaume waliooa, na lazima wawe baba wenye watoto, na ili kuwa na uwezekano wa kuwa zaidi ya wengine walitarajiwa wawe na utu na kujali watu. Mahali pao pa kukutania palikuwa ni katika chumba kulichokuwa sehemu ya jengo la hekalu kule Yerusalemu. Mnamo siku za uhuru wa Wayahudi Sanhedrin ilikuwa ndiyo ngazi ya juu ya mahakama ya taifa, ikiwa na mamlaka ya kiserikali na ya kidini. Ingawa sasa ilikuwa chini ya watawala wa Kirumi, ilikuwa bado ina ushawishi wa nguvu katika mambo ya kiraia na ya kidini.

Sanhedrin haikuacha kufuatilia kazi ya Yohana. Wapo baadhi ambao walikumbuka ufunuo wa Zakaria mle hekaluni, na unabii wa baba yule, ambao ulikuwa umeonyesha kwamba mwanae ni mtangulizi wa Masihi. Katika mikiki-mikiki na mabadiliko ya miaka thelathini, mambo hayo yalikuwa yamesahaulika kwa kiasi kikubwa. Sasa yalikumbukwa kuhusu kazi ya Yohana.

Muda mrefu ulikuwa umepita tangu Israeli ilipokuwa na nabii, muda mrefu tangu matengenezo kama haya yaliyokuwa yanaendelea yalipokuwa yameshuhudiwa. Madai ya kutakiwa kutubu dhambi yalionekana kuwa mapya na ya kushtua. Wengi miongoni mwa viongozi wasingeenda kusikiliza wito wa Yohana na masuto yake, ili wasije wakaweka wazi siri ya maisha yao. Lakini mahubiri yake yalikuwa ni matangazo ya moja kwa moja kuhusu Masihi. Ilikuwa inajulikana bayana kwamba majuma saba ya uabii wa Danieli, yanayohusu kuja kwa Masihi, yalikuwa kama yamekwisha; na wote walikuwa na hamu ya kushiriki zama zile mpya za utukufu wa taifa uliokuwa unatarajiwa wakati ule. Huo ndio uliokuwa wasiwasi ambao muda si mrefu Sanhedrin ingelazimisha ama kukubaliana au kuikataa kazi ya Yohana. Mamlaka yao kwa watu ilikuwa inapwaya tayari. Namna ya kudumisha mamlaka yao ilikuwa inakuwa suala tete. Wakitumaini kufikia hitimisho fulani, walituma kundi la uwakilishi wa makuhani na Walawi ili likaonane na mwalimu huyu mpya.

Umati mkubwa wa watu walikuwa wamekusanyika, wakisikiliza maneno yake, wakati msafara ulipokaribia. Wakiwa na mazingira ya kimamlaka yaliyopangwa ili kuvuta hisia za watu **(134)** na kuweza kushawishi hali ya kutambuliwa na nabii, marabi wale walikuja. Wakisogea kwa mwendo wa kuheshimu, kama kwa hofu, mkutano ulipisha njia ili wapite. Watu hawa wakuu, katika majoho yao ya kitajiri, wakiwa na fahari ya cheo na madaraka, walisimama mbele ya nabii huyu wa jangwani.

"Wewe u nani?" waliuliza. Akijua kilichokuwa mawazoni mwao, Yohana alijibu, "Mimi siye Kristo." "Ni nini basi? U Eliya wewe?" Waliuliza. Naye akasema, "Mimi siye." Wakauliza, "Wewe u nabii yule?" Akajibu, "La." Basi

wakamwuliza, "U nani? Tuwape majibu wale waliotupeleka. Wanenaje juu ya nafsi yako?" Akasema, "Mimi ni sauti ya mtu aliaye nyikani, Inyosheni njia ya Bwana! Kama vile alivyonena nabii Isaya."

Andiko ambalo Yohana alirejea ni ule unabi mzuri wa Isaya usemao: "Watulizeni mioyo, watulizeni mioyo, watu wangu, asema Mungu wenu. Semeni **(135)** na moyo wa Yerusalemu, kauambieni kwa sauti kuu ya kwamba vita vyake vimekwisha, uovu wake umeachiliwa . . . Sikiliza, ni sauti ya mtu aliaye, Itengenezeni nyikani njia ya Bwana; Nyosheni jangwani njia kuu kwa Mungu wetu. Kila bonde litainuliwa, Na kila mlima na kilima kitashushwa; Palipopotoka patakuwa pamenyoka, Na palipoparuza patasawazishwa; Na utukufu wa Bwana utafunuliwa, Na wote wenye mwili watauona pamoja. Isaya 40:1-5.

Mnamo zama za kale, wakati mfalme aliposafiri akipita katika maeneo ya miliki yake ambayo hayatembelewi mara kwa mara, kundi la watu lilitumwa kutangulia mbele ya msafara wa mfalme kusawazisha mitelemko mikali na kufukia mashimo, ili kwamba mfalme apate kusafiri kwa salama na bila vikwazo. Desturi hii ndiyo inayotumiwa na nabii kuelezea kazi ya injili. "Kila bonde litainuliwa, Na kila mlima na kilima kitashushwa." Wakati Roho wa Mungu, akiwa na nguvu yake ya ajabu ya kuamsha, anapougusa moyo, anashusha kiburi cha mwanadamu. Raha za dunia na cheo na mamlaka vinaonekana kuwa si kitu. "Mawazo na kila kitu kilichoinuka, kijiinuacho juu ya elimu ya Mungu" vinashushwa; kila wazo linaletwa katika hali ya kuwa nyara ili ipate "kumtii Kristo." 2 Wakorintho 10:5. Halafu unyenyekevu na upendo wa kujikana, ambavyo huthaminiwa kidogo sana, vinatukuzwa na kuonekana kwamba ndivyo pekee vyenye kufaa. Hii ni kazi ya injili, ambayo ujumbe wa Yohana ulikuwa sehemu yake.

Marabi waliendelea na maswali yao hivi: "Mbona basi wabatiza, ikiwa wewe si Kristo, wala Eliya, wala nabii yule?" Maneno haya "nabii yule" yanarejea kwa Musa. Wayahudi walikuwa wameelekezwa katika imani ya kwamba Musa angefufuliwa kutoka kwa wafu, na kupelekwa mbinguni. Hawakujua kwamba alikuwa amekwishafufuliwa. Wakati Mbatizaji alipoanza kazi yake, wengi walidhani kwamba atakuwa ni nabii Musa aliyefufuka kutoka kwa wafu, maana anaonekana kuwa na ufahamu wa unabii na historia ya Israeli.

Ilikuwa inaaminika pia kwamba kabla ya kuja kwa Masihi, Eliya angetokea katika mwili. Katika kukataa kwake, Yohana alikutana na matarajio haya ya watu; lakini maneno yake haya yalikuwa na maana ya kina. Baadaye Yesu alisema, akirejea habari ya Yohana, "Na ikiwa mnataka kukubali, yeye ndiye Eliya atakayekuja." Mathayo 11:14. Yohana alikuja katika roho na nguvu ya Eliya, kufanya kazi kama aliyoifanya Eliya. Ikiwa Wayahudi wangemkubali, kazi ingekuwa imekamilika kwa ajili yao. Lakini hawakupokea ujumbe wake. Kwao hakuwa Eliya. Hakuweza kutimiza kazi yake aliyokuja kufanya kwa ajili yao.

**(136)** Wengi miongoni mwa wale waliokusanyika pale Yordani walikuwa watu waliokuwepo wakati Yesu alipobatizwa; lakini ishara iliyotolewa wakati ule ilidhihirika kwa wachache tu miongoni mwao. Katika miezi iliyofuata ya huduma ya Mbatizaji, wengi walikuwa wamekataa kuitikia wito wa kutubu. Hivyo walikuwa wameifanya mioyo yao kuwa migumu na kuutia giza ufahamu wao. Mbingu ilipotoa ushuhuda wakati wa ubatizo wa Yesu, hawakuelewa. Macho yale ambayo kamwe hayajageuzwa kwa imani kumwelekea Yeye asiyeonekana hayakuona utukufu wa Mungu; masikio ambayo hayajasikia kamwe sauti yake hayakusikia maneno ya ushuhuda. Hivyo ndivyo ilivyo hata sasa. Mara nyingi uwepo wa Kristo na huduma ya malaika inadhihirishwa katika makusanyiko ya watu, lakini bado wapo watu ambao hawaijui. Hawagundui lolote lisilo la kawaida. Lakini kwa baadhi uwepo wa Mwokozi unafunuliwa. Amani na furaha huhuisha mioyo yao. Wanafarijiwa, wanatiwa moyo, na wanabarikiwa.

Wale wawakilishi kutoka Yerusalemu walikuwa wamemwuliza Yohana hivi, "Kwa nini wabatiza?" na walikuwa wanasubiri jibu lake. Ghafla, kadiri alivyowaangalia makutano, macho yake yaliwaka, uso wake uliangaza kwa nuru, mwili wake wote ulisisimka kwa hisia ya kina. Akiwa amenyosha mikono alisema kwa sauti kubwa, "Mimi nabatiza kwa maji. Katikati yenu amesimama yeye msiyemjua ninyi. Ndiye yule ajaye nyuma yangu, ambaye mimi sistahili kuilegeza gidamu ya kiatu chake." Yohana 1:27.

Ujumbe huo ulikuwa wa moja kwa moja na usio na utata, ujumbe wa kurudisha kule Sanhedrin. Maneno ya Yohana yasingehusu kitu kingine ila Yeye aliyeahidiwa muda mrefu. Masihi alikuwa miongoni mwao! Kwa mshangao makuhani na wakuu waliwaangalia makutano, wakitumaini kumbainisha Huyo ambaye Yohana amesema habari zake. Lakini hakuweza kubainishika miongoni mwa makutano.

Wakati wa ubatizo wa Yesu, Yohana alipowaelekeza watu kwake Yeye aliye Mwana-kondoo wa Mungu, nuru mpya ilifunika kazi ya Masihi. Mawazo ya nabii yalielekezwa kwa maneno ya Isaya, "Kama mwana-kondoo apelekwaye machinjoni." Isa. 53:7. Katika majuma yaliyofuata, Yohana alijifunza kwa hamu mpya unabii na mafundisho ya huduma ya kafara. Hakutofautisha kwa uwazi vipindi viwili vya kazi ya Kristo, - kama kafara katika mateso na kama mfalme aliyeshinda, - lakini aliona kwamba kuja **(137)** kwake kulikuwa na umuhimu wa kina kuliko vile makuhani au watu walivyokuwa wanajua. Alipomwona Yesu akiwa miongoni mwa makutano akirudi kutoka jangwani, kwa ujasiri alimwangalia kwa matarajio ya Yeye kuwapatia watu ishara fulani-fulani za tabia yake halisi. Huku akikaribia kuchoka bado alisubiri kumsikia Mwokozi akitangaza utume wake; lakini hakuna neno lililosemwa, hakuna ishara iliyotolewa. Yesu hakuitikia tangazo la Mbatizaji kumhusu Yeye, lakini alikuwa amejichanganya na wanafunzi wa Yohana, akiwa hatoi ushahidi wowote wa nje kuhusu kazi yake maalum, na akiwa hachukui hatua yoyote ya kujiweka katika hali ya kujulikana.

Siku iliyofuata Yohana anamwona Yesu akija. Akiwa na nuru ya utukufu wa Mungu juu yake yeye, Yohana, huku akinyosha mikono yake kuelekeza kwa Yesu, alitangaza akisema, "Tazama, Mwana-kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu! Huyu ndiye niliyenena habari zake ya kwamba, Yuaja mtu nyuma yangu, ambaye amekuwa mbele yangu. . . . Wala mimi sikumjua; lakini kusudi adhihirishwe kwa Israeli ndiyo maana mimi nalikuja nikibatiza kwa maji. . . . Nimemwona Roho akishuka kama hua kutoka mbinguni; naye akakaa juu yake. Wala mimi sikumjua; lakini yeye aliyenipeleka kubatiza kwa maji, huyo aliniambia, Yeye ambaye utamwona Roho akishuka na kukaa juu yake, huyo ndiye abatizaye kwa Roho Mtakatifu. Nami nimeona, tena nimeshuhudia ya kuwa huyu ni Mwana wa Mungu." Yohana 1:29-34

Je huyu alikuwa Kristo? Wakiwa na butwaa na mshangao watu walimwangalia Yeye aliyesemwa kuwa Mwana wa Mungu. Walikuwa wameshangazwa sana na maneno ya Yohana. Alikuwa ameongea nao katika jina la Mungu. Walikuwa wamemsikiliza Yohana siku hadi siku kadiri alivyokemea dhambi zao, na kila siku ushawishi kwamba alikuwa ametumwa na Mungu ulikuwa umeongezeka. Lakini sasa huyu mwingine aliyekuwa mkuu kuliko Yohana Mbatizaji ni nani? Katika mavazi yake na mwonekano hakukuwa na kitu kilichoonyesha kuwa na ukuu. Alikuwa mtu rahisi wa kawaida, akiwa amevaa mavazi ya hali ya chini na ya kimaskini kama wao.

Kulikuwa na baadhi miongoni mwao ambao waliona utukufu wa mbinguni wakati wa kubatizwa kwake, na walikuwa wameisikia sauti ya Mungu. Lakini tangu wakati ule mwonekano wa Mwokozi ulikuwa umebadilika sana. Wakati wa kubatizwa kwake walikuwa wameona sura yake ikiwa imebadilishwa na nuru ya mbinguni; sasa, akiwa katika hali ya kufifia, uchovu, kukonda, alikuwa ametambuliwa na nabii Yohana peke yake.

Lakini kadiri ambavyo watu walimwangalia, waliona uso ambao umechanganya huruma ya kimbingu na uwezo wa umakini. Kila namna jicho lilivyoangalia, kila mwonekano wake, vilionyesha unyenyekevu, na upendo usiotamkika. Alionekana kama alikuwa amezungukwa na **(138)** mazingira ya nguvu ya kiroho. Wakati tabia zake zilikuwa za upole na kutojikweza, aliwaonyesha watu hali ya uwezo uliokuwa umefichika, lakini bado haukuwa umesitirika wote. Je huyu ndiye Yule ambaye alikuwa amesubiriwa na Israeli kwa muda mrefu?

Yesu alikuja akiwa maskini na mnyenyekevu, ili ya kwamba awe mfano wetu na Mkombozi wetu. Ikiwa angetokea na mwonekano wake wa kifalme, angewezaje kufundisha kuhusu unyenyekevu? Angewezaje kufundisha ukweli unaokata kama ule wa Hubiri la Mlimani? Tumaini la maisha ya kujishusha katika maisha lingekuwa wapi ikiwa Yesu angekuwa amekuja kuishi kama mfalme miongoni mwa wanadamu?

Kwa makutano, hata hivyo, ilionekana kama ni jambo lisilowezekana kwa Yule aliyetukuzwa na Yohana kuhusianishwa na matazamio ya kifahari. Kwa hiyo wengi walivunjika moyo, na walitatanika sana.

Maneno yale ambayo makuhani na marabi walitamani kusikia, kwamba Yesu angerejesha ufalme wa Israeli sasa, hayakuwa yamesemwa. Walikuwa wamemsubiri na kukesha kwa ajili ya mfalme kama huyo; walikuwa tayari kumpokea mfalme huyo. Lakini wasingempokea Yeye aliyetaka kuanzisha ufalme wa haki na amani mioyoni mwao.

Siku iliyofuata, wakati wale wanafunzi wawili walipokuwa wamesimama karibu, Yohana alimwona Yesu tena akiwa miongoni mwa watu. Kwa mara nyingine sura ya nabii huyu iliwaka kwa utukufu wa Yeye asiyeonekana, na akapaza sauti akisema, "Tazama Mwana-kondoo wa Mungu!" Maneno yale yalishtua mioyo ya wanafunzi

wale. Hawakuyaelewa kwa ukamilifu. Nini maana ya jina hili ambalo Yohana amempa, - "mwana-kondoo wa Mungu"? Yohana mwenyewe hakuwa amelifafanua.

Walienda kumtafuta Yesu, wakimwacha Yohana. Mmoja wa wale wawili alikuwa ni Andrea, nduguye Simoni; mwingine alikuwa Yohana mwinjilisti. Hawa ndio waliokuwa wanafunzi wa kwanza wa Yesu. Wakiwa wanasukumwa na msukumo usiopingika, walimfuata Yesu, - wakitafuta kuongea naye, lakini wakiwa kimya katika mshangao, wakiwa wamemezwa katika mawazo kwamba, "Je, huyu ni Masihi?"

Yesu alijua kwamba wale wanafunzi walikuwa wanamfuata Yeye. Walikuwa matunda ya kwanza ya kazi yake, na kulikuwa na furaha katika moyo wa mwalimu huyu atokaye mbinguni kwa kadiri roho hizi zilivyoitikia neema yake. Hata hivyo alipogeuka, aliwauliza tu hivi, "Mnatafuta nini?" Alikuwa radhi kuwaachia uhuru wa kurudi walikotoka au waseme hitaji lao.

Hamu yao ilikuwa ya kusudi moja. Hali moja ilijaza mawazo yao. Wakasema, "Rabi, . . . unakaa wapi?" Katika mahojiano yao kando ya njia hawakuweza kupata kile walichotamani kupata. Walitamani wawe peke yao na Yesu, wakae miguuni pake, na wasikie maneno yake. **(139)** "Akawaambia, Njoni, nanyi mtaona. Wakaenda, wakaona akaapo, wakakaa kwake siku ile."

Ikiwa Yohana na Andrea wangekuwa na roho ile isiyoamini ya makuhani na wakuu, wasingepatikana na kuwa wanafunzi miguuni pa Yesu. Wangemjia kama wakosoaji, ili kuhukumu maneno yake. Hivyo ndivyo wengi wanavyofungia mlango fursa za thamani kubwa sana. Lakini hawa wanafunzi wa kwanza hawakufanya hivyo. Walikuwa wameitikia wito wa Roho Mtakatifu katika mahubiri ya Yohana Mbatizaji. Sasa waliitambua sauti ya Mwalimu wa mbinguni. Maneno ya Yesu yalikuwa yamejaa upya, ukweli na uzuri kwao. Nuru ya kimbingu ilimwagwa kwenye mafundisho ya Maandiko ya Agano la Kale. Mada zile zenye mitazamo mingi-mingi zilisimama zikiwa katika nuru mpya.

Toba na imani na upendo ndivyo vinavyomwezesha mtu kuipokea hekima ya kutoka mbinguni. Imani inayofanya kazi kwa upendo ndio ufunguo wa maarifa, na kila mmoja apendaye "anamjua Mungu." 1 Yohana 4:7.

Yohana mwanafunzi alikuwa mtu mwema na mwenye moyo mkuu, mwenye huruma, lakini mwenye kutafakari. Alikuwa ameanza kuuona utukufu wa Kristo, - hakuwa amefundishwa kutumainia kujionyesha kwa kidunia na madaraka, bali "utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba; amejaa neema na kweli." Yohana 1:14. Alikuwa amemezwa katika kutafakari habari ile ya ajabu.

Andrea alitafuta kueneza furaha iliyokuwa imejaza moyo wake. Alienda kumtafuta ndugu yake Simoni, akapaza sauti akisema, "Tumemwona Masihi." Simoni hakusubiri hata kwa sekunde moja. Naye pia alikuwa amesikia mahubiri ya Yohana Mbatizaji, na aliharakisha kwenda kwa Mwokozi. Jicho la Kristo lilikuwa juu ya Simoni, likisoma tabia yake na historia ya maisha yake. Hali yake ya kuwa na harara, moyo wake wa upendo na huruma, tamaa yake ya makuu na kujiamini, historia ya maisha yake yajayo, toba yake, kazi zake, na kifo chake cha kufia imani, - Mwokozi alisoma hayo yote, na akasema, "Wewe u Simoni, mwana wa Yohana; nawe utaitwa Kefa (tafsiri yake Petro, au Jiwe)."

"Siku ya pili yake alitaka kuondoka kwenda Galilaya, naye akamwona Filipo. Yesu akamwambia, Nifuate." Filipo alitii ile amri, na moja kwa moja akawa mtenda-kazi kwa ajili ya Kristo.

Filipo alimwita Nathanaeli. Huyu Nathanaeli alikuwa miongoni mwa kusanyiko pale Yohana alipowaelekeza watu kwa Yesu kama Mwana-kondoo wa Mungu. Nathanaeli alimtazama Yesu, akafadhaika. Je, mtu huyu, mwenye alama za umaskini na uchovu, aweza kuwa Masihi? Lakini Nathanaeli hakuweza kuamua kumkataa Yesu, maana ujumbe wa Yohana ulikuwa umeleta usadikisho katika moyo wake.

**(140)** Wakati huu Filipo alipomwita, Nathanaeli alikuwa amejitenga katika eneo tulivu lenye miti akitafakari juu ya tangazo la Yohana na unabii unaomhusu Masihi. Aliomba kwamba ikiwa yule aliyesemwa na Yohana ndiye mkombozi, ijulishwe kwake, na Roho Mtakatifu alikuja juu yake akimletea uhakika kwamba Mungu alikuwa amewajilia watu wake na kuinua pembe ya wokovu kwa ajili yao. Filipo alijua kwamba rafiki yake alikuwa anachunguza unabii, na wakati Nathanaeli alipokuwa akiomba chini ya mtini, Filipo alipajua mahali pake pa faragha. Mara kwa mara walikuwa wameomba naye katika sehemu hii ya faragha iliyofichwa na majani. Maneno, "Tumemwona yeye aliyeandikiwa na Musa katika torati, na manabii," yalionekana kwa Nathanaeli kama jibu la

moja kwa moja la ombi lake. Lakini Filipo alikuwa bado na imani ya mashaka. Aliongeza maneno haya kwa mashaka, "Yesu, mwana wa Yusufu, mtu wa Nazareti." Kwa mara nyingine mtazamo wa awali uliibuka katika moyo wa Nathanaeli. Aliuliza, "Laweza neno jema kutoka Nazareti?"

Filipo hakuingia katika mabishano. Alimwambia, “Njoo uone. Basi Yesu akamwona Nathanaeli anakuja kwake, akanena habari zake, Tazama, Mwisraeli kweli kweli, hamna hila ndani yake!" Kwa mshangao Nathanaeli aliuliza, "Umepataje kunitambua? Yesu akajibu, akamwambia, Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwapo chini ya mtini nilikuona."

Ilikuwa imetosha. Roho wa mbinguni aliyekuwa amemshuhudia Nathanaeli katika maombi yake ya faragha chini ya mtini sasa alisema naye katika maneno ya Yesu. Ingawa katika mashaka, na akikubali kwa namna fulani mawazo yake potofu ya kabla, Nathanaeli alikuwa amekuja kwa Kristo akiwa na hamu ya dhati ya kutaka ukweli, na sasa hitaji lake lilikuwa limejibiwa. Imani yake iliendа mbele zaidi ya ile ya yule aliyekuwa amemleta kwa Yesu. Alijibu na kusema, "Rabi, wewe u Mwana wa Mungu, ndiwe Mfalme wa Israeli."

Ikiwa Nathanaeli angelitegemea uongozi wa marabi, asingelimwona Yesu kamwe. Ilikuwa ni kwa kuona na kuamua yeye mwenyewe ndipo **(141)** alipopata kuwa mwanafunzi. Hivyo ndivyo ilivyo kwa wengi leo ambao wana mawazo yasiyo sahihi ambayo yanawashikilia mbali na wema. Je, kungekuwa na tofauti kiasi gani ikiwa wao wenyewe wangefuata wito kwamba "njoo uone"!

Wakati watu wanategemea kuongozwa na mamlaka za wanadamu, hakuna hata mmoja atakayefikia maarifa yaokoayo ya ukweli. Kama Nathanaeli, tunahitaji kujifunza neno la Mungu kwa ajili yetu wenyewe, na kuomba kuangaziwa na Roho Mtakatifu. Yeye aliyemwona Nathanaeli chini ya mti wa mtini atatuona hata sisi katika maeneo yetu ya faragha ya maombi. Malaika kutoka katika ulimwengu wa nuru wako karibu na wale ambao kwa unyenyekevu wanatafuta uongozi wa mbinguni.

Kuitwa kwa Yohana na Andrea na Simoni, pamoja na kwa Filipo na Nathanaeli, ndio mwanzo wa kusimika kanisa la Kristo. Yohana alielekeza wawili kati ya wanafunzi wake kwa Kristo. Halafu mmoja kati ya hao, Andrea, alimpata kaka yake, akamwita aje kwa Mwokozi. Halafu aliitwa Filipo, naye akaenda kumtafuta Nathanaeli. Mifano hii itufundishe sisi umuhimu wa jitihada za mtu, za kuwakatisha shauri moja kwa moja jamaa, rafiki, na jirani zetu. Wapo wale ambao wanajidai kumfahamu Kristo, lakini bado hawajafanya juhudi yoyote ya kuleta hata roho moja kwa Mwokozi. Kazi yote wanawaachia wahubiri. Mtu anaweza akawa na sifa za kutosha kwa utume, lakini bado hafanyi lile ambalo Mungu amewaachia washiriki wa kanisa.

Wapo wengi wanaohitaji huduma ya Kikristo ya mioyo ya upendo. Wengi wameshuka hadi katika uharibifu ambao huenda wangeokolewa ikiwa majirani, wanaume na wanawake wa kawaida, wangekuwa wamefanya jitihada kwa ajili yao. Wengi wanasubiri mpaka wapelekwe. Miongoni mwa jamaa, kwa majirani, katika mji, mahali tunapoishi, kuna kazi ya sisi kufanya kama wamishonari wa Kristo. Ikiwa tu Wakristo, kazi hii itakuwa furaha yetu. Kadiri mtu anavyoongoka haichukui muda kuwa na hamu ndani yake ya kuwafanya wengine wajue urafiki wa thamani aliopata katika Yesu. Ukweli uokoao na kutakasa hauwezi kufungiwa ndani ya moyo wake.

Wote ambao wamejitoa wakfu kwa Mungu watakuwa mifereji ya nuru. Mungu anawafanya kuwa mawakala wake kuwasilisha utajiri wa neema yake kwa watu wengine. Ahadi yake ni, "Nami nitawafanya wao, na mahali palipo pande zote za mlima wangu, kuwa baraka, nami nitaleta manyunyu kwa wakati wake; yatakuwako manyunyu ya baraka." Ezekieli 34:26.

Filipo alimwambia Nathanaeli, "Njoo uone." Hakumtaka apokee ushuhuda wa mtu mwingine, bali amwone Kristo yeye mwenyewe. Sasa kwamba Yesu amepaa mbinguni, wanafunzi wake ndio wawakilishi wake miongoni mwa wanadamu, na moja ya njia zenye mafanikio ya kuongoa roho kwa Kristo iko katika **(142)** kudhihirisha tabia yake katika maisha yetu ya kila siku. Mvuto wetu kwa wengine hautegemei sana kile tunachosema kama unavyotegemea vile tulivyo. Wanadamu wanaweza kupinga na kukataa maneno yetu yenye mantiki, wanaweza wakapinga wito wetu; lakini maisha ya upendo usiotafuta mambo binafsi ni hoja ambayo hawawezi kuipinga. Maisha ya uaminifu, yenye sifa ya upole wa Kristo, ni nguvu kubwa katika ulimwengu.

Mafundisho ya Kristo yalikuwa ni udhihirisho wa usadikishaji na uzoefu wa ndani, na wale wajifunzao kwake wanakuwa walimu kwa kufuata mpango wa mbingu. Neno la Mungu, linaposemwa na mtu ambaye mwenyewe

ametakaswa nalo, lina nguvu ya kuleta uzima unaolifanya livutie kwa wasikilizaji, na huwafanya wasadiki kwamba ni uhalisia ulio hai. Wakati mtu anapokuwa amepokea ukweli kwa kuupenda, ataufanya udhihirike katika kuirekebisha tabia yake na toni ya sauti yake. Anawafanya na wengine wajue kile ambacho hata yeye amekisikia, kukiona, na kilichotolewa kwa neno la uzima, ili ya kwamba na wengine washiriki naye katika kumjua Kristo. Ushuhuda wake, utokao katika midomo iliyoguswa na kaa la moto lililotwaliwa kutoka madhabahuni, ni ukweli kwa moyo upokeao, na hufanya kazi ya utakaso wa tabia.

Na yeye anayetafuta kuwapatia wengine nuru naye atabarikiwa. "Yatakuwako manyunyu ya baraka." "Anyweshaye atanyweshwa mwenyewe." Mithali 11:25. Mungu aweza kufikia kusudi lake la kuwaokoa wadhambi bila msaada wetu; lakini ili tukuze tabia kama ya Kristo, lazima tushiriki katika kazi yake. Ili tuingie katika furaha yake, - furaha ya kuziona roho zikikombolewa kwa kafara ya Yesu – lazima tushiriki katika kazi zake kwa ajili ya ukombozi wao.

Udhihirisho wa kwanza wa imani ya Nathanaeli, uliokuwa wa kweli na wa dhati, ulisikika kama muziki mtamu katika masikio ya Yesu. Alijibu, "akamwambia, Kwa sababu nilikuambia, Nilikuona chini ya mtini, waamini? Utaona mambo makubwa kuliko haya." Kwa furaha Yesu alitarajia kwamba kazi yake ya kuhubiri habari njema itafanywa na wanyenyekevu, ikiwaganga waliovunjika moyo, na kutangaza uhuru kwa mateka wa Shetani. Juu ya wazo la baraka za thamani alizokuwa amewaletea wanadamu, Yesu aliongeza hivi, "Amin, amin, nawaambia, Mtaziona mbingu zimefunguka na malaika wa Mungu wakikwea na kushuka juu ya Mwana wa Adamu."

Hapa ni kama Kristo anasema, kwenye kingo za Yordani mbingu zilifunguka, na Roho alishuka kama hua juu yangu. Tukio lile lilikuwa ishara tu kwamba mimi ni Mwana wa Mungu. Mkiniamini hivyo, imani yenu itaimarishwa. Mtaona kwamba mbingu zimefunguliwa, na hazitafungwa kamwe. Nimezifungua kwenu. **(143)** Malaika wa Mungu wanapanda, wakipeleka kwa Baba maombi ya wenye kuhitaji na waliochoka, na wanashuka, wakileta baraka na tumaini, ujasiri, msaada, na uzima, kwa wana wa wanadamu.

Daima malaika wa Mungu wanapita kutoka duniani kwenda mbinguni, na kutoka mbinguni kwenda duniani. Miujiza ya Kristo kwa walioonewa na wanaoteseka ilifanywa kwa nguvu za Mungu kupitia huduma ya malaika hao. Na kupitia Kristo, kwa huduma ya wajumbe wake wa mbinguni, kila baraka inakuja kwetu kutoka kwa Mungu. Kwa kutwaa ubinadamu, Mwokozi anaunganisha shauku yake na ile ya wana na binti za Adamu walioanguka, wakati kupitia uungu wake anashikilia kiti cha enzi cha Mungu. Na kwa hiyo Kristo ndiye njia ya mawasiliano ya wanadamu kwa Mungu, na ya Mungu kwa watu wake.

## Sura ya 15

# Kwenye Sherehe ya Arusi

[Sura hii imejengwa katika Yohana 2:1-11.]

Yesu hakuanza kazi yake kwa matendo makubwa mbele ya Sanhedrin kule Yerusalemu. Uwezo wake ulipelekwa katika kusanyiko la nyumbani katika kijiji kidogo kilichoko kule Galilaya ili kuongezea katika furaha ya karamu ya arusi. Hivyo ndivyo alivyoonyesha huruma kwa watu, na hamu yake ya kutumika kwa ajili ya furaja yao. Katika jangwa la majaribu Yeye mwenyewe alikuwa amekunywa kikombe cha huzuni. Hapa alikuja kuwapa watu kikombe cha baraka, kwa kutoa kwake kwa kuheshimu mahusiano katika maisha ya wanadamu.

Yesu alikuwa amerudi Galilaya kutoka Yordani. Kulikuwa na arusi kule Kana, mji mdogo ambao hauko mbali na Nazareti; wahusika wa ndoa walikuwa na uhusiano na Yusufu na Mariamu; na Yesu, hali akijua kuhusu kusanyiko hili la kifamilia, alienda Kana, na alikuwa amealikwa karamuni Yeye na wanafunzi wake.

Kwa mara nyingine alikutana na mama yake, ambaye alikuwa ametengwa naye kwa muda fulani. Mariamu alikuwa ameshasikia habari ya udhihirisho uliotokea kule Yordani, wakati wa kubatizwa kwake. Habari zilikuwa zimepelekwa Nazareti, na zilikuwa zimemkumbusha Mariamu mambo yale ambayo yalikuwa yamefichwa moyoni mwake kwa miaka mingi. Pamoja na watu wote wa Israeli, Mariamu alikuwa amesisimshwa na kazi ya Johana Mbatizaji. Alikumbuka vema unabii uliotolewa wakati wa kuzaliwa kwake Yohana. Sasa mwunganiko wake na Yesu uliwasha matumaini yake **(145)** upya. Lakini habari zilikuwa zimemfikia pia kuhusu kuondoka kwake kimaajabu kwenda jangwani, na huyu mama aliumia sana akihisi kwamba mabaya yatampata Yesu.

Tangu katika siku aliposikia tamko la malaika nyumbani kule Nazareti Mariamu alikuwa amehifadhi kila kiashirio kinachoonyesha kwamba Yesu alikuwa Masihi. Maisha yake matamu na yasiyo na ubinafsi yalimhakikishia kwamba asingekuwa mwingine bali Aliyetumwa na Mungu. Lakini kwa mama huyu yalikuja mashaka pia na kukata tamaa, na alikuwa akisubiri muda wa utukufu wa Yesu kufunuliwa. Kifo kilikuwa kimemtenga na Yusufu, ambaye ndiye aliyekuwa ameshiriki kujua siri za kuzaliwa kwa Yesu. Sasa hakukuwa na mtu wa kumshirikisha matumaini yake na hofu zake. Miezi miwili iliyokuwa imepita ilikuwa ya huzuni sana. Alikuwa ametengana na Yesu, ambaye ndani ya huruma yake mama huyu alipata faraja. Alitafakari maneno ya Simeoni, "upanga utaingia moyoni mwako." (Luka 2:35); alikumbuka siku tatu za mahangaiko wakati alipodhani kwamba Yesu amempotea moja kwa moja; na kwa moyo usiotulia alimsubiri arudi.

Anakutana naye katika karamu ya arusi, mwana wake yule yule ampendaye. Lakini hayuko vile alivyokuwa. Mwonekano wake umebadilika. Unaonekana mwonekano wa mapambano kule jangwani, na mwonekano mpya wa tabia na uwezo unaonyesha udhihirisho wa utume wake wa kimbingu. Pamoja naye kuna kundi la vijana, ambao macho yao yanamfuata kwa heshima, na ambao wanamwita Bwana. Hawa wanamsimulia Mariamu mambo waliyoyaona na kuyasikia wakati wa kubatizwa na kwingineko. Wanahitimisha kwa kusema kwamba, "Tumemwona yeye aliyeandikiwa na Musa katika torati, na manabii." Yohana 1:45.

Kadiri wageni wanavyokusanyika, wengi wanaonekana kuendelea na mada zao walizokuwa nazo. Mshangao unawaingia ghafla watu wale waliokuwepo. Vikundi vidogo-vidogo vinasogeleana kwa shauku lakini kwa ukimya, na mtazamo wa mshangao unaelekezwa kwa mwana wa Mariamu. Kadiri Mariamu alivyokuwa amesikia ushuhuda wa wanafunzi kuhusu Yesu, alikuwa amefurahishwa na uhakika kwamba matumaini yake ya muda mrefu hayakuwa bure. Hata hivyo angekuwa ni zaidi ya mwanadamu ikiwa ile furaha yake takatifu isingechanganyika na chembechembe za kuona fahari. Kadiri alivyoona watu wengi wakimwangalia Yesu, alitamani Yesu athibitishie watu wale kwamba alikuwa Aliyeheshimiwa na Mungu. Alitamani kuwe na fursa ya Yeye kufanya mwujiza mbele yao.

Ilikuwa desturi ya wakati huo kwa sherehe za ndoa kuendelea kwa siku kadhaa. Katika tukio hili, divai iliisha kabla ya sherehe kufika mwisho. Hali hii ilisababisha wasiwasi na masikitiko makubwa. Ilikuwa si kawaida kukosekana divai katika matukio ya sherehe, na **(146)** kukosekana kwake kungeashiria utovu wa ukarimu. Akiwa kama ndugu wa wahusika wa ndoa, Mariamu alikuwa amesaidia katika maandalizi ya sherehe, na sasa

alimwambia Yesu hivi, "Hawana divai." Maneno haya yalikuwa yanapendekeza kwamba Yesu atoe suluhisho. Lakini Yesu alijibu, "Mama, tuna nini mimi nawe? Saa yangu haijawadia."

Jibu hili, lililo la ghafla kama lionekanavyo kwetu, lilionyesha kutojali na utovu wa adabu. Namna ile Yesu alivyosema kwa mama yake ilikuwa sahihi kulingana na desturi za Asia Mashariki. Usemi huo ulitumika kwa watu ambao walikuwa wanaonyeshwa kuheshimiwa. Kila tendo lililotendwa katika maisha ya Yesu duniani lilikuwa linakubaliana na amri aliyokuwa ametoa isemayo, "Waheshimu baba yako na mama yako." Kutoka 20:12. Alipokuwa msalabani, katika tendo lake la mwisho la kuonyesha huruma kwa mama yake, Yesu alizungumza na mama yake kwa namna hiyo hiyo, wakati alipomkabidhi uangalizi wa mwanafunzi yule aliyempenda sana. Katika matukio yote haya mawili ya arusini na msalabani, upendo ulioonyeshwa katika sauti na mwonekano na adabu vilionyesha tafsiri ya maneno yake.

Alipotembelea hekalu wakati wa uvulana wake, kadiri siri ya kazi ya maisha yake ilivyofunuliwa, Kristo alikuwa amemwambia Mariamu, "Hamkujua ya kuwa imenipasa kuwamo katika nyumba ya Baba yangu?" Luka 2:49. Maneno haya **(147)** yaliongoza huduma ya maisha yake yote. Sasa hapa alirudia somo hilo. Kulikuwa na hatari ya Mariamu kudhani kwamba uhusiano wake na Yesu ungempatia uwezo maalum juu ya Yesu, na haki, kwa kiasi fulani, ya kumpa maelekezo katika kazi yake ya utume. Kwa miaka thelathini Yesu alikuwa amekuwa mwana mwenye upendo na utii kwa Mariamu, na upendo wake ulikuwa usiobadilika; lakini sasa lazima aingie katika kazi ya Baba yake. Akiwa kama Mwana wa Aliye Juu, na Mwokozi wa ulimwengu, hakuna vifungo vya kidunia ambavyo vinalazimisha kumzuia katika huduma yake, au kuwa na ushawishi katika mwenendo wake. Lazima asimame katika kutenda mapenzi ya Mungu akiwa huru. Somo hili ni kwa ajili yetu pia. Matakwa ya Mungu yako juu ya vyote hata vifungo vya mahusiano ya kibinadamu. Hakuna kivutio cha kidunia ambacho kinastahili kugeuza miguu yetu kutoka katika njia ambayo Mungu anatutaka tuipite.

Tumaini pekee la jamii yetu iliyoanguka liko katika Kristo; Mariamu angepata wokovu kupitia Mwana-kondoo wa Mungu tu. Hata Mariamu hakuwa na la kujivunia ndani yake mwenyewe. Ukaribu wake na Yesu haukumweka katika nafasi ya kuwa na mahusiano ya kiroho na Yesu yaliyo tofauti na yale yaliyopo kati ya wanadamu wengine na Yesu. Jambo hili linadhihirika katika maneno ya Mwokozi. Anabainisha kwa uwazi tofauti ya uhusiano kati ya mama yake na Yeye akiwa Mwana wa Adamu na ule uhusiano akiwa Mwana wa Mungu. Mahusiano ya kifamilia yaliyokuwepo kati yao hayakumweka Mariamu kwa namna yoyote ya kuwa sawa na Yesu.

Maneo haya, "Saa yangu haijawadia," yanaonyesha kwamba kila tendo katika maisha ya Kristo ya duniani lilikuwa utimilifu wa mpango ambao ulikuwepo tangu milele. Kabla hajaja duniani, mpango wote ulikuwa mbele yake, ukiwa umekamilika katika sehemu zake zote. Kwa hiyo kadiri alivyotembea miongoni mwa wanadamu, alilindwa na mapenzi ya Mungu hatua kwa hatua. Hakuacha kutenda katika wakati ulioamuriwa. Kwa kujisalimisha huko alisubiri mpaka wakati ulipofika.

Kwa kumwambia Mariamu kwamba saa yake ilikuwa haijawadia, Yesu alikuwa anajibu mawazo ya Mariamu ambayo yalikuwa hayajasemwa, - matarajio yake ambayo hata watu wengine walikuwa nayo. Alitarajia kwamba Yesu angejifunua kwa watu kama Masihi, na kuchukua kiti cha enzi cha Israeli. Lakini saa ilikuwa haijawadia. Yesu alikuwa amekubali kuhesabiwa miongoni mwa wanadamu si ili kuwa kama Mfalme, bali "Mtu wa huzuni nyingi, ajuaye sikitiko."

Lakini ingawa Mariamu hakuwa na dhana sahihi kuhusu kazi ya Yesu, alimtumainia Yesu kikamilifu. Yesu aliiitikia imani hiyo. Mwujiza wa kwanza ulifanywa kwa heshima ya imani ya Mariamu, na kwa lengo la kuimarisha imani ya wanafunzi wake Yesu. Wanafunzi wale walikuwa wakabiliane na majaribu mengi na makubwa dhidi ya hali ya kutokuamini. Kwao unabii ulikuwa umeonyeshwa **(148)** kwa uwazi pasipo shaka kwamba Yesu alikuwa ndiye Masihi. Walitarajia kwamba viongozi wa dini wangempokea Yesu kwa uhakika mkubwa zaidi kuliko hata ule wa kwao. Walitangaza miongoni mwa watu kazi za ajabu za Kristo na tumaini lao katika huduma yake, lakini kwa uchungu walishangazwa na kufadhaishwa na jinsi makuhani na marabi walivyoonyesha kutokuamini, chuki iliyokita mizizi, na uadui dhidi ya Yesu. Miujiza ya awali ya Yesu iliwaimarisha wanafunzi hawa ili kusimama dhidi ya upinzani huu.

Bila kusumbuliwa kwa namna yoyote na maneno ya Yesu, Mariamu aliwaambia wale wanaohudumu mezani, "Lolote atakalowaambia, fanyeni." Hivyo ndivyo alivyosema kile alichoweza ili kutayarisha njia kwa ajili ya kazi ya Kristo.

Kando ya mlango kulikuwa na mabalasi makubwa sita ya mawe, na Yesu akawaambia mahudumu wale wayajaze maji. Ikafanyika hivyo. Kisha wakati divai ilipotakiwa ili kutumika, aliwaambia, "Sasa tekeni, mkampelekee mkuu wa meza." Badala ya maji yaliyokuwa yamejazwa, kulimiminika divai katika vyombo vile. Si mkuu wa meza wala wageni waalikwa waliojua kwamba divai ilikuwa imepwelea. Alipoonja hii divai iliyoletwa na wahudumu, mkuu wa meza aliona ikiwa njema kuliko nyingine yoyote aliyokuwa amepata kunywa kabla, na ikiwa tofauti sana na ile iliyokuwa imetolewa mwanzoni mwa sherehe ile. Akimgeukia bwana arusi, alisema, "Kila mtu kwanza huandaa divai iliyo njema; hata watu wakiisha kunywa sana ndipo huleta iliyo dhaifu; wewe umeiweka divai iliyo njema hata sasa."

Kama vile ambavyo watu huleta divai njema kwanza, halafu ndipo huleta iliyo dhaifu, ndivyo ilivyo kwa ulimwengu na thawabu zake. Kile kinachotolewa na dunia kinapendeza macho na kusisimua hisia, lakini hakileti hali ya kutosheka. Divai hugeuka kuwa uchungu, furaha kuwa huzuni. Kile kilichoanza na nyimbo na kicheko huishia katika shida na karaha. Lakini thawabu za Yesu daima ni njema na mpya. Sherehe anayotoa kwa mtu haitindikiwi na hali ya kuleta furaha. Kila thawabu mpya inaongeza uwezo wa yeye anayeipokea kutambua na kufurahia mibaraka ya Bwana. Anatoa neema kwa ajili ya neema. Haiwezekani kutindikiwa. Ukikaa ndani yake, kupokea zawadi nono leo kunaleta uhakika wa kupata zawadi nono zaidi kesho. Maneno ya Yesu kwa Nathanaeli yanaonyesha sheria ya namna Mungu anavyoshughulika na watoto waaminio. Anautangazia moyo umpokeao kwa kila ufunuo mpya wa upendo wake, akisema, "Waamini? Utaona mambo makubwa kuliko haya." Yohana 1:50.

Zawadi ya Kristo katika sherehe ile ya arusi ilikuwa ishara. Maji yale yaliwakilisha ubatizo katika mauti yake; divai ile iliwakilisha kumwagika kwa damu yake **(149)** kwa ajili ya dhambi za ulimwengu. Maji ya kujaza mabalasi yaliletwa kwa mikono ya wanadamu, lakini ni neno la Yesu pekee ambalo lingeyapa uhai. Hivyo ndivyo yalivyo matendo ya kiibada yanayoaashiria kifo cha Mwokozi. Yanakuwa na uwezo wa kunawirisha moyo kwa uwezo wa Kristo tu, ufanyao kazi kwa imani.

Neno la Kristo lilitoa kiburudisho kwa ajili ya sherehe. Hivyo ndivyo neema yake ilivyo tele kuondoa uovu wa wanadamu, na kuhuisha na kufanya moyo upya.

Katika sherehe hii ya kwanza aliyohudhuria pamoja na wanafunzi wake, Yesu aliwapa kikombe kilichokuwa ishara ya kazi yake kwa ajili ya wokovu wao. Wakati wa karamu ya mwisho alikitoa tena, wakati wa kusimika lile tendo takatifu ambalo kwalo kifo chake kingetangazwa "mpaka ajapo." 1 Wakorintho 11:26. Na huzuni ya wanafunzi wakati wa kuachana na Bwana wao ilifarijiwa na ahadi ya kuungana, kama alivyosema, "Sitakunywa kabisa tangu sasa uzao huu wa mzabibu, hata siku ile nitakapokunywa mpya pamoja nanyi katika ufalme wa Baba yangu." Mathayo 26:29.

Ile divai ambayo Kristo alitoa wakati wa sherehe, na ile aliyotoa kwa wanafunzi wake kama ishara ya damu yake, ilikuwa ni juisi safi ya zabibu. Nabii Isaya anairejea anaposema kuhusu divai mpya "katika kichala," na anasema, "Usikiharibu kwa maana mna baraka ndani yake." Isaya 65:8.

Ni Kristo ambaye aliwapa onyo Israeli katika Agano la Kale akisema, "Mvinyo hudhihaki, kileo huleta ugomvi; Na akosaye kwa vitu hivyo hana hekima." Prov. 20:1. Hata Yeye hakutoa kinywaji kama hicho. Shetani anawajaribu watu katika kutimiza hamu zao kwa kile kinachoharibu akili na kuchafua ufahamu wa kiroho, lakini Yesu anatufundisha kutawala tamaa zetu. Maisha yake yote yalikuwa kielelezo cha kujikana. Ili kuvunja nguvu za hamu ya kula na kunywa, aliumia katika jaribu kali mno ambalo hakuna mwanadamu anayeweza kustahimili jaribu zaidi ya hilo. Ni Kristo aliyeagiza kwamba Yohana Mbatizaji asinywe divai wala kileo. Ni Yeye pia aliyetaka kujitawala huko huko kwa mke wa Manoa. Na alitamka laana kwa mtu yeyote ambaye angeweka chupa katika midomo ya jirani yake. Kristo hakujipinga katika mafundisho yake mwenyewe. Divai isiyochachushwa aliyotoa kwa wageni wa arusi ilikuwa kinywaji kizuri cha kuburudisha. Kazi yake ilikuwa ni kuleta ladha inayokubaliana na hamu inayozingatia afya.

Kadiri wageni katika sherehe walivyosifia ubora wa divai ile, maswali yaliulizwa na kupata majibu kwa wahudumu kuhusu **(150)** mwujiza uliokuwa umetendeka. Watu waliokuwepo walipigwa butwaa kwa muda wakifikiria kuhusu Yeye aliyekuwa amefanya mwujiza wa ajabu. Baada ya kutafuta kwa muda mrefu kumwona, iligundulika kwamba alikuwa ameondoka kimya kimya kwa namna ambayo hata wanafunzi wake hawakujua.

Sasa watu waliwageukia wanafunzi wake. Mwanzoni walikuwa na fursa ya kuonyesha imani yao kwa Yesu. Walisimulia waliyoyaona na kusikia kule Yordani, na tumaini kwamba Mungu alikuwa ameinua Mkombozi wa watu wake liliwaka mioyoni mwa watu wengi. Habari za mwujiza ule zilisambaa katika eneo lote lile, na zilipelekwa hata Yerusalemu. Kwa hamu mpya makuhani na wazee walichunguza unabii unaomhusu Masihi ajaye. Kulikuwa na mwitikio mkubwa wa kujifunza kazi ya mwalimu huyu mpya, aliyeonekana kwa watu kama asiye na fahari.

Huduma ya Yesu ilikuwa tofauti kabisa na mtazamo wa wazee wa Kiyahudi. Heshima yao kwa desturi za mazoea ilikuwa imeharibu uhuru halisi wote wa mawazo na matendo. Waliishi katika uchafu wa kutisha wa kudumu. Wakikwepa kukutana na "walio najisi," walidumu kujitenga, si tu na Mataifa, bali na hata walio wengi miongoni mwa watu wa taifa lao, wakitafuta kwamba wasinufaike nao kwa lolote wala wasipate urafiki kwao. Kwa kuzama katika mambo haya wakati wote, walikuwa wamepotosha mawazo yao na kufanya upeo wa maisha yao kuwa finyu. Kielelezo chao kilifundisha kujipenda na kukosa uvumilivu miongoni mwa matabaka yote ya watu.

Yesu aliianza kazi yake ya matengenezo kwa kuja katika huruma ya karibu na wanadamu. Wakati alionyesha heshima kubwa kwa sheria ya Mungu, alikemea uchaji-Mungu wa kujionyesha wa Mafarisayo, na alijaribi kuwafanya watu wawe huru pasipo kufungwa na taratibu zisizo maana ambazo zilikuwa zimewafunga. Alikuwa anajitahidi kuvunja vizuizi vilivyotenganisha matabaka tofauti-tofauti ya jamii, ili kwamba awalete watu pamoja kama watoto wa jamaa moja. Kuhudhuria kwake kwenye sherehe ya arusi kulipangwa kama hatua ya kuelekea katika kutekeleza nia hii.

Mungu alikuwa amemwongoza Yohana kuishi jangwani, ili ya kwamba apate kukingwa na chachu ya makuhani na marabi, na ili aandaliwe kwa ajili ya kazi maalum. Lakini ugumu na upwekee wa maisha yake havikuwa kielelezo kwa watu. Yohana mwenyewe hakuwaagiza watu kuacha majukumu yao. Aliwataka waonyeshe matunda ya toba kwa uaminifu wao kwa Mungu wakiwa mahali alipowaita kuwa.

Yesu alikemea ubinafsi katika aina zake zote, lakini alikuwa na hali ya kuhusiana na wengine. Alikubali ukarimu wa watu wa matabaka yote, akitembelea nyumba **(151)** za matajiri na maskini, waliosoma na wasio na kisomo, na akitafuta kuinua mawazo yao kutoka katika mambo ya kawaida ya mahali walipokuwa kwenda katika mambo ya kiroho ya milele. Hakutoa kibali cha kufanya ufujaji, na mwenendo wake haukuwa na uvuli wa kukosa staha; lakini alipata raha katika matukio ya furaha isiyo na hatia. Ndoa ya Kiyahudi ilikuwa tukio la kuvutia, na furaha ya ndoa ile haikuwa mbaya kwa Mwana wa Adamu. Kwa kuhudhuria sherehe hii, Yesu aliheshimu ndoa kama jambo lililowekwa na Mungu.

Katika Agano la Kale na Jipya, mahusiano ya ndoa yanatumika kuwakilisha mwunganiko mtakatifu uliopo kati ya Kristo na watu wake. Katika mawazo ya Yesu ile furaha ya sherehe ya arusi ilielekeza katika furaha ya siku ile atakapomleta bibi arusi wake katika nyumba ya Baba, na waliokombolewa watakapokaa pamoja na Mkombozi katika karamu ya arusi ya Mwana-kondoo. Anasema, "Kama vile bwana arusi amfurahiavyo bibi arusi, ndivyo Mungu wako atakavyokufurahia wewe." "Hutaitwa tena Aliyeachwa, . . . bali utaitwa Hefsiba; . . . "Bwana, Mungu wako, yu katikati yako . . . Atakushangilia kwa furaha kuu, Atakutuliza katika upendo wake, Atakufurahia kwa kuimba.." Isaya 62:5, 4; Sefania 3:17. Wakati maono ya mambo ya mbinguni yalipotolewa kwa Yohana mtume, aliandika hivi: "Nikasikia sauti kama sauti ya makutano mengi, na kama sauti ya maji mengi, na kama sauti ya radi yenye nguvu, ikisema, Haleluya; kwa kuwa Bwana Mungu wetu, Mwenyezi, amemiliki. Na tufurahi, tukashangilie, tukampe utukufu wake; kwa kuwa arusi ya Mwana-Kondoo imekuja, na mkewe amejiweka tayari." "Heri walioalikwa karamu ya arusi ya Mwana-Kondoo. Akaniambia, Maneno haya ni maneno ya kweli ya Mungu." Ufunuo 19:6, 7, 9.

Ndani ya kila mtu Kristo aliona mtu anayepaswa kupewa mwaliko kwa ajili ya ufalme wake. Aliifikia mioyo ya watu kwa njia ya kuwa miongoni mwao kama mtu anayewatakia mema. Aliwatafuta mitaani, majumbani mwa watu, katika mashua, katika sinagogi, kando-kando ya ziwa, na katika sherehe ya arusi. Alikutana nao katika

maeneo yao ya kawaida ya kazi, na alionyesha kuvutwa katika mambo yao yasiyo ya kidini. Alipeleka maelekezo yake katika nyumba za watu, akizileta familia chini ya uwepo wake wa kimbingu zikiwa huko huko majumbani. Huruma yake kubwa ilisaidia kuongoa mioyo. Mara kwa mara alienda milimani kwa ajili ya maombi ya faragha, lakini haya yalikuwa ni kwa maandalizi kwa ajili ya kazi yake miongoni mwa wanadamu. Baada ya hapo alikuja kutuliza wagonjwa, kufundisha wasiojua, kuvunja minyororo kutoka kwa mateka wa Shetani.

**(152)** Yesu aliwafundisha wanafunzi wake kwa njia ya kukutana na kushirikiana. Wakati mwingine aliwafundisha akiwa ameketi miongoni mwao kando ya mlima; wakati mwingine kando ya bahari, au akitembea pamoja nao njiani, akiwafunulia siri za ufalme wa Mungu. Hakuwahutubia kama watu wafanyavyo sasa. Aliwafunulia njia ya ukweli wa wokovu mahali popote mioyo ilipokuwa wazi kupokea ujumbe wa mbinguni. Hakuwaamrisha wanafunzi wake wafanye hili au lile, bali alisema, "Nifuate." Katika safari zake kupitia mashambani na mijini alienda nao, ili ya kwamba waone jinsi alivyofundisha watu. Aliunganisha matarajio yao na yake, nao waliungana naye katika kazi.

Kielelezo cha Yesu katika kujiunganisha na shauku ya wanadamu kinapaswa kifuatwe na wote wanaolitangaza neno lake, na wote ambao wamepokea injili ya neema yake. Hatupaswi kukwepa mashirikiano ya kijamii. Hatupaswi kujitenga na watu wengine. Lazima tukutane na watu wa matabaka yote pale pale walipo ili tuweze kuwafikia. Ni kwa nadra sana kwa wao kututafuta sisi mahali tuliko. Mioyo ya watu haiguswi kwa mahubiri ya mimbarani tu. Hapa lipo eneo jingine la kufanyia kazi, ambalo linahitaji kujinyenyekeza, lakini likiwa la kutia matumaini sana. Linapatikana katika nyumba za watu wa hali ya chini, na katika makazi ya watu wakubwa; katika huduma kwa wasafiri vyomboni, na katika mikusanyiko ya kijamii isiyo mibaya.

Kama wanafunzi wa Yesu hatupaswi kuchangamana na walimwengu katika kupenda kujifurahisha nafsi, tukiungana nao katika ufedhuli. Mashirikiano kama hayo yanaweza kuleta madhara. Yatupasa tusihalalishe dhambi kwa maneno yetu au matendo yetu, kwa kukaa kimya kwetu au kwa kuwepo kwetu mahali. Mahali popote tuendapo tubebe jina la Yesu, na tuwafunulie wengine uthamani wa Mwokozi wetu. Lakini wale wanaojaribu kuhifadhi dini yao kwa kuificha ndani ya kuta za mawe wanapoteza fursa ya thamani ya kutenda mema. Kupitia katika mahusiano ya kijamii, Ukristo unakutanishwa na ulimwengu. Kila mmoja ambaye amepokea nuru ya mbinguni anapaswa aangazie njia ya wale wasiojua Nuru ya uzima.

Lazima sote tuwe mashahidi wa Yesu. Lazima nguvu za mafungamano ya kijamii, yaliyotakaswa kwa neema ya Kristo, yafanywe bora kutumika katika kuzielekeza roho kwa Yesu. Hebu dunia na ione kwamba hatukuzama katika ubinafsi wa matakwa yetu wenyewe, bali kwamba tunatamani na wengine washiriki baraka zetu na kupendelewa kwetu. Hebu na waone kwamba dini yetu haitufanyi kukosa huruma au kukazania sana kulazimisha utii. Hebu wote wanaoona kwamba wamempata Kristo na watoe huduma kwa ajili ya manufaa ya watu wengine kama Yeye alivyofanya.

Kamwe tusiupatie ulimwengu mtazamo usio sahihi kwamba Wakristo ni watu wa majonzi wasio na furaha. Ikiwa maisha yetu yamekazwa kwa Yesu, **(153)** tutamwona Mkombozi mwenye huruma, na tutanasa nuru kutoka kwake. Mahali popote ambapo Roho wake anatawala, pana amani. Na patakuwa na furaha pia, maana pana tumaini tulivu na takatifu katika Mungu.

Kristo anapendezwa na wafuasi wake wakati wanapoonyesha kwamba, ingawa ni wanadamu, ni washirika wa hali ya uungu. Wao si sanamu, bali wanaume na wanawake ambao wako hai. Mioyo yao, inayofanywa upya kwa umande wa neema ya mbinguni, hufunguka na kutanuka kulielekea Jua la Haki. Nuru inapomlika kwao wanaiakisi kuielekeza kwa wengine katika kazi zinazoangaziwa na pendo la Yesu.

## Sura ya 16

# Katika Hekalu Lake

[Sura hii imejengwa katika Yohana 2:12-22.]

"Baada ya hayo akashuka mpaka Kapernaumu, yeye na mama yake na ndugu zake na wanafunzi wake; wakakaa huko siku si nyingi. Na Pasaka ya Wayahudi ilikuwa karibu; naye Yesu akakwea mpaka Yerusalemu."

Katika safari hii, Yesu aliungana na kundi kubwa la watu waliokuwa wanakwenda katika mji mkuu. Alikuwa bado hajatangaza hadharani kuhusu kazi yake, na alijichanganya na msafara pasipo kujulikana. Katika matukio ya namna hii, ujio wa Masihi, ambao umuhimu wake ulikuwa ametolewa kupitia huduma ya Yohana, ulikuwa mara nyingi ndiyo mada. Matarajio ya ukuu wa taifa hili yaliangaliwa kwa shauku kubwa. Yesu alijua kwamba tumaini hilo litaleta mfadhaiko, maana lilikuwa limejengwa katika tafsiri ya Maandiko isiyo sahihi. Alifafanua unabii kwa dhati, na kujaribu kuwaamsha watu kujifunza neno la Mungu kwa ukaribu.

Viongozi wa Wayahudi walikuwa wamefundisha watu kwamba kule Yerusalemu wangefundishwa kumwabudu Mungu. Hapa ndipo watu wengi walipokusanyika wakati wa juma la pasaka, wakitoka katika sehemu zote za Palestina, na hata kutoka nchi za mbali zaidi. Viwanja vya hekalu vilikuwa vimejaa mchanganyiko wa watu. Wengi hawakuwa na uwezo wa kuja na kafara ambayo **(155)** ingetolewa ikiashiria ile Kafara moja kuu. Ili kuwarahisishia watu hawa, wanyama waliletwa na kuuzwa katika viwanja vya nje ya hekalu. Watu wa tabaka zote walikusanyika hapa ili kununua wanyama wa kutoa kama sadaka zao. Pesa zote za kigeni zilibadilishwa hapa ili kupata sarafu ya patakatifu.

Kila Myahudi alitakiwa kulipa nusu shekel kila mwaka kama "ukombozi kwa ajili ya roho yake;" na pesa hiyo iliyokusanywa ilikuwa inatumika katika kulitegemeza hekalu. Kutoka 30:12-16. Licha ya hii, matoleo makubwa mengine yaliletwa kama sadaka za hiari, ili kuwekwa katika hazina ya hekalu. Na ilitakiwa kwamba sarafu zote za kigeni zibadilishwe katika sarafu iliyoitwa shekeli ya hekalu, ambayo ilipokelewa kwa ajili ya huduma za patakatifu. Kazi hii ya kubadilisha fedha ilitoa fursa ya kufanya udanganyifu na kutoza bei kubwa, na hali hiyo ilikua na kuwa biashara haramu, iliyokuwa chanzo cha mapato cha makuhani.

Waendeshaji wa biashara hizo waliuza wanyama kwa bei ya juu sana, na waligawanya faida kwa makuhani na wakuu pia, ambao kama matokeo yake walijitajirisha kwa kuwanyonya watu. Waabudu walikuwa wamefundishwa kuamini kwamba kama wasipotoa sadaka, mibaraka ya Mungu isingekuwepo kwa watoto wao au katika nchi yao. Kwa njia hiyo kulikuwa na uhakika wa kuuza wanyama kwa bei kubwa; maana baada ya kufika pale, watu wasingerudi majumbani kwao bila kukamilisha tendo la ibada ambalo walikuwa wamekuja kwa ajili yake.

Idadi kubwa ya kafara ilitolewa wakati wa Pasaka, na mauzo pale hekaluni yalikuwa makubwa sana. Matokeo ya mchanganyiko wa fujo ya sauti katika uuzaji huu ulifanya eneo lile liwe kama mnada wa mifugo wenye kelele badala ya kuwa hekalu takatifu la Mungu. Kulikuwa kunasikika sauti za majadiliano ya bei, sauti za milio ya ng'ombe, miguno ya kondoo, milio ya njiwa, vikiwa vimechanganyika na mlio wa sarafu na sauti za hasira za watu wanaoshindwa kukubaliana. Kwa hiyo mchanganyiko ulikuwa mkubwa sana kiasi cha kuwasumbua wanaoabudu, na maneno yaliyoelekezwa kwake Aliye Juu yalifunikwa na kelele zilizovamia hekalu. Wayahudi walikuwa wakijivunia sana ibada zao. Walifurahia hekalu lao, na walichukulia neno lolote lililosemwa dhidi ya hekalu lile kama makufuru; walikuwa makini sana katika kutekeleza matendo ya kiibada yaliyohusiana nalo; lakini kupenda pesa kulikuwa kumetawala zaidi. Walielewa kwa nadra jinsi walivyokuwa wametanga mbali na kusudi halisi la huduma zile zilizoanzishwa na Mungu.

Wakati Bwana aliposhuka kwenye Mlima Sinai, eneo lile lilitakasika kwa uwepo wake. Musa aliagizwa kuweka mipaka kuzunguka mlima na kuutakasa, na neno la Bwana lilisikika **(156)** likionya: "Jihadharini, msipande mlima huu, wala msiuguse, hata mapambizo yake; kila mtu atakayeugusa mlima huu, bila shaka atauawa." Kutoka 19:12, 13. Hivyo somo lilitolewa kwamba mahali popote ambapo Mungu anadhihirisha uwepo wake, hiyo sehemu ni takatifu. Viwanja vya hekalu la Mungu vingechukuliwa kama vitakatifu. Lakini katika kutafuta faida, yote haya hayakuonwa.

Makuhani na wakuu waliitwa wawakilishi wa Mungu kwa taifa lao; iliwapasa kusahihisha matumizi mabaya ya viwanja **(157)** vya hekalu. Iliwapasa kuonyesha kielelezo cha uadilifu na huruma. Badala ya kutafuta faida yao wenyewe, walipaswa kuzingatia hali halisi na mahitaji ya waumini, na walipaswa kuwa tayari kuwasaidia wale ambao hawakuwa na uwezo wa kununua kafara zilizotakiwa. Lakini hawakufanya hayo. Tamaa ya mali ilikuwa imeifanya mioyo yao kuwa migumu.

Katika sikukuu hii walikuja watu wenye mateso, wenye uhitaji na wenye maisha magumu. Vipofu, viwete, viziwi walikuwepo. Wengine waliletwa wakiwa kwenye machela. Wengi walikuja wakiwa maskini kiasi ambacho wasingeweza kununua hata kafara iliyo ya hali ya chini kabisa kwa ajili ya Bwana, wakiwa maskini kupita kiasi hata wasiweze kununua chakula cha kupoza njaa waliyokuwa nayo. Hawa walisononeshwa sana na maneno ya makuhani. Makuhani walijidai kuwa watu wema; walidai kuwa walezi wa watu; lakini hawakuwa na upole wala huruma. Maskini, wagonjwa, wanaokufa waliomba msaada bila mafanikio. Maumivu yao hayakuamsha huruma yoyote katika mioyo ya makuhani.

Yesu alipoingia hekaluni, aliangalia mandhari yote. Aliona miamala isiyo ya haki. Aliona shida za maskini, ambao walidhani kwamba pasipo kumwaga damu hakuna msamaha wa dhambi. Aliona ukumbi wa nje wa hakalu lake ukiwa umebadilishwa kuwa mahali pa biashara isiyo takatifu. Eneo takatifu lilikuwa limefanywa kuwa kituo kikubwa cha kuuzia na kubadilishia.

Kristo aliona kwamba lazima jambo fulani lifanyike. Sikukuu nyingi zilikuwa zimeletwa kwa watu bila mafundisho sahihi kuhusu umuhimu wake. Waabudu walitoa kafara bila kuelewa kwamba zilikuwa mfano wa Kafara kamilifu moja. Na miongoni mwao, alisimama Yeye aliyeashiriwa na ibada zile, akiwa hatambuliwi wala kuheshimiwa. Ndiye aliyekuwa ametoa maelekezo kuhusu kafara zile. Alielewa thamani ya ishara zile, na aliona kwamba sasa zimepotoshwa na kueleweka isivyo. Ibada ya kiroho ilikuwa inatoweka kwa haraka. Hakukuwa na mwunganiko kati ya Mungu na makuhani na wakuu. Kazi ya Kristo ilikuwa ni kuanzisha ibada iliyo toauti kabisa na ile.

Kristo aliyaangalia matukio yaliyokuwepo pale mbele yake akiwa amesimama kwenye ngazi za viwanja vya hekalu. Akiwa na jicho la kinabii alitazama siku za mbele, na akaona mbali, si miaka tu bali karne na vizazi. Anaona jinsi makuhani na wakuu watakavyopotosha haki ya wahitaji, na kuzuia kwamba injili isihubiriwe kwa maskini. Anaona jinsi upendo wa Mungu utakavyofichwa usionekane kwa wenye dhambi, na jinsi watu watakavyouza na kununua neema ya Mungu kama bidhaa. Anapoona matukio hayo, anapatwa na ghadhabu, mamlaka, na nguvu. Watu wanavutwa kwake. Macho ya wale wanaofanya biashara isiyo takatifu **(158)** yanaelekezwa katika uso wake. Wanashindwa kuacha kumwangalia. Wanahisi kwamba mtu huyu anasoma mawazo yao ya ndani, na kugundua nia yao iliyofichika. Baadhi wanajaribu kuficha nyuso zao, kama vile matendo yao maovu yalikuwa yameandikwa usoni pao, ili kusomwa na macho yale yaliyokuwa yanachunguza.

Mara kunakuwa na ukimya katika biashara ile. Sauti za biashara na mapatano ya bei zimekoma. Mshangao wa hofu unaukumba mkutano. Ilikuwa kama vile wamewekwa mbele ya mahakama ya Mungu ili wajibu mashtaka juu ya matendo yao. Wakimwangalia Yesu wanaona nuru ya uungu ikimlika-mlika katika mwili ule wa kibinadamu. Aliye Mkuu wa mbinguni asimamaye kama hakimu atasimama siku ya mwisho, - akiwa na utukufu ambao si kama huu wa sasa tu, bali akiwa na uwezo kama ule ule wa kusoma moyo. Jicho lake linapita juu ya makutano, na kumwona kila mtu. Umbile lake lilikuwa kama vile liko juu ya wote akiwa na amri, na nuru ya mbinguni inamlika. Anatamka kwa sauti yake ya wazi kama ya mlio – kama sauti ile ile ambayo iliitamka kwenye Mlima Sinai sheria yake ambayo inakiukwa na makuhani na wakuu – ikitoa mwangwi kupitia katika matao ya hekalu aliposema: " Yaondoeni haya; msiifanye nyumba ya Baba yangu kuwa nyumba ya biashara."

Akishuka katika ngazi taratibu, aliinua mjeledi wa kamba zilizofungwa pamoja na kuwaendea, akiwataka wanaofanya biashara waondoke katika viwanja vya hekalu. Akiwa na ushujaa na hasira ambazo hajawahi kuonyesha kabla, alisukuma na kupindua-pindua meza za wale wanaobadili pesa. Sarafu zinadondoka, zikitoa sauti kwenye sakafu ya marumaru. Hakuna anayediriki kuhoji mamlaka yake. Hakuna anayezuia na kutaka biashara iendelee. Yesu hawachapi kwa ule mjeledi wa kamba, lakini mkononi mwake mjeledi ule ulitisha kama upanga uwakao. Maofisa wa hekalu, makuhani, wachuuzi na wafanya biashara ya ng'ombe, wakiwa na kondoo na punda wao, wanakimbia kutoka pale, wakiwa na wazo moja la kuikimbia hukumu ya uwepo wa Yesu.

Hofu ya ghafla iliupata mkutano wote, ambao unahisi kufunikwa na kivuli cha Yesu cha uungu. Kilio cha hofu kinatoka katika midomo ya mamia ya watu. Hata wanafunzi wake wanatetemeka. Wanatiwa hofu na maneno ya Yesu na mwonekano wake, maana si kawaida yake. Wanakumbuka kwamba imeandikwa kuhusu Yeye, "Maana wivu wa nyumba yako umenila." Zaburi 69:9. Muda si mrefu fujo ya makutano na biashara zao imeondoshewa mbali na hekalu la Bwana. Viwanja vile havina tena biashara zisizo takatifu, na ukimya wa kina na utulivu unatawala mahali pa fujo za biashara. **(161)** Uwepo wa Bwana, ule wa zamani uliotakasa mlima, umelitakasa hekalu sasa liliwekwa kwa heshima yake Bwana.

Katika kule kutakasa hekalu, Yesu alikuwa anatangaza kazi yake kama Masihi, na alikuwa akiingia katika kazi yake. Kanisa lile ambalo lilijengwa ili kuwa makao ya Mungu lilipangwa kuwa kama somo kwa Israeli na kwa ulimwengu. Tangu milele ilikuwa kusudi la Mungu kwamba kila kiumbe, tangu serafi mtakatifu na mwenye utukufu mpaka mwanadamu, awe ni hekalu kwa ajili ya makao ya Mwumbaji. Kwa sababu ya dhambi, mwanadamu alikoma kuwa hekalu la Mungu. Ukiwa umetiwa giza na kuchafuliwa na uovu, moyo wa mwanadamu haukuweza tena kufunua utukufu wa Mungu. Lakini kwa Mwana wa Mungu kufanyika mwanadamu, kusudi la mbingu linatimizwa. Mungu anakaa ndani ya mwanadamu, na kwa njia ya neema iokoayo moyo wa mwanadamu unakuwa hekalu lake. Mungu alipanga kwamba hekalu la Yerusalemu liwe ushuhuda wa kuendelea kuelekeza katika hatima ya juu iliyofunuliwa kwa kila mtu. Lakini Wayahudi hawakuwa wameelewa maana ya lile ambalo walikuwa wamelichukulia kwa fahari kubwa. Hawakujitoa wenyewe kuwa hekalu takatifu la Roho wa Mungu. Vile viwanja vya hekalu, vilivyojawa na fujo za biashara isiyo takatifu, viliwakilisha kwa usahihi kabisa hekalu la moyo, ambalo limechafuliwa na uwepo wa hisia za tamaa na mawazo yasiyo na utakatifu. Katika kule kusafisha hekalu kutokana na wauzaji na wanunuzi wa kiulimwengu, Yesu alitangaza kazi yake ya kusafisha moyo kwa kuondoa uchafu wa dhambi, - kutokana na tamaa ya mambo ya kidunia, ubinafsi, tabia za uovu, ambazo zinaharibu roho. "Bwana mnayemtafuta atalijilia hekalu lake ghafla; naam, yule mjumbe wa agano mnayemfurahia, angalieni, anakuja, asema Bwana wa majeshi. Lakini ni nani atakayestahimili siku ya kuja kwake? Au ni nani atakayesimama atakapoonekana yeye? Kwa maana yeye ni mfano wa moto wa mtu asafishaye fedha, ni mfano wa sabuni ya mtu afuaye nguo; naye ataketi kama asafishaye fedha na kuitakasa, naye atawatakasa wana wa Lawi, atawasafisha kama dhahabu na fedha." Mal. 3:1-3.

"Hamjui ya kuwa ninyi mmekuwa hekalu la Mungu, na ya kuwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu? Kama mtu akiliharibu hekalu la Mungu, Mungu atamharibu mtu huyo. Kwa maana hekalu la Mungu ni takatifu, ambalo ndilo ninyi." 1 Wakorintho 3:16, 17. Hakuna mtu ambaye anaweza yeye mwenyewe kuondoa mkusanyiko wa maovu ambao umetawala moyo. Kristo pekee ndiye anaweza kulisafisha hekalu la moyo. Lakini hatalazimisha kuingia. Haji moyoni kama alivyofanya alipoingia katika hekalu la zamani; bali anasema, "Tazama, nasimama mlangoni, nabisha; mtu akiisikia sauti yangu, na kuufungua mlango, nitaingia kwake." Ufunuo 3:20. Hatakuja kwa siku moja pekee; maana anasema, "Nitakaa ndani yao, na kati yao nitatembea; . . . nao watakuwa **(162)** watu wangu." "Atayakanyaga maovu yetu; nawe utazitupa dhambi zao zote katika vilindi vya bahari." 2 Wakorintho 6:16; Mika 7:19. Uwepo wake utasafisha na kutakasa moyo, ili upate kuwa hekalu takatifu kwa Bwana, na kuwa "maskani ya Mungu katika Roho." Waefeso 2:21, 22.

Wakiwa wameshindwa na hofu, makuhani na wakuu walikuwa wamekimbia kutoka katika maeneo ya hekalu, na kutoka mbele ya macho yasomayo mioyo. Walipokuwa wanakimbia walikutana na watu wengine wanaoenda hekaluni, na waliwataka warudi watokako, baada ya kuwaambia mambo waliyoyaona huko. Kristo aliwaangalia watu wale waliokuwa wanakimbia kwa aibu na hofu, na kuona kwamba walikuwa hawajui vitu vinavyoifanya ibada iwe ya kweli. Katika tukio hili aliona ishara ya kutawanyika kwa taifa lote la Kiyahudi kwa sababu ya uovu na kutojutia makosa.

Kwa nini makuhani walikimbia kutoka hekaluni? Kwa nini hawakuisimamia sehemu yao? Yeye aliyewaamuru kwenda alikuwa mwana wa seremala, maskini wa Galilaya, akiwa hana cheo cha duniani wala mamlaka. Kwa nini hawakupingana naye? Kwa nini waliacha mapato waliyopata kwa jinsi ile, na kukimbia kwa amri ya Yeye ambaye mwonekano wake wa nje ulikuwa wa hali ya chini?

Kristo alizungumza kwa mamlaka ya mfalme, na katika mwonekano wake, na toni ya sauti yake kulikuwa na kitu ambacho wao hawakuwa na nguvu za kukipinga. Kwa neno la amri yake walitambua, kwa namna ambayo walikuwa hawajawahi kuelewa, hali yao ya kweli ya kuwa wanafiki na wanyan'anyi. Wakati uungu ulipomlika

ndani ya ubinadamu, si tu kwamba waliona ghadhabu katika uso wa Kristo; walitambua umuhimu wa maneno yake. Walihisi kama wako mbele ya kiti cha enzi cha Hakimu wa milele, wakiwa wametamkiwa hukumu ya wakati huo na milele. Kwa muda fulani walishawishika kwamba Kristo alikuwa nabii; na wengi walimwamini kwamba ni Masihi. Roho Mtakatifu alimlikia katika akili zao yale maneno ya nabii kuhusu Kristo. Je, wangejisalimisha katika usadikishaji huu?

Wasingeweza kutubu. Walijua kwamba huruma ya Yesu kwa maskini ilikuwa imeamshwa. Walijua kwamba walikuwa na hatia ya kujipatia kipato isivyo halali katika kushughulika kwao na watu. Walimchukia Yesu kwa sababu alibaini mawazo yao. Kuwakemea kwake hadharani kulikuwa kunaaibisha kiburi chao, na walikuwa na wivu juu ya mvuto wake uliokuwa ukiongezeka machoni pa watu. Waliazimia kumpinga katika habari ya mamlaka yake ya kuwafukuza pale, kwamba aliipata wapi mamlaka ile.

Taratibu na kwa mawazo mengi, lakini wakiwa na chuki mioyoni mwao, walirudi hekaluni. Lakini ni badiliko kubwa kiasi gani lililokuwa limefanyika kwa wakati ambao hawakuwepo! **(163)** Wakati walipokimbia, maskini walibaki pale; sasa hawa maskini walikuwa wanamwangalia Yesu, ambaye alikuwa na mwonekano wa upendo na huruma. Machozi yakilenga-lenga machoni mwake, aliwaambia watu wale waliomzunguka pande zote ambao walikuwa wanatetemeka: Msiogope; nitawaokoa, nanyi mtanitukuza. Maana nilikuja ulimwenguni kwa ajili ya haya.

Wale watu walisonga karibu na Yesu kwa hamu, na kila mmoja akaomba kwa dhati: Bwana, unibariki. Sikio lake lilisikia kilio cha kila mtu. Kwa huruma iliyo zaidi ya ile ya upendo wa mama alivutwa na mateso ya watu wale walio wadogo. Wote walimvutia. Kila mmoja aliponywa ugonjwa aliokuwa nao. Mabubu walifumbua vinywa vyao na kusifu; vipofu waliona uso wa Mponyaji wao. Mioyo ya watu wasumbukao ilifanywa kuwa na furaha.

Makuhani na maofisa wa hekalu waliposhuhudia kazi hii kubwa, ni mafunuo kiasi gani yaliyoletwa na sauti iliyoyafikia masikio yao! Watu walikuwa wanasimulia machungu yaliyokuwa yamewapata, habari za kukatishwa tamaa kwao, habari ya siku za maumivu na matukio ya kukesha pasipo kulala usiku. Wakati cheche ya mwisho ya matumaini ilipoonekana kufifia, Kristo akawa amewaponya. Mmoja angeweza kusema, Mzigo ulikuwa mzito sana; lakini nimempata wa kunisaidia. Ni Masihi wa Mungu, nami nitatoa maisha yangu kwa kazi yake. Wazazi waliwaambia watoto wao, Ameokoa maisha yenu; inueni sauti zetu juu kumsifu. Sauti za watoto na vijana, akina baba na akina mama, marafiki na watazamaji, waliungana katika kutoa sifa na shukrani. Matumaini na furaha vilijaza mioyo yao. Amani ilikuja mawazoni mwao. Walihuishwa katika mwili na roho, na walirudi nyumbani wakiutangaza kila mahali upendo wa Yesu usiofananishwa na kitu chochote.

Wakati wa kusulibishwa kwa Kristo, hawa waliokuwa wameponywa hawakuungana na makutano wenye fujo katika kupiga kelele wakisema, "Msulibishe. Msulibishe." Walikuwa na huruma kwa Yesu; maana walikuwa wameguswa na huruma yake kuu na uweza wake wa ajabu. Walimjua kwamba ni Mwokozi wao; maana alikuwa amewapa afya ya mwili na roho. Walisikiliza mahubiri ya mitume, na kuingia kwa neno la Mungu mioyoni mwao kuliwapatia ufahamu. Waligeuka kuwa mawakala wa neema ya Mungu, na nyezo za wokovu wake.

Makutano wale waliokuwa wamekimbia kutoka hekaluni walirejea taratibu baada ya muda. Kidogo walikuwa wameondokana na hofu ile iliyokuwa imewafukuza, lakini nyuso zao zilionyesha hali ya kusitasita na woga. Waliziangalia kazi za Yesu kwa mshangao, na walisadikishwa kwamba unabii unaomhusu Masihi ulitimizwa ndani yake. Dhambi ya kulinajisi hekalu iliwakalia makuhani kwa kiasi kikubwa zaidi kuliko hawa. Ilikuwa **(164)** imepangiliwa na makuhani kwamba viwanja vya hekalu vigeuke mahali pa gulio. Watu hawa wa kawaida hawakuwa na hatia ukilinganisha na makuhani hao. Waliguswa na mamlaka ya Yesu ya kimbingu; lakini kwao ushawishi wa makuhani na wakuu ulikuwa bado una mamlaka ya juu zaidi. Waliiona kazi ya Yesu kama uvumbuzi wa jambo jipya, na wakahoji uhalali wa Yeye kuingilia kile kilichokuwa kimeruhusiwa na mamlaka ya hekalu. Walijiona kuwa na hatia kwa sababu biashara ile iliingiliwa, walisongwa na usadikisho wa Roho Mtakatifu.

Makuhani na wakuu walipaswa wawe wamemtambua Yesu kwamba ni mpakwa-mafuta wa Bwana kuliko vile ambavyo wengine wote wangeona; maana magombo matakatifu yaliyoeleza utume wa Yesu yalikuwa mikononi mwao wao, na walijua kwamba kutakaswa kwa hekalu kulikuwa ni udhihirisho wa nguvu iliyo zaidi ya ile ya mwanadamu. Kadiri walivyomchukia Yesu, ndivyo ambavyo wasingeweza kujiweka huru dhidi ya mawazo

kwamba huenda Yesu alikuwa nabii aliyetumwa na Mungu kurejesha utakatifu wa hekalu. Kwa kukubali kushindwa na hofu hiyo, walimwendea Yesu na swali hili, "Ni ishara gani utuonyeshayo, kwamba unafanya haya?"

Yesu alikuwa amewaonyesha ishara. Kwa kumlika nuru katika mioyo yao, na kwa kutenda mbele yao kazi zile ambazo yampasa Masihi kuzifanya, alikuwa amewapa ushahidi wa kutosha wa tabia yake. Sasa walitaka ishara, aliwajibu kwa kutumia mfano, kuonyesha kwamba aliisoma nia yao mbaya, na aliona jinsi ambavyo nia ile ingewapeleka mbali sana. Aliwaambia, "Livunjeni hekalu hili, nami katika siku tatu nitalisimamisha."

Maana yake katika maneno haya ilikuwa na sehemu mbili. Si tu kwamba aliongelea uharibifu wa hakalu la Wayahudi na ibada zao, bali pia kifo chake, - kuharibiwa kwa hekalu la mwili wake. Tayari Wayahudi hawa walikuwa wanamwinda. Wakati makuhani na wakuu waliporudi hekaluni, walikuwa wamepanga kumwua Yesu, ili kwa njia hiyo waondokane na mtaabishaji huyu. Lakini Yeye alilifunua kusudi lao mbele yao, hawakumwelewa. Walichukulia kwamba maneno yake yanahusu tu hekalu la Yerusalemu, na wakasema kwa hasira, "Hekalu hili lilijengwa katika muda wa miaka arobaini na sita, nawe utalisimamisha katika siku tatu?" Walihisi kwamba sasa Yesu ameamua kuonyesha kwamba wao hawaamini, na walithibitishwa kwamba wamemkataa.

Kristo hakupanga kwamba maneno yake yaeleweke kwa Wayahudi wasioamini, wala hata kwa wanafunzi wake wa wakati ule. Alijua kwamba yangeeleweka vibaya kwa adui zake, na yangegeuzwa na kutumiwa dhidi yake. Wakati wa kuhukumiwa kwake yangeletwa kama mashtaka, na pale Kalvari yangevurumishwa kwake kama masuto ya dhihaka. Lakini kuyafafanua sasa kungewapa wanafunzi wake uelewa wa mateso yake, na kuwaletea **(165)** huzuni ambayo kwa wakati ule walikuwa bado hawana uwezo wa kuistahimili. Na kuyafafanua kungewafunulia Wayahudi, kabla ya wakati wake, matokeo ya chuki na kutoamini kwao. Tayari walikuwa wameingia katika njia ambayo wangeifuata kwa nguvu mpaka wakati ambapo Kristo angeongozwa kama mwana-kondoo apelekwaye majinjoni.

Maneno haya yalisemwa na Kristo kwa ajili ya wale ambao wangemwamini. Alijua kwamba maneno hayo yangerudiwa tena. Yakitamkwa wakati wa Pasaka, yangeingia masikioni mwa maelfu ya watu, na kupelekwa katika sehemu zote za ulimwengu. Baada ya kufufuka kutoka kwa wafu, maana ya maneno hayo ingekuwa wazi. Maneno hayo yangekuwa hitimisho la kuthibitisha uungu wake kwa watu wengi.

Kwa sababu ya giza la kiroho, hata wanafunzi wa Yesu walishindwa kupambanukiwa masomo yake. Lakini mfululizo wa matukio uliweka wazi kwao mengi ya masomo haya. Wakati alipokuwa hayuko nao tena, maneno yao yalikaa mioyoni mwao.

Kama vile yanahusu hekalu la Yerusalemu, maneno ya Mwokozi kwamba, "Livunjeni hekalu hili, nami katika siku tatu nitalisimamisha," yalikuwa na maana ya kina zaidi kuliko vile wasikilizaji wake walivyoelewa. Kristo alikuwa msingi na uhai wa hekalu. Huduma za hekalu zilikuwa mfano wa kafara ya Mwana wa Mungu. Ukuhani ulianzishwa kuwakilisha tabia ya upatanishi ya kazi ya Yesu. Mpango mzima wa ibada ya kafara ulikuwa kivuli cha kifo cha Mwokozi ili kuukomboa ulimwengu. Likiishakutimizwa tukio kuu lililoashiriwa na kafara hizo kwa vizazi vingi kusingekuwa na kazi tena katika kafara hizo.

Kwa kuwa mfumo wote wa kutoa fidia kwa njia ya kafara ulikuwa ishara ya Kristo, haukuwa na thamani unapowekwa mbali ya huyo Kristo. Wakati Wayahudi walipotia muhuri hali yao ya kumkataa Kristo walipomtoa afe, maana yake ni kwamba walikuwa wamekataa mambo yote yaliyoleta umuhimu wa hekalu na huduma zake. Utakatifu wa hekalu ulikuwa umetoweka. Lilikuwa linasubiri kuharibiwa. Kuanzia siku hiyo matoleo ya kafara na ibada zilizofungamanishwa nayo havikuwa na maana. Kama yalivyokuwa yale matoleo ya Kaini, hayakuonyesha imani kwa Mwokozi. Kwa kitendo cha kumwua Yesu, ni kama Wayahudi walikuwa wameharibu hekalu lao. Wakati Kristo aliposulibiwa, pazia la ndani ya hekalu lilipasuliwa katika vipande viwili kuanzia chini hadi juu, kuashiria kwamba kafara kuu ya mwisho ilikuwa imetolewa, na ya kwamba mfumo wa kutoa kafara ulikuwa umekoma milele.

"Katika siku tatu nitalisimamisha." Katika kifo cha Mwokozi nguvu za giza zilionekana kushinda, na zilishangilia ushindi. Lakini kutoka katika kaburi lililofunguka, Yesu alitoka akiwa mshindi. "Akiisha kuzivua enzi na mamlaka, na kuzifanya kuwa mkogo kwa ujasiri, akizishangilia katika msalaba huo." Wakolosai 2:15. Kwa njia ya

kifo na kufufuka kwake **(166)** alikuwa mhudumu wa ile "hema ya kweli, ambayo Bwana aliiweka wala si mwanadamu." Waebrania 8:2. Wanadamu waliinua hema takatifu ya Wayahudi; wanadamu walijenga hekalu la Wayahudi; lakini patakatifu pa huko juu, ambapo pale pa duniani palikuwa kivuli chake, hapakujengwa kwa usanifu wa mwanadamu. "Tazama, mtu huyu ndiye ambaye jina lake ni Chipukizi; . . . Naam, yeye atalijenga hekalu la Bwana; naye atauchukua huo utukufu; ataketi akimiliki katika kiti chake cha enzi; na kutakuwa na kuhani katika kiti chake cha enzi." Zekaria 6:12, 13.

Huduma za kafara zilizosonda kidole kwa Kristo zilikoma; bali macho ya wanadamu yaligeuzwa ili yaiangalie kafara ya kweli kwa ajili ya dhambi za ulimwengu. Ukuhani wa duniani ulikoma; bali tunamwangalia Yesu, mjumbe wa agano jipya, na "damu ya kunyunyizwa, inenayo mema kuliko ile ya Habili." "Njia ya kupaingia patakatifu ilikuwa haijadhihirishwa bado, hapo hema ya kwanza ilipokuwa ingali ikisimama; . . . Lakini Kristo akiisha kuja, aliye kuhani mkuu wa mambo mema yatakayokuwapo, kwa hema iliyo kubwa na kamilifu zaidi, isiyofanyika kwa mikono, . . . bali kwa damu yake mwenyewe aliingia mara moja tu katika Patakatifu, akiisha kupata ukombozi wa milele." Waebrania 12:24; 9:8-12.

"Naye, kwa sababu hii, aweza kuwaokoa kabisa wao wamjiao Mungu kwa yeye; maana yu hai sikuzote ili awaombee." Waebrania 7:25. Ingawa huduma ile ilikuwa inaondolewa katika hekalu la duniani kwenda katika hekalu la mbinguni; ingawa patakatifu na kuhani wetu mkuu wasingeonekana kwa macho ya kibindamu, bado wanafunzi wasingepata hasara yoyote. Wasingeona mpasuko wowote katika ushirika wao, na kusingekuwa na mapungufu yoyote ya nguvu kwa sababu ya kutokuwepo kwa Mwokozi. Wakati Yesu akihudumu katika patakatifu pa huko juu, bado ni mhudumu wa kanisa duniani kwa njia ya Roho wake. Ameondolewa katika macho ya kawaida, lakini ahadi yake wakati wa kuondoka kwake imetimizwa, aliposema, "Tazama, nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari." Mathayo 28:20. Wakati ambapo anakasimisha nguvu zake kwa watenda-kazi walio dhaifu, uwepo wake utiao nguvu bado uko pamoja na kanisa lake.

"Basi, iwapo tunaye kuhani mkuu, . . . Yesu, Mwana wa Mungu, na tuyashike sana maungamo yetu. Kwa kuwa hamna kuhani mkuu asiyeweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu; bali yeye alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote, bila kufanya dhambi. Basi na tukikaribie kiti cha neema kwa ujasiri, ili tupewe rehema, na kupata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji." Waebrania 4:14-16.

# Sura ya 17

## Nikodemo

[Msingi wa sura hii uko katika Yohana 3:1-17.]

Nikodemo alikuwa na nafasi ya juu ya kutumainiwa katika taifa la Uyahudi. Alikuwa mtu aliyeelimika sana, na alikuwa na vipaji ambavyo si vya tabia ya kawaida, na alikuwa mjumbe wa heshima katika baraza la taifa. Kama wengine, alikuwa amechanganywa na kitendo cha kufundisha cha Yesu. Ingawa alikuwa tajiri, aliyesoma, na mwenye kuheshimiwa, alikuwa amevutiwa na huyu Mnazareti mnyenyekevu kwa hali isiyo ya kawaida. Masomo yaliyokuwa yametoka katika midomo ya Mwokozi yalikuwa yamemgusa sana, na alitamani kujifunza zaidi kuhusu kweli hizi za ajabu.

Kitendo cha Kristo kutumia mamlaka kulisafisha hekalu kilikuwa kimeamsha chuki kubwa ya makuhani na wakuu. Waliiogopa nguvu ya mtu huyu mgeni. Ujasiri kama huo unaoonyeshwa na Mgalilaya asiyejulikana vema ulikuwa jambo ambalo lisingevumiliwa. Waliazimu kuikomesha kazi yake. Lakini si wote waliokubaliana na kusudi hili. Walikuwepo baadhi ambao waliogopa kumpinga Yeye ambaye alishuhudiwa akijiliwa na Roho wa Mungu. Walikumbuka jinsi manabii walivyokuwa wameuawa kwa sababu ya kukemea dhambi za viongozi wa Israeli. Walijua kwamba kutiwa utumwani kwa Wayahudi chini ya wapagani ilikuwa ni matokeo ya usumbufu wao katika kukataa maonyo kutoka kwa Mungu. Walihofu kwamba kwa kitendo chao cha kufanya njama dhidi ya Yesu makuhani na wakuu walikuwa wakifuata katika nyayo za mababa, na wangeleta majanga mapya juu ya taifa. Nikodemo alikuwa na hisia hizo pia. Katika **(168)** baraza la Sanhedrin, wakati njia ya kumshughulikia Yesu ilipokuwa inajadiliwa, Nikodemo alishauri kuwe na tahadhari na utulivu. Alisisitiza kwamba ikiwa Yesu alikuwa amepewa mamlaka kutoka kwa Mungu, ingekuwa ni hatari kukataa maonyo yake. Makuhani hawakudiriki kujali ushauri huu, na kwa muda hawakuchukua hatua za wazi dhidi ya Kristo.

Tangu amsikie Yesu, Nikodemo alikuwa amevutwa kuchunguza unabii unaomhusu Masihi; na kadiri alivyochunguza zaidi, ndivyo alivyosadikishwa zaidi kuwa huyu ndiye Yeye aliyekuwa anakuja. Pamoja na wengine wengi katika Israeli alikuwa ametatanishwa na jinsi hekalu lilivyokuwa limechafuliwa. Alikuwa shuhuda wakati Yesu alipowafukuza wauzaji na wanunuzi; aliona udhihirisho wa ajabu wa nguvu ya kimbingu; alimwona Mwokozi akiwapokea maskini na kuponya wagonjwa; aliona walivyoonekana kwa furaha, na alisikia maneno yao ya kusifu; na hakuweza kuwa na mashaka kwamba Yesu wa Nazareti ni Yeye Aliyetumwa na Mungu.

Alitamani sana ahojiane na Yesu, lakini aliogopa kumtafuta waziwazi. Ingekuwa jambo la kudhalilisha sana kwa mkuu wa Wayahudi kujisalimisha kwa mwalimu ambaye alikuwa bado anajulikana kidogo namna ile. Na ikiwa habari ya jambo kama hilo ingewafikia wajumbe wa Sanhedrin, lingemletea kudharauliwa na kushutumiwa. Aliazimia kufanya mahojiano ya siri, akitolea sababu kwamba ikiwa angeenda waziwazi, na wengine wangefuata mfano wake. Akitumia njia maalum ya kuulizia-ulizia kuhusu mahali Yesu anapopumzikia katika Mlima wa Mizeituni, alisubiri mpaka mji ulipokuwa kimya watu wakiwa wamelala, ndipo alipomtafuta.

Mbele ya uwepo wa Yesu, Nikodemo alikosa hali ya kujiamini kwa namna ambayo haikutarajiwa, ambayo aliamua kuificha kwa kutulia na kuwa na heshima. Alisema, "Rabi, twajua ya kuwa u mwalimu, umetoka kwa Mungu; kwa maana hakuna mtu awezaye kuzifanya ishara hizi uzifanyazo wewe, isipokuwa Mungu yu pamoja naye." Kwa kuongea kuhusu vipawa maalum vya Kristo kama mwalimu, na kuhusu uwezo wake wa ajabu wa kutenda miujiza, alitumaini kwamba anaweka njia kwa ajili ya mahojiano yake. Maneno yake yalipangwa kuonyesha na kukaribisha hali ya kujiamini; lakini kumbe yalionyesha hasa kutokuamini. Hakukiri kwamba Yesu ni Masihi, bali kwamba ni mwalimu aliyetumwa kutoka kwa Mungu.

Badala ya kutambua maneno haya ya salamu, Yesu alimkazia macho huyo aliyesema, kama vile alikuwa anasoma moyo wake. Katika hekima yake isiyo mwisho pale alimwona mtu anayetafuta ukweli. Alijua lengo la ujio huu, na akiwa na hamu ya kuimarisha kwa kina imani iliyokuwa katika ufahamu wa msikilizaji wake huyu, alikuja kwenye kiini chenyewe, akisema wazi, lakini kwa upendo, "Amin, amin, nakuambia, Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuona ufalme wa Mungu." Yohana 3:3.

**(171)** Nikodemo alikuwa amekuja kwa Bwana akidhani ya kwamba atafanya naye majadiliano, lakini Yesu aliweka wazi kanuni za msingi za ukweli. Alimwambia Nikodemo, unachohitaji zaidi si ufahamu wa kinadharia bali kufanywa upya kiroho. Unachohitaji si kutosheleza udadisi wako, bali kuwa na moyo mpya. Lazima upokee maisha mapya kutoka juu kabla haujafahamu vyema mambo ya mbinguni. Kabla ya badiliko hili kutokea, likafanya mambo yote kuwa mapya, kujadiliana na Mimi kuhusu mamlaka yangu au kazi yangu hakutakufaa jambo lolote jema.

Nikodemo alikuwa amekwishasikia mahubiri ya Yohana Mbatizaji kuhusu toba na ubatizo, na jinsi alivyowaelekeza watu kwake Yeye ambaye angebatiza kwa Roho Mtakatifu. Hata yeye mwenyewe alikuwa amehisi kwamba kulikuwa na ukosefu wa hali ya kiroho miongoni mwa Wayahudi, kiasi kwamba, kwa kiasi kikubwa, walikuwa wanatawaliwa na misimamo ya kiitikadi na tamaa za kidunia. Alikuwa ametumainia hali nzuri zaidi ya mambo wakati Masihi ajapo. Lakini bado ujumbe upelelezao moyo wa Mbatizaji ulikuwa umeshindwa kufanya kazi ya kumsadikisha hatia ya dhambi. Alikuwa Farisayo hasa, na alijivunia matendo yake mema. Alikuwa mtu wa kutukuzwa sana kwa ukarimu wake na utayari wa kuwezesha huduma za hekalu, na alifikiri yuko salama mbele za Mungu. Alishtushwa na mawazo kwamba kuna ufalme ulio safi kiasi ambacho yeye katika hali yake hii asingeweza kuuona.

Stiari ya kuzaliwa upya iliyotumiwa na Yesu si kwamba ilikuwa haijulikani kabisa kwa Nikodemo. Waongofu waliotoka upaganini kuja katika imani ya Israeli walilinganishwa mara nyingi na watoto ambao wamezaliwa. Kwa hiyo lazima atakuwa alielewa kwamba maneno ya Kristo hayakuwa na maana ya moja kwa moja ya kawaida. Lakini kwa kuzaliwa kwake kama Mwisraeli alijiona kuwa na uhakika wa nafasi katika ufalme wa Mungu. Alifikiri kwamba hakuhitaji badiliko. Ndiyo sababu alishangazwa na maneno ya Mwokozi. Alisumbuliwa na hali ya meneno hayo kuhusishwa naye. Kiburi cha Farisayo kilikuwa kinapambana na hamu ya uaminifu ya kutafuta ukweli. Alishangaa kwamba ni kwa nini Kristo alimsema vile, pasipo kuheshimu nafasi yake kama mkuu katika Israeli.

Akishangazwa na kushindwa kujitawala, alimjibu Kristo kwa maneno yaliyo kinyume, "Awezaje mtu kuzaliwa, akiwa mzee?" Kama walivyo wengi wengine pindi ukweli mkali ukatao unapoletwa mahali pake katika dhamiri zao, alidhihirisha ukweli kwamba mwanadamu kwa asili hapokei mambo ya Roho wa Mungu. Ndani yake hamna kitu kinachoitikia mambo ya kiroho; maana mambo ya kiroho yanatambuliwa na roho.

Lakini Mwokozi hakwenda na hoja kwa hoja. Akiunyoosha mkono wake kwa nguvu, kwa heshima, aliubandika ukweli mahali pake kwa **(172)** uhakika mkubwa, akasema, "Amin, amin, nakuambia, Mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuuingia ufalme wa Mungu." Nikodemo alijua kwamba hapa Kristo aliongea kuhusu ubatizo wa maji na moyo kufanywa upya na Roho Mtakatifu. Aliridhika kwamba alikuwa mbele za Yeye ambaye Yohana Mbatizaji alitabiria.

Yesu aliendelea: "Kilichozaliwa kwa mwili ni mwili; na kilichozaliwa kwa Roho ni roho." Moyo ni muovu kwa asili, na "ni nani awezaye kutoa kitu kilicho safi kitoke katika kitu kichafu? Hapana awezaye." Ayubu 14:4. Hakuna uvumbuzi wa mwanadamu unaoweza kupata tiba ya moyo utendao dhambi. "Nia ya mwili ni uadui juu ya Mungu, kwa maana haitii sheria ya Mungu, wala haiwezi kuitii." "Kwa maana moyoni hutoka mawazo mabaya, uuaji, uzinzi, uasherati; wivi, ushuhuda wa uongo, na matukano." Warumi 8:7; Mathayo 15:19. Lazima chemchemi ya moyo isafishwe kabla ya vijito kuwa safi. Yeye anayejaribu kwenda mbinguni kwa matendo yake ya kushika sheria anajaribu kufanya lisilowezekana. Hakuna usalama kwa mtu ambaye ana dini ya sheria, ucha-Mungu wa mazoea. Maisha ya Mkristo si mageuzi au maboresho ya maisha ya kale, bali ni badiliko la jumla la hali ya asili. Kuna kufa kwa nafsi na dhambi, na kupata maisha mapya kabisa. Badiliko hili linaweza kuletwa na kazi ya Roho Mtakatifu tu.

Nikodemo alikuwa bado ametatizwa, na Yesu akatumia upepo kufafanua maana yake: "Upepo huvuma upendako, na sauti yake waisikia, lakini hujui unakotoka wala unakokwenda; kadhalika na hali yake kila mtu aliyezaliwa kwa Roho."

Upepo husikika katika matawi ya miti, yakitikisa majani na maua na kuyafanya yatoe sauti; lakini hauonekani, na hakuna mtu anayejua unakotoka na unakokwenda. Hivyo ndivyo ilivyo kazi ya Roho Mtakatifu katika moyo. Haiwezi kuelezeka zaidi ya vile upepo uvumavyo. Mtu hawezi kueleza muda hasa au mahali, au kufuatilia

mazingira yote ya kuongoka kwake; lakini hali hii haimfanyi kwamba awe hajaongoka. Kwa njia isiyoonekana kama ulivyo upepo, Kristo anafanya kazi na moyo wakati wote. Kidogo-kidogo, pengine bila mhusika kujua, mawazo ambayo yana tabia ya kuuvuta moyo kwa Yesu yanawekwa. Haya yanaweza kupatikana kwa kumtafakari Yesu, kwa kusoma Maandiko, au kwa njia ya kusikiliza neno moja kwa moja kwa mhubiri. Ghafla, kadiri Roho anavyokuja kwa ushawishi wa moja kwa moja, roho hujisalimisha kwa furaha kwa Yesu. Kwa wengi hali hii inaonekana kama uongofu wa ghafla; lakini ni matokeo ya kubembeleza kwa Roho wa Mungu kwa muda mrefu, - mchakato wa muda mrefu wa uvumilivu.

**(173)** Wakati upepo kwa wenyewe hauonekani, unaleta matokeo ambayo yanaonekana na kuweza kuyahisi. Vivyo hivyo kazi ya Roho katika moyo itajifunua katika kila tendo la mtu ambaye amepokea nguvu yake iokoayo. Wakati Roho Mtakatifu anapoumiliki moyo, anabadilisha maisha. Mawazo ya dhambi yanawekwa mbali, matendo maovu yanaachwa; upendo, unyenyekevu, na amani vinachukua nafasi ya hasira, husuda, na magomvi. Furaha huchukua nafasi ya huzuni, na uso huakisi nuru ya mbinguni. Hakuna mtu anayeona mkono unaobeba mzigo, au kuona nuru inavyoshuka kutoka mbinguni juu. Mbaraka unakuja pindi moyo unapojisalimisha kwa imani kwa Mungu. Hapo nguvu ile ambayo haiwezi kuonekana kwa jicho la mwanadamu huumba utu upya katika sura ya Mungu.

Haiwezekani kwa mawazo finyu ya mwanadamu kuelewa kazi ya ukombozi. Siri yake inazidi ufahamu wa mwanadamu; lakini yeye apitaye kutoka mautini kwenda uzimani anagundua kwamba ni uhalisia wa kimbingu. Tunaweza kujua mwanzo wa ukombozi kupitia uzoefu binafsi. Matokeo yake yanaenda hadi vizazi vya milele.

Wakati Yesu alipokuwa anaongea, miale ya ukweli ilikuwa inapenya mawazo ya mkuu yule. Ushawishi wa Roho Mtakatifu unaolainisha na kushusha kiburi ulisonga moyo wake. Lakini bado hakuelewa kwa ukamilifu maneno ya Mwokozi. Hakuguswa sana na umuhimu wa kuzaliwa upya. Aliuliza kama kwa mshangao, "Yawezekanaje kuwa mambo haya?"

"Je! Wewe u mwalimu wa Israeli, na mambo haya huyafahamu?" Yesu alimwuliza. Kwa kweli mtu aliyepewa kazi ya kufundisha watu mambo ya dini asingekuwa mtu asiyejua ukweli muhimu hivyo. Maneno yake yalitoa somo kwamba badala ya kuhisi kudhalilishwa na maneno ya wazi ya ukweli, Nikodemo alipaswa kuwa na mawazo ya kujishusha, kwa sababu ya kutokujua kwake. Lakini bado Yesu aliongea kwa heshima na upendo, na mtazamo wake na sauti vilionyesha upendo huo wa dhati, kiasi kwamba Nikodemo hakujisikia kuhukumiwa.

Lakini kadiri Yesu alivyoeleza kwamba kazi yake duniani ilikuwa ni kuanzisha ufalme wa kiroho badala ya ufalme wa muda, msikilizaji wake huyu alisumbuka. Kwa kuona hilo, Yesu aliongeza hivi, "Ikiwa nimewaambia mambo ya duniani, wala hamsadiki, mtasadiki wapi niwaambiapo mambo ya mbinguni?" Ikiwa Nikodemo hakuweza kupokea mafundisho ya Yesu, yakifafanua kazi ya neema katika moyo, angewezaje kuelewa ufalme wa Kristo wa mbinguni? Kwa kule kushindwa kuelewa kazi ya Yesu duniani, asingeelewa kazi yake mbinguni.

Wayahudi waliofukuzwa na Yesu kule hekaluni walidai kuwa wana wa Ibrahimu, lakini waliukimbia uwepo wa Mwokozi kwa sababu **(174)** hawakuweza kustahimili utukufu wa Mungu uliodhihirishwa ndani yake. Kwa hiyo walitoa uthibitisho kwamba hawakustahili neema ya Mungu kushiriki katika huduma takatifu za hekalu. Walikuwa na bidii katika kutunza mwonekano wa utakatifu, lakini walipuuza utakatifu wa moyo. Wakati walikuwa wang'ang'anizi wa urasmi wa maandiko ya sheria, walikuwa wanakiuka kiini chake wakati wote. Hitaji lao kubwa lilikuwa ni lile badiliko lililoelezwa na Kristo kwa Nikodemo, - kuzaliwa upya katika maadili, kusafishwa kutoka katika dhambi, na kufanywa upya katika ufahamu na utakatifu.

Upofu wa Israeli kuhusu kufanywa upya haukuwa na udhuru. Kwa uvuvio wa Roho Mtakatifu, Isaya alikuwa ameandika hivi, "Kwa maana sisi sote tumekuwa kama mtu aliye mchafu, na matendo yetu yote ya haki yamekuwa kama nguo iliyotiwa unajisi." Daudi alikuwa amesali akisema, "Ee Mungu, uniumbie moyo safi, Uifanye upya roho iliyotulia ndani yangu." Na kupitia kwa Ezekieli ahadi ilikuwa imetolewa, "Nami nitawapa ninyi moyo mpya, nami nitatia roho mpya ndani yenu, nami nitatoa moyo wa jiwe uliomo ndani ya mwili wenu, nami nitawapa moyo wa nyama. Nami nitatia roho yangu ndani yenu, na kuwaendesha katika sheria zangu, nanyi mtazishika hukumu zangu, na kuzitenda." Isaya 64:6; Zaburi 51:10; Ezekieli 36:26, 27.

Nikodemo alikuwa ameshasoma maandiko akiwa na mawazo yaliyotiwa wingu; lakini sasa alianza kuelewa maana ya maandiko hayo. Aliona kwamba msimamo wa kutii herufi za sheria uliofanywa katika maisha ya nje tu

usingemfaa mtu kuingia katika ufalme wa mbinguni. Kwa mtazamo wa wanadamu, maisha yake yalikuwa ya haki na yaliyotukuzwa; lakini mbele ya Kristo alijisikia kwamba moyo wake haukuwa safi, na maisha yake hayakuwa matakatifu.

Nikodemo alikuwa anavutwa kwa Kristo. Kadiri Mwokozi alivyofafanua kwake kuhusu kuzaliwa upya, alitamani kupata badiliko hilo ndani yake. Ingefanyikaje? Yesu alijibu swali hilo ambalo halikusemwa: "Na kama vile Musa alivyomwinua yule nyoka jangwani, vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa; ili kila mtu aaminiye awe na uzima wa milele katika yeye."

Huu ulikuwa uwanja uliokuwa unafahamika kwa Nikodemo. Ishara ya nyoka aliyeinuliwa iliweka kwake uwazi wa kazi ya Yesu. Wakati watu wa Israeli walipokuwa wanakufa kwa kuumwa na nyoka wa moto, Mungu alimwagiza Musa kufanya nyoka wa shaba, na kumtundika juu katikati ya kusanyiko. Halafu tangazo lilitolewa katika mahema yote kwamba wote ambao wangemwangalia yule nyoka wangeishi. Watu walijua vema kwamba yule nyoka hakuwa na uwezo ndani yake mwenyewe wa kuwasaidia. Alikuwa ishara ya Kristo. Kama vile sanamu ile ya nyoka iliyofanywa katika mfano wa **(175)** nyoka aharibuye ilivyoinuliwa juu kwa ajili ya uponyaji wao, ndivyo ambavyo Yeye aliyefanywa "katika mfano wa mwili ulio wa dhambi" angekuwa Mkombozi. Warumi 8:3. Wengi miongoni mwa Waisraeli walichukulia kwamba huduma za kafara zilikuwa na uwezo wa kuwaweka huru kutoka katika dhambi. Mungu alitaka kuwafundisha kwamba hazikuwa na thamani tena zaidi ya vile alivyokuwa nyoka wa shaba. Lengo lilikuwa ni kuongoza mawazo yao kwenda kwa Mwokozi. Iwe ni kwa kuponya majeraha yao au kusamehewa dhambi zao, wasingejifanyia lolote bali kuonyesha imani yao katika Zawadi ya Mungu. Walipaswa waiangalie ili waishi.

Wale walioumwa na nyoka wangetamani kuchelewa kumwangalia yule nyoka. Wangehitaji kuhoji kwamba inakuwaje uponyaji unapatikana katika ishara ile ya kuaibisha. Wangehitaji kudai ufafanuzi wa kisayansi. Lakini hakuna ufafanuzi uliotolewa. Lazima wakubali neno la Mungu kwao kupitia Musa. Kukataa kuangalia kulimaanisha kuangamia.

Kumlikiwa kwa moyo hakufanyiki kwa njia ya mabishano na majadiliano. Lazima tuangalie ili tuishi. Nikodemo alipata somo, na kwenda nalo. Alichunguza Maandiko katika njia mpya, si kwa lengo la kujadili nadharia, bali ili kupata uzima wa roho. Alianza kuona ufalme wa mbinguni kadiri alivyojisalimisha katika uongozo wa Roho Mtakatifu.

Kuna maelfu ya watu leo ambao wanahitaji kujifunza ukweli ule uliofundishwa kwa Nikodemo kwa njia ya nyoka aliyeinuliwa. Wanategemea kwamba utii wao wa sheria ya Mungu utawafanya wakubalike kwa Mungu. Wanapotakiwa kumwangalia Yesu, na kuamini kwamba anawaokoa kwa neema yake, wanauliza kwa mshangao kwamba, "Yawezekanaje mambo hayo?"

Kama Nikodemo, lazima tuwe na utashi wa kuingia katika uzima kwa jinsi kama ya mkuu wa wadhambi. Zaidi ya Kristo, "hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo." Matendo 4:12. Kwa njia ya imani tunapokea neema ya Mungu; lakini imani si Mwokozi wetu. Haileti kitu. Dawa ya dhambi ni mkono tunaonyosha kumshikilia Kristo, na kujitwalia wema wake. Wala hatuwezi hata kutubu bila msaada wa Roho wa Mungu. Maandiko yanasema kuhusu Kristo, "Mtu huyo Mungu amemtukuza kwa mkono wake wa kuume, awe Mkuu na Mwokozi, awape Waisraeli toba na msamaha wa dhambi." Matendo 5:31. Toba inatoka kwa Kristo kama ilivyo kwa msamaha.

Sisi, basi, tutawezaje kuokoka? "Kama vile Musa alivyoinua nyoka jangwani," ndivyo hivyo Mwana wa Adamu ameinuliwa, na kila mmoja ambaye amedanganywa na kuumwa na nyoka aangalie ili aishi. "Tazama Mwana-kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya **(176)** ulimwengu." Yohana 1:29. Nuru inayomlika kutoka msalabani inadhihirisha upendo wa Mungu. Upendo wake unatuvuta kwake. Ikiwa hatupingi kuvutwa huku, tutaongozwa kwenda chini ya msalaba kwa toba ya dhambi zilizomsulibisha Mwokozi. Halafu Roho wa Mungu kwa imani anaweka maisha mapya moyoni. Mawazo na shauku vinaletwa katika kutii mapenzi ya Kristo. Moyo, akili, vinaumbwa upya katika sura yake Yeye awekaye uwezo ndani yetu wa kusalimisha vitu vyote kwake yeye mwenyewe. Hapo ndipo sheria ya Mungu huandikwa katika nia na moyo, na tunaweza kusema pamoja na Kristo, "Kuyafanya mapenzi yako, Ee Mungu wangu, ndiyo furaha yangu." Zaburi 40:8.

Katika mahojiano na Nikodemo, Yesu aliufunua mpango wa wokovu, na utume wake kwa ulimwengu. Hakuna mahali pengine ambapo katika mafundisho yake alifafanua kwa ukamilifu hivi, hatua kwa hatua, kazi ya muhimu kufanywa katika mioyo ya wote watakaourithi ufalme wa mbinguni. Mwanzoni mwa huduma yake alifunua ukweli kwa wajumbe wa Sanhedrin, kwa akili ambazo zilikuwa radhi kupokea, na kwa mwalimu wa watu aliyeheshimika. Lakini viongozi wa Israeli hawakupokea nuru hiyo. Nikodemo alificha ukweli huu moyoni mwake, na kwa miaka mitatu kulikuwa na matunda kidogo yaliyokuwa dhahiri.

Lakini Yesu alifahamu vema udongo ule ambamo alikuwa amepanda mbegu ile. Maneno yale yaliyosemwa usiku akiambiwa mtu mmoja mahali pa faragha mlimani hayakupotea. Kwa muda Nikodemo hakumkiri Kristo hadharani, lakini alichunga maisha yake, na alitafakari mafundisho ya Kristo. Katika baraza la Sanhedrin alionyesha mara kwa mara kupingana na mipango ya makuhani ya kumwondosha Kristo. Wakati Yesu alipoinuliwa msalabani hatimaye, Nikodemo alikumbuka mafundisho yale ya Mlima wa Mizeituni kwamba: "Na kama vile Musa alivyomwinua yule nyoka jangwani, vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa; ili kila mtu amwaminiye **(177)** asipotee, bali awe na uzima wa milele." Nuru kutoka katika yale mahojiano ya faragha ilimlikia msalaba wa Kalvari, na Nikodemo, ndani ya Yesu, alimwona Yeye aliye Mkombozi wa ulimwengu.

Baada ya kupaa kwa Bwana, wakati wanafunzi walipokuwa wametawanyika kwa sababu ya mateso, Nikodemo alisimama mbele kwa ujasiri. Alitumia utajiri wake kulitegemeza kanisa lile changa ambalo Wayahudi walikuwa wametarajia kwamba lingefutika mara Yesu alipokufa. Yeye aliyekuwa mwenye wasiwasi na maswali alikuwa imara kama mwamba wakati wa hatari, akitia nguvu imani ya wanafunzi, na kutoa mahitaji kwa ajili ya kuipeleka mbele kazi ya injili. Alibezwa na kuteswa na wale waliokuwa wanamheshimu sana siku za nyuma. Aligeuka kuwa maskini wa mali za dunia hii; lakini hakupoteza ujasiri katika imani ile iliyokuwa imeanzia katika ule mkutano wa usiku pamoja na Yesu.

Nikodemo alimsimulia Yohana habari za mahojiano yale, na kwa kalamu yake habari zile ziliandikwa kwa ajili ya kufundishia mamilioni ya watu. Kweli zile zilizofundishwa ni za muhimu leo kama vile zilivyokuwa muhimu katika usiku ule mlimani, wakati yule mtu mkubwa katika taifa laa Wayahudi alipokuja kujifunza njia ya uzima kwa mwalimu wa hali ya chini wa Galilaya.

# Sura ya 18

## "Yeye Hana Budi Kuzidi"

[Msingi wa sura hii uko katika Yohana 3:22-36.]

Kwa muda sasa ushawishi wa Yohana Mbatizaji katika taifa ulikuwa umekuwa mkubwa kuzidi ule wa wakuu, makuhani, au watawala. Ikiwa angelijitangaza kama Masihi, na kuanzisha upinzani dhidi ya Rumi, makuhani na watu wangemiminika kumfuata. Shetani alikuwa ameweka mbele ya Yohana Mbatizaji kila hali inayoelekeza katika tamaa ya kushinda na kutwaa mamlaka ya ulimwengu. Lakini pamoja na uhakika wa madaraka uliokuwa mbele yake, alikuwa amekataa katakata kupokea hongo ya ufahari. Mtazamo wa kutukuzwa ulikuwa umeelekezwa kwake, yeye akauelekeza kwa Yule Mwingine.

Sasa aliona wimbi la umaarufu likigeuka kutoka kwake kwenda kwa Mwokozi. Siku baada ya siku ukubwa wa mkutano wake ulipungua. Wakati Yesu alipotoka Yerusalemu kuja katika eneo la karibu na Yordani, watu walikusanyika kumsikiliza. Idadi ya wanafunzi wake iliongezeka kila siku. Wengi walikuja ili wabatizwe, wakati Yesu mwenyewe hakubatiza, aliwapa mamlaka wanafunzi wake kutekeleza kaida hiyo ya kidini. Hivyo ndivyo alivyoitia muhuri wake kazi ya mtangulizi wake. Lakini wanafunzi wa Yohana walipatwa na wivu kwa sababu umaarufu wa Yesu ulikuwa unaongezeka sana. Walijiweka tayari kuikosoa kazi yake, na haukupita muda mrefu kabla ya wao kupata fursa hiyo. Swali liliibuka kati yao na Wayahudi likiuliza ikiwa ubatizo ulilenga kutakasa moyo dhidi ya dhambi; wao wakashikilia msimamo kwamba ubatizo wa Yesu ulitofautiana na ule wa Yohana. Baada ya muda mfupi kulikuwa na mabishano kati yao na wanafunzi wa Yesu kuhusu maneno yanayofaa kutumiwa wakati wa kubatiza, na mwishowe wakahoji uhalali wa huo ubatizo mwingine.

**(179)** Wanafunzi wa Yohana walimjia Yohana wakiwa na malalamiko, wakisema, "Rabi, yeye aliyekuwa pamoja nawe ng'ambo ya Yordani, yeye uliyemshuhudia, tazama, huyo anabatiza na watu wote wanamwendea." Kwa maneno haya, Shetani alileta majaribu kwa Yohana. Ingawa utume wa Yohana ulikuwa kama unafikia mwisho wake, ilikuwa bado inawezekana kwa yeye kusababisha kizuizi kwa kazi ya Kristo. Ikiwa angelijiangalia yeye binafsi, na kuonyesha huzuni au kukata tamaa kwa sababu ya kuzidiwa heshima, angelikuwa amepanda mbegu za upinzani, angelikuwa ameleta moyo wa husuda na wivu, na angelikuwa amekwaza sana maendeleo ya injili.

Kwa asili Yohana alikuwa na mapungufu na udhaifu wa kawaida kwa mwanadamu, lakini mguso wa upendo wa kimbingu ulikuwa umembadilisha. Alikuwa amekaa katika mazingira ambayo hayakuchafuliwa na ubinafsi na tamaa ya kutaka makuu, na zaidi sana tatizo la wivu. Hakuonyesha huruma kwa kutoridhishwa kwa wanafunzi wake, bali alionyesha jinsi ambavyo alielewa uhusiano wake na Masihi, na jinsi alivyomkaribisha kwa furaha Yeye ambaye alikuwa amemtayarishia njia.

Alisema, "Hawezi mtu kupokea neno lolote isipokuwa amepewa kutoka mbinguni. Ninyi wenyewe mwanishuhudia ya kwamba nalisema, Mimi siye Kristo, bali nimetumwa mbele yake. Aliye naye bibi arusi ndiye bwana arusi; lakini rafiki yake bwana arusi, yeye anayesimama na kumsikia, aifurahia sana sauti yake bwana arusi." Yohana alijionyesha kama rafiki aliyefanya kazi kama ya rafiki mshenga asimamaye katikati ya wachumba wawili, wanaojiandaa kufunga ndoa. Wakati Bwana arusi alipokuwa amempokea bibi arusi wake, kazi ya rafiki yule ilikuwa imekamilika. Alifurahi katika furaha ya wale ambao amechangia kufanikisha kuungana kwao. Kwa hiyo Yohana alikuwa ameitwa ili kuwaelekeza watu kwa Yesu, na furaha yake ilikuwa ni kushuhudia mafanikio ya kazi ya Yesu. Alisema, "Basi hii furaha yangu imetimia. Yeye hana budi kuzidi, bali mimi kupungua."

Akimwangalia Mkombozi kwa imani, Yohana alikuwa amefika juu katika kilele cha kujinyima. Hakutafuta kuwavuta watu kwake mwenyewe, bali kuinua mawazo yao juu na juu zaidi, mpaka yatulie kwa Mwana-kondoo wa Mungu. Yeye alikuwa amekuwa sauti tu, kilio cha nyikani. Sasa kwa furaha alikubali kufichika na kutoonekana yeye, ili ya kwamba macho ya wote yapate kugeuzwa kuielekea Nuru ya uzima.

Wale ambao ni wakweli kwa wito wao kama wajumbe kwa ajili ya Mungu hawatatafuta heshima zao wenyewe. Kujipenda wenyewe kutakuwa kumemezwa katika kumpenda Yesu. Kwao hakuna kushindana ambako kutaharibu njia ya thamani ya injili. Watagundua kwamba kazi yao ni kuwatangazia watu, kama alivyofanya Yohana Mbatizaji, kwamba **(180)** "Tazama Mwana-kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu."

Yohana 1:29. Watamwinua Yesu, na ndani yake uanadamu utainuliwa juu. “Maana yeye aliye juu, aliyetukuka, akaaye milele; ambaye jina lake ni Mtakatifu; asema hivi; Nakaa mimi mahali palipoinuka, palipo patakatifu; tena pamoja na yeye aliye na roho iliyotubu na kunyenyekea, ili kuzifufua roho za wanyenyekevu, na kuifufua mioyo yao waliotubu." Isaya 57:15.

Nafsi ya nabii, ikiwa tupu pasipo ubinafsi, ilijazwa na nuru ya mbingunini. Aliposhuhudia utukufu wa Mwokozi, maneno yake yalikuwa yanakaribia kuendana na yale yaliyosemwa na Kristo wakati wa mahojiano yake na Nikodemo. Yohana alisema, "Yeye ajaye kutoka juu, huyo yu juu ya yote. Yeye aliye wa dunia, asili yake ni ya dunia, naye anena mambo ya duniani. Yeye ajaye kutoka mbinguni yu juu ya yote. . . . Kwa kuwa yeye aliyetumwa na Mungu huyanena maneno ya Mungu; kwa sababu hamtoi Roho kwa kipimo." Kristo naye angesema, "Siyatafuti mapenzi yangu mimi, bali mapenzi yake aliyenipeleka." Yoahana 5:30. Kwake imesemwa kwamba, "Umependa haki, umechukia maasi; Kwa hiyo Mungu, Mungu wako, amekutia mafuta, Mafuta ya shangwe kupita wenzio." Waebrania 1:9. Baba "hamtoi Roho kwa kipimo."

**(181)** Hivyo ndivyo ilivyo kwa wafuasi wa Kristo leo. Tunaweza kupokea nuru ya mbinguni ikiwa tu tuna utashi wa kubaki watupu tukiwa tumeondoa ubinafsi. Hatuwezi kutambua tabia ya Mungu, au kumpokea Yesu kwa imani, tusipokubali hali ya kila wazo kushikiliwa mateka kwa kuletwa katika utii wa Kristo. Kwa wote wafanyao haya Roho Mtakatifu hutolewa bila kipimo. Katika Kristo "unakaa utimilifu wote wa Mungu, kwa jinsi ya kimwili. Na ninyi mmetimilika katika yeye." Wakolosai 2:9, 10.

Wanafunzi wa Yohana walikuwa wamesema kwamba watu wote walikuwa wanakwenda kwa Kristo; lakini kwa muono wa wazi zaidi, Yohana alisema, "Hakuna anayeukubali ushuhuda wake;" kwa hiyo wachache ndio walikuwa tayari kumkubali kama Mwokozi wa kutoa watu dhambini. Lakini "yeye aliyeukubali ushuhuda wake ametia muhuri ya kwamba Mungu ni kweli." Yohana 3:33. "Amwaminiye Mwana yuna uzima wa milele." Hakuna sababu ya malumbano kwamba labda ubatizo wa Kristo au wa Yohana ulitakasa kutokana na dhambi. Ni neema ya Mungu inayotoa uzima kwa roho. Mbali na Kristo, ubatizo, kama ilivyo kaida nyingine yoyote ya kidini, ni desturi isiyo na thamani. "Yeye asiyemwamini Mwana hataona uzima."

Habari za mafanikio ya kazi ya Kristo, ambayo Mbatizaji alikuwa amepokea kwa furaha, zilipelekwa pia kwa mamlaka za Yerusalemu. Makuhani na marabi walikuwa wamepata wivu juu ya ushawishi wa Yohana kadiri walivyoona watu wanaacha masinagogi na kwenda jangwani; lakini sasa hapa alikuwepo Yeye ambaye alikuwa hata na nguvu zaidi kuvuta kwake makutano makubwa. Wale viongozi wa Israeli hawakuwa tayari kuungana na Yohana kwa kusema kwamba, "Yeye hana budi kuzidi, bali mimi kupungua." Waliinuka kwa nia moja kuikomesha kazi ile iliyokuwa ikiondoa watu kwao kuwapeleka mbali nao.

Yesu alijua kwamba wasingebakiza hata jitihada moja katika kutengeneza mgawanyiko kati ya wanafunzi wake na wale wa Yohana. Alijua kwamba dhoruba ilikuwa inakusanyika ili kumkumba mmoja wa manabii wakuu mno waliopata kutolewa kwa ulimwengu. Akitaka kuepusha matukio yote ambayo yangesababisha mfarakano au mgawanyiko, Yesu aliachana na kazi yake, na akaondoka kwenda Galilaya. Hata sisi pia tunatakiwa kukwepa yale yote yanayoweza kuleta upinzani na uelewa usio sahihi, huku tukidumu kuwa waaminifu kwa ukweli. Maana kila yanapoibuka haya, matokeo yake ni upotevu wa roho. Wakati wowote mazingira yanayotishia kusababisha mgawanyiko yanapotokea, tunapaswa kufuata mfano wa Yesu na wa Yohana Mbatizaji.

Yohana alikuwa ameitwa ili kuongoza akiwa kama mwanamatengenezo. Kwa sababu ya hili, wanafunzi wake walikuwa katika hatari ya kukaza macho yao kwake, wakidhani kwamba mafanikio ya kazi ile yalitegemea utendaji wake, na wakikosa kuona uhalisia kwamba alikuwa ni nyezo tu ambayo Mungu alikuwa ameitumia kufanya kazi. Lakini kazi ya Yohana haikutosha kuweka msingi wa **(182)** kanisa la Kikristo. Wakati alipokuwa amekamilisha kazi yake, kazi nyingine ilikuwa ifanyike, ambayo isingekamilishwa na ushuhuda wake. Wanafunzi wake hawakuelewa hili. Wakati walipomwona Kristo akiingilia kuifanya kazi, waliona wivu na kutoridhishwa.

Hatari zile zile bado zipo. Mungu humwita mtu kufanya kazi fulani; na pindi anapokuwa ameifanya mpaka mahali anapostahili kuifikisha, Mungu huleta watu wengine, kuipeleka mbele zaidi. Lakini, kama walivyokuwa wanafunzi wa Yohana, wengi hufikiri kwamba mafanikio ya kazi yanategemea mtenda-kazi yule wa kwanza. Mawazo yanakazwa kwa mwanadamu badala ya Mungu, wivu unakuja, na kazi ya Mungu inapata vikwazo. Yule anayetukuzwa hivyo kupita kiasi anajaribiwa kutegemea uwezo wake mwenyewe. Hatambui utegemezi wake

kwa Mungu. Watu wanafundishwa kumwangalia mtu kama kiongozi, na kwa njia hiyo wanaanguka katika makosa, nao wanaongozwa kwenda mbali na Mungu.

Kazi ya Mungu isipewe sura wala alama ya mwanadamu. Katika vipindi tofauti Mungu ataleta mawakala tofauti, ambao kupitia kwao kusudi lake linaweza kukamilishwa kwa mafanikio. Wana furaha wale ambao wanakubali nafsi zao zishushwe, wakisema pamoja na Yohana Mbatizaji kwamba, "Yeye hana budi kuzidi, bali mimi kupungua."

## Sura ya 19

# Penye Kisima cha Yakobo

[Msingi wa somo hili uko katika Yohana 4:1-42.]

Akiwa njiani kwenda Galilaya Yesu alipita katikati ya Samaria. Ilikuwa mchana yapata saa sita wakati alipofika katika Bonde la Shekemu lililokuwa zuri. Mwanzoni mwa bonde hili kulikuwa na kisima cha Yakobo. Akiwa amechoshwa na safari, alikaa chini ili apumzike huku wanafunzi wake wakiwa wameenda kununua chakula.

Wayahudi na Wasamaria walikuwa mahasimu wakubwa, na waliepuka mashirikiano yoyote baina yao kwa kiasi kikubwa iwezekanavyo. Kwa mujibu wa marabi, kushirikiana na Wasamaria pindi kunapokuwa na ulazima ilikuwa halali, lakini kushirikiana nao kote katika mambo ya kijamii hakukuruhusiwa. Myahudi asingeazima kitu kutoka kwa Msamaria, wala kupata huduma ya ukarimu, hata kipande cha mkate tu au kikombe cha maji. Kwa kule kununua chakula, wanafunzi walikuwa wakifanya jambo linalokubaliana na desturi za taifa lao. Lakini hawakwenda zaidi ya hapo. Kuomba kitu kutoka kwa Wasamaria, au kutafuta kunufaika kutoka kwao, ni jambo ambalo halikuingia katika mawazo hata ya wanafunzi wa Kristo.

Yesu alipokuwa amekaa kando ya kisima, alikuwa na nja na kiu. Safari ya tangu asubuhi ilikuwa ndefu, na sasa alikuwa anapigwa na jua la mchana-kati. Kiu yake iliongezwa zaidi na mawazo ya uwepo wa maji baridi ya kuburudisha pale karibu, lakini akiwa hawezi kuyafikia; maana alikuwa hana kamba wala chombo cha kuchotea, na kisima kilikuwa na kina kirefu. Alikuwa na hali ya ubindamu, na alisubiri mtu aje achote maji.

Mwanamke wa Samaria alikuja, na akionekana kama hajali uwepo wa Yesu, alijaza maji katika mtungi wake. Wakati alipogeuka ili aondoke, Yesu alimwomba maji anywe. Hakuna mtu wa nchi za Asia Mashariki ambaye angekataa upendeleo kama huo. Katika nchi za mashariki, maji yaliitwa "zawadi ya Mungu." Kumpa maji ya kunywa msafiri mwenye kiu ilichukuliwa kama wajibu mtakatifu ambao Waarabu wa **(184)** jangwani wangeacha kwanza mambo yao mengine ili kuufanya. Chuki iliyokuwepo kati ya Wayahudi na Wasamaria ilimzuia yule mwanamke kumfanyia ukarimu ule Yesu; lakini Mwokozi alikuwa anatafuta kupata ufunguo wa kuingilia katika moyo huu, na kwa mbinu yenye upendo wa kimbingu, aliomba fadhila, si kutoa fadhila. Ile fadhila ya ukarimu ingeweza kukataliwa; lakini tumaini huamsha tumaini. Mfalme wa mbinguni aliijia nafsi hii ya mwanamke iliyotengwa mbali, akiomba huduma mikononi mwake. Yeye aliyefanya bahari, anayetawala vilindi vya maji, aliyefungua chemchemi za maji na mifereji ya nchi, alijipumzisha panapo kisima cha Yakobo kwa uchovu, na alikuwa mtegemezi wa ukarimu wa mgeni kwa zawadi ya maji ya kunywa.

Yule mwanamke aliona kwamba Yesu alikuwa Myahudi. Kwa mshangao alisahau kutekeleza ombi la Yesu, badala yake akajaribu kutafuta sababu ya ombi lile. Alisema, "Imekuwaje wewe Myahudi kutaka maji kwangu, nami ni mwanamke Msamaria?"

Yesu alijibu, "Kama ungaliijua karama ya Mungu, naye ni nani akuambiaye, Nipe maji ninywe, ungalimwomba yeye, naye angalikupa maji yaliyo hai." Unashangaa kwa mimi kukuomba kitu kidogo sana kama maji ambayo yanatoka katika kisima kilicho chini ya miguu yetu. Ungaliniomba mimi, Ningalikupa kunywa maji ya uzima wa milele.

Yule mwanamke hakuwa ameelewa maneno ya Kristo, lakini aliguswa na umuhimu wa maneno yale. Hali yake nyepesi ya mzaha ilianza kubadilika. Akidhani kwamba Yesu amenena kuhusu kisima kile kilichokuwa mbele yao, alisema, "Bwana, huna kitu cha kutekea, na kisima ni kirefu; basi umeyapata wapi hayo maji yaliyo hai? Je! Wewe u mkubwa kuliko baba yetu, Yakobo, aliyetupa kisima hiki, naye mwenyewe akanywa maji yake, na wanawe pia, na wanyama wake?" Yule mwanamke alikuwa anaona mbele yake huyu msafiri tu mwenye kiu, akiwa amechoshwa na safari na amejawa na mavumbi. Katika mawazo yake alimlinganisha na mzee Yakobo aliyeheshimika. Alikuwa na hisia, ambazo ni za kawaida kabisa, kwamba hakuna kisima ambacho kingeweza kuwa sawa na kile kilichotolewa na mababa. Alikuwa anaangalia nyuma kwa mababa, na akitazamia ujio wa Masihi siku za usoni, wakati lile tumaini la mababa, yaani Masihi mwenyewe, lilikuwa karibu naye, wala hakulifahamu. Ni roho ngapi zenye kiu ambazo leo ziko karibu na kisima cha uzima, lakini bado zinaangalia mbali zikitafuta visima vya maji ya uzima! "Usiseme moyoni mwako, Ni nani atakayepanda kwenda mbinguni?

(Yaani, ni kumleta Kristo chini), au, Ni nani atakayeshuka kwenda kuzimuni? (Yaani, ni kumleta Kristo juu, kutoka kwa wafu.) . . . Lile neno li karibu nawe, katika kinywa chako, na katika moyo wako: . . . ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka." Warumi 10:6-9.

**(187)** Yesu hakujibu haraka swali la kumhusu Yeye mwenyewe, bali alisema kwa dhati kwamba, "Kila anywaye maji haya ataona kiu tena; walakini yeyote atakayekunywa maji yale nitakayompa mimi hataona kiu milele; bali yale maji nitakayompa yatakuwa ndani yake chemchemi ya maji, yakibubujikia uzima wa milele."

Yeye anayetafuta kupoza kiu yake katika visima vya ulimwengu huu atakunywa na kuona kiu tena. Kila mahali wanadamu hawatosheki. Wanatafuta kitu cha kuleta mahitaji ya moyo. Ni Mmoja tu anayeweza kukidhi mahitaji hayo. Hitaji la ulimwengu, Tumaini la mataifa yote, ni Kristo. Neema ya kimbingu ambayo inaweza kutolewa na Yeye tu, ni maji ya uzima, yasafishayo, yaburudishayo, na kuutia moyo nguvu.

Maana aliyotoa Yesu si kwamba maji ya kunywa mara moja tu yangemtosha yeye aliyeyapokea. Yeye anayeonja upendo wa Kristo ataendelea kutamani zaidi; lakini hatafuti kitu kingine. Havutiwi na utajiri, ukuu, wala anasa za dunia. Kilio cha moyo wake wakati wote ni kusema, Zaidi kutoka kwako Bwana. Na Yeye anayeufunulia moyo yaliyo mahitaji ya moyo huo yuko tayari akisubiri ili kutosheleza njaa na kiu. Kila rasilimali-mtu na utegemezi vitaanguka. Matanki ya maji yatabaki matupu, madimbwi yanakauka; lakini Mkombozi wetu ni kisima kisichoishiwa. Tunaweza kunywa, na kunywa, na kudumu kupata burudiko. Yeye ambaye anakuwa na Kristo ndani yake ana chemchemi ya baraka ndani yake mwenyewe, - "chemchemi ya maji yakibubujikia uzima wa milele." Kutoka katika chanzo hiki anaweza kuchota nguvu na neema inayotosheleza mahitaji yake yote.

Wakati Yesu alipoongea juu ya maji ya uzima, yule mwanamke alimwangalia kwa mshangao. Ameamsha hamu yake, na aliamsha hitaji la zawadi aliyokuwa amesema. Alielewa kwamba Yesu hakuongelea maji ya kisima cha Yakobo; maana ameyazoea maji ya kisima hiki, akiyanywa, na kuona kiu tena. Akasema, "Bwana, unipe maji hayo, nisione kiu, wala nisije hapa kuteka."

Sasa Yesu aligeuza maongezi. Kabla nafsi hii haijapokea zawadi aliyotaka kuipatia, lazima ifanywe kutambua dhambi yake na kumtambua Mwokozi wake. "Yesu akamwambia, Nenda kamwite mumeo, uje naye hapa." Mwanamke akajibu, "Sina mume." Hapo alitaka azuie maswali yote ambayo yangeelekezwa katika jambo hilo. Lakini Yesu akaendelea, "Umesema vema, Sina mume; kwa maana umekuwa na waume watano, naye uliye naye sasa siye mume wako; hapo umesema kweli.

Yule msikilizaji wake alitetemeka. Mkono wa siri ulikuwa unafunua kurasa za historia ya maisha yake, ukionyesha kile ambacho yule mwanamke alitamani kifichwe **(188)** milele. Ni nani huyu ambaye aliweza kusoma siri za maisha yake? Mawazo ya umilele yalimjia yule mwanamke, ya kuhusu Hukumu ijayo, wakati ambapo yote yanayofichwa yatawekwa wazi. Katika hali hiyo, dhamiri iliamshwa.

Mwanamke hakuweza kukana kitu; lakini alijaribu kukwepa kutaja-taja habari hiyo isiyopendeza. Kwa heshima kubwa, alisema, "Bwana, naona ya kuwa u nabii!" halafu, akitaraji kunyamazisha hali ya kusadikishwa, aligeukia katika mambo ya kidini yanayotofautiana. Ikiwa huyu alikuwa nabii, kwa kweli angempa mafundisho kuhusu mambo haya ambayo yalikuwa yameleta mashaka.

Kwa uvumilivu Yesu alimruhusu apeleke maongezi huko alikotaka. Alisubiri ili baadaye apate fursa nyingine ya kuuleta ukweli mahali pake moyoni. Mwanamke akasema, "Baba zetu waliabudu katika mlima huu, nanyi husema ya kwamba huko Yerusalemu ni mahali patupasapo kuabudia." Machoni pao tu kulikuwa na Mlima wa Gerizimu. Hekalu la hapo lilikuwa limeharibiwa, madhabahu tu ndiyo yaliyokuwa yamesalia. Suala la mahali pa kuabudia lilikuwa ni habari ya kubishaniwa kati ya Wayahudi na Wasamaria. Baadhi ya wazee wa zamani sana wa Wasamaria wakati fulani walikuwa Waisraeli; lakini kwa sababu ya dhambi zao, Mungu aliwaacha washindwe na taifa la waabudu sanamu. Kwa vizazi vingi walichanganyika na waabudu sanamu, watu ambao dini yao ilichafua ile ya Wasamaria taratibu. Ni kweli walidai kwamba sanamu zao zilitumika tu kuwakumbusha kuhusu Mungu aliye hai, Mtawala wa malimwengu; hata hivyo watu waliongozwa kuziheshimu sanamu zao za kuchongwa.

Wakati hekalu la Yerusalemu lilipojengwa tena mnamo siku za Ezra, Wasamaria walitamani kujiunga na Wayahudi katika kulijenga. Walikataliwa nafasi hiyo, na uhasama mchungu uliibuka baina ya jamii hizo mbili. Wasamaria walijenga hekalu la kiushindani kwenye Mlima Gerizimu. Hapa waliabudu kulingana na taratibu za torati ya Musa, ingawa hawakuacha kabisa sanamu. Lakini majanga yaliwakumba, hekalu lao liliharibiwa na adui zao, na walionekana kama wako chini ya laana; lakini bado waling'ang'ania mapokeo yao na namna zao za ibada. Hawakutambua hekalu la Yerusalemu kama nyumba ya Mungu, wala kukiri kwamba dini ya Wayahudi ilikuwa bora kuliko yao.

Katika kumjibu mwanamke yule, Yesu alisema, "Unisadiki, saa inakuja ambayo hamtamwabudu Baba katika mlima huu, wala kule Yerusalemu. Ninyi mnaabudu msichokijua; sisi tunaabudu tukijuacho; kwa kuwa wokovu watoka kwa Wayahudi." Yesu alikuwa ameonyesha kwamba hakutawaliwa na nadharia iliyokuwa inawapinga Wasamaria. Sasa alitaka kuvunja **(189)** nadharia ya Wasamaria dhidi ya Wayahudi. Wakati akionyesha kwamba imani ya Wasamaria ilikuwa imechafuliwa na ibada ya sanamu, alimwambia kwamba ukweli mkuu wa ukombozi umekabidhiwa kwa Wayahudi, na ya kwamba kutoka miongoni mwao Masihi angetokea. Katika Maandiko Matakatifu walikuwa na mwonekano wa tabia ya Mungu na kanuni za utawala wake. Yesu alijiweka miongoni mwa tabaka la Wayahudi kama watu ambao Mungu amewapa kumjua.

Alitamani kuinua mawazo ya msikilizaji wake juu kuliko mambo ya taratibu na maadhimisho, na mambo ya kushindana. Akamwambia, "Saa inakuja, nayo sasa ipo, ambayo waabuduo halisi watamwabudu Baba katika roho na kweli. Kwa maana Baba awatafuta watu kama hao wamwabudu. Mungu ni Roho, nao wamwabuduo yeye imewapasa kumwabudu katika roho na kweli."

Hapa unasemwa ukweli ule ule ambao Yesu alikuwa ameusema kwa Nikodemo aliposema, "Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuona ufalme wa Mungu." Yohana 3:3. Watu hawaletwi katika ushirika na mbingu kwa kutafuta mlima mtakatifu au hekalu takatifu. Dini isifungwe katika maadhimisho na taratibu zinazoonekana kwa nje. Dini itokayo kwa Mungu ni dini ile tu itakayoongoza kwenda kwa Mungu. Ili kumtumikia Mungu kwa usahihi, lazima tuzaliwe kwa Roho wa mbinguni. Hili litasafisha moyo na kuifanya upya akili, likitupatia uwezo mpya wa kumfahamu na kumpenda Mungu. Litatupatia utii wa matakwa yake yote kwa hiari yetu. Hii ndiyo ibada ya kweli. Ndilo tunda la utendaji wa Roho Mtakatifu. Kila ombi la dhati linaadikwa na Roho, na ombi kama hilo linakubalika kwa Mungu. Mahali popote ambapo nafsi inafika ikimtafuta Mungu, utendaji wa Roho unadhihirishwa hapo, na Mungu anajifunua kwa nafsi hiyo. Mungu anawatafuta waabudu wa jinsi hiyo. Anasubiri kuwapokea, ili kuwafanya wana na binti zake.

Kadiri mwanamke yule alivyoongea na Yesu, aliguswa na maneno yale ya Yesu. Kamwe alikuwa hajapata mguso kama ule kwa maneno ya makuhani wa jamii yake au wa Wayahudi. Kwa kuwa maisha yake ya nyuma yalikuwa yamewekwa wazi mbele zake, alipata hisia ya kuona mapungufu yake makubwa. Aligundua kiu yake ya moyoni, ambayo isingetoshelezwa na maji ya kisima cha pale Sikari. Hakuna jambo ambalo alikuwa amepata kukutana nalo likamwamsha katika uhitaji mkubwa kama huu. Yesu alikuwa amemshawishi kwamba alikuwa amesoma moyo wa maisha yake; lakini yule mwanamke alikuwa amefikiri kwamba Yesu alikuwa rafiki yake, alikuwa anampenda na kumhurumia. Huku usafi wa uwepo wake ukiihukumu dhambi yake, Yesu hakuwa amesema neno lolote la kumhukumu wazi wazi, bali alikuwa amweleza kuhusu neema yake, ambayo ingeweza kuufanya **(190)** moyo kuwa mpya. Mwanamke alianza kusadikishwa kuhusu tabia ya Yesu. Swali liliibuka mawazoni mwake, Je, huyu hawezi kuwa yule Masihi atarajiwaye kwa muda mrefu? Akamwambia, "Najua ya kuwa yuaja Masihi, (aitwaye Kristo); naye atakapokuja, yeye atatufunulia mambo yote." Yesu akajibu, "Mimi ninayesema nawe, ndiye."

Mara mwanamke yule aliposikia maneno yale, imani ikachanua moyoni mwake. Alikubali tangazo lile la ajabu lililotoka katika midomo ya Mwalimu wa kimbingu.

Mwanamke huyu alikuwa katika hali ya kutambua na kufurahi. Alikuwa tayari kupokea ufunuo wa hali ya juu; maana alipendezwa na Maandiko, na Roho Mtakatifu alikuwa amemwandaa kupokea nuru zaidi. Alikuwa amechunguza ahadi zilizo katika Agano la Kale, "Bwana, Mungu wako, atakuondokeshea nabii miongoni mwa ndugu zako kama nilivyo mimi; msikilizeni yeye." Kumbukumbu 18:15. Alitamani kuelewa unabii huu. Nuru ilikuwa inapita-pita mawazoni mwake tayari. Maji ya uzima, maisha ya kiroho ambayo Kristo hutoa kwa kila

nafsi yenye kiu, yalikuwa yameanza kutiririka moyoni mwake. Roho wa Bwana alikuwa anafanya kazi pamoja naye.

Kauli ya wazi iliyotolewa na Kristo kwa mwanamke huyu isingekuwa imesemwa kwa Wayahudi waliojihesabia haki. Kristo alijibana sana alipoongea nao. Kile ambacho kilikuwa kimefichwa kutolewa kwa Wayahudi, na ambacho wanafunzi waliungana baadaye kukihifadhi kama siri, kilifunuliwa kwa mwanamke huyu. Yesu aliona kwamba angeweza kutumia uelewa wake kuwaleta wengine kuja kushiriki neema yake.

Wanafunzi waliporudi kutoka huko walikotumwa, walishangaa kumkuta Bwana wao akiongea na mwanamke yule. Hakuwa amekunywa yale maji aliyoomba, na hakuacha kula chakula kilicholetwa na wanafunzi wake. Wakati mwanamke yule alipokuwa ameondoka, wanafunzi wake walimsihi ale chakula. Walimwona akiwa kimya, akiwa na mawazo, kama vile katika tafakari ya kina. Uso wake ulikuwa unaangaza nuru, na waliogopa kuingilia mawasiliano yale kati yake na mbingu. Lakini walijua kwamba amedhoofu na amechoka, na walifikiri kwamba wanao wajibu wa kumkumbusha kuhusu mahitaji ya kimwili. Yesu alitambua upendo wao, na akasema, "Mimi ninacho chakula msichokijua ninyi."

Wanafunzi walishangaa kwamba ni nani huenda amemletea chakula; lakini alieleza, "Chakula changu ndicho hiki, niyatende mapenzi yake aliyenipeleka, nikaimalize kazi yake." Yohana 4:34. Wakati maneno yake yalipokuwa yameamsha dhamiri ya mwanamke yule, Yesu alifurahi. Aliona yule mwanamke akinywa yale maji **(191)** ya uzima, na akatosheleza njaa na kiu yake. Kukamilisha utume ambao kwa huo aliacha mbingu ili kuja kuukamilisha kulimtia nguvu Yesu kwa ajili ya kazi yake, na kulimwinua juu zaidi ya mahitaji ya kibinadamu. Kuihudumia nafsi inayoumia kwa njaa na kiu ya kutaka ukweli lilikuwa kwake jambo la kutia moyo zaidi kuliko kula au kunywa. Kwake ilikuwa ni faraja, burudani. Ukarimu ulikuwa ni uzima wa nafsi yake.

Mkombozi wetu huona kiu ya kuwatambua watu. Anaona njaa ya huruma na upendo kwa ajili ya wale ambao amewanunua kwa damu yake. Anatamani kwa hamu isiyoelezeka kwamba waje kwake ili wapate uzima. Kama vile mama anavyoangalia akitarajia tabasamu ya mtoto wake mdogo ya kumtambua kama mama, ambayo inaonyesha kuanza kwa uelewa, ndivyo Kristo anavyoangalia akitarajia mtu kuonyesha upendo, ambao unaonyesha kwamba uzima wa kiroho umeanza ndani yake.

Yule mwanamke alikuwa amejazwa na furaha kadiri alivyosikiliza maneno ya Kristo. Ufunuo wa ajabu ulikuwa kama unampa nguvu za ziada. Akiacha mtungi wake wa maji, alirudi mjini, kuwapelekea wengine ujumbe. Yesu alijua ni kwa nini yule mwanamke alikuwa ameenda. Kwa kuacha mtungi wake alitamka pasipo kukosea matokeo ya maneno yale yale ya Yesu. Ilikuwa ni hamu ya moyo wake kupata maji ya uzima; na alisahau hata lengo la safari yake ya kisimani, alisahau ile kiu ya Mwokozi, ambayo alikuwa amekusudia kuifanyia kazi. Akiwa na moyo unaotiririka furaha, aliharakisha njiani, kuwajulisha wengine nuru ya thamani aliyokuwa amepokea.

Mwanamke aliwaambia watu wa mji ule, "Njoni, mtazame mtu aliyeniambia mambo yote niliyoyatenda. Je! Haimkini huyu kuwa ndiye Kristo?" Maneno yake yaligusa mioyo yao. Uso wake ulikuwa na mwonekano mpya, badiliko la mwonekano wake wote. Walikuwa na hamu ya kumwona Yesu. "Basi wakatoka mjini, wakamwendea."

Kadiri Yesu alivyoendelea kukaa pembeni pa kisima, aliyatazama mashamba ya nafaka yaliyokuwa yametanda mbele yake, yakiwa ya kijani na yakiguswa na mwanga wa jua. Akiwaelekeza wanafunzi wake kwa mandhari ile, aliitumia kama kielelezo akisema: "Hamsemi ninyi, Bado miezi minne, ndipo yaja mavuno? Tazama, mimi nawaambieni, Inueni macho yenu myatazame mashamba, ya kuwa yamekwisha kuwa meupe, tayari kwa mavuno." Na aliposema, aliangalia makundi ya watu waliokuwa wanakuja kisimani. Ilikuwa bado miezi minne ndipo ufike muda wa kuvuna nafaka, lakini kumbe hapa kulikuwa na mavuno ambayo yako tayari kwa ajili ya mvunaji.

Akasema, "Avunaye hupokea mshahara, na kukusanya matunda kwa uzima wa milele, ili yeye apandaye na yeye avunaye wapate kufurahi **(192)** pamoja. Kwa maana hapo neno hilo huwa kweli, Mmoja hupanda akavuna mwingine." Hapa Yesu anaelekeza kwa huduma takatifu ambayo Mungu anaitaka kwa wale walioipokea injili. Wanapaswa wawe mawakala wake walio hai. Anahitaji huduma yao binafsi. Na ikiwa tunapanda au kuvuna, tunafanya kazi kwa ajili ya Mungu. Mmoja anatawanya mbegu; mwingine anakusanya mavuno; na wote mpandaji na mvunaji wanapokea ujira. Wanafurahia pamoja katika ujira wa kazi yao.

Yesu aliwaambia wanafunzi wake, "Mimi naliwatuma myavune yale msiyoyataabikia; wengine walitaabika, nanyi mmeingia katika taabu yao." Hapa Mwokozi alikuwa anaangalia ukusanyaji mkuu wa sikukuu ya Pentekoste. Wanafunzi walitakiwa wsilione jambo hili kama matokeo ya jitihada zao wenyewe. Walikuwa wanaingia katika kazi ya watu wengine. Daima tangu wakati wa Adamu Kristo amekuwa akiwakabidhi watumishi waliochaguliwa mbegu ya neno, ya kupandwa katika mioyo ya wanadamu. Na nguvu isiyoonekana, na uweza wake Aliye Juu, vilikuwa vimefanya kazi kimya-kimya lakini kwa nguvu kiasi cha kuzaa mavuno. Umande na mvua na nuru ya neema ya Mungu vilikuwa vimetolewa. Kristo alikuwa karibu kuimwagilia mbegu kwa damu yake. Wanafunzi walikuwa wamejaaliwa. Walikuwa wafanya kazi pamoja na Kristo. Kwa kumwagwa kwa Roho Mtakatifu siku ya Pentekoste, maelfu walikuwa waongoke katika siku moja. Haya yalikuwa matokeo ya kupanda mbegu kwa Yesu, mavuno ya kazi yake.

Katika maneno yaliyotamkwa kwa mwanamke yule pale kisimani, mbegu njema ilikuwa imepandwa, na mavuno yalipokewa kwa haraka kiasi gani! Wasamaria walikuja na kumsikiliza Yesu, kumwamini. Wakikusanyika kwake pale kisimani, walimwuliza maswali, na wakapokea kwa hamu ufafanuzi wake wa mambo mengi ambayo yalikuwa yamejificha kwao. Kadiri walivyosikiliza, mashaka yao yalitoweka. Walikuwa kama watu walio katika giza kuu la usiku wanaokutana na mionzi ya nuru ya ghafla hadi wakauona mchana. Lakini hawakutosheka na mkutano huu mfupi. Walitamani kusikia zaidi, na kuwafanya rafiki zao nao wamsikilize huyu mwalimu wa ajabu. Walimwalika aingie katika mji wao, na kumsihi abaki pamoja nao. Alibaki pale Samaria kwa siku mbili, na wengine wengi walimwamini.

Mafarisayo walidharau urahisi wa Yesu. Walipuuza miujiza yake, na kumdai ishara ya kuonyesha kama alikuwa Mwana wa Mungu. Lakini Wasamaria hawakudai kupewa ishara yoyote, na wala Yesu hakufanya mwujiza miongoni mwao, ila tu kumfunulia yule mwanamke siri za maisha yake pale kisimani. Lakini wengi walimwamini. Wakiwa katika furaha yao mpya walimwambia yule mwanamke, **(193)** "Sasa tunaamini, wala si kwa sababu ya maneno yako tu; maana sisi tumesikia wenyewe, tena twajua ya kuwa hakika huyu ndiye Mwokozi wa ulimwengu."

Wasamaria waliamini kwamba Masihi angekuja kama Mkombozi, si kwa ajili ya Wayahudi tu, bali kwa ajili ya ulimwengu. Roho Mtakatifu kupitia Musa alikuwa amemtabiri Masihi kama nabii atakayetumwa na Mungu. Kupitia Yakobo ilikuwa imesemwa kwamba watu watakusanywa kwake Masihi; na kupitia kwa Ibrahimu, ilisemwa kwamba katika Masihi mataifa yote watabarikiwa. Kutokana na maandiko haya watu wa Samaria waliweka imani yao kwa Masihi. Hali ya kwamba Wayahudi walikuwa wametafsiri vibaya unabii wa baada ya huo, wakiuhusisha utukufu wa kuja kwa Kristo mara ya pili katika kule kuja kwake mara ya kwanza, ilikuwa imesababisha Wasamaria kukataa maandiko matakatifu yote isipokuwa yale yaliyotolewa na Musa tu. Lakini wakati Yesu alipofagilia mbali hizi tafsiri potofu, wengi walikubali unabii wa baadaye na maneno ya Kristo mwenyewe kuhusu ufalme wa Mungu.

Yesu alikuwa ameanza kubomoa ukuta unaotenganisha Wayahudi na Mataifa, na kuhubiri wokovu kwa ulimwengu. Ingawa alikuwa Myahudi, alichangamana kabisa na Wasamaria, akionyesha kwamba desturi za Kifarisayo za taifa lake si kitu. Pamoja na imani yao potofu alipokea ukarimu kutoka kwa watu hawa waliodharauliwa. Alilala chini ya paa za nyumba zao, alikula pamoja nao katika meza zao, - akishiriki nao kula chakula kilichoandaliwa na kuhudumiwa kwa mikono yao, - alifundisha katika mitaa yao, na aliwatendea kwa wema na huruma ya hali ya juu.

Katika hekalu la Yerusalemu ukuta mfupi ulitenganisha ukumbi wa nje na sehemu nyingine za jengo takatifu. Kwenye ukuta huu kulikuwa na maandishi yaliyo katika lugha tofauti-tofauti, yakisema kwamba mtu asiye Myahudi haruhusiwi kuvuka mpaka huu. Ikiwa mtu wa Mataifa yeyote angethubutu kuingia ndani ya ukuta huu angekuwa amenajisi hekalu, na angelipa fidia ya maisha yake. Lakini Yesu, aliye mwanzilishi wa hekalu na huduma zake, aliwavuta Mataifa kwake kwa kifungo cha huruma ya kibinadamu, huku neema yake ya kimbingu ikiwaletea wokovu ambao ulikataliwa na Wayahudi.

Kukaa kwa Yesu Samaria kulipangwa kuwa mbaraka kwa wanafunzi wake, ambao walikuwa bado wamezingwa na itikadi za Kiyahudi. Walidhani kwamba uaminifu kwa taifa lao uliwataka wadumishe uadui dhidi ya Wasamaria. Walishangazwa na mwenendo ule wa Yesu. Wasingeweza kukataa kufuata mfano wake, na katika siku zile walizokuwa Samaria, utiifu wao kwake ulidhibiti ile imani yao potofu; lakini mioyoni mwao hawakuwa

na mwafaka. Walikuwa na kasi ndogo sana ya kujifunza kwamba lazima dharau **(194)** na chuki yao viondoshwe na mahali pake pawe na wema na huruma. Lakini baada ya kupaa kwa Bwana, masomo yake yaliwarudia yakiwa na maana mpya. Baada ya kumwagiwa Roho Mtakatifu, walikumbuka mtazamo, maneno, heshima na wema wa Mwokozi kwa wageni hawa waliodharauliwa. Wakati Petro alipoenda kuhubiri huko Samaria, alileta mtazamo huo huo katika kazi yake. Wakati Yohana alipoitwa kwenda Efeso na Simirna, alikumbuka uzoefu ule wa kule Shekemu, na alijawa na shukrani kwa Mwalimu wa kimbingu, ambaye, akiona kwa mbali ugumu ambao wangekutana nao, alikuwa amewasaidia kwa kuwapa kielelezo chake.

Mwokozi bado anaendeleza kazi kama ile ile ya wakati alipompatia maji ya uzima mwanamke wa Samaria. Wale wanaojiita wanafunzi wake wanaweza kudharau na kuwakataa waliotengwa; lakini hakuna hali ya kuzaliwa au ya utaifa, hakuna hali ya maisha, inayoweza kugeuzia mbali upendo wake kwa watoto wa wanadamu. Kwa kila nafsi, hata iwe na dhambi jinsi gani, Yesu anasema, Ungeniomba, ningekupa maji ya uzima.

Mwaliko wa injili usifanywe kuwa finyu, na kuwasilishwa kwa wachache tu waliochaguliwa, ambao, tunadhani kwamba watatufaidi ikiwa wataipokea injili hiyo. Ujumbe utolewe kwa wote. Mahali popote ambapo mioyo iko wazi kupokea ukweli, Kristo yu tayari kuwafundisha. Anamfunua Baba kwao, na kuwafunulia ibada inayokubalika kwake Yeye asomaye moyo. Kwa hilo hatumii mafundisho kwa mifano. Kama ilivyokuwa kwa mwanamke pale kisimani, nao pia atawaambia, "Mimi ninayesema nawe ndiye."

Wakati Yesu alipokaa chini ili kupumzika pale penye kisima cha Yakobo, alikuwa amekuja kutoka Uyahudi, ambako kazi yake ilikuwa imezaa matunda kidogo sana. Alikuwa amekataliwa na makuhani na walimu, na hata watu waliojiona kuwa wanafunzi wake walikuwa wameshindwa kuelewa tabia yake ya kimbingu. Alikuwa amedhoofika na kuchoka; lakini hakupuuza fursa ya kuongea na mwanamke mmoja, ingawa mwanamke huyo alikuwa mgeni, aliyetengwa na Israeli, na aliyeishi katika dhambi ya wazi.

Mwokozi hakusubiri mpaka watu wakusanyike pamoja. Mara nyingi alianza masomo yake kwa wachache tu waliokusanyika kwake, lakini wapita-njia mmoja baada ya mwingine walisimama kumsikiliza, mpaka wakawa mkutano mkubwa uliosikiliza kwa mshangao na butwaa maneno ya Mungu kupitia Mwalimu huyu aliyetumwa na mbingu. Mtenda-kazi kwa ajili ya Kristo asijisikie kwamba hawezi kuongea na watu wachache kwa uthabiti kama ambavyo angeongea na mkusanyiko mkubwa zaidi. Kunaweza kuwa na mtu mmoja tu wa kusikiliza ujumbe; lakini ni nani anayeweza kujua ushawishi wa ujumbe ule unafika mbali kiasi gani? Lilionekana kama jambo dogo, hata kwa wanafunzi wake, kwa kitendo cha Yesu kutumia **(195)** muda wake kwa mwanamke wa Samaria. Lakini alifikiri kwa dhati na ufuatiliaji zaidi kuliko alivyofanya kwa wafalme, wajumbe wa baraza, na wakuu wa makuhani. Masomo aliyotoa kwa mwanamke yule yamerudiwarudiwa hata katika maeneo ya dunia yasiyofikika kwa urahisi.

Muda mfupi baada ya kumpata Mwokozi mwanamke Msamaria aliwaleta wengine kwake. Alijipambanua kuwa na uwezo wa umishonari kuliko hata wanafunzi wenyewe wa Yesu. Wanafunzi wale hawakuona chochote pale Samaria kilichoonyesha kuvutia kazi ya utume. Mawazo yao yalikuwa yamekazwa kwa kazi kuu ambayo ingefanyika siku za usoni. Hawakuona kwamba katika maeneo ya pale pale tu panapowazunguka kulikuwa na mavuno ya kukusanywa. Lakini kupitia mwanamke ambaye walimdharau, wakazi wa mji wote waliletwa kumsikia Mwokozi. Mara tu aliipeleka nuru kwa watu wa nchi yake.

Mwanamke huyu anawakilisha utendaji wa imani katika Kristo. Kila mwanafunzi wa kweli anazaliwa ili kuingia katika ufalme wa Mungu kama mmishonari. Yeye anayekunywa kutoka katika maji ya uzima anakuwa chemchemi ya uzima. Anayepokea huwa mtoaji. Neema ya Kristo katika nafsi ya mtu ni kama chemchemi jangwani, inayotoa maji ili kuwaburudisha watu wote, na kuwafanya walio karibu kuangamia kuwa na hamu ya kunywa katika maji ya uzima.

## Sura ya 20

# "Msipoona Ishara na Maajabu"

[Msingi wa somo hili uko katika Yohana 4:43-54]

Watu wa Galilaya waliorudi kutoka katika Pasaka walileta habari za matendo ya ajabu ya Yesu. Hukumu iliyopitishwa na wakuu kule Yerusalemu kwa sababu ya matendo yake ilimfanya Yesu ashike njia kwenda Galilaya. Watu wengi walikuwa wamelalamikia matumizi mabaya ya hekalu na tamaa ya makuhani. Walitumaini kwamba Mtu huyu, aliyekuwa amesababisha wakuu kukimbia huenda ndiye Mkombozi anayetarajiwa. Sasa zimekuja habari zilizokuwa kama zinathibitisha matarajio yao hayo. Taarifa zilitolewa kwamba nabii huyu alikuwa amejitangaza kwamba ni Masihi.

Lakini watu wa Nazareti hawakumwamini. Kwa sababu hii, Yesu hakutembelea Nazareti wakati alipokuwa anaenda Kana. Mwokozi aliwaambia wanafunzi wake kwamba nabii haheshimiwi katika nchi yake. Wanadamu wanapima tabia kulingana na kile ambacho wanafahamu. Watu walio na mawazo finyu ya kiulimwengu walimtambua Kristo kwa kutazama kuzaliwa kwake katika hali duni, mavazi yake ya hali ya chini, na kazi zake za jasho za kila siku. Hawakuweza kutambua usafi wa roho ile ambayo haikuwa na doa la dhambi.

Habari kwamba Kristo alikuwa amerudi Kana zilisambaa kote Galilaya, zikileta matumaini kwa wenye shida na wanaoteseka. Kule Kapernaumu habari hizo zilivuta usikivu wa Myahudi aliyekuwa diwani katika **(197)** utumishi wa mfalme. Kijana wa mtumshi huyo alikuwa anaumwa ugonjwa ambao ulionekana kama usiotibika. Matabibu walikuwa wameshindwa na kumwacha afe; lakini pindi baba yule aliposikia habari za Yesu, aliamua kutafuta msaada kwake. Mtoto alikuwa katika hali mbaya sana, na, iliogopesha kwamba baba yule asingerudi na kumkuta bado yuko hai; lakini mtumishi yule wa mfalme aliona kwamba lazima alifikishe kwa Yesu jambo hilo yeye mwenyewe. Alitumaini kwamba huenda ombi linalowasilishwa na baba lingeweza kuamsha huruma ya Tabibu Mkuu.

Alipofika Kana alikuta umati mkubwa ukiwa umemzunguka Yesu. Akiwa na moyo wenye dukuduku alipenya hadi mahali alipokuwa Mwokozi. Imani yake ilipungua alipomwona mtu aliyevaa nguo za kawaida, mwenye mavumbi na uchovu wa safari. Alipata mashaka ikiwa kweli Mtu huyu angefanya kile ambacho amekuja kuomba; lakini bado alipata nafasi ya kuongea na Yesu, akamwambia sababu ya ujio wake kwake, na kumsihi Mwokozi aongozane naye kwenda nyumbani kwake. Lakini tayari huzuni **(198)** ilikuwa inajulikana kwa Yesu. Diwani yule alipokuwa hajaondoka nyumbani kwake, Mwokozi alikuwa ameshaona shida yake.

Lakini alijua pia kwamba baba yule alikuwa, mawazoni mwake, ameweka masharti kuhusu imani yake kwa Yesu. Ikiwa ombi lake lisingefanyiwa kazi, asingempokea Yesu kama Masihi. Wakati diwani yule akisubiri kwa uchungu wa wasiwasi, Yesu alisema, "Msipoona ishara na maajabu hamtaamini kabisa?"

Licha ya ushahidi wote kwamba Yesu alikuwa ni Kristo, yule aliyeleta ombi alikuwa ameazimia kuifanya imani yake iwe ya sharti la ombi lake kufanyiwa kazi. Mwokozi alilinganisha huku kutoamini ambako kuna maswali na imani ile rahisi ya Wasamaria, ambao hawakutaka mwujiza wala ishara. Neno lake, ushahidi uliopo siku zote wa uungu wake, lilikuwa na nguvu ya kushawishi ambayo iliifikia mioyo yao. Yesu aliumia kwa sababu watu wake mwenyewe, ambao walikabidhiwa Maneno Matakatifu, wangeshindwa kuisikia sauti ya Mungu akiongea nao katika Mwana wake.

Lakini bado diwani yule alikuwa na kiasi fulani cha imani; maana alikuwa amekuja kuomba kile ambacho kwake kilionekana kuwa baraka ya thamani kubwa zaidi kuliko zote. Yesu alikuwa na zawadi ya kutoa iliyo kubwa zaidi. Alitaka, si kuponya tu mtoto yule, bali pia kumfanya diwani na nyumba yake kuwa washiriki wa mibaraka ya wokovu, na kuwasha nuru pale Kapernaumu, ambapo baada ya muda mfupi pangekuwa sehemu ya kazi yake. Lakini lazima diwani huyu afanikishe hitaji lake kabla ya kutamani neema ya Yesu. Mtu huyu mkuu aliwakilisha watu wengi wa taifa lake. Walivutiwa na Yesu kwa sababu za manufaa binafsi. Walitarajia kupata faida fulani maalum kupitia uwezo wake, na waliweka imani yao katika kupewa mema ya ulimwengu; lakini hawakuwa wanajua kuhusu ugonjwa wao wa kiroho, na hawakuona hitaji la neema ya mbinguni.

Kama kumlika kwa nuru, maneno ya Mwokozi kwa diwani yaliuweka wazi moyo wake. Aliona kwamba misukumo yake ya kumtafuta Yesu ilikuwa ya ubinafsi. Imani yake isiyo na msimamo ilionekana kwake kama tabia yake kweli kweli. Katika shida aliyokuwa nayo alitambua kwamba mashaka yake yangeweza kugharimu maisha ya mwanawe. Alijua kwamba alikuwa mbele yake Yeye aliyeweza kusoma mawazo, na ambaye kwake mambo yote yalikuwa yanawezekana. Katika maumivu ya kuomba alisema, "Bwana, ushuke asijakufa mtoto wangu." Imani yake ilimshikilia Kristo kama alivyofanya Yakobo, wakati, alipokuwa akipambana mieleka na Malaika, alipolia akisema, "Sikuachi, usiponibariki." Mwanzo 32:26.

Alishinda kama ilivyokuwa kwa Yakobo. Yesu hawezi kuondokana na nafsi inayomng'ang'ania, ikiomba kwa ajili ya hitaji kubwa. Alisema, "Enenda; mwanao yu hai." Yule diwani aliondoka kwa Yesu kwa amani **(199)** na furaha kwa kiasi ambacho hakupata kujua kabla. Si tu kwamba alijua mwana wake alikuwa amepona, bali pia kwa ujasiri mkubwa alimwamini Kristo kama Mkombozi.

Katika saa ile ile waangalizi waliokuwa kando ya yule mtoto aliye karibu kufa kule nyumbani Kapernaumu waliona badiliko la ghafla na la ajabu. Uvuli wa mauti uliondolewa katika uso wa mgonjwa. Kuhisi homa kulitoweka na mahali pake kukawa na mwonekano wa afya njema. Macho maangavu yanayoonyesha uwezo mzuri wa akili, na nguvu, vilirejea kwa mgonjwa. Hakuna dalili za ugonjwa zilizoendelea kuonekana kwa mtoto yule. Mwili wake uliokuwa wa moto ulikuwa umelainika na kuwa na unyevunyevu, na alizama katika usingizi. Homa ilimwacha katika hali ya joto la mchana. Watu wa nyumba ile walishangazwa, na wakawa na furaha kuu.

Kana haikuwa mbali kutoka Kapernaumu kiasi kwamba afisa yule angefika nyumbani jioni ile ile baada ya kuongea na Yesu; lakini hakuharakisha katika safari yake ya kwenda nyumbani. Asubuhi ya siku iliyofuata ndipo alipofika Kapernaumu. Huku kulikuwa kurudi nyumbani kwa namna gani! Wakati alipoenda kumtafuta Yesu, moyo wake ulikuwa mzito na wenye huzuni. Nuru ya jua ilionekana kama yenye ukatili kwake, nyimbo za ndege zilikuwa kama dhihaka kwake. Hisia zake za sasa ni tofauti kiasi gani! Viumbe vya asili vyote viko katika mtazamo mpya. Anaona kwa macho mapya. Kadiri anavyosafiri katika ukimya wa asubuhi na mapema, viumbe vya asili vyote vinakuwa kama vile vinamsifu Mungu pamoja naye. Wakati bado yuko umbali fulani kutoka katika nyumba ya makazi yake, watumishi wanakuja kumkaribisha, wakiwa na hamu ya kutuliza furaha iliyopitiliza ambayo wana hakika kwamba angeipata ghafla. Haonekani kushangazwa na habari wanazomletea, lakini akiwa na shauku ambayo hawakuweza kujua, anauliza kuhusu saa ya wakati ambapo mtoto alipata nafuu. Wakamjibu, "Jana, saa saba, homa ilimwacha." Katika muda ule ule imani ya baba huyo ilipopewa uhakika kwamba, "Mwanao yu hai," upendo wa kimbingu ulimgusa mtoto aliyekuwa kifoni. **(200)** Baba anaharakisha kwenda kumsalimu mwanawe. Anamkumbatia kifuani kama mtu ambaye amerejea kutoka kifoni, na anamshukuru Mungu tena na tena kwa uponyaji huu wa ajabu.

Diwani yule alitamani kujua zaidi kuhusu Kristo. Pindi aliposikia mafundisho ya Kristo baadaye, yeye na nyumba yake yote wakawa wanafunzi. Shida yao ilitakaswa hadi kuwa uongofu wa nyumba yote. Habari za mwujiza ule zilisambaa; na mle mle Kapernaumu, mahali ambako mingi ya miujiza yake mikubwa ilifanyika, njia ilitayarishwa kwa ajili ya huduma ya Yesu.

Yeye aliyembariki diwani kule Kapernaumu anatamani kutubariki sisi pia. Lakini kama ilivyokuwa kwa yule baba mwenye shida, mara nyingi tunaelekea kumtafuta Yesu kwa hamu ya kupata vitu vya ulimwengu; na tunaweka imani yetu katika upendo wake tunapojua kwamba atatupatia kile tunachoomba. Mwokozi anatamani kutupatia mbaraka mkuu zaidi ya kile tunachoomba; na anakawiza jibu la kile tunachoomba ili ya kwamba atuonyeshe uovu wa mioyo yetu, na uhitaji wetu wa kina wa neema yake. Anatamani tuukane unafsi unaotusukuma kumtafuta. Tukikiri kwamba hatuna msaada na tuko katika uhitaji mchungu, ndipo tutakapojitumainisha kabisa katika upendo wake.

Yule diwani alitaka kuona utimizwaji wa ombi lake kabla ya kuamini; lakini alipaswa kukubali neno la Yesu kwamba ombi lake lilisikika na baraka kutolewa. Hili ni somo ambalo tunapaswa kujifunza. Hatupaswi kuamini kwa sababu tunaona au kuhisi kwamba Mungu anatusikia. Tunapaswa tuamini katika ahadi zake. Tunapokuja kwake kwa imani, kila ombi linaingia katika moyo wa Mungu. Wakati tunapokuwa tumeomba mbaraka wake, tunatakiwa tuamini kwamba tunaupokea, na kumshukuru kwamba tumeupata. Halafu tunatakiwa tuendelee na majukumu yetu, tukiwa na hakika kwamba mbaraka ule utadhihirishwa wakati ule tunapouhitaji zaidi. Wakati tutakapokuwa tumejifunza kufanya hivi, tutajua kwamba maombi yetu hujibiwa. Mungu atatufanyia "mambo ya

ajabu mno kuliko yote tuyaombayo," "kwa kadiri ya utajiri wa utukufu wake," na "kadiri ya utendaji wa nguvu za uweza wake." Wefeso 3:20, 16; 1:19.

**Sura ya 21**

# Bethzatha na Sanhedrin

[Sura hii imejengwa katika Yohana 5.]

"Na huko Yerusalemu penye mlango wa kondoo pana birika, iitwayo kwa Kiebrania Bethzatha, nayo ina matao matano. Ndani ya hayo jamii kubwa ya wagonjwa walikuwa wamelala, vipofu, viwete, nao waliopooza, wakingoja maji yachemke."

Katika nyakati fulani maji ya birika hili yalikuwa yakitibuliwa, na ilikuwa inaamika kote kwamba hali hii ilikuwa inasababishwa na nguvu isiyo ya kibinadamu, na ya kwamba yeyote aliyekuwa wa kwanza kurukia birikani baada ya maji kuvurugwa au kusukwasukwa alipona ugonjwa wowote aliokuwa nao. Mamia ya wagonjwa walitembelea mahali pale; lakini umati mkubwa ulikuwepo baada hasa ya maji kuvurugwa ambapo walikimbia mbele, wakiwakanyaga wanaume, wanawake, na watoto, waliokuwa dhaifu zaidi kuliko wao. Wengi hawakuweza kusogea karibu na kingo za birika. Wengi waliokuwa wamefanikiwa kulifikia birika hili walifia pale kwenye kingo zake. Vibanda vilikuwa vimejengwa mahali pale, ili kwamba wagonjwa wahifadhiwe dhidi ya joto la mchana na baridi ya usiku. Walikuwepo wengi waliosubiri usiku mzima katika matao haya, wakisogea karibu katika ukingo wa birika siku baada ya siku, wakitafuta pasipo mafanikio kupona.

Yesu alikuwako Yerusalemu kwa mara nyingine. Akiwa anatembea peke yake, akiwa katika maombi na kutafakari, alikuja birikani. Alimwona mgonjwa asiye na tumaini akisubiri kuona kile walichodhania kuwa fursa pekee ya kuponywa. Alitamani kuweka kazini uwezo wa uponyaji, na kumponya kila mgonjwa. Lakini ilikuwa siku ya Sabato. Makutano walikuwa wanaenda hekaluni kwa ajili ya ibada, **(202)** na alijua kwamba kitendo kama kile cha kuponya kingeamsha hasira ya Wayahudi na kukatisha kazi yake.

Lakini Mwokozi aliona mfano mmoja wa asiye na tumaini kabisa. Alikuwa ni mtu aliyekuwa kiwete asiye na msaada kwa miaka thelathini na nane. Kwa kiasi kikubwa, ugonjwa wake ulikuwa ni matokeo ya dhambi yake, na uliangaliwa kama hukumu kutoka kwa Mungu. Akiwa peke yake na asiye na rafiki, akijihisi kuwa amefungiwa mbali na neema ya Mungu, mgonjwa huyu alikuwa amepitia miaka mingi ya maumivu. Katika wakati ilipotarajiwa kwamba maji yangetibuliwa, wale waliomhurumia katika hali yake ya kukosa msaada walimbeba kumpeleka mahali penye matao. Lakini mnamo wakati muafaka wa kuingia majini hakuwa na mtu wa kumsaidia kuingia. Aliona kusukwasukwa kwa maji, lakini hakuweza kamwe kwenda mbali zaidi ya ukingo wa birika. Wengine walio na nguvu kuliko yeye walirukia majini kabla yake. Hakuweza kufanikiwa kushindana na watu waliokuwa wanagombania kwa ubinafsi. Jitihada alizoendelea kufanya ili kufikia lengo lile, na huzuni na mfadhaiko wa wakati wote, vilikuwa vinazidi kumdhoofisha na kumaliza hata nguvu aliyokuwa amesalia nayo.

Yule mgonjwa alikuwa amelala kwenye mkeka wake, na mara kwa mara akiinua kichwa chake kuchungulia birikani, wakati uso wa wema na huruma ulipomwelekea kwa maneno haya, "Wataka kuwa mzima?" na kuvuta usikivu wake. Tumaini lilikuja moyoni mwake. Alifikiri kwamba anaweza kupata msaada fulani. Lakini baada ya muda mfupi furaha yake ilitoweka. Alikumbuka jinsi alivyojaribu mara nyingi kulifikia birika, na jinsi ambavyo alikuwa na matarajio kidogo sana ya kuendelea kuwa hai mpaka aifikie awamu nyingine ya maji yale kutibuliwa. Aligeuka na kuangalia kando kwa uchovu, akisema, "Bwana, mimi sina mtu wa kunitia birikani, maji yanapotibuliwa; ila wakati ninapokuja mimi, mtu mwingine hushuka mbele yangu."

Yesu hamwulizi mgonjwa huyu kufanya tendo la kuwa na imani kwa Yesu. Anamwambia tu kwamba, "Simama, jitwike godoro lako, uende." Imani ya mtu yule inalishikilia **(203)** lile neno. Kila neva na msuli vilipata uzima upya, na uwezo wa afya ulikuja katika miguu yake iliyolemaa. Pasipo kuhoji aliweka utashi wake katika kutii maelekezo ya Kristo, na misuli yake yote iliitika kuufuata utashi ule. Alijitegemeza kwenye miguu yake, akajikuta yuko imara.

Yesu hakuwa amempatia uhakika wa msaada wa uungu. Yule mtu angeweza kuacha kwa mashaka, na angepoteza nafasi ya kupona. Lakini aliamini neno la Kristo, na kwa kuliweka katika vitendo alipata nguvu.

Kwa imani kama ile ile tunaweza kupata uponyaji wa kiroho. Kwa sababu ya dhambi tunatengwa na maisha ya Mungu. Nafsi zetu zimelemazwa. Sisi wenyewe hatuwezi tena kuishi maisha matakatifu kama ambavyo mtu yule mlemavu hakuwa na uwezo wa kutembea. Wapo wengi wanaotambua kwamba hawajiwezei lolote, na ambao wanatamani maisha yale ya kiroho yatakayowaleta katika kupatana na Mungu; wanajitahidi kuyapata pasipo mafanikio. Katika hali ya kukosa tumaini wanalia wakisema, "Ole wangu maskini mimi! Ni nani atakayeniokoa na mwili huu wa mauti?" Warumi 7:24. Hebu watu hawa wasio na tumaini na wanaohangaika wainue macho juu mara moja. Mwokozi anasihi kwa damu yake iliyowanunua, akisema kwa huruma isiyosemekana, "Wataka kuwa mzima?" Anakusihi usimame katika afya na amani. Usisubiri mpaka utakapojisikia kama umepona. Amini neno lake, na itatendeka. Weka utashi wako upande wa Kristo. Hiari kumtumikia, na kwa kufanyia kazi neno lake utapata nguvu. Hata kama kuna mambo gani ya uovu, mateso makubwa ya mwili na roho, Kristo anaweza na anatamani kuokoa. Ataweka uzima katika nafsi ile ambayo ni mojawapo ya “wafu kwa sababu ya makosa na dhambi.” Waefeso 2:1. Atamweka huru mateka aliyeshikiliwa na udhaifu na kukosa furaha na minyororo ya dhambi.

Mwenye kupooza aliyeponywa aliinama ili kuchukua godoro lake, ambalo lilikuwa ni kirago na blanketi tu, mara alipoinuka tena kwa hisia ya furaha, aliangalia huku za huku kumtafuta Mponyaji wake; Yesu hakuonekana bali alikuwa amejichanganya katika umati wa watu. Yule mtu alihofu kwamba hatamfahamu tena ikiwa atamwona. Alipokuwa akitembea haraka kwa nguvu na hatua za kupona, alimsifu Mungu na kufurahia nguvu zake mpya alizopata, alikutana na Mafarisayo kadhaa, na akawaambia haraka kuhusu kupona kwake. Alishangazwa kwa jinsi ambavyo hawakufurahishwa na kisa kile walichokuwa wanasikiliza.

Wakiwa wameinamisha nyuso zao waliingilia na kumkatiza, wakimwuliza kwamba ni kwa nini anabeba godoro lake siku ya Sabato. Walimkumbusha kwa msisitizo kwamba haikuruhusiwa kubeba mizigo katika siku ya Bwana. Katika furaha yake mtu yule alikuwa amesahau kwamba ilikuwa siku ya Sabato; lakini hakuhisi hatia maana alitii amri yake Yeye aliyekuwa na nguvu namna ile kutoka kwa Mungu. Alijibu **(204)** kwa kujiamini, "Yeye aliyenifanya kuwa mzima ndiye aliyeniambia, Jitwike godoro lako, uende." Walimwuliza kuhusu huyo aliyefanya hivyo, lakini hakuweza kueleza. Wakuu hawa walijua kwamba yupo Mmoja tu aliyekuwa ameonyesha uwezo wa kutenda miujiza; lakini walitaka wapate ushahidi wa moja kwa moja kwamba alikuwa ni Yesu, ili wamwone kwamba ana hatia ya kuvunja Sabato. Katika hukumu yao ni kwamba alikuwa amekiuka si tu kwa kuponya mtu siku ya Sabato, bali pia kwa kuacha kuheshimu kitakatifu kwa kumtaka mtu yule kubeba godoro lake.

Wayahudi walikuwa wamepotosha sheria kiasi cha kuifanya kuwa kongwa la utumwa. Matakwa yao yasiyo maana yalikuwa yamekuwa kama mithali katika mataifa mengine. Hasa hasa Sabato ilikuwa imewekewa namna za makatazo yasiyo na maana. Kwao haikuwa siku ya furaha, takatifu ya Bwana, na ya heshima. Waandishi na Mafarisayo walikuwa wameyafanya maadhimisho ya Sabato kuwa mzigo usiovumilika. Myahudi hakuruhusiwa kuwasha moto wala kuwasha mshumaa. Kama matokeo yake watu waliwategemea Wamataifa kwa ajili ya huduma nyingi ambazo wasingeweza kuzifanya wao wanyewe kwa kuwa taratibu zilikataza. Hawakuona kwamba kuajiri watu wengine kufanya vitendo vilivyodhaniwa kuwa dhambi ilikuwa ni kutenda dhambi sawasawa kama vile walikuwa wamevifanya wao wenyewe. Walifikiri kwamba wokovu ulikuwa kwa ajili ya Wayahudi tu, na kwamba hali ya watu wengine, ambao tayari hawana matumaini, isingefanywa kuwa mbaya zaidi. Lakini Mungu hakutoa amri ambayo haiwezi kutiiwa na watu wote. Sheria zake haziruhusu kuwa na vizuizi visivyo na sababu au vya ubinafsi.

Kule hekaluni Yesu alikutana na mtu yule aliyeponywa. Alikuwa amekuja kutoa sadaka ya dhambi kwa neema kubwa aliyokuwa amepata. Alipomkuta miongoni mwa waabudu wengine, Yesu alijiruhusu kujulikana kwa mtu yule, na kusema, "Angalia, umekuwa mzima; usitende dhambi tena, lisije likakupata jambo lililo baya zaidi."

Yule mtu aliyeponywa alikuwa na furaha sana kukutana na Mponyaji wake. Pasipokujua uadui wao kwa Yesu, aliwaambia Mafarisayo waliokuwa wamemwuliza, kwamba huyu ndiye aliyemfanyia uponyaji. "Kwa sababu hiyo Wayahudi wakamwudhi Yesu, kwa kuwa alitenda hayo siku ya sabato."

Yesu aliletwa mbele ya Sanhedrin kujibu mashtaka ya kuvunja Sabato. Ikiwa Wayahudi wagekuwa taifa huru wakati huo, shtaka kama hilo lingekidhi lengo lao kwa kumwua. Warumi walizuia lengo lao hili. Wayahudi hawakuwa na mamlaka ya kutekeleza adhabu kubwa, na mashtaka ambayo wangeyaleta dhidi yake **(205)**

yasingekuwa na uzito katika mahakama ya Warumi. Kulikuwa na malengo mengine pia ambayo walitamani kufikia. Licha ya jitihada zao za kupinga kazi yake, Kristo alikuwa anaongezeka kuwa na ushawishi kwa watu kuliko hao, hata Yerusalemu. Makutano ambao hawakupendezwa na upinzani wa marabi walivutiwa na mafundisho yake. Waliweza kuelewa maneno yake, na mioyo yao ilitiwa joto na kufarijiwa. Aliongea kuhusu Mungu, akimwonyesha kuwa si kama hakimu aadhibuye, bali kama baba mwenye upendo, na alifunua sura ya Mungu kama ilivyoakisiwa ndani yake. Maneno yake yalikuwa kama mafuta kwenye roho iliyojeruhiwa. Kwa maneno yake na matendo yake ya neema alikuwa akivunja nguvu za ukandamizaji za mapokeo na amri za wanadamu, na akiwakilisha upendo wa Mungu katika ukamilifu wake.

Katika mojawapo ya unabii wa kale kabisa wa Kristo imeandikwa, "Fimbo ya enzi haitaondoka katika Yuda, Wala mfanya sheria kati ya miguu yake, Hata atakapokuja Yeye, mwenye milki, Ambaye mataifa watamtii." Mwanzo 49:10. Watu walikuwa wanakusanyika kwa Kristo. Mioyo ya huruma ya makutano ilipokea masomo ya upendo na ukarimu kuliko maadhimisho magumu yaliyotakiwa na makuhani. Ikiwa makuhani na marabi wasingekuwa wameingilia, mafundisho yake yangeleta matengenezo ambayo hayajawahi kushuhudiwa ulimwenguni. Lakini ili kuendeleza mamlaka yao, viongozi hawa waliazimia kuvunja ushawishi wa Yesu. Mashtaka yake mbele ya Sanhedrin, na upinzani wa wazi wa mafundisho yake, vingesaidia kufanikisha hili; maana watu walikuwa bado na heshima kwa viongozi wao wa dini. Yeyote aliyethubutu kupinga matakwa ya marabi, au kuthubutu kupunguza uzito wa mizigo ile waliyokuwa wameweka juu ya watu, alichukuliwa kwamba ana hatia, si tu kwa kukufuru, bali pia kwa usaliti. Kwa sababu ya mambo hayo marabi walitarajia kuibua tuhuma dhidi ya Yesu. Walionyesha kwamba Yeye anajaribu kupindua desturi zilizowekwa, na hivyo kusababisha mgawanyiko katika jamii, na kutaka kuleta mazingira ya kutawaliwa na Warumi kwa nguvu katika nyanja zote.

Lakini chanzo cha mipango ile ambayo marabi walikuwa wanaifanyia kazi kwa hila kilikuwa ni baraza jingine tofauti na Sanhedrin. Baada ya Shetani kushindwa kumshinda Yesu kule jangwani, aliunganisha majeshi yake ili kumpinga Yesu katika huduma yake, na ikiwezekana kuikwamisha kabisa. Aliazimia kutekeleza kwa mkakati mwingine kile ambacho hakuweza kufanikisha kwa jitihada zake za moja kwa moja. Baada tu ya kushindwa pambano la jangwani aliienda na malaika walio upande wake katika baraza kuimarisha mipango yake kwa kupofusha akili za Wayahudi, ili kwamba **(206)** wasimtambue Mkombozi wao. Alipanga kufanya kazi kwa kutumia mawakala wake walio wanadamu katika ulimwengu wa kidini, kwa njia ya kuwajaza na wao ule uadui alio nao dhidi ya mkuu wa ile kweli. Alipanga kuwafanya wamkatae Kristo na kuyafanya maisha yake kuwa machungu mno iwezekanavyo, akitarajia kumkatisha tamaa katika kazi yake. Na viongozi katika Israeli wakawa vitendea-kazi vya Shetani katika kupigana vita dhidi ya Mwokozi.

Yesu alikuwa amekuja "kuitukuza sheria, na kuiadhimisha." Asingeweza kupunguza nafasi yake, bali kuiinua. Maandiko yanasema, "Hatazimia, wala hatakata tamaa, hata atakapoweka hukumu duniani." Isaya 42:21, 4. Alikuwa amekuja kuiweka huru Sabato mbali na masharti yaliyokuwa yameifanya kuwa laana badala ya baraka.

Kwa sababu hii alikuwa amechagua Sabato moja ili katika hiyo afanye tendo la uponyaji kule Bethzatha. Angeweza kumponya mgonjwa yule katika siku nyingine yoyote katika juma; au angeweza kumponya bila kumtaka abebe godoro aondoke nalo. Lakini hayo yasingempatia fursa aliyohitaji. Kusudi lenye hekima lilikuwemo katika kila tendo la maisha ya Yesu duniani. Kila alilofanya lilikuwa na umuhimu kwa lenyewe na kwa fundisho lililomo. Miongoni mwa wagonjwa waliokuwa pale birikani alichagua mwenye tatizo baya kuliko wote ili afanye kwake tendo la nguvu ya uponyaji, na kumwagiza mtu yule abebe godoro lake na kupita katika mji ili kuutangaza mwujiza mkubwa uliofanyika kwake. Jambo hili lingeibua swali kwa watu kwamba ni jambo lipi ambalo ni halali kufanywa siku ya Sabato, na lingemfungulia Yeye njia ya kukataa vizuizi vya Wayahudi kuhusu siku ya Bwana, na kumwezesha kutangaza kukataa mapokeo yao.

Yesu alitamka kwamba kazi ya kumponya mgonjwa ilikuwa inapatana na sheria ya Sabato. Ilikuwa inapatana na kazi ya malaika za Mungu, ambao wanashuka na kupanda daima kati ya mbingu na dunia wakiwahudumia wanadamu wanaoteseka. Yesu alisema, "Baba yangu anatenda kazi hata sasa, nami ninatenda kazi." Siku zote ni za Mungu, ambamo mipango yake kwa wanadamu inafanywa. Ikiwa tafsiri ya Wayahudi ya sheria ingekuwa sahihi, basi Yehova angekuwa amefanya makosa, kwa ile kazi yake ya kuwezesha na kutegemeza kila kiumbe hai tangu alipouweka msingi wa dunia; hapo ndipo Yeye aliyeitamka kazi yake kuwa njema, na aliyeanzisha Sabato

kuadhimisha ukamilishaji wa kazi hiyo, atalazimika kukoma kufanya kazi yake, na kusitisha mzunguko usiokoma wa utendaji-kazi katika malimwengu yote.

Je, Mungu asitishe jua kutenda kazi yake siku ya Sabato, akatishe miale kuipasha dunia joto na kustawisha mimea? Je, mifumo ya malimwengu isimame na kutulia katika siku takatifu? Je, **(207)** aamuru vijito viache kunywesha mashamba na misitu, na ayatake mawimbi ya bahari yatulize msukumo na mtiririko wake usiokoma? Je, lazima ngano na nafaka zikome kukua, na kishada kilichokomaa cha mazao kiache kuchanua? Je, lazima miti na maua yasiotеshe matawi wala kuchanua siku ya Sabato?

Katika hali kama hiyo, wanadamu wangekosa matunda ya dunia, na kukosa mibaraka inayofanya maisha kuvutia. Lazima mambo ya asili yaendelee katika njia yake. Mungu asingeweza kuzuia mkono wake, la sivyo mwanadamu angezimia na kufa. Hata mwanadamu pia anayo kazi ya kufanya katika siku hiyo. Lazima mambo muhimu ya maisha yashughulikiwe, lazima wagonjwa watunzwe, lazima mahitaji ya wahitaji yatolewe. Yeye anayepuuza kutuliza wanaoteseka siku ya Sabato hatahesabiwa kwamba hana hatia. Siku ya Mungu ya kupumzika ilifanywa kwa ajili ya mwanadamu, na matendo ya huruma yanapatana na kusudi la siku hiyo kwa ukamilifu. Mungu hapendi viumbe vyake viteseke hata kwa saa moja ya maumivu ambayo yangeweza kupozwa siku ya Sabato au siku nyingine yoyote.

Majukumu kwa ajili ya Mungu ni makubwa zaidi siku ya Sabato kuliko siku nyingine za juma. Watu wake huacha ajira zao za kawaida, na kutumia muda wao kumtafakari Mungu na kuabudu. Wanaomba mibaraka zaidi siku ya Sabato kuliko wakati wa siku nyinginezo. Wanaomba mwitikio wa Mungu kwao kwa namna ya pekee zaidi. Kwa namna ya pekee zaidi wanatamani mibaraka aliyowachagulia. Mungu hasubiri Sabato ipite ndipo awape watu mambo haya wanayoomba. Kazi ya mbingu haikomi kamwe, na wanadamu yawapasa wasipumzike na kuacha kutenda mema. Sabato haikusudiwi kuwa muda usiotumika. Sheria inakataza kufanya kazi zisizo za kidini katika siku ya Bwana ya kupumzika; lazima kazi za kutafuta mapato zikome; hakuna kazi ya kutafuta raha za kiulimwengu na za kutafuta faida zinazoruhusiwa katika siku hiyo; bali kama vile Mungu alivyokoma kufanya kazi yake ya kuumba, akapumzika siku ya Sabato na kuibariki, ndivyo mwanadamu anavyopaswa kuacha kazi zake za maisha ya kila siku, na kutumia saa hizi takatifu kwa ajili ya pumziko la afya, kuabudu, na kufanya matendo matakatifu. Kazi ya Kristo katika kumponya mgonjwa yule ilikuwa inakubaliana na sheria. Iliitukuza Sabato.

Yesu alidai haki sawa na Mungu katika kufanya kazi yenye utakatifu, na yenye sifa, sawa na ile anayofanya Mungu kule mbinguni. Lakini Mafarisayo walikuwa wamechukizwa sana. Si kwamba alikuwa amevunja sheria tu, kwa mujibu wa ufahamu wao, bali kwa kumwita Mungu "Baba yake" alikuwa amejitaja kuwa sawa na Mungu. Yohana 5:18.

Taifa lote la Wayahudi walimwita Mungu Baba yao, kwa hiyo wasingechukizwa hivyo Kristo anapojionyesha kuwa katika uhusiano na Mungu kama vile walivyokuwa. Lakini walimtuhumu **(208)** kwa kukufuru, kuonyesha kwamba walimwelewa kwa kudai dai hilo lililo bayana.

Wapinzani hawa wa Kristo hawakuwa na hoja za kubishana na ukweli ambao Yesu aliufikisha mahali pake katika dhamiri zao. Wangerejea katika desturi na mila zao tu, na hizi zilionekana dhaifu sana zikilinganishwa na hoja za Yesu zilizotoka katika neno la Mungu na mizunguko isiyokoma ya maumbile ya asili. Ikiwa marabi wangehisi hamu yoyote ya kuipokea nuru, wangeshawishika kwamba Yesu alisema ukweli. Lakini walikwepesha pointi alizotoa kuhusu Sabato, na walitafuta kuibua hasira dhidi yake kwa sababu alidai kuwa sawa na Mungu. Ghadhabu za wakuu wale hazikujua mipaka. Ikiwa wasingeogopa watu, makuhani na marabi wangemwua Yesu pale pale. Lakini mvuto wa watu kwake ulikuwa na nguvu sana. Ndani ya Yesu wengi waliona rafiki aliyekuwa ameponya na kufariji huzuni zao, na walihalalisha kitendo chake cha kumponya mgonjwa kule Bethzatha. Kwa hiyo wale viongozi walilazimika kuzuia chuki zao.

Yesu alipinga tuhuma ya kukufuru. Alisema kwamba, mamlaka yangu ya kufanya kazi ambayo mnanishtakia ni hii ya kwamba, Mimi ni Mwana wa Mungu, mmoja naye kwa hali, dhamira, na kusudi. Katika kazi zake zote za uumbaji na uhuishaji, ninashiriki pamoja naye. "Mwana hawezi kutenda neno mwenyewe ila lile ambalo amwona Baba analitenda." Makuhani na marabi walikuwa wakimchukia Mwana wa Mungu kwa kufanya kazi alizotumwa kuzifanya ulimwenguni. Kwa dhambi zao walikuwa wamejitenga na Mungu, na kwa majivuno yao walienenda

wakiwa mbali naye. Walijiona kujitosheleza katika mambo yote, na hawakuona hitaji la matendo yao kuongozwa na hekima ya juu zaidi kuliko ya kwao. Lakini Mwana wa Mungu alikuwa amejisalimisha katika mapenzi ya Baba, na alitegemea nguvu zake Baba. Kwa hiyo Kristo alijiondoa kabisa katika kutegemea nafsi yake kiasi kwamba hakuna mipango aliyofanya kwa ajili yake mwenyewe. Alikubali mipango ya Mungu kwa ajili yake, na siku kwa siku Baba alifunua mipango yake. Vivyo hivyo nasi tunapaswa kumtegemea Mungu, ili kwamba maisha yetu yawe ni utendaji-kazi wa mapenzi yake.

Wakati Musa alipotakiwa kujenga patakatifu kama makao ya Mungu, alielekezwa kufanya mambo yote kulingana na mfano alioonyeshwa mlimani. Musa alikuwa na bidii ya kufanya kazi ya Mungu; watu wenye vipaji na ustadi mkubwa kuliko wote walikuwa tayari kufanya yale ambayo angewaambia. Lakini hakupaswa kutengeneza njuga, makomamanga, shada, ukingo, pazia, au chombo chochote cha patakatifu, isipokuwa kulingana na mfano ule alioonyeshwa. Mungu alimwita mlimani, akamfunulia mambo ya mbinguni. Mungu alimfunika kwa utukufu wake, ili ya kwamba aone **(209)** ule mfano, na kulingana nao vitu vyote vilifanywa. Kwa hiyo kwa Israeli, ambaye ndani yake alikusudia kupafanya mahali pa makazi yake, alikuwa amefunua utukufu wa tabia yake. Mfano ule ulionyeshwa kwao mlimani wakati sheria ilipotolewa kwao mlimani Sinai, na wakati Bwana alipopita mbele ya Musa na kutangaza, "Bwana, Bwana, Mungu mwingi wa huruma, mwenye fadhili, si mwepesi wa hasira, mwingi wa rehema na kweli; mwenye kuwaonea huruma watu elfu elfu, mwenye kusamehe uovu na makosa na dhambi." Kutoka 34:6, 7.

Waisraeli walikuwa wamechagua njia yao wenyewe. Hawakuwa wamejenga kulingana na mfano ule; lakini Kristo, aliye hekalu la kweli la makazi ya Mungu, alidhihirisha kila chembe ya maisha yake ya duniani kuwa katika mpango wa Mungu. Alisema hivi, "Kuyafanya mapenzi yako, Ee Mungu wangu, ndiyo furaha yangu; Naam, sheria yako imo moyoni mwangu." Zaburi 40:8. Hivyo ndivyo tabia yetu inavyopaswa kujengwa "kuwa maskani ya Mungu katika Roho." Waefeso 2:22. Na yatupasa kuvifanya "vitu vyote kwa mfano ule," kama kwake Yeye ambaye "aliteswa kwa ajili yetu, akatuachia kielelezo, mfuate nyayo zake." Waebrania 8:5; 1 Petro 2:21.

Maneno ya Kristo yanafundisha kwamba tunapaswa tujione kuwa tumefungamanishwa na Baba yetu wa mbinguni kwa namna isiyotenganishika. Katika cheo chochote, utegemezi wetu uko kwa Mungu, ambaye ameshikilia hatima zetu zote mikononi mwake. Ametuchagua katika kazi zetu, ametujalia uwezo na nyenzo za kufanyia kazi. Kwa kadiri tunavyosalimisha nia zetu kwa Mungu, na kuzitumainia nguvu zake na hekima yake, tutaongozwa katika njia zilizo salama, ili kutekeleza sehemu yetu tuliyopangiwa katika ule mpango wake mkuu. Lakini yeye anayetegemea hekima na nguvu zake mwenyewe yuko anajitenga mbali kutoka kwa Mungu. Badala ya kufanya kazi katika umoja na Kristo, anatimiza kusudi la adui wa Mungu na wanadamu.

Mwokozi aliendelea kusema: "Kwa maana yote ayatendayo yeye (Baba), ndiyo ayatendayo Mwana vile vile. . . . Maana kama Baba awafufuavyo wafu na kuwahuisha, vivyo hivyo na Mwana awahuisha wale awatakao." Masadukayo walishikilia fundisho ya kwamba hakutakuwa na ufufuo wa mwili; lakini Yesu anawaambia kwamba moja ya kazi kubwa kabisa za Baba yake ni kufufua wafu, na ya kwamba hata Yeye mwenyewe ana nguvu za kufanya hivyo. "Saa inakuja, na sasa ipo, wafu watakapoisikia sauti ya Mwana wa Mungu, na wale waisikiao watakuwa hai." Mafarisayo waliamini juu ya ufufuo wa wafu. Kristo alisema kwamba hata sasa nguvu ile inayowapa wafu uhai iko miongoni mwao, na wanapaswa watazame udhihirisho wake kwao. Hii nguvu ndiyo ile ya ufufuaji inayowapa uhai watu ambao ni "wafu kwa sababu ya makosa na dhambi." Waefeso 2:1. Roho hiyo ya uzima iliyo ndani ya Yesu Kristo, "uweza wa kufufuka kwake," inawaweka watu kuwa huru "mbali **(210)** na sheria ya dhambi na mauti." Wafilipi 3:10; Warumi 8:2. Nguvu za uovu zimevunjwa, na kwa imani nafsi inahifadhiwa dhidi ya dhambi. Yeye anayefungua moyo wake kwa ajili ya Roho Mtakatifu anakuwa mshirika wa ule uweza wa nguvu ambao utafufua mwili wake kutoka kaburini.

Huyo Mnazareti mnyenyekevu anaonyesha uweza wake halisi. Anainuka juu kuliko mwanadamu, anatupilia mbali mwonekano wa dhambi na aibu, na anasimama akiwa amefunuliwa, Yeye aliye Mtukufu miongoni mwa malaika, Mwana wa Mungu, aliye Mmoja pamoja na Mwumbaji wa malimwengu yote. Wasikilizaji wake wametekewa. Hakuna mtu aliyepata kunena maneno kama yake, au kuvishwa uwezo wa kifalme kama huo. Maneno yake yako wazi, yakitangaza kazi yake kikamilifu, na wajibu wa ulimwengu. "Tena Baba hamhukumu mtu yeyote, bali amempa Mwana hukumu yote; ili watu wote wamheshimu Mwana kama vile wanavyomheshimu Baba. Asiyemheshimu Mwana hamheshimu Baba aliyempeleka . . . . Maana kama vile Baba

alivyo na uzima nafsini mwake, vivyo hivyo alimpa na Mwana kuwa na uzima nafsini mwake. Naye akampa amri ya kufanya hukumu kwa sababu ni Mwana wa Adamu."

Makuhani na wakuu walikuwa wamejiweka kuwa waamuzi wa kuihukumu kazi ya Kristo, lakini alijitangaza kuwa Yeye ndiye hakimu wao, na hakimu wa dunia yote. Ulimwengu umekabidhiwa kwa Kristo, na kupitia kwake kila mbaraka umekuja kwa wanadamu kutoka kwa Mungu. Alikuwa Mkombozi kabla ya kufanyika mwili kama alivyokuwa baada ya hapo. Muda mfupi tu baada ya kuwepo kwa dhambi kulikuwa na Mwokozi. Amewapatia watu wote nuru, na kulingana na kipimo cha nuru iliyotolewa, kila mmoja atahukumiwa. Na Yeye ambaye ametoa nuru, Yeye ambaye ameifuata roho kwa kusihi kwa upendo, akitafuta kuiokoa kutoka dhambini na kuileta katika utakatifu, Yeye ndiye mtetezi na hakimu. Tangu pambano kuu lilipoanza mbinguni, Shetani ameendelea na kazi yake ya udanganyifu; na Kristo amekuwa anafanya kazi ya kuweka wazi mipango ya Shetani na kuvunja nguvu zake. Atakayeamua hukumu ya kila mtu ni Yeye aliyekutana uso kwa uso na mwongo huyo, na ambaye kwa vizazi vingi amekuwa akitafuta kuwanyakua mateka kutoka mitegoni mwake mwovu, Yeye atakayefanya hukumu ya kila nafsi.

Na Mungu amempa “amri ya kufanya hukumu kwa sababu ni Mwana wa Adamu." Kwa kuwa ameonja mpaka na masimbi ya shida na majaribu ya mwanadamu, na anaelewa madhaifu na dhambi za wanadamu; kwa sababu amestahimili kwa ushindi majaribu ya Shetani, na atashughulika na nafsi ambayo damu yake imemwagika ili kuiokoa, - kwa sababu hii, Mwana wa Adamu ameteuliwa ili kufanya hukumu.

Lakini kazi ya Kristo haikuwa kwa ajili ya kuhukumu, bali kwa ajili ya wokovu. "Mungu hakumtuma Mwana ulimwenguni ili auhukumu ulimwengu, bali **(211)** ulimwengu uokolewe katika yeye." Yohana 3:17. Na mbele ya Sanhedrin Yesu alisema, "Yeye alisikiaye neno langu na kumwamini yeye aliyenipeleka yuna uzima wa milele; wala haingii hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia uzimani." Yohana 5:24.

Akitaka wasikilizaji wake wasistajabu, Kristo alifungua machoni pao, katika upeo mpana zaidi, siri ya siku za usoni. Aliwaambia, "Saa yaja, ambayo watu wote waliomo makaburini wataisikia sauti yake. Nao watatoka; wale waliofanya mema kwa ufufuo wa uzima, na wale waliotenda mabaya kwa ufufuo wa hukumu." Yohana 5:28, 29.

Hili hakikisho la maisha yajayo lilikuwa lile ambalo Israeli alikuwa amesubiri kwa muda mrefu, na ambalo walikuwa wametarajia kulipokea wakati wa kuja kwa Masihi. Nuru pekee ambayo inaweza kuangazia huzuni ya kaburi ilikuwa ikiwaangazia. Lakini ubinafsi una upofu. Yesu alikuwa amekiuka mila za marabi, na hakujali mamlaka yao, nao hawakuwa tayari kuamini.

Wakati, mahali, tukio, na nguvu ya hisia iliyopotosha mkutano ule, vyote hivyo vilikusanyika pamoja na kuyafanya maneno ya Yesu mbele ya Sanhedrin kuwa na mguso zaidi. Mamlaka za kidini za ngazi ya juu kabisa katika taifa zilikuwa zinawinda maisha yake Yeye aliyejitangaza kuwa mhuishaji wa Israeli. Bwana wa Sabato alishtakiwa katika mahakama ya kidunia ili kujibu tuhuma ya kuvunja sheria ya Sabato. Wakati alipotangaza kazi yake pasipo woga, wahukumu wake walimwangalia kwa mshangao na ghadhabu; lakini maneno yake yalikuwa yasiyopingika. Hawakuweza kumtia hatiani. Aliikana haki ya makuhani na waalimu ya kumhoji Yeye, au kuingilia kazi yake. Hawakuwa na mamlaka hiyo. Madai yao yalisababishwa na majivuno na kiburi chao. Alikataa kukiri makosa ya tuhuma zao, au kuhojiwa nao mambo ya dini.

Badala ya kuomba radhi kwa kitendo walichokuwa wanamlalamikia, au kueleza sababu za kukifanya, Yesu aliwageukia wale wakuu, na mara mshtakiwa akageuka kuwa mshtaki. Aliwakemea kwa ugumu wa mioyo yao, na kutokujua kwao Maandiko. Alitamka kwamba walikuwa wamelikataa neno la Mungu, kwa kule kumkataa Yeye aliyetumwa na Mungu. Aliwaambia, "Mwayachunguza maandiko, kwa sababu mnadhani kwamba ninyi mna uzima wa milele ndani yake; na hayo ndiyo yanayonishuhudia." Yohana 5:39.

Katika kila ukurasa, iwe ni historia, sheria, au unabii, Maandiko ya Agano la Kale yanaangazia utukufu wa Mwana wa Mungu. Kwa kuwa ulianzishwa na mbingu, mfumo wote wa Kiyahudi ulikuwa ni unabii wa injili. "Manabii wote humshuhudia" Kristo. Matendo 10:43. Tangu ile ahadi iliyotolewa kwa Adamu, na kushuka kupitia **(212)** mtiririko wa wazee wa zamani na mfumo wao wa kisheria, nuru ya utukufu ya mbinguni iliweka alama za nyayo za Mkombozi. Watabiri waliiona Nyota ya Bethlehemu, Shilo ajaye, kadiri mambo ya usoni yalivyopita machoni pao katika mtiririko wa mafumbo. Katika kila kafara kifo cha Kristo kilionyeshwa. Katika kila wingu la moshi wa

uvumba uliofukizwa haki yake ilipaa. Katika kila tarumbeta ya yubile iliyopigwa jina lake liliimbwa. Katika fumbo kuu la patakatifu pa patakatifu utukufu wake ulikaa.

Wayahudi walikuwa na Maandiko mikononi mwao, na walidhani kwamba katika yale maarifa yao ya nje ya neno walikuwa na uzima wa milele. Lakini Yesu alisema, "Wala neno lake hamnalo likikaa ndani yenu." Wakishakumkataa Kristo katika neno lake, walimkataa yeye halisi katika umbo. Alisema, "Wala hamtaki kuja kwangu mpate kuwa na uzima."

Wakuu wa Wayahudi walikuwa wamejifunza mafundisho ya manabii kuhusu ufalme wa Masihi; lakini walikuwa wamefanya hili, si kwa hamu ya kweli ya kuujua ukweli, bali kwa lengo la kutafuta vigezo vya kuhalalisha tamaa zao kwa vitu vya kidunia. Wakati Kristo alipokuja katika namna inayotofautiana na matarajio yao, hawakuweza kumpokea; na kwa lengo la kuhalalisha msimamo wao, walijaribu kumwonyesha kama mwongo. Mara walipokuwa wameweka miguu yao katika njia hii, ilikuwa rahisi kwa Shetani kuimarisha upinzani wao dhidi ya Kristo. Maneno yale yale ambayo yangepokelewa kama uthibitisho wa uungu wake yalitafsiriwa dhidi yake. Kwa hiyo walibadili ukweli wa Mungu na kuufanya uongo, na kadiri Mwokozi alivyokaza kuongea nao kwa matendo yake ya huruma, ndivyo walivyodhamiria zaidi kuipinga nuru ile.

Yesu alisema, "Mimi siupokei utukufu kwa wanadamu." Hakutamani kuungwa mkono na Sanhedrin, wala kutumainia mamlaka hiyo. Hakupata heshima kutokana na idhini yao. Alikuwa amepewa heshima na mamlaka ya mbinguni. Ikiwa angetaka heshima, malaika wangekuja na kumpa heshima; Baba angekuwa pia amemthibitisha katika uungu wake. Lakini kwa ajili ya manufaa yao, kwa ajili ya taifa ambalo wao walikuwa viongozi wake, alitamani wakuu wa Wayahudi kuelewa tabia yake, na kupokea baraka ambazo alikuwa amekuja kuleta.

"Mimi nimekuja kwa jina la Baba yangu, wala ninyi hamnipokei; mwingine akija kwa jina lake mwenyewe, mtampokea huyo." Yesu alikuja kwa mamlaka ya Mungu, akiwa katika sura yake, akilitimiza neno lake, na akiutafuta utukufu wake; lakini hakupokelewa na viongozi wa Israeli; lakini pindi ambapo wengine wangetokea, wakitaja kuwa na sifa za Kristo, lakini wakisukumwa na matakwa yao wenyewe na kutafuta utukufu wao wenyewe, wangepokelewa. Ni kwa nini? Ni kwa sababu yeye anayetafuta utukufu wake mwenyewe anatafuta kukidhi hamu yake ya kujitukuza juu ya wengine. Wayahudi wangeitikia mivuto kama hiyo. **(213)** Wangempokea mwalimu wa uongo kwa kuwa angewasifu katika majivuno yao na kukubali mawazo na mapokeo waliyokuwa wakiendeleza. Lakini mafundisho ya Kristo hayakupatana na mawazo yao. Yalikuwa ya kiroho, na yalidai kuitoa nafsi kama kafara; kwa hiyo wasingeyapokea. Walikuwa hawamjui Mungu, na kwao sauti ya Mungu kupitia Kristo ilikuwa sauti ya mtu mgeni.

Je, kitu kile kile hakiko kinarudiwa leo? Je, hawako wengi, hata viongozi wa dini, ambao wanaifanya mioyo yao kuwa migumu dhidi ya Roho Mtakatifu, wakifanya isiwezake kwao kuitambua sauti ya Mungu? Hawako wanalikataa neno la Mungu, ili wapate kushika mapokeo yao?

Yesu alisema, "Kwa maana kama mngalimwamini Musa, mngeniamini mimi; kwa sababu yeye aliandika habari zangu. Lakini msipoyaamini maandiko yake, mtayaamini wapi maneno yangu?" Ni Kristo aliyekuwa ameongea na Israeli kupitia Musa. Ikiwa wangekuwa waliisikiza sauti ya kimbingu iliyosema kupitia kiongozi wao mkuu, wangeitambua katika mafundisho ya Kristo. Ikiwa wangemwamini Musa, wangemwamini Yeye ambaye Musa aliandika habari zake.

Yesu alijua kwamba makuhani na waalimu walikuwa wameazimia kuyaondoa maisha yake; lakini aliwafafanulia kwa uwazi umoja alio nao na Baba, na uhusiano wake na ulimwengu. Waliona kwamba upinzani wao kwake haukuwa na udhuru, lakini chuki ya kiuaji haikuweza kuzimwa. Hofu iliwateka kadiri walivyoshuhudia nguvu ya ushawishi iliyokuwa katika huduma yake, lakini walipinga mwito wake, na walijifungia katika giza.

Walikuwa wameshindwa kuitambua mamlaka ya Yesu au kumwondolea heshima na ushawishi wake miongoni mwa watu, wengi wao wakiwa wale waliosadikishwa na maneno yake. Wakuu wenyewe walikuwa wamejisikia kuhukumiwa kwa kina kadiri alivyosukumia hatia yao mahali pake katika dhamiri zao; lakini hili liliwafanya kuwa wachungu zaidi. Walikuwa wameazimia kuchukua uhai wake. Walituma wajumbe maeneo kote katika nchi yote kuwaonya watu dhidi ya Yesu kama mwingiliaji. Wapelelezi walitumwa kumwangalia, na kutoa taarifa ya

kile alichosema na alichotenda. Mwokozi wa Maandiko sasa alikuwa. Mwokozi wa thamani sasa alikuwa amesimama chini ya kivuli cha msalaba.

# Sura ya 22

## Kifungo na Kifo cha Yohana

[Sura hii imejengwa katika Mathayo 11:1-11; 14:1-11; Marko 6:17-28; Luka 7:19-28.]

Yohana Mbatizaji alikuwa wa kwanza kuutangaza ufalme wa Kristo, na alikuwa wa kwanza pia katika mateso. Kutoka katika hewa iliyo huru ya jangwani na kutoka kwa makutano walioyasikia maneno yake, alifungiwa katika kuta za chumba cha gereza. Alikuwa amekuwa mfungwa katika gereza la kijeshi la Herode Antipa. Sehemu kubwa ya huduma ya Yohana ilikuwa imefanyika katika eneo lililo mashariki mwa Yordani, ambalo lilikuwa chini ya utawala wa Antipa. Herode mwenyewe alikuwa amesikiliza mahubiri ya Mbatizaji. Mfalme huyu mwenye anasa alikuwa ametetemeka alipoitwa kwa ajili ya toba. "Herode alimwogopa Yohana; akimjua kuwa ni mtu wa haki, mtakatifu, . . . na alipokwisha kumsikiliza alifadhaika sana; naye alikuwa akimsikiliza kwa furaha." Yohana alishughulika na mfalme huyu kwa uaminifu, akipinga mwunganiko mwovu aliofanya na Herodia, mke wa ndugu yake. Kwa muda Herode alitaka kukwepa kwa kuvunja mnyororo wa tamaa uliomfunga; lakini Herodia alikaza zaidi kumfunga, na akatafuta kulipiza kisasi kwa Yohana kwa kumshawishi Herode amtupe gerezani.

Maisha ya Yohana yalikuwa yamekuwa maisha ya kazi, na utusitusi wa gerezani na ile hali ya kushindwa kufanya kazi vilikuwa mzigo mzito sana juu yake. Kadiri juma moja baada ya jingine yalivyopita, kukiwa hakuna badiliko, huzuni na mashaka vilimjia. Wanafunzi wake hawakumwacha. Walikuwa wanaruhusiwa kufika gerezani, na walimletea habari za kazi za Yesu, na wakamwambia jinsi watu walivyokuwa wanamjia Yesu kwa wingi. Lakini walihoji ni kwa nini, ikiwa huyu **(215)** mwalimu mpya alikuwa Masihi, hakufanya lolote kuwezesha kufunguliwa kwa Yohana. Kwa nini aruhusu mtangulizi wake mwaminifu kunyang'anywa uhuru wake na huenda hata maisha yake?

Maswali haya hayakukosa matokeo. Mashaka ambayo hayakupaswa kuibuka kamwe yaliletwa kwa Yohana. Shetani alishangilia kusikia maneno hayo ya wale wanafunzi, na kuona jinsi yalivyojeruhi nafsi ya mjumbe huyo wa Bwana. Lo, ni mara ngapi wale wanaojidhania kuwa rafiki wa mtu mwema, na ambao wanajitahidi kuonyesha ukaribu naye, wanavyokuwa hatimaye maadui zake wa hatari zaidi! Ni mara ngapi ambapo maneno yao yanadhoofisha na kuvunja moyo badala ya kuimarisha imani yake!

Kama ilivyokuwa kwa wanafunzi wa Mwokozi, Yohana Mbatizaji hakuelewa uhalisia wa ufalme wa Kristo. Alitarajia kwamba Yesu angechukua kiti cha enzi cha Daudi; na kadiri muda ulivyopita, na Kristo hakusema lolote kuhusu mamlaka ya kifalme, Yohana alikata tamaa na kutatanishwa. Alikuwa ametangaza kwa watu kwamba ili kutengeneza njia kwa ajili ya Bwana, lazima unabii wa Isaya utimizwe; lazima milima na vilima vishushwe, palipopotoka panyooshwe, na palipoparuza pasawazishwe. Alikuwa anatafuta kuona kuangushwa kwa nafasi za juu za fahari na mamlaka ya mwanadamu. Alikuwa ameelekeza kwa Masihi kama Yeye ambaye pepeto lake li mkononi mwake, naye atausafisha sana uwanda wake; na kuikusanya ngano yake ghalani, bali makapi atayateketeza kwa moto usiozimika. Kama alivyokuwa nabii Eliya, ambaye katika roho yake na nguvu zake huyu alikuwa amekuja kwa Israeli, alimtazamia Bwana kujifunua kama Mungu ajibuye kwa moto.

Katika kazi yake Yohana Mbatizaji alikuwa amesimama kama mkemeaji wa uovu, kote kwa wenye hadhi ya juu na ya chini. Alikuwa amethubutu kumkabili Mfalme Herode kwa kemeo la wazi la dhambi yake. Hakuhesabu maisha yake kama kitu cha kupenda zaidi, ili kwamba aweze kuifanya kazi aliyoamuliwa. Na sasa akiwa katika gereza la chini ya ardhi alisubiri kumwona Simba wa kabila la Yuda akiangusha kiburi cha mkandamizaji, na kuwaokoa maskini na yeye mwenyewe waliokuwa wakilia. Lakini Yesu alionekana kuridhika na mkutano wa wanafunzi waliokuwa wamemzunguka, akiponya na kufundisha watu. Alikuwa akila kwenye meza za watoza ushuru, wakati siku hadi siku kongwa la Warumi lilikuwa linaongezeka uzito juu ya Israeli, wakati Mfalme Herode na kimada wake walikuwa wanatenda watakavyo, na vilio vya maskini na wanaoteseka vikienda hadi mbinguni.

**(216)** Kwa nabii huyu wa jangwani yote haya yalionekana kuwa kama siri iliyo ng'ambo ya ufahamu wake. Kuna nyakati ambapo minong'ono ya sauti za mapepo ilisumbua sana roho yake, na kivuli cha hofu ya kutisha kikawa juu yake. Je, yawezekana kwamba Mkombozi aliyetarajiwa kwa muda mrefu alikuwa hajatokea? Kwa hiyo ni nini

maana ya ujumbe ule ambao yeye mwenyewe alisukumwa kuubeba? Katika matokeo ya kazi yake Yohana alikuwa amefadhaishwa kwa uchungu. Alikuwa ametarajia kwamba ujumbe kutoka kwa Mungu ungekuwa na matokeo kama yale ya wakati ule sheria ilipokuwa inasomwa mnamo siku za Yosia na Ezra (2 Nyakati 34; Nehemia 8, 9); kwamba kazi ya toba ya dhati na watu kumrudia Mungu ingefuata. Maisha yake yote yalikuwa yametolewa kafara kwa ajili ya mafanikio ya kazi hii. Je, imekuwa ni kazi bure?

Yohana alitaabika kuona kwamba kupitia upendo wao kwake, wanafunzi wake mwenyewe walikuwa wanaonyesha kutokuamini kuhusu Yesu. Je kazi yake kwao ilikuwa haikuwa na matunda? Je, alikosa uaminifu katika kazi yake, kwamba amekatishwa kutoka katika kazi? Ikiwa Mkombozi aliyeahidiwa amekuja, na wito wa Yohana umeonekana kuwa wa kweli, je, sasa Yesu si angepindua mamlaka ya ukandamizaji, na kumweka huru mtangulizi wake?

Lakini Mbatizaji huyu hakusalimu amri katika imani yake kwa Kristo. Kumbukumbu ya sauti iliyotoka mbinguni na hua aliyeshuka, usafi wa Yesu usio na doa, nguvu ya Roho Mtakatifu iliyokuwa juu ya Yohana wakati alipokutana na Yesu, na ushuhuda wa maandiko ya unabii, - vyote vilishuhudia kwamba Yesu wa Nazareti ndiye Yeye Aliyeahidiwa.

Yohana hakujadiliana na wenzake kuhusu mashaka na taabu zake. Aliazimia kutuma kwa Yesu ujumbe wa kuuliza. Aliutuma ujumbe huo kupitia wanafunzi wake wawili, akitumaini kwamba mazungumzo ya Yesu na hao yangethibitika katika imani yao hao, na kuleta uthibitisho kwa ndugu zao. Na alitamani neno kutoka kwa Yesu lisemwe moja kwa moja kwake.

Wanafunzi wale walikuja kwa Yesu wakiwa na ujumbe usemao, "Wewe ndiwe yule ajaye, au tumtazamie mwingine?"

Ni muda mfupi kiasi gani ulikuwa umepita tangu Yohana Mbatizaji alipomwona Yesu, akatangaza kwamba, "Tazama Mwana-kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu." "Ndiye yule ajaye nyuma yangu, ambaye mimi sistahili kuilegeza gidamu ya kiatu chake." Yohana 1:29, 27. Na sasa swali hili, "Wewe ndiwe yule ajaye?" Ilikuwa hali ya uchungu na mfadhaiko wa hali ya kibinadamu. Ikiwa Yohana, mtangulizi mwaminifu, alishindwa kuelewa vema kazi ya Kristo, ingekuwaje kwa makutano waliokuwa wakitumainia mafanikio ya ubinafsi?

Mwokozi hakujibu swali lile la wanafunzi wale wakati ule ule. Kadiri walivyosimama pale wakishangazwa na kukaa kwake kimya, wagonjwa na wanaoteseka walikuwa wanakuja kwake kuponywa. Vipofu walikuwa wanapapasa kutafuta njia ya kupenya miongoni mwa makutano ili kufika kwake; **(217)** wenye matatizo wa matabaka yote, wengine wakitembea wenyewe njiani, wengine wakiwa wamebebwa na rafiki zao, walikuwa wakija mbele za Yesu. Sauti ya Mponyaji mkuu ilipenya sikio la kiziwi. Neno, mguso wa mkono wake, vilifungua macho ya kipofu na kumruhusu kuona nuru ya mchana, vitu vya asili, nyuso za marafiki, na uso wa Mwokozi. Yesu alikemea magonjwa na kuondosha homa. Sauti yake iliyafikia masikio ya waliokuwa kifoni, nao walisimama wakiwa na nguvu na afya. Watu wenye kupooza kwa sababu ya mapepo waliitii sauti yake, na mapepo yakawaacha, nao wakamsujudia. Wakati akiponya magonjwa yao aliwafundisha watu. Wakulima maskini na watumishi, waliokataliwa na marabi kwamba ni wachafu, walimkusanyikia wakiwa wamemkaribia sana, naye aliwaambia maneno ya uzima wa milele.

Hivyo siku ilikuwa inakwisha, wanafunzi wa Yohana wakiona na kusikia yote. Hatimaye Yesu aliwaita kwake, na kuwataka waende kwa Yohana na kumwambia yote waliyoshuhudia, na kuongeza kwamba, "Naye heri mtu yeyote asiyechukizwa nami." Luka 7:23. Ushahidi wa uungu wake ulionekana katika kushughulikia mahitaji ya wanadamu waliokuwa wanateseka. Utukufu wake ulionekana katika kule kujishusha mpaka kufikia hali yetu ya chini.

Wanafunzi wale walibeba ule ujumbe, na ikatosha. Yohana alikumbuka unabii unaomhusu Masihi, "Roho ya Bwana MUNGU i juu yangu; kwa sababu Bwana amenitia mafuta niwahubiri wanyenyekevu habari njema; amenituma ili kuwaganga waliovunjika moyo, kuwatangazia mateka uhuru wao, na hao waliofungwa habari za kufunguliwa kwao. Kutangaza mwaka wa Bwana uliokubaliwa, na siku ya kisasi cha Mungu wetu; kuwafariji wote waliao." Isaya 61:1, 2. Kazi za Kristo si tu kwamba zilimtangaza kuwa Masihi, bali pia zilionyesha ni kwa namna gani ufalme wake ungeanzishwa. Ukweli ule ule uliokuwa umekuja kwa Eliya jangwani ulifunuliwa kwa

Yohana, kwamba "upepo mwingi wa nguvu ukaipasua milima, ukaivunja-vunja miamba mbele za Bwana; lakini Bwana hakuwamo katika upepo ule; na baada ya upepo, tetemeko la nchi; lakini Bwana hakuwamo katika lile tetemeko la nchi; na baada ya tetemeko la nchi kukawa na moto; lakini Bwana hakuwamo katika moto ule; na baada ya moto sauti ndogo, ya utulivu." 1 Wafalme 19:11, 12. Hivyo ndivyo ambavyo Yesu angefanya kazi yake, si kwa mvumo wa silaha na mapinduzi ya viti vya enzi na falme, bali kwa kuzungumza na mioyo ya watu kwa njia ya maisha ya huruma na kujitoa mwenyewe.

**(218)** Kanuni ya maisha ya Yohana Mbatizaji ya kujinyima ilikuwa ndiyo kanuni ya ufalme wa Masihi. Yohana alijua jinsi haya yote yalivyokuwa jambo geni kwa kanuni na matarajio ya wakuu wa Israeli. Kile ambacho kwake kilikuwa kigezo cha kutambua uungu wa Kristo kisingeonekana kama kigezo kwao. Walikuwa wakimtarajia Masihi ambaye hakuahidiwa. Yohana aliona kwamba kile ambacho kazi ya Mwokozi ingepata kutoka kwao ni chuki na malaumu. Yeye, aliye mtangulizi, alikuwa anakinywea kikombe ambacho Kristo mwenyewe hakuwa na budi kukinywea chote mpaka na masimbi yake.

Maneno yale ya Mwokozi kwamba, "Heri mtu yeyote asiyechukizwa nami," yalikuwa maneno ya kemeo la upole kwa Yohana. Wala hayakupotea. Baada ya kuelewa vema kiini cha utume wa Kristo, alijitoa kwa Mungu kwa uzima au kifo, kulingana na vile itakavyoonekana inafaa kwa ajili ya kazi ile ambayo aliiipenda.

Baada ya wajumbe wale kuondoka, Yesu alisema na watu kuhusu Yohana. Moyo wa Mwokozi ulienda katika huruma mbali mpaka kwa shahidi mwaminifu ambaye sasa amezikwa katika gereza la chini la Herode. Asingewaacha watu wahitimishe kwamba Mungu alikuwa amemwacha Yohana, au kwamba imani yake ilishindwa katika siku ya majaribu. Alisema, "Mlitoka kwenda nyikani kutazama nini? Unyasi ukitikiswa na upepo?"

Nyasi ndefu zilizokua kando ya Yordani, zikipinda katika upepo, zilikuwa zinawakilisha kwa usahihi marabi waliokuwa wamesimama ili kupinga kazi ya ubatizo. Walikuwa wakiyumba huku na huko kufuata mawazo ya wengi. Hawakuweza kujishusha ili kupokea ujumbe wenye kuchunguza moyo wa Yohana Mbatizaji, lakini kwa kuogopa watu hawakuthubutu kuipinga kazi yake wazi wazi. Lakini mjumbe huyu wa Mungu hakuwa na roho isiyo ya kishujaa. Makutano waliokuwa wamekusanyika kwa Yesu walikuwa mashuhuda wa kazi ya Yohana. Walikuwa wamesikia maneno yake ya kukemea dhambi bila woga. Yohana alikuwa amesema wazi kwa Mafarisayo wenye kujihesabia haki, Masadukayo wa kikuhani, Mfalme Herode na watu wa nyumba ya mfalme, wana wa kifalme na askari, watoza ushuru na wakulima. Hakuwa mwanzi utikisikao, ukiyumbishwa na upepo wa sifa za wanadamu na tamaa. Katika gereza alikuwa vile vile mcha Mungu na mtenda haki kama wakati ule alipokuwa akihubiri ujumbe wa Mungu jangwani. Katika uaminifu wake katika kanuni alikuwa imara ka mwamba.

Yesu aliendelea, "Lakini mlitoka kwenda kuona nini? Mtu aliyevikwa mavazi mororo? Jueni, watu wenye mavazi ya utukufu, wanaokula raha, wamo katika majumba ya kifalme." Yohana alikuwa ameitwa ili kukemea dhambi anasa za wakati wake, na mavazi yake mepesi na maisha ya kujikana **(219)** yalikuwa yakipatana na tabia ya kazi yake. Mavazi ya kitajiri na anasa za maisha haya si sehemu ya watumishi wa Mungu, bali ya wale wanaoishi "katika majumba ya kifalme," wakuu wa ulimwengu huu, ambao mamlaka na utajiri wa ulimwengu unawahusu. Yesu alikusudia kuonyesha tofauti iliyopo kati ya uvaaji wa Yohana, na ule wa makuhani na wakuu. Maafisa hawa walijivika majoho ya kitajiri na nakshi za gharama kubwa. Walipenda kuonekana, na walitaka kushtua watu, na hivyo kuvuta usikivu wa watu kwao. Walitaka kutazamwa na watu zaidi kuliko kupata usafi wa moyo ambao ungewafanya wakubalike kwa Mungu. Kwa hiyo walionyesha kwamba heshima yao haikutolewa kwa Mungu, bali kwa ufalme wa ulimwengu huu.

Yesu akasema, "Lakini, mlitoka kwenda kuona nini? Nabii? Naam, nawaambia, na aliye zaidi ya nabii. Huyo ndiye aliyeandikiwa haya,

" Tazama, namtuma mjumbe wangu Mbele ya uso wako,<br>
Atakayeitengeneza njia yako mbele yako."

"Nami nawaambia, Katika wale waliozaliwa na wanawake hakuna aliye mkuu kuliko Yohana." Katika tangazo lile lililotolewa kwa Zakaria kabla ya kuzaliwa kwa Yohana, malaika alikuwa amesema, "Atakuwa mkuu mbele za Bwana." Luka 1:15. Katika mtazamo wa mbinguni, ni kitu gani kinachofanya ukuu? Si kile ambacho ulimwengu

unakiita ukuu; si mali, wala cheo, wala ukoo wa watawal, wala vipaji vya uwezo wa akili, vinapoangaliwa kwa vyenyewe. Ikiwa ukuu wa akili, bila kuzingatia mambo ya juu, unastahilishwa heshima, hapo heshima yetu inakwenda kwa Shetani, ambaye uwezo wake wa akili ni mkubwa kiasi kwamba hakuna mwanadamu aliyepata kulingana naye kamwe. Kadiri kipawa kinavyozidi kuongezeka, ikiwa kinapopotoshwa kuelekea katika ubinafsi, ndivyo laana inavyozidi kuwa kubwa. Mungu anathamini thamani ya uadilifu. Upendo na usafi ndivyo vitu anavyothamini zaidi. Yohana alikuwa mkuu machoni pa Mungu, wakati ambapo, mbele ya Sanhedrin, mbele ya watu, na mbele ya wanafunzi wake, hakutafuta heshima yake yeye mwenyewe, bali alielekeza vyote kwa Yesu kwamba ndiye Yeye Aliyeahidiwa. Furaha yake isiyo na ubinafsi katika huduma ya Yesu inaweka mfano wa juu wa ukuu ambao haujapata kufunuliwa katika maisha ya mwanadamu.

Ushuhuda uliotolewa kumhusu baada ya kifo chake, uliotolewa na wale waliomsikia akimshuhudia Yesu, ulikuwa hivi, "Yohana kweli hakufanya ishara yoyote, lakini yote aliyoyasema Yohana katika habari zake huyu yalikuwa kweli." Yohana 10:41. Yohana hakupewa kushusha moto kutoka mbinguni, au kufufua wafu, kama Eliya alivyofanya, wala **(220)** kutumia fimbo ya Musa katika jina la Mungu. Alitumwa kutayarisha kuja kwa Mwokozi, na kuwaita watu wajitayarishe kwa kuja kwake. Hivyo ndivyo alivyoitekeleza kazi yake kwa uaminifu, kiasi kwamba watu walipokumbuka yale aliyokuwa amewafundisha kuhusu Yesu, wangeweza kusema, "Yote aliyoyasema Yohana katika habari zake huyu yalikuwa kweli." Kila mwanafunzi wa Bwana anaitwa ili kubeba ushuhuda kama huo.

Akiwa mtangulizi wa Masihi, Yohana alikuwa mtu "aliye zaidi ya nabii." Maana wakati manabii walikuwa wamekuona kuja kwa Kristo kwa mbali, Yohana yeye alipewa kumwona, kusikia ushuhuda kutoka mbinguni kuhusu Umasihi wake, na kumwasilisha kwa Israeli kama Aliyetumwa na Mungu. Lakini bado Yesu alisema, "Aliye mdogo katika ufalme wa Mungu ni mkuu kuliko yeye."

Nabii Yohana alikuwa kiunganishi kati ya vipindi viwili vya kidini. Akiwa kama mwakilishi wa Mungu alisimama kuonyesha jinsi kipindi cha sheria na manabii kinavyohusiana na kipindi cha Yesu. Alikuwa nuru ndogo, ambayo ilikuwa ifuatiwe na nuru kuu. Akili ya Yohana ilimlikiwa na Roho Mtakatifu, ili ya kwamba aangaze mwanga kwa watu; lakini kamwe hakukuwahi kuwa na nuru nyingine ambayo imepata kuangaza au ambayo itapata kuangaza kwa uwazi tena kama ile iliyotoka katika mafundisho na kielelezo cha maisha ya Yesu. Kristo na kazi yake vilikuwa vimeeleweka kwa uhafifu katika mfano kivuli cha kafara. Hata Yohana hakuwa ameelewa vizuri mambo yaliyokuwa yanakuja, uzima usiokufa kupitia Mwokozi.

Kando ya furaha ambayo Yohana alipata katika kazi yake, maisha yake yalikuwa ya huzuni. Sauti yake ilikuwa imesikika kwa nadra isipokuwa kule jangwani. Alikuwa na sehemu yake ya kuishi katika hali ya upweke. Na hakuruhusiwa kuona matokeo ya kazi yake. Hakupata nafasi ya kuwa na Kristo na kushuhudia udhihirisho wa nguvu ya kimbingu iliyokuwa ikiipeleka nuru kubwa. Asingeona vipofu wakiona, wagonjwa wakipona, na wafu wakifufuka. Hakuona nuru ile iliyoangaza katika kila neno la Kristo, ikimwaga utukufu katika ahadi za unabii. Kwa mtazamo huu mwanafunzi mdogo kuliko wote aliyeziona kazi kuu za Kristo na kusikia maneno yake alikuwa amependelewa zaidi kuliko Yohana Mbatizaji, na kwa hiyo anasemekana kuwa alikuwa mkuu kuliko yeye.

Kupitia makutano wale waliokuwa wakisikiliza mahubiri ya Yohana, sifa zake zilisambaa katika nchi yote. Mguso wa kina uliwapata watu waliposikia habari za kufungwa kwake. Lakini bado maisha yake yasiyolaumiwa kitu, na nguvu ya ushwishi wa umma iliyompenda, iliwafanya watu waamini kwamba hakuna hatua mbaya ambazo zingechukuliwa dhidi yake.

Herode aliamini kwamba Yohana ni nabii wa Mungu, na alikuwa na mpango kabisa **(221)** wa kumwachia huru. Lakini alikawia kutekeleza hilo kwa kumwogopa Herodia.

Herodia alijua kwamba kwa njia za moja kwa moja asingweza kamwe kumfanya Herode akubaliane na kuuawa kwa Yohana, na aliamua kutimiza makusudi yake kwa hila. Wakati wa siku ya kuzaliwa ya mfalme burudani ilikuwa itolewe kwa maafisa wa ufalme na wana wa nyumba ya mfalme. Kungekuwa na karamu na ulevi. Hapo ndipo Herode angewekwa mbali na mawazo yake, angeshawishiwa na matakwa ya Herodia.

Ile siku kubwa ilipofika, na wakati mfalme na mabwana walipokuwa wakisherehekea kwa kula na kunywa, Herodia alimtuma binti yake katika ukumbi wa sherehe ili acheze na kuburudisha wageni waalikwa. Huyu

Salome alikuwa binti ambaye yuko katika hatua za mwanzo za kuwa na mwonekano wa mwanamke, na mvuto wa uzuri wake uliziteka hisia za mabwana wale. Halikuwa jambo la kawaida kwa mabinti wa kifalme kujitokeza katika karamu kama hizi, na sifa zilimwendea Herode wakati binti huyu wa makuhani na wa nyumba ya kifalme alipocheza na kuwafurahisha wageni.

Mfalme alikuwa amelevywa na mvinyo. Mapenzi yalimyumbisha, akili ya kifalme ilipumbazwa. Aliona ukumbi wa raha, wageni wanaofurahia sherehe, meza ya vyakula, mvinyo inayong'aa na taa zinazometameta, na binti yule mdogo anayecheza mbele yake. Pasipo kutafakari madhara yake, aliamua kufanya jambo la kujionyesha ambalo lingemtukuza mbele ya wakuu wale wa ufalme. Kwa kiapo aliahidi kumpa yule binti wa Herodia lolote ambalo angeomba, hata kama ni nusu ya ufalme wake.

Salome akaharakisha kwa mama yake, ili ajue kitu atakachoomba. Jibu lilikuwepo tayari, - kichwa cha Yohana Mbatizaji. Salome hakujua kiu iliyokuwa moyoni mwa mama yake kutaka kulipiza kisasi, na alisita kuwasilisha ombi hilo; lakini azma ya Herodia ikashinda. Yule binti alirudi na ombi kwamba, "Nataka unipe sasa hivi katika kombe kichwa cha Yohana Mbatizaji." Marko 6:25.

Herode alishtushwa na kufadhaishwa. Shamrashamra ya kujionyesha ilikoma, ukimya wa hofu ukajitokeza. Mfalme alitishwa na wazo la kuondoa uhai wa Yohana. Lakini neno lake lilikuwa limeapiwa, na hakutaka kuonekana kwamba alikurupuka au hana msimamo. Kiapo kilikuwa kimefanywa kwa heshima ya wageni waalikwa, na ikiwa yeyote miongoni mwao angesema neno linalosihi kusitisha ahadi ya mfalme, mfalme angefurahi kumwacha salama yule nabii. Aliwapa fursa ili waseme neno kwa niaba ya mfungwa yule. Walikuwa watu waliopata kusafiri umbali mrefu kwenda kusikiliza mahubiri ya Yohana, na walimjua kwamba ni mtu asiye mhalifu, na mtumishi wa Mungu. Lakini ingawa walishtushwa na ombi la yule binti, walikuwa **(222)** wamelevywa sana kiasi cha kutoweza kuingilia kati na kupinga. Hakuna sauti iliyotolewa ili kuokoa uhai wa mjumbe wa mbinguni. Watu hawa walishikilia vyeo vya juu katika taifa, na walikuwa wamepewa mamlaka ya hali ya juu sana; lakini walikuwa wamejitumbukiza katika burudani na ulevi mpaka akili zikakosa uwezo wa kufikiri. Vichwa vyao vilibadilishwa kwa kule kuliwazwa na muziki na machezo, na dhamiri ikawa na ganzi. Kukaa kimya vile ilikuwa ni sawa na kutamka hukumu ya kifo kwa nabii wa Mungu ili kuridhisha hamu ya kisasi ya mwanamke mwasherati.

Herode alisubiri ili kuondolewa katika kiapo chake wala hakuna aliyekiondoa; ndipo kwa kutopenda akaamuru nabii auawe. Muda mfupi tu baada ya pale kichwa cha Yohana kikaletwa pale mbele yake na mbele ya wageni wake. Midomo ile ambayo kwa uaminifu ilikuwa imemwonya Herode ili aachane na maisha yake ya dhambi ikawa imefungwa milele. Kamwe sauti ile isingesikika tena ikiwaita watu waje watubu. Sherehe za usiku mmoja tu zilikuwa zimegharimu maisha ya mmojawapo wa manabii wakuu sana.

Lo, ni mara ngapi maisha ya watu wasio na hatia yametolewa kafara kupitia kukosa kiasi kwa wale ambao wangekuwa viongozi wa kusimamia haki! Yeye awekaye kikombe cha kileo midomoni mwake anawajibika kwa mabaya yote atendayo kwa kusukumwa na nguvu ya kileo hicho. Kwa kuhafifisha uwezo wake wa kutambua anafanya isiwezekane kwake kufanya uamzi kwa utulivu au kuwa na uekewa mzuri wa jambo lililo sahihi au lisilo sahihi. Anafungua mlango kwa ajili ya Shetani kumtumia kufanya kazi zake za kuwakandamiza na kuwaharibu watu wasio na hatia. "Mvinyo hudhihaki, kileo huleta ugomvi; Na akosaye kwa vitu hivyo hana hekima." Mithali 20:1. Hivyo ndivyo ilivyo kwamba "hukumu imegeuka ikaenda nyuma, . . . na yeye auachaye uovu ajifanya kuwa mateka." Isaya 59:14, 15. Wale ambao wana mamlaka juu ya maisha ya watu wengine wanakuwa na hatia ya uhalifu wanapojiingiza katika kushindwa kujitawala. Wote wanaosimamia sheria wanapaswa wawe washika sheria. Yawapasa wawe watu wanaojitawala. Lazima wawe na uwezo wa kudhibiti kikamilifu nguvu zao za mwili, za akili na za kimaadili, ili waweze kuwa na nguvu za ufahamu, na uwezo mkubwa wa kutenda haki.

Kichwa cha Yohana Mbatizaji kilipelekwa kwa Herodia, ambaye alikipokea kwa jeuri ya kuridhika. Alijisifu kwa kisasi chake kile, na kujigamba kwamba dhamiri ya Herode isingesumbuliwa tena. Lakini hakuna furaha aliyopata katika dhambi yake hiyo. Jina lake lilivuma kwa sifa mbaya na likachukiwa sana, huku Herode akawa na maumivu makali ya hatia zaidi ya yale aliyokuwa nayo kabla ya kuonywa na nabii yule. Nguvu ya ushawishi wa mafundisho ya Yohana haukunyamazishwa; utaendelea kwa kila kizazi hadi mwisho wa wakati.

**(223)** Dhambi ya Herode ilikuwa machoni pake daima. Wakati wote alitafuta kupata kuwa huru na hatia ya dhamiri iliyokuwa inamsuta. Imani ya Yohana ilikuwa ile isiyotikisika. Kadiri alivyokumbuka maisha ya Yohana ya kujikana nafsi, umakini wake, kusihi kwake kwa upendo, maamuzi yake sahihi katika mashauri, halafu akakumbuka jinsi alivyokifikia kifo chake, Herode hakupata utulivu. Akiwa anashughulikia mambo ya kifalme, akipata heshima kutoka kwa watu, alikuwa na uso wa tabasamu na mwonekano wa kuheshimiwa, lakini alificha moyo wa wasiwasi, ambao daima ulikuwa umekandamizwa na hofu kwamba laana ilikuwa juu yake.

Herode alikuwa ameguswa sana na maneno ya Yohana, kwamba hakuna kinachoweza kufichwa Mungu asikione. Alikuwa ameelewa kwamba Mungu yuko kila mahali, kwamba alikuwa ameshuhudia lile tukio la tafrija katika chumba kile, kwamba alikuwa amesikia agizo la kumkata Yohana kichwa, alikuwa ameona jeuri ya Herodia, na kejeli aliyokifanyia kichwa kile cha yeye akemeaye. Na vitu vingi ambavyo Herode alikuwa amesikia katika midomo ya nabii yule viliongea na dhamiri yake sasa kwa uthabiti zaidi kuliko mahubiri ya jangwani yalivyokuwa.

Wakati Herode aliposikia kazi za Kristo, alitaabika kupita kiasi. Alifikiri kwamba Mungu amemfufua Yohana, na kwamba alikuwa amemtuma kukemea dhambi kwa nguvu zaidi. Alikuwa katika hofu wakati wote kwamba huenda Yohana angelipiza kisasi kwa kumhukumu yeye na nyumba yake. Herode alikuwa anavuna kile ambacho Mungu alikuwa ametangaza kuwa ndiyo matokeo ya dhambi, - "moyo wa kutetema, na macho ya kuzimia, na roho ya kudhoofika; na uzima wako utakuwa na wasiwasi mbele yako; nawe utakuwa na woga usiku na mchana, wala hutaamini kamwe maisha yako; asubuhi utasema, Laiti ingekuwa jioni! Na jioni utasema, Laiti ingekuwa asubuhi! Kwa kicho cha moyo wako utakavyokucha, na kuona kwa macho yako utakavyoona." Kumbukumbu 28:65-67. Mawazo ya mdhambi ndiyo mshtaki wake; na hakuna mateso makali zaidi kuliko kuuma kwa hatia ya dhamiri, ambako hakumpi utulivu mchana wala usiku.

Katika mawazo ya watu wengi kuna fumbo kubwa linaloizunguka hatima ya Yohana Mbatizaji. Wanahoji kwamba ni kwa nini aachwe bila msaada na kufia gerezani. Uwezo wetu wa kibinadamu wa kuona hauwezi kuipenya siri hii ya giza iliyowekwa na Mungu; lakini haiwezi kutikisa imani yetu kwa Mungu tunapokumbuka kwamba Yohana alikuwa mshirika tu katika mateso ya Kristo. Wote wanaomfuata Kristo watavaa taji ya kafara. Kwa kweli hawataeleweka vizuri kwa watu wenye ubinafsi, na watafanywa kuwa alama ya mashambulizi makali ya Shetani. Ufalme wake umejikita katika kuharibu kanuni hii ya kujitoa kafara, na ataipiga vita kanuni hii mahali popote itakapooneka.

**(224)** Utoto, ujana, na utu uzima wa Yohana ulikuwa na sifa ya uthabiti na uadilifu. Wakati sauti yake iliposikika nyikani ikisema, "Itengenezeni njia ya Bwana, Yanyosheni mapito yake." (Mathayo 3:3), Shetani alihofia usalama wa ufalme wake. Udhambi wa dhambi ulifunuliwa kiasi kwamba watu walitetemeka. Nguvu za Shetani juu ya wale anaowatawala ilivunjika. Alikuwa amefanya kazi bila kuchoka kumwondoa Mbatizaji katika maisha ya kujitoa kikamilifu kwa Mungu; lakini alikuwa ameshindwa. Na alikuwa ameshindwa kumwangusha Yesu. Katika majaribu ya nyikani, Shetani alikuwa ameshindwa, na hasira yake ilikuwa kubwa. Sasa aliamua kuleta huzuni kwa Yesu kwa kumpiga Yohana. Aliamua kuleta maumivu kwake Yeye ambaye hakuweza kumwingiza katika dhambi.

Yesu hakuingilia kati amwokoe mtumishi wake. Alijua kwamba Yohana angestahimili jaribu lile. Yesu angeweza kufurahia kuja kumwona Yohana, kuondoa hali yake ya upweke ya gerezani. Lakini hakutaka kujiweka katika mikono ya maadui na kuhatarisha kazi yake mwenyewe. Angeweza kufurahia kumwokoa mtumishi wake huyu mwaminifu. Lakini ilikuwa Yohana akinywee kikombe cha kuifia imani kwa faida ya maelfu ya watu ambao watapitia katika gereza hadi kufa kwa miaka mingi baadaye. Wakati wafuasi wa Yesu wahuzunikapo katika vyumba vya upweke vya magereza, au kuangamia kwa upanga, kwenye vitanda vya kutesea, au kwa moto, wakionekana kama vile wamesahauliwa na Mungu na mwanadamu, ni jinsi gani ambavyo yangewakaa moyoni mawazo ya kwamba Yohana Mbatizaji, ambaye imani yake ilishuhudiwa na Kristo mwenyewe, alikuwa amepita katika uzoefu kama huo!

Shetani aliruhusiwa kukatiza maisha ya duniani ya mjumbe wa Mungu; lakini mharibu huyo hakuyafikia maisha yale ambayo yamefichwa "pamoja na Kristo katika Mungu." Wakolosai 3:3. Alijigamba kwamba alikuwa ameleta huzuni kwa Kristo, lakini alikuwa ameshindwa kupata ushindi kwa Yohana. Kile kifo chenyewe kilikuwa kimemweka Yohana ng'ambo ya uwezo wa majaribu milele. Katika vita hii, Shetani alikuwa anafunua tabia yake

halisi. Mbele ya macho ya malimwengu yaliyokuwa yanashuhudia alidhihirisha uadui wake dhidi ya Mungu na mwanadamu.

Ingawa hakuna wokovu wa kimiujiza uliotolewa kwa Yohana, hakuachwa. Wakati wote alikuwa na malaika, ambao walimfunulia unabii unaomhusu Kristo, na ahadi za thamani za Maandiko. Alishikilia mambo hayo, kama yanavyopaswa kushikiliwa na watu wa Mungu wa vizazi vilivyokuwa vinafuata. Hakikisho hili lilitolewa kwa Yohana, na kwa wale waliokuja baada yake: "Tazama, nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari." Mathayo 28:20.

Kamwe Mungu hawaongozi watoto wake kwa namna tofauti na vile ambavyo wangechagua waongozwe, ikiwa wangeuona mwisho kutokea mwanzo, na kupambanua utukufu **(225)** wa kusudi wanalotekeleza wakiwa watenda-kazi pamoja naye. Henoko, aliyetwaliwa mbinguni, na Eliya, aliyepaa katika gari la moto, hawakuwa wakuu au watu waliotukuzwa kuliko Yohana Mbatizaji, aliyeangamia katika upweke wa gereza. "Mmepewa kwa ajili ya Kristo, si kumwamini tu, ila na kuteswa kwa ajili yake." Wafilipi 1:29. Miongoni mwa vipawa ambavyo mbingu inatoa kwa wanadamu, hakuna chenye amana nzito na ya heshima ya juu mno kama kushiriki na Kristo katika mateso yake.

## Sura ya 23

# "Ufalme wa Mungu Umekaribia"

"Yesu akaenda Galilaya, akiihubiri Habari Njema ya Mungu, akisema, Wakati umetimia, na ufalme wa Mungu umekaribia; tubuni, na kuiamini Injili." Mark 1:14, 15.

Kuja kwa Masihi kulikuwa kumetangazwa kwanza katika Uyahudi. Katika hekalu la Yerusalemu kuzaliwa kwa mtangulizi wake kulikuwa kumetabiriwa kwa Zakaria wakati alipokuwa anahudumu madhabahuni. Katika vilima vya Bethlehemu malaika walikuwa wamekutangaza kuzaliwa kwa Yesu. Mamajusi walikuwa wamekuja Yerusalemu wakimtafuta Yeye. Katika hekalu Simeoni na Ana walikuwa wametoa ushuhuda wa uungu wake. "Yerusalemu, na Uyahudi wote" walikuwa wamesiliza mahubiri ya Yohana Mbatizaji; na wale wajumbe waliotumwa kutoka Sanhedrin, na makutano, walikuwa wamesikia ushuhuda wake kuhusu Yesu. Katika Uyahudi, Kristo alikuwa amewapata wanafunzi wake wa kwanza. Sehemu kubwa ya huduma yake ya awali ilikuwa imefanyika hapa. Kuonekana kwa uungu wake wakati wa kulisafisha hekalu, miujiza yake ya kuponya, na masomo ya ukweli wa mbinguni yaliyotoka midomoni mwake, vyote vilitangaza kile ambacho baada ya uponyaji wa Bethzatha alikuwa amekitangaza kwa Sanhedrin, - hali yake ya kuwa Mwana wa Mungu.

Ikiwa viongozi wa Israeli wangempokea Kristo, angewatukuza kama wajumbe wake wa kuipeleka injili ulimwenguni. Fursa ya kuwa watangazaji wa ufalme na neema **(232)** ya Mungu ilitolewa kwao kwanza. Lakini Israeli hakujua wakati wa kujiliwa kwake. Wivu na kutoamini kwa viongozi wa Wayahudi vilikomaa na kuwa chuki ya wazi, na mioyo ya watu ikageuziwa mbali na Yesu.

Sanhedrin ilikuwa imekataa ujumbe wa Kristo na ilitafuta kumwua; kwa hiyo Yesu aliondoka Yerusalemu, akiondoka kutoka kwa makuhani, viongozi wa dini, watu waliokuwa wamefundishwa sheria, akageukia jamii nyingine ili atangaze kwao ujumbe wake, na kuwakusanya huko wale ambao wangeipeleka injili kwa mataifa yote.

Kama vile ambavyo nuru na maisha ya watu vilikataliwa na mamlaka za kidini mnamo wakati wa siku za Kristo, ndivyo ambavyo vitu hivyo vimekuwa vikikataliwa katika kila kizazi kinachofuata baada ya pale. Historia ya Kristo kuondoka kutoka Yudea imekuwa ikirudiwa tena na tena. Wakati Wanamatengenezo walipohubiri neno la Mungu, hawakuwa na wazo la kujitenga kutoka katika kanisa lililokuwepo; lakini viongozi wa dini wasingeivumilia nuru ile, na wale walioibeba walilazimika kutafuta kundi jingine ya watu waliokuwa wanauhitaji ukweli. Katika siku zetu hizi watu wachache miongoni mwa wale wanaodaiwa kuwafuata Wanamatengenezo wanahimizwa na roho ile ile. Wachache huisikia sauti ya Mungu, na wako tayari kuukubali ukweli ukiwasilishwa katika mwonekano wowote ule. Mara nyingi wale wanaofuata nyayo za Wanamatengenezo wanalazimika kugeukia mbali na kuyaacha makanisa wanayoyapenda, ili kuweza kutangaza mafundisho ya kweli ya neno la Mungu. Na mara nyingi wale wanoitafuta nuru nao wanalazimika kuliacha kanisa la mababa zao kwa sababu ile ile, ili waweze kutii.

Watu wa Galilaya walikuwa wanadharauliwa na marabi wa Yerusalemu kama washenzi na wasioelimika, lakini walionyesha hali ya kuwa mahali bora kwa ajili ya kazi ya Mwokozi. Walikuwa thabiti na wanyofu; wakiwa hawashikiliwi sana na kiburi cha ujuzi; mawazo yao yalikuwa wazi zaidi kwa ajili ya kuupokea ukweli. Kwa kule kwenda Galilaya, Yesu hakuwa anatafuta mahali pa faragha au kutaka kujitenga. Wakati huo jimbo hili lilikuwa linakaliwa na watu wengi, kukiwa na mchanganyiko mkubwa wa watu wa mataifa mengine kuliko ilivyokuwa kule Uyahudi.

Kadiri Yesu alivyotembea katika Galilaya, akifundisha na kuponya, watu wengi walikuja kwake wakitoka mijini na vijijini. Wengine wengi walikuja kutoka Uyahudi na majimbo yaliyo jirani. Mara nyingi alilazimika kujificha mbali na watu. Wasiwasi ulikuwa mkubwa kiasi kwamba ilikuwa muhimu kuchukua tahadhari ili mamlaka za Kirumi zisiinuke kwa kuogopa kuibuka kwa upinzani. Ulimwengu ulikuwa haujapata kushuhudia kipindi kama hicho kamwe. Mbingu zilishushwa kwa wanadamu. Roho zenye njaa na kiu zilizokuwa zimesubiri ukombozi wa Israeli kwa muda mrefu zilifanya sherehe ya rehema ya Mwokozi mwenye neema.

**(233)** Mzigo wa mahubiri ya Kristo ulikuwa ni, "Wakati umetimia, na ufalme wa Mungu umekaribia; tubuni, na kuiamini Injili." Ujumbe wa injili, kama ulivyotolewa na Mwokozi mwenyewe, ulijikita katika unabii. Huo "wakati" aliotangaza kuwa umetimia ni ule ambao malaika Gabrieli alifanya ujulikane kwa Danieli. Malaika alisema, "Muda wa majuma sabini umeamriwa juu ya watu wako, na juu ya mji wako mtakatifu, ili kukomesha makosa, na kuishiliza dhambi, na kufanya upatanisho kwa ajili ya uovu, na kuleta haki ya milele, na kutia muhuri maono na unabii, na kumtia mafuta yeye aliye mtakatifu." Danieli 9:24. Katika unabii siku inasimama mahali pa mwaka. Angalia Hesabu 14:34; Ezekieli 4:6. Majuma hayo sabini, au siku mia nne na tisini, huwakilisha miaka mia nne na tisini. Mahali pa kuanzia kipindi hiki pametajwa: "Basi ujue na kufahamu, ya kuwa tangu kuwekwa amri ya kutengeneza na kuujenga upya Yerusalemu hata zamani zake masihi aliye mkuu; kutakuwa na majuma saba; na katika majuma sitini na mawili," au miaka mia nne na themanini na tatu. Danieli 9:25. Amri ya kujenga upya Yerusalemu, kama ilivyokamilishwa na tamko la Artashasta Longimanus (tazama Ezra 6:14; 7:1, 9), ilitolewa rasmi katika majira ya kupukutisha ya mwaka 457 K.K. Tangu wakati huu miaka mia nne na themanini na tatu inaenda hadi majira ya kupukutisha ya mwaka wa 27 B.K. Kulingana na unabii huo, kipindi hiki kilikuwa kifike kwa Masihi, Mtiwa Mafuta. Mwaka wa 27 B.K., Yesu alipata kupakwa mafuta na Roho Mtakatifu wakati wa kuzaliwa kwake, na baada ya pale alianza kazi yake. Halafu ujumbe huu ulitangazwa. "Wakati umetimia."

Halafu, malaika akasema, "Naye atafanya agano thabiti na watu wengi kwa muda wa juma moja [miaka saba]." Kwa miaka saba baada ya Yesu kuingia katika huduma yake, injili ilikuwa ihubiriwe hasa kwa Wayahudi; kwa miaka mitatu na nusu na Yesu mwenyewe; na baada ya hapo mitume. "Na kwa nusu ya juma hiyo ataikomesha sadaka na dhabihu." Danieli 9:27. Mnamo majira ya kuchipua ya mwaka 31 B.K., Kristo aliye kafara ya kweli alitolewa Kalvari. Wakati huo pazia la hekalu lilipasuka vipande viwili, kuonyesha kwamba utakatifu na umuhimu wa huduma za kafara vilikuwa vimepita. Muda ulikuwa umekuja kwa ajili ya kafara na matoleo ya duniani kukoma.

Lile juma moja – miaka saba – liliishia mwaka 34 B.K. Wakati huo Wayahudi, kwa kumpiga mawe Stefano, walitia muhuri tendo la kuikataa injili; wanafunzi waliokuwa wametawanywa na mateso nchi nyingine "walienda kila mahali wakilihubiri neno." (Matendo 8:4); na muda mfupi baadaye, Sauli mtesaji aliongoka, na akawa Paulo, mtume kwa Mataifa.

**(234)** Wakati wa kuja kwa Kristo, kupakwa mafuta na Roho Mtakatifu, kifo chake, na kule kuwapatia Mataifa injili, vilikuwa vimeonyeshwa dhahiri. Wayahudi walikuwa wamependelewa kwamba waelewe unabii huu, na kutambua kutimia kwake katika kazi ya Kristo. Kristo aliwasisitiza wanafunzi wake kuhusu umuhimu wa kuchunguza unabii. Akirejea katika unabii uliotolewa kwa Danieli kuhusu wakati wao, alisema, "Asomaye na afahamu." Mathayo 24:15. Baada ya kufufuka kwake aliwaeleza wanafunzi wake "mambo yaliyomhusu yeye mwenyewe" yaliyokuwa katika "manabii wote" Luka 24:27. Mwokozi alikuwa amesema kupitia manabii wote. "Roho wa Kristo aliyekuwa ndani yao" aliweza "kuyashuhudia mateso yatakayompata Kristo, na utukufu utakaokuwako baada ya hayo." 1 Petro 1:11.

Ni Gabrieli, yule malaika ambaye ukuu wake unafuata baada ya ule wa Mwana wa Mungu, aliyekuja kwa Danieli akiwa na ujumbe wa kimbingu. Alikuwa Gabrieli aliyetumwa na Kristo kufunua siku zijazo kwa Yohana mpendwa; na mbaraka unatajwa kwa wale wanaosoma na kusikia maneno ya unabii, na kuyashika yaliyoandikwa humo. Rev. 1:3.

"Bwana MUNGU hatafanya neno lolote, bila kuwafunulia watumishi wake manabii siri yake." Wakati "mambo ya siri ni ya Bwana, Mungu wetu;" "mambo yaliyofunuliwa ni yetu sisi na watoto wetu." Amosi 3:7; Kumbukumbu 29:29. Mungu ametupatia vitu hivi, na mibaraka yake itaandamana na ujifunzaji wa maandiko ya unabii kwa unyenyekevu na maombi.

Kama vile ujumbe wa kuja kwa Kristo mara ya kwanza ulivyoutangaza ufalme wa neema yake, ndivyo ujumbe wa kuja kwake mara ya pili utakavyotangaza ufalme wa utukufu wake. Na ujumbe wa pili, kama ulivyo wa kwanza, umejengwa katika unabii. Maneno ya malaika kwa Danieli kuhusiana na siku za mwisho yangeeleweka mnamo siku za mwisho. Wakati huo, "wengi wataenda mbio huko na huko, na maarifa yataongezeka." "Wabaya watatenda mabaya; wala hataelewa mtu mbaya awayeyote; bali wao walio na hekima ndio watakaoelewa." Danieli 12:4, 10. Mwokozi mwenyewe ametoa ishara za kuja kwake, na anasema, "Mwonapo mambo hayo yanaanza kutokea, tambueni ya kwamba ufalme wa Mungu u karibu." "Basi, jiangalieni, mioyo yenu isije

ikalemewa na ulafi, na ulevi, na masumbufu ya maisha haya; siku ile ikawajia ghafla." "Basi, kesheni ninyi kila wakati, mkiomba, ili mpate kuokoka katika haya yote yatakayotokea, na kusimama mbele za Mwana wa Adamu." Luka 21:31, 34, 36.

**(235)** Tumekifikia kipindi kilichotabiriwa katika maandiko haya. Wakati wa mwisho umekuja, maono ya unabii yaliyokuwa yametiwa muhuri yamefunguliwa, na maonyo yake yanatuonyesha kwamba kuja kwa Bwana katika utukufu kumekaribia.

Wayahudi walilitafsiri na kulitumia isivyo sahihi neno la Mungu, hawakujua wakati wa kujiliwa kwao. Waliitumia miaka ya kazi ya Kristo na mitume wake, - ile miaka ya mwisho ya thamani ya neema kwa taifa hili la waliochaguliwa, - kula njama ya kuwaangamiza wajumbe wa Bwana. Tamaa ya kutafuta mambo ya dunia iliwateka, na zawadi ya ufalme wa roho iliwajia wala haikuwafaa kitu. Vivyo hivyo hata leo ufalme wa ulimwengu huu unayateka mawazo ya watu, wala hawazingatii unabii unaotimia kwa haraka na dalili za kuja kwa haraka kwa ufalme wa Mungu.

"Bali ninyi, ndugu, hammo gizani, hata siku ile iwapate kama mwivi. Kwa kuwa ninyi nyote mmekuwa wana wa nuru, na wana wa mchana; sisi si wa usiku, wala wa giza." Wakati hatutajua saa ya kurudi kwa Bwana wetu, tunaweza kujua ni wakati gani imekaribia. "Basi tusilale usingizi kama wengine, bali tukeshe, na kuwa na kiasi." 1 Wathesalonike 5:4-6.

## Sura ya 24

# "Huyu Si Mwana wa Seremala?"

[Sura hii imejengwa katika Luka 4:16-30.]

Katika siku angavu za huduma ya Yesu kule Galilaya, kulikuwa na hali moja iliyotia uvuli. Watu wa Nazareti walimkataa. Wakasema, "Huyu si mawana wa seremala?"

Katika siku zake za utoto na ujana, Yesu alikuwa ameabudu miongoni mwa ndugu zake katika sinagogi la Nazareti. Tangu kuanza kwa kazi yake hakuwa pamoja nao, lakini si kwamba hawakujua kilichompata. Alipojitokeza tena miongoni mwao, hamu na matarajio yao yalisisimka hadi katika kilele. Hapa kulikuwa na maumbo na nyuso za watu ambao amewafahamu tangu utotoni mwake. Hapa alikuwepo mama yake, kaka na dada zake, na macho yote yalimgeukia wakati alipoingia katika sinagogi siku ya Sabato, na kuchukua nafasi yake miongoni mwa wanaoabudu.

Katika ibada ya kawaida ya siku hiyo, mzee alisoma kutoka katika maandiko ya manabii, na kuwasisitiza watu kuendelea kumtarajia Yeye Ajaye, ambaye angeleta utawala wa utukufu, na kuondosha ukandamizaji wote. Alitafuta kuwatia moyo wasikilizaji wake kwa kuzoeza kutambua viashiria kwamba kuja kwa Masihi kulikuwa kunakaribia. Aliufafanua utukufu wa kuja kwake, akibainisha wazo kwamba Masihi angejitokeza akiyaongoza majeshi kuja kuikomboa Israeli.

Wakati rabi alipokuwa mahali pa sinagogi, alitarajiwa kuhubiri, na Mwisraeli yeyote angesoma aya kutoka katika manabii. Katika Sabato hii Yesu aliombwa kushika nafasi hiyo katika ibada. "Akasimama ili asome. Akapewa chuo cha nabii Isaya." Luka 4:16, 17. Maandiko aliyosoma yalikuwa yale yaliyokuwa yanaeleweka kwamba yanamhusu Masihi:
**(237)** "Roho wa Bwana yu juu yangu, Kwa maana amenitia mafuta kuwahubiri maskini habari njema.
Amenituma kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao, Na vipofu kupata kuona tena,
Kuwaacha huru waliosetwa, Na kutangaza mwaka wa Bwana uliokubaliwa."

"Akakifunga chuo, akamrudishia mtumishi, . . . na watu wote waliokuwamo katika sinagogi wakamkazia macho. . . . Wakamshuhudia wote, wakiyastaajabia maneno ya neema yaliyotoka kinywani mwake." Luka 4:20-22.

Yesu alisimama mbele ya watu kama mfafanuzi wa unabii uliomhusu Yeye mwenyewe. Akiwa anaelezea maneno yale aliyokuwa amesoma, alimwongelea Masihi kama mtoa uhuru kwa waliokandamizwa, mwokoaji wa waliofungwa, mponyaji wa wagonjwa, anayewarejeshea watu kuona, na anayeufunulia ulimwengu nuru ya ukweli. Hali yake ya mvuto na umuhimu wa ajabu wa maneno yake uliamsha nguvu miongoni mwa wasikilizaji wake kwa namna ambayo walikuwa hawajapata kuona kabla. Wimbi la uwezo wa kimbingu ulivunja kila kizuizi; kama Musa, walimwona Asiyeonekana. Kadiri mioyo yao ilivyosukumwa na Roho Mtakatifu, waliitikia kwa hamasa wakisema amen na kumsifu Bwana.

Lakini Yesu alipotangaza kwamba, "Leo maandiko haya yametimia masikioni mwenu," ghafla walirudi kujifikiria wao, na madai yake Yeye aliyekuwa anawahutubia. Wao, Waisraeli, wana wa Ibrahamu, wawakilishwe na hali ya kuwa katika utumwa. Walikuwa wametajwa kama wafungwa wanaohitaji kufunguliwa kutoka katika uovu; kama katika giza, wakiihitaji nuru ya ukweli. Majivuno yao yalitiwa hasira, na hofu zao ziliamshwa. Maneno ya Yesu yalionyesha kwamba kazi yake kwao ingekuwa tofauti kabisa na vile walivyotamani iwe. Matendo yao yangepelelezwa kwa ukaribu sana. Licha ya kwamba walizingatia sana maadhimisho ya ibada kwa nje, walikataa kukaguliwa na macho yale angavu yapelelezayo ndani.

Huyu Yesu ni nani? Waliuliza. Yeye aliyedai kuwa utukufu wa Masihi ni wake alikuwa mwana wa seremala, na alikuwa amefanya kazi katika sehemu yake ya kazi ya ufundi pamoja na baba yake Yusufu. Walikuwa wamemwona akitaabika kupanda na kushuka milima katika kazi zake, waliwafahamu kaka na dada zake, na waliyajua maisha yake na kazi zake. Walikuwa wamemwona katika kukua kwake kutoka utotoni hadi ujanani, na kutoka ujanani hadi utu uzima. Ingawa maisha hayakuwa na mawaa, wasingeamini kwamba alikuwa Yeye Aliyeahidiwa. **(238)** Ni tofauti iliyoje iliyokuwa kati ya mafundisho yake kuhusu ufalme huu mpya na ule

waliokuwa wamesikia ukihubiriwa na yule mzee! Yesu hakuwa amesema lolote kuhusu kuwaokoa kutoka mikononi mwa Warumi. Walikuwa wamesikia kuhusu miujiza yake, na walikuwa wametarajia kwamba uwezo wake ungetumika kwa manufaa yao, lakini hawakuwa wameona kiashiria chochote cha kusudi hilo.

Kadiri walivyofungua mlango wa mashaka, mioyo yao ilikuwa migumu sana isiyoweza kulainishwa. Shetani alikuwa ameazimia kwamba macho yaliyo na upofu yasifunguke siku ile, wala roho zilizofungwa utumwani zisiwekwe huru. Aliwafanya wasiamini kwa kukaza kwa nguvu sana. Hawakujali ishara iliyokuwa imetolewa tayari, wakati walipoamshwa na kusadikishwa kwamba aliyekuwa ananena nao ni Mkombozi wao.

Lakini sasa Yesu aliwapa ushahidi wa uungu wake kwa kufunua mawazo yao ya siri. "Akawaambia, Hapana shaka mtaniambia mithali hii, Tabibu, jiponye nafsi yako; mambo yote tuliyosikia kwamba yametendeka Kapernaumu, yatende na hapa pia katika nchi yako mwenyewe. Akasema, Amin, nawaambia ya kwamba, Hakuna nabii mwenye kukubaliwa katika nchi yake mwenyewe. Lakini, kwa hakika nawaambia, Palikuwa na wajane wengi katika nchi ya Israeli zamani za Eliya, wakati mbingu zilipofungwa miaka mitatu na miezi sita, njaa kuu ikaingia nchi nzima; wala Eliya hakutumwa kwa mmojawapo, ila kwa mjane mmoja wa Sarepta katika nchi ya Sidoni. Tena, palikuwa na wenye ukoma wengi katika Israeli zamani za nabii Elisha, wala hapana aliyetakaswa ila Naamani, mtu wa Shamu." Luka 4:23-27.

Kwa masimulizi haya ya matukio katika maisha ya manabii, Yesu alijibu maswali ya wasikilizaji wake. Watumishi ambao walikuwa wamechaguliwa na Mungu kwa ajili ya kazi maalum hawakuruhusiwa kufanya kazi kwa watu wenye mioyo migumu na wasioamini. Bali wale waliokuwa na moyo wenye hisia na imani yenye kuamini walipendelewa hasa na ushuhuda wa nguvu za Mungu kupitia manabii. Mnamo siku za Eliya, Israeli walikuwa wamemwacha Mungu. Waling'ang'ania dhambi zao, na walikataa maonyo ya Roho kupitia wajumbe wa Bwana. Hivyo walijikata kutoka katika mfereji unaotumiwa kuwafikishia mibaraka ya Mungu. Bwana alizipita nyumba za Israeli, na kupata hifadhi kwa ajili ya mtumishi wake katika nchi ya wapagani, kwa mwanamke ambaye hakuwa miongoni mwa watu wake waliochaguliwa. Lakini mwanamke huyu alipendelewa kwa sababu aliifuata nuru aliyokuwa amepokea, na moyo wake ulikuwa wazi kupokea nuru kubwa zaidi ambayo Mungu angempelekea kupitia nabii wake.

**(239)** Kwa sababu hiyo hiyo mnamo wakati wa Elisha wakoma waliokuwa katika Israeli walipitwa. Lakini Naamani, mtu mkuu mpagani, alikuwa mwaminifu kwa usadikisho aliopewa, na alikuwa amehisi kuwa na hitaji kubwa la kusaidiwa. Alikuwa katika hali ya kupokea zawadi ya rehema ya Mungu. Si tu kwamba alitakaswa ukoma wake, bali pia alikuwa amebarikiwa hali ya kumjua Mungu wa kweli.

Kusimama kwetu mbele ya Mungu hakutegemei kiasi cha nuru tulichopokea, bali jinsi tunavyotumia kile tulicho nacho. Kwa hiyo hata wapagani wanaochagua jambo sahihi kulingana na jinsi wanavyoweza kulibainisha wako katika nafasi nzuri kuliko ile waliyomo wale ambao wamekuwa na nuru kubwa, na wakidai kwamba wanamtumikia Mungu, lakini wakiwa wanapuuza nuru hiyo, na kwa maisha yao ya kila siku wakiyakana madai yao hayo.

Maneno ya Yesu kwa wasikilizaji wake katika sinagogi yalipiga kwenye mzizi wa hali yao ya kujihesabia haki, yakisukumia kwao hadi mahali pake ukweli mchungu kwamba walikuwa wamemwacha Mungu na kunyang'anywa haki yao ya kuwa watu wake. Kila neno lilikata kama kisu kadiri hali yao halisi ilivyowekwa wazi mbele yao. Sasa wakabeza imani ile ambayo Yesu alikuwa amewavuvia mwanzoni. Hawakuweza kukiri kwamba Yeye aliyekulia katika umaskini na hali ya chini alikuwa zaidi ya mwanadamu wa kawaida.

Kutokuamini kwao kulizaa nia ovu. Shetani aliwaongoza, na kwa ghadhabu walipiga kelele kumpinga Mwokozi. Walikuwa wamegeukia mbali na Yeye ambaye nia yake **(240)** ilikuwa ni kuwaponya na kuwarejesha; sasa walidhihirisha sifa za mwuaji.

Wakati Yesu alipoongelea mibaraka iliyotolewa kwa Mataifa, kiburi kikubwa cha utaifa kiliamshwa kwa wasikilizaji wake, na sauti yake ilimezwa na maneno yao ya ghasia. Watu hawa walikuwa wamejivunia sana kuishika sheria; lakini sasa kwamba imani yao potofu ilikuwa imetiliwa shaka, walikuwa tayari kuua. Mkutano ulivurugika, na wakiwa wameweka mikono yao juu ya Yesu, walimtoa nje ya sinagogi, na nje ya mji. Wote walionekana kutaka aangamizwe. Waliharakisha kumpeleka penye ukingo wa kilima, wakidhamiria kumdondosha chini kwa kutanguliza kichwa. Kelele na maneno ya kulaani yalilijaza anga lile. Baadhi walikuwa

wakimtupia mawe, na mara akawatoka na kutoweka ghafla. Wajumbe wa mbinguni waliokuwa kando yake alipokuwa katika sinagogi walikuwa naye pia katikati ya umati wenye hasira. Walimfungia mbali na adui zake, na wakamwongoza hadi mahali salama.

Hivyo ndivyo malaika walivyomlinda Lutu, na wakamwongoza salama kutoka ndani ya Sodoma. Ndivyo walivyomwongoza Elisha katika mji mdogo wa milimani. Wakati vilima vinavyozunguka pande zote vilipojazwa na farasi na magari ya vita ya mfalme wa Shamu, na wakuu wa watu wake wa vita, Elisha aliona mitelemko ya vilima vya karibu zaidi vikiwa vimejawa na majeshi ya Mungu, - farasi na magari ya vita ya moto yakimzunguka mtumishi wa Bwana.

Hivyo ndivyo ambavyo, katika zama zote, malaika wamekuwa wako karibu na wafuasi waaminifu wa Kristo. Jeshi kubwa la mwovu limepangwa dhidi ya wote wanaotarajia kushinda; lakini Kristo anatutaka tutazame yale yasiyoonekana, tuone majeshi ya mbinguni ambayo yameweka kambi kuwazunguka wote wampendao Mungu, ili kuwaokoa. Kamwe hatutajua hatari, zinazoonekana na zisizoonekana, ambazo tumeepushwa nazo kwa malaika kuingilia kati, mpaka tutakapouona uwezo wa Mungu katika nuru ya milele. Hapo ndipo tutakapojua kwamba jamaa yote ya mbinguni ilivutiwa na jamaa ya hapa chini, na wajumbe wale watokao penye kiti cha enzi walilinda hatua zetu kila siku.

Yesu aliposoma maandiko ya unabii katika sinagogi, alifupisha maelezo yanayohusu kazi ya Masihi. Alipokuwa amesoma maneno, "Kuutangaza mwaka wa Bwana uliokubaliwa," aliondoa maneno, "na siku ya kisasi cha Mungu wetu." Isaya 61:2. Maneno haya yalikuwa na ukweli sawaswa na yale ya kwanza ya unabii huo, na kwa kukaa kwake kimya Yesu hakuukana ukweli huo. Lakini sehemu hii ya mwisho ilikuwa ile ambayo wasikilizaji wake waliazimia kusimama juu yake, na ambayo walishabikia kuitimiza. Walizitangaza hukumu dhidi ya wapagani, bila kuona **(241)** kwamba hatia yao wao ilikuwa kubwa zaidi kuliko wengine. Wao wenyewe walikuwa katika uhitaji mkubwa wa rehema waliyokuwa wanawazuilia wapagani. Siku ile Yesu aliposimama miongoni mwao katika sinagogi ilikuwa ndiyo fursa yao ya kupokea wito wa Mbingu. Yeye ambaye "hufurahia rehema" (Mika 7:18) angetamani kuwaokoa kutoka katika maangamizi yaliyokuwa yanaletwa na dhambi zao.

Hakuacha kuwapa wito mwingine wa kutubu. Karibu na mwisho wa kazi yake Galilaya, alitembelea tena mahali pa nyumbani pa utoto wake. Kwa kuwa kitendo cha kukataliwa kwake, umakini wa mafundisho yake na miujiza yake vilikuwa vimeijaza nchi ile, kusingekuwa na mtu sasa ambaye angekana kwamba alikuwa na nguvu zaidi ya mwanadamu wa kawaida. Watu wa Nazareti walijua kwamba alienenda kwa kutenda mema, na kuwaponya wote walioonewa na Shetani. Pale kulikuwa na vijiji ambavyo havikuwa na nyumba yoyote yenye miguno inayosababishwa na magonjwa; maana alikuwa amepita pote hapo, na kuponya wagonjwa wote. Rehema iliyofunuliwa katika kila tendo la maisha yake lilidhihirisha kupakwa kwake mafuta ya kimbingu.

Kwa mara nyingine Wanazareti hawa walipoyasikiliza maneno yake walisukumwa na Roho wa Mungu. Hata wakati huu hawakukiri kwamba Mtu huyu, aliyekuwa ameletwa kwao, alikuwa tofauti au mkuu kuliko wao. Bado kulikuwa na kumbukumbu mbaya kwamba wakati alipodai kuwa ni Yeye Aliyeahidiwa, alikuwa amewanyima nafasi kwa Israeli; maana aliwaonyesha kuwa ni watu wenye kustahili upendeleo wa Mungu kidogo sana kuliko mwanamume na mwanamke mpagani. Kwa hiyo ingawa waliuliza kwamba, "Huyu amepata wapi hekima hii na miujiza hii?" wasingempokea kama Kristo wa Mungu. Kwa sababu ya kutoamini kwao, Mwokozi hakuweza kufanya miujiza mingi kwao. Mioyo michache tu ilikuwa wazi kupokea mbaraka wake, na pasipokupenda aliondoka kwao, na kamwe asingerudi.

Kule kutoamini kulikong'ang'aniwa kuliendelea kuwatawala watu wa Nazareti. Ndivyo pia kulivyotawala Sanhedrin na taifa lote. Kwa makuhani na watu, kule kukataa mara ya kwanza udhihirisho wa Roho Mtakatifu ulikuwa ndio mwanzo wa mwisho. Ili kuthibitisha kwamba walikuwa sahihi kumkataa mara ile ya kwanza, waliendelea kumpinga daima. Hali yao ya kumkataa Roho ilifika katika hali yake ya juu katika msalaba wa Kalvari, katika uharibifu wa mji wao, katika kutawanyika kwa taifa katika pepo nne za mbinguni.

Tazama, Kristo alijitahidi jinsi gani kutafuta kuwafungulia Israeli hazina ya thamani ya ukweli! Lakini upofu wao ulikuwa mkubwa kiasi kwamba ilikuwa haiwezekani **(242)** kufunua kwao ukweli kuhusu ufalme wake. Waling'ang'ania mafundisho ya kanisa lao na maadhimisho yasiyo na faida wakati ambapo ukweli wa mbinguni ulikuwa unasubiri ukubali wao. Walitumia pesa zao kwa ajili ya maganda na makapi, wakati mkate wenyewe wa

uzima ulikuwa mahali pale walipokuwa. Kwa nini hawakuliendea neno la Mungu, na kuchunguza kwa makini ili wajue kwamba walikuwa katika makosa? Maandiko ya Agano la Kale yalitamka wazi wazi kila kitu kuhusu huduma ya Kristo, na alinukuu tena na tena kutoka katika manabii, na akatangaza kwamba, "Leo maandiko haya yametimia masikioni mwenu." Ikiwa wangeyachunguza Maandiko kwa uaminifu, wakileta nadharia zao katika kipimo cha neno la Mungu, Yesu asingehitaji kulia kwa sababu ya hali yao ya kutojutia makosa. Asingelazimika kutangaza kwamba, "Angalieni, mmeachiwa nyumba yenu!" Luka 13:35. Walipaswa wawe wamevielewa vithibitisho vya Umasihi wake, na huenda wangeepusha janga lile lililokuwa linaukabili mji wao wa kifahari. Lakini akili za Wayahudi zilikuwa zimefanywa kuwa finyu kwa sababu ya misimamo yao. Mafundisho ya Kristo yaliwaonyesha mapungufu katika tabia zao, na yaliwataka watubu. Kama wangekubali mafundisho yake, lazima matendo yao yangebadilishwa, na matakwa yao yangetoweshwa. Ili kuweza kutukuzwa na mbingu, lazima watu waachane na heshima kutoka kwa watu. Ikiwa wangetii maneno ya rabi huyu aliye mpya, iliwapasa kwenda kinyume na mawazo ya wajuaji wakubwa wa falsafa na walimu wa wakati wao.

Ukweli ulikuwa haupendwi na wengi mnamo wakati wa Yesu. Haupendwi na wengi hata mnamo siku zetu hizi. Haujapata kupendwa tena na wengi tangu pale Shetani alipompatia mwanadamu kwa mara ya kwanza hali ya kutoupenda kwa kumletea hadithi za uongo zinazomwelekeza katika kujitukuza binafsi. Je, leo hatukutani na nadharia na mafundisho ya dini ambayo hayana msingi katika neno la Mungu? Watu wanayang'ang'ania kwa nguvu kama Wayahudi walivyofanya kuhusu mapokeo yao.

Viongozi wa Wayahudi walikuwa wamejawa na kiburi cha kiroho. Tamaa yao ya kujitukuza wenyewe ilijidhihirisha hata katika huduma za patakatifu. Walipenda viti vya juu sana katika sinagogi. Walipenda kusalimiwa masokoni, na walipendezwa na midomo ya watu iliyotoa sauti zinazotukuza majina ya vyeo vyao. Kadiri kujitoa halisi kulivyopungua, ndivyo walivyoongezeka kuwa na wivu zaidi katika kyapenda mapokeo na maadhimisho yao ya kidini.

Kwa kuwa uelewa wao ulitiwa giza kwa sababu ya tamaa binafsi, hawakuweza kuona upatanifu kati ya nguvu ya maneno ya Kristo yenye mguso mkuu na maisha yake ya unyenyekevu. Hawakutambua kwamba ukuu halisi hauna uhusiano na maonyesho ya mwonekano wa nje. Umaskini wa mtu huyu ulionekana kutokuendana kabisa na madai yake kuwa ni Masihi. Walihoji kwamba, Ikiwa alikuwa vile alivyodai kuwa, kwa nini hakujionyesha hivyo kwa mwonekano? Kama aliridhika kutokuwa na jeshi lenye silaha, hatima ya taifa lao **(243)** ingekuwaje? Ikiwa uwezo na utukufu uliosibiriwa kwa muda mrefu ndio huu utawezaje kuyaleta mataifa chini ya utawala wa mji huu wa Wayahudi? Je, makuhani hawakuwa wamefundisha kwamba Israeli angeitawala dunia yote? Na je, ingewezekana kwamba walimu wakubwa wa dini walikuwa na mafundisho ya makosa?

Lakini si kwamba kukosekana kwa utukufu wa nje katika maisha ya Yesu ndiko hasa kulisababisha wamkatae. Alikuwa na udhihirisho wa usafi, wakati wao walikuwa si safi. Aliishi miongoni mwa wanadamu akiwa na uadilifu usio na doa. Maisha yake yasiyolaumiwa kitu yalimlika nuru katika mioyo yao. Uaminifu wake ulifunua kutokuwa waaminifu kwao. Nuru ile ilidhihirisha wema wao wa bandia, na ilionyesha uovu ndani yao. Nuru kama hiyo ilikuwa isiyokaribishika.

Ikiwa Kristo angewavutia Mafarisayo, na kama angesifia elimu yao na msimamo wao wa kidini, wangemkubali kwa furaha. Lakini alipoongelea habari za ufalme wa mbinguni kama vile ni kuwapa rehema wanadamu wote, alikuwa analeta dini ambayo ilikuwa haivumiliki kwao. Kielelezo chao na mafundisho yao havikupata kuifanya ibada yao kwa Mungu kuwa kitu cha kutumainiwa. Walipoona Yesu akijali watu ambao wao waliwachukia na kuwakatalia mbali, hasira ziliamshwa katika mioyo yao ya kiburi. Licha ya kujigamba kwao kwamba wako chini ya "Simba wa kabila la Yuda" (Ufunuo 5:5), Israeli atainuliwa juu ya mataifa yote, wangestahimili mfadhaiko wa kuvunjika kwa matarajio yao kuliko kustahimili makemeo ya Kristo kwa dhambi zao, na kemeo lilifanywa na hali yake ile ya usafi.

# Sura ya 25

## Wito Kando ya Bahari

[Sura hii imejengwa katika Mathayo 4:18-22; Marko 1:16-20; Luka 5:1-11.]

Nuru ya pambazuko la asubuhi ilikuwa inaanza penye Bahari ya Galilaya. Wanafunzi, wakiwa wamechoshwa na kazi isiyo na mafanikio ya usiku kucha, walikuwa bado wako katika vyombo vyao vya kuvulia samaki baharini. Yesu alikuwa amekuja kupata nafasi ya utulivu kandokando ya maji. Wakati wa asubuhi na mapema alitarajia kupata wasaa wa kupumzika mbali na makutano waliomfuata siku hadi siku. Lakini muda si muda watu wakaanza kukusanyika kwake. Idadi yao iliongezeka ghafla, kiasi kwamba alisongwa pande zote. Wakati huo wanafinzi wale walikuwa wamekuja nchi kavu. Ili kuondokana na msongamano wa makutano, Yesu aliingia katika chombo cha Petro, na kumtaka akisukume kidogo kutoka pale pwani. Mahali hapa Yesu angeonekana na kusikika vizuri zaidi kwa watu wote, na aliwafundisha makutano waliokuwa ufukoni akiwa katika chombo kile.

Hii ilikuwa ni mandhari nzuri kiasi gani kwa malaika; Kamanda wao mtukufu akiwa amekaa katika mtumbwi wa mvuvi, akiyumba-yumba kwa sababu ya mawimbi, na akitangaza habari njema za wokovu kwa umati uliokuwa ukisikiliza ukiwa umesogea mpaka kwenye ukingo wa maji! Yeye aliyekuwa Mtukufu wa mbinguni alikuwa anatangza mambo makuu ya ufalme wake katika anga la wazi, kwa wakati wa kawaida. Lakini hakuweza kupata madhari inayofaa kwa kazi zake zaidi ya hii. Ziwa, milima, mashamba **(245)** yaliyotawanyika, miale ya jua iliyoijaza dunia, vyote vilifanya vielelezo vya kufafanulia masomo yake na kuyaweka katika akili za watu. Na hakuna somo la Kristo lililopotea bila kuzaa matunda. Kila ujumbe kutoka midomoni mwake ulikuja kwa watu kadhaa kama uzima wa milele.

Kila wakati watu waliongezeka pale pwani. Vikongwe waliokuwa wakitembea na mikongojo yao, wakulima majasiri kutoka milimani, wavuvi waliotoka katika kazi zao za ziwani, wafanya biashara na marabi, matajiri na wasomi, wazee na vijana, wakiwaleta wagonjwa wao na wenye shida, wakisongamana kusikia maneno ya Mwalimu wa kimbingu. Manabii walikuwa wametazamia mandhari kama hizi, na wakaandika hivi:
" Nchi ya Zabuloni na nchi ya Naftali, Njia ya bahari, ng'ambo ya Yordani, Galilaya ya mataifa,
Watu wale waliokaa katika giza Wameona mwanga mkuu,
Nao waliokaa katika nchi na uvuli wa mauti Mwanga umewazukia."

Ukiacha umati huu uliokuwa katika pwani ya Genesareti, katika mahubiri yake Yesu alikuwa na wasikilizaji wengine mawazoni mwake. Akiangalia mbali katika vizazi vijavyo, aliona watu waaminifu wakiwa gerezani na katika kumbi za hukumu, katika majaribu na upweke na mateso. Kila hali ya mwonekano wa furaha na mapambano na kutatanika ilikuwa wazi machoni pake. Kwa maneno yaliyotamkwa kwa wale waliokuwa wamekusanyika pale, alikuwa anawaeleza na hawa watu wengine wa baadaye maneno ambayo yangewajia yakiwa kama ujumbe wa tumaini wakati wa majaribu, ya kufariji wakati wa huzuni, na ya nuru ya mbinguni wakati wa giza. Kwa njia ya Roho Mtakatifu, sauti ile iliyokuwa ikinena kutoka katika mtumbwi wa mvuvi kwenye Bahari ya Galilaya, ingesikika ikitamka amani katika mioyo ya wanadamu mpaka mwisho wa wakati.

Hotuba iliisha, Yesu akamgeukia Petro, na kumtaka aende baharini, na ashushe nyavu ili kuvua samaki. Petro alikosa matumaini. Katika usiku wote hakuwa amepata kitu. Katika saa za upweke alikuwa ametafakari kuhusu hatima iliyomfikia Yohana Mbatizaji, alivyokuwa amehangaika peke yake kule katika gereza. Alikuwa amefikiria kuhusu matarajio yapatikanayo kwa Yesu na wanafunzi wake, kuhusu kukosekana kwa mafanikio ya utume kule Uyahudi, na hila ya makuhani na marabi. Hata fani yake tu ilikuwa imeshindwa kumletea mafanikio, na alipokuwa amekesha na nyavu zisizo na kitu, hatima yake ya usoni ilionekana kuwa na giza na ya kukatisha tamaa. Akasema, "Bwana mkubwa, tumefanya kazi ya kuchosha usiku kucha, tusipate kitu; lakini kwa neno lako nitazishusha nyavu."

**(246)** Usiku ndio uliokuwa wakati unaofaa tu kuvua samaki kwa nyavu katika maji ya ziwa. Baada ya kusumbuka usiku wote bila mafanikio, ilionekana kama jambo lisilotarajiwa kushusha nyavu mchana; lakini Yesu alikuwa ametoa amri, na upendo wa wanafunzi kwa Mwalimu wao uliwafanya watii. Simoni pamoja na ndugu yake wakashusha nyavu. Walipojaribu kuzivuta, kiasi cha samaki walionaswa kilikuwa kikubwa sana kiasi

kwamba nyavu zilianza kukatika. Walilazimika kumwita Yakobo na Yohana kuja kusaidia. Baada ya kupata samaki hao, mitumbwi yote miwili ilikuwa na mzigo mzito sana kiasi cha kuwa katika hatari ya kuzama.

Lakini Petro hakuwa anafikiria sasa kuhusu mitumbwi na mzigo ule. Mwujiza huu, zaidi ya mwingine wowote aliopata kushuhudia, kwake ulikuwa ni udhihirisho wa uwezo wa kimbingu. Ndani ya Yesu alimwona Yeye anayeshikilia maumbile yote ya asili katika himaya yake. Uwepo wa uungu ulidhihirisha hali yake yeye ya kutokuwa mtakatifu. Upendo wa Mwalimu wake, aibu ya kutokuamini kwake, utambuzi wa hali ya Kristo ya kujishusha, zaidi ya yote, hisia ya kuwa mchafu mbele ya usafi ule usio na mwisho, vilimfanya kutekewa. Wakati wenzake wakishughulikia vile vilivyokuwa katika vyavu, Petro alianguka miguuni pa Mwokozi, na kusema, "Ondoka kwangu, kwa kuwa mimi ni mtu mwenye dhambi, Bwana."

Ilikuwa ni kwa utakatifu wa kimbingu kama huo uliomfanya Danieli kuanguka kama mtu aliyekufa mbele ya malaika wa Mungu. Maana alisema, "Uzuri wangu uligeuzwa ndani yangu kuwa uharibifu, wala sikusaziwa nguvu." Hivyo ndivyo Isaya pia alivyouona utukufu wa Bwana, akasema kwa mshangao, "Ole wangu! Kwa maana nimepotea; kwa sababu mimi ni mtu mwenye midomo michafu, nami ninakaa kati ya watu wenye midomo michafu; na macho yangu yamemwona Mfalme, Bwana wa majeshi." Danieli 10:8; Isaya 6:5. Ubinadamu, pamoja na udhaifu wake na dhambi, uliletwa katika ukinzani kati yake na ukamilifu wa uungu, naye akajihisi mwenye kupungua na asiye mtakatifu kabisa. Hivyo ndivyo ambavyo imekuwa kwa watu wote waliopewa kuona ukuu na uweza wa Mungu.

Petro alihamaki, "Ondoka kwangu, kwa kuwa mimi ni mtu mwenye dhambi, Bwana;" lakini bado aling'ang'ania miguu ya Yesu, akihisi kwamba hawezi kuondokana na Yesu. Yesu alimjibu, "Usiogope, tangu sasa utakuwa ukivua watu." Ilikuwa baada ya Isaya kuuona utakatifu wa Mungu na kutokustahili kwake ndipo alipokabidhiwa ujumbe wa kimbingu. Ni baada ya Petro kuongozwa katika kutojiamini na kutegemea nguvu za kimbingu ndipo alipopokea wito wa kuingia kazini kwa ajili ya Kristo.

Mpaka wakati huu hakuna hata mwanafunzi mmoja aliyekuwa amejiunga kikamilifu kuwa mtenda-kazi pamoja na Yesu. Walikuwa wameshuhudia miujiza yake mingi, na walikuwa wamesikiliza mafundisho yake; lakini walikuwa hawajaacha kabisa kazi zao za nyuma. **(249)** Kufungwa kwa Yohana Mbatizaji kulikuwa kumekuwa kitu cha kufadhaisha sana kwao. Ikiwa ile ndiyo ingekuwa matokeo ya utume wa Yohana, wangekuwa na matumaini kidogo sana na Masihi wao huyu, huku viongozi wote wa dini wakiwa kinyume cha Masihi huyo. Katika mazingira hayo ilikuwa nafuu kwao kurudi kwanza katika kazi yao ya uvuvi. Lakini sasa Yesu aliwaita waache maisha yao ya kabla, na kuunganisha nia yao na yake. Petro alikuwa amekubali wito ule. Baada ya kuja ufukweni, Yesu aliwaita wanafunzi wake wengine watatu, akisema, "Nifuateni, nami nitawafanya kuwa wavuvi wa watu." Mara wakaacha vyote, wakamfuata.

Kabla ya kuwataka waache nyavu zao na mitumbwi ya kuvulia, Yesu alikuwa amewahakikishia kwamba Mungu angewapatia mahitaji yao. Matumizi ya mtumbwi wa Petro kwa kazi ile ya injili yalikuwa yamelipiwa sana. Yeye aliye "mwenye utajiri kwa wote wamwitao," amesema, "Wapeni watu vitu, nanyi mtapewa; kipimo cha kujaa na kushindiliwa, na kusukwa-sukwa hata kumwagika." Warumi 10:12; Luka 6:38. Kwa kipimo hiki alikuwa ameipatia thawabu huduma ya mwanafunzi wake huyu. Na kila kafara inayofanywa katika kazi yake itafidiwa kulingana na "wingi wa neema yake upitao kiasi." Waefeso 3:20; 2:7.

Wakati wa usiku ule wa huzuni ziwani, walipokuwa wametengwa na Kristo, wanafunzi walikuwa wamekandamizwa na hali ya kutoamini, na uchovu wa masumbuko ya kazi isiyo na mafanikio. Lakini uwepo wake uliwasha imani yao, na uliwaletea furaha na mafanikio. Hivyo ndivyo ilivyo kwetu; mbali na Kristo, kazi zetu hazina mafanikio, na ni rahisi kukata tamaa na kunung'unika. Lakini anapokuwa karibu, na tunapofanya kazi kulingana na maelekezo yake, tunafurahia ushahidi wa uweza wake. Kazi ya Shetani ni kukatisha tamaa roho zetu; kazi ya Kristo ni kuhuisha imani na tumaini.

Fundisho la kina ambalo mwujiza ule ulileta kwa wanafunzi wale ni fundisho kwetu pia, - kwamba Yeye ambaye neno lake liliweza kukusanya samaki kutoka baharini angeweza pia kugusa mioyo ya watu, na kuwavuta kwa kamba za upendo wake, ili ya kwamba watumishi wake wapate kuwa "wavuvi wa watu."

Wale wavuvi wa Galilaya walikuwa watu wanyenyekevu na wasio wasomi; lakini Kristo, nuru ya ulimwengu, aliweza sana kuwastahilisha kushika nafasi ambazo alikuwa amewachagulia kufanya. Yesu hakudharau elimu;

maana inapotawaliwa na upendo wa Mungu, na kujitoa katika kazi yake, hali ya kuwa na kisomo ni mbaraka. Lakini aliwapita wenye hekima wa wakati wake, kwa sababu walikuwa wakijiamini wenyewe kiasi kwamba hawakuweza kuwaonea huruma watu watesekao, na hawakuwa tayari kuwa watenda-kazi pamoja na Mtu wa Nazareti. Wakiwa katika misimamo ya nadharia zao waliibeza hali ya wao kufundishwa na Kristo. Bwana Yesu hutafuta ushirikiano kutoka kwa wale ambao wanakuwa **(250)** mifereji isiyo na vizuizi kwa ajili ya kupitisha neema yake kwao. Jambo la kwanza ambalo wote wanaotaka kufanya kazi pamoja na Mungu wanahitaji kujifunza ni somo la kutojiamini binafsi; hapo ndipo wanakuwa tayari kuingiziwa tabia ya Kristo. Hali hii haipatikani kwa kuelimishwa katika shule kuu za kisayansi. Ni tunda la hekima inayopatikana kutoka kwa mwalimu wa kimbingu peke yake.

Yesu alichagua wavuvi kwa sababu hawakuwa wameelimishwa katika mila na desturi zenye makosa za wakati wao. Walikuwa watu wenye uwezo wa kienyeji, na walikuwa wanyenyekevu na wanaofundishika, - watu ambao angewaelimisha kwa ajili ya kazi yake. Katika mienendo ya kawaida ya maisha wapo watu wengi ambao wako kama mtu yule anayetembea katika shughuli za mahangaiko yake ya kila siku, akiwa hajui kwamba anao uwezo ambao, kama ungeletwa katika utendaji, ungemwinua hadi kumweka katika kiwango kilicho sawasawa na cha wale wanaoheshimika sana ulimwenguni. Mguso wa mkono wenye ujuzi unahitajika ili kuziinua fahamu hizi zilizolala. Watu wa namna hiyo ndio walioitwa na Yesu ili kuwa watenda-kazi pamoja naye; na aliwapa nafasi ya kujumuika pamoja naye. Kamwe hakujapata kuwepo watu wakuu wa ulimwengu kama mwalimu huyo. Wakati wanafunzi walipokuja wakitoka katika mafunzo yaliyofanywa na Mwokozi, hawakuwa wasio na elimu tena wala wasio na ustaarabu. Walikuwa wamekuwa kama Yeye katika akili na tabia, na watu walijua kwamba walikuwa wamekuwa na Yesu.

Kazi kubwa ya elimu hasa si kupitisha maarifa kutoka kwa mtu kwenda kwa mwingine; bali ni kuleta ndani ya mtu nguvu ile ya uhai ambayo inapatikana kupitia kule kugusana kwa nia ya dhamira na nia ya dhamira, na nafsi na nafsi. Maisha tu ndiyo yanayoweza kuzaa maisha. Sasa walikuwa na bahati kiasi gani, basi, wale ambao kwa miaka mitatu kila siku walikuwa katika kugusana na yale maisha ya kimbingu ambayo kutoka kwayo ulitiririka msukumo wa nguvu ya uzima ambayo imeubariki ulimwengu! Zaidi ya washirika wake wote, Yohana yule mwanafunzi aliyependwa sana alijisalimisha katika nguvu ya uzima huo wa ajabu. Anasema, "Uzima huo ulidhihirika, nasi tumeona, tena twashuhudia, na kuwahubiri ninyi ule uzima wa milele, uliokuwa kwa Baba, ukadhihirika kwetu." "Katika utimilifu wake sisi sote tulipokea, na neema juu ya neema." 1 Yohana 1:2; Yohana 1:16.

Katika mitume wa Bwana wetu hakukuwa na chochote cha kuwaletea utukufu wao wenyewe. Ilidhihirika kwamba mafanikio ya kazi zao yalikuwa kwa ajili ya Mungu. Maisha ya watu hawa, tabia zilizokuzwa kwao, na matendo makuu ambayo Mungu alitenda kupitia wao, ni ushuhuda wa yale atakayofanya kwa wote ambao wanafundishika na wanatii.

Yeye ampendaye Kristo zaidi atafanya kiasi kikubwa zaidi cha mambo mema. Hakuna ukomo wa kutumika kwa mtu ambaye, kwa kuweka kando ubinafsi, **(251)** anatoa nafasi kwa ajili ya Roho Mtakatifu kutenda kazi moyoni mwake, na anaishi maisha ambayo yametolewa wakfu kwa Mungu. Ikiwa watu watastahimili kuwa na nidhamu iliyo muhimu, pasipo kulalamika wala kuzimia njiani, Mungu atawafundisha kila saa na kila siku. Anatamani kuifunua neema yake. Ikiwa watu wataondoa vizuizi, atamwaga maji ya wokovu kwa njia ya vijito vingi kupitia mifereji ya kibinadamu. Ikiwa watu wangetiwa moyo kutenda kwa unyenyekevu wema wote wanaoweza kutenda, ikiwa mikono iwazuiayo isingekuwa imewekwa juu yao ili kuminya ari yao, kungekuwa na mamia ya watenda-kazi wa Kristo mahali ambapo hakuna hata mmoja.

Mungu huwachukua watu kama walivyo, na huwaelimisha kwa ajili ya kazi yake, ikiwa watajisalimisha kwake. Roho wa Mungu, apokelewaye moyoni, ataharakisha fahamu zote. Chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu, nia ya dhamira ambayo imesalimishwa kikamilifu kwa Mungu hukuzwa katika upatanifu, na inatiwa nguvu ili kupambanua na kutimiza matakwa ya Mungu. Tabia dhaifu isiyo na msimamo hubadilishwa na kuwa yenye nguvu na ya msimamo. Kuendelea kujitoa kunaweka uhusiano wa karibu kati ya Yesu na mwanafunzi wake kiasi cha kumfanya Mkristo kuwa kama Yeye katika mawazo na tabia. Kupitia mwunganiko na Kristo atakuwa na mtazamo wa wazi na mpana. Utambuzi wake utakuwa wenye kupenya, maamuzi yatakuwa yaliyo sawa. Yeye

anayetaka kuwa katika kazi ya Kristo anaharakishwa na nguvu itoayo uzima ya Jua la Haki ili apate kuwezeshwa kuzaa matunda mengi kwa ajili ya utukufu wa Mungu.

Watu wenye elimu ya juu katika sanaa na sayansi mbalimbali wamejifunza mafunzo ya thamani kutoka kwa Wakristo wenye maisha ya unyenyekevu ambao ulimwengu uliwaona kama wasiosoma. Lakini hawa wanafunzi wasiotambuliwa walikuwa wamepata elimu katika shule ya juu mno kuliko shule zote. Walikuwa wamekaa miguuni pa Yeye aliyenena kwa namna ambayo "hajanena kamwe mtu yeyote."

## Sura ya 26

# Kule Kapernaumu

Kule Kapernaumu Yesu alizoea kuwa na safari za mara kwa mara akienda na kurudi, na mji huo ulikuja kujulikana kama "mjini kwao." Ulikuwa kwenye pwani ya Bahari ya Galilaya, na karibu na mipaka ya tambarare nzuri za Genesareti, kama si mipakani kabisa.

Bonde la kina la ziwa hili linaipatia tambarare hii inayopakana na pwani hali ya hewa nzuri upande wa kusini. Mnamo siku za Kristo hapa palistawi miti ya mitende na mizeituni, kulikuwa na bustani za matunda na mashamba ya mizabibu, mashamba ya kijani, na maua yaliyochanua yaking'aa kwa uzuri, vyote vikinyweshwa na vijito vinavyoshuka kwenye majabali. Pwani za ziwa lile, na vilima vinavyolizunguka kwa mbali, vilikuwa na miji na vijiji vilivyotawanyika. Ziwa lilikuwa limejawa na mitumbwi ya kuvulia. Kila mahali kulikuwa na mchanganyiko wa shughuli za maisha.

Mji wa Kapernaumu ulikidhi hali ya kuwa kitovu cha kazi ya Mwokozi. Ukiwa kwenye barabara kuu itokayo Dameski kwenda Yerusalemu na Misri, na kwenda Bahari ya Mediterania, ilikuwa mahali rahisi kusafiri. Watu kutoka sehemu nyingi walipita katika mji huo, au walipumzikia hapo kabla ya kuendelea na safari zao. Mahali hapa Yesu aliweza kukutana na watu wa mataifa yote na wa matabaka yote, matajiri na watu wakubwa pamoja na maskini na watu wa hali ya chini, na mafundisho yake yangeweza kupelekwa katika nchi nyingine na katika nyumba nyingi. **(253)** Hivyo moyo wa kuchunguza unabii ungeamshwa, mawazo yangeelekezwa kwa Mwokozi, na kazi yake ingefikishwa ulimwenguni.

Licha ya kitendo cha Sanhedrin kumpinga Yesu, injili ilisubiri kazi yake kwa hamu. Mbingu yote ilikuwa imesisimuka kwa hamu. Malaika walikuwa wanatayarisha njia kwa ajili ya kazi yake, wakiitembelea mioyo, na kuivuta kuja kwa Mwokozi.

Mtoto wa diwani aliyekuwa ameponywa na Yesu katika mji wa Kapernaumu alikuwa ni shahidi wa uwezo wake. Na diwani huyo pamoja na nyumba yake waliidhihirisha imani yao kwa furaha. Ilipojulikana kwamba Mwalimu yu miongoni mwao, mji mzima uliamka. Makutano walimjia. Siku ya Sabato watu walifurika katika sinagogi kiasi cha wengi kurudi, baada ya kushindwa kuingia.

Wote waliomsikiliza Mwokozi "walishangaa mno kwa mafundisho yake, kwa kuwa neno lake lilikuwa na uwezo." "Alikuwa akiwafundisha kama mtu mwenye amri, wala si kama waandishi." Luka 4:32; Mathayo 7:29. Mafundisho ya waandishi na wazee yalikuwa yamepoa na ya mazoea, kama somo la kujifunza kwa kukariri. Kwao neno la Mungu halikuwa na nguvu muhimu. Badala yake, mawazo na mapokeo yao wenyewe ndiyo yaliyofundishwa. Katika desturi zao za vipindi vya ibada walijifanya kufafanua sheria, lakini hakuna uvuvio kutoka kwa Mungu ambao uliamsha mioyo yao au mioyo ya wasikilizaji wao.

Yesu hakuwa na la kufanya kuhusu mada mbalimbali ambazo hazikuwa na muafaka miongoni mwa Wayahudi. Kazi yake ilikuwa ni kuwasilisha ukweli. Maneno yake yalimwaga mafuriko ya nuru kwenye mafundisho ya wazee na manabii, na Maandiko yaliwajia watu kama ufunuo mpya. Kamwe wasikilizaji wake hawakuwa wamepata kuelewa kiasi kile maana ya kina ya neno la Mungu.

Yesu alikutana na watu katika mahali pao, kama mtu ambaye anajua matatizo yao. Aliufanya ukweli kuwa mzuri kwa kuuwasilisha kwa njia ya moja kwa moja na nyepesi. Lugha yake ilikuwa safi, ikiwa imechujwa na ya kueleweka kama maji ya mto yatiririkayo. Sauti yake ilikuwa kama muziki kwa watu wale waliokuwa wamesikiliza sauti za kujirudia-rudia za marabi. Lakini licha ya kuwa mafundisho yake yalikuwa rahisi, aliongea kama mtu mwenye mamlaka. Sifa hii iliyaweka mafundisho yake kuwa tofauti na wengine wote. Marabi waliongea kwa mashaka na kusita, kama vile Maandiko yangeweza kutafsiriwa kitu kimoja au kinyume chake kabisa. Wasikiliza wao walikuwa katika mashaka makubwa kila siku. Lakini Yesu alifundisha Maandiko kama kitu chenye mamlaka isiyohojiwa. Somo lolote la Maandiko, lilifundishwa kwa nguvu, kama vile maneno yake yalikuwa yasiyopingwa.

**(254)** Ingawa alifundisha kwa msisitizo, hakulazimisha. Aliongea kama mtu ambaye ana kusudi mahsusi la kutimiza. Alikuwa anaonyesha uhalisia wa ulimwengu udumuo. Katika kila mada Mungu alifunuliwa. Yesu alitafuta kuvunja vivutio vya tamaa vinavyowafanya watu wazame katika mambo ya dunia. Aliyaweka mambo ya maisha haya mahali panapostahili, kwamba ni mambo yanayotiishwa chini ya yale mambo ya milele; lakini hakupuuza umuhimu wake. Alifundisha kwamba mbingu na dunia zimeunganishwa pamoja, na ya kwamba kufahamu ukweli wa kimbingu huwaanda watu kutekeleza majukumu yao ya maisha ya kila siku. Aliongea kama mtu anayeijua mbingu, mwenye uelewa wa uhusiano wake na Mungu, lakini bado akitambua mwunganiko wake na kila mtu aliye katika jamaa ya wanadamu.

Ujumbe wake wa rehema ulikuwa tofauti-tofauti ili kukidhi haja ya walioupokea. Alijua "jinsi ya kumtegemeza kwa maneno yeye aliyechoka" (Isaya 50:4); maana rehema ilimwagwa midomoni mwake, ili ya kwamba aifikishe kwa watu katika namna ya kuvutia mno ikiwa kama hazina ya ukweli. Alikuwa na busara ya kupambana na mawazo potofu, na aliwashangaza kwa kutumia vielelezo vilivyovuta usikivu wao. Kwa kutumia ubunifu huo aliufikia moyo. Vielelezo vyake vilipatikana katika maisha ya kila siku, na ingawa vilikuwa rahisi ndani yake vilikuwa na mafundisho ya kina. Ndege wa angani, maua ya kondeni, mbegu, mchungaji na kondoo, - kwa kutumia vitu hivi Yesu alieleza ukweli wa milele; na daima baada ya pale, wakati wasikilizaji wake walipoona vitu hivyo vya asili, walikumbuka maneno yake. Vielelezo vya Kristo vilirudia masomo yake wakati wote.

Kamwe Kristo hakuwasifia watu. Kamwe hakusema jambo ambalo lingeinua sifa na maarifa ya mtu, wala hakuwasifu kwa uvumbuzi wao wa busara; bali watu wenye upotofu mkubwa waliojikinai walipokea mafundisho yake, na kuona kwamba yanapima hekima yao. Walishangazwa na ukweli wa kiroho uliodhihirishwa kwa lugha rahisi. Wale waliokuwa wasomi wakubwa sana walivutiwa na maneno yake, na wale wasio wasomi walinufaika kila mara. Alikuwa na ujumbe kwa ajili ya wasio wasomi; na aliwafanya hata wapagani kuelewa kwamba alikuwa na ujumbe kwa ajili yao.

Huruma yake ilileta mguso wa uponyaji kwa mioyo iliyochoka na kutaabika. Hata katikati ya misukosuko ya maadui wenye hasira alizungukwa na hali ya amani. Uzuri wa uso wake, tabia yake ya upendo, zaidi ya yote, upendo uliodhihirishwa na macho na sauti, uliwavuta kwake wote ambao hawakuwa na ugumu wa kuamini. Isingekuwa roho yake tamu na ya huruma iliyoonyeshwa katika kutazama kwake na kuongea kwake, asingevutia kusanyiko kubwa vile ilivyokuwa. Wale walioteseka ambao walikuja kwake walijisikia kama vile ameunganisha **(255)** hisia zake na zao kama rafiki yao mpendwa na mwaminifu, na walitamani kujua zaidi kuhusu ukweli aliofundisha. Mbingu ililetwa karibu. Walitamani kukaa mahali alipo, ili kwamba faraja ya upendo wake iwe pamoja nao wakati wote.

Yesu aliangalia kwa shauku nyuso za wasikilizaji wake zilizokuwa zinabadilika. Nyuso zilizoonyesha hamu na raha zilimpa hali ya kuridhika. Kadiri ambavyo mishale ya ukweli ilichoma moyo, ikivunjilia mbali vizuizi vya ubinafsi, na kuleta hali ya kujutia mabaya, na hatimaye kuleta moyo wa shukrani, Yesu alifurahi. Macho yake yalipopita katika makutano ya wasikilizaji wake, na akatambua humo nyuso ambazo alikuwa ameshaziona kabla, alipatwa na furaha kubwa. Ndani yao aliona watu ambao wangetumainiwa kuwa wana wa ufalme wake. Lakini wakati ukweli, uliosemwa wazi, ulipogusa miungu waliyokuwa wameshikilia, aliona mwonekano tofauti, ubaridi, hali ya kutishwa, kuonyesha kwamba nuru haikukaribishwa. Alipowaona watu wakikataa ujumbe wa amani, moyo wake ulichomwa mpaka ndani sana.

Katika hekalu Yesu alizungumzia ufalme ule aliokuja kuanzisha, na kazi yake ya kuwaweka huru mateka wa Shetani. Alikatizwa na kelele ya kushtua. Mtu aliyepagawa alikimbia mbele akitoka katikati ya watu, huku akilia, "Acha! Tuna nini nawe, Yesu wa Nazareti? Umekuja kutuangamiza? Nakujua u nani, Mtakatifu wa Mungu."

Mambo yote sasa yaliharibika na kuvurugika. Usikivu wa watu ulihama kutoka kwa Kristo, na maneno yake hayakusikika. Hili lilikuwa kusudi la Shetani kumpeleka yule mhanga katika sinagogi. Lakini Yesu alimkemea yule pepo, akisema, "Fumba kinywa, mtoke. Ndipo yule pepo akamwangusha katikati, akamtoka asimdhuru neno."

Akili ya mhanga huyu mnyonge ilikuwa imetiwa giza na Shetani, lakini katika uwepo wa Mwokozi mwale wa nuru ulikuwa umepenya giza hilo. Aliamshwa kutafuta kuwa huru kutoka katika utawala wa Shetani; lakini pepo alishindana na uwezo wa Kristo. Wakati yule mtu alipojaribu kuomba msaada kwa Yesu, roho mchafu aliweka

maneno mdomoni mwake, na akalia kwa masumbuko na hofu. Yule aliyepagawa alitambua japo kidogo kwamba alikuwa mbele yake Yeye ambaye angeweza kumweka huru; lakini wakati alipojaribu kuujia mkono ule wenye uweza, utashi wa pepo ulimzuia, maneno ya huyo pepo yalitamkwa kupitia kinywa cha mtu yule. Kulikuwa na pambano la kutisha kati ya nguvu za Shetani na hamu ya mtu yule kutaka kuwa huru.

**(256)** Yeye aliyekuwa amemshinda Shetani katika majaribu ya kule jangwani alileta tena mbele ya adui yake yule uso kwa uso. Pepo alikita nguvu zake zote ili kuendelea kumtawala mhanga yule. Kusalimu amri hapa ingekuwa ni kumpa Yesu ushindi. Ilionekana kama vile ni lazima adui yule aliyemtesa mtu yule asababishe maisha yake kupotea katika pambano lile dhini ya adui aliyeharibu utu wake. Lakini Mwokozi alitamka kwa amri, na kumweka huru yule mateka. Yule mtu aliyekuwa amepagawa na pepo alisimama mbele ya watu waliokuwa katika mshangao akiwa na furaha ya kuwekwa huru. Hata pepo yule alikuwa ametambua uweza wa kimbingu wa Mwokozi.

Yule mtu alimsifu Mungu kwa ukombozi ule. Jicho lake lile lililokuwa likitazama likiwa na moto wa wazimu, sasa liling'aa likiwa na ufahamu, likifurika machozi ya shukrani. Watu walikuwa wameduwazwa kwa mshangao. Mara waliporejewa na hali ya kuzungumza, waliambiana wao kwa wao kwa mshangao, "Nini hii? Ni elimu mpya! Maana kwa uweza awaamuru hata pepo wachafu, nao wamtii!" Marko 1:27.

Siri ya sababu ya mateso yaliyokuwa yamemfanya mtu huyu kuwa kioja cha kuogopesha machoni pa rafiki zake na kuwa mzigo kwake ilikuwa katika maisha yake mwenyewe. Alikuwa ametekwa na anasa za dhambi, na alikuwa amefikiria kuyafanya maisha yawe ya burudani kubwa. Hakuota kwamba angeleta hofu kwa ulimwengu na fadhaa kwa jamaa yake mwenyewe. Alitumaini kwamba maisha yake yangekuwa ya raha pasipo hatia. Lakini wakati akiwa katika njia hiyo ielekeayo chini, miguu yake ikashuka ghafla. Kukosa kiasi na kufanya upuuzi vilipotosha tabia yake njema ya asili, na Shetani akamtawala kikamilifu.

Majuto ya kujutia hatia yalikuja yakiwa yamechelewa. Wakati alipotaka kutoa mhanga utajiri na anasa ili kupata tena utu wake uliokuwa umepotea, alikuwa hana msaada katika himaya ya yule mwovu. Alikuwa amejiweka mwenyewe katika viwanja vya adui, na Shetani alikuwa amejipatia umiliki wote wa fahamu zake. Mjaribu alikuwa amemvutia kwa maonyesho ya kuvutia; lakini pindi mhanga yule alipokuwa amefika tayari katika himaya ya Shetani, hakuwa na msaada katika ukatili wake, na akawa katika hatari wakati alipojiliwa na hasira yake. Hivyo ndivyo ilivyo kwa wote wanaosalimu amri katika uovu; anasa zinazowavuta mwanzoni huishia katika giza lisilo na tumaini au wazimu wa uharibifu.

Roho ile ile chafu iliyomshawishi Kristo kule jangwani, na ambayo ilimpagaa mtu yule asiyejitawala wa Kapernaumu, iliwatawala Wayahudi wasioamini. Lakini ilipokuwa nao ilijionyesha kuwa na hali ya utauwa, ikitafuta kuwadanganya katika mwelekeo wao wa kumkataa Mwokozi. Hali yao ilikuwa mbaya kuliko hata ya yule aliyepagawa na pepo, maana hawakujisikia kumhitaji Kristo na kwa hiyo walishikiliwa kabisa katika nguvu za Shetani.

**(257)** Kipindi cha huduma ya Kristo miongoni mwa watu kilikuwa cha kuushughulisha sana ufalme wa giza kuliko wakati wowote. Kwa zama na zama Shetani na malaika zake waovu walikuwa wametafuta kutawala miili na roho za watu, kuwaletea dhambi na maumivu; halafu akaelekeza kwa Mungu lawama kwa mabaya yote hayo. Yesu alikuwa anawafunulia watu tabia ya Mungu. Alikuwa anavunja nguvu za Shetani, na kuwaweka huru mateka wake. Maisha mapya na upendo na nguvu kutoka mbinguni vilikuwa vikitembea katika mioyo ya watu, na mfalme wa uovu aliamshwa ili kupambania ukuu wa ufalme wake. Shetani akaamrisha majeshi yake yote, wakashindana na kazi ya Kristo katika kila hatua.

Hivyo ndivyo itakavyokuwa katika pambano kuu la mwisho wa mapambano yote kati ya haki na dhambi. Wakati maisha mapya na nuru na nguvu vikishuka kutoka juu na kuwajia wanafunzi wa Kristo, maisha mapya yatabubujika pia kutoka chini, na kuwatia nguvu mawakala wa Shetani. Nguvu za mwovu zitashikilia kila kitu cha kiulimwengu. Kwa kutumia uzoefu wa werevu uliopatikana katika mapambano karne nyingi, mfalme wa uovu afanya kazi kwa hali ya kuficha mwonekano wake halisi. Anajitokeza akiwa amejivika mwonekano kama wa malaika wa nuru, na makutano watakuwa "wakisikiliza roho zidanganyazo, na mafundisho ya mashetani." 1 Tim. 4:1.

Mnamo siku za Kristo viongozi na waalimu wa Israeli hawakuwa na nguvu za kuipinga kazi ya Shetani. Walikuwa wanapuuza njia pekee ambayo ingewawezesha kusimama dhidi ya roho chafu. Kristo alimshinda mwovu kwa neno la Mungu. Viongozi wa Israeli walijigamba kwamba wao ndio waliokuwa wafasiri wa neno la Mungu, kumbe walikuwa wamelisoma ili tu kukidhi mahitaji ya mila zao, na kusimamia uongozaji wa maadhimisho yaliyowekwa na wanadamu. Kwa ufafanuzi wao walilifanya neno la Mungu kuonyesha vitu ambavyo havikutolewa na Mungu. Mifumo ya kidini waliyotengeneza wenyewe iliyafanya kuwa fumbo mambo ambayo Mungu aliyaweka wazi. Walipigania ustadi katika mambo yasiyo na umuhimu, na wakakana kwa vitendo mambo yaliyo muhimu sana. Kwa hiyo waliongeza kiwango cha kutokuamini. Neno la Mungu liliporwa uwezo wake, na roho wachafu wakaendesha utashi wa watu wale.

**(258)** Historia inajirudia. Huku wakijigamba kwamba wanaheshimu mafundisho ya Biblia, viongozi wa kidini wa siku zetu hizi walio wengi wanaharibu imani kwamba Biblia ni neno la Mungu, wakati Biblia iko wazi kwao. Wanajishughulisha sana katika kulichambua neno, na kuweka maoni yao wenyewe juu ya kauli za Biblia zilizo wazi. Katika mikono yao neno la Mungu linapoteza nguvu ya kuhuisha. Hiyo ndiyo sababu ya kufumuka kwa hali ya kutoamini, na uovu kuongezeka.

Shetani akiisha kuihafifisha Biblia, anawaelekeza watu katika vyanzo vingine vya nuru na nguvu. Kwa njia hiyo anajipenyeza ndani yao kwa hila. Wale wanaogeukia mbali na mafundisho rahisi ya Maandiko na nguvu isadikishayo ya Roho Mtakatifu wanaualika utawala wa mashetani. Hali ya kukosoa na kukisia mambo yahusuyo Maandiko imefungua mlango wa ibada ziitwazo za roho na teosofia – mifumo ya kisasa ya upagani wa kale – kupata mahali pa kusimama hata katika kile kinachoitwa makanisa ya Bwana wetu Yesu Kristo.

Nguvu mbalimbali ziko kazini zikiwa kama njia ya kazi za roho zidanganyazo, zikifanya kazi bega kwa bega na mahubiri ya injili. Watu wengi wako kama mtu anayecheza na nguvu hizo kama kwa kufanya udadisi tu, lakini aonapo ushahidi wa kazi zilizo juu ya uwezo wa kibinadamu, anashawishika zaidi na zaidi, mpaka anatawaliwa na utashi ulio zaidi ya utashi wake mwenyewe. Hawezi kukwepa tena nguvu hiyo ya ajabu.

Ngome za roho zinavunjika. Hana kizuizi tena dhidi ya kutenda dhambi. Mara vizuizi vya neno la Mungu na Roho wake vinapokataliwa, hakuna mtu ajuaye kwamba kiwango chake cha uharibifu kitazama mpaka katika vina vya chini kiasi gani. Dhambi ya siri au hisia kali vinaweza kumshikilia mateka akiwa hana msaada kama alivyokuwa yule mwenye kupagawa wa Kapernaumu. Lakini hali yake si kwamba haina tumaini.

Mbinu tunayoweza kutumia kumshinda yule mwovu ni ile ile iliyotumiwa na Yesu kushinda, – nguvu ya neno. Mungu hatawali akili zetu bila ukubali wetu; bali kama tunatamani kujua na kufanya mapenzi yake, ahadi zake ni zetu: "Mtaifahamu kweli, nayo hiyo kweli itawaweka huru." "Mtu akipenda kuyatenda mapenzi yake, atajua habari ya yale mafunzo." Yohana 8:32; 7:17. Kupitia katika imani juu ya ahadi hizi, kila mtu anaweza kuokolewa kutoka katika mitego ya makosa na kutawaliwa na dhambi.

Kila mtu yu huru kuchagua mamlaka ya kumtawala. Hakuna watu ambao wameshushwa chini sana, hakuna ambao wametiwa aibu sana, isipokuwa ili kwamba waweze kupata ukombozi katika Kristo. Yule aliyepagawa, katika kuomba, aliweza kutamka maneno ya Shetani tu; lakini bado ombi la moyo wake ambalo halikutamkwa lilisikiwa. Hakuna kilio cha moyoni ambacho hakitasikiwa, hata kama inashindikana kukitamka kwa maneno. Wale watakaoridhia kuingia katika mahusiano ya agano na Mungu wa mbinguni hawajaachwa katika nguvu za Shetani au katika udhaifu wao wa **(259)** asili. Wanaalikwa na Mwokozi akisema, "Azishike nguvu zangu, Afanye amani nami; Naam, afanye amani nami." Isaya 27:5. Roho wa giza watapambana kwa ajili ya mtu aliyepata kuwa chini ya miliki yao, lakini malaika wa Mungu watampigania mtu huyo kwa nguvu za kushinda. Bwana anasema, "Je! Aliye hodari aweza kunyang'anywa mateka yake, au jeshi lao waliofungwa halali wataokoka? . . . Bwana asema hivi, Hata jeshi la wafungwa wake aliye hodari watapokonywa mikononi mwake, na mateka yake aliye jabari wataokoka; kwa maana nitateta na yeye atetaye nawe, nami nitawaletea wana wako wokovu." Isaya 49:24, 25.

Wakati makutano katika sinagogi walipokuwa bado wako katika mshangao, Yesu alitoka akaenda kupumzika kidogo nyumbani kwa Petro. Lakini hapa napo pia palikuwa pamefunikwa na kivuli. Mama wa mke wa Petro alikuwa mgonjwa amelala kitandani, akiwa na “homa kali.” Yesu alikemea ugonjwa ule, na mgonjwa akaamka, na akamhudumia Yesu na wanafunzi wake kwa mahitaji yao.

Habari za matendo ya Yesu zilienea haraka katika eneo lote la Kapernaumu. Kwa kuwaogopa marabi, watu hawakudiriki kuja kuponywa siku ya Sabato; lakini muda mfupi tu baada ya jua kutoweka kwa kuzama magharibi kulikuwa na makutano wengi. Kutoka majumbani, madukani, masokoni, wakazi wa mji ule walikuja kusongamana katika kibanda cha hali ya chini ambacho kilitoa hifadhi kwa Yesu. Wagonjwa waliletwa wakiwa kwenye viti vyao, walikuja wakijikongoja kwenye magongo yao, au wakisaidiwa na rafiki zao, walitembea katika hali ya udhaifu mpaka mahali alipokuwa Mwokozi.

Saa baada ya saa watu walikuja kwake na kuondoka; maana hakuna aliyejua kama kesho wangemkuta Mponyaji akiwa bado katikati yao. Kapernaumu ilikuwa haijawahi kushuhudia siku kama hii. Anga lilikuwa limejazwa na sauti za ushindi na za kuponywa. Mwokozi alifurahishwa na furaha aliyokuwa ameamsha. Wakati alipoona mateso ya wale waliokuja kwake, moyo wake ulijawa na huruma, na alifurahi katika uwezo wake wa kuwarejesha katika hali ya afya njema na furaha.

Yesu hakuacha kazi yake mpaka mgonjwa wa mwisho alipokuwa ameponywa. Mpaka baadaye sana muda wa usiku ndipo makutano walipotawanyika, na utulivu ukawepo katika nyumba ya Simoni. Siku ndefu ya kusisimua ilikuwa imepita, na Yesu alihitaji kupumzika. Lakini watu wa mji walipokuwa bado wamelala usingizi, "alfajiri na mapema sana akaondoka, akatoka akaenda zake mahali pasipokuwa na watu, akaomba huko."

Hivyo ndivyo siku za maisha ya Yesu zilivyotumika. Mara nyingi aliwatawanya wanafunzi wake waende majumbani mwao na kupumzika; lakini alipinga kwa upole jitihada zao za kumwondoa katika kazi zake. Siku nzima alifanya kazi, **(260)** akiwafundisha wasiojua, kuwaponya wagonjwa, akiwapa vipofu kuona, akiwalisha makutano; na wakati wa jioni na asubuhi, aliondoka kwenda katika patakatifu milimani kuwasiliana na Baba yake. Mara nyingi alitumia usiku wote akiomba na kutafakari, na kutoka huko asubuhi kuja kufanya kazi zake miongoni mwa watu.

Asubuhi na mapema, Petro na wenzake walikuja kwa Yesu, wakisema kwamba watu wa Kapernaumu walikuwa tayari wanamtafuta. Kabla ya pale, wanafunzi walikuwa wamefadhaishwa mno kwa mapokezi ambayo Kristo alikuwa amekutana nayo. Wenye mamlaka wa Yerusalemu walikuwa wanatafuta kumwua, hata watu wa mji wa nyumbani kwake walikuwa wamejaribu kuondoa maisha yake. Lakini pale Kapernaumu alipokelewa kwa furaha, na matumaini ya wanafunzi yakarejea upya. Huenda ilikuwa ya kwamba miongoni mwa Wagalilaya wapenda uhuru kungekuwa na watu wanaounga mkono ufalme huu mpya. Lakini kwa mshangao waliyasikia maneno ya Yesu akisema, "Imenipasa kuihubiri habari njema ya ufalme wa Mungu katika miji mingine pia; maana kwa sababu hiyo nalitumwa."

Katika ule msisimko ulioijaza Kapernaum, kulikuwa na hatari kwamba kusudi la kazi yake lisingefikiwa. Yesu hakuridhishwa na hali ya kuvuta mtazamo wa watu wamwone Yeye kama mtenda maajabu au mponyaji wa magonjwa ya mwili tu. Alikuwa anatafuta kuwavuta watu kwake kama Mwokozi wao. Wakati watu walikuwa na hamu kuamini kwamba alikuwa amekuja kama mfalme, kuweka utawala wa kidunia, alitaka ageuze mawazo yao kutoka katika mambo ya kidunia kwenda katika mambo ya kiroho. Mafanikio ya kiulimwengu yangeathiri kazi yake.

Na hali ya kushangaa kwa makutano wale wasiojali ilisumbua roho yake. Hakuna hali ya kujisifu iliyojichanganya na maisha yake. Heshima ambazo ulimwengu unaonyesha kwa kuangalia cheo, au mali, au kipaji, ilikuwa jambo geni kwa Mwana wa Adamu. Katika njia zinazotumiwa na wanadamu kupata ukuu au heshima, Yesu hakutumia yoyote miongoni mwa hizo. Karne kadhaa kabla ya kuzaliwa kwake, ilikuwa imetabiriwa kumhusu, kwamba, **(261)** "Hatalia, wala hatapaza sauti yake, wala kuifanya isikiwe katika njia kuu. Mwanzi uliopondeka hatauvunja, wala utambi utokao moshi hatauzima; atatokeza hukumu kwa kweli. Hatazimia, wala hatakata tamaa, hata atakapoweka hukumu duniani." Isaya 42:2-4.

Mafarisayo walitafuta heshima kwa kuwa makini katika kuzingatia maadhimisho, na maonyesho ya mafanikio yao katika ibada na matendo mema. Walithibitisha bidii yao ya dini kwa kuifanya kuwa mjadala wa kukariri. Ubishi kati ya vikundi tofauti vya imani ulikuwa mkubwa na wa muda mrefu, na halikuwa jambo lisilo la kawaida kusikia katika njia kuu sauti za mabishano ya hasira yaliyofanywa na madaktari wasomi wa sheria.

Maisha ya Yesu yalikuwa katika hali tofauti na hiyo. Hakukupata kushuhudiwa ubishi wa kelele katika maisha yake, wala ibada ya kifahari, wala tendo la kupenda kusifiwa kwa kupigiwa makofi. Kristo alifichwa ndani ya

Mungu, na Mungu aliweka ufunuo wake katika tabia za Mwana wake. Yesu alitaka mawazo ya watu yaelekezwe katika ufunuo huo, na heshima yao itolewe kuuelekea huo.

Yeye aliye Jua la Haki hakujionyesha ulimwenguni katika hali ya ufahari, ili kuvutia hisia za watu kwa kutumia utukufu wake. Imeandikwa kuhusu Kristo kwamba, "Kutokea kwake ni yakini kama asubuhi." Hosea 6:3. Nuru ya pambazuko la asubuhi huja kimya kimya na polepole, ikifukuza kivuli cha giza, na ikiuamsha ulimwengu na kuupatia uhai. Hivyo ndivyo Jua la Haki lilivyozuka, "lenye kuponya katika mbawa zake." Malaki 4:2.

# Sura ya 27

## "Waweza Kunitakasa"

[Sura hii imejengwa katika Mathayo 8:2-4; 9:1-8, 32-34; Marko 1:40-45; 2:1-12; Luka 5:12-28.]

Ukoma ulikuwa ugonjwa wa kutisha kuliko magonjwa yote yaliyojulikana katika nchi za Mashariki. Tabia ya ugonjwa huu ya kutokuwa na tiba na kule kuambukiza kwa kugusana, na matokeo yake ya kusikitisha kwa mwenye ugonjwa huo, viliwajaza woga hata watu werevu sana. Miongoni mwa Wayahudi ugonjwa huo ulichukuliwa kama mapatilizo kwa dhambi, na kwa sababu hiyo ugonjwa huo uliitwa "pigo," "kidole cha Mungu." Kwa ile hali ya ugonjwa huu kuwa na tabia ya kuzama kwa kina, kutototokomezwa, na utisho wake, uliangaliwa kama ishara ya dhambi. Kwa sheria ya kidini, mkoma alitajwa kama mtu aliye najisi. Kama vile ni mtu aliyekwishakufa, alifungiwa mbali na makao ya watu. Kila kitu alichokigusa kilikuwa najisi. Hewa ilihesabika kama imechafuliwa kwa upumuaji wake. Kila mtu aliyetiliwa shaka kuwa ana ugonjwa huo alikuwa lazima akajionyeshe kwa kuhani, ambao walipaswa kupima na kuamua kuhusu habari yake. Akitamkwa kwamba ni mwenye ukoma, alitengwa na jamaa yake, kuwekwa mbali na makutano ya Israeli, na alitakiwa kuwa pamoja na watu waliokuwa na tatizo kama lake tu. Sheria ile ilikuwa haibadiliki katika matakwa hayo. Hata wafalme na wakuu hawakuachwa kando na sheria hii. Mtawala aliyeshikwa na ugonjwa huu wa kutisha alilazimika kukabidhi fimbo ya utawala, na kuondoka katika jamii.

Akiwa mbali na rafiki zake na watu wa jamaa yake, lazima mwenye ukoma abebe laana ya ugonjwa wake. Alilazimishwa kutangaza janga lake hilo, kurarua mavazi yake, na kupiga yowe, akiwaonya wote waende mbali na mahali alipo ili wasiambukizwe. Sauti iliyolia ikisema, "Ni najisi, Ni najisi," ikiwa sauti ya maombolezo itokayo kwa mtu aliye katika hali ya upweke ya kutengwa, ilikuwa sauti ya ishara iliyosikiwa kwa hofu na ya hali ya kuepukwa.

Katika eneo la huduma ya Yesu, kulikuwa na watu wengi walioathiriwa na ugonjwa huu, na habari za kazi zake ziliwafikia, zikiwaletea mwale wa matumaini. Lakini tangu siku za Elisha nabii, hakikupata kujulikana tena kitu kinachoweza **(263)** kumtakasa mtu aliyekuwa amekandamizwa na ugonjwa huu. Hawakudiriki kumtarajia Yesu kuwafanyia kitu ambacho hakupata kufanya kwa mtu yeyote. Lakini, hata hivyo, kulikuwa na mtu ambaye imani ya moyo wake ilianza kububujika. Lakini mtu huyu hakujua namna ya kumfikia Yesu. Akiwa haruhusiwi kukaribiana na watu wengine, angejifikishaje mbele ya Mponyaji? Na aliuliza ikiwa Yesu angemponya yeye. Je, Yesu angejisumbua kumwangalia mtu ambaye iliaminika kwamba anateseka kwa sababu ya hukumu za Mungu? Je, kama walivyofanya Mafarisayo, na hata matabibu, Yeye pia asingemtamkia laana, na kumwonya akimtaka aende mbali kutoka mahali watu wengine walipo? Alifikiri kuhusu yote aliyokuwa ameambiwa kuhusu Yesu. Hakuna hata mtu mmoja aliyekuwa ametafuta msaada kwa Yesu akafukuzwa. Mtu yule aliyekuwa matesoni aliazimia kumtafuta Mwokozi. Ingawa alikuwa amefungiwa nje ya miji, huenda ingewezekana akapita katika njia ya Yesu kwa bahati tu katika njia za milimani, au akampata wakati alipokuwa akifundisha nje ya miji. Kulikuwa na ugumu mkubwa, lakini hili ndilo lilikuwa tumaini lake pekee.

Mwenye ukoma anaongozwa kwenda kwa Mwokozi. Yesu anafundisha kando ya ziwa, na watu wamekusanyika kumzunguka. Akiwa amesimama mbali kidogo, mwenye ukoma anadaka maneno machache kutoka midomoni mwa Mwaokozi. Anamwona akiwa amenyosha mikono yake juu ya wagonjwa. Anawaona viwete, vipofu, wenye kupooza, na wale wanaokaribia kufa kwa sababu ya magonjwa mbalimbali wakiinuka wakiwa na afya njema, wakimsifu Mungu kwa kuwaponya. Imani inapata nguvu moyoni mwake. Anasogea karibu na karibu zaidi ya umati. Vizuizi alivyowekewa, habari ya usalama wa watu, na hofu ya vile watu wote wanavyomchukulia vinasahaulika. Anafikiria tu kuhusu tumaini la baraka la uponyaji.

Huyu ni mtu asiyetakiwa. Ugonjwa ule umemletea hali mbaya, na mwili wake unaooza unatisha kuangalia. Watu wamwonapo hupomoka kurudi nyuma kwa kutishwa. Wanasukumana na kuangukiana wakikwepa kugusana naye. Baadhi wanajaribu kumzuia asisogee karibu na Yesu, lakini bila mafanikio. Yeye hawaoni wala hawasikii. Hali yao ya kuonyesha kumkataza haina maana kwake. Anachoona ni Mwana wa Mungu tu. Anachosikia tu ni sauti inayonena maisha kwa wanaokufa. Akijipenyeza mpaka kwa Yesu, anajibwaga miguuni pake Yesu huku akilia, "Bwana, ukitaka, waweza kunitakasa."

Yesu akajibu akisema, "Nataka; takasika," na akanyosha mkono wake juu yake. Mathayo 8:3.

Wakati huo huo badiliko likamtokea yule mwenye ukoma. Mwili wake ukawa na afya njema, hisia za mwili wake zikafanya kazi, misuli yake ikawa na nguvu. Uso ule mgumu, wenye magamba-magamba ya ukoma ukatoweka, na ngozi laini, kama ya mtoto mwenye afya njema, ikawepo mahali palipokuwa na ile ya awali.

**(264)** Yesu alimtaka mtu yule asimjulishe mtu yeyote habari ya tendo lile alilotendewa, bali aende moja kwa moja akajionyeshe hekaluni akiwa na sadaka yake. Sadaka ile isingepokelewa mpaka aangaliwe kwanza na kuhani na kutangazwa naye kwamba yu mzima kabisa kutoka katika ugonjwa ule. Hata kama wasingependa kufanya huduma hiyo, wasingekwepa kumwangalia na kutoa maamuzi kuhusu hali yake.

Haya maneno ya Yesu yalionyesha uharaka ambao Kristo aliutaka katika ulazima wa kuwa na ukimya na utekelezaji wa mtu yule. "Akamkataza kwa nguvu, akamwondoa mara, akamwambia, Angalia, usimwambie mtu neno lolote, ila enenda zako ukajionyeshe kwa kuhani, ukatoe alivyoamuru Musa kwa kutakasika kwako, iwe ushuhuda kwao." Ikiwa makuhani wangejua ukweli kuhusu jinsi mwenye ukoma alivyopona, chuki yao kwa Kristo ingewaongoza kufanya maamuzi yasiyo haki. Yesu alitaka mtu yule ajionyeshe hekaluni kabla tetesi zozote hazijawafikia kule. Hivyo maamuzi yasiyoegemea upande wowote yangepatikana, na mwenye ukoma aliyeponywa angeruhusiwa kuungana tena na jamaa yake na rafiki zake.

Yesu alikuwa na makusudi mengine aliyoona katika kule kumwagiza yule mtu akae kimya. Mwokozi alijua kwamba wakati wote adui zake walikuwa wakitafuta kuzuia kazi yake, na kuwageuza watu kuachana naye. Alijua kwamba ikiwa habari ya kuponywa kwa mwenye ukoma ingesemwa-semwa mahali pengi, wagonjwa wengine wenye tatizo hili la kutisha wangekusanyika kwake, na kilio kingeongezeka kwamba watu wangeambukizana ugonjwa huo. Wenye ukoma wengi wasingetumia zawadi ya afya njema kama mbaraka kwao au kwa watu wengine. Na kwa kuvuta wenye ukoma wengi kwake, angetoa nafasi ya kulaumiwa kwamba alikuwa anakiuka vizuizi vilivyowekwa kwa mujibu wa sheria za kidini. Kwa hiyo kazi yake ya kuihubiri injili ingekwamishwa.

Tukio hili lilithibitisha onyo la Kristo. Umati wa watu ulikuwa umeshuhudia kuponywa kwa mwenye ukoma, na walikuwa na hamu ya kupata habari ya uamuzi wa makuhani. Mtu yule aliporejea kwa rafiki zake, kulikuwa na hali ya **(265)** kusisimua sana. Licha ya tahadhari ya Yesu, yule mtu hakufanya jitihada zaidi za kuficha habari ya uponyaji aliofanyiwa. Kwa kweli ingekuwa jambo lisilowezekana kuificha, lakini yule aliyekuwa na ukoma alizisambaza sehemu mbalimbali. Akielewa kwamba ni unyenyekevu wa Yesu tu uliosababisha amzuie, alienda huko na huko akitangaza uwezo wa huyu Mponyaji Mkuu. Hakuelewa kwamba kila udhihirisho wa namna ile uliwafanya makuhani na wazee kusukumwa zaidi katika makusudi ya kumwangamiza Yesu. Yule aliyeponywa aliona kwamba ile zawadi ya afya njema ilikuwa ya thamani sana. Alishangilia kwa nguvu, na kwa kurejeshwa kwake katika jamaa yake na jamii, na aliona haiwezekani kuacha kumtukuza Tabibu aliyemponya. Lakini kitendo chake cha kutangaza jambo hilo mahali pengi kilisababisha kuzuiwa kwa kazi ya Mwokozi. Kilisababisha watu kumiminika kuja kwa Yesu kwa wingi kiasi kwamba kwa muda fulani alilazimika kuacha kufanya kazi zake.

Kila tendo katika huduma ya Kristo lilikuwa na lengo linalofika mbali. Ndani yake lilikuwa na kitu kilichokuwa zaidi ya vile lilivyoonekana lenyewe. Hivyo ndivyo ilivyokuwa kwa mwenye ukoma. Wakati Yesu alipowahudumia wote waliokuja kwake, alikusudia kuwabariki wale ambao hawakuja kwake. Wakati alipowavuta watoza ushuru, wapagani, na Wasamaria, alikusudia kuwafikia makuhani na waalimu ambao walikuwa wamefungwa katika misimamo potofu na mapokeo. Hakuacha kujaribu mbinu yoyote ambayo ingewezesha kuwafikia. Katika kumpeleka yule aliyeponywa kwa makuhani, aliwapa ushuhuda uliokadiriwa sawasawa ili kuondoa kwao misimamo potofu.

Mafarisayo walikuwa wamedai kwamba mafundisho ya Kristo yalikuwa yanapingana na sheria ambayo walipewa na Mungu kupitia Musa, lakini maelekezo yake kwa mwenye ukoma aliyetakaswa kupeleka sadaka kulingana na sheria yalithibitisha kwamba madai hayo si ya kweli. Huu ulikuwa ushuhuda tosha kwa wote ambao walikuwa radhi kushawishika.

Viongozi wa Yerusalemu walikuwa wametuma wapelelezi kwenda kutafuta sababu za kuhalalisha kumwua Yesu. Aliwaitikia kwa kuonyesha ushahidi wa upendo wake kwa wanadamu, heshima yake kwa sheria, na uwezo wake wa kuponya kutoka katika dhambi na mauti. Hivi ndivyo alivyotoa ushuhuda kuhusu wao: "Wamenichukuza

mabaya badala ya mema, Na chuki badala ya upendo wangu." Zaburi 109:5. Yeye ambaye aliitoa sheria mlimani akisema, "Wapendeni adui zenu," alitoa kielelezo cha mfano wa kanuni hiyo yeye mwenyewe kwa kuacha kulipa “baya kwa baya, au laumu kwa laumu;” bali kwa kubariki." Mathayo 5:44; 1 Petro 3:9.

Makuhani wale wale waliomhukumu yule mkoma kutengwa na jamii ndio waliothibitisha kupona kwake ugonjwa ule. Hukumu hii, iliyotangazwa hadharani na kuandikishwa, ilikuwa ushuhuda halisi kwa ajili ya Kristo. Na pindi yule aliyeponywa alipotangazwa tena katika kusanyiko la Waisraeli, kwa makuhani wenyewe kuthibisha kwamba **(266)** hapakuwa na unajisi wowote wa ugonjwa kwake, yeye mwenyewe aliyeponywa alikuwa ni ushuhuda ulio hai kwa ajili ya Mpaji wake. Alitoa sadaka yake kwa furaha, na kulitukuza jina la Yesu. Makuhani walishawishiwa na uwezo wa kiungu wa Mwokozi. Fursa ilitolewa kwao kuujua ukweli na kunufaika na na nuru hiyo. Kama ingekataliwa, ingewapita na kwenda zake, wala isingerudi kamwe. Nuru ilikataliwa na wengi; lakini haikutolewa na kwenda bure. Mioyo mingi iliguswa ila haikuonyesha dalili yoyote kwa wakati ule. Wakati wa maisha ya Mwokozi, kazi yake ilionekana kuwa na mwitikio mdogo tu wa makuhani na waalimu; lakini baada ya kupaa kwake "jamii kubwa ya makuhani wakaitii ile Imani." Matendo 6:7.

Kazi ya Kristo katika kumtakasa mwenye ukoma kutoka katika ugonjwa wake wa kutisha ni kielelezo cha kazi yake katika kuutakasa moyo kutoka katika dhambi. Yule mtu aliyekuja kwa Yesu alikuwa "amejaa ukoma." Sumu ya ugonjwa huo ya kufisha ilipenya katika mwili wake wote. Wanafunzi walijitahidi kumzuia Bwana wao asimguse; maana mtu aliyemgusa mwenye ukoma alihesabika najisi. Lakini kwa kunyosha mkono wake kumshika mwenye ukoma, Yesu hakupata unajisi. Mguso wake ulileta nguvu iletayo uzima. Ukoma ulitakasika. Hivyo ndivyo ukoma wa dhambi ulivyo, - umezama kwa kina, unafisha, na hauwezekani kutakaswa kwa uwezo wa mwanadamu. "Kichwa chote ni kigonjwa, moyo wote umezimia. Tangu wayo wa mguu hata kichwani hamna uzima ndani yake; bali jeraha na machubuko na vidonda vitokavyo usaha; havikufungwa, havikuzongwa-zongwa, wala havikulainishwa kwa mafuta." Isaya 1:5, 6. Lakini Yesu, ajapo kukaa ndani ya mwanadamu, hapatwi na uchafu. Uwepo wake una nguvu ya kuponya kwa ajili ya mdhambi. Yeyote aangukaye migguni pake, akisema kwa imani kwamba, "Bwana, ukitaka, waweza kunitakasa," atasikia jibu kwamba, "Nataka; takasika." Mathayo 8:2, 3.

Katika baadhi ya matukio ya uponyaji, Yesu hakutoa wakati huo huo mbaraka uliokuwa unafutwa. Lakini kwa tukio hili la ukoma, ombi lilipofanywa tu lilijibiwa hapo hapo. Wakati tunapoomba mibaraka ya mambo ya kidunia, jibu la ombi letu linaweza kukawizwa, au Mungu anaweza kutupatia kitu kingine tofauti na kile tulichoomba, lakini si hivyo pindi tunapoomba kuponywa kutoka dhambini. Mapenzi yake ni kutuponya kutoka dhambini, kutufanya kuwa watoto wake, na kutuwezesha kuishi maisha matakatifu. Kristo "alijitoa nafsi yake kwa ajili ya dhambi zetu, ili atuokoe na dunia hii mbovu iliyopo sasa, kama alivyopenda Mungu, Baba yetu." Wagalatia 1:4. "Na huu ndio ujasiri tulio nao kwake, ya kuwa, tukiomba kitu sawasawa na mapenzi yake, atusikia. Na kama tukijua kwamba atusikia, tuombachochote, twajua kwamba tunazo zile haja tulizomwomba." 1 Yohana 5:14, 15. "Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote." 1 Yohana 1:9.

**(267)** Katika kumponya yule mwenye kupooza kule Kapernaumu, Kristo alifundisha ukweli huo huo. Mwujiza ulitendwa ili kudhihirisha uwezo wake wa kusamehe dhambi. Na kuponywa kule kwa mwenye kupooza kunatoa kielelezo cha ukweli mwingine pia. Kumejaa matumaini na hali ya kutia moyo, na kutokana na mwunganiko wake na Mafarisayo wenye upinzani kunatoa somo la onyo pia.

Kama alivyokuwa mwenye ukoma, huyu mwenye kupooza alikuwa amepoteza tumaini la kupona. Ugonjwa wake ulikuwa matokeo ya maisha ya dhambi, na maumivu yake yaliongezwa na hali ya kujihisi hatia. Tangu zamani kabla ya pale alikuwa amewaendea Mafarisayo na madaktari, akitaraji kufunguliwa kutoka katika mateso ya kiakili na maumivu ya kimwili. Lakini walimtangazia kwamba haponyeki, na walionyesha kwamba yuko vile kwa sababu ya ghadhabu ya Mungu. Mafarisayo walichukulia mateso kama ushahidi wa kuchukizwa kwa Mungu, na walijiweka mbali na wagonjwa na wahitaji. Lakini mara nyingi watu hawa waliojitukuza kwamba walikuwa watakatifu walikuwa na hatia kubwa zaidi kuliko wale waliohukumiwa nao wakiwa katika mateso.

Mtu yule asiyeweza kutembea hakuwa na msaada kabisa, na, kwa kuona hana matarajio ya kupata msaada wowote katika eneo lile, alikuwa amezama katika hali ya kukata tamaa. Ndipo aliposikia matendo ya ajabu ya Yesu. Aliambiwa kwamba watu wengine waliokuwa wadhambi na wasio na msaada kama yeye walikuwa wameponywa; hata mwenye ukoma alikuwa ameponywa. Na rafiki waliomweleza mambo hayo walimtia moyo

aamini kwamba yeye pia anaweza kuponywa kama angepelekwa kwa Yesu. Lakini tumaini lake lilitoweka alipokumbuka jinsi ugonjwa ule ulivyomfikia. Aliogopa kwamba yule Tabibu aliye safi asingevumilia kwamba huyu awe mahali alipo.

Lakini hakuhitaji zaidi uponyaji wa kimwili kama alivyohitaji kuwekwa huru kutokana na mzigo wa dhambi. Ikiwa angemwona Yesu, na kupokea hakikisho la Mbingu kuhusu msamaha na amani, angeridhika katika kuishi au kufa, kulingana na mapenzi ya Mungu. Kilio cha mtu yule aliyekuwa kifoni kilikuwa, Laiti ningefika mahali Yesu alipo! Hakukuwa na muda wa kupoteza; tayari mwili wake uliokuwa umechoka ulikuwa unaonyesha viashiria vya kuharibika. Aliwasihi rafiki zake wambebe akiwa kitandani kwake kwenda kwa Yesu, na walifanya hivyo kwa furaha. Lakini umati wa watu uliokuwa pale ndani ya nyumba na kuzunguka nyumba mahali alipokuwa Yesu ulikuwa mkubwa kiasi kwamba ilikuwa haiwezekani kwa mgonjwa yule na rafiki zake kumfikia, au hata kufika mahali pa kuisikia sauti yake.

Yesu alikuwa anafundisha nyumbani mwa Petro. Kulingana na desturi zao, wanafunzi wake walikaa karibu naye, na "Mafarisayo na waalimu wa torati walikuwa wameketi hapo, waliotoka katika kila kijiji cha Galilaya, na Uyahudi, na Yerusalemu." Hawa walikuja kama wapelelezi, wakitafuta mambo ya kumshtaki Yesu. Nje ya maafisa hawa kulisongamana mchanganyiko wa watu, wenye hamu, wenye kuonyesha uchaji, wenye kutaka kujua, na wasioamini. Watu wa **(268)** mataifa tofauti na madaraja tofauti katika jamii waliwakilishwa. "Na uweza wa Bwana ulikuwapo apate kuponya." Mkusanyiko ulighubikwa na Roho ya uzima, lakini Mafarisayo na madaktari hawakubaini uwepo huo. Hawakuhisi hali ya kuhitaji, na uponyaji haukuwa kwa ajili yao. "Wenye njaa amewashibisha mema, Na wenye mali amewaondoa mikono mitupu." Luka1:53.

Tena na tena wale waliombeba yule mwenye kupooza walijaribu kusukuma wakitafuta njia katika umati ule, lakini hawakufanikiwa. Yule mgonjwa alimwangalia kwa majonzi yasiyosemekana. Wakati msaada ule uliokuwa unatafutwa ulipokuwa karibu, angekosaje tumaini? Kwa kufuata pendekezo lake rafiki zake walimpandisha kwenye paa ya nyumba na, wakiwa wametoboa paa, wakamshusha miguuni pa Yesu. Hotuba ile iliingiliwa. Mwokozi aliiangalia sura ile ya majonzi, na akayaona macho yale yanayobembeleza yakimtazama. Alielewa tatizo; alikuwa ameivuta ile roho iliyotatanika na kuwa na mashaka. Wakati yule mwenye kupooza alipokuwa bado yuko nyumbani, Mwokozi alikuwa ameleta usadikisho katika dhamiri yake. Wakati alipoungama dhambi zake, na kuamini uwezo wa Yesu kumponya, rehema za Mwokozi zitiazo uzima zilikuwa zimebariki moyo wake kwanza. Yesu aliona mwako wa kwanza wa imani ukikua na kuamini kwamba Yeye alikuwa msaada wa mdhambi, na alikuwa ameiona ikiongezeka nguvu katika kila jitihada za kuja mahali alipo.

Sasa, kwa maneno yaliyokuwa kama muziki mtamu masikioni mwa mgonjwa, Mwokozi alisema, "Jipe moyo mkuu, mwanangu, umesamehewa dhambi zako."

Mzigo wa kukataa tamaa unakunjuka kutoka moyoni mwa mgonjwa yule; amani ya msamaha inakaa katika roho yake, nayo inaangaza katika uso wake. Uchungu aliokuwa nao unatoweka, na utu wake wote unabadilishwa. Mwenye kupooza asiye na msaada ameponywa! Mdhambi mwenye hatia amesamehewa!

Kwa imani rahisi alikubali maneno ya Yesu kama tunu ya maisha mapya. Hakutaka kuomba chochote zaidi, bali alitulia kwa furaha, furaha isiyosemeka. Nuru ya mbinguni iliangazia uso wake, na watu waliliangalia tukio hilo kwa mshangao.

Marabi walikuwa wamesubiri kwa hisia kali kuona mwelekeo wa Yesu katika jambo lile. Walikumbuka jinsi mtu yule alivyokuwa amekuja kutafuta msaada kwao, nao wakakataa kumpa matumaini wala kumhurumia. Kama vile hilo halikuwa limetosha, walikuwa wametangaza kwamba alipatwa na mabaya yale kama laana ya Mungu kwa sababu ya dhambi zake. Mambo haya yaliwajia upya katika kumbukumbu zao wakati huu walipomwona yule mgonjwa akiwa mbele yao. Waliona mwitikio wa watu wote waliokuwa wakitazama tukio lile, na walipatwa na hofu kubwa ya kupoteza ushawishi wao kwa watu.

**(269)** Wakuu hawa hawakuzungumza kwa maneno, lakini kwa kuangaliana wao kwa wao usoni waliona kwa kila mmoja wao wazo moja, ya kwamba lazima jambo fulani lifanyike kuondosha wimbi lile. Yesu alikuwa ametangaza kwamba dhambi za mwenye kupooza yule zilikuwa zimesamehewa. Mafarisayo wakayashikilia maneno hayo na kuyaona ya makufuru, na wakaona kuwa wanaweza kuonyesha kwamba hiyo ni dhambi

inayomstahilisha kifo. Mioyoni mwao walisema, "Anakufuru. Ni nani awezaye kusamehe dhambi isipokuwa mmoja, ndiye Mungu?" Marko 2:7.

Akiwakazia macho, ambayo yaliwatia woga, Yesu alisema, "Mbona mnafikiri hivi mioyoni mwenu? Vyepesi ni vipi, kumwambia mwenye kupooza, Umesamehewa dhambi zako, au kusema, Ondoka, ujitwike godoro lako, uende? Lakini mpate kujua ya kwamba Mwana wa Adamu anayo amri duniani ya kusamehe dhambi, (hapo amwambia yule mwenye kupooza), Nakuambia, Ondoka, ujitwike godoro lako uende nyumbani kwako."

Ndipo yule aliyekuwa ameletwa kwa Yesu akiwa kwenye machela anapoinuka na kusimama kwa miguu yenye afya na nguvu za ujana. Damu iletayo uhai ikatembea katika mishipa yake. Kila kiungo cha mwili wake kinafanya kazi ghafla. Furaha ya afya njema inachukua nafasi ya hali ya kifo kilichokuwa kinamjia. "Mara akaondoka, akajitwika godoro lake, akatoka mbele yao wote; hata wakastaajabu wote, wakamtukuza Mungu, wakisema, Namna hii hatujapata kuiona kamwe."

Jamani! Upendo wa Kristo wa ajabu, anayeshuka ili kumponya mwenye dhambi atesekaye! Uungu unaohuzunishwa na maumivu ya mwanadamu anayeteseka na kutafuta kumpoza! Uwezo wa ajabu sana ulioonyeshwa kwa wana wa wanadamu! Ni nani awezaye kuwa na mashaka na ujumbe wa wokovu? Ni nani awezaye kuhafifisha rehema za Mwokozi mwenye huruma?

Kurejesha afya ya mwili ule uliokuwa unaoza hakukuhitaji kitu kilicho kidogo zaidi ya nguvu ya uumbaji. Sauti ile ile iliyotamka neno la uhai kwa mwanadamu aliyekuwa ameumbwa kutoka **(270)** katika mavumbi ya nchi ndiyo iliyotamka neno la uhai kwa mwenye kupooza aliyekuwa katika hali ya kufa. Na nguvu ile ile iliyoleta uhai kwa mwili ule ilikuwa imeufanya moyo kuwa mpya. Yeye ambaye wakati wa uumbaji "alisema, ikawa," ambaye "aliamuru, ikasimama," (Zaburi 33:9), alikuwa ametamka uhai kwa nafsi iliyokuwa imekufa katika dhambi. Kuponywa kwa mwili kulikuwa uthibitisho wa nguvu iliyokuwa imeufanya moyo kuwa mpya. Kristo alimtaka mwenye kupooza asimame atembee, akisema, ili "mpate kujua ya kwamba Mwana wa Adamu anayo amri duniani ya kusamehe dhambi."

Mwenye kupooza alipata kwa Yesu uponyaji wa mwili na roho. Uponyaji wa kiroho ulifuatiwa na uponyaji wa kimwili. Somo hili lisipuuzwe. Kuna maelfu ya watu leo wanaoteseka kwa magonjwa ya mwili, ambao, kama alivyokuwa mwenye kupooza, wanatamani ujumbe usemao, "Umesamehewa dhambi zako." Mzigo wa dhambi, na tamaa zake zisizokoma wala zisizotoshelezeka, ndio msingi wa maradhi yao. Hawawezi kupata uponyaji isipokuwa mpaka waje kwa mponyaji wa roho. Amani ile inayoweza kutolewa na Yeye peke yake, ingewatia nguvu akilini mwao, na kuwapa afya ya mwili.

Yesu alikuja "azivunje kazi za Ibilisi." "Ndani yake ndimo ulimokuwa uzima," na anasema, "Mimi nalikuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele." Yeye ni "roho yenye kuhuisha." 1 Yohana 3:8; Yohana 1:4; 10:10; 1 Wakorintho 15:45. Na bado anayo nguvu iletayo uzima ile ile aliyokuwa nayo duniani alipoponya mgonjwa, na kutamka msamaha kwa mdhambi. Anasamehe "maovu yako yote," anaponya "magonjwa yako yote." Zaburi 103:3.

Matokeo ya kule kuponywa kwa mwenye kupooza kwa watu ilikuwa kama vile mbingu ilikuwa imefunguka, na kufunua utukufu wa ulimwengu mzuri zaidi. Kadiri yule mtu aliyeponywa alivyopita katikati ya umati wa watu, akimhimidi Mungu katika kila hatua, huku akiubeba mzigo wake ule ukiwa kama vile una uzito kidogo sana, watu walisogea nyuma ili kumpa nafasi, na walimtazama wakiwa na nyuso za kustaajabu, huku wakinong’onezana kwa kusema, "Leo tumeona mambo ya ajabu."

Mafarisayo walikuwa kimya kwa mshangao na kutekewa kwa kushindwa. Waliona kwamba hapa hakukuwa na fursa ya wivu wao kuingizwa kwa makutano. Matendo ya ajabu yaliyofanywa kwa mtu yule waliyekuwa wamemtangazia ghadhabu ya Mungu yaliwagusa watu kiasi kwamba kwa muda marabi wale walisahaulika. Waliona kwamba Kristo alikuwa na uweza ambao walijua kwamba ni wa Mungu peke yake; lakini unyenyekevu wa tabia yake ulikinzana na tabia yao ya kupenda kuonekana kuwa ni wakuu. Walifadhaika na kuaibika, wakimtambua, lakini bila kukiri, kuwa ni uwepo wa kiumbe wa hali ya juu zaidi. Kadiri ilivyothibitika zaidi kwamba Yesu alikuwa na mamlaka duniani ya kusamehe dhambi, ndivyo **(271)** walivyojizamisha zaidi katika hali ya kutoamini. Kutoka pale nyumbani kwa Petro, mahali walipokuwa wamemwona mwenye kupooza akiponywa kwa neno la Mwana wa Mungu, waliondoka kwenda zao kubuni mipango mipya ya kumnyamazisha.

Ugonjwa wa kimwili, hata uwe wa kutisha na uliojikita kiasi gani, uliponywa kwa nguvu za Kristo; lakini ugonjwa wa roho ulijiimarisha kwa wale waliofumba macho yao wasiione nuru. Ukoma na ulemavu havikuwa na hali ya kutisha sana kama ilivyo hali ya kuwa na msimamo katika imani potofu na kutokuamini.

Katika nyumba ya yule mwenye kupooza aliyeponywa kulikuwa na shangwe kubwa wakati aliporudi, akiibeba kwa urahisi machela aliyoondoka nayo akiwa amebebewa na watu wengine muda mfupi uliokuwa umepita. Walikusanyika pale kwa machozi ya furaha, ikiwa nadra sana kuamini macho yao. Alisimama mbele yao akiwa na nguvu. Ile mikono waliyozoea kuona ikiwa haina uhai ilikuwa na haraka sana kutekeleza kile alichoitaka ifanye. Nyama ya mwili wake iliyokuwa imesinyaa na kuwa na rangi-rangi ya kijivu ikawa na afya mpya na rangi ya wekundu. Alitembea kwa uhuru na uimara. Furaha na matumaini viliingia katika kila namna ya mwonekano wake, na mwonekano wa usafi na amani vilikuwa vimechukua nafasi iliyokuwa na alama za dhambi na mateso. Furaha na shukrani vilipanda kutoka katika nyumba ile, na Mungu alitukuzwa kupitia kwa Mwana wake, aliyekuwa amerejesha tumaini kwa watu wasio na tumaini, na kurejesha nguvu kwa wanyonge. Mtu huyu pamoja na nyumba yake walikuwa tayari kuyatoa maisha yao kwa ajili ya Yesu. Hakuna mashaka yaliyohafifisha imani yao, hakuna kutokuamini kulikoharibu uaminifu wao kwake Yeye aliyekuwa ameleta nuru katika nyumba yao iliyokuwa na giza.

## Sura ya 28

# Lawi - Mathayo

[Sura hii imejengwa katika Mathayo 9:9-17; Marko 2:14-22; Luka 5:27-39.]

Miongoni mwa watumishi wa serikali ya Kirumi kule Palestina, hakuna waliochukiwa zaidi ya watoza ushuru. Ile hali ya kwamba kodi zilitozwa na utawala wa kigeni iliifanya kuwa kero ya muda wote kwa Wayahudi, ikiwa ni ukumbusho kwamba uhuru ulikuwa umetoweka. Na wakusanyaji wa kodi wenyewe hawakuwa tu vyombo vya kuitumikia serikali ya Kirumi; walikuwa wakikusanya ili kujinufaisha wenyewe, wakijitajirisha kwa gharama ya watu wa kawaida. Myahudi aliyeikubali kazi hii kutoka kwa Warumi aliangaliwa kama mtu anayesaliti heshima ya taifa lake. Alidharauliwa kama muasi, na alijumuishwa miongoni mwa waovu wakubwa katika jamii.

Katika kundi hili alikuwemo Lawi – Mathayo, ambaye ndiye aliyeitwa katika kazi ya utumishi ya Kristo baada ya wale wanafunzi wanne walioitwa kule Genesareti. Mafarisayo walikuwa wamemhukumu Mathayo kwa kuangalia kazi yake, lakini Yesu aliona ndani ya mtu huyu moyo ulio wazi kuupokea ukweli. Mathayo alikuwa amesikiliza mafundisho ya Yesu. Usadikisho wa Roho wa Mungu ulipomfunulia hali yake ya dhambi, alitafuta msaada kwa Kristo; lakini alikuwa na mazoea ya kuwaona marabi kama watu maalum walio juu sana kuliko wengine, na hakudhani kama Mwalimu Mkuu huyu angemtambua. **(273)** Akiwa amekaa katika banda la kupokelea kodi (forodhani) siku moja, mtoza ushuru huyu alimwona Yesu akija. Alishtuka sana kusikia maneno yaliyoelekezwa kwake yakisema, "Nifuate."

Mathayo "akaacha vyote, akaondoka, akamfuata." Hakukuwa na kusita, wala kuuliza swali, wala wazo kuhusu ile kazi ya manufaa ambayo ingeachwa na mahali pake kuwa na umaskini na maisha magumu. Ilitosha kwake kuwa na Yesu, ya kwamba atasikiliza maneno yake, na kuungana naye katika kazi yake.

Hivyo ndivyo ilivyokuwa hata kwa wanafunzi walioitwa kabla. Wakati Yesu alipomtaka Petro na wenzake kumfuata, mara ile ile waliacha vyombo vyao na nyavu zao. Baadhi ya wanafunzi hawa walikuwa na wategemezi; lakini walipopata mwaliko wa Kristo, hawakusita, na kuuliza kwamba, Nitaishije, na kutegemeza nyumba yangu? Walikuwa watiifu kwa ule wito; na pindi Yesu alipowauliza baadaye akisema, "Je! Hapo nilipowatuma hamna mfuko, wala mkoba, wala viatu, mlipungukiwa na kitu?” walisema, “La!” Luka 22:35.

Kwa Mathayo aliyekuwa katika utajiri wake, na kwa Andrea na Petro waliokuwa katika umaskini wao, kipimo kile kile kililetwa; kujitoa kule kule kulifanywa na kila mmoja. Mnamo wakati wa mafanikio, wakati nyavu zilipokuwa zimejaa samaki; na misukumo ya maisha ya uzee ilikuwa imepanda juu mno, Yesu aliwataka wanafunzi wale waliokuwa pale baharini waache vyote kwa ajili ya kazi ya injili. Kila mtu anajaribiwa hivyo kuona kama chenye nguvu zaidi kwake ni kupenda mali za dunia au ushirika pamoja na Kristo.

Kanuni inadai muda wote. Hakuna mtu anayeweza kufanikiwa katika kazi ya Mungu isipokuwa moyo wake wote uko katika kazi hiyo na anahesabu mambo yote kama hasara akilinganisha na uzuri wa kumjua Kristo. Mtu anayesaza sehemu hawezi kuwa mwanafunzi wa Kristo, wala hawezi kabisa kuwa mshirika wake katika kazi. Pale watu wanapotambua wokovu mkuu, kujitoa kafara kunakoonekana katika maisha ya Kristo kutaonekana katika maisha yao. Popote aongozapo njia, watafuata kwa furaha.

Kuitwa kwa Mathayo kuja kuwa mmoja kati ya wanafunzi wa Yesu kulileta chuki kubwa. Kwa mwalimu wa kidini kumchagua mtoza ushuru kumfanya mmoja wa watu wanaoandamana naye ilikuwa ni jinai dhidi ya desturi za dini, za jamii na za taifa. Kwa kutumia itikadi hizo potofu za watu Mafarisayo walitarajia kugeuza mkondo wa hisia za watu uwe kinyume cha Yesu.

Hamasa kubwa iliamshwa miongoni mwa watoza ushuru. Mioyo yao ilivutwa kumwelekea mwalimu huyu wa kimbingu. Katika furaha ya uanafunzi wake mpya, Mathayo alifanya kazi ya kuwaleta kwa Yesu wafanya-kazi wenzake wa zamani. Vivyo hivyo **(274)** alifanya karamu katika nyumba yake, na kuwaita pamoja jamaa na rafiki zake. Waliojumuishwa si watoza ushuru tu, bali pia wengine wengi waliotiliwa mashaka sana, na walioshuhudiwa hivyo na majirani walioaminika sana kwa uadilifu.

Burudani ilitolewa kwa heshima ya Yesu, naye hakuacha kupokea tendo hilo la heshima. Alijua vema kwamba jambo hili lingehesabika kama kosa kwa upande wa Mafarisayo, na lingemletea hatari pia machoni pa watu. Lakini hakuna jambo lolote la mambo ya kawaida ambalo lingedhibiti mienendo yake. Tofauti-tofauti za mambo ya nje hazikuwa na uzito wowote kwake. Kitu kilichovuta moyo wake ilikuwa ni nafsi iliyokuwa na kiu ya maji ya uzima.

Yesu alikaa kama mgeni wa heshima kwenye meza ya watoza ushuru, kwa huruma yake na wema wake wa kijamii akionyesha kwamba alitambua thamani ya mwanadamu; na watu walionyesha kukidhi kuwa na thamani ile aliyojali. Maneno yake yalianguka katika mioyo yao yenye kiu yakiwa na nguvu ya baraka iletayo uzima. Msukumo mpya uliamshwa, na uwezekano wa maisha mapya ulifunguka kwa watu hawa waliotengwa na jamii.

Katika mikutano inayofanana na huu, si watu wachache walioguswa na mafundisho ya Mwokozi ambao bado hawakumkiri mpaka wakati wa baada ya kupaa kwake. Wakati **(275)** Roho Mtakatifu alipomwagwa, na watu elfu tatu wakaongoka kwa siku moja, kulikuwa na wengi miongoni mwao ambao walikuwa wamesikia ukweli kwa mara ya kwanza pale kwenye meza ya watoza ushuru, na baadhi ya hawa wakawa wajumbe wa injili. Kwa Mathayo yeye kielelezo cha Yesu katika karamu hii kilikuwa somo la kudumu. Mtoza ushuru aliyekuwa amedharauliwa sana anakuwa mmoja wa wainjilisti waliojitoa sana, katika huduma yake akifuata sana katika hatua za Bwana wake.

Wakati marabi walipojua kuhusu kuwepo kwa Yesu katika karamu ya Mathayo, walitafuta nafasi ya kumshtaki. Lakini walichagua kufanya hayo kwa kuwatumia wanafunzi wake. Kwa kuamsha itikadi zao zisizo sahihi walitarajia kuwaondoa kwa Bwana wao. Mpango wao ulikuwa ni kumshtaki Kristo kwa wanafunzi, na kuwashtaki wanafunzi kwa Kristo, wakiilenga mishale yao mahali ambapo ingejeruhi zaidi. Hivi ndivyo ambavyo Shetani amekuwa akifanya kazi tangu alipoasi mbinguni; na wote wanaojaribu kupinga na kuasi wanasukumwa na roho wake.

"Mbona mwalimu wenu anakula pamoja na watoza ushuru na wenye dhambi?" wale marabi wenye wivu waliuliza.

Yesu hakusubiri kwamba wanafunzi wake wajibu madai hayo, bali Yeye mwenyewe alijibu: "Wenye afya hawahitaji tabibu, bali walio hawawezi. Lakini nendeni, mkajifunze maana yake maneno haya, Nataka rehema, wala si sadaka; kwa maana sikuja kuwaita wenye haki, bali wenye dhambi." Mafarisayo walijidai kuwa wakamilifu kiroho, na kwa hiyo ni kwamba hawakuhitaji tabibu, wakati waliwachukulia watoza ushuru na Mataifa kama watu wanaoangamizwa na magonjwa ya roho. Sasa je, haikuwa kazi yake, kama tabibu, kuwaendea watu wa kundi hili waliohitaji msaada wake?

Ingawa Mafarisayo walijidhania wenyewe kuwa watu wa kiwango cha juu, kiuhalisia walikuwa katika hali mbaya zaidi kuliko wale waliowadharau. Watoza ushuru walikuwa watu wasioshikiliwa sana na itikadi na wasiojiona kujitosheleza sana, na kwa hiyo walikuwa wazi kushawishiwa na ukweli. Yesu akawaambia marabi, "Nendeni, mkajifunze maana yake maneno haya, Nataka rehema, wala si sadaka." Kwa hayo alionyesha kwamba wakati wao walidai kulifafanua vema neno la Mungu, walikuwa hawajui kabisa kiini chake.

Mafarisayo walinyamazishwa kwa muda, lakini walijiimarisha zaidi katika uadui wao. Kilichofuata waliwatafuta wanafunzi wa Yohana, na kujaribu kuwapanga kumpinga Mwokozi. Mafarisayo hawa hawakuwa wameikubali kazi ya Yohana Mbatizaji. Walikuwa wamekejeli maisha yake ya kujinyima, tabia yake rahisi, mavazi yake magumu-magumu, na walikuwa wamemtangaza kwamba ni mshupavu. Kwa kuwa alipinga unafiki wao, walikuwa wamepinga maneno yake, na walikuwa wamewahamasisha watu ili kumpinga. Roho **(276)** wa Mungu alikuwa ametia msukumo katika mioyo ya wenye kejeli hawa, akiwasadikisha kuhusu dhambi yao; lakini walikuwa wamekataa mashauri ya Mungu, na walikuwa wametangaza kwamba Yohana alikuwa amepagawa na shetani.

Sasa Yesu alipokuja akichangamana na watu, akila na kunywa katika meza zao, walimshtaki kuwa ni mlafi na mlevi. Wale wale walioleta madai hayo walikuwa ndio wenye hatia. Kama vile ambavyo Mungu anaonyeshwa isivyo sahihi, akivalishwa na Shetani sifa zilizo zake Shetani, ndivyo waovu walivyowatambulisha wajumbe wake isivyo sahihi.

Mafarisayo wasingeona kwamba Yesu alikuwa akila na watoza ushuru na wenye dhambi ili kuleta nuru ya mbinguni kwa wale waliokuwa wamekaa gizani. Wasingeona kwamba kila neno lililodondoshwa na Mwalimu wa mbinguni lilikuwa mbegu yenye uhai ambayo ingeota na kuzaa matunda kwa utukufu wa Mungu. Walikuwa wameazimia kutoipokea nuru; na ingawa walikuwa wamepinga kazi ya Mbatizaji, sasa walikuwa tayari kukubali kuwa na urafiki na wanafunzi wake, wakitaraji kupata ushirikiano wao katika kumpinga Yesu. Walionyesha kwamba Yesu alikuwa anafutilia mbali mila za wazee wa zamani; na walionyesha tofauti kati ya dini ya kujikana ya Yohana na tabia ya Yesu ya anasa katika karamu alizofanya pamoja na watoza ushuru na wenye dhambi.

Wakati huu wanafunzi wa Yohana walikuwa katika majonzi makubwa. Ilikuwa ni kabla ya kumtembelea Yesu wakiwa na ujumbe kutoka kwa Yohana. Mwalimu wao mpendwa alikuwa gerezani, na ziku zote walikuwa katika maombolezo. Yesu naye alikuwa hafanyi jitihada yoyote ya kumfungua Yohana, na hata alionekana kufedhehesha mafundisho ya Yohana. Ikiwa Yohana alikuwa ametumwa na Mungu, kwa nini Yesu na wanafunzi wake walikuwa na mwelekeo ulio tofauti naye kiasi hiki?

Wanafunzi wa Yohana hawakuwa na uelewa mzuri kuhusu kazi ya Kristo; walidhani kwamba yawezekana madai ya Mafarisayo yakawa ya msingi. Walichunguza taratibu mbalimbali zilizoelezwa na marabi, na hata kutumaini kuwa zimehalalishwa na sheria. Kufunga kuliadhimishwa na Wayahudi kama tendo la kiroho, na wale wenye msimamo zaidi walifunga siku mbili katika kila juma. Mafarisayo na wanafunzi wa Yohana walikuwa wamefunga wakati ule hilo kundi la pili lilipokuja kwa Yesu likiwa na swali hili: "Kwa nini sisi na Mafarisayo twafunga, bali wanafunzi wako hawafungi?

Yesu aliwajibu kwa upole sana. Hakujaribu kusahihisha ufahamu wao usio sahihi wa maana ya kufunga, bali kuwaweka katika mtazamo sahihi tu wa kazi yake. Na alifanya hivi kwa kutumia kielelezo kile kile kilichotumiwa na Yohana alipomshuhudia Yesu. Yohana alikuwa amesema kwamba, "Aliye naye bibi arusi ndiye bwana arusi; lakini rafiki yake bwana arusi, yeye anayesimama na kumsikia, aifurahia sana **(277)** sauti yake bwana arusi. Basi hii furaha yangu imetimia." Yohana 3:29. Wanafunzi wa Yohana hawakushindwa kukumbuka maneno haya ya mwalimu wao kadiri Yesu alivyoyatumia na kusema, "Walioalikwa arusini wawezaje kuomboleza, muda bwana arusi akiwapo pamoja nao?"

Mfalme wa mbinguni alikuwa pamoja na watu wake. Zawadi kuu ya Mungu ilikuwa imetolewa kwa ulimwengu. Furaha kwa maskini; maana Kristo alikuwa amekuja kuwafanya kuwa warithi wa ufalme wake. Furaha kwa matajiri; maana angewafundisha namna ya kupata utajiri wa milele. Furaha kwa wajinga; angewafanya wawe na hekima ya kuokolewa. Furaha kwa wasomi; angewafungulia siri za kina zaidi kuliko walivyopata kueleweka; ukweli uliokuwa umefichika tangu kuwekwa msingi wa ulimwengu ungefunuliwa na kazi ya Mwokozi.

Yohana Mbatizaji alikuwa ameshangilia kumwona Mwokozi. Ilikuwa nafasi ya pekee jinsi gani kwa wanafunzi waliopendelewa kutembea na kuzungumza na Mkuu wa mbinguni! Huu haukuwa wakati wa kuomboleza na kufunga. Lazima wafungue mioyo yao kuipokea nuru ya utukufu wake, ili ya kwamba wapate kuangaza nuru yake kwa wale waliokuwa wamekaa gizani na katika kivuli cha mauti.

Maneno ya Yesu yalikuwa yameleta mwonekano wenye uangavu, lakini kulikuwa na kivuli kizito kilichokatiza katika maneno hayo, nacho kilionwa na macho yake tu. Akasema, "Lakini siku zitakuja watakapoondolewa bwana arusi; ndipo watakapofunga." Wakati ambapo wangemwona Bwana wao akisalitiwa na kusulibishwa, ndipo wanafunzi wangeomboleza na kufunga. Katika maneno yake ya mwisho kwao katika kile chumba cha ghorofani, alisema, "Bado kitambo kidogo nanyi hamnioni, na tena bado kitambo kidogo nanyi mtaniona. Amin, amin, nawaambia, Ninyi mtalia na kuomboleza, bali ulimwengu utafurahi; ninyi mtahuzunishwa, lakini huzuni yenu itageuka kuwa furaha." Yohana 16:19, 20.

Wakati ambapo angefufuka kutoka kaburini, huzuni yao ingegeuka kuwa furaha. Baada ya kupaa kwake uwepo wake kama nafsi usingekuwepo; lakini bado angekuwa pamoja nao kwa njia ya Mfariji, na wasingetumia muda wao kuomboleza tena. Shetani alichotaka ni hiki. Alitaka waupatie ulimwengu mawazo ya kwamba walikuwa wamedanganywa na kukatishwa tamaa, bali kwa imani wangetazama patakatifu pa juu, mahali ambapo Yesu alikuwa akihudumu kwa ajili yao; wangepaswa kuifungua mioyo yao kwa ajili ya kuingia kwa Roho Mtakatifu, aliye mwakilishi wa Yesu, na kufurahia katika nuru ya uwepo wake. Lakini bado siku za majaribu na mateso zingekuja, wakati ambapo wangeletwa katika mgogoro na watawala wa ulimwengu huu, na viongozi wa ufalme

wa giza; wakati ambapo Kristo asingekuwa **(278)** nao tena katika umbo, na wao kushindwa kumwona Mfariji, ndipo hapo ingewafaa kufunga.

Mafarisayo walitafuta kujitukuza kwa kuadhimisha kawaida za kidini, wakati mioyo yao iikuwa imejawa na wivu na chuki. Maandiko yanasema, "Tazama, ninyi mwafunga mpate kushindana na kugombana, na kupiga kwa ngumi ya uovu. Hamfungi siku hii ya leo hata kuisikizisha sauti yenu juu. Je! Kufunga namna hii ni saumu niliyoichagua mimi? Je! Ni siku ya mtu kujitaabisha nafsi yake? Ni kuinama kichwa kama unyasi, na kutanda nguo za magunia na majivu chini yake? Je! Utasema ni siku ya kufunga, na ya kukubaliwa na Bwana?" Isaya 58:4, 5.

Kufunga ambako ni kwa kweli si kwa kufanya ibada rasmi. Maandiko yanafafanua kufunga ambako Mungu amechagua, - "kufungua vifungo vya uovu, kuzilegeza kamba za nira, kuwaacha huru walioonewa, na kwamba mvunje kila nira;" to "ukimkunjulia mtu mwenye njaa nafsi yako, na kuishibisha nafsi iliyoteswa." Isaya 58:6, 10. Hapo ndipo kiini na tabia ya kazi ya Kristo vinapodhihirishwa. Maisha yake yote yalikuwa ya kujikana kwa ajili ya kuuokoa ulimwengu. Iwe ni kwa kufunga kule katika jangwa la majaribu au kula pamoja na watoza ushuru katika karamu ya Mathayo, alikuwa akiyatoa maisha yake kwa ajili ukombozi wa walio upotevuni. Roho ya kweli ya kujitoa haidhihirishwi kwa kukaa bila kazi na kuomboleza, au kwa kujitesa mwili na wingi wa kafara, bali inaonyeshwa katika kusalimisha ubinafsi katika huduma ya hiari ifanywayo kwa Mungu na kwa mwanadamu.

Akiendelea kuwajibu wanafunzi wa Yohana, Yesu alieleza kwa mfano akisema, "Hakuna mtu atiaye kiraka cha nguo mpya katika vazi kuukuu; maana kile kilichotiwa huondoa kipande cha lile vazi, na pale palipotatuka huzidi." Ujumbe wa Yohana ulikuwa usichanganywe na mapokeo ya mila na udanganyifu. Jaribio la kuchanganya huduma ya kujitoa ya Yohana na mambo ya Mafarisayo yasiyo sahihi yangeishia tu kuthibitisha zaidi tofauti zilizopo kati ya hayo.

Wala kanuni za mafundisho ya Kristo zisingeunganika na desturi za Ufarisayo. Yesu asingeziba pengo lililoletwa na mafundisho ya Yohana. Angeifanya tofauti kati ya mambo ya kale na mapya kuwa bayana zaidi. Yesu alieleza zaidi habari hii kwa kielelezo kingine akiesema, "Wala hakuna mtu atiaye divai mpya katika viriba vikuukuu; na kama akitia, ile divai mpya itavipasua vile viriba, divai yenyewe itamwagika, na viriba vitaharibika." Chupa za ngozi zilizokuwa zikitumika kama vyombo vya kuwekea divai, baada ya muda vilikauka na kuwa vigumu-vigumu vinavyovunjika kwa urahisi, na havikufaa kufanya kazi yake ile ile. Katika kielelezo hiki kinachoeleweka Yesu alikuwa akieleza hali ya viongozi wa Wayahudi. Makuhani na waandishi na wakuu walikuwa na **(279)** taratibu zenye kukinaisha za maadhimisho na mapokeo. Mioyo yao ilikuwa imesinyaa, kama ngozi kavu za divai alizokuwa amewafananisha nazo. Wakiwa wamebaki katika hali ya kutosheka na dini yao ya kisheria, ilikuwa haiwezekani kwao kuwa hazina za ukweli ulio hai wa mbinguni. Walidhani kwamba haki yao wenyewe ilitosha, wala hawakutaka jambo jipya liletwe katika dini yao. Hawakukubali kwamba mapenzi mema ya Mungu kwa wanadamu yaweza kuwa kitu kilicho mbali nao. Waliyaunganisha na wema wao wenyewe kwa sababu ya matendo yao mema. Imani ile itendayo kazi kwa upendo na isafishayo nafsi haikuweza kuungana na dini ya Mafarisayo, iliyoundwa katika maadhimisho na maelekezo ya wanadamu. Jitihada za kuunganisha mafundisho ya Yesu na dini ile iliyokuwepo zisingefaa kitu. Ukweli wa thamani wa Mungu, kama divai inayochocheleza, ungepasua chupa zilizokuwa katika kuoza za dini ya Kifarisayo.

Mafarisayo walijiona kuwa watu wenye kujua sana kiasi cha kutohitaji kufundishwa, kuwa na haki ya kutosha kiasi cha kutohitaji wokovu, kuwa na heshima ya juu sana kiasi cha kutohitaji heshima itokayo kwa Kristo. Kristo aliwaacha akageuka kwenda kutafuta wengine ambao wangepokea ujumbe kutoka mbinguni. Ndani ya wavuvi ambao hawakusomeshwa, kwa watoza ushuru waliokuwa masokoni, kwa mwanamke wa Samaria, kwa watu wa kawaida waliomsikiliza kwa furaha, ndimo alimopata viriba vipya kwa ajili ya divai mpya. Nyezo zinazotakiwa kutumika katika kazi ya injili ni watu wale wanaopokea kwa furaha nuru ambayo Mungu anawaletea. Hawa ndio mawakala wake katika kuupatia ulimwengu hali ya kuujua ukweli. Ikiwa watu wake Kristo watakuwa viriba vipya kwa neema yake, atawajaza divai mpya.

Mafundisho ya Kristo, pamoja na kwamba yaliwakilishwa na divai mpya, hayakuwa mafundisho ya imani mpya, bali mafunuo ya kile kilichokuwa kimefundishwa tangu mwanzo. Lakini kwa Mafarisayo ukweli wa Mungu ulikuwa umepoteza umuhimu na uzuri wake halisi. Kwao mafundisho ya Kristo yalikuwa mapya karibu katika kila nyanja, na yalikuwa hayatambuliki wala kukubalika.

Yesu alionyesha nguvu ya mafundisho potofu katika kuharibu hali ya mtu ya kukubali na kutamani ukweli. Akasema, "Wala hakuna anywaye divai ya kale akatamani divai mpya; kwa kuwa asema, Ile ya kale ndiyo iliyo njema." Ukweli wote ambao umetolewa kwa ulimwengu kupitia wazee na manabii uliangaza katika uzuri mpya katika maneno ya Kristo. Lakini waandishi na Mafarisayo hawakuwa na haja ya kupata divai mpya iliyo ya thamani. Kwa kuwa hawabaki tupu wasiojawa mila, desturi, na matendo ya zamani, hawakuwa na nafasi mawazoni mwao au mioyoni mwao kwa ajili ya kupokea mafundisho ya Kristo. Waling'ang'ania taratibu zilizopitwa na wakati, na wakageukia mbali kutoka kwa ukweli ulio hai na nguvu za Mungu.

**(280)** Hiki ndicho kilicholeta uangamivu wa Wayahudi, na kitaleta uangamivu wa watu wengi mnamo wakati wetu. Maelfu wanafanya makosa yale yale yaliyofanywa na Mafarisayo waliokemewa na Yesu kwenye karamu ya Mathayo. Badala ya kuachana na mawazo kadhaa yanayoshikiliwa, au badala ya kufuta sanamu kadhaa za maoni ndani yao, wengi wanaukataa ukweli unaoshuka kutoka kwa Baba wa mwanga. Wanajiamini wao wenyewe, na kutegemea hekima yao wenyewe, na hawatambui umaskini wao wa kiroho. Wanasisitiza kuhusu kuokolewa kwa njia fulani za matendo muhimu ambayo wanatenda. Wakati wanapoona kwamba hakuna njia ya kuchanganya utegemezi wa nafsi zao wenyewe katika kazi ile, wanaukataa wokovu utolewao.

Dini ya kufuata sheria haiwezi kamwe kuongoza roho kwenda kwa Kristo; maana ni dini isiyo na upendo, isiyo na Kristo. Kufunga na kuomba kunakohimizwa na roho ya kujihesabia haki ni machukizo machoni pa Mungu. Makusanyiko ya heshima kwa ajili ya ibada, taratibu za maadhimisho ya kidini, kujitesa kwa nje, utoaji wa dhabihu, ni mambo ambayo yanatangaza kwamba anayeyafanya anajiona kuwa ni mwenye haki, na kwamba ana nafasi ya kuingia mbinguni; lakini yote hayo ni udanganyifu. Matendo yetu wenyewe hayawezi kuununua wokovu.

Kama ilivyokuwa katika siku za Kristo, ndivyo ilivyo hata sasa; Mafarisayo hawajui hali yao ya umaskini wa kiroho. Ujumbe unawajia, ukisema, "Kwa kuwa wasema, Mimi ni tajiri, nimejitajirisha, wala sina haja ya kitu; nawe hujui ya kuwa wewe u mnyonge, na mwenye mashaka, na maskini, na kipofu, na uchi. Nakupa shauri, ununue kwangu dhahabu iliyosafishwa kwa moto, upate kuwa tajiri, na mavazi meupe upate kuvaa, aibu ya uchi wako isionekane." Ufunuo 3:17, 18. Imani na upendo ni dhahabu iliyojaribiwa kwa moto. Lakini kwa wengi dhahabu imefifia, na utajiri wa hazina umepotea. Haki ya Kristo iko kama vazi ambalo halikuvaliwa kwao, ni chemchemi isiyoguswa. Kwao maneno haya yanasemwa, "Nina neno juu yako, ya kwamba umeuacha upendo wako wa kwanza. Basi, kumbuka ni wapi ulikoanguka; ukatubu, ukayafanye matendo ya kwanza. Lakini, usipofanya hivyo, naja kwako, nami nitakiondoa kinara chako katika mahali pake, usipotubu." Ufunuo 2:4, 5.

"Dhabihu za Mungu ni roho iliyovunjika; Moyo uliovunjika na kupondeka, Ee Mungu, hutaudharau." Zaburi 51:17. Lazima mtu abaki mtupu asiye na kujitumainia kabla hajawa muumini wa kweli wa Yesu. Pindi kujitegemea kunapoachwa, ndipo Bwana aweza kumfanya mtu kuwa kiumbe kipya. Vyombo vipya vinaweza kubeba divai mpya. Upendo wa Kristo utatia uhai mpya ndani ya mtu aaminiye. Kutakuwa na udhihirisho wa tabia ya Kristo ndani ya mtu amtazamaye yeye aliye Mwanzilishi na Mkamilishaji wa imani yetu.

# Sura ya 29
# Sabato

Sabato ilitukuzwa wakati wa uumbaji. Ikiwa imewekwa kwa ajili ya mwanadamu, asili yake ni wakati ule "nyota za asubuhi zilipoimba pamoja, na wana wote wa Mungu walipopiga kelele kwa furaha." Ayubu 38:7. Amani ilitawala ulimwenguni; maana dunia ilikuwa katika hali ya kupatana na mbingu. "Mungu akaona kila kitu alichokifanya, na tazama, ni chema sana;" na akapumzika katika furaha ya kazi yake iliyokuwa imekamilika. Mwanzo 1:31.

Kwa kuwa alipumzika siku ya Sabato, "Mungu akaibarikia siku ya saba, akaitakasa," – aliitenga ili iwe na matumizi matakatifu. Aliitoa na kumpa Adamu ikiwa kama siku ya kupumzika. Ilikuwa kumbukumbu ya kazi ya uumbaji, na kwa hiyo ikiwa ishara ya uwezo wa Mungu na upendo wake. Maandiko yanasema, "Amefanya ukumbusho wa matendo yake ya ajabu." "Kwa sababu mambo yake yasiyoonekana tangu kuumbwa ulimwengu yanaonekana, na kufahamika kwa kazi zake; yaani, uweza wake wa milele na Uungu wake." Mwanzo 2:3; Zaburi 111:4; Warumi 1:20.

Vitu vyote viliumbwa na Mwana wa Mungu. "Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu . . . . Vyote vilifanyika kwa huyo; wala pasipo yeye hakikufanyika chochote kilichofanyika." Yohana 1: 1-3. Na kwa kuwa Sabato ni kumbukumbu ya kazi ya uumbaji, ni zawadi ya upendo na uweza wa Kristo.

Sabato inayavuta mawazo yetu kuelekea kwa vitu vya asili, na hutuleta katika ushirikiano na Muumbaji. Katika nyimbo za ndege, sauti itolewayo na miti inapopigwa na upepo, na muziki unaoimbwa na bahari, bado tunaisikia sauti yake yeye aliyezungumza **(282)** na Adamu mle Edeni wakati wa jua kupunga. Na kadiri tunavyotazama uweza wake katika vitu vya asili tunapata faraja, maana neno lile lililoumba vitu vyote ndilo litamkalo uzima kwa mtu. Yeye aliyeamuru kwamba "Nuru itang'aa toka gizani, ndiye aliyeng'aa mioyoni mwetu, atupe nuru ya elimu ya utukufu wa Mungu katika uso wa Yesu Kristo." 2 Wakorintho 4:6.

Wazo hilo ndilo lililoamsha wimbo huu,

“Kwa kuwa umenifurahisha, Bwana, Kwa kazi yako; nitashangilia Kwa ajili ya matendo ya mikono yako.
Ee Bwana, jinsi yalivyo makuu matendo yako! Mawazo yako ni mafumbo makubwa."
Zaburi 92:4, 5.

Na Roho Mtakatifu kupitia nabii Isaya alitangaza: "Basi, mtamlinganisha Mungu na nani? Au mtamfananisha na mfano wa namna gani?. . . Je! Hamkujua? Hamkusikia? Hamkuambiwa tokea mwanzo? Hamkufahamu tangu kuwekwa misingi ya dunia? Yeye ndiye anayeketi juu ya duara ya dunia, na hao wanaokaa ndani yake huwa kama panzi; yeye ndiye azitandazaye mbingu kama pazia na kuzikunjua kama hema ya kukaliwa. . . . Mtanifananisha na nani, basi, nipate kuwa sawa naye? Asema yeye aliye Mtakatifu. Inueni macho yenu juu, mkaone; ni nani aliyeziumba hizi; aletaye nje jeshi lao kwa hesabu; aziita zote kwa majina; kwa ukuu wa uweza wake, na kwa kuwa yeye ni hodari kwa nguvu zake; hapana moja isiyokuwapo mahali pake. Mbona unasema, Ee Yakobo, mbona unanena, Ee Israeli, Njia yangu imefichwa, Bwana asiione, na hukumu yangu imempita Mungu wangu asiiangalie? Je! Wewe hukujua? Hukusikia? Yeye Mungu wa milele, Bwana, Muumba miisho ya dunia, hazimii, wala hachoki? . . . Huwapa nguvu wazimiao, humwongezea nguvu **(283)** yeye asiyekuwa na uwezo." "Usiogope, kwa maana mimi ni pamoja nawe; usifadhaike, kwa maana mimi ni Mungu wako; nitakutia nguvu, naam, nitakusaidia, naam, nitakushika kwa mkono wa kuume wa haki yangu." "Niangalieni mimi, mkaokolewe, enyi ncha zote za dunia; maana mimi ni Mungu; hapana mwingine." Huu ni ujumbe ulioandikwa katika vitu vya asili, ambavyo Sabato imeamuriwa ili kuviweka katika kumbukumbu. Wakati Bwana alipowataka Wisraeli waitukuze Sabati, alisema, "Zitakuwa ishara kati ya mimi na ninyi, mpate kujua ya kuwa mimi ndimi Bwana, Mungu wenu." Isaya 40:18-29; 41:10; 45:22; Ezekieli 20:20.

Sabato ilijumuishwa katika sheria iliyotolewa kutoka Sinai; laki hiyo haikuwa mara ya kwanza kwa Sabato kujulikana kwa watu kama siku ya kupumzika. Watu wa Israeli walikuwa wanaifahamu kabla ya kufika Sinai. Katika njia yao hadi Sinai waliitunza. Wakati baadhi walipoikiuka, Bwana aliwakemea, akisema, "Mtakataa kuyashika maagizo yangu na sheria zangu hata lini?" Kutoka 16:28.

Sabato haikuwa kwa ajili ya Israeli hasa, bali kwa ajili ya ulimwengu wote. Ilitambulishwa kwa mwanadamu kule Edeni, na kama matamko mengine ya Amri Kumi, ni wajibu usiokoma. Kuhusu sheria ile ambayo Sabato inafanya sehemu yake, Kristo alisema, "Mpaka mbingu na nchi zitakapoondoka, yodi moja wala nukta moja ya torati haitaondoka katika torati." Kwa kadiri ambavyo mbingu na nchi zinaendelea kuwepo, Sabato itaendelea kuwa kama ishara ya uweza wa Muumba. Na wakati Edeni itakapostawi duniani tena, siku takatifu ya Mungu ya kupumzika itaheshimiwa na wote chini ya jua. "Sabato hata Sabato" wakazi wa nchi mpya iliyotukuzwa watakuja "kuabudu mbele zangu, asema Bwana." Mathayio 5:18; Isaya 66:23.

Hakuna sheria nyingine iliyotolewa kwa Wayahudi iliyokuwa na tabia ya kuwatenganisha kwa ukamilifu kutokana na mataifa yaliyokuwa yanawazunguka kama ilivyokuwa Sabato. Mungu alipanga kwamba kuishika kutawatambulisha wao kama wanaomwabudu Yeye. Ilikuwa iwe kitu cha kuwatenganisha na ibada ya sanamu, na kiunganishi kati yao na Mungu wa kweli. Lakini ili kuitunza kwa utakatifu siku ya Sabato, lazima watu wenyewe wawe watakatifu. Kwa njia ya imani lazima wawe washiriki wa haki ya Kristo. Wakati amri ilipotolewa kwa Waisraeli kwamba, "Ikumbuke siku ya Sabato, uitakase," Bwana aliwaambia pia kwamba, "Mtakuwa watakatifu kwangu." Kutoka 20:8; 22:31. Hivyo tu ndivyo Sabato ingewatambulisha Waisraeli kama watu wanaomwabudu Mungu.

Kadiri Wayahudi walivyoenda mbali na Mungu, na kushindwa kuifanya haki ya Kristo kuwa yao kwa imani, Sabato ilipoteza umuhimu wake kwao. Shetani alikuwa anataka kujitukuza na kuwavuta watu kwenda mbali na Kristo, na alijitahidi kupotosha kuhusu Sabato, kwa sababu ni ishara ya **(284)** uwezo wa Kristo. Viongozi wa Wayahudi walitimiza mapenzi ya Shetani kwa kuizungushia siku ya Mungu ya pumziko mizigo na masharti. Mnamo siku za Kristo Sabato ilikuwa imepotoshwa sana kiasi kwamba utunzaji wake ulikuwa na hali ya ubinafsi na watu wa sheria badala ya sifa ya kumpenda Baba wa mbinguni. Marabi walikuwa karibu kabisa ya kumwonyesha Mungu kana kwamba anatoa sheria ambazo haiwezekani kwa wanadamu kuzitii. Waliwaongoza watu kumtazama Mungu kama mtawala dhalimu, na kufikiri kwamba utunzani wa Sabato, kama alivyotaka, uliwafanya watu wawe na mioyo migumu na kuwa wakatili. Kazi ya Kristo ilikuwa ni kuondosha dhana hizi zisizo sahihi. Ingawa marabi walimfuata kwa shari bila huruma, hakuonekana kwenda sawa na matakwa yao, bali aliendelea mbele, akiishika Sabato kwa mujibu wa sheria ya Mungu.

Siku moja ya Sabato, wakati Mwokozi na wanafunzi wake walipokuwa wanarudi kutoka mahali pa ibada, walitembea kupita katika shamba la nafaka zilizoiva. Yesu alikuwa ameendelea na kazi yake zaidi ya saa za kawaida, na wakati wakipita mashambani, wanafunzi walianza kuchuma masuke, na kula zile punje baada ya kuyafikicha masuke katika mikono yao. Kama ingekuwa siku nyingine tukio hili lisingekuwa na neno lolote, maana mtu apitaye katika shamba la nafaka, bustani ya matunda, au shamba la mizabibu, alikuwa na ruhusa ya kuchuma kiasi alichopenda kula. Angalia Kumbukumbu 23:24, 25. Lakini kufanya hivyo siku ya Sabato kulichukuliwa kama kitendo cha kuhalifu utakatifu. Si tu kwamba kule kuchuma masuke kulikuwa kama namna fulani ya kuvuna, bali pia kule kufikicha masuke katika mikono ilikuwa namna ya kupura nafaka. Hivyo, kwa maoni ya marabi, kulikuwa na kashifa ya makosa mawili.

Mara wapelelezi wale wakamlalamikia Yesu, wakisema, "Tazama! Wanafunzi wako wanafanya neno ambalo si halali kulifanya siku ya sabato."

Wakati Yesu alipolalamikiwa kwa kuvunja Sabato kule Bethzatha, alijitetea kwa kuthibitisha kwamba ni Mwana wa Mungu, na kutangaza kwamba alifanya mambo katika upatanifu na Baba. Na sasa wanafunzi wanaposhtakiwa, anawaelekeza **(285)** washtaki wake katika mfano ulio katika Agano la Kale, vitendo vilivyofanywa siku ya Sabato na wale waliokuwa katika huduma takatifu ya Mungu.

Waalimu wa Wayahudi walijivuna kwa ufahamu wao wa Maandiko, na katika jibu la Mwokozi kulikuwemo kemeo kwao kwa kutojua Maandiko Matakatifu. Alisema, "Hamkulisoma hata hilo alilolifanya Daudi, alipokuwa na njaa, yeye na wale aliokuwa nao? Jinsi alivyoingia katika nyumba ya Mungu, akaitwaa mikate ile ya Wonyesho, akaila akawapa na hao wenziwe, ambayo si halali kuila ila kwa makuhani peke yao." "Akawaambia, Sabato ilifanyika kwa ajili ya mwanadamu, si mwanadamu kwa ajili ya sabato." "Wala hamkusoma katika torati, kwamba siku ya sabato makuhani hekaluni huinajisi sabato wasipate hatia? Lakini nawaambieni, kwamba hapa yupo aliye mkuu kuliko hekalu." "Kwa maana Mwana wa Adamu ndiye Bwana wa sabato." Luke 6:3, 4; Mark 2:27, 28; Matt. 12:5, 6.

Ikiwa ilikuwa sahihi kwa Daudi kukidhi haja ya njaa kwa kuila mikate iliyotengwa wakfu kwa matumizi matakatifu, basi ilikuwa sahihi kwa wanafunzi kukidhi mahitaji yao kwa kuchuma nafaka katika saa takatifu za Sabato. Pia makuhani hekaluni walifanya kazi kubwa siku ya Sabato kuliko siku nyinginezo. Kazi kama ile ile ikifanywa katika mambo yasiyo ya kidini siku ya Sabato ingekuwa dhambi; lakini sasa kazi ile ya makuhani ilikuwa katika huduma ya kazi ya Mungu. Walikuwa wakifanya zile kaida zilizosonda kidole kwa nguvu ya ukombozi ya Kristo, na kazi yao ilikuwa katika upatanifu wa makusudi ya Sabato. Na sasa Kristo mwenyewe amekuja. Wale wanafunzi, wakiwa katika kazi ya Kristo, walikuwa katika kazi ya Mungu, na kile kilichokuwa cha lazima ili kuitekeleza kazi hii ilikuwa sahihi kukifanya siku ya Sabato.

Kristo alikuwa anawafundisha wanafunzi wake na adui zake kwamba huduma kwa Mungu ndiyo ya kwanza kabla ya yote. Kusudi la kazi ya Mungu katika ulimwengu huu ni ukombozi wa mwanadamu; kwa hiyo kile ambacho ni cha muhimu kufanywa siku ya Sabato kwa ajili ya kutekeleza kazi hii kinakubaliana na sheria ya Sabato. Halafu Yesu alifunika hoja yake kwa kujitangaza kuwa Yeye ndiye "Bwana wa Sabato," – Yu juu ya hoja yote na juu ya sheria yote. Mwamuzi huyu asiye na ukomo anawafanya wanafunzi kuondokana na kulalamikiwa kule, akitumia amri zile zile wanazolalamikiwa kuzikiuka.

Kwa kufanya kemeo kwa adui zake Yesu hakuacha mada ile ipite. Alionyesha kwamba kwa upofu wao walikuwa wamekosea kuelewa kusudi la Sabato. Alisema, "Lakini kama mngalijua maana yake maneno haya, Nataka rehema, wala si sadaka, msingaliwalaumu wasio na hatia." Mathayo 12:7. Desturi zao za kidini zisizo za moyoni zilizokuwa nyingi hazikuweza kuwajazia **(286)** upungufu wao wa uadilifu wa kweli na upendo wa huruma ambavyo vitadumu kuwa sifa ya mtu mwenye ibada ya kweli kwa Mungu.

Kwa mara nyingine Kristo aliurudia ukweli ya kwamba dhabihu hazikuwa na thamani yoyote kwa zenyewe tu. Zilikuwa ni nji tu, wala siyo mwisho. Kusudi la hizo ilikuwa ni kuwaelekeza watu kwa Mwokozi, na hivyo kuwaleta katika hali ya kuwa na upatanifu na Mungu. Kitu ambacho Mungu anathamini ni utumishi wa upendo. Wakati jambo hili linapokosekana, mifululizo ya maadhimisho ya ibada tu ni machukizo kwa Mungu. Hivyo ndivyo ilivyo kwa Sabato pia. Ilifanywa ili kuwaleta katika ushirika pamoja na Mungu; lakini akili zilipomezwa katika desturi za kidini zinazochosha, kusudi la Sabato lilizuiwa kutimilika. Kule kuitunza Sabato kwa nje tu kulikuwa ni dhihaka.

Siku nyingine ya Sabato, Yesu alipoingia katika sinagogi, aliona mle mtu mwenye mkono uliopooza. Mafarisayo wakatazama wakiwa na hamu ya kutaka kuona kwamba angefanya nini. Mwokozi alijua vema kwamba kwa kuponya siku ya Sabato angehesabika kama anakiuka, lakini hakusita kuvunjilia mbali ukuta ule wa matakwa ya kimapokeo ulioizunguka Sabato. Yesu alimtaka yule mgonjwa kusimama, halafu akauliza, "Ni halali siku ya sabato kutenda mema, au kutenda mabaya? Kuponya roho au kuiua?" Ilikuwa kanuni ya kawaida miongoni mwa Wayahudi kwamba kushindwa kutenda jambo jema, mahali ambapo mtu alikuwa na fursa ya kufanya hivyo, ilikuwa ni jambo ovu; kupuuza kuokoa maisha ilikuwa ni kuua. Kwa hiyo Yesu alikutana na marabi katika eneo lao. "Wakanyamaza. Akawakazia macho pande zote kwa hasira, akiona huzuni kwa ajili ya ugumu wa mioyo yao, akamwambia yule mtu, Nyosha mkono wako. Naye akaunyosha; mkono wake ukawa mzima tena." Marko 3:4, 5.

Alipoulizwa kwamba, "Ni halali kuponya watu siku ya sabato? Yesu alijibu, "Ni mtu yupi miongoni mwenu mwenye kondoo mmoja, na yule kondoo ametumbukia shimoni siku ya sabato, asiyemshika akamwopoa? Je! Mtu ni bora kuliko kondoo mara ngapi? Basi ni halali kutenda mema siku ya sabato." Mathayo. 12:10-12.

Wapelelezi wale hawakuthubutu kumjibu Kristo mbele ya umati wa watu, kwa hofu ya kujiweka katika matatizo. Walijua kwamba alikuwa amesema ukweli. Kuliko kukiuka mapokeo yao, walikuwa radhi kumwacha mtu akiteseka, lakini wangeweza kumwokoa mnyama ili kuokoa hasara ambayo mmiliki wa mnyama angeipata ikiwa uokoaji wa mnyama huyo ungepuuzwa. Kwa hiyo kujali kukubwa kulielekezwa kwa mnyama kuliko kwa mwanadamu, aliyefanywa kwa sura ya Mungu. Jambo hili ni kielelezo cha jinsi dini za uongo zinavyofanya kazi. Zinaanzisha ndani ya mwanadamu tamaa ya kujitukuza hadi juu kuliko Mungu, lakini zinaishia katika kumshusha mwanadamu **(287)** chini zaidi kuliko mnyama. Kila dini inayofanya vita dhidi ya Mungu inamnyang'anya mtu utukufu uliokuwa wake wakati alipoumbwa, na ambao utarejeshwa ndani yake katika Kristo. Kila dini ya uongo inafundisha watu wanaoifuata kutojali kukidhi mahitaji, mateso na haki za wanadamu. Injili inaweka uthamani mkubwa katika wanadamu kama vitu vilivyonunuliwa kwa damu ya Kristo, na

inafundisha watu kujali kwa huruma mahitaji na matatizo ya mtu. Bwana anasema, "Nitafanya wanadamu kuadimika kuliko dhahabu safi, na watu kuliko dhahabu ya Ofiri." Isaya 13:12.

Wakati Yesu alipowageukia Mafarisayo akiwauliza ikiwa ni halali kutenda mema au mabaya siku ya Sabato, kuokoa maisha au kuua, aliwakanganya na makusudi yao maovu. Wakati Yeye alikuwa akiokoa maisha na kuleta furaha kwa makutano, wao walikuwa wanawinda maisha yake kwa chuki kubwa. Je, ilikuwa bora zaidi kuua siku ya Sabato, kama walivyokuwa wanapanga kufanya, kuliko kuponya mgonjwa, kama alivyokuwa amefanya? Je, ilikuwa ni jambo la haki kuwa na mawazo ya kuua moyoni mnamo siku takatifu ya Mungu kuliko kuwa na upendo kwa watu wote, unaodhirika katika matendo ya huruma?

Katika kuuponya mkono uliopooza, Yesu alihukumu desturi za Wayahudi, na aliiacha amri ya nne ikisimama kama Mungu alivyoileta. "Ni halali kutenda mema siku ya sabato," alisema. Kwa kufagilia mbali vizuizi visivyo maana vya Wayahudi, Kristo aliitukuza Sabato, wakati wale waliomlalamikia walikuwa wanaiharifu siku takatifu ya Mungu.

Wale wanaoshikilia kwamba Kristo aliikomesha sheria wanafundisha kwamba aliivunja Sabato na kuwahalalisha wanafunzi wake kufanya hivyo pia. Kwa hali hiyo wanasimama mahali pale pale walipokuwa Wayahudi wale wabishi. Katika hali hii wanapingana na ushuhuda wa Yesu mwenyewe, aliyesema kwamba, "kama vile mimi nilivyozishika amri za Baba yangu na kukaa katika pendo lake." Yohana 15:10. Mwokozi na wanafunzi wake hawakuivunja sheria ya Sabato. Kristo alikuwa mwakilishi hai wa sheria. Hakuna ukiukaji wa amri takatifu uliokuwemo katika maisha yake. Akiliangalia taifa la mashahidi hawa waliokuwa wanatafuta sababu ya kumhukumu, alisema pasipo kukosoleka kwamba, "Ni nani miongoni mwenu anishuhudiaye ya kuwa nina dhambi?" Yohana 8:46.

Mwokozi hakuwa amekuja kuweka kando kile kilichosemwa na wazee na manabii; maana Yeye mwenyewe ndiye aliyekuwa amenena kupitia wawakilishi hao wa wanadamu. Ukweli wote wa neno la Mungu ulikuja kutoka kwake. Lakini tunu hizi za thamani kubwa isiyo na bei zimewekwa katika mazingira ya uongo. Nuru ya hizo ya thamani imefanywa itumikie makosa. Mungu alitaka ziondolowe katika **(288)** mazingira ya makosa na kuwekwa katika mfumo wa ukweli. Ni nguvu ya uungu tu ambayo ingeweza kufanya kazi hii. Kwa kuunganishwa kwake na makosa, ukweli umekuwa ukitumika kuinufaisha kazi ya adui wa Mungu na mwanadamu. Kristo alikuja kuuweka mahali ambapo utamtukuza Mungu, na kufanya kazi ya wokovu wa mwanadamu.

"Sabato ilifanyika kwa ajili ya mwanadamu, si mwanadamu kwa ajili ya sabato," Yesu alisema. Mambo ambayo yalianzishwa rasmi na Mungu ni kwa ajili ya manufaa ya mwanadamu. "Mambo yote ni kwa ajili yenu." "Kwamba ni Paulo, au Apolo, au Kefa; au dunia, au uzima, au mauti; au vile vilivyopo sasa, au vile vitakavyokuwapo; vyote ni vyenu; nanyi ni wa Kristo, na Kristo ni wa Mungu." 2 Wakorintho 4:15; 1 Wakorintho 3:22, 23. Sheria ya amri kumi, ambayo Sabato ni sehemu yake, ilitolewa na Mungu kwa watu kama mbaraka. Musa alisema, "Bwana akatuamuru kuzifanya amri hizi zote, tumche Bwana, Mungu wetu, tuone mema sikuzote ili atuhifadhi hai kama hivi leo." Kumbukumbu 6:24. Na kupitia kwa mwimbaji wa zaburi ujumbe ulitolewa kwa Israeli, "Mtumikieni Bwana kwa furaha; Njoni mbele zake kwa kuimba; Jueni kwamba Bwana ndiye Mungu; Ndiye aliyetuumba na sisi tu watu wake; Tu watu wake, na kondoo wa malisho yake. Ingieni malangoni mwake kwa kushukuru; Nyuani mwake kwa kusifu; Mshukuruni, lihimidini jina lake." Zaburi 100:2-4. Na kuhusu wote waitunzao sabato wasiivunje, Bwana anasema, "Nitawaleta hao nao hata mlima wangu mtakatifu, na kuwafurahisha katika nyumba yangu ya sala." Isaya 56:6, 7.

"Kwa maana Mwana wa Adamu ndiye Bwana wa sabato." Maneno haya yamejawa na mafundisho na faraja. Kwa kuwa Sabato ilifanyika kwa ajili ya mwanadamu, ni siku ya Bwana. Ni mali ya Kristo. Maana "vyote vilifanyika kwa huyo; wala pasipo yeye hakikufanyika chochote kilichofanyika." Yohana 1:3. Kwa kuwa alifanya vitu vyote, aliifanya Sabato. Ilitengwa na Yeye kama kumbukumbu ya kazi ya uumbaji. Inaelekeza kwake Yeye kama Muumba na Mtakasaji. Inatangaza kwamba Yeye aliyeumba vitu vyote vya mbinguni na duniani, na ambaye vitu vyote vinashikiliwa pamoja kwake, ndiye mkuu wa kanisa, na ya kwamba kwa nguvu zake tumepatanishwa na Mungu. Maana, akiongea kuhusu Israeli, alisema, "Tena naliwapa sabato zangu, ziwe ishara kati ya mimi na wao, wapate kujua ya kuwa mimi, Bwana, ndimi niwatakasaye" – kuwafanya watakatifu. Ezekieli 20:12. Kumbe Sabato ni ishara ya uwezo wa Kristo kutufanya watakatifu. Na inatolewa kwa wote ambao Kristo anawafanya

kuwa watakatifu. Kama ishara ya uwezo wake wa kutakasa, Sabato imetolewa kwa wote ambao kupitia Kristo wanakuwa sehemu ya Israeli wa Mungu.

**(289)** Na Bwana anasema, "Kama ukigeuza mguu wako usihalifu sabato, usifanye anasa yako siku ya utakatifu wangu; ukiita sabato siku ya furaha, na siku takatifu ya Bwana yenye heshima; . . . ndipo utakapojifurahisha katika Bwana." Isaya 58:13, 14. Kwa wote waipokeao Sabato kama ishara ya uwezo wa uumbaji na uokoaji wa Kristo, itakuwa furaha. Kwa kumwona Kristo ndani ya hiyo, wanapata raha ndani yake Yeye. Sabato inawaelekeza katika kazi za uumbaji kama ushuhuda wa uweza wake mkuu wa kuokoa. Wakati inakumbusha mawazoni amani ile ya Edeni iliyopotea, inaeleza kitu kuhusu amani irejeshwayo kupitia Mwokozi. Na kila kitu cha asili kinarudia maneno yake Kristo ya mwaliko kwamba, "Njoni kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha." Mathayo 11:28.

# Sura ya 30
# "Akaweka Watu Kumi Na Wawili"

[Sura hii imejengwa katika Marko 3:13-19; Luka 6:12-16.]

"Akapanda mlimani, akawaita aliowataka mwenyewe; wakamwendea. Akaweka watu kumi na wawili, wapate kuwa pamoja naye, na kwamba awatume kuhubiri."

Chini ya vivuli vya miti iliyo katika kingo za mlima, lakini mbali kidogo kutoka Bahari ya Galilaya, ndipo wale kumi na wawili walipoitwa kuingia katika utume, na ndipo Hubiri la Mlimani lilipotolewa. Mbugani na milimani ndipo palikuwa mahali pa Yesu kutembelea mara kwa mara, na mengi ya mafundisho yake yalitolewa nje mahali pa wazi, kuliko hekaluni au katika sinagogi. Hakuna sinagogi ambalo lingeweza kupokea umati wa watu waliomfuata, lakini si kwa sababu hii tu kwamba alichagua kufundishia mashambani na misituni. Yesu alipenda mandhari ya maumbile ya asili. Kwake kila mahali pa utulivu palikuwa ni hekalu takatifu.

Wakazi wa kwanza wa dunia walichagua mahali pa chini ya miti ya Edeni kuwa hekalu lao takatifu. Pale ndipo Kristo alipokuwa anakutana na baba wa wanadamu wote. Walipofukuzwa kutoka Paradiso, wazazi wetu wa kwanza waliendelea kuabudu mbugani na misituni, na pale Kristo alikutana nao akiwa na injili ya neema yake. Ni Kristo aliyeongea na Ibrahimu chini ya **(291)** mwaloni wa More; na Isaka wakati alipoenda kuabudu kondeni wakati wa jioni; na Yakobo katika mtelemko wa mlima kule Betheli; na Musa katika milima ya Midiani; pamoja na kijana Daudi alipokuwa akichunga kondoo. Ilikuwa ni kwa maelekezo ya Kristo kwamba kwa karne kumi na tano Waebrania walikuwa na kawaida ya kuondoka majumbani mwao kwa juma moja kila mwaka; wakawa wanaishi katika vibanda vilivyotengenezwa kwa matawi ya kijani ya "miti mizuri, na makuti ya mitende, na matawi ya miti minene, na mierezi ya vijitoni." Walawi 23:40.

Katika kuwafundisha wanafunzi wake, Yesu alichagua kuondoka katika vurugu za mjini kwenda mahali pa ukimya makondeni na milimani; ikiwa inaendana na masomo ya kujinyima aliyotaka kuwafundisha. Na wakati wa huduma yake alipenda kuwakusanya watu kwake chini ya mbingu za rangi ya bluu, kwenye mitelemko ya milima yenye nyasi, au pwani kando ya ziwa. Hapa, akiwa amezungukwa na kazi za uumbaji wake, aliweza kubadilisha mawazo ya wasikilizaji wake kutoka katika vitu vya bandia kwenda katika vitu vya asili. Katika kukua na kuendelea kwa vitu vya asili kanuni za ufalme wake zilifunuliwa. Kadiri ambavyo watu wangeinua macho yao kuangalia vilima vya Mungu, na kuzitazama kazi za ajabu za mikono yake, wangejifunza masomo ya thamani ya ukweli wa kimbingu. Mafundisho ya Yesu yangekuwa yanajirudia kwao katika vitu vya asili. Hivyo ndivyo ilivyo kwa wote wanaoenda makondeni wakiwa na Yesu mioyoni mwao. Watahisi kuzungukwa na ushawishi mtakatifu. Vitu vya asili vinabeba mafundisho ya Yesu kwa mifano, na vinayarudia mashauri yake. Kwa kukaa pamoja na Mungu katika vitu vya asili, mawazo yanapaishwa juu, na moyo unapata pumziko.

Hatua ya kwanza ilichukuliwa sasa kulipanga kanisa ambalo baada ya kuondoka kwa Kristo lingekuwa mwakilishi wake duniani. Hakuna hekalu la gharama lililoagizwa kwao, bali Mwokozi aliwaongoza wanafunzi wake kutembelea maeneo aliyopenda, na mawazoni mwao uzoefu mtakatifu wa siku hiyo uliunganishwa daima na uzuri wa milima na mabonde na bahari.

Yesu alikuwa amewaita wanafunzi wake ili kwamba awatume kama mashahidi wake, kuutangazia ulimwengu kile walichokuwa wameona na kusikia kumhusu Yeye. Mamlaka yao ilikuwa ya muhimu kuliko zote ambazo mwanadamu amepata kuitiwa, na ilikuwa ya pili tu kutoka kwa ile ya Kristo mwenyewe. Walikuwa wawe watenda-kazi pamoja na Mungu katika kuuokoa ulimwengu. Kama vile wazee kumi na wawili katika Agano la Kale wasimamavyo kama wawakilishi wa Israeli, hivyo ndivyo ambavyo mitume kumi na wawili wangesimama kama wawakilishi wa kanisa la kiinjili.

Mwokozi alijua tabia za watu wale aliowachagua; udhaifu na mapungufu yao yote yalikuwa wazi kwake; alizijua **(292)** hatari ambazo lazima wangezipitia; wajibu ambao ungewekwa juu yao; na moyo wake uliguswa na watu hawa aliowachagua. Alitumia usiku mzima akiomba kwa ajili yao akiwa peke yake mlimani karibu na Bahari ya Galilaya, wakati wao walikuwa wamelala chini ya mlima. Wakati wa nuru ya kwanza ya mapambazuko aliwaita ili wakutane naye; maana alikuwa na kitu cha muhimu kuwajulisha.

Wanafunzi hawa walikuwa wameshirikiana na Yesu wakati mwingine katika kazi. Yohana na Yakobo, Andrea na Petro, pamoja na Filipo, Nathanaeli, na Mathayo, walikuwa wamekuwa karibu zaidi na Yeye kuliko wengine, na walikuwa wameshuhudia miujiza yake zaidi. Bado Petro, Yakobo na Yohana walikuwa na uhusiano wa karibu zaidi na Yesu. Walikuwa na Yeye karibu muda wote, wakiishuhudia miujiza yake, na kuyasikia maneno yake. Yohana alikuwa na ukaribu zaidi na Yesu, kiasi kwamba anabainishwa kama yeye ambaye Yesu alimpenda. Yesu aliwapenda wote, lakini upendo wake kwa Yohana ulikuwa wa roho ya upendeleo. Alikuwa na umri mdogo kuliko wengine, na akiwa na imani zaidi kama ya mtoto alifungua moyo wake kwa Yesu. Kwa hiyo alipata huruma ya Yesu zaidi, na kupitia kwake mafundisho ya kiroho ya kina zaidi yalipelekwa kwa watu wake Yesu.

Katika orodha ya uongozi wa kundi mojawapo kati ya yale ambamo mitume waligawanywa lipo jina la Filipo. Alikuwa mwanafunzi wa kwanza kupewa amri na Yesu ya kwamba, "Nifuate." Filipo alikuwa mtu wa Bethsaida, mji wa Andrea na Petro. Alikuwa ameyasikiliza mafundisho ya Yohana Mbatizaji, na alisikia tamko la Yohana kuhusu Kristo kama Mwana-kondoo wa Mungu. Filipo alikuwa mtafutaji wa dhati wa ukweli, lakini moyo wake haukuwa mwepesi wa kuamini. Ingawa alikuwa amejiunga kwa Kristo, namna alivyomtangaza Yesu kwa Nathanaeli inaonyesha kwamba alikuwa hajashawishika kikamilifu kuhusu uungu wa Yesu. Ingawa Kristo alikuwa ametamkwa na sauti kutoka mbinguni kwamba ni Mwana wa Mungu, kwa Filipo alikuwa ni "Yesu wa Nazareti, mwana wa Yusufu." Yohana 1:45. Pia, wale watu elfu tano **(293)** walipolishwa, ukosefu wa imani kwa Filipo ulionyeshwa. Yesu aliuliza akiwa anajaribu imani yake akisema, "Tununue wapi mikate, ili hawa wapate kula?" Jibu la Filipo lilikuwa la upande wa kutokuamini, akisema: "Mikate ya dinari mia mbili haiwatoshi, kila mmoja apate kidogo tu." Yohana 6:5, 7. Yesu alihuzunishwa. Ingawa Filipo alikuwa ameona kazi zake na kuhisi uwezo wake, hakuwa na imani. Wakati Wayunani walipomwuliza Filipo kuhusu Yesu, hakutafuta kutumia fursa hiyo kuwatambulisha kwa Mwokozi, bali alienda kumwambia Andrea. Pia, katika saa za mwisho kabla ya kusulibiwa, maneno ya Filipo yalikuwa kama ya kuikatisha tamaa imani. Wakati Tomaso alipomwambia Yesu, "Bwana, sisi hatujui uendako; nasi twaijuaje njia?" Mwokozi alijibu, "Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima. . . . Kama mngalinijua mimi, mngalimjua na Baba." Kutoka kwa Filipo yalikuja maneno yasiyo ya imani kwamba: "Bwana, utuonyeshe Baba, yatutosha." Yohana 14:5-8. Mwanafunzi huyu aliyekuwa na Yesu kwa miaka mitatau alikuwa na moyo wa polepole, mdhaifu wa imani.

Kinyume na kutokuamini kwa Filipo ni imani ya kufurahisha kama ya mtoto ya Nathanaeli. Alikuwa mtu mpole kwa asili, mtu ambaye imani yake ilikuwa imejengwa katika uhalisia usioonekana. Lakini Filipo alikuwa mwanafunzi katika shule ya Kristo, na Mwalimu wa kimbingu alivumilia kwa subira ubutu na kutoamini huku. Wakati Roho Mtakatifu alipomwagwa kwa wanafunzi wale, Filipo alikuja kuwa mwalimu anayefuata utaratibu wa kimbingu. Alijua kuhusu kile alichosema, na alifundisha kwa uhakika ambao ulileta usadikisho kwa watu waliomsikia.

Wakati ambapo Yesu alikuwa akiwaanda wanafunzi wake kwa ajili ya kuwekwa wakfu, mtu ambaye hakuwa ameitwa alijitokeza miongoni mwao. Ni Yuda Iskariote, mtu aliyedai kuwa mfuasi wa Kristo. Sasa alikuja mbele, akitafuta nafasi ndani ya mzingo huu wa katikati wa wanafunzi. Kwa dhati na uchaji mkubwa alisema, "Mwalimu, nitakufuata ko kote uendako." Yesu hakumkataa wala hakumkaribisha, bali alitamka maneno ya kilio: "Mbweha wana pango, na ndege wa angani wana viota; lakini Mwana wa Adamu **(294)** hana pa kulaza kichwa chake." Mathayo 8:19, 20. Yuda aliamini kwamba Yesu ni Masihi; na kwa kujiunga na mitume, alitumaini kupata cheo cha juu katika ufalme mpya. Hii ndiyo hamu ambayo Yesu alitaka kuiondosha kwa kauli yake ile ya kuonyesha umaskini wake.

Wanafunzi walikuwa na hamu kwamba Yuda awe mmoja wao. Alikuwa na umbo la kimamlaka, mtu mwenye maono makini na uwezo wa kutekeleza mambo, na walimthibitisha kwa Yesu kwamba alikuwa mtu ambaye angemsaidia sana kufanikisha mambo katika kazi yake Yesu. Walishangazwa na vile Yesu alivyompokea kwa namna ya kupoa sana.

Wanafunzi walikuwa wamefadhaishwa sana kwamba Yesu hakuwa amejaribu kutafuta kushirikiana na viongozi wa Israeli. Walidhani kwamba ilikuwa ni kosa kwa kuacha kuimarisha kazi yake kwa kupata kuungwa mkono na watu hawa maarufu wenye ushawishi. Ikiwa angemkataa Yuda, mawazoni mwao wangehoji kuhusu hekima ya Bwana wao. Historia ya baadaye ya Yuda ingewaonyesha hatari ya kuruhusu jambo lolote la kidunia liwe na

uzito wakati wa kuamua kuhusu kustahili kwa watu kwa ajili ya kazi ya Mungu. Ushirikiano na watu kama hao ambao wanafunzi walitamani kupata ungeisaliti kazi kwa kuitumbukiza mikononi mwa adui wabaya sana.

Lakini Yuda alipoungana na wanafunzi si kwamba alikuwa hajui uzuri wa tabia ya Kristo. Alihisi ushawishi wa nguvu ile ya uungu iliyokuwa ikiwavuta watu kwa Mwokozi. Yeye ambaye hakuja kuuvunja mwanzi uliopondeka wala kuuzima utambi utokao moshi asingeikataa roho ile ikiwa hata chembe moja tu ya hamu ilikuwa inaifikia nuru. Mwokozi aliusoma moyo wa Yuda; alijua kina cha uovu ambamo Yuda angezama, isipokuwa kama angeokolewa kwa neema ya Mungu. Katika kumwunganisha mtu huyu na Yeye, alimweka mahali ambapo, siku kwa siku, angekutanishwa na upendo wake Yesu usio na ubinafsi. Ikiwa angeufungua moyo wake kwa Kristo, neema ya mbinguni ingeondoa pepo la ubinafsi, na hivyo hata Yuda angekuwa raia wa ufalme wa Mungu.

Mungu huwachukua watu kama walivyo, wakiwa na chembe za kibinadamu katika tabia zao, na huwafundisha kwa ajili ya utumishi wake, ikiwa watafundishika na kujifunza kuhusu Yeye. Hawachaguliwi kwa sababu ya kukamilika kwao, bali ya kwamba licha ya kutokukamilika kwao, kupitia kuujua na kuutenda ukweli, kwa neema ya Kristo, wapate kubadilishwa na kuwa katika sura yake Mungu.

Yuda alikuwa na fursa iliyo sawa na ile ya wanafunzi wengine. Alisikiliza masomo yale yale ya thamani. Lakini kuutenda ukweli, **(295)** ambao ulitakiwa na Kristo, lilikuwa jambo lililo tofauti na matakwa na makusudi ya Yuda, na asingeweza kuachana na maoni yake kwamba apokee hekima kutoka mbinguni.

Ni kwa upendo kiasi gani Mwokozi alishughulika na yeye ambaye angemsaliti! Katika mafundisho yake, Yesu alizama katika kanuni za ukarimu ambazo zilipiga katika mzizi wenyewe wa tamaa ya mali. Aliweka mbele ya Yuda uovu wa tabia ya tamaa, na mara nyingi mwanafunzi huyo aligundua kwamba tabia yake ndiyo inayoonyeshwa, na dhambi yake kuwekwa wazi; lakini hakuweza kuungama wala kuacha tabia yake ya kutokuwa mwenye haki. Alikuwa mtu wa kujitafutia manufaa binafsi, na badala ya kuyapinga majaribu, aliendelea kufuata matendo yake ya udanganyifu. Kristo alikuwa machoni pake, kielelezo kilicho hai cha vile anavyopaswa kuwa kama angeingia katika tafakari na huduma ya kimbingu; lakini somo baada ya somo lilipita katika masikio ya Yuda pasi na kuzingatiwa.

Yesu hakufanya kemeo kali kwake kwa ile tabia yake ya tamaa, bali kwa subira ya kimbingu alimvumilia mtu huyu mwenye makosa, hata kwa kumpa viashiria kwamba aliusoma moyo wake kama kitabu kilicho wazi. Alileta mbele yake vishawishi vya hali ya juu vya kumfanya atende kwa usahihi; na kwa kuikataa nuru ya mbinguni, Yuda asingekuwa na udhuru.

Badala ya kutembea katika nuru, Yuda alichagua kuendeleza mabaya yake. Mawazo maovu ya tamaa, hisia za kisasi, mawazo ya giza na wiza, yaliendelezwa, mpaka Shetani alipokuwa na udhibiti kamili kwake. Yuda akawa mwakilishi wa adui wa Kristo.

Wakati alipokuja karibu na Yesu, alikuwa na baadhi ya sifa za thamani za tabia ambazo zingeweza kufanywa kuwa baraka kwa kanisa. Kama angependa kuvaa nira ya Kristo, huenda angeweza kuwa miongoni mwa wakuu wa mitume; lakini aliufanya moyo wake kuwa mgumu wakati mapungufu yake yalipoonyeshwa, na akiwa katika majivuno na uasi alichagua mivuto yake ya ubinafsi, na kwa njia hiyo aliacha kujistahilisha kwa ajili ya kazi ambayo Mungu angempatia.

Wanafunzi wote walikuwa na mapungufu makubwa sana wakati Yesu alipowaita kuja katika utumishi wake. Hata Yohana, aliyekuwa karibu sana na Yeye aliye mpole na mnyenyekevu, kwa asili hakuwa mpole na mnyenyekevu. Yeye na ndugu yake waliitwa "wana wa ngurumo." Wakati walipokuwa na Yesu, kitendo chochote cha dharau kilichoonyeshwa kwa Yesu kilidhihirisha hasira yao na magomvi. Hisia ovu, kisasi, roho ya ukosoaji, vyote vilikuwa ndani ya mwanafunzi yule. Alikuwa na majivuno, na akipenda kuwa wa kwanza katika ufalme wa Mungu. Lakini siku kwa siku, kwa mkinzano na roho yake ya fujo, aliona huruma na subira ya Yesu, na alisikia mafundisho yake ya unyenyekevu na uvumilivu. Aliufungua moyo wake ili upate mvuto wa kimbingu, **(296)** na akawa si mbebaji tu wa maneno ya Mwokozi bali mtendaji pia. Ubinafsi ulifichwa ndani ya Kristo. Alijifunza kuvaa nira ya Kristo na kubeba mzigo wake.

Yesu aliwakemea wanafunzi wake, aliwaonya na kuwatahadharisha; lakini Yohana na ndugu yake hawakumwacha; walimchagua Yesu, licha ya makemeo yote. Yesu hakuondokana nao kwa sababu ya uovu wao

na makosa yao. Waliendelea mpaka mwisho kushiriki majaribu yake na kujifunza masomo ya maisha yake. Kwa kule kumtazama Kristo, walibadilishwa tabia zao.

Wanafunzi wale walikuwa na tofauti zao katika tabia na silika. Kulikuwa na mtoza ushuru, Lawi-Mathayo, na Simoni mkereketwa mwenye harara, mtu achukiaye mamlaka ya Rumi pasipo kusalimu amri; Petro mkarimu na mwenye mhemko, na Yuda mwenye kujitoa nusu; Tomaso, mwenye moyo wa kweli, lakini mwoga na mwenye hofu, Filipo, mtu wa pole pole sana na mwenye mashaka, na wana wa Zebedayo wenye tamaa ya makuu, na wenzao. Hawa waliletwa pamoja, wakiwa na mapungufu yao tofauti, wote wakiwa na mielekeo ya uovu za kurithi na kuendelezwa; lakini katika Kristo na kupitia Kristo walikuwa wakae katika familia ya Mungu, wakijifunza kuwa kitu kimoja katika imani, katika mafundisho, na katika roho. Wangepata majaribio yao, manung'uniko yao, kutofautiana kwao katika maoni; lakini wakati Yesu anapokaa moyoni, kusingekuwa na kutofikia muafaka. Upendo wake ungewaongoza kupendana; mafundisho ya Mwalimu yangewaongoza katika kuondoa tofauti zote, kuwaleta wanafunzi katika umoja, mpaka wanapokuwa na nia moja na mwelekeo mmoja wa maamuzi. Kristo ndiye kitovu kikuu, nao wangesogeleana wao kwa wao kwa uwiano wa jinsi walivyokisogelea kitovu hicho.

Wakati Yesu alipokuwa amemaliza mafundisho yake kwa wanafunzi, alikusanya lile kundi dogo karibu yake, akiwa amepiga magoti katikati yao, na akiwa amenyosha mikono yake juu ya vichwa vyao, akaomba akiwaweka wakfu kwa ajili ya kazi yake takatifu. Kwa njia hiyo wanafunzi wa Bwana wakawa wametengwa kwa kazi ya injili.

Kristo hachagui malakika ambao kamwe hawajaanguka kuwa wawakilishi wake, bali wanadamu, watu wenye hisia sawa na zile za hao wanaotafuta kuwaokoa. Kristo alichukua uanadamu, kusudi amfikie mwanadamu. Uungu ulihitaji uanadamu; maana ilihitaji uungu na uanadamu ili kuleta wokovu kwa ulimwengu. Uungu ulihitaji uanadamu, ili kusudi uanadamu upate njia ya mawasiliano kati ya Mungu na mwanadamu. Hivyo ndivyo ilivyo kwa watumishi na wajumbe wa Kristo. Mwanadamu anahitaji nguvu nje na zaidi yake mwenyewe, ili kumrejesha katika mfanano na Mungu, na kumwezesha kuifanya kazi ya Mungu; lakini hili **(297)** haliufanyi uwakala wa mwanadamu kutokuwa muhimu. Uanadamu unategemea nguvu za uungu, Kristo hukaa moyoni kwa imani; na kupitia ushirikiano pamoja na uungu, nguvu ya mwanadamu inakuwa na ufanisi kwa ajili ya mema.

Yeye aliyeita mvuvi wa Galilaya bado anaita watu katika utumishi wake. Na yuko tayari kudhihirisha nguvu kupitia sisi vile vile kama alivyofanya kupitia wanafunzi wale wa kwanza. Hata tuwe na mapungufu na dhambi kiasi gani, Bwana ananyosha mkono kwetu kutupatia nafasi ya kushirikiana naye. Anatualika tuje katika mafunzo ya kimbingu, ili, tukiungana naye, tupate kufanya kazi za Mungu.

"Lakini tuna hazina hii katika vyombo vya udongo, ili adhama kuu ya uwezo iwe ya Mungu, wala si kutoka kwetu." 2 Wakorintho 4:7. Hiyo ndiyo sababu injili ilikabidhiwa kwa wanaokosea, badala ya malaika. Inadhihirishwa kwamba nguvu ifanyayo kazi kupitia udhaifu wa mwanadamu ni nguvu ya Mungu; na kwa hiyo tunatiwa moyo kuamini kwamba nguvu inayoweza kusaidia watu wengine ambao ni wadhaifu kama sisi inaweza kutusaidia. Na wale ambao wako "katika hali ya udhaifu" waweze "kuwachukulia kwa upole wao wasiojua na wenye kupotea." Waebrania 5:2. Wakiwa wamekuwa wenyewe pia katika hatari, wanafahamu hatari na ugumu wa njia, na kwa sababu hii wanaitwa ili kuwafikia wengine walio katika hatari. Wapo watu ambao wanatatanika katika mashaka, wakiwa wamelemewa na udhaifu, dhaifu wa imani, na hawana uwezo wa kumtambua Asiyeonekana; lakini rafiki ambaye wanaweza kumwona, akiwajia kwa niaba ya Kristo, anaweza kuwa kiunganishi cha kuifungamanisha kwa Kristo imani yao iliyolegea.

Tunatakiwa kuwa watenda-kazi pamoja na malaika wa mbinguni kwa kumfikisha Yesu ulimwenguni. Malaika wanasubiri kwa hamu ushirikiano wetu; maana lazima mwanadamu awe njia ya kumfikia mwanadamu mwingine. Na pale tunapojitoa kwa Kristo kwa moyo wote, malaika hufurahi ili waongee kupitia sauti zetu kuufunua upendo wa Mungu.

## Sura ya 31

# Hotuba ya Mlimani

[Sura hii imejengwa katika Mathayo 5; 6; 7.]

Ilikuwa nadra kwa Yesu kuwakusanya wanafuzi wake peke yao ili wasikilize maneno yake. Hakuchagua wale tu walioijua njia ya uzima kuwa wasikilizaji wake. Kazi yake ilikuwa ni kuwafikia watu wengi waliokuwa katika ujinga na makosa. Alipeleka mafundisho yake ya ukweli mahali ambapo yangeyafikia mawazo yaliyo gizani. Yeye mwenyewe alikuwa ni Kweli, akiwa amesimama akijifunga kiunoni na mikono iliyonyoshwa daima kubariki, na kwa maneno ya maonyo, kusihi, na kutia moyo, akitafuta kuwainua wote ambao wangekuja kwake.

Hotuba ya Mlimani, ingawa ilitolewa kwa ajili ya wanafunzi hasa, ilitolewa ikisikiwa na makutano wote. Baada ya kuwaweka wakfu mitume, Yesu alienda nao kando ya bahari. Asubuhi na mapema watu walikuwa wameanza kukusanyika mahali hapo. Licha ya umati wa kawaida wa watu kutoka miji ya Galilaya, kulikuwa na watu kutoka Yudea, na hata kutoka Yerusalem kwenyewe; kutoka Perea, kutoka Dikapoli, kutoka Idumaya, mbali zaidi ya kusini mwa Yudea; na kutoka Tiro na Sidoni, miji ya Foenikia katika pwani ya Mediterania. "Waliposikia habari za mambo yote aliyokuwa akiyatenda" walikuja "kumsikiliza na kuponywa magonjwa yao: . . . uweza ulikuwa ukimtoka ukiwaponya wote." Marko 3:8; Luka 6:17-19.

Ule ufukwe mwembamba haukutosha hata kuwapatia nafasi ya kusimama mahali ambapo sauti yake ingewafikia wote waliotamani kumsikia, na Yesu akaongoza njia kurudi maeneo ya pembezoni mwa mlima. Walipofika katika usawa wa nafasi ambao ungeweza kuwapatia mahali panapofaa kukutanika kwa watu wengi, aliketi kwenye majani, na wanafunzi na makutano walifanya hivyo hivyo.

**(299)** Wakati wote nafasi ya wanafunzi ilikuwa karibu na Yesu. Watu walisongamana kwake wakati wote, lakini wanafunzi wakijua kwamba hawakupaswa kusongwa hadi kuondolewa mahali Yesu alipokuwa. Walikaa karibu pembeni yake, ili ya kwamba wasikose hata neno moja katika mafundisho yake. Walikuwa wasikilizaji makini, wakiwa na hamu ya kuelewa ukweli ambao wangeufanya ujulikane katika nchi zote na vizazi vyote.

Wakihisi kwamba jambo fulani ambalo si la kawaida linapaswa litarajiwe, sasa walisogea karibu na Bwana wao. Waliamini kwamba ufalme ulikuwa unakaribia kuanzishwa, na kutoka katika matukio yale ya asubuhi walikusanya uhakika kwamba matangazo fulani yalikuwa yanakaribia kutolewa. Hisia za matarajio yaliughubika umati wote pia, na nyuso zenye hamu ziliashiria matarajio yao. Watu walipokuwa wamekaa kwenye ubavu wa mlima, wakisubiri maneno ya Mwalimu wa kimbingu, mioyo yao ilijazwa na mawazo ya utukufu uliokuwa unakuja. Kulikuwa na waandishi na Mafarisayo ambao walitarajia kuiona siku watakapotawala juu ya Warumi waliochukiwa, na kuwa na utajiri na fahari ya himaya ile kuu ya ulimwengu. Wakulima na wavuvi maskini walitumaini kusikia uhakika kwamba vijumba vyao vya hali ya chini, chakula haba, maisha ya shida, na hofu ya kukosa mahitaji ingebadilika na mahali pake kuwa na makao mazuri ya vitu tele na siku za furaha. Mahali pa vazi lao gumu lile lile moja walilojifunika mchana, na kugeuka blanketi yao usiku, walitumaini kwamba Kristo angewapa majoho ya waliowatawala ya kitajiri na ubora ubora mkubwa. Mioyo yote iliamka kwa matumaini ya majivuno kwamba Israeli ilikuwa inakaribia kutukuzwa machoni pa mataifa kama taifa teule la Mungu, Yerusalemu utukuzwe kama mji mkuu wa ufalme wa ulimwengu wote.

Kristo alikatisha tamaa matumaini ya ukuu wa ulimwenguni. Katika Hotuba ya Mlimani alifanya kazi ya kuiondoa kazi ambayo ilikuwa imeletwa na elimu ya uongo, na kuwapa wasikilizaji wake dhana sahihi ya ufalme wake na ya tabia yake. Lakini hakuyakabili makosa ya watu moja kwa moja. Aliona shida ya ulimwengu kuhusu dhambi, lakini hakuwaonyesha upotofu wao wazi wazi. Aliwafundisha kitu fulani kizuri kwa mbali sana kuliko kile walichokuwa wanajua. Bila kupingana na mawazo yao kuhusu ufalme wa Mungu, aliwaeleza masharti ya kuingia humo, akiwaacha wenyewe wafanye hitimisho lao kuhusu ufalme huo ulivyo. Ukweli ule aliofundisha hauna umuhimu mdogo kwetu kuliko vile ulivyokuwa kwa makutano wale waliomfuata. Uhitaji wetu wa kujifunza kanuni za msingi za ufalme wa Mungu si mdogo kuliko wa watu wale.

Maneno ya kwanza ya Yesu pale mlimani yalikuwa maneno ya baraka. Alisema, Wana heri wale, wanaotambua umaskini wao wa kiroho, na **(300)** wanaohisi kuhitaji kukombolewa. Injili inapaswa ihubiriwe kwa maskini.

Haifunuliwi kwa watu wenye majivuno kiroho, wale wanaojidai kuwa matajiri na wasiohitaji kitu, bali kwa wale wanyenyekevu na watubuo. Chemchemi moja tu imefunuliwa kwa ajili ya dhambi, chemchemi kwa ajili ya walio maskini katika roho.

Moyo wenye kiburi unapambana kupata wokovu; lakini haki yetu ya kuingia mbinguni na kustahili kwetu kuingia humo vinapatikana katika haki ya Kristo. Bwana hawezi kufanya lolote kumrejesha mtu mpaka anapojisalimisha chini ya utawala wa Mungu, akiwa amesadikishwa kuhusu udhaifu wake, na kuondokewa na hali ya kuhisi kujitosheleza mwenyewe. Hapo ndipo anapoweza kupokea kipawa ambacho Mungu anasubiri kutoa. Hakuna kinachofichika katika moyo wake unaohisi kuhitaji. Anaweza kumfikia pasipo vizuizi Yeye ambaye ndani yake utimilifu wote wakaa. "Maana yeye aliye juu, aliyetukuka, akaaye milele; ambaye jina lake ni Mtakatifu; asema hivi; Nakaa mimi mahali palipoinuka, palipo patakatifu; tena pamoja na yeye aliye na roho iliyotubu na kunyenyekea, ili kuzifufua roho za wanyenyekevu, na kuifufua mioyo yao waliotubu." Isaya. 57:15.

"Heri wenye huzuni; Maana hao watafarijika." Kwa maneno haya Bwana hafundishi kwamba huzuni kwa yenyewe tu ina nguvu ya kuondoa hatia ya dhambi. Hatoi ruhusa ya kujionyesha au kuamua kuwa na unyenyekevu wa kujionyesha. Huzuni anayosema hapa siyo ile yenye kuhuzunika na kuomboleza. Wakati tunahuzunika kwa sababu ya dhambi, tunatakiwa tufurahie upendeleo wa thamani wa kuwa watoto wa Mungu.

Mara nyingi tunahuzunika kwa sababu matendo yetu maovu huleta matokeo yasiyo mazuri kwetu; lakini hii siyo toba. Huzuni halisi kwa ajili ya dhambi ni matokeo ya kufanya kazi kwa Roho Mtakatifu. Roho huyo hufunua hali ya kutokuwa na shukrani ya mioyoni mwetu ambayo imemshusha na kumhuzunisha Mwokozi; na hutuleta katika toba chini ya msalaba. Kila dhambi inamfanya Yesu kujeruhiwa upya; na pindi tunapomtazama Yeye tuliyemchoma, tunahuzunika kwa sababu ya dhambi ambazo zimeleta huzuni nyingi kwake. Huzuni ya namna hiyo itaongoza kwenda katika hali ya kuikataa dhambi.

Mtu apendaye vitu vya ulimwengu anaweza akaona kwamba huzuni hii ni udhaifu; lakini ni nguvu zinazomfunga mtu atubuye kwake Yeye wa Milele kwa vifungo ambavyo haviwezekani kuvunjwa. Inaonyesha kwamba malaika wa Mungu wanarudisha kwa nafsi hiyo neema iliyopotea kwa sababu ya ugumu wa moyo na uovu. Machozi yake huyo atubuye ni kama matone ya mvua tu yanayoutangulia mwanga wa jua wa utakatifu. Huzuni hii huja kabla ya furaha ambayo itakuwa chemchemi ya uzima nafsini. "Ungama uovu wako tu; ya kwamba umemwasi Bwana, Mungu wako;" "sitakutazama kwa hasira; maana mimi ni mwenye rehema, asema Bwana." Yeremia 3:13, 12. "Hao waliao katika Sayuni," ameamua kwamba kuwapa **(301)** "taji ya maua badala ya majivu, mafuta ya furaha badala ya maombolezo, vazi la sifa badala ya roho nzito." Isaya 61:3.

Na kwa wale wanaougua katika majaribu na huzuni kuna faraja. Uchungu wa maumivu na kudharauliwa ni mambo mazuri zaidi kuliko kujifurahisha nafsi katika dhambi. Kupitia mateso Mungu hutufunulia madoa katika tabia zetu, ili ya kwamba kwa neema yake tushinde mapungufu yetu. Sura zisizojulikana kuhusu maisha yetu hufunuliwa kwetu, na jaribu huja, kuona kama tutakubali maonyo na mashauri ya Mungu. Tunapoletwa majaribuni, tusiwe na wasiwasi wala kulalamika. Hatupaswi kupinga, au kuwa na mashaka na kwenda nje ya mkono wa Kristo. Tunapaswa tunyenyekeze nafsi mbele za Mungu. Njia za Mungu zimefichika kwake yeye anayetaka kuona vitu katika nuru inayompendeza yeye mwenyewe. Kwa asili ya mwanadamu, njia hizo zinaonekana kuwa na giza sana na zisizo na furaha. Lakini njia za Mungu ni njia za rehema na mwisho wake ni wokovu. Eliya hakujua alichokuwa anafanya wakati aliposema akiwa jangwani kwamba alikuwa ameishi muda wa kutosha, na akaomba kwamba afe. Mungu kwa rehema zake hakumchukua sawasawa na maneno yake. Kulikuwa bado na kazi kubwa ya kufanywa na yeye; na wakati kazi yake ilipokuwa imefanywa, asingepotea katika kukata tamaa na kuwa mpweke jangwani. Hatima yake haikuwa kushuka chini katika mavumbi ya kifo, bali kupanda juu katika utukufu, akibebwa na magari ya mbinguni, kwenda juu penye kiti cha enzi.

Neno la Mungu kwa anayehuzunika ni kwamba, "Nimeziona njia zake; nami nitamponya; nitamwongoza pia, nitamrudishia faraja zake, yeye na hao wanaomlilia." "Nitageuza masikitiko yao kuwa furaha, nami nitawafariji, na kuwafurahisha waache huzuni zao." Isaya 57:18; Yeremia 31:13.

"Heri wenye upole." Magumu ambayo tunapaswa kukutana nayo yanaweza kupunguzwa sana na upole ule unaojificha ndani ya Kristo. Ikiwa tunao unyenyekevu wa Bwana wetu, tutapanda juu kuliko viwango vya matwezo, kupuuzwa, maudhi, ambayo tunakutanishwa nayo kila siku, na yatakoma kutuletea majonzi rohoni.

Kiashirio cha juu zaidi cha uungwana wa Mkristo ni kujitawala. Mtu anayeshindwa kuendeleza utulivu na roho ya tumaini atendewapo mabaya au ukatili anamwibia Mungu haki yake ya kufunua ndani ya mtu huyo ukamilifu wake Mungu wa tabia. Unyenyekevu wa moyo ni nguvu ziletazo ushindi kwa wafuasi wa Kristo; ni kiwakilishi cha mwunganiko wao na mbingu.

"Ingawa Bwana yuko juu, amwona mnyenyekevu." Zaburi 138:6. Wale wanaofunua roho ya upole na ya kujishusha ya Kristo wanapendwa na Mungu. Wanaweza kuonekana kwa ulimwengu kama watu duni, lakini wana thamani kubwa machoni pa Mungu. Si wenye hekima tu, wakuu, wenye fahari, watakaojipatia kibali cha kwenda mbinguni; si **(302)** tu wanaofanya kazi sana, wakiwa na bidii katika kazi pasipo kupumzika. La; maskini katika roho, wanaoutafuta uwepo wa Kristo, wanyenyekevu moyoni, ambao hamu yao kubwa kuliko zote ni kufanya mapenzi ya Mungu, - hawa watapata nafasi tele ya kuingia. Watakuwa miongoni mwa wale ambao wameosha mavazi yao na kuyafanya meupe kwa damu ya Mwana-kondoo. "Kwa hiyo wako mbele ya kiti cha enzi cha Mungu, nao wanamtumikia mchana na usiku katika hekalu lake, na yeye aketiye katika kiti cha enzi atatanda hema yake juu yao." Ufunuo 7:15.

"Heri wenye njaa na kiu ya haki." Hisia ya kutostahili itasababisha moyo kuwa na njaa na kiu kwa ajili ya haki, na hamu hii haitafadhaishwa. Wale wanaotoa nafasi mioyoni mwao kwa ajili ya Yesu watauona upendo wake. Wote wanaotafuta kuwa na tabia inayofanana na Mungu watatoshelezwa. Kamwe Roho Mtakatifu hamwachi bila msaada mtu anayemtazama Yesu. Anachukua mambo yaliyo ya Kristo na kumwonyesha mtu huyo. Ikiwa jicho linakazwa likimtazama Kristo, kazi ya Roho haikomi mpaka mtu huyo anapofananishwa na sura yake Kristo. Hali ile safi ya upendo inatanua nafsi, ikiipatia uwezo wa kupata zaidi, kwa ajili ya ongezeko la kujua mambo ya mbinguni, ili ya kwamba isikose kujazwa. "Heri wenye njaa na kiu ya haki; maana hao watashibishwa."

Wenye rehema watapata rehema, na wenye moyo safi watamwona Mungu. Kila wazo chafu huchafua moyo, inalemaza hisia za maadili, na lina tabia ya kuharibu hali ya uwepo wa Roho Mtakatifu. Linahafifisha maono ya kiroho, kiasi kwamba watu hawawezi kumwona Mungu. Bwana anaweza na huwa anamsamehe mdhambi atubuye; lakini ingawa husamehewa, nafsi inakuwa imechafuliwa. Lazima uchafu wote wa maneno au mawazo uepukwe na yeye ambaye anapenda kuwa na maono angavu ya ukweli wa roho.

Lakini maneno ya Kristo yanahusu mambo zaidi ya hali ya kutokuwa na uchafu wa kihisia, ni zaidi ya kutokuwa na unajisi wa maadhimisho ambayo Wayahudi walijitahidi kuyaepuka. Ubinafsi unatuzuia kumwona Yesu. Roho itafutayo mambo yake binafsi inachukulia mambo ya Mungu yote kwa ujumla kwamba yako vile ilivyo. Tusipoacha tabia hii, hatuwezi kumwelewa Yeye aliye pendo. Moyo usio na ubinafsi tu, roho yenye unyenyekevu na uaminifu, ndio utakaomwona Mungu kama "mwingi wa huruma, mwenye fadhili, si mwepesi wa hasira, mwingi wa rehema na kweli." Kutoka 34:6.

"Heri wapatanishi." Amani ya Kristo inazaliwa na ukweli. Inakubaliana na Mungu. Ulimwengu uko katika uadui na sheria ya Mungu; **(305)** wadhambi wako katika uadui dhidi ya Muumba wao; na kama matokeo yake wamekuwa katika uadui baina ya wao kwa wao. Lakini mwimbaji wa zaburi anasema, "Wana amani nyingi waipendao sheria yako, Wala hawana la kuwakwaza." Zaburi 119:165. Wanadamu hawawezi kutengeneza amani. Mipando ya mwanadamu kwa ajili ya kusafisha na kumwinua mtu au jamii itashindwa kuzalisha amani, kwa sababu haiufikii moyo. Nguvu pekee inayoweza kuumba au kuendeleza amani ya kweli ni neema ya Kristo. Hii inapopandikizwa moyoni, itaondoa tamaa za uovu zinazosababisha mapigano na kutoelewana. "Badala ya michongoma utamea msonobari, na badala ya mibigili, mhadesi;" na jangwa la maisha "litashangilia na kuchanua maua kama waridi." Isaya 55:13; 35:1.

Makutano walishangazwa na mafundisho haya, ambayo yalionekana kuwa tofauti na amri walizozijua na mafundisho ya Mafarisayo. Watu walikuwa wanadhani kwamba furaha ilikuwa katika vitu vya ulimwengu huu, na ya kwamba umaarufu na heshima ya watu vilikuwa vitu vya kutamaniwa sana. Lilikuwa jambo la kufurahisha sana kwa mtu kuitwa “Rabi,” na kusifiwa kama mwenye kujua sana na mtu wa dini, wema wake ukianikwa hadharani upate kuonekana. Hali hii ilichukuliwa kama ndiyo kilele cha furaha. Lakini kwa makutano wale, Yesu alitangaza kwamba vitu na heshima za dunia ni zawadi zote ambazo mtu wa namna hiyo angeweza kupata daima. Alisema kwa uhakika, maneno yake yakiwa na nguvu ya kushawishi. Watu walinyamazishwa, na hisia ya hofu ikawajia. Waliangaliana mtu na mwenzake kwa mashaka. Ikiwa maneno ya mtu huyu ni ya kweli ni nani

angeokoka? Wengi walishawishika kuamini kwamba Mwalimu huyu wa pekee aliwezeshwa na Roho wa Mungu, na ya kwamba mambo aliyotamka yalikuwa na uungu.

Baada ya kufafanua mambo yanayounda furaha ya kweli, na namna inavyopatikana, Yesu alionyesha kwa uwazi zaidi wajibu wa wanafunzi wake, kama walimu waliochaguliwa na Mungu kuwaongoza wengine katika njia ya haki na uzima wa milele. Alijua kwamba wangepatwa na fadhaa na kukata tamaa, kwamba wangekumbana na upinzani mkali, kwamba wangetukanwa, na ushuhuda wao ungekataliwa. Alijua vema kwamba wakati wa kutekeleza wajibu wao, watu haya wanyenyekevu ambao walisikiliza maneno yake kwa makini wangekubwa na mashtaka ya uongo, mateso, kufungwa gerezani, na kifo, na akaendelea hivi:

"Heri wenye kuudhiwa kwa ajili ya haki; Maana ufalme wa mbinguni ni wao. Heri ninyi watakapowashutumu na kuwaudhi na kuwanenea kila neno baya kwa uongo, kwa ajili yangu. Furahini, na kushangilia; kwa kuwa **(306)** thawabu yenu ni kubwa mbinguni; kwa maana ndivyo walivyowaudhi manabii waliokuwa kabla yenu."

Ulimwengu unapenda dhambi, na unachukia haki, na hii ndiyo iliyokuwa sababu ya chuki yake kwa Yesu. Wote wanaolikataa pendo lisilo mwisho la Kristo watauona Ukristo kama kitu kinacholeta usumbufu. Nuru ya Kristo hufagilia mbali giza linalofunika dhambi zao, na uhitaji wa matengenezo unakuwa dhahiri. Wakati wale wanaojikabidhi katika nguvu za Roho Mtakatifu wanaanza kujipiga vita wao wenyewe, wale wanaong'ang'ania dhambi hupiga vita ukweli na wale wanaouwakilisha.

Mapambano hutokea, na wafuasi wa Kristo hushtakiwa kwamba ni wataabishaji wa watu. Lakini ni kule kuwa pamoja na Mungu kunakowaletea uadui dhidi ya ulimwengu. Wanakutana na dhihaka alizofanyiwa Kristo. Wanatembea katika njia aliyopita mtu mwema kuliko wote duniani. Lazima wakutane na mateso kwa furaha, wala si kwa huzuni. Kila moto wa majaribu ni njia ya Mungu ya kuwatakasa. Kila jaribu linawafanya kufaa kuwa watenda-kazi pamoja naye. Kila shida ina nafasi yake katika lile pambano kuu kwa ajili ya haki, na kila moja litaongeza kitu katika furaha ya ushindi wao wa mwisho. Wakiwa na picha hii, kujaribiwa kwa imani yao na subira vitakubaliwa kwa furaha badala ya kuonekana kuwa vitu vya kutisha na vya kujikinga navyo. Wakiwa na hamu ya kutimiza wajibu wao kwa ulimwengu, wakikaza tumaini lao katika kukubaliwa na Mungu, watumishi wake watatekeleza kila jukumu, bila kujali hofu au kupendwa na wanadamu.

"Ninyi ni chumvi ya dunia," alisema Yesu. Msijitenge na ulimwengu ili kukwepa mateso. Lazima mkae miongoni mwa wanadamu, ili ladha ya upendo wa mbinguni iwe kama chumvi katika kukinga ulimwengu usiharibike.

Mioyo inayoitikia ushawishi wa Roho Mtakatifu ni mifereji ambayo mibaraka ya Mungu hutiririshiwa humo. Ikiwa wale wamtumikao Mungu wataondolewa duniani, na Roho wake akaondolewa kati ya wanadamu, ulimwengu huu utaachwa katika uharibifu na uangamivu, tunda la utawala wa Shetani. Ingawa waovu hawajui hilo, wanapata mibaraka ya maisha haya kwa sababu ya kuwepo duniani humu kwa watu wa Mungu ambao wao wanawadharau na kuwakandamiza. Lakini ikiwa Wakristo ni wa jina tu, wanakuwa kama chumvi ambayo imeharibika. Haina ushawishi wowote kwa ajili ya jambo jema ulimwenguni. Kwa kule kumwakilisha Mungu isivyo sahihi wanakuwa wabaya zaidi kuliko hata wasioamini.

"Ninyi ni nuru ya ulimwengu." Wayahudi walitafuta kuyabania manufaa ya wokovu katika taifa lao peke yake; lakini Kristo aliwaonyesha kwamba **(307)** wokovu ni kama mwanga wa jua. Ni kwa ajili ya ulimwengu wote. Dini ya Biblia haipaswi kufunikwa ndani ya majalada ya kitabu hicho, wala ndani ya kuta za jengo la kanisa. Haipaswi kutolewa nje katika matukio fulani tu kwa ajili yetu wenyewe, na halafu kuhifadhiwa vizuri kwa kuwekwa kando tena. Ni kwa ajili ya kutakasa maisha ya kila siku, kujidhihirisha katika kila muamala wa shughuli na katika mahusiano yetu yote ya kijamii.

Tabia ya kweli haitengenezwi kutokea nje, na kuvaliwa; inaangaza kutoka ndani. Ikiwa tunataka kuwaelekeza wengine katika njia ya haki, lazima kanuni za haki zimulike katika mioyo yetu. Kutangaza kwetu imani kunaweza kutangaza nadharia ya dini, lakini kujitoa kwetu kwa vitendo ndiko kunakobeba neno la kweli. Maisha thabiti, mazungumzo matakatifu, uadilifu usioyumba, roho yenye uhai, ya ukarimu, kielelezo cha uchaji wa Mungu, - hizi ndizo njia zinazopitishiwa nuru kuja ulimwenguni.

Yesu hakuzama katika mambo ya sheria, lakini hakuwaacha wasikilizaji wake kuhitimisha kwamba alikuwa amekuja kuondoa matakwa ya sheria. Alijua kwamba wapelelezi walikuwa tayari kufuatilia kila neno ambalo

lingetimiza kusudi lao. Alijua itikadi zilizokuwa katika mawazo ya wengi wa wasikilizaji, na hakusema lolote la kuondoa imani yao katika dini na taratibu walizokabidhiwa na Musa. Kristo mwenyewe alikuwa ameweka sheria ya maadili na sheria ya maadhimisho. Hakuja kuharibu kile alichoweka mwenyewe. Ilikuwa ni kwa sababu ya heshima yake kwa sheria na manabii kwamba alitafuta kuuvunja ukuta wa mapokeo uliowafunga Wayahudi. Huku akiondoa na kuweka kando tafsiri zisizo sahihi za sheria, aliwaongoza wanafunzi kwa uangalifu dhidi ya kuachana na ukweli wa thamani uliokabidhiwa kwa Waebrania.

Mafarisayo walijivuna kwamba wanaitii sheria; lakini walijua kidogo sana kuhusu kanuni za sheria katika matendo ya kila siku kiasi kwamba maneno ya Mwokozi yalikuwa kama uzushi kwao. Kadiri alivyofagilia mbali uchafu uliokuwa umefunika ukweli, wao walifikiri kwamba alikuwa anafagilia mbali ukweli wenyewe. Walinong'onezana kwamba alikuwa anahafifisha sheria. Yeye alisoma mawazo yao, na akawajibu, akisema:

"Msidhani ya kuwa nalikuja kuitangua torati au manabii; la, sikuja kutangua, bali kutimiliza." Hapa Yesu anafuta madai ya Mafarisayo. Kazi yake kwa ulimwengu ni kuhalalisha matakwa matakatifu ya sheria waliyodai kwamba anaivunja. Ikiwa sheria **(308)** ya Mungu ingekuwa imebadilishwa au kuondolewa, Kristo asingeteseka kama matokeo ya kuasi kwetu. Alikuja kufafanua uhusiano kati ya sheria na mwanadamu, na kufafanua maagizo yaliyomo kwa njia ya maisha yake mwenyewe ya utii.

Mungu ametupatia amri zake takatifu, kwa sababu anampenda mwanadamu. Anafunua kanuni za haki ili kutukinga na matokeo ya kuasi. Sheria ni udhihirisho wa mawazo ya Mungu; inapopokelewa katika Kristo, inakuwa ndiyo mawazo yetu. Inatuinua juu zaidi ya tamaa na mienendo ya asili, juu ya vishawishi vinavyoongoza kwenda dhambini. Mungu anatamani tuwe na furaha, na alitupatia maagizo ya sheria ili ya kwamba kwa kuyatii tupate furaha. Yesu alipozaliwa wakati malaika walipoimba, "Atukuzwe Mungu juu mbinguni, Na duniani iwe amani kwa watu aliowaridhia." (Luke 2:14), walikuwa wakiitangaza misingi ya sheria aliyokuwa amekuja kuitukuza na kuiheshimisha.

Wakati sheria ilipotamkwa pale Sinai, Mungu aliufanya utakatifu wa tabia yake ujulikane kwa watu, ya kwamba kwa tofauti iliyopo kati yao na Mungu wagundue tabia yao ya dhambi. Sheria ilitolewa kuwasadikisha kuhusu dhambi, na kufunua namna walivyomhitaji Mwokozi. Ingefanya kazi hiyo kwa kadiri kanuni zake zilivyofanyishwa kazi moyoni na Roho Mtakatifu. Bado inapaswa kuendelea kufanya kazi hiyo. Katika maisha ya Kristo kanuni za sheria zinawekwa wazi; na kadiri Roho Mtakatifu anavyougusa moyo, kadiri nuru ya Kristo inavyowafunulia watu hitaji lao la damu yake itakasayo na haki yake istahilishayo, sheria bado ni njia ya kutuleta kwa Kristo, ili tupate kuhesabiwa haki (kustahilishwa) kwa imani. "Sheria ya Bwana ni kamilifu, Huiburudisha nafsi. Ushuhuda wa Bwana ni amini, Humtia mjinga hekima." Zaburi 19:7.

"Mpaka mbingu na nchi zitakapoondoka," alisema Yesu, "yodi moja wala nukta moja ya torati haitaondoka katika torati, hata yote yatimie." Jua linaloangaza mbinguni, nchi tunayokanyaga, ni mashahidi wa Mungu washuhudiao kwamba sheria ya Mungu haibadiliki na ni ya milele. Ingawa hivyo vinaweza kupita, amri za kimbingu zitadumu. "Lakini ni vyepesi zaidi mbingu na nchi vitoweke, kuliko itanguke nukta moja ya torati." Luka 16:17. Mifumo ya mfano iliyosonda kidole kwa Yesu kama Mwana-kondoo wa Mungu ingekomeshwa wakati wa kifo chake; lakini maagizo ya Amri Kumi hayafutiki kama kilivyo kiti cha enzi cha Mungu.

Kwa kuwa "sheria ya Bwana ni kamilifu," lazima kila tendo lililo tofauti na hiyo ni uovu. Wale wasiotii amri za Mungu, na kuwafundisha wengine **(309)** hivyo, wanahukumiwa na Kristo. Maisha ya Mwokozi ya utiifu yalidumisha matakwa ya sheria; yalithibitisha kwamba kumbe sheria ilikuwa inawezekana kushikwa na mwanadamu, na yalionyesha uzuri wa tabia ambao ungeletwa na utii. Wote wanaotii kama alivyofanya wanatangaza vile vile kwamba sheria ni "takatifu, na ya haki, na njema." Warumi 7:12. Kwa upande mwingine, wote wanaovunja amri za Mungu wanaendeleza madai ya Shetani kwamba amri si za haki na haziwezekani kushikwa. Kwa njia hiyo wanaunga mkono udanganyifu wa mpinzani mkuu, na kuonyesha kutokumheshimu Mungu. Hao ni watoto wa yule mwovu, aliyekuwa muasi wa kwanza wa kupinga sheria ya Mungu. Kuwakubali hao waingie mbinguni ingekuwa ni kuingiza humo vitu visivyokubaliana na tena vya uasi, na kuhatarisha ustawi wa viumbe vya malimwengu. Hakuna mtu ambaye kwa makusudi anaacha kujali kanuni moja ya sheria atakayeingia katika ufalme wa mbinguni.

Marabi walichukulia haki yao kama tiketi ya kwenda mbinguni; lakini Yesu aliitangaza kuwa haitoshi na haistahili. Maadhimisho ya nje na kujua nadharia na ukweli ndizo zilizounda haki ya Kifarisayo. Marabi walidai kuwa watakatifu kwa njia ya jitihada zao za kuishika sheria; lakini matendo yao yalikuwa yameiondoa haki kutoka katika dini. Wakati walikuwa wakijali sana kuadhimisha desturi za kidini, maisha yao yalikuwa yasiyo na maadili na ya viwango vya chini. Kile kilichoitwa haki kwao kisingeingia kamwe katika ufalme wa mbinguni.

Udanganyifu mkuu kuliko wote katika akili ya mwanadamu mnamo wakati wa Kristo ulikuwa ni kwamba ukubali tu wa ukweli ndio kuhesabiwa haki. Katika uzoefu wote wa mwanadamu kujua nadharia ya ukweli kumethibitika kuwa hakutoshi kuiokoa nafsi ya mtu. Hakuzai matunda ya haki. Mtazamo wenye wivu wa kile kinachoitwa ukweli wa kithiolojia mara nyingi unaenda pamoja na chuki dhidi ya ukweli halisi unaodhihirishwa katika maisha. Vipindi vya giza kubwa mno vya historia vimebeba kumbukumbu ya uhalifu uliofanywa na wanadini wasio na uvumilivu. Mafarisayo walijidai kuwa ni watoto wa Ibrahimu, na walijivuna kwa kuwa na mausia ya Mungu; lakini manufaa haya hayakuwazuia kuwa na ubinafsi, mwelekeo wa kutenda maovu, tamaa ya mali, na unafiki mkubwa. Walijidhania kuwa ni wanadini wakubwa wa dunia, lakini kile kiitwacho kushika dini kiliwaongoza katika kumsulibisha Bwana wa utukufu.

Hatari ile ile bado ipo. Wengi wanachukulia kwa mzaha kwamba wao ni Wakristo, kwa kuwa tu wamesajiliwa katika itikadi ya imani fulani. Lakini hawajauleta ukweli katika maisha kwa vitendo. Hawajauamini na kuupenda, kwa hiyo hawajapokea nguvu na **(310)** neema ile ijayo kwa njia ya utakaso wa ukweli. Watu wanaweza kutangaza imani katika ukweli wake; lakini kama haiwafanyi kuwa wanyofu, wema, wenye subira, wastahimilivu, wanaotafakari ya mbinguni, imani hiyo ni laana kwao walio nayo, na kwa ushawishi wao inakuwa laana kwa ulimwengu.

Haki iliyofundishwa na Yesu ni hali ya moyo na maisha kuwa katika upatanifu na mapenzi ya Mungu. Wenye dhambi wanaweza kuwa na haki tu pale wanapokuwa na imani katika Mungu na kuendeleza mwunganiko thabiti na Yeye. Uchaji wa Mungu utainua mawazo yao na kuyafanya maisha kuwa mema. Halafu miundo ya nje ya kidini itafuata usafi wa ndani wa Mkristo. Hapo ndipo taratibu za maadhimisho zinazotakiwa katika ibada ya Mungu haziwi kaida zisizo na maana, kama zile za Mafarisayo wanafiki.

Yesu alizichukua amri moja moja, na kufafanua kina na mapana ya matakwa yaliyomo. Badala ya kuondoa yodi moja ya nguvu zake, anaonyesha jinsi kanuni zake zinavyofika mbali, na anaweka wazi makosa makubwa ya Wayahudi katika utii wao wa kujionyesha kwa nje. Anatangaza kwamba kwa wazo ovu au kuangalia kwa kutamani amri ya Mungu inavunjwa. Yeye anayeshiriki katika jambo dogo kabisa lisilo la haki anaivunja sheria na kuhafifisha asili yake mwenyewe ya maadili. Uuaji unakuwepo mawazoni kwanza. Yeye anayeipatia chuki nafasi moyoni mwake anauweka mguu wake katika njia ya mwuaji, na matoleo yake hayakubaliki kwa Mungu.

Wayahudi waliendeleza roho ya kisasi. Katika chuki yao dhidi ya Warumi walitoa matamko magumu ya hukumu, na walimfurahisha yule mwovu kwa kule kudhihirisha tabia zake. Kwa njia hiyo walikuwa wakijipatia mafunzo ya kutenda mambo ya kutisha ambayo aliwaongoza kuyatenda. Katika maisha ya kidini ya Mafarisayo hakukuwa na kitu kilichowahimiza kuwa na huruma kwa Wamataifa. Yesu aliwataka wasijidanganye mioyoni mwao kwa mawazo kwamba wangeweza kuwainukia wale waliowakandamiza, na kuendeleza hamu yao ya kuwalipizia kisasi cha mabaya yao.

Ni kweli kwamba ipo hasira ambayo ina uhalali, hata miongoni mwa wafuasi wa Kristo. Wakati wanapoona kwamba Mungu haheshimiwi, na ibada zake zinawekwa katika ubatili, wakati wanapoona asiye na hatia akionewa, hasira ya haki inawaka rohoni. Hasira ya namna hiyo, inayotokana na hisia za maadili, si dhambi. Lakini wale ambao wanahisi kuwa na uhuru wa kuamsha hasira katika jambo lolote au kuchukizwa na lolote wanamfungulia moyo Shetani. Lazima uchungu na hisia za uadui ziondolewe moyoni kama tunataka kuwa katika upatanifu na mbingu.

Mwokozi anaenda mbali zaidi kuliko hapo. Anasema, "Basi ukileta sadaka yako madhabahuni, na huku ukikumbuka ya kuwa ndugu yako ana neno juu yako, iache sadaka yako mbele ya madhabahu, uende zako, upatane kwanza **(311)** na ndugu yako, kisha urudi uitoe sadaka yako." Wengi wana juhudi katika mambo ya ibada, wakati baina yao na ndugu zao kuna tofauti mbaya zinazopaswa kupatanishwa. Mungu anawataka

wafanye yote yaliyo ndani ya uwezo wao kurejesha mapatano. Wasipofanya hivyo, Mungu hapokei ibada zao. Wajibu wa Mkristo katika jambo hili umewekwa bayana kwa uwazi.

Mungu humwaga mibaraka yake kwa wote. "Huwaangazia jua lake waovu na wema, huwanyeshea mvua wenye haki na wasio haki." Yeye ni "mwema kwa wasiomshukuru, na waovu." Luka 6:35. Anatutaka tuwe kama Yeye. "Wapendeni adui zenu," alisema Yesu; "watendeeni mema wale ambao wawachukia ninyi, . . .ili mpate kuwa wana wa Baba yenu aliye mbinguni." Hizi ndizo kanuni za sheria, na ndizo chemchemi za visima vya uzima.

Kanuni za maisha atakazo Mungu kwa ajili ya watoto wake ziko juu kuliko mahali ambapo mawazo ya juu mno ya mwanadamu yanaweza kufika. "Basi ninyi mtakuwa wakamilifu, kama Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu." Amri hii ni ahadi. Mpango wa wokovu unatafakari kuhusu ureshwaji wetu ulio mkamilifu kutoka katika nguvu za Shetani. Mara zote Kristo huitenganisha nafsi itubuyo na dhambi. Alikuja kuziharibu kazi za mwovu, na ameahidi ya kwamba Roho Mtakatifu ataingizwa ndani ya kila nafsi inayotubu, ili kuifanya isitende dhambi.

Kujaribiwa na mwovu kusitumiwe kama udhuru kwa jambo baya linalotendwa. Shetani anashangilia ushindi anaposikia watu wanaoitwa wafuasi wa Kristo wakitoa udhuru kwa tabia yao mbaya. Udhuru huu ndio unaoongoza kuelekea katika dhambi. Hakuna udhuru kwa dhambi. Tabia takatifu, maisha ya Kikristo, yanapatikana kwa kila mtoto wa Mungu aaminiye na kutubu.

Tabia inayotakiwa kwa Mkristo ni kule kuwa kama Kristo. Kama vile Mwana wa Adamu alivyokuwa mkamilifu katika maisha yake, ndivyo wafuasi wake wanavyotakiwa kuwa wakamilifu katika maisha yao. Katika mambo yote Yesu alifanyika kuwa kama ndugu zake. Alifanyika kuwa mwili, kama tulivyo. Alipatwa na njaa na kiu na uchovu. Alipata nguvu kwa chakula na kurejesha hali nzuri kwa usingizi. Alishiriki sehemu ya mwanadamu; lakini bado alikuwa Mwana wa Mungu asiye na waa. Alikuwa Mungu katika mwili. Tabia yake na iwe yetu. Bwana anasema hivi kuhusu wale wanaomwamini, "Nitakaa ndani yao, na kati yao nitatembea, nami nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu wangu." 2 Wakorintho 6:16.

Kristo ndiye ile ngazi iliyoonwa na Yakobo, miguu ya ngazi hiyo ikiwa chini duniani, na sehemu yake ya juu ikifika katika lango la mbinguni, kwenye utukufu wenyewe. Ikiwa ile ngazi ingeshindwa kufika duniani hata kwa hatua moja, tungekuwa tumepotea. Lakini Kristo alitufikia mahali tulipo. Alichukua hali yetu na akashinda, ili ya kwamba na sisi kwa kuchukua **(312)** hali yake tupate kushinda. Katika kufanyika "katika mfano wa mwili ulio wa dhambi" (Warumi 8:3), aliishi maisha yasiyo ya dhambi. Kwa uungu wake anashikilia kwenye kiti cha enzi, wakati kwa ubinadamu wake anatufikia. Anatubidisha tuuendee utukufu wa tabia ya Mungu kwa imani katika Yeye. Kwa hiyo yatupasa kuwa wakamilifu, kama vile Baba yetu "aliye mbinguni alivyo mkamilifu."

Yesu alikuwa ameonyesha vitu vinavyounda haki, na alikuwa ameelekeza kwa Mungu kwamba ndiye chanzo cha haki hiyo. Sasa aligeukia wajibu wa mambo ya matendo. Alisema kwamba, katika sadaka, katika sala, katika kufunga, kisifanyike chochote kwa kusudi la kuvutia watu au kujipatia sifa binafsi. Toa kwa dhati, kwa manufaa ya maskini wanaoteseka. Katika maombi, hebu roho ijisikie kuwa pamoja na Mungu. Katika kufunga, usiende na kichwa kilichoinamishwa, na moyo ukiwa umejawa na mawazo ya ubinafsi. Moyo wa Farisayo ni udongo usio na mimea na usio na faida, ambao ndani yake hakustawi mbegu za maisha ya kimbingu. Mtu ajitoaye kikamilifu kwa Mungu ndiye tu atakayemtolea Yeye ibada ya kukubalika. Maana kwa kujumuika pamoja na Mungu wanadamu wanakuwa watenda-kazi pamoja naye kwa kuonyesha tabia yake miongoni mwa wanadamu.

Huduma itolewayo kwa moyo wa dhati ina thawabu kubwa. "Baba yako aonaye sirini atakujazi." Kwa maisha tuishiyo kwa rehema ya Kristo tabia inajengeka. Upendo ule ulio halisi unaanza kurejeshwa nafsini. Sifa za tabia ya Kristo zinajazwa, na sura ya Mungu inaanza kuangaza. Nyuso za wanaume na wanawake wanaotembea na kufanya kazi pamoja na Mungu huonyesha amani ya mbinguni. Wanazungukwa na hali ya mbinguni. Kwa nafsi hizi ufalme wa Mungu unakuwa umeanza. Wanayo furaha ya Kristo, furaha ya kuwa mbaraka kwa wanadamu. Wana heshima ya kukubaliwa kwa ajili ya kutumiwa na Bwana; wameaminiwa kufanya kazi yake katika jina lake.

"Hakuna mtu awezaye kutumikia mabwana wawili." Hatuwezi kumtumikia Mungu tukiwa na moyo uliogawanyika. Dini ya Biblia si mvuto mmoja ulio miongoni mwa mivuto mingine; lazima mvuto wa dini ya Biblia uwe wa juu zaidi, ulioenea kote na kutawala mingine yote. Haipaswi kuwa kama vistari vya rangi

vilivyochorwa hapa na pale kwenye turubai, bali lazima ienee katika maisha yote, kama vile turubai iliyotoswa katika rangi, hadi kila uzi wake uwe umeshika rangi kwa njia ya kutoswa kabisa.

"Basi jicho lako likiwa safi, mwili wako wote utakuwa na nuru. Lakini jicho lako likiwa bovu, mwili wako wote utakuwa na giza." Usafi na uthabiti wa nia ni masharti ya kupokea nuru kutoka kwa Mungu. Yeye atamaniye kuujua ukweli lazima awe radhi kukubali vyote vinavyofunuliwa katika huo. Hawezi kufanya maafikiano na makosa. Kuyumbayumba **(313)** na kushika ukweli nusu ni kuchagua giza la makosa na imani potofu ya kishetani.

Taratibu za ulimwengu na kanuni zisipinda za haki havichangamani pamoja hata kidogo, kama ilivyo kwa rangi za upinde wa mvua. Mstari mpana na unaoonekana umechorwa na Mungu wa milele katikati ya mambo hayo mawili. Mwonekano wa Kristo unasimama ukiwa bora sana tofauti na ule wa Shetani kama vile mchana wa adhuhuri unavyokinzana na usiku wa manane. Na ni wale tu wanaoishi maisha ya Kristo walio watenda-kazi pamoja naye. Ikiwa kuna dhambi moja inayoendelea kubebwa nafsini, au kuna tendo baya linaloendelezwa maishani, mtu anakuwa umenajisika katika mambo yote. Mtu huyo anakuwa kitendea-kazi katika kuleta hali ya watu kutokuwa wenye haki.

Wote waliochagua kazi ya Mungu wanapaswa kukaa katika utunzaji wake. Kristo alielekeza kwa ndege warukao mbinguni, akaelekeza kwa maua ya kondeni, na kuwataka watu watafakari kuhusu viumbe hawa walioumbwa na Mungu. Akasema, "Ninyi je! Si bora kupita hao?" Mathayo 6:26. Kipimo cha uangalizi wa Mungu ufanywao kwa kitu huwiana na nafasi ya kitu hicho katika mtiririko wa madaraja ya viumbe. Shomoro wadogo wanaangaliwa na Mungu. Maua ya kondeni, nyansi zilizotanda chini kwenye dunia, zinapata kuonwa na kutunzwa na Baba wa mbinguni. Bwana wa Usanifu mkuu anafikiria kuhusu maua, akiyafanya kupendeza kiasi cha kuzidi fahari ya Sulemani. Ni mbali zaidi kiasi gani anavyotunza mwanadamu, ambaye ni sura na utukufu wa Mungu. Anapenda kuona watoto wake wakidhihirisha tabia kama yake. Kama vile mwale wa jua unavyoingiza rangi nzuri katika maua, ndivyo Mungu anavyoingiza moyoni mwa mtu uzuri wa tabia yake.

Wote wanaochagua ufalme wa Kristo wa upendo na haki na amani, huku wakiifanya hamu yao kwa huo kuwa juu sana kuliko kitu kingine chochote, wanaunganishwa na ulimwengu ule ulio juu, na kila baraka zinazohitajika kwa ajili ya maisha haya ni zao. Katika kitabu cha Mungu, kitabu cha kumbukumbu ya maisha, kila mmoja wetu amepewa ukurasa. Kitabu hicho kina kumbukumbu ya kila kitu kuhusu historia ya maisha yetu; hata idadi ya nywele za kichwa zimehesabiwa. Kamwe watoto wa Mungu hawasahauliwi katika mawazo ya Mungu.

"Basi msisumbukie ya kesho." Mathayo 6:34. Tunapaswa tumfuate Yesu kila siku. Mungu hatupatii msaada kwa ajili ya kesho. Yeye hawapatii watoto wake maelekeo yote ya safari ya maisha yao kwa mara moja, wasije wakachanganyikiwa. Anawaambia kiasi kile wanachoweza kukumbuka na kufanyia kazi. Nguvu na hekima iliyowekwa kwa mtu ni kwa ajili ya mambo ya sasa. "Lakini mtu wa kwenu akipungukiwa na hekima," - kwa ajili ya sasa, - "na aombe dua kwa Mungu, awapaye wote, kwa ukarimu, wala hakemei; naye atapewa." Yakobo 1:5.

**(314)** Msihukumu, msije mkahukumiwa ninyi." Usijidhanie kwamba wewe ni bora kuliko watu wengine, na kujiweka kama mhukumu wao. Kwa kuwa huwezi kuelewa nia, hauna uwezo wa kumhukumu mtu mwingine. Kwa kumkosoa mwingine, unajiwekea hukumu mwenyewe; maana unaonyesha kwamba wewe ni mshirika pamoja na Shetani, aliye mshtaki wa ndugu. Bwana anasema hivi, "Jijaribuni wenyewe kwamba mmekuwa katika imani; jithibitisheni wenyewe." Hii ndiyo kazi yetu. "Lakini kama tungejipambanua nafsi zetu, tusingehukumiwa." 2 Wakorintho 13:5; 1 Wakorintho 11:31.

Mti mwema unazaa matunda mema. Ikiwa matunda ni machungu na yasiyofaa, mti huo ni mwovu. Kwa hiyo tunda linalozaliwa katika maisha hushudia hali ya moyo na uzuri wa tabia. Matendo mema hayawezi kununua wokovu kamwe, lakini ni ushahidi wa imani itendayo kwa upendo na kusafisha nafsi. Ingawa thawabu ya milele haitolewi kwa wema wetu, bado itakuwa katika uwiano wa kazi ambayo imefanywa kwa rehema ya Kristo.

Hivyo ndivyo Yesu alivyozionyesha kanuni za ufalme wake, na kuzionyesha kwamba ndizo zinazoongoza maisha. Ili kukoleza fundisha aliongeza kielelezo. Alisema kwamba, haitoshi kwenu kusikia maneno yangu. Lazima myafanye kuwa msingi wa tabia yenu kwa kuyatii. Ubinafsi ni mchanga tu unaohama. Ikiwa mtajenga katika nadharia na mavumbuzi ya wanadamu, nyumba yenu itaanguka. Pepo za majaribu, na uvumi wa maonjo, vitaifagilia mbali. Lakini kanuni hizi ambazo nimewapa zitadumu. Nipokeeni; jengeni kwenye maneno yangu.

"Basi kila asikiaye hayo maneno yangu, na kuyafanya, atafananishwa na mtu mwenye akili, aliyejenga nyumba yake juu ya mwamba; mvua ikanyesha, mafuriko yakaja, pepo zikavuma, zikaipiga nyumba ile, isianguke; kwa maana misingi yake imewekwa juu ya mwamba." Mathayo 7:24, 25.

# Sura ya 32

## Akida

[Sura hii imejengwa katika Mathayo 8:5-13; Luka 7:1-17.]

Kristo alikuwa amemwambia yule diwani ambaye mwanae alikuwa ameponywa kwamba, "Msipoona ishara na maajabu hamtaamini kabisa." Yohana 4:48. Alihuzunishwa kwamba taifa lake mwenyewe lilikuwa linadai ishara hizi za nje kuhusu Umasihi wake. Alikuwa ameshangazwa tena na tena kwa kutokuamini kwao. Lakini alishangazwa na imani ya akida aliyekuja kwake. Akida hakuhoji kuhusu uwezo wa Kristo. Hata hakumwomba aje mwenyewe akafanye mwujiza. Alisema, "Sema neno tu, na mtumishi wangu atapona."

Mtumishi wa akida huyu alikuwa amepatwa na ugonjwa wa kupooza, na alikuwa amelala akiwa katika hali ya kufa. Katika jamii za Warumi, watumishi walikuwa watumwa, waliouzwa na kununuliwa sokoni, wakitendewa matendo ya kikatili na ya kudhalilisha, lakini akida huyu alifungamanishwa na pendo kwa mtumishi wake, na alitamani sana apone. Aliamini kwamba Yesu angeweza kuponya. Alikuwa hajapata kumwona Yesu, lakini habari alizosikia zilimpa imani. Licha ya urasimu wa dini ya Wayahudi, Mrumi huyu alishawishika kwamba dini yao ilikuwa bora kuliko yake. Tayari alikuwa ametoboa ukuta wa kizuizi cha itikadi na chuki za taifa zilizotenganisha kati ya washindi wanaotawala na wale walioshindwa. Alikuwa amedhihirisha heshima kwa ibada ya Mungu, na alikuwa ameonyesha wema kwa Wayahudi kwamba wanamwabudu Mungu. Katika mafundisho ya Yesu, kama yalivyosimuliwa kwake, alipata kitu kilichompatia mahitaji ya roho. Yote yaliyokuwa ya kiroho ndani yake yaliitikia maneno ya Kristo. Lakini alijihisi kutostahili kuja mbele ya Yesu, na aliwaomba wazee wa Kiyahudi kumfikishia ombi la kutaka kuponywa kwa mtumishi wake. Alidhani kwamba walikuwa wanamfahamu vema **(316)** Mwalimu Mkuu, na wangejua namna ya kumfikia ili wapate ukubali wake.

Yesu alipoingia Kapernaumu, alikutanishwa na kundi la wazee, ambao walimwambia shida ya yule akida. Walisisitiza kwamba, "Amestahili huyu umtendee neno hili; maana, analipenda taifa letu, naye alitujengea sinagogi."

Mara ile ile Yesu aliondoka kwenda nyumbani kwa afisa yule; lakini, akiwa amesongwa na umati, alipenya pole pole. Habari za kuja kwake zilimtangulia kule, na akida yule, katika kutojiamini kwake, alimpelekea ujumbe kwamba, "Bwana, usijisumbue, maana mimi sistahili wewe uingie chini ya dari yangu." Lakini Mwokozi aliendelea kwenda, na akida yule, hatimaye akiamua tu kuja kukutana naye, alikamilisha ujumbe wake ule, kwa kusema, "Nilijiona sistahili mwenyewe kuja kwako; lakini, sema neno tu, na mtumwa wangu atapona. Kwa maana mimi nami ni mtu niliyewekwa chini ya mamlaka, mwenye askari chini yangu; nikimwambia huyu, Nenda, huenda; na huyu, Njoo, huja; na mtumwa wangu, Fanya hivi, hufanya." Kama vile ambavyo mimi nawakilisha mamlaka ya Rumi, na askari wangu wanavyotambua mamlaka yangu kuu, ndivyo Wewe unavyowakilisha mamlaka ya Mungu Mkuu, na vyote vilivyoumbwa vinatii neno lako. Unaweza kuamuru ugonjwa kuondoka na ukakutii. Unaweza kuitisha wajumbe wa mbinguni, nao wakatia nguvu ya uponyaji. Sema neno tu, na mtumishi wangu atapona.

"Yesu aliposikia hayo alimstaajabia, akaugeukia mkutano uliokuwa ukimfuata, akasema, Nawaambia, hata katika Israeli sijaona imani kubwa namna hii." Na akamwambia yule akida, "Na iwe kwako kama ulivyoamini. Mtumishi wake akapona saa ile ile."

Wazee wa Kiyahudi waliomthibitisha yule akida kwa Kristo walikuwa **(317)** wameonyesha ni jinsi gani walivyokuwa mbali na hali ya kuwa na roho ya injili. Hawakugundua kwamba hitaji letu kuu ni kudai rehema ya Mungu tu. Katika hali yao ya kujihesabia haki walimuidhinisha akida yule kwa sababu ya upendeleo aliokuwa ameonyesha kwa "taifa letu." Lakini akida yeye alijisema kwamba, "Nilijiona sistahili." Moyo wake ulikuwa umeguswa na neema ya Kristo. Aliona kutostahili kwake; lakini aliogopa kuomba msaada. Hakutumainia wema wake mwenyewe; hoja yake ilikuwa ndiyo hitaji lake kubwa. Imani yake ilimshikilia Kristo katika tabia yake halisi. Hakumwamini Yesu kama mtenda miujiza tu, bali kama rafiki na Mwokozi wa mwanadamu.

Hivyo ndivyo kila mdhambi anavyoweza kuja kwa Kristo. "Si kwa sababu ya matendo ya haki tuliyoyatenda sisi; bali kwa rehema yake." Tito 3:5. Shetani anapokuambia kwamba wewe ni mdhambi, na kwamba huwezi

kutumaini kupata baraka kutoka kwa Mungu, mwambie kwamba Kristo alikuja ulimwenguni kuokoa wenye dhambi. Hatuna kitu cha kututhibitisha kwenda kwa Mungu; bali ombi tuombalo sasa na daima ni hali yetu isiyojiwezea jambo lolote inayofanya nguvu yake ya ukombozi iwe muhimu. Tukiacha mambo yote ya kujitumainia wenyewe, tunaweza kuutazama msalaba wa Kalvari tukisema,

"Sina malipo mkononi mwangu;
Ila msalabani pako nang'ang'ania."

Wayahudi walikuwa wamefundishwa tangu utoto wao kuhusu kazi ya Masihi. Maneno ya uvuvio ya wazee wa zamani na manabii na mafundisho kupitia vielelzo vya ibada za kafara vilikuwa vimekuwepo kwao. Lakini walikuwa wameipuuza nuru; na sasa hawakuona cha kutumainiwa kwa Yesu. Lakini akida, aliyezaliwa katika upagani, aliyeelimishwa katika ibada za sanamu za himaya ya Rumi, aliyefunzwa kuwa askari, ikionekana kama vile amekatiliwa mbali na maisha ya kiroho kwa sababu ya elimu yake na mazingira yake, na bado akifungiwa mbali kwa sababu ya itihadi za Wayahudi, na dharau ya watu wa nchi yake kwa watu wa Israeli, - aliuelewa ule ukweli ambao kwa huo watoto wa Ibrahimu walikuwa vipofu. Hakusubiri kuona kama Wayahudi wenyewe wangempokea Yeye aliyedai kuwa Masihi wao. Kadiri "nuru halisi, amtiaye nuru kila mtu, akija katika ulimwengu" (Yohana 1:9) alivyokuwa ameangaza kwake, alikuwa ameuona utukufu wa Mwana wa Mungu japo kwa mbali.

Kwa Yesu hii ilikuwa kazi njema mno ambayo ingekamilishwa na injili miongoni mwa Wamataifa. Kwa furaha alitazamia kuona katika ufalme wake kusanyiko la watu wa mataifa yote. Lakini kwa huzuni kubwa aliona picha ya matokeo ya Wayahudi kuikataa neema yake, akasema: "Nami **(318)** nawaambieni, ya kwamba wengi watakuja kutoka mashariki na magharibi, nao wataketi pamoja na Ibrahimu, na Isaka, na Yakobo katika ufalme wa mbinguni; bali wana wa ufalme watatupwa katika giza la nje, ndiko kutakuwako kilio na kusaga meno." Maskini! Ni watu wengi kiasi gani ambao bado wanajiandaa kuelekea katika mfadhaiko ule ule wa kufisha! Wakati roho zilizo katika upagani wa giza zinapoipokea neema ya Kristo, wengi wako katika maeneo ya Ukristo mahali ambapo nuru inamlika nao wakiipuuza.

Zaidi ya maili ishirini kutoka Kapernaumu, kwenye mwinuko wa tambarare unaokabiliana na uwanda mzuri, mpana wa Esdraeloni, kulikuwa na kijiji cha Naini, na hapa ndipo Yesu alipoelekeza miguu yake. Wengi wa wanafuzi wake na watu wengine walikuwa pamoja naye, na wengine wa pembezoni mwa njia walikuja, wakihitaji maneno yake ya upendo na huruma, wakiwaleta wagonjwa wao ili waponywe, na wakiwa na tumaini kwamba Yeye aliyeonyesha uwezo wa maajabu angejitambulisha rasmi kama Mfalme wa Israeli. Umati wa watu ulimfuata, na lile lilikuwa kundi la watu wenye furaha na matarajio likifuata katika njia ya miamba kuelekea katika lango la kijiji kile kilichoko mlimani.

Wakati wakikaribia pale, wanaona msafara wa kwenda kwenye mazishi unakuja kutokea katika lango. Kwa hatua za pole pole na majonzi msafara unaendelea kuelekea mahali pa kuzikia. Kwenye machela iliyo wazi ikiwa imebebwa mbele ya msafara kuna mwili wa mtu aliyekufa, na karibu yake kuna waombolezaji, wakiwa wamelijaza anga kwa sauti zao za kilio. Ilionekana kama vile watu wote wa mji ule walikuwa wamekusanyika kuonyesha heshima zao kwa yule aliyekufa na kuonyesha huruma kwa waliofiwa na mpendwa wao.

Lilikuwa ni tukio lililoamsha huruma. Yule aliyekufa alikuwa mwana wa pekee wa mama yake, na mama yule alikuwa mjane. Mfiwa huyu mpweke alikuwa akimsindikiza kwenda kaburini mtu pekee aliyekuwa tegemeo lake na faraja yake duniani. "Bwana alipomwona alimwonea huruma." Kadiri alivyoendelea kwenda kama haoni, akilia, bila kuona uwepo wa Yesu, Yesu alikuja karibu yake zaidi, na kusema kwa upole, "Usilie." Yesu alikuwa anakaribia kubadili majonzi yake kuwa furaha, lakini hakuweza kuzuia hisia hii ya huruma.

"Akakaribia, akaligusa jeneza;" kwake Yeye hata kugusana na maiti hakukuweza kumtia unajisi. Wale waliobeba jeneza walisimama, na maombolezo ya waombolezaji yakakoma. Makundi yale mawili yalikusanyika pale kwenye jeneza. Yeye aliyekuwa ameondosha magonjwa na kufukuza pepo alikuwa pale; je, kifo nacho kilikuwa chini ya uweza wake?

Maneno haya yakatamkwa kwa sauti ya kusikika vizuri na ya mamlaka, "Kijana, nakuambia, Inuka." Sauti ile ilipenya katika masikio ya mfu yule. Kijana anafungua macho yake. Yesu anamshika mkono, na kumwinua. Macho yake Yesu yanakazwa kwa yule mama aliyekuwa analia kando ya kijana yule, na mama na mwanae

wanaungana kwa kukumbatiana kwa furaha kuu. Umati ule **(319)** unatazama kwa ukimya, kama vile kwa kutekewa. "Hofu ikawashika wote." Kwa utulivu na heshima walisimama kwa muda, kama vile wako mbele za Mungu. Halafu "wakamtukuza Mungu, wakisema, Nabii mkuu ametokea kwetu; na, Mungu amewaangalia watu wake." Msafara wa mazishi uligeuka na kurudi Naini ukiwa kama msafara wa kifahari wa ushindi. "Habari hii ikaenea katika Uyahudi wote, na katika nchi zote za kando kando."

Yeye aliyesimama kando ya mama mwenye majonzi panapo lango la Naini, anamtazama kila mtu aombolezaye kando ya jeneza. Anaguswa na huruma kwa majonzi yetu. Moyo wake, ule uliopenda na kuhurumia, ni moyo wenye pendo lisilobadilika. Neno lake, lile lililomwita aliyekufa akawa hai, si kwamba halina nguvu siku hizi ikilinganishwa na wakati ule lilipotamkwa kwa yule kijana wa Naini. Anasema, "Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani." Mathayo 28:18. Pendo lile halimaliziki kulingana na muda miaka inavyoenda, wala halimalizwi na kazi zake zisizokoma zinazotiririsha neema. Kwa wote wamwaminio bado yu Mwokozi aliye hai.

**(320)** Yesu alibadilisha majonzi ya mama na kuyageuza kuwa furaha wakati alipomreshea mwana wake; lakini yule kijana alikuwa ameitwa tu kurudi katika maisha ya dunia hii, kukabiliana na huzuni zake, mahangaiko yake ya maisha, na hatari zake, halafu apite tena katika nguvu ya mauti. Lakini Yesu anafariji huzuni zetu tunapofiwa kwa ujumbe wenye matumaini ya milele anaposema: "Nami nalikuwa nimekufa, na tazama, ni hai hata milele na milele. Nami ninazo funguo za mauti, na za kuzimu." "Basi, kwa kuwa watoto wameshiriki damu na mwili, yeye naye vivyo hivyo alishiriki yayo hayo, ili kwa njia ya mauti amharibu yeye aliyekuwa na nguvu za mauti, yaani, Ibilisi, awaache huru wale ambao kwamba maisha yao yote kwa hofu ya mauti walikuwa katika hali ya utumwa." Ufunuo 1:18; Waebrania 2:14, 15.

Shetani hawezi kushikilia mtu katika kifo pale Mwana wa Mungu anapotaka kwamba aishi. Hawezi kumshikilia katika kifo cha kiroho mtu ambaye kwa imani anapokea neno la nguvu la Kristo. Mungu anawaambia wote ambao wamekufa katika dhambi, "Amka wewe ulalaye, ufufuke katika wafu." Waefeso 5:14. Neno hilo ni uzima wa milele. Kama vile neno la Mungu lilivyomwagiza yule kijana kuamka, bado linatupatia uzima; kama vile neno la Kristo kwamba, "Kijana, nakuambia, inuka," lilivyomrejeshea uhai yule kijana wa Naini, vivyo hivyo neno lile lisemalo, "Ufufuke katika wafu," ni uzima kwa nafsi ilipokeayo. Mungu "alituokoa katika nguvu za giza, akatuhamisha na kutuingiza katika ufalme wa Mwana wa pendo lake." Wakolosai 1:13. Yote yametolewa kwetu katika neno lake. Ikiwa tunapokea neno, tunao ukombozi.

Na "ikiwa Roho yake yeye aliyemfufua Yesu katika wafu anakaa ndani yenu, yeye aliyemfufua Kristo Yesu katika wafu ataihuisha na miili yenu iliyo katika hali ya kufa, kwa Roho wake anayekaa ndani yenu." "Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu; nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza. Kisha sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani; na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele." Warumi 8:11; 1 Wathesalonike16, 17. Hili ni neno la faraja mahali ambapo anatutaka tufarijiane sisi kwa sisi.

## Sura ya 33

# Ndugu Zangu ni Akina Nani?

[Sura hii imejengwa katika Mathayo 12:22-50; Marko 3:20-35.]

Wana wa Yusufu walikuwa mbali na hali ya kumthamini Yesu katika kazi yake. Taarifa zilizowafikia kuhusu maisha na kazi yake ziliwajaza hali ya mshtuko na fadhaa. Walisikia kwamba alikuwa akitumia usiku mzima katika kuomba, kwamba mchana mzima alikuwa akizungukwa na makundi makubwa ya watu, na wala hakujipa muda wa kutosha hata kula. Rafiki zake walimdhania kwamba alikuwa anajidhoofisha kwa kazi zake zisizoisha; hawakuweza kupata sababu za mtazamo aliokuwa nao kwa Mafarisayo, na walikuwepo baadhi waliohofu kwamba huenda akili yake haikuwa sawasawa.

Kaka zake walisikia mambo haya, na madai pia yaliyoletwa na Mafarisayo kwamba anatoa pepo kwa kutumia nguvu za Shetani. Walipatwa na aibu kutokana na kejeli zilizoelekezwa kwao kwa sababu ya kuwa na uhusiano na Yesu. Walijua kishindo cha vurugu kilichosababishwa na maneno yake, na hawakuwa wameshtushwa tu kwa maneno yake yenye msimamo, bali hasira dihidi yake kwa kuwadharau waandishi na Mafarisayo. Waliamua kwamba ni lazima ashawishiwe au alazimishwe kuacha kazi ya namna hii, na walimshawishi Mariamu kuungana nao, wakidhani kwamba kwa kupitia katika upendo wa Yesu kwa mama yake wanaweza wakashinda na kwamba Yesu angekubali mawazo yao.

Muda mfupi tu kabla ya haya ndipo Yesu alikuwa ametenda mwujiza wa pili kwa kumponya mtu aliyepagawa, kipofu na bubu, na Mafarisayo walikuwa wamerudia madai yao kwamba, "Kwa nguvu za mkuu wa pepo atoa pepo." Mathayo 9:34. Kristo aliwaambia wazi wazi kwamba kwa kuihusisha na Shetani **(322)** kazi ya Roho Mtakatifu, walikuwa wanajiweka mbali na chemchemi ya baraka. Wale waliokuwa wamempinga Yesu mwenyewe, wasiione tabia yake ya kimbingu, wangeweza kusamehewa; maana kwa njia ya Roho Mtakatifu wangeweza kufikishwa mahali pa kuyaona makosa yao wakatubu. Kwa dhambi yoyote ile, mtu anapotubu na kuamini, hatia yake huoshwa katika damu ya Kristo; bali yeye akataaye kazi ya Roho Mtakatifu anajiweka mahali ambapo toba na imani haviwezi kumjia. Mungu hutenda kazi moyoni kwa njia ya Roho; wakati watu wanapomkataa Roho kwa makusudi, na kutangaza kwamba anatoka kwa Shetani, wanakuwa wameikata njia ambayo Mungu hutumia kuwasiliana nao. Wakati Roho anapokuwa amekataliwa kabisa, hakuna kitu zaidi ambacho Mungu anaweza kufanya kwa ajili ya nafsi hiyo.

Hata Mafarisayo wenyewe walioambiwa na Yesu onyo hilo hawakuyaamini yale mashtaka waliyofanya dhidi ya Kristo. Hakukuwa na hata mmoja miongoni mwa wakuu wale aliyehisi kuvutwa kwenda kwa Mwokozi. Walikuwa wameisikia sauti ya Roho mioyoni mwao ikimtangaza Yesu kuwa Mpakwa Mafuta wa Israeli, na ikiwahimiza kukiri na kuwa wanafunzi wake. Katika nuru ya uwepo wake walikuwa wamejigundua kuwa si watakatifu, na walikuwa wametamani kupata kuhesabiwa haki ambayo hawakuweza kuifanya iwepo. Lakini walipokwisha kumkataa hali ya kumpokea kama Masihi ilikuwa jambo la kudhalilisha. Wakishakuweka mguu wao katika njia ya kutokuamini, walikuwa na kiburi kiasi kwamba hawakuweza kukiri makosa. Na ili kuzuia wasiukiri ukweli, walijaribu kupambana na mafundisho yake kwa nguvu. Ushahidi wa uweza wake na rehema zake viliwaghadhibisha. Hawakuweza kumzuia Mwokozi kufanya miujiza, hawakuweza kunyamazisha mafundisho yake; lakini walifanya kila wawezalo kumsema vibaya isivyo sahihi na kuonyesha kwamba maneno yake ni ya uongo. Bado Roho wa Mungu anayesadikisha aliwafuata, na iliwalazimu kujenga vizuizi vingi ili kustahimili nguvu zake. Nguvu kubwa mno inayoweza kuletwa kwenye moyo wa mwanadamu ilikuwa inapambana nao, lakini hawakujisalimisha.

Si Mungu anayepofusha macho ya watu na kuifanya mioyo yao kuwa migumu. Yeye huwapelekea nuru ili kusahihisha makosa yao, na kuwaongoza katika njia salama; macho yao hupofushwa na mioyo yao kufanywa migumu kwa sababu ya wao kuikataa nuru hiyo. Mara nyingi hali hii hutokea taratibu, na kama vile pasipo kuonekana. Nuru huja moyoni kwa njia ya neno la Mungu, kupitia watumishi wake, au kupitia kazi za moja kwa moja za Roho wake; lakini pale hata mshale mmoja wa nuru unapopuuzwa, kunakuwa na sehemu ya uhafifisho wa uelewa wa kiroho, na udhihirisho wa pili wa nuru huonekana kwa uwazi uliopungua. Hivyo giza huongezeka, mpaka kunapokuwa usiku moyoni. Hivyo ndivyo ilivyokuwa imekuwa kwa **(323)** viongozi hawa wa Kiyahudi.

Walishawishika kwamba nguvu za kimbingu zilikuwa pamoja na Kristo, lakini ili kuupinga ukweli, waliuhusisha ule utendaji wa Roho Mtakatifu na Shetani. Kwa kufanya hivyo walichagua udanganyifu kwa hiari yao; walijisalimisha kwa Shetani, na matokeo yake waliendeshwa na nguvu zake.

Kilichounganishwa na onyo la Kristo kuhusu dhambi ya kumpinga Roho Mtakatifu ni onyo dhidi ya maneno yasiyo na maana na maneno maovu. Maneno ni udhihirisho wa kile kilichoko moyoni. "Kinywa cha mtu huyanena yaujazayo moyo wake." Lakini ni zaidi ya udhihirisho wa tabia; yana nguvu ya kuathiri tabia. Watu wanaathiriwa na maneno yao. Mara kwa mara wanaweza kuwa na msukumo wa muda, wakisukumwa na Shetani, wakanena maneno ya wivu au ya uovu, na kusema kile ambacho hawaamini kwa yakini; lakini hali hiyo hufanya kazi katika mawazo. Wanadanganywa na mawazo yao wenyewe, na kuja kuamini kile kilichosemwa kilichoanzishwa na Shetani. Watu wakishaonyesha maoni au uamuzi fulani, wanakuwa na majivuno kiasi cha kushindwa kuyakana na kuyatangua, na hujaribu kujionyesha kwamba wako sahihi, mpaka wanapofikia hatua ya kuamini kwamba hivyo ndivyo ilivyo. Ni hatari kubwa kutamka neno ulilo na mashaka nalo, hatari ya kuhoji na kukosoa nuru ya kimbingu. Mazoea ya kupinga pasipo uangalifu na heshima huathiri tabia, na huelekeza katika utovu wa heshima na kutoamini. Watu wengi wanaokuwa na mazoea haya wameendelea hivyo pasipo kutambua hatari iliyopo, mpaka walipokuwa katika hali ya kupinga na kukataa kazi ya Roho Mtakatifu. Yesu alisema, "Kila neno lisilo maana, watakalolinena wanadamu, watatoa hesabu ya neno hilo siku ya hukumu. Kwa kuwa kwa maneno yako utahesabiwa haki, na kwa maneno yako utahukumiwa."

Halafu aliongeza onyo jingine kwa wale waliokuwa wameguswa na maneno yake, waliokuwa wamemsikiliza kwa furaha, lakini ambao hawakuwa wamejisalimisha ili kuingiwa na Roho Mtakatifu. Roho haiharibiwi kwa kupinga tu bali pia kwa kupuuza. Akasema, "Pepo mchafu, amtokapo mtu, hupitia mahali pasipo maji, akitafuta mahali pa kupumzika, asipate. Halafu husema, Nitarudi nyumbani kwangu nilikotoka; hata akija, aiona tupu, imefagiwa, na kupambwa. Mara huenda, akachukua pamoja naye pepo wengine saba walio waovu kuliko yeye mwenyewe, nao huingia na kukaa humo."

Kulikuwa na watu mnamo siku za Kristo, kama ilivyo leo, ambao kwao utawala wa Shetani ulionekana kama umevunjwa kwa wakati fulani; kwa neema ya Mungu waliwekwa huru kutokana na pepo wachafu ambao walikuwa wametawala **(324)** nafsi zao. Walishangilia pendo la Mungu; lakini, kama walivyo wale wasikiaji wa neno waliofananishwa na walio kwenye udongo wenye miamba katika mfano wa Yesu, hawakudumu kuwa katika pendo lake. Hawakujisalimisha kwa Mungu kila siku, ili kwamba Yesu akae moyoni; na pepo mchafu aliporudi, akiwa pamoja na "pepo wengine saba walio waovu kuliko yeye mwenyewe," walitawaliwa kikamilifu na nguvu za uovu.

Nafsi inapojisalimisha kwa Kristo, nguvu mpya hutawala moyo mpya. Badiliko ambalo mwanadamu hawezi kujiletea linafanyika. Ni kazi ya kimwujiza, inayoleta hali ya kimwujiza kwa mwanadamu. Nafsi inayojisalimisha kwa Kristo inakuwa ngome yake, ambamo humo anaweka upinzani dhidi ya ulimwengu, na anadhamiria kwamba hakuna mamlaka itakayojulikana humo isipokuwa yake Yeye Kristo. Nafsi ambayo inamilikwa na nguvu za mbinguni namna hiyo haiwezekani kupenywa na mashambulizi ya Shetani. Lakini tusipojisalimisha katika utawala wa Kristo, tutatawaliwa na yule mwovu. Ni lazima mtu awe chini ya utawala wa huyu au yule, ambao ni mamlaka kuu mbili zinazopambana ili kuwa na nguvu ya kuutawala ulimwengu. Kuwa chini ya utawala wa giza si lazima tuchague wazi wazi kuutumikia ufalme huo; ni kule tu kupuuza kujishikamanisha na ufalme wa nuru. Ikiwa hatushirikiani na nguvu za kimbingu, Shetani anajitwalia umiliki wa moyo, na anaufanya kuwa mahali pa makao yake. Ulinzi pekee dhidi ya uovu ni kumruhusu Kristo akakaa moyoni kwa imani ya kuhesabiwa haki yake. Ikiwa hatuunganishwi na Mungu kwa dhati, hatuwezi kuyapinga matokeo machafu ya kujipenda wenyewe, kujinufaisha wenyewe, na kujaribiwa kutenda dhambi. Tunaweza tukaachana na mazoea mabaya, tunaweza tukatengana na Shetani kwa muda; lakini pasipokuwa na muunganiko wa dhati na Mungu, kwa njia ya kujisalimisha kwake kila wakati, tutashindwa. Bila mtu binafsi kumfahamu Kristo, na kuwa naye wakati wote, tunakuwa katika himaya ya adui, na mwishowe tutafanya matakwa yake.

Yesu alisema, "Na mtu yule hali yake ya mwisho huwa mbaya kuliko ya kwanza. Ndivyo itakavyokuwa kwa kizazi hiki kilicho kibaya." Hakuna watu ambao mioyo yao imefanywa kuwa migumu sana kama wale ambao wamepuuza mwaliko wa rehema, na kutenda kinyume na Roho wa neema. Udhihirisho uliozoeleka mno wa dhambi ya kumpinga Roho Mtakatifu uko katika hali ya kudumu kupuuza mwaliko wa mbinguni unaotaka toba

ifanywe. Kila hatua katika kumkataa Kristo ni hatua katika kuelekea kuukataa wokovu, na kuelekea katika dhambi ya kumpinga Roho Mtakatifu.

Katika kule kumkataa Kristo Wayahudi walitenda dhambi isiyosameheka; na kwa kukataa mwaliko wa rehema, tunaweza kufanya kosa **(325)** lile lile. Tunamfedhehesha Mfalme wa uzima, na kumfanya kuwa aibu katika sinagogi la Shetani na mbele za malimwengu ya mbinguni tunapokataa kuwasikiliza wajumbe wake aliowatuma, na badala yake kuwasikiliza mawakala wa Shetani, ambao wanatafuta kutuvuta kwenda mbali na Kristo. Kadiri mtu anavyofanya hivi, hawezi kupata tumaini wala msamaha, na hatimaye atapoteza hamu yote ya kutaka kupatanishwa na Mungu.

Wakati Yesu akiendelea kuwafundisha watu wale, wanafunzi wake walimletea ujumbe kwamba mama yake na ndugu zake walikuwa nje, na walitaka kumwona. Alijua kilichokuwa mioyoni mwao, na "Akajibu, akamwambia yule aliyempasha habari, Mama yangu ni nani? Na ndugu zangu ni akina nani? Akawanyoshea mkono wanafunzi wake, akasema, Tazama, Mama yangu na ndugu zangu! Kwa maana yeyote atakayeyafanya mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni, huyu ndiye ndugu yangu, na umbu langu, na mama yangu."

Wote ambao wangempokea Kristo kwa imani waliunganishwa kwa kifungo kinachowaweka karibu zaidi kuliko undugu wa kibinadamu. Wangekuwa kitu kimoja na Yeye, kama alivyokuwa katika umoja na Baba. Akiwa kama mwamini na mtendaji wa maneno ya Kristo, mama yake alikuwa na ukaribu naye zaidi na kuwa na uhusiano naye katika mambo ya wokovu zaidi kuliko alivyokuwa katika mambo ya uhusiano wa kawaida. Kaka zake nao wasingepokea manufaa kutokana na kuwa na uhusiano naye ikiwa hawakumkubali kama Mwokozi wao.

Kristo angepata msaada mkubwa kiasi gani kutoka kwa jamaa wa undugu wa kidunia ikiwa wangemwamini Yeye kwamba ametoka mbinguni, na ikiwa wangeshirikiana naye katika kufanya kazi ya Mungu! Lakini kutokuamini kwao kulitia kivuli maisha yake ya duniani. Kulichangia uchungu uliokuwa katika kikombe kile cha huzuni alichonywea kwa ajili yetu.

**(326)** Uadui uliowaka katika moyo wa mwanadamu dhidi ya injili ulimpata kikweli kweli Mwana wa Mungu, na wa maumivu makubwa zaidi ulikuwa katika nyumba yake; maana moyo wake ulijawa na wema na upendo, na alijali sana mahusiano ya kifamilia. Kaka zake walimtaka akubaliane na mawazo yao, wakati njia hiyo isingepatana kabisa na utume wake wa kimbingu. Walimwona kama mtu anayehitaji ushauri wao. Walimpima kwa mtazamo wa kibinadamu, na kudhani kwamba kama angeongea vitu vinavyokubaliwa na waandishi na Mafarisayo, angeepusha msuguano wa kutokukubaliana uliosababishwa na maneno yake. Walidhani ya kwamba alikuwa amejitenga kwa kudai kuwa na mamlaka ya uungu, na kwa kujiweka juu ya marabi kama mkemeaji wa dhambi zao. Walijua kwamba Mafarisayo walikuwa wakitafuta uwezekano wa kumshtaki, na waliona kwamba alikuwa amewapa uwezekano wa kutosha kumshtaki.

Kwa kutumia kamba yao fupi hawakuweza kupima kina cha kazi aliyokuja kutimiza, na kwa hiyo hawakuweza kumhurumia katika huzuni zake za majaribu. Maneno yao magumu-magumu na yasiyo na shukrani yalionyesha kwamba hawakuwa na uelewa wa kweli wa tabia yake, na hawakuona kwamba uungu uliungana na ubinadamu. Mara nyingi walimwona akiwa amejaa majonzi; lakini badala ya kumfariji, roho zao na maneno yao yalijeruhi tu moyo wake. Hali yake ya hisia iliteswa; mivuto yake haikueleweka kwa usahihi, kazi yake haikufahamika.

Mara nyingi ndugu zake walimletea falsafa za Mafarisayo, ambazo zilikuwa za kizamani na zilizopitwa na wakati, na kudhani kwamba wangeweza kumfundisha Yeye aliyejua kweli yote, na aliyefahamu siri zote. Kwa kujiamini walifanya hukumu kuhusu mambo ambayo hawakufahamu. Lawama zao zilimletea hisia kali za maumivu, na moyo wake uliumia na kuchoka. Walijiamini kwamba walikuwa na imani kwa Mungu, na walifikiri kwamba walikuwa wanamdhihirisha Mungu, wakati kumbe Mungu alikuwa pamoja nao katika mwili, wala hawakumjua.

Mambo haya yaliifanya njia yake kuwa ya miiba sana kwa anayeipita. Mtazamo potofu wa watu wa nyumbani mwake ulimsababishia Kristo maumivu makali sana kiasi kwamba ilikuwa nafuu kwake kwenda mahali ambapo haukuwepo. Kulikuwa na nyumba moja aliyopenda kutembelea – nyumbani kwa Lazaro, na Mariamu, na Martha; maana roho yake ilipata kupumzika katika mazingira ya imani na upendo. Lakini hakukuwa na hata mtu mmoja duniani aliyeweza kuelewa utume wake wa kimbingu, au kujua mzigo aliokuwa amebeba kwa ajili ya mwanadamu. Mara nyingi ilikuwa nafuu ya pumziko kwake alipokuwa peke yake, akiwa pamoja na Baba yake wa mbinguni.

**(327)** Wale wanaoitwa ili kuteseka kwa ajili ya Kristo, ambao lazima wapatwe na shida ya kutoeleweka vema na kukejeliwa, hata katika majumba yao wenyewe, wanaweza kupata faraja katika wazo kwamba Yesu alistahimili mambo hayo hayo. Anawahurumia sana. Anawahimiza wasijione wapweke bali wamwone kama mwenzao, na wapate pumziko mahali alipolipata, kwa kuwa pamoja na Baba.

Wale wanaompokea Kristo kama Mwokozi wao hawajaachwa kama yatima wabebe maonjo ya maisha wakiwa peke yao. Anawapokea kama watu wa familia ya mbinguni; anawaruhusu wamwite Baba yake kuwa ni Baba yao. Wao ni watu wake "walio wadogo," wapendwa wa moyo wa Mungu, waliofungamanishwa naye kwa vifungo vya upendo. Anao upendo wa hali ya juu kwao, ambao kwa mbali, kama vile uungu ulivyo mbali juu ya uanadamu, unazidi ule ambao baba yetu na mama yetu wametuonyesha tukiwa katika hali ya kukosa msaada.

Kuna kielelezo kizuri cha mahusiano kati ya Yesu na watu wake katika sheria zilizotolewa kwa Israeli. Wakati Mwebrania alipokuwa amelazimika kutengana na urithi wa nyumba ya baba yake kwa sababu ya umaskini, na kujiuza mwenyewe kama mtumwa, wajibu wa kumkomboa yeye na urithi wake ulikuwa kwa ndugu aliyekuwa wa jamaa ya karibu. Angalia Walawi 25:25, 47-49; Ruthi 2:20. Hivyo ndivyo kazi ya kutukomboa sisi na urithi wetu, vilivyopotea kwa sababu ya dhambi, ilivyomwangukia Yeye "aliye wa jamaa" kwetu. Alikuja kuwa mtu wa mbari yetu ili kutukomboa. Bwana Mwokozi wetu yuko karibu zaidi kuliko baba, mama, kaka, rafiki, au mpendwa. "Usiogope, maana nimekukomboa; nimekuita kwa jina lako, wewe u wangu." "Kwa kuwa ulikuwa wa thamani machoni pangu, na mwenye kuheshimiwa, nami nimekupenda; kwa sababu hiyo nitatoa watu kwa ajili yako; na kabila za watu kwa ajili ya maisha yako." Isaya 43:1, 4.

Kristo anavipenda viumbe vya mbinguni vinavyokizunguka kiti chake cha enzi; lakini tutasema nini kuhusu upendo wake mkuu aliotupenda sisi? Hatuwezi kuuelewa, bali tunaweza kuujua kwa kweli kupitia uzoefu wetu. Na tukishikilia uhusiano naye kama wa wa jamaa ya karibu, ni kwa upendo kiasi gani tunapaswa kuwajali wale ambao ni kaka na dada wa Bwana wetu! Je, haitupasi kuwa wepesi wa kugundua madai yetu ya ushirikiano na Mungu? Tukiwa tumepokelewa katika familia ya Mungu, je haitupasi kumheshimu Baba na ndugu aliye wa mbari yetu?

## Sura ya 34

# Mwaliko

[Sura hii imejengwa katika Mathayo 11:28-30.]

"Njoni kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha."

Maneno haya ya faraja yalisemwa kwa makutano waliokuwa wakimfuata Yesu. Mwokozi alikuwa amesema kwamba wanadamu wanaweza kumjua Mungu kupitia Yeye tu. Alikuwa ameongelea wanafunzi wake kama watu waliokuwa wamepewa kujua vitu vya mbinguni. Lakini hakuacha watu wa aina yoyote kujisikia kufungiwa nje ya utunzaji na upendo wake. Wote wanaosumbuka na kulemewa na mizigo wanaweza kuja kwake.

Waandishi na marabi, wakiwa na umakini uliopitiliza katika kufuatilia ushikaji wa taratibu za kidini, walikuwa na hali ya kupungukiwa kile ambacho kisingetoshelezwa na kaida na kujitesa. Watoza ushuru na wenye dhambi wangeweza kujifanya kutosheka na tamaa za mwili na vitu vya dunia, lakini katika mioyo yao kulikuwa na kutoamini na hofu. Yesu aliwatazama watu hao waliochoka na wenye mizigo mioyoni, wale ambao matumaini yao yalikuwa yameharibiwa, na ambao kwa njia ya raha za dunia walikuwa wanatafuta kunyamazisha hamu ya moyo, na aliwaalika wote ili wapate pumziko ndani.

Kwa upendo aliwasihi watu wasumbukao akisema, "Jitieni nira yangu, mjifunze kwangu; kwa kuwa mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo; nanyi mtapata raha nafsini mwenu."

Katika maneno haya Kristo anamwambia kila mwanadamu. Iwe wanajua au hawajui, watu wote wamechoka na kulemewa na mizigo. Wote wamedhoofishwa na mizigo ambayo inaweza kuondolewa na Kristo tu. Mizigo mizito zaidi tunayobeba ni mizigo ya dhambi. Ikiwa tungeachwa tubebelee mizigo hii, **(329)** ingetukandamiza. Lakini Yeye asiye na dhambi amechukua mahali petu. "Bwana ameweka juu yake maovu yetu sisi sote." Isaya 53:6. Amebeba mzigo wa hatia yetu. Atachukua mzigo kutoka katika mabega yetu yaliyochoka. Atatupatia pumziko. Mzigo wa matunzo na huzuni ataubeba pia. Anatualika tumkabidhi Yeye mahitaji yote ya kutunzwa; maana anatubeba moyoni mwake.

Kaka Mkubwa wa jamii yetu ya wanadamu yuko mahali pa kiti cha enzi cha milele. Anaiangalia kila nafsi inayomgeuzia uso na kumtazama kama Mwokozi. Kwa uzoefu anajua yaliyo madhaifu ya wanadamu, yaliyo mapungufu yetu, na mahali palipo na nguvu zetu kwa ajili ya majaribu; maana alijaribiwa katika maeneo yote kama ilivyo kwetu, lakini hakutenda dhambi. Anakuangalia wewe, mtoto wa Mungu unayetetemeka. Uko katika majaribu? Ataokoa. U dhaifu? Atatia nguvu. Haujui? Ataangazia. Umejeruhiwa? Ataponya. Bwana "huihesabu idadi ya nyota;" lakini "huwaponya waliopondeka moyo, na kuziganga jeraha zao." Zaburi 147:4, 3. "Njoni kwangu," ndio mwaliko wake. Hata wasiwasi na maonjo yaweje, zianike shida zako mbele za Bwana. Roho yako itatiwa nguvu ili kuhimili. Njia itafunguliwa kwa ajili ya wewe kutokea na kuponyoka kutoka katika hisia za maumivu na ugumu wa mambo. Kadiri unavyojiona kuwa mdhaifu sana na anayehitaji msaada, ndivyo unavyopata nguvu zaidi kutoka katika nguvu zake. Kadiri mizigo yako inavyokuwa mizito zaidi, ndivyo baraka za pumziko zinavyopatikana zaidi pindi mizigo inavyoletwa kwake aliye Mbeba Mzigo. Pumziko linalotolewa na Yesu linategemea masharti, lakini masharti hayo yamefafanuliwa wazi. Ni yale ambayo watu wote wanaweza kuyatekeleza. Anatueleza tu vile pumziko lake linavyoweza kupatikana.

"Jitieni nira yangu," Yesu alisema. Nira ni zana ya kufanyia kazi. Ng'ombe wanafungiwa nira ili kufanya kazi, na nira ni ya muhimu katika kuwawezesha kufanya kazi kwa ufanisi. Kwa kielelezo hiki Kristo anatufundisha kwamba tumeitwa ili kutumika kwa maisha yote. Lazima tujitwike nira yake, ili ya kwamba tuwe watenda-kazi pamoja naye.

Nira inayofunga watu kwa ajili ya huduma ni sheria ya Mungu. Sheria kuu ya upendo iliyodhihirishwa kule Edeni, iliyotangazwa kwenye mlima Sinai, na ambayo katika agano jipya imeandikwa moyoni, ndiyo inayowafunga wanadamu walio watenda-kazi katika mapenzi ya Mungu. Kama tungeachwa tufuate vile tuonavyo wenyewe, kwenda kokote matashi yetu yanakotuongoza kwenda, tungeangukia katika njia za Shetani na kuwa na tabia zake. Kwa hiyo Mungu hutuweka katika mipaka ya mapenzi yake, ambayo yako juu, yenye wema, na ya kuinua.

Anatamani kwamba tutafanya majukumu yetu kwa ustahimilivu na hekima. Kristo mwenyewe alijifunga nira ya kazi akiwa katika ubinadamu. Alisema, "Kuyafanya mapenzi yako, Ee Mungu wangu, ndiyo furaha yangu; Naam, sheria yako imo moyoni mwangu." Zaburi 40:8. "Mimi sikushuka **(330)** kutoka mbinguni ili niyafanye mapenzi yangu, bali mapenzi yake aliyenipeleka." Yohana 6:38. Upendo kwa Mungu, ari ya utukufu wake, na upendo kwa wanadamu walioanguka, vilimleta Yesu duniani kuteseka na kufa. Hii ndiyo nguvu iliyotawala maisha yake. Hiyo ndiyo kanuni anayotaka tuikubali.

Wapo wengi ambao mioyo yao inauma kwa sababu ya mzigo wa mahitaji ya maisha kwa kuwa wanatafuta kufikia viwango vya ulimwengu. Wamechagua kuutumikia ulimwengu, wamekubaliana na mikanganyiko yake, wamekubali desturi zake. Kwa hiyo tabia zao zimeharibiwa, na maisha yao yamefanywa kuwa ya uchovu. Ili kuridhisha tamaa za mwili na hamu za mambo ya dunia, wanajeruhi dhamiri, na kujiletea juu yao mizigo ya ziada na hatia. Uendelevu wa mashaka unachosha nguvu za maisha. Bwana wetu anatamani waweke kando kongwa hili la utumwa. Anawaalika ili wapokee nira yake; anasema, "Nira yangu ni laini, na mzigo wangu ni mwepesi." Anawahimiza watafute kwanza ufalme wa Mungu na haki yake, na ahadi yake ni kwamba mambo yote wanayohitaji kwa ajili ya maisha haya wataongezewa. Mashaka ni upofu, wala hayawezi kuona mambo yajayo; lakini Yesu anauona mwisho tokea mwanzo. Katika kila ugumu Yeye anayo njia iliyoandaliwa tayari ili kuleta unafuu. Baba yetu wa mbinguni ana njia elfu kwa ajili ya mahitaji yetu, ambazo hatuzijui kabisa. Wale wanaokubali kanuni hiyo ya huduma na kumheshimu Mungu mwenye uweza wataona mkanganyiko ukitoweka, na kuona njia nyoofu mbele ya miguu yao.

"Mjifunze kwangu," Yesu anasema; "kwa kuwa mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo; nanyi mtapata raha nafsini mwenu." Tunatakiwa kuingia katika shule ya Kristo, kujifunza upole na unyenyekevu kwake. Ukombozi ni mchakato ule ambao kwa huo nafsi hufunzwa kwa ajili ya mbingu. Mafunzo haya yana maana ya kumjua Mungu. Yanalenga katika kuwekwa huru kutokana na maoni, mazoea, na vitendo vilivyopatikana kwa kujifunza katika shule ya mfalme wa giza. Lazima nafsi iokolewe kutoka katika yote yanayopingana na uaminifu kwa Mungu.

Katika moyo wa Kristo, mahali ambapo kuna upatanifu mkamilifu na Mungu, kulikuwa na amani kamilifu. Kamwe hakupendezwa na kupigiwa makofi, wala hakuhuzunishwa na makaripio na kukatishwa tamaa. Katikati ya upinzani mkuu mno na katika kutendewa ukatili mkubwa kuliko wote, alidumu kuwa na ujasiri. Lakini wengi wanaodai kuwa wafuasi wake wana moyo wenye shida na hisia za hasira, kwa sababu wanaogopa kujiaminisha kwa Mungu. Hawajisalimishi kikamilifu kwake; maana wanaogopa matokeo yanayoendana na kujisalimisha huko. Ikiwa hawaingii katika kujisalimisha huku, hawawezi kupata amani.

Kujipenda nafsi ndiko kunakoleta msukosuko. Tunapokuwa tumezaliwa kutoka juu, mawazo yale yale yaliyokuwa ndani ya Yesu yanakuwa ndani yetu, mawazo yaliyomwongoza **(331)** Yeye kujinyenyekeza ili kwamba tupate kuokolewa. Hapo hatutakuwa tunatafuta vyeo vya juu. Tutatamani kukaa miguuni pa Yesu, na kujifunza kwake. Tutaelewa kwamba thamani ya kazi yetu haihitaji kuwa na mambo ya kujionyesha na kupiga kelele ulimwenguni, na katika kutenda sana na kuwa na bidii kwa nguvu zetu wenyewe. Thamani ya kazi yetu iko katika uwiano unaoendana na kiwango cha kujawa na Roho Mtakatifu. Tumaini kwa Mungu huleta hali ya mawazo iliyo takatifu zaidi, ili kwamba tuweze kutawala nafsi zetu kwa uvumilivu.

Ng'ombe hufungwa nira ili kuwawezesha kuvuta mzigo, kuufanya kuwa mwepesi. Hivyo ndivyo ilivyo nira ya Kristo. Wakati mapenzi yetu yanapomezwa katika mapenzi ya Mungu, na sisi kutumia zawadi alizotupatia katika kuwabariki wengine, tutauona mzigo wa maisha ukiwa mwepesi. Yeye anayetembea katika njia ya amri za Mungu anatembea pamoja na Kristo, na moyo wake unapata raha katika pendo lake. Musa alipoomba kwamba, "Unionyeshe njia zako, nipate kukujua," Bwana alimjibu kwamba, "Uso wangu utakwenda pamoja nawe, nami nitakupa raha." Na kupitia kwa manabii ujumbe huu ulitolewa, "Bwana asema hivi, Simameni katika njia kuu, mkaone, mkaulize habari za mapito ya zamani, I wapi njia iliyo njema? Mkaende katika njia hiyo, nanyi mtajipatia raha katika nafsi zenu." Kutoka 33:13, 14; Yeremia 6:16. Na anasema, "Laiti ungalisikiliza amri zangu! Ndipo amani yako ingalikuwa kama mto wa maji, na haki yako kama mawimbi ya bahari." Isaya 48:18.

Wale wanamchukua Kristo kulingana na neno lake, na kusalimisha nafsi zao katika utunzaji wake, kuweka maisha yao katika mpango wake, watapata amani na utulivu. Hakuna kitu cha ulimwengu kinachoweza kuwahuzunisha pale Yesu anapowapatia furaha kwa kuwepo kwake. Katika ukubali mkamilifu kuna raha kamilifu. Bwana anasema, "Utamlinda yeye ambaye moyo wake umekutegemea katika amani kamilifu, kwa kuwa

anakutumaini." Isaya 26:3. Maisha yetu yanaweza kuonekana kama mvurugano wa mambo; lakini kadiri tunavyojikabidhi kwa Mtendaji Mkuu mwenye hekima, ataleta kielelezo cha maisha na tabia kitakachokuwa kinaelekeza katika utukufu wake. Na tabia ile inayoonyesha utukufu – tabia – ya Kristo itapokelewa katika Paradiso ya Mungu. Jamii ya watu waliofanywa upya watatembea pamoja naye katika weupe, maana wamestahili.

Kadiri tunavyoingia rahani kupitia Yesu, mbingu huanzia hapa hapa. Tunaitikia mwaliko wake usemao, Njoni, jifunzeni kwangu, na kwa kuja huko tunaanza maisha ya umilele. Mbingu ni kule kumsogelea bila kukoma Mungu kwa njia ya Kristo. Kadiri tunavyokuwa katika mbingu ya furaha, ndivyo utukufu zaidi na zaidi utakavyofunguliwa kwetu; na kadiri tunavyomjua Mungu zaidi, ndivyo kina cha furaha yetu kinavyoongezeka. Kadiri tunavyotembea na Yesu katika maisha haya, tunaweza kujazwa na pendo lake, na kutoshelezwa na uwepo wake. Yote ambayo asili ya mwanadamu **(332)** inaweza kuhimili, tutayapokea hapa hapa. Lakini haya ni nini ikilinganishwa na ya baada ya haya? Kuna wale ambao "wako mbele ya kiti cha enzi cha Mungu, nao wanamtumikia mchana na usiku katika hekalu lake, na yeye aketiye katika kiti cha enzi atatanda hema yake juu yao. Hawataona njaa tena, wala hawataona kiu tena, wala jua halitawapiga, wala hari iliyoyote. Kwa maana huyo Mwana-Kondoo, aliye katikati ya kiti cha enzi, atawachunga, naye atawaongoza kwenye chemchemi za maji yenye uhai, na Mungu atayafuta machozi yote katika macho yao." Ufunuo 7:15-17.

## Sura ya 35

# "Nyamaza, Utulie"

[Sura hii imejengwa katika Mathayo 8:23-34; Marko 4:35-41; 5:1-20; Luka 8:22-39.]

Ilikuwa siku yenye matukio mengi muhimu katika maisha ya Yesu. Kando ya Bahari ya Galilaya alikuwa ameisema mifano yake ya kwanza, akitumia vielelezo vinavyofahamika katika kuwafafanulia watu kuhusu ufalme wake na namna ambavyo ufalme huo ungeanzishwa. Alikuwa ameifananisha kazi yake sawa na mpanzi; akafananisha maendeleo ya ufalme wake sawa na kukua kwa mbegu ya haradali na kazi ya chachu katika kipimo fulani cha chakula. Alikuwa ameonyesha picha ya tukio kuu la kutenganisha mara ya mwisho kati ya wenye haki na waovu katika mfano wa ngano na magugu na juya la kuvulia samaki. Uthamani wa hali ya juu wa kweli ambazo alizifundisha ulikuwa umeelezwa kwa kutumia mfano wa hazina iliyositirika na lulu ya thamani kubwa, wakati katika mfano wa mwenye nyumba aliwafundisha wanafunzi wake namna ambavyo wangefanya kazi kama wawakilishi wake.

Siku nzima alikuwa amefundisha na kuponya; na pindi jioni ilipofika umati uliendelea kusongamana kwake. Siku kwa siku alikuwa amewahudumia, akipumzika kwa nadra ili kula chakula na kupumzika. Vitendo vya chuki vya upinzani na kumsema vibaya vilivyotumiwa na Mafarisayo wakati wote kukabiliana naye viliifanya kazi yake kuwa mbaya sana na ya mateso mengi; na sasa mwisho wa siku alikuwa amechoka sana kiasi kwamba alitafuta kupumzika mahali pa faragha ng'ambo ya ziwa.

Pwani ya mashariki ya Genesareti haikukaliwa sana na watu, maana kulikuwa na miji hapa na pale kando kando ya ziwa; lakini sehemu hiyo haikuwa na watu **(334)** ikilinganishwa na upande wa magharibi. Ilikuwa na watu ambao ni wapagani zaidi kuliko Wayahudi, na walikuwa na mawasiliano kidogo sana na Galilaya. Kwa hiyo eneo hili lilikidhi hitaji la Yesu, na sasa aliwataka wanafunzi wake wamsindikize kuja mahali hapa.

Baada ya kuwaaga makutano na kuwatawanya, walimchukua, "vile vile alivyo," katika chombo, wakaondoka. Lakini haikuwa waondoke peke yao. Pale karibu na upwa kulikuwa na vyombo vingine vya kuvulia samaki, haraka navyo vilijawa na watu waliomfuata Yesu, wakiwa bado na hamu ya kumwona na kumsikiliza.

Hatimaye Mwokozi aliondokana na msongamano wa makutano, na, akiwa ameelemewa na uchovu na njaa, alijilaza katika shetri, na mara tu akasinzia. Jioni ilikuwa tulivu na njema, na ziwa lilikuwa tulivu; lakini ghafla giza lilitanda mawinguni, upepo ulifagia katika makorongo ya milima kando kando ya pwani ile ya mashariki, na tufani kali ikapiga ziwani.

Jua lilikuwa limezama, na weusi wa usiku ulikuwa juu ya uso wa bahari yenye tufani. Mawimbi, yaliyoinuka kwa sababu ya upepo mkubwa, yalipiga na kurusha maji katika chombo cha wanafunzi wale, na yakatishia kukizamisha. Wale wavuvi mashuhuri walikuwa wametumia muda mwingi wa maisha yao ziwani, walikuwa wamepitia tufani nyingi na kuviongoza vyombo vyao kwa usalama; lakini sasa nguvu zao na ujuzi wao havikusaidia kitu. Hawakuwa na msaada katika dhoruba ile, na wakapoteza tumaini walipoona kwamba chombo kinazidi kujaa maji.

Wakiwa wamezama katika jitihada zao za kujiokoa, walikuwa wamesahau kwamba Yesu alikuwa katika chombo kile. Sasa, walipoona kwamba kazi yao yote ni bure na kifo tu ndicho kilichokuwa machoni pao, walimkumbuka Yeye ambaye walikuwa wanavuka kwa amri yake. Tumaini lao pekee lilikuwa kwa Yesu. Katika hali yao ya kukosa msaada na tumaini waliita, "Bwana, Bwana!" Lakini giza nene lililokuwepo liliwazuia wasimwone. Sauti zao zilimezwa na mvumo wa tufani, na kwa hiyo hakukuwa na jibu lolote. Walijawa na mashaka na hofu. Je, Yesu alikuwa amewaacha? Je, Yeye aliyekuwa ameshinda magonjwa na mapepo, na hata kifo, hakuwa na uwezo wa kuwasaidia wanafunzi wake sasa? Je, alikuwa hajui habari yao katika balaa ile?

Wanaita tena, lakini hakuna jibu isipokuwa mvumo wa hasira ya tufani. Tayari chombo chao kiko kinazama. Ndani ya muda mfupi, ni wazi kwamba walikuwa wanamezwa na maji yale yenye hasira.

Ghafla, mwako wa umeme unapenya katika giza na kuangaza, nao wanamwona Yesu akiwa amelala usingizi, akiwa hasumbuliwi na ghasia ile. Wakiwa katika mshangao na hamaki wanasema, "Mwalimu, si kitu kwako kuwa tunaangamia?" Yeye anawezaji kupumzika hivyo kwa amani, wakati wako hatarini na wanapambana na kifo?

**(335)** Kilio chao kilimwamsha Yesu. Pale mwako wa umeme unapomdhihirisha, wanaona amani ya mbinguni katika uso wake; wanapomwona wanasoma kwake hali ya kutojiangalia, upendo wa dhati, na mioyo yao inamgeukia, na wanalia wakisema, "Bwana, tuokoe, tunaangamia."

Kamwe hakuna kilio cha moyoni kinachopita pasipo kusikiwa. Wanafunzi wanapopaza sauti zao za vilio kama jitihada yao ya mwisho, Yesu anaamka. Anasimama katikati ya wanafunzi, wakati tufani inavyozidi, mawimbi yakiwapiga, na umeme ukiangazia mwonekano wake. Anainua mkono wake, uliokuwa umetumika mara nyingi katika matendo ya huruma, na kuiambia bahari iliyokuwa imechafuka, "Nyamaza, utulie."

Dhoruba ilikoma. Mawimbi yakatulia. Mawingu yakatoweka, na nyota zikaangaza. Chombo kikatulia kwenye bahari tulivu. Halafu akiwageukia wanafunzi wake, Yesu anawauliza kwa huzuni, "Mbona mmekuwa waoga? Hamna imani bado?" Marko 4:40.

Wale wanafunzi wakatekewa. Hata Petro hakudiriki kuonyesha mshangao uliokuwa umeujaza moyo wake. Vile vyombo vilivyokuwa vimetoka vikimsindikiza Yesu vilikuwa vimepatwa na hatari ile ile iliyokuwa imewapata wanafunzi. Hofu na fadhaa ilikuwa imewapata wale waliokuwemo; lakini amri ya Yesu ilileta utulivu wa hali ile ile. Kuchafuka kwa ile tufani kulikuwa kumevisukuma vyombo vile na kuvifanya kukaribiana sana, na wote waliokuwa katika vyombo vile walishuhudia mwujiza ule. Katika utulivu uliofuata, ule woga ulisahaulika. Watu wakanong'onezana wakisema, "Huyu ni mtu wa namna gani hata pepo na bahari zamtii?"

**(336)** Yesu alipoamshwa ili akabiliane na tufani, alikuwa katika amani kamili. Hakukuwa na hali yoyote ya woga katika neno lake wala mwonekano wake, maana kakuna hofu iliyokuwa moyoni mwake. Lakini hakutumainia katika hali ya kuwa na uweza. Hakuwa katika utulivu ule kwa sababu ya kuwa Bwana wa nchi na bahari na anga. Alikuwa ameweka pembeni uweza huo, na anasema, "Mimi siwezi kufanya neno mwenyewe." Yohana 5:30. Alitumainia uweza wa Baba. Yesu alijitegemeza katika imani – imani katika upendo na utunzaji wa Mungu, - na nguvu ya neno lile lililotuliza dhoruba ilikuwa nguvu ya Mungu.

Kama vile ambavyo Yesu alitulia kwa imani katika ulinzi wa Baba, ndivyo tunavyopaswa kutulia katika ulinzi wa Mwokozi. Wanafunzi wale wangekuwa walimtumainia, wangehifadhiwa kwa amani. Woga wao katika wakati wa hatari ulidhihirisha kutokuamini kwao. Katika jitihada za kujiokoa wao wenyewe, walimsahau Yesu; na aliwapa msaada wakati walipomgeukia tu wakiwa na hofu ya kujitumainia wenyewe.

Ni mara nyingi kiasi gani tunapopatwa na uzoefu wa wanafunzi hao! Wakati tufani ya majaribu inapojikusanya, na mwanga mkali unapoangaza, na mawimbi yanapotupiga, tunapambana na mawimbi tukiwa peke yetu, tukisahau kwamba yupo Yeye anayeweza kutusaidia. Tunatumainia nguvu zetu wenyewe mpaka matumaini yetu yanapotea, na tunakuwa tayari kupotea. Halafu tunamkumbuka Yesu, na kama tutamwita atuokoe, kilio chetu hakitakuwa bure. Ingawa anatukemea kwa kutoamini kwetu na kujitumainia wenyewe, haachi kamwe kutupatia msaada tunaohitaji. Iwe tuko nchi kavu au baharini, tukiwa na Mwokozi mioyoni mwetu, hakuna haja ya kuogopa. Imani iliyo hai ndani ya Mkombozi itatuliza bahari ya maisha, nayo itatuokoa kutoka katika hatari kwa njia anayojua kuwa ndiyo njema zaidi.

Lipo fundisho la kiroho jingine tunalopata katika mwujiza huu wa kutuliza dhoruba. Uzoefu wa kila mtu unashuhudia ukweli wa maneno ya Maandiko kwamba, "Wabaya wanafanana na bahari iliyochafuka; maana haiwezi kutulia. . . . Hapana amani kwa wabaya; asema Mungu wangu." Isaya 57:20, 21. Dhambi imeharibu amani yetu. Nafsi isiposalimishwa, hatuwezi kupata utulivu. Hakuna nguvu za mwanadamu zinazoweza kutawala tamaa za mivuto ya moyoni. Tuko katika hali isiyo na msaada sasa kama vile ambavyo wanafunzi hawakuwa na uwezo wa kutuliza dhoruba. Lakini Yeye aliyeitamka amani kwenye mawimbi ya Galilaya ametamka maneno ya amani kwa kila nafsi. Hata dhoruba iwe kali kiasi gani, wale wanaomgeukia Yesu wakilia kwamba, "Bwana, tuokoe," watapata kuokolewa. Neema yake, ipatanishayo moyo kwa Mungu, hutuliza dhoruba ya mhemuko wa mwanadamu, na moyo unatulia katika pendo lake. "Huituliza dhoruba, ikawa shwari, Mawimbi yake yakanyamaza. Ndipo walipofurahi kwa kuwa yametulia; **(337)** Naye huwaleta mpaka bandari waliyoitamani." Zaburi 107:29, 30. "Basi tukiisha kuhesabiwa haki itokayo katika imani, na mwe na amani kwa Mungu, kwa njia

ya Bwana wetu Yesu Kristo." "Na kazi ya haki itakuwa amani; na mazao ya haki yatakuwa ni utulivu na matumaini daima." Warumi 5:1; Isaya 32:17.

Asubuhi na mapema Mwokozi na wale waliokuwa naye waliifikilia pwani, na nuru ya jua lililokuwa likichomoza iligusa bahari na nchi kavu kama udhihirisho wa amani. Lakini muda si muda baada tu ya kutia mguu ufukweni walikutana na jambo la kutisha kuliko hata mvumo wa tufani. Watu wawili waliopagawa na pepo, wakitoka makaburini, waliwajia kwa haraka kama vile kuja kuwararua na kuwavunja vunja. Vipande vya minyororo waliyokuwa wamefungwa ili kudhibitiwa wakaikatakata vilikuwa vinaning'inia. Walikuwa wakitokwa na damu kwa sababu ya kujikatakata kwa mawe makali. Walikuwa na macho makali ya hasira yaliyokazwa kupitia katikati ya nywele zao nyingi na ndefu, mwonekano wa mwanadamu ukiwa umeondolewa na mapepo yale yaliyowapagaa, nao wakaonekana kama wanyama wa mwitu zaidi kuliko mwonekano wa wanadamu.

Wanafunzi na wenzao wengine walikimbia mbali kwa hofu; lakini wakati huo wakagundua kwamba Yesu hakuwa pamoja nao, nao wakarudi kumtafuta. Alikuwa amesimama pale pale walipomwacha. Yeye aliyekuwa ametuliza dhoruba, ambaye kabla alikuwa amekutana na Shetani na akamshinda, hakukimbia mapepo haya. Watu wale, waliokuwa wakisaga meno, wakitokwa na mapovu mdomoni, walipomkaribia, Yesu alinyosha mkono ule uliokuwa umetumika kuyapa mawimbi ishara ya kutulia, na watu wale wakaweza kusogea karibu. Mapepo yale yakasimama yakipiga kelele mbele yake pasipo msaada.

Kwa mamlaka aliwaamuru wale pepo wachafu kuwatoka watu wale. Maneno yake yalipenya hadi katika fahamu za waathirika wale zilizokuwa zimetiwa giza. Kwa uhafifu **(338)** walitambua kwamba pale karibu alikuwepo Yeye ambaye angeweza kuwaokoa kutoka katika kuteswa na pepo wale. Walianguka miguuni pa Yesu ili kumwabudu; lakini pindi vinywa vyao vilipofunguka kuomba rehema yake, pepo wale waliongea kupitia vinywa hivyo, kila mmoja akilia kwa nguvu kwamba, "Nina nini nawe, Yesu, Mwana wa Mungu aliye juu? Nakuapisha kwa Mungu usinitese."

Yesu aliuliza, "Jina lako nani?" Na jibu lilikuwa, "Jina langu ni Legioni: kwa kuwa tu wengi." Wakiwatumia waathirika wale kama njia ya kuwasiliana, walimwomba Yesu asiwapeleke nje ya nchi ile. Kwenye ubavu wa mlima mahali ambapo si mbali sana kulikuwa na kundi kubwa la nguruwe wakilisha. Pepo wale wakaomba waruhusiwe kuingia kwa nguruwe hawa, naye Yesu akawaruhusu. Mara taharuki ikawajaa. Wakiwa wamepagawa wakatelemka haraka kuelekea penye ukuta wa ukingo wa bahari, na pasipokuwa na uwezo wa kujidhibiti, wakaporomoka na kutumbukia ziwani, wakaangamia.

Hayo yakiendelea badiliko zuri la kushangaza lilikuwa limekuja kwa wale waliokuwa wamepagawa. Nuru ilikuwa imeangaza katika mawazo yao. Macho yao yaliangaziwa na mwale wa ufahamu. Sura yao, ambayo ilikuwa imebadilishwa na kuwa katika sura ya Shetani, iligeuka ghafla na kuwa sura nzuri ya mwanadamu, mikono ile iliyokuwa na makovu ilitulia, na kwa sauti ya kupendeza watu wale walimsifu Mungu kwa wokovu waliopata.

Kule kwenye ukingo wa bahari wachungaji wa nguruwe walikuwa wameona yote yaliyotokea, na waliharakisha kwenda kuwapasha habari zile waajiri wao na watu wengine. Wakiwa na hofu na mshangao watu wote walikuja kukutana na Yesu. Wale wenye kupagawa wawili walikuwa kitisho kwa nchi. Hakuna mtu aliyeweza kupita kwa usalama mahali walipokuwa; maana walimkimbilia kwa hasira za pepo kila msafiri. Sasa watu hawa walikuwa wamevishwa nguo na wakiwa katika hali nzuri, wakiwa wamekaa miguuni pa Yesu, wakisikiliza maneno yake, na kulitukuza jina lake Yeye aliyekuwa amewaponya. Lakini watu walioona tukio hili la kushangaza hawakufurahi. Hasara ya nguruwe wale ilionekana kuwa kubwa zaidi kuliko kuokolewa kwa mateka hawa wa Shetani.

Ile hasara ilikuwa imeruhusiwa kuja kwa wale wamiliki wa nguruwe kama neema kwao. Walikuwa wamezama katika vitu vya kidunia, na hawakujali faida kuu za maisha ya kiroho. Yesu alitaka kuvunja kivutio cha maisha ya ubinafsi, ili ya kwamba wapokee rehema yake. **(339)** Lakini majuto na lawama kwa ajili ya hasara ya mali vilipofusha macho yao wasione neema ya Mwokozi.

Udhihirisho wa uwezo ule usio wa kibinadamu uliamsha imani za kishirikina miongoni mwa watu wale, na ulizua hofu kwao. Wakadhani kwamba huenda majanga mengine yakafuata kwa kuwepo kwa Mgeni huyu. Walihofia uharibifu wa mali, na wakaazimia kuwekwa huru mbali na uwepo wake. Wale waliokuwa wamevuka ziwa pamoja na Yesu walisimlia yote yaliyokuwa yametokea usiku uliokuwa umetangulia, habari za hatari ya

tufani, na jinsi ambavyo upepo na bahari vilikuwa vimetulizwa. Lakini maneno yao hayakuwa na maana kwa watu hawa. Walizidi kumsonga Yesu kwa hofu, wakimsihi aondoke kwao, naye akakubali, akachukua chombo na kwenda pwani ya ng'ambo.

Watu wa kule katika nchi ya Wagerasi walikuwa na ushahidi wa nguvu na neema ya Kristo machoni pao. Waliwaona watu waliokuwa wamepagawa wakarejeshwa katika akili nzuri; lakini walikuwa na hofu ya kuhatarisha faida zao za kidunia kiasi kwamba Yeye aliyekuwa amemshinda mfalme wa giza mbele yao alionekana kwao kama mtu anayeingilia mambo yao, na huyo ambaye ni Zawadi aliyetoka mbinguni akaondoka katika malango yao. Sisi hatuna mazingira ya kugeuka kutoka kwa Kristo kama yale waliyokuwa nayo wale Wagerasi; lakini bado wapo wengi ambao wanakataa kutii neno lake, kwa sababu kutii kunaweza kuendana na kupoteza faida fulani za kidunia. Kwa kuwa uwepo wake utawasababishia hasara ya pesa, wengi wanaikataa rehema yake, na kumfukuza Roho wake kutoka kwao.

Lakini kilichokuwa tofauti kwa mbali ni hisia za wale waliokuwa wamepagawa. Walitamani kuwa pamoja na huyo aliyewaokoa. Katika uwepo wake walijisikia kuwa salama kutokana na pepo waliokuwa wametesa maisha yao na kuharibu utu wao. Wakati Yesu alipotaka kuingia chomboni, waliendelea kuwa karibu yake, wakapiga magoti miguuni pake, na kumwomba awaweke karibu yake muda wote, mahali ambapo wangeendelea kuyasikia maneno yake daima. Lakini Yesu aliwataka waende nyumbani wakasimulie mambo makuu ambayo Bwana alikuwa amewatendea.

Hapa ndipo palipokuwa na kazi yao ya kufanya, - kwenda katika nyumba zao za kipagani, na kueleza habari za mbaraka waliokuwa wamepata kutoka kwa Yesu. Ilikuwa vigumu kwao kutengana na Mwokozi. Magumu makubwa yangewakumba kwa hakika katika kujumuika na wapagani wa nchi yao. Na ile hali ya kutengwa na jamii yao kwa muda mrefu ilionekana kutowastahilisha kufanya kazi aliyokuwa amewaonyesha. Lakini mara tu Yesu alipowaonyesha wajibu wao walikuwa tayari kutii. Si tu kwamba waliwaambia habari za Yesu watu wa nyumbani mwao na majirani, bali walienda pia katika Dekapoli yote, wakitangaza kila mahali uweza wake wa kuokoa, na kueleza jinsi alivyowaweka huru mbali na mapepo. Katika kufanya kazi hii walipata baraka **(340)** kuu zaidi kuliko vile ambavyo wangebaki naye tu kwa ajili ya manufaa yao wenyewe. Tunaletwa karibu na Mwokozi zaidi kwa njia ya kufanya kazi ya kutangaza habari njema.

Wale watu walioponywa mapepo walikuwa wamishonari wa kwanza waliotumwa na Yesu kuihubiri injili katika eneo la Dekapoli. Ni watu hawa tu waliokuwa wamejaliwa kusikia mafundisho ya Kristo kwa muda mfupi. Hakukupata kutokea hata hubiri moja lililosikika katika masikio yao. Wasingeweza kuwafundisha watu vile ambavyo ingewezekana kufanywa na wanafunzi wake waliokuwa naye kila siku. Lakini walibeba katika sura zao wenyewe ushahidi kwamba Yesu alikuwa Masihi. Wangesimulia kile walichokuwa wanajua; kile ambacho wao wenyewe walikuwa wameona, na kusikia, na kuhisi kuhusu uweza wa Kristo. Hiki ndicho anachoweza kufanya kila mmoja ambaye moyo wake umeguswa na neema ya Mungu. Yohana, yule mwanafunzi aliyependwa sana na Yesu, aliandika hivi: "Lile lililokuwako tangu mwanzo, tulilolisikia, tulililoliona kwa macho yetu, tulilolitazama, na mikono yetu ikalipapasa, kwa habari ya Neno la uzima; . . . hilo tulililoliona na kulisikia, twawahubiri na ninyi." 1 Yohana 1:1-3. Kama mashahidi wa Kristo, tunapaswa tusimulie kile tunachojua, kile ambacho sisi wenyewe tumeona na kusikia na kugusa. Ikiwa tumekuwa tukimfuata Yesu hatua kwa hatua, tutakuwa na kitu fulani sahihi kinachofaa kusimulia kuhusu njia ambayo ametuongoza kuipita. Tunaweza kusimulia jinsi ambavyo tumezijaribu ahadi zake, na kuona kwamba ni za kweli. Tunaweza kutoa ushuhuda wa kile ambacho tumekijua kuhusu neema ya Kristo. Huu ndio ushuhuda ambao Bwana anatuitia, na ambao ulimwengu unaangamia kwa kuukosa.

Ingawa Wagerasi hawakuwa wamempokea Yesu, hakuwaacha katika giza walilokuwa wamechagua. Wakati wao walimtaka aondoke kwao, hawakuwa wamesikia maneno yake. Walikuwa hawajui kile walichokuwa wanakikataa. Kwa hiyo alituma nuru tena kwao, tena kupitia watu ambao wenyeji wale wasingekataa kuwasikiliza.

Kwa kusababisha kuangamia kwa nguruwe, Shetani alikusudia kuwageuza watu waende mbali na Mwokozi, na kuzuia kuhubiriwa kwa injili katika eneo lile. Lakini tukio lenyewe likaamsha nchi yote kuliko vile ambavyo kitu kingine chochote kingeweza kufanya, na kuelekeza usikivu wao kwa Kristo. Ingawa Mwokozi mwenyewe aliondoka pale, wale watu waliokuwa wameponywa naye walibaki wakiwa mashuhuda wa uweza wake. Watu

wale ambao kabla walikuwa njia ya mawasiliano ya mfalme wa giza wakageuka kuwa mifereji ya nuru, wajumbe wa Mwana wa Mungu. Watu walishangazwa walipozisikia habari zile za ajabu. Mlango ulifunguka kwa ajili ya injili katika eneo lote lile. Yesu aliporudi Dekapoli kwa mara nyingine, watu walijazana kwake, na kwa muda wa siku **(341)** tatu, si tu wakazi wa mji ule mmoja, bali maelfu ya watu kutoka maeneo yanayozunguka mji ule, waliusikia ujumbe wa wokovu. Hata nguvu za mapepo ziko chini ya udhibiti wa Mwokozi wetu, na kazi za mwovu zinadhibitiwa kwa ajili ya mema.

Kule kukutana na wale waliopagawa na pepo katika nchi ya Wagerasi kulikuwa na fundisho kwa ajili ya wanafunzi. Kulionyesha vina vya uharibifu ambamo Shetani anatafuta kuwasukumia wanadamu wote, na kazi ya Kristo ya kuwaweka wanadamu huru kutokana na nguvu za Shetani. Wale watu waliokuwa wanasumbuka, wakiishi mahali pa makaburi, wakiwa wamepagawa na pepo, wakiwa wamefungwa katika hisia mbaya zisizotawalika, na tamaa zisizozuilika, wanawakilisha vile ambavyo wanadamu wangekuwa ikiwa wangewekwa katika utawala wa kishetani. Ushawishi wa Shetani unakandamizwa kwa watu ili kuharibu hisia za fahamu, na kutawala mawazo ili yawe ya uovu, na kuamsha vurugu na uhalifu. Hudhoofisha mwili, hutia giza katika ufahamu, na kuihafifisha nafsi. Watu wanapokataa mwaliko wa Mwokozi, wanajiweka chini ya mamlaka ya Shetani. Watu wengi katika kila idara maishani, nyumbani, kazini, na hata kanisani, wanafanya hivyo leo. Ni kwa sababu ya haya kwamba vurugu na uhalifu vimejaa kote duniani, na giza la kimaadili, kama tambala zito jeusi la kifo, limeyafunika makazi ya wanadamu. Kupitia majaribu yake ya thamani kwake Shetani huwaongoza watu kwenda katika uovu mbaya zaidi na zaidi, mpaka matokeo yake yanapokuwa kuharibu na maangamizi ya jumla. Salama pekee dhidi ya nguvu zake inapatikana katika uwepo wa Yesu. Shetani amefunuliwa mbele ya wanadamu na malaika kama mharibifu na adui wa mwanadamu; huku Kristo akiwa kama mkombozi na rafiki wa mwanadamu. Roho wake atayaendeleza ndani ya mtu yale yote yatakayoifanya tabia kuwa njema na kuiinua hali ya mwanadamu. Atamjenga mtu kwa ajili ya utukufu wa Mungu katika mwili na nafsi na roho. "Maana Mungu hakutupa roho ya woga, bali ya nguvu na ya upendo na ya moyo wa kiasi." 2 Timotheo 1:7. Ametuita " ili kuupata utukufu" – tabia – "wa Bwana wetu Yesu Kristo;" ametuita ili tufananishwe "na mfano wa Mwana wake." 2 Wathesalonike 2:14; Warumi 8:29.

Na nafsi zile ambazo zimeshushwa na kuwa vitendea-kazi vya Shetani bado zinabadilishwa kwa nguvu ya Kristo na kufanywa kuwa wajumbe wa haki, na Mwana wa Mungu humtuma mtu kama huyo akimwambia, Nenda ukasimulie "ni mambo gani makuu aliyokutendea Bwana, na jinsi alivyokurehemu."

## Sura ya 36

# Mguso wa Imani

[Sura hii imejengwa katika Mathayo 9:18-26; Marko 5:21-43; Luka 8:40-56.]

Akirudi katika pwani ya magharibi kutoka katika nchi ya Wagerasi, Yesu alikuta umati wa watu unasubiri kumpokea, nao walimsalimu kwa furaha. Alibaki pale kando ya bahari kwa muda kitambo, akifundisha na kuponya, halafu akaenda katika nyumba ya Lawi-Mathayo kukutana na watoza ushuru katika karamu ile. Hapa ndipo Yairo, mtu mkuu wa sinagogi, alipomkuta.

Huyu mzee wa Wayahudi alikuja kwa Yesu akiwa katika huzuni, na alijitupa miguuni pa Yesu, na kusihi, "Binti yangu mdogo yu katika kufa; nakuomba uje, uweke mkono wako juu yake, apate kupona, na kuishi."

Yesu aliondoka mara moja pamoja na mkuu yule kwenda nyumbani kwake. Ingawa wanafunzi wake walikuwa wameona mengi ya matendo yake ya huruma, walishangazwa na jinsi alivyokubaliana na ombi la rabi yule; lakini walimsindikiza Bwana wao, na watu walifuata, wakiwa na hamu na matarajio ya kuona.

Nyumba ya yule mtu mkuu haikuwa mbali na pale, lakini Yesu na wale aliokuwa nao walienda taratibu, kwa kuwa umati ulimsonga kila upande. Yule baba hakuridhishwa na kukawia kule; lakini Yesu akionyesha upendo kwa watu, alisimama hapa na pale kutuliza baadhi waliokuwa wanaumwa, au kufariji wenye shida moyoni.

Wakati wakiwa bado wako mbali, mjumbe alikuja akijipenyeza katika umati, akiwa na ujumbe unaokuja kwa Yairo kwamba yule binti yake alikuwa amekufa, na hakukuwa na sababu ya kumsumbua Bwana zaidi. Ule ujumbe ulinaswa na sikio la **(343)** Yesu. Akamwambia, "Usiogope, amini tu, naye ataponywa."

Yairo aliendа karibu zaidi na Yesu, na wakatoka pamoja kwa haraka kwenda nyumbani kwa yule mtu mkuu. Tayari waombolezaji wa kukodiwa na wapiga filimbi walikuwepo pale, wakilijaza anga kwa sauti zao. Kule kuwepo kwa umati wa watu na ghasia, viliitia simanzi roho ya Yesu. Alijaribu kuwanyamazisha, akisema, "Mbona mnafanya ghasia na kulia? Kijana hakufa, bali amelala tu." Walichukizwa kwa maneno hayo ya Mgeni. Walikuwa wamemwona yule mtoto alipokuwa anakufa, kwa hiyo wakamcheka Yesu kwa kejeli. Akiwataka wote waondoke ndani ya nyumba, Yesu alienda na baba na mama wa yule binti, pamoja na wale wanafunzi watatu, yaani Petro, Yakobo na Yohana, wakaingia katika chumba alichokuwemo marehemu.

Yesu alisogea kando ya kitanda, na, huku akiuweka mkono wa mtoto yule mkononi mwake, alitamka kwa upole, katika lugha iliyokuwa ikieleweka pale nyumbani, maneno haya, "Msichana, Nakuambia, inuka."

Mara hiyo hiyo mtetemo ulipita katika mwili ule usio na fahamu. Mapigo ya moyo unaoishi yakaanza tena. Midomo ilifunguka kwa tabasamu. Macho yalifunguka sana kama aliyetoka usingizini, na yule binti akalikazia macho kwa mshangao kundi la watu waliokuwa pembeni yake. Aliinuka, na wazazi wake wakamkumbatia, na wakalia kwa furaha.

Alipokuwa njiani kwenda nyumbani kwa mkuu yule, Yesu alikuwa amekutana, katika umati ule, na mwanamke maskini aliyekuwa ameugua kwa miaka kumi na miwili ugonjwa uliosababisha maisha yake kuwa mzigo. Alikuwa ametumia vyote alivyo navyo kwa matabibu na tiba, akiishia kuambiwa kwamba ugonjwa hautibiki. Lakini matumaini yake yalirejea pindi aliposikia habari za uponyaji uliofanywa na Yesu. Alijisikia kuhakikishiwa kwamba ikiwa angeenda kwa Yesu tu angeponywa. Katika hali ya udhaifu na maumivu yule mwanamke alikuja kando ya bahari mahali ambapo Yesu alikuwa akifundisha, na akajaribu kujipenyeza katikati ya umati, lakini asiweze. Kwa mara nyingine tena alimfuata akitoka katika nyumba ya Lawi-Mathayo, lakini bado hakuweza kumfikia. Alikuwa ameanza kukata tamaa, ndipo Yesu akaja karibu yake, wakati alipokuwa anatembea katikati ya umati ule.

Nafasi adimu ilikuwa imemjia. Alikuwa mbele ya Tabibu Mkuu! Lakini katika mchanganyiko ule mwanamke yule hakuweza kumwambia Yesu kitu, wala hakuweza kukamata kitu zaidi ya kuona mwili wa Yesu uliokuwa unapita. Akihofia kupoteza ile fursa moja pekee, alisogea mbele, akisema moyoni mwake, "Nikiyagusa mavazi yake tu, nitapona." Kadiri Yesu alivyokuwa anapita, mwanamke yule alisogea mbele, na akafanikiwa kugusa sehemu ya

mwisho ya vazi la Yesu. Lakini ghafla alijua kwamba amepona. Alikuwa amekusanya imani ya maisha yake katika mguzo ule mmoja, na mara ile ile maumivu yake na udhaifu wake vilikoma na mahali pake akawa na nguvu na afya njema.

**(344)** Akiwa na moyo wa shukrani alijaribu kujiondoa katika umati ule; lakini ghafla Yesu alisimama, na watu wakasimama pamoja naye. Aligeuka, naye akiangalia huku na huku aliuliza kwa sauti kubwa iliyosikiwa ikiwa juu ya kelele zilizokuwepo katika umati ule, "Ni nani aliyenigusa?" Watu walimjibu kwa swali lake kwa mshangao. Vile alivyokuwa, akiwa anagongana katika pande zote, na akiwa amesongwa sana hapa na pale, swali lake lilionekana kuwa la kushangaza.

Petro, ambaye wakati wote huwa yuko tayari kusema, akasema, "Bwana mkubwa, makutano haya wanakuzunguka na kukusonga, nawe wasema, Ni nani aliyenigusa?" Yesu akajibu akasema, "Mtu alinigusa, maana naona ya kuwa nguvu zimenitoka." Mwokozi aliweza kutofautisha kati ya mguso wa imani na migusano ya kawaida tu ya msongamano wa watu wasiojali. Imani ya namna hiyo haiwezi kupita tu bila kuzungumziwa. Alitaka kumwambia yule mwanamke maneno ya faraja ambayo yangekuwa chemchemi ya kisima cha furaha kwake, - maneno ambayo yangekuwa baraka kwa wafuasi wa Yesu hadi mwisho wa wakati.

Akimwangalia yule mwanamke, Yesu alisisitiza ili kutaka kujua mtu aliyemgusa. Baada ya kuona kujificha hakuna mafanikio, mwanamke yule alikuja mbele akitetemeka, **(347)** na kujitupa miguuni pa Yesu. Akiwa na machozi ya shukrani alisimulia kisa cha ugonjwa wake, na jinsi alivyopona. Kwa upole Yesu akasema, "Binti, imani yako imekuponya, enenda zako kwa amani, uwe mzima." Hakutoa nafasi ya mawazo ya ushirikina kujiingiza kuhusu nguvu ya kuponya kwa kugusa vazi lake tu. Uponyaji ule haukupatikana kwa mgusano wa nje tu, bali kwa imani iliyoshikilia nguvu yake ya uungu.

Umati wa watu wale waliokuwa wanashangaa wakiwa wamemsonga Kristo hawakuifikia nguvu ile ya thamani. Lakini pindi mwanamke mgonjwa aliponyosha mkono wake na kumgusa Yesu, akiamini kwamba anaweza kuponywa, aliisikia nguvu inayoponya. Hivyo ndivyo ilivyo katika mambo ya kiroho. Kuongea kuhusu dini katika hali ya kawaida, kusali pasipo kuwa na imani iliyo hai na moyo wenye njaa, hakuna msaada wowote. Imani katika Kristo kwa jina tu, ambayo inamkubali tu kama Mwokozi wa ulimwengu, haiwezi kuleta uponyaji wa moyo. Imani inayoelekeza katika wokovu si ufahamu wa ukweli tu. Yeye asubiriye kujua mambo mengi kabla hajafanyia kazi imani, hawezi kupokea baraka kutoka kwa Mungu. Kuamini *kuhusu* Kristo hakutoshi; lazima tuamini *katika* Yeye. Imani pekee itakayotufaidi ni ile inayomkumbatia kama Mwokozi wa mtu binafsi; ndiyo inayoleta mema yake kwetu. Wengi huishikilia imani kama maoni. Imani iokoayo ni muamala ambao kupitia huo wale wanaompokea Kristo wanajiunga katika uhusiano wa agano na Mungu. Imani halisi ni maisha. Imani ilyo hai ina maana ya kuongezeka kwa nguvu, kutumaini kwa kujitoa, ambapo nafsi huwa na nguvu ya ushindi.

Baada ya kumponya yule mwanamke, Yesu alimtaka atangaze baraka alizokuwa amepokea. Zawadi zitolewazo na injili hazipaswi kupatikana kwa kificho wala kufurahiwa kwa siri. Hivyo Bwana anatuita tutangaze wema wake. "Ninyi ni mashahidi wangu, asema Bwana, nami ni Mungu." Isaya 43:12.

Kazi yetu ya kuutangaza uaminifu wake Bwana ndiyo njia iliyochaguliwa na mbingu kwa ajili ya kumfunua Kristo ulimwenguni. Yatupasa tukiri neema yake kama ilivyojulishwa kwetu na watu wa zamani; lakini kitakachokuwa na ufanisi zaidi ni ushuhuda wa uzoefu wa yale ambayo tumeyashuhudia. Tu mashahidi wa Mungu kadiri tunavyofunua utendaji wa nguvu ya uungu ndani yetu. Kila mtu ana maisha ambayo yanajipambanua tofauti na wengine, na uzoefu unaotofautiana na wa wale wengine. Mungu anatamani kwamba sifa zetu kwake zipande juu, zikiwa zimewekwa alama za tabia zetu. Hizi shukrani za thamani za sifa za utukufu wa neema yake, zikitegemezwa na maisha kama ya Kristo, zina nguvu zisizopingika zifanyazo kazi kwa ajili ya wokovu wa watu.

**(348)** Wale wenye ukoma kumi walipokuja kwa Yesu ili waponywe, aliwataka waende kujionyesha kwa kuhani. Njiani wakiwa wanaenda, walitakasika, lakini mmoja wao tu ndiye aliyerudi kumpa utukufu. Wengine walienda zao, wakimsahau Yeye aliyekuwa amewaponya. Ni wangapi ambao bado wanafanya kitu kile kile! Bwana anafanya kazi wakati wote kwa ajili ya kumnufaisha mwanadamu. Daima anatoa zawadi zake. Anainua wagonjwa kutoka katika vitanda vya machungu, anaokoa watu kutoka katika hatari ambazo hawaoni, anawakabidhi malaika wa mbinguni kazi ya kuwaokoa kutoka katika majanga, kuwaongoza kuondokana na "tauni ipitayo gizani," na ule “uharibuo adhuhuri" (Zaburi 91:6); lakini mioyo yao haijaguswa. Ametoa utajiri

wote wa mbinguni kuwakomboa; lakini bado hawajali upendo wake mkuu. Kwa kutokuwa kwao na shukrani wanaifunga mioyo yao isipate ya neema ya Mungu. Kama ilivyo mbuga katika jangwa hawajui kwamba mema yanakuja wakati gani, na mioyo yao iko mahali pakavu jangwani.

Kutunza kumbukumbu ya kila zawadi ya Mungu ni kwa manufaa yetu wenyewe. Kwa njia hiyo imani inaimarishwa ili kudai na kupokea zaidi na zaidi. Katika mbaraka mdogo tunaopokea sisi wenyewe kutoka kwa Mungu tunatiwa moyo zaidi kuliko habari zote tunazoweza kusoma kuhusu imani na uzoefu wa watu wengine. Mtu anayeitikia neema ya Mungu atakuwa kama bustani imwagiliwayo. Afya yake itastawi haraka; nuru yake itazuka katika giza; na utukufu wa Mungu utaonekana kwake. Kwa hiyo hebu na tukumbuke wema wa upendo wa Bwana, na wingi wa rehema zake. Kama ilivyokuwa kwa watu wa Israeli, hebu na tusimike mawe yetu ya ushuhuda, na tuandike juu ya mawe hayo visa vya thamani kuhusu mambo ambayo Mungu ametutendea. Na kadiri tunavyoyasoma kuangalia jinsi Mungu alivyoshughulika nasi katika safari yetu, basi, kwa mioyo iliyoyeyuka kwa shukrani, tutangaze kwamba, "Nimrudishie Bwana nini kwa ukarimu wake wote alionitendea? Nitakipokea kikombe cha wokovu; na kulitangaza jina la Bwana; nitaziondoa nadhiri zangu kwa Bwana, naam, mbele ya watu wake wote." Zaburi 116:12-14.

## Sura ya 37

# Wainjilisti wa Kwanza

[Sura hii imejengwa katika Mathayo 10; Marko 6:7-11; Luka 9:1-6.]

Mitume walikuwa watu wa familia ya Yesu, na walikuwa wamemsindikiza alipokuwa akisafiri kwa mguu katika Galilaya yote. Walikuwa wameshiriki naye masumbufu na ugumu waliokutana nao. Walikuwa wamesikiliza masimulizi yake, walikuwa wametembea na kuzungumza na Mwana wa Mungu, na kutokana na mafunzo aliyowapa kila siku walikuwa wamejifunza namna ya kufanya kazi ya kuwainua wanadamu. Kadiri Yesu alivyowahudumia makutano wengi waliokusanyika kwake, wanafunzi wake walikuwepo, wakiwa tayari kufanya kile alichowataka kufanya na kuifanya kazi yake kuwa nyepesi. Walisaidia katika kuwapanga watu, kuwaleta walio wagonjwa kwa Mwokozi, na kuhakikisha kwamba wote wanafarijika. Waliwaangalia wasikilizaji walioonyesha kuvutiwa, wakawafafanulia Maandiko, na kwa namna tofauti-tofauti walifanya kazi kwa ajili ya manufaa yao kiroho. Walifundisha yale waliyokuwa wamejifunza kwa Yesu, na kila siku walikuwa wanapata uzoefu mwingi. Lakini walihitaji pia uzoefu wa kufanya kazi peke yao. Walikuwa bado wanahitaji mafunzo mengi, uvumilivu mwingi na upole. Sasa, wakati alipokuwa nao, ili kuwaonyesha makosa yao, na kuwashauri na kuwasahihisha, Mwokozi aliwatuma waende kama wawakilishi wake.

Wakati walipokuwa naye Yesu, wanafunzi wale walikuwa wametatanishwa na mafundisho ya waandishi na Mafarisayo, lakini walikuwa wameuleta utata ule kwa Yesu. Alikuwa ameweka mbele yao ukweli wa Maandiko kama unavyotofautiana na mapokeo. Hivyo alikuwa ameimarisha ujasiri wao katika neno la Mungu, na kwa kiwango kikubwa alikuwa amewaweka huru kutokana na woga wao kwa marabi na utumwa wao katika mapokeo. Katika **(350)** kuwafunza wanafunzi wale kielelezo cha maisha ya Mwokozi kilikuwa na ufanisi mkubwa kwa mbali sana kuliko mafundisho ya kuwahubiri. Walipokuwa wametengana na kuondoka, kila mwonekano wake na sauti na neno vilirejea mawazoni mwao. Mara nyingi walipokuwa katika mgogoro na maadui wa injili, waliyarudia maneno yake, na walipoona ufanisi wao kwa watu, walifurahi sana.

Akiwaita kwake wale kumi na wawili, Yesu aliwataka waondoke wawili wawili katika miji na vijiji. Hakuna aliyetumwa akiwa peke yake, ndugu aliienda na ndugu, rafiki aliienda na rafiki. Kwa njia hiyo wangeweza kusaidiana na kutiana moyo, wakishauriana na kuomba pamoja, nguvu za mmoja zikijazia mapungufu ya mwingine. Kwa namna ile ile aliwatuma wale sabini baadaye. Kusudi la Mwokozi lilikuwa ni kwamba wajumbe wa injili wajumuike namna hii. Katika wakati wetu kazi ya uinjilisti ingefanikiwa kwa mbali sana ikiwa kielelezo hiki kingefuatwa.

Ujumbe wa wanafunzi hawa ulikuwa ule ule wa Yohana Mbatizaji na wa Kristo mwenyewe, kwamba: "Ufalme wa mbinguni umekaribia." Haikuwapasa kuingia katika mabishano na watu kwamba Yesu wa Nazareti ni Masihi au la; bali kwa jina lake wangefanya kazi zile zile za rehema alizokuwa amefanya. Aliwaagiza kwamba, "Pozeni wagonjwa, fufueni wafu, takaseni wenye ukoma, toeni pepo; mmepata bure, toeni bure."

Wakati wa huduma yake Yesu alitumia muda mwingi kuponya wagonjwa kuliko kuhubiri. Miujiza yake ilishuhudia ukweli wa maneno yake, kwamba hakuja kuangamiza bali kuokoa. Haki yake ilimtangulia, na utukufu wa Bwana ulikuwa nyuma yake. Kila alikokwenda, habari za wema wake zilimtangulia. Mahali alipokuwa amepita, wale waliopokea huruma zake walikuwa wakishangilia wakiwa na afya, na kufanya majaribio ya nguvu mpya waliyokuwa wamepata. Makutano walikuwa wakiwakusanyikia ili kusikia kutoka midomoni mwao kazi ambazo Bwana alikuwa amezifanya kwao. Sauti yake ilikuwa ya kwanza kwa wengi kupata kusikiwa, jina lake lilitajwa kwao kwa mara ya kwanza maishani mwao, uso wake ulikuwa haujapata kuonekana kwao. Kwa nini wasimpende Yesu, na kuimba sifa zake? Kadiri alivyopita katika miji na majiji alikuwa kama mkondo muhimu, uliokuwa ukieneza uzima na furaha kila mahali alikoenda.

Wafuasi wa Kristo wanapaswa kufanya kazi kama alivyofanya. Yatupasa tuwalishe wenye njaa, tuwavike walio uchi, na tuwafariji wanaoumwa na kuteseka. Tunapaswa kuwahudumia wanaopoteza tumaini, na kuleta matumaini mahali pasipokuwa na matumaini. Na kwetu pia ahadi hii itatimizwa, "Haki yako itakutangulia; utukufu wa Bwana utakufuata nyuma ukulinde." Isaya 58:8. Upendo wa Yesu, unaodhihirishwa katika huduma isiyo ya ubinafsi, utakuwa na ufanisi zaidi kumbadilisha mtenda maovu kuliko vile inavyowezekana kwa upanga

au mahakama. **(351)** Mambo hayo ni ya muhimu katika kuleta hofu tu kwa mvunja sheria, lakini umishonari wa upendo unaweza kufanya mengi zaidi ya hayo. Mara nyingi moyo utakuwa mgumu unapokemewa; lakini chini ya pendo la Yesu moyo utayeyuka. Mmishenari hawezi kutuliza magonjwa ya kimwili tu, bali anaweza kumwongoza mdhambi kwenda kwa Tabibu Mkuu, awezaye kutakasa moyo kutokana na ukoma wa dhambi. Kupitia watumishi wake, Mungu anapanga kwamba wagonjwa, wenye shida, wenye kupagawa na roho chafu, wataisikia sauti yake. Kupitia mawakala wake wa kibinadamu anatarajia awe Mfariji ambaye ulimwengu haujapata kumjua.

Katika safari yao hii ya kimeshonari ya kwanza wanafunzi wale walitakiwa kwenda tu kwa "kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli." Ikiwa wakati huu wangehubiri injili kwa Mataifa na Wasamaria, wangepoteza ushawishi wao kwa Wayahudi. Kwa kuchochea chuki za Mafarisayo wangekuwa wamejiingiza katika upinzani ambao ungewakatisha tamaa katika mwanzo huu wa kazi yao. Hata mitume walikuwa wazito kuelewa kwamba injili ingepelekwa kwa mataifa yote. Hawakuwa tayari kufanya kazi kwa Mataifa mpaka wakati ambapo wao wenyewe wangegundua ukweli huu. Ikiwa Wayahudi wangepokea injili, Mungu alikusudia kuwafanya kuwa wajumbe wake kwa Mataifa. Kwa hiyo walikuwa wawe wa kwanza kuusikia ujumbe.

Kila mahali pa kazi ya Kristo kulikuwa na watu walioamshwa na kuwekwa katika hali ya kuhitaji, kuwa na njaa na kiu kwa ajili ya ukweli. Wakati ulikuwa umefika wa kupelekea habari za upendo wake kwa mioyo hii yenye hamu. Wanafunzi wangeenda kwa wote hawa wakiwa kama wawakilishi wake. Vivyo hivyo waamini wangeongozwa kuwaangalia hawa kama walimu waliochaguliwa na mbingu, na wakati ambapo Mwokozi angechukuliwa kutoka kwao wasingeachwa pasipo waalimu.

Katika safari yao hii ya kwanza wanafunzi walitakiwa kwenda katika maeneo yale ambayo Yesu alikuwa ameenda kabla yao, ambako alikuwa amepata marafiki. Maandalizi yao kwa ajili ya safari hii yalipaswa kuwa mepesi mno. Hakuna ambacho kinapaswa kuruhusiwa kuhamisha mawazo yao kutoka katika kazi yao kuu, au kwa namna yoyote kikaamsha upinzani na kufunga mlango kwa ajili ya kazi zaidi. Hawakupaswa kutumia mavazi rasmi ya waalimu wa kidini, au kutumia mwonekano wa nje wa mavazi ambayo yangewatofautisha na watu wa hali ya chini. Hawakupaswa kwenda katika masinagogi na kuwaita watu kukusanyika kwa ajili ya ibada ya hadhara; jitihada zao zilipaswa zielekezwe kwenye kazi ya nyumba kwa nyumba. Hawakupaswa kupoteza muda katika kusalimiana isivyohitajika, au katika kwenda nyumba moja hadi nyingine kwa ajili ya kujifurahisha. Bali kila mahali walipaswa kupokea ukarimu wa wale waliostahili, wale ambao wangewapokea kwa moyo mkunjufu kama wampokeao Kristo mwenyewe. Walipaswa kuingia katika nyumba wakiwa na salamu nzuri isemayo, "Amani iwemo nyumbani humu." Luka 10:5. Nyumba hiyo ingebarikiwa kwa maombi yao, nyimbo **(352)** zao za sifa, na kuyafunua Maandiko kwa watu wa nyumba ile.

Wanafunzi hawa walikuwa wawe wapiga mbiu wenye ukweli, kutayarisha njia kwa ajili ya kuja kwa Bwana. Ujumbe ambao wangebeba ulikuwa ni neno la uzima wa milele, na hatima ya watu ilitegemea kama wangeupokea au kuukataa. Akiwahimiza kuhusu umuhimu wa ujumbe huo, Yesu aliwasisitiza wanafunzi wake kwamba, "Na mtu asipowakaribisha wala kuyasikiliza maneno yenu, mtokapo katika nyumba ile, au mji ule, kung'uteni mavumbi ya miguuni mwenu. Amin, nawaambia, itakuwa rahisi nchi ya Sodoma na Gomora kustahimili adhabu ya siku ya hukumu, kuliko mji ule."

Sasa macho yake Mwokozi yalipenya hadi wakati wa mbele; aliona uwanja mkubwa ambamo wanafunzi wake wanapaswa kuwa mashahidi wake baada ya Yeye kufa. Maono yake ya kinabii yanahusisha uzoefu wa watumishi wake katika zama zote hadi ajapo mara ya pili. Anawaonyesha wafuasi wake upinzani watakaokutana nao; anafunua tabia na mpango wa vita hiyo. Anawawekea wazi hatari ambazo ni lazima wakutane nazo, kujikana ambako kutahitajika. Anatamani wahesabu gharama, ili wasije wakachukuliwa na adui bila kujua. Vita yao haipaswi kuwa ya nyama na damu, bali "juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho." Efeso 6:12. Lazima wapambane na nguvu za hali ya juu kupita za kibinadamu, lakini wamehakikishiwa msaada wa hali ya juu zaidi kuliko wa kibinadamu. Ufahamu wote wa mbinguni uko katika jeshi hili. Kilichopo katika safu za vikosi vya jeshi hili ni zaidi ya malaika. Roho Mtakatifu, mwakilishi wa Jemadari wa jeshi la Bwana, anashuka kuja kuongoza vita. Udhaifu wetu unaweza kuwa mwingi; dhambi na makosa yetu vyaweza kuwa vizito; lakini neema ya Mungu ni kwa wote waitafutao kwa toba. Uwezo wa Mweza wa yote umetolewa kwa ajili ya wote wamtumainio Mungu.

**(353)** "Angalieni," alisema Yesu, "mimi nawatuma kama kondoo kati ya mbwa-mwitu; basi iweni na busara kama nyoka, na kuwa watu wapole kama hua." Kristo mwenyewe hakuondosha neno lolote la ukweli, bali alilinena kwa upendo. Katika kujihusisha na watu alizingatia hekima kwa kiasi kikubwa mno. Hakuwa na harara kamwe, kamwe hakunena neno kali isivyohitajika, kamwe hakusababisha maumivu ya nafsi yasiyo ya lazima. Hakupuuza udhaifu wa mwanadamu. Pasipo woga alikosoa unafiki, kutokuamini, na uovu, lakini machozi yalikuwa katika sauti yake wakati alipotamka maneno makubwa ya kukemea. Aliulilia Yerusalemu, mji alioupenda, ambao ulikataa kumpokea, Yeye aliye Njia, Kweli, na Uzima. Walimkataa, Mwokozi, lakini aliwachukulia kwa huruma, na huzuni ya kina kiasi cha kuuvunja moyo wake. Kila mtu alikuwa wa thamani machoni pake. Ingawa alijionyesha kuwa na hadhi ya kimbingu, aliinama kwa huruma yenye kumjali kila mshirika wa familia ya Mungu. Aliwaona watu wote kama nafsi zilizoanguka ambazo lengo la utume wake ilikuwa ni kuziokoa.

Watumishi wa Kristo hawapaswi kutenda matakwa ya moyo wa asili. Wanahitaji kuwa karibu sana na Mungu, la sivyo, kujitumainia nafsi kutainuka, halafu watatiririsha maneno yasiyofaa ambayo si kama umande au manyunyu ya mvua yanayohuisha mmea ulio katika hali ya kukauka. Hiki ndicho ambacho Shetani anataka wafanye; maana hizo ndizo njia zake. Yule joka ndiye mwenye ghadhabu; kinachodhihirika katika hasira na malaumu ni roho ya Shetani. Bali watumishi wa Mungu wanapaswa kuwa wawakilishi wake. Anawataka wajishughulishe na mambo ya mbinguni, yaani, ukweli ule udhihirishao sura na tabia ya Mungu. Nguvu ya kuwashindisha maovu ni uweza wa Kristo. Utukufu wa Kristo ndiyo nguvu yao. Wanapaswa wayakaze macho yao wakiyaelekeza katika upendo wake. Hapo ndipo watakapoiwasilisha injili kwa hekima na upole wa kimbingu. Na roho ambayo inadumu kuwa ya upole katikati ya mazingira yenye hasira itautamka ukweli kwa ufasaha zaidi kuliko vile hoja nyingine yoyote inavyoweza, hata iwe hoja ya nguvu kiasi gani.

Wale wanaofikishwa katika hali ya kupingana na adui wa ukweli hawakabiliani tu na wanadamu, bali pia lazima wakabiliane na Shetani mwenyewe na mawakala wake. Hebu na wakumbuke maneno ya Mwokozi kwamba, "Angalieni, nawatuma kama wanakondoo kati ya mbwa-mwitu." Luka 10:3. Hebu na wakae katika pendo la Mungu, na roho yao itadumu katika kutulizwa, hata katika hali ya kutendewa mabaya. Bwana atawavisha deraya za kimbingu. Roho Mtakatifu wake atahimiza akili na moyo, kiasi kwamba sauti zao hazitatishwa na kule kubweka kwa mbwa-mwitu.

**(354)** Akiendelea na mafundisho yake kwa wanafunzi wake, Yesu alisema, "Jihadharini na wanadamu." Hawakupaswa kuwaamini watu ambao walikuwa hawamjui Mungu, wala hawakupaswa kutegemea mashauri yao; maana hili lingewapa faida mawakala wa Shetani. Mabunifu ya mwanadamu mara nyingi yanapinga mipango ya Mungu. Wale wanaojenga hekalu la Bwana wanapaswa walijenge kwa mfano ule ulioonyeshwa mlimani, - mfano wa mbinguni. Pindi watumishi wake wanapotegemea mashauri ya wanadamu wasiokuwa katika uongozi wa Roho Mtakatifu, Mungu haheshimiwi na injili inasalitiwa. Hekima ya ulimwengu ni ujinga kwa Mungu. Wale wanaoitegemea hakika wataangukia katika makosa.

"Watawapeleka mabarazani, . . . nanyi mtachukuliwa mbele ya maliwali na wafalme kwa ajili yangu, kuwa ushuhuda kwao na kwa mataifa." Mathayo 10:17, 18. Mateso yataieneza nuru. Watumishi wa Kristo wataletwa mbele ya wakuu wa ulimwengu huu, ambao, kama isingekuwa kwa njia hii, wakuu hao wasingeisikia injili kamwe. Ukweli umeonyeshwa isivyo sahihi kwa watu hawa. Wamesikiliza mashtaka ya uongo kuhusu imani ya wanafunzi wa Yesu. Mara nyingi njia pekee ya wao kujifunza uhalisia wa imani hiyo ni hawa wanaoletwa mbele yao kuhojiwa kwa ajili ya imani hiyo. Katika kuhojiwa, hawa wanatakiwa kujibu, na mahakimu wao wanatakiwa kusikiliza ushahidi unaotolewa. Neema ya Mungu itatolewa kwa watumishi wake ili kukidhi hali inayotakiwa. Yesu anasema, "Mtapewa saa ile mtakayosema. Kwa kuwa si ninyi msemao, bali ni Roho wa Baba yenu asemaye ndani yenu." Kadiri Roho wa Mungu anavyoangaza katika mawazo ya watumishi wake, ukweli utatolewa katika uweza wake wa kimbingu na thamani yake ya kimbingu. Wale wanaoukataa ukweli watasimama wakiwashtaki na kuwakandamiza wanafunzi. Lakini katika hali ya kukubali hasara na mateso, na hata kifo, watoto wa Mungu watadhihirisha unyenyekevu ule wa Yule aliye Kielelezo. Hapo ndipo itakapoonekana tofauti kati ya mawakala wa Shetani na wawakilishi wa Kristo. Mwokozi atainuliwa juu mbele ya wakuu wa watu.

Wanafunzi wale hawakujaliwa ujasiri wa kufia dini mpaka wakati ambapo neema hiyo ilikuwa inahitajika. Hapo ndipo ahadi hiyo ya Mwokozi ilipotimizwa. Petro na Yohana walitoa ushuhuda mbele ya baraza la Sanhedrin,

watu "wakastaajabu, wakawatambua ya kwamba walikuwa pamoja na Yesu." Matendo 4:13. Kuhusu Stefano imeandikwa kwamba, "Watu wote walioketi katika ile baraza wakamkazia macho yao, wakamwona uso wake kuwa kama uso wa malaika." Watu "hawakuweza kushindana na hiyo hekima na huyo Roho aliyesema naye." Matendo 6:15, 10. Na Paulo, akiandika kuhusu kushtakiwa kwake katika mahakama ya Kaisari, anasema, "Katika jawabu langu la kwanza hakuna mtu aliyesimama **(355)** upande wangu, bali wote waliniacha. . . . Lakini Bwana alisimama pamoja nami akanitia nguvu, ili kwa kazi yangu ule ujumbe utangazwe kwa utimilifu, hata wasikie Mataifa yote; nami nikaokolewa katika kinywa cha simba." 2 Timotheo 4:16, 17.

Watumishi wa Mungu hawakupaswa kuandaa hotuba iliyowekwa tayari pindi waletwapo katika mashtaka. Maandalizi yao yalipaswa kufanywa siku kwa siku kwa kujiwekea hazina ya ukweli wa thamani wa neno la Mungu, na kuimarisha imani yao kwa njia ya maombi. Wakati walipoletwa katika mashtaka, Roho Mtakatifu angewaletea hali ya kukumbuka ukweli ule uliohitajika kwa wakati huo.

Jitihada ya dhati ya kila siku ya kutaka kumjua Mungu, na Yesu Kristo aliyemtuma, ingeleta nguvu na ufanisi kwa mtu. Maarifa ambayo yangepatikana kwa kuyachunguza Maandiko kwa dhati yangemlikwa katika kumbukumbu kwa wakati husika. Lakini watu wale waliopuuza kupata kuyafahamu maneno ya Kristo, ambao hawakupata kuijaribu kwa njia ya mateso nguvu ya neema yake, wasingetarajia Roho Mtakatifu kuwaletea maneno ya Kristo katika kumbukumbu zao. Walipaswa wamtumikie Mungu kila siku pasipokuwa na moyo uliogawanyika, na hapo ndipo wangemtumainia Yeye.

Uadui dhidi ya injili ulionyeshwa kuwa ungekuwa mkali sana kiasi kwamba hata mafungamano ya mahusiano ya undugu wa duniani yasingezingatiwa. Wanafunzi wa Yesu wangesalitiwa na watu wa nyumbani mwao ili wauawe. "Mtakuwa mkichukiwa na watu wote kwa ajili ya jina langu," ndivyo Yesu alivyoongezea; "lakini mwenye kusaburi hata mwisho, ndiye atakayeokoka." Marko 13:13. Lakini aliwataka wasijielekeze matesoni pasipo ulazima huo. Yeye mwenyewe aliacha kazi yake katika eneo moja na kukimbilia katika eneo jingine, akiwakimbia watu waliokuwa wanayatafuta maisha yake. Wakati alipokataliwa Nazareti, na watu wa mjini kwake walipotaka kumwua, alishuka kwenda Kapernaumu, na kule watu wakashangazwa kwa mafundisho yake; "kwa kuwa neno lake lilikuwa na uweza." Luka 4:32. Vivyo hivyo pia watumishi wake hawakutakiwa kukatishwa tamaa na mateso, bali watafute mahali pengine ambako wangeendelea kufanya kazi kwa ajili ya wokovu wa watu.

Mtumwa si mkuu kuliko bwana wake. Mfalme wa mbinguni aliitwa Beelzebuli, hata wanafunzi wake watasemwa vibaya kwa namna ile ile. Lakini hata kuwe na hatari gani, wafuasi wa Kristo watashikilia usahihi wa imani yao. Lazima wapuuze kujificha. Hawawezi kubaki katika hali ya kutojitoa mpaka watakapohakikishiwa kwamba wamepata usalama katika kuukiri ukweli. Wamewekwa kama walinzi, kuonya watu kuhusu hatari ya kuangamia kwao. Lazima ukweli uliopokelewa kutoka kwa Yesu utolewe kwa wote, bure na kwa uwazi. Yesu alisema, "Niwaambialo ninyi katika giza, lisemeni katika nuru; na msikialo kwa siri, lihubirini juu ya nyumba."

**(356)** Kamwe Yesu mwenyewe hakutafuta amani kwa maafikiano ya kulegeza msimamo. Moyo wake ulifurikishwa na pendo kwa wanadamu wote, lakini kamwe hakuendekeza dhambi zao. Alikuwa rafiki yao sana kiasi kwamba asingeendelea kunyamaza kimya wakati walipokuwa katika njia iongozayo kwenda katika uangamivu wa roho zao, - roho zile alizokuwa amenunua kwa damu yake. Alifanya kazi ili kwamba mwanadamu abaki kuwa mkweli kwake mwenyewe, mtu wa kweli kwa mambo yake ya juu na ya milele. Watumishi wa Kristo wanaitwa kwa ajili ya kazi kama hiyo, na wangepaswa kuwa macho wasije wakasalimu amri kuuacha ukweli kwa kutaka kuepusha hali ya kutofautiana na wengine. Yawapasa wafuate "mambo ya amani" (Warumi 14:19); lakini amani halisi haiwezi kupatikana kwa kufanya maafikiano ya kulegeza ukweli. Na hakuna mtu yeyote anayeweza kuwa katika kanuni ya ukweli halafu asiamshe hali ya upinzani. Ukristo ulio wa kiroho utapingwa na watoto wasio watiifu. Lakini Yesu aliwasisitizia wanafunzi wake akisema, "Msiwaogope wauuao mwili, wasiweze kuiua na roho." Wale walio wa kweli mbele za Mungu hawapaswi kuogopa nguvu za wanadamu wala uadui wa Shetani kwao. Uzima wao wa milele uko salama katika Kristo. Hofu yao pekee iwe kwamba wasisalimu amri kwa kuushusha chini ukweli, na kwa njia hiyo wakaisaliti heshima ambayo Mungu amewapa kwa kuwaamini.

Kazi ya Shetani ni kujaza mashaka katika mioyo ya wanadamu. Anawaongoza kumchukulia Mungu kama hakimu mkali. Anawajaribu na kuwafanya watende dhambi, halafu wajione kwamba ni wachafu kiasi kwamba hawastahili kumkaribia Baba yao wa mbinguni au kushawishi huruma yake kwao. Bwana anajua haya yote. Yesu

anawapa wanafunzi wake uhakika wa huruma ya Mungu kwa ajili yao wawapo katika uhitaji au katika udhaifu. Hakuna kuhema kokote kunakoashiria maumivu, maumivu yoyote yanayosikiwa, au majonzi yanayoupenya moyo, bila kuwepo kwa mtetemo unaogonga katika moyo wa Baba kuashiria hayo.

Biblia inatuonyesha Mungu aliye katika mahali pake pa juu na patakatifu, akiwa hayuko katika hali ya kutulia tu bila kazi, akiwa hayuko kimya tu na katika faragha, bali akizungukwa na elfu kumi mara elfu kumi ya malaika zake wenye maarifa, wote wakisubiri kufanya mapenzi yake. Kupitia njia ambazo hatuwezi kuzielewa yuko kazini akiwasiliana na kila sehemu ya himaya yake. Lakini hamu ya kusudi lake na ya mbingu yote imejikita katika doa hili la ulimwengu huu, katika roho hizi, kiasi kwamba alimtoa Mwana wake wa pekee ili aliokoe. Mungu anainama kutoka kwenye kiti chake cha enzi ili kusikia kilio cha wale wanaoonewa. Kwa kila ombi la dhati anajibu akisema, "Mimi hapa." Anawainua wao waliochoshwa na kunyanyaswa. Anateseka katika mateso yetu yote. Katika kila jaribu na maonjo malaika wake wako karibu ili kuokoa.

Hata shomoro haanguki chini bila Mungu kujua. Chuki ya Shetani kwa Mungu inamfanya achukie kila kitu kinachohitaji utunzaji wa Kristo. Anatafuta kuharibu kila kazi ya mikono ya Mungu, na anafurahia kuharibu **(357)** hata viumbe vya hali ya chini. Ni kwa ulinzi na utunzaji wa Mungu tu kwamba hata ndege wanahifadhiwa ili kutufurahisha kwa nyimbo zao za furaha. Lakini hawasahau hata mashomoro. "Msiogope basi; bora ninyi kuliko mashomoro wengi."

Yesu aliendelea kwa kusema hivi: Mkinikiri mimi mbele za watu, nami nitawakiri ninyi mbele za Mungu na malaika zake. Mnapaswa mwe mashahidi wangu duniani, mifereji ambayo kupitia kwa hiyo neema yangu inaweza kutiririka kwa ajili ya kuuponya ulimwengu. Nami nitakuwa mwakilishi wenu mbinguni. Baba haoni kwenu tabia zenu zenye mapungufu, bali anawaona mkiwa mmevishwa katika ukamilifu wangu. Mimi ndimi njia ambayo kupitia hiyo mibaraka ya mbinguni itakuja kwenu. Na kila mmoja anayenikiri kwa kushiriki kafara yangu kwa ajili ya waliopotea nami nitamkiri kama mshirika katika utukufu na furaha ya waliokombolewa.

Yeye ambaye angemkiri Kristo lazima Kristo awe anakaa ndani yake. Mtu hawezi kusema kile ambacho hajapokea. Huenda wanafunzi wangeweza kuongea kwa ufasaha maneno ya mafundisho ya kiroho, wangeweza kuyakariri maneno ya Kristo kama yalivyo; lakini pasipo upole na upendo kama wa Yesu, wangekuwa hawako katika kumkiri. Roho ambayo ni kinyume cha roho ya Kristo ingemkana, hata kama inajitangaza kwamba inamkiri. Watu wanaweza kumkana Kristo kwa kuzungumza mambo maovu, kuzungumza upumbavu, maneno yasiyo ya kweli au yasiyo na huruma. Wanaweza kumkana kwa kukwepa kubeba mizigo ya maisha, kujielekeza katika anasa za dhambi. Wanaweza kumkana kwa kufuata matakwa ya ulimwengu, tabia isiyo ya upole, kupenda maoni yao wenyewe, kujihesabia haki wenyewe, kuendekeza mashaka, kuleta shida, na kukaa gizani. Kwa njia zote hizi wanatangaza kwamba Kristo hayuko ndani yao. Na alisema, "Mtu yeyote atakayenikana mbele ya watu, nami nitamkana mbele za Baba yangu aliye mbinguni."

Mwokozi aliwataka wanafunzi wake kutotarajia kwamba uadui wa ulimwengu kwa injili ungeshindwa, na ya kwamba baada ya muda upinzani ungekoma. Alisema, "Sikuja kuleta amani, bali upanga." Hali hii ya vurugu si matokeo ya injili, bali matokeo ya upinzani kwa injili. Mateso ambayo ni magumu kukabili kuliko yote ni tofauti zilizo miongoni mwa watu wa jamaa moja, kukoma kwa urafiki wa marafiki wapendanao kuliko wote duniani. Lakini Yesu alisema, "Apendaye baba au mama kuliko mimi, hanistahili; wala apendaye mwana au binti kuliko mimi, hanistahili. Wala mtu asiyechukua msalaba wake akanifuata, hanistahili."

Utume wa watumishi wa Kristo ni heshima ya juu, hali ya kuaminiwa yenye utakatifu. Yesu alisema, "Awapokeaye ninyi, anipokea mimi; naye anipokeaye **(358)** mimi, ampokea yeye aliyenituma." Hakuna tendo la huruma linaloonyeshwa nao kwa jina lake ambalo halitatambuliwa na kupatiwa thawabu. Na katika kutambua huko kwa dhati anajumuisha wale walio dhaifu zaidi na wa hali ya chini zaidi katika familia ya Mungu: "Na mtu awayeyote atakayemnywesha mmojawapo wa wadogo hawa" – wale ambao wako kama watoto katika imani yao na katika kumjua kwao Kristo - "ngaa kikombe cha maji ya baridi kwa kuwa ni mwanafunzi, amin, nawaambia, haitampotea kamwe thawabu yake."

Hivyo ndivyo Kristo alivyomaliza mafundisho yake. Wale thenashara waliochaguliwa wakaenda, kama alivyokuwa ameenda, "kuwahubiri maskini habari njema . . . . kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao, na

vipofu kupata kuona tena, kuwaacha huru waliosetwa. Na kutangaza mwaka wa Bwana uliokubaliwa." Luka 4:18, 19.

## Sura ya 38

# Njoni Mkapumzike Kidogo

[Sura hii imejengwa katika Mathayo 14:1, 2, 12, 13; Marko 6:30-32; Luka 9:7-10.]

Waliporudi kutoka katika safari yao ya kimishonari, "mitume wakakusanyika mbele ya Yesu; wakampa habari za mambo yote waliyoyafanya, na mambo yote waliyoyafundisha. Akawaambia, Njoni ninyi peke yenu kwa faragha, mahali pasipokuwa na watu, mkapumzike kidogo. Kwa sababu walikuwako watu wengi, wakija, wakienda, hata haikuwapo nafasi ya kula."

Wanafunzi wale walikuja kwa Yesu wakamwambia mambo yote. Uhusiano wao wa upendo wa karibu pamoja naye uliwatia moyo kumweleza uzoefu wao wa mazuri na mabaya waliyokutana nayo, furaha yao ya kuona matokeo ya kazi yao, na huzuni ya mambo waliyoshindwa, mapungufu yao, na madhaifu yao. Walikuwa wamefanya makosa katika kazi yao hii ya kwanza kama wainjilisti, na pindi walipomsimulia Kristo ukweli wa mambo kuhusu uzoefu waliopitia, aliona kwamba bado wanahitaji mafundisho zaidi. Pia, aliona kwamba walikuwa wamechoka katika kazi zao, na ya kwamba walihitaji kupumzika.

Lakini mahali hapa walipokuwa hawakuweza kupata faragha iliyohitajika; "Kwa sababu walikuwako watu wengi, wakija, wakienda, hata haikuwapo nafasi ya kula." Watu walikuwa wakija kwa Kristo, wakitaka kuponywa, na wakiwa na hamu ya kusikiliza maneno yake. Wengi walihisi kuvutwa kwenda kwake; maana alionekana kwao kama chemchemi ya baraka zote. Wengi wa wale waliokusanyika kwa Kristo ili kupata zawadi ya afya walimpokea kama Mwokozi wao. Wengi wengine, wakiogopa kumkiri, kwa sababu ya Mafarisayo, waliongoka wakati wa kushuka **(360)** kwa Roho Mtakatifu, nao, wakiwa mbele ya makuhani na wakuu wenye hasira, walimkiri Kristo kama Mwana wa Mungu.

Lakini sasa Yesu alitaka kupumzika, ili ya kwamba awe na wanafunzi wake; maana alikuwa na mengi ya kuwaambia. Katika kazi yao walikuwa wamepita katika jaribio la shida, na walikuwa wamekabiliwa na upinzani wa aina mbalimbali. Mahali hapa walikuwa wamemwuliza Kristo kuhusu kila kitu; lakini kwa muda fulani walikuwa wamekuwa peke yao, na nyakati fulani walikuwa wamesumbuka sana wakishindwa kujua la kufanya. Walikuwa wamepata ujasiri mwingi katika kazi yao; maana Yesu hakuwatuma pasipo Roho wake, na kwa imani kwake Kristo walifanya miujiza mingi; lakini walitaka sasa wapate kula Mkate wa Uzima. Walihitaji kwenda mahali pa kupumzikia, ambapo wangejumuika na Yesu na kupata maelekezo kwa ajili ya kazi yao wakati ujao.

"Akawaambia, Njoni ninyi peke yenu kwa faragha, mahali pasipokuwa na watu, mkapumzike kidogo." Kristo amejawa huruma na upendo kwa wote walio katika kazi yake. Aliweza kuwaonyesha wanafunzi wake kwamba Mungu hahitaji kafara, bali huruma. Walikuwa wameweka nafsi zao zote katika kazi kwa ajili ya watu, na hili lilikuwa likitafuna nguvu zao za mwili na za akili. Ulikuwa muda wao wa kupumzika.

Kwa vile wanafunzi wale walikuwa wameona mafanikio ya kazi zao, walikuwa katika hatari ya kujitwalia sifa, hatari ya kuendeleza kiburi cha kiroho, na hivyo kuanguka katika majaribu ya Shetani. Kazi kubwa ilikuwa mbele yao, na kwanza kabisa lazima wajifunze kwamba nguvu zao hazikuwa ndani yao wenyewe, bali katika Mungu. Kama vile Musa katika jangwa la Sinai, kama Daudi katika vilima vya kule Yudea, au Eliya kando ya kijito cha Kerithi, wanafunzi hawa walipaswa kuondokana na mazingira ya jitihada za kufanya kazi, ili wajumuike na Kristo, wajumuike na maumbile ya asili, na wajumuike na mioyo yao wenyewe.

Wakati ambapo wanafunzi hawakuwepo wakiwa wameenda katika safari ya umishonari, Yesu alikuwa ametembelea miji mingine na vijiji, akihubiri injili ya ufalme. Ilikuwa ni wakati huu huu alipopata habari za kifo cha Yohana Mbatizaji. Tukio hili lilimletea kwa uwazi picha ya mahali ambapo pangekuwa mwisho wa hatua za miguu yake Yeye mwenyewe. Vivuli vilikuwa vinakusanyika vikiwa vizito katika njia yake. Makuhani na marabi walikuwa wakitazama kukipata kifo chake, wapelelezi wakiwa wamewekwa katika hatua zake, na mipango ya njama za kumwangamiza ikizidishwa katika kila upande wa mikono yake. Habari za mahubiri ya mitume katika Galilaya yote zilimfikia Herode, akivuta hisia zake kuhusu Yesu na kazi zake. Akasema, "Huyo ndiye Yohana Mbatizaji; amefufuka katika wafu;" na akaonyesha hamu ya kumwona Yesu. Herode alikuwa na hofu wakati wote kwamba mapinduzi yasije yakatokea kwa siri, kwa kusudi la kumwondoa kwenye kiti cha enzi, na kulivunja

kongwa la Kirumi kwa kuliondoa kwa taifa la Kiyahudi. Roho ya upinzani na kutoridhika **(361)** ilikuwa kubwa miongoni mwa watu. Ilikuwa wazi kwamba kazi ya Kristo ya hadharani isingeendelea kwa muda mrefu kule Galilaya. Matukio ya mateso yake yalikuwa yanakaribia, na alitafuta kuwa mbali na michanganyo ya makutano kwa muda.

Kwa mioyo ya huzuni wanafunzi wa Yohana walikuwa wameuchukua mwili wake uliochinjwa kwenda kuuzika. Halafu "wakaenda wakampasha Yesu habari." Kabla, wanafunzi hawa walikuwa wamekuwa na wivu kwa Yesu wakati alipoonekana kuwavuta watu mbali na Yohana. Walikuwa wameshirikiana na Mafarisayo kumshtaki Yesu wakati alipokaa na watoza ushuru katika karamu ya Mathayo. Walikuwa wamekuwa na mashaka kuhusu kazi yake ya kimbingu kwa sababu hakumweka huru Yohana Mbatizaji. Lakini sasa kwa kuwa mwalimu wao alikuwa amekufa, na kwamba walihitaji kufarijiwa katika majonzi yao haya makubwa, na kuhitaji maelekezo kwa kazi yao ya siku zilizokuwa usoni, walikuja kwa Yesu, na wakaunganisha matarajio yao na yake. Hata wao pia walihitaji muda wa kutulia na kujumuika na Mwokozi.

Jirani tu na Bethsaida, upande wa kaskazini wa mwisho wa ziwa, kulikuwa na eneo la faragha, sasa likiwa la kupendeza lenye majani mabichi ya majira ya kuchipua, ambalo lilimvutia Yesu na wanafunzi wake kuja hapo. Waliondoka kwenda mahali hapo, wakivuka kwa mashua. Hapa wangekuwa mbali na mahali panapopitwa na watu wengi wanaosafiri, tena ni mbali na shughuli na harakati za mjini. Madhari ya asili ilikuwa yenyewe tu ni pumziko, badiliko linalofurahisha hisia. Hapa ndipo ambapo wangesikilizia maneno ya Kristo bila sauti za kuingilia, miitikio mikali na mashutumu ya hasira kutoka kwa waandishi na Mafarisayo. Hapa wangefurahia mjumuiko mzuri pamoja na Bwana wao kwa muda mfupi.

Pumziko ambalo lilifanywa na Yesu na wanafunzi wake halikuwa pumziko la kujifurahisha nafsi. Muda waliotumia katika pumziko hili haukutumika kujipatia anasa. Waliongea kwa pamoja kuhusu kazi ya Mungu, na uwezekano wa kuleta ufanisi mkubwa zaidi katika kazi. Wanafunzi wale walikuwa wamekuwa na Kristo, na wangeweza kumwelewa; kwao hahitaji kunena kwa mifano. Alisahihisha makosa yao, na akawawekea wazi njia sahihi ya kuwaendea watu. Aliwafunulia kwa ukamilifu zaidi hazina za thamani za ukweli wa kimbingu. Walihimizwa na nguvu ya kimbingu, na wakajazwa tumaini na ujasiri.

Ingawa Yesu angeweza kutenda miujiza, na alikuwa amewawezesha wanafunzi wake kufanya miujiza, aliwaelekeza wanafunzi wake waliochoka kwenda katika nchi isiyo na watu wengi kupumzika. Wakati aliposema kwamba mavuno ni mengi, na watenda kazi ni wachache, hakuwataka wanafunzi kulazimika kufanya kazi muda wote, bali alisema, "Basi mwombeni Bwana wa mavuno, apeleke watenda kazi katika mavuno yake." Mathayo 9:38. Mungu **(362)** amemchagulia kila mtu kazi yake, kulingana na uwezo wake (Waefeso 4:11-13), na asingependa kuona watu wachache wakibebelea majukumu mazito huku wengine hawana mzigo wowote, hakuna kazi nzito kwa mtu.

Maneno yale ya Kristo ya huruma yanasemwa kwa watenda kazi wake leo kwa uhakika kama ule ule yaliposemwa kwa wanafunzi wake. "Njoni ninyi peke yenu kwa faragha, . . . mkapumzike kidogo," ndivyo anavyowaambia waliochoka na kudhoofu. Si jambo la busara kuwa katika mahangaiko na pilikapilika ya kazi, hata kama ni kazi ya kushughulikia mahitaji ya kiroho ya watu; maana kwa njia hii huruma kwa mtu inakuwa imepuuzwa, na uwezo wa akili na roho na mwili vinatwishwa mzigo mkubwa zaidi ya uwezo wake. Kujikana nafsi kunatakiwa kwa wanafunzi wa Kristo, na kafara lazima zifanywe; lakini lazima pia kuwe na uangalifu ili kwamba kupitia juhudi zinazopita kiasi Shetani asipate nafasi kwa kupitia udhaifu wa mwanadamu, na kazi ya Mungu ikaharibiwa.

Katika makadirio ya marabi maisha ya dini ni kuwa katika hali ya kukurukakara za kazi muda wote. Walitegemea katika matendo ya kuonekana nje ili kuonyesha hali yao ya juu ya utauwa. Kwa njia hiyo walizitenga nafsi zao mbali na Mungu, na wakajijengea mahali pao wenyewe katika kujitosheleza wenyewe. Hatari zile zile bado zipo. Kadiri shughuli zinavyoongezeka na watu kufanikiwa katika kazi yoyote kwa ajili ya Mungu, kuna hatari ya kutumainia mipango ya wanadamu na njia zao. Kuna mazoea ya kuomba kidogo zaidi, na kuwa na imani pungufu zaidi. Kama walivyokuwa wanafunzi wale, tuko katika hatari ya kupoteza hali ya kuona utegemezi wetu kwa Mungu, na kutafuta kuzifanya kazi zetu kuwa mwokozi wetu. Tunahitaji kumwangalia Yesu wakati wote, tukifahamu kwamba kinachofanya kazi ni nguvu zake. Wakati tunatakiwa kufanya kazi kwa bidii kwa ajili ya wokovu wa wale waliopotea, lazima pia tutumie muda kuwa na Mungu, kwa maombi, na kwa kujifunza neno

lake. Ni kazi ile tu itakayofanywa kwa maombi, na kutakaswa na wema wa Kristo, ambayo hatimaye itathibitika kuwa na ufanisi kwa ajili ya mema.

Hakuna maisha mengine yaliyokuwa yamesongwa sana na kazi na majukumu kama yalivyokuwa maisha Yesu; lakini ni mara ngapi alipoonekana akiwa katika kuomba! Ni jinsi gani alivyojumuika na Mungu wakati wote! Tena na tena maisha yake ya duniani hapa yamesemwa na maandiko kama haya: "Hata alfajiri na mapema sana akaondoka, akatoka akaenda zake mahali pasipokuwa na watu, akaomba huko." "Wakakutanika makutano mengi wamsikilize na kuponywa magonjwa yao. Lakini yeye alikuwa akijiepua, akaenda mahali pasipokuwa na watu, akaomba." "Ikawa siku zile aliondoka akaenda mlimani ili kuomba, akakesha usiku kucha katika kumwomba Mungu." Marko 1:35; Luka 5:15, 16; 6:12.

Akiwa katika maisha ya kujitoa kwa ajili ya mema ya watu wengine, Mwokozi aliona **(363)** ulazima wa kujiondoa mahali penye misafara ya watu wengi na kutoka kwa makutano waliokuwa wakimfuata siku kwa siku. Lazima ageuke na kuacha maisha ya kazi zisizokoma na hali ya kukutana na mahitaji ya watu muda wote, na kwenda kutafuta mahali pa kupumzikia na kuwa karibu na Baba yake. Akiwa kama yeye aliye pamoja nasi, yeye ashirikiye mahitaji yetu na udhaifu wetu, alimtegemea Mungu kabisa, na akiwa mahali palipojificha pa maombi alizitafuta nguvu za mbinguni, ili kwamba aondoke akiwa ameimarishwa kwa kazi na kwa majaribu. Akiwa katika ulimwengu huu wa dhambi Yesu alistahimili mapambano na mateso ya moyo. Akiwa katika kujumuika pamoja na Mungu aliweza kutua mzigo wa huzuni uliokuwa juu yake. Hapa ndipo alipoipata faraja na furaha.

Katika Kristo kilio cha mwanadamu kilimfikia Baba wa huruma isiyo na mwisho. Akiwa mwanadamu alipeleka sala kwenye kiti cha enzi cha Mungu mpaka ubinadamu wake ulipopata chaji ya mkondo wa nguvu za kimbingu ambao unauunganisha ubinadamu kwa uungu. Kupitia kujumuika pamoja na Mungu Yesu alipata uzima kutoka kwa Mungu, ili ya kwamba aupatie ulimwengu uzima. Uzoefu wake unapaswa kuwa wetu.

"Njoni ninyi peke yenu kwa faragha," ndivyo anavyotuhimiza. Ikiwa tungesikia neno lake hilo, tutapata nguvu zaidi na kutumika zaidi. Wanafunzi walimtafuta Yesu, na wakamweleza mambo yote, naye akawatia moyo na kuwafundisha. Ikiwa sisi leo tungetumia muda kwenda kwa Yesu na kumwambia mahitaji yetu, tusingefadhaika; angekuwa katika mkono wetu wa kuume ili kutusaidia. Tunahitaji kuwa na urahisi zaidi, imani zaidi na ujasiri katika Mwokozi wetu. Yeye ambaye jina lake anaitwa "Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele, Mfalme wa amani;" Yeye ambaye kumhusu yeye imeandikwa kwamba, "Uweza wa kifalme utakuwa begani mwake," ni Mshauri wa Ajabu. Tunashauriwa kumwomba atupatie hekima. Anawapa "wote, kwa ukarimu, wala hakemei." Isaya 9:6; Yakobo 1:5.

Ndani ya wote walio katika mafunzo ya Mungu kunatakiwa kudhihirishwa maisha ambayo hayapatani na ulimwengu, desturi za ulimwengu, wala matendo ya ulimwengu; na kila mmoja anahitaji kupata uzoefu binafsi wa kupata kuyajua mapenzi ya Mungu. Lazima kila mmoja wetu sote tumsikie Mungu akinena moyoni. Wakati sauti nyingine zote zinapovuma, sisi tukiwa katika ukimya tunamsubiri, ukimya wa moyo unaifanya sauti ya Mungu ibainike kwetu. Anatuhimiza akisema, "Acheni, mjue ya kuwa Mimi ni Mungu." Zaburi 46:10. Hapa tu ndipo pa kupata pumziko la kweli. Na haya ndiyo maandalizi kwa ajili ya wote wanaotaka kufanya kazi kwa ajili ya Mungu. Katikati ya mvumo wa watu wengi, na masumbuko ya shughuli za maisha, nafsi inayoburudishwa hivyo inazungukwa na mazingira ya nuru na amani. Maisha yatatoa manukato ya kunukia, na yatadhihirisha nguvu ya kimbingu itakayoifikia mioyo ya watu.

## Sura ya 39

# "Wapeni Ninyi Chakula"

[Sura hii imejengwa katika Mathayo 14:13-21; Marko 6:32-44; Luka 9:10-17; Yohana 6:1-13.]

Kristo alikuwa amepumzika mahali pa faragha akiwa na wanafunzi wake, lakini wasaa huu adimu wa utulivu ulivunjika baada ya muda mfupi. Wanafunzi walifikiri kwamba walikuwa wamepumzika mahali ambapo wasingebughudhiwa; kumbe muda mfupi tu baada ya makutano kumkosa Mwalimu wa kimbingu, waliulizia, "Yuko wapi huyo?" Baadhi miongoni mwao walikuwa wameona uelekeo ambako Yesu na wanafunzi wake walikuwa wameelekea. Wengi walitembea kwa njia ya nchi kavu kuwaendea, wakati wengine walifuata kwa mashua kupitia majini. Pasaka ilikuwa imekaribia, na, kutoka mbali na karibu, makundi ya wasafiri waliokuwa njiani kwenda Yerusalemu walikusanyika kumwona Yesu. Idadi ya watu iliongezeka, mpaka wakakusanyika wanaume elfu tano bila kuhesabu wanawake na watoto. Kabla ya Yesu kufika pwani, makutano wengi walikuwa wanamsubiri. Lakini alifika ufukweni bila wao kumwona, na alitumia muda mfupi kwanza kuwa na wanafunzi wake pembeni.

Kutokea kwenye mtelemko wa mlima alilitazama kundi lile kubwa la watu lililokuwa likisogea, na moyo wake ukajawa na huruma. Akiwa amebughudhiwa vile, na akiwa ameporwa nafasi ya pumziko lake, hakusubiri zaidi. Aliona hitaji kubwa la kutaka mwitikio wake kwa watu waliokuwa wanaendelea kuja. Naye "akawahurumia; kwa sababu walikuwa kama kondoo wasio na mchungaji." Akiondoka katika mahali pake alipokuwa ametembelea, alitafuta mahali panapofaa ili aweze kuwahudumia. Hawakupata msaada kutoka **(365)** kwa makuhani na wakuu; lakini maji ya uzima yanayoponya yalitiririka kutoka kwa Kristo kadiri alivyowafundisha makutano njia ya wokovu.

Watu walisikiliza maneno ya rehema yakitiririka kutoka katika midomo ya Mwana wa Mungu. Walisikia maneno ya neema, yakiwa rahisi na ya wazi kiasi kwamba yalikuwa kama zeri ya Gileadi katika mioyo yao. Uponyaji uliofanywa na mkono wake wa uungu ulileta furaha na uzima kwa watu waliokuwa kifoni, na faraja na afya kwa wale waliokuwa wanateseka katika magonjwa. Siku ile ilikuwa kwao kama vile mbingu ilikuwa duniani, na hawakuwa na kumbukumbu kabisa kuhusu muda uliokuwa umepita tangu walipokuwa wamekula chakula.

Muda mrefu wa siku ile ulikuwa umetumika. Jua lilikuwa linazama magharibi, lakini bado watu waliendelea kuwepo. Yesu alikuwa amefanya kazi siku nzima pasipo kula wala kupumzika. Alikuwa amedhoofu kwa uchovu na njaa, na wanafunzi walimsihi aache kushughulika na kazi. Lakini hakuweza kuwaacha makutano waliomsonga pande zote.

Hatimaye wanafunzi walimjia, wakimsihi awaage watu waondoke kwa manufaa yao. Wengi walikuwa wamekuja kutoka mbali, na walikuwa hawajala kitu tangu asubuhi. Huenda wangeweza kununua chakula katika miji na vijiji vinavyozunguka mahali pale. Lakini Yesu akasema, "Wapeni ninyi chakula," halafu akamgeukia Filipo, na kumwuliza, "Tununue wapi mikate, ili hawa wapate kula?" Alisema hivyo ili kujaribu imani ya mwanafunzi huyo. Filipo akaitazama ile bahari ya vichwa vya watu waliokuwa wengi pale, na akafikiria jinsi isivyowezekana kuwapatia chakula cha kuwatosha wote. Akajibu kwamba mikate ya dinari mia mbili hata isingekaribia kutosha kuwagawia wote ili kila mmoja apate kidogo-kidogo. Yesu aliulizia kuhusu kiasi cha chakula ambacho kilikuwepo miongoni mwao pale pale. Andrea akasema, "Yupo hapa mtoto, yuna mikate mitano ya shayiri na samaki wawili, lakini hivi ni nini kwa watu wengi kama hawa?" Yesu aliagiza vitu hivyo viletwe kwake. Halafu aliwataka wanafunzi wawaketishe watu kwenye majani katika makundi ya watu hamsini au mia moja, ili kuwa na mpangilio, na ya kwamba wote wapate kushuhudia kile ambacho angefanya. Hili lilipokamilika, Yesu alichukua chakula kile, "akatazama juu mbinguni, akabariki, akaimega ile mikate, akawapa wanafunzi, wanafunzi wakawapa makutano." "Wakala wote wakashiba. Wakaokota vipande vilivyomegwa vya kuweza kujaza vikapu kumi na viwili; na vipande vya samaki pia."

Yeye aliyewafundisha watu njia ya kupata amani na furaha alizingatia mahitaji yao ya kimwili kama alivyozingatia mahitaji ya kiroho. Watu walikuwa wamechoka wakizimia. Kulikuwa na wazazi wenye watoto wachanga mikononi mwao, na watoto wadogo wakizing'ang'ania sketi za mama zao. Watu wengi walikuwa

wamesimama kwa masaa mengi. Walikuwa wamevutiwa sana **(366)** na maneno ya Kristo kiasi kwamba hakuna muda waliofikiria kuhusu hitaji la kukaa chini, na umati ulikuwa mkubwa sana kiasi kwamba kulikuwa na hatari ya kukanyagana wao kwa wao. Yesu alitaka awape nafasi ya kupumzika, na aliwataka wakae chini. Kulikuwa na majani mengi mahali pale, na watu wote wangekaa kwa raha.

Kamwe Kristo hakufanya mwujiza isipokuwa kwa kusudi la kuwapatia watu hitaji muhimu, na kila mwujiza ulikuwa na sifa ya kuwaongoza watu kuelekea kwenye mti wa uzima, ambao majani yake ni ya kuwaponya mataifa. Chakula kile rahisi **(367)** kilichogawiwa kwa mikono ya wanafunzi wale kilikuwa na hazina kamilifu ya mafundisho. Chakula kile kilikuwa na sifa ya unyenyekevu; wale samaki na ile mikate ya shayiri vilikuwa ndicho chakula cha kila siku cha jamii ile ya wavuvi wa kando-kando ya Bahari ya Galilaya. Kristo angeweza kutandaza mbele ya wale watu chakula cha hadhi ya kitajiri, lakini chakula kitayarishwacho kwa lengo la kufurahisha ladha ya ulimi tu kisingebeba fundisho kwa ajili ya mafanikio ya watu wale. Katika jambo hili Kristo aliwafundisha somo kwamba vitu vya asili alivyotoa Mungu kwa mwanadamu vimepotoshwa. Watu wanaofurahia karamu za anasa zitayarishwazo kwa ajili ya kuridhisha mivuto ya hamu potofu hawajawahi kamwe kuzifurahia kama vile watu hawa walivyofurahia pumziko hili na chakula hiki rahisi kilichotolewa na Yesu kutoka miongoni mwa makazi ya watu.

Ikiwa watu wa leo wangekuwa rahisi katika mazoea yao, wakiishi kulingana na sheria za mambo ya asili, kama alivyofanya Adamu na Hawa hapo mwanzo, mahitaji ya jamii ya wanadamu yangekidhiwa mno kwa wingi wa vitu. Kungekuwa na upungufu wa mahitaji ulio mdogo sana wa kufikirika tu, na kungekuwa na fursa nyingi zaidi za kufanya kazi katika njia za Mungu. Lakini ubinafsi na kutaka kuridhisha hamu ya tamaa isiyo ya asili vimeleta ulimwenguni dhambi na umaskini mkubwa, vikisababishwa na hali ya kuwa na ziada kuliko mahitaji kwa upande mmoja, na tatizo la kuwa katika hali ya kukosa mahitaji kabisa kwa upande mwingine.

Yesu hakutafuta kuwavuta watu kwake kwa njia ya kufurahisha tamaa ya anasa. Kwa umati ule wa watu, waliochoka na kuumwa njaa baada ya siku yenye msisimko wa muda mrefu, chakula rahisi kilikuwa ni cha kuwahahakishia kwamba Yesu si tu kwamba alikuwa na uwezo, bali pia alikuwa mwema kwao katika kukidhi mahitaji ya kawaida ya maisha. Mwokozi hajawaahidi wafuasi wake kupata maisha ya anasa ulimwenguni; chakula chao kingekuwa chepesi, au hata kidogo; wanaweza wakawa katika fungu la watu waliofungwa na umaskini; lakini neno lake linatoa ahadi kwamba watapatiwa mahitaji yao, na ameahidi kitu ambacho ni chema kwa mbali kuliko mali ya ulimwengu, - faraja ya uwepo wake pamoja nao.

Katika kuwalisha wale watu elfu tano, Yesu anafunua pazia la ulimwengu wa asili, na anadhihirisha uweza ambao unafanya kazi muda wote kwa ajili ya manufaa yetu. Katika kuzalisha mazao ya dunia Mungu anatenda mwujiza kila siku. Kupitia nguvu za asili inafanyika kazi ile ile iliyofanywa katika kuwalisha makutano wale. Watu huandaa udongo na kupanda mbegu, lakini uhai utokao kwa Mungu ndio huifanya mbegu kuota. Mvua na hewa na mwanga wa jua ni vitu vya Mungu vinavyoifanya izae, "kwanza jani, tena suke, kisha ngano pevu katika suke." Marko 4:28. Mungu ndiye anayewalisha mamilioni kutokana na mazao ya mashamba. Wanadamu wanaalikwa kushirikiana na Mungu katika kutunza nafaka na kuandaa mkate, na kwa sababu hii wanafika mahali wanapoteza kuona nguvu za kimbingu. Hawampi Mungu utukufu unaostahili **(368)** jina lake takatifu. Ufanyaji kazi wa uweza wake umewekwa katika nguvu za asili au katika utendaji wa wanadamu anaowatumia. Lakini mwanadamu anatukuzwa mahali pa Mungu, na zawadi za Mungu za neema zinapotoshwa kwa kutumiwa kwa ubinafsi, na kufanywa kuwa laana badala ya kuwa baraka. Mungu anataka kubadili haya yote. Anatamani kwamba fahamu zetu zisizo na ufahamu zihimizwe kuona wema wake wa rehema na kumtukuza Yeye kwa sababu ya kazi za uweza wake. Anatamani tumtambue katika thawabu zake, ili zipate kuwa mbaraka kwetu kama alivyokusudia. Miujiza ya Kristo ilitendwa ili kutimiza kusudi hili.

Baada ya kuwa makutano wamelishwa, kulikuwa na vyakula vingi vilivyosalia. Lakini Yeye aliyekuwa na vyanzo vyote visivyo na mwisho aliamuru akisema, "Kusanyeni vipande vilivyobaki, kisipotee chochote." Maneno haya yalikuwa na maana iliyo zaidi ya kuweka mikate ile katika vikapu. Fundisho lile lilikuwa na sehemu mbili. Hakuna kitu cha kutupwa. Hatupaswi kuruhusu kitu chochote cha manufaa kiponyoke. Hatupaswi kupuuza kitu chochote kinachoweza kumfaa mwanadamu. Hebu kila kitu kinachoweza kusaidia kukidhi mahitaji ya wanadamu walio na njaa duniani kikusanywe. Na pia kuwe na uangalifu kama huo huo katika mambo ya kiroho. Wakati vikapu vya mabaki ya chakula vilipokusanywa, watu wale walifikiria habari ya wenzao waliokuwa

nyumbani. Walitaka na wao wapate sehemu katika mkate uliobarikiwa na Kristo. Vile vilivyokuwa katika vikapu vile viligawiwa kwa umati ule wenye hamu, na vilipelekwa katika maeneo yote yalizunguka mahali pale. Kwa hiyo wale waliokuwa karamuni walitakiwa kuwapa wengine pia mkate ulioshuka kutoka mbinguni, ili kushibisha njaa ya roho. Walitakiwa kurudia kile walichokuwa wamejifunza kuhusu mambo ya ajabu ya Mungu. Hakuna kitu kilichotakiwa kutupwa. Hakuna hata neno moja lihusulo wokovu wao wa milele ambalo lingeanguka chini pasipo kufanya kazi.

Mwujiza wa mikate hufundisha somo la kumtegemea Mungu. Wakati Kristo alipowalisha watu elfu tano, chakula kile hakikuwepo pale pale karibu. Kwa hali ya kawaida ni kwamba hakuwa na namna yoyote ya kufanya. Hapa alikuwa nyikani akiwa na watu elfu tano, bila kuhesabu wanawake na watoto. Hakuwa amewaita makutano wale kuja kumfuata; walikuja bila mwaliko wala pasipo kuagizwa; lakini alijua kwamba baada ya kuwa walikuwa wamesikiliza mafundisho yake kwa muda mrefu vile, wangeumwa njaa na kuzimia; maana alikuwa pamoja nao katika uhitaji wa chakula. Walikuwa mbali na nyumbani, na usiku ulikuwa unakaribia sana. Wengi wao hawakuwa na uwezo wa kununua chakula. Yeye ambaye alifunga kwa siku arobaini jangwani kwa ajili yao asingewaruhusu warudi nyumbani wakiwa katika hali ya kufunga. Ukuu wa Mungu ulikuwa umemweka Kristo mahali pale alipokuwa; naye alimtegemea Baba yake wa mbinguni kutoa vitu vya kukidhi mahitaji.

**(369)** Na sisi tunapoletwa katika hali ngumu, tunapaswa tumtegemee Mungu. Yatupasa tutumie hekima na busara katika kila tendo tutendalo maishani, ili ya kwamba tusijiweke majaribuni kwa kwenda pasipo tahadhari. Hatupaswi kujitumbukiza katika matatizo, tukipuuza vitu ambavyo Mungu ametoa, na kutumia vibaya akili ambazo Mungu ametupatia. Yawapasa wafanyakazi wa Kristo watii mafundisho yake. Kazi ni ya Mungu, na kama tungependa kuwabariki wengine lazima mipango yake ifuatwe. Kujitumainia nafsi hakuwezi kuwa kitovu; kujitumainia nafsi hakuwezi kupata heshima. Ikiwa tunapanga kwa mawazo yetu wenyewe, Mungu atatuacha katika makosa yetu wenyewe. Lakini, baada ya kufuata maelekezo yake, tunapoletwa katika hali ngumu, atatuokoa. Hatupaswi kukata tamaa na kusalimu amri, bali katika kila hali tunatakiwa kutafuta msaada kwake Yeye ambaye rasilimali zote zi chini ya amri yake. Mara nyingi tutazungukwa na matukio ya majaribu, na wakati huo ndipo tunalazimika, kwa ujasiri mkubwa mno, kumtegemea Mungu. Atamhifadhi kila mtu anayeletwa katika hali ya kutatanika anapojitahidi kuishika njia ya Bwana.

Kristo ametuhimiza, kupitia kwa nabii, kwamba tuwe na tabia ya "kuwagawia wenye njaa chakula" chetu na "kuishibisha nafsi iliyoteswa;" "Umwonapo mtu aliye uchi, umvike nguo," na "kuwaleta maskini waliotupwa nje nyumbani kwako." Isaya 58:7-10. Ametuhimiza kwamba, "Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe." Marko 16:15. Lakini ni mara nyingi kiasi gani mioyo yetu hutuzamisha, na imani yetu kutuangusha, tunapoona uhitaji ulivyo mkubwa, na jinsi vitu vya kukidhi mahitaji vilivyo kidogo sana mikononi mwetu. Kama alivyouwa Andrea alipoangalia ile mikate mitano na samaki wadogo wawili, tunasema kwa mshangao, "Hivi ni nini kwa watu wengi kama hawa?" Mara nyingi tunasita, tunakosa uhiari wa kutoa vyote tulivyo navyo, tukiogopa kutumia na kutumika kwa ajili ya watu wengine. Lakini Yesu ametuhimiza kwamba, "Wapeni ninyi chakula." Agizo lake ni ahadi; na nyuma ya hilo kuna uweza ule ule uliolisha umati wa watu kando ya bahari.

Katika kitendo cha kutoa mahitaji ya mwili kwa umati wa watu wenye njaa kumefungamanishwa fundisho la kina la kiroho kwa ajili ya wafanyakazi wake. Kristo alipokea kwa Baba; aliwapatia wanafunzi wake; wakawapatia makutano; na watu wakapeana wao kwa wao. Hivyo ndivyo wote waliounganishwa na Kristo watakavyopokea kwake mkate wa uzima, chakula cha mbinguni, na kukitoa kwa wengine.

Akiwa katika kumtegemea Mungu kikamilifu, Yesu alichukua kiasi kile kidogo cha mikate; na ingawa kulikuwa na kiasi kidogo tu kwa ajili ya familia yake ya wanafunzi wale, hakuwaita ili kula kile chakula, bali kuwagawia wengine, akiwahimiza wawahudumie watu. Chakula kilizidishiwa katika mikono yake; na mikono ya wanafunzi wake, iliyokuwa inamfikia Kristo mwenyewe aliye Mkate wa **(370)** Uzima haikukaa ikiwa mitupu pasipo kitu. Kiasi kile kidogo kilitosha kwa ajili ya watu wote. Baada ya mahitaji ya watu kutoshelezwa, mabaki yalikusanywa, na Kristo na wanafunzi wake wakala pamoja sehemu ya chakula kile cha thamani kilichotolewa na Mbingu.

Wanafunzi walikuwa ndio mfereji wa mawasiliano kati ya Kristo na watu. Jambo hili linapaswa liwe la kuwatia shime wanafunzi wake wa leo. Kristo ndiye kitovu kikuu, chanzo cha nguvu zote. Wanafunzi wake wanapaswa wapokee vitu vyao vya kutoa kutoka kwake. Ufahamu wa hali ya juu, hali ya juu ya mambo ya kiroho, vinaweza

kutolewa kwa kadiri wanavyovipokea. Wao wenyewe hawawezi kutoa kitu chochote cha kukidhi mahitaji ya nafsi. Tunaweza kufundisha kile tu tunachopokea kutoka kwa Kristo; na tunaweza kupokea kiasi kile tu ambacho tunaweza kuwafundisha watu wengine. Kadiri tunavyoendelea kuwapa watu ndivyo tunavyoendelea kupokea; na kadiri tunavyotoa vingi ndivyo tutakavyopokea vingi. Hivyo tunaweza tukaamini muda wote, tukitumaini, tukipokea, na kufundisha.

Kazi ya kuujenga ufalme wa Kristo itasonga mbele, ingawa kwa mwonekano wote inaonekana kwenda pole pole na hali za kutowezekana zinaonekana kukwamisha maendeleo yake. Kazi ni ya Mungu, naye atatoa vitu vinavyohitajika, na atawatuma wanafuzi wake walio wasaidizi wa kweli na wa dhati, ambao mikono yao itajawa na chakula kwa ajili ya makutano wanaokufa kwa njaa. Mungu anawajali watu wanaofanya kazi kwa upendo kuwapa watu wanaoangamia neno la uzima, ambao hugeuka wakiinyosha mikono yao kuchukua chakula kwa ajili ya kuwapa watu wengine wenye njaa.

Katika kazi yetu kwa ajili ya Mungu kuna hatari ya kujikita sana katika kuangalia jambo ambalo mwanadamu na talanta zake na uwezo wake anaweza kulifanya. Kwa njia hiyo tunapoteza hali ya kumwona Bwana wa Kazi. Mara nyingi mfanyakazi kwa ajili ya Kristo hushindwa kutambua wajibu wake yeye. Yuko katika hatari ya kuhamisha mzigo wake kuuweka juu ya mashirika, badala ya kumtegemea Yeye aliye chanzo cha nguvu zote. Katika kazi ya Mungu ni kosa kubwa sana kutegemea hekima ya mwanadamu au kutegemea idadi ya watu. Ufanisi wa kazi ya Kristo hautegemei sana idadi au talanta zaidi ya vile inavyotegemea usafi wa kusudi, urahisi wa dhati wa imani ya utegemezi wa kweli kwa Mungu. Lazima wajibu wa mtu ubebwe, lazima majukumu ya mtu yafanywe, lazima jitihada za mtu zifanywe kwa ajili ya wale wasiomjua Kristo. Badala ya kuhamisha wajibu wako kupeleka kwa mtu fulani unayedhani kwamba amejaliwa sana kuliko ulivyo wewe, fanya kazi kulingana na uwezo wako.

Pindi swali linapokuja moyoni mwako kwamba, "Tununue wapi mikate, ili hawa wapate kula?" hebu jibu lako lisiwe la kutokuamini. Wakati wanafunzi waliposikia maelekezo ya Yesu kwamba, "Wapeni ninyi chakula," utata wote mgumu uliwajia akilini. Waliuliza kwamba, **(371)** Je, twende katika vijiji tukanunue chakula? Hivyo ndivyo ilivyo leo, wakati watu wanapokuwa na haja ya mkate wa uzima, watoto wa Bwana wanauliza kwamba, Je, tuite mtu fulani kutoka mbali aje awalishe? Lakini Kristo alisemaje? "Waketisheni watu," naye akawalisha pale. Kwa hiyo unapokuwa umezungukwa na roho zenye kuhitaji, jua kwamba Kristo yuko hapo. Shirikiana naye. Leta kwake mikate yako ya shayiri.

Rasilimali tulizo nazo zinaweza kuonekana zisizotosha kwa ajili ya kazi; lakini ikiwa tutasonga mbele kwa imani, tukiamini katika uweza wa Mungu aliye na vitu vyote, rasilimali za kutosha zitafunguka mbele yetu. Ikiwa kazi ni ya Mungu, Yeye mwenyewe atatoa rasilimali kwa ajili ya kuikamilisha. Ataipa thawabu hali ya utegemezi kwake ulio rahisi, wa dhati na wa uaminifu. Kidogo kinachotumika katika kazi ya Bwana wa mbinguni kwa busara na uangalifu kitaongezeka katika tendo lile lile la kukitoa. Katika mikono ya Kristo kiasi kidogo cha chakula kiliendelea kuwepo bila kuisha mpaka pale mkutano wa watu wenye njaa ulipotosheka. Ikiwa tutaenda kwake aliye Chanzo cha nguvu zote, tukiwa na mikono ya imani iliyonyooshwa ili kupokea, tutategemezwa katika kazi yetu, hata katika mazingira magumu mno, na tutawezeshwa kuwapa wengine mkate wa uzima.

Bwana anasema hivi, "Wapeni watu vitu, nanyi mtapewa." "Apandaye haba atavuna haba; apandaye kwa ukarimu atavuna kwa ukarimu. . . . Na Mungu aweza kuwajaza kila neema kwa wingi, ili ninyi, mkiwa na riziki za kila namna siku zote, mpate kuzidi sana katika kila tendo jema; kama ilivyoandikwa,
Ametapanya, amewapa maskini,
Haki yake yakaa milele.

Na yeye ampaye mbegu mwenye kupanda, na mkate uwe chakula, atawapa mbegu za kupanda na kuzizidisha, naye atayaongeza mazao ya haki yenu; mkitajirishwa katika vitu vyote mpate kuwa na ukarimu wote, umpatiao Mungu shukrani kwa kazi yetu." Luka 6:38; 2 Wakorintho 9:6-11.

## Sura ya 40

# Usiku Ziwani

[Sura hii imejengwa katika Mathayo 14:22-33; Marko 6:45-52; Yohana 6:14-21.]

Wakiwa wamekaa katika uwanda wa majani, wakati wa jua kuzama mnamo jioni ya majira ya kuchipusha, watu walikula chakula kile alichotoa Yesu. Maneno waliyokuwa wamesikia siku ile yalikuwa yamewajia kama sauti ya Mungu. Matendo ya kuponya waliyokuwa wameshuhudia yalikuwa kama yale yanayoweza kufanywa na nguvu ya mbinguni tu. Lakini mwujiza wa mikate ulimgusa kila mmoja katika umati ule mkubwa. Wote walikuwa wamekuwa washiriki katika huduma hii. Mnamo siku za Musa, Mungu alikuwa amewalisha Israeli kwa mana kule jangwani; na sasa huyu aliyekuwa amewalisha siku hii ni nani ikiwa si yule ambaye alitabiriwa na Musa? Hakuna uwezo wa mwanadamu ambao ungeweza kufanya chakula cha kutosha kulisha maelfu ya watu wenye njaa kutokana na mikate mitano ya shayiri na samaki wadogo wawili. Nao wakaambiana wao kwa wao, "Hakika huyu ni nabii yule ajaye ulimwenguni."

Kwa siku nzima hali ya kusadikishwa ilikuwa imeimarishwa. Kitendo kile chenye utukufu kilikuwa uhakika kwamba Mkombozi aliyetarajiwa kwa muda mrefu alikuwa miongoni mwao. Matumaini ya watu yanapanda juu zaidi na zaidi. Huyu ndiye Yeye atakayeifanya Uyahudi kuwa paradiso ya duniani, nchi itiririkayo maziwa na asali. Anaweza kutosheleza kila hamu. Anaweza kuvunja nguvu za Warumi waliochukiwa sana. Anaweza kuikomboa Yuda na Yerusalemu. Anaweza kuwaponya askari watakaojeruhiwa katika mapigano. Anaweza kutoa chakula cha kutosha jeshi lote. Anaweza kuyashinda mataifa, na kuiletea Israeli ufalme uliotafutwa kwa muda mrefu.

**(378)** Katika hamasa yao hiyo watu wale wako tayari mara moja kumvisha taji ya kifalme. Wanamwona akiwa hafanyi jitihada za kutaka hilo au kujiletea heshima. Katika hili yuko tofauti na makuhani na wakuu, nao watu wanahofu kwamba hatakubali kamwe madai ya kutaka kiti cha enzi cha Daudi. Walipojadiliana pamoja, walikubaliana kumchukua kwa nguvu, na kumtangaza kuwa mfalme wa Israeli. Wanafunzi wanaungana na makutano katika kutangaza kwamba kiti cha enzi cha Daudi ni halali ya kurithiwa na Bwana wao. Walisema kwamba, Kujinyenyekeza kwa Kristo ndiko kunakomsababisha akatae heshima hiyo. Hebu watu na wamwinue Mwokozi wao. Hebu makuhani na wakuu wenye kujivuna walazimishwe kumheshimu Yeye ajaye akiwa amevikwa mamlaka ya Mungu.

Kwa hamu wanapanga kutekeleza kusudi lao hilo; lakini Yesu anaona mguu wao unakoelekea, na anaelewa, kwa namna ambavyo wao hawawezi, kile ambacho kingekuwa matokeo ya uelekeo wao ule. Hata sasa makuhani na wakuu wako wanawinda maisha yake. Wanamshtaki kwa kuwavuta watu kwake kutoka kwao. Matumizi ya nguvu na ghasia vingefuata baada ya jitihada zao za kumweka kwenye kiti cha enzi, na kazi ya ufalme wa kiroho ingekwamishwa. Lazima mpango wao ule uzimwe. Akiwaita wanafunzi wake, Yesu aliwataka wachukue chombo na kurudi mara moja Kapernaumu, wakimwacha ili awaage watu watawanyike.

Kabla ya hapo hakukuwahi kamwe kuwa na agizo la Yesu lililo gumu kulitii kama hili. Wanafunzi walikuwa wamezitarajia kwa muda mrefu harakati za watu kumweka Yesu kwenye kiti cha enzi; hawakuweza kustahimili wazo kwamba matarajio yote haya yangekuwa si kitu. Umati wa watu waliokuwa wanakusanyika kuisherehekea Pasaka walikuwa na hamu ya kumwona nabii mpya. Kwa wafuasi wake Yesu hali hii ilionekana kuwa fursa ya thamani ya kumsimika Bwana wao kwenye kiti cha enzi cha Israeli. Katika hamasa ya hamu yao hii ilikuwa vigumu kwao kwenda zao peke yao, wakimwacha Yesu peke yake katika pwani ile ya upweke. Walipinga mpango huo; lakini sasa Yesu alisema kwa mamlaka ambayo hakuwahi kuitumia kwao. Wakajua kwamba kuendelea kukataa zaidi kusingesaidia lolote kwao, na wakiwa kimya waliondoka kuelekea baharini.

Sasa Yesu anawaamuru makutano kutawanyika; na mwonekano wake ni wa dhati kiasi kwamba hawakuthubutu kuacha kutii. Maneno ya kusifu na kutukuza yanakoma midomoni mwao. Hatua za miguu yao katika tendo la kumsogelea ili kumshika na kumtawaza zinazuiliwa pale pale, na mwonekano wao wa furaha na hamu unatoweka. Katika umati ule kulikuwa na watu wenye mawazo ya ushawishi na nguvu za maamuzi; lakini mwonekano wa kifalme wa Yesu, na maneno yake machache ya amri, yanatuliza purukushani, na kukatisha

mipango yao. Wanagundua **(379)** kwamba ndani yake kuna uweza zaidi ya ule wa mamlaka zote za dunia, na pasipo kuhoji wanaheshimu.

Alipoachwa peke yake, Yesu "alipanda mlimani faraghani, kwenda kuomba." Aliendelea kumwomba Mungu kwa saa kadhaa. Maombi yale hayakuwa kwa ajili yake bali kwa ajili ya wanadamu. Aliomba nguvu ya kuwafunulia watu tabia ya kimbingu ya kazi yake, ili kwamba Shetani asipofushe mawazo yao na kupotosha akili zao. Mwokozi alijua kwamba siku zake za kuhudumu duniani zilikuwa karibu na kwisha, na ya kwamba wachache ndio wangempokea kama Mkombozi wao. Katika hali ya ugumu na mapambano ya moyoni aliwaombea wanafunzi wake. Walikuwa wajaribiwe vikali. Matarajio yao ya muda mrefu, yaliyokitwa katika imani potofu ya wengi, yangekatishwa tamaa kwa namna ya kuumiza na kufadhaisha mno. Badala ya kutawazwa kwake kwenye kiti cha enzi cha Daudi wangeshuhudia kusulibiwa kwake. Hii ndiyo ingekuwa sherehe yake ya kweli ya kutawazwa. Lakini wao hawakuona hili, na matokeo yake majaribu makali yangewajia, ambayo ingekuwa vigumu kwao kugundua kwamba ni majaribu. Pasipo Roho Mtakatifu kumlikia mawazo yao na kupanua ufahamu wao imani ya wanafunzi wale ingeanguka. Lilikuwa jambo la kumwumiza Yesu sana kwamba uelewa wao kuhusu ufalme wake ulikuwa, kwa kiasi kikubwa sana, umeishia kwenye heshima na utukufu wa ulimwenguni. Kwa ajili yao mzigo mzito ulikuwa umelemea moyo wake, naye akamwaga sala zake akiwa na maumivu machungu na machozi.

Wale wanafunzi hawakuwa wameondoka muda ule ule pale nchi kavu, kama Yesu alivyowaagiza. Walisubiri kwa muda kidogo, wakidhani kwamba angekuja **(380)** kwao. Lakini walipoona kwamba giza la usiku linakuja haraka, "wakapanda chomboni, wakaanza kuivuka bahari kwenda Kapernaumu." Walikuwa wamemwacha Yesu wakiwa na mioyo ambayo haikuridhika, wakiwa wamesononeshwa naye kuliko ilivyopata kutokea tangu walipomkubali kuwa Bwana wao. Walinung'unika kwa sababu hawakuruhusiwa kumtangaza kuwa mfalme. Walijilaumu wenyewe kwa kukubaliana na agizo lake haraka vile. Walitoa hoja kwamba kama wangeng'ang'ania zaidi wangetimiza kusudi lao.

Kutokuamini kulikuwa kunajaa katika mawazo na mioyo yao. Kupenda heshima kulikuwa kumewapofusha. Walijua kwamba Yesu alikuwa anachukiwa na Mafarisayo, kwa hiyo walikuwa na hamu ya kumwona akitawazwa kama walivyofikiri kwamba ingekuwa hivyo. Kuunganishwa na mwalimu aliyeweza kutenda miujiza mikubwa, halafu wasutwe kuwa ni waongo, lilikuwa jaribu ambalo wangelistahimili kwa uchungu mkubwa sana. Je, wangeendelea kuonekana kama wafuasi wa nabii wa uongo? Je, Kristo asingedai tena mamlaka yake kama mfalme? Kwa nini Yeye aliye na uwezo kama ule hakujifunua katika tabia yake halisi, na kuifanya njia yao iwe na maumivu kidogo zaidi? Kwa nini hakumwokoa Yohana Mbatizaji kutokana na kifo kile cha kikatili? Hivyo ndivyo wanafunzi wale walivyohoji mpaka wakajiletea giza kuu la kiroho. Waliuliza hivi, Yawezekana Yesu akawa ni laghai, kama walivyodai Mafarisayo?

Wanafunzi wale walikuwa wameshuhudia kazi za ajabu za Kristo siku ile. Ilikuwa imeonekana kama vile mbingu ilikuwa imeshuka chini duniani. Kumbukumbu za siku ile ya utukufu wa thamani zingepaswa kuwajaza imani na tumaini. Ikiwa wangekuwa wanasemezana kuhusu mambo haya, wasingeingia katika majaribu. Lakini mfadhaiko wao ulivuta mawazo yao. Maneno yale ya Kristo kwamba, "Kusanyeni vipande vilivyobaki, kisipotee chochote," hayakusikika kwao. Zile zilikuwa saa za mbaraka mpana wa wanafunzi wale, lakini walikuwa wamesahau yote hayo. Walikuwa katikati ya maji ya bahari iliyochafuka. Mawazo yao yalikuwa ya tufani na yasiyo na maana, naye Bwana akawapa kitu kingine ili kisumbue mioyo yao na kujaza mawazo yao. Mungu hufanya hivi mara nyingi watu wanapojitengenezea mizigo na shida. Wanafunzi wale hawakuhitaji kufadhaika tena. Tayari hatari ilikuwa inakaribia.

Upepo mkali ulikuwa unawajia, nao hawakuwa wamejiandaa kwa ajili ya huo. Ilikuwa ni hali ya tofauti ya ghafla, maana siku ile ilikuwa shwari; na upepo mkali wa dhoruba ulipowapiga, waliogopa. Walisahau kule kutoridhishwa kwao, kutokuamini kwao, kutokuwa na subira kwao. Kila mmoja alifanya kazi ya kukinusuru chombo kisizame. Lakini kulikuwa na umbali mfupi tu wa kupitia baharini kutoka Bethsaida kwenda kule walikotarajia kukutana na Yesu, na katika hali ya hewa ya kawaida safari ile ingetumia saa chache tu; lakini sasa walisukumwa kwenda mbali zaidi **(381)** na zaidi kutoka mahali pale walipokuwa wakienda. Walisumbuka na makasia mpaka muda wa zamu ya nne ya usiku. Halafu watu wale wakiwa wamechoka walikata tamaa na

kukubali kuangamia. Katika tufani na giza bahari ilikuwa imewafundisha kuhusu hali yao ya kutoweza kujisaidia, nao wakatamani uwepo wa Bwana wao.

Yesu hakuwa amewasahau. Yeye aliyekuwa Mtazamaji pale pwani aliwaona wale watu waliopigwa na hofu wakipambana na upepo wa mpisho. Hakuacha kuwatazama wanafunzi wake hata kwa muda mfupi. Akiwa katika hali ya kujali kwa kina macho yake yalifuatilia kile chombo kilichokuwa kikipigwa na dhoruba kikiwa na shehena ya thamani ndani yake; maana watu hawa wangekuwa nuru ya ulimwengu. Kama vile mama mwenye upendo anavyomwangalia mtoto wake, ndivyo Bwana wa huruma alivyowaangalia wanafunzi wake. Mioyo yao ilipokuwa imenyenyekezwa, mawazo yao yasiyo matakatifu yakiwa yameondoshwa, na kwa unyenyekevu wakaomba msaada, ndipo msaada ulipotolewa kwao.

Wakati ule walipoamini kwamba wanaangamia, ndipo kumlika kwa mwanga kunaonyesha kitu chenye umbile la ajabu kikiwa kwenye maji kuelekea upande walipo. Lakini hawajui kama ni Yesu. Yeye Yule aliyekuwa anakuja ili kuwaokoa wakamwona kama adui. Hofu kuu ikawashika. Mikono ile iliyokuwa imeshikilia makasia ikiwa na misuli iliyokakamaa kama chuma ikaachia na kudondosha makasia yale. Chombo kikaenda kulingana na matakwa ya mawimbi; macho yote yakawa yamekazwa kwa mwonekano huu wa mtu anayetembea kwenye uso mweupe wa maji ya bahari yenye mwonekano wa povu-povu.

Walidhania kwamba kitu kile ni zimwi linalotaka kuwaharibu, nao wakalia kwa hofu. Yesu anaendelea mbele kama vile anataka kuwapita; lakini wanamtambua, na kulia, wakiomba msaada wake. Bwana wao mpendwa anageuka, sauti yake inanyamazisha hofu yao anaposema, "Changamkeni; ni mimi, msiogope."

Haraka sana kadiri ilivyowezekana kulifurahia tukio hili, Petro alikuwa kama siyo yeye tena kwa furaha. Kama mtu ambaye bado aliamini kwa shida, aliita, "Bwana, ikiwa ni wewe, niamuru nije kwako juu ya maji. Akasema, Njoo."

Akiwa anamwangalia Yesu, Petro anatembea salama kwenye maji; lakini anapokuwa na hali ya kujitosheleza mwenyewe anatazama nyuma kwa wenzake walio katika chombo, macho yake yamegeuzwa kutoka kwa Mwokozi. Upepo unasukuma. Mawimbi yanapanda juu, na kuja katikati ya yeye na Bwana; naye anaogopa. Kwa muda mfupi Yesu amefichwa asionekane kwake, imani yake inaondoka. Anaanza kuzama. Lakini wakati mawimbi hayo yanapoashiria kifo, Petro anainua macho yake kutoka katika maji yale yenye ghadhabu, na kuyakaza kwa Yesu, akilia, "Bwana, niokoe." Yesu ananyosha mkono wake na kumshika mkono haraka, akisema, "Ewe mwenye imani haba, mbona uliona shaka?"

Wakitembea pamoja, mkono wa Petro ukiwa umeshikwa na ule wa Bwana wake, waliingia katika chombo pamoja. Lakini sasa Petro alikuwa amenyenyekeshwa na kuwa kimya. Hakuwa na sababu ya kujikweza juu ya wenzake, maana kwa sababu ya kutokuamini na kujikweza **(382)** alikaribia kupoteza maisha yake. Wakati alipogeuza macho kutoka kwa Yesu, mahali pa kukanyaga mguu palipotea, naye akazama katika mawimbi.

Ni mara ngapi tunakuwa kama Petro pindi shida zinapotujia! Tunayaangalia mawimbi badala ya kukaza macho yetu kwa Mwokozi. Hatua zetu huteleza, na maji ya kiburi hujaa katika mioyo yetu. Yesu hakumtaka Petro aje kwake ili aangamie; yeye hatuiti kumfuata, halafu akatuacha. Anasema, "Usiogope, maana nimekukomboa; nimekuita kwa jina lako. . . Upitapo katika maji mengi nitakuwa pamoja nawe; na katika mito, haitakugharikisha; uendapo katika moto, hutateketea; wala mwali wa moto hautakuunguza. Maana mimi ni Bwana, Mungu wako; Mtakatifu wa Israeli." Isaya 43:1-3.

Yesu alisoma tabia ya wanafunzi wake. Alijua jinsi ambavyo imani yao ingejaribiwa kweli kweli. Katika tukio hili la baharini alitaka kumwonyesha Petro udhaifu wake, - kuonyesha kwamba usalama wake ulikuwa katika kutegemea uwezo wa kimbingu wakati wote. Katikati ya dhoruba za majaribu angetembea salama ikiwa tu angeachana na kujitumainia mwenyewe amtumainie Mwokozi. Wakati alipojiona kuwa ana nguvu ndipo mahali Petro alipokuwa dhaifu; na mpaka pale alipoona udhaifu wake ndipo alipotambua hitaji lake la kumtegemea Mwokozi. Ikiwa angejifunza somo hilo ambalo Yesu alitaka kumfundisha katika uzoefu huo wa baharini, asingeshindwa wakati jaribu kubwa lilipomjia.

Mungu anawafundisha watoto wake siku kwa siku. Kwa kutumia matukio ya maisha ya kila siku anawaandaa kutekeleza sehemu yao katika hatua pana ambayo Mwenye uwezo wote ameamuru kwao. Ni katika kushinda na kushindwa mambo ya majaribu ya kila siku ndipo mtu anaweza kushinda au kushindwa jaribu kubwa maishani.

Wale wanaoshindwa kutambua umuhimu wa kumtegemea Mungu wakati wote watashindwa na majaribu. Tunaweza tukadhani sasa kwamba miguu yetu imesimama imara, na ya kwamba hatutatikiswa kamwe. Tunaweza kusema kwa ujasiri kwamba, "Namjua yeye ninayemwamini; hakuna kitu kinachoweza kutikisa imani yangu kwa Mungu na neno lake." Lakini Shetani anapanga kutumia tabia zetu za kibinadamu za kurithi na za namna tulivyolelewa, na kupofusha mawazo yetu yaelekee mahitaji yetu binafsi na madhaifu yetu. Ni katika kutambua udhaifu wetu tu na kumwangalia Yesu ndipo tunaweza kutembea tukiwa salama.

Baada tu ya Yesu kutia mguu wake chomboni upepo ulikoma, "mara hiyo chombo kikaifikilia nchi waliyokuwa wakiiendea." Usiku wa kutisha ulifuatwa na nuru ya pambazuko. Wanafunzi, na watu wengine waliokuwa katika chombo, walisujudu miguuni pa Yesu kwa mioyo ya shukrani, wakisema, "Hakika wewe u Mwana wa Mungu!"

## Sura ya 41

# Wakati Mgumu Kule Galilaya

[Sura hii imejengwa katika Yohana 6:22-71.]

Kristo alipowakataza watu kumfanya kuwa mfalme, alijua kwamba kipindi muhimu sana katika historia ya maisha yake kilikuwa kimefika. Makundi ya watu ambao wana hamu ya kumtawaza kuwa mfalme leo kesho wangegeuka na kumwacha. Mfadhaiko ambao ungetokana na matarajio yao ya kibinafsi ungebadili upendo wao kuwa chuki, na kumsifia kwao kuwa kulaani. Lakini akijua hilo hakuchukua hatua zozote za kuzuia hatari hiyo. Tangu mwanzo alikuwa amewaonyesha wafuasi wake wasitumainie thawabu za kidunia. Alikuwa amemwambia kila mtu aliyetamani kuwa mwanafunzi wake kwamba, "Mbweha wana pango, na ndege wa angani wana viota; lakini Mwana wa Adamu hana pa kulaza kichwa chake." Mathayo 8:20. Ikiwa watu wangeweza kuwa na ulimwengu pamoja na Kristo, makutano wengi wangemheshimu kama mtu mkuu; lakini Yeye asingekubali ibada ya namna hiyo. Miongoni mwa wale waliojiunga naye walikuwemo wengi waliokuwa wamevutwa na matarajio ya ufalme wa kidunia. Lazima hawa wasidanganyike. Lile fundisho la kina la mwujiza wa mikate halikuwa limeeleweka. Hili lilitakiwa liwekwe wazi. Na ufunuo huu mpya ungekuja ukiwa pamoja na jaribu la karibu zaidi.

Mwujiza wa mikate ulisimuliwa maeneo ya mbali na karibu, na asubuhi sana na mapema umati mkubwa wa watu walikusanyika kuja Bethsaida kumwona Yesu. Walikuja kwa wingi sana kupitia nchi kavu na baharini. Wale waliokuwa wametoka kwake usiku uliokuwa umepita walirudi, wakitazamia kumkuta pale pale, maana hakukuwa na mashua ambayo angesafiria kwenda upange mwingine. Lakini kumtafuta kwao hakukuzaa matunda, na wengi wakaazimia kwenda Kapernaumu, wakiendelea kumtafuta.

**(384)** Punde tu alikuwa amewasili huko Genesareti, baada ya kutokuwepo pale kwa siku moja. Muda mfupi tu baada ya kujulikana kwamba amefika nchi ile, watu "wakaenda mbio, wakizunguka nchi ile yote, wakaanza kuwachukua vitandani walio hawawezi, kwenda kila mahali waliposikia kwamba yupo." Marko 6:55.

Baada ya muda alienda katika sinagogi, na wale waliokuja kutoka Bethsaida wakamkuta huko. Walijulishwa na wanafunzi wake jinsi alivyokuwa amevuka bahari. Habari za kutishwa na dhoruba, masaa mengi ya kukabiliana na upepo wa mpisho bila mafanikio, kutokea kwa Kristo akitembea kwenye maji, hofu iliyowapata wakati huo, maneno yake ya kuwatuliza, tukio la ajabu la Petro na matokeo yake, pamoja na kutulia ghafla kwa dhoruba na kufika pwani kwa chombo, zilisimuliwa zote kwa uaminifu kwa umati wa watu uliokuwa ukishangaa. Wakiwa hawaridhishwi na haya, wengi walikusanyika kwa Yesu, wakiuliza, "Rabi, wewe umekuja lini hapa?" walitamani kupata habari zaidi za mwujiza ule kutoka midomoni mwake mwenyewe.

Yesu hakuridhisha udadisi wao. Alisema kwa huzuni kwamba, "Ninyi mnanitafuta, si kwa sababu mliona ishara, bali kwa sababu mlikula ile mikate mkashiba." Hawakumtafuta kwa ajili ya msukumo wowote wa maana; bali kama vile walivyokuwa wamelishwa mikate, walitamani kupata faida za kimwili kwa kujiunganisha naye. Mwokozi aliwahimiza kwamba, "Msikitendee kazi chakula chenye kuharibika, bali chakula kidumucho hata **(385)** uzima wa milele; ambacho Mwana wa Adamu atawapa, kwa sababu huyo ndiye aliyetiwa muhuri na Baba, yaani, Mungu." Msitafute faida za vitu vya kidunia. Juhudi zenu kubwa zisiwe kwa ajili ya kujipatia vitu kwa ajili ya maisha yalipo sasa, bali tafuteni chakula cha kiroho, na ile hekima itakayodumu hata kwa uzima wa milele. Hivi vinaweza kutolewa na Mwana wa Mungu tu; "kwa sababu huyo ndiye aliyetiwa muhuri na Baba, yaani, Mungu."

Kwa muda fulani hamu ya wasikilizaji iliamshwa. Waliuliza kwa mshangao, "Tufanyeje ili tupate kuzitenda kazi za Mungu?" Walikuwa wamefanya matendo mengi na magumu ili kujithibitisha mbele za Mungu; na walikuwa tayari kusikia habari ya maadhimisho yoyote mapya ambayo yangewahesabia wema mkubwa zaidi. Swali lao lilikuwa na maana kwamba, Tufanye nini ili tuistahili mbingu? Tunatakiwa kulipa gharama gani ili kuyapata maisha yajayo?

"Yesu akajibu, akawaambia, Hii ndiyo kazi ya Mungu, mmwamini yeye aliyetumwa na yeye." Gharama ya mbinguni ni Yesu. Njia ya kwenda mbinguni ni kupitia imani kwake "Mwana-kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu." Yohana 1:29.

Lakini watu hawakukubali kupokea kauli hii ya ukweli wa kimbingu. Yesu alikuwa amefanya kazi ile ile ambayo ilitabiriwa na unabii kwamba angeifanya; lakini hawakuwa wameshuhudia kile ambacho matarajio yao ya kibinafsi yalikuwa yanatarajia kwamba ndivyo kazi yake ingekuwa. Kweli Kristo alikuwa amepata kuwalisha makutano kwa mikate ya shayiri; lakini mnamo siku za Musa wana wa Israeli walikuwa wamelishwa mana kwa miaka arobaini, na miujiza mingine mikubwa zaidi ilikuwa inatarajiwa kwamba itendwe na Masihi. Mioyo yao isiyoridhika ilihoji kwamba, ikiwa Yesu alikuwa na uwezo wa kufanya matendo ya ajabu kama walivyokuwa wameshuhudia, kwa nini hakuwapa watu wake wote afya, nguvu, na utajiri, kuwaweka huru kutokana na watesi wao waliowaonea, na kuwatawaza katika madaraka na heshima? Ile hali ya Yeye kudai kuwa ni Aliyetumwa na Mungu, lakini bado akakataa kuwa mfalme wa Israeli, ilikuwa ni fumbo ambalo hawakuweza kulipambanua. Kukataa kwake kulitafsiriwa vibaya. Wengi walihitimisha kwamba hakuthubutu kutaka kutimiza madai yake kwa sababu Yeye mwenyewe alikuwa na mashaka na kazi yake kama ilikuwa na sifa za kimbingu. Kwa njia hiyo wakafungua mioyo yao kupokea kutokuamini, na mbegu ambayo Shetani alikuwa amepanda ikazaa matunda ya aina yake, katika kuelewa isivyo sahihi na kwa makosa.

Sasa, katika hali ya nusu ya dhihaka, rabi mmoja alimwuliza, "Unafanya ishara gani basi, ili tuione tukakuamini? Unatenda kazi gani? Baba zetu waliila mana jangwani kama vile ilivyoandikwa, Aliwapa chakula cha mbinguni ili wale."

Wayahudi walimheshimu Musa kama mtoaji wa mana, wakielekeza sifa kwa chombo tu, wakipoteza hali ya kumwona Yeye aliyewezesha kazi ile kufanyika. Baba zao walikuwa wamemnung'unikia Musa, na walikuwa wameona mashaka na kukana kazi yake ya kimbingu. Sasa kwa namna ile ile **(386)** watoto walimkataa Yeye aliyeleta ujumbe wa Mungu kwao. "Yesu akawaambia, Amin, amin, nawaambieni, Siye Musa aliyewapa chakula kile cha mbinguni." Mtoaji wa mana alikuwa amesimama miongoni mwao. Ni Kristo mwenyewe aliyekuwa amewaongoza Waebrania katika jangwa, na kila siku alikuwa amewalisha kwa mkate kutoka mbinguni. Chakula kile kilikuwa ni mfano wa mkate halisi utokao mbinguni. Roho ile iletayo uzima, inayotiririka kutoka katika utimilifu wa Mungu, ndiyo mana ya kweli. Yesu alisema, "Chakula cha Mungu ni kile kishukacho kutoka mbinguni na kuupa ulimwengu uzima." Yohana 6:33.

Wakiwa bado wanafikiri kwamba Yesu alikuwa anaongelea chakula cha kawaida cha kimwili, baadhi ya wasikilizaji wake walisema, "Bwana, sikuzote utupe chakula hiki." Hapo ndipo Yesu akasema wazi wazi: "Mimi ndimi chakula cha uzima."

Lugha ya mfano ambayo Kristo alikuwa ametumia ilikuwa inaeleweka kwa Wayahudi. Akivuviwa na Roho Mtakatifu, Musa alikuwa amesema, "Mwanadamu haishi kwa mkate tu, bali huishi kwa kila litokalo katika kinywa cha Bwana." Na nabii Yeremia alikuwa ameandika kwamba, "Maneno yako yalionekana, nami nikayala; na maneno yako yalikuwa ni furaha kwangu, na shangwe ya moyo wangu." Deut. 8:3; Jer. 15:16. Hata marabi wenyewe walikuwa na msemo kwamba, kula mkate, katika umuhimu wake wa kiroho, ilikuwa ni kujifunza sheria na kutenda matendo mema; na ilikuwa imesemwa mara kwa mara kwamba wakati wa kuja kwa Masihi Isareli wote watalishwa. Mafundisho ya unabii yaliyafanya wazi yale mafundisho ya kina ya kiroho yaliyokuwa katika mwujiza wa mikate. Kristo alikuwa anataka afunue fundisho hili kwa wasikilizaji wake wale waliokuwa katika sinagogi. Ikiwa wangekuwa wameelewa Maandiko, wangekuwa wameelewa maneno yake wakati aliposema kwamba, "Mimi ndimi chakula cha uzima." Siku moja tu iliyokuwa imepita, umati ule mkubwa wa watu, uliokuwa unazimia kwa njaa, ulikuwa umelishwa kwa mkate aliokuwa ametoa. Kama vile ambavyo walikuwa wamepata nguvu za mwili na kiburudisho kutokana na mkate ule, ndivyo pia kutokana na Kristo wangepata nguvu za kiroho zielekezazo katika uzima wa milele. "Yeye ajaye kwangu hataona njaa kabisa, naye aniaminiye hataona kiu kamwe," alisema. Lakini aliongeza kwamba, "Mmeniona wala hamwamini."

Walikuwa wamemwona Kristo kwa kushuhudiwa na Roho Mtakatifu, kwa mafunuo ya Mungu mioyoni mwao. Ushahidi ulio hai wa uweza wake ulikuwa mbele yao siku baada ya siku, lakini bado walidai ishara nyingine. Ikiwa hii ingefanywa kwao wangeendelea kubaki katika hali ya kutoamini kama walivyokuwa kabla. Ikiwa hawakushawishika kwa kile walichokuwa wameona na kusikia, kuwaonyesha matendo ya ajabu mengine zaidi ingekuwa kazi bure. Hali ya kutokuamini itaendelea kupata udhuru wa sababu ya kuwa na mashaka, na itapatiwa sababu zinazoonekana kuwa na ushahidi ulio chanya.

Kwa mara nyingine tena Kristo alinena na mioyo ile misumbufu. "Yeyote ajaye **(387)** kwangu sitamtupa nje kamwe." Alisema kwamba wote waliompokea kwa imani wangekuwa na uzima wa milele. Hakuna hata mmoja ambye angepotea. Hakuna sababu ya Mafarisayo na Masadukayo kubishana kuhusu hatima ya maisha yajayo. Hakuna haja tena ya watu kuomboleza pasipo matumaini kuhusu watu wao wanaokufa. "Kwa kuwa mapenzi yake Baba yangu ni haya, ya kwamba kila amtazamaye Mwana na kumwamini yeye, awe na uzima wa milele; nami nitamfufua siku ya mwisho."

Lakini viongozi wa watu walichukizwa, "wakasema, Je! Huyu siye Yesu, mwana wa Yusufu, ambaye twamjua babaye na mamaye? Sasa asemaje huyu, Nimeshuka kutoka mbinguni?" Walijaribu kuamsha mawazo potofu kwa kuongelea kwa kejeli asili ya hali ya chini ya Yesu. Walidhihaki kwa chuki maisha yake kama mtu wa kazi za sulubu wa kule Galilaya, na wakaielezea familia yake kama ya kimaskini na ya hali ya chini. Walisema kwamba, Madai ya huyu seremala asiye na elimu hayakustahili kuvuta hata usikivu wao. Na kuhusu ajabu ya kuzaliwa kwake walikejeli kwamba alikuwa mtu ambaye anatiliwa mashaka kuhusu wazazi wake, wakiionyesha ile hali ya kibinadamu ya kuzaliwa kwake kama dosari katika historia ya maisha yake.

Yesu hakujaribu kueleza fumbo la kuzaliwa kwake. Hakujibu swali lolote lililohusu kushuka kwake kutoka mbinguni, kama vile ambavyo hakuwa amejibu maswali yaliyohusu vile alivyoivuka bahari. Hakuelekeza mawazo ya watu katika miujiza iliyohusu maisha yake. Kwa kupenda kwake alikuwa amejifanya mtu asiyeheshimika, na akiwa amejivika namna ya kuwa mtumwa. Lakini maneno na matendo yake yalidhihirisha sifa yake. Wote waliokuwa na mioyo iliyo wazi kuangaziwa na nuru ya kimbingu ndani yake walimgundua "Mwana pekee atokaye kwa Baba; amejaa neema na kweli." Yohana 1:14.

Udhalimu wa Mafarisayo ulijikita kwa kina zaidi kuliko kile kulichoonyeshwa na maswali yao; ulikuwa na mizizi yake katika ukaidi wa mioyo yao. Kila neno na tendo la Yesu liliamsha upinzani ndani yao; maana roho waliyokuwa nayo haikuweza kupata majibu sahihi ndani yake.

"Hakuna mtu awezaye kuja kwangu, asipovutwa na Baba aliyenipeleka; nami nitamfufua siku ya mwisho. Imeandikwa katika manabii, Na wote watakuwa wamefundishwa na Mungu. Basi kila aliyesikia na kujifunza kwa Baba huja kwangu." Hakuna mtu atakayepata kuja kwa Kristo, isipokuwa wale wanaouitikia mvuto wa pendo la Baba. Lakini Mungu anaivuta mioyo yote kwake, na ni wale tu wanaopinga kuvutwa naye ndio wanaokataa kuja kwa Kristo.

Katika yale maneno kwamba, "Watakuwa wamefundishwa na Mungu," Yesu alirejea katika unabii wa Isaya: "Na watoto wako wote watafundishwa na Bwana; na amani ya watoto wako itakuwa nyingi." Isaya 54:13. Wayahudi **(388)** walilihusisha andiko hili na wao wenyewe. Walikuwa wakijidai kwamba Mungu ndiye mwalimu wao. Lakini Yesu aliwaonyesha jinsi madai yao yalivyokuwa bure; maana alisema, "Basi kila aliyesikia na kujifunza kwa Baba huja kwangu." Ni kupitia Kristo tu ndipo wangeweza kupata kumjua Baba. Mwanadamu asingeweza kustahimili mwonekano wa utukufu wake. Waliokuwa wamejifunza kuhusu Mungu walikuwa wameisikiliza sauti ya Mwana wake, na katika Yesu wa Nazareti wangeweza kumwona Yeye ambaye amemtangaza Baba kupitia vitu vya asili na ufunuo.

"Amin, amin, nawaambia, Yeye aaminiye yuna uzima wa milele." Kupitia kwa Yohana aliyependwa, aliyeyasikia maneno haya, Roho Mtakatifu anayatangazia makanisa akisema, "Na huu ndio ushuhuda, ya kwamba Mungu alitupa uzima wa milele; na uzima huu umo katika Mwanawe. Yeye aliye naye Mwana, anao huo uzima." 1 Yohana 5:11, 12. Na Yesu alisema, "Nitamfufua siku ya mwisho." Kristo alikuwa mwili mmoja na sisi, ili ya kwamba tupate kuwa roho moja na Yeye. Ni kwa nguvu ya mwunganiko huu kwamba tutafufuka kutoka kaburini, - si kwa ajili ya udhihirisho wa uweza wa Kristo tu, bali kwa kuwa maisha yake yamekuwa yetu kwa imani. Wale wanaomwona Yesu katika tabia yake halisi, na kumpokea moyoni, wanao uzima wa milele. Kristo anakaa ndani yetu kwa njia ya Roho; na Roho wa Mungu, apokelewaye moyoni kwa imani, ndiye mwanzo wa uzima wa milele.

Watu walikuwa wamemrejesha Kristo kwenye mana iliyoliwa na mababa zao kule jangwani, kama vile kutolewa kwa chakula kile kulikuwa mwujiza mkuu zaidi kuliko ule aliokuwa ametenda; lakini anaonyesha jinsi zawadi ile ilivyo ndogo isiyotosheleza ikilinganishwa na mibaraka aliyokuja kutoa. Mana ile iliweza kukidhi mahitaji ya maisha ya duniani hapa tu; haikuwakinga na ujio wa kifo, wala kuwahakikishia hali ya kutokufa; bali mkate wa

mbinguni ungenawirisha roho kwa ajili ya uzima wa milele. Mwokozi alisema, "Mimi ndimi chakula cha uzima. Baba zenu waliila mana jangwani; wakafa. Hiki ni chakula kishukacho kutoka mbinguni, kwamba mtu akile wala asife. Mimi ndimi chakula chenye uzima kilichoshuka kutoka mbinguni; mtu akila chakula hiki, ataishi milele." Katika lugha hii ya alama Kristo sasa anaongeza kitu kingine. Ni kwa njia ya kufa tu ndipo angeweza kuwapa wanadamu uzima, na katika maneno yanayofuata anaelekeza katika kifo chake kama njia ya wokovu. Anasema, "Na chakula nitakachotoa mimi ni mwili wangu, kwa ajili ya uzima wa ulimwengu."

Wayahudi walikuwa wanakaribia kusherehekea Pasaka kule Yerusalemu, katika kukumbuka usiku wa kukombolewa kwa Israeli, wakati malaika aharibuye alipozipiga nyumba za Misri. Katika mwana-kondoo wa pasaka Mungu aliwataka **(389)** wamwone Mwana-kondoo wa Mungu, na kwa kupitia alama hiyo wampokee Yeye aliyejitoa kwa ajili ya uzima wa ulimwengu. Lakini Wayahudi walikuwa wameifanya alama kuwa ndiyo yenye umuhimu wote, wakaacha kuelewa umuhimu wake. Hawakuuona mwili wa Bwana. Ukweli ule ule uliowakilishwa kwa alama ya ibada ya pasaka ulifundishwa katika maneno ya Yesu. Lakini bado haukuonekana.

Sasa marabi waliuliza kwa mshangao na hasira, "Awezaje mtu huyu kutupa sisi mwili wake ili tuule?" Waliyafanya maneno yake yaeleweke kwa maana yake ya kawaida kama vile ilivyokuwa kwa Nikodemo alipouliza kwamba, "Awezaje mtu kuzaliwa, akiwa mzee?" Yohana 3:4. Kwa kiasi fulani waliipambanua maana ya Yesu, lakini hawakuwa na utashi wa kuikubali. Kwa kuyafanya maneno yake yawe na maana tofauti, walitarajia kuwakoroga watu ili wawe kinyume chake.

Kristo hakupunguza nafasi ya alama ile ya mfano iliyomwakilisha. Aliurudia ukweli ule lakini kwa lugha yenye nguvu zaidi akisema: "Amin, amin, nawaambieni, Msipoula mwili wake Mwana wa Adamu na kuinywa damu yake, hamna uzima ndani yenu. Aulaye mwili wangu na kuinywa damu yangu anao uzima wa milele; nami nitamfufua siku ya mwisho. Kwa maana mwili wangu ni chakula cha kweli, na damu yangu ni kinywaji cha kweli. Aulaye mwili wangu na kuinywa damu yangu hukaa ndani yangu, nami hukaa ndani yake."

Kuula mwili wake na kuinywa damu yake ni kumpokea Yeye kama Mwokozi, tukiamini kwamba anatusamehe dhambi zetu, na ya kwamba tu kamili ndani yake. Ni kwa kuliangalia pendo lake, kwa kukaa katika hilo, kwa kulinywa hilo, ili tupate kuwa washiriki wa namna alivyo. Lazima vile chakula kilivyo katika mwili ndivyo Kristo awe katika moyo. Chakula hakiwezi kutufaa isipokuwa hadi tukile, mpaka kiwe sehemu ya sisi. Vivyo hivyo Kristo hana thamani kwetu ikiwa hatumjui kama Mwokozi wetu binafsi. Kuyajua mambo kwa nadharia hakutatufaa lolote jema. Lazima tumle, tumpokee moyoni, ili kwamba maisha yake yawe maisha yetu.

Lakini hata lugha hizi za alama zinashindwa kuwasilisha upendeleo wa uhusiano kati ya mtu aaminiye na Kristo. Yesu alisema, "Kama vile Baba aliye hai alivyonituma mimi, nami ni hai kwa Baba; kadhalika naye mwenye kunila atakuwa hai kwa mimi." Kama vile Mwana wa Mungu alivyoishi kwa imani katika Baba, ndivyo nasi tunavyopaswa kuishi kwa imani katika Kristo. Yesu alikuwa amejisalimisha kikamilifu katika mapenzi ya Mungu kiasi kwamba Baba peke yake ndiye aliyedhihirika katika maisha yake. Ingawa alijaribiwa katika maeneo yote kama sisi, alisimama mbele ya ulimwengu bila mawaa ya uchafu uliomzunguka. Hivyo nasi pia yatupasa kushinda kama Kristo alivyoshinda.

Je, wewe ni mfuasi wa Kristo? Basi yote yaliyoandikwa kuhusu maisha ya kiroho yameandikwa kwa ajili yako, na yanawezekana kwa njia ya wewe kujiunganisha **(390)** na Yesu. Je, ari yako imepungua? Upendo wako wa kwanza umepoa? Pokea tena upendo utolewao na Kristo. Kula mwili wake, kunywa damu yake, nawe utakuwa kitu kimoja na Baba pamoja na Mwana.

Wayahudi wasioamini walikataa kuona kitu katika maneno ya Yesu isipokuwa maana ya kawaida ya maneno yake. Kwa sheria ya kidini walikatazwa kuonja damu, na sasa waliitafsiri lugha ya Kristo kama usemi usioheshimu mambo ya dini, na walibishana wao kwa wao kuhusu hilo. Hata wengi miongoni mwa wanafunzi wake walisema, "Neno hili ni gumu, ni nani awezaye kulisikia?"

Mwokozi aliwajibu akisema: "Je! Neno hili linawakwaza? Itakuwaje basi, mmwonapo Mwana wa Adamu akipaa huko alikokuwako kwanza? Roho ndiyo itiayo uzima, mwili haufai kitu; maneno hayo niliyowaambia ni roho, tena ni uzima."

Uzima wa Kristo uletao uzima kwa ulimwengu uko katika neno lake. Yesu aliponya magonjwa na kutoa pepo kwa neno; kwa neno lake alituliza bahari, na kufufua waliokufa; na watu walitoa ushuhuda kwamba neno lake lilikuwa na nguvu. Alitamka neno la Mungu, kama alivyokuwa ametamka kupitia manabii na walimu wa kipindi cha Agano la Kale. Biblia yote ni udhihirisho wa Kristo, na Kristo alitaka kuisimika imani ya wafuasi wake katika neno. Wakati ambapo uwepo wake wa kimwili ungeondolewa, lazima neno ndilo liwe chanzo chao cha uweza. Kama alivyokuwa Bwana wao, walipaswa kuishi "kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu." Mathayo 4:4.

Kama vile maisha yetu ya kimwili yanavyowezeshwa na chakula, ndivyo maisha yetu ya kiroho yanavyowezeshwa na neno la Mungu. Na kila nafsi inatakiwa ipokee yenyewe uzima kutoka katika neno la Mungu. Kama vile ambavyo tunapaswa kula sisi wenyewe ili kupata lishe mwilini, ndivyo tunavyopaswa kupata neno sisi wenyewe. Hatupaswi kulipata kupitia njia ya akili ya mtu mwingine. Tunahitaji kujifunza Biblia kwa uangalifu, tukimwuliza Mungu kwa msaada wa Roho Mtakatifu, ili ya kwamba tuelewe neno lake. Tunahitaji kuchukua aya moja, na kuelekeza akili katika kazi ya kupata uhakika wa wazo ambalo Mungu ameweka katika aya hiyo kwa ajili yetu. Yatupasa kukaa katika wazo hilo mpaka linapokuwa letu, na mpaka tujue kwamba "hivi ndivyo asemavyo Bwana."

Katika ahadi zake na maonyo yake, Yesu ananilenga mimi. Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, kiasi cha kumtoa Mwana wake wa pekee, ili kwamba mimi kwa kumwamini, nisipotee, bali niwe na uzima wa milele. Uzoefu unaosimuliwa katika neno la Mungu unapaswa kuwa uzoefu wangu. Sala na ahadi, kanuni na maonyo, ni yangu. "Nimesulibiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda, akajitoa nafsi yake **(391)** kwa ajili yangu." Wagalatia 2:20. Kadiri imani inavyopokea na hivyo kujioanisha na kanuni za ukweli, zinakuwa sehemu ya mtu na kuwa nguvu ya msukumo wa maisha. Neno la Mungu, likipokelewa moyoni, linafinyanga mawazo, na kuingia katika kuendeleza tabia.

Kwa kumwangalia Yesu muda wote kwa macho ya imani, tutaimarishwa. Mungu atafanya mafunuo ya thamani mno kwa watu wake wenye nja na kiu. Wataona kwamba Kristo ni Mwokozi wa mtu. Kadiri wanavyokula neno lake, wanalikuta likiwa nguvu na uzima. Neno linaharibu hali ya asili ya kidunia, na huleta maisha mapya katika Kristo Yesu. Roho Mtakatifu huja nafsini akiwa kama Mfariji. Kwa nguvu ya neema yake ibadilishayo, sura ya Mungu huzalishwa ndani ya mwanafunzi; anakuwa kiumbe kipya. Upendo huchukua nafasi mahali pa chuki, na moyo hupokea sura ya uungu. Hii ndiyo maana ya kuishi "kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu." Huku ndiko kuula Mkate ushukao kutoka mbinguni.

Kristo alikuwa ametamka ukweli mtakatifu wa milele kuhusu uhusiano kati yake na wafuasi wake. Alijua tabia ya wale waliodai kuwa ni wanafunzi wake, na maneno yake yaliijaribu imani yao. Alisema kwamba walipaswa kuamini mafundisho yake na kuyafanyia kazi. Wote waliompokea wangekuwa washirika wa vile alivyo, na wangepatana na tabia yake. Jambo hili lilihusisha kuachana na matarajio ya tamaa waliyokuwa nayo. Lilihitaji kujisalimisha kikamilifu kwa Yesu. Waliitwa ili wawe watu wa kujikana nafsi, wapole na wanyenyekevu wa moyo. Lazima watembee katika njia nyembamba iliyopitwa na yule Mtu wa Kalvari, ili wapate kushiriki thawabu ya uzima na utukufu wa mbinguni.

Jaribio lile lilikuwa kubwa mno. Hamu ya wale waliotaka kumchukua kwa nguvu na kumfanya kuwa mfalme ilipoa na kuwa baridi. Walisema kwamba haya mazungumzo yaliyofanyikia katika sinagogi yalikuwa yamefungua macho yao. Sasa hawakuwa watu wa kudanganywa tena. Katika mawazo yao maneno yake yalikuwa uthibitisho wa moja kwa moja kwamba alikuwa siyo Masihi, na ya kwamba hakuna faida ya maisha ya duniani ambayo wangepata kwake. Walikuwa wamekubali uweza wake wa kufanya miujiza; walikuwa na hamu ya kuwekwa huru kutoka katika magonjwa na mateso; lakini wasingekubaliana na maisha yake ya kujikana. Hawakujali ufalme wa kiroho aliokuwa anausema. Wale watu wasiojali, wabinafsi, waliokuwa wamehangaika kumtafuta, hawakumhitaji tena. Kama asingetumia uweza na ushawishi wake kuwapatia uhuru kutoka kwa Warumi, wasingekuwa na haja naye.

Yesu akawaambia wazi wazi kwamba, "Lakini kuna wengine miongoni mwenu wasioamini;" akaongeza kwamba, "Kwa sababu hiyo nimewaambia ya kwamba hakuna mtu awezaye kuja kwangu **(392)** isipokuwa amejaliwa na Baba yangu." Alitamani waelewe kwamba ikiwa hawakuvutwa kwake ni kwa sababu mioyo yao haikufunguliwa kwa Roho Mtakatifu. "Mwanadamu wa tabia ya asili hayapokei mambo ya Roho wa Mungu; maana kwake huyo

ni upuzi, wala hawezi kuyafahamu, kwa kuwa yatambulikana kwa jinsi ya rohoni." 1 Wakorintho 2:14. Nafsi inauona utukufu wa Yesu kwa imani. Utukufu huu umefichwa, mpaka imani iwashwe moyoni kwa njia ya Roho Mtakatifu.

Kwa kule kukemewa kwao hadharani wanafunzi hawa walizidi kutengana na Yesu zaidi. Walichukizwa sana, wakatamani kumjeruhi Mwokozi na kufurahisha chuki ya Mafarisayo, walimgeuzia migongo yao, wakamwacha kwa dharau. Walikuwa wamefanya chaguo lao, - walikuwa wamechukua mwili bila roho, ganda lisilo na kiini. Uamuzi wao ule haukurudishwa nyuma tena baadaye; maana kamwe hawakutembea na Yesu tena.

"Ambaye pepeto lake li mkononi mwake, naye atausafisha sana uwanda wake; na kuikusanya ngano yake ghalani." Mathayo 3:12. Huu ulikuwa mmoja kati ya nyakati za kusafisha. Kwa kutumia maneno ya ukweli, makapi yalikuwa yantenganishwa na ngano. Kwa kuwa hawakuwa na kitu na walikuwa na hali ya kujihesabia haki kiasi kwamba hawkuwa tayari kupokea maonyo, wakiwa watu wenye kupenda ulimwengu sana kiasi cha kutoweza kuyakubali maisha ya kujishusha, wengi waligeuka wakamwacha Yesu. Wengi bado wanafanya kitu kile kile. Watu wanajaribiwa leo kama ilivyokuwa kwa wale wanafunzi katika sinagogi la kule Kapernaumu. Pindi ukweli unapoletwa mahali pake mioyoni mwao, wanaona kwamba maisha yao hayaendi kwa kupatana na mapenzi ya Mungu. Wanaona hitaji la badiliko la jumla ndani yao; lakini hawako tayari kuifanya kazi ya kujikana. Kwa hiyo wanakuwa na hasira dhambi zao zinapowekwa wazi. Wanaondoka wakiwa wamekwazwa, vile vile kama wanafunzi wale walivyomwacha Yesu, wakinung'unika kwamba, "Neno hili ni gumu, ni nani awezaye kulisikia?"

Kuwasifu na kuwapongeza kunakuwa jambo la kufurahisha masikio yao; lakini ukweli haupendwi; hawawezi kuusikia. Wakati umati wa watu unapokuwepo, na makutano wanapolishwa, na milio ya tarumbeta ikasikika, sauti zao zinainuliwa juu zikisifu; lakini wakati Roho wa Mungu apelelezaye anapoifunua dhambi yao, na kuwahimiza kuiacha, wanaugeuzia ukweli migongo yao, na hawatembei tena na Yesu.

Wakati wale wanafunzi ambao hawakuridhishwa walipogeuka na kumwacha Kristo, roho iliyo tofauti ilichukua utawala kwao. Katika Yeye waliyekuwa wamemwona akiwa na mvuto kwao hawakuona tena kitu cha kuvutia. Walitafuta kwenda kwa adui zake maana waliona hali ya kupatana na roho na matendo yao hao. Waliyatafsiri maneno yake vibaya, wakaziona kauli zake kuwa ni za uongo, na kupuuza mitazamo yake. Waliimarisha njia yao kwa kukusanya kila kitu ambacho kingeweza **(393)** kutumika kumpinga; na hasira iliyokuwepo iliamshwa zaidi na habari hizo za uongo kiasi kwamba maisha yake yalikuwa hatarini.

Habari zilienea haraka kwamba Yesu mwenyewe alikiri kwamba hakuwa Masihi. Na kwa hiyo kule Galilaya mkondo wa hisia za watu uligeuzwa na kumpinga, kama vile ilivyokuwa kule Uyahudi mwaka mmoja uliokuwa umepita. Ole kwa Israeli! Walimkataa Mwokozi wao, kwa kuwa walimtaka mshindi wa vita ambaye angewapatia mamlaka ya kidunia. Walitaka chakula kiharibikacho, na wala si kile kidumucho kwa uzima wa milele.

Kwa moyo wa huzuni Yesu aliwaona watu wale waliokuwa wanafunzi wake wakiondoka kwake, aliye Uzima na Nuru ya wanadamu. Hali ya kuona kwamba hawakujali huruma yake, hakulipwa kwa upendo wake, rehema yake ikiwa imepuuzwa, wokovu wake ukiwa umekataliwa, ilimjaza huzuni isiyosemekana. Ni mambo kama haya ambayo yalimfanya kuwa mtu wa huzuni nyingi, ajuaye sikitiko.

Pasipo kujaribu kuwazuia wale waliokuwa wanaondoka, Yesu aliwageukia wale kumi na wawili na kuwauliza, "Je! Ninyi nanyi mwataka kuondoka?"

Petro akajibu kwa kukuuliza, "Bwana! Twende kwa nani?" "Wewe unayo maneno ya uzima wa milele." "Nasi tumesadiki, tena tumejua, ya kuwa wewe ndiwe Mtakatifu wa Mungu."

"Twende kwa nani?" Walimu wa Israeli walikuwa watumwa wa kushika desturi na taratibu za kidini. Mafarisayo na Masadukayo walikuwa katika upinzani wa muda wote. Kumwacha Yesu kungekuwa ni kuangukia miongoni mwa watu hawa wanaoshika taratibu kwa ajili ya desturi na maadhimisho ya kidini, tena watu wenye tamaa waliojitafutia sifa zao. Wanafunzi wale walikuwa wamejipatia amani na furaha zaidi tangu pale walipokuwa wamemkubali Kristo kuliko wakati wa maisha yao yote ya kabla. Wangewezaje kurudi kwa wale waliomdharau na kumfanyia ukatili huyu Rafiki wa wenye dhambi? Kwa muda mrefu walikuwa wamesubiri Masihi; sasa

alikuwa amekuja, na wasingeweza kugeuka kutoka kwake kwenda kwa wale waliokuwa wakiwinda maisha yake, na walikuwa wamewakatili kwa sababu ya kuwa wafuasi wake.

"Twende kwa nani?" Haiwezi kuwa kutoka kwenye mafundisho ya Kristo, masomo yake ya upendo na rehema, kwenda katika giza na kutokuamini, katika uovu wa dunia. Wakati Mwokozi alipoachwa na watu waliokuwa wameshuhudia matendo yake ya ajabu, Petro alionyesha imani ya wanafunzi wale, - "Wewe ndiwe Mtakatifu wa Mungu." Mawazo yale yale ya kupoteza nanga hii ya mioyo yao iliwajaza hofu na maumivu. Kumkosa Mwokozi ilikuwa ni kusukumwa na mawimbi kwenye bahari yenye giza na dhoruba.

Mengi ya maneno na matendo ya Yesu huonekana kama ya fumbo katika mawazo finyu ya wanadamu, lakini kila neno na tendo lilikuwa na kusudi lake mahsusi katika kazi ya kutukomboa; kila moja lilipimwa ili kuleta matokeo yake tarajiwa. Ikiwa **(394)** tungekuwa na uwezo wa kuelewa makusudi ya Yesu, yote yangeonekana muhimu, kamilifu, na yanayopatana na utume wake.

Wakati sisi hatuwezi kuelewa kazi na njia za Mungu, tunaweza kuona pendo lake kuu, ambalo linaambatana na vile anavyoshughulika na wanadamu. Yeye aishiye karibu na Yesu ataelewa mambo mengi ya kimungu. Atagundua rehema inayofanya makemeo, ile inayojaribu tabia, na kuleta kusudi la moyo kwenye nuru.

Wakati Yesu alipousema ukweli wenye kujaribu uliosababisha wengi wa wanafunzi wake kugeuka nyuma, alijua kile ambacho kingekuwa matokeo ya maneno yake; lakini alikuwa na kusudi jema la kutimiza. Aliona mbele kwamba katika saa ya kujaribiwa kila mmoja wa wanafunzi wake angejaribiwa vikali. Masumbuko yake ya Gethsemani, kusalitiwa kwake na kusulibishwa kwake, kwao yangekuwa majaribu magumu mno. Ikiwa kusingekuwa na jaribio la kutolewa kabla, wengi ambao walikuwa wamesukumwa na mivuto ya ubinafsi wangekuwa wamefungamanishwa nayo. Wakati Bwana wao alipohukumiwa katika ukumbi wa hukumu; wakati makutano waliokuwa wamemtukuza kuwa ni mfalme wao walipopiga kelele za kumkataa na kumtukana; wakati umati wa watu wale waliokuwa wakimdhihaki walipopiga kelele wakisema, "Msulibishe!" – wakati ambapo wangekatishwa tamaa kwa kukosa matarajio yao ya kiulimwengu, watu hawa ambao wanajitafutia manufaa binafsi, watu hawa wangeikana heshima ya Yesu na kuwasababishia wanafunzi wake huzuni chungu ilemeayo moyo, kama nyongeza kwa majonzi yao na kufadhaika kwa kuharibiwa kwa matumaini yao. Wakati wa saa ile ya giza, watu wale waliogeuka na kumwacha wangekuwa mfano mbaya kwa kuondoka na watu wengine pamoja nao. Lakini Yesu alileta huu wakati mgumu kwao ili akiwa bado yupo wazi wazi ana kwa ana apate kuendelea kuimarisha imani ya wafuasi wake wa kweli.

Mwokozi mwenye huruma, ambaye akiwa anajua kwa ukamilifu zahama iliyokuwa inamsubiri, alilainisha njia kwa ajili ya wanafunzi kupita, aliwaandaa kwa ajili ya kujaribiwa, na aliwatia nguvu kwa ajili ya jaribio la mwisho!

## Sura ya 42

# Mapokeo

[Sura hii imejengwa katika Mathayo 15:1-20; Marko 7:1-23.]

Waandishi na Mafarisayo walikuwa wamemwekea Yesu mtego, wakitarajia kumwona kwenye Pasaka. Lakini Yesu, akijua makusudi yao, aliacha kujitokeza katika mkusanyiko huu. "Kisha Mafarisayo, na baadhi ya waandishi waliotoka Yerusalemu, wakakusanyika mbele yake." Kwa kuwa hakwenda kwao, wao walikuja kwake. Kwa muda fulani ilikuwa imeonekana kama vile watu wa Galilaya wangempokea Yesu kama Masihi, na ya kwamba nguvu ya mfumo wa utawala wa eneo lile ungevunjwa. Kazi ya utume ya wale kumi na wawili, ikionyesha kupanuka kwa kazi ya Kristo, na ikiwaleta wanafunzi hao katika hali ya kukabiliana moja kwa moja na marabi, ilikuwa imeamsha upya wivu wa viongozi wa Yerusalemu. Wale wapepelezi ambao waliwatuma kule Kapernaumu katika sehemu ya mwanzoni mwa kazi yake Yesu, ambao walikuwa wamejaribu kumwekea mashtaka ya kuvunja Sabato, walikuwa wamefikia hali ya kuchanganyikiwa; lakini marabi walikuwa wamekusudia kuendelea na azima yao. Sasa wawakilishi wengine walitumwa kwenda kufuatilia mienendo yake, ili kutafuta mashtaka dhidi yake.

Kama ilivyokuwa awali, sababu za malalamiko yao zilikuwa kwenye tabia yake ya kutojali kanuni za mapokeo zilizotwishwa kwenye sheria ya Mungu. Ilidaiwa kuwa hizi ziliwekwa ili kulinda utunzaji wa sheria, lakini zilikuwa zinaheshimiwa kama takatifu kuliko hata sheria yenyewe. Wakati kanuni hizi zilipogongana na amri zilizotolewa Sinai, kipaumbele kiliwekwa kwenye kanuni hizi za marabi.

Miongoni mwa maadhimisho yaliyohimizwa sana ilikuwemo ile ya usafi. Tendo la kupuuza desturi zilizotakiwa kufuatwa kabla ya kula **(396)** ilihesabiwa kama dhambi ya kutisha, iliyostahili kuadhibiwa kote katika ulimwengu huu na ule ujao; na ilichukuliwa kuwa ni tendo jema kumwangamiza mvunjaji wa sheria hiyo.

Taratibu zilizohusu mambo ya utakaso hazikuwa na idadi. Ingekuwa nadra sana kwa kipindi cha maisha ya mtu kutosha kujifunza taratibu zile. Maisha ya watu waliojaribu kuyashika matakwa ya marabi yalikuwa ni mapambano ya muda wote dhidi ya maadhimisho ya kuondokana na unajisi, marudio ya mizunguko ya kunawa na kutakasika. Wakati watu wakiwa wamegubikwa na mambo haya yaliyo madogo sana, na maadhimisho ambayo Mungu hakudai yafanywe, mawazo yao yaligeuziwa mbali na misingi mikuu ya sheria.

Kristo na wanafunzi wake walikuwa hawafuati matendo haya ya maadhimisho ya utakaso, na wale wapelelezi wakaona kwamba vitendo hivi vya kupuuza haya viwe sababu ya mashtaka yao. Hata hivyo hawakumkabili Kristo moja kwa moja, bali walimjia kwa namna ya kuwapinga wanafunzi wake. Wakiwa mbele ya umati wa watu, walisema, "Mbona wanafunzi wako huyahalifu mapokeo ya wazee, kwa maana hawanawi mikono walapo chakula."

Kila wakati ujumbe wa ukweli unapokuja kwa nguvu iliyo maalum moyoni mwa mtu, Shetani huwahamasisha mawakala wake kuanzisha upinzani katika mambo fulani-fulani yaliyo madogo. Kwa njia hiyo huyavuta mawazo na kuyaondoa katika jambo lenyewe lililo muhimu. Kila wakati kazi nzuri inapoanzishwa, kunakuwa na wapinzani walio tayari kuleta ubishi kuhusu miundo au taratibu rasmi za kiufundi, ili kuyaondoa mawazo ya watu kwenye ukweli ulio hai. Wakati inapotokea kwamba Mungu anataka kufanya kazi kwa namna iliyo ya pekee kwa ajili ya watu, hebu watu wasishawishi kuwepo kwa hali ya mabishano ambayo huishia kuleta uharibifu tu. Maswali ambayo yanahusika zaidi kwetu ni haya, Je, naamini katika imani iokoayo ya Mwana wa Mungu? Je, maisha yangu yanapatana na sheria ya kimbingu? "Amwaminiye Mwana yuna uzima wa milele; asiyemwamini Mwana hataona uzima, bali ghadhabu ya Mungu inamkalia." "Na katika hili twajua ya kuwa tumemjua yeye, ikiwa tunashika amri zake." Yohana 3:36; 1 Yohana 2:3.

Yesu hakufanya jambo lolote kujaribu kujitetea au kuwatetea wanafunzi wake. Hakurejelea katika mashtaka waliyomshtaki, bali aliendelea kuwaonyesha roho iliyowasukuma wapinzani hawa wanaojali maadhimisho ya desturi za kidini. Aliwapa mfano wa kile walichokuwa wakirudia-rudia kufanya, na walichokuwa wamefanya hata muda mfupi kabla ya kuja kumtafuta. Alisema, "Vema! Mwaikataa amri ya Mungu mpate kuyashika mapokeo yenu. Maana Musa alisema, Waheshimu baba yako na mama yako, na, Amtukanaye babaye au mamaye

kufa na afe. Bali ninyi husema, Mtu akimwambia babaye au mamaye, Ni Korbani, yaani, wakfu, kitu changu chochote kikupasacho kufaidiwa nacho, huwa basi; wala hammruhusu baada ya hayo kumtendea neno babaye au mamaye." Waliweka kando amri ya tano kama vile **(397)** haina maana, lakini walikuwa makini sana katika kutekeleza mapokeo ya wazee. Walifundisha watu kwamba kutoa mali zao hekaluni lilikuwa tendo la wajibu ulio mtakatifu zaidi hata ya kuwasaidia wazazi; na ya kwamba, hata kuwe na uhitaji kiasi gani, tendo la kumpa baba au mama sehemu ya kitu kilichowekwa wakfu kutolewa lilikuwa ni kosa la kutoheshimu vitu vitakatifu. Mtoto asiyetekeleza wajibu wake alikuwa na kazi tu ya kutamka neno "Korbani" kuhusu mali yake, kwa njia hiyo anakuwa ameitoa kwa Mungu, na ingehifadhi kwa ajili ya matumizi yake katika maisha yake ya baadaye, na akiisha kufa mali ile ingepelekwa hekaluni kwa ajili ya matumizi ya hekalu. Kwa njia hiyo alikuwa huru, akiwa hai na hata baada ya kufa, kutowaheshimu wazazi wake na kuwanyang'anya haki yao, kwa kisingizio cha kuitoa kwa Mungu.

Iwe kwa neno au kwa tendo, Yesu hakupunguza jukumu la mtu kutoa sadaka na dhabihu kwa Mungu. Kristo ndiye aliyetoa maelekezo ya sheria kuhusu zaka na dhabihu. Alipokuwa duniani alimkubali yule mwanamke maskini aliyetia katika hazina ya hekalu vyote alivyokuwa navyo. Bali juhudi kubwa ya makuhani na marabi kwa ajili ya Mungu ilikuwa ya kuigiza tu ili kufunika tamaa yao ya kujionyesha. Walikuwa wanadanganya watu. Walikuwa wanabeba mizigo mizito ambayo Mungu hakuwatwisha. Hata wale wanafunzi wa Yesu hawakuwa huru mbali na kongwa ambalo walikuwa wamefungwa na imani potofu waliyorithi pamoja na mamlaka ya marabi. Sasa, kwa kule kuifunua roho halisi ya marabi, Yesu alitaka kuwaweka huru mbali na kifungo cha mapokeo watu wote waliotamani kumtumikia Mungu.

Akiwaambia wapelelezi wale alisema, "Enyi wanafiki, ni vema alivyotabiri Isaya kwa habari zenu, akisema, Watu hawa huniheshimu kwa midomo; Ila mioyo yao iko mbali nami. Nao waniabudu bure, Wakifundisha mafundisho Yaliyo maagizo ya wanadamu." Maneno yale ya Kristo yalikuwa yanautuhumu mfumo wote wa Kifarisayo. Alisema kwamba kitendo cha marabi wale kuweka matakwa yao juu kuliko matakwa ya Mungu walikuwa wamejiweka juu ya Mungu.

Wale wapizani kutoka Yerusalemu walijawa na ghadhabu. Hawakuweza kumshtaki Kristo kwamba ni mvunjaji wa sheria iliyotolewa Sinai, maana alitamka kwa kuitetea dhidi ya mapokeo. Kanuni kuu za sheria, alizokuwa ameonyesha, zilionekana wazi kukinzana na kanuni zile ambazo zilitengenezwa na wanadamu.

Yesu aliwaambia makutano wale, na baadaye wanafunzi wake, kwamba unajisi hautoki nje, bali hutoka ndani. Usafi na uchafu unahusu moyo. Kinachomnajisi mtu ni matendo maovu, maneno maovu, mawazo maovu, uvunjaji wa sheria ya Mungu, wala si kuacha kufanya mambo ya nje, maadhimisho yaliyowekwa na wanadamu.

**(398)** Wanafunzi wale waligundua ghadhabu ile ya wapelelezi pindi mafundisho yao ya uongo yalipowekwa wazi. Waliona nyuso za hasira, na walisikia maneno yaliyokatika-katika ya kuashiria kutoridhishwa na nia ya kulipiza kisasi. Wakisahau jinsi ambavyo Kristo alionyesha viashiria kwamba ana uwezo wa kusoma mioyo kama vile kitabu kilicho wazi, walimweleza kuhusu madhara ya maneno yake. Wakitarajia kwamba anaweza kufanya suluhu na maafisa wale walioghadhibika, walimwambia Yesu hivi, "Wajua ya kuwa Mafarisayo walipolisikia neno lile walichukizwa?"

Yeye alijibu, "Kila pando asilolipanda Baba yangu wa mbinguni litang'olewa." Desturi na mapokeo vilivyothaminiwa sana na marabi vilikuwa vya ulimwengu huu, si vya kutoka mbinguni. Hata viwe na mamlaka kwa watu kiasi gani, haviwezi kustahimili kupita katika jaribio la Mungu. Kila ubunifu wa mwanadamu unaochukua nafasi ya amri za Mungu utaonekana usiostahili siku ile wakati ambapo "Mungu ataleta hukumuni kila kazi, pamoja na kila neno la siri, likiwa jema au likiwa baya." Mhubiri 12:14.

Kuweka mafundisho ya wanadamu mahali pa amri za Mungu si kwamba kumekoma. Hata miongoni mwa Wakristo kuna mabunifu na mazoea ambayo hayana msingi ulio mzuri zaidi ya mapokeo ya mababa. Mabunifu hayo, ambayo yameanzishwa na mamlaka ya wanadamu, yamechukua nafasi ya yale ya kimbingu. Watu wanang'ang'ania mapokeo yao, na wanaheshimu desturi zao, nao huendeleza chuki dhidi ya wale wanaojitahidi kuwaonyesha makosa yao. Mnamo wakati huu, tunapohimizwa kuzingatia amri za Mungu na imani ya Yesu, tunaona uadui kama ule ule uliodhihirishwa mnamo nyakati za Kristo. Kuhusu masalia wa Mungu imeandikwa

hivi, "Joka akamkasirikia yule mwanamke, akaenda zake afanye vita juu ya wazao wake waliosalia, wazishikao amri za Mungu, na kuwa na ushuhuda wa Yesu." Ufunuo 12:17.

Lakini "kila pando asilolipanda Baba yangu wa mbinguni litang'olewa." Badala ya kusikiliza mamlaka ya kile kinachoitwa mababa wa kanisa, Mungu anatuhimiza tulishike neno la Baba wa milele, Bwana wa mbingu na nchi. Hapa peke yake ndipo penye ukweli ambao haukuchanganywa na makosa. Daudi alisema, "Ninazo akili kuliko wakufunzi wangu wote, Maana shuhuda zako ndizo nizifikirizo. Ninao ufahamu kuliko wazee, Kwa kuwa nimeyashika mausia yako." Zaburi 119:99, 100. Hebu wote wanaokubali mamlaka ya wanadamu, desturi za kanisa, au mapokeo kutoka kwa mababa, wasikie onyo lililotolewa katika maneno ya Kristo, kwamba, "Nao waniabudu bure, wakifundisha mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu."

**Sura ya 43**

# Vikwazo Viletavyo Ubaguzi Vyavunjwa

[Sura hii imejengwa katika Mathayo 15:21-28; Marko 7:24-30.]

Baada ya kukabiliana na Mafarisayo wale, Yesu aliondoka Kapernaumu, naye akishaivuka Galilaya, alienda katika nchi ya milima iliyo katika mipaka ya Foinike. Alipoangalia upande wa magharibi, aliweza kuona miji ya kale ya Tiro na Sidoni ikiwa katika tambarare kwa chini, pamoja na mahekalu ya kipagani ya miji hiyo, majumba ya kifahari ya watawala wa miji hiyo, na bandari iliyojawa na shughuli za usafirishaji. Kwa mbele kulikuwa na mwonekano wa rangi ya blue wa Bahari ya Mediterania, ambayo juu yake wajumbe wa injili wangepita wakipeleka habari njema katika vituo vya himaya kuu ya ulimwengu. Lakini muda huo ulikuwa haujafika. Kazi iliyokuwa mbele yake sasa ilikuwa ya kuwaanda wanafunzi wake kwa kazi yao. Alikuja katika eneo hili akitarajia kupata mahali pa utulivu ambapo alishindwa kupapata kule Bethsaida. Lakini hili halikuwa kusudi lake pekee la safari yake hii.

"Na tazama, mwanamke Mkananayo wa mipaka ile akatokea, akampazia sauti akisema, Unirehemu, Bwana, Mwana wa Daudi; binti yangu amepagawa sana na pepo." Mathayo 15:22. Watu wa eneo hili walikuwa wa asili ya Kanaani ya zamani. Walikuwa waabudu miungu, na walikuwa wanadharauliwa na kuchukiwa na Wayahudi. Mwanamke huyu aliyekuja kwa Yesu alikuwa wa jamii hiyo. Alikuwa mpagani, na kwa hiyo alikuwa mtu wa kutengwa na mema yale ambayo Wayahudi walikuwa wakiyapata kila siku. Kulikuwa **(400)** na Wayahudi wengi waliokuwa wanaishi miongoni mwa Wafoinike wale, na habari za matendo ya Kristo zilikuwa zimeshapenya hadi katika eneo hili. Baadhi ya watu walikuwa wamepata kusikiliza maneno yake na kushuhudia kazi zake. Mwanamke huyu alikuwa amepata kusikia habari za nabii huyu ambaye, kama alivyosimuliwa, alikuwa anaponya magonjwa ya kila namna. Aliposikia kuhusu uwezo wake, matumaini yalibubujika moyoni mwake. Akisukumwa na upendo wa mama, aliazimia kulifikisha tatizo la binti yake kwa nabii huyo. Ilikuwa azima yake kumleta yule mgonjwa kwa Yesu. Lazima amponye mtoto wake. Alikuwa ametafuta msaada kwa miungu ya kipagani, lakini hakupata mafanikio. Na wakati fulani-fulani alikuwa amejaribiwa kufikiri hivi, Huyu mwalimu wa Kiyahudi anaweza kunifanyia nini huyu? Lakini neno lilikuwa limemjia kwamba, anaponya magonjwa ya kila namna, iwe wale wanaomjia ni matajiri au maskini. Akaamua asipoteze tumaini lake pekee.

Kristo alijua mazingira aliyokuwemo mama yule. Alijua kwamba alikuwa anatafuta kumwona, naye alijiweka katika njia ya yule mama. Kwa kuhudumia huzuni yake, angeweza kutoa fundisho hai alilokuwa amepanga kufundisha. Alikuwa amewaleta wanafunzi wake katika eneo hili kwa ajili ya fundisho hili. Alitaka waone hali ya kutojua iliyopo katika miji na vijiji vilivyo karibu na nchi ya Waisraeli. Watu waliokuwa wamepewa kila fursa ya kuufahamu ukweli walikuwa hawajui mahitaji ya wale waliokuwa karibu yao. Hakuna jitihada zilizofanywa kuwasaidia waliokuwa gizani. Ukuta unaowatenga uliokuwa umejengwa na kiburi cha Wayahudi, uliwafungia hata na wanafunzi wasiwe na huruma kwa ulimwengu wa kipagani. Lakini vizuizi hivi vilikuwa vivunjwe.

Kristo hakujibu ombi la yule mwanamke wakati huo huo. Alimpokea mwakilishi huyu wa jamii iliyodharaulika vile ambavyo Wayahudi wangefanya. Katika hili alitaka wanafunzi wake wapate kuguswa na hali ya kutoonyesha huruma na upendo ambayo ndivyo Wayahudi wangefanya katika hali kama ile, kama inavyoonyeshwa na namna alivyompokea mwanamke yule, na huruma ambayo angependa waionyeshe kwa hali kama ile ya huzuni, kama ilivyoonyeshwa na kile alichofanya baadaye kwa kumpa kile alichoomba.

Lakini ingawa Yesu hakujibu, mwanamke yule hakukata tamaa kuamini. Kadiri Yesu alivyoendelea kwenda, kama vile hamsikii, mwanamke yule aliendelea kumfuata, akiendelea na ombi lake. Kwa kukerwa na usumbufu wa yule mwanamke, wanafunzi walimwomba Yesu amtake aondoke zake. Waliona kwamba Bwana wao hakumjali, na kwa hiyo waliona kwamba itikadi ile ya Wayahudi kuwa dhidi ya Wakaanani ilikuwa inamfurahisha. Lakini mwanamke yule alikuwa anamwomba Mwokozi mwenye huruma, na Yesu alisema, akiwajibu wale Wanafunzi, "Sikutumwa ila kwa kondoo waliopotea wa nyumba **(401)** ya Israeli." Ingawa jibu hili lilionekana kuendana na itikadi ile ya Wayahudi, ndani yake lilikuwa na kemeo kwa wale wanafunzi, ambalo baadaye walilielewa kwamba linawakumbusha kile alichokuwa amewaambia mara kwa mara, - alikuja ulimwenguni kuwaokoa wote ambao wangempokea.

Mwanamke yule aliendelea kusisitiza haja yake kwa dhati zaidi, akiinama miguuni pa Yesu, huku akisema, "Bwana, unisaidie." Yesu, akiendelea kukataa, kulingana na imani ile ya Wayahudi isiyo na hisia ya upendo, alijibu hivi, "Si vema kukitwaa chakula cha watoto na kuwatupia mbwa." Hii ilikuwa namna ya kusema kwamba haikuwa haki kunyang'anya mibaraka iliyoletwa kwa ajili ya watu wa Mungu waliopendelewa na kuwapa wageni na watu waliotengwa na Israeli. Jibu hili lingeweza kumkatisha tamaa kabisa mtu yule aliyekuwa anaomba kwa dhati. Lakini yule mwanamke aliona kwamba fursa yake imekuja. Ndani ya mwonekano wa Yesu wa kukataa, aliona huruma ambayo Yesu hakuweza kuificha. Akasema, "Ndiyo, Bwana, lakini hata mbwa hula makombo yaangukayo mezani pa bwana zao." Wakati watoto wa nyumbani hula mezani pa baba yao, hata mbwa hawaachwi bila kupewa chakula. Wana haki ya kupata makombo yanayoanguka kutoka kwenye meza iliyosheheni chakula. Kwa hiyo kwa kuwa kulikuwa na mibaraka mingi iliyotolewa kwa Israeli, je, hakukuwa pia na mbaraka kwa ajili yake? Alikuwa ametazamwa kama mbwa, na kwa hiyo si angekuwa na haki ya kudai makombo kutoka katika zawadi za Yesu?

Wakati huo ndipo Yesu alikuwa ameondoka tu katika eneo la kazi kwa sababu waandishi na Mafarisayo walikuwa wanawinda uhai wake. Walinung'unika na kulalamika. Walidhihirisha kutokuamini na uadui, na waliukataa wokovu uliotolewa kwao bure. Hapa Kristo anakutana na mtu wa jamii iliyotengwa na kudharauliwa, ambayo haikupendelewa kuwa na nuru ya neno la Mungu; lakini anajitiisha chini ya mvuto wa kimbingu wa Kristo, na anaamini kwamba ana uwezo wa kumpatia kile anachoomba. Anaomba makombo yanayoanguka kutoka mezani pa Bwana. Ikiwa angepata upendeleo kama wa mbwa, yuko tayari achukuliwe kama mbwa. Hana stahili ya kawaida wala ya kidini ya kuhalalisha upande ule aliotaka, na hapo anamkiri Yesu kama Mwokozi, na kumwona kama aliye na uwezo wa kufanya chochote ambacho angemwomba.

Mwokozi ameridhika. Ameijaribu imani ya yule mwanamke kwake. Kwa kushughulika naye, Yesu ameona kwamba yeye aliyekuwa ameonekana kama aliyetengwa na Israeli si mtu wa kutengwa tena, bali ni mtoto nyumbani mwa Mungu. Kwa kuwa ni mtoto ana haki ya kushiriki katika zawadi za Baba. Sasa Yesu anampatia ombi lake, na kumaliza fundisho lake kwa wanafunzi. Akimgeukia kwa mtazamo wa huruma na upendo, Yesu anasema, "Mama, imani yako ni kubwa; **(402)** na iwe kwako kama utakavyo." Tangu saa ile binti yake akapona. Pepo halikumsumbua tena. Mwanamke yule aliondoka, akimkiri Mwokozi wake, na akiwa na furaha ya kupewa sawa na ombi lake.

Huu ndio mwujiza pekee ambao Yesu aliufanya katika safari hii. Alienda katika mipaka ya Tiro na Sidoni kwa ajili ya kufanya tendo hili. Alitamani kumtuliza mwanamke yule mwenye huzuni, na wakati huo huo akiacha mfano wa kazi yake ya rehema kwa mmoja wa watu waliodharauliwa kwa faida ya wanafunzi wake wakati ule ambao asingekuwa pamoja nao. Alitaka kuwaongoza waondoke katika hali ya kuwa katika urasmi wa Kiyahudi ili kuvutwa kuwahudumia wengine mbali na watu wa taifa lao.

Yesu alitaka kufunua siri za kina za ukweli uliofichwa kwa vizazi na vizazi, kuwaonyesha kwamba Mataifa nao ni warithi pamoja na Wayahudi, na washiriki wa ahadi yake iliyo katika Kristo Yesu kwa njia ya Injili. Waefeso 3:6. Wanafunzi walikuwa watu wa kukawia kuelewa ukweli huu, na Mwalimu wa kimbingu aliwapa somo juu ya somo kuhusu ukweli huu. Kwa kutoa thawabu kwa imani ya akida kule Kapernaumu, na kwa kuhubiri injili kwa wakazi wa kule Sikari, alikuwa tayari ameshawapa uthibitisho kwamba Yeye hakukubaliana na tabia ya ubaguzi ya Wayahudi. Lakini Wasamaria walikuwa na ufahamu fulani kuhusu Mungu, na akida alikuwa ameonyesha wema kwa Israeli. Kwa sasa Yesu aliwaleta wanafunzi kukutana na mpagani uso kwa uso, ambaye walimdhania kwamba hana lolote jema lililo zaidi ya wengine wa kwao, kiasi cha kupata upendeleo wa Yesu. Alitaka kutoa mfano wa namna mtu huyo alivyopaswa kutendewa. Wanafunzi wale walikuwa wamefikiri kwamba alitoa vipawa vyake bure kupita kiasi. Alitaka aonyeshe kwamba upendo wake ulikuwa hautegemei sifa za kabila wala taifa.

Wakati aliposema kwamba, "Sikutumwa ila kwa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli," alitamka ukweli, na katika tendo lake lile kwa mwanamke Mkananayo alikuwa anatimiza utume wake. Mwanamke huyu alikuwa mmoja wa kondoo waliopotea anayetakiwa kuokolewa. Kazi hii iliyokuwa inafanywa na Kristo ilikuwa kazi waliyokabidhiwa Wayahudi, lakini wakawa wanaipuuza.

Tukio hili lilifungua mawazo ya wanafunzi kwa uwazi zaidi kwa ajili ya kazi iliyokuwa mbele yao ya kufanya miongoni mwa Mataifa. Waliona eneo pana la kazi yao nje ya Uyahudi. Waliziona roho zenye kujawa na huzuni

isiyoonekana kwa wale waliokuwa wamependelewa kwa kiasi cha juu sana. Miongoni mwa wale ambao wao walifundishwa kuwadharau kulikuwa na watu ambao walikuwa wanahitaji msaada kutoka kwa Mponyaji mkuu, wakiwa na njaa kwa ajili ya nuru ya ukweli, ambayo ilikuwa imetolewa kwa wingi kwa Wayahudi.

Baada ya pale, Wayahudi walipogeuka na kuachana na wanafunzi wale, kwa sababu ya wao kumwita Yesu kuwa ni Mwokozi wa ulimwengu, **(403)** na wakati kifo cha Kristo kilipovunja ukuta unaotenganisha kati ya Myahudi na Mataifa, somo hili, pamoja na masomo mengine kama hilo yaliyoelekeza katika kazi ya injili isiyo na vizuizi vya desturi wala utaifa, lilikuwa na msukumo wenye nguvu kwa wawakilishi wa Kristo, katika kuzielekeza kazi zao.

Matembezi ya Mwokozi kule Foinike na mwujiza uliotendwa kule bado vilikuwa na kusudi jingine pana zaidi. Kazi ile haikufanywa tu kwa ajili ya mwanamke yule aliyekuwa na masikitiko, wala si kwa wanafunzi wake na wale waliopokea huduma za kazi zao tu; bali pia "ili mpate kuamini ya kwamba Yesu ndiye Kristo, Mwana wa Mungu; na kwa kuamini mwe na uzima kwa jina lake." Yohana 20:31. Nguvu zile zile zilizowafungia watu mbali na Kristo miaka elfu moja na mia tisa iliyopita ziko kazini leo. Roho ile iliyojenga ukuta unaotenganisha Wayahudi na Mataifa bado inafanya kazi. Kiburi na majivuno vimejenga kuta ngumu za kutenganisha makundi mbalimbali ya watu. Kristo na kazi yake vimeelezwa vibaya, na makundi ya watu wanajisikia kwamba wamefungiwa mbali na huduma ya injili. Lakini hebu wasijisikie kwamba wamefungiwa mbali kutoka kwa Kristo. Hakuna ukuta ambao mwanadamu au Shetani anaweza kuuinua halafu imani ikashindwa kuupenya.

Kwa imani mwanamke yule wa Foinike alijirusha na kuupita mlima wa vizuizi vilivyokuwa vinawatenga Wayahudi na Mataifa. Akipingana na hali ya kukata tamaa, bila kujali mionekano ambayo ingeweza kumletea mashaka, alitumainia upendo wa Mwokozi. Hivyo ndivyo Kristo anavyotaka tumtumainie. Mibaraka ya wokovu ni kwa kila mtu. Hakuna kitu kingine kinachoweza kumzuia mtu kuwa mshirika wa ahadi za Kristo zinazotolewa na injili isipokuwa uchaguzi wa mtu mwenyewe.

Matabaka ni chukizo kwa Mungu. Yeye hupuuza kila kitu chenye hali hiyo. Machoni pake nafsi za watu wote zina thamani sawa. Yeye "alifanya kila taifa la wanadamu kutoka katika mmoja, wakae juu ya uso wa nchi yote, akiisha kuwawekea nyakati alizoziamuru tangu zamani, na mipaka ya makazi yao; ili wamtafute Mungu, ingawa ni kwa kupapasa-papasa, wakamwone, ijapokuwa hawi mbali na kila mmoja wetu." Bila kubagua kwa kuangalia umri, au cheo, au utaifa, au haki ya kidini, wote wanaalikwa kuja kwake ili wapate kuishi. "Kila amwaminiye hatatahayarika. Kwa maana hakuna tofauti." "Hapana Myahudi wala Myunani. Hapana mtumwa wala huru." "Tajiri na maskini hukutana pamoja; Bwana ndiye aliyewaumba wote wawili." "Maana yeye yule ni Bwana wa wote, mwenye utajiri kwa wote wamwitao. Kwa kuwa, Kila atakayeliitia Jina la Bwana ataokoka." Matendo 17:26, 27; Wagalatia 3:28; Mithali 22:2; Warumia 10:11-13.

## Sura ya 44

# Ishara ya Kweli

[Sura hii imejengwa katika Mathayo 15:29-39; 16:1-12; Marko 7:31-37; 8:1-21.]

"Akatoka tena katika mipaka ya Tiro, akapita katikati ya Sidoni, akaenda mpaka bahari ya Galilaya, kati ya mipaka ya Dekapoli." Marko 7:31.

Katika eneo la Dekapoli ndipo mahali wale wenye pepo wa Genesareti walipoponywa. Hapa ndipo pale ambapo watu walioshtushwa na kuangamizwa kwa nguruwe walipomtaka Yesu aondoke mipakani mwa nchi yao. Lakini walikuwa wamewasikiliza wale wajumbe ambao alikuwa amewaacha kule, na hamu ya watu kutaka kumwona iliamshwa. Sasa alipokuja tena katika eneo hili, umati wa watu ulimkusanyikia, na kiziwi, mwenye kigugumizi aliletwa kwake. Kama ilivyokuwa desturi yake, Yesu hakumponya mtu yule kwa neno tu. Akimpeleka kando ya umati, aliweka vidole vyake masikioni mwake, na akaugusa ulimi wake; na akiwa anatazama mbinguni, aliugua kwa kuwazia masikio yale ambayo yalikuwa hayataki kufunguka ili kuusikia ukweli, na ulimi uliokuwa umekataa kumkiri Mwokozi. Baada ya neno, "Funguka," akapona na kupata uwezo wa kuzungumza, naye, pasipo kujali agizo la kutomwambia mtu yeyote, akatangaza habari za kuponywa kwake.

Yesu akaenda juu mlimani, na makutano wakamjia, wakiwaleta wagonjwa wao, na viwete, na kuwalaza miguuni pake. Aliwaponya wote; na watu wale, vile vile walivyokuwa wapagani, wakamtukuza Mungu wa Israeli. Waliendelea kusongamana kwa Yesu kwa muda wa siku tatu, wakilala usiku mahali pa wazi, na mchana wakisukumana kwa hamu ya kutaka kusikiliza mananeo ya Kristo, na kuona kazi zake. Mwishoni mwa zile siku **(405)** chakula chao kiliisha. Yesu hakutaka kuwaaga waondoke wakiwa na njaa, naye aliwataka wanafunzi wake wawapatie chakula. Kwa mara nyingine tena wanafunzi wale walidhihirisha kutokuamini kwao. Kule Bethsaida walikuwa wameona jinsi kiasi chao kidogo cha chakula kilivyotosha kulisha umati mkubwa wa watu kwa mbaraka wa Kristo; lakini sasa hawakutoa vyote walivyokuwa navyo, na kutumaini kwamba uweza wa Kristoungekizidisha kwa ajiliya umati ule uliokuwa na njaa. Zaidi ya hayo, ni kwamba wale aliowalisha kule Bethsaida walikuwa Wayahudi; hawa wa sasa walikuwa Mataifa na wapagani. Chuki za kibaguzi za Wayahudi zilikuwa bado zina nguvu katika mioyo ya wanafunzi wale, na wakamjibu wakisema, "Je! Ataweza wapi mtu kuwashibisha hawa mikate hapa nyikani?" lakini kwa kuwa watiifu kwa neno lake walimletea kile walichokuwa nacho, - mikate saba na samaki wawaili. Makutano wale wakalishwa, vikabaki vyakula vinavyojaza makanda saba. Watu mia nne, ukiacha wanaume na watoto, waliburudishwa, na Yesu akawaaga kwa moyo wenye furaha.

Halafu alichukua chombo akiwa na wanafunzi wake wakavuka ziwa kwenda Magadani (Magdala), katika mpaka wa kusini wa uwanda wa Genesareti. Roho yake ilikuwa imeburudishwa na imani kubwa ya yule mwanamke wa Kifoinike kule katika mpaka wa Tiro na Sidoni. Wapagani wa kule Dekapoli nao walikuwa wamempokea kwa furaha. Sasa alipofika tena katika ardhi ya Galilaya, mahali ambapo uwezo wake ulikuwa umedhihirishwa waziwazi zaidi, mahali ambapo kazi zake nyingi za rehema zilikuwa zimefanyika, na mahali ambapo mafundisho yake yametolewa, alikutana na chuki ya kutokuamini.

Wawakilishi wa Mafarisayo walikuwa wameungana na wawakilishi wa Masadukayo walio matajiri na wenye kuheshimiwa, waliokuwa upande wa waandishi, wenye ushupavu, na watu wakubwa katika taifa. Madhehebu haya mawili yalikuwa katika uadui mkubwa sana. Masadukayo walifanikiwa kupata kuungwa mkono na mamlaka ya utawala ili waweze kudumisha nafasi na mamlaka yao. Kwa upande mwingine, Mafarisayo wao waliendelea kukuza chuki ya watu dhidi ya Warumi, wakisubiri wakati watakapolitua chini kongwa la watawala hao. Lakini sasa Mafarisayo na Masadukayo waliungana katika kumpinga Kristo. Vitu vifananavyo hutafutana; na uovu, popote ulipo, huungana na uovu mwingine kwa ajili ya kuharibu jambo jema.

**(406)** Sasa Mafarisayo na Masadukayo walikuja kwa Kristo, wakiomba kupata ishara kutoka mbinguni. Wakati Israeli ilipoenda kupigana vita na Wakanaani kule Bethhoron mnamo siku za Yoshua, jua lilisimama kwa amri ya kiongozi mpaka ushindi ulipopatikana; na maajabu mengi kama hayo yalidhihirishwa katika historia yao. Ishara fulani kama hizo ilitakiwa kwa Yesu. Lakini ishara hazikuwa ndiyo mahitaji ya Wayahudi. Hakuna udhihirisho wa nje tu ambao ungewafaa kitu. Walichohitaji siyo kueleweshwa kiakili, bali kufanywa upya kiroho.

Yesu alisema, "Enyi wanafiki, mwajua kuutambua uso wa mbingu;" - kwa kufuatilia hali ya anga waliweza kutabiri hali ya hewa, - "lakini, je! Ishara za zamani hizi hamwezi kuzitambua?" Maneno yenyewe ya Kristo, yaliyosemwa kwa nguvu ya Roho Mtakatifu iliyowasadikisha kuhusu dhambi, yalikuwa ni ishara ambayo Mungu alikuwa amewapatia kwa ajili ya wokovu wao. Na ishara kutoka mbinguni zilikuwa zimetolewa kuthibitisha kazi ya Kristo. Wimbo wa malaika ulioimbwa kwa wale wachungaji, nyota iliyowaongoza mamajusi, yule hua na sauti iliyotoka mbinguni wakati wa kubatizwa kwake, vilikuwa ni ushuhuda kwa ajili yake.

"Akaugua rohoni mwake, akasema, Mbona kizazi hiki chatafuta ishara?" "Wala hakitapewa ishara, isipokuwa ishara ya Yona." Kama vile Yona alivyokuwa tumboni mwa nyangumi kwa siku tatu mchana na usiku, kwa muda kama huo huo Kristo angekuwa "katika moyo wa nchi." Na kama vile kuhubiri kwa Yona kulivyokuwa ishara kwa Waninawi, ndivyo Kristo alivyokuwa ishara kwa kizazi chake. Lakini ona jinsi upokeaji wa neno unavyokinzana! Twale watu wa mji wa kipagani walitetemeka waliposikia onyo kutoka kwa Mungu. Wafalme wa wakuu walijishusha, watu wa tabaka la juu na wale wa chini kwa pamoja walimlilia Mungu wa mbinguni, nao wakapewa rehema yake. Yesu alisema, "Watu wa Ninawi watasimama siku ya hukumu pamoja na watu wa kizazi hiki, nao watawahukumu kuwa wamekosa; kwa sababu wao walitubu kwa mahubiri ya Yona; na hapa yupo aliye mkuu kuliko Yona." Mathayo 12:40, 41.

Kila mwujiza ambao Yesu aliufanya ulikuwa ni ishara ya uungu wake. Alikuwa anafanya kazi ile ile iliyotabiriwa kufanywa na Masihi; lakini kwa Mafarisayo kazi hizi za rehema zilikuwa ni chukizo. Viongozi wa Wayahudi waliyaangalia mateso ya mwanadamu pasipo kujali. Katika matukio mengi ubinafsi na uonevu wao ulikuwa umesababisha mateso yale ambayo Kristo aliyapoza. Kwa hiyo miujiza yake ilikuwa kemeo kwao.

Kile kilichowafanya Wayahudi wakatae kazi ya Mwokozi kilikuwa ushahidi wa hali ya juu wa tabia yake ya kiungu. Umuhimu mkubwa mno wa miujiza yake unaonekana katika ukweli kwamba ilifanywa kwa ajili ya kuwabariki wanadamu. **(407)** Uthibitisho wa hali ya juu kwamba alitoka kwa Mungu ni kwamba maisha yake yalidhihirisha tabia ya Mungu. Alifanya kazi za Mungu na kusema maneno ya Mungu. Maisha ya namna hiyo ni mwujiza mkuu kuliko yote.

Ujumbe wa ukweli unapowasilishwa katika siku zetu, wapo wengi ambao wanauliza kama Wayahudi, wakisema, Tuonyeshe ishara. Tufanyie mwujiza. Kristo hakufanya mwujiza kwa matakwa ya Mafarisayo. Hakufanya mwujiza nyikani katika kujibu ushawishi wa Shetani. Yeye hatupatii uwezo wa sisi kujihalalisha au kuridhisha matakwa ya kutoamini na kiburi. Lakini si kwamba injili haina ishara yenye asili ya kimbingu. Je kuvunja na kutoka katika utumwa wa Shetani si mwujiza? Uadui dhidi ya Shetani si jambo la hali ya kawaida kwa moyo wa mwanadamu; linapandikizwa kwa neema ya Mungu. Wakati mtu ambaye amekuwa akitawaliwa na msumbufu, akiwa na mawazo ya ukaidi, anapowekwa huru, akajisalimisha kikamilifu chini ya uongozi wa nguvu za kimbingu za Mungu, mwaujiza unakuwa umefanyika; hivyo ndivyo ilivyo pia wakati mtu ambaye amekuwa chini ya nguvu ya imani potofu anapokuja kuelewa ukweli wenyewe. Kila wakati mtu anapoongoka, na kujifunza kumpenda Mungu na kuzishika amri zake, ahadi hii ya Mungu inatimizwa: "Nami nitawapa ninyi moyo mpya, nami nitatia roho mpya ndani yenu." Ezekieli 36:26. Badiliko la ndani ya moyo wa mwanadamu, mageuzi ya tabia ya mwanadamu, ni mwujiza unaomfunua Mwokozi aliye hai daima, ukifanya kazi ya kuiponya mioyo. Kuwa na maisha yanayopatana na Kristo ni mwujiza mkuu. Katika kuhubiri neno la Mungu, ishara ambayo inapaswa kudhihirishwa sasa na kila mara ni uwepo wa Roho Mtakatifu, kulifanya neno kuwa nguvu iletayo wongofu kwa wale wanaolisikia. Huu ni ushuhuda wa Mungu mbele ya ulimwengu kwa ajili ya kazi ya kimbingu ya Mwana wake.

Wale waliodai mwujiza kutoka kwa Yesu walikuwa wameifanya mioyo yao kuwa migumu katika hali ya kutokuamini kiasi kwamba hawakuona ndani ya tabia yake hali ya kufanana na Mungu. Hawakupenda kuona kwamba kazi yake ilikuwa utimilifu wa Maandiko. Katika mfano wa tajiri na Lazaro, Yesu alimwambia yule Farisayo, "Wasipowasikia Musa na manabii, hawatashawishiwa hata mtu akifufuka katika wafu." Luka 16:31. Hakuna mwujiza ambao unaweza kutolewa mbinguni au duniani ukawafaa watu hao.

Yesu "akaugua rohoni mwake,"na, akigeuka kutoka kwa kundi lile la wabishi, alipanda tena chomboni pamoja na wanafunzi wake. Wakiwa na ukimya wa huzuni walivuka ng'ambo ya ziwa. Hata hivyo hawakurudi mahali walipotoka, bali walielekeza njia yao kwenda Bethsaida, karibu na mahali wale elfu tano walipokuwa wamelishiwa. Wakishafika upande wa mbali, Yesu alisema, " Angalieni, jilindeni na chachu ya Mafarisayo na

**(408)** Masadukayo." Tangu siku za Musa Wayahudi walikuwa wamezoezwa kuweka chachu mbali na nyumba zao wakati wa msimu wa Pasaka, na kwa hiyo walikuwa wamefundishwa kuiona chachu kama mfano wa dhambi. Lakini wanafunzi wale walishindwa kumwelewa Yesu. Katika kuondoka kwao Magadani kwa ghafla walikuwa wamesahau kuchukua mikate, na kwa hiyo walikuwa na mkate mmoja tu. Walielewa kwamba Yesu alikuwa ameongelea hali hii, kwamba anawaonya wasinunue mikate ya Mafarisayo na Masadukayo. Hali yao ya kukosa imani na uwezo wa kiroho wa kuona vilikuwa vimewasababishia mara nyingi hali kama ile ile ya kuelewa vibaya maneno yake. Sasa Yesu aliwakemea kwa kuwa walifikiri kwamba yawezekana Yeye aliyekuwa amelisha maelfu ya watu kwa samaki wachache na mikate ya shayiri michache alikuwa anawaonya kwa kuzungumzia chakula cha kimwili tu. Kulikuwa na hatari kwamba hoja za ujanja za Mfarisayo na Masadukayo zingewachachusha wanafunzi wake kwa kuwaletea hali ya kutoamini, na kuwafanya wazichukulie kazi za Kristo kwa wepesi.

Wanafunzi wale walikuwa na mwelekeo wa kufikiri kwamba bora Bwana wao angekubaliana na matakwa ya wale waliotaka ishara katika mbingu. Waliamini kwamba alikuwa na uwezo mkubwa wa kufanya hili, na kwamba ishara kama hiyo ingewanyamazisha kabisa adui zake. Hawakuweza kuona hali ya unafiki iliyokuwa ndani ya wabishi wale.

Miezi kadhaa baadaye, "makutano walipokutanika elfu elfu, hata wakakanyagana," Yesu alirudia fundisho lile lile. "Alianza kuwaambia wanafunzi wake kwanza, Jilindeni na chachu ya Mafarisayo, ambayo ni unafiki." Luka 12:1.

Chachu iwekwayo katika chakula hufanya kazi taratibu, ikibadili chakula chote na kukifanya kiwe na hali ya chachu. Ndivyo ilivyo unafiki unaporuhusiwa kukaa moyoni, unapenya hadi katika tabia na maisha. Mfano wa wazi wa unafiki wa Mafarisayo unaonyeshwa na vile Kristo alivyokemea akipinga matendo ya "Korbani," ambapo kupitia tabia hiyo hali ya kupuuza wajibu wa watoto kwa wazazi ilifichwa katika kujifanya kuwa na uhuru wa kuwajibika kwa ajili ya hekalu. Waandishi na Mafarisayo walikuwa wakionyesha kanuni ya uongo. Walificha mwenendo halisi wa mafundisho yao, na walitumia kila fursa ya tukio lililopatikana kuyaingiza mawazoni mwa wasikilizaji wao. Kanuni hizi za uongo, kila zilipopokelewa, zilifanya kazi kama chachu katika chakula, zikipenya na kugeuza tabia. Ni mafundisho haya ya udanganyifu ambayo yalifanya iwe vigumu kwa watu kupokea maneno ya Kristo.

Nguvu ile ile inafanya kazi leo kupitia kwa watu wanaojaribu kuifafanua sheria ya Mungu kwa namna ambayo itakubaliana na matendo yao. Watu hawa hawaipingi sheria wazi wazi, bali huleta **(409)** dhana za kudhani zinazoshusha misingi ya sheria. Wanaifafanua sheria kwa namna ya kuharibu nguvu yake.

Unafiki wa mafarisayo ulikuwa ni matokeo ya kujitafutia manufaa binafsi. Hali ya kujitukuza wenyewe ilikuwa ndiyo lengo la maisha yao. Ndilo hili lililowafanya kupotosha Maandiko na kuyatumia isivyo sahihi, nalo likawapofusha wasijue kusudi la kazi ya Kristo. Hata wanafunzi wale walikuwa katika hatari ya kupenda uovu huu uliojificha. Wale waliojiweka katika kundi la wafuasi wa Kristo, lakini wakiwa hawakuacha vyote ili kuwa wanafunzi wake, kwa kiasi kikubwa waliathiriwa na mawazo yale ya Mafarisayo. Mara nyingi walikuwa wakiyumba-yumba kati ya imani na kutoamini, na hawakuona hazina ya hekima iliyojificha ndani ya Kristo. Hata wanafunzi wale, ingawa kwa nje walikuwa wameacha vyote kwa ajili ya Yesu, mioyoni mwao hawakuwa wamekoma kujitafutia mambo makuu kwa ajili yao. Ni roho hii iliyosukuma kuibuka kwa mashindano miongoni mwao kuhusu nani awe mkuu kuliko wengine. Ndicho kitu kilichosimama kati ya wao na Kristo, kikiwafanya kuwa na upendo kidogo tu kwa kazi yake ya kujikana nafsi, na kuchelewa sana kuielewa siri ya ukombozi. Kama ilivyo chachu, ambayo ikiachwa ifanye kazi yake husababisha uharibifu na kuchacha, ndivyo roho ya kujitukuza nafsi inavyonajisi na kuharibu moyo, pindi inapoendekezwa.

Ni kwa ukubwa kiasi gani dhambi idanganyayo kwa kificho imeenea miongoni mwa wafuasi wa Bwana leo, kama ilivyokuwa kwa wale wa zamani! Ni mara ngapi huduma yetu kwa Kristo, ushirika wetu kwa mtu na mwenzake, unavyoharibiwa na tamaa za siri za kujitukuza wenyewe! Ni kiasi gani mawazo yalivyo tayari kujisifia, na kutafuta kupendwa na wanadamu! Hali iliyopo ni kujipenda, kutamani kuwa na njia nyepesi kuliko ile iliyochaguliwa na Mungu inayopita katika hali ya kuongozwa na maagizo ya kimbingu mahali pa nadharia na mapokeo ya wanadamu. Maneno ya onyo yanasemwa kwa wanafunzi wake Yesu kwamba, "Angalieni na jilindeni na chachu ya Mafarisayo."

Dini ya Kristo ni unyofu wenyewe. Hamu ya kuona utukufu kwa Mungu ni msukumo upandikizwao na Roho Mtakatifu; na ni kazi ya Roho huyo tu inayoweza kupandikiza msukumo huu. Ni nguvu ya Mungu tu inayoweza kuondosha tabia ya kujitukuza na unafiki. Badiliko hili ni ishara ya utendaji wake. Wakati imani tupokeayo inapoharibu ubinafsi na unafiki, wakati inapotuongoza kutafuta utukufu kwa Mungu na wala si utukufu wetu, tunaweza tukajua kwamba ni imani iliyo katika mpango sahihi. Habari kubwa ya maisha ya Kristo ilikuwa ni, "Baba, ulitukuze jina lako" (Yohana 12:28), na ikiwa tutamfuata, hiyo itakuwa ndiyo habari kubwa ya maisha yetu. Yeye anatuagiza kwamba tupate kuenenda vile vile kama yeye alivyoenenda; na "katika hili twajua ya kuwa tumemjua yeye, ikiwa tunashika amri zake."1 Yohana 2:6, 3.

## Sura ya 45

# Kuonyesha Kivuli cha Msalaba

[Suara hii imejengwa katika Mathayo 16:13-28; Marko 8:27-38; Luka 9:18-27.]

Kazi ya Kristo duniani ilikuwa ikiharakisha kwenda mwishoni. Mbele yake, katika mstari ulio bayana, kulikuwa na mwonekano wa mandhari iliyo mahali ambako miguu yake ilikuwa inaelekea. Hata kabla hajavaa hali ya kibindamu, aliona marefu yote ya njia ambayo ni lazima aipite ili kuokoa kilichopotea. Kila maumivu yaliyochoma moyo wake, kila dhihaka iliyorundikwa kichwani pake, kila hali ya upweke aliyoitwa kustahimili, vilikuwa wazi machoni pake kabla hajaweka kando taji yake na vazi la kifalme, kushuka chini kutoka kwenye enzi yake, ili kuuvisha ubinadamu uungu wake. Njia yake itokayo katika hori la ng'ombe hadi Kalvari ilikuwa wazi machoni pake. Alijua machungu ambayo yangekuja juu yake. Aliyajua yote, lakini bado akasema, "Tazama nimekuja, (Katika gombo la chuo nimeandikiwa), Kuyafanya mapenzi yako, Ee Mungu wangu, ndiyo furaha yangu; Naam, sheria yako imo moyoni mwangu." Zaburi 40:7, 8.

Muda wote aliona matokeo ya kazi yake yaliyokuwa mbele yake. Maisha yake ya duniani, yenye kujawa na masumbuko na kujikana, yalifarijiwa na matarajio ya kwamba asingepatwa na masumbuko yote haya bure. Kwa kuyatoa maisha yake kwa ajili ya maisha ya wanadamu, angeukomboa ulimwengu na kuuresha kwa Mungu. Ingawa ni lazima kwanza ubatizo wa damu upokelewe; ingawa dhambi za ulimwengu zingeielemea nafsi yake isiyo na hatia; ingawa uvuli wa shida isiyosemekana ulikuwa juu yake; lakini kwa ajili ya furaha iliyokuwa imewekwa mbele zake, alichagua kuustahimili msalaba, na akaidharau dhambi.

Kwa muda huo mandhari hiyo iliyokuwa mbele yake ilikuwa bado imefichwa machoni pa washirika wake waliokuwa wamechaguliwa kwa ajili ya kazi yake; lakini muda ambao ni lazima **(411)** wayaone mateso yake ulikuwa unakaribia. Lazima wamwone Yeye waliyekuwa wamempenda sana na kumtumainia akitiwa mikononi mwa adui zake, na kuangikwa kwenye msalaba. Baadaye lazima awaache wakabiliane na ulimwengu pasipokuwa na faraja yake yake ionekayo kwa macho. Alijua jinsi ambavyo chuki chungu na kutokuamini vingewatesa, na alitaka awaandae kwa ajili ya majaribu hayo.

Yesu na wanafunzi wake walikuwa wamekuja katika mji mmowapo maeneo ya Kaisaria-Filipi. Walikuwa ng'ambo ya mipaka ya Galilaya, katika eneo ambalo ibada ya sanamu ilikuwa katika kiwango cha juu. Katika eneo hili wanafunzi wake walikuwa wameondolewa kutoka katika mivuto ya ushawishi wa dini ya Kiyahudi, na wameletwa mahali pa kukutanishwa kwa karibu zaidi na ibada za kipagani. Karibu yao kulikuwa na uwakilishi wa mifumo ya kishirikina ambayo ilikuwa katika sehemu zote za ulimwengu. Yesu alitamani kwamba mwonekano wa vitu hivi uwasukume kuona wajibu walio nao kwa wapagani. Katika muda aliokaa katika eneo hili, aliamua kuondokana na kazi ya kuwafundisha watu, na kujitoa kikamilifu zaidi kuwafundisha wanafunzi wake.

Alikuwa anakaribia kuwaeleza habari za mateso yaliyokuwa yanamsubiri. Lakini alienda mbali nao kwanza, na akaomba kwamba mioyo yao iandaliwe kuyapokea maneno yake. Baada ya kuungana nao tena, hakuwajulisha haraka kile alichotaka wajue. Kabla ya kufanya hivyo, aliwapatia fursa ya kuikiri imani yao katika Yeye ili ya kwamba watiwe nguvu kwa ajili ya jaribio lililokuwa linakuja. Aliwauliza hivi, "Watu hunena Mwana wa Adamu kuwa ni nani?"

Kwa huzuni wanafunzi wale wakalazimika kukiri kwamba Waisraeli walikuwa wameshindwa kumtambua Masihi wao. Kweli, baadhi walipoona miujiza yake walikuwa wamesema kwamba ni Mwana wa Daudi. Makutano wale waliokuwa wamelishwa kule Bethsaida walikuwa wameazimia kumtangaza kuwa mfalme wa Israeli. Wengi walikuwa tayari kumkubali kama nabii; lakini hawakumwamini kwamba ni Masihi.

Sasa Yesu akauliza swali la pili, likiwahusu wanafunzi wenyewe: "Nanyi mwaninena mimi kuwa ni nani?" Petro akajibu akisema, "Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai."

Tangu mwanzo wake, Petro alikuwa ameamini kwamba Yesu ni Masihi. Wanafunzi wengine wengi waliokuwa wamesadikishwa na mahubiri ya Yohana Mbatizaji, na wakawa wamemkubali Kristo, walianza kuwa na mashaka

na kazi ya utume wa Yohana wakati alipotiwa gerezani na kuuawa; na sasa walikuwa na mashaka kuhusu Yesu kama kweli ni Masihi, ambaye walikuwa wamemtazamia kwa muda mrefu. Wengi wa wanafunzi ambao walikuwa wametarajia kwa hamu kumwona Yesu akichukua nafasi yake kwenye kiti cha enzi cha Daudi walimwacha wakati walipoona kwamba hakuwa na nia ya namna hiyo. Lakini Petro na **(412)** wenzake hawakugeuka na kumwacha. Njia yenye kuyumba-yumba ya wale waliokuwa na mwenendo wa kumsifu jana na kumpinga leo haikuvunja imani ya wafuasi wa kweli wa Mwokozi. Petro alitangaza, "Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai." Hakusubiri kwamba mpaka heshima za kifalme zipambe utukufu kwa Bwana wake, bali alimkubali katika hali yake ya kujishusha.

Petro alikuwa ameonyesha imani ya wale kumi na wawili. Lakini wanafunzi wale bado walikuwa mbali kutoka katika hali ya kuielewa kazi ya Kristo. Upinzani na upotoshaji wa makuhani na wakuu, ingawa haukuweza kuwageuzia mbali na Kristo, bado uliwasababishia hali ya kutatanika sana. Hawakuiona njia yao kwa uwazi. Ushawishi uliotokana na mafundisho yao ya awali, mafundisho ya marabi, nguvu ya mila zao za mapokeo, bado vilizuia hali yao ya kuuona ukweli. Katika nyakati tofauti-tofauti mishale ya nuru ya thamani itokayo kwa Yesu ilikuwa imewamlikia, lakini mara nyingi walikuwa kama watu wanaopapasa-papasa tu katika vivuli. Hata hivyo katika siku hii, kabla ya kuletwa kukabiliana uso kwa uso na jaribu kuu la imani yao, Roho Mtakatifu aliweka ndani yao nguvu. Kwa muda kitambo macho yao yalielekezwa mbali na vitu vinavyoonekana, ili kuona vitu visivyoonekana." 2 Wakorintho 4:18. Ndani ya mwonekano wa vazi la nje la mwanadamu waliona utukufu wa Mwana wa Mungu.

Yesu alimjibu Petro, akisema, "Heri wewe Simoni Bar-yona; kwa kuwa mwili na damu havikukufunulia hili, bali Baba yangu aliye mbinguni."

Ule ukweli ambao Petro alikuwa ameukiri ndio msingi wa imani ya waaminio. Ni kile ambacho Kristo amekitangaza kwamba ndio uzima wa milele. Lakini hali ya kujua hivi haikumruhusu mtu kujitukuza. Petro hakufunuliwa hayo kwa hekima yake na wema wake. Kamwe mwanadamu, kwa nguvu zake, hawezi kujua mambo ya kimbingu. "Ni juu mno kama mbingu; waweza kufanya nini wewe? Ni wenye kina kuliko kuzimuni; waweza kujua nini wewe?" Ayubu 11:8. Roho ibadilishayo tu ndiyo inayoweza kutufunulia mambo ya kina ya Mungu, ambayo "jicho halikuyaona wala sikio halikuyasikia, wala hayakuingia katika moyo wa mwanadamu." "Mungu ametufunulia sisi kwa Roho. Maana Roho huchunguza yote, hata mafumbo ya Mungu." 1 Korintho 2:9, 10. "Siri ya Bwana iko kwao wamchao, Naye atawajulisha agano lake." Na ile hali ya kwamba Petro aliuona utukufu wa Kristo ilikuwa ni ushahidi kwamba alikuwa amefundishwa na Mungu. Zaburi 25:14; Yohana 6:45. Kweli, "heri wewe Simoni Bar-yona; kwa kuwa mwili na damu havikukufunulia hili."

Yesu aliendelea kusema kwamba: "Nami nakuambia, Wewe ndiwe Petro, na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu; wala milango ya kuzimu **(413)** haitalishinda." Neno Petro humaanisha jiwe, - jiwe linalobingirika. Petro hakuwa mwamba ambao kanisa lilijengwa juu yake. Milango ya kuzimu ilimshinda alipomkana Bwana wake kwa kuapa na kulaani. Kanisa lilijengwa juu yake Yeye ambaye milango ya kuzimu haikumshinda.

Karne nyingi kabla ya kuja kwa Mwokozi Musa alikuwa ameelekeza kwa mwamba wa wokovu wa Israeli. Mwimbaji wa zaburi alikuwa ameimba kuhusu "Mwamba wa nguvu zangu." Isaya alikuwa ameandika kwaba, "Bwana, MUNGU, asema hivi, Tazama, naweka jiwe katika Sayuni, liwe msingi, jiwe lililojaribiwa, jiwe la pembeni lenye thamani, msingi ulio imara." Kumbukumbu 32:4; Zaburi 62:7; Isaya 28:16. Petro mwenyewe, akiandika kwa uvuvio, alielekeza unabii huo kwa Yesu. Anasema, "Ikiwa mmeonja ya kwamba Bwana ni mwenye fadhili. Mmwendee yeye, jiwe lililo hai, lililokataliwa na wanadamu, bali kwa Mungu ni teule, lenye heshima. Ninyi nanyi, kama mawe yaliyo hai, mmejengwa mwe nyumba ya Roho." 1 Petro 2:3-5.

"Maana msingi mwingine hakuna mtu awezaye kuuweka, isipokuwa ni ule uliokwisha kuwekwa, yaani, Yesu Kristo." 1 Wakorintho 3:11. "Juu ya mwamba huu," Yesu alisema, "nitalijenga kanisa langu." Mbele za Mungu, na mbele ya jeshi lote la malaika wa mbinguni, na mbele ya uwepo wa jeshi la kuzimu lisiloonekana, Kristo alilianzisha kanisa lake juu ya Mwamba ulio hai. Mwamba huo ni Yeye mwenyewe, - mwili wake mwenyewe, ambao umevunjwa na kuchubuliwa kwa ajili yetu. Malango ya kuzimu hayawezi kulishinda kanisa lililojengwa kwenye msingi huu.

Ni jinsi gani kanisa lilivyoonekana dhaifu wakati ule Kristo aliposema maneno haya! Kulikuwa na waamini wachache tu; ambapo nguvu zote za mapepo na za watu waovu zingekuwa dhidi yao; lakini wafuasi wa Kristo hawakutakiwa kuogopa. Wakiwa wamejengwa kwenye Mwamba wa nguvu zao, wasingeshindwa.

Kwa miaka elfu sita, imani imejengwa juu ya Kristo. Kwa miaka elfu sita gharika na tufani za ghadhabu za kishetani zimepiga kwenye Mwamba huo wa wokovu wetu; lakini umesimama bila kutikiswa.

Petro alikuwa ameonyesha ukweli ambao ni msingi wa imani ya kanisa, na sasa Yesu alimheshimu kama mwakilishi wa kundi zima la waamini. Alisema hivi, "Nami nitakupa wewe funguo za ufalme wa mbinguni; na lolote utakalolifunga duniani, litakuwa limefungwa mbinguni; na lolote utakalolifungua duniani, litakuwa limefunguliwa mbinguni."

"Funguo za ufalme wa mbinguni" ni maneno ya Kristo. Maneno yote ya Maandiko Matakatifu ni yake, nayo yanajumuishwa hapa. Maneno haya yana nguvu za kufungua mbingu na kuzifunga. Yanatangaza masharti **(414)** yanayoamua ikiwa watu wanakubaliwa au kukataliwa. Kwa hiyo kazi ya wale wanaolihubiri neno la Mungu ni kuamua kwa ajili ya uzima au mauti. Kazi yao hiyo ni kipimo kwa ajili ya matokeo ya milele.

Mwokozi hakuikabidhi kazi ya injili kwa Petro kama mtu binafsi. Wakati fulani baadaye, alirudia maneno yale aliyoambiwa Petro akiyatumia kwa kanisa. Kitu kile kile kilisemwa kwa wale kumi na wawili kama wawakilishi wa jamii ya waamini. Ikiwa Yesu alikuwa amekasimisha madaraka rasmi yoyote kwa mmoja wa wanafunzi wake, tusingetarajia kuwakuta mara kwa mara wakibishana kuhusu nani awe mkubwa wa wote. Wangetii matakwa ya Bwana wao, na kumheshimu yeye ambaye alimchagua.

Badala ya kumteua mtu mmoja kuwa mkubwa kwao, Kristo aliwaambia wale wanafunzi kwamba, "Bali ninyi msiitwe Rabi" "wala msiitwe viongozi; maana kiongozi wenu ni mmoja, naye ndiye Kristo." Mathayo 23:8, 10.

"Kichwa cha kila mwanamume ni Kristo." Mungu, aliweka vitu vyote chini ya miguu ya Mwokozi, "akamweka awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa; ambalo ndilo mwili wake, ukamilifu wake anayekamilika kwa vyote katika vyote." 1 Wakorintho 11:3; Waefeso 1:22, 23. Kanisa linajengwa juu ya Kristo kama msingi wake; linapaswa kumheshimu Mungu kama kichwa chake. Halipaswi kumtegemea mwanadamu, wala halipaswi kutawaliwa na mwanadamu. Wengi wanadai kwamba nafasi yao ya kuaminiwa kanisani inawapa mamlaka ya kuamua mambo ambayo watu wengine wanapaswa kuamini na mambo wanayopaswa kutenda. Mungu hakuruhusu mamlaka hayo. Mwokozi alitamka kwamba, "Nanyi nyote ni ndugu." Wote wanakabiliwa na majaribu, na wanaweza kukosea. Hatuwezi kutegemea uongozi wa mwanadamu yeyote. Mwamba wa imani ni uwepo ulio hai wa Kristo katika kanisa. Walio dhaifu sana na wautegemee Mwamba huu, nao wajidhaniao kwamba wana nguvu kuliko wengine watathibitika kuwa ndio wadhaifu kuliko wote, ikiwa hawatamfanya Kristo kuwa nguvu yao. "Amelaaniwa mtu yule amtegemeaye mwanadamu, Amfanyaye mwanadamu kuwa kinga yake." Bwana ni "Mwamba, kazi yake ni kamilifu." "Wamebarikiwa wote wawekao tumaini lao katika Yeye." Yeremia 17:5; Kumbukumbu 32:4; Zaburi 2:12.

Baada ya kukiri kwa Petro, Yesu aliwataka wanafunzi wale wasimwambie mtu yeyote kwamba Yeye ni Kristo. Katazo hili lilifanywa kwa sababu ya kuwepo kwa upinzani mkali kutoka kwa waandishi na Mafarisayo. Zaidi ya hilo, hata wanafunzi wenyewe walikuwa na uelewa usio sahihi kuhusu Masihi kiasi kwamba kitendo cha kumtangaza hadharani kisingewapatia dhana nzuri ya tabia yake au kazi yake. Lakini siku kwa siku alikuwa anajifunua kwao kama Mwokozi, na kwa njia hiyo alitaka awapatie uelewa ulio sahihi kuhusu Yeye kama Masihi.

**(415)** Wale wanafunzi bado walitarajia kwamba Kristo angetawala kama mfalme wa duniani. Ingawa alikuwaameficha mipango yake kwa muda mrefu, waliamini kwamba asingedumu kubaki kuwa maskini na mtu asiye maarufu wakati wote; wakati wa Yeye kuanzisha ufalme wake ulikuwa umekaribia. Kwamba chuki ile ya makuhani na marabi isingeshindwa kamwe, kwamba Kristo angekataliwa na watu wa taifa lake mwenyewe, akihukumiwa kama mdanganyifu, na kusulibiwa kama mhalifu, - wazo kama hilo lisingepata kudhaniwa na wanafunzi kama wale. Lakini saa ya nguvu za giza ilikuwa inasogea karibu, na lazima Yesu awafungulie wanafunzi wake pambano lililo mbele yao. Alipatwa na huzuni alipofikiria majaribu yaliyokuwa yanakuja.

Mpaka wakati huu alikuwa amezuia kisijulikane kwao chochote kile kinachohusiana na mateso yake na kifo chake. Katika mazungumzo yake na Nikodemo, alikuwa amesema kwamba, "Kama vile Musa alivyomwinua yule

nyoka jangwani, vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa." Yohana 3:14, 15. Lakini wanafunzi wale hawakusikia maneno haya, na ikiwa wangeyasikia, wasingekuwa wameelewa. Lakini sasa wamekuwa na Yesu, wakisikiliza maneno yake, wakiziona kazi zake, mpaka kufika mahali ambapo, pasipo kujali mazingira yake ya kujiweka katika hali ya chini, na upinzani kutoka kwa makuhani na watu, wanaweza kuungana na ushuhuda wa Petro kwa kusema, "Wewe ni Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai." Sasa wakati umefika wa kuondoa pazia linalouficha wakati ujao. "Tangu wakati huo Yesu alianza kuwaonya wanafunzi wake ya kwamba imempasa kwenda Yerusalemu, na kupata mateso mengi kwa wazee na wakuu wa makuhani, na waandishi, na kuuawa, na siku ya tatu kufufuka."

Wakiwa kimya kwa mshangao wa huzuni, wanafunzi wale walisikiliza. Kristo alikuwa amekubali kukiri kwa Petro kwamba Yeye ni Mwana wa Mungu; na sasa maneno yake yakiwa yanaelekeza kwenye mateso yake na kifo chake yalionekana kama yasiyoeleweka. Petro hakuweza kunyamaza. Alimzuia Bwana, kama vile kutaka kumzuia na mabaya yale, huku akisema, "Hasha, Bwana, hayo hayatakupata."

Petro alimpenda Bwana wake; lakini Yesu hakumsifu kwa kuonyesha hali ile ya kutaka kumkinga na mateso. Maneno ya Petro hayakuwa yale ambayo yangekuwa msaada na faraja kwa Yesu wakati wa jaribu lile kubwa lililokuwa linakuja. Hayakuwa maneno yanayopatana na kusudi la Mungu la neema kwa ulimwengu uliopotea, wala hayakupatana na fundisho la kujikana nafsi ambalo Yesu alikuwa amekuja kulifundisha kupitia kielelezo chake mwenyewe. Petro hakutarajia kuuona msalaba katika kazi ya Kristo. Wazo ambalo lingeletwa na maneno yale lilikuwa linapingana kabisa na lile ambalo Kristo alitaka kuliweka katika akili za wanafunzi wake, na Mwokozi akasukumwa kutamka maneno ambayo ni moja ya makemeo makali **(416)** yaliyopata kutoka midomoni mwake: "Nenda nyuma yangu, Shetani; u kikwazo kwangu; maana huyawazi yaliyo ya Mungu, bali ya wanadamu."

Shetani alikuwa anajaribu kumkatisha tamaa Yesu, na kumgeuza aondoke katika kazi yake; Petro naye, katika upendo wake wenye upofu alikuwa anayapatia majaribu nguvu. Mfalme wa giza ndiye aliyekuwa mwasisi wa wazo lile. Mwanzo wake ulikuwa katika maneno yale. Kule nyikani, Shetani alikuwa amemwahidi Kristo falme zote za ulimwengu kwa sharti la kuacha njia ya kujishusha na kujikana. Sasa alikuwa analeta jaribu lile lile kwa wanafunzi wa Kristo. Alikuwa anatafuta namna ya kuelekeza mtazamo wa Petro katika utukufu wa dunia, ili kwamba asiuone msalaba ambao Kristo alimtaka ageuze macho yake na kuuangalia huo. Na kupitia kwa Petro, Shetani alikuwa anasukumia jaribu lile kwa Yesu. Lakini Mwokozi hakulisikiliza; mawazo yake yalikuwa kwa ajili ya wanafunzi. Shetani alikuwa ameingilia kati ya Petro na Bwana wake, ili ya kwamba moyo wa mwanafunzi huyo usiguswe kwa kuyaona mateso ya Kristo kwa ajili yake. Maneno yale ya Kristo hakuambiwa Petro, bali yule aliyekuwa anajaribu kumtenga Petro na kumweka mbali na Mwokozi wake. "Nenda nyuma yangu, Shetani." Usiendelee kuingilia na kukaa katikati yangu na mtumwa wangu anayekosa. Niache niwe uso kwa uso na Petro, ili nipate kumfunulia siri ya upendo wangu.

Hili lilikuwa somo chungu kwa Petro, ambalo alijifunza lakini kwa kuchukua muda mrefu sana, kwamaba njia ya Kristo duniani inapita katika mateso na kujidhili. Mwanafunzi huyu alirudi nyuma asishiriki na Bwana wake katika mateso. Lakina angejifunza mbaraka wa njia hiyo akiwa katikati ya tanuru la moto. Muda mrefu baadaye, wakati ambapo mwili wake wenye nguvu ulikuwa na mzigo wa umri na kazi alizofanya, aliandika hivi, "Wapenzi, msione kuwa ni ajabu ule msiba ulio kati yenu, unaowapata kama moto ili kuwajaribu, kana kwamba ni kitu kigeni kiwapatacho. Lakini kama mnavyoyashiriki mateso ya Kristo, furahini; ili na katika ufunuo wa utukufu wake mfurahi kwa shangwe." 1 Petro 4:12, 13.

Sasa Yesu aliwafafanulia wanafunzi wake kwamba maisha yake ya kujikana yalikuwa kielelezo cha vile ambavyo maisha yao yanapaswa kuwa. Akiwaita kwake watu waliokuwa pale karibu, pamoja na wanafunzi wake, alisema, "Mtu yeyote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake, anifuate." Msalaba ulikuwa unahusianishwa na mamlaka ya Rumi. Ilikuwa ndiyo njia ya kutekeleza kifo cha kikatili zaidi na cha kudhalilisha zaidi kuliko vifo vingine vyote. Waharifu wa hadhi ya chini zaidi walitakiwa kubeba msalaba kwenda mahali pa kutekelezea adhabu hiyo; na mara nyingi msalaba ulipokaribia kutwishwa mabegani mwao, walileta upinzani kwa nguvu na fujo, mpaka wakati walipozidiwa nguvu, na **(417)** mara hiyo zana hii ya kutesea ikatua juu yao. Lakini Yesu anawataka wafuasi wake wachukue msalaba na kuubeba nyuma yake. Kwa wanafunzi wale, maneno yake yalieleweka, ingawa kwa uhafifu, kwamba yalielekeza katika kujitoa kwao hata katika kujidhili ambako ni

kuchungu mno, - kujishusha hata kama ni mpaka kufa kwa ajili ya Kristo. Hakuna kujisalimisha kikamilifu kwingine ambako maneno ya Mwokozi yanaweza kuwa yalionyesha. Lakini aliyakubali haya yote kwa ajili yao. Yesu hakupaona mbinguni kama mahali pazuri kwake wakati ambapo tulikuwa tumepotea. Aliacha nyumba ya mbingu na kuchukua maisha ya kukejeliwa na kutukanwa, na kifo cha aibu. Yeye aliyekuwa tajiri katika hazina ya mbinguni ya thamani kubwa isiyohesabika, akawa maskini, ili kwamba kupitia umaskini wake tuwe matajiri. Yatupasa tufuate katika njia aliyopita.

Upendo kwa watu ambao Kristo alikufa kwa ajili yao humaanisha kuisulibisha nafsi. Yeye aliye mwana wa Mungu anapaswa ajione kama kiungo katika mnyororo ulioshushwa ili kuokoa ulimwengu, mmoja pamoja na Kristo katika mpango wake wa rehema, akienda pamoja na Kristo kuwatafuta na kuwaokoa waliopotea. Mkristo anatambua daima kwamba amejitoa wakfu kwa Mungu, na ya kwamba kwa tabia yake anatakiwa amfunue Kristo kwa ulimwengu. Kujitoa kafara, huruma, upendo, vilivyodhihirishwa katika maisha ya Kristo vinapaswa vionekane tena katika maisha ya mtenda-kazi wa Mungu.

"Kwa kuwa mtu atakaye kuiponya nafsi yake, ataiangamiza, na mtu atakayeiangamiza nafsi yake kwa ajili yangu na kwa ajili ya Injili, huyu ataisalimisha." Ubinafsi ni kifo. Hakuna kiungo chochote cha mwili ambacho kingekuwa hai ikiwa kingejifungia huduma chenyewe peke yake. Ikiwa moyo ungeshindwa kupeleka damu ya uhai katika mikono na kichwa, utaishiwa nguvu zake. Kama damu yenye uhai ilivyo, ndivyo ulivyo upendo wa Kristo unaotawanywa katika kila sehemu ya mwili wake wa fumbo. Sisi tu washirika mtu na mtu mwingine, na nafsi inayokataa kutoa itaangamia. Na "itamfaidia mtu nini," Yesu alisema, "kuupata ulimwengu wote, akipata hasara ya nafsi yake? Ama mtu atoe nini badala ya nafsi yake?

Ng'ambo ya maisha haya ya umaskini na kujishusha, aliwaelekeza wanafunzi wake katika habari ya kuja kwake katika utukufu, si katika fahari ya enzi ya kidunia, bali akiwa na utukufu wa Mungu na majeshi ya mbinguni. Na halafu akasema, "Ndipo atakapomlipa kila mtu kwa kadiri ya matendo yake." Halafu kwa lengo la kuwatia moyo, alitoa ahadi hii, "Amin, nawaambieni, Pana watu katika hawa wasimamao hapa, ambao hawataonja mauti kabisa, hata watakapomwona Mwana wa Adamu akija katika ufalme wake." Lakini wanafunzi wale hawakuelewa maneno yake. Utukufu ule ulionekana kuwa mbali sana. Macho yao yalikuwa yamekazwa katika mambo ya karibu, maisha ya duniani ya umaskini, kudhalilika, na mateso. Je, lazima matarajio yao ya ufalme wa Masihi yaachwe? Je, wasingemwona Bwana wao akitawazwa kwenye enzi ya **(418)** Daudi? Je, yawezekanaje kwamba Kristo alikuwa aishi maisha ya mtu atangatangaye bila makazi huku akijinyenyekeza, halafu aishie kudharauliwa, kukataliwa, na kuuawa? Huzuni zililemea mioyo yao, maana walimpenda Bwana wao. Mashaka pia yalitesa mawazo yao, maana kilionekana kuwa kitu kisichoingia akilini kwamba Mwana wa Mungu ataingia katika hali ya kudhalilishwa kwa ukatili. Walihoji kwamba ni kwa nini anajipeleka Yerusalemu yeye mwenyewe kwa kutaka ili akabiliwe na zahama hizo alizowaambia. Inakuwaje anapanga kujipeleka katika hatima hiyo, na kuwaacha katika giza kuu zaidi kuliko lile walilokuwemo kabla hajajifunua kwao?

Wale wanafunzi walitoa hoja kwamba, Katika eneo la Kaisaria-Filipi, Kristo alikuwa mbali mahali pasipofikiwa na Herode wala Kayafa. Hakuwa na hofu yoyote ya chuki ya Wayahudi au ya utawala wa Kirumi. Kwa nini asifanyie kazi mahali pale, mahali ambapo pako mbali na Mafarisayo? Kwa nini anataka kujipeleka mwenyewe katika kifo? Ikiwa alikuwa afe, basi sasa ingekuwaje ufalme wake uanzishwe na kuimarishwa hata milango ya kuzimu isiushinde? Habari hizi zilikuwa ni fumbo kweli kweli kwa wanafunzi wale.

Hata sasa walikuwa wanasafiri kando-kando ya pwani ya Bahari ya Galilaya wakielekea katika jiji lile mahali ambapo matumaini yao yote yangekanyagwa-kanyagwa. Hawakuthubutu kuhojiana na Kristo, bali walizungumza wao kwa wao kwa sauti ya chini yenye huzuni kuhusu namna siku za usoni zitakavyokuwa. Hata katikati ya maswali yao walishikilia mawazo kwamba mazingira fulani yasiyotabirika huenda yakaondosha utusitusi ule ulioonekana kumngoja Bwana wao. Hivyo ndivyo walivyohuzunika na kuwa na mashaka, walivyotarajia na kuogopa, kwa muda wa siku sita ndefu na za majonzi.

## Sura ya 46

# Alibadilika Sura

[Sura hii imejengwa katika Mathayo 17:1-8; Marko 9:2-8; Luka 9:28-36.]

Jioni inaingia wakati Yesu anapowaita kwake watatu miongoni mwa wanafunzi wake, Petro, Yakobo na Yohana, na kuwaongoza kupita katika mashamba, na kupanda kwenda mbali wakipita katika njia ya mawe-mawe, hadi katika upande wa mlima uliojitenga. Mwokozi na wanafunzi wake walikuwa wametumia siku nzima katika kusafiri na kufundisha, na kule kupanda mlima kunaongeza uchovu wao. Kristo ameondoa mizigo kutoka katika akili na mwili wa wagonjwa wengi; amepeleka furaha ya maisha kupitia nguzo zilizo imara; lakini pia amezungukwa na hali ya kibinadamu, kwa hiyo Yeye na wanafunzi wake wamechoka.

Nuru ya jua ambalo linazama bado inaangaza kwenye kilele cha mlima, na kuangaza mwanga hafifu katika njia yao walipokuwa wakitembea. Lakini muda si mrefu nuru inakwisha kote kilimani na bondeni, jua linatoweka katika upeo wa macho wa magharibi, na wasafiri hawa wanafunikwa na giza la usiku. Ukimya wa mazingira yao unaonekana kama vile kuendana na maisha yao ya huzuni, ambayo yalikuwa yanakusanyikiwa na mawingu yaliyokuwa yanaendelea kuwa mazito.

Wanafunzi hawadiriki kuuliza kwamba Kristo alikuwa anaenda wapi, na kwa kusudi gani. Alikuwa ametumia muda wote wa usiku kwa siku kadhaa akiwa milimani kuomba. Yeye ambaye mkono wake ndio uliofanya milima na mabonde yuko mahali pake hapo pa asili, akifurahia utulivu uliopo. Wanafunzi wale wanamfuata Kristo anakoongoza kwenda; lakini wanashangaa ni kwa nini Bwana wao anawapandisha mlimani kwa safari hii yenye usumbufu wakati wamechoka, na Yeye mwenyewe akihitaji kupumzika.

Sasa Yesu anawaambia kwamba wasiende zaidi. Akienda pembeni kidogo kutoka mahali walipo, huyu Mtu wa huzuni nyingi alimwaga **(420)** maombi kwa kilio cha nguvu na kwa machozi. Anaomba nguvu ya kustahimili jaribio kwa niaba ya wanadamu. Lazima Yeye mwenyewe binafsi ajishikize kwake Aliye Mwenye nguvu zote, maana ni kwa njia hiyo tu angeweza kuyaelewa mambo yaliyokuwa yanakuja. Halafu alimimina moyo wake akiomba kwa ajili ya wanafunzi wake, ili ya kwamba imani yao isipungue mnamo wakati wa saa ya nguvu za giza. Umande unakuwa mzito kwenye mwili wake ulioinama, lakini hausikii. Vivuli vya giza la usiku vinakusanyika haraka kumzunguka pote, lakini hajali hali ya utusitusi iliyopo. Saa zinapita taratibu. Mwanzoni wanafunzi wale wanaungana naye katika maombi ya kujitoa; lakini baada ya muda wanashindwa na uchovu, lakini, hata katika hali yao ya kuwa na hamu ya kuendelea na jambo lile, wanashikwa na usingizi. Yesu amewaambia kuhusu mateso yao; amewachukua na kwenda nao ili ya kwamba waungane naye katika maombi; hata sasa anawaombea. Mwokozi ameona sononeko la wanafunzi wake, na ametamani kupunguza uzito wa huzuni yao kwa kuwahakikishia kwamba imani yao haikuwa bure. Si wote, hata miongoni mwa wanafunzi wake, ambao wangeweza kupokea mafunuo aliyotamani kuwapa. Watatu tu ambao wangeshuhudia uchungu mkubwa ambao angeupata kule Gethsemani ndio waliochaguliwa kuwa pamoja naye pale mlimani. Sasa mzigo wa maombi yake ni kwamba wapate udhihirisho **(421)** wa utukufu aliokuwa nao alipokuwa na Baba yake kabla ya ulimwengu kuwepo, ili ya kwamba ufalme wake upate kufunuliwa katika macho ya wanadamu, na kwamba wanafunzi wake wapate kutiwa nguvu kwa kuuona huo. Anaomba kwamba wapate kushuhudia udhihirisho wa uungu wake ambao utawafariji wakati wa mateso yake makali sana wakijua kwamba kwa hakika Yeye ni Mwana wa Mungu na kwamba kifo chake cha aibu ni sehemu ya mpango wa ukombozi.

Ombi lake linasikiwa. Wakati akiwa ameinama chini mahali penye mawe katika hali ya kujishusha, mbingu zinafunguka ghafla, malango ya dhahabu ya mji wa Mungu yanafunguka, na mwangaza mtakatifu unashuka kwenye mlima ule, ukilifunika umbo la Mwokozi. Uungu utokao ndani unamlika kupitia umbo la mwanadamu, unakutana na mwanga wa utukufu unaoshuka kutoka juu. Kristo anainuka kutoka mahali alipokuwa amelala kifudifudi, na kusimama akiwa na ukuu kama wa kimungu. Nafsi yenye mwonekano wa shida inaondoka. Sasa sura yake inang'aa "kama jua," na mavazi yake ni "meupe kama nuru."

Wanafunzi wale walipoamka, waliona mafuriko ya nuru ya utukufu iliyouangazia mlima ule. Wakiwa na hofu na hali ya kushangazwa wanautazama mwonekano ule wa mng'ao wa Bwana wao. Kadiri wanavyopata uwezo wa

kuustahimili mng'ao ule wa ajabu, wanaona kwamba Yesu hayuko peke yake. Kando yake kuna viumbe wawili wa mbinguni, wakizungumza naye kwa karibu. Nao ni Musa, aliyezungumza na Mungu kwenye Mlima Sinai; na Eliya, aliyepewa upendeleo wa juu – ambao haujatolewa kwa mtu mwingine isipokuwa mmoja wa wana wa Adamu – kwamba hatapita katika nguvu ya mauti.

Kwenye kilele cha Mlima Pisga, karne kumi na tano zilizokuwa zimepita, Musa alikuwa amesimama akilitazama bonde la Nchi ya ahadi. Lakini kwa sababu ya dhambi yake aliyofanya kule Meriba, asingeingia katika nchi ile. Furaha ya kuyaongoza majeshi ya Israeli kuuendea urithi wa baba zao haikuwa kwa ajili yake. Kusihi kwake kwa uchungu kwamba, "Nami nakuomba nivuke, nikaione hiyo nchi nzuri iliyoko ng'ambo ya Jordani, mlima ule mzuri, na Lebanoni." (Kumbukumbu 3:25), kulikataliwa. Lazima lile tumaini ambalo kwa miaka arobaini lilikuwa limemlika katika giza la kuzunguka-zunguka jangwani likataliwe. Kaburi la kule nyikani ndilo lilikuwa lengo la miaka yote ile ya masumbuko na ya mzigo wa moyoni. Lakini Yeye "awezaye kufanya mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyaombayo au tuyawazayo" (Waefeso 3:20), alikuwa amejibu ombi la mtumishi wake kwa kipimo hicho. Musa alipita chini ya nguvu za mauti, lakini asingebaki kaburini. Kristo mwenyewe ndiye aliyemwita kwamba apate kuishi. Shetani aliye mjaribu alidai kwamba mwili wa Musa ni wake kwa sababu alitenda dhambi; lakini Kristo aliye Mwokozi alimtoa kaburini. Yuda1:9.

Pale kwenye mlima wa kubadilikia sura Musa alikuwa shahidi wa ushindi wa Kristo dhidi ya dhambi na mauti. Aliwakilisha wale watakaofufuka **(422)** kutoka makaburini wakati wa ufufuo wa wenye haki. Eliya, aliyekuwa amebadilishwa na kutwaliwa mbinguni pasipo kuona mauti, anawakilisha wale watakaokuwa hai duniani wakati Kristo atakapokuja mara ya pili, na ambao watabadilika "kwa dakika moja, kufumba na kufumbua, wakati wa parapanda ya mwisho;" wakati ambao "huu uharibikao" utavaa "kutokuharibika, nao huu wa kufa uvae kutokufa." 1 Wakorintho 15:51-53. Yesu alivalishwa nuru ya mbinguni, vile atakavyoonekana wakati atakapokuja "mara ya pili, pasipo dhambi, kwa hao wamtazamiao kwa wokovu." Maana atakuja "katika utukufu wa Baba yake pamoja na malaika watakatifu." Waebrania 9:28; Marko 8:38. Sasa ile ahadi ya Mwokozi kwa wanafunzi ilitimizwa. Kwenye mlima ule utukufu wa ufalme ujao uliwakilishwa japo kwa kiasi kidogo, - Kristo Mfalme, Musa aliye mwakilishi wa watakatifu waliofufuliwa, na Eliya anayewakilisha wale watakaobadilishwa na kutwaliwa wakiwa hai.

Bado wanafunzi wale hawaelewi hali ile; lakini wanafurahia kwamba Mwalimu yule mwenye subira, mpole na mnyenyekevu, ambaye amezunguka-zunguka huku na huko akiwa mgeni mwenye kuhitaji, anaheshimiwa na viumbe waliopendelewa kuwa mbinguni. Wanaamini kwamba Eliya amekuja kutangaza rasmi utawala wa Masihi, na ya kwamba ufalme wa Kristo unakaribia kuanzishwa duniani. Kumbukumbu za hofu yao na hali yao ya kufadhaika ingetoweka milele. Walitamani kukawilia mahali hapa penye udhihirisho wa utukufu wa Mungu. Petro akasema kwa kushangaa kwamba, "Rabi, ni vizuri sisi kuwapo hapa; na tufanye vibanda vitatu, kimoja chako wewe, kimoja cha Musa, na kimoja cha Eliya." Wanafunzi hawa wana uhakika kwamba Musa na Eliya walikuwa wametumwa ili kumlinda Bwana wao, na kuanzisha mamlaka yake kama mfalme.

Lakini lazima msalaba uje kabla ya taji. Somo la mkutano wao na Yesu si uzinduzi wa ufalme wake, bali kifo kitakachotekelezwa kule Yerusalemu. Akiwa amebeba udhaifu wa kibinadamu, na kuelemewa na huzuni na dhambi za wanadamu, Yesu alienenda peke yake katikati ya wanadamu. Kadiri giza la mateso yaliyokuwa mbele yake lilivyomfunika, alikuwa katika upweke wa roho, katika ulimwengu ambao haukumjua. Hata na wanafunzi wake wapendwa, waliokuwa wamemezwa katika mashaka yao na huzuni na matarajio ya tamaa, hawakuwa wameelewa siri ya utume wake. Alikuwa amekaa katika upendo na mjumuiko pamoja na mbingu; lakini katika ulimwengu aliouumba, alikuwa katika hali ya upweke. Sasa mbingu ilikuwa imetuma wajumbe wake kwa Yesu; si malaika, bali wanadamu waliokuwa wamestahimili mateso na huzuni, na ambao wangemfariji Mwokozi katika wakati huu wa kujaribiwa kwa maisha yake ya duniani. Musa na Eliya walikuwa wamekuwa watenda-kazi pamoja na Kristo. Walikuwa wameshirikiana kutumika kwa ajili ya wokovu wa watu. Musa alikuwa amewahimiza Waisraeli akisema: "Walakini sasa, ikiwa utawasamehe dhambi yao . . . na kama sivyo, unifute, nakusihi, katika kitabu chako ulichoandika." Kutoka 32:32. Eliya **(425)** alikuwa amepata kujua upweke wa roho, maana kwa muda wa miaka mitatu na nusu ya njaa alikuwa amebeba mzigo wa kuchukiwa na taifa hilo. Alikuwa amesimama peke yake kwa ajili Mungu pale kwenye Mlima Karmeli. Akiwa peke yake alikuwa amekimbilia jangwani kwa sononeko na kukosa tumaini. Watu hawa, wakiwa wamechaguliwa juu ya kila malaika anayekizunguka kiti cha enzi, walikuwa wamekuja kushiriki na Yesu habari za matukio ya mateso yake, na

kumpa uhakika wa faraja ya mbinguni. Tumaini la ulimwengu, wokovu wa kila mwanadamu, ulikuwa ndio mzigo wa mazungumzo yao.

Kwa kuzidiwa na usingizi, wanafunzi wale walisikiliza kidogo sana katika yale yaliyozungumzwa kati ya Kristo na wajumbe wale wa mbinguni. Wakiwa wameshindwa kukesha na kuomba, wakawa hawakupokea kile ambacho Mungu alitaka kuwapa, - kujua habari za mateso ya Kristo, na ule utukufu ambao ungefuata. Walipoteza mibaraka ambayo ingekuwa yao kwa kushiriki katika kujitoa kwake kafara. Wanafunzi hawa walikuwa na mioyo isiyo na wepesi wa kuamini, wakitambua kidogo ile hazina ambayo mbingu ilitaka kuwabariki kwayo.

Lakini walipokea nuru kuu. Walihakikishiwa kwamba mbingu ilijua dhambi ya Wayahudi kwa kumkataa Kristo. Walipewa uelewa zaidi wa kazi ya Mkombozi. Waliona kwa macho yao na kusikia kwa masikio yao kilichokuwa mbali na uwezo wa mwanadmu kuelewa. Walikuwa wameuona wenyewe ukuu wake (2 Peter 1:16), na waliona kwamba Yesu alikuwa Masihi kweli, aliyeshuhudiwa na wazee na manabii, na kwamba alitambuliwa hivyo na malimwengu.

Walipokuwa bado wanaangalia mambo yale pale mlimani, "tazama, wingu jeupe likawatia uvuli; na tazama, sauti ikatoka katika lile wingu, ikasema, Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye; msikieni yeye." Pindi walipoliangalia wingu lile la utukufu, liking'aa zaidi ya lile lililotangulia mbele ya makabila ya Israel kule jangwani; pindi waliposikia sauti ya Mungu akitamka kwa utisho ule uliosababisha mlima kutetemeka, wale wanafunzi walianguka chini. Walibaki wamelala kifudifudi, nyuso zao zikiwa zimefichwa, mpaka Yesu alipokuja karibu, akawagusa, akiondosha hofu yao kwa sauti yake iliyojulikana kwao akisema, "Inukeni, wala msiogope." Walipojaribu kuinua macho yao, waliona kwamba utukufu ulikuwa umeondoka, mwonekano wa sura za Musa na Elija ulikuwa umetoweka. Walikuwa mlimani, wakiwa na Yesu peke yake.

## Sura ya 47

# Huduma

[Sura hii imejengwa katika Mathayo 17:9-21; Marko 9:9-29; Luka 9:37-45.]

Usiku wote ulikuwa umepita wakiwa mlimani; na wakati jua lilipochomoza, Yesu na wanafunzi wake wale walishuka kutoka mlimani kwenda kwenye uwanda ulio tambarare. Wakiwa wamezama mawazoni, wanafunzi wale walikuwa wameduwazwa na kubaki kuwa kimya. Hata Petro hakuwa na la kusema. Kwa furaha walitamani kuendelea kukawilia katika mlima ule uliokuwa umeguswa na nuru ya mbinguni, na mahali ambapo Mwana wa Mungu alikuwa amedhihirisha utukufu wake; lakini kulikuwa na kazi ya kufanya kwa ajili ya watu, ambao tayari walikuwa wakimtafuta Yesu sehemu za mbali na za karibu.

Chini ya mlima ule kulikuwa na kundi la watu waliokwisha kukusanyika, wakiwa wameletwa hapo na wanafunzi wale waliobaki, lakini wakijua alikokuwa amekwenda Yesu. Mwokozi alipokaribia, aliwataka wale wanafunzi watatu wasiseme kuhusu yale waliyoyaona, akisema, "Msimwambie mtu yeyote habari ya maono hayo, hata Mwana wa Adamu atakapofufuka katika wafu." Ufunuo ule uliofanywa kwa wale wanafunzi ulikuwa utafakariwe mioyoni mwao tu, na wala si wa kutangazwa mbali. Kuusimulia kwa makutano kungeamsha dhihaka na hamaki isiyo na maana. Hata wale wanafunzi tisa wasingejua habari hizo mpaka baada ya kufufuka kwake. Ni kwa kiasi gani hata wale wanafunzi watatu waliopendelewa walivyokuwa bado na hali ya kuchelewa kuelewa, inaonekana wakiwa katika ile hali ya kwamba licha ya Kristo kuwaonyesha mambo yatakayokuwa, walijiuliza maana ya kufufuka kutoka **(427)** kwa wafu. Lakini hawakuomba ufafanuzi kwa Yesu. Maneno yake kuhusu mambo yajayo yalikuwa yamewajaza huzuni; hawakutaka mafunuo zaidi kuhusu mambo yale ambayo walipenda kuamini kwamba yasingetokea kamwe.

Watu waliokuwa chini katika uwanda ule walipomwona Yesu, walikimbia kwenda kumlaki, wakimsalimu kwa nyuso za furaha na heshima. Lakini jicho lake la haraka liliona kwamba walikuwa wanatatanika. Wanafunzi walionekana kama wanasumbuka. Hali iliyokuwa imetokea ilikuwa imesababisha mfadhaiko mchungu na maumivu.

Wakati walipokuwa wanasubiri pale chini ya mlima, baba mmoja alikuwa ameleta kwa wanafunzi mwana wake, ili aponywe na roho chafu waliomtia kifafa na kumtesa. Mamlaka juu ya roho wachafu, kuwatoa nje ya watu, ilikuwa imetolewa kwa wanafunzi wakati ule Yesu alipowatuma wale kumi na wawili kwenda katika Galilaya yote. Na walipoenda wakiwa na imani yenye nguvu, roho wachafu walikuwa wametii maneno yao. Sasa wakati huu walimwamuru kwa jina la Yesu yule pepo amtoke mtu yule; lakini pepo akawa anawadhihaki tu kwa kuonyesha uwezo wake. Wanafunzi wale, kwa kukosa neno la kueleza sababu ya kushindwa kwao, wakaona kwamba walikuwa wanashusha heshima yao na ya Bwana wao. Na katika umati huo kulikuwa na waandishi ambao walitumia nafasi hii vizuri kuwadhalilisha. Wakisogea karibu na wanafunzi wale, waliwauliza-uliza maswali, wakitaka kuthibitisha kwamba wale wanafunzi na Bwana wao walikuwa wadanganyaji. Wale marabi walitangaza kwa majigambo kwamba, hapa kulikuwa na pepo chafu ambaye asingeweza kushindwa na wanafunzi wale wala Bwana wao mwenyewe. Watu waliokuwepo walivutwa kuungana na upande wa waandishi wale, na hisia ya kejeli na dhihaka iliushika mkutano ule.

Lakini ghafla mashtaka yale yalikoma. Yesu na wanafunzi wale watatu walionekana wakija, na kwa haraka watu waligeuka kwenda kuwalaki. Ule usiku wa kuwa katika utukufu wa mbinguni ulikuwa umeacha alama za utukufu kwa Yesu na wenzake wale. Usoni mwao kulikuwa na nuru ambayo iliwashangaza waliowaona. Waandishi walirudi nyuma kwa hofu, wakati watu walipokuwa wakimkaribisha Yesu.

Kama mtu ambaye alishuhudia yote yaliyokuwa yametokea, Mwokozi aliingia katika tukio lile walilokuwa wanashindania, na akiwakazia macho wale waandishi aliuliza, "Mnajadiliana nini nao?"

Lakini mahali pa sauti za kujiamini na za ubishi zilizokuwepo kabla kukawa na ukimya. Ukimya ulikuwa umeuangukia umati wote. Sasa yule baba mwenye shida alipita katikati ya umati, naye akianguka miguuni pa Yesu, alisimulia habari za shida yake na kukata tamaa kwake. **(428)** Alisema, "Mwalimu, nimemleta mwanangu

kwako, ana pepo bubu; na kila ampagaapo, humbwaga chini, naye hutoka povu na kusaga meno na kukonda; nikasema na wanafunzi wako wamtoe pepo, wasiweze."

Akiwa anaangaliwa na umati ulioduwazwa, waandishi wabishi, na wale wanafunzi waliokuwa katika utata, Yesu aliisoma hali ya kutoamini katika kila moyo; na kwa sauti ya huzuni alisema, "Enyi kizazi kisichoamini, nikae nanyi hata lini? Nichukuliane nanyi hata lini?" Halafu akamwambia yule baba mwenye shida, "Mlete mwanao hapa."

Yule mvulana aliletwa, na mara macho ya Yesu yalipomwona, pepo yule akamwangusha chini na kumtia kifafa. Aligaagaa na kutoa povu, akitoa sauti zisizo za kawaida.

Kwa mara nyingine tena Mfalme wa uzima na mfalme wa nguvu za giza walikuwa wamekutana katika uwanja wa mapambano, - Kristo akiwa katika utimizaji wa kazi yake ya "kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao, . . . kuwaacha huru waliosetwa" (Luka 4:18), Shetani naye akiwa anatafuta kuwashikilia mateka katika utawala wake. Malaika wa nuru na majeshi ya malaika waovu, pasipo kuonekana, walikuwa wanasogea karibu ili kuliona lile pambano. Kwa muda kitambo, Yesu alimruhusu roho mchafu kudhihirisha nguvu zake, ili kwamba watazamaji waelewe uponyaji ambao ungefanyika muda si mrefu.

Umati ule ulitazama kwa hisia kali, yule baba akiwa na mahangaiko ya matumaini na hofu. Yesu akauliza, "Amepatwa na haya tangu lini?" Yule baba alisimulia kisa cha miaka mingi ya mateso, halafu akiwa kama mtu ambaye asingevumilia zaidi, alisema, "Lakini ukiweza neno lolote, utuhurumie, na kutusaidia." "Ukiweza!" Hata sasa bado yule baba alikuwa anahoji uwezo wa Kristo.

Yesu akamjibu, "Ukiweza! Yote yawezekana kwake aaminiye." Hakuna upungufu wa nguvu kwa upande wa Kristo; kupona kwa kijana yule kunategemea imani ya yule baba. Akibubujikwa machozi, kwa kutambua udhaifu wake, yule baba alijitupa katika wema wa Kristo, akilia hivi, "Naamini, nisaidie kutokuamini kwangu."

Yesu akamgeukia yule mgonjwa na kusema, "Ewe pepo bubu na kiziwi, mimi nakuamuru, mtoke huyu, wala usimwingie tena." Kukawa na kilio, mapambano yenye uchungu. Katika kutoka, pepo yule anaonekana kama vile anararua uhai wa mhanga yule. Yule mvulana akalala pasipo kutikisika, akiwa kama asiye na uhai. Makutano wananong'ona wakisema, "Amekufa." Lakini Yesu anamshika mkono, na kumwinua, anampeleka kwa babaye, akiwa amekamilika mwili na akili. Baba na mwanae wanalisifu jina la **(429)** Mponyaji wao. Makutano "wakashangaa, wakiuona ukuu wa Mungu," wakati wale waandishi, wakiwa wameshindwa na kuaibika, wanageuka na kuondoka zao kimya kimya kwa chuki.

"Ukiweza neno lolote, utuhurumie, na kutusaidia." Roho nyingi za watu zilizolemewa na dhambi zinatoa mwangwi wa ombi hilo. Na kwa wote hao, jibu la huruma la Mwokozi ni, "Ukiweza kuamini! Yote yawezekana kwake aaminiye." Imani ndiyo inayotuunganisha na mbingu, na kutuletea nguvu ya kukabiliana na nguvu za giza. Katika Kristo, Mungu ametoa nguvu kwa ajili ya kutiisha kila mvuto wa dhambi, na kupinga kila jaribu, hata liwe na nguvu kiasi gani. Lakini wengi huhisi kupungukiwa imani, na kwa hiyo wanabaki mbali na Kristo. Hebu nafsi hizi, zikiwa katika hali hiyo ya kukosa msaada na kutokustahili, zijitupe katika wema wa Mwokozi mwenye huruma. Usijiangalie wewe, bali mwangalie Kristo. Yeye aliyeponya wagonjwa na kutoa pepo wakati alipokaa miongoni mwa wanadamu ni yule yule Mwokozi mwenye uweza hata leo. Imani huja kwa neno la Mungu. Halafu chukua ahadi yake kwamba, "Yeyote ajaye kwangu sitampa nje kamwe." Yohana 6:37. Jitupe miguuni pake ukilia hivi, "Bwana, Naamini; nisaidie kutokuamini kwangu." Huwezi kupotea kamwe unapofanya hivyo - kamwe.

Ndani ya muda mfupi wale wanafunzi waliopendelewa wameona kiasi kikubwa cha utukufu na cha mateso. Wameona ubinadamu ukibadilika sura na kuwa katika mwonekano wa mfano wa Mungu, na halafu wakaona kama uliohafifishwa na kuwa na mfanano wa Shetani. Kutoka mlimani mahali ambapo Kristo ameongea na wajumbe kutoka mbinguni, na mahali sauti kutoka katika mng'ao wa utukufu ilipomtangaza kama Mwana wa Mungu, wamemwona Yesu akishuka kuja kukutana na mandhari ile ya kusisimua ya vurugu, yule kijana mwenye fujo, sura iliyopotoshwa, akisaga meno kwa maumivu ambayo hakuna uwezo wa mwanadamu ambao ungeyatuliza. Na Mponyaji huyu mwenye uweza, ambaye saa chache tu kabla alikuwa amesimama katika utukufu machoni pa wanafunzi wake waliokuwa wakishangaa, anainama ili kumwinua mateka huyu wa Shetani kutoka chini alipokuwa amelala akigaagaa, na anamrejeshea afya yake ya akili na mwili na kumrejesha kwa baba yake na nyumbani mwake.

Hili lilikuwa fundisho kupitia kielelezo cha ukombozi, - Yeye mwenye Uungu atokaye katika utukufu wa Baba anajishusha chini ili kuokoa kilichopotea. Liliwakilisha pia kazi ya wanafunzi wale. Maisha ya watumishi wa Mungu wale yasingekuwa tu kama yale ya kuwa pamoja na Yesu juu ya mlima, wakiwa katika saa za kuangaziwa na mwanga wa kiroho. Kuna kazi kwa ajili yao kule uwandani. Roho zilizo katika utumwa wa Shetani zinasubiri neno la imani na maombi ili kuziweka huru.

Wale wanafunzi tisa walikuwa bado wanatafakari katika uchungu wa kushindwa kwao; na wakati Yesu alipokuwa nao peke yao mara nyingine, walimwuliza, "Mbona sisi hatukuweza kumtoa?" Yesu akawajibu hivi, **(430)** "Kwa sababu ya upungufu wa imani yenu. Kwa maana, amin, nawaambia, Mkiwa na imani kiasi cha punje ya haradali mtauambia mlima huu, Ondoka hapa uende kule; nao utaondoka; wala halitakuwako neno lisilowezekana kwenu. Lakini namna hii haitoki ila kwa kusali na kufunga." Kule kutokuamini kwao, kulikowafungia mbali na vina vya huruma ya **(431)** Kristo, na hali waliyokuwa nayo ya kutojali kazi takatifu iliyokabidhiwa kwao, vilisababisha kushindwa kwao katika pambano lile dhidi ya nguvu za giza.

Maneno ya Kristo yanayoelekeza kwa kifo chake yalikuwa yameleta huzuni na mashaka. Na kile kitendo cha Yesu kuwachagua wanafunzi watatu tu na kwenda nao mlimani kiliamsha wivu wa wale tisa. Badala ya kuimarisha imani yao kwa maombi na kutafakari maneno ya Kristo, walizama katika kufadhaika na kulalamikiana. Katika hali hii ya giza walikuwa wameandamana na Shetani katika pambano.

Ili kufanikiwa katika pambano kama hilo lazima waje kazini wakiwa na roho iliyo tofauti na hiyo. Lazima imani yao iimarishwe kwa maombi ya dhati na kufunga, na kujinyenyekeza moyo. Lazima wawe watupu pasipo ubinafsi, nao wajazwe na Roho na nguvu za Mungu. Kumwomba Mungu kwa dhati na subira katika imani – imani iongozayo mtu kumtegemea Mungu katika mambo yote, na kujitoa kwa kazi yake kikamilifu bila kubakiza kitu – kunaweza kuwawezesha watu kupata msaada wa Roho Mtakatifu wakati wa vita ya kupambana na mamlaka na nguvu, watawala wa giza wa ulimwengu huu, na roho ovu zilizo katika nafasi za juu.

"Mkiwa na imani kiasi cha punje ya haradali mtauambia mlima huu, Ondoka hapa uende kule; nao utaondoka." Ingawa punje ya haradali ni ndogo sana, ina kanuni ile ile ya siri ya uhai inayofanya kazi ya kukuza miti mikubwa. Wakati punje ya haradali inaposihwa udongoni, kiini kile kidogo kinakuwa na kila kitu ambacho Mungu alitoa ili kuilisha, na kwa haraka inaota na kukua. Mkiwa na imani ya namna hiyo, mtalitegemea neno la Mungu, na kwa nguvu zote za msaada ambazo Mungu ameamuru. Kwa njia hiyo imani yenu itakuwa na nguvu, nayo itawasaidia kupata nguvu kutoka mbinguni. Vizuizi vyote vinavyorundikwa na Shetani njiani mwenu, ingawa kwa kawaida vinaonekana kama havivukiki kama ilivyo milima ya milele, vitatowesha na madai ya imani kwamba, "Halitakuwako neno lisilowezekana kwenu."

## Sura ya 48

# Nani Aliye Mkuu?

[Sura hii imejengwa katika Mathayo 17:22-27; 18:1-20; Marko 9:30-50; Luka 9:46-48.]

Aliporudi Kapernaumu, Yesu hakutembelea sehemu zilizojulikana sana mahali alikokuwa amefundisha watu, bali Yeye na wanafunzi wake walitafuta kimya-kimya nyumba ambayo ingekuwa makazi yake ya muda. Katika muda uliobaki wa kukaa kwake Galilaya lengo lake lilikuwa kuwafundisha wanafunzi kuliko kufanya kazi kwa ajili ya makutano.

Katika safari yake kupitia Galilaya, kwa mara nyingine tena Kristo alijaribu kuandaa akili za wanafunzi wake kwa ajili ya matukio yaliyokuwa mbele yake. Aliwaambia kwamba ilikuwa aende Yerusalemu kuuawa na kufufuka. Na aliongeza kwao tangazo geni kwao na muhimu kwamba angesalitiwa mikononi mwa adui zake. Hata sasa wanafunzi wale hawakuelewa maneno yake. Ingawa kivuli cha huzuni kuu kilikuwa juu yao, roho ya mashindano ilipata nafasi mioyoni mwao. Walibishana wao kwa wao kuhusu nani aliye mkuu katika ufalme wa mbinguni. Walifikiria kwamba wafiche hali hiyo ili Yesu asijue magomvi hayo, na kama kawaida yao, hawakumsogelea kwa karibu, bali walibaki kwa nyuma, kiasi kwamba Yeye aliwatangulia mbele wakati huu walipokuwa wakiingia Kapernaumu. Yesu alisoma mawazo yao, naye alitamani kuwashauri na kuwafundisha. Lakini alisubiri wakati wa utulivu ndipo afanye hilo, wakati ambapo mioyo ingekuwa wazi kupokea maneno yake.

Mara walipokuwa wamefika mjini, mtu akusanyaye mapato ya hekalu alikuja kwa Petro na kumwuliza swali, "Je! Mwalimu wenu hatoi nusu-shekeli?"

**(433)** Huu ushuru haukuwa kodi ya serikali, bali malipo ya kidini, ambayo yalitakiwa kulipwa na kila Myahudi kila mwaka kwa ajili ya kulitegemeza hekalu. Kukataa kulipa mchango huu kungechukuliwa kama kitendo cha kukosa heshima kwa hekalu, - na kwa maoni ya marabi ilikuwa ni dhambi kubwa sana. Mtazamo wa Mwokozi kwa sheria za kirabi, na kemeo lake la wazi kwa watu wanaotetea mapokeo, vilisababisha tuhuma kwamba alikuwa anataka kupindua shuguli za hekaluni. Sasa adui zake walipata nafasi ya kuonyesha mashaka yao kwake. Walipata njia ya kumpinga kupitia kwa yule mkusanyaji wa ushuru.

Katika swali lile la mkusanyaji wa ushuru wa hekalu, Petro aliona viashiria vinavyogusia heshima ya Kristo kwa hekalu. Akiwa na bidii katika kutunza heshima ya Mwalimu wake, alijibu kwa haraka, hata bila kumwuliza kwanza, kwamba Yesu angelipa kodi hiyo.

Lakini Petro alielewa kwa sehemu tu kusudi la mwuliza-swali yule. Kulikuwa na makundi fulani ya watu ambao hawakutakiwa kulipa kodi hiyo. Mnamo wakati wa Musa, wakati Walawi walipotengwa rasmi kwa ajili ya huduma ya patakatifu, hawakupewa urithi miongoni mwa watu. Bwana alisema hivi, "Ndipo asiwe na fungu Lawi, wala urithi pamoja na nduguze; Bwana ndiye urithi wake, kwa mfano wa vile alivyomwambia Bwana, Mungu wako." Kumbukumbu 10:9. Mnamo nyakati za Kristo makuhani na Walawi walikuwa bado wanachukuliwa kama waliotengwa namna hiyo kwa ajili ya hekalu, na hawakutakiwa kutoa michango kwa ajili ya kulitegemeza hekalu. Hata manabii pia hawakudaiwa kulipa mchango huo. Katika kule kutaka kodi hiyo kutoka kwa Yesu, marabi hawakujali hadhi yake kwamba Yeye ni nabii na mwalimu, na walimchukulia kama mtu wa kawaida. Kukataa kwake kulipa kodi hiyo kungechukuliwa kama kutoheshimu hekalu; wakati, kwa upande mwingine, kulipa kodi hiyo kungechukuliwa kama uhalalishaji wa sababu ya kutomtambua kama nabii.

Muda mfupi tu kabla, Petro alikuwa amemkiri Yesu kwamba ni Mwana wa Mungu; lakini sasa alijikosesha fursa ya kuonyesha tabia hiyo ya Mwalimu wake. Kwa jibu lake lile alilompa mkusanyaji wa ushuru, kwamba Yesu angelipa kodi, alikuwa ameweka wazo lisilo sahihi kumhusu Yesu, ambalo kwalo makuhani na wakuu walikuwa wanalifanya likubalike.

Petro alipoingia katika nyumba, Mwokozi hakuongelea kile kilichokuwa kimetokea, bali aliuliza hivi, "Waonaje, Simoni? Wafalme wa dunia hutwaa kodi ama ushuru kwa watu gani? Kwa wana wao au kwa wageni??" Petro akajibu, "Kwa wageni." Na Yesu akasema, "Basi, kama ni hivyo, wana ni mahuru." Wakati wenyeji wa nchi wanalipishwa kodi kwa ajili ya shughuli za mfalme, watoto wenyewe wa mtawala hawahusishwi kuilipa. Ndivyo

ilivyo kwa Israeli, watu waliotajwa kuwa watu wa Mungu, walitakiwa **(434)** kukidhi mahitaji ya huduma zake, lakini Yesu, Mwana wa Mungu, hakuwa na jukumu hilo. Ikiwa makuhani na Walawi hawakuhusika kulipa huo ushuru kwa sababu ya kuhusika kwao na hekalu, itakuwa kiasi gani kwa Yeye ambaye hekalu ni la Baba yake.

Ikiwa Yesu angelipa ushuru ule bila kupinga, angekuwa amekubali uhalali wa madai yale, na hivyo angekuwa ameukana uungu wake. Lakini wakati Yeye aliona ni vema kulitekeleza hilo, aliukana msingi wa Yeye kulifanya hilo. Katika kuwezesha kulipa ushuru huo alitoa ushahidi wa uungu wake. Ilidhihirika kwamba alikuwa mmoja na Mungu, na kwa hiyo hakuwa chini ya matakwa ya ushuru ule kama alivyo raia wa kawaida.

"Enenda baharini ukatupe ndoana," alisema Yesu, "ukatwae samaki yule azukaye kwanza; na ukifumbua mdomo wake utaona shekeli; ichukue hiyo ukawape kwa ajili yangu na kwa ajili yako."

Ingawa alikuwa ameuvalisha uungu wake uanadamu, katika mwujiza huu alidhihirisha utukufu wake. Iliwekwa wazi kwamba huyu alikuwa Yule ambaye kupitia Daudi ilitangazwa kwamba, "Maana kila hayawani ni wangu, Na makundi juu ya milima elfu. Nawajua ndege wote wa milima, Na wanyama wote wa mashamba ni wangu. Kama ningekuwa na njaa singekuambia, Maana ulimwengu ni wangu, navyo viujazavyo." Zaburi 50:10-12.

Wakati Yesu aliweka wazi kwamba hakuwa na wajibu wa kulipa ushuru ule, hakuingia katika mapambano na Wayahudi kuhusu jambo hilo; maana wangeyatafsiri vibaya maneno yake, na kuyageuza ili kuyatumia kumpinga. Ili asionekane mhalifu kwa kuacha kulipa ushuru, alifanya kile ambacho kwa haki asingetakiwa kukifanya. Fundisho hili lingekuwa la thamani kubwa kwa wanafunzi wake. Muda si mrefu mabadiliko yaliyo bayana yalikuwa yatokee kuhusiana na huduma za hekalu, na Kristo aliwafundisha kutojiweka katika upinzani pasipo ulazima ili kuwa na utaratibu. Kwa kiasi kikubwa iwezekanavyo walipaswa wazuie hali ya kutoa nafasi ya kueleweka vibaya kwa imani yao. Wakati Wakristo hawapaswi kuacha hata kanuni moja ya ukweli, wanapaswa wazuie mapambano kila inapowezekana kufanya hivyo.

Wakati Kristo na wanafunzi walipokuwa peke yao mle ndani ya nyumba, wakati Petro alipokuwa ameenda baharini, Yesu aliwaita wale wengine kwake, na akawauliza, "Mlishindania nini njiani??" Kule kuwepo kwa Yesu, na swali lake, kuliliweka jambo lile katika nuru kubwa iliyo tofauti na vile lilivyokuwa wakati walipokuwa wakishindana **(435)** kule njiani. Aibu na hali ya kuhukumiwa ndani viliwafanya kuwa kimya. Yesu alikuwa amewaambia kwamba angekufa kwa ajili yao. Na tamaa yao ya ubinafsi ilikuwa inakinzana na upendo wake usio na ubinafsi.

Wakati Yesu alipowaambia kwamba angeuawa na kufufuka tena, alikuwa anajaribu kuwavutia katika mazungumzo yanayohusu jaribu kuu la imani yao. Ikiwa wangekuwa tayari kupokea kile alichotamani wajue, wangeepuka maumivu machungu na kukata tamaa. Maneno yake yangekuwa faraja katika saa ya kuondokewa na mpendwa wao iliyo ya kufadhaisha. Lakini ingawa alisema kwa uwazi kile kilichokuwa kinamngoja, kule kutaja kwake kwamba baadaye angeenda Yerusalemu tena kuliamsha matumaini yao kwamba ufalme wake ulikuwa uanzishwe. Hali hii ilisababisha maswali yao kuhusu nani watakaoshika nafasi za juu kabisa katika serikali yake. Petro aliporudi kutoka baharini, wanafunzi wale walimwambia kuhusu swali waliloulizwa na Yesu, na hatimaye mtu mmoja aliamua kumwuliza Yesu swali, "Ni nani basi aliye mkuu katika ufalme wa mbinguni?"

Yesu aliwakusanya wanafunzi wake kwake, akawaambia, "Mtu atakaye kuwa wa kwanza atakuwa wa mwisho kuliko wote, na mtumishi wa wote." Katika maneno haya kulikuwa na umakini na mguso ambao wanafunzi walikuwa mbali sana kiasi kwamba hawakuuelewa. Hawakuweza kuona kile ambacho Kristo aliona. Hawakuuelewa ufalme wa Kristo, na kutokujua huku kulikuwa ndiyo sababu ya juu juu ya mashindano yao. Lakini sababu halisi ilikuwa ya kina zaidi. Kwa kueleza jinsi ulivyo hasa ufalme wake, Kristo angeweza kukomesha magomvi yao; lakini hili lisingeweza kugusa sababu yenyewe iliyojificha. Hata baada ya kujua jambo hilo kwa ukamilifu, suala jingine lolote ambalo lingeonekana kuwa kipaumbele lingeleta shida ile ile. Kwa hiyo janga lingeletwa kwa kanisa baada ya Yeye kuondoka. Kugombania cheo cha juu ilikuwa ishara ya nje ya utendaji wa roho ile ile iliyokuwa ndiyo mwanzo wa pambano kuu katika malimwengu ya huko juu, na ambalo limemleta Kristo kutoka mbinguni ili afe. Mbele ya Kristo yalikuja maono kuhusu Lusifa, "mwana wa asubuhi," aliye na utukufu upitao ule wa malaika wote wazungukao kiti cha enzi, na aliyeunganishwa na Mwana wa Mungu kwa vifungo vya karibu zaidi. Lusifa alikuwa amesema, "Nitafanana na Yeye Aliye Juu" (Isaya 14:12, 14); na tamaa ya kujiinua ilikuwa imeleta magomvi katika viwanja vya kule mbinguni, na ilikuwa imeondosha kundi kubwa la

majeshi ya Mungu. Ikiwa Lusifa angetamani kweli kufanana na Yeye Aliye Juu, asingeondoka kamwe katika nafasi yake aliyopewa mbinguni; maana roho yake Aliye Juu inadhihirika katika utumishi usio na ubinafsi. Lusifa alitamani mamlaka ya Mungu, wala si tabia ya Mungu. Alijitafutia **(436)** cheo cha juu, na kila kiumbe anayesukumwa na roho yake atafanya hivyo hivyo. Kwa hiyo kujitenga, hali ya kupishana, na magomvi havitaepukika. Utawala huchukuliwa na mwenye nguvu zaidi. Ufalme wa Shetani ni ufalme wa kulazimisha; kila mtu anamwona mtu mwingine kama kizuizi kinachomzuia kuifikia nafasi ya juu, au anamtumia kama jiwe la kukanyaga ili kupigia hatua ya kwenda katika nafasi ya juu zaidi.

Wakati Lusifa aliona ni jambo muhimu kwake kuonekana kuwa sawa na Mungu, Kristo, Yeye Aliyetukuzwa, "alijifanya kuwa hana utukufu, akatwaa namna ya mtumwa, akawa ana mfano wa wanadamu; tena, alipoonekana ana umbo kama mwanadamu, alijinyenyekeza akawa mtii hata mauti, naam, mauti ya msalaba." Wafilipi 2:7, 8. Sasa msalaba ulikuwa mbele yake; na wanafunzi wake walikuwa wamejawa na hali ya tamaa binafsi – kanuni ile ile ya ufalme wa Shetani – kiasi kwamba hawakuweza kuwa na moyo wa huruma pamoja na Bwana, au hata kumwelewa alipoongea kuhusu kufedheheshwa kwake kwa ajili yao.

Kwa upole sana, lakini kwa msisitizo wa nguvu, Yesu alijaribu kusahihisha ule uovu. Alionyesha kanuni ile iliyo katika ufalme wa mbinguni, na kuonyesha kile kinachounda ukuu wa kweli, kama zinavyoonwa katika viwango vya huko juu mbinguni. Wale waliokuwa wanasukumwa na kiburi na kupenda makuu walikuwa wakijiwazia wenyewe, na kuwazia thawabu ambazo wangepata, badala ya namna ambavyo wangemrudishia Mungu thawabu ambazo walikuwa wamepata. Wasingekuwa na nafasi katika ufalme wa mbinguni, maana wangekuwa wamejiweka katika fungu la Shetani.

Kabla ya kuheshimiwa kuna unyenyekevu. Ili kukalia nafasi ya juu machoni pa wanadamu, Mbingu huchagua mtenda-kazi ambaye, kama alivyokuwa Yohana Mbatizaji, anachukua nafasi ya chini mbele za Mungu. Mwanafunzi aliye kama mtoto zaidi ndiye aliye na ufanisi katika kazi kwa ajili ya Mungu. Hekima za mbinguni zinaweza kushirikiana na yeye anayetafuta kuokoa roho, wala si atafutaye kujiinua binafsi. Yeye anayejihisi kuwa na uhitaji wa kina wa msaada wa kimbingu ataupata, na Roho Mtakatifu atampatia viasharia vya kumwona Yesu ambavyo vitamtia nguvu na kuiinua roho yake. Akitokea katika hali ya kujumuika pamoja na Kristo ataenda kufanya kazi kwa ajili ya wale wanaopotea katika dhambi zao. Ametiwa mafuta kwa ajili ya kazi yake; na anafanikiwa mahali ambapo watu wengi waliosoma na wenye akili sana wangeshindwa.

Lakini wanadamu wanapojikweza, wakijidhania kwamba wao ni muhimu kwa ajili ya mafanikio ya mpango mkuu wa Mungu, Mungu anasababisha wawekwe kando. Inafanywa idhihirike kwamba Bwana hategemei watu hao. Kazi yake haisimami kwa sababu ya wao kuondolewa kazini humo, bali ndipo inasonga mbele kwa nguvu zaidi.

**(437)** Kwa wanafunzi wa Yesu kufundishwa kuhusu ukweli wa ufalme wake ilikuwa haitoshi kwao. Walichohitaji ilikuwa ni badiliko la moyo ambalo lingewaleta katika hali ya kupatana na kanuni za ufalme ule. Yesu alimwita kwake mtoto mdogo, akamweka katikati yao; halafu akimwinua yule mtoto mikononi mwake alisema, "Msipoongoka na kuwa kama vitoto, hamtaingia kamwe katika ufalme wa mbinguni." Urahisi, hali ya kujisahau, na upendo wa kutojitumainia wa mtoto mdogo ndizo sifa ambazo Mbingu inathamini. Hizi ndizo sifa za ukuu wa kweli.

Kwa mara nyingine tena Yesu aliwafafanulia wanafunzi wale kwamba ufalme wake hauna sifa za ukuu na mwonekano wa kidunia. Miguuni pa Yesu sifa zote hizi husahaulika. Tajiri na maskini, msomi na asiyesoma, wanakutana pamoja, bila wazo la hadhi wala cheo cha ulimwenguni. Wote wanakutana kama roho zilizonunuliwa kwa damu, kwa namna iliyo sawa wakiwa wategemezi kwake Yeye aliyewakomboa kwa ajili ya Mungu.

Nafsi iliyotubu na iliyo na uaminifu ni ya thamani mbele za Mungu. Anagonga muhuri wake kwa watu, si kwa kuangalia vyeo vyao, si kwa utajiri wao, si kwa ukuu wa elimu yao, bali kwa hali yao ya kuwa na umoja na Kristo. Bwana wa utukufu anaridhishwa na wale walio wapole na wanyenyekevu wa moyo. Daudi alisema, "Nawe umenipa ngao ya wokovu wako, . . . Na unyenyekevu wako" – kama sehemu katika tabia ya mwanadamu – "umenikuza." Zaburi 18:35.

"Mtu akimpokea mtoto mmoja wa namna hii kwa jina langu," Yesu alisema, "anipokea mimi; na mtu akinipokea mimi, humpokea, si mimi, bali yeye aliyenituma." "Bwana asema hivi, Mbingu ni kiti changu cha enzi, na dunia ni mahali pa kuweka miguu yangu; . . . lakini mtu huyu ndiye nitakayemwangalia, mtu aliye mnyonge, mwenye roho iliyopondeka, atetemekaye asikiapo neno langu." Isaya 66:1, 2.

Maneno ya Mwokozi yaliamsha hali ya kujiwekea mashaka katika hisia zao. Hakuna mtu mahsusi aliyekuwa amesemwa bayana katika jibu lile; lakini Yohana alisukumwa kuuliza kama kwa hali fulani kitendo chake kilikuwa sahihi. Akiwa na roho ya mtoto aliliweka jambo lake mbele za Yesu. Alisema, "Mwalimu, tulimwona mtu akitoa pepo kwa jina lako, ambaye hafuatani nasi; tukamkataza, kwa sababu hafuatani nasi."

Yakobo na Yohana walikuwa wamedhani kwamba kwa kumzuia mtu huyu walikuwa wamezingatia kuhifadhi heshima ya Bwana wao; walianza kuona kwamba walikuwa na wivu wao wenyewe. Walikiri kosa lao, nao wakakubali kemeo la Yesu kwamba, "Msimkataze, kwa kuwa hakuna mtu atakayefanya mwujiza kwa jina langu akaweza mara kuninenea mabaya." Hakuna watu ambao walijionyesha **(438)** kwa njia yoyote kuwa na urafiki na Yesu ambao wangekataliwa. Kulikuwa na watu wengi ambao walisukumwa na tabia na kazi za Kristo kwa kina, na ambao mioyo yao ilikuwa inafunguka katika imani; na lazima wanafunzi wale, ambao hawakuweza kusoma misukumo ya ndani, wawe waangalifu wasije wakakatisha tamaa nafsi hizi. Wakati ambapo Yesu hakuwa tena pamoja nao katika mwili, na kazi ikiwa imeachwa mikononi mwao, lazima wasipende kuwa na roho finyu ya kujiona kuwa rasmi, bali wadhihirishe tabia yenye upeo wa mbali inayowatia moyo watu ambayo walikuwa wameiona kwa Mwalimu wao.

Hali ya kwamba mtu haendani na mawazo au maoni yetu katika mambo yote tunayodhani ndiyo haitatuhalalisha kumzuia kufanya kazi kwa ajili ya Mungu. Kristo ni Mwalimu Mkuu; haitupasi kuhukumu wala kuamrisha, bali kwa unyenyekevu kila mmoja akae miguuni pa Yesu, na kujifunza kwake. Kila nafsi ambayo Mungu ameipa uhiari ni mfereji ambao kupitia huo Kristo atafunua upendo wake unaosamehe. Ni jinsi gani inatupasa kuwa waangalifu tusije tukakatisha tamaa mmoja wa wanaoibeba nuru ya Mungu, na kwa hiyo tukaizuia miale ambayo Mungu angeifanya iuangazie ulimwengu!

Hali ya mwanafunzi wa Yesu kuonyesha ukali au kutopendezwa na mtu aliyekuwa anavutwa na Kristo – kitendo kama kile cha Yohana cha kumkataza mtu kufanya miujiza katika jina la Yesu – ingeweza kuwa na matokeo ya kuigeuza miguu ya mtu huyo kwenda katika njia ya adui, na kusababisha kupotea kwa roho. Kwa yule afanyaye hivyo, Yesu alisema, "afadhali afungiwe jiwe la kusagia shingoni mwake, na kutupwa baharini.." halafu aliongeza kwamba, "Mkono wako ukikukosesha, ukate; ni afadhali kuingia katika uzima u kigutu, kuliko kuwa na mikono miwili, na kwenda zako jehanum, kwenye moto usiozimika; ambamo humo funza wao hafi, wala moto hauzimiki. Na mguu wako ukikukosesha, ukate; ni afadhali kuingia katika uzima, u kiwete, kuliko kuwa na miguu miwili, na kutupwa katika jehanum." Marko 9:43-45.

Kwa nini kuna lugha hii kali, ambapo hakuna nyingine kali zaidi ya hiyo? Ni kwa sababu "Mwana wa Adamu alikuja kukiokoa kilichopotea." Je wanafunzi wake waonyeshe hali ya kujali kidogo nafsi za wanadamu wenzao kuliko vile Aliye Mkuu wa mbinguni alivyoonyesha? Kila nafsi imegharimu bei isiyo na kipimo, na kwa hiyo inatisha kama nini dhambi ya kumgeuza mtu kwenda mbali na Kristo, ili kwamba kwake huyo upendo, fedheha na mateso ya Mwokozi yanakuwa kazi bure.

"Ole ni wa ulimwengu kwa sababu ya mambo ya kukosesha! Maana hayana budi kuja mambo ya kukosesha." Mathayo 18:7. Ulimwengu, ukisukumwa na Shetani, kwa hakika utawapinga wafuasi wa Kristo, na utajitahidi kuharibu imani yao; lakini ole wake yeye ambaye amebeba jina la Kristo, lakini bado anaonekana **(439)** akifanya kazi hiyo. Bwana wetu anaaibishwa na wale wanaodai kwamba wanamtumikia, lakini wakionyesha tabia yake isivyo sahihi; na watu wengi wanadanganywa, na kuongozwa kufuata njia za uongo.

Mazoea au matendo yoyote ambayo yanaweza kupeleka mtu dhambini, na kuleta hali ya kutoheshimiwa kwa Kristo, afadhali yangeachwa, kwa gharama yoyote. Kitu kisichomtukuza Mungu hakiwezi kumfaidi mtu. Mbaraka wa Mungu hauwezi kuandamana na mtu yeyote katika kukiuka kanuni za haki. Na dhambi moja inayofanywa inatosha huiharibu tabia, na kuwakosesha wengine. Ikiwa mguu au mkono unahitajika kukatwa, au hata jicho kung'olewa, ili kuuokoa na kifo mwili wote, tunahitaji bidii kiasi gani kuachana na dhambi, iileteayo nafsi kifo!

Katika huduma ya kaida za kidini, chumvi iliwekwa katika kila dhabihu. Hii, kama ulivyo ufukizaji wa uvumba, ilionyesha kwamba haki ya Kristo pekee ndiyo ingeifanya huduma ikubalike kwa Mungu. Akirejelea katika tendo hilo, Yesu alisema, "Kila dhabihu itatiwa chumvi." [Marko 9:49: maneno hayo hayaonekani katika aya hii katika toleo la Biblia la Kiswahili]. "Mwe na chumvi ndani yenu, mkakae kwa amani ninyi kwa ninyi." Wote ambao wangejitoa kama "dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu" (Warumi 12:1), lazima wapokee chumvi ihifadhiyo, haki ya Mwokozi wetu. Halafu wanakuwa "chumvi ya dunia," wakiyazuia maovu miongoni mwa wanadamu, kama vile chumvi izuiavyo kuharibika. Mathayo 5:13. Lakini ikiwa chumvi imepoteza nguvu yake; ikiwa kuna maneno tu kwamba kuna kumcha Mungu, bila kuwepo kwa upendo wa Kristo, hakuna nguvu kwa ajili ya mema. Maisha hayawezi kuleta nguvu ya ushawishi ulimwenguni. Ni kama Yesu asema kwamba, Nguvu zako na uwezo wako katika kuujenga ufalme wangu hutegemea vile unavyopokea Roho yangu. Lazima uwe mshirika wa neema yangu, ili kuwa mhifadhi wa uzima hadi uzima. Hapo ndipo kutakuwa hakuna mashindano, hakuna kujitafutia faida binafsi, hakuna tamaa ya cheo cha juu. Mtakuwa na upendo ule ambao haujitafutii faida, bali mafanikio ya mwingine.

Hebu mwenye dhambi atubuye akaze macho yake kwa "Mwana-kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu" (Yohana 1:29); na kwa kutazama, anapata kubadilishwa. Hofu yake inageuzwa na kuwa furaha, na mashaka yake huwa tumaini. Shukrani hububujika ndani yake. Moyo wa jiwe unavunjwa. Wimbi la upendo hufagia moyoni. Kristo anakuwa kisima cha maji yabubujikiayo uzima wa milele. Tunapomwona Yesu, aliye Mtu wa huzuni nyingi ajuaye sikitiko, afanyaye kazi ya kuokoa waliopotea, akifedheheshwa, akikejeliwa, akidhihakiwa, akifukuzwa kutoka mji mmoja hadi mwingine mpaka kazi yake ilipokamilika; tunapomtazama akiwa Gethsemane, akitokwa na matone makubwa ya jasho la damu, na akiwa msalabani akifa kwa maumivu, - tunapoona haya, ubinafsi hautakuwa na kitu kwetu tena. Kwa kumwangalia Yesu, tutaona aibu ya kutokupenda kwetu, udhaifu wetu, na kujipenda kwetu. **(440)** Tutahiari wenyewe kuwa kitu fulani au kutokuwa kitu chochote, ili ya kwamba tufanye huduma kwa moyo kwa ajili ya Bwana. Tutafurahi kuubeba msalaba nyuma ya Yesu, kustahimili majaribu, au mateso kwa ajili yake.

"Basi imetupasa sisi tulio na nguvu kuuchukua udhaifu wao wasio na nguvu, wala haitupasi kujipendeza wenyewe." Warumi 15:1. Hakuna nafsi iaminiyo katika Kristo itakayodharauliwa, hata kama imani yake ni dhaifu, na hatua za miguu yake ni dhaifu kama zile za mtoto mdogo. Katika yote ambayo yametupatia nafasi ya kuonekana kuwa juu kuliko wengine, - iwe ni elimu na ustaarabu, hali ya ukuu na uungwana, mafunzo ya Kikristo, uzoefu wa kidini, - tunalo deni kwa wale ambao wamejaliwa kidogo; na kwa namna iliyo katika uwezo wetu, tunatakiwa kuwahudumia. Ikiwa tuna nguvu, tunapaswa kuiinua mikono ya walio dhaifu. Malaika wa utukufu, ambao wakati wote wanautazama uso wa Baba aliye mbinguni, wanafurahia katika kuwahudumia wale walio wadogo. Watu wanaotetemeka, ambao wana tabia zinazokuwa vizuizi kwao, wako katika wajibu wetu maalum. Daima malaika wako mahali pale wanapohitajika zaidi, wakiwa pamoja na wale walio na vita ngumu zaidi ya kupambana na mambo yao binafsi, na ambao mazingira yanayowazunguka ni ya kukatisha tamaa zaidi. Na wafuasi wa kweli wa Kristo watashiriki katika huduma hii.

Ikiwa mmoja wa walio wadogo hawa atashindwa, na kutenda jambo baya dhidi yako, ni kazi yako kumrejesha. Usisubiri yeye ndiye aanze kuonyesha jitihada ya kupatana na wewe. Yesu alisema, "Mwaonaje? Mtu akiwa na kondoo mia, mmoja akampotea, je! Hawaachi wale tisa na tisini, akaenda milimani, na kumtafuta yule aliyepotea? Hata akipata kumwona, amin, nawaambia, amfurahia huyo zaidi, kuliko wale tisa na tisini wasiopotea. Vivyo hivyo haipendezi mbele za Baba yenu aliye mbinguni kwamba mmoja wa wadogo hawa apotee."

Katika roho ya upole, "ukijiangalia nafsi yako usije ukajaribiwa wewe mwenyewe," (Wagalatia 6:1), nenda kwa mtu aliyekukosea, na "ukamwonye, wewe na yeye peke yenu." Usimwaibishe kwa kuanika makosa yake kwa watu wengine, wala usilete hali ya kumwaibisha Kristo kwa kuitangaza dhambi au kosa la mtu alichukuaye jina la Kristo. Mara nyingi lazima ukweli usemwe wazi wazi kwa mtu aliyekosa; lazima aongozwe kuliona kosa lake, ili ya kwamba ageuke. Lakini haupaswi kumwamulia wala kumhukumu. Usijaribu kuonyesha kuwa u mwenye haki. Hebu jitihada zako zote ziwe ni kwa ajili ya kumrejesha. Katika kutibu majeraha ya moyo, kuna uhitaji wa kugusa kwa uangalifu sana, kuwa mwororo. Upendo pekee utiririkao kutoka kwake Yeye Atesekaye Kalvari ndio unaotumika hapa. Kwa upendo wa huruma, hebu ndugu na ashughulike na ndugu yake, akijua kwamba, ikiwa atafanikiwa, "ataokoa roho na mauti, na kufunika wingi wa dhambi." Yakobo 5:20.

**(441)** Lakini hata jitihada hii inaweza isifanikiwe. Hapo ndipo Yesu anaposema, "chukua pamoja nawe tena mtu mmoja au wawili." Huenda ushawishi wenu wa pamoja ukashinda pale mahali ambapo ushawishi wa awali haukufanikiwa. Kwa kule kutokuwa wahusika katika tatizo lile, watakuwa na uwezekano wa kutotenda kwa kupendelea, na hali hii itayapatia mashauri yao uzito mkubwa kwa mtu yule aliyekosa.

Ikiwa hatawasikia wao, mpaka hapo, jambo lile liletwe mbele ya kundi lote la waamini. Hebu washirika wa kanisa, kama wawakilishi wa Kristo, waungane kwa maombi na huruma ya dhati ili ya kwamba mkosaji apate kurejea. Roho Mtakatifu ataongea kupitia kwa watumishi wa Kristo, wakimsihi aliyetanga mbali arejee kwa Mungu. Paulo mtume, akiongea kwa uvuvio, anasema, "Kana kwamba Mungu anasihi kwa vinywa vyetu; twawaomba ninyi kwa ajili ya Kristo mpatanishwe na Mungu." 2 Wakorintho 5:20. Ikiwa akataa mambo yote haya amevunja kifungo kinachomfunga na Kristo, na kwa hiyo amejitenga na ushirika wa kanisa. Baada ya hapo, Yesu alisema, "na awe kwako kama mtu wa mataifa na mtoza ushuru." Lakini asiende akitambuliwa kama aliyefungiwa mbali na rehema ya Mungu. Hebu asidharauliwe wala kupuuzwa na watu waliokuwa nduguze, bali atendewe kwa wema na uvumilivu, kama mmoja wa kondoo waliopotea ambao bado Kristo anawatafuta awalete katika hema lake.

Fundisho la Kristo kuhusu kushughulika na mkosaji linarudia kwa umahsusi zaidi fundisho lililotolewa kwa Waisraeli kupitia Musa kwamba: "Usimchukie ndugu yako moyoni mwako; ni lazima kumkemea jirani yako, wala usichukue dhambi kwa ajili yake." Walawi 19:17. Maana yake ni kwamba, ikiwa mtu anapuuza wajibu aliopewa na Kristo, wa kujaribu kuwarejesha wale walio katika makosa na dhambi, anakuwa mshirika katika dhambi ile. Tunawajibika kwa maovu ambayo tungeweza kuyazuia kwa namna ambayo ni kama vile tunakuwa na hatia ya kuyatenda sisi wenyewe.

Lakini tunapaswa kuyasema maovu kwa mtu yule yule aliyeyatenda. Hatupaswi kulifanya kuwa suala la kutolea maoni na ukosoaji miongoni mwetu wenyewe; wala hata baada ya kuliambia kanisa, hatuna uhuru wa kuwasimulia wengine. Kujua makosa ya Wakristo kutakuwa sababu ya walimwengu wasioamini kujikwaa; na kwa kuzama katika mambo haya, sisi wenyewe tunaweza kupata madhara; maana kwa kuona tunabadilishwa. Tunapotafuta kusahihisha makosa ya ndugu, Roho ya Kristo itatuongoza kumfunika mtu huyo, kwa kiasi kikubwa iwezekanavyo, dhidi ya ukosoaji hata wa ndugu zake mwenyewe, na ikiwa ni hivyo ni kiasi gani tunatakiwa kufanya dhidi ya ukosoaji wa walimwengu wasioamini. Sisi wenyewe tunaanguka katika makosa, na tunahitaji upendo na msamaha wa Kristo, na vile tunavyotamani ashughulike nasi, ndivyo anavyotuhimiza tushughulikiane sisi kwa sisi.

**(442)** "Yoyote mtakayoyafunga duniani yatakuwa yamefungwa mbinguni; na yoyote mtakayoyafungua duniani yatakuwa yamefunguliwa mbinguni." Unatenda kama balozi wa mbingu, na suala la kazi yako ni kwa ajili ya umilele.

Lakini hatupaswi kubeba wajibu huu peke yetu. Popote neno lake linapotiiwa kwa moyo mkunjufu, Kristo anakuwepo mahali hapo. Si kwamba yuko katika mikusanyiko ya kanisa peke yake, bali popote wanafunzi, hata wawe wachache kiasi gani, wanapokutana kwa jina lake, yupo. Na anasema, "Wawili wenu watakapopatana duniani katika jambo lolote watakaloliomba, watafanyiwa na Baba yangu aliye mbinguni."

Yesu anasema, "Baba yangu aliye mbinguni," kama kuwakumbusha wanafunzi wake kwamba wakati akiwa katika uanadamu ameunganishwa nao, mshiriki katika majaribu yao, na akifarijiana nao katika mateso yao, kwa uungu wake ameunganishwa na kiti cha enzi cha Yeye wa Milele. Uhakika wa ajabu! Hekima za mbinguni zinaungana na wanadamu katika faraja na kazi kwa ajili ya kuokoa kile kilichopotea. Na nguvu zote za mbinguni huletwa kuunganishwa na uwezo wa wanadamu katika kuzivuta roho kwa Kristo.

## Sura ya 49

# Kwenye Sikukuu ya Vibanda

[Sura hii imejengwa katika Yohana 7:1-15, 37-39.]

Wayahudi walitakiwa kukusanyika Yerusalemu mara tatu katika mwaka kwa ajili ya mambo ya kidini. Akiwa amefunikwa na wingu, Kiongozi wa Israeli asiyeonekana alikuwa ametoa maagizo kuhusu mikusanyiko hii. Mnamo wakati wa kushikiliwa mateka kwa Wayahudi, mikusanyiko hii haikutekelezwa; lakini watu hao waliporejeshwa katika nchi yao, utunzaji wa kumbukumbu hizo ulianzishwa tena. Ilikuwa ni mpango wa Mungu kwamba sherehe hizi za kumbukumbu zimlete katika mawazo ya watu. Lakini makuhani na viongozi wa taifa walikuwa wamepoteza kuona makusudi ya maadhimisho hayo, isipokuwa katika vitu vichache. Yeye aliyekuwa ameweka wakfu makusanyiko haya ya kitaifa na kuelewa umuhimu wake alishuhudia upotokaji wao.

Sikukuu ya Vibanda ilikuwa kusanyiko la mwisho katika mwaka. Ilikuwa ni mpango wa Mungu kwamba wakati huu watu watafakari kuhusu wema na rehema zake. Nchi yote ilikuwa chini ya uongozi wake, ikipokea baraka zake. Utunzaji wake ulikuwa umeendelea usiku na mchana. Jua na mvua vilikuwa vimeifanya nchi izae mazao yake. Mazao yalikuwa yamekusanywa kutoka katika mabonde na milima ya Palestina. Mazao ya mizeituni yalikuwa yameokotwa, na mafuta yale ya thamani yalikuwa yamehifadhiwa katika chupa zao. Mitende ilikuwa imetoa mazao yake. Vichala vya mizabibu vilikuwa vimekamuliwa.

**(448)** Sikukuu hiyo iliendelea kwa siku saba, na kwa ajili ya kuisherehekea wakazi wa Palestina, pamoja na wengine kutoka katika nchi nyinginezo, waliondoka majumbani mwao, na kuja Yerusalemu. Watu hao walikuja kutoka maeneo ya mbali na karibu, wakija na zawadi za shukrani mikononi mwao. Wazee kwa vijana, matajiri kwa maskini, wote walikuja na matoleo kama mchango wa shukrani kwake Yeye aliyekuwa ameupamba mwaka mzima kwa wema wake, na kuzifanya njia zake zijazwe. Kila kitu ambacho kingeweza kupendezesha jicho, na kuleta mandhari ya kufurahisha kwa wote, kililetwa kutokana na miti; mji ulipata mwonekano wa msitu mzuri.

Sikukuu hii haikuwa kwa ajili ya shukrani za mavuno tu, bali kumbukumbu ya ulinzi wa utunzaji wa Mungu kwa Waisraeli walipokuwa jangwani. Kama kumbukumbu ya maisha yao ya mahemani wakati ule, wakati wa sherehe hizi Waisraeli waliishi katika mahema au makazi yaliyojengwa kwa matawi ya miti yenye kijani-kijani. Vibanda hivi vilijengwa mitaani, katika viwanja vya hekalu, au juu ya mapaa ya majumba. Milima na mabonde yanayozunguka mji wa Yerusalemu yalikuwa pia na mtawanyiko wa makazi haya ya majani, na yalionekana kuwa na watu.

Kwa wimbo mtakatifu na shukrani waabudu wale walisherehekea tukio hili. Muda mfupi kabla ya sherehe hii kulikuwa na Siku ya Upatanisho, ambapo, baada ya kuungama dhambi zao, watu walitangaziwa kuwa wana amani na Mbingu. Kwa hiyo njia ilikuwa imeandaliwa kwa ajili yao kufurahia sikukuu. Sauti za "Haleluya. Mshukuruni Bwana kwa kuwa ni mwema, Kwa maana fadhili zake ni za milele." (Zaburi 106:1) zilipanda juu kwa ushindi, wakati aina zote za muziki, zilichanganyika na sauti za shangwe, ziliandamana na kuimba kule. Hekaluni ndiko kulikuwa kitovu cha furaha. Hapa ndipo palipokuwa na maadhimisho hasa. Mahali hapa, kila upande wa ngazi za marumaru za jengo lile takatifu zilijipanga kwaya za Walawi walioongoza huduma ya nyimbo. Umati wa waabudu, wakipeperusha matawi ya mitende na mihadasi, waliimba nyimbo; na sauti zilipokelewa na watu waliokuwa sehemu za karibu na mbali, hadi vilima vilivyozunguka pale vikaitika kwa sauti za sifa.

Wakati wa usiku hekalu liliangazwa na nuru ya kutengenezwa. Ule muziki, matawi ya miti yanayopeperushwa, shangwe za hosanna, uwepo wa makutano ya watu wengi, ambao waliangaziwa na taa zilizoning'inizwa juu yao, mwonekano wa mapambo ya makuhani, na ukuu wa sherehe zile, viliunganika na kufanya mandhari yenye mvuto mkubwa kwa waliouona. Lakini tukio lenye mvuto mkubwa kuliko yote katika sherehe hizi, lile lililoleta furaha kubwa zaidi, ni lile la kumbukumbu yenyewe ya maisha ya ugenini jangwani.

Wakati wa kupambazuka kwa siku ya kwanza, makuhani walizipiga tarumbeta za fedha, na kelele za furaha za watu kutoka katika makambi yao, zikitoa mwangwi milimani na mabondeni, ziliikaribisha **(449)** siku hiyo ya sikukuu. Halafu kuhani alichota maji yanayotiririka ya kijito cha Kedroni kwa kombe, naye, akilinyenyua juu sana, huku tarumbeta zikipigwa, alizipanda ngazi za hekalu, akitembea kuendana na muziki uliokuwa unapigwa,

wakati mwingine akiimba-imba kwa kusema, "Miguu yetu imesimama Ndani ya malango yako, Ee Yerusalemu." Zaburi 122:2.

Alilibeba lile kombe mpaka kwenye madhabahu, ambayo ilikuwa katikati. Hapa kulikuwa na mabeseni mawili ya fedha, na kulikuwa na kuhani asimamaye mahali pa kila beseni. Maji ya lile kombe yalimiminwa katika beseni moja, na kombe jingine la divai lilimiminwa katika beseni nyingine; na kile kilichomiminwa katika kila moja ya yale mabeseni mawili kilitiririka kuelekea katika bomba lililounganishwa na kijito cha Kedroni, na vilivyotiririka humo vilielekea katika Bahari ya Chumvi. Onyesho hili la maji yaliyowekwa wakfu liliwakilisha lile bubujiko la maji ambalo kwa amri ya Mungu lilitoka katika mwamba na kupoza kiu ya wana wa Israeli. Halafu muziki wa sherehe ulipigwa ukiimba kwamba, "Bwana YEHOVA ni nguvu zangu na wimbo wangu;" "Basi, kwa furaha mtateka maji katika visima vya wokovu." Isaya 12:2, 3.

**(450)** Wakati wana wa Yusufu walipofanya maandalizi ya kwenda katika Sikukuu ya Vibanda, waliona kwamba Kristo alikuwa hafanyi jambo lolote linaloashiria nia yake ya kwenda kwenye sikukuu. Walimtazama kwa wasiwasi. Tangu ule uponyaji wa Bethzatha hakuwa amehudhuria mikusanyiko ya kitaifa. Ili kuzuia migongano na watawala wa Yerusalemu isiyo na sababu, kazi zake alizifanyia huko Galilaya. Mwonekano wake wa kupuuza mikutano mikuu ya kidini, na uadui aliofanyiwa na makuhani na marabi, viliwasababishia watu kutatanika kumhusu Yeye, na hata kuhusu wanafunzi wake na jamaa yake. Katika mafundisho yake alikuwa amejikita katika mibaraka inayopatikana kwa kuitii sheria ya Mungu, lakini Yeye mwenyewe alionekana kutoheshimu ibada ambazo zilikuwa zimewekwa kwa mamlaka ya kimbingu. Kuchangamana kwake na watoza ushuru na wengine wanaodhaniwa kutostahili, kutokujali kwake maadhimisho ya kirabi, na uhuru wake wa kuweka kando matakwa ya kimapokeo kuhusu Sabato, yote hayo yakionyesha kumweka katika hali ya uadui dhidi ya mamlaka za kidini, yaliibua maswali mengi. Kaka zake walifikiri kuwa ni kosa kwake kujitenga na wakuu wale na wasomi wa taifa lao. Walidhani kwamba lazima watu hawa wako sahihi, na ya kwamba Yesu alikuwa na makosa kwa kujiweka katika nafasi ya kuwapinga. Lakini walikuwa wameshuhudia maisha yake yasiyolaumiwa kitu, na ingawa hawakujilinganisha na nafasi ya wanafunzi, walikuwa wameguswa sana na kazi zake. Umaarufu wake huko Galilaya ulikuwa unawavuta hisia zao; bado walitarajia kwamba angetoa uthibitisho wa nguvu zake ambazo zingewafanya Mafarisayo waone kwamba alikuwa vile alivyodai kuwa. Yawezekana akawa ni Masihi, Mfalme wa Israeli! Waliendelea na mawazo haya kwa majivuno.

Walikuwa na dukuduku kuhusu mambo hayo kiasi kwamba walimtaka aende Yerusalemu. Walisema, "Ondoka hapa uende Uyahudi, wanafunzi wako nao wapate kuzitazama kazi zako unazozifanya. Kwa maana hakuna mtu afanyaye neno kwa siri, naye mwenyewe ataka kujulikana. Ukifanya mambo haya, basi jidhihirishe kwa ulimwengu." Hilo neno "ukifanya" linaashiria mashaka mashaka na kutokuamini. Walimhusianisha na tabia ya woga na udahifu. Ikiwa alijua kwamba Yeye ni Masihi, kwa nini anaonyesha hali ngeni ya kujificha na kuacha kutenda? Ikiwa kweli amejazwa nguvu hivyo, kwa nini asiende Yerusalemu kwa ujasiri, na kusema madai yake? Kwa nini kazi zile zinazosimuliwa kuwa alizifanya huko Galilaya asizifanyie Yerusalemu? Usijifiche katika majimbo yasiyo maarufu na kufanya maajabu makubwa kwa ajili ya wakulima na wavuvi wasio na elimu. Jionyeshe katika mji mkuu, pata kuungwa mkono na makuhani na wakuu, na unganisha taifa katika kuanzisha ufalme mpya.

**(451)** Hawa kaka za Yesu walitoa hoja zenye mwelekeo wa ubinafsi ulioonekana mara nyingi katika mioyo ya wale waliotamani kujionyesha wenyewe. Roho hii ilikuwa ndiyo roho itawalayo ulimwengu. Walichukizwa kwa sababu, badala ya kutafuta kiti cha enzi cha duniani, Kristo alijitangaza kuwa mkate wa uzima. Walikatishwa tamaa sana wakati wanafunzi wake wengi walipomwacha. Wao wenyewe wakageuka kutoka kwake ili kuukwepa msalaba wa kukiri kile ambacho kilidhihirishwa na kazi zake – kwamba Yeye ni Aliyetumwa na Mungu.

Ndipo Yesu akawaambia, "Haujafika bado wakati wangu; ila wakati wenu sikuzote upo. Ulimwengu hauwezi kuwachukia ninyi; bali hunichukia mimi, kwa sababu mimi naushuhudia ya kuwa kazi zake ni mbovu. Kweeni ninyi kwenda kula sikukuu; mimi sikwei bado kwenda kula sikukuu hii, kwa kuwa haujatimia wakati wangu. Naye alipokwisha kuwaambia hayo, alikaa vivi hivi huko Galilaya." Kaka zake walikuwa wamemwambia kwa sauti ya mamlaka, wakimwelekeza jambo ambalo anapaswa kufanya. Anarudisha karipio lao kwao wenyewe, akiacha kuwahesabu katika kundi lile la wanafunzi wake wenye kujikana nafsi, bali kwamba wako katika kundi

la ulimwengu. Alisema, "Ulimwengu hauwezi kuwachukia ninyi; bali hunichukia mimi, kwa sababu mimi naushuhudia ya kuwa kazi zake ni mbovu." Ulimwengu hauwachukii wale ambao wako vile ulivyo katika roho; unawapenda kama watu wake.

Kwa Kristo ulimwengu haukuwa mahali pa raha na pa kujikuza. Hakuwa anatafuta nafasi ya kupata madaraka au utukufu wa ulimwengu. Hiyo haikuwa zawadi ya ulimwengu kwa ajili yake. Ulimwengu ulikuwa mahali ambamo Baba yake alikuwa amemtuma. Alikuwa ametolewa kwa ajili ya uzima wa ulimwengu, ili kushughulikia mpango wa ukombozi. Alikuwa anafanya kazi yake kwa ajili ya wanadamu walioanguka. Lakini hakupaswa kujiamini sana, hakupaswa kujiingiza katika hatari, hakupaswa kuharakisha kuleta matatizo. Kila tukio katika kazi yake lilikuwa na saa yake iliyoamuriwa. Lazima asubiri kwa ustahimilivu. Alijua kwamba alikuwa akutane na chuki ya ulimwengu; alijua kwamba kazi yake ingeleta matokeo ya kifo chake; lakini kujiweka wazi kwa ajili ya hayo kabla ya wakati wake kusingekuwa mapenzi ya Baba yake.

Habari za miujiza ya Kristo zilikuwa zimeenea kutoka Yerusalemu kwenda kila mahali walikotawanyika Wayahudi; na ingawa kwa miezi mingi hakuwepo katika sherehe zilizofanyika, hamu ya watu kwake haikuwa imepungua. Watu wengi kutoka pande zote za ulimwengu walikuwa wamekuja kwenye Sikukuu ya Vibanda wakitumaini kumwona. Mwanzoni kabisa mwa sikukuu watu wengi walimwulizia. Mafarisayo na wakuu walimsubiria afike, wakitumainia kupata fursa ya kumhukumu. Waliulizia kwa hamu, "Yuko wapi yule?" lakini hakuna aliyejua. Kumfikiria kulikuwa kwa hali ya juu katika vichwa vya watu wote. Kwa kuogopa makuhani na wakuu, hakuna aliyethubutu kumkiri **(452)** kama Masihi, lakini kila mahali kulikuwa na mjadala wa kimya-kimya lakini mkali kumhusu Yeye. Wengi walimtetea kama Yeye aliyetumwa na Mungu, wakati wengine walimpinga kwamba ni mdanganyaji wa watu.

Wakati huo Yesu alikuwa amefika Yerusalemu kimya-kimya. Alikuwa amechagua kutumia njia ya kwenda ambayo haitumiwi na watu wengi, kwa lengo la kuepukana na wasafiri waliokuwa wanaenda mjini kutoka sehemu mbalimbali. Ikiwa angeungana na moja ya misafara iliyokuwa inaenda kwenye sikukuu, mwitikio wa watu wengi ungevutwa kwake wakati wa kuingia kwake katika mji ule, na maandamano makubwa ya watu kuonyesha kumpenda yangeziamsha mamlaka kusimama dhidi yake. Ili kuzuia hali hii aliamua kusafiri peke yake.

Katikati ya sikukuu, wakati msisimko wa shauku ya watu kumtafuta ulipokuwa katika kiwango cha juu, aliingia katika kiwanja cha hekalu mahali walipokuwa makutano. Kwa kule kutokuwepo katika sikukuu ile, watu walikuwa wamedhani kwamba hakupenda kujileta katika nguvu za makuhani na wakuu. Sasa wote walishangazwa na kuwepo kwake. Kila sauti ilinyamazishwa. Wote walishangazwa na heshima na ujasiri aliokuwa nao alipokuwa katikati ya adui zake wenye nguvu ambao walikuwa na kiu ya uhai wake.

Akiwa amesimama hivyo, katika mwonekano awe kama kitovu cha mvuto wa umati wote, Yesu aliwahutubia kwa namna ambavyo hajapata mtu kufanya. Maneno yake yalionyesha hali ya kuzijua **(453)** sheria na taasisi za Waisraeli, kujua ibada za kafara na mafundisho ya manabii, akionyesha kuwazidi kwa mbali makuhani na marabi. Alivunja na kuvuka vizuizi vya dini ya matendo yaliyo rasmi ya nje na ya mapokeo. Matukio ya siku za usoni yalikuwa kama yanaonekana mbele yake. Kama mtu aliyemwona Yeye Asiyeonekana, aliongelea mambo ya duniani na ya mbinguni, ya kibinadamu na ya kimbingu, akiwa na mamlaka. Maneno yake yalikuwa wazi sana na kushawishi, na kwa mara nyingine, kama ilivyokuwa kule Kapernaumu, watu walishangazwa na mafundisho yake; "Kwa kuwa neno lake lilikuwa na uwezo." Luka 4:32. Kwa kutumia mwonekano tofauti-tofauti aliwaonya wasikilizaji wake kuhusu ole ambayo ingewafuata wote waliokataa mibaraka aliyoleta. Alikuwa amewapatia kila aina ya uthibitisho uliowezekana kuonyesha kwamba alitoka kwa Mungu, na alifanya kila jitihada iliyowezekana kuwaleta katika toba. Asingekataliwa na kuuawa na watu wa taifa lake ikiwa angeweza kuwaokoa na hatia ya vitendo hivyo.

Watu wote walishangazwa na hali yake ya kujua sheri na manabii; na wakaulizana wao kwa wao, "Amepataje huyu kujua elimu, ambaye hakusoma?" Hakuna mtu aliyetambuliwa kuwa mwalimu wa dini isipokuwa amesoma katika shule za marabi, na wote wawili, Yesu na Yohana Mbatizaji, walikuwa wameelezwa kama watu wasio wasomi kwa sababu hawakuwa wamepata mafunzo hayo. Wale waliowasikiliza walishangazwa na kule kujua Maandiko kwa watu hawa ambao hawakusoma." Ni kweli hawakusomeshwa na wanadamu; lakini Mungu wa mbinguni ndiye aliyekuwa mwalimu wao, na kutoka kwake walikuwa wamepokea hekima ya hali ya juu.

Wakati Yesu alipokuwa akisema katika kiwanja kile cha hekalu, watu walishikwa na bumbuwazi. Watu wale wale waliokuwa na ubishi na waliompinga kwa kutumia mabavu walijikuta wakiwa hawana nguvu ya kumdhuru. Kwa muda, mambo mengine yote yalisahauliwa.

Siku baada ya siku aliwafundisha watu, mpaka siku ya mwisho, "siku ile kubwa ya sikukuu." Asubuhi ya siku hii watu walikuwa wamechoka kwa sababu ya vipindi virefu vya sikukuu hii. Ghafla Yesu alipaza sauti yake, kwa kubwa iliyosikika katika viwanja vya hekalu, akisema: "Mtu akiona kiu, na aje kwangu anywe. Aniaminiye mimi, kama vile maandiko yalivyonena, mito ya maji yaliyo hai itatoka ndani yake." Hali ya watu iliufanya wito huu kuwa na nguvu sana. Walikuwa wamejihusisha na maadhimisho ya kifahari ya maonyesho, macho yao yalikuwa yameg'arizwa kwa taa na rangi, na masikio yao yalikuwa yameshibishwa muziki wa kutosha; lakini hakukuwa na kitu katika mfululizo wote wa maadhimisho haya kilichokidhi mahitaji ya roho, hakuna **(454)** kilichotuliza kiu ya moyo kutaka kupata kile kisichoharibika. Yesu aliwaita waje wanywe kutoka katika chemchemi ya uzima, ambayo ingekuwa ndani yao kisima cha maji, yatiririkiayo uzima wa milele.

Asubuhi ile kuhani alikuwa ameongoza adhimisho la kumbukumbu la kuupiga mwamba kule jangwani. Mwamba ule ulikuwa ishara yake Yeye ambaye kwa kifo chake angesababisha mito iliyo hai ya wokovu kutiririka kwa wote walio na kiu. Maneno ya Kristo yalikuwa ni maji ya uzima. Pale mbele ya makutano wa waliokusanyika alijiweka pembeni apigwe, ili maji ya uzima yautiririkie ulimwengu. Katika kumpiga Kristo, Shetani alikuwa anatafuta kumwangamiza Mfalme wa uzima; lakini kutoka kwa mwamba huo uliopigwa kulitiririka maji ya uzima. Yesu alipowaambia watu mambo hayo, mioyo yao ilisisimshwa kwa mshangao usio wa kawaida, na wengi walikuwa tayari kusema, kama alivyosema yule mwanamke wa Samaria, kwamba, "Nipe maji hayo, nisione kiu tena." Yohana 4:15.

Yesu alijua mahitaji ya moyo. Maadhimisho ya kifahari, utajiri, heshima haviwezi kutosheleza mahitaji ya moyo. "Mtu akiona kiu, na aje kwangu." Walio matajiri, maskini, wenye cheo, walio wa hadhi ya chini, wanapokelewa kwa hali moja. Anaahidi kutuliza mawazo yenye mizigo, kufariji wenye huzuni, na kuwapa tumaini waliokata tamaa. Wengi wa wale waliomsikia Yesu walikuwa waombolezaji waliokata tamaa ya kupata tumaini, wengi walikuwa wanaishi katika majonzi ya siri, wengi walikuwa wanatafuta kutosheleza tamaa zao zisizokoma za kutaka vitu vya ulimwengu huu na za kutaka sifa za watu; lakini mara vyote vilipopatikana, walijikuta kwamba walikuwa tu wamesumbuka ili kulifikia tanki la maji lililopasuka, ambamo kutoka humo wasingepata kitu cha kupoza kiu yao. Walisalia kusimama katikati ya mandhari ya mng'ao wa furaha, pasipo kuridhika na wakiwa na huzuni. Ile sauti ya ghafla kwamba, "Mtu akiona kiu," iliwaghutua kutoka katika tafakari za majonzi, na kadiri walivyosikia maneno yaliyofuata, mawazo yao yaliamshwa na matumaini mapya. Roho Mtakatifu alionyesha ishara mbele yao mpaka walipoona ndani ya ishara hiyo zawadi ya thamani kubwa ya wokovu.

Sauti ya Yesu kwa roho zenye kiu bado inatolewa, na inatoa wito kwetu kwa nguvu kubwa zaidi kuliko hata vile ilivyosikika hekaluni mnamo siku ya mwisho ya sikukuu ile. Chemchemi imewekwa wazi kwa ajili ya watu wote. Waliochoka na kukata tamaa wanapewa kuchota maji ya uzima wa milele. Yesu bado analia akisema, "Mtu akiona kiu, na aje kwangu, anywe." "Naye mwenye kiu na aje; na yeye atakaye, na ayatwae maji ya uzima bure." "Yeyote atakayekunywa maji yale nitakayompa mimi hataona kiu milele; bali yale maji nitakayompa yatakuwa ndani yake chemchemi ya maji, yakibubujikia uzima wa milele." Ufunuo 22:17; Yohana 4:14.

## Sura ya 50

# Katikati ya Mitego

[Sura hii imejengwa katika Yohana 7:16-36, 40-53; 8:1-11.]

Kwa muda wote ambao Yesu alikuwa Yerusalemu wakati wa sikukuu alikuwa amezingirwa na wapelelezi. Siku kwa siku mipango mipya ya kumnyamazisha ilifanywa. Makuhani na wakuu walikuwa wakifuatilia namna ya kumnasa. Walikuwa wanapanga kumsitisha kwa mabavu. Lakini hii haikuwa makusudi yao yote. Walitaka kumtweza rabi huyu wa Galilaya mbele za watu.

Katika siku yake ya kwanza kuwepo katika sikukuu ile wakuu walikuwa wamemjia, wakimtaka aeleze ni kwa mamlaka gani alikuwa anafundisha. Walitaka kupotosha kwamba suala si Yeye na kuelekeza katika suala la haki yake ya kufundisha, na katika umuhimu wao na mamlaka yao.

"Mafunzo yangu si yangu mimi," Yesu alisema, "ila ni yake yeye aliyenipeleka. Mtu akipenda kuyatenda mapenzi yake, atajua habari ya yale mafunzo, kwamba yatoka kwa Mungu, au kwamba mimi nanena kwa nafsi yangu tu." Yohana 7:16, 17. Yesu hakukabiliana na swali la wapinzani hawa kwa ubishi, bali kwa kuufunua ukweli wa thamani kwa wokovu wa watu. Alisema kwamba kufahamu na kuukubali ukweli hakutegemei sana akili bali moyo. Lazima ukweli upokelewe moyoni; unahitaji kupokelewa katika utashi. Ikiwa ukweli ungetegemea akili tu, kiburi kisingekuwa kikwazo katika njia ya kuupokea. Lakini lazima upokelewe kwa njia ya kazi ya neema moyoni; na upokeaji wa ukweli huo hutegemea uachaji wa kila dhambi ambayo hufunuliwa na Roho wa Mungu. Uwezo wa mwanadamu kupata kuuelewa ukweli, hata uwezo huo uwe mkubwa kiasi gani, hautakuwa na faida yoyote ikiwa moyo hauko wazi kuupokea **(456)** ukweli huo, na kuwa na nia ya kusalimisha kila aina ya mazoea na matendo yanayopingana na kanuni za ukweli huo. Kwa wale wanaojisalimisha kwa Mungu, wakiwa na hamu ya kweli ya kujua mapenzi yake na kuyafanya, ukweli unafunuliwa kwao kama nguvu ya Mungu iliyo kwa ajili ya wokovu wao. Hawa watakuwa na uwezo wa wa kutofautisha kati ya mtu anayemhubiri Mungu, na yule anayehubiri kwa ajili yake mwenyewe tu. Mafarisayo hawakuwa wameweka mapenzi yao katika upande wa mapenzi ya Mungu. Walikuwa hawatafuti kuujua ukweli, bali walikuwa wanatafuta visingizio vya kuukwepa; Kristo alionyesha kwamba hii ndiyo iliyokuwa sababu ya kushindwa kuelewa mafundisho yake.

Sasa aliwapa kipimo cha kutumia kumtambua mwalimu wa kweli na mdanganyaji: "Yeye anenaye kwa nafsi yake tu hutafuta utukufu wake mwenyewe; bali yeye anayetafuta utukufu wake aliyempeleka, huyo ni wa kweli, wala ndani yake hamna udhalimu." Yohana 7:18. Anayetafuta utukufu wake mwenyewe ananena kutoka ndani yake mwenyewe. Roho ya kujitafutia manufaa binafsi husaliti chanzo chake. Lakini Kristo alikuwa anatafuta utukufu wa Mungu. Alitamka maneno ya Mungu. Huu ndio uliokuwa ushahidi wa mamlaka yake kama mwalimu wa ukweli.

Yesu aliwapa marabi wale ushahidi wa uungu wake kwa kuwaonyesha kwamba alisoma mioyo yao. Muda wote tangu uponyaji wa kule Bethzatha walikuwa wanatafuta kumwua. Kwa njia hiyo wao wenyewe walikuwa wanavunja sheria waliyodai kwamba walikuwa wanaitetea. "Je! Musa hakuwapa torati?" alisema, "Wala hakuna mmoja wenu aitendaye torati. Mbona mnatafuta kuniua?"

Kama ilivyo mwangaza wa nuru wa ghafla, maneno haya yaliwafunulia marabi wale dimbwi la uharibifu walimotaka kutumbukia. Kwa muda fulani walijawa na utisho. Waliona kwamba walikuwa wanapambana na Nguvu ya Mungu. Lakini hawakuweza kuonyeka. Kwa lengo la kuendelea kuwa na ushawishi wa kuheshimiwa na watu, lazima wafiche mipango yao ya uuaji. Wakilikwepa kwa ujanja lile swali la Yesu, walisema, "Ama! Una pepo! Ni nani anayetafuta kukuua?" Waliashiria kwamba kazi za maajabu za Yesu zilikuwa zinawezeshwa na roho chafu.

Yesu hakusikiliza kauli zao hizi. Aliendelea kuwaonyesha kwamba kazi yake ya kuponya kule Bethzatha ilikuwa inapatana na sheria ya Sabato, na kwamba ilihalalishwa na tafsiri ambayo Wayahudi wenyewe waliiweka kuhusu sheria hiyo. Alisema, "Musa aliwapa tohara; . . . nanyi siku ya sabato humtahiri mtu." Kwa mujibu wa sheria, kila mtoto lazima atahiriwe mnamo siku ya nane. Ikiwa muda huo ulioamuriwa ungeangukia siku ya Sabato, lazima desturi hiyo itimizwe siku hiyo hiyo. Ni zaidi kiasi gani kwamba **(457)** kiini cha sheria hiyo kinapatana na tendo

la kumfanya mtu "kuwa mzima kabisa siku ya sabato." Na akawaonya wasihukumu hukumu ya macho tu, bali hukumu iliyo ya haki.

Wale wakuu walinyamazishwa; na watu wengi walisema kwa mshangao, "Je! Huyu siye wanayemtafuta ili wamwue? Na kumbe! Anena waziwazi, wala hawamwambii neno! Yamkini hao wakuu wanajua hakika ya kuwa huyu ndiye Kristo?"

Wengi miongoni mwa waliomsikia Yesu waliokuwa wakazi wa pale Yerusalemu, na ambao hawakujua njama za wakuu dhidi yake, walijihisi kuvutwa kwake kwa nguvu isiyopingika. Walisadikishwa kwamba alikuwa Mwana wa Mungu. Lakini Shetani alikuwa tayari kuwaletea mashaka; na kwa ajili ya jambo hilo njia iliandaliwa kupitia kwa mawazo yao wenyewe ya makosa kuhusu Masihi na kuja kwake. Kwa ujumla iliaminika kwamba Kristo angezaliwa Bethlehemu, lakini kwamba baada ya muda angetoweka, na katika kuja kwake mara ya pili hakuna ambaye angejua atokako. Si watu wachache walioamini kwamba Masihi asingekuwa na mahusiano ya kawaida na wanadamu. Na kwa kuwa uelewa wa wengi kuhusu utukufu wa Masihi haukuendana na vile Yesu wa Nazareti alivyokuwa, wengi waliyasikiliza madai kwamba, "Lakini huyu twamjua atokako; bali Kristo atakapokuja hakuna ajuaye atokako."

Wakati walipokuwa wakiyumba-yumba katikati ya mashaka na kuamini, Yesu aliyachukua mawazo yao na kuwajibu: "Mimi mnanijua, na huko nitokako mnakujua; wala sikuja kwa nafsi yangu; ila yeye aliyenipeleka ni wa kweli, msiyemjua ninyi." Walidai kujua mahali ambako Kristo angetoka, lakini walikuwa katika ujinga kuhusu hilo. Ikiwa wangekuwa wameishi kulingana na mapenzi ya Mungu, wangemjua Mwana wake wakati alipodhihirishwa kwao.

Wale wasikilizaji waliyaelewa maneno ya Kristo. Yalikuwa marudio ya wazi ya madai yale aliyokuwa ametoa mbele ya Sanhedrin miezi mingi iliyopita, wakati alipojitangaza kama Mwana wa Mungu. Kadiri wakuu walivyojaribu kufuatilia mauti yake, ndivyo walivyotafuta kumkamata; lakini walizuiwa na nguvu isiyoonekana, ambayo iliweka ukomo wa hasira zao, ikiwaambia, Mtaenda mpaka hapo, lakini si zaidi.

Wengi miongoni mwa watu walimwamini, na walisema, "Atakapokuja Kristo, je! Atafanya ishara nyingi zaidi kuliko hizi alizozifanya huyu?" Viongozi wa Mafarisayo, ambao walikuwa wanaangalia kwa hamu mwenendo wa matukio, waliona kwamba watu wanamkubali. Wakiharakisha kwenda kwa wakuu wa makuhani, waliweka mipango ya kumkamata.

**(458)** Hata hivyo walipanga kumchukua akiwa peke yake; maana hawakuthubutu kumkamata mbele ya watu. Kwa mara nyingine tena Yesu alifanya idhihirike kwamba alisoma makusudi yao. Akasema, "Bado kitambo kidogo nipo pamoja nanyi; kisha naenda zangu kwake yeye aliyenipeleka. Mtanitafuta wala hamtaniona; nami nilipo ninyi hamwezi kuja." Muda si mrefu angepata hifadhi mbali asikoweza kufikiwa na bezo na chuki. Angeenda kwa Baba, kuwa wa Kuabudiwa na malaika; na mahali hapa wauaji wake wale wasingepafika.

Kwa kubeza marabi wale walisema, "Huyu atakwenda wapi hata sisi tusimwone? Ati! Atakwenda kwa Utawanyiko wa Wayunani, na kuwafundisha Wayunani?" Wapinzani wale hawakuota kwamba katika maneno yao ya dhihaka walikuwa wanaielezea kazi ya Kristo! Kwa siku nzima alikuwa amenyosha mikono yake kwa watu wasiotii na wanaokana ukweli; lakini angeonekana kwa hao ambao hawakumtafuta; miongoni mwa watu ambao hawakuwa wameliitia jina lake angedhihirika. Warumi 10:20, 21.

Wengi walioshawishika kwamba Yesu alikuwa ni Mwana wa Mungu walipotoshwa na hoja za uongo za makuhani na marabi. Hawa walikuwa wamerudia-rudia kwa nguvu unabii uliomhusu Masihi, kwamba angetawala "katika mlima wa Sayuni, na katika Yerusalemu, na mbele ya wazee wake kwa utukufu;" kwamba angekuwa na "enzi toka bahari hata bahari, Toka Mto hata miisho ya dunia." Isaya 24:23; Zaburi 72:8. Halafu walifanya ulinganishaji wa chuki kati ya utukufu ulioonyeshwa hapa na mwonekano wa kujishusha kwa Yesu. Maneno yale yale ya unabii yalipotoshwa kiasi cha kuonyesha makosa. Ingekuwa kwamba watu walikuwa wamejifunza neno wao wenyewe kwa uaminifu, wasingepotoshwa. Sura ya sitini na moja ya Isaya inashuhudia kwamba angefanya kazi ile ile aliyofanya. Sura ya hamsini na tatu inaonyesha kukataliwa kwake na mateso yake ulimwenguni, na sura ya hamsini na tisa inaelezea tabia za makuhani na marabi.

Mungu hawalazimishi watu kuachana na kutokuamini kwao. Mbele yao kuna nuru na giza, ukweli na uongo. Ni wajibu wao kuamua kipi cha kukubali. Akili ya mwanadamu imejaliwa uwezo wa kutenganisha kati ya kilicho sahihi na kisicho sahihi. Mungu anapenda kwamba wanadamu wasiamue kwa msisimko, bali kwa kupima uthibitisho, kulinganisha andiko na andiko kwa umakini. Ikiwa Wayahudi wangeacha msimamo wao potofu na kulinganisha unabii ulioandikwa na sifa za maisha ya Yesu, wangeelewa upatanifu mzuri uliopo kati ya unabii na vile ulivyotimilika katika maisha na utumishi wa yule Mgalilaya wa hali ya chini.

**(459)** Watu wengi wanadanganywa leo kwa namna ile ile Wayahudi walivyokuwa. Walimu wa dini husoma Biblia kulingana na uelewa wao na mapokeo yao; na watu hawajifunzi Maandiko kwa ajili yao wenyewe, na kuamua wao wenyewe kuhusu upi ni ukweli; bali wanasalimisha maamuzi yao, na kukabidhi roho zao kwa viongozi wao. Kuhubiri na kufundisha ni moja ya njia ambazo Mungu hutumia kuitawanya nuru; lakini lazima tulete mafundisho ya kila mwanadamu katika kipimo cha neno la Mungu. Yeyote yule atakayejifunza Biblia kwa maombi, akitamani kuujua ukweli, kwa kusudi la kuutii, atapokeo hali ya kuangaziwa na mbingu. Atayaelewa Maandiko. "Mtu akipenda kuyatenda mapenzi yake, atajua habari ya yale mafunzo." Yohana 7:17.

Siku ya mwisho ya sikukuu, wale maofisa waliotumwa na makuhani na wakuu ili kumkamata Yesu, walirudi bila kwenda naye. Waliulizwa kwa hasira, "Mbona hamkumleta?" Kwa mwonekano thabiti walijibu, "Hajanena kamwe mtu yeyote kama huyu anavyonena." Wakiwa wamefanywa wagumu kama mioyo yao ilivyokuwa, walikuwa wameyeyushwa na maneno yake. Wakati alipokuwa ananena katika kiwanja cha hekalu, walikuwa wamekawilia-kawilia karibu, ili kunasa kitu ambacho kingetumika kumpinga. Lakini kadiri walivyosikiliza, lile lengo walilotumwa kulitekeleza lilisahaulika. Walisimama walipoona watu wakiingia. Kristo alijidhihirisha nafsini mwao. Waliona kile ambacho makuhani na wakuu wasingeona, - uanadamu ulifurikishwa utukufu wa kimbingu. Walirudi, wakiwa wamejazwa na mawazo haya, wakiwa wameguswa na maneno yake, kiasi ambacho majibu yao kwa swali, "Mbona hamkumleta?" yalikuwa, "Hajanena kamwe mtu yeyote kama huyu anavyonena."

Wale makuhani na wakuu, walipokuja kwa Kristo kwa mara ya kwanza, walikuwa wamekutana na usadikisho kama huo huo. Mioyo yao iliguswa kwa kina, na mwazo yao yalilazimishwa kusema, "Hajanena kamwe mtu yeyote kama huyu anavyonena." Lakini walikuwa wamepinga usadikisho wa Roho Mtakatifu. Sasa, wakighadhabishwa na hali kwamba hata vyombo vya sheria vingeshawishiwa na Mgalilaya huyu aliyekuwa anachukiwa, walipaza sauti na kusema, "Je! Ninyi nanyi mmedanganyika? Ni nani katika wakuu amwaminiye, au katika Mafarisayo? Lakini makutano hawa wasioifahamu torati wamelaaniwa."

Wale ambao wanaambiwa ujumbe wa ukweli wakati mwingine huuliza, "Ni kweli?" kwani, "Ujumbe unahubiriwa na nani?" Watu wengi hupima ujumbe kwa kuangalia idadi ya watu wanaoupokea; na swali hili bado linaulizwa, "Je, kuna wasomi au viongozi wa dini ambao wameamini?" Watu wana hali ya kutokuwa na wema halisi leo zaidi kuliko mnamo siku za Kristo. Wameazimia kutafuta mali za dunia, wakipuuza utajiri wa milele; wala si **(460)** kwa hoja iliyo dhidi ya ukweli, kwamba idadi kubwa ya watu hawako tayari kuupokea, au kwamba haupokelewi na watu wakuu wa ulimwengu, au hata na viongozi wa dini.

Kwa mara nyingine tena makuhani na wakuu waliendelea kuweka mipango ya kumtia Yesu nguvuni. Ilisemwa kwamba ikiwa ataachwa kwa muda zaidi kuwa huru angevuta watu mbali na wale viongozi waliotambulika rasmi, na suluhisho pekee ilikuwa ni kumnyamazisha pasipo kukawia. Katika mkondo wa mjadala wao, walikatizwa ghafla. Nikodemo alihoji, "Je! Torati yetu humhukumu mtu kabla ya kumsikia kwanza, na kujua atendavyo?" Ukimya uliuangukia mkutano. Maneno ya Nikodemo yalifika mahali pake katika dhamiri zao. Wasingeweza kumhukumu mtu bila kumsikiliza. Lakini si kwa sababu hii peke yake kwamba wakuu wale walinyamaza kimya, wakimkazia macho yule aliyethubutu kuongea kwa kutetea haki. Walishtuka na kuudhika kwa hali ya kwamba miongoni mwao kulikuwa na mtu aliyekuwa ameguswa sana na tabia ya Yesu kiasi cha kusema neno la kumtetea Yesu. Wakirejea kutoka katika hali ya kupigwa butwaa, walimwuliza Nikodemo kwa maneno makali yanayoashiria kuwa kinyume, "Je! Wewe nawe umetoka Galilaya! Tafuta, ukaone ya kuwa kutoka Galilaya hakutokea nabii."

Lakini matokeo ya mabishano yale yalikuwa ni kukawiza maendeleo ya maamuzi ya baraza lile. Wale wakuu hawakuweza kuendelea na makusudi yao ya kumhukumu Yesu bila kumsikiliza. Wakiwa wameshindwa kwa muda, "walikwenda kila mtu nyumbani kwake; naye Yesu akaenda mpaka mlima wa Mizeituni."

Kutoka katika msisimko na ghasia za pale mjini, kutoka kwa makutano wenye hamu na marabi wenye kusaliti, Yesu alirudi katika sehemu ya utulivu ya bustani ya mizeituni, mahali ambapo angekuwa peke yake pamoja na Mungu. Lakini asubuhi mapema alirudi hekaluni, na kadiri walivyokusanyika kwake, alikaa chini na kuwafundisha.

Baada ya muda mfupi alikatizwa. Kundi la Mafarisayo na waandishi walikaribia, wakimkokota mwanamke aliyekuwa chini ya vitisho, ambaye walimshtaki kwa sauti za fujo na hasira kwamba amevunja amri ya saba. Wakishakumsukumizia mbele ya Yesu, walimwambia Yesu, kwa kuonyesha heshima ya kinafiki, "Katika torati Musa alituamuru kuwapiga kwa mawe wanawake namna hii; nawe wasemaje?"

Ile heshima ya kuigiza ilificha njama kubwa ya kumwangamiza. Walikuwa wametumia fursa hii ili kupata kumhukumu, wakifikiri kwamba uamuzi wowote ambao angefanya, ungewapatia uwezekano wa kumshtaki. Ikiwa angemwachia huru yule mwanamke, angetuhumiwa kwa kudharau sheria ya Musa. Ikiwa angemtangaza kustahili kifo, **(461)** angeshtakiwa kwa Warumi kama mtu aliyejipatia mamlaka ambayo ilikuwa yao peke yao.

Yesu aliliangalia kidogo tukio lile, - yule mhanga aliyekuwa anatetemeka katika aibu yake, waheshimiwa wale wenye nyuso zilizokakamaa, wakiwa hawana huruma hata ya kibinadamu. Roho yake iliyo safi ilisinyaa kwa tukio lile. Alijua vema kusudi la shauri hili kuletwa kwake. Alisoma moyo, na alijua tabia na historia ya maisha ya kila mmoja aliyekuwa pale. Hawa watu waliotarajiwa kuwa wasimamiaji wa haki ndio ambao walikuwa wamemfanya mhanga huyu kuangukia dhambini, ili ya kwamba wapate kuweka mtego kwa ajili ya kumnasa Yesu. Akiwa haonyeshi ishara yoyote kwamba amesikia swali lao, aliinama, naye akikaza macho yake chini, alianza kuandika katika mavumbi.

Kwa kukosa subira kwa kukawia kwake na kuonekana kama hatoi ushirikiano, wale washtaki walisogea karibu zaidi, wakisisitiza jambo lile kwake. Lakini macho yao, baada ya yale ya Yesu, yalipotazama pale chini miguuni pake, sura zao zilibadilika. Kilichokuwa pale kilikuwa ni siri za makosa ya siri ya maisha yao. Watu waliokuwa wanatazama waliona badiliko la ghafla la mwonekano wao, na wakasogea mbele kuja kuona kwamba walikuwa wamekuwaje kwa mshangao wao ule na aibu waliyokuwa nayo.

Pamoja na madai yao yote ya kuiheshimu sheria, marabi hawa, kwa kuleta mashtaka dhidi ya mwanamke yule, walikuwa hawajali taratibu za sheria hiyo. Ilikuwa ni wajibu wa mume kuchukua hatua kama ile kwa yule mwanamke, na wale walioshirikiana katika dhambi ile wangeadhibiwa kwa namna inayofanana. Kitendo cha washtaki wale kilikuwa hakiruhusiwi kabisa. Hata hivyo, Yesu alikutana nao huko huko. Sheria ilionyesha kwamba katika adhabu ya kupiga kwa mawe, wale walioshuhudia ndio huwa wa kwanza kutupa mawe. Sasa akiwa anainuka, na kukaza macho yake kwa wazee wale wenye njama, Yesu alisema, "Yeye asiye na dhambi miongoni mwenu na awe wa kwanza wa kumtupia jiwe." Na akiwa ameinama tena, aliendelea kuandika chini.

Hakuwa ameweka kando sheria iliyotolewa kupitia Musa, wala hakuingilia mamlaka ya Rumi. Washtaki walikuwa wameshindwa. Sasa, kanzu yao ya utakatifu wa bandia ilichanika kutoka kwao, wakasimama mbele ya Mwenye Usafi wote, wakiwa katika kuhukumiwa na aibu. Walitetemeka wakihofu kwamba maovu ya maisha yao yaliyofichwa yangeanikwa wazi kwa makutano; na mmoja baada ya mwingine, wakiwa wameinamisha vichwa na macho yao, waliondoka, wakimwacha nyuma yule mhanga na Mwokozi mwenye huruma.

Yesu aliinuka na, akimwangalia yule mwanamke, alisema, "Mwanamke, wako wapi wale washtaki wako? Je! Hakuna aliyekuhukumu kuwa na hatia? Akamwambia, Hakuna, Bwana. Yesu akamwambia, Wala mimi sikuhukumu."

**(462)** Yule mwanamke alikuwa amesimama mbele za Yesu, akihofu kwa woga. Maneno ya Yesu kwamba, "Yeye asiye na dhambi miongoni mwenu na awe wa kwanza wa kumtupia jiwe," yalikuwa yamemfikia huyu mwanamke kama hukumu ya kifo. Hakuthubutu kuinua macho yake kuuona uso wa Mwokozi, bali alisubiri kifo chake akiwa kimya. Kwa mshangao aliwaona washtaki wake wakiondoka bila kusema kitu na wakiwa wameaibika; halafu hayo maneno ya tumaini yalifika masikioni mwake, "Wala mimi sikuhukumu. Enenda zako; wala usitende dhambi tena." Moyo wa mwanamke yule uliyeyuka, na alijitupa miguuni pa Yesu, akisema kwa kikweukweu kwa shukrani ya upendo, na kwa machozi machungu akiungama dhambi zake.

Huu ulikuwa mwanzo wa maisha mapya kwa mwanamke yule, maisha ya usafi na amani, ya kujitoa kwa huduma ya Mungu. Katika kuiinua nafsi hii iliyoanguka, Yesu alitenda mwujiza mkubwa zaidi kuliko hata kuponya ugonjwa wa mwili ulio mkubwa kuliko yote; aliponya ugonjwa wa kiroho ambao ni wa kifo cha milele. Mwanamke huyu mwenye majuto alikuja kuwa mmoja wa wafuasi wa Yesu waliokuwa imara. Akiilipa rehema ya msamaha wa Kristo kwa upendo na kujitoa kwa kujikana nafsi.

Katika kitendo chake cha kumsamehe yule mwanake na kumtia moyo kuishi maisha mazuri zaidi, tabia ya Yesu hung'ariza uzuri kuhesabiwa haki kikamilifu. Huku akiwa haondoi madhara ya dhambi, wala hapunguzi hali ya kujijutia hatia, Yeye hatafuti kuhukumu bali kuokoa. Kwa huyu mwanamke mwenye makosa ulimwengu ulikejeli na kudhihaki; bali Yesu hunena maneno ya faraja na tumaini. Yeye Asiye na dhambi anawaonea huruma watu wenye udhaifu na dhambi, na anaufikisha kwao mkono wenye msaada. Wakati Mafarisayo wanafiki wao walimdhihaki, Yesu anamhimiza huyu mama, akisema, "Nenda zako, usitende dhambi tena."

Mtu ambaye, kwa macho yasiyo na huruma, humgeuzia kisogo mkosaji si mfuasi wa Kristo. Wale ambao wako mbele katika kuwashtaki wengine, na wakiwa na hamu ya kuwaleta katika vyombo vya haki, maisha yao yako katika hatia kubwa kuliko jinsi walivyo. Wanapenda dhambi. Kristo anaichukia dhambi, lakini anampenda mdhambi. Hii ndiyo itakuwa roho ya wote wanaomfuata. Upendo wa Kristo ni wa pole pole, wa haraka kuona toba, tayari kusamehe, kutia moyo, kumweka atangatangaye katika njia nyofu, na kusimika miguu ya mtu humo.

**Sura ya 51**

# "Nuru ya Uzima"

[Sura hii imajengwa katika Yohana 8:12-59; 9.]

“Basi Yesu akawaambia tena akasema, Mimi ndimi nuru ya ulimwengu, yeye anifuataye hatakwenda gizani kamwe, bali atakuwa na nuru ya uzima."

Wakati aliposema maneno haya, Yesu alikuwa katika kiwanja cha hekaluni akiwa ameunganishwa na shughuli za Sikukuu ya Vibanda. Katikati ya kiwanja hiki ziliinuka nguzo ndefu mbili, zilizobeba vinara vya taa vikubwa. Baada ya dhabihu ya jioni, taa zote ziliwashwa, na kuuangazia mwanga mji wa Yerusalemu. Maadhimisho haya yalikuwa ya kumbukumbu ya nguzo ya nuru iliyowaongoza wana wa Israeli kule jangwani, na ilichukuliwa pia kwamba inaashiria ujio wa Masihi. Wakati wa jioni taa zilipokuwa zimewashwa, kiwanja kile kilikuwa kinafurahisha sana. Wanaume wenye vichwa vyenye mvi, makuhani wa hekalu na wakuu wa watu, waliunganika katika kucheza kulingana na sauti za muziki wa ala na maneno ya kurudia-rudia ya wimbo yaliyoimbwa na Walawi.

Katika kule kuuangazia mji wa Yerusalemu, watu walionyesha tumaini lao la kuja kwa Masihi kuangaza nuru yake kwa Israeli. Lakini kwa Yesu mandhari ile ilikuwa na maana pana zaidi. Kadiri taa za hekalu zilivyowaangazia pande zote, ndivyo ambavyo Kristo, aliye chanzo cha nuru ya kiroho, anavyoangaza katika giza la ulimwengu. Lakini bado alama ile haikuwa na ukamilifu. Nuru ile kuu ambayo ilikuwa imewekwa mbinguni kwa mkono wake ilikuwa ndiyo kiwakilishi cha kweli zaidi cha kazi yake.

Ilikuwa asubuhi; mara tu jua lilikuwa limechomoza juu ya upeo wa Mlima wa Mizeituni, na miale yake ilipiga kwenye marumaru za kiwanja cha hekalu zilizokuwa zikimetameta, na **(464)** iling’arisha dhahabu iliyokuwa katika kuta za hekalu, wakati Yesu alipoonyesha kwenye hekalu hilo na kusema, "Mimi ndimi nuru ya ulimwengu."

Maneno haya yalirudiwa kama mwangwi kupitia kwa mtu mwingine aliyeyasikia anaposema, "Ndani yake ndimo ulimokuwa uzima, nao ule uzima ulikuwa nuru ya watu. Nayo nuru yang'aa gizani, wala giza halikuiweza." "Kulikuwako Nuru halisi, amtiaye nuru kila mtu, akija katika ulimwengu." Yohana 1:4, 5, 9. Na muda mrefu baadaye Yesu akiwa ameshapaa mbinguni, Petro naye pia, akiandika kwa kuangaziwa na Roho wa mbinguni, alivuta kumbukumbu ya kielelezo kile alichokuwa ametumia Kristo: "Nasi tuna lile neno la unabii lililo imara zaidi, ambalo, mkiliangalia, kama taa ing'aayo mahali penye giza, mwafanya vyema, mpaka kutakapopambazuka, na nyota ya asubuhi kuzuka mioyoni mwenu." 2 Petro 1:19.

Katika udhihirisho wa Mungu kwa watu wake, daima nuru ilikuwa imetumika kama ishara ya uwepo wake. Kutokana na neno la uumbaji hapo mwanzo, nuru ilikuwa imeangaza katika giza. Wakati wa kuyaongoza majeshi ya Israeli, nuru ilikuwa imezunguka nguzo ya wingu mchana na nguzo ya moto wakati wa usiku. Mwangaza uliangaza kwa mng’ao mkuu kumzunguka Bwana kwenye Mlima Sinai. Mwangaza ulikuwa mahali pa kiti cha rehema katika patakatifu. Mwangaza ulilijaza hekalu la Sulemani wakati wa kuwekwa wakfu hekalu hilo. Mwangaza uliangaza katika vilima vya Bethlehemu wakati malaika walipowaletea wachungaji wale habari ya ukombozi.

Mungu ni nuru; na katika maneno kwamba, "Mimi ndimi nuru ya ulimwengu," Kristo anatangaza umoja wake na Mungu, na uhusiano wake na jamaa yote ya wanadamu. Ni Yeye ambaye hapo mwanzo alisababisha "nuru kuangaza gizani." 2 Wakorintho 4:6. Yeye ni nuru ya jua na ya mwezi na ya nyota. Alikuwa nuru ya kiroho ambayo kupitia uwakilishi wa ishara, mfano na unabii ilikuwa imewaangazia Waisraeli. Lakini nuru haikutolewa kwa taifa la Wayahudi peke yake. Kadiri miale ya jua inavyopenya mpaka katika pembe za mbali za dunia, ndivyo Jua la Haki linavyoangaza.

"Kulikuwako Nuru halisi, amtiaye nuru kila mtu, akija katika ulimwengu." Dunia imepata kuwa na walimu wakubwa, watu wakuu wenye ufahamu na waliofanya utafiti wa ajabu, watu wenye uwezo wa kunena maneno ya kusisimua mawazo, na ambao wameweza kufungua macho ya watu ili kupata maarifa mapana; na watu hawa

wameheshimiwa kama waongozi na wategemezaji wa jamii zao. Lakini yupo Mmoja asimamaye juu zaidi kuliko hao. "Wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu." "Hakuna mtu aliyemwona Mungu wakati wowote; Mwana pekee aliye katika kifua cha Baba, huyu ndiye aliyemfunua." Yohana 1:12, 18. Tunaweza kufuatilia mlolongo wa walimu wakuu wa ulimwengu hadi huko nyuma katika historia kwa kadiri kumbukumbu zinavyoweza kupatikana; lakini **(465)** kulikuwa na Nuru mbele yao. Kama vile mwezi na nyota zilizo katika mfumo wa jua zinavyotoa mwanga kwa kuakisi mwanga wa jua, hivyo ndivyo wenye akili (wanafalsafa) wa ulimwengu, ikiwa mafundisho yao ni ya kweli, wanavyoaksi miale ya Jua la Haki. Kila fikira njema, kila mwanga umlikao katika akili, unatoka kwa Nuru ya ulimwengu. Katika miale hii tunasikia habari za "elimu ya juu." "Elimu ya juu ya kweli" ni ile inayoletwa na Yeye "ambaye ndani yake yeye hazina zote za hekima na maarifa zimesitirika." "Ndani yake ndimo ulimokuwa uzima, nao ule uzima ulikuwa nuru ya watu." Wakolosai 2:3; Yohana 1:4. Yesu alisema, "Yeye anifuataye hatakwenda gizani kamwe, bali atakuwa na nuru ya uzima."

Katika maneno, "Mimi ndimi nuru ya ulimwengu," Yesu alijitangaza kama Masihi. Yule kikongwe Simeoni, katika hekalu hili hili ambamo sasa Yesu alikuwa anafundisha, alikuwa amepata kumtaja Yeye kama "nuru ya kuwa mwangaza wa Mataifa, na kuwa utukufu wa watu wako Israeli." Luka 2:32. Katika maneno haya alikuwa anamhusianisha na unabii uliokuwa unafahamika kwa Israeli wote. Kupitia nabii Isaya, Roho Mtakatifu alikuwa ametangaza kwamba, "Ni neno dogo sana wewe kuwa mtumishi wangu ili kuziinua kabila za Yakobo, na kuwarejeza watu wa Israeli waliohifadhiwa; zaidi ya hayo nitakutoa uwe nuru ya mataifa, upate kuwa wokovu wangu hata miisho ya dunia." Isaya 49:6. Unabii huu ulieleweka kwa ujumla kwamba ulimhusu Masihi, na Yesu aliposema, "Mimi ndimi nuru ya ulimwengu," watu hawakushindwa kugundua dai lake la kuwa Yeye Aliyeahidiwa.

Kwa Mafarisayo na wakuu dai hili lilionekana kuwa la kujivuna kwa ufidhuli. Kitendo cha mtu wa kawaida aliye kama wao kujifanya hivyo kilikuwa hakiwezi kuvumilika kwao. Wakionekana kupuuza maneno yake, waliuliza, "U nani wewe?" Walikuwa wanataka kumlazimisha ajitangaze kuwa ni Kristo. Mwonekano wake na kazi zake vilikuwa tofauti kabisa na matarajio ya watu, kiasi kwamba, kulingana na vile adui zake walivyoamini, tamko lake la moja kwa moja la kujitangaza kama Masihi lingesababisha akataliwe kwa kuonekana kuwa laghai.

Lakini jibu la Yesu kwa swali lao kwamba, "U nani wewe?" lilikuwa, "Hasa neno lilo hilo ninalowaambia." Yohana 8:25. Kile kilichokuwa kimefunuliwa katika maneno yake kilifunuliwa pia katika tabia yake. Alikuwa ni mwonekano halisi wa ukweli aliofundisha. Aliendelea kwamba, "Sifanyi neno kwa nafsi yangu, ila kama Baba alivyonifundisha ndivyo ninenavyo. Naye aliyenipeleka yu pamoja nami, hakuniacha peke yangu; kwa sababu nafanya sikuzote yale yampendezayo." Hakuthibitisha madai yake ya Umasihi, bali alionyesha umoja wake na Mungu. Ikiwa akili yao ingekuwa imefungukia upendo wa Mungu, wangempokea Yesu.

**(466)** Miongoni mwa wasikilizaji wake wale wengi walivutwa kwake kwa imani, naye akawaambia hao waliomwamini, "Ninyi mkikaa katika neno langu, mmekuwa wanafunzi wangu kweli kweli; tena mtaifahamu kweli, nayo hiyo kweli itawaweka huru."

Maneno haya yaliwachukiza Mafarisayo. Taifa lao likiwa chini ya kongwa la kigeni kwa muda mrefu, hawakujali lolote, wakasema kwa hasira, "Sisi tu uzao wake Ibrahimu, wala hatujawa watumwa wa mtu wakati wowote; nawe wasemaje, Mtawekwa huru?" Yesu aliwaangalia watu hawa, watumwa wa kutafuta kudhuru, wenye mawazo yaliyoelekezwa katika visasi, na akajibu kwa huzuni, "Amin, amin, nawaambia, Kila atendaye dhambi ni mtumwa wa dhambi." Walikuwa katika aina mbaya zaidi ya utumwa, - wakitawaliwa na roho chafu.

Kila mtu anayekataa kujitoa kwa Mungu yuko chini ya utawala wa mamlaka nyingine. Wala si yeye kama yeye. Anaweza kuzungumza kwamba yu huru, kumbe yuko katika utumwa wa kutisha. Haruhusiwi kuona uzuri wa ukweli, maana akili yake iko chini ya udhibiti wa Shetani. Wakati akijisifu kwamba anaongozwa na akili yake, anatii mapenzi ya mfalme wa giza. Kristo alikuja kuvunja vifungo vya utumwa wa dhambi kwa mtu. "Basi Mwana akiwaweka huru, mtakuwa huru kweli kweli." "Sheria ya Roho wa uzima ule ulio katika Kristo Yesu" hutuweka "huru, mbali na sheria ya dhambi na mauti." Warumi 8:2.

Katika kazi ya ukombozi hakuna kulazimisha kwa nguvu. Hakuna nguvu ya nje inayotumika. Chini ya ushawishi wa Roho wa Mungu, mwanadamu huachwa huru kuchagua nani wa kumtumikia. Katika badiliko linalotokea wakati mtu anapojisalimisha kwa Kristo, kuna kiwango cha juu kabisa cha uhuru. Kuilazimisha dhambi ni tendo

la moyo wenyewe. Kweli, hatuna nguvu ya kutuwezesha kutoka katika utawala wa Shetani; lakini tunapoamua kuwa huru mbali na dhambi, na katika uhitaji mkubwa tukalilia nguvu iliyo nje na juu yetu wenyewe, nguvu za moyo zinajazwa na nguvu ya mbinguni ya Roho Mtakatifu, na zinatii maongozi ya matakwa ya kutimiza mapenzi ya Mungu.

Hali pekee ambayo uhuru wa mwanadamu unawezekana ni ile ya kuwa kitu kimoja na Kristo. "Kweli itawaweka huru;" na Kristo ndiye kweli. Dhambi inaweza kushinda tu kwa njia ya kudhoofisha akili, na kuharibu uhuru wa moyo. Kutiishwa kwa Mungu ni njia ya mtu kurejeshwa, - kwenda katika utukufu na heshima ya kweli ya mtu. Sheria ya kimbingu, ambayo tumetiishwa kwayo, ni "sheria ya uhuru." Yakobo 2:12.

Mafarisayo wale walikuwa wamejitangaza kuwa ni wana wa Ibrahimu. Yesu aliwaambia kwamba dai hili lingefanywa tu kwa kufanya matendo ya Ibrahimu. Watoto wa kweli wa Ibrahimu wangeishi maisha ya utiifu kwa Mungu, kama alivyokuwa. Wasingejaribu kumwua Yeye aliyekuwa anasema ukweli aliopewa na Mungu. Katika kule kufanya njama **(467)** dhidi ya Kristo, marabi wale hawakuwa wanafanya kazi za Ibrahimu. Kule kuwa katika uzao wa Ibrahimu wa kawaida hakukuwa na thamani. Pasipokuwa na mwunganiko wa kiroho kati yao na Ibrahimu, ambao ungedhihirika kwa kuwa na roho kama yake, na kufanya kazi kama zake, hawakuwa watoto wake.

Kanuni hiyo imebeba uzito huo huo katika suala ambalo limeutikisa ulimwengu wa Kikristo kwa muda mrefu, - suala la mafundisho kuhusu mamlaka ya kitume ya maaskofu. Kuwa na chimbuko katika Ibrahimu kulihakikishwa kwa kuangalio mfanano na tabia, si kwa jina wala ukoo. Vivyo hivyo mfumo wa mamlaka za kitume za uaskofu haziko katika kuhamisha mamlaka ya kitume, bali mahusiano ya kiroho. Maisha yanayosukumwa na roho ya mitume, kuamini na kufundisha ukweli walioufundisha, ndio ushahidi wa kurithi mamlaka ya mitume. Hiki ndicho kinachowafanya watu kurithi nafasi za walimu wa injili wa kwanza.

Yesu alikataa kuwaona Wayahudi kama wana wa Ibrahimu. Alisema, “Ninyi mnazitenda kazi za baba yenu." Kwa dhihaka walimjibu hivi, “Sisi hatukuzaliwa kwa zinaa; sisi tunaye Baba mmoja, yaani, Mungu." Maneno haya, yakiwa katika upotofu waliohusisha na mazingira ya kuzaliwa kwa Yesu, yalikusudiwa kumhafifisha machoni pa wale waliokuwa wanaanza kumwamini. Yesu hakusikiliza mabezo hayo, bali alisema, "Kama Mungu angekuwa baba yenu, mngenipenda mimi; kwa maana nalitoka kwa Mungu."

Matendo yao yaliuthibitisha uhusiano wao na yeye aliyekuwa mwongo na muuaji. Yesu akasema, "Ninyi ni wa baba yenu, Ibilisi, na tamaa za baba yenu ndizo mpendazo kuzitenda. Yeye alikuwa mwuaji tangu mwanzo; wala hakusimama katika kweli, kwa kuwa hamna hiyo kweli ndani yake. . . . Kwa sababu nasema iliyo kweli, hamnisadiki." Yohana 8:44, 45. Ile hali ya kwamba Yesu alisema ukweli, na kwa uhakika, ndiyo sababu hakupokelewa na viongozi wa Wayahudi. Ukweli ndio uliowachukiza watu hao wanaojihesabia haki. Ukweli ule uliweka wazi makosa yao; ulihukumu mafundisho na matendo yao, kwa hiyo haukupokelewa. Wangetamani kufumba macho wasione ukweli kuliko kujishusha na kukiri kwamba walikuwa katika makosa. Hawakuupenda ukweli. Hawakuutamani, ingawa ulikuwa ukweli.

"Ni nani miongoni mwenu anishuhudiaye ya kuwa nina dhambi? Nami nikisema kweli, mbona ninyi hamnisadiki?" Siku kwa siku kwa muda wa miaka mitatu adui zake walikuwa wamemfuatilia Kristo, wakijaribu kutafuta doa katika tabia yake. Shetani na majeshi yake yote ya uovu walikuwa wametafuta namna ya kumshinda, lakini ndani yake hawakupata dosari ya kuwasaidia. Hata mapepo yenyewe yalilazimika kukiri kwamba Yeye ni "Mtakatifu wa Mungu." Marko 1:24 (maneno hayo yako katika Marko 1:25 katika Biblia za toleo la Kiswahili). Yesu aliishika sheria machoni pa mbingu, **(468)** machoni pa malimwengu ambayo hayakuanguka, na machoni pa wanadamu wenye dhambi. Mbele za malaika, wanadamu na mapepo, alikuwa amesema, bila kubishiwa, maneno yafuatayo ambayo ikiwa yangesemwa na midomo mingine yangekuwa ni ya kukufuru: "Nafanya sikuzote yale yampendezayo."

Ile hali ya kwamba Wayahudi wale hawakumpokea Kristo hata kama hawakuona dhambi ndani yake ilithibitisha kwamba wao ndio hawakuwa na mwunganiko na Mungu. Hawakutambua sauti ya Mungu ndani ya Mwana wake. Walifikiria tu kumhukumu; lakini kwa kumkataa walikuwa wanajitamkia hukumu yao wenyewe. "Yeye aliye wa Mungu huyasikia maneno ya Mungu; hivyo ninyi hamsikii kwa sababu ninyi si wa Mungu."

Somo hilo ni la kweli wakati wote. Watu wengi wako katika nafasi ya mtu anayependa kukwepa kujadili mambo ya msingi, anayekosoa-kosoa, atafutaye kitu cha kuhoji katika neno la Mungu, akidhani kwamba kwa njia hiyo anatoa ushahidi wa kuwa huru kufuata maoni yake na ufahamu wa akilini mwake mwenyewe. Anajichukulia kwamba yuko katika nafasi ya kukaa na kuihukumu Biblia, wakati kwa kweli yuko anajihukumu mwenyewe. Anafanya hali ionekane kwamba hawezi kuutambua ukweli unaotoka mbinguni, na unaohusu mambo ya milele. Mbele ya mlima mkuu wa haki ya Mungu, roho ya mtu huyo haitishwi. Anajishughulisha sana katika kazi ya kuwinda fimbo na bakora, na katika hili anaisaliti hali finyu na ya asili ya duniani, yaani moyo unaopoteza haraka uwezo wa kumtambua Mungu. Yeye ambaye moyo wake umeuitikia mguso wa kimbingu atakuwa anatafuta kile kitakachoongeza ufahamu wake kuhusu Mungu, naye atasafisha na kukuza tabia yake. Kama vile ua linavyoligeukia jua, ili kwamba miale yake yenye mwanga iliguse kwa mwako wenye uzuri, ndivyo moyo utakavyomgeukia Yeye aliye Jua la Haki, ili kwamba nuru ya mbinguni ipate kuifanya tabia kuwa nzuri kwa neema za tabia ya Kristo.

Yesu aliendelea kusema, huku akionyesha ukinzani mkubwa kati ya nafasi walipokuwa Wayahudi na pale alipokuwa Ibrahimu: "Ibrahimu, baba yenu, alishangilia kwa vile atakavyoiona siku yangu; naye akaiona, akafurahi."

Ibrahamu alitamani kwa furaha kumwona Mwokozi aliyeahidiwa. Alitoa ombi la dhati mno kwamba kabla ya kifo chake amwone Masihi. Naye alimwona Kristo. Nuru ya ajabu isiyo ya kibinadamu ilitolewa kwake, naye aliikubali tabia ya kimbingu ya Kristo. Aliiona siku ya Kristo, naye alifurahi. Alipewa kuiona kafara ya mbinguni kwa ajili ya dhambi. Alipata kielelezo cha uzoefu wake mwenyewe kuhusu kafara hii. Amri ilimjia, ikisema, "Umchukue mwanao, mwana wako wa pekee, umpendaye, Isaka, . . . ukamtoe sadaka ya kuteketezwa." Mwanzo 22:2.

**(469)** Alimlaza mwana wake wa ahadi, mwana aliyekuwa kitovu cha matumaini yake, kwenye madhabahu ya kafara. Halafu, kadiri alivyokuwa anasubiri pale karibu na madhabahu akiwa ameinua kisu chake ili kumtii Mungu, alisikia sauti kutoka mbinguni ikisema, "Usimnyoshee kijana mkono wako, wala usimtendee neno; kwa maana sasa ninajua ya kuwa unamcha Mungu, iwapo hukunizuilia mwanao, mwanao wa pekee." Mwanzo 22:12. Uzoefu huu wa kutisha uliwekwa juu ya Ibrahimu ili ya kwamba apate kuiona siku ya Kristo, na atambue pendo kuu la Mungu kwa ulimwengu, ambalo ni kuu kiasi cha kuuinua ulimwengu kutoka katika uharibifu wake, alimtoa Mwana wake wa pekee ili afe kifo cha aibu mno.

Ibrahamu alijifunza somo kuu ambalo kamwe halijapata kutolewa kwa mwanadamu yeyote kuhusu Mungu. Ombi lake kwamba apate kumwona Kristo kabla hajafa lilijibiwa. Alimwona Kristo; aliona mambo yote ambayo mwanadamu wa kufa anaweza kuona, na bado akaishi. Kwa kujisalimisha kikamilifu, aliweza kuelewa maono ya Kristo, yaliyokuwa yametolewa kwake. Alionyeshwa kwamba katika kumtoa Mwana wake wa pekee ili kuwaokoa wadhambi kutoka katika kuangamia, Mungu alikuwa anatoa kafara kuu zaidi na ya ajabu kuliko yoyote ambayo mwanadamu angeweza kutoa.

Uzoefu wa Ibrahimu ulijibu swali hii: "Nimkaribie Bwana na kitu gani, na kuinama mbele za Mungu aliye juu? Je! Nimkaribie na sadaka za kuteketezwa, na ndama za umri wa mwaka mmoja? Je! Bwana atapendezwa na elfu za kondoo waume, au na elfu kumi za mito ya mafuta? Je! Nimtoe mzaliwa wangu wa kwanza kwa kosa langu, mzao wa mwili wangu kwa dhambi ya roho yangu?" Mika 6:6, 7. Katika maneno ya Ibrahamu kwamba, "Mungu atajipatia mwana-kondoo kwa hiyo sadaka, mwanangu," (Mwanzo 22:8), na katika kile kitendo cha utoaji wa Mungu wa sadaka mahali pa Isaka, ilitangazwa kwamba hakuna mtu anayeweza kutoa fidia ya kosa kwa ajili yake mwenyewe. Mfumo huo wa kipagani wa kafara ulikuwa haukubaliki kabisa kwa Mungu. Hakuna baba ambaye angemtoa mwana wake au binti yake kama sadaka ya dhambi. Mwana wa Mungu peke yake ndiye angebeba hatia ya ulimwengu.

Kupitia katika maumivu yake mwenyewe, Ibrahimu alipewa kuiona kazi ya Mwokozi ya kafara. Lakini Waisraeli wasingeelewa kile ambacho hakikukaribishwa na mioyo yao ya kiburi. Maneno ya Kristo kuhusu Ibrahimu hayakuwafikishia umuhimu wowote wa kina. Mafarisayo waliona tu sababu mpya ya kumpinga. Waliamua kumbeza, kama waliotaka kuthibitisha kwamba Yesu alikuwa kichaa, "Wewe hujapata bado miaka hamsini, nawe umemwona Ibrahimu?"

Kwa uthabiti Yesu alijibu akisema, "Amin, amin, nawaambia, Yeye Ibrahimu asijakuwako, mimi niko."

Ukimya uliwajaa wale makutano. Jina la Mungu, lililotolewa kwa Musa kuonyesha dhana ya uwepo wa milele, lilikuwa limedaiwa kuwa **(470)** ni la Rabi huyu wa Galilaya. Alikuwa amejitangaza kuwa Yeye ni mwenye kujitosheleza, Yeye aliyekuwa ameahidiwa kwa Israeli kwamba, "ambaye matokeo yake yamekuwa tangu zamani za kale, tangu milele." Mika 5:2.

Kwa mara nyingine tena makuhani na marabi walipiga kelele dhidi ya Yesu kwamba anakufuru. Madai yake ya kuwa mmoja na Mungu yalikuwa yamewachochea kabla kutaka kuuchukua uhai wake, na miezi michache baadaye walitangaza kwa wazi, "Kwa ajili ya kazi njema hatukupigi kwa mawe; bali kwa kukufuru, na kwa sababu wewe uliye mwanadamu wajifanya mwenyewe u Mungu." Yohana 10:33. Kwa sababu alikuwa, na alithibitisha kwamba ni, Mwana wa Mungu, waliazimia kumwangamiza. Wakati huu watu wengi, wakiunga mkono upande wa makuhani na marabi, waliokota mawe ili wampige. "Yesu akajificha, akatoka hekaluni, akipita katikati yao, akaenda zake."

Nuru ilikuwa inaangaza gizani; lakini "giza halikuitambua." Yohana 1:5.

"Hata alipokuwa akipita alimwona mtu, kipofu tangu kuzaliwa. Wanafunzi wake wakamwuliza wakisema, Rabi, ni yupi aliyetenda dhambi, mtu huyu au wazazi wake, hata azaliwe kipofu? Yesu akajibu, Huyu hakutenda dhambi, wala wazazi wake; bali kazi za Mungu zidhihirishwe ndani yake. . . . Alipokwisha kusema hayo, alitema mate chini, akafanya tope kwa yale mate. Akampaka kipofu tope za macho, akamwambia, Nenda kanawe katika birika ya Siloamu, (maana yake, Aliyetumwa). Basi akaenda na kunawa; akarudi anaona."

**(471)** Kwa ujumla ilikuwa inaaminiwa na Wayahudi kwamba dhambi inaadhibiwa katika maisha haya haya. Kila ugonjwa ulichukuliwa kama adhabu ya makosa fulani, ama ya mgonjwa mwenyewe au wazazi wake. Ni kweli kwamba magonjwa yote ni matokeo ya uvunjaji wa sheria ya Mungu, lakini ukweli huu ulikuwa umepotoshwa. Shetani, mwasisi wa dhambi na matokeo yake yote, alikuwa amewaongoza watu kuuona ugonjwa na kifo kama vile vinatoka kwa Mungu, - kama adhabu iliyoletwa kwa sababu ya dhambi. Kwa hiyo yeye aliyeangukiwa na ugonjwa au janga kubwa alikuwa na mzigo wa ziada wa kuchukuliwa kama mdhambi mkuu.

Kwa namna hiyo njia ilikuwa imeandaliwa kwa Wayahudi kumkataa Yesu. Yeye ambaye "ameyachukua masikitiko yetu, amejitwika huzuni zetu" aliangaliwa na Wayahudi kama vile "amepigwa, amepigwa na Mungu, na kuteswa. Isaya 53:4, 3.

Mungu alikuwa ametoa somo lililopangwa kuzuia jambo hili. Historia ya Ayubu ilikuwa imeshaonyesha kwamba magonjwa huletwa na Shetani, lakini yanatawaliwa kwa ujumla na Mungu kwa kusudi jema. Lakini Waisraeli hawakuelewa somo hilo. Kosa lile lile ambalo wale rafiki wa Ayubu walikemewa kwalo lilikuwa linarudiwa na Wayahudi hawa katika kumkataa Kristo.

Imani ya Wayahudi kuhusu uhusiano uliopo kati ya dhambi na ugonjwa ilikuwa inashikiliwa na wanafunzi wa Kristo pia. Wakati Yesu alisahihisha kosa lao, hakufafanua sababu ya magonjwa, bali aliwaambia kile ambacho kingekuwa matokeo yake. Kwa sababu ya ugonjwa kazi za Mungu zingedhihirishwa. "Muda nilipo ulimwenguni, mimi ni nuru ya ulimwengu." Kisha akishayapaka macho ya yule kipofu, alimwagiza aende kunawa katika birika la Siloamu, na mtu yule akapata kuona. Kwa hiyo Yesu alijibu swali lile la wanafunzi kwa njia ya vitendo, kama alivyokuwa mara nyingi akijibu maswali yaliyoulizwa kwa kusukumwa na udadisi. Wale wanafunzi hawakupewa nafasi ya kujadili swali lile kwamba ni nani aliyetenda dhambi au nani hakutenda dhambi, bali kuelewa uwezo na wema wa Mungu kwa kumpa kuona huyu kipofu. Ilidhihirika kwamba hakuna nguvu ya uponyaji katika tope, au katika dimbwi la maji ambamo aliagizwa kwenda kunawa, bali kwamba nguvu ile ilikuwa ndani ya Kristo.

Mafarisayo walibaki wameshangazwa na uponyaji ule. Lakini walijawa na chuki zaidi kuliko walivyopata kuwa kabla; maana mwujiza huu ulikuwa umefanyika siku ya Sabato.

Jamaa zake kijana yule aliyeponywa, na watu waliomjua kabla akiwa kipofu, walisema, "Je! Huyu siye yule aliyekuwa akiketi na kuomba?" Walimwangalia kwa mashaka; maana macho yake yalipofunguliwa, sura yake ilibadilika na kuwa angavu, naye alionekana kama mtu mwingine ambaye si yule. Waliulizana **(472)** swali hilo. Wengine walisema, "Ndiye;" wengine wakasema, "Amefanana naye." Lakini yeye aliyekuwa amepokea mbaraka huo alijibu lile swali kwa kusema, "Mimi ndiye." Halafu aliwaambia habari za Yesu, na jinsi alivyopata kuponywa, nao wakauliza, "Yuko wapi huyo? Akasema, Mimi sijui."

Kisha wakamleta mbele ya baraza la Mafarisayo. Kwa mara nyingine yule mtu akaulizwa jinsi alivyopata kuona. "Akawaambia, Alinitia tope juu ya macho, nami nikanawa, na sasa naona. Basi baadhi ya Mafarisayo wakasema, Mtu huyo hakutoka kwa Mungu, kwa sababu haishiki sabato." Mafarisayo walitamani kumfanya Yesu kuwa mwenye dhambi, kwa hiyo asionekane kuwa ni Masihi. Hawakujua kwamba Yeye ndiye aliyeifanya Sabato na kwamba alijua matakwa yote ya Sabato, yeye aliyekuwa amemponya kipofu. Walionekana kushupalia ushikaji wa Sabato, lakini kumbe walikuwa wanapanga mipango ya mauaji siku hiyo hiyo ya Sabato. Lakini watu wengi waliguswa kusikia mwujiza huu, walisadikishwa kwamba huyu aliyefungua macho ya mtu huyu alikuwa ni zaidi ya mwanadamu wa kawaida. Wakijibu dai kwamba Yesu alikuwa mwenye dhambi kwa sababu hakuishika siku ya Sabato, walisema, "Awezaje mtu mwenye dhambi kufanya ishara kama hizo? Kukawa matengano kati yao?"

Kwa mara nyingine tena marabi walimwuliza yule aliyekuwa kipofu, "Wewe wasemaje katika habari zake kwa vile alivyokufumbua macho? Akasema, Ni nabii." Ndipo wale Mafarisayo wakadai kwamba huenda hakuzaliwa akiwa kipofu na kwamba amepata kuona. Waliwaita wazazi wake, wakawauliza, "Huyu ndiye mwana wenu, ambaye mnasema kwamba alizaliwa kipofu?"

Yule mtu mwenyewe alikuwa pale pale, akisema kwamba alikuwa kipofu, na kwamba amepata kuona; lakini Mafarisayo wale walikuwa radhi kuukana ushuhuda wa moja kwa moja waliokuwa wanashuhudia pale kuliko kukiri kwamba walikuwa katika makosa. Upotofu una nguvu sana, kujihesabia haki kwa Kifarisayo kunapotosha sana.

Wale Mafarisayo walikuwa wamebakiwa na tumaini moja, nalo lilikuwa ni kuwashurutisha kwa kuwaogopesha wazazi wa yule mtu. Kwa wema wa uongo walisema, "Amepataje, basi, kuona sasa?" Wale wazazi waliogopa kujiingiza matatani; maana ilikuwa imeshatangazwa kwamba yeyote atakayemkiri Yesu kuwa Kristo "atatengwa na sinagogi;" yaani, atatengwa na sinagogi kwa siku thelathini. Katika kipindi hicho cha kutengwa hakuna mtoto ambaye angetahiriwa wala hakuna mtu ambaye akifa angeombolezewa katika nyumba ya mtu mwenye adhabu hiyo. Hukumu hiyo ilionekana kama janga; na iliposhindikana kusababisha toba kwa mtu huyo, adhabu nzito zaidi ilifuata. Mwujiza ule mkubwa uliofanywa kwa kijana wao uliwaletea wale wazazi hali ya kusadikishwa, lakini wakajibu, "Tunajua ya kuwa huyu ndiye mwana wetu, tena ya kuwa alizaliwa kipofu; lakini jinsi **(473)** aonavyo sasa hatujui; wala hatujui ni nani aliyemfumbua macho. Mwulizeni yeye mwenyewe; yeye ni mtu mzima; atajisemea mwenyewe." Kwa njia hiyo walihamisha majukumu yote kutoka kwao kwenda kwa mwana wao yule; maana hawakuthubutu kumkiri Kristo.

Ile hali ya kutanzika ambamo Mafarisayo waliwekwa, maswali yao ya kuhoji na imani potofu, hali yao ya kutoamini mambo halisi yaliyokuwa yamefanyika katika tukio lile, yalikuwa yanafungua macho ya makutano waliokuwepo, hasa ya watu wa kawaida. Mara nyingi Yesu alikuwa amefanya miujiza yake hadharani katika maeneo ya wazi, na kazi yake ilikuwa ya kuponya magonjwa. Swali lililokuwa akilini mwa watu wengi ni, Je, Mungu angefanya kazi hizo za ajabu kupitia kwa mtu laghai, kama Mafarisayo walivyosisitiza kwamba Yesu alikuwa laghai? Makabiliano yalikuwa yanaongezeka nguvu katika pande zote mbili.

Mafarisayo waliona kwamba walikuwa wanaitangaza ile kazi iliyofanywa na Yesu. Hawakuweza kuukana mwujiza. Yule mtu aliyekuwa kipofu alikuwa amejazwa na furaha na shukrani; alivitazama viumbe vya asili vilivyoonekana vya ajabu kwake, alipendezwa na mwonekano wa uzuri wa dunia na anga. Alijisikia huru kusimulia kilichomtokea, lakini wakajaribu kumnyamazisha tena, wakisema, "Mpe Mungu utukufu. Sisi tunajua ya kuwa mtu huyo ni mwenye dhambi." Maana yake ni kwamba, Usiseme tena kwamba Mtu huyu ndiye aliyekupatia kuona; Mungu ndiye amefanya hili.

Yule aliyekuwa kipofu akasema, "Kwamba yeye ni mwenye dhambi sijui. Najua neno moja, kuwa mimi nalikuwa kipofu na sasa naona."

Kisha wakauliza tena, "Alikutendea nini? Alikufumbua macho jinsi gani?" Kwa kutumia maneno mengi-mengi walijaribu kumchanganya mawazo, ili ya kwamba ajifikirie kwamba ameamini uongo. Shetani na malaika zake waovu walikuwa katika upande wa Mafarisayo, nao waliunganisha nguvu zao na mawazo ya mwanadamu ili kushindana na ushawishi wa Kristo. Walihafifisha usadikisho uliokuwa unaingia mawazoni mwa watu wengi. Malaika wa Mungu nao pia walikuwa pale kumtia nguvu yule aliyekuwa amepata kuona.

**(474)** Mafarisayo hawakugundua kwamba walikuwa na kazi ya kushughulika na kitu ambacho ni zaidi ya yule mtu asiye na elimu aliyekuwa kipofu; hawakumjua Yeye waliyekuwa wanapambana naye. Nuru ya kimbingu ilikuwa inamulika katika sehemu za ndani ya moyo wa yule aliyekuwa kipofu. Kadiri wanafiki hawa walivyomfanya asiamini, Mungu alimsaidia kuonyesha, kwa nguvu na msimamo wa majibu yake, kiasi kwamba asingenaswa na mitego. Alijibu hivi, "Nimekwisha kuwaambia, wala hamkusikia; mbona mnataka kusikia tena? Ninyi nanyi mnataka kuwa wanafunzi wake? Basi wakamshutumu, wakasema, Wewe u mwanafunzi wake yule; sisi tu wanafunzi wa Musa. Sisi tunajua ya kuwa Mungu alisema na Musa; bali yule hatujui atokako."

Bwana Yesu alijua uzoefu mgumu ambao yule mtu alikuwa anapitia, naye alimpa neema na maneno ya kusema, kiasi kwamba akawa shahidi wa Kristo. Aliwajibu Mafarisayo kwa maneno ambayo yalikuwa kemeo lenye kukata kwa waulizaji wale. Walidai kuwa wao ni hazina ya Maandiko, waongozi wa dini ya taifa; lakini bado hapa alikuwepo Yeye afanyaye miujiza, na wao hawakujua chanzo cha uwezo wake huu, na cha tabia na madai yake. Akasema yule aliyekuwa kipofu, "Hii ni ajabu! Kwamba ninyi hamjui atokako, naye alinifumbua macho! Twajua ya kuwa Mungu hawasikii wenye dhambi; bali mtu akiwa ni mcha Mungu, na kuyafanya mapenzi yake, humsikia huyo. Tokea hapo haijasikiwa ya kuwa mtu ameyafumbua macho ya kipofu, ambaye alizaliwa hali hiyo. Kama huyo asingalitoka kwa Mungu, asingeweza kutenda neno lolote."

Huyu mtu alikutana na wadodosaji wake mahali pake. Hoja yake haikupingika. Mafarisayo walishangazwa, wakatulia, - wakiwa wamepigwa butwaa kwa sababu ya maneno yake makini na ya dhati. Kwa muda fulani kulikuwa na ukimya. Kisha makuhani na marabi hawa wasio na furaha walikusanya majoho yao, kama vile wanaoogopa unajisi kwa kukutana na mtu yule; walikung’uta mavumbi ya miguu yao, na kusema maneno ya kumkejeli, kwamba, "Wewe ulizaliwa katika dhambi tupu, nawe unatufundisha sisi?" Wakamtenga kidini.

Yesu alisikia kilichokuwa kimefanywa; naye alipomwona baadaye, alimwuliza, "Wewe wamwamini Mwana wa Mungu?"

Kwa mara ya kwanza huyu aliyekuwa kipofu aliuona uso wa Mponyaji wake. Kule mbele ya baraza alikuwa amewaona wazazi wake wakipata shida na kutatanika; alikuwa ameziona nyuso za kutokupendezwa za marabi; sasa macho yake yaliiona sura ya upendo na ya amani ya Yesu. Tayari, kwa gharama kubwa kwake, alikuwa amemkiri kwamba ana nguvu ya kimbingu; na sasa alipatiwa mafunuo ya juu zaidi.

**(475)** Yule aliyekuwa kipofu alilijibu lile swali la Yesu kwamba, "Wewe wamwamini Mwana wa Mungu?" kwa kuuliza hivi, "Ni nani, Bwana, nipate kumwamini?" Yesu akasema, "Umemwona, naye anayesema nawe ndiye." Yule mtu akajitupa miguuni pa Mwokozi na kumsujudia. Si tu kwamba alikuwa ameponywa kuona kwa kawaida, bali macho ya uelewa wake yalikuwa yamefunguliwa pia. Kristo alikuwa amefunuliwa moyoni mwake, naye alimpokea Kristo kama Aliyetumwa na Mungu.

Kundi la Mafarisayo lilikuwa limekusanyika karibu, na mwonekano wao ulionyesha mawazoni mwa Yesu ukinzani ambao haujapata kudhihirika ulioletwa na maneno na matendo yake. Akasema, "Mimi nimekuja ulimwenguni humu kwa hukumu, ili wao wasioona waone, nao wanaoona wawe vipofu." Kristo alikuwa amekuja kufumbua macho ya vipofu, kuwapa nuru wale walio gizani. Alikuwa amejitangaza kwamba ni nuru ya ulimwengu, na mwujiza uliokuwa umefanyika ulikuwa ushuhuda wa kazi yake. Watu waliomwona Mwokozi wakati alipokuja duniani mara ya kwanza walijaliwa kuona udhihirisho kamili wa uwepo wa uungu kuliko ulimwengu ulivyopata kushuhudia. Maarifa ya kumjua Mungu yalifunuliwa kwa ukamilifu zaidi. Lakini katika ufunuo wenyewe huo, watu walihukumiwa. Tabia zao zilijaribiwa, hatima zao ziliamuriwa.

Ule udhihirisho wa uwezo wa kimbingu uliokuwa umempatia yule kipofu hali ya kuona kimwili na kiroho ulikuwa umewaacha Mafarisayo katika giza zito zaidi kuliko kabla. Baadhi ya watu waliosikia, wakihisi kwamba maneno ya Kristo yaliwahusu wao, waliuliza, "Je! Sisi nasi tu vipofu?" Yesu akajibu, "Kama mngekuwa vipofu, msingekuwa na dhambi." Ikiwa Mungu angekuwa amefanya isiwezekane ninyi kuuona ukweli kusingekuwa na hatia. "Lakini sasa mwasema, Twaona." Mnajiamini wenyewe kwamba mna uwezo wa kuona, nanyi mnakataa njia ambayo kwayo pekee mngepata kuona. Kristo alikuja na msaada usio na ukomo kwa wote wanaogundua hitaji lao. Lakini Mafarisayo wasingekiri kuhitaji kitu; walikataa kuja kwa Kristo, na kwa hiyo waliachwa katika upofu wao, - upofu ambao uliwafanya wao wenyewe wakawa na hatia. Yesu akasema, "Basi dhambi yenu inakaa."

## Sura ya 52

# Mchungaji wa Kimbingu

[Sura hii imejengwa katika Yohana 10:1-30.]

"Mimi ndimi mchungaji mwema. Mchungaji mwema huutoa uhai wake kwa ajili ya kondoo." "Mimi ndimi mchungaji mwema; nao walio wangu nawajua; nao walio wangu wanijua mimi; kama vile Baba anijuavyo, nami nimjuavyo Baba. Nami nautoa uhai wangu kwa ajili ya kondoo."

Kwa mara nyingine tena Yesu aliyafikia mawazo ya wasikilizaji wake katika pilikapilika ya mambo waliyozoea kufanya. Alikuwa amefananisha ushawishi unaofanywa na Roho sawa na maji yabubujikayo. Alikuwa amejitaja kwa uwakilishi wa nuru, iliyo chanzo cha uhai na ustawi wa viumbe vya asili na mwanadamu. Sasa katika picha nzuri ya mchungaji anaeleza uhusiano wake na wale wanaomwamini. Hakuna picha iliyokuwa inaeleweka zaidi kwa wasikilizaji wake kama hii, na maneno ya Kristo yaliiunganisha na Yeye daima. Kamwe wanafunzi wale wasingeweza kuwaangalia wachungaji wanaochunga kondoo wasikumbuke fundisho hili la Mwokozi. Wangemwona Kristo ndani ya kila mchungaji aliye mwaminifu. Wangejiona wenyewe wakiwa katika kila kundi la kondoo lisilo na msaada na lenye utegemezi.

Kielelezo hiki kilikuwa kimetumiwa na nabii Isaya akikihusisha na kazi ya Masihi, katika maneno haya ya faraja, "Wewe uuhubiriye Sayuni habari njema, Panda juu ya mlima mrefu; Wewe uuhubiriye Yerusalemu habari njema, Paza sauti kwa nguvu; Paza sauti yako, usiogope; Iambie miji ya Yuda, Tazameni, Mungu wenu. . . . Atalilisha kundi lake kama mchungaji, Atawakusanya wana-kondoo mikononi mwake; Na kuwachukua kifuani mwake." Isaya 40:9-11. Daudi alikuwa ameimba hivi, "Bwana ndiye mchungaji wangu; **(477)** sitapungukiwa na kitu." Zaburi 23:1. Na Roho Mtakatifu kupitia kwa Ezekieli alikuwa amesema: "Nami nitaweka mchungaji mmoja juu yao, naye atawalisha." "Nami nitawatafuta waliopotea, nitawarudisha waliofukuzwa, nitawafunga waliovunjika, nitawatia nguvu wagonjwa." "Nami nitafanya agano la amani nao." "Hawatakuwa mateka ya makafiri tena, . . . bali watakaa salama salimini, wala hapana mtu atakayewatia hofu." Ezekieli 34:23, 16, 25, 28.

Kristo alielekeza unabii huu kwake mwenyewe, na alionyesha tofauti iliyokuwepo kati ya tabia yake na ile ya viongozi wa Israeli. Muda si mrefu Mafarisayo walikuwa wamemfukuza mtu kutoka katika zizi lao, kwa sababu alithubutu kutoa ushuhuda kuhusu uweza wa Kristo. Walikuwa wameikatilia mbali roho ambayo Mchungaji wa Kweli alikuwa anaivuta kwake. Katika hili walikuwa wameonyesha kwamba hawajui kazi iliyokabidhiwa kwao, na ya kwamba hawaistahili ile hali ya kutumainiwa waliyokuwa wamepewa kama wachungaji wa kondoo. Sasa Yesu alionyesha mkinzano uliokuwepo kati yao na Mchungaji Mwema, na alijionyesha kwamba Yeye ndiye mwangalizi halisi wa kundi la kondoo la Bwana. Kabla ya kufanya hilo, hata hivyo, alijiongelea katika kielelezo kingine.

Alisema hivi, "Yeye asiyeingia mlangoni katika zizi la kondoo, lakini akwea penginepo, huyo ni mwivi naye ni mnyang'anyi. Aingiaye mlangoni ni mchungaji wa kondoo." Wale Mafarisayo hawakuona kwamba maneno haya yalisemwa dhidi yao. Walipokuwa wakitafakari mioyoni mwao kuhusu maana ya maneno hayo, Yesu aliwaambia wazi wazi kwamba, "Mimi ndimi mlango; mtu akiingia kwa mimi, ataokoka; ataingia na kutoka, naye atapata malisho. Mwivi haji ila aibe na kuchinja na kuharibu; mimi nalikuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele."

Kristo ndiye mlango wa kuingilia katika zizi la Mungu. Watoto wake wote, tangu kale na kale, wamepata kuingia kupitia mlango huu. Katika Yesu, kama ilivyoonyeshwa katika mifano ya agano la kale, kama ilivyoonyeshwa katika alama za kivuli, kama ilivyodhihirishwa katika mafunuo ya manabii, kama ilivyofunguliwa katika mafundisho yaliyotolewa kwa wanafunzi wake, na katika miujiza iliyotendwa kwa wana wa wanadamu, watu wamemwona “Mwana-kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu" (Yohana 1:29), na kupitia kwake wanaletwa zizini mwa neema yake. Watu wengi wamekuja wakionyesha vitu vingine kwa ajili ya imani ya ulimwengu; maadhimisho na mifumo vimebuniwa ambavyo kwa hivyo watu hutumainia kupokea hali ya kuhesabiwa haki na amani katika Mungu, ili kwa njia hiyo wapate kuingia katika zizi lake. Lakini mlango pekee ni Kristo, na wote ambao wameingiza kitu fulani mahali **(478)** pa Kristo, wote ambao wamejaribu kuingia zizini kwa njia nyingine, ni wevi na wanyang’anyi.

Mafarisayo hawakuwa wameingia kupitia katika mlango huu. Walikuwa wamekwea ili kuingia zizini kupitia njia nyingine ambayo si Kristo, na hawakuwa wanatekeleza kazi ya mchungaji wa kweli. Makuhani na wakuu, waandishi na Mafarisayo, waliharibu malisho yaliyo hai, na walichafua visima vya chemchemi ya maji ya uzima. Kwa uaminifu maneno ya uvuvio yanawafafanua hao wachungaji wa uongo, yakisema: "Wagonjwa hamkuwatia nguvu, wala hamkuwaponya wenye maradhi, wala hamkuwafunga waliovunjika, wala hamkuwarudisha waliofukuzwa, . . . bali kwa nguvu na kwa ukali mmewatawala." Ezekieli 34:4.

Katika zama zote, wanafalsafa na walimu wamekuwa wakiwasilisha kwa ulimwengu nadharia ili kutosheleza mahitaji ya watu. Kila taifa la kipagani limekuwa na walimu wake wakuu na mifumo yake mikuu ya dini vyote hivi vikitoa njia nyingine za wokovu tofauti na Kristo, vikigeuza macho ya watu kuyapeleka mbali na uso wa Baba, na kujaza mioyo yao woga wa kumwogopa Yeye ambaye amewapatia baraka tupu. Mwenendo wa kazi yao ni kumwibia Mungu kile ambacho ni chake kwa njia zote mbili, uumbaji na ukombozi. Na walimu hawa wa uongo wanamwibia mwanadamu pia. Mamilioni ya wanadamu wamefungwa katika dini za uongo, katika vifungo vya hofu ya kitumwa, katika ganzi ya kutokujali, wakitumikishwa kama wanyama wabebao mizigo, wakiwa hawana matumaini wala furaha wala matarajio hapo, na wakiwa tu na woga wa kile kinachokuja baada ya wakati huu. Ni injili ya neema ya Mungu peke yake inayoweza kuinua moyo. Kutafakari upendo wa Mungu uliodhihirishwa ndani ya Mwana wake utaughutusha moyo na kuamsha nguvu za mtu kwa namna ambayo kitu kingine chochote hakiwezi. Kristo alikuja ili kwamba aumbe tena sura ya Mungu ndani ya mwanadamu; na yeyote ageuzaye wanadamu kuwapeleka mbali na Kristo anawageuzia mbali na chanzo cha maendeleo ya kweli; anawatapeli lile tumaini na kusudi na utukufu wa maisha. Huyo ni mwizi na mnyang'anyi.

"Aingiaye mlangoni ni mchungaji wa kondoo." Kristo ni vyote viwili, mlango na mchungaji. Anaingia ndani kupitia Yeye mwenyewe. Anakuwa mchungaji wa kondoo kupitia kafara yake mwenyewe. "Bawabu humfungulia huyo, na kondoo humsikia sauti yake; naye huwaita kondoo wake kwa majina yao, na kuwapeleka nje. Naye awatoapo nje kondoo wake wote, huwatangulia; na wale kondoo humfuata, kwa maana waijua sauti yake."

Katika viumbe wote kondoo yuko miongoni mwa wale walio waoga zaidi na wasiojiwezea kitu, na huko katika nchi za Mashariki uangalizi wa mchungaji kwa kondoo wake ni kazi isiyokoma na isiyohitaji kuchoka. **(479)** Zamani za kale kama ilivyo sasa kulikuwa na usalama mdogo nje ya miji iliyozungushiwa kuta. Wanyang'anyi kutoka katika makabila ya mipaka jirani, au wanyama watafutao mawindo waliotoka katika maficho yao katika miamba, walikuwa wakikamata na kuiba kondoo. Mchungaji alikuwa na kazi ya kulinda, akijua kwamba kazi hiyo ilikuwa ya hatari kwa maisha yake mwenyewe. Yakobo, aliyechunga kondoo wa Labani katika mbuga za malisho ya Harani, akielezea kazi yake mwenyewe ambayo hakuchoka kuifanya, alisema, "Hii ilikuwa hali yangu; mchana jua likanipata, na baridi usiku, usingizi ukanitoka machoni mwangu." Mwanzo 31:40. Na alipokuwa akichunga kondoo wa baba yake, kijana Daudi, akiwa peke yake bila msaada, alikabiliana na simba na dubu, na alimponya mwana-kondoo kwa kumpokonya kutoka katika meno ya wanyama hao.

Kama vile mchungaji anavyoongoza kundi lake la kondoo katika vilima vya miamba, kupitia katika msitu na makorongo ya mwituni, hadi katika sehemu tulivu yenye majani iliyo kando ya kijito; anavyowalinda milimani katika usiku wote wa upweke, akiwakinga dhidi ya wanyang'anyi, akiwahudumia kwa upendo wale kondoo walio dhaifu na wagonjwa, maisha yake hatimaye yanakuwa kama yao. Ule mwunganiko wenye nguvu na upendo unamwunganisha na wale anaowatunza. Hata kundi liwe kubwa kiasi gani, mchungaji anamjua kila kondoo. Kila kondoo ana jina lake, naye huitikia pale mchungaji anapoita jina lake.

Vile mchungaji wa kondoo wa kidunia anavyojua kondoo wake, ndivyo Mchungaji wa kimbingu anavyojua kondoo wake waliotawanyika katika ulimwengu wote. "Na ninyi, kondoo zangu, kondoo za malisho yangu, ni wanadamu, na mimi ni Mungu wenu, asema Bwana MUNGU." Yesu anasema, "Nimekuita kwa jina lako, wewe u wangu." "Nimekuchora katika vitanga vya mikono yangu." Ezekieli 34:31; Isaya 43:1; 49:16.

Yesu anatujua mmoja mmoja, na anaguswa na hisia za udhaifu wetu. Anatujua sote kwa majina. Anaijua hata nyumba tunamoishi, na jina la kila mtu anayeishi humo. Katika nyakati tofauti amewaelekeza watumishi wake kwenda katika mtaa fulani katika mji fulani, katika nyumba kama hiyo, ili kumtafuta mmoja wa kondoo wake. **(480)** Kila mtu anajulikana kikamilifu kwa Yesu kwa namna ambayo ni kama vile Mwokozi alikufa kwa ajili ya huyo peke yake. Shida ya kila mmoja inaugusa moyo wa Kristo. Kilio cha kutaka msaada hulifikia sikio lake. Alikuja kuwavuta watu wote kwake. Anawahimiza kwamba, "Nifuate," na Roho wake husukuma mioyo yao na

kuwavuta kuja kwake. Watu wengi hukataa kuvutwa. Yesu anawajua kwamba ni watu gani. Anawajua pia wale wanaosikiliza kwa furaha wito wake, na wakawa tayari kuja chini ya utunzaji wake wa kichungaji. Anasema, "Kondoo wangu waisikia sauti yangu; nami nawajua, nao wanifuata." Yeye anamtunza kila mtu kwa namna ambayo ni kama vile hakuna mtu mwingine ambaye yuko kwenye uso wa dunia.

"Huwaita kondoo wake kwa majina yao, na kuwapeleka nje. . . . Na wale kondoo humfuata, kwa maana waijua sauti yake." Mchungaji wa kondoo huko katika nchi za Mashariki hawasukumi kondoo wake. Hatumii mabavu wala kuwaogopesha; bali huenda mbele yao, na huwaita. Wanaijua sauti yake, nao huitikia wito wake. Hivyo ndivyo inavyofanyika kwa Mwokozi-Mchungaji na kondoo wake. Maandiko yanasema, "Uliwaongoza watu wako kama kundi, Kwa mkono wa Musa na Haruni." Kupitia kwa nabii, Yesu alisema hivi, "Naam nimekupenda kwa upendo wa milele, ndiyo maana nimekuvuta kwa fadhili zangu." Hamlazimishi yeyote kumfuata Yeye. Anasema, "Naliwavuta kwa kamba za kibinadamu, kwa mafungo ya upendo." Zaburi 77:20; Yeremia 31:3; Hosea 11:4.

Kinachowasukuma wanafunzi wa Kristo kumfuata si kuogopa adhabu, wala kutumainia thawabu ya milele. Wanauona upendo wa Mwokozi ambao haulinganishwi na chochote, ukiwa umefunuliwa katika maisha yake yote ya kuishi duniani, tangu katika hori la ng'ombe kule Yerusalemu hadi kwenye msalaba wa Kalvari, na kule kumwona Yeye kunavuta, kulainisha na kutiisha moyo. Upendo huamshwa katika mioyo ya watu wanaomwona. Wanaisikia sauti yake, nao humfuata.

Kama vile mchungaji anavyoenda mbele ya kondoo wake, yeye mwenyewe akikabiliana kwanza na hatari za njiani, ndivyo afanyavyo Yesu pamoja na watu wake. "Awatoapo nje kondoo wake wote, huwatangulia." Njia ya kwenda mbinguni imetakaswa kwa alama za nyayo za Mwokozi. Njia inaweza kuwa na mtelemko mkali na hali ya kuparuza, lakini Yesu amepita kwenye njia hiyo; Miguu yake imeisukumia chini miiba yenye kuumiza, akayafanya mapito kuwa mepesi zaidi kwa ajili yetu. Kila mzigo ambao tunaitwa kuubeba Yeye mwenyewe ameubeba.

Ingawa sasa amepaa kwenda mbele ya uwepo wa Mungu, na kushiriki katika kiti cha enzi cha malimwengu, Yesu hakupoteza sehemu yoyote ya hali yake ya huruma. Leo moyo ule ule wa upendo na huruma umefunguka katika shida zote za wanadamu. Leo mkono ule uliotobolewa unafikiwa na watu walio ulimwenguni ili kuwabariki watu wake kwa baraka tele. "Wala hawatapotea kamwe; wala hakuna mtu atakayewapokonya katika mkono wangu." **(483)** Mbele ya Kristo, mtu ambaye amejitoa wakfu kwake ana thamani kubwa zaidi kuliko ulimwengu wote. Mwokozi angeweza kupita katika maumivu yale ya Kalvari ili mtu mmoja apate wokovu na kuingia katika ufalme wake. Kamwe hatamwacha mtu ambaye kwa ajili yake amekufa. Atawashikilia wafuasi wake kwa mkono imara, isipokuwa wao wenyewe wakichagua kumwacha.

Katika majaribu yetu yote tunaye Msaidizi asiyeshindwa kamwe. Yeye hatuachi tupambane na majaribu tukiwa peke yetu, tupambane na uovu, na hatimaye tukandamizwe na mizigo na huzuni. Ingawa sasa amefichwa kutoka katika kuonekana kwa macho ya mwili wa kufa, sikio la kiroho linaweza kusikia sauti yake akisema, Usiogope; Niko pamoja nawe. "Nami nalikuwa nimekufa, na tazama, ni hai hata milele na milele." Ufunuo 1:18. Nimestahimili huzuni zako, nimepitia mapambano yako, nimekabiliana na majaribu yako. Nayajua machozi yako; mimi pia nimelia. Nayajua majonzi ambayo yamezama katika kina cha chini sana kiasi cha kutoweza kusikika katika sikio lolote la mwanadamu. Usidhani ya kwamba uko peke yako au umeachwa. Ingawa maumivu yako hayagusi hisia yoyote ya moyo ulio duniani, niangalie mimi, upate kuishi. "Milima itaondoka, na vilima vitaondolewa; bali wema wangu hautaondoka kwako, wala agano langu la amani halitaondolewa; asema Bwana akurehemuye." Isaya 54:10.

Hata kama mchungaji anawapenda kondoo wake kiasi gani, anawapenda zaidi wana wake na binti zake. Yesu si mchungaji wetu tu; Yeye kwetu ni "Baba wa milele." Na anasema, "Nao walio wangu nawajua; nao walio wangu wanijua mimi; kama vile Baba anijuavyo, nami nimjuavyo Baba." Yohana 10:14, 15. Kauli gani hii! – Mwana wa pekee, Yeye aliye kifuani mwa Baba, Yeye ambaye Baba amemtangaza kuwa "Mtu aliye mwenzangu" (Zekaria 13:7), - ushirika ulio kati yake na Mungu wa milele unachukuliwa kuwakilisha ushirika uliopo kati ya Kristo na watoto wake duniani!

Kwa kuwa sisi tu zawadi ya Baba yake, na thawabu ya kazi yake, Yesu anatupenda. Anatupenda kama watoto wake. Msomaji, anakupenda. Mbingu yenyewe haiwezi kutoa kitu kingine kilicho zaidi, hakuna kingine chema zaidi. Kwa hiyo amini.

Yesu alifikiria kuhusu watu walioko ulimwenguni kote ambao walipotoshwa na wachungaji wa uongo. Wale aliotafuta kuwakusanya kama kondoo wa malisho yake walikuwa wametawanyika katikati ya mbwa-mwitu, naye akasema, "Na kondoo wengine ninao, ambao si wa zizi hili; na hao nao imenipasa kuwaleta; na sauti yangu wataisikia; kisha kutakuwako kundi moja na mchungaji mmoja." Yohana 10:16.

"Ndiposa Baba anipenda, kwa sababu nautoa uhai wangu ili niutwae tena." Maana yake, Baba yangu amewapenda sana, kiasi kwamba **(484)** ananipenda hata Mimi zaidi kwa ajili ya kuyatoa maisha yangu kuwakomboa ninyi. Katika kuwa mbadala na uhakika wenu, kwa kusalimisha maisha yangu, kwa kuchukua hali zenu, maovu yenu, nimependelewa na Baba yangu.

"Nautoa uhai wangu ili niutwae tena. Hakuna mtu aniondoleaye, bali mimi nautoa mwenyewe. Nami ninao uweza wa kuutoa, ninao na uweza wa kuutwaa tena." Wakati akiwa mshirika wa jamaa ya wanadamu alikuwa na mwili wa kufa, akiwa kama Mungu alikuwa chemchemi ya uzima kwa ajili ya ulimwengu. Angeweza kusimama juu kuliko penye kifo, na kukataa kuja chini ya nguvu ya kifo; lakini kwa hiari yake aliyatoa maisha yake, ili kwamba apate kuiweka wazi hali ya kutokufa. Aliibeba dhambi ya ulimwengu, alistahimili laana, aliutoa uhai wake kama kafara, ili ya kwamba wanadamu wasife kifo cha milele. "Hakika ameyachukua masikitiko yetu, Amejitwika huzuni zetu; . . . . Alijeruhiwa kwa makosa yetu, Alichubuliwa kwa maovu yetu; Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake, Na kwa kupigwa kwake sisi tumepona. Sisi sote kama kondoo tumepotea; Kila mmoja wetu amegeukia njia yake mwenyewe; Na Bwana ameweka juu yake Maovu yetu sisi sote." Isaya 53:4-6.

## Sura ya 53

# Safari ya Mwisho Kutoka Galilaya

[Sura hii imejengwa katika Luka 9:51-56; 10:1-24.]

Kadiri mwisho wa huduma ya Kristo ulivyokaribia, kulikuwa na badiliko katika namna alivyofanya kazi. Mpaka wakati huu alikuwa ametafuta kuzuia hali ya kusisimua na kujitangaza. Alikuwa amekataa kupokea heshima za watu, na alikuwa ameondoka haraka kutoka sehemu moja kwenda nyingine pindi alipoona hamu za watu zilizompendelea zikiwaka bila kujizuia. Tena na tena aliamuru kwamba mtu yeyote asimtangaze kuwa ni Masihi.

Mnamo wakati wa Sikukuu ya Vibanda safari yake ya kwenda Yerusalemu ilifanywa kimya-kimya na kwa siri. Wakati alipotakiwa na ndugu zake kujionyesha wazi-wazi kama Masihi, Yeye alijibu kwamba, "Haujafika bado wakati wangu." Yohana 7:6. Alishika njia kwenda Yerusalemu bila kuonekana, na akaingia mjini bila kutangazwa, na bila kuheshimiwa na makutano. Lakini haikuwa hivyo katika safari yake ya mwisho. Alikuwa ameondoka Yerusalemu kwa muda fulani kwa sababu ya ubaya aliotaka kufanyiwa na makuhani na marabi. Lakini sasa aliazimia kurudi, akisafiri kwa namna ya wazi zaidi, kwa njia ndefu ya mzunguko, na akitanguliwa na mbiu ya kuja kwake kiasi ambacho alikuwa hajapata kufanya kabla. Alikuwa anaelekea kwenye tukio la kafara yake kuu, na lazima usikivu wa watu uvutwe kuelekea katika tukio hilo.

"Na kama vile Musa alivyomwinua yule nyoka jangwani, vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa." Yohana 3:14. Kama vile ambavyo macho yote ya Israeli yalielekezwa kwa nyoka aliyeinuliwa, alama iliyoamriwa kwa uponyaji wao, ndivyo macho yote yanavyotakiwa kuvutwa kwa Kristo, kafara iliyoleta wokovu kwa ulimwengu uliopotea.

Dhana isiyo sahihi kuhusu kazi ya Masihi, na ukosefu wa imani **(486)** katika tabia ya kimbingu ya Yesu, ndivyo vilivyowafanya wale ndugu zake kumhimiza kujitangaza hadharani kwa watu katika Sikukuu ya Vibanda. Sasa, katika roho inayofanana na hii, wanafunzi walitamani kumzuia asiende Yerusalemu. Walikumbuka maneno yake kuhusu mambo ambayo yangempata kule, walijua uadui mkubwa walio nao viongozi wa dini, na walipenda kumkataza Mwalimu wao asiende kule.

Moyo wa Kristo ulikuwa na kazi yenye uchungu ya kulazimisha safari yake katikati ya woga, kukata tamaa, na kutokuamini kwa wanafunzi wake aliowapenda. Ilikuwa vigumu kuwasongesha mbele kwenda katika majonzi na kufadhaika kulikokuwa kunawasubiri kule Yerusalemu. Shetani naye alikuwa karibu ili kuingiza majaribu yake kwa Mwana wa Adamu. Kwa nini sasa aende Yerusalemu, kwenye kifo cha hakika? Katika pande zake zote kulikuwa na roho zenye njaa kwa ajili ya mkate wa uzima. Katika kila upande wake kulikuwa na wagonjwa wanaosubiri neno lake la uponyaji. Kazi ambayo ilikuwa ifanywe na injili ya neema yake ilikuwa tu ndipo imeanza. Na alikuwa amejawa na nguvu zilizofikia kipeo chake. Kwa nini asiendelee kwenda katika maeneo mengine ya ulimwengu akapeleka maneno ya neema, yaani mguso wa nguvu yake ya uponyaji? Kwa nini asijichukulie raha ya kuwapatia nuru na furaha mamilioni ya watu walio gizani na katika huzuni? Kwa nini aache kazi ya kukusanya mavuno kwa wanafunzi, ambao walikuwa na imani dhaifu, wenye uelewa hafifu, na wazito wa kutenda? Kwa nini akabiliwe na mauti wakati huu, na kuiacha kazi ikiwa bado katika hatua changa? Adui yule aliyekabiliana naye kule nyikani alimhusuru sasa kwa nguvu na majaribu ya dhati. Ikiwa Yesu angesalimu amri hata kwa muda mfupi, ikiwa angebadili mwelekeo wake hata katika jambo dogo ili kujiokoa, majeshi ya Shetani yangekuwa yameshinda, na ulimwengu ungekuwa umepotea.

Lakini Yesu alikuwa ameukaza "uso wake kwenda Yerusalemu." Sheria moja katika maisha yake ilikuwa ni mapenzi ya Baba. Katika kule kutembelea hekalu wakati akiwa mvulana, alikuwa amemwambia Mariamu kwamba, "Hamkujua ya kuwa imenipasa kuwamo katika nyumba ya Baba yangu?" Luka 2:49. Kule Kana, wakati Mariamu alipotamani Yesu adhihirishe uwezo wake wa miujiza, jibu lake lilikuwa, "Saa yangu haijawadia." Yohana 2:4. Maneno hayo hayo ndiyo aliyotumia kuwajibu nduguze waliokuwa wanamhimiza aende kwenye sikukuu. Lakini katika mpango mkuu wa Mungu kulikuwa na saa iliyoamuriwa ya kujitoa mwenyewe kwa ajili ya dhambi za wanadamu, na saa ile ilikuwa karibu kufika. Asingeshindwa wala kukata tamaa. Hatua za miguu yake zinageuzwa kwenda Yerusalemu, mahali ambako wabaya wake wamekula njama za muda mrefu za kuondoa

uhai wake; sasa atautoa. Aliukaza uso wake kwenda mahali pa mateso, pa kukanwa, pa kukataliwa, pa kuhukumiwa, na pa kifo.

Naye "akatuma wajumbe kutangulia mbele ya uso wake; wakaenda wakaingia katika kijiji cha Wasamaria, ili kumtengenezea mahali." Lakini **(487)** watu wa pale walikataa kumpokea, kwa sababu alikuwa njiani kwenda Yerusalemu. Walitafsiri jambo hili kama kitendo cha Yesu kuonyesha upendeleo kwa Wayahudi, ambao walichukiwa sana na watu hawa. Ikiwa angekuwa amekuja kurejesha hekalu lile la ibada kwenye Mlima Gerizimu, wangalimpokea kwa furaha; lakini sasa alikuwa anaenda Yerusalemu, nao wasingemwonyesha ukarimu. Hawakuelewa kwamba walikuwa wanafungia nje zawadi nzuri mno kutoka mbinguni. Yesu alialika watu ili wampokee, aliomba kuhudumiwa na mikono yao, ili ya kwamba aje karibu yao, ili kuwapatia mibaraka ya thamani kubwa. Kwa kila huduma iliyoonyeshwa kwake, alilipa neema ya thamani kubwa. Lakini yote hayo yalipotezwa na Wasamaria kwa sababu ya imani potofu na chuki.

Yakobo na Yohana, wajumbe wa Kristo, walichukizwa sana na dharau hii aliyofanyiwa Bwana wao. Walijawa na ghadhabu kwa kuwa alikuwa ametendewa jambo baya na Wasamaria ambao walikuwa wameonyeshwa kuheshimiwa kwa kuwepo kwake kwao. Wajumbe hawa walikuwa wamekuwa naye kwenye mlima alipobadilika sura, na walikuwa wamemwona akitukuzwa na Mungu, na kuheshimiwa na Musa na Eliya. Walidhani kwamba kitendo hiki cha kutomheshimu kilichofanywa na Wasamaria hakiwezi kuachwa kivyo hivyo bila adhabu.

Walikuja kwa Kristo, na kumjulisha maneno yaliyokuwa yamesemwa na watu wale, wakimwambia kwamba walikuwa wamekataa hata kumpa mahali pa kulala kwa usiku mmoja tu. Walifikiri kwamba alikuwa amefanyiwa jambo baya sana, na huku wakiuona Mlima wa Karmeli kwa mbali, mahali ambapo Eliya aliwaulia manabii wa uongo, walisema, "Wataka tuagize moto ushuke kutoka mbinguni, uwaangamize; kama Eliya naye alivyofanya?" Walishangazwa kuona kwamba Yesu aliumizwa na maneno yao, na kushangazwa zaidi walipoona maneno haya ya kukanya yakishuka masikioni mwao, "Hamjui ni roho ya namna gani mliyo nayo. Kwa maana Mwana wa Adamu hakuja kuziangamiza roho za watu, bali kuziokoa." Naye akaenda katika kijiji kingine.

Kulazimisha watu kumpokea Kristo si sehemu ya kazi yake. Kutafuta kulazimisha dhamiri ni kazi ya Shetani, na watu wanaosukumwa naye. Wakijifanya kuwa na juhudi katika kuonyesha haki, wanadamu ambao wanashirikiana na malaika waovu huleta maumivu kwa wanadamu wenzao, eti ili kuwaongoa na kuwaingiza katika mawazo ya imani yao ya kidini; lakini daima Yesu anaonyesha rehema, daima akitafuta kuongoa kwa njia ya kuonyesha upendo wake. Hawezi kuruhusu ushindani ndani ya mtu, wala kukubali kujitoa nusu; bali anahitaji tu kujitoa kwa hiari, utashi wa kusalimisha moyo chini ya vizuizi vya upendo. Hakuna ushahidi hitimishi mwingine wa kuonyesha kwamba tumejawa na roho wa Shetani zaidi ya mwelekeo wa kutaka kuwaumiza na kuwaangamiza wale wasiokubaliana na kazi yetu, au wanaotenda kinyume na mawazo yetu. **(488)** Kila mwanadamu, katika mwili, nafsi, na roho, ni mali ya Mungu. Kristo alikufa ili kuwakomboa wote. Hakuna kitu kinachoweza kuwa cha kumkosea Mungu zaidi kuliko hali ya wanadamu, kwa njia ya kushikilia itikadi ya kidini, kuleta mateso kwa watu walionunuliwa kwa damu ya Mwokozi.

"Akaondoka huko akafika mipakani mwa Uyahudi, na ng'ambo ya Yordani; makutano mengi wakakutanika tena wakamwendea; akawafundisha tena kama alivyozoea." Marko 10:1.

Sehemu muhimu ya miezi ya kuifunga kazi ya Kristo ilitumiwa katika eneo la Perea, jimbo lililoko upande wa ng'ambo ya Yordani kutokea Uyahudi. Makutano walimkutanikia na kumfuata huko, kama vile ilivyokuwa mwanzoni mwa kazi yake huko Galilaya, na mengi ya mafundisho yake ya awali yalirudiwa.

Kama vile alivyokuwa amewatuma wale kumi na wawili, vivyo hivyo "aliweka na wengine, sabini, akawatuma wawili wawili wamtangulie kwenda kila mji na kila mahali alipokusudia kwenda mwenyewe." Luka 10:1. Wanafunzi hao walikuwa wamekuwa naye kwa nyakati fulani-fulani, wakifundishwa kwa ajili ya kazi yao. Wakati wale kumi na wawili walipotumwa mara ya kwanza kwenda kazini peke yao, wanafunzi wengine waliandamana na Yesu katika safari yake ya Galilaya. Kwa njia hiyo walipata wasaa wa kuwa na ushirika wa karibu naye, na kupata mafunzo ya moja kwa moja kutoka kwake. Sasa watu hawa wengi zaidi walitakiwa waingie kazini peke yao.

Maelekezo yaliyotolewa kwa hawa sabini yalikuwa yale yale yaliyokuwa yametolewa kwa wale kumi na wawili; lakini amri ya wale kumi na wawili, ya kuwakataza kuingia katika mji wa Mataifa au wa Wasamaria, haikutolewa

kwa hawa sabini. Ingawa Kristo alikuwa mara tu amefukuzwa na Wasamaria, upendo wake kwao ulikuwa usiobadilika. Wale sabini walipotoka kwenda katika jina lake, walitembelea, kwanza kabisa, miji ya Wasamaria.

Safari ya Mwokozi mwenyewe ya kutembelea Samaria, na baadaye, sifa iliyotolewa kwa Msamaria mwema, na furaha ya shukrani ya mwenye ukoma, Msamaria, ambaye katika wale kumi yeye peke yake ndiye aliyerudi kumshukuru Kristo, yalikuwa yamesheheni mambo muhimu kwa wale wanafunzi. Fundisho hilo lilizama katika mioyo yao. Katika kuwatuma kwake, muda mfupi tu kabla ya kupaa kwake, Yesu aliitaja Samaria pamoja na Yerusalemu na Uyahudi kama mahali ambapo walipaswa kuanzia kuihubiri injili. Mafundisho yake yalikuwa yamewaandaa kutimiza agizo hili la utume. Walipoenda Samaria katika jina la Bwana wao, walikuta watu wako tayari kuwapokea. Wasamaria walikuwa wamesikia maneno ya Kristo ya kuwakubali na kazi zake za rehema kwa watu wa taifa lao. Waliona kwamba, licha ya jinsi walivyomtenda mabaya, Yeye alikuwa tu na mawazo ya upendo kwao, na mioyo yao iliongolewa. Baada ya kupaa kwake waliwakaribisha wajumbe wake, na wanafunzi walikusanya mavuno ya thamani kutoka miongoni mwa wale ambao hapo kwanza walikuwa adui zao wakubwa sana. **(489)** "Mwanzi uliopondeka hatauvunja, wala utambi utokao moshi hatauzima; atatokeza hukumu kwa kweli." "Na jina lake Mataifa watalitumainia." Isaya 42:3; Mathayo 12:21.

Katika kuwatuma hao sabini, Yesu aliwaagiza, kama alivyoagiza wale kumi na wawili, wasilazimishe kukaa mahali wasipopokelewa. Alisema, "Na mji wowote mtakaouingia, nao hawawakaribishi, tokeni humo, nanyi mkipita katika njia zake semeni, Hata mavumbi ya mji wenu yaliyogandamana na miguu yetu tunayakung'uta juu yenu. Lakini jueni hili, ya kuwa Ufalme wa Mungu umekaribia." Hawakupaswa kufanya hivyo kwa misukumo ya hisia au kwa msisimko tu, bali kuonyesha jinsi lilivyo baya tendo la kuukata ujumbe wa Bwana au wajumbe wake. Kuwakataa watumishi wa Bwana ni kumkataa Kristo mwenyewe.

Yesu aliongeza hivi, "Nawaambia ya kwamba siku ile itakuwa rahisi zaidi Sodoma kuistahimili adhabu yake kuliko mji huo." Halafu mawazo yake yalirejea na kuelekezwa kwenye miji ya Galilaya mahali ambapo sehemu kubwa ya huduma yake ilikuwa imefanyika. Kwa sauti ya huzuni sana alisema, "Ole wako Korazini! Ole wako, Bethsaida! Kwa kuwa kama miujiza hiyo iliyofanyika kwenu ingalifanyika katika Tiro na Sidoni, wangalitubu tangu hapo, huku wakiketi katika nguo za kigunia na majivu. Lakini, siku ya hukumu itakuwa rahisi Tiro na Sidoni kustahimili adhabu zake kuliko ninyi. Nawe Kapernaumu, je! Utakuzwa hata mbinguni? Utashushwa hata kuzimu."

Miji hii yenye shughuli nyingi iliyokuwa kando-kando ya Bahari ya Galilaya ilikuwa imepewa bure baraka nyingi kutoka mbinguni. Siku kwa siku Mfalme wa uzima alikuwa ameingia na kutoka katika miji hii. Utukufu wa Mungu, ambao manabii na wafalme walikuwa wametamani kuuona, ulikuwa umewaangazia makutano waliokutana katika nyayo za Mwokozi. Lakini bado walikuwa wameikataa Zawadi ya mbinguni.

Kwa hali ya kujionyesha kuwa makini marabi walikuwa wamewaonya watu dhidi ya kupokea mafundisho mapya ya dini yaliyofundishwa na mwalimu huyu mpya; maana nadharia zake na matendo yake yalikuwa yanakinzana na mafundisho ya wazee wao. Watu waliheshimu mambo yaliyofundishwa na makuhani na Mafarisayo, badala ya kutafuta wao wenyewe kulielewa neno la Mungu. Waliwaheshimu makuhani na wakuu badala ya kumheshimu Mungu, na waliukataa ukweli ili wapate kuyashika mapokeo yao wenyewe. Wengi walikuwa wameguswa na kuvutwa; lakini hawakutenda sawa na kusadikishwa kwao, na hawakujali kuwa katika upande wa Kristo. Shetani alileta vishawishi vyake, mpaka nuru ikaonekana kama giza. Kwa hiyo wengi waliukataa ukweli ambao ungewahakikishia wokovu wa nafsi zao.

Shahidi Mwaminifu anasema, "Tazama, nasimama mlangoni, nabisha." Ufunuo 3:20. Kila onyo, kemeo, na shauri lililo katika neno la Mungu au **(490)** litolewalo kwa njia ya wajumbe wake ni namna ya kubisha hodi mlangoni pa moyo. Ni sauti ya Yesu anayeomba kuingia. Kwa kila tendo la kubisha hodi ambalo haliitikiwi, huufanya mwelekeo wa kufungua mlango kuwa hafifu zaidi. Ushawishi wa Roho Mtakatifu ulivyo leo unapodharauliwa hautakuwa na nguvu kama hizo hizo kesho. Mguso ulio moyoni huzidi kupungua, na huzidi kuongeza pengo lililopo kati ya mawazo ya hatari ya maisha haya mafupi na yale makuu ya umilele ulio ng'ambo. Hatia yetu wakati wa hukumu haitatokana na hali ya kwamba tumekuwa katika uovu, bali itatokana na hali kwamba tumepuuza fursa za kujifunza ukweli tulizoletewa na mbingu.

Kama wale mitume walivyokuwa, hawa sabini pia walikuwa wamejaliwa kupokea uwezo ulio zaidi ya ule wa kibinadamu kama muhuri wa kazi yao. Kazi yao ilipokamilika, walirudi kwa furaha, wakisema, "Bwana, hata pepo wanatutii kwa jina lako." Yesu akajibu, akasema, "Nilimwona Shetani, akianguka kutoka mbinguni."

Matukio ya wakati uliopita na ujao yaliwekwa wazi mawazoni mwa Yesu. Alimwona Lusifa vile alivyotupwa chini kutoka mahali pa mbinguni hapo kwanza. Alitazama mbele katika matukio ya mateso yake, wakati tabia ya mdanganyifu itakapowekwa wazi mbele ya malimwengu yote. Alisikia sauti kwamba, "Imekwisha" (Yohana 19:30), ikitangaza kwamba ukombozi wa jamii ya waliopotea ulikuwa umekuwa wa uhakika milele, kwamba mbingu ilikuwa imefanywa kuwa salama milele dhidi ya mashtaka, madanganyo, upinzani, ambavyo vingeanzishwa na Shetani.

Ng'ambo ya msalaba wa Kalvari, pamoja na maumivu yake na aibu, Yesu alitazama siku ile kuu ya mwisho, wakati mfalme wa nguvu za pepo atakapokutana na uangamivu wake katika dunia iliyopotoshwa na uasi wake. Yesu aliiona kazi ya uovu ikiwa imekomeshwa milele, na amani ya Mungu ikiijaza mbingu na nchi.

Tangu pale wafuasi wa Kristo walipaswa kumwona Shetani kama mshindani aliyeshindwa. Kwenye msalaba, Yesu alikuwa anaenda kupata ushindi kwa ajili yao, na alitaka waupokee ushindi huo kama wa kwao. Alisema, "Tazama, nimewapa amri ya kukanyaga nyoka na nge, na nguvu zote za yule adui, wala hakuna kitu kitakachowadhuru."

Nguvu zisizo na kikomo za Roho Mtakatifu ni ulinzi wa kila nafsi iungamayo. Hakuna mtu aombaye ulinzi wake kwa dhati na imani ambaye Kristo ataruhusu achukuliwe na nguvu ya adui yule. Mwokozi yuko katika upande wa watu wake wanaojaribiwa na kupimwa. Kwake hakuwezekani kuwa na kitu kinachoitwa kuanguka, kupotea, kutowezekana, au kushindwa; tunaweza kufanya mambo yote katika Yeye atutiaye nguvu. Majaribu na kupimwa **(493)** vinapokuja, usisubiri kurekebisha kwanza magumu yote, bali mwangalie Yesu, msaada wako.

Kuna Wakristo ambao hufikiria sana na kusema mengi kuhusu uwezo wa Shetani. Wanafikiria kuhusu adui yao huyo, wanaomba kuhusu huyo, wanamzungumzia huyo, naye anajaa zaidi na zaidi katika mawazo yao. Ni kweli kwamba Shetani ni kiumbe mwenye nguvu; lakini, shukuru Mungu, tuna Mwokozi mwenye nguvu aliyemfukuza mwovu kutoka mbinguni. Shetani anapendezwa tunapokuza uwezo wake. Kwa nini tusiongee habari za Yesu? Kwa nini tusitukuze uweza wake na upendo wake?

Ule upinde wa mvua wa ahadi unaokizunguka kiti cha enzi huko juu ni ushuhuda wa daima kwamba "Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele." Yohana 3:16. Unashuhudia kwa malimwengu kwamba Mungu hatawaacha watu wake kamwe katika mapambano yao dhidi ya uovu. Ni uhakikisho kwetu wa nguvu na ulinzi kwa kadiri kiti cha enzi chenyewe kitakavyodumu.

Yesu aliongeza kwamba, "Lakini, msifurahi kwa vile pepo wanavyowatii; bali furahini kwa sababu majina yenu yameandikwa mbinguni." Msifurahi katika kuwa na uwezo, msije mkapoteza hali ya kumtegemea Bwana. Mwe waangalifu hali ya kujitumainia isije ikaingia, mkafanya kazi kwa nguvu zenu wenyewe, badala ya kufanya kazi kwa nguvu za Bwana wenu. Unafsi uko tayari daima kuchukua nafasi ikiwa hatua yoyote ya kupima mafanikio itaambatanishwa na kazi hii. Unafsi husifiwa na kutukuzwa, na mawazo hayawekwi katika fikra za wengine kwamba Mungu ndiye yote katika yote. Mtume Paulo anasema, "Niwapo dhaifu ndipo nilipo na nguvu." 2 Wakorintho 12:10.

Tunapokuwa na utambuzi wa udhaifu wetu, tunajifunza kutegemea nguvu ya juu isiyo ya kawaida. Hakuna kitu kinachoweza kujikita katika mioyo yetu kama uelewa wetu kuhusu wajibu wetu kwa Mungu. Hakuna kitu kinachozama chini kabisa katika vina vya tabia kama uelewa wa upendo wa Kristo unaosamehe. Yatupasa tuje kwa Mungu, hapo ndipo tutakapojazwa Roho Mtakatifu, ambaye hutuwezesha kuja kwa wanadamu wenzetu. Halafu shangilieni kwamba kupitia kwa Kristo mmeunganishwa na Mungu, na wana wa jamaa ya mbinguni. Mnapoangalia juu zaidi kuliko ninyi wenyewe, mtakuwa na uelewa wa daima wa udhaifu wa mwanadamu. Kadiri mnavyopunguza hali ya kutegemea ubinadamu, ndivyo mtakavyopata zaidi uelewa kamili na wa hakika kuhusu uzuri wa Mwokozi wenu. Kadiri mnavyojifungamanisha zaidi na chanzo cha nuru na nguvu, nuru kubwa zaidi itaangazwa kwenu, na mtakuwa na nguvu kubwa zaidi ya kufanya kazi kwa ajili ya Mungu. Shangilieni kwamba ninyi ni kitu kimoja na Mungu, kitu kimoja na Kristo, na kitu kimoja na jamaa yote ya mbinguni. **(494)** Wale

sabini waliposikiliza maneno hayo ya Kristo, Roho Mtakatifu alikuwa akisukuma fahamu zao kwa kutumia vitu halisi vilivyokuwepo, na akiandika ukweli katika mbao za moyo. Ingawa walikuwa wamezungukwa na makutano walikuwa kama vile wamefungiwa ndani pamoja na Mungu.

Akijua kwamba walikuwa wamepata kuvuviwa katika saa ile, Yesu "alishangilia kwa Roho Mtakatifu, akasema, Nakushukuru, Baba, Bwana wa mbingu na nchi, kwa kuwa mambo haya umewaficha wenye hekima na akili; umewafunulia watoto wachanga; Naam, Baba, kwa kuwa ndivyo ilivyokupendeza. Nimekabidhiwa vyote na Baba yangu, wala hakuna amjuaye Mwana ila Baba; wala hakuna amjuaye Baba ila Mwana, na yeyote ambaye Mwana apenda kumfunulia."

Wenye heshima wa ulimwengu, wale waitwao wakuu na wenye akili, pamoja na hekima zote wanazodai kuwa nazo, hawakuweza kuielewa tabia ya Kristo. Walimpima kwa mwonekano wake wa nje, kutokana na kushushwa kulikompata kama mwanadamu. Lakini wavuvi na watoza ushuru walipewa kuona kisichoonekana. Hata wanafunzi wake wenyewe walishindwa kuona yote ambayo Yesu alinia kuwafunulia; lakini katika nyakati tofauti-tofauti baadaye, kadiri walivyojisalimisha katika nguvu za Roho Mtakatifu, akili zao ziliangaziwa. Waligundua kwamba Mungu mwenye nguvu, akiwa amevishwa vazi la uanadamu, alikuwa miongoni mwao. Yesu alishangilia kwamba ingawa nuru hii haikuwa kwa wenye hekima na akili, ilikuwa imefunuliwa kwa watu hawa wa hali ya chini. Mara nyingi alipokuwa amefundisha Maandiko ya Agano la Kale, na kuonyesha jinsi yanavyomhusu Yeye na kazi yake ya upatanisho, walikuwa wameamshwa na Roho wake, na kuinuliwa kwenda katika mazingira ya mbinguni. Walipata uelewa wa wazi zaidi wa ukweli wa kiroho ulionenwa na manabii kuliko hata waandishi wenyewe wa ukweli huo walivyouelewa. Baada ya pale wangesoma Maandiko ya Agano la Kale, si kama mafundishop ya kidini ya waandishi na Mafarisayo, si kama matamko ya wenye hekima waliokufa, bali kama ufunuo mpya kutoka kwa Mungu. Walimtazama Yeye "ambaye ulimwengu hauwezi kumpokea, kwa kuwa haumwoni wala haumtambui; bali ninyi mnamtambua, maana anakaa kwenu, naye atakuwa ndani yenu." Yohana 14:17.

Njia pekee ambayo kwayo tunaweza kupata uelewa kamili zaidi wa ukweli ni kwa kunyenyekesha na kutiisha moyo chini ya Roho Mtakatifu. Lazima moyo usafishwe na kuondokana na kujiona na kiburi, na kuondokana na mambo yote yanayoufanya kupagawa, na lazima Kristo apewe kiti cha enzi ndani ya moyo. Sayansi ya wanadamu ina ukomo kiasi kwamba haiwezi kuelewa kazi ya upatanisho. Mpango wa ukombozi ni mrefu sana kiasi kwamba falsafa haiwezi kuueleza. Daima utabaki kuwa **(495)** fumbo ambalo haliwezi kueleweka katika hoja za wenye akili sana. Sayansi ya wokovu haiwezi kuelezwa; bali inaweza kujulikana kwa uzoefu. Anayeweza kuona uthamani wa Mwokozi ni yule tu anayeona maisha yake ya dhambi.

Masomo yaliyofundishwa na Kristo kadiri alivyotembea kutoka Galilaya kwenda Yerusalemu yalikuwa yamejaa mafundisho. Watu wale waliyasikiliza maneno yake kwa hamu. Katika eneo lile la Perea kama ilivyokuwa Galilaya watu hawakuwa chini ya udhibiti wa misimamo ya Kiyahudi kama ilivyokuwa kule Uyahudi, na mafundisho yake yalipata mwitikio mioyoni mwao.

Wakati huu wa miezi ya mwisho-mwisho ya kazi yake, ndipo ilipotolewa sehemu kubwa ya mifano aliyofundisha. Makuhani na marabi walimkabili kwa uchungu mkubwa kuliko kabla, na maonyo yake kwao yalitolewa kwa lugha ya mifano. Hawakukosea kuipata maana ya mifano yake kwao, lakini katika maneno yake hawakuona lolote la kutumia kumshtaki. Katika mfano wa Farisayo na mtoza ushuru, sala ya kusifia hali ya kujitosheleza binafsi kwamba, "Ee Mungu, nakushukuru kwa kuwa mimi si kama watu wengine," ilisimama ikionyesha tofauti kubwa ikilinganishwa na ombi la dhati kwamba, "Uniwie radhi mimi mwenye dhambi." Luka 18:11, 13. Hivyo ndivyo Kristo alivyokemea unafiki wa Wayahudi. Na kwa kutumia kielelezo cha mtini usiozaa na karamu kubwa alitabiria uangamivu utakaoliangukia taifa lisilotubu. Wale waliokataa kwa kejeli mwaliko wa karamu ya injili waliyasikia maneno yake ya onyo yasemayo: "Maana nawaambia ya kwamba katika wale walioalikwa, hapana hata mmoja atakayeionja karamu yangu." Luka 14:24.

Mafundisho yaliyotolewa kwa wanafunzi wale yalikuwa ya thamani sana. Mfano wa mjane asihiye na rafiki aombaye mkate usiku wa manane uliyapa maneno yake nguvu mpya, "Ombeni, nanyi mtapewa; tafuteni, nanyi mtaona; bisheni, nanyi mtafunguliwa." Luka 11:9. Na mara kwa mara imani yao inayoyumbayumba ilitiwa nguvu kwa kumbukumbu ya kile alichokuwa amesema Yesu kwamba, "Na Mungu, je! Hatawapatia haki wateule wake wanaomlilia mchana na usiku, naye ni mvumilivu kwao? Nawaambia, atawapatia haki upesi." Luka 18:7, 8.

Kristo aliurudia mfano mzuri wa kondoo aliyepotea. Na alisogeza fundisho la mfano huo mbali zaidi, aliposimulia mfano wa sarafu iliyopotea na wa mwana mpotevu. Wanafunzi wale hawakuweza kuona kikamilifu nguvu ya masomo haya; lakini baada ya kumwagwa kwa Roho Mtakatifu, wakati walipoona ujio wa makusanyiko ya Mataifa na hasira za wivu wa Wayahudi, walielewa vizuri zaidi somo la mwana mpotevu, nao waliweza kuingia katika raha ya maneno ya Kristo kwamba, "Kufanya furaha na shangwe ilipasa, **(496)** kwa kuwa huyu ndugu yako alikuwa amekufa, naye amefufuka; alikuwa amepotea, naye ameonekana." Luka 15:32, 24. Na walipotoka na kwenda katika jina la Bwana, wakikabiliwa na upinzani na umaskini na mateso, mara kwa mara walijitia nguvu mioyoni kwa kurudia agizo lake, lile lilosemwa katika safari hii ya mwisho, kwamba, "Msiogope, enyi kundi dogo; kwa kuwa Baba yenu ameona vema kuwapa ule ufalme. Viuzeni mlivyo navyo, mtoe sadaka. Jifanyieni mifuko isiyochakaa, akiba isiyopungua katika mbingu, mahali pasipokaribia mwivi, wala nondo haharibu. Kwa kuwa hazina yenu ilipo, ndipo itakapokuwapo na mioyo yenu." Luka 12:32-34.

## Sura ya 54

# Msamaria Mwema

[Sura hii imejengwa katika Luka 10:25-37.]

Katika kisa cha Msamaria mwema, Kristo anaelezea hali ya dini ya kweli. Anaonyesha kwamba dini ya kweli haiko katika mifumo, kauli za misingi ya imani ya kidini, au maadhimisho, bali katika kutenda matendo ya upendo, katika kuleta mazuri makuu kwa watu wengine, katika wema ulio wa kweli.

Wakati Yesu alipokuwa anawafundisha watu, "mwana-sheria mmoja alisimama amjaribu; akisema, Mwalimu, nifanye nini ili niurithi uzima wa milele?" Kwa hamu kusanyiko lile kubwa lilikaa kimya kungoja jibu. Makuhani na marabi walikuwa wamefikiria kumtatanisha Kristo kwa njia ya swali lile lililoulizwa na mwanasheria. Lakini Mwokozi hakuingia katika mabishano. Alitaka jibu litoke kwa mwulizaji yule yule. Akasema, "Imeandikwa nini katika torati? Wasomaje?" Bado Wayahudi walikuwa wanamshutumu Yesu kwa kuipa uzito mdogo sheria iliyotolewa kule Sinai; lakini Yeye aligeuzia habari ya wokovu kwenye ushikaji wa amri.

Mwanasheria yule akasema, "Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote, na kwa akili zako zote; na jirani yako kama nafsi yako. Yesu akasema, "Umejibu vema; fanya hivi nawe utaishi."

Mwanasheria yule hakuridhishwa na nafasi na matendo ya Mafarisayo. Alikuwa amejifunza Maandiko kwa nia ya kujifunza maana yake halisi. Alikuwa na nia kweli kweli katika jambo hilo, naye alikuwa ameuliza kwa nia na dhamiri njema kwamba, "Nifanye nini?" Katika lile jibu lake kulingana na matakwa **(498)** ya sheria, aliyapita maadhimisho yote ya kushika desturi na kaida za kidini. Hakuonyesha thamani ya vitu hivyo, bali alionyesha kanuni kuu mbili ambazo zinaishikilia sheria yote na manabii. Jibu hili, ambalo lilikubaliwa na Kristo, lilimweka Mwokozi katika nafasi nzuri dhidi ya marabi. Wasingeweza kumhukumu kwa kuruhusu kile ambacho kiliwekwa na mtoaji wa sheria.

Yesu alisema, "Fanya hivi nawe utaishi." Aliionyesha sheria kama kitu cha mwunganiko wa kimbingu, na katika somo hilo alifundisha kwamba haiwezekani kuitunza amri moja, na kuvunja nyingine; maana msingi wa zote ni mmoja. Hatima ya mwanadamu inaamriwa na utii wake kwa sheria yote. Upendo wa juu kwa Mungu na upendo usiogawanyika kwa mwanadamu ndizo kanuni zinazotakiwa kutawala maishani.

Yule mwanasheria alijikuta ni mvunja sheria. Maneno ya Kristo yanayopeleleza ndani yalimwonyesha hatia yake. Ile haki ya sheria, aliyodai kuifahamu, hakuwa ameifanyia kazi kwa vitendo. Hakuwa ameonyesha upendo kwa mwanadamu mwenzake. Toba ilitakiwa; lakini badala ya kutubu, alijaribu kujihalalisha. Badala ya kuukubali ukweli ule, alitafuta kuonyesha jinsi ilivyo vigumu kuitimiza amri ile. Kwa njia hiyo alitaka kufanya mambo mawili ambayo ni kuepuka ule usadikisho na kujionyesha machoni pa watu kwamba hana hatia. Maneno ya Mwokozi yalikuwa yameonyesha kwamba swali alilouliza halikuwa linahitajika, maana alikuwa ameweza kulijibu yeye mwenyewe. Lakini bado alileta swali jingine, akisema, "Na jirani yangu ni nani?"

Swali hili lilisababisha ubishi usiokoma miongoni mwa Wayahudi. Hawakuwa na mashaka kuhusu wapagani na Wasamaria; hawa walikuwa wageni na adui. Lakini mpaka ungewekwa wapi miongoni mwa watu wa taifa lao, na miongoni mwa matabaka yale tofauti katika jamii yao? Ni mtu gani ambaye angeonekana kuwa jirani kwa kuhani, rabi na mtu mkuu? Walitumia muda wa maisha yao katika marudio ya desturi za kidini za kujifanya safi. Walifundisha kwamba kugusana na makundi ya watu wasiojua kitu na wasiojali kungeleta unajisi ambao ungesababisha kazi ya kuchosha kuuondoa. Je, wangewaona "wanajisi" kama majirani?

Kwa mara nyingine tena Yesu alikataa kuingizwa katika mabishano. Hakushutumu msimamo mbaya wa wale waliokuwa wanafuatilia kumshtaki. Bali kwa kutumia kisa chepesi aliwaonyesha wasikilizaji wake picha ya kutiririka kwa upendo utokao mbinguni kwa namna iliyogusa mioyo yote, na kumvuta yule mwanasheria kuukiri ukweli.

Njia ya kufukuza giza ni kuikubali nuru. Njia nzuri zaidi ya kushughulika na makosa ni kuonyesha ukweli. Udhihirisho wa upendo wa Mungu ndio unaodhihirisha uovu na dhambi ya moyo ambayo kitovu chake kiko katika kujipenda binafsi.

**(499)** Yesu akasema, "Mtu mmoja alishuka toka Yerusalemu kwenda Yeriko, akaangukia kati ya wanyang'anyi; wakamvua nguo, wakamtia jeraha, wakaenda zao, wakimwacha karibu ya kufa. Kwa nasibu kuhani mmoja alishuka kwa njia ile; na alipomwona alipita kando. Na Mlawi vivyo hivyo, alipofika pale akamwona, akapita kando." Luka 10:30-32. Hili halikuwa tukio la kufikirika tu, bali tukio halisi lililotokea, ambalo lilijulikana kuwa vile vile lilivyosimuliwa. Yule kuhani na Mlawi waliopita kando walikuwa miongoni mwa watu waliokuwa wanasikiliza maneno ya Yesu.

Katika safari ile ya kutoka Yerusalemu kwenda Yeriko, msafiri yule alilazimika kupita katika sehemu ya jangwa la Uyahudi. Barabara ile ilipita katika makorongo ya mawe porini, ambayo yalikuwa na wanyang'anyi, na yalikuwa ni mahali penye mashambulizi. Hapa ndipo mahali msafiri huyu alipovamiwa, akinyang'anywa vitu vyote vya thamani, akijeruhiwa na kutokwa na damu, na kuachwa kando ya njia akiwa nusu ya kufa. Akiwa amelala hapo, kuhani alikuja kwa njia hiyo; lakini alimchungulia kidogo tu yule mtu aliyejeruhiwa. Halafu alitokea Mlawi. Akitaka kujua kilichotokea, alisimama na kumwangalia yule mhanga. Aliguswa kuhusu kile alichopaswa kufanya; lakini haukuwa wajibu unaokubaliwa kufanywa. Alitamani kwamba heri asingeipita njia ile, kusudi kwamba asiwe amemwona mtu yule. Alijiliwaza kwamba kazi ile haikuwa yake.

Watu wote hawa wawili walikuwa na nafasi katika utumishi mtakatifu, na walisemekana kuwa wafundishaji wa Maandiko. Walikuwa watu wa tabaka rasmi lililochaguliwa ili kumwakilisha Mungu kwa watu. Walipaswa wawe wenye "kuwachukulia kwa upole wao wasiojua na wenye kupotea" (Waebrania 5:2), ili ya kwamba wapate kuwaongoza **(500)** watu katika kuujua upendo wa Mungu ulio mkuu kwa wanadamu. Kazi waliyokabidhiwa kuifanya ilikuwa ile ile ambayo Yesu alikuwa ameeleza kwa watu wake aliposema, "Roho wa Bwana yu juu yangu, Kwa maana amenitia mafuta kuwahubiri maskini habari njema. Amenituma kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao, Na vipofu kupata kuona tena, Kuwaacha huru waliosetwa." Luka 4:18.

Malaika wa mbinguni wanawaangalia watu wa jamaa ya Mungu wanaoteseka duniani, nao wako tayari kushirikiana na wanadamu katika kuondoa maumivu na mateso kwa watu. Kwa uongozi wake Mungu alikuwa amewaleta kuhani na Mlawi katika barabara ile aliyokuwemo majeruhi yule, ili kwamba wapate kuona hitaji lake la huruma na msaada. Mbingu yote ilisubiri kuona kama mioyo ya watu hawa ingeguswa na huruma kwa maumivu ya mwanadamu. Mwokozi ndiye aliyekuwa amewafundisha Waebrania kule jangwani; kutoka katika nguzo ya wingu na ya moto alikuwa amefundisha somo lililo tofauti kabisa likilinganishwa na lile ambalo watu walikuwa wanafundishwa na makuhani na waalimu. Wema ulioagizwa na sheria ulienda mbali hadi kwa wanyama walio wadogo, ambao hawawezi kuonyesha mahitaji na maumivu yao kwa maneno. Maelekezo yalikuwa yametolewa kwa Musa kwa ajili ya wana wa Israeli kutekeleza kiasi hiki: "Ukimwona ng'ombe wa adui wako, au punda wake, amepotea, sharti umrudishie mwenyewe tena. Ukimwona punda wake huyo akuchukiaye hali ameanguka chini ya mzigo wake, nawe ungejizuia usimsaidie, lazima umsaidie." Kutoka 23:4, 5. Lakini kupitia mtu huyu aliyejeruhiwa na wanyang'anyi, Yesu alifundisha habari ya ndugu aliye katika shida. Mioyo yao ingeguswa na huruma kiasi gani zaidi ya vile ilivyo kwa mnyama! Ujumbe ulikuwa umetolewa kwao kupitia kwa Musa kwamba Bwana Mungu wao, "Mungu mkuu, mwenye kuogofya," "huwafanyia yatima na mjane hukumu ya haki, naye humpenda mgeni." Kwa hiyo aliamuru kwamba, "Mpendeni mgeni." "Mpende kama nafsi yako." Kumbukumbu 10:17-19; Walawi 19:34.

Ayubu alisema, "Mgeni hakulala njiani; Lakini nilimfungulia msafiri milango yangu." Na malaika wale wawili katika mwonekano wa wanadamu walipokuja Sodoma, Lutu alishuka chini akainamisha uso wake mpaka nchi, na kusema, "Bwana zangu, karibuni nawasihi mwingie nyumbani mwa mtumwa wenu, mkalale." Ayubu 31:32; Mwanzo 19:2. Kuhani na Mlawi walikuwa wanaelewa masomo yote haya, lakini hawakuyaweka katika maisha halisi ya vitendo. Wakiwa wamefunzwa katika shule ya fahari ya taifa lile, walikuwa wabinafsi, finyu na wenye kujiona upekee. Walipomwangalia yule aliyejeruhiwa, hawakuweza kujua kwamba alikuwa mtu wa taifa lao au la. Walidhani kwamba huenda ni mtu wa jamii ya Wasamaria, nao wakageuka na kupita kando. **(503)** Katika kitendo chao, kwa kadiri Kristo alivyosimulia, mwanasheria yule hakuona jambo tofauti na vile alivyofundishwa kuhusu matakwa ya sheria. Lakini sasa tukio jingine lilionyeshwa:

Msamaria mmoja, katika kusafiri kwake, alifika mahali hapo alipokuwa yule mhanga, akamhurumia. Hakuuliza kama msafiri yule alikuwa Myahudi au Mataifa. Yule Msamaria alijua vema kwamba ikiwa yule mtu angekuwa Myahudi na hali yao hao wawili ikawa kinyume cha vile ilivyokuwa, mtu yule angemtemea Msamaria mate usoni, na kumpita bila huruma. Lakini yeye hakusita kwa sababu ya hilo. Hakujali kwamba yeye mwenyewe angekuwa katika hatari ya kuvamiwa kwa kitendo chake cha kukawia mahali pale. Ilitosha kwake kuona kwamba mbele yake kulikuwa na mwanadamu aliye katika uhitaji na maumivu. Alivua vazi lake alilokuwa amejifunika. Alitumia mafuta na divai vilivyoandaliwa kwa ajili ya safari yake kumganga na kumpoza majeruhi yule. Alimwinua na kumweka juu ya mnyama wake, na kuondoka naye kwa hatua za pole pole, ili kwamba mhanga asipate mtikisiko mkubwa, na hivyo kuzidisha maumivu yake. Alimleta katika nyumba ya wageni, na kumwangalia usiku mzima, akimtunza kwa upendo. Asubuhi, wakati yule mgonjwa alipokuwa amepata nafuu, Msamaria aliamua kuendelea na safari yake. Lakini kabla ya kufanya hivyo, alimweka mikononi mwa mwangalizi wa nyumba ya wageni, akalipia gharama, na akaacha amana nyingine kwa ajili ya matumizi ya mhanga yule; na akiwa kama vile hajaridhishwa na hayo, alitoa ahadi ya kugharimia mahitaji yoyote ya ziada, akimwambia yule mwenyeji wa nyumba kwamba, "Mtunze huyu, na chochote utakachogharimiwa zaidi, mimi nitakaporudi nitakulipa."

Kisa kiliishia hapo, Yesu akawa ameyakaza macho yake kwa yule mwanasheria, katika mtazamo ulioonekana kama wa kusoma moyo wake, na akasema, "Waonaje wewe, katika hao watatu, ni yupi aliyekuwa jirani yake yule aliyeangukia kati ya wanyang'anyi?" Luka 10:36.

Hata sasa, bado yule mwanasheria hakuweza kutamka neno Msamaria midomoni mwake, bali alijibu, "Ni huyo aliyemwonea huruma." Yesu akasema, "Enenda zako, nawe ukafanye vivyo hivyo."

Hivyo ndivyo ambavyo swali, "Jirani yangu ni nani?" linavyojibiwa daima. Kristo ameonyesha kwamba jirani yetu haina maana ya mtu aliye katika kanisa au imani tuliyo nayo. Ujirani hauhusishwi na uzuri wa kabila, rangi au kundi fulani. Jirani yetu ni kila mtu anayehitaji msaada wetu. Jirani yetu ni kila mtu ambaye amejeruhiwa na kuchubuliwa na yule adui. Jirani yetu ni kila mtu ambaye ni mali ya Mungu.

Katika kisa cha Msamaria mwema, Yesu alionyesha picha ya Yeye mwenyewe na kazi yake. Mwanadamu alikuwa amedanganywa, akachubuliwa, akanyang'anywa, na kuharibiwa na Shetani, na akaachwa aangamie; lakini Mwokozi akawa na huruma juu ya **(504)** hali yetu ya kutokuwa na msaada. Aliacha utukufu wake, akaja kutuokoa na hatari. Alitukuta tunakaribia kufa, akabeba shida yetu. Alituponya majeraha yetu. Alitufunika kwa kanzu yake ya kuhesabiwa haki. Alitufungulia mahali pa kukimbilia pa salama, na kutupatia nafasi katika mahali pakamilifu kwa gharama zake mwenyewe. Alikufa ili kutukomboa. Akielekeza kwa kielelezo cha Yeye mwenyewe, aliwaambia wafuasi wake, "Haya nawaamuru ninyi, mpate kupendana." "Kama vile nilivyowapenda ninyi, nanyi mpendane vivyo hivyo." Yohana 15:17; 13:34.

Swali la mwanasheria yule kwa Yesu lilikuwa ni, "Nifanye nini?" na Yesu, akitambua kwamba upendo kwa Mungu na kwa mwanadamu ndio ujumla wa haki yote, alikuwa amesema, "Fanya hivi nawe utaishi." Yule Msamaria alikuwa ametii misukumo ya moyo wake wenye wema na upendo, na katika hili alikuwa amejionyesha kuwa mtendaji wa sheria. Kristo alimwambia yule mwanasheria, "Enenda zako, nawe ufanye vivyo hivyo." Kutenda, na wala si kusema tu, ndiko kunakotarajiwa kuonekana kwa watoto wa Mungu. "Yeye asemaye ya kuwa anakaa ndani yake, imempasa kuenenda mwenyewe vile vile kama yeye alivyoenenda." 1 Yohana 2:6.

Somo hilo linatakiwa ulimwenguni leo kwa kiasi ambacho si kidogo kuliko wakati ule lilipotoka katika midomo ya Yesu. Ubinafsi na urasmi wa dini usio na wema ni kama vimeuzima moto wa upendo, na kuondosha huruma ambazo zingestawisha tabia. Wengi wanaolitaja jina lake wamepoteza hali ya kuona uhalisia kwamba Wakristo wanatakiwa kumwakilisha Kristo. Hata tujidai kwa maneno gani, sisi si Wakristo ikiwa hakutakuwa na kujikana nafsi kwa vitendo ili kuonyesha wema kwa watu wengine, katika mazingira ya familia, kwa majirani, kanisani, na mahali popote tunapokuwa.

Kristo ameunganisha matakwa yake na yale ya wanadamu, naye anatutaka tuwe kitu kimoja na Yeye katika kuwaokoa wanadamu. Anasema, "Mmepewa bure, toeni bure." Mathayo 10:8. Dhambi ni kuu mno kuliko uovu wote, na ni wajibu wetu kumhurumia na kumsaidia mwenye dhambi. Kuna watu wengi wanaofanya makosa, na ambao wanaihisi aibu yao na madhaifu yao. Wana njaa ya maneno ya kutia moyo. Wanayaangalia makosa na maanguko yao, mpaka kiasi ambacho wanasukumiwa karibu na hali ya kukosa tumaini. Tusizipuuze roho hizi.

Ikiwa sisi ni Wakristo, hatutapita pembeni na kuziacha, tukijiweka mbali na wale ambao wanahitaji sana msaada wetu. Tunapowaona wanadamu wakiwa katika shida, iwe katika mateso ya mwili au dhambi, kamwe tusiseme kwamba, Hili halinihusu mimi.

"Ninyi mlio wa Roho mrejezeni upya mtu kama huyo kwa roho ya upole." Wagalatia 6:1. Kwa imani na sala rudisheni nyuma nguvu za yule adui. Semeni maneno ya imani na kutia moyo ambayo yatakuwa kama mafuta yatibuyo kwa mtu aliyechubuliwa na kujeruhiwa. Watu wengi, wengi, wamezimia na kuvunjika moyo **(505)** katika mapambano ya maisha, wakati ambao neno moja la ukarimu na furaha lingeweza kuwatia moyo wakashinda. Kamwe tusimpite mtu anayeteseka bila kutafuta nafasi ya kumpatia faraja kwa kutumia faraja tuliyopewa na Mungu.

Yote haya ndiyo utimilifu wa msingi wa sheria, - msingi ule ulioelezwa katika kisa cha Msamaria mwema, na kudhihirishwa katika maisha ya Yesu. Tabia yake inafunua umuhimu wa kweli wa sheria, na inaonyesha kile ambacho ndiyo maana ya kumpenda jirani yetu kama tunavyojipenda wenyewe. Na pindi watoto wa Mungu wanapodhihirisha rehema, wema, na upendo kwa watu wote, hapo ndipo pia wanapoishuhudia tabia ya sheria ya mbinguni. Wanaonyesha ushuhuda kwamba "sheria ya Bwana ni kamilifu, huiburudisha nafsi." Zaburi 19:7. Na yeyote anayeshindwa kuonyesha upendo huu anaivunja sheria hiyo anayodai kwamba anaiheshimu. Maana roho ile tunayodhihirisha kwa ndugu zetu inatangaza roho tuliyo nayo kwa Mungu wetu. Upendo wa Mungu ulio moyoni ni chemchemi pekee ya upendo kwa jirani yetu. "Mtu akisema, Nampenda Mungu, naye anamchukia ndugu yake, ni mwongo; kwa maana asiyempenda ndugu yake ambaye amemwona, hawezi kumpenda Mungu ambaye hakumwona?" Wapendwa, "tukipendana, Mungu hukaa ndani yetu, na pendo lake limekamilika ndani yetu." 1 Yohana 4:20, 12.

## Sura ya 55

# Si kwa Mwonekano wa Nje

[Sura hii imejengwa katika Luka 17:20-22.]

Mafarisayo kadhaa walikuwa wamekuja kwa Yesu wakitaka kujua "ufalme wa Mungu utakuja lini." Miaka zaidi ya mitatu ilikuwa imepita tangu Yohana Mbatizaji alipotoa ujumbe ambao ulikuwa umeita kama mlio wa tarumbeta katika nchi ukisema, "Ufalme wa mbinguni umekaribia." Mathayo 3:2. Lakini Mafarisayo hao hawakuona dalili ya kuanzisha ufalme huo. Wengi wa wale waliomkataa Yohana, na katika kila hatua wakawa wamempinga Yesu, walikuwa wanadhihaki kwamba kazi yake imeshindwa.

Yesu alijibu, "Ufalme wa Mungu hauji kwa kuuchunguza; wala hawatasema, Tazama, upo huku, au, kule, kwa maana, tazama, ufalme wa Mungu umo ndani yenu." Ufalme wa Mungu huanzia moyoni. Mstafute hapa wala pale ili kuona udhihirisho wa mamlaka ya kidunia kuonyesha kuja kwa ufalme huo.

"Siku zitakuja," alisema huku akiwageukia wanafunzi wake, "mtakapotamani kuona siku moja katika siku zake Mwana wa Adamu, msiione." Mko katika hatari ya kushindwa kuona utukufu wa kazi yangu kwa sababu haiandamani na fahari ya ulimwengu. Hamwoni kwamba katikati yenu kuna upendeleo ulio mkuu kiasi gani kwa kuwa na Yeye ambaye ndiye uzima na nuru ya wanadamu, ingawa amefunikwa na ubinadamu. Siku zitakuja ambapo mtatazama nyuma kwa hamu ya kupata fursa mliyo nayo sasa ya kutembea na kuzungumza na Mwana wa Mungu.

Kwa sababu ya ubinafsi wao na kujali mambo ya dunia, hata wanafunzi wa Yesu **(507)** hawakuweza kuelewa utukufu wa kiroho ambao alitafuta kuwafunulia. Ni mpaka Yesu alipopaa kwenda kwa Baba yake, Roho Mtakatifu alipomwagwa kwa wanaoamini, ndipo wanafunzi walipoelewa kikamilifu tabia na kazi ya Mwokozi. Baada ya wao kupokea ubatizo wa Roho, walianza kungundua kwamba walikuwa wamekuwa mbele ya uwepo wa Bwana wa utukufu. Kadiri misemo ya Kristo ilivyoletwa katika kumbukumbu, akili zao zilifunguliwa na kuelewa unabii, na kuelewa miujiza aliyokuwa ameitenda. Maajabu ya maisha yake yalipita mbele yao, na wakawa kama watu ambao wameamshwa kutoka katika ndoto. Waligundua kwamba "Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu; nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba; amejaa neema na kweli." Yohana 1:14. Kristo alikuja kwa uhalisia kutoka kwa Mungu kuja katika ulimwengu wa dhambi ili kuwaokoa wana na binti za Adamu walioanguka. Sasa wanafunzi wale walijiona, machoni pao wenyewe, kama vile walikuwa na umuhimu kidogo sana kuliko kabla wakati walipokuwa hawajagundua hivyo. Kamwe hawakuchoka kufanyia mazoezi maneno na kazi za Yesu. Mafundisho yake, ambayo walikuwa wameelewa kwa uhafifu tu, sasa yaliwajia kama mafunuo maalum. Maandiko yalikuja kuwa kitabu kipya kwao.

Kadiri wanafunzi wale walivyotafuta unabii uliomshuhudia Kristo, waliletwa katika ushirika na Uungu, nao wakajifunza kuhusu Yeye aliyekuwa amepaa mbinguni kwenda kuikamilisha kazi aliyokuwa ameianza duniani. Walitambua uhalisia kwamba ndani yake yalikuwemo maarifa ambayo mwanadamu asingepambanukiwa bila kusaidiwa na nguvu ya kimbingu. Walihitaji msaada wa Yeye ambaye alitabiriwa na wafalme, manabii na wanadamu wenye haki. Kwa mshangao walisoma na kusoma tena ufafanuzi wa unabii kuhusu tabia na kazi yake. Uelewa wao wa kabla wa maandiko ya unabii ulikuwa hafifu kiasi gani! Walikuwa wamekuwa wazito kiasi gani kwa kuchelewa kuelewa ukweli mkuu unaomshuhudia Kristo! Wakimwangalia Yeye katika kujishusha kwake, kadiri alivyotembea kama mwanadamu miongoni mwa wanadamu, hawakuwa wameelewa fumbo la kufanyika kwake kuwa mwanadamu, hali yake ya namna mbili. Macho yao yalikuwa yamefumbwa, kiasi kwamba hawakugundua kikamilifu uungu ndani ya uanadamu. Lakini baada ya kuwa wameangaziwa na Roho Mtakatifu, ni jinsi gani walivyotamani kumwona tena, na kujiweka wenyewe miguuni pake! Ni namna gani walivyotamani kuja kwake, na kuwa naye akifafanua maandiko ambayo hawakuweza kupambanukiwa! Ni jinsi gani ambavyo wangesikiliza kwa umakini maneno yake! Kristo alikuwa na maana gani aliposema kwamba, "Bado nikali ninayo mengi ya kuwaambia, lakini hamwezi kuyastahimili hivi sasa"? Yohana 16:12. Walikuwa na hamu jinsi gani ya kuyajua yote! Walihuzunika kwamba imani ilikuwa **(508)** hafifu sana, kwamba mawazo yao yalikuwa yametanga mbali, kiasi kwamba walikuwa wameshindwa kiasi hicho kuuelewa uhalisia.

Mjumbe alikuwa ametumwa kutoka kwa Mungu kuja kuutangaza ujio wa Kristo, na kutoa wito wa kuamsha usikivu wa taifa la Wayahudi na ulimwengu wote kwa kazi yake, ili kwamba watu wajiandae kumpokea. Huyo mtu wa ajabu aliyetangazwa na Yohana alikuwa amekuwa miongoni mwao kwa miaka zaidi ya thelathini, lakini hawakuwa wamemfahamu kwamba ni Yeye aliyetumwa kutoka kwa Mungu. Hisia ya hatia iliwashika wanafunzi wale kwa sababu walikuwa wameiruhusu hali ya kutoamini iliyokuwepo ikachachusha mawazo yao na kutia wingu uelewa wao. Yeye aliye Nuru ya ulimwengu huu wenye giza alikuwa ameangaza katikati ya giza, lakini walikuwa wameshindwa kuelewa ilikotoka miale ya nuru ile. Walijiuliza kwamba ni kwa nini walikuwa wamefuata njia ambayo ilimlazimu Kristo kuwakemea. Mara nyingi walirudia-rudia mazungumzo yake, na kusema, Kwa nini tuliruhusu hali ya kujali mambo ya kidunia na kuruhusu upinzani uliofanywa na makuhani na marabi uvuruge fahamu zetu, hata hatukuelewa kwamba aliye mkuu kuliko Musa alikuwa katikati yetu, kwamba aliye na hekima kuliko Sulemani alikuwa anatufundisha? Masikio yetu yalikuwa mazito kiasi gani! Ufahamu wetu ulikuwa dhaifu jinsi gani!

Tomaso asingeamini mpaka alipoweka kidole chake katika jeraha liliofanywa na askari wa Kirumi. Petro alikuwa amemkana Kristo wakati wa kuaibishwa na kukataliwa kwake. Kumbukumbu hizi zenye uchungu ziliwajia zikiwa bayana. Walikuwa wamekuwa pamoja naye, lakini hawakuwa wamemjua wala kumtambua. Lakini ni jinsi gani mambo haya yalivyochochea mioyo yao pindi walipogundua kutokuamini kwao!

Kadiri makuhani na wakuu walivyoungana dhidi yao, na wakaletwa mbele ya mabaraza na kutupwa gerezani, wafuasi hao wa Kristo walishangilia "kwa sababu wamehesabiwa kuwa wamestahili kuaibishwa kwa ajili ya Jina hilo." Matendo 5:41. Walishangilia kuthibitisha, mbele ya wanadamu na malaika, kwamba walitambua utukufu wa Kristo, na walichagua kumfuata kwa gharama ya kupoteza vitu vyote.

Ndivyo ilivyo sasa kama ilivyokuwa mnamo siku za mitume, kwamba pasipo kuangaziwa na Roho wa kimbingu, mwanadamu hawezi kuona utukufu wa Kristo. Ukweli na kazi ya Mungu havitambuliwi na Ukristo unaopenda ulimwengu na kuafikiana nao. Wafuasi wa Bwana hawapatikani katika njia za anasa, heshima za dunia au maafikiano na ulimwengu. Wako juu kwa mbali sana, katika njia za masumbufu, kudhalilika, na upinzani, katika mstari wa mbele wa vita "juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho." Waefeso 6:12. Hata sasa, kama ilivyokuwa mnamo **(509)** siku za Kristo, wafuasi wake hao hawaeleweki vema na wanapingwa na kukandamizwa na makuhani na Mafarisayo wa wakati wao huu.

Ufalme wa Mungu hauji ukiwa na mwonekano wa nje. Injili ya neema ya Mungu, pamoja na kiini chake cha roho ya kujikana nafsi, haiwezi kamwe kuwa katika upatanifu na roho ya ulimwengu. Misingi hiyo miwili inapingana. "Mwanadamu wa tabia ya asili hayapokei mambo ya Roho wa Mungu; maana kwake huyo ni upuzi, wala hawezi kuyafahamu, kwa kuwa yatambulikana kwa jinsi ya rohoni." 1 Wakorintho 2:14.

Lakini leo katika ulimwengu wa kidini kuna watu wengi ambao, kadiri wanavyoamini, wanajitahidi kujenga ufalme wa Kristo kama mamlaka ya kidunia ya muda. Wanatamani kumfanya Bwana wetu kuwa mtawala wa falme za ulimwengu, mtawala wa majumba na kambi za kifalme, kumbi zake za kutunga sheria, mahali pake pa kuheshimika na masoko yake. Wanamtarajia atawale kwa kutumia sheria zilizotungwa, zinazosimamiwa na mamlaka za wanadamu. Kwa kuwa Kristo hayupo sasa katika mwonekano halisi, wao wenyewe watajifanya kukaimu mahali pake, kusimamia sheria za ufalme wake. Uanzishwaji wa ufalme kama huo ndio uliotamaniwa na Wayahudi mnamo siku za Kristo. Wangelimpokea Yesu, ikiwa angekuwa radhi kuanzisha utawala wa duniani, ili kusimamia kile walichochukulia kama sheria za Mungu, na kuwafanya wao kuwa wasimamizi wa mapenzi yake na watekelezaji wa mamlaka yake. Lakini Yeye alisema, "Ufalme wangu si wa ulimwengu huu." Yohana 18:36. Asingekubali kiti cha enzi cha dunia.

Serikali iliyokuwepo wakati wa maisha ya Yesu ilikuwa ya kidhalimu na ya kikandamizaji; kila upande kulikuwa na vilio vya unyanyasaji, - matumizi ya nguvu, ukosefu wa uvumilivu, na ukatili mkubwa. Lakini Mwokozi hakujaribu kufanya mageuzi yoyote ya kiraia. Hakushambulia manyanyaso ya kitaifa, wala hakuwashutumu adui wa taifa. Hakuingilia mamlaka au utawala wa wale walio madarakani. Yeye aliyekuwa kielelezo chetu alijiweka mbali na serikali za kidunia. Si kwa sababu hakujali shida ambazo watu walikuwa wakipata, bali ni kwa kuwa tiba ya matatizo hayo haikuwa ndani ya mwanadamu kwa hali ya kawaida na kupimwa kwa nje nje. Ili kuleta tija, lazima tiba imfikie mwanadamu mmoja mmoja, nayo lazima iwe yenye kuhuisha moyo.

Ufalme wa Kristo hauwekwi kwa njia ya maamuzi ya mahakama au mabaraza au mikutano ya bunge, wala si kwa kudhaminiwa na wakuu wa ulimwengu huu, bali kwa kupandikiza hali ya Kristo ndani ya mwanadamu kwa njia ya kazi ya Roho Mtakatifu. "Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake; waliozaliwa, si kwa damu, wala si kwa mapenzi ya mwili, wala si kwa mapenzi ya mtu, bali kwa Mungu." Yohana 1:12, 13. Hapa ndipo penye nguvu pekee ambayo **(510)** inaweza kufanya kazi ya kuiinua jamii ya wanadamu. Na kazi ya mwanadamu katika kukamilisha kazi hii ni kufundisha na kutenda neno la Mungu.

Paulo alipoanza huduma yake kule Korintho, mji ule mashuhuri, wenye utajiri, na uovu, uliochafuliwa na ukosefu wa uadilifu usiotamkika wa upagani, alisema, "Naliazimu nisijue neno lolote kwenu ila Yesu Kristo, naye amesulibiwa." 1 Wakorintho 2:2. Akiandika baadaye kwa baadhi ya wale waliokuwa wamechafuliwa na dhambi chafu mno, aliweza kusema hivi, "Lakini mlioshwa, lakini mlitakaswa, lakini mlihesabiwa haki katika jina la Bwana Yesu Kristo, na katika Roho wa Mungu wetu." "Namshukuru Mungu sikuzote kwa ajili yenu, kwa sababu ya neema ya Mungu mliyopewa katika Kristo Yesu." 1 Wakorintho 6:11; 1:4.

Sasa, kama ilivyokuwa wakati wa Kristo, kazi ya ufalme wa Mungu haiko kwa watu wanaotaka kutambuliwa na kusaidiwa na watawala wa kidunia na sheria za wanadamu, bali kwa watu wale wanaowatangazia watu katika jina la Kristo zile kweli za kiroho zitakazofanya kazi ya kuleta ndani ya mtu anayezipokea uzoefu kama wa Paulo kwamba: "Nimesulibiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu." Wagalatia 2:20. Halafu watafanya kazi kama Paulo alivyofanya kwa manufaa ya watu. Alisema, "Basi tu wajumbe kwa ajili ya Kristo, kana kwamba Mungu anasihi kwa vinywa vyetu; twawaomba ninyi kwa ajili ya Kristo mpatanishwe na Mungu." 2 Wakorintho 5:20.

# Sura ya 56

## Kuwabariki Watoto

[Sura hii imejengwa katika Mathayo 19:13-15; Marko 10:13-16; Luka 18:15-17.]

Daima Yesu alikuwa mwenye kuwapenda watoto. Alikubali huruma yao ya kitoto na upendo wao wa wazi usioathiriwa. Sifa zao za shukrani zilizotoka katika vinywa vyao vilivyo safi zilikuwa muziki mtamu katika masikio yake, na ziliburudisha roho yake wakati alipokabiliwa na watu walio wajanja na wenye unafiki. Kila mahali ambapo Mwokozi alienda, unyoofu wa mwonekano wake, na unyenyekevu wake, mwonekano wa wema ulivuta upendo na ujasiri wa watoto.

Ilikuwa ni desturi miongoni mwa Wayahudi kwa watoto kuletwa kwa rabi fulani, ili ya kwamba apate kunyosha mikono yake juu yao kwa kuwabariki; lakini wanafunzi wa Mwokozi walifikiri kwamba kazi yake ilikuwa ya muhimu sana kiasi kwamba haikupaswa kuingiliwa kwa njia hii. Wakati wamama walipomjia wakiwa na watoto wao wadogo, wanafunzi wake waliwaangalia kwa kutopendezwa. Walifikiri kwamba watoto hawa ni wadogo mno kiasi kwamba hawawezi kufaidi kitu kwa kumjia Yesu, na wakahitimisha kwamba Yesu asingefurahishwa na uwepo wao. Lakini wanafunzi wale ndio ambao Yesu hakufurahishwa nao. Mwokozi alielewa utunzaji na mzigo wa wamama waliokuwa wakitafuta kuwafundisha watoto wao kulingana na neno la Mungu. Alikuwa amesikia maombi yao. Yeye mwenyewe ndiye aliyekuwa amewavuta kuja kwake.

Mama mmoja akiwa na mtoto wake alikuwa ameondoka nyumbani kwake kwenda kwa Yesu. Akiwa njiani alimweleza jirani yake kuhusu lengo la safari yake, na jirani yule akatamani Yesu ambariki mtoto wake pia. Kwa namna hiyo wamama kadhaa walikuja wakiwa pamoja, wakiwa na watoto wao. Baadhi ya watoto walikuwa wamevuka miaka ya **(512)** uchanga kwenda katika hatua ya watoto wakubwa na vijana. Wale wamama walipotambulisha kusudi lao, Yesu alisikia kwa huruma habari hizo za ombi lao la machozi. Lakini alisubiri aone jinsi wanafunzi watakavyowatendea. Alipowaona wakiwafukuza wamama wale, wakidhani wanamfanyia wema, aliwaonyesha makosa yao, akisema, "Waacheni watoto wadogo waje kwangu; wala msiwazuie; kwa maana walio mfano wa hao, ufalme wa mbinguni ni wao." Aliwachukua watoto mikononi mwake, akanyosha mikono yake juu yao, naye akawapatia baraka walizojia.

Wale wamama walifarijika. Walirudi majumbani mwao wakiwa wametiwa nguvu na kubarikiwa na maneno ya Kristo. Walikuwa wametiwa moyo ili kubeba mzigo wao wakiwa na hamasa mpya, na kuwatumikia watoto wao kwa matumaini. Wamama wa leo wanatakiwa kupokea maneno yake kwa imani kama ile. Hakika Kristo ni Mwokozi wa mtu leo kama alivyokuwa akiishi kama mwanadamu miongoni mwa wanadamu. Hakika Yeye ni msaada wa wamama leo kama alivyokuwa wakati ule alipowakusanya watoto mikononi mwake kule Uyahudi. Watoto walio majumbani mwetu wamenunuliwa kwa damu yake kama walivyokuwa wale watoto wa zamani zilizopita.

Yesu anajua mzigo wa moyo wa kila mama. Yeye aliyekuwa na mama ambaye alihangaika kupambana na umaskini na ukosefu wa mahitaji muhimu anaonyesha huruma kwa kila mama aliye katika kazi. Yeye aliyesafiri umbali mrefu kwenda kuupatia ahueni moyo wa mwanamke Mkananayo atafanya mengi pia kwa wamama wa leo. Yeye aliyemrejeshea mjane wa Naini mwanaye wa pekee, na ambaye hata katika mateso yake msalabani alimkumbuka mama yake, anaguswa na huzuni za mama leo. Katika kila huzuni na uhitaji atatoa faraja na msaada.

Waacheni akina mama waje kwa Yesu pamoja na shida zao. Watapata rehema inayotosha kuwasaidia kuwasimamia watoto wao. Malango yako wazi kwa kila mama anayetaka kuweka mizigo yake miguuni pa Mwokozi. Yeye aliyesema, "Waacheni watoto wadogo waje kwangu, wala msiwazuie," bado anawaalika wamama kuwaongoza watoto wadogo kwenda kwake kubarikiwa naye. Hata mtoto aliye katika mikono ya mama anaweza kuwa chini ya kivuli cha Mwenyezi kwa njia ya imani ya mama aombaye. Yohana Mbatizaji alijazwa Roho Mtakatifu tangu kuzaliwa kwake. Ikiwa tutaishi kwa kushiriki pamoja na Mungu, sisi pia tunaweza kutarajia kuwajenga watoto wetu wadogo, hata tangu nyakati zao za mapema.

Katika wale watoto walioletwa kukutana naye, Kristo aliona wanaume na wanawake watakaokuwa warithi wa neema yake na raia wa ufalme wake, na baadhi ambao wangekuwa wafia dini kwa ajili yake. **(515)** Alijua kwamba watoto hawa wangemsikiliza na kumkubali kama Mwokozi wao kwa utayari mkubwa mno kuliko wale walio watu wazima, amabao wengi wao walikuwa wenye hekima wa kidunia na wenye mioyo migumu. Katika kufundisha kwake alishuka chini mpaka akawa sawa na wao. Yeye, Mkuu wa mbinguni, hakuacha kujali kujibu maswali yao, na kurahisisha masomo yake ili kukidhi hali yao ya uelewa wa kitoto. Alipandikiza akilini mwao mbegu za ukweli, ambazo katika miaka ya baadaye zingestawi, na kuzaa matunda kwa uzima wa milele.

Bado kuna ukweli kwamba watoto ndio wenye uwezekano mkubwa wa kupokea mafundisho ya injili; mioyo yao i wazi kwa ajili ya ushawishi wa kimbingu, na ina nguvu ya kuhifadhi mafundisho yanayopokelewa. Watoto wadogo wanaweza kuwa Wakristo, wakiwa na uzoefu unaolingana na miaka yao. Wanahitaji kuelemishwa katika mambo ya kiroho, na wazazi wanatakiwa kuwapatia kila fursa, ili kwamba wajenge tabia inayofuata kielelezo cha tabia ya Kristo.

Wababa na wamama na wawaangalie watoto wao kama washirika walio watoto katika familia ya Bwana, ambao wamekabidhiwa kwao ili wawaelimishe kwa ajili ya mbingu. Masomo ambayo sisi wenyewe tunajifunza kwa Kristo yanatakiwa yatolewe na sisi kwa watoto, kwa namna ambavyo akili yao changa inaweza kuyapokea, kidogo kidogo yakifungua uzuri wa kanuni za mbinguni. Kwa njia hiyo nyumba ya Mkristo inakuwa shule, mahali ambapo wazazi wanatumika kama walimu wadogo, huku Kristo mwenyewe akiwa ndiye mfundishaji mkuu.

Katika kufanya kazi kwa ajili ya wongofu wa watoto wetu, hatutakiwi kutafuta msukumo wa kulazimisha kama ushahidi wa kusadikisha dhidi ya dhambi. Wala siyo muhimu sana kujua muda hasa watoto wanapoongoka. Tunatakiwa tuwafundishe kuzileta dhambi zao kwa Yesu, wakiomba msamaha wake, na wakiamini kwamba anawasamehe na kuwapokea kama alivyowapokea wale watoto wakati alipokuwa duniani katika mwili.

Kadiri mama anavyowafundisha watoto wake kumtii yeye kwa sababu wanampenda, anawafundisha masomo ya mwanzo katika maisha ya Ukristo. Upendo wa mama unawakilisha kwa mtoto upendo wa Kristo, na watoto wadogo wanaomtumaini na kumtii mama yao wanajifunza kumtumaini na kumtii Mwokozi.

Yesu alikuwa kielelezo cha watoto, na pia alikuwa kielelezo cha wababa. Alinena kama mtu mwenye mamlaka, na neno lake lilikuwa na nguvu; lakini bado katika mahusiano yote pamoja na watu wakaidi na wakorofi hakuonyesha hali yoyote isiyo ya wema. Neema ya Kristo moyoni itaweka akilini wema na uadilifu utokao mbinguni. Italainisha hali yoyote ya ukali, na kushusha kila hali iliyo ngumu-ngumu na isiyo na wema. Itawaongoza wababa na wamama kushughulika na watoto wao kwa kuwachukulia kama viumbe wenye akili, vile vile ambavyo wao wenyewe wangependa kutendewa.

**(516)** Wazazi, katika kuwafundisha watoto wenu, jifunzeni masomo ambayo yametolewa na Mungu katika vitu vya asili. Ikiwa ungetaka kukuza mmea wa waridi ungefanyaje? Mwulize mtunza bustani kwamba ni namna gani anavyolifanya kila tawi na jani kustawi kwa uzuri, na kulifanya kuwa sawia na lenye kupendeza. Atakwambia kwamba kazi hiyo haikufanywa kwa kushika-shika pasipo umakini, wala kufanya juhudi za fujo; maana ikiwa hivyo angeuvunja mmea. Ilikuwa ni kwa uangalifu, tena wa kurudiwa-rudiwa. Aliutia maji udongo, akailinda mimea ikuayo isipigwe na upepo uvumao sana na jua liunguzalo, naye Mungu akaifanya kustawi na kuwa katika hali ya kupendeza. Katika kushughulika na watoto wenu, fuateni njia ya mtunza bustani. Kwa kugusa kwa upole, kwa kuhudumia kwa upendo, tafuteni kuendeleza tabia zao kwa kufuata mfano wa tabia ya Kristo.

Hamasisheni hali ya kuonyesha upendo kwa Mungu na miongoni mwa wao kwa wao. Jambo linalosababisha kuwepo ulimwenguni kwa wanaume na wanawake wengi wenye mioyo migumu ni kwamba upendo wa kweli umechukuliwa kwamba ni udhaifu, nao unawekewa vikwazo na kukataliwa. Hali nzuri zaidi ya watu hawa iliharibiwa wakati wa utoto wao; na ikiwa ubinafsi wao hautayeyushwa na nuru ya upendo wa mbingu, furaha yao itaharibiwa milele. Ikiwa tunataka watoto wetu wawe na roho ya upendo ya Yesu, na huruma ile inayoonyeshwa na malaika kwa ajili yetu, lazima tuhamasishe hisia za ukarimu na upendo wakati wa utoto.

Wafundisheni watoto namna ya kumwona Kristo katika vitu vya asili. Wapeleke mahali pa wazi, chini ya miti mizuri, bustanini; na katika uumbaji wote wa ajabu wafundishe kuona udhihirisho wa upendo wake. Wafundishe kwamba Mungu alifanya sheria zinazoongoza viumbe hai vyote, kwamba amefanya sheria kwa ajili yetu, na ya

kwamba sheria hizi ni kwa ajili ya furaha na raha yetu. Msiwachoshe **(517)** kwa maombi na sala ndefu zinazochosha, bali kwa kutumia masomo ya vielelezo vya viumbe vya asili wafundisheni kuitii sheria ya Mungu.

Mnapowafanya watoto wawe na imani na ninyi kadiri wanavyokuwa wafuasi wa Kristo, itakuwa rahisi kuwafundisha kuhusu upendo mkuu ambao kwa huo ametupenda. Kadiri mnavyojaribu kuziweka wazi kweli za wokovu, na kuwaelekeza watoto kwa Kristo kama Mwokozi wao binafsi, malaika watakuwa karibu yenu. Bwana atawapatia wababa na wamama neema ili kuwafanya watoto wao wadogo kuvutiwa na kisa cha Mtoto wa Bethlehemu, ambaye ndiye hasa tumaini la ulimwengu.

Wakati Yesu alipowaambia wanafunzi wake wasiwazuie watoto kuja kwake, alikuwa anawaambia wafuasi wake katika zama zote – aliwaambia maofisa wa kanisa, wahudumu, wasaidizi, na Wakristo wote. Yesu anawavuta kwake watoto, naye anatuhimiza akisema, Waacheni waje kwangu; kama vile angetaka kusema kwamba, Watakuja ikiwa hamwazuii.

Hebu tabia yenu isiyo ya Kikristo isimwakilishe Yesu vibaya. Msiwapeleke watoto wenu mbali na Yeye kwa kutojali kwenu au ukali wenu. Kamwe msiwape sababu ya kufikiri kwamba mbingu haitakuwa mahali pazuri kwao ikiwa mtakuwepo kule. Msiiseme dini kama kitu ambacho watoto hawawezi kuelewa, au mkatenda jambo fulani linaloonyesha kwamba wao hawatarajiwi kumpokea Kristo wakati wa utoto wao. Msiwape mawazo ya uongo kwamba dini ya Kristo ni dini ya huzuni, na kwamba katika kumjia Mwokozi ni lazima waachane na vitu vyote vinavyoyafanya maisha kuwa ya raha.

Kadiri Roho Mtakatifu anavyosukuma mioyo ya watoto, shirikianeni na kazi yake. Wafundisheni kwamba Mwokozi anawaita, kwamba hakuna kitu kinachoweza kumpa furaha kubwa zaidi ya pale wao wanapojitoa kwake mnamo miaka yao ya mapema na utotoni.

Mwokozi anazijali sana kwa upendo usio na kikomo roho alizozinunua kwa damu yake mwenyewe. Wao ndio madai ya upendo wake. Anawaangalia kwa hamu isiyotamkika. Moyo wake unavutwa, si tu kwa mtoto mwenye tabia njema sana, bali hata kwa wale ambao kwa njia ya kurithi wana mapungufu katika tabia. Wazazi wengi hawaelewi ni kiasi gani wanahusika katika sifa hizi za tabia za watoto wao. Hawana upendo na hekima ya namna ya kushughulika na waliopotoka ambao wamekuwa hivyo kwa sababu yao. Lakini Yesu anawatazama watoto hawa kwa shauku. Anafuatilia tangu kisababishi hadi matokeo.

Mfanyakazi aliye Mkristo aweza kuwa wakala wa Kristo katika kuwavuta watoto hawa kwenda kwa Mwokozi. Kwa hekima na uwezo anaweza kuwaunganisha na moyo wake, mtu huyo anaweza kuwapa uvumilifu na tumaini, ili kwamba kuwaruhusu kuingia katika ufalme wa Mungu

# Sura ya 57

## "Umepungukiwa na Neno Moja"

[Sura hii imejengwa katika Mathayo 19:16-22; Marko 10:17-22; Luka 18:18-23.]

“Hata alipokuwa akitoka kwenda njiani, mtu mmoja akaja mbio, akampigia magoti, akamwuliza, Mwalimu mwema, nifanye nini nipate kuurithi uzima wa milele?”

Huyo kijana aliyeuliza swali hilo alikuwa mtawala. Alikuwa na mali nyingi, na alikuwa na cheo. Aliona upendo ambao Kristo alionyesha kwa watoto walioletwa kwake; aliona jinsi alivyowapokea kwa upendo, na kuwabeba mikononi mwake, na moyo wake ukawaka kwa sababu ya upendo wa Mwokozi. Alihisi hamu ya kuwa mwanafunzi wake. Alikuwa amesukumwa kiasi kwamba wakati Kristo alipokuwa anatembea njiani, alimkimbilia, naye akipiga magoti miguuni pake, aliuliza kwa moyo wa dhati swali lililo muhimu kwa roho yake na roho ya kila mwanadamu kwamba, "Mwalimu mwema, nifanye nini nipate kuurithi uzima wa milele?"

"Kwa nini kuniita mwema?" Kristo alisema, "hakuna aliye mwema ila mmoja, ndiye Mungu." Yesu alitaka kujaribu udhati wa yule mtawala, na kuona mtazamo wake uliomfanya kumwona mwema. Je, aliona uhalisia kwamba Yeye aliyekuwa anazungumza naye ni Mwana wa Mungu? Hisia yake halisi ya moyo ilikuwa ipi?

Mtawala huyu alikuwa amejikadiria kiwango cha juu cha kujihesabia haki. Hakudhani kabisa kwamba angekuwa na mapungufu katika jambo lolote, lakini hata hivyo hakuridhika moja kwa moja. Alihisi kupungukiwa na kitu ambacho hakuwa nacho. Je, Yesu asingeweza kumbariki kama alivyowabariki watoto wadogo, na hivyo kujazia mapungufu ya nafsi yake?

Katika kujibu swali hili Yesu alimwambia kwamba utii kwa amri za Mungu lilikuwa jambo muhimu ikiwa alitaka kuupata uzima wa milele; na alinukuu baadhi ya amri zinazoonyesha wajibu wa mwanadamu kwa **(519)** wanadamu wenzake. Jibu la mtawala yule lilikuwa chanya: “Haya yote nimeyashika tangu utoto wangu: nimepungukiwa na nini tena?"

Kristo aliuangalia uso wa yule kijana, kama vile akisoma maisha yake na kupeleleza tabia yake. Alimpenda, na alikuwa na hamu ya kumpa ile amani na neema na raha ambavyo vingebadili tabia yake. Akasema, "Umepungukiwa na neno moja. Enenda, ukauze ulivyo navyo vyote, uwape maskini, nawe utakuwa na hazina mbinguni; kisha njoo unifuate."

Kristo alivutiwa na kijana huyu. Alimjua kwamba anasema kwa dhati kwamba, "Haya yote nimeyashika tangu utoto wangu." Mkombozi alitaka kuweka ndani ya kijana huyu utambuzi ambao ungemwezesha kuona umuhimu wa kujitoa moyo na wema wa Kikristo. Alitafuta kuona ndani yake moyo wa unyenyekevu na wa toba, utambuzi wa upendo wa hali ya juu unaotakiwa kuonyeshwa kwa Mungu, na hitaji la kuficha mapungufu yake ndani ya ukamilifu wa Kristo.

Yesu aliona ndani ya mtawala yule uwezekano wa kupata msaada ule aliokuwa anatafuta ikiwa angeshirikiana naye katika kazi ya wokovu. Ikiwa angejiweka chini ya uongozi wa Kristo, angekuwa nyenzo kwa ajili ya jambo jema. Yule mtawala angemwakilisha Kristo kwa kiwango kikubwa, ambacho, ikiwa angeunganiaka na Mwokozi, kingemwezesha kuwa nguvu ya kimbingu katikati ya wanadamu. Kwa kuona tabia yake, Kristo alimpenda. Upendo kwa Kristo ulikuwa unawaka ndani ya moyo wa yule mtawala; maana upendo huzaa upendo. Yesu alitamani kumwona kama mtenda-kazi pamoja naye. Alitamani kumfanya kuwa kama Yeye, kioo ambacho ndani yake kufanana na Mungu kungeakisiwa. Alitamani kuendeleza uzuri wa tabia yake, na kuitakasa kwa ajili ya kutumiwa na Bwana. Ikiwa mtawala angejitoa kwa Kristo, angekuwa amestawi katika mazingira ya uwepo wake. Ikiwa angefanya uchaguzi huu, wakati wake ujao ungekuwa tofauti kiasi gani!

"Umepungukiwa na neno moja," Yesu alisema. "Ukitaka kuwa mkamilifu, enenda ukauze ulivyo navyo, uwape maskini, nawe utakuwa na hazina mbinguni; kisha njoo unifuate." Kristo aliusoma moyo wa yule mtawala. Alipungukiwa kitu kimoja tu, lakini kilikuwa ni kanuni muhimu sana. Alihitaji upendo wa Mungu moyoni. Upungufu huu, usipojazwa, ungemletea maangamizi; hali yake yote ingechafuliwa. Tabia ya kujifurahisha nafsi

ingesabisha kuimarika kwa ubinafsi. Ili kuweza kupokea upendo wa Mungu, lazima hali yake ya kujipenda binafsi isalimishwe.

Kristo alimpatia mtu huyu jaribio. Alimtaka achague kati ya hazina ya mbinguni na ukuu wa ulimwenguni. Alihakikishiwa hazina ya mbinguni ikiwa angemfuata Kristo. Lakini lazima umimi usalimishwe; lazima matakwa yake yawekwe chini ya udhibiti wa Kristo. Utakatifu wenyewe wa Mungu **(520)** ulitolewa kwa yule kijana mtawala. Alikuwa na fursa ya kuwa mwana wa Mungu, na mrithi pamoja na Kristo katika hazina ya mbinguni. Lakini lazima aubebe msalaba, na kumfuata Mwokozi katika njia ya kujikana nafsi.

Hakika maneno ya Kristo yalikuwa mwaliko kwa yule mtawala kwamba, "Chagueni hivi leo mtakayemtumikia." Yoshua 24:15. Uchaguzi uliachwa kwake. Yesu alikuwa anatamani wongofu wa kijana huyu. Alikuwa amemwonyesha doa la pigo lililo katika tabia yake, na kwa hiyo alisubiri kwa hamu ya kina kiasi gani kadiri yule kijana alivyoendelea kupima uzito wa swali lile! Ikiwa aliamua kumfuata Kristo, lazima atii maneno yake katika kila jambo. Lazima aachane na mipango ya miradi yake aliyoipenda. Mwokozi alimtazama yule kijana kwa subira ya dhati na moyo wenye hamu kiasi gani, akitumaini kwamba angejisalimisha katika mwaliko huo wa Roho wa Mungu!

Kristo aliweka masharti yale tu ambayo yangemweka mtawala yule mahali ambapo pangefaa kabisa kuwa na tabia ya Kikristo. Maneno yake yalikuwa ya hekima, japokuwa yanaweza kuonekana makali na yasiyopinda. Tumaini pekee la wokovu kwa mtawala yule lilikuwa katika kuyakubali na kuyatii. Cheo chake cha juu na mali zake vilikuwa vinakandamiza upande mwingine na kuleta kazi ya uovu katika tabia yake. Ikiwa vitu hivyo vingeendelea kushikiliwa vingekuwa na ushawishi wa juu katika tabia yake kuliko ule wa Mungu. Kitendo cha kubakiza kidogo au kingi mbali na Mungu kingekuwa ni kubakiza kitu ambacho kingepunguza nguvu yake ya uadilifu na tija; maana ikiwa vitu vya dunia hii vimeendekezwa, hata viwe havina uhakika au thamani kiasi gani, vitammeza mtu.

Yule mtawala alikuwa mwepesi wa kutambua vitu vyote vilivyoambatishwa katika maneno ya Kristo, naye akawa na huzuni. Ikiwa angetambua thamani ya zawadi iliyokuwa imetolewa, angejisajili haraka sana kuwa mmoja wa wafuasi wa Kristo. Alikuwa mjumbe wa baraza lililoheshimiwa la Wayahudi, na Shetani alikuwa anamjaribu kwa matarajio ya fahari ya siku za usoni. Alihitaji hazina ya mbinguni, lakini pia alihitaji manufaa ya kidunia ambayo angeyapata katika utajiri wake. Aliumia kwa sababu ya kuwepo kwa masharti hayo; alitamani uzima wa milele, lakini hakuwa tayari kutoa kafara. Bei ya uzima wa milele ilionekana kuwa kubwa sana, na akaenda zake kwa huzuni; "kwa sababu alikuwa na mali nyingi."

Madai yake kwamba alikuwa ameishika sheria ya Mungu yalikuwa ni udanganyifu. Alionyesha kwamba utajiri ulikuwa ndio miungu yake. Asingeweza kuzishika amri za Mungu wakati ulimwengu ndio uliokuwa wa kwanza katika matakwa yake. Alipenda zawadi zilizotolewa na Mungu kuliko alivyompenda Mtoaji. Kristo alikuwa amemzawadia kijana yule nafasi ya kushiriki naye. Alisema, "Unifuate." Lakini Mwokozi hakuwa kitu kikubwa kwake kama lilivyokuwa jina lake katikati ya watu au kama ilivyokuwa mali yake. Kuacha hazina yake ya duniani, ile iliyokuwa inaonekana, kwa ajili ya hazina ya mbinguni, ile iliyokuwa haionekani, kulionekana kama hatari kubwa mno. Alikataa zawadi ya uzima wa milele, na akaenda zake, na daima baada ya pale ulimwengu ungepokea ibada yake.

**(523)** Maelfu ya watu wanapita katika jaribu hilo gumu, wakipima kati ya uzito wa Kristo na wa ulimwengu; na wengi huchagua ulimwengu. Kama alivyokuwa yule mtawala kijana, wanageuka wakiondoka kwa Mwokozi, wakisema mioyoni mwao kwamba, Mtu huyu hawezi kuwa kiongozi wangu.

Namna ile Kristo alivyoshughulika na kijana yule imetolewa kama somo hai la kielelezo. Mungu ametupatia kanuni ya mwenendo ambayo inatakiwa kufuatwa na kila mtumishi wake. Nayo ni utii wa sheria, siyo utii kama wa kisheria-sheria, bali utii unaoingia maishani, na kudhihirishwa katika tabia. Mungu ameweka kiwango chake cha tabia kwa ajili ya wote wanaotaka kuwa raia wa ufalme wake. Wale tu watakaokuwa watenda-kazi pamoja na Kristo, wale tu watakaosema kwamba, Bwana, vyote nilivyo navyo na vyote nilivyo mimi ni vyako, ndio watakaokubaliwa kuwa wana na binti za Mungu. Watu wote wanatakiwa kupima maana ya mtu kuitamani mbingu, lakini bado akarudi na kuondoka zake kwa sababu ya masharti yaliyowekwa. Fikiria ina maana gani kumwambia Kristo "Hapana." Yule mtawala alisema, Hapana, siwezi kukupatia vyote. Je, tunasema vile vile?

Mwokozi anatupatia zawadi ya kushiriki pamoja nasi katika kazi ambayo Mungu ametupatia sisi ili tuifanye. Anatupatia zawadi ya kutumia mali ambazo Mungu ametupatia, kuendeleza kazi yake ulimwenguni. Anaweza kutuokoa kwa njia hii tu.

Mali zile za mtawala zilikabidhiwa kwake ili adhihirishe kuwa wakili mwaminifu; alitakiwa agawe mali hizi ili kuwabariki waliokuwa wahitaji. Vivyo hivyo sasa Mungu anawakabidhi wanadamu mali, pamoja na talanta na fursa, ili kwamba wapate kuwa nyenzo zake katika kuwasaidia maskini na wenye shida. Yeye atumiaye zawadi hizo alizokabidhiwa kama Mungu alivyopanga anakuwa mtenda-kazi pamoja na Mwokozi. Anaongoa roho kwa Kristo, maana ni mwakilishi wa tabia ya Kristo.

Kwa wale ambao, kama yule mtawala kijana, wako katika vyeo vya juu vya kutumainiwa na wanazo mali nyingi, kutoa vyote na kumfuata Kristo inaweza kuonekana kuwa kafara kubwa sana. Lakini hiyo ndiyo kanuni ya mwenendo kwa ajili ya wote wanaotaka kuwa wafuasi wake. Hakuna jambo lolote linalopungukiwa na utii ambalo linaweza kukubaliwa. Kujisalimisha binafsi ndilo jambo ambalo ni kiini cha mafundisho ya Kristo. Mara nyingi linasemwa na kuunganishwa likiwa katika lugha ya kimamlaka, kwa sababu hakuna njia nyingine ya kumwokoa mwanadamu zaidi ya kukatilia mbali vitu vile ambavyo, ikiwa vitaendekezwa, vitaharibu uadilifu wote wa mtu.

Wafuasi wa Kristo wanapomrudishia Bwana kilicho chake, wanakuwa wanakusanya hazina ambayo watapewa wakati watakaposikia maneno, "Vema, mtumwa mwema na mwaminifu; . . . ingia katika furaha ya bwana wako." "Ambaye kwa ajili ya furaha iliyowekwa mbele yake aliustahimili msalaba na kuidharau aibu, naye ameketi mkono wa kuume wa kiti cha enzi cha Mungu." Mathayo 25:23; Waebrania 12:2. Furaha ya kuona roho zilizokombolewa, roho ambazo zimeokolewa milele, ndiyo thawabu ya wote wanaokanyaga miguu yao katika nyayo za Yeye aliyesema, "Unifuate."

# Sura ya 58

## "Lazaro, Njoo Huku Nje"

[Sura hii imejengwa katika Luka 10:38-42; Yohana 11:1-44.]

Miongoni mwa wanafunzi wa Kristo waliokuwa imara alikuwemo Lazaro wa Bethania. Tangu walipokutana kwa mara ya kwanza imani yake katika Kristo ilikuwa na nguvu; upendo wake kwa Kristo ulikuwa wa kina, na alikuwa anapendwa na Mwokozi sana. Mwujiza mkuu kuliko yote iliyofanywa na Kristo ulifanywa kwa ajili ya Lazaro. Mwokozi aliwabariki wote waliotafuta msaada wake; anapenda jamii yote ya wanadamu, lakini kwa baadhi amefungamanishwa na mahusiano maalum ya ukaribu. Moyo wake ulikuwa umeunganishwa sana na familia hiyo ya Bethania kwa kifungo cha upendo, na kwa ajili ya mmoja wa hao kazi yake ya ajabu mno ilifanyika.

Pale nyumbani kwa Lazaro, Yesu alikuwa amepata mahali pa kupumzikia. Mwokozi hakuwa na nyumbani kwake mwenyewe; alikuwa tegemezi wa ukarimu wa rafiki zake na wanafunzi wake, na mara kwa mara, alipokuwa amechoka, akiwa na kiu ya kujumuika na wanadamu, alikuwa akifurahia kukimbilia katika nyumba hii tulivu, mahali palipo mbali na kufuatiliwa na Mafarisayo waliokuwa na wivu. Alipata ukaribisho wa dhati mahali hapa na kupata urafiki safi na wenye utakatifu. Hapa ndipo alipoweza kusema kwa wepesi na uhuru kamili, akijua kwamba maneno yake yangeeleweka na kuhifadhiwa.

Mwokozi wetu alifurahia nyumba tulivu na wasikilizaji wenye usikivu. Alitafuta wema, upole, na upendo. Wale waliopokea mafundisho ya kimbingu ambayo alikuwa tayari kila wakati kuyatoa walibarikiwa sana. Kadiri makutano walivyomfuata Kristo kupita katika **(525)** maeneo ya wazi, aliwafunulia uzuri wa ulimwengu wa asili. Alitafuta kufungua macho ya fahamu zao, ili ya kwamba wapate kuona mkono wa Mungu unavyoushikilia ulimwengu. Ili kuvuta ukubali wa watu kuhusu wema na ukarimu wa Mungu, aliwaelekeza wasikilizaji wake kwa umande ushukao taratibu, manyunyu laini ya mvua na nuru angavu ya jua, vikitolewa kwa wema na waovu kwa namna inayofanana. Alitaka watu watambue kwa ukamilifu zaidi namna Mungu anavyojali wanafamu aliowaumba. Lakini makutano wale walikuwa wazito wa kusikia, na katika nyumba ya Bethania Kristo alipata kupumzika kutokana na kazi ya kuchosha ya kupambana na maisha ya huduma za hadhara. Hapa ndipo alipoifunulia hadhira kitabu cha Mweza wa yote. Katika mahojiano haya ya faragha aliwafunulia wasikilizaji wake kile ambacho hakudiriki kuwaambia makutano waliochanganyika. Hakuhitaji kuwaambia rafiki zake kwa mifano.

Kristo alipotoa masomo yake ya kustaajabisha, Mariamu alikaa miguuni pake, akiwa msikilizaji mwenye heshima na aliyejitoa. Katika tukio moja, Martha, akiwa anahangaika na kazi za kuandaa chakula, alimwendea Kristo, akisema, "Bwana, huoni vibaya hivyo ndugu yangu alivyoniacha nitumike peke yangu? Basi mwambie anisaidie." Hii ilikuwa mara ya kwanza kwa Kristo kutembelea Bethania. Mwokozi na wanafunzi wake walikuwa ndio tu wamefanya safari yao ya kuchosha kwa mguu kutokea Yeriko. Martha alikuwa na hamu ya kuwahudumia, na katika masumbufu yake alisahau hata upole unaostahili kuonyeshwa kwa Mgeni. Yesu alimjibu kwa maneno ya upole na subira, "Martha, Martha, unasumbuka na kufadhaika kwa ajili ya vitu vingi; lakini kinatakiwa kitu kimoja tu; na Mariamu amelichagua fungu lililo jema, ambalo hataondolewa." Mariamu alikuwa anahifadhi katika akili yake maneno ya thamani yaliyokuwa yakishuka kutoka midomoni mwa Mwokozi, maneno yaliyokuwa na thamani zaidi kuliko lulu ya thamani sana ya duniani.

Kile "kitu kimoja tu" ambacho kilitakiwa kwa Martha kilikuwa ni moyo wa utulivu na kujitoa, mahangaiko ya kina kwa ajili ya kujua mambo yajayo, yaani maisha ya kutokufa, na neema zilizo muhimu kwa ajili ya kukua kiroho. Alihitaji kupunguza hali ya kusumbuka kwa ajili ya vitu vinavyopita, na kuongeza hali ya kusumbuka kwa ajili ya vitu vinavyodumu milele. Yesu angewafundisha watoto wake kutumia kila fursa ya kupata ule ufahamu utakaowafanya kuwa na hekima kwa ajili ya wokovu. Kazi ya Kristo inahitaji watenda-kazi makini na wenye nguvu. Upo uwanja mkubwa wa kazi kwa ajili ya kina Martha, pamoja na bidii yao katika kazi za kidini. Lakini hebu kwanza wakae pamoja na Mariamu miguuni pa Yesu. Hebu juhudi, uwajibikaji, na nguvu vitakaswe na neema ya Kristo; hapo ndipo maisha yatakuwa ni nguvu ya wema usiowezekana kushindwa.

Huzuni iliingia katika nyumba hiyo ya amani mahali ambapo Yesu alikuwa akipumzikia. Lazaro alishikwa na ugonjwa wa ghafla, na dada zake wakatuma ujumbe kwa Mwokozi, **(526)** wakisema, "Bwana, yeye umpendaye hawezi." Waliiona nguvu ya ugonjwa uliokuwa umemshika kaka yao, lakini walijua kwamba Kristo alikuwa ameonyesha uwezo wa kuponya namna zote za magonjwa. Waliamini kwamba angewaonea huruma katika shida yao; kwa hiyo hawakumhimiza kuwepo haraka, bali walimpelekea ujumbe wa imani kwamba, "Yeye umpendaye hawezi." Walidhani kwamba angeitikia haraka, na kuwa nao mara tu afikapo Bethania.

Walisubiri kwa hamu neno kutoka kwa Yesu. Kwa muda wote ambao uhai ulikuwa bado ndani ya kaka yao, waliomba na kusubiri Yesu aje. Lakini mjumbe aliyetumwa hakurudi na Yesu. Bali alileta ujumbe kwamba, "Ugonjwa huu si wa mauti," nao wakashikilia tumaini hilo kwamba Lazaro angeishi. Kwa upendo walijaribu kusema maneno ya kutia moyo na tumaini kwa mgonjwa yule aliyekuwa karibu ya kupoteza fahamu. Lazaro alipokufa walifadhaika sana kwa uchungu; lakini walifikiria kuhusu neema ya Kristo iwezeshayo, na hili liliwafanya wasifikirie malaumu yoyote kwa Mwokozi.

Kristo aliposikia ule ujumbe, wanafunzi wake walifikiri kwamba hakuupokea inavyostahili. Hakudhihirisha huzuni ambayo walitarajia kwamba angeonyesha. Akiwa anawatazama, alisema hivi, "Ugonjwa huu si wa mauti, bali ni kwa ajili ya utukufu wa Mungu, ili Mwana wa Mungu atukuzwe kwa huo." Kwa muda wa siku mbili alisalia pale pale alipokuwa. Kukawia huku kulikuwa ni fumbo kwa wanafunzi wale. Walifikiri kwamba, Kuwepo kwake katika nyumba ile yenye shida kungekuwa ni faraja jinsi gani! Upendo wake mkubwa kwa familia ile ya Bethania ulikuwa unajulikana vema kwa wanafunzi wale, na walishangazwa kwamba hakuitikia ule ujumbe uliosema, "Yeye umpendaye hawezi."

Kwa zile siku mbili Kristo alionekana kama vile amepuuza ule ujumbe; maana hakusema lolote kuhusu Lazaro. Wale wanafunzi walifikiria kuhusu Yohana Mbatizaji, mtangulizi wa Yesu. Walikuwa wameshangaa kwamba ni kwa nini Yesu, mwenye uwezo wa kufanya miujiza ya ajabu, alikuwa ameruhusu Yohana atelekezwe gerezani, na kufa kifo cha kikatili. Akiwa na uwezo kama huo, kwa nini Kristo hakuokoa maisha ya Yohana? Mafarisayo walikuwa wameuliza mara kwa mara swali hili, ambao walilionyesha kama hoja isiyopingika dhidi ya madai ya Kristo kuwa ni Mwana wa Mungu. Mwokozi alikuwa amewaonya wanafunzi wake kuhusu majaribu, kupata hasara, na mateso. Je, angewaacha wakati wa majaribu? Baadhi walihoji kama huenda wameikosea kazi yake. Wote walifadhaika sana.

Baada ya kusubiri kwa siku mbili, Yesu aliwaambia wale wanafunzi, "Twendeni Uyahudi tena." Wale wanafunzi walihoji ni kwa nini Yesu alikuwa amesubiri kwa siku mbili ikiwa alikuwa aende Uyahudi. Lakini wasiwasi kwa ajili ya Yesu na wao wenyewe **(527)** ulikuwa umefikia kiwango cha juu mawazoni mwao. Hawakuona kitu kingine katika mwelekeo aliokuwa nao isipokuwa hatari. Wakasema, "Rabi, juzijuzi tu Wayahudi walikuwa wakitafuta kukupiga kwa mawe, nawe unakwenda huko tena? Yesu akajibu, Je! Saa za mchana si kumi na mbili?" Niko chini ya uongozi wa Baba yangu; maadam nafanya mapenzi yake, maisha yangu yako salama. Saa zangu kumi na mbili za mchana hazijaisha. Nimeingia katika sehemu ya mwisho ya siku yangu; lakini kwa kuwa sehemu yoyote ya muda huo bado ipo, niko salama.

Aliendelea hivi, "Mtu akienda mchana hajikwai; kwa sababu aiona nuru ya ulimwengu huu." Yeye afanyaye mapenzi ya Mungu, atembeaye katika njia ambayo imeonyeshwa na Mungu, hawezi kujikwaa na kuanguka. Nuru ya roho wa Mungu aongozaye humpatia uelewa mzuri wa wajibu wake, nayo humwongoza kwa usahihi mpaka mwisho wa kazi ya mtu huyo. "Bali akienda usiku hujikwaa; kwa sababu nuru haimo ndani yake." Yeye atembeaye katika njia aliyojichagulia mwenyewe, mahali ambapo Mungu hakumwita kuwa, atajikwaa. Kwake yeye mchana unageuka kuwa usiku, na popote awapo, hayuko salama.

"Aliyasema hayo; kisha, baada ya hayo, akawaambia, Rafiki yetu, Lazaro, amelala; lakini ninakwenda nipate kumwamsha." "Rafiki yetu, Lazaro, amelala." Maneno haya yanagusa jinsi gani! Yamejaa huruma jinsi gani! Kwa mawazo yao kuhusu hatari ambayo Bwana wao alikuwa anaelekea kukutana nayo alipokuwa akielekea Yerusalemu, wanafunzi wale walikuwa wameshasahau habari za familia iliyopotelewa na mpendwa wao kule Bethania. Lakini kwa Kristo haikuwa hivyo. Wale wanafunzi walijihisi kuhukumiwa. Walikuwa wamefadhaika kwa sababu Kristo hakuitikia ule ujumbe kwa haraka. Walikuwa wamejaribiwa kufikiri kwamba hakuwa na upendo wa dhati kwa Lazaro na dada zake kwa kiasi kile walichodhani kwamba anawapenda, la sivyo angekuwa alifanya haraka kwenda na yule mjumbe aliyetumwa. Lakini maneno haya kwamba, "Rafiki yetu, Lazaro,

amelala," yaliamsha hisia sahihi mawazoni mwao. Walishawishika kwamba Kristo hakuwa amewasahau rafiki zake wale waliokuwa katika shida.

"Basi wale wanafunzi wakamwambia, Bwana, ikiwa amelala, atapona. Lakini Yesu alikuwa amenena habari ya mauti yake; nao walidhania ya kuwa ananena habari ya kulala usingizi." Kristo huonyesha kifo cha watoto wake wanaoamini kwa kukiwakilisha na kusinzia. Maisha yao yanafichwa na Kristo ndani ya Mungu, na wale wanaokufa watalala mle ndani yake mpaka parapanda ya mwisho itakapolia.

"Basi hapo Yesu akawaambia waziwazi, Lazaro amekufa. Nami nafurahi kwa ajili yenu kwamba sikuwako huko, ili mpate kuamini; lakini na twendeni kwake." Tomaso hakuona jambo jingine isipokuwa kifo kilichokuwa kinamsubiri Bwana wake ikiwa alikuwa anaenda Uyahudi; lakini aliikaza roho yake, na kuwaambia wanafunzi wenzake, "Twendeni na sisi, ili tufe pamoja naye." Aliijua chuki ya Wayahudi kwa Kristo. Tangu kabla ya hapo lengo lao lilikuwa **(528)** ni kukamilisha kifo chake, lakini lengo hili halikuwa limefanikiwa, kwa sababu sehemu ya muda wake aliopangiwa ulikuwa haujaisha. Mnamo wakati huu Yesu alilindwa na malaika wa mbinguni, na hata katika maeneo ya Uyahudi, mahali ambapo marabi walikuwa wanapanga njama za namna watakavyomkamata na kumwua, hakuna dhara ambalo lingempata.

Wale wanafunzi waliduwazwa na maneno ya Kristo wakati aliposema, "Lazaro amekufa. Nami nafurahi . . . kwamba sikuwako huko." Je, Mwokozi alichagua kwa makusudi kuiacha nyumba ya rafiki zake wenye shida. Ilionekana kama vile Mariamu na Martha na Lazaro aliyekuwa anakufa walikuwa wameachwa peke yao. Lakini hawakuwa peke yao. Kristo alitazama tukio lote, na baada ya kufa kwa Lazaro wale waliofiwa walishikiliwa na neema yake. Yesu alishuhudia huzuni ya mioyo yao iliyoraruka, wakati kaka yao alipokuwa akipambana na adui yule mwenye nguvu, yaani kifo. Aliihisi kila hisia ya maumivu, alipowaambia wanafunzi wake kwamba, "Lazaro amekufa." Lakini si kule Bethania tu ambako Kristo alikuwa na wapendwa wa kuwafikiria; alikuwa na kazi pia ya kuwafundisha wanafunzi wake. Walitarajiwa kuwa wawakilishi wake kwa ulimwengu, ili ya kwamba mbaraka kutoka kwa Baba uwafikie wote. Kwa manufaa yao aliruhusu kwamba Lazaro afe. Ikiwa angemponya kutoka katika ugonjwa ule, mwujiza ambao ndio uthibitisho mkubwa mno wa tabia yake ya kiungu usingepata kufanyika.

Ikiwa Kristo angelikuwa katika chumba cha mgonjwa, Lazaro asingelikufa; maana Shetani asingekuwa na nguvu juu yake. Kifo kisingeweza kulenga mshale wake kwa Lazaro mbele ya uwepo wa Mpaji wa uzima. Kwa hiyo Kristo alibaki mbali. Alimwacha adui atekeleze mamlaka yake, ili ya kwamba apate kumfukuzia mbali, adui aliyeshindwa. Aliruhusu kwamba Lazaro apite chini ya nguvu ya kifo; na wale wadada wenye majonzi walimwona kaka yao akilazwa kaburini. Kristo alijua kwamba kadiri ambavyo wangeutazama uso wa kaka yao aliyekufa imani yao kwa Mkombozi ingejaribiwa kwa hali ya juu sana. Lakini alijua kwamba kwa sababu ya pambano walilokuwa wanalipitia kwa sasa imani yao ya baadaye ingeangaza kwa nguvu kubwa zaidi sana. Aliruhusu kila mchomo wa huzuni waliostahimili. Si kwamba aliwapenda kidogo kwa kule kukawia; bali alijua kwamba kwa ajili yao, kwa ajili ya Lazaro, kwa ajili yake, na kwa ajili ya wanafunzi wake, ushindi ulikuwa unaenda kupatikana.

"Kwa ajili yenu," "ili mpate kuamini." Kwa wote wanaotoka na kwenda kuhisi uongozi wa mkono wa Mungu, wakati wa mfadhaiko mkubwa zaidi ndio muda ambapo msaada wa kimbingu u karibu zaidi. Watageuka nyuma na kuitazama kwa shukrani kubwa sehemu yenye giza kubwa zaidi katika njia yao. "Bwana ajua kuwaokoa watauwa," 2 Petro 2:9. Kutokana na kila jaribu na kishawishi atawaleta mbele wakiwa na imani imara zaidi na uzoefu mkubwa zaidi.

**(529)** Kwa kule kukawia kwake kuja huku kwa Lazaro, Kristo alikuwa na kusudi jema kwa wale ambao hawakuwa wamempokea. Alikawia, ili kwamba kwa kumfufua Lazaro awapatie wale watu wenye mioyo migumu na wasioamini uthibitisho mwingine kwamba Yeye alikuwa kweli ni “huo ufufuo, na uzima." Hakupenda kupoteza tumaini lote la watu, maskini, na kondoo watangatangao wa nyumba ya Israeli. Moyo wake ulikuwa unavunjika kwa sababu ya kutokutubu kwao. Kwa huruma yake alikusudia kuwapatia uthibitisho mwingine zaidi kwamba alikuwa Mponyaji, Yeye pekee ambaye angeweza kuleta uzima na kutokufa katika uhalisia wake. Huu ulikuwa uwe uthibitisho ambao makuhani wasingeweza kuutafsiri isivyo sahihi. Hii ndiyo iliyokuwa sababu ya kukawia kwenda Bethania. Mwujiza huu unaofunika miujiza yote, yaani kufufuliwa kwa Lazaro, ulikuwa wa kugonga muhuri wa Mungu kwenye kazi yake na kwenye madai yake ya uungu.

Katika safari yake ya kwenda Bethania, Yesu, kama ilivyokuwa kawaida yake, aliwahudumia wagonjwa na wenye mahitaji. Alipofika mjini alituma ujumbe kwa wale wadada kuhusu habari za kuja kwake. Kristo hakuingia katika nyumba ile mara, bali alibaki mahali pa utulivu huko kando ya njia. Maadhimisho makubwa ya maonyesho ya nje yaliyofanywa na Wayahudi pindi marafiki au ndugu walipokufa yalikuwa hayapatani na mtazamo wa Kristo. Alisikia sauti kubwa za maombolezo zilizofanywa na waombolezaji waliokodiwa, na kwa hiyo hakutaka kukutana na wale wadada katika hali hiyo ya fujo. Miongoni mwa marafiki waliokuwa wanaomboleza walikuwemo ndugu wa familia ile, baadhi yao wakiwa na vyeo vya juu mle Yerusalemu. Miongoni mwa hao walikuwemo baadhi ambao walikuwa adui wakubwa sana wa Kristo. Kristo alijua makusudi yao, na kwa hiyo hakutaka ajulikane haraka.

Ule ujumbe ulifikishwa kwa Martha kimya kimya kiasi kwamba watu wengine waliokuwa katika chumba kile hawakusikia. Mariamu, akiwa amemezwa katika majonzi, hakusikia maneno yale. Martha aliinuka haraka na kwenda kumlaki Bwana wake, lakini Mariamu alibaki katika huzuni zake pasipo kupiga kelele, akidhani kwamba Martha alikuwa ameenda mahali Lazaro alipozikwa.

Martha aliharakisha kwenda kukutana na Yesu, moyo wake ukiwa unasukumwa na hisia zinazopingana. Katika mwonekano wa sura ya Yesu aliona wema na upendo ule ule ambao ulikuwepo wakati wote. Imani ya Martha kwake ilikuwa isiyovunjika, lakini alifikiria kuhusu kaka yake mpendwa, ambaye pia alikuwa amependwa na Yesu. Akibanwa na majonzi moyoni mwake kwa sababu Kristo hakuwa amekuja kabla, lakini akiwa na matumaini kwamba hata sasa angeweza kufanya jambo fulani la kuwafariji, alisema, "Bwana, kama ungalikuwapo hapa, ndugu yangu hangalikufa." Mara tena na tena, hata katikati ya kelele zilizokuwa zinafanywa na waombolezaji, wadada wale waliyarudiarudia maneno hayo.

Akiwa na huruma ya kibinadamu na ya kimungu Yesu aliuangalia uso wa Martha wenye majonzi na uchovu. **(530)** Martha hakuwa na mwelekeo wa kuhesabu yaliyopita; yote yalionyeshwa katika maneno ya huzuni kwamba, "Bwana, kama ungalikuwapo hapa, ndugu yangu hangalikufa." Lakini kadiri alivyouangalia ule uso wa Yesu wa upendo, aliongeza kusema, "Lakini hata sasa najua ya kuwa yoyote utakayomwomba Mungu, Mungu atakupa."

Yesu alimtia moyo imani yake, kwa kusema, "Ndugu yako atafufuka." Jibu lake hili halikukusudiwa kuleta tumaini la badiliko la muda mfupi. Aliyapeleka mawazo ya Martha mbali sana kupita ufufuo wa kaka yake wakati huo, na kuyafikisha kwenye ufufuo wa wenye haki. Yesu alifanya haya ili kwamba katika kufufuliwa kwa Lazaro Martha aione ahadi ya kufufuliwa kwa wenye haki wote waliokufa, na uhakika ya kwamba itakamilishwa kwa uweza wa Mwokozi.

Martha akajibu, akasema, "Najua ya kuwa atafufuka katika ufufuo siku ya mwisho."

Akiwa bado anatafuta kuweka uelekeo wa kweli katika imani ya Martha, Yesu alisema wazi, "Mimi ndimi huo ufufuo, na uzima." Katika Kristo kuna uzima, uzima halisi, ambao si wa kuazimwa, ambao si wa kutengeneza. "Yeye aliye naye Mwana, anao huo uzima." 1 Yohana 5:12. Uungu wa Kristo ni uthibitisho wa uzima wa milele kwa anayeamini. Yesu alisema, "Yeye aniaminiye mimi, ajapokufa, atakuwa anaishi; naye kila aishiye na kuniamini hatakufa kabisa hata milele. Je! Unayasadiki hayo?" Hapa Kristo anatazama wakati ule wa kuja kwake mara ya pili. Hapo ndipo wenye haki waliokufa watakapofufuliwa wakiwa katika hali ya kutoharibika, na wenye haki walio hai watabadilishwa na kwenda mbinguni bila kuona mauti. Mwujiza ambao Kristo alitaka kuufanya, kwa kumfufua Lazaro, ungewakilisha ufufuo wa wenye haki wote waliokufa. Kwa maneno na matendo yake alijitangaza kuwa Yeye ndiye Mamlaka ya ufufuo. Yeye ambaye mwenyewe angekufa msalabani muda si mrefu alikuwa na funguo za mauti, akiwa mshindi wa kaburi, na alikuwa na haki na nguvu ya kuwapa watu uzima wa milele.

Martha alijibu maneno ya Mwokozi yasemayo, "Je! Unayasadiki haya?" kwa kusema, "Naam, Bwana, mimi nimesadiki ya kwamba wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu, yule ajaye ulimwenguni." Hakupambanukiwa maana ya maneno yote yaliyotamkwa na Kristo, lakini aliikiri imani yake katika uungu wake, na imani yake kwamba alikuwa na uwezo wa kufanya lolote lililompendeza kufanya.

"Naye alipokwisha kusema hayo, alikwenda zake; akamwita umbu lake Mariamu faraghani, akisema, Mwalimu yupo anakuita." Aliufikisha ujumbe wake kimya kimya kwa kadiri ilivyowezekana; maana makuhani na wakuu

walikuwa wamejiandaa kumtia nguvuni Yesu wakati wowote ambapo fursa ingewaruhusu kufanya hivyo. Vilio vya waombolezaji vilizuia maneno yake kusikika.

**(533)** Aliposikia ujumbe huo, Mariamu aliinuka haraka, akaondoka katika chumba akiwa mwenye uso wenye hamu. Waombolezaji walimfuata wakidhani kwamba ameenda mahali pa kaburi kuomboleza. Alipofika mahali alipokuwa Yesu alipiga magoti miguuni pake, akasema kwa midomo yenye kwikwi ya kulia, "Bwana, kama ungalikuwapo hapa, ndugu yangu hangalikufa." Vilio vya waombolezaji vilikuwa vikimtia uchungu; maana alitamani kupata mazungumzo mafupi ya utulivu pamoja na Yesu. Lakini alijua chuki na wivu dhidi ya Kristo vilivyokuwa mioyoni mwa baadhi ya waliokuwepo, na alikuwa amezuiliwa kuonyesha majonzi yake kikamilifu.

"Basi Yesu alipomwona analia, na wale Wayahudi waliofuatana naye wanalia, aliugua rohoni, akafadhaika roho yake." Alisoma mioyo ya wote walikuwa wamekusanyika pale. Aliona kwamba kwa wengi, kile kilichoonekana kama mwonekano wa majonzi kilikuwa ni uigizaji. Alijua kwamba baadhi ya wale waliokuwa katika mkusanyiko ule, ambao walikuwa wakionyesha huzuni za unafiki, muda si mrefu wangekuwa wakipanga kuhusu kifo, si cha mtenda miujiza mkuu tu, bali pia yeye ambaye angefufuliwa kutoka katika wafu. Kristo angeweza kuwavua vazi lao la kujifanya wenye huzuni. Lakini alihifadhi hasira yake ya haki. Maneno ambayo angeyasema katika ukweli wote, hakuyasema, kwa sababu ya mpendwa aliyekuwa amepiga magoti miguuni pake akiwa na huzuni, ambaye alimwamini kweli kweli.

Yesu aliuliza, "Mmemweka wapi? Wakamwambia, Bwana, njoo utazame." Walielekea kwa pamoja mahali penye kaburi. Lilikuwa tukio la kuhuzunisha. Lazaro alikuwa mtu wa kupendwa sana, na dada zake walimwombolezea kwa mioyo iliyovunjika, huku wale waliokuwa rafiki zake wakichanganya kilio chao na cha wale dada zake. Katika mwonekano huu wa majonzi ya wanadamu, na hali halisi kwamba marafiki waliofiwa walimwombolezea aliyekufa wakati Mwokozi huyu wa ulimwengu akiwa amesimama hapo hapo, - "Yesu akalia machozi." Ingawa alikuwa Mwana wa Mungu, bado alikuwa amechukua hali ya mwanadamu juu yake, naye alisukumwa na huzuni ya kibinadamu. Daima moyo wake wa huruma na upendo huamshwa na mateso ya watesekao. Analia pamoja na waliao, na kufurahi pamoja na wanaofurahi.

Lakini si tu kwamba alilia kwa sababu ya huruma yake ya kibinadamu aliyomhurumia Mariamu na Martha. Katika machozi yake kulikuwa na huzuni iliyo juu mno kuliko huzuni ya kibinadamu kama vile mbingu zilivyo juu sana kuliko dunia. Kristo hakulia kwa ajili ya Lazaro; maana alikuwa anataka kumwita atoke kaburini. Alilia kwa sababu wengi wa wale ambao walikuwa wanamlilia Lazaro sasa muda si mrefu wangepanga kutekeleza kifo chake Yeye aliyekuwa ufufuo na uzima. Lakini ni jinsi gani ambavyo Wayahudi wasioamini hawakuwa na uwezo wa kutafsiri kwa usahihi maana ya machozi yake! Baadhi, ambao **(534)** hawakuweza kuona kitu kingine ambacho kilikuwa sababu ya huzuni yake zaidi ya mwonekano ule wa nje wa tukio lililokuwa mbele yake pale, walisema kimya kimya kwamba, "Angalieni jinsi alivyompenda!" Wengine, wakitafuta kudondoshea mbegu ya kutokuamini katika mioyo ya wale waliokuwepo pale, walisema kwa dhihaka, "Je! Huyu aliyemfumbua macho yule kipofu, hakuweza kumfanya na huyu asife?" Ikiwa kumponya Lazaro kulikuwa ndani ya uwezo wa Kristo, kwa nini basi alimwacha akafa?

Kwa kutumia jicho la kinabii Kristo aliona uadui wa Mafarisayo na Masadukayo. Alijua kwamba walikuwa wanapanga kuhusu kifo chake. Alijua kwamba baadhi ya hao ambao wanaonekana sasa kama wana huruma muda si mrefu wangejifungia mlango wa matumaini na malango ya jiji la Mungu. Tukio moja lilikuwa litokee, la kuteswa na kusulibiwa kwake, ambalo lingesababisha uharibifu wa Yerusalemu, na wakati huo hakuna ambaye angeomboleza kwa ajili ya waliokufa. Taabu iliyokuwa inakuja juu ya Yerusalemu ilionyeshwa wazi mbele yake. Aliuona Yerusalemu ukiwa umezungukwa na majeshi ya Kirumi. Alijua kwamba wengi wa wale waliokuwa wakimwombolezea Lazaro sasa wangekufa pindi mji ule utakapohusuriwa, na kifo chao kisingekuwa na matumaini.

Kristo hakulia kwa sababu ya mandhari iliyokuwa mbele yake tu. Uzito wa huzuni ya vizazi na vizazi ilikuwa juu yake. Aliona madhara ya kutisha ya uasi wa sheria ya Mungu. Aliona kwamba katika historia ya ulimwengu, kuanzia kwa kifo cha Habili, pambano kati ya wema na uovu limekuwa lisilokoma. Akiangalia mbele katika miaka ya usoni, aliona mateso na huzuni, machozi na mauti, ambayo ndiyo yangekuwa hatima ya watu. Moyo wake ulichomwa na uchungu wa jamaa ya wanadamu wa vizazi vyote na nchi zote. Ole za wanadamu wenye dhambi zilikuwa nzito nafsini mwake, na chemchemi ya machozi ikafumka kadiri alivyotafuta kutuliza shida zao hizo.

"Basi Yesu, hali akiugua tena nafsini mwake, akafika kwenye kaburi." Lazaro alikuwa amelazwa katika pango lililo mwambani, na jiwe kubwa sana lilikuwa limewekwa mahali pa kuingilia. "Liondoeni jiwe," Kristo alisema. Akidhani kwamba alitaka tu kumwangalia yeye aliyekufa, Martha alizuia, akisema kwamba mwili ule ulikuwa umezikwa kwa siku nne, kwa hiyo uharibikaji ulikuwa umeanza kazi yake. Kauli hii, iliyotolewa kabla ya kufufuliwa kwa Lazaro, haikuacha nafasi kwa ajili ya maadui wa Kristo kusema kwamba udanganyifu ulikuwa umefanyika. Siku za nyuma Mafarisayo walikuwa wamesambaza kauli za uongo kuhusu maajabu yale makubwa ya udhihirisho wa nguvu za Mungu. Wakati Kristo alipomfufua binti wa Yairo, alikuwa amesema kwamba, "Kijana hakufa, bali amelala tu." Marko 5:39. Kwa kuwa alikuwa ameugua **(535)** kwa muda mfupi tu, na alifufuliwa mara tu baada ya kufa, Mafarisayo walitangaza kwamba yule mtoto hakuwa amekufa; kwamba Kristo mwenyewe alikuwa amesema kwamba alikuwa amelala tu. Walikuwa wamejaribu kufanya ionekane kwamba Kristo hakuwa na uwezo wa kuponya magonjwa, kwamba kulikuwa na mchezo wa udanganyifu katika miujiza yake. Lakini katika tukio hili, hakuna ambaye angekana kwamba Lazaro alikuwa amekufa.

Bwana anapotaka kufanya kazi, Shetani humsukuma mtu fulani kuzuia. "Liondoeni jiwe," Yesu alisema. Kwa kiasi kiwezekanacho, itengenezeni njia kwa ajili ya kazi yangu. Lakini tabia chanya na ya wema ya Martha ilijionyesha. Hakupenda kwamba mwili unaooza uwekwe wazi. Moyo wa mwanadamu ni mzito kuelewa maneno ya Kristo, na imani ya Martha ilikuwa haijaelewa maana ya kweli ya ahadi ya Kristo.

Kristo alimkanya Martha, lakini maneno yake yalitamkwa kwa namna ya upole wa hali ya juu. "Mimi sikukuambia ya kwamba ukiamini utauona utukufu wa Mungu?" Kwa nini uwe na mashaka kuhusu uwezo wangu? Kwa nini unawaza kinyume na matakwa yangu? Una neno langu. Ikiwa utaamini, utauona utukufu wa Mungu. Mambo yasiyowezekani kwa asili hayawezi kuzuia kazi yake Yeye aliye Mweza wa yote. Mashaka na kutoamini si unyenyekevu. Imani ya dhati katika neno la Kristo ndio unyenyekevu wa kweli, kujisalimisha kwa kweli.

"Liondoeni jiwe." Kristo angeweza kuliamuru jiwe litoke, nalo lingeitii sauti yake. Angeweza kuwaagiza malaika ambao walikuwa karibu naye pale kando ili wafanye kazi hiyo. Kwa kuagiza kwake kule, hata mkono usioonekana ungeliondoa lile jiwe. Lakini lilitakiwa liondolewe na mikono ya mwanadamu. Kwa njia hiyo Kristo alitaka kuonyesha kwamba uanadamu unatakiwa kushirikiana na uungu. Nguvu ya uungu haiagizwi kutenda kile ambacho nguvu ya kibinadamu inaweza kukifanya. Mungu hamgawii mwanadamu mahitaji. Yeye anamtia nguvu mwanadamu, na kushirikiana naye wakati anapotumia nguvu na uwezo aliopewa.

Amri ile ikatiiwa. Jiwe likavingirishiwa mbali. Kila kitu kikafanywa wazi wazi na bayana. Wote wakapewa wasaa wa kuona kwamba hakuna udanganyifu unaofanywa. Ndani ya kaburi lile la mwambani umelala mwili wa Lazaro, ukiwa wa baridi na kimya katika mauti. Vilio vya waombolezaji vinanyamazishwa. Wakiwa katika mshangao na hamu, watu waliokusanyika wanalizunguka kaburi, wakisubiri kuona kitu ambacho kingefuata.

Kwa utulivu Kristo anasimama mbele ya kaburi. Utulivu mtakatifu unakuwepo pale. Kristo anasogea karibu zaidi ya kaburi. Huku akiinua macho yake kuelekea mbinguni, anasema, "Baba, nakushukuru kwa kuwa umenisikia." Si muda mrefu kabla ya tukio hili, maadui wa Kristo walikuwa wamemshutumu kwa kukufuru, na walikuwa wameokota mawe ili kumpiga kwa sababu alidai kuwa ni Mwana wa **(536)** Mungu. Walimshutumu kwamba anafanya miujiza kwa nguvu za Shetani. Lakini hapa Kristo anadai kwamba Mungu ni Baba yake, na kwa ujasiri kamili anatangaza kwamba Yeye ni Mwana wa Mungu.

Katika yote aliyofanya, Kristo alikuwa anashirikiana na Baba yake. Daima alikuwa mwangalifu kudhihirisha kwamba hakufanya kazi kwa kujitegemea; alifanya miujiza kwa imani na sala. Kristo alitaka wote wajue uhusiano wake na Baba yake. Alisema, "Baba, nakushukuru kwa kuwa umenisikia. Nami nalijua ya kuwa wewe wanisikia sikuzote; lakini kwa ajili ya mkutano huu wanaohudhuria nalisema haya, ili wapate kusadiki kwamba ndiwe uliyenituma." Hapa wanafunzi na watu wengine walikuwa wanapewa uthibitisho wa kutosha kuhusu uhusiano uliopo kati ya Kristo na Mungu. Walikuwa waonyeshwe kwamba madai ya Kristo hayakuwa ya udanganyifu.

"Naye akiisha kusema hayo, akalia kwa sauti kuu, Lazaro, njoo huku nje." Sauti yake, iliyo wazi na ya kupenya, ilipenya katika sikio la aliyekufa. Wakati anapoongea, uungu unamlika ndani ya ubinadamu. Usoni mwake, ambapo pameangaziwa na utukufu wa Mungu, watu wanaona uthibitisho wa uweza wake. Kila jicho linakazwa

kwenye mlango wa kaburi. Kila sikio linategwa kusikiliza sauti itokayo pale. Wote wakiwa na hamu kubwa na uchungu wanasubiri kuona mtihani wa uungu wa Kristo, ushahidi ambao utathibitisha madai yake kuwa ni Mwana wa Mungu, la sivyo kuzima matumaini milele.

Kuna hali ya kujongea katika kaburi lililo na ukimya, na yeye aliyekuwa amekufa anasimama mlangoni pa kaburi. Kujongea kwake kunaathiriwa na mavazi ya kaburini ambayo alizikwa nayo, na Kristo anawaambia watazamaji waliokuwa wanashangaa, "Mfungueni, mkamwache aende zake." Kwa mara nyingine tena wanaonyeshwa kwamba mwanadamu atendaye kazi anatakiwa kushirikiana na Mungu. Mwanadamu anatakiwa atende kwa ajili ya mwanadamu. Lazaro anawekwa huru, na anasimama mbele ya umati ule, akiwa si kama mtu ambaye amedhoofishwa na ugonjwa, na mwenye miguu inayoweweseka kwa udhaifu, bali kama mtu aliye katika hatua ya ujana, na kama mwanaume mwenye nguvu. Macho yake yanang'aa kwa ufahamu na upendo kwa Mwokozi wake. Anajitupa kwa heshima miguuni pa Yesu.

Wale watazamaji wako kimya kwanza wakiwa wameduwaa. Halafu zinafuata shangwe na maneno ya shukrani. Wale wadada wanampokea tena kaka yao maishani kama zawadi kutoka kwa Mungu, na kwa machozi ya furaha wanaonyesha furaha zao kwa Mwokozi. Lakini wakati kaka, madada, na marafiki wanashangilia katika hali hii ya kuonana tena, Yesu anajiondoa katika mandhari ile. Wanapomtafuta huyu Mpaji wa uzima, haonekani popote.

## Sura ya 59

# Njama za Makuhani

[Sura hii imejengwa katika Yohana 11:47-54.]

Bethania ilikuwa karibu na Yerusalemu kiasi kwamba habari za kufufuliwa kwa Lazaro muda si mrefu zilipelekwa katika mji huo. Kwa njia ya wapelelezi waliokuwa wameshuhudia mwujiza ule wakuu wa Wayahudi walizipata habari kwa haraka. Kikao cha Sanhedrin kiliitishwa haraka ili kuamua nini kifanyike. Sasa Kristo alikuwa amedhihirisha kikamilifu uwezo wake juu ya mauti na kaburi. Mwujiza ule wa uweza mkubwa ulikuwa ni wa ushahidi mkubwa uliotolewa na Mungu kwa wanadamu ukionyesha kwamba alikuwa amemtuma Mwana wake ulimwenguni kwa ajili ya wokovu wao. Ilikuwa ni udhihirisho wa nguvu za kimbingu unaotosha kushawishi kila akili iliyokuwa inatawaliwa na mawazo na dhamiri sahihi. Wengi walioshuhudia kufufuliwa kwa Lazaro waliongozwa kumwamini Yesu. Lakini chuki ya makuhani dhidi yake iliongezeka. Walikuwa wamekataa ushahidi wote mdogo kuliko huu kuhus uungu wake, na kwa hiyo walighadhibishwa tu na mwujiza huu. Aliyekufa alikuwa amefufuliwa mchana kweupe, tena mbele ya umati wa mashuhuda. Hakuna mazingaombwe ambayo yangeharamisha ushahidi huo. Kwa kutumia sababu hii tu uadui wa makuhani ungekuwa umekufa. Waliazimia kwa dhati zaidi kuliko awali kuhakikisha wanakomesha kazi ya Kristo.

Masadukayo, ingawa hawakupendezwa na Kristo, hawakuwa wameazimia kikamilifu kufanya ubaya kwake kama Mafarisayo walivyokuwa. Chuki yao kwake haikuwa kubwa sana. Lakini na wao sasa waliamka. Walikuwa **(538)** hawaamini juu ya ufufuo wa wafu. Wakitumia kile kilichoitwa sayansi, walitoa hoja kwamba ingekuwa jambo lisilowezekana kwa mwili uliokufa kurejeshwa tena kuwa hai. Lakini kwa maneno machache ya Kristo nadharia yao ilikuwa imepinduliwa. Walikuwa wameonyeshwa kwamba hawajui Maandiko wala uweza wa Mungu. Hawakuweza kupata uwezekano wa kuondoa mtazamo wa watu waliopata kutokana na mwujiza ule. Watu wangewezaje kugeuzwa mbali kutoka kwake Yeye aliyekuwa amelishinda na kulipokonya kaburi mfu aliyekuwemo? Taarifa za uongo zilisambazwa, lakini mwujiza ule haukuweza kukanushika, na hawakujua namna ya kupiku madhara yake. Mpaka wakati huo Masadukayo walikuwa hawaungi mkono mpango wa kumwua Kristo. Lakini baada ya ufufuo wa Lazaro waliamua kwamba ni kwa njia ya kifo chake tu ndipo dharau zake zisizo na woga zingekomeshwa.

Mafarisayo waliamini katika ufufuo, na hawakuweza kuona kitu kingine katika mwujiza ule isipokuwa kwamba ulikuwa ushahidi ya kwamba Masihi alikuwa miongoni mwao. Lakini daima walikuwa wamepinga kazi ya Kristo. Tangu mwanzo kabisa walikuwa wamemchukia kwa sababu alikuwa ameweka wazi unafiki wao. Alikuwa amelichana vazi lao la desturi za kidini ambamo ndimo udhalimu wao ulimokuwa umefichwa. Dini safi aliyofundisha ilikuwa imehukumu hali yao ya kujisifia utakatifu. Walikuwa na kiu ya kulipiza kisasi kwake kwa makemeo aliyoyafanya kwao. Walikuwa wamejaribu kumchokoza ili aseme au kutenda jambo ambalo lingewapa nafasi ya kumhukumu. Walikuwa wamejaribu kumpiga kwa mawe mara kadhaa, lakini yeye akawa anatoweka kimya-kimya, na wao kukosa kumwona.

Miujiza aliyotenda siku ya Sabato ilikuwa yote ni kwa ajili ya kuwapa ahueni waliokuwa wanateseka, lakini Mafarisayo walikuwa wametafuta kuitumia hiyo kumhukumu kama mvunja-Sabato. Walikuwa wamejaribu kuwahamasisha wafuasi wa Herode kumpinga. Walionyesha kwamba alikuwa anatafuta kuanzisha ufalme mwingine dhidi ya uliokuwepo, na wakashauriana nao namna ya kumwangamiza. Ili kuwahamasisha Warumi kuwa dhidi yake, walikuwa wameonyesha kwamba Yeye anajaribu kupindua mamlaka yao. Walikuwa wamejaribu kila sababu ya kumkatilia mbali asiwashawishi watu. Lakini mpaka hapo majaribio yao yalikuwa yameshindwa kufanikiwa. Makutano walioshuhudia matendo yake ya huruma na kusikia mafundisho yake safi na matakatifu walijua kwamba haya hayakuwa matendo na maneno ya mvunja-Sabato wala mwenye kukufuru. Hata maafisa waliotumwa na Mafarisayo walikuwa wameshawishiwa na maneno yake kiasi kwamba hawakuweza kunyosha mikono juu yake. Kwa kushindwa hatimaye Wayahudi walipitisha amri kwamba mtu yeyote anayekiri imani katika Yesu atatengwa na sinagogi.

Hivyo kadiri makuhani, wakuu, na wazee walivyokusanyika ili kufanya shauri, nia yao ilijikita katika kumnyamazisha mtu huyo aliyefanya **(539)** matendo hayo ya ajabu kiasi cha watu wote kushangazwa.

Mafarisayo na Masadukayo walikuwa nusura ya kuungana zaidi kuliko ilivyowahi kutokea kabla. Wakati pale kabla walikuwa katika mgawanyiko, walikuja kuwa kitu kimoja katika kumpinga Kristo. Nikodemo na Yusufu, katika mabaraza ya huko nyuma, walikuwa wameepusha hali ya kumhukumu Yesu, na kwa sababu hiyo wakati huu hawakuitwa. Katika baraza hili walikuwepo watu wengine wenye ushawishi mkubwa waliomwamini Yesu, lakini ushawishi wao haukuweza jambo lolote dhidi ya Mafarisayo hawa wenye chuki.

Lakini bado wajumbe wa baraza hawakukubaliana wote. Wakati huu Sanhedrin haikuwa chombo cha kisheria. Baraza hili lilikuwepo tu kwa kuvumiliwa. Baadhi ya wajumbe wake walihoji hekima ile ya kutaka kumwua Kristo. Walihofu kwamba jambo hili lingeamsha vurugu za upinzani kutoka kwa watu, na hivyo kusababisha Warumi kushikilia mamlaka mengine zaidi kwa kuyaondoa kwa makuhani, na kuwaondolea nguvu ambazo walikuwa bado wanazo. Masadukayo waliungana katika chuki yao dhidi ya Kristo, lakini walikuwa tofauti kidogo kwa kuwa na tahadhari katika mienendo yao, wakihofu kwamba Warumi wangeweza kuwanyang'anya nafasi yao ya juu waliyokuwa nayo.

Katika baraza hili, lililokutanika ili kupanga kuhusu kifo cha Kristo, alikuwepo Shahidi aliyesikia maneno ya Nebukadneza, aliyeshuhudia karamu ya miungu ya Belshaza, aliyekuwepo wakati Kristo alipojitangaza kule Nazareti kuwa ni Mtiwa Mafuta. Shahidi huyo alikuwa sasa anawagusa wakuu hao katika kazi waliyokuwa wanafanya. Matukio ya maisha ya Yesu yalisimama mbele yao yakiwa na uzuri ambao uliwatisha. Walikumbuka lile tukio la hekaluni, Yesu, wakati huo akiwa na miaka kumi na miwili, alivyosimama mbele ya madaktari wasomi wa sheria, akiwauliza maswali yaliyowashangaza. Mwujiza wa kumfufua Lazaro uliokuwa umefanywa muda mfupi tu ulitoa ushuhuda kwamba Yesu hakuwa mwingine isipokuwa Mwana wa Mungu. Katika umuhimu wake ulio sahihi, Maandiko ya Agano la Kale yamhusuyo Kristo yalimlika katika akili zao. Wakiwa wametatanishwa na kufadhaishwa, wale wakuu waliuliza, "Tunafanya nini?" Kulikuwa na mgawanyiko katika baraza. Chini ya msukumo wa Roho Mtakatifu, makuhani na wakuu hawakuweza kukomesha usadikisho ya kwamba walikuwa wanapambana na Mungu.

Lile baraza lilipokuwa liko katika kiwango kikubwa cha kutatanika, Kayafa aliyekuwa kuhani mkuu alisimama. Kayafa alikuwa mtu mwenye kiburi na katili, mwenye misimamo na asiye na uvumilivu. Miongoni mwa watu aliokuwa na uhusiano nao kifamilia walikuwa Masadukayo, waliokuwa na kiburi, wagumu, wasioogopa kitu, wenye tamaa na wakatili, ambao walificha mambo hayo katika vazi la kuwa wenye haki ya bandia. Kayafa alikuwa amejifunza unabii, na ingawa alikuwa hajui maana yake, alitamka kwa mamlaka kubwa na uthabiti mkubwa kwamba: "Ninyi hamjui neno lolote; wala hamfikiri ya kwamba yafaa mtu mmoja afe kwa ajili ya watu, wala **(540)** lisiangamie taifa zima." Huyo kuhani mkuu alisema kwamba, Hata kama angekuwa hana hatia lazima awekwe pembeni. Alikuwa msumbufu, akiwavuta watu kwake, na akipunguza mamlaka ya wakuu. Alikuwa peke yake; ilikuwa vema zaidi kwamba yapasa afe kuliko mamlaka ya watawala idhoofike. Ikiwa watu wangepoteza imani na watawala wao, nguvu ya kitaifa ingeharibiwa. Kayafa alisisitiza kwamba baada ya mwujiza huu wafuasi wa Yesu huenda wangeinuka na kufanya ghasia. Alisema kwamba, Hapo ndipo Warumi watakapokuja, nao watafunga hekalu letu, na kupiga marufuku sheria zetu, na kutuharibu sisi kama taifa. Maisha ya Mgalilaya huyu yana thamani gani ikilinganishwa na maisha ya taifa hili? Ikiwa anasimama katika njia kuzuia ustawi wa Israeli, je, kumwondoa si kumtumikia Mungu? Heri mtu mmoja aangamie kuliko taifa zima kuharibiwa.

Katika kule kutamka kwamba yafaa mtu mmoja afe kwa ajili ya taifa, Kayafa alionyesha kwamba alikuwa na ufahamu fulani wa unabii, ingawa ulikuwa finyu sana. Lakini Yohana, akiongelea tukio hili, anauchukua unabii huo, na kuonyesha maana yake pana na ya kina. Anasema, "Wala si kwa ajili ya taifa hilo tu; lakini pamoja na hayo awakusanye watoto wa Mungu waliotawanyika." Ni jinsi gani Kayafa mwenye kupenda ukuu alivyotambua kwa upofu kazi ya Mwokozi!

Katika midomo ya Kayafa ukweli huu wa thamani uligeuzwa na kuwa uongo. Sera aliyokuwa anatetea imejengwa katika misingi iliyochukuliwa kutoka upaganini. Miongoni mwa wapagani, imani isiyo wazi kwamba mtu alipaswa kufa kwa ajili ya jamii ilikuwa imejitokeza katika hali ya kutoa wanadamu kama kafara. Kwa hiyo Kayafa alipendekeza kumtoa Yesu kafara ili kuliokoa taifa lenye hatia, si kulitoa katika uasi, bali kuwa katika uasi, ili ya kwamba wadumu katika dhambi. Na kwa mawazo yake alifikiria hivyo ili kunyamazisha hoja ya wale ambao wangediriki kusema kwamba hakuna jambo linalostahili kifo lililoonekana kwa Yesu.

Wakati wa baraza hili maadui wa Kristo walikuwa wamesadikishwa kwa kina. Roho Mtakatifu alikuwa amegusa akili yao. Lakini Shetani alipambana ili kuwaongoza. Aliwaletea kuona vurugu ambazo ziliwasumbua kwa sababu ya Kristo. Namna ambavyo aliheshimu kwa kiasi kidogo sana hali yao ya kuwa wenye haki. Aliiweka hali ya kuwa mtu mwenye haki kuwa kubwa mno kwa mbali, ambayo lazima wote wanaotaka kuwa watoto wa Mungu wawe nayo. Pasipo kuzingatia taratibu zao za kidini, alikuwa amewaelekeza wenye dhambi kwenda moja kwa moja kwa Mungu aliye Baba mwema, na kupeleka mahitaji yao kwake moja kwa moja. Kwa njia hiyo, kwa mawazo yao, alikuwa amedharau ukuhani. Alikuwa amekataa kutambua thiolojia ya shule za marabi. Alikuwa ameweka wazi vitendo viovu vya makuhani, **(541)** na kuharibu ushawishi wao kwa jinsi isivyorekebishika. Alikuwa amejeruhi matokeo ya kawaida zao na mapokeo yao, akitangaza kwamba ingawa zililazimisha sana ushikaji wa sheria za kaida za dini, zilihafifisha sheria ya Mungu. Shetani alileta yote haya mawazoni mwao.

Shetani aliwaambia kwamba ili kuendelea kuwa na mamlaka yao, lazima wamwue Yesu. Walifuata ushauri huo. Walifikiri kwamba, ile hali ya kwamba wangepoteza madaraka waliyokuwa nayo, ilikuwa sababu tosha ya kufikia maamuzi fulani. Ukiacha watu wachache ambao hawakudiriki kusema mawazo yao, Sanhedrin ilipokea maneno ya Kayafa kama maneno ya Mungu. Unafuu ulipatikana katika baraza; kutokukubaliana kulikoma. Walikubaliana kumleta Kristo katika kifo pindi fursa ya kwanza kabisa itakapojitokeza. Katika kule kukataa uthibitisho wa uungu wa Yesu, hawa makuhani na wakuu walikuwa wamejifungia katika giza lisilopenyeka. Walikuwa wamekuja kikamilifu katika mamlaka ya Shetani, kuharakishwa naye kuja juu ya ukingo wa uangamivu wa milele. Lakini bado ule ulikuwa udanganyifu ambao walipendezwa nao. Walijiona wenyewe kama mihimili, waliokuwa wanatafuta wokovu wa taifa.

Hata hivyo, Sanhedrin iliogopa kuchukua hatua dhidi ya Yesu pasipo uangalifu, watu wasije wakakasirishwa, na mabaya yaliyopangwa dhidi ya Yesu yakawapata wao wenyewe. Kwa sababu hii baraza lilikawia kutekeleza uamuzi huo waliokuwa wameamua. Mwokozi alielewa njama za makuhani. Alijua kwamba walitafuta kumwondoa, na ya kwamba kusudi lao baada ya muda mfupi lingekamilishwa. Lakini Yeye hakutaka kuharakisha shida, aliondoka haraka katika eneo lile, akiwachukua wanafunzi wake pamoja naye. Kwa njia hiyo kwa kielelezo chake mwenyewe aliweka katika vitendo mafundisho yake aliyowapa wanafunzi wake kwamba, "Watakapowafukuza katika mji huu, kimbilieni mwingine." Mathayo 10:23. Kuna eneo pana la kazi ambamo kazi ya wokovu wa roho ingefanywa; na isipokuwa pale ambapo heshima kwake ilihitaji vinginevyo, watumishi wa Bwana hawakutakiwa kuhatarisha maisha yao.

Sasa Yesu alikuwa ametumia miaka mitatu ya kazi ya hadhara ulimwenguni. Kielelezo chake cha kujikana nafsi na ukarimu usio na upendeleo vilikuwa vimeonyeshwa. Maisha yake yasiyo na doa, maisha ya shida na kujitoa, yalijulikana kwa wote. Hata hivyo kipindi hiki kifupi kilikuwa kirefu kulingana na vile ambavyo ulimwengu ungeweza kustahimili uwepo wa Mkombozi.

Maisha yake yalikuwa ya mateso na kushutumiwa. Akiondoka Bethlehemu kwa kufukuzwa na mfalme mwenye wivu, akikataliwa na watu wa nyumbani huko Nazareti, akihukumiwa kifo bila sababu huko Yerusalemu, Yesu, pamoja na wafuasi wake wachache waliokuwa waaminifu, alipata kimbilio la muda katika miji ya kigeni. Yeye ambaye **(542)** daima aliguswa na shida za wanadamu, aliyeponya wagonjwa, aliyewarejeshea vipofu kuona, akawarejeshea viziwi kusikia, na mabubu kusema, aliyewalisha wenye njaa na kuwafariji wenye huzuni, alifukuzwa kutoka kwa watu aliokuwa akiwatumika ili kuwaokoa. Yeye aliyetembea katika misukosuko, na kwa neno akanyamazisha mwungurumo wa hasira, aliyefukuza mapepo ambayo wakati wa kutoka yalimkiri kwamba ni Mwana wa Mungu, aliyevunja ukimya wa waliokufa, aliyewakusanya maelfu waliovutiwa na maneno yake ya hekima, hakuwa na uwezo wa kuifikia mioyo ya wale waliopofushwa na itikadi potofu na chuki, na ambao kwa ukaidi waliikataa nuru.

## Sura ya 60

# Sheria ya Ufalme Mpya

[Sura hii imejengwa katika Mathayo 20:20-28; Marko 10:32-45; Luka 18:31-34.]

Wakati wa Pasaka ulikuwa unakaribia, na kwa mara nyingine Yesu aligeuka na kuelekea Yerusalemu. Moyoni mwake kulikuwa na amani ya umoja mkamilifu kati yae na mapenzi ya Baba yake, na kwa hatua zenye shauku alitembea kuelekea mahali pa kafara. Lakini hisia ya fumbo, mashaka na woga, viliwaangukia wanafunzi wake. Mwokozi "alikuwa akiwatangulia, wakashangaa, nao katika kufuata wakaogopa."

Kwa mara nyingine Kristo aliwaita kwake wale kumi na wawili, na kwa ubayana mkubwa zaidi kuliko ilivyokuwa kabla, aliwafunulia habari za kusalitiwa na kuteswa kwake. Akasema, "Tazameni, tunapanda kwenda Yerusalemu, na mambo yote yatatimizwa, Mwana wa Adamu aliyoandikiwa na manabii. Kwa kuwa atatiwa mikononi mwa Mataifa, atafanyiwa dhihaka; atatendwa jeuri, na kutemewa mate; nao watampiga mijeledi, kisha watamwua; na siku ya tatu atafufuka. Walakini hawakuelewa maneno hayo hata kidogo, na jambo hilo lilikuwa limefichwa kwao, wala hawakufahamu yaliyonenwa."

Je, muda mfupi tu uliokuwa umepita hawakuwa wametangaza kila mahali kwamba, "Ufalme wa mbinguni umekaribia"? Kristo mwenyewe hakuwa ameahidi kwamba wengi wataketi na Ibrahimu na Isaka na Yakobo katika ufalme wa Mungu? Hakuwa ameahidi kwa wote waliokuwa wameacha vyote kwa ajili yake kwamba watapata mara mia katika maisha haya, na sehemu nyingine katika ufalme wake? Na hakuwa amewapatia wale kumi na wawili ahadi maalum ya ukuu wa heshima katika ufalme wake, - kukaa katika viti vya enzi wakihukumu makabila kumi na mbili ya Israeli? Hata **(548)** sasa tu alikuwa amesema kwamba mambo yote yaliyoandikwa katika manabii kumhusu Yeye lazima yatimizwe! Na je, manabii hawakutabiri kuhusu utukufu wa enzi ya Masihi? Kwa fikira ya mambo haya, maneno ya Yesu kuhusu kusalitiwa, mateso, na kifo yalionekana kuwa yasiyoeleweka na yasiyo wazi. Hata ugumu wa namna gani uingilie, waliamini kwamba ufalme ulikuwa unakaribia kuanzishwa.

Yohana, mwana wa Zebedayo, alikuwa mmoja wa wanafunzi wawili wa kwanza kumfuata Yesu. Yeye na kaka yake Yakobo walikuwa wamekuwa miongoni mwa kundi la kwanza la watu waliokuwa wameacha vyote kwa ajili ya kumtumikia. Kwa furaha walikuwa wameziacha nyumba na marafiki kusudi wawe naye; walikuwa wametembea na kuzungumza naye, walikuwa wamekuwa naye mahali pa faragha, na katika mikusanyiko ya hadhara. Alikuwa ameondosha hofu zao, akawaokoa na hatari, akatuliza maumivu yao, akafariji huzuni zao, na kwa uvumilivu na upendo akawafundisha, hadi mioyo yao ikaonekana kama vile imeunganishwa naye, na katika hisia za upendo wao walitamani kuwa karibu zaidi naye katika ufalme wake. Katika kila nafasi iliyowezekana, Yohana alikuwa katika nafasi iliyofuata baada ya Mwokozi, na Yakobo alitamani kuheshimiwa kwa kuwa karibu sana na Mwokozi.

Mama yao alikuwa mfuasi wa Kristo, na alikuwa amemhudumia kwa vitu vyake bure. Akiwa na upendo wa umama na shauku kwa wana wake, alitamani wapate nafasi ya juu katika ufalme ule. Aliwahamasisha waombe jambo hilo.

Mama na wanawe hao kwa pamoja walikuja kwa Yesu, wakiomba kwamba awape ruhusa waomba kile mioyo yao ilichotaka kuomba.

"Mwataka niwafanyie nini?" Aliuliza.

Mama akajibu, "Agiza kwamba hawa wanangu wawili waketi mmoja mkono wako wa kuume, na mmoja mkono wako wa kushoto, katika ufalme wako."

Yesu akawavumilia kwa upendo, pasipo kukemea ubinafsi wao kwa kile kitendo chao cha kutafuta upendeleo zaidi ya ndugu zao wengine. Alisoma mioyo yao, akajua kina cha mafungamano yao na Yeye. Upendo wao si wa kibinadamu tu; ingawa wamenajisiwa na mambo ya kidunia ya njia za kibinadamu, upendo wao ule unatiririka kutoka katika chemchemi ya upendo wake uokoao. Hataki kukemea, bali kuwaongezea kina na kuwafanya kuwa safi. Alisema, "Mwaweza kunywea kikombe ninyweacho mimi, au kubatizwa ubatizo nibatizwao mimi?" Wakakumbuka maneno yake ya fumbo, yaliyokuwa yakielekeza kwenye majaribu na mateso yake, lakini bado

wanajibu kwa kujiamini, "Twaweza." Walihesabu kama ni kuonyesha heshima kubwa kwa kuthibitisha utii wao kwake katika kushiriki mambo yote yatakayompata Bwana wao.

"Kikombe ninyweacho mimi mtakinywea, na ubatizo nibatizwao mimi mtabatizwa," alisema; mbele yake kukiwa na msalaba badala ya **(549)** kiti cha enzi, na wanyang'anyi wawili ndio wangekuwa naye upande wake wa kulia na wa kushoto. Yohana na Yakobo wangeshiriki mateso ya Bwana wao, mmoja, akiwa wa kwanza miongoni mwa ndugu wote kufa kwa upanga; na mwingine, mtu aliyepitia masumbufu, mashutumu na mateso kwa muda mrefu kuliko wote.

Akaendelea, "Lakini kuketi mkono wangu wa kuume na mkono wangu wa kushoto, sina amri kuwapa, bali watapewa waliowekewa tayari na Baba yangu." Katika ufalme wa Mungu, nafasi haipatikani kwa kupendelewa. Haitafutwi, wala kupokelewa kwa kugawiwa tu. Ni matokeo ya tabia. Taji na enzi ni thawabu ya hali iliyofikiwa na mtu; ni thawabu ya mtu kujishinda yeye mwenyewe kupitia Bwana wetu Yesu Kristo.

Muda mrefu baada ya hapo, wakati wanafunzi hao walipokuwa wamefikia mahali pa kushiriki mateso yake, Bwana alimfunulia Yohana kile ambacho ni sharti la kukaa karibu katika ufalme wake. Kristo alisema, "Yeye ashindaye, nitampa kuketi pamoja nami katika kiti changu cha enzi, kama mimi nilivyoshinda nikaketi pamoja na Baba yangu katika kiti chake cha enzi." "Yeye ashindaye, nitamfanya kuwa nguzo katika hekalu la Mungu wangu, wala hatatoka humo tena kabisa, nami nitaandika juu yake jina la Mungu wangu, . . . na jina langu mwenyewe, lile jipya." Ufunuo 3:21, 12. Hivyo ndivyo Paulo mtume alivyoandika pia, "Kwa maana, mimi sasa namiminwa, na wakati wa kufariki kwangu umefika. Nimevipiga vita vilivyo vizuri, mwendo nimeumaliza, Imani nimeilinda; baada ya hayo nimewekewa taji ya haki, ambayo Bwana, mhukumu mwenye haki, atanipa siku ile; wala si mimi tu, bali na watu wote pia waliopenda kufunuliwa kwake." 2 Timotheo 4:6-8.

Atakayesimama karibu zaidi na Kristo ni yule ambaye akiwa duniani alikunywa kwa kina zaidi roho ya Kristo ya upendo wa kujikana nafsi, - upendo ule ambao "hautakabari, haujivuni, . . . hautafuti mambo yake, hauoni uchungu, hauhesabu mabaya" (1 Wakorintho 13:4, 5), - upendo ule uliowasukuma wanafunzi wale, kama ulivyomsukuma Bwana, kutoa vyote, kuishi, kufanya kazi na kujitoa, hata kufa, kwa ajili ya wokovu wa watu. Roho hii ilidhihirishwa katika maisha ya Paulo. Alisema, "Kwa maana kwangu mimi kuishi ni Kristo;" maana maisha yake yalimdhihirisha Kristo kwa watu; "na kufa ni faida," – faida kwa Kristo; kifo chenyewe kingedhihirisha nguvu ya neema ya Kristo, na kuzikusanya roho kwenda kwake. Akasema, "Kristo ataadhimishwa katika mwili wangu; ikiwa kwa maisha yangu, au ikiwa kwa mauti yangu." Wafilipi 1:21, 20.

Wale wengine kumi waliposikia ombi hilo la Yakobo na Yohana hawakupendezwa. Cheo cha juu katika ufalme ule kilikuwa ni jambo ambalo kila mmoja wao alikuwa anajitafutia, na walipata hasira kwa sababu hao wanafunzi wawili walikuwa wanataka kupata upendeleo kabla yao.

**(550)** Kwa mara nyingine ugomvi kuhusu nani ambaye angekuwa mkubwa zaidi ulionekana kama kutaka kuanza upya, wakati Yesu, akiwaita kwake, alipowaambia wanafunzi wale waliokuwa wakinung'unikiana, "Mwajua ya kuwa wale wanaohesabiwa kuwa wakuu wa Mataifa huwatawala kwa nguvu, na wakubwa wao huwatumikisha. Lakini haitakuwa hivyo kwenu."

Katika ufalme wa ulimwenguni, maana ya cheo ilikuwa ni kujilimbikizia kwa ubinafsi. Watu wa kawaida walitakiwa kuishi kwa kunufaisha tabaka la watawala. Madaraka, utajiri, elimu, zilikuwa ni nyenzo nyingi za kujipatia nafasi ya kutawala watu kwa manufaa ya viongozi. Tabaka la juu kabisa la utawala lilikuwa na watu wanaopanga, kuamua, kufurahia, na kutawala; tabaka la chini lilikuwa na jukumu la kutii na kutumikia. Dini pia ilikuwa ni suala la madaraka kama jinsi vitu vingine vyote vilivyokuwa. Watu walitakiwa kuamini na kutenda vile wakubwa wa dini walivyoelekeza. Haki ya mtu kama mtu, kufikiri na kutenda kwa ajili yake mwenyewe, ilikuwa haitambuliki kabisa.

Kristo alikuwa anaanzisha ufalme ulio katika misingi mingine. Aliwaita watu, si kuja kutawala, bali kutumikia, mwenye nguvu aje kubeba mapungufu ya aliye dhaifu. Madaraka, cheo, talanta, elimu, viliwaweka wenye navyo katika wajibu mkubwa zaidi wa kuwatumikia wenzao. Hata kwa mwanafunzi wa Yesu wa chini kabisa maneno haya yalisemwa, "Mambo yote ni kwa ajili yenu." 2 Wakorintho 4:15.

"Kwa maana Mwana wa Adamu naye hakuja kutumikiwa, bali kutumika, na kutoa nafsi yake iwe fidia ya wengi." Kristo alikuwa mwangalizi kwa maana zote miongoni mwa wanafunzi wake, mbeba mizigo. Alishiriki katika umaskini wao, alionyesha matendo ya kujikana nafsi kwa ajili yao, aliwatangulia kwenda kulainisha mahali pagumu kabla yao, na muda si mrefu angekamilisha kazi yake duniani kwa kuyatoa maisha yake. Kanuni hiyo aliyotenda Yesu inatakiwa kutendwa na washiriki wa kanisa ambalo ni mwili wake. Mpango na mazingira ya wokovu ni upendo. Katika ufalme wa Kristo walio wakuu zaidi ni wale wanaofuata kielelezo hicho alichoonyesha, na kufanya kazi kama ya mchungaji wa kondoo wake.

Maneno ya Paulo yanafunua uchaji wa kweli na heshima ya maisha ya Kikristo: "Ingawa nimekuwa huru kwa watu wote, nalijifanya mtumwa wa wote," "nisitake faida yangu mwenyewe, ila faida yao walio wengi, wapate kuokolewa." 1 Wakorintho 9:19; 10:33.

Katika mambo ya dhamiri lazima moyo uachwe bila kufungwa. Hakuna mtu anayetakiwa kudhibiti mawazo ya mtu mwingine, kuamua kwa ajili ya mtu mwingine, wala kuamua kuhusu majukumu ya mtu mwingine. Mungu anaipa kila nafsi uhuru wa kufikiri, na kufuata msimamo wake anavyosadikishwa. "Kila mtu miongoni mwetu atatoa habari zake mwenyewe mbele za Mungu." Hakuna mtu mwenye haki ya kuchanganya tabia zake katika tabia za mwingine. Katika mambo yote yanayohusisha kanuni, "kila mtu na athibitike katika akili zake mwenyewe." Warumi 14:12, 5. Katika ufalme wa Kristo hakuna ukandamizaji wa **(551)** wakuu, hakuna kulazimisha tabia. Malaika wa mbinguni hawaji duniani kutawala, na kudai kuheshimiwa, bali huja kama wajumbe wa wema, kushirikiana na watu katika kuwainua wanadamu.

Kanuni hizo na maneno ya mafundisho ya Mwokozi, katika uzuri wa kimbingu wa hayo, yalikaa katika kumbukumbu ya mwanafunzi yule mpendwa. Kuelekea katika siku zake za mwisho-mwisho mzigo wa Yohana wa ushuhuda kwa makanisa ulikuwa ni, "Maana, hii ndiyo habari mliyoisikia tangu mwanzo, kwamba tupendane sisi kwa sisi." "Katika hili tumelifahamu pendo, kwa kuwa yeye aliutoa uhai wake kwa ajili yetu; imetupasa na sisi kuutoa uhai wetu kwa ajili ya hao ndugu." 1 Yohana 3:11, 16.

Hii ndiyo roho iliyoenea katika kanisa la kale. Baada ya kumwagwa kwa Roho Mtakatifu, "jamii ya watu walioamini walikuwa na moyo mmoja na roho moja; wala hapana mmoja aliyesema ya kuwa kitu chochote alicho nacho ni mali yake mwenyewe." "Wala hapakuwa na mtu mmoja miongoni mwao mwenye mahitaji." "Na mitume wakatoa ushuhuda wa kufufuka kwake Yesu kwa nguvu nyingi, na neema nyingi ikawa juu yao wote." Matendo 4:32, 34, 33.

## Sura ya 61

# Zakayo

[Sura hii imejengwa katika Luka 19:1-10.]

Akiwa njiani kuelekea Yerusalemu, Yesu "alipoingia Yeriko alipita katikati yake." Maili chache kutoka Mto Yordani, kwenye ukingo wa magharibi wa bonde ambalo lilikuwa limetanda na kutengeneza tambarare, ndipo mji huo ulipokuwa ukiwa katika kijani kibichi cha hali ya kitropiki na uzuri wa kuvutia. Ukiwa na miti ya mitende na bustani nzuri zilizonyweshwa na chemchemi hai, uling'aa kama zumaridi katika mandhari ile ya vilima vyenye miamba ya chokaa na makorongo vilivyotenganisha kati ya Yerusalemu na mji huo wa tambarare.

Misafara mingi iliyokuwa inaelekea kwenye sikukuu ilipita ndani ya mji wa Yeriko. Kufika kwa misafara hiyo ilikuwa mara zote ni msimu wa sikukuu, lakini kwa sasa shauku iliamshwa ndani ya watu. Ilikuwa imejulikana kwamba Rabi wa Galilaya ambaye siku chache tu alikuwa amemrejesha Lazaro katika hali ya kuishi tena alikuwa katika msafara; na ingawa minong'ono ilikuwa mingi kuhusu njama za makuhani, makutano ya watu yalikuwa na hamu ya kuonyesha heshima kwake.

Yeriko ulikuwa mmoja kati ya miji ya kale iliyotengwa rami kwa ajili ya makuhani, na kwa hiyo wakati huu idadi kubwa ya makuhani walikuwa na makazi yao hapa. Lakini mji huu ulikuwa pia na watu walio tofauti-tofauti. Ulikuwa ni kituo kikubwa cha usafirishaji, na maafisa na askari wa Kirumi, na wageni kutoka maeneo tofauti-tofauti, walikuwa hapo, wakati ukusanyaji wa kodi ya forodha uliufanya mji huu kuwa nyumbani kwa watoza ushuru.

"Mkubwa mmoja katika watoza ushuru," Zakayo, alikuwa Myahudi, na akiwa mwenye kuchukiwa sana na watu wa taifa lake. Cheo chake na utajiri wake vilikuwa ni zawadi ya kazi hiyo **(553)** waliyochukia, na ambayo ilichukuliwa kama jina jingine la kutotenda haki na kutoza isivyo haki. Hata hivyo afisa huyu wa forodha aliye tajiri hakuwa mtu mwenye moyo mgumu kwa ujumla kama alivyoonekana. Chini ya mwonekano wa hali ya kupenda ulimwengu na kiburi kulikuwa na moyo wenye uwezekano wa kupokea ushawishi wa kimbingu. Zakayo alisikia habari za Yesu. Taarifa ya Yeye aliyekuwa amejibebesha wema na upole hata kwa makundi ya watu waliokataliwa ilikuwa imeenea mbali na kwa mapana. Ndani ya mkuu huyu wa watoza-ushuru kuliamshwa hamu ya kutaka maisha mazuri zaidi. Maili chache tu kutoka Yeriko, Yohana Mbatizaji alikuwa amehubiri pale Yordani, na Zakayo alikuwa amesikia wito wa kufanya toba. Yale mafundisho kwa watoza ushuru kwamba, "Msitoze kitu zaidi kuliko mlivyoamriwa" (Luka 3:13), ingawa kwa nje hayakutiliwa maanani, yalikuwa yamegusa mawazo yake. Aliyajua Maandiko, na alisadikishwa kwamba matendo yake hayakuwa sahihi. Sasa kwa kusikia maneno kwamba Mwalimu Mkuu anakuja, alijihisi kwamba alikuwa mwenye dhambi mbele za Mungu. Lakini bado kile alichokuwa amesikia kuhusu Yesu kuliangaza matumaini katika moyo wake. Toba, matengenezo ya maisha, ilikuwa inawezekana, hata kwake; kwani mmoja wa wanafunzi wa Mwalimu huyu mpya waliotumainiwa zaidi si alikuwa mtoza ushuru kabla? Mara moja Zakayo alianza kufuata ule usadikisho uliokuwa ndani yake, na kuwarudishia wale aliokuwa amewakosea.

Tayari alikuwa ameanza kupiga hatua zake, wakati habari ziliposikika katika mji wote kwamba Yesu alikuwa anauingia. Zakayo aliazimia kumwona. Alikuwa anaanza kugundua jinsi matunda ya dhambi yalivyokuwa machungu, na jinsi ilivyo ngumu njia ya mtu anayejaribu kugeuka kutoka katika njia mbaya. Ilikuwa vigumu kukabili hali ya kutoeleweka vema, kuangaliwa kwa wasiwasi na mashaka katika juhudi zake za kusahihisha makosa yake. Huyu mkuu wa watoza ushuru alitamani kuuona uso wa Yeye ambaye maneno yake yalikuwa yamemletea matumaini moyoni mwake.

Barabara zilikuwa zimejaa watu, na Zakayo, aliyekuwa mdogo wa umbo, hakuweza kuona chochote juu ya vichwa vya watu. Hakuna mtu ambaye angempisha njia; kwa hiyo, baada ya kukimbia mbele kidogo ya umati, mpaka mahali ambako mti wa mkuyu uliokuwa na matawi mengi ulining'inia juu ya njia, mtoza ushuru huyu aliye tajiri alipanda ule mti na kukaa katikati ya matawi makubwa, mahali ambapo angeuona msafara wote kwa namna ulivyokuwa unapita. Ule umati unazidi kuja, unapita pale, Zakayo naye anakaza macho ili kumwona yule aliyetaka kumwona.

Zaidi ya fujo za ghasia zilizofanywa na makuhani na marabi na kelele za shangwe za kumkaribisha zilizofanywa na watu, ile hamu ya mkuu wa watoza ushuru isiyosemeka ilizungumza na moyo wa Yesu. Ghafla, pale pale chini ya mti, kundi lote likasimama, watu wote walioko mbele na nyuma wakasimama, na Yeye ambaye mtazamo wake unaonekana kama unasoma moyo anaangalia juu. Akiwa kama vile anaonekana mwenye mashaka na akili yake, **(554)** yule mtu aliye katika matawi ya mti anasikia maneno, "Zakayo, shuka upesi, kwa kuwa leo imenipasa kushinda nyumbani mwako."

Umati wa watu unapisha, Zakayo anaongoza msafara kwenda nyumbani kwake akitembea kama vile katika ndoto. Lakini marabi wanaangalia tukio hilo kwa nyuso za hasira, na wananung'unika kwa kutofurahishwa wakisema, "Ameingia kukaa kwa mtu mwenye dhambi."

Zakayo alikuwa ametekewa, amestaajabu, na kunyamazishwa na upendo na kujishusha kwa Kristo kwa kuja katika hali yake, asiyestahili. Sasa upendo na heshima kwa Bwana wake huyu mpya unaifungua midomo yake. Anataka kukiri na kutangaza toba yake hadharani **(555)** Mbele ya umati wa watu, "Zakayo akasimama, akamwambia Bwana, Tazama, Bwana, nusu ya mali yangu nawapa maskini, na ikiwa nimenyang'anya mtu kitu kwa hila namrudishia mara nne.

"Yesu akamwambia, Leo wokovu umefika nyumbani humu, kwa sababu huyu naye ni mwana wa Ibrahimu."

Wakati yule kijana mtawala mwenye mali alipokuwa ameondoka kutoka kwa Yesu, wanafunzi walikuwa wameshangaa maneno ya Bwana wao kwamba, "Jinsi ilivyo shida wenye kutegemea mali kuingia katika ufalme wa Mungu!" Walikuwa wameambiana wao kwa wao kwa mshangao kwamba, "Ni nani, basi, awezaye kuokoka?" Sasa walikuwa na onyesho la kielelezo cha ukweli wa maneno yale ya Kristo, "Yasiyowezekana kwa wanadamu yawezekana kwa Mungu." Marko 10:24, 26; Luka 18:27. Waliona jinsi ambavyo, kwa neema ya Mungu, yule tajiri angeingia katika ufalme.

Kabla ya Zakayo kuangalia uso wa Kristo, alikuwa ameanza kazi iliyomfanya aonekane kama mwenye toba ya kweli. Kabla ya kushutumiwa na mtu, alikuwa ameshaungama dhambi zake. Alikuwa amejisalimisha kwa usadikisho wa Roho Mtakatifu, na alikuwa ameanza kutekeleza mafundisho ya maneno yaliyoandikwa kwa ajili ya Israeli ya zamani na kwa ajili yetu pia. Bwana alikuwa amesema muda mrefu kabla, "Na ikiwa ndugu yako amekuwa maskini, na mkono wake umelegea kwako, ndipo utamsaidia, atakaa nawe kama mgeni, na msafiri. Usitake riba kwake wala faida, bali mche Mungu wako, ili ndugu yako akae nawe. Usimpe fedha yako upate riba, wala usimpe vyakula vyako kwa kujitakia faida." "Wala msidanganyane; lakini utamcha Mungu wako; kwa kuwa mimi ndimi Bwana, Mungu wenu." Walawi 25:35-37, 17. Maneno haya yalitamkwa na Kristo mwenyewe wakati ule akiwa amezungukwa na nguzo ya wingu, na mwitikio wa kwanza kabisa wa Zakayo kwa upendo wa Kristo ulikuwa katika kudhihirisha huruma kwa maskini na watu wanaoteseka.

Watoza ushuru walikuwa na ushirikiano wao, ili kuwakandamiza watu, na kuwezeshana katika matendo yao ya udhalimu. Katika kule kutoza isivyo halali walikuwa tu wanatekeleza jambo ambalo lilikuwa kama desturi ya kawaida mahali pote. Hata makuhani na marabi ambao walidharau watoza ushuru walikuwa na hatia ya kujitajirisha kwa vitendo visivyo vya uadilifu vilivyofichwa ndani ya vazi la kazi takatifu. Lakini mara tu Zakayo alipojisalimisha kwa ushawishi wa Roho Mtakatifu alitupilia kando kila tendo lililo kinyume na uadilifu.

Hakuna toba halisi ambayo haina kazi ya matengenezo. Haki ya Kristo siyo vazi linalofunika dhambi isiyotubiwa wala **(556)** kuachwa; ni kanuni ya maisha inayobadilisha tabia na kutawala mwenendo. Utakatifu ni hali ya mzima-mzima kuwa kwa ajili ya Mungu; ni kujisalimisha kikamilifu moyo na maisha ili vikaliwe na kanuni za mbinguni.

Mkristo aliye katika maisha ya kujishughulisha anatakiwa kuwakilisha ulimwenguni tabia ile ambayo Bwana angeonyesha katika kuendesha shughuli hizo. Katika kila muamala anatakiwa kudhihirisha kwamba Mungu ndiye mwalimu wake. Maneno "Utakatifu kwa Bwana" yanapaswa kuandikwa katika vitabu vya kumbukumbu za kila siku na vitabu vya hesabu za fedha, hati za umiliki, stakabadhi za malipo, na hati za madai. Wale wanaojitaja kuwa wafuasi wa Kristo, ambao hujishughulisha na mambo kwa jinsi isiyo ya haki, wanatoa ushuhuda wa uongo kinyume na tabia takatifu, ya haki na njema ya Mungu. Kila mtu anayeongoka, kama Zakayo, ataashiria kuingia kwa Kristo moyoni mwake kwa kuachana na vitendo visivyo vya haki vilivyokuwa vimetawala maisha yake. Kama alivyokuwa yule mtoza ushuru mkuu, atathibitisha wema wake kwa kufanya marejesho. Bwana anasema,

"Kama mtu mwovu akirudisha rehani, na kumrudishia mtu mali yake aliyomnyang'anya, akizifuata sheria za uzima, asitende uovu wowote; . . . katika dhambi zake zote alizozitenda, hata mojawapo haitakumbukwa juu yake; . . . hakika ataishi." Ezek. 33:15, 16.

Ikiwa tumewajeruhi wengine katika muamala wa shughuli yoyote isiyo haki, ikiwa tumerusha bei katika biashara, au tumemtapeli mtu yeyote, hata kama ni jambo ambalo lipo kisheria, tunapaswa kuungama kosa letu, na kufanya marejesho kwa kadiri uwezo wetu unapofikia. Ni haki kwetu kurejesha si tu kiasi kile tulichochukua, bali kile ambacho kingefikia baada ya kuongezeka ikiwa kingewekezwa kwa usahihi na busara kwa wakati wote ambapo kimekuwa katika umiliki wetu.

Yesu alimwambia Zakayo, "Leo wokovu umefika nyumbani humu." Si Zakayo peke yake aliyebarikiwa, bali nyumba yake yote pamoja naye. Kristo alienda nyumbani kwake kumpa masomo ya ukweli, na kuifundisha nyumba yake mambo yahusuyo ufalme. Chuki na dharau za marabi na wenye kuabudu zilikuwa zimewafukuzia mbali na sinagogi; lakini sasa, wakiwa kama nyumba ambayo imependelewa kuliko zote ndani ya mji wa Yeriko, walikusanyika kwa Mwalimu wa kimbingu ndani ya nyumba yao wenyewe, wakasikiliza wao wenyewe maneno ya uzima.

Pale Kristo anapopokelewa kama Mwokozi wa mtu binafsi ndipo wokovu unapokuja moyoni. Zakayo alikuwa amempokea Yesu, si kama mgeni anayepita tu nyumbani kwake, bali kama Yeye ambaye atafanya makao katika hekalu la moyo. Waandishi na Mafarisayo walimshtaki kwamba ni mwenye dhambi, walimnung'unikia Kristo kwa kuwa mgeni wake, lakini Bwana alimtambua kama mwana wa Ibrahimu. Maana "wale walio wa imani, hao ndio wana wa Ibrahimu." Wagalatia 3:7.

# Sura ya 62

## Karamu Nyumbani kwa Simoni

[Sura hii imejengwa katika Mathayo 26:6-13; Marko 14:3-11; Luka 7:36-50; Yohana 11:55-57; 12:1-11.]

Simoni wa Bethania alitajwa kuwa mwanafunzi wa Yesu. Alikuwa mmoja wa Mafarisayo wachache ambao waliungana na wafuasi wa Kristo wazi-wazi. Alimkiri Yesu kama mwalimu, na alitumaini kwamba huenda akawa ndiye Masihi, lakini hakuwa amemkubali kama Mwokozi. Tabia yake haikuwa imebadilishwa; misingi haikuwa imebadilika.

Simoni alikuwa mtu aliyeponywa ukoma, na ni jambo hili lililomvuta kwa Yesu. Alitamani kuonyesha shukrani zake, na katika safari ya mwisho ya Yesu kutembelea Bethania alifanya karamu kwa ajili ya Yesu na wanafunzi wake. Karamu hii iliwaleta pamoja Wayahudi wengi. Wakati huu kulikuwa na hamasa kubwa Yerusalemu. Kristo na kazi yake alikuwa anavuta usikivu mkubwa kuliko ilivyokuwa kabla. Wale waliokuwa wamekuja karamuni walifuatilia kwa makini mienendo ya Yesu, baadhi kwa macho yasiyo rafiki.

Mwokozi alikuwa amewasili Bethania siku sita kabla ya Pasaka, na kama ilivyokuwa desturi yake alikuwa amepata mahali pa kufikia nyumbani kwa Lazaro. Umati wa wasafiri waliokuwa wanapita kuelekea jijini walisambaza habari kwamba Yesu alikuwa njiani kuelekea Yerusalemu, na ya kwamba siku ya Sabato angepumzikia Bethania. Kulikuwa na wasiwasi miongoni mwa watu. Watu wengi walitiririka kwenda Bethania, baadhi kwa kumpenda Yesu, na wengine kwa udadisi ili kumwona yule aliyefufuliwa kutoka katika wafu.

Wengi walitarajia kumsikia Lazaro akisimulia mambo aliyoshuhudia baada ya kufa. Walishangaa kuona kwamba hakuwaeleza chochote. **(558)** Hakuwa na jambo linalohusu hayo la kuwaambia. Uvuvio unatangaza kwamba, "Wafu hawajui neno lolote. . . . Mapenzi yao na machukio yao, na husuda yao, imepotea yote pamoja." Muhubiri 9:5, 6. Lakini Lazaro alikuwa na ushuhuda wa kushangaza kuhusu kazi ya Kristo. Alikuwa amefufuliwa kwa kusudi hili. Kwa uhakika na nguvu alitangaza kwamba Yesu alikuwa Mwana wa Mungu.

Taarifa zilizorudishwa Yerusalemu zikipelekwa na watu waliotembelea Bethania ziliongeza hamasa kule. Watu walikuwa na hamu ya kumwona na kumsikia Yesu. Kulikuwa na maswali kutaka kujua ikiwa Lazaro ataambatana naye kwenda Yerusalemu, na ikiwa nabii huyo atatawazwa kuwa mfalme wakati wa sikukuu hiyo. Makuhani na wakuu waliona kwamba tegemeo lao kwa watu lilikuwa linadhoofika, na ghadhabu yao dhidi ya Yesu iliongezeka zaidi. Kwa ugumu walisubiri fursa ya kumfutilia mbali milele kutoka katika njia yao. Kadiri muda ulivyopita, walianza kuogopa kwamba huenda hatakuja Yerusalemu. Walikumbuka jinsi ambavyo mara nyingi alikuwa ameepuka mipango yao ya kumwua, na kwa hiyo waliogopa kwamba alikuwa ameshajua makusudi yao dhidi yake, na akabaki mbali. Waliweza kusitiri nia zao, na wakaulizana wao kwa wao, "Mwaonaje? Haji kabisa sikukuu hii?"

Baraza la makuhani na Mafarisayo liliitishwa. Tangu kufufuliwa kwa Lazaro watu walimuunga mkono Kristo kiasi kwamba ilikuwa hatari kumtia nguvuni wazi-wazi. Kwa wale wenye mamlaka waliazimia kumchukua kwa siri, na kuendesha mahojiano ya uchunguzi kimya-kimya. Walitumaini kwamba hukumu yake ikishajulikana, badiliko la upepo wa mwelekeo wa mawazo ya watu ungekuwa wa kuwaunga mkono.

Hivyo ndivyo walivyopanga kumwangamiza Yesu. Lakini kwa kuwa Lazaro alikuwa anaishi, makuhani na marabi walijua kwamba hawakuwa salama. Uwepo wenyewe wa mtu ambaye alikuwa kaburini kwa siku nne, na ambaye alirejeshwa kuwa hai kwa neno la Yesu, ungesababisha mwitikio fulani. Watu wangewaadhibu viongozi kwa kuondoa uhai wa Yeye ambaye aliweza kutenda mwujiza kama huo. Kwa hiyo Sanhedrin iliamua kwamba lazima na Lazaro pia afe. Wivu na chuki ziliwapeleka mbali katika utumwa wa kiasi hicho. Chuki na kutoamini kwa viongozi wa Wayahudi vilikuwa vimeongezeka kiasi ambacho vingeweza kuchukua hata uhai wa mtu ambaye uweza usio na kikomo ulikuwa umemwokoa na mauti.

Wakati njama hizi zikiendelea huko Yerusalemu, Yesu na rafiki zake walikuwa wamealikwa kwenye karamu ya Simoni. Mezani Yesu alikaa pamoja na Simoni, ambaye alikuwa amemponya ugonjwa mbaya, katika upande mmoja, na Lazaro, aliyekuwa amemfufua kutoka katika wafu, upande mwingine. Martha alihudumia mezani,

lakini Mariamu alikuwa anasikiliza kwa makini kila neno lililotoka midomoni mwa **(559)** Yesu. Kwa wema wake, Yesu alikuwa amemsamehe Mariamu dhambi zake, alikuwa amemwita kaka yake mpendwa kumtoa kaburini, kwa hiyo moyo wa Mariamu ulijawa na shukrani. Alikuwa amemsikia Yesu akisema kuhusu kifo chake kilichokuwa kinakaribia, na katika upendo wake wa kina na huzuni alikuwa ametafuta kuonyesha heshima kwake. Kwa gharama kubwa ya kibinadamu alikuwa amenunua ratli ya “marhamu ya nardo safi yenye thamani nyingi," kwa ajili ya kuupaka mwili wa Yesu. Lakini sasa wengi walikuwa wakitangaza kwamba alikuwa atawazwe kuwa mfalme. Huzuni yake iligeuzwa kuwa furaha, na alikuwa na hamu ya kutaka kuwa mtu wa kwanza kuonyesha heshima kwa Bwana. Akikivunja kibweta chake cha marhamu, alimimina mafuta yake kichwani na miguuni kwa Yesu; halafu, akishuka magotini huku akilia, aliimwagia miguu ya Yesu machozi, na kuipangusa kwa nywele zake ndefu.

Mariamu alikuwa ametafuta kuepuka kuonekana, na hata kujongea kwake kulifanyika bila kusikika, lakini marhamu yale yalikijaza chumba hali ya kunukia kwa marhamu yale, na kwa hiyo watu wote wakajua kitendo kilichofanyika. Yuda alikiangalia kitendo hicho kwa kutopendezwa. Badala ya kusubiri asikie Yesu atasema nini kuhusu jambo hilo, alianza kunong’ona na waliokuwa karibu naye maneno ya kulalamika, akielekeza lawama kwa Kristo kwa kuruhusu hasara kubwa kiasi hicho. Kwa ujanja alitoa mapendekezo ambayo yangeweza kusababisha kutokukubalika.

Yuda alikuwa mweka hazina kwa ajili ya wanafunzi, na alikuwa amechukua kwa siri sehemu kutoka katika akiba yao ndogo kwa ajili ya matumizi yake binafsi, kwa njia hiyo akipunguza fedha waliyokuwa nayo na ikabaki kidogo. Alikuwa na hamu ya kuweka katika mkoba wake kila kitu ambacho angepata. Hazina iliyokuwa ndani ya mkoba ule mara nyingi ilitumika kukidhi mahitaji ya maskini; na wakati kiliponunuliwa kitu ambacho Yuda hakuona kama ni muhimu, alisema, Kwa nini tunapoteza fedha kwa hiki? Kwa nini gharama ya hiki isingewekwa katika mkoba ninaobeba kwa ajili ya maskini? Sasa kitendo cha Mariamu kilikuwa kinyume na ubinafsi wake namna hiyo kiasi kwamba aliaibika; na kulingana na desturi yake, alitafuta kuihesabia thamani zawadi ile ya Mariamu ili apate sababu ya kuipinga. Akiwageukia wanafunzi, aliuliza hivi, "Mbona marhamu hii haikuuzwa kwa dinari mia tatu, wakapewa maskini? Naye aliyasema hayo, si kwa kuwahurumia maskini; bali kwa kuwa ni mwivi, naye ndiye aliyeshika mfuko, akavichukua vilivyotiwa humo." Yuda hakuwa na moyo kwa ajili ya maskini. Ikiwa marhamu ya Mariamu ingeuzwa, na kile kinachopatikana kikaangukia mikononi mwake, maskini wasingenufaika kwa chochote.

Yuda alikuwa na maarifa na uwezo mkubwa. Akiwa kama mtu wa fedha alijidhania kuwa mkubwa kwa wanafunzi wenzake, na alikuwa amewafanya hata wao kumwona katika mtazamo huo. Alikuwa amejiaminisha kwao, na alikuwa na nguvu kubwa ya ushawishi kwao. Ile hali ya kujionyesha kuwajali maskini iliwadanganya, na ujanja wake wa kupinga jambo lile uliwafanya waangalie **(560)** kujitoa kule kwa Mariamu kwa mashaka. Minong’ono ilipita katika meza kwamba, "Ni wa nini upotevu huu? Maana marhamu hii ingaliweza kuuzwa kwa fedha nyingi wakapewa maskini."

Mariamu aliyasikia yale maneno ya kukosoa. Moyo wake ulitetemeka ndani yake. Aliogopa kwamba dada yake angemshutumu kwa matumizi mabaya ya vitu. Bwana, naye, angemdhania kuwa hajali mahitaji ya baadaye. Bila kuomba radhi au udhuru alitaka kuondoka, wakati sauti ya Bwana wake iliposikika ikisema, "Mwacheni; mbona mnamtaabisha?" Aliona kwamba alikuwa amedhalilika na kuumia. Alijua kwamba katika tendo hili la huduma alikuwa ameonyesha shukrani yake kwa msamaha wa dhambi zake, na alileta utulivu katika mawazo yake. Akiinua sauti yake juu kuliko maneno yao ya minong’ono, alisema, "Amenitendea kazi njema; maana sikuzote mnao maskini pamoja nanyi, na kila mpendapo mwaweza kuwatendea mema; lakini mimi hamnami sikuzote. Ametenda alivyoweza; ametangulia kuupaka mwili wangu marhamu kwa ajili ya maziko."

Zawadi ile ya manukato ambayo Mariamu alifikiria kuupaka mwili wa Kristo akiwa amekufa ilipakwa kwenye mwili wake ulio hai. Wakati wa maziko utamu wake ungejaza kaburi; sasa ilifurahisha moyo wa Kristo kwa hakikisho la imani na upendo wa Mariamu. Yusufu wa Arimathaya na Nikodemo hawakutoa zawadi ya upendo kwa Yesu katika maisha yake. Wakiwa na machozi ya uchungu walileta manukato yao ya gharama kwa ajili ya mwili wake uliokufa usio na fahamu. Wanawake walioleta manukato kaburini walikuwa wameenda bure, maana alikuwa amefufuka. Lakini Mariamu, kwa kummiminia Mwokozi upendo wake wakati Mwokozi akiwa na ufahamu wa kujitoa kwa Mariamu, alikuwa anampaka mafuta kwa ajili ya maziko. Na pindi aliposhuka kwenda

katika giza la mateso, alienda pamoja na kumbukumbu ya tendo lile, udhihirisho wa upendo ambao Kristo angeonyeshwa na waliokombolewa milele.

Wapo wengi ambao wanaleta zawadi za thamani kwa ajili ya waliokufa. Wanaposimama mbele ya mwili wenye baridi na ukimya, maneno ya upendo yanatamkwa bure. Upendo, kutambua, kujitoa, vyote vinatolewa kwa kitu kisichoona wala kusikia. Laiti kama maneno haya yangetamkwa wakati ambapo mtu huyu aliyekuwa amechoka alikuwa anayahitaji sana, wakati amabapo sikio lingesikia na moyo ukapata hisia, manukato yao haya yangekuwa na thamani kubwa kiasi gani!

Mariamu hakujua maana kamili ya tendo la upendo alilofanya. Hakuweza kuwajibu washtaki wake. Hakuweza kueleza ni kwa nini alikuwa amechagua tukio lile kuwa la kumpaka mafuta Yesu. Roho Mtakatifu alikuwa amepanga kwa ajili yake, naye alikuwa ametii misukumo ya Roho huyo. Uvuvio hauhangaiki kutoa sababu. Uwepo wa kisichoonekana unazungumza na akili na roho, na kuusukuma moyo kutenda. Unajihalalisha wenyewe.

Kristo alimwambia Mariamu maana ya tendo lake, na katika hili alimpa Mariamu **(563)** zaidi ya kile alichopokea Yeye. Alisema, "Maana kwa kunimwagia mwili wangu marhamu hiyo, ametenda hivyo ili kuniweka tayari kwa maziko yangu." Kile kibweta cha marhamu kilipovunjwa, na harufu ya marhamu kuijaza nyumba yote, ndivyo ambavyo Kristo angekufa, mwili wake ungevunjwa; lakini angefufuka kutoka kaburini, na harufu nzuri ya maisha yake ingeijaza dunia. Kristo alitupenda "tena akajitoa kwa ajili yetu, sadaka na dhabihu kwa Mungu, kuwa harufu ya manukato." Waefeso 5:2.

Kristo alisema, "Amin, nawaambieni, Kila patakapohubiriwa Injili hii katika ulimwengu wote, tendo hilo alilolitenda huyu litatajwa pia kwa kumbukumbu lake." Akitazama siku za usoni, Mwokozi alisema kwa uhakika kuhusu injili yake. Ingehubiriwa katika ulimwengu wote. Na kadiri ambavyo injili ingetawanyika mbali, zawadi ya Mariamu ingemwaga harufu yake nzuri, na mioyo ingebarikiwa kwa njia ya tendo lake ambalo alilitenda bila kufundishwa na mtu. Falme zingeinuka na kuanguka; majina ya wafalme na mashujaa yangesahauliwa; lakini tendo hili la huyu mwanamke lingedumu katika kurasa za historia takatifu. Mpaka wakati utakapokuwa umekwisha, kile kibweta cha marhamu kitasimulia kisa cha upendo wa Mungu ulio mwingi kwa ajili ya wanadamu.

Tendo la Mariamu lilikuwa katika mkinzano mkubwa na kile ambacho Yuda alitaka kufanya. Ni fundisho kali kiasi gani ambalo Kristo angeweza kumpa yule aliyedondoshea mbegu ya kukosoa na mawazo maovu katika mawazo ya wanafunzi wale! Ni kwa namna gani ambavyo mshtaki huyu angeshtakiwa kwa haki! Yeye asomaye hisia za kila moyo, na kuelewa kila kitendo, angeweza kuwafungulia wale waliokuwa karamuni kurasa za giza katika uzoefu wa Yuda. Unafiki wa uongo ambao ndio ulikuwa msingi wa msaliti huyu ungeweza kuanikwa; maana, badala ya kuwahurumia maskini, alikuwa anawaibia fedha iliyowekwa kwa ajili yao. Hasira ingeweza kuamshwa dhidi yake kwa kumkandamiza mjane, yatima, na wafanyakazi waliokodiwa. Lakini ikiwa Kristo angemfunua Yuda, hili lingetumika kama sababu ya usaliti wake. Na ingawa alituhumiwa kuwa mwizi, Yuda angepata utetezi, hata miongoni mwa wanafunzi. Mwokozi hakumshutumu, na kwa njia hiyo aliepusha kumpa udhuru wa usaliti wake.

Lakini namna Yesu alivyomwangalia Yuda ilimshawishi kusadikishwa kwamba Mwokozi aliupenya unafiki wake, na alisoma moyo wake na tabia yake. Na katika kukubali tendo la Mariamu, ambalo lilikuwa limepingwa vikali, Kristo alikuwa amemkemea Yuda. Kabla ya hili, Mwokozi hakuwa amempa kemeo la moja kwa moja. Sasa kemeo lile lilimwumiza Yuda moyoni mwake. Aliazimia kwamba tendo hilo lilipiziwe kisasi. Kutoka katika karamu hii alienda moja kwa moja kwa **(564)** jumba la kuhani mkuu, mahali alipokuta baraza limekutana, na aliahidi kumsaliti Yesu mikononi mwao.

Makuhani walifurahi sana. Viongozi hawa wa Israeli walikuwa wamepewa fursa ya upendeleo ya kumpokea Kristo kama Mwokozi wao, bila fedha wala malipo. Lakini waliikataa zawadi hii ya thamani iliyotolewa kwao katika roho ya upendo usio na mpaka. Walikataa kuupokea huo wokovu ambao una thamani kubwa kuliko dhahabu, na wakamnunua Bwana kwa vipande thelathini tu vya fedha.

Yuda alijifurahisha katika ulafi wa mali mpaka tabia hiyo ikaishinda kila sifa nzuri ya tabia yake. Aliona kinyongo kwa zawadi iliyotolewa kwa Yesu. Moyo wake uliwaka kwa wivu kwamba Mwokozi amepata zawadi ya thamani

inayostahili wafalme wa dunia. Alimkana Bwana kwa kiasi cha fedha ambacho kwa mbali sana ni pungufu ya kile kibweta cha marhamu.

Wanafunzi hawakuwa kama Yuda. Walimpenda Mwokozi. Lakini hawakukubali ile hali ya kukwezwa kwake kiasi kile. Laiti wangegundua alichokuwa ametenda kwa ajili yao, wangeona kwamba hakuna kilichotolewa kwake ambacho kilikuwa kimetumika vibaya. Wale mamajusi kutoka Mashariki, ambao walijua kidogo sana kuhusu Yesu, walikuwa wameonyesha kutambua kwa kweli heshima aliyostahili. Walileta zawadi za thamani kwa Mwokozi, na walimsujudia kwa heshima hata alipokuwa bado mtoto mchanga, aliyelala katika hori la ng'ombe.

Kristo anathamini matendo ya upole wa moyoni. Mtu yeyote alipomfanyia ukarimu kwa upole wa kimbingu alimbariki. Hakukataa ua dogo lililochumwa na mkono wa mtoto, na likatolewa kwake kwa upendo. Alikubali zawadi za watoto, na kuwabariki watoaji hao, huku akiandika majina yao katika kitabu cha uzima. Katika Maandiko, kitendo cha Mariamu kumpaka mafuta Yesu kinatajwa kikimtofautisha na akina Mariamu wengine. Matendo ya upendo na heshima kwa Yesu ni ushahidi wa kuwa na imani kwake Yeye kama Mwana wa Mungu. Na Roho Mtakatifu anasema kuhusu wanawake, kama ushuhuda wa heshima ya upendo ya mwanamke: "Ikiwa amewaosha watakatifu miguu, ikiwa amewasaidia wateswao, ikiwa amefuata kwa bidii kila tendo jema." 1 Timotheo 5:10.

Kristo aliifurahia hamu ya Mariamu kuyafanya yaliyo mapenzi ya Bwana wake. Alikubali utajiri wa upendo safi ambao wanafunzi wake hawakuelewa, wasingeelewa. Ile hamu ya Mariamu kufanya huduma ile kwa Bwana wake, kwa Kristo ilikuwa ya thamani kubwa zaidi ya marhamu zote za thamani zilizomo ulimwenguni, kwa sababu ilidhihirisha ukubali wake wa Mkombozi wa ulimwengu. Upendo wa Kristo ndio uliomsukuma. Tabia njema ya Kristo isiyofananishwa na chochote ndiyo iliyomjaa moyoni. Yale marhamu yalikuwa alama tu ya moyo wa mtoaji. Yalikuwa ni udhihirisho wa nje wa upendo uliojazwa na vijito vya mbinguni mpaka vikafurika.

**(565)** Ile kazi ya Mariamu ilikuwa ni somo ambalo wale wanafunzi walihitaji liwaonyeshe kwamba kuonyesha upendo wao kwa Kristo kungekuwa jambo la kumpendeza. Alikuwa kila kitu kwao, na hawakugundua kwamba muda si mrefu wangeondoshewa uwepo wake, kwamba muda si mrefu wasingeweza kumpa zawadi zao za shukrani kwa upendo wake mkuu. Upweke wa Kristo, akiwa ametenganishwa na mbingu, akiishi maisha ya kibinadamu, haukuelewa daima wala kutambuliwa na wanafunzi kwa namna ambavyo ilistahili kuwa. Mara nyingi alihuzunika kwa sababu wanafunzi wake hawakumpa kile alichostahili kupokea kutoka kwao. Alijua kwamba kama walikuwa chini ya ushawishi wa wale malaika wa mbinguni walioandamana naye, wao pia wasingefikiria kupata zawadi yenye thamani ya kutosha kutangaza upendo wa kiroho wa moyoni.

Uelewa waliopata hapo uliwapa utambuzi wa kweli kuhusu vitu vingi ambavyo wangepaswa kumfanyia Yesu kudhihirisha upendo na shukrani za mioyo yao, wakati ule walipokuwa karibu yake. Wakati Yesu alipokuwa hayuko pamoja nao tena, na wakajihisi kama kondoo wasio na mchungaji, walianza kuona jinsi ambavyo walipaswa kumwonyesha hali ya kujali ambayo ingemletea furaha ya moyo wake. Hawakurusha lawama kwa Mariamu tena, bali walijirushia lawama wao wenyewe. Oo! Laiti ingewezekana kurudisha maisha nyuma na kuondoa kitendo chao cha kupinga, na kuchukulia kwamba maskini wanastahili zawadi ile zaidi kuliko Kristo! Walihisi hatia sana wakati walipoushusha kutoka msalabani mwili wa Bwana wao uliochubuliwa.

Mapungufu yale yale yanadhihirika katika ulimwengu wetu leo. Ni wachache tu wanaotambua vile Kristo alivyo kwao. Kama watu wangalifanya kwa kudhihirisha upendo mkubwa wa Mariamu, kitendo cha kupaka mafuta kingefanywa bure. Marhamu ya thamani kubwa yasingeitwa matumizi mabaya. Hakuna kitu ambacho kingedhaniwa kuwa cha gharama kubwa kiasi kwamba hakiwezi kutolewa kwa ajili ya Kristo, hakuna kujikana au kujitoa kafara ambako ni kukubwa sana kiasi kwamba hakuwezi kustahimiliwa kwa ajili yake.

Maneno ya kupinga yaliyosemwa kwamba, "Ni wa nini upotevu huu?" yalileta machoni pa Kristo kafara kubwa mno ambayo haijawahi kutolewa, - zawadi ya Yeye mwenyewe kama mpatanishi wa ulimwengu uliopotea. Bwana alikuwa awe mkarimu sana kwa jamii ya wanadamu kiasi kwamba hakuna ambaye angedai kwamba angefanya zaidi ya pale. Katika zawadi ile ya Yesu, Mungu aliitoa mbingu yote. Kutoka katika mtazamo wa kibinadamu, kujitoa kiasi hicho ilikuwa ni upotevu mkubwa. Kwa mujibu wa akili ya mwanadamu, mpango mzima wa wokovu ni matumizi mabaya ya wema na rasilimali. Katika hiyo kila mahali tunakutana na hali ya kujitoa na kujikana kwa moyo. Kweli jeshi la mbinguni linaweza kuiangalia kwa mshangao sana jamii ya

wanadamu inapokataa kuinuliwa na kujazwa upendo usio na kikomo unaodhihirishwa na Kristo. Kweli nao wangesema kwa mshangao kwamba, Ni wa nini upotevu huu?

Lakini upatanisho kwa ajili ya ulimwengu uliopotea ulitakiwa uwe uliojaa, mwingi, na **(566)** uliokamilika. Sadaka ya Kristo ilikuwa nyingi kupitiliza kiasi cha kumfikia kila mtu aliyeumbwa na Mungu. Haikutolewa kwa kiasi kisichozidi idadi ya wale ambao wangeipokea Zawadi hiyo. Si wanadamu wote ambao wameokolewa; lakini bado mpango wa ukombozi si upotevu eti kwa sababu haukamilishi mambo yote ambayo uhuru wake umetoa fursa ya kuyakamilisha. Lazima yawe ya kutosha na kubaki.

Simoni mwenyeji alikuwa ameshawishiwa na ukosoaji ule wa Yuda kuhusu zawadi ya Mariamu, na alishangazwa na mwelekeo wa Yesu kuhusu hilo. Kiburi chake cha Kifarisayo kilihukumiwa. Alijua kwamba wengi wa wageni wake walikuwa wanamwangalia Kristo kwa kutomwamini na kupendezwa. Simoni akasema moyoni mwake, "Mtu huyu kama angekuwa nabii, angemtambua mwanamke huyu amgusaye, ni nani, naye ni wa namna gani, ya kwamba ni mwenye dhambi."

Kwa kumponya Simoni ukoma, Kristo alikuwa amemponya mauti inayoishi. Lakini sasa Simoni alihoji kama Mwokozi alikuwa nabii. Kwa kuwa Kristo alimruhusu mwanamke huyu kumkaribia, kwa sababu hakumkataa kwa hasira kama mtu ambaye dhambi zake zilikuwa kubwa kiasi cha kutosameheka, kwa sababu hakuonyesha kwamba anatambua kwamba Mariamu alikuwa ameanguka, Simoni alijaribiwa kufikiri kwamba Kristo alikuwa siyo nabii. Alifikiri kwamba, Yesu hajui lolote kuhusu mwanamke huyu ambaye hana nidhamu katika matendo yake, la sivyo asingemruhusu amguse.

Lakini kilichomsukuma Simoni kufikiri hivyo alivyofikiri ni ujinga wake kuhusu Mungu na kuhusu Kristo. Hakutambua kwamba lazima Mwana wa Mungu atende katika njia ya Mungu, kwa huruma, upendo na wema. Njia ya Simoni haikutakiwa kuacha kutambua huduma ya Mariamu ya kuungama. Tendo lake la kubusu miguu ya Yesu na kuipaka marhamu ilikasirisha moyo wa Simoni uliokuwa mgumu. Alidhani kwamba ikiwa Kristo alikuwa nabii, angegundua wadhambi na kuwakemea.

Yesu aliyajibu mawazo hayo ambayo hayakusemwa kwa maneno: "Simoni, nina neno nitakalo kukuambia. . . . Mtu mmoja mkopeshaji alikuwa na wadeni wawili; mmoja amwia dinari mia tano, na wa pili hamsini. Nao walipokuwa hawana cha kumlipa, aliwasamehe wote wawili. Katika hao wawili ni yupi atakayempenda zaidi? Simoni akajibu akasema, Nadhani ni yule ambaye alimsamehe nyingi. Akamwambia, Umeamua haki."

Kama Nathani alivyofanya na Daudi, Kristo alisitiri ukali wa maneno ndani ya mfano. Alimrushia mwenyeji wake yule kazi ya kujitamkia hukumu yake mwenyewe. Simoni alikuwa ndiye aliyemsukumia dhambini mwanamke yule ambaye sasa alikuwa anamdharau. Mwanamke yule alikuwa amekoseshwa na Simoni kwa kiwango kikubwa. Simoni na mwanamke yule waliwakilishwa na wadeni wale wawili waliotajwa katika mfano ule. Yesu hakupanga kufundisha kwamba wale watu wawili wajione katika viwango tofauti **(567)** vya kuwajibika, maana kila mmoja alidaiwa shukrani ambayo kamwe isingelipiwa. Lakini Simoni alijiona mwenye haki zaidi kuliko Mariamu, na Yesu alitamani Simoni aone ni kiasi gani hasa alivyokuwa na hatia. Alitaka kumwonyesha kwamba dhambi yake yeye ni kubwa kuliko ya mwanamke yule, kubwa sana kama deni la dinari mia tano linavyozidi la dinari hamsini.

Sasa Simoni alianza kujiona katika nuru mpya. Aliona jinsi Mariamu alivyoonwa na Yeye aliyekuwa zaidi ya nabii. Aliona kwamba Kristo alisoma moyo wa Mariamu wa upendo na kujitoa. Alitekewa kwa aibu, na aligundua kwamba alikuwa mbele ya Yeye aliye mkuu kuliko yeye.

Yesu akaendelea, "Niliingia nyumbani kwako, hukunipa maji kwa miguu yangu;" bali Mariamu ameosha miguu yangu kwa machozi ya toba, akisukumwa na upendo, na kuipangusa kwa nywele za kichwa chake. "Wewe hukunibusu; lakini huyu" mwanamke, ambaye unamdharau, "tangu nilipoingia hakuacha kunibusu sana miguu yangu." Kristo alihesabu tena fursa ambazo Simoni alikuwa nazo za kuonyesha upendo kwa ajili ya Bwana wake, na kutambua kile ambacho kilikuwa kimefanywa kwa ajili yake. Kwa uwazi, lakini kwa upole wa tahadhari, Mwokozi aliwahakikishia wanafunzi wake kwamba moyo wake unahuzunika pindi watoto wake wanapoacha kuonyesha shukrani zao kwake kwa maneno na matendo ya upendo.

Mpelelezi wa Moyo alisoma msukumo uliosababisha kitendo kile cha Mariamu, na aliona pia roho iliyomsukuma Simoni kusema maneno aliyosema. Akasema, "Wamwona mwanamke huyu?" Ni mwenye dhambi. "Nakuambia, Amesamehewa dhambi zake ambazo ni nyingi, kwa kuwa amependa sana; lakini asamehewaye kidogo, huyo hupenda kidogo."

Ubaridi na kupuuza kwa Simoni kwa Mwokozi vilionyesha jinsi alivyotambua kidogo tu wema aliokuwa amepokea. Alikuwa amedhani kwamba anamheshimu Yesu kwa kitendo cha kumwalika nyumbani kwake. Lakini sasa alijiona vile alivyokuwa hasa. Wakati yeye alidhani kwamba anamsoma Mgeni wake, Mgeni wake ndiye aliyekuwa anamsoma yeye. Aliona jinsi hukumu ya Kristo kwake ilivyokuwa ya kweli. Dini yake ilikuwa ni kanzu ya Ufarisayo. Alikuwa amedharau huruma ya Yesu. Hakuwa amemtambua kama mwakilishi wa Mungu. Wakati Mariamu alikuwa ni mwenye dhambi aliyesamehewa, yeye alikuwa mwenye dhambi ambaye hajasamehewa. Kanuni ngumu ya haki aliyotaka kuisimamia dhidi ya Mariamu ilimhukumu yeye mwenyewe.

Simoni aliguswa na wema wa Yesu kwa kuacha kumkemea waziwazi mbele ya wageni. Hakuwa ametendewa vile alivyotaka Mariamu atendewe. Aliona kwamba Yesu hakutaka kufunua hatia yake kwa watu, lakini alitafuta kushawishi mawazo yake kwa kutumia kauli za kweli, na alitumia upendo wa wema kuutiisha moyo wake. Kumhukumu sana kwa waziwazi kungeufanya moyo wake kuwa mgumu asiungame, bali kemeo la upole lilimshawishi **(568)** kujutia kosa lake. Aliuona ukubwa wa deni alilodaiwa na Bwana wake. Kiburi chake kilishushwa, akatubu, na Farisayo yule mwenye kiburi akawa mwanafunzi mwenye kujishusha na kujikana nafsi.

Mariamu alikuwa ameonekana kama mwenye dhambi mkubwa, lakini Kristo alijua mazingira ambayo yalikuwa yameyafanya maisha yake kuwa vile. Angeweza kuamua kuzima kila cheche za matumaini ndani ya moyo wa mwanamke huyu, lakini hakufanya hivyo. Ni Yeye aliyekuwa amemwinua kutoka katika hali ya kukosa tumaini na kuangamia. Mariamu alikuwa amesikia mara saba Yesu akikemea mapepo yaliyotawala moyo wake na akili yake. Alikuwa amesikia kilio cha Yesu cha nguvu kwa Baba yake kwa niaba yake. Alijua jinsi dhambi inavyochafua usafi wa Yesu ambao hauna doa, na Mariamu alikuwa ameshinda kwa nguvu ya Yesu.

Wakati hali yake ilipoonekana haina matumaini kwa mtazamo wa mwanadamu, Kristo aliona ndani ya Mariamu uwezo wa kutenda mema. Aliona sifa njema zaidi za tabia yake. Mpango wa ukombozi umewekeza kwa mwanadamu uwezekano mkubwa, na uwezekano huu ulikuwa uwe halisi ndani ya Mariamu. Kwa neema ya Kristo Mariamu akawa mshirika wa hali ya uungu. Yeye aliyekuwa ameanguka, na ambaye akili yake ilikuwa makao ya mapepo, aliletwa karibu sana na Mwokozi katika ushirika na huduma. Ni Mariamu aliyekaa miguuni pa Kristo na kujifunza habari zake. Ni Mariamu aliyemimina kichwani kwa Kristo mafuta, na kuosha miguu yake kwa machozi. Mariamu alisimama karibu na msalaba, na kumfuata Kristo alipopelekwa kaburini. Mariamu alikuwa wa kwanza kufika kaburini baada ya Kristo kufufuka. Ni Mariamu aliyekuwa wa kwanza kumtangaza Mwokozi aliyefufuka.

Yesu anajua mazingira ya kila mtu. Unaweza kusema kwamba, Mimi ni mdhambi, mdhambi sana. Unaweza kuwa; lakini kadiri unavyokuwa mbaya zaidi, ndivyo unavyomhitaji zaidi Yesu. Hamfukuzii mbali mtu mwenye toba anayelia. Hamwambii mtu yeyote mambo yote ambayo angefunua kwa watu, bali anamtaka kila mtu anayetetemeka kuwa na moyo mkuu. Atawasamehe bure wote wamjiao wakitafuta masamaha wake na kurejeshwa.

Kristo angeweza kuwaagiza malaika wa mbinguni wamimine vikombe vya hasira yake katika ulimwengu wetu, ili kuwaharibu wale waliojawa na chuki kwa Mungu. Angeweza kufutilia mbali hili doa moja la giza kutoka katika malimwengu yake. Lakini hafanyi hivyo. Leo amesimama kwenye madhabahu ya uvumba, akiwasilisha kwa Mungu maombi ya wale wanaotaka msaada wake.

Watu wanapomgeukia Yeye kutafuta kimbilio, Yesu anainua juu mashtaka na upinzani wanaofanyiwa. Hakuna mwanadamu wala malaika mwovu anayeweza kuwashtaki watu hao. Kristo huwaunganisha na hali yake ya uungu-ubinadamu. Wanasimama karibu na huyu Mbeba Dhambi mkuu, katika nuru inayotoka kwenye kiti cha enzi cha Mungu. "Ni nani atakayewashtaki wateule wa Mungu? Mungu ndiye mwenye kuwahesabia haki. Ni nani atakayewahukumia adhabu? Kristo Yesu ndiye aliyekufa; naam, na zaidi ya hayo, amefufuka katika wafu, naye yuko mkono wa kuume wa Mungu; tena ndiye anayetuombea." Warumi 8:33, 34.

## Sura ya 63

# "Mfalme Wako Anakuja"

[Sura hii imejengwa katika Mathayo 21:1-11; Marko 11:1-10; Luka 19:29-44; Yohana 12:12-19.]

"Furahi sana, Ee binti Sayuni; Piga kelele, Ee binti Yerusalemu; Tazama, mfalme wako anakuja kwako; Ni mwenye haki, naye ana wokovu; Ni mnyenyekevu, amepanda punda, Naam, mwana-punda, mtoto wa punda." Zekaria 9:9.

Miaka mia tano kabla ya kuzaliwa kwa Kristo, nabii Zekaria alitabiri hivyo kuhusu kuja kwa Mfalme wa Israeli. Unabii huu unataka sasa utimizwe. Yeye ambaye kwa muda mrefu amekataa heshima ya kifalme sasa anakuja Yerusalemu akiwa kama mrithi aliyeahidiwa wa kiti cha enzi cha Daudi.

Ilikuwa siku ya kwanza ya juma wakati Yesu alipoingia Yerusalemu kwa ushindi. Makutano waliokuwa wameenda Bethania kumwona sasa waliandamana naye, wakiwa na hamu ya kushuhudia mapokezi yake. Watu wengi walikuwa njiani wakielekea katika jiji lile ili kusherehekea Pasaka, na hawa waliungana na umati unaoandamana na Yesu. Viumbe vyote vya asili vilionekana kama vinashangilia. Miti ilikuwa imevishwa ukijani, na maua ya miti hiyo yalimwaga harufu nzuri hewani. Maisha mapya na ya furaha yalijaza watu. Tumaini la ufalme mpya lilibubujika tena.

Akikusudia kupanda punda wakati wa kuingia Yerusalemu, Yesu alikuwa amewatuma wawili miongoni mwa wanafunzi wake kuleta punda na mwana-punda wake. Wakati wa kuzaliwa kwake Mwokozi alikuwa tegemezi kwa ukarimu wa wageni. Lile hori la ng'ombe alimolala lilikuwa limeazimwa ili liwe mahali pa kupumzikia. Na sasa, ingawa wanyama wa kufugwa walio kwenye maelfu ya milima ni wake, anakuwa tegemezi kwa ukarimu wa mgeni ili kupata mnyama **(570)** wa kupanda anapoingia Yerusalemu akiwa kama mfalme. Lakini kwa mara nyingine tena uungu unafunuliwa, hata katika maelekezo madogo aliyowapa wanafunzi wake katika safari hii fupi. Kama alivyotabiri, ombi lake kwamba, "Bwana anawahitaji," lilikubaliwa kwa utayari. Yesu alichagua kutumia mwana-punda ambaye hajatumiwa na mtu yeyote. Wale wanafunzi, wakiwa na udadisi wa furaha, walitandika nguo zao juu ya yule mnyama, na wakamkalisha Bwana wao juu ya yule mnyama. Kabla ya wakati huu Yesu alitembea mara zote kwa mguu, na wanafunzi wake walishangaa kwamba sasa alichagua kupanda mnyama. Lakini matumaini yaliwajaa mioyoni mwao kwa mawazo ya furaha kwamba alikuwa anataka kuingia katika mji mkuu, kujitangaza kuwa mfalme, na kutangaza mamlaka yake ya kifalme. Wakiwa katika msafara ule waliyasema matarajio yao mema wakiwaambia rafiki za Yesu, na msisimko ulitawanyika mbali na karibu, ukipaisha matarajio ya watu hadi vilele vya juu mno.

Kristo alikuwa anafuata desturi za Kiyahudi za uingiaji wa mfalme. Mnyama aliyekuwa amempanda alikuwa yule anayepandwa na wafalme wa Israeli, na unabii ulikuwa umetabiri kwamba hivyo ndivyo Masihi atakavyokuja katika ufalme wake. Haukupita muda baada ya kupanda yule mwana-punda kelele za shangwe zikalipasua anga. Umati alimsifu kwa shangwe kwamba ndiye Masihi, mfalme wao. Kwa sasa Yesu aliiruhusu heshima ambayo kabla alikuwa haruhusu, na wanafunzi walipokea hali hii kama ushahidi kwamba matumaini yao ya furaha kumwona Yesu akitawazwa kwenye kiti cha enzi yangekuwa halisi. Makutano walishawishika kuamini kwamba ile saa ya kuwekwa kwao huru ilikuwa imekaribia. Katika mawazo yao waliona majeshi ya Kirumi yakifukuzwa kutoka Yerusalemu, na Israeli ikiwa taifa huru tena. Wote walikuwa na furaha na mwamko; watu walishindana katika kuonyesha heshima kwake. Hawakuweza kuonyesha mandhari ya maonyesho ya kuonekana, lakini walimpa ibada ya mioyo yenye furaha. Hawakuwa na uwezo wa kumpa zawadi za gharama, bali walitandika mavazi yao yakawa kama zulia katika njia yake, na walitandika pia majani ya matawi ya mitende njiani mwake. Waliuongoza msafara wa ushindi bila kuwa na viwango vya kifalme, bali walikata matawi makubwa ya mitende, kama nembo ya ushindi wa Asili, na kuyapepea wakiimba hosana.

Kadiri walivyosonga mbele, ndivyo umati ulivyoendelea kuongezeka kwa sababu ya ujio wa wengine waliosikia habari za kuja kwake nao wakaharakisha kujiunga na msafara. Watazamaji waliendelea kujichanganya na msafara, huku wakiuliza, Ni nani huyu? Madhari hii ya msafara ina maana gani? Wote walikuwa wameshasikia habari za Yesu, na walitarajia kwamba angeenda Yerusalemu; lakini walijua kwamba kabla ya hapo alikataa

jitihada zote za kumtawaza kama mfalme, na walishangazwa sana kuona kwamba huyu alikuwa ni Yeye. Walishangaa kwamba ni nini kimembadilisha huyu aliyesema kwamba ufalme wake si wa ulimwengu huu.

**(571)** Maswali yao yananyamazishwa na kelele za furaha. Tena na tena kelele hizo zinarudiwa na msafara ule, zinaitikiwa na watu walio mbali na pale, na kutoa mwangwi katika milima na mabonde. Na sasa msafara ule unaungana na makundi ya watu kutoka Yerusalemu. Kutokana na makutano waliokusanyika kusherehekea Pasaka, maelfu wanaenda kumlaki Yesu. Wanamsalimu kwa kutumia matawi ya mitende yanayopepea na mlipuko wa wimbo mtakatifu. Makuhani walioko hekaluni wanapiga baragumu ya kuita watu kwenye ibada ya jioni, lakini inaitikiwa na watu wachache, ndipo wakuu wale wanasemezana wao kwa wao kwa wasiwasi kwamba, "Ulimwengu umekwenda nyuma yake."

Katika maisha yake ya duniani Yesu hakuwahi kamwe kuruhusu mandhari kama hii. Aliona kwa uwazi matokeo yake. Yangemleta msalabani. Lakini lilikuwa kusudi lake kwamba ajionyeshe hadharani kwamba Yeye ni Mwokozi. Alitaka kuvuta hisia kuzielekeza kwenye kafara ambayo ingefunika kazi yake kwa ulimwengu ulioanguka. Wakati watu wakikusanyika Yerusalemu kusherehekea Pasaka, Yeye, aliye Mwana-kondoo halisi, alijitoa kwa hiari kuwa sadaka. Ingehitajika kwa kanisa lake katika zama zote ambazo zingefuata kukifanya kifo chake kwa ajili ya dhambi kuwa somo la kutafakari kwa kina na kujifunza. Kila jambo linalohusianishwa na kifo hicho linapaswa kuhakikishwa pasipo kuacha shaka. Wakati huo ilikuwa lazima kwamba macho ya watu yaelekezwe kwake; lazima matukio yaliyotangulia kafara yake kuu yawe yale ya kuvuta kuelekeza kwenye kafara yenyewe. Baada ya maandamano yale yaliyoambatana naye wakati wa kuingia Yerusalemu, macho yote yangefuata njia yake kuelekea kwenye lile tukio kuu.

Matukio yaliyoungana na kuingia huku kwa shangwe yangekuwa mazungumzo ya kila ulimi, na yangemleta Yesu mbele ya kila mawazo. Baada ya kusulibiwa kwake, wengi wangekumbuka matukio haya katika kuyahusianisha na kuteswa na kifo chake. Wangeongozwa kujifunza unabii, na wangeshawishika kwamba Yesu alikuwa Masihi; na waongofu wa imani hii wangeongezeka na kuzidi katika nchi zote.

Katika mandhari hii ya shangwe katika maisha yake ya duniani, Yesu angeweza kujitokeza akisindikizwa na malaika wa mbinguni, huku akitangulia na parapanda ya Mungu; lakini maonyesho hayo yangekuwa kinyume na kusudi la kazi yake, kinyume na sheria iliyokuwa inatawala maisha yake. Alibaki kuwa wa kweli katika fungu la wanyenyekevu alilokuwa amekubali. Lazima abebe mzigo wa ubinadamu mpaka maisha yake yake yalipotolewa kwa ajili ya uzima wa ulimwengu.

Siku hii, iliyoonekana kwa wanafunzi kama siku iliyotukuka katika maisha yao, ingekuwa imefunikwa na kivuli cha mawingu ya huzuni ikiwa wangejua kwamba madhari ya tukio hili la kufurahisha ilikuwa ni utangulizi tu wa mateso na kifo cha Bwana wao. Ingawa alikuwa amewaambia tena na tena kuhusu **(572)** kafara yake ya hakika, katika shangwe zao za furaha walisahau maneno yake ya huzuni, nao wakatarajia ustawi wa kutawazwa kwake kwenye kiti cha enzi cha Daudi.

Watu wengine wapya waliendelea kuungana na msafara ule, na wote waliojiunga nao, isipokuwa wachache, walipatwa na msisimko uliokuwepo, na walisaidia kupanua zaidi shangwe za hosana zilizotoa mwangwi kutoka kilima hadi kilima na bonde hadi bonde. Sauti za shangwe ziliendelea kuwa juu kwa muda zikiimba, "Hosana, Mwana wa Daudi; ndiye mbarikiwa, yeye ajaye kwa jina la Bwana; Hosana juu mbinguni."

Kamwe ulimwengu haukupata kuona kabla msafara wa shangwe kama ule. Haukuwa kama ule wa washindi mashuhuri wa vita za kidunia. Katika tukio hili hakukuwa na msururu wa mateka waombolezao, wakiwa kama nyara za vita za kuashiria ushindi wa mfalme. Bali katika pande zote za Mwokozi kulikuwa na nyara za utukufu wa kazi zake za upendo kwa ajili ya mwanadamu mwenye dhambi. Kulikuwa na mateka ambao aliwaokoa kutoka katika nguvu za Shetani, wakimtukuza Mungu kwa kuwaponya. Wale vipofu aliokuwa amewarejeshea kuona walikuwa wanaongoza njia. Mabubu ambao alikuwa amefungua ndimi zao walikuwa wanaimba hosana kwa sauti kubwa zaidi. Viwete ambao alikuwa amewaponya walikuwa wakitembea kwa kuruka wakiwa na furaha, na ndio walioongoza katika kuvunja matawi ya mitende na kuipepea kwa Mwokozi. Wajane na yatima walikuwa wanalitukuza jina la Yesu kwa sababu ya kazi zake za huruma kwao. Wenye ukoma ambao alikuwa amewatakasa walitandika nguo zao zisizo na unajisi katika njia yake, na walimtukuza kama Mfalme wa utukufu. Wale ambao sauti yake ilikuwa imewaamsha kutoka katika usingizi wa mauti walikuwemo katika msafara ule.

Lazaro, yule ambaye mwili wake ulikuwa umeshaharibikia kaburini, lakini ambaye sasa alikuwa anashangilia akiwa na nguvu, ndiye aliyemtangulia yule punda aliyekuwa amepandwa na Mwokozi.

Mafarisayo wengi walishuhudia tukio hili, nao, wakijawa na wivu na chuki, walitafuta namna ya kubadilisha hisia za watu. Kwa kutumia mamlaka yao yote walijaribu kunyamazisha watu, lakini kusihi kwao na vitisho vyao viliishia tu kuongeza hali ya udadisi kwa watu. Wao walihofu kwamba umati huu, kwa nguvu ya wingi wao, wangeweza kumsimika Yesu kuwa mfalme. Kama juhudi zao za mwisho walipenya kwa nguvu katika umati mpaka mahali Mwokozi alipokuwa, na wakamkabili kwa makemeo na vitisho wakisema, "Mwalimu, uwakanye wanafunzi wako." Walitangaza kwamba maandamano yale yalikuwa kinyume cha sheria, na kwamba yasingeruhusiwa na mamlaka husika. Lakini walinyamazishwa na jibu la Yesu kwamba, "Nawaambia ninyi, wakinyamaza hawa, mawe yatapiga kelele." Tukio lile la shangwe za ushindi lilikuwa limeamuriwa na Mungu mwenyewe. Lilikuwa limetabiriwa na nabii, na mwanadamu hakuwa na nguvu ya kugeuzia kando kusudi la Mungu. Ikiwa wanadamu wangeshindwa kutekeleza mpango wake, angeyapa mawe yaliyowezeshwa sauti, nayo yangemsifu Mwana wake kwa sifa. Wale Mafarisayo walionyamazishwa **(575)** waliorudi nyuma, maneno ya Zekaria yalichukuliwa na kuimbwa na mamia ya sauti: "Furahi sana, Ee binti Sayuni; Piga kelele, Ee binti Yerusalemu; Tazama, mfalme wako anakuja kwako; Ni mwenye haki, naye ana wokovu; Ni mnyenyekevu, amepanda punda, Naam, mwana-punda, mtoto wa punda."

Ule msafara ulipofika pale kwenye kilele cha mlima, ukiwa tayari kushuka jijini, Yesu aliusimamisha pamoja naye. Mbele yao ilikuwepo Yerusalemu ikiwa katika utukufu wake, sasa ikiwa imeoshwa kwa mng'ao wa nuru ya jua linalozama. Hekalu lake lilivutia macho ya wote. Kwa uzuri na ukubwa wake lilipanda juu zaidi kuliko kitu kingine chochote, likionekana kugusa mbinguni kama vile inawaelekeza watu wote kwake aliye Mungu wa kweli aliye hai. Kwa muda mrefu hekalu lile lilikuwa fahari na utukufu wa taifa la Wayahudi. Warumi nao pia waliona fahari kwa uzuri wa hekalu lile. Mfalme aliyeteuliwa na Warumi alikuwa ameungana na Wayahudi kulijenga na kulipamba, na mfalme mkuu wa Roma alikuwa amelijaza vitu vyake vya thamani. Uimara wake, utajiri, na fahari yake vilikuwa vimelifanya kuwa moja ya maajabu ya ulimwengu.

Jua la magharibi lilipokuwa likiangaza na kuzing'arisha mbingu, utukufu wa hekalu lile uliangaza kwa marumaru nyeupe za ukuta wake, na kumetametesha nguzo zake za dhahabu. Kutokea kwenye kilele cha kilima kile pale Yesu na wanafunzi wake walipokuwa, hekalu lile lilikuwa na mwonekano kama wa jengo kubwa la theluji, lililowekewa juu yake mnara wa dhahabu. Mahali pa kuingilia hekalu kulikuwa na mzabibu wa dhahabu na fedha, ukiwa na majani ya kijani na vichala vikubwa vya zabibu vikiwa vilivyotengenezwa na msanii mwenye ufundi mkubwa sana. Ishara hii iliwakilisha Israeli aliyekuwa kama mzabibu wenye kustawi. Ile dhahabu, fedha, na kijani vilipangwa kwa mchanganyiko wa kuvutia kwa ubunifu adimu wa kazi nzuri ya fundi stadi; kadiri mmea huu ulivyoviringishwa karibu na zile nguzo nyeupe zimeremetazo, ukining'inia kwenye fito za kuutegemeza zing'aazo kwa sababu ya mafuta ya dhahabu ziliyopakwa, hekalu lile lilinasa mwako wa jua linalotua, liking'aa kama vile kwa utukufu ulioazimwa kutoka mbinguni.

Yesu aliitazama mandhari ile, na umati ule mkubwa ukakoma kutoa kelele za shangwe, wakiduwazwa na mwonekano ule wa uzuri. Macho yote yakaelekezwa kwa Mwokozi, yakitarajia kuona usoni pake mshangao kama ule waliokuwa nao. Lakini badala ya hilo waliona wingu la huzuni. Wanashangazwa na kufadhaishwa kwa kuona macho yake yamejawa na machozi, na mwili wake ukiyumba kwenda mbele na nyuma kama mti ulio katika tufani, huku kilio kikilipuka midomoni mwake, kama kinachotoka katika vina vya moyo uliopasuka. Huu ulikuwa ni mwonekano gani machoni pa malaika! Jemadari wao mpendwa yuko katika shida ya kulia machozi! Huu ulikuwa mwonekano gani kwa msafara uliokuwa na kelele za shangwe na kupepea matawi ya mitende wakati ukimsindikiza katika mji mtukufu, mahali walipodhani kwamba alikuwa anaenda kutawazwa kuwa mfalme! Yesu alikuwa amelia mahali pa kaburi la Lazaro, lakini ilikuwa ni katika **(576)** huzuni ya huruma kwa sababu ya shida za mwanadamu. Lakini huzuni hii ya ghafla ilikuwa kama kilio kibaya katikati ya kibwagizo cha sauti za shangwe. Katikati ya mandhari ya furaha, mahali ambapo watu wote walikuwa wakimtukuza, Mfalme wa Israeli alikuwa akilia machozi; si machozi ya kimya ya furaha, bali machozi ya kulia kwa sauti na maumivu yasiyotulizika. Umati wote ukagubikwa na simanzi ya ghafla. Sauti zao za shangwe zikanyamaza. Wengi walilia kwa kumhurumia wakiwa na huzuni ambazo hawakuweza kupambanua.

Machozi ya Yesu hayakuhusiana na matarajio ya mateso yake yaliyokuwa yanakuja. Mbele yake kidogo tu kulikuwa na Gethsemane, mahali ambapo muda si mrefu tukio baya la giza lingemfunika. Lango la kondoo pia lilikuwa wazi machoni pake, mahali ambapo kondoo wa kafara walikuwa wamepitishwa kwa karne nyingi. Muda si mrefu lango hili lingewekwa wazi kwa ajili yake yeye ambaye, kama Kondoo Halisi mkuu, kafara hizi zilisonda kidole kwake aliye kafara kwa ajili ya dhambi za ulimwengu. Mahali ambapo si mbali ulionekana mlima wa Kalvari, mahali pa yeye kusulibishiwa. Lakini Mwokozi hakulia na kuumia moyo kwa sababu ya kukumbuka kifo hiki cha kikatili. Huzuni yake haikuwa ya binafsi. Kuwazia shida yake mwenyewe hakukuitisha ile nafsi njema yenye kujikana. Mwonekano wa Yerusalemu ndio uliouchoma moyo wa Yesu – Yerusalemu ule uliokuwa umemkataa Mwana wa Mungu na kulikejeli pando lake, ambao ulikataa kushawishiwa na miujiza yake, na sasa ulikuwa unaelekea kuyachukua maisha yake. Aliona jinsi ulivyokuwa katika hatia ya kumkataa Mwokozi wake, na vile ambavyo ungekuwa ikiwa ungempokea Yeye ambaye pekee angeliponya jeraha la mji huo. Alikuwa amekuja kuuokoa; angewezaje kuuacha?

Waisraeli walikuwa watu waliopendelewa; Mungu alikuwa amelifanya hekalu lao kuwa makao yake; Israeli alikuwa "mzuri sana, ni furaha ya dunia yote." Zaburi 48:2. Kumbukumbu ya zaidi ya miaka elfu ya uongozi wa Kristo na upendo wake, kama ule wa baba kwa mtoto wake, ulikuwa pale. Katika hekalu lile manabii walikuwa wametamka maonyo yao ya dhati. Pale chetezo kilikuwa kimepepea, wakati ambapo uvumba, uliochanganyika na maombi ya wanaoabudu, ulikuwa umepanda kwa Mungu. Damu za wanyama zilikuwa zimetiririka pale, zikiwa mfano wa damu ya Kristo. Yehova alikuwa amedhihirisha utukufu wake pale juu ya kiti cha rehema. Makuhani walikuwa wamehudumu pale, na maadhimisho ya kielelezo na sikukuu vilikuwa vimeendelea pale kwa vizazi na vizazi. Lakini lazima haya yote yawe na mwisho.

Yesu aliinua mkono wake, - ule uliokuwa mara nyingi umewabariki wagonjwa na wenye shida, - naye akiupepea kuuelekea mji ule wenye ole, alilia kwa uchungu akisema: "Laiti ungalijua, hata wewe katika siku hii, yapasayo amani!" Yesu alitulia hapo, na akaacha bila kusema kile ambacho kingekuwa hali ya Yerusalemu **(577)** ikiwa ungekubali msaada ambao Mungu alitamani kuupa, - zawadi ya Mwana wake mpendwa. Ikiwa Yerusalemu ungejua kile ambacho ulitakiwa kujua, kuitii nuru ile ambayo Mbingu ilikuwa imeuletea, ungeendelea kusimama katika fahari na ustawi wake, kama malkia wa falme, ukiwa huru katika uimara wa nguvu ulizopewa na Mungu. Kusingekuwa na askari wenye silaha ambao wangesimama katika malango yake, wala kusingekuwa na bendera za Warumi za kupepea kwenye kuta za mji huo. Hatima tukufu ambayo ingeubariki mji wa Yerusalemu ikiwa ungempokea Mwokozi wake iliinuka machoni pa Mwana wa Mungu. Aliona kwamba kupitia kwake huenda mji ule ungeponywa na taabu yake ya huzuni, ukawekwa huru kutoka utumwani, na kusimamishwa kama mji mkuu wa dunia. Hua wa amani angeruka kwenda katika mataifa yote kutokea katika kuta za mji huu. Ungekuwa mji wa utukufu wa ulimwengu.

Lakini picha njema hiyo ambayo Yesu alikuwa nayo kuhusu Yerusalemu inafutika machoni pake. Anaona uhalisia wa hali ya mji huo kwamba uko chini ya kongwa la Warumi, ukibeba hasira ya Mungu, ukipata mapigo ya hukumu yake. Anaendelea kulia akisema: "Lakini sasa yamefichwa machoni pako. Kwa kuwa siku zitakuja, adui zako watakapokujengea boma, likuzunguke; watakuzingira na kukuhusuru pande zote; watakuangusha chini wewe na watoto wako ndani yako, wasikuachie jiwe juu ya jiwe, kwa sababu hukutambua majira ya kujiliwa kwako."

Kristo alikuja kumwokoa Yerusalemu pamoja na watoto wake; lakini kiburi cha Kifarisayo, unafiki, wivu, nia ya kudhuru vilikuwa vimemzuia kukamilisha kusudi lake. Yesu alijua ole za kutisha ambazo zingeujilia mji ule. Aliona Yerusalemu ukiwa umezingirwa na majeshi, watu wa mji waliohusuriwa wakiwekwa katika hali ya njaa kubwa na kifo, wamama wakila miili ya watoto wao waliokufa, na wazazi na watoto wakinyang'anyana chakula kidogo kilichosalia, upendo wa asili wa mahusiano ya damu ukiharibiwa na baa la njaa. Aliona kwamba usumbufu wa Wayahudi, kama ulivyoonyeshwa katika kukataa kwao wokovu wa Kristo, ungewafanya pia kukataa kujisalimisha kwa majeshi ya kivamizi. Aliiona Kalvari, mahali ambapo angeinuliwa, ukiwa umejawa na misalaba iliyoonekana kama msitu wa miti. Aliwaona wakazi wa mji wakipata mateso kwenye vitanda vya kutesea na kwa kuangikwa misalabani, viwanja vizuri vya majumba ya kifalme vikiharibiwa, hekalu likiwa limeharibiwa, na kuta zake nene zikiwa hazina jiwe lililoachwa juu ya jiwe, huku jiji likiwa limelimwa kama shamba lililosafishwa. Kweli lazima Mwokozi alie kwa maumivu kwa kuona hali hii.

Yerusalemu ulikuwa umekuwa mtoto aliye katika matunzo ya Kristo, na kama vile baba mwenye upendo aombolezavyo kwa mwanae aliyeasi, ndivyo Yesu alivyoulilia mji huu uliopendwa. Nawezaje **(578)** kukuacha? Nawezaje kukuona hivi ukielekea katika uangamivu? Je, nikuache uelekee katika kukijaza kikombe cha uovu wako? Roho moja ni ya thamani sana kiasi kwamba, kwa kulinganishwa nayo, malimwengu yote yalionekana kutokuwa muhimu; lakini sasa hapa kulikuwa na kupotea kwa taifa zima. Wakati ambapo lile jua la magharibi lingekoma kuonekana siku ile, ndipo na siku ya neema kwa Yerusalemu ingekuwa imekoma. Msafara ule ulipokuwa unasimama pale kwenye kilele cha mlima wa Mizeituni, Yerusalemu ulikuwa haujachelewa kutubu. Malaika wa rehema alikuwa ndipo bado anakunja mbawa zake ili kushuka chini kutoka kwenye kiti cha enzi cha dhahabu akiipisha haki na fagio – hukumu iliyokuwa inakuja. Lakini moyo mkuu wa upendo ulikuwa bado unaubembeleza mji wa Yerusalemu, ambao ulikuwa umekataa huruma zake, ukiwa umedharau maonyo yake, na sasa ulikuwa unaenda kuipaka mikono yake doa la damu yake Yesu. Ikiwa Yerusalemu ungetubu, ulikuwa haujachelewa. Wakati ambapo mionzi ya jua linalotua ilikuwa bado inamlika kwenye hekalu, mnara na nguzo zake, je, malaika mwema asingeuongoza mji ule kwenda kwenye upendo wa Mwokozi, na kuepuka hatima yake ya uangamivu? Siku ya rehema ya mji huu mzuri usiokuwa mtakatifu, uliokuwa umewapiga kwa mawe manabii, uliokuwa umemkataa Mwana wa Mungu, uliokuwa unajifungia katika utumwa kwa kutotubu, ilikuwa inapita!

Lakini kwa mara nyingine tena Roho wa Mungu ananena na Yerusalemu. Kabla siku hii kuisha, ushuhuda mwingine unaletwa kwa Kristo. Sauti ya shahidi inainuliwa juu, ikiitikia wito wa unabii wa zamani. Ikiwa Yerusalemu atausikia wito huu, ikiwa atampokea Mwokozi anayeyaingia malango yake, bado anaweza kuokoka.

Taarifa zimewafikia wakuu wa mle Yerusalemu kwamba Yesu anaingia mjini akiwa pamoja na umati mkubwa wa watu. Lakini hawaonyeshi hali ya kumkaribisha Mwana wa Mungu. Kwa hofu wanaenda kumlaki, wakitaraji kutawanya msafara ule. Msafara ulipokaribia kushuka Mlima wa Mizeituni, unakabiliwa na wakuu wale. Wanaulizia kuhusu sababu ya kelele zile. Walipouliza kwamba, "Ni nani huyu?" wanafunzi, wakiwa wamejawa na roho ya uvuvio, wanajibu swali hilo. Kwa nguvu wanaurudia-rudia unabii uliomhusu Kristo, wakisema:

Adamu atawaambia kwamba, Ni uzao wa mwanamke ambao utaponda kichwa cha nyoka. Mwulizeni Ibrahimu, atawaambia kuwa, Ni "Melkizedeki Mfalme wa Salemu," Mfalme wa amani. Mwanzo 14:18. Yakobo atawaambia kwamba, Huyu ni Shilo wa kabila la Yuda. Isaya atawaambia hivi, "Imanueli," "Mshauri wa ajabu, Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele, Mfalme wa amani." Isaya 7:14; 9:6. Yeremia atawaambia kwamba, ni Tawi la Daudi, "Bwana ni haki yetu." Yeremia 23:6. **(579)** Danieli atawaambia kwamba, Yeye ni Masihi. Hosea atawaambia kwamba, Yeye ni "Bwana, Mungu wa majeshi; Bwana ndilo kumbukumbu lake." Hosea 12:5. Yohana Mbatizaji atawaambia kwamba, Yeye ni "Mwana-kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu." Yohana 1:29. Yehova mkuu ametangaza kutoka katika kiti chake cha enzi kwamba, "Huyu ni Mwanangu mpendwa." Mathayo 3:17. Sisi wanafunzi wake tunatangaza kwamba, Huyu ni Yesu, Masihi, Mfalme wa uzima, Mkombozi wa ulimwengu. Na mfalme wa nguvu za giza anamkiri akisema, "Nakutambua u nani, Mtakatifu wa Mungu." Marko 1:25.

## Sura ya 64

# Watu Walio katika Hukumu ya Kuangamia

[Sura hii imejengwa katika Marko 11:11-14, 20, 21; Mathayo 21:17-19.]

Kule kuingia kwa Kristo Yerusalemu kwa shangwe ya ushindi kulikuwa utabiri hafifu wa kuja kwake katika mawingu ya mbinguni pamoja na nguvu na utukufu, akiwa katikati ya shangwe za malaika na furaha ya watakatifu. Hapo ndipo yatakapotimizwa maneno ya Kristo kwa makuhani na Mafarisayo kwamba: "Hamtaniona kamwe tangu sasa, hata mtakaposema, Amebarikiwa ajaye kwa jina la Bwana." Mathayo 23:39. Katika maono ya kinabii Zekaria alionyeshwa siku ile ya shangwe ya mwisho; na aliona pia hatima ya kuangamia ya wale ambao wakati wa kuja kwake mara ya kwanza walimkataa Kristo: "Nao watamtazama yeye ambaye walimchoma; nao watamwombolezea, kama vile mtu amwombolezeavyo mwanawe wa pekee; nao wataona uchungu kwa ajili yake, kama vile mtu aonavyo uchungu kwa ajili ya mzaliwa wake wa kwanza." Zekaria 12:10. Kristo aliiona hali hii kwa mbali wakati alipouona mji akalia kwa ajili yake. Katika uangamivu wa Yerusalemu wa muda aliona uangamivu wa mwisho wa watu wale waliokuwa na hatia ya damu ya Mwana wa Mungu.

Wanafunzi waliiona chuki ya Wayahudi dhidi ya Kristo, lakini walikuwa hawajaona kile kinachoweza kusababishwa na chuki hiyo. Bado hawakuelewa hali yenyewe ya Israeli, wala kupambanua mapatilizo ambayo yangeuangukia Yerusalemu. Kristo aliwafunulia hili kwa kutumia mfano wa kielelezo halisi.

Wito wa mwisho kwa Yerusalemu ulikuwa umetolewa bila mafanikio. Makuhani na wakuu walikuwa wamesikia sauti ya unabii wa wakati uliopita ikitoa mwangwi wake ndani ya ule umati, kama jibu la swali kwamba, "Ni nani huyu?" lakini hawakuikubali kama **(581)** sauti ya Uvuvio. Kwa hasira na kiburi walijaribu kunyamazisha watu. Kulikuwa na maafisa kadhaa wa Kirumi katika ule msafara, na adui zao walimshtaki Yesu kwa hao kwamba alikuwa anaongoza ghasia za uasi. Walimsema kwamba alikuwa anataka kujimilikisha hekalu, na atawale kama mfalme wa Yerusalemu.

Lakini sauti ya utulivu ya Yesu ilinyamazisha kelele za msafara wakati aliposema tena kwamba hakuwa amekuja kuanzisha utawala wa duniani; kwamba muda si mrefu angepanda kwenda kwa Baba yake, na kwamba washtaki wake wasingemwona tena mpaka atakaporudi katika utukufu. Hapo ndipo wangemkiri, wakiwa wamekwishachelewa kwa wokovu wao. Yesu alisema maneno haya kwa huzuni. Maafisa wa Kirumi walinyamazishwa na kutiishwa. Ingawa mioyo yao ilikuwa migeni kwa ushawishi wa mbingu, iliguswa kwa namna ambayo haikupata kuguswa kabla. Katika uso mtulivu wa Yesu waliona upendo, wema na kustahili heshima. Walisisimuliwa na mguso ambao hawakuuelewa. Badala ya kumtia Yesu nguvuni, walipata zaidi mwelekeo wa kumtukuza. Wakiwageukia wale makuhani na wakuu, waliwatuhumu kwa kusababisha fujo. Viongozi hawa, kwa hasira na kushindwa, waliwageukia watu na kuwalaumu, huku wakigombana wao kwa wao kwa hasira.

Wakati ule ule Yesu alipita hekaluni bila kujulikana. Kulikuwa kimya pale, maana tukio la kule mlima wa Mizeituni lilikuwa limevutia watu kule. Kwa muda mfupi Yesu alibaki pale hekaluni, akiliangalia kwa macho ya huzuni. Halafu aliondoka pamoja na wanafunzi wake, na kurudi Bethania. Watu walipomtafuta ili wamtawaze kuwa mfalme, hakuonekana.

Yesu alitumia usiku wote akiomba, wakati wa asubuhi alirudi tena hekaluni. Njiani alipita karibu na bustani ya mitini. Alikuwa na njaa, na "akaona kwa mbali mtini wenye majani, akaenda ili labda aone kitu juu yake; na alipoufikilia hakuona kitu ila majani; maana si wakati wa tini."

Huu haukuwa msimu wa kuiva kwa tini, isipokuwa katika sehemu fulani-fulani; na katika nyanda za juu zilizozunguka Yerusalemu ingekuwa sahihi kusema, "si wakati wa tini." Lakini katika bustani ile alipopita Yesu, mti mmoja ulionekana kuwa umeitangulia kwa mbali miti mingine. Ulikuwa tayari umefunikwa na majani. Kawaida ya miti ya tini ni kwamba kabla majani hayajafunguka, tunda linalokua hutokea. Kwa hiyo huu mti uliojaa majani ulileta tumaini la kuwa na matunda. Lakini kumbe mwonekano wake ulikuwa wa udanganyifu. Baada ya kutafuta katika matawi yake, kuanzia tawi kubwa la chini mpaka tawi changa la juu, Yesu "hakuona kitu ila majani." Yalikuwa majani mengi yaliyo ya bandia, hakuna zaidi. **(582)** Kristo aliutamkia ule mti maneno ya

laana. Alisema, "Tangu leo hata milele mtu asile matunda kwako." Asubuhi iliyofuata, wakati Mwokozi na wanafunzi walipokuwa njiani tena kwenda mjini, matawi yaliyonyauka na majani yanayodondoka yaliwavuta kuangalia. Petro akasema. "Rabi, tazama, mtini ulioulaani umenyauka."

Kitendo cha Kristo kuulaani ule mtini kiliwashtua wanafunzi. Kilionekana kama kisichofanana na kawaida zake na matendo yake. Mara nyingi walikuwa wamemsikia akisema hakuja kuuhukumu ulimwengu, bali ya kwamba ulimwengu upate kuokolewe katika Yeye. Waliyakumbuka maneno yake kwamba, "Mwana wa Adamu hakuja kuziangamiza roho za watu, bali kuziokoa." Luka 9:56. Kazi zake za ajabu zilikuwa zimefanywa ili kuokoa, wala si kuangamiza. Wanafunzi walikuwa wamemjua tu kama Mrejeshaji, Mponyaji. Kitendo hiki alichofanya kilikuwa cha tofauti. Kusudi lake lilikuwa nini? Waliuliza.

Mungu "hufurahia rehema." "Kama mimi niishivyo, asema Bwana Mungu, sikufurahii kufa kwake mtu mwovu." Mika 7:18; Ezekieli 33:11. Kwake Yeye kazi ya kuharibu na kutangaza hukumu ni "tendo lake la ajabu." Isaya 28:21. Lakini ni kwa huruma na upendo kwamba anafunua pazia la wakati ujao, na kuwafunulia watu matokeo ya njia ya dhambi.

Kule kuulaani mtini kulikuwa ni fundisho kwa njia ya mfano wa jambo lililotendwa. Mti ule usiozaa, ukionyesha kustawi kwa majani yasiyo na kitu machoni pa Yesu, ulikuwa ni alama ya kuwakilisha taifa la Wayahudi. Mwokozi alitaka aweke wazi kwa wanafunzi wake sababu na uhakika wa hukumu ya Israeli. Kwa kusudi hili aliupatia mti huo maadili bora, na kuufanya kuwa hazina ya ukweli wa mbinguni. Wayahudi walisimama wakijiona bora sana kuliko mataifa mengine, wakidai kuwa **(583)** na heshima kwa Mungu. Walikuwa wamependelewa na Mungu kwa namna ya pekee, na walidai kwamba wao ni wenye haki kuliko mtu mwingine yeyote. Lakini walikuwa na ufidhuli wa kuupenda ulimwengu na tamaa ya mali. Walijikweza kwa kujua kwao dini, lakini walikuwa wajinga wasiojua matakwa ya Mungu, na walikuwa wamejaa unafiki. Kama ulivyo mtini usiozaa, walitandaza matawi yao ya kinafiki juu, wakionekana wa kuvutia, na wema kwa macho, lakini hawakuzaa "kitu ila majani." Dini ya Wayahudi, ikiwa na hekalu la fahari, madhabahu zake takatifu, makuhani wake wenye taji na maadhimisho ya kuvutia, ilikuwa nzuri sana kwa mwonekano wa nje, lakini unyenyekevu, upendo, na ukarimu vilikuwa vinakosekana.

Miti yote iliyokuwa katika bustani ya mitini haikuwa na matunda; lakini miti ile isiyo na majani haikuamsha hamu, nayo haikusababisha mfadhaiko. Mataifa waliwakilishwa na miti hii. Hawakuwa na kitu kama Wayahudi walivyokuwa kuhusiana na kumcha Mungu; lakini wao hawakujigamba kwamba wanamcha Mungu. Hawakujidai kwa unafiki kwamba ni watu wema. Walikuwa vipofu kuhusu kazi na njia za Mungu. Kwao msimu wa mitini ulikuwa bado. Walikuwa bado wanasubiri siku ambayo ingewaletea nuru na tumaini. Wayahudi, ambao walikuwa wamepata baraka kuu kutoka kwa Mungu, walikuwa na deni kwa kutumia isivyo sahihi zawadi hizi. Ule upendeleo ambao walijidai kuwa nao uliwaongezea tu hatia.

Yesu alikuwa ameujia mtini ule akiwa na njaa, ili kupata chakula. Hivyo ndivyo alivyokuja kwa Israeli, akiwa na njaa ya kukuta ndani yao matunda ya haki. Alikuwa amewapatia zawadi zake, ili ya kwamba wazae matunda ya kuubariki ulimwengu. Walikuwa wamepewa kila fursa na upendeleo, na kwa hiyo alihitaji matokeo yake ya wema na ushirikiano katika kazi ya neema. Alitafuta kuona ndani yao hali ya kujikana nafsi na huruma, bidii kwa ajili ya Mungu, na kuhangaikia wokovu wa roho za wanadamu wenzao. Ikiwa wangeshika sheria ya Mungu, wangefanya kazi isiyo na ubinafsi kama aliyofanya Kristo. Lakini upendo kwa Mungu na mwanadamu ulikingwa na kiburi na kujiona hali ya kutosheka. Walijiletea maangamivu kwa kukataa kuhudumia watu wengine. Hawakuupatia ulimwengu hazina za ukweli ambazo Mungu alikuwa amekabidhi kwao. Huenda katika mti usiozaa wangesoma dhambi yao na adhabu yao. Kwa ile hali ya mtini kunyauka kwa sababu ya laana ya Mwokozi, kuendelea kusimama huku ukiwa mkavu ulionyauka, kukauka kwa mizizi yake, ilikuwa inaonyesha vile ambavyo Wayahudi wangekuwa baada ya neema ya Mungu kuondolewa kwao. Kwa kukataa kutawanya nuru, wasingeipata tena. Bwana anasema, "Ee Israeli, ya kuwa wewe u kinyume changu mimi, kinyume cha msaada wako." Hosea 13:9.

**(584)** Hilo ni onyo la wakati wote. Kitendo cha Kristo kuulaani mti ambao nguvu zake mwenyewe ziliuumba kinasimama kama onyo kwa makanisa yote na kwa Wakristo wote. Hakuna mtu anayeweza kuishi maisha ya sheria ya Mungu asiwahudumie watu wengine. Lakini wapo wengi ambao hawaishi maisha ya huruma na yasiyo na ubinafsi kama ya Kristo. Baadhi ambao wanajiona kwamba ni Wakristo wazuri hawajui maana ya kumtumikia

Mungu. Wanapanga na kujifunza ili kujifurahisha wenyewe. Wanatenda kwa kujitazama wao binafsi. Muda una thamani kwao katika yale wanayokusanya kwa ajili yao wenyewe. Lengo lao pekee ni mambo ya maisha. Hawahudumu kwa ajili ya wengine bali kwa ajili yao wenyewe. Mungu aliwaumba kusudi waishi katika ulimwengu ambapo lazima huduma isiyo ya ubinafsi ifanywe. Aliwaweka ili wawasaidie wanadamu wenzao katika kila njia inayowezekana. Lakini umimi ni mpana kiasi kwamba hawawezi kuona kitu kingine chochote. Hawaguswi na ubinadamu. Wale wanaoishi kwa ubinafsi hivyo wako kama ule mtini, ambao ulijionyesha kwa kila namna kwamba unafaa wakati hauna matunda. Wanafuata taratibu za desturi za ibada, lakini pasipokuwa na toba wala imani. Wanaheshimu sheria ya Mungu kwa kujionyesha kwa bure, lakini wanakosa utii. Wanasema, lakini hawatendi. Katika hukumu iliyotamkwa kwa mtini ule Kristo alionyesha jinsi kujionyesha kwa namna hii kunavyochukiza. Alitangaza kwamba mwenye dhambi anayeonekana wazi ana hatia kidogo kuliko yule anayejidai kumtumikia Mungu, wakati hazai matunda ya utukufu wa Mungu.

Mfano wa mtini, uliosemwa kabla ya Kristo kutembelea Yerusalemu, ulikuwa na mwunganiko wa moja kwa moja na somo alilofundisha katika kuulaani mtini huu usiozaa. Kwa ajili ya mti usiozaa wa mfano ule mtunzaji wa shamba aliomba akisema, Uuache mwaka huu nao, hata niupalilie, niutilie samadi; nao ukizaa matunda baadaye, vema! La, usipozaa, ndipo uukate. Utunzaji wa ziada ulikuwa ufanywe kwa mti usiozaa. Ungepewa kila mahitaji. Lakini kama ukidumu bila kuzaa, hakuna kitu ambacho kingeuokoa kutoka katika kuangamizwa. Katika mfano huo matokeo ya kazi ya mtunzaji wa bustani hayakufunuliwa. Yalitegemeana na watu wale ambao maneno ya Kristo yalisemwa kwao. Walikuwa wanawakilishwa na mti usiozaa, na hatima yao ilikuwa inaamuliwa na wao wenyewe. Kila hitaji ambalo mbingu iliweza kutoa lilitolewa kwao, lakini hawakuonyesha faida ya ongezeko la baraka kwao. Kwa kitendo cha Kristo kuulaani mtini usiozaa, matokeo yalionyeshwa. Walikuwa wameamua kuhusu kuangamia kwao.

Kwa zaidi ya miaka elfu taifa la Wayahudi lilikuwa limetumia vibaya rehema ya Mungu na kuzialika hukumu zake zije. Walikuwa wamekataa maonyo yake na kuwaua manabii wake. Kwa dhambi hizi watu wa wakati wa Kristo walijipatia hatia ya kufuata njia hiyo hiyo. Katika kuukataa **(587)** wema na maonyo yaliyokuwepo mnamo wakati wao waliifanya hatia kuwepo katika kizazi kile. Watu wa wakati wa Kristo walikuwa wanajifunga wenyewe kwa minyororo ambayo taifa lile lilikuwa limeitengeneza kwa karne nyingi.

Katika kila kizazi watu wamepewa siku yao ya nuru na upendeleo, muda wa matazamio ambao wanaweza kuutumia kupatanishwa na Mungu. Lakini neema hii ina mpaka. Rehema inaweza kusihi kwa miaka mingi na ikapuuzwa na kukataliwa; lakini hufika muda ambao neema inafanya wito wake wa mwisho. Moyo huwa mgumu sana kiasi kwamba unakoma kuitikia ushawishi wa Roho Mtakatifu. Halafu sauti ile tamu inayoongoa haimbembelezi mwenye dhambi tena, na kemeo na maonyo hukoma.

Siku hiyo ilikuwa imeujia Yerusalemu. Yesu alilia kwa huzuni kwa ajili ya mji uliokuwa unaangamia, lakini hakuweza kuuponya. Alikuwa ametumia kila rasilimali. Katika kule kukataa maonyo ya Roho wa Mungu, Israeli ilikuwa imekataa njia pekee ya msaada. Hakukuwa na uwezo mwingine ambao ungeweza kuwaokoa.

Taifa la Israeli lilikuwa alama inayowakilisha watu wa zama zote wanaopuuza wito wa Upendo Mkuu. Machozi ya Kristo alipoulilia Yerusalemu yalikuwa ni kwa ajili ya dhambi za nyakati zote. Katika hukumu zilizotamkwa kwa Israeli, wale wanaokataa marudi na maonyo ya Roho wa Mungu wanaweza wakasoma hukumu zao wenyewe.

Katika kizazi hiki wapo watu wengi wanaotembea katika mazingira kama yale yale ya Wayahudi waliokuwa hawaamini. Wameshuhudia udhihirisho wa nguvu za Mungu; Roho Mtakatifu amezungumza na mioyo yao; lakini wao wanang'ang'ania kutokuamini kwao na upinzani wao. Mungu anawapelekea maonyo na makemeo, lakini wao hawataki kuhiari kuungama makosa yao, na wanakataa ujumbe wake na wajumbe wake. Njia zile zile anazotumia ili kuwarejesha zinakuwa jiwe wanalojikwaa.

Manabii wa Mungu walichukiwa na Israeli yenye kuasi kwa sababu kupitia hao dhambi zao zilizofichwa ziliwekwa wazi. Ahabu alimwona Eliya kama adui kwa sababu nabii huyo alikuwa mwaminifu kukemea maovu ya siri ya mfalme huyo. Hivyo ndivyo mtumishi wa Mungu leo, mkemeaji wa dhambi, anavyokabiliwa na mabezo ya dharau na kupuuzwa kikatili. Ukweli wa Biblia, dini ya Kristo, hupambana dhidi ya mkondo imara wa uchafu wa maadili. Kwa sasa, itikadi za imani za mapokeo zina nguvu zaidi katika mioyo ya watu kuliko ilivyokuwa

wakati wa Kristo. Kristo hakutimiza matarajio ya watu; maisha yake yalikuwa ya kemeo kwa dhambi zao, nao wakamkataa. Hivyo ndivyo ambavyo hata sasa neno la Mungu halipatani na matendo ya wanadamu na mielekeo yao ya asili, na maelfu wanaikataa nuru yake. Watu ambao wanasukumwa na Shetani wanakuwa na mashaka na neno la Mungu, nao huchagua kufuata **(588)** maamuzi yao kwa uhuru. Wanachagua giza badala ya nuru, lakini wanafanya hivyo kwa hatari ya maangamizi ya nafsi zao wenyewe. Wale waliopinga maneno ya Kristo, waliona njia ya kuyapinga ikidumu kuongezeka, mpaka walipogeuka kabisa kutoka kwake aliye Kweli na Uzima. Hivyo ndivyo ilivyo hata sasa. Mungu hakusudii kuondoa kila kikwazo ambacho moyo wa kiburi unaweza kuleta dhidi ya ukweli wake. Kwa wale wanaokataa miale ya nuru ya thamani ambayo ingelimlika giza, siri za neno la Mungu zinasalia hivyo hivyo milele. Ukweli umefichwa kutoka kwao. Wanatembea wakiwa vipofu, wasijue uangamivu ambao uko mbele yao.

Kutoka kwenye kilele cha Mlima wa Mizeituni Kristo aliutazama ulimwengu wote na vizazi vyote; na maneno yake yale yanahusu kila mtu anayepuuza rehema ya mbinguni inayosihi. Wewe unayekejeli upendo wake, anasema hayo kwako leo. Ni wewe, wewe mwenyewe, ambaye ungepaswa kujua mambo yapasayo amani. Kristo anamwaga machozi ya uchungu kwa ajili yako, wewe ambaye huna machozi ya kumwaga kwa ajili yako mwenyewe. Ule moyo mgumu uliokuwa ndani ya Mafarisayo tayari unadhihirika ndani yako. Na kila ushahidi wa neema ya Mungu, kila mwale wa nuru ya kimbingu, ama unayeyusha na kuutiisha moyo wako, au unauthibitisha ya kwamba uko katika hali isiyojutia makosa na isiyo na tumaini.

Kristo aliona kwa mbali kwamba Yerusalemu ingebaki kuwa na moyo mgumu na usio na toba; lakini hatia yote, matokeo yote ya kuikataa rehema, iko mlangoni pa mji huo wenyewe. Hivyo ndivyo itakavyokuwa kwa kila nafsi inayofuata njia kama hiyo. Bwana anasema, “Ee Israeli, ya kuwa wewe u kinyume changu mimi, kinyume cha msaada wako." "Sikia, Ee nchi; tazama, nitaleta mabaya juu ya watu hawa, naam, matunda ya mawazo yao, kwa sababu hawakuyasikiliza maneno yangu; tena kwa habari ya sheria yangu, wameikataa." Hosea 13:9; Yeremia 6:19.

## Sura ya 65

# Hekalu Latakaswa Tena

[Sura hii imejengwa katika Mathayo 21:12-16, 23-46; Marko 11:15-19, 27-33; 12:1-12; Luko 19:45-48; 20:1-19.]

Mwanzoni mwa huduma yake, Kristo alikuwa amewafukuza kutoka hekaluni wale waliolinajisi kwa biashara zisizo takatifu; na mtazamo wake pamoja na tabia yake ya uchaji Mungu vilikuwa vimeleta hofu katika mioyo ya wachuuzi wale. Wakati wa kuifunga kazi yake alikuja hekaluni tena, na kulikuta likiwa linachafuliwa kama ilivyokuwa kabla. Hali ya mambo ilikuwa mbaya kuliko hata awali. Viwanja vya nje ya hekalu vilikuwa kama kiwanja cha mifugo. Sauti ya hasira za wachuuzi wanaobadili fedha, miongoni mwa sauti hizo zikiwemo za watu waliokuwa wamekabidhiwa kutekeleza kazi ya huduma takatifu, zilichanganyika pamoja na milio ya wanyama na sauti kali za sarafu zilizokuwa zinagonganagongana. Hata wakuu wa hekalu walikuwa miongoni mwa watu waliouza, kununua na kubadili fedha. Kwa hiyo walizama kabisa katika hali ya kuongozwa na tamaa ya mali kiasi kwamba machoni pa Mungu hawakuwa wema zaidi ya wezi.

Makuhani na wakuu walifahamu kidogo sana kuhusu heshima ya kazi waliyokabidhiwa kufanya. Katika kila Pasaka na Sikukuu ya Vibanda, maelfu ya wanyama walichinjwa, na damu yao ilikingwa na makuhani na kumwagwa kwenye madhabahu. Wayahudi walikuwa wanafahamu habari ya kutoa sadaka ya damu, na ni kama walikuwa wamepoteza ufahamu kwamba dhambi ndiyo iliyosababisha ulazima wa kumwaga damu yote hiyo ya wanyama. Hawakuweza kuona kwamba damu ile ilikuwa ni kivuli cha damu ya Mwana mpendwa wa Mungu, **(590)** ambayo ingemwagwa kwa ajili ya uzima wa ulimwengu, na kwamba kwa kutoa kafara wanadamu wangegeuziwa kwa Mkombozi aliyesulibiwa.

Yesu aliwaangalia wale wanyama wa kafara wasio na hatia, na kuona jinsi ambavyo Wayahudi walikuwa wameyafanya makusanyiko haya makuu kuwa matukio ya kumwaga damu na kufanya ukatili. Badala ya kutubu dhambi kwa unyenyekevu, wao walikuwa wamezidisha kafara za wanyama, kama vile Mungu angetukuzwa kwa ibada isiyo ya moyo. Makuhani na wakuu walikuwa wameifanya mioyo kuwa migumu kwa njia ya ubinafsi na tamaa ya mali. Walikuwa wanajipatia mapato kwa kutumia alama zile zile zinazosonda kidole kwa Mwanakondoo wa Mungu. Kwa hiyo katika macho ya watu utakatifu wa ibada ya kafara ulikuwa umeharibiwa kwa kiasi kikubwa. Hasira ya Yesu iliwaka; alijua kwamba damu yake, ambayo muda si mrefu ingemwagwa kwa ajili ya dhambi za ulimwengu, ingetambuliwa na makuhani na wazee kwa kiasi kidogo sana kuliko ilivyokuwa kwa damu ya wanyama ambayo waliendelea kumwaga bila kukoma.

Yesu alikuwa amenena dhidi ya matendo haya kupitia kwa manabii. Samweli alisema, "Je! Bwana huzipenda sadaka za kuteketezwa na dhabihu sawasawa na kuitii sauti ya Bwana? Angalia, kutii ni bora kuliko dhabihu, Na kusikia kuliko mafuta ya beberu." Naye Isaya, akiona kwa muono wa kinabii uasi wa Wayahudi, aliwasema wakiwa kama wakuu wa Sodoma na Gomora: "Lisikieni neno la Bwana, enyi waamuzi wa Sodoma; tegeni masikio msikie sheria ya Mungu wetu, enyi watu wa Gomora. Huu wingi wa sadaka zenu mnazonitolea una faida gani? Asema Bwana. Nimejaa mafuta ya kafara za kondoo waume, na mafuta ya wanyama walionona; nami siifurahii damu ya ng'ombe wala ya wana-kondoo wala ya mbuzi waume. Mjapo ili kuonekana mbele zangu, ni nani aliyetaka neno hili mikononi mwenu, kuzikanyaga nyua zangu?" "Jiosheni, jitakaseni; ondoeni uovu wa matendo yenu usiwe mbele za macho yangu; acheni kutenda mabaya; jifunzeni kutenda mema; takeni hukumu na haki; wasaidieni walioonewa; mpatieni yatima haki yake; mteteeni mjane." 1 Samweli 15:22; Isaya 1:10-12, 16, 17.

Yeye aliyekuwa ametoa unabii huo sasa kwa mara ya mwisho alirudia maonyo hayo. Katika kutimiza unabii watu walikuwa wamemtangaza Yesu kwamba ni mfalme wa Israeli. Lazima atende kwa sifa hiyo. Alijua kwamba jitihada zake za kuugeuza mfumo wa kikuhani uliokuwa umechafuka zisingefanikiwa; lakini hata hivyo lazima kazi yake ifanyike; lazima ushahidi wa kazi yake ya kimbingu utolewe kwa watu hawa wasioamini.

Kwa mara nyingine alipita katika viwanja vya hekalu akiangalia kwa namna inayochoma. Macho yote yalielekezwa kwake. Makuhani na wakuu, Mafarisayo **(591)** na Mataifa, kwa mshtuko na kuduwaa walimwangalia Yeye aliyesimama mbele yao akiwa na uweza wa Mfalme wa mbinguni. Uungu ulimlika ndani ya

ubinadamu, ukimpatia Kristo ukuu na utukufu ambao haukuwahi kuonekana kabla. Wale waliokuwa wamesimama karibu naye walisogea mbali kwa kiasi ambacho umati ule wa watu uliwaruhusu kufanya hivyo. Ukiacha wachache miongoni mwa wanafunzi wake, Mwokozi alisimama peke yake. Kila sauti ilinyamza. Ukimya ule mkubwa ulionekana kama usiovumilika. Kristo akaongea kwa nguvu iliyowayumbisha watu kama waliopigwa na tufani yenye nguvu: "Imeandikwa, Nyumba yangu itaitwa nyumba ya sala; bali ninyi mmeifanya kuwa pango la wanyang'anyi." Sauti yake ilisikika kama tarumbeta katika maeneo yote ya hekalu. Mwonekano wake wa kutopendezwa ulikuwa kama moto ulao. Kwa mamlaka aliamuru, "Yaondoeni haya." Yohana 2:16.

Miaka mitatu iliyokuwa imepita, wakuu wa hekalu hili walikuwa wamekimbia kwa amri ya Yesu. Walikuwa wamejishangaa kwa woga wao, na hali ya kumtii Mtu mmoja wa hali ya chini bila **(592)** kuhoji. Walikuwa wamedhani kwamba haiwezekani kurudia kujisalimisha tena namna ile. Lakini sasa waliogopeshwa zaidi kuliko hata kabla, na wakatii amri yake kwa haraka kubwa zaidi. Hakuna hata mmoja aliyethubutu kuhoji mamlaka yake. Makuhani na wachuuzi wale walikimbia kutoka kwake, huku wakiswaga ng'ombe wao.

Huko njiani walikutana na halaiki ya watu waliokuwa wanakuja na wagonjwa wao wakimtafuta Mponyaji Mkuu. Taarifa walizopewa na wale waliokuwa wanakimbia zilisababisha baadhi yao kurudi nyuma. Waliogopa kukutana na Yeye aliye na nguvu namna hiyo, ambaye mwonekano wake tu ulikuwa umekimbiza makuhani na wakuu. Lakini idadi kubwa ya watu walihimili kuja kwake, wakiwa na hamu ya kumfikia Yeye aliye tumaini lao pekee. Wakati umati ule ulipokimbia kutoka hekaluni, wengi walikuwa wamebaki pale. Sasa hao waliungana na wale wapya waliokuja. Kwa mara nyingine tena viwanja vya hekalu vikajawa na wagonjwa na watu walio mahututi, na kwa mara nyingine tena Yesu akawahudumia.

Baada ya kipindi fulani wale makuhani na wakuu walirudi hekaluni. Hofu ilipokuwa imepungua, walishikwa na wasiwasi wa kutaka kujua kwamba Yesu angefanya nini tena baada ya pale. Walimtarajia kwamba angechukua kiti cha enzi cha Daudi. Wakiwa wanarudi hekaluni kimya-kimya, walisikia sauti za wanaume, wanawake, na watoto wakimsifu Mungu. Walipokuwa wanaingia, walisimama hapo hapo kwa kuduwaa wakishangaa hali iliyokuwepo. Waliona wagonjwa wakiponywa, vipofu wakipewa kuona, viziwi wakipata kusikia, na viwete wakiruka kwa furaha. Watoto ndio waliokuwa wakifurahia zaidi. Yesu alikuwa ameponya maradhi yao; alikuwa amewashikilia mikononi mwake, akiwa amepokea busu zao za upendo, na baadhi yao walikuwa wamesinzia wakiwa kifuani mwake wakati alipokuwa akifundisha watu. Sasa kwa sauti kubwa watoto waliimba nyimbo za kumsifu. Walirudia zile hosana za jana yake, na kupepea matawi ya mitende ya ushindi mbele yake. Hekalu lilitoa mwangwi tena na tena wa nyimbo zao zilizosema, "Na abarikiwe yeye ajaye kwa jina la Bwana!" "Tazama, mfalme wako anakuja kwako; Ni mwenye haki, naye ana wokovu!" Zaburi 118:26; Zekaria 9:9. "Hosana, Mwana wa Daudi!"

Mlio wa sauti hizi za furaha zisizo na kizuizi zilikuwa ni machukizo kwa wakuu wa hekalu. Walipanga kuyanyamazisha mambo hayo. Waliwaambia watu kwamba ile nyumba ya Mungu ilikuwa inanajisiwa na miguu ya watoto na makelele yale ya furaha. Walipoona kwamba maneno yao hayasikizwi kwa watu wale, wakuu wale walileta ombi kwa Yesu, wakisema: "Wasikia hawa wasemavyo? Yesu akawaambia, Naam; hamkupata kusoma, Kwa vinywa vya watoto wachanga na wanyonyao **(593)** umekamilisha sifa?" Unabii ulikuwa umesema kwamba Kristo atatangazwa kuwa mfalme, na neno hilo lazima litimizwe. Makuhani na wakuu wa Israeli walikataa kuutangaza utukufu wake, na Mungu akawasukuma watoto ili kuwa mashuhuda wake. Ikiwa sauti za watoto zingenyamaza, hata nguzo zenyewe za haekalu zingeimba sifa za Mwokozi.

Wale Mafarisayo walitatanishwa na kufadhaika. Yeye ambaye hawawezi kumtisha alikuwa anatawala. Yesu alikuwa amechukua nafasi yake kama mtunzaji wa hekalu lile. Kabla ya hapo hakupata kuchukua kamwe mamlaka ya kifalme kama hayo. Kabla ya hapo maneno na matendo yake hayakuwahi kamwe kuwa na msukumo wa nguvu kiasi hicho. Alikuwa amefanya kazi njema sana katika Yurusalemu, lakini wakati huo wa kabla hazikuwahi kuwa za heshima na mguso kiasi hiki. Mbele ya watu wale waliokuwa wameshuhudia matendo yake ya ajabu, makuhani na wakuu hawakuthubutu kuonyesha upinzani kwa Yesu. Ingawa walikuwa wameghadhibishwa na kukwazwa na jibu lake, hawakuwa na uwezo wa kuafanya jambo lolote baya siku ile.

Asubuhi iliyofuata baraza la Sanhedrin lilikutana tena kuangalia jambo la kufanya kuhusu Yesu. Miaka mitatu iliyokuwa imepita walidai ishara ya Umasihi wake. Tangu wakati ule alikuwa amefanya matendo makuu katika nchi yote. Alikuwa amewaponya wagonjwa, alikuwa amelisha maelfu ya watu kimiujiza, alikuwa ametembea

kwenye mawimbi ya bahari, na kuamuru utulivu kwa bahari iliyochafuka. Mara nyingi alikuwa amesoma mioyo ya watu kama mtu asomaye kitabu; alikuwa ametoa pepo, na kufufua wafu. Wakuu walikuwa na ushahidi wa Umasihi wake. Sasa waliamua wasidai ishara ya mamlaka yake, bali waliamua kumshawishi aseme maneno ya kukiri au atoe matamko ambayo yangetumika kumhukumu.

Walienda hekaluni mahali alipokuwa akifundisha, wakamwuliza: "Ni kwa mamlaka gani unatenda mambo haya? Naye ni nani aliyekupa mamlaka hii uyatende haya?" Walitarajia kwamba angesema mamlaka yake yametoka kwa Mungu. Walikusudia kuikataa kauli hiyo. Lakini Yesu alikabiliana nao kwa swali ambalo linaonekana kwa ujumla kana kwamba linahusu mada tofauti, na alilifanya jibu liwe na sharti la kujibiwa kwanza ndipo naye ajibu swali lao. Alisema, "Ubatizo wa Yohana ulitoka mbinguni, au kwa wanadamu?"

Wale makuhani waliona kwamba wako katika mtanziko ambao hakuna ujanja ambao ungewaokoa humo. Ikiwa wangesema kwamba ubatizo wa Yohana ulitoka mbinguni, hali yao ya kutokukubaliana nao ingekuwa bayana. Kristo angesema, Kwa nini basi hamkumwamini? Yohana alikuwa ameshuhudia habari za Kristo kwamba, "Tazama **(594)** Mwana-kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu." Yohana 1:29. Ikiwa makuhani waliamini ushuhuda wa Yohana, wangewezaji sasa kukana Umasihi wa Kristo? Ikiwa wangesema kulingana na imani halisi waliyokuwa nayo, kwamba huduma ya Yohana ilitoka kwa wanadamu, wangejiletea dhoruba ya kukasirikiwa; maana watu waliamini kwamba Yohana ni nabii.

Makutano walisubiri uamuzi wao kwa hamu kubwa sana. Walijua kwamba makuhani wamekuwa wakisema kwamba wanaikubali huduma ya Yohana, na waliwatarajia kukiri pasipo swali kwamba alitumwa na Mungu. Lakini baada ya kushauriana kwa faragha, wale makuhani waliamua wasijiingize kwenye tatizo. Kwa unafiki wakijifanya kwamba hawajui, walisema, "Hatujui." Yesu akawaambia, "Wala mimi siwaambii ninyi ni kwa mamlaka gani nayatenda haya."

Waandishi, makuhani, na wakuu walinyamazishwa wote. Wakiwa wametatanishwa na kufadhaika, walisimama wakiwa wameinamisha nyuso, pasipo kudiriki kuuliza maswali zaidi kwa Kristo. Kwa kukosa ujasiri na maamuzi walikuwa wamejishushia heshima yao kwa watu ambao sasa walikuwa wako tayari kuwaona watu hawa wenye kiburi na wenye kujihesabia haki wanavyoshindwa.

Maneno na matendo yote haya ya Kristo yalikuwa muhimu, na ushawishi wake ungeonekana katika hali ya kuongezeka daima baada ya kusulibiwa na kupaa kwake. Wengi kati ya wale waliokuwa wanasubiri kwa hamu majibu ya swali la Yesu hatimaye wangekuwa wanafunzi wake, wakiwa wamevutwa kwake kwa mara ya kwanza katika tukio hilo la siku hiyo. Mandhari hiyo ya hekaluni isingefutika vichwani mwao kamwe. Tofauti iliyokuwepo kati ya Yesu na kuhani mkuu wakati walipokuwa wakijibizana ilionekana wazi. Yule mheshimiwa mwenye kiburi wa hekaluni alikuwa amevalia mavazi ya kitajiri ya gharama. Kichwani pake alikuwa amevalia taji inayometameta. Mwonekano wake ulikuwa wa ukuu, nywele zake na ndevu zake ndefu zilikuwa na rangi inayoashiria umri mkubwa. Mwonekano wake uliduwaza waliomtazama. Aliyekuwa amesimama mbele ya mtu huyu mwenye heshima na fahari alikuwa ni Mtukufu wa mbinguni, akiwa hana mapambo wala maonyesho. Mavazi yake yalikuwa yamefungwa kama ya msafiri; uso wake ulikuwa umepauka, naye alionyesha mwonekano wa huzuni; lakini kilichokuwa kimeandikwa pale kwake ni heshima na ukarimu uliotofautiana kwa namna ya ajabu sana na ule wa kuhani mkuu mwenye kiburi, kujiamini binafsi, na mwenye hasira. Wengi miongoni mwa wale walioshuhudia maneno na matendo hayo ya Yesu mle hekaluni walimtawaza mioyoni mwao kama nabii wa Mungu tangu siku ile. Lakini kadiri hisia za wengi zilivyogeukia katika kumuunga mkono, chuki ya makuhani kwa Yesu iliongezeka. Ile hekima aliyotumia kukwepa mitego iliyotegwa miguuni pake, ikiwa ni ushahidi mpya wa uungu wake, viliongeza nguvu ya kuchochea ghadhabu zao.

Katika mapambano yake dhidi ya marabi wale, kusudi la Kristo halikuwa kuwaaibisha wapinzani wake wale. Hakufurahi kuwaona wakiwa katika wakati mgumu. Alikuwa na **(595)** somo muhimu la kufundisha. Alikuwa amewaaibisha adui zake kwa kuwaacha wabanwe katika wavu ambao walikuwa wamemtega Yeye. Kukiri kwao ujinga kuhusu asili ya ubatizo wa Yohana kulimpatia fursa ya kusema, naye alitumia zaidi fursa hiyo kwa kuwaonyesha hali yao halisi, akiongeza onyo jingine juu ya yale mengi ambayo yalikuwa yameshatolewa.

Alisema, "Lakini mwaonaje? Mtu mmoja alikuwa na wana wawili; akamwendea yule wa kwanza, akasema, Mwanangu, leo nenda kafanye kazi katika shamba la mizabibu. Akajibu akasema, Naenda, Bwana; asiende.

Akamwendea yule wa pili, akasema vile vile. Naye akajibu akasema, Sitaki; baadaye akatubu, akaenda. Je! Katika hao wawili ni yupi aliyefanya mapenzi ya babaye?"

Swali hili la ghafla liliwaamsha wasikilizaji wake. Walikuwa wamefuatilia mfano huo kwa umakini, na sasa walijibu haraka, "Ni yule wa pili." Akiwakazia macho yake, Yesu aliwaambia: "Amin nawaambia, watoza ushuru na makahaba wanatangulia mbele yenu kuingia katika ufalme wa Mungu. Kwa sababu Yohana alikuja kwenu kwa njia ya haki, ninyi msimwamini; lakini watoza ushuru na makahaba walimwamini, nanyi hata mlipoona, hamkutubu baadaye, ili kumwamini."

Wale makuhani na wakuu hawakuwa na namna ila kutoa jibu sahihi kujibu swali la Kristo, na kwa hiyo aliona mawazo yao yaliyopendezwa na mwana yule wa pili. Mwana huyu aliwakilisha watoza ushuru, wale waliokuwa wakidharauliwa na kuchukiwa na Mafarisayo. Kwa ujumla watoza ushuru walikuwa waovu wasio na maadili. Walikuwa wavunjifu wa sheria ya Mungu kweli kweli, maisha yao yakionyesha hali ya kupingana na matakwa ya sheria hiyo. Hawakuwa na shukrani wala utakatifu; walipoambiwa kwenda kufanya kazi katika shamba la mizabibu la Bwana, walikataa kwa jeuri. Lakini pindi Yohana alipokuja, akihubiri toba na ubatizo, watoza ushuru walipokea ujumbe wake na wakabatizwa.

Mwana yule wa kwanza aliwakilisha viongozi wa taifa la Wayahudi. Baadhi ya Mafarisayo walikuwa wametubu na kupokea ubatizo wa Yohana; lakini viongozi hao hawakuweza kukiri kwamba alitoka kwa Mungu. Maonyo yake na makemeo yake hayakuwapeleka katika hitaji la kufanya matengenezo. "Walilipinga shauri la Mungu juu yao, kwa kuwa hawakubatizwa naye." Luka 7:30. Waliutendea jeuri ujumbe wake. Kama yule mwana wa kwanza ambaye, alipoitwa, alisema, "Naenda, bwana," lakini asiende, makuhani na wakuu walijisema kwamba ni watiifu, lakini walitenda yasiyo ya utii. Walijifanya kuonekana wenye huruma, walidai kwamba wanaitii sheria ya Mungu, lakini walionyesha utii wa uongo. Watoza ushuru walipingwa na kulaaniwa na Mafarisayo kwamba ni waovu; lakini walionyesha kwa imani na matendo kwamba **(596)** walikuwa wanaingia katika ufalme wa mbinguni kabla ya wale watu wajihesabiao haki ambao walikuwa wamepewa nuru kubwa, lakini matendo yakawa hayaendani na madai yao ya kuwa wacha Mungu.

Makuhani na wakuu hawakuwa na utashi wa kubeba ukweli huu bainifu; walibaki kimya, hata hivyo, wakitumaini kwamba Yesu angesema jambo ambalo wangelitumia kumshtaki; lakini walikuwa bado wanayo mengi zaidi ya kustahimili kusikia.

Kristo akasema, "Sikilizeni mfano mwingine. Kulikuwa na mtu mwenye nyumba, naye alipanda shamba la mizabibu, akalizungusha ugo, akachimba shimo la shinikizo ndani yake, akajenga mnara, akapangisha wakulima, akasafiri. Wakati wa matunda ulipokuwa karibu, akawatuma watumwa wake kwa wale wakulima, wapokee matunda yake. Wale wakulima wakawakamata watumwa wake, huyu wakampiga, na huyu wakamwua, na huyu wakampiga kwa mawe. Akawatuma tena watumwa wengine wengi kuliko wa kwanza wakawatenda vile vile. Mwishowe akamtuma mwanawe kwao, akisema, Watamstahi mwanangu. Lakini wale wakulima walipomwona yule mwana, wakasemezana wao kwa wao, Huyu ni mrithi; haya na tumwue, tuutwae urithi wake. Wakamkamata, wakamtupa nje ya shamba la mizabibu, wakamwua. Basi atakapokuja yule bwana wa shamba la mizabibu, atawatendaje wale wakulima?"

Yesu alikuwa anawahutubia watu wote waliokuwa pale; lakini makuhani na wakuu ndio waliojibu. Walisema, "Atawaangamiza vibaya wale wabaya; na shamba la mizabibu atawapangisha wakulima wengine, watakaomlipa matunda kwa wakati wake." Mwanzoni wale wasemaji waliojibu hawakuwa wameelewa kwamba mfano huo unahusu watu gani, lakini sasa waliona kwamba walikuwa wametamka hukumu yao wenyewe. Katika mfano huo, mwenye nyumba humwakilisha Mungu, shamba la mizabibu ni taifa la Wayahudi, ule ugo ni sheria ya Mungu iliyokuwa inawalinda. Ule mnara ulikuwa alama ya hekalu. Bwana wa shamba hili la mizabibu alikuwa amefanya kila kitu kwa ajili ya ustawi wa shamba. Anasema, "Je! Ni kazi gani iliyoweza kutendeka ndani ya shamba langu la mizabibu nisiyoitenda?" Isaya 5:4. Hivyo ndivyo utunzaji wa Mungu usiochoka kwa Isaraeli ulivyowakilishwa. Na kama vile ambavyo wakulima wale wangerudisha kwa bwana sehemu stahili ya matunda ya shamba la mizabibu, ndivyo ambavyo watu wa Mungu walipaswa kumheshimu Mungu kwa njia ya maisha yanayolingana na upendeleo waliopewa. Lakini kama vile wakulima wale walivyokuwa wamewaua watumishi ambao walikuwa wametumwa na bwana kuchukua matunda, ndivyo ambavyo Wayahudi walikuwa wameua manabii waliotumwa na Mungu kwao ili kuwapa wito wa kutubu. Mjumbe baada ya mjumbe walikuwa

wameuawa. Mpaka hapo maana ya mfano huo haikuweza kuhojiwa, na kuhusu kwamba mfano huo ulifuatiliwa kiasi gani ushahidi haukuwa mdogo. Ndani ya mwana mpendwa ambaye hatimaye alitumwa na bwana wa shamba kwenda kwa watumwa wale wasiotii, na ambaye **(597)** alikamatwa nao na kuuawa, makuhani na wakuu waliiona picha ya Yesu na hatima yake iliyokuwa inakaribia. Tayari walikuwa wanapanga kumwua Yeye aliyekuwa ametumwa na Baba kama hatua ya mwisho. Katika ile hukumu iliyotajwa kuwastahili wale wakulima waovu kuliashiriwa hatima ya uangamivu wa wale ambao wangemwua Kristo.

Akiwa anawatazama kwa huruma, Mwokozi aliendelea, "Hamkupata kusoma katika maandiko, Jiwe walilolikataa waashi, Hilo limekuwa jiwe kuu la pembeni; Neno hili limetoka kwa Bwana, Nalo ni ajabu machoni petu? Kwa sababu hiyo nawaambia, Ufalme wa Mungu utaondolewa kwenu, nao watapewa taifa lingine lenye kuzaa matunda yake. Naye aangukaye juu ya jiwe hilo atavunjika-vunjika; naye yeyote ambaye litamwangukia, litamsaga tikitiki."

Wayahudi walikuwa wamerudia mara kwa mara unabii huu katika sinagogi, wakiuhusianisha na Masihi ajaye. Kristo alikuwa jiwe la pembeni la jamii ya Wayahudi, na la mpango mzima wa wokovu. Jiwe hili la msingi ndilo ambalo sasa makuhani na wakuu wa Israeli wanalikataa. Mwokozi alivuta mawazo yao kuelekea katika unabii ambao ungewaonyesha hatari yao. Kwa kutumia kila njia iliyowezekana kwake alitafuta namna ya kuwaonyesha hali halisi ya matendo waliyotaka kufanya.

Tena maneno yake yalikuwa na kusudi jingine. Katika kule kuuliza swali kwamba, "Basi atakapokuja yule bwana wa shamba la mizabibu, atawatendaje wale wakulima?" Kristo alitarajia wale Mafarisayo wajibu kama walivyojibu. Alipanga kwamba wao wajihuku wenyewe. Maonyo yake, ambayo yalikuwa yanashindwa kuwaamsha ili kutubu, yangetia muhuri uangamivu wao, na alitaka waone kwamba wamejiletea uharibifu wao wenyewe. Alitaka kuwaonyesha haki ya Mungu katika kuondoa upendeleo wake kwa taifa lile, ambayo ilikuwa imekwisha kuanza tayari, na ambayo ingeishia, si katika uharibifu wa hekalu lao na mji wao tu, bali katika kusambaratika kwa taifa hilo.

Wale wasikilizaji walilielewa hilo onyo. Lakini licha ya kauli ya hukumu waliyotoa wenyewe, makuhani na wakuu walikuwa wako tayari kuitimiza picha ile kwa kusema, "Huyu ni mrithi; haya na tumwue." "Nao walipotafuta kumkamata, waliwaogopa makutano," maana hisia za watu wengi zilikuwa katika upande wa Kristo.

Katika kunukuu unabii wa jiwe lililokataliwa, Kristo alirejea katika tukio halisi lililotokea katika historia ya Israeli. Tukio hilo lilihusianishwa na ujenzi wa hekalu lile la kwanza. Wakati lilikuwa na maana yake katika ujio wa Kristo mara ya kwanza, na lilipaswa kuleta msukumo maalum kwa Wayahudi, lina somo pia kwetu. Wakati hekalu la Sulemani **(598)** lilipokuwa linajengwa, mawe makubwa mazuri kwa ajili ya ukuta na msingi yaliandaliliwa kwa sehemu kubwa kule kule yalikochimbwa; baada ya kuletwa mahali pa jengo, hakuna zana iliyotakiwa kutumika kuchonga mawe hayo; wajenzi walipaswa tu kuyabandika mahali pake. Kwa ajili ya kutumika katika ujenzi wa msingi, jiwe moja lenye ukubwa usio wa kawaida na lenye umbo la pekee lilikuwa limeletwa; lakini wajenzi hawakuweza kupata mahali palipofaa kwa ajili ya jiwe lile, na kwa hiyo hawakulikubali. Lilikuwa kero kwao maana lilikuwepo tu katika njia yao bila kutumika. Lilibaki pale kwa muda mrefu likiwa jiwe lililokataliwa. Lakini pindi wajenzi walipokuja katika hatua ya kuweka jiwe la pembeni, walitafuta kwa muda mrefu ili kupata jiwe lenye ukubwa uliofaa na lenye nguvu iliyotakiwa, na lenye umbo sahihi, ili kuchukua nafasi ile, na lenye kuweza kuhimili uzito ambao ungejengwa juu yake. Ikiwa wangefanya uamuzi usio wa busara kwa ajili ya sehemu hii muhimu, usalama wa jengo lote ungekuwa hatarini. Lazima wapate jiwe lenye uwezo wa kuhimili nguvu za jua, za theluji, na za dhoruba. Mawe kadhaa yalikuwa yamechaguliwa kwa nyakati tofauti-tofauti, lakini chini ya mgandamizo wa uzito ule mkubwa yalikuwa yamevunjika vipande vipande. Mengine hayakuweza kustahimili matokeo ya mabadiliko ya ghafla ya hali ya hewa. Lakini hatimaye mwitikio ulielekea kwenye jiwe lile lililokataliwa kwa muda mrefu. Lilikuwa limewekwa mahali lilipokutana na hewa, jua, na dhoruba, lakini halikuonyesha ufa hata kidogo. Wale wajenzi walilichunguza jiwe hili. Lilikuwa limepitia kila kipimo isipokuwa kimoja tu. Waliamua kwamba ikiwa lingehimili ule uzito mkubwa sana, basi wangelikubali kutumika kama jiwe la pembeni. Kipimo kilifanywa. Lile jiwe likakubalika, likaletwa katika nafasi yake iliyokubalika, na likaonekana kufaa kabisa mahali pale. Katika kuona kinabii, Isaya alionyeshwa kwamba jiwe hili lilikuwa kiwakilishi cha Yesu. Anasema:

"Bwana wa majeshi ndiye mtakayemtakasa; na awe yeye hofu yenu, na awe yeye utisho wenu. Naye atakuwa ni mahali patakatifu; bali ni jiwe la kujikwaza na mwamba wa kujikwaa kwa nyumba za Israeli zote mbili, na mtego na tanzi kwa wenyeji wa Yerusalemu. Na wengi watajikwaa juu yake, na kuanguka na kuvunjika, na kunaswa na kukamatwa." Akichukuliwa kwenda mbele katika maono ya unabii mpaka wakati wa kuja kwa Kristo mara ya kwanza, nabii huyo anaonyeshwa kwamba Kristo atastahimili majaribu na mateso yaliyowakilishwa na jiwe kuu la pembeni la hekalu la Sulemani. "Kwa ajili ya hayo Bwana, MUNGU, asema hivi, Tazama, naweka jiwe katika Sayuni, liwe msingi, jiwe lililojaribiwa, jiwe la pembeni lenye thamani, msingi ulio imara; yeye aaminiye hatafanya haraka." Isaya 8:13-15; 28:16.

Katika hekima ya kimbingu, Mungu alichagua jiwe la msingi, naye akaliweka. Aliliita "msingi ulio imara." Ulimwengu wote unaweza kuweka mizigo na masumbuko yake yote juu ya huo; unaweza kuyastahimili yote hayo. Wote wanaweza kujenga juu ya huo kwa usalama kamili. Kristo ni "jiwe lililojaribiwa." Wale wanaomwamini, hatawafadhaisha kamwe. Ameshinda kila kipimo. Amestahimili uzito **(599)** wa hatia ya Adamu, na hatia ya uzao wake wote uliofuata, naye ameibuka akiwa zaidi ya mshindi aliyeshinda nguvu za uovu. Amebeba mizigo aliyotupiwa na kila mdhambi aliyetubu. Katika Kristo moyo wenye hatia umepata kuwa huru. Yeye ni msingi wa uhakika. Wote wanaomfanya kuwa tegemeo lao wako katika usalama ulio mkamilifu.

Katika unabii wa Isaya, Kristo anatajwa kuwa vitu viwili, msingi ulio imara na jiwe la kujikwaa. Mtume Petro, akiandika kwa uvuvio wa Roho Mtakatifu, anawaonyesha kwa uwazi watu wale ambao kwao Kristo ni jiwe la msingi, na kwa wale ambao kwao ni mwamba uangushao:

"Ikiwa mmeonja ya kwamba Bwana ni mwenye fadhili. Mmwendee yeye, jiwe lililo hai, lililokataliwa na wanadamu, bali kwa Mungu ni teule, lenye heshima. Ninyi nanyi, kama mawe yaliyo hai, mmejengwa mwe nyumba ya Roho, ukuhani mtakatifu, mtoe dhabihu za roho, zinazokubaliwa na Mungu, kwa njia ya Yesu Kristo. Kwa kuwa imeandikwa katika maandiko Tazama, naweka katika Sayuni jiwe kuu la pembeni, teule, lenye heshima, Na kila amwaminiye hatatahayarika. Basi, heshima hii ni kwenu ninyi mnaoamini. Bali kwao wasioamini, Tena, Jiwe la kujikwaza mguu na mwamba wa kuangusha. Kwa maana hujikwaza kwa neno lile, wasiliamini, nao waliwekwa kusudi wapate hayo." 1 Ptro 2:3-8.

Kwa wale waaminio, Kristo ni msingi ulio imara. Hawa ni wale waangukiao kwenye Mwamba na wakavunjika. Kinachowakilishwa hapa ni hali ya kujisalimisha kwa Kristo na kuwa na imani katika Yeye. Kuangukia kwenye Mwamba na kuvunjika ni kusalimisha hali ya kujihesabia haki na kwenda kwa Kristo kwa unyenyekevu wa mtoto, tukitubu maovu yetu, na tukiamini katika upendo wake unaosamehe. Vivyo hivyo pia, kwa imani na utii tunajenga kwenye msingi wetu ambao ni Kristo.

Kwa namna iliyo sawa, Wayahudi na Mataifa wanaweza kujenga kwenye jiwe hili lililo hai. Hili ndilo jiwe pekee ambalo tunaweza kujenga kwake kwa usalama. Ni pana sana kiasi cha kuwatosha wote, nalo lina nguvu sana kiasi cha kustahimili kubeba uzito wa mzigo wa ulimwengu wote. Na kuunganishwa na Kristo, aliye jiwe lililo hai, wote wanaojenga kwenye msingi huu wanakuwa mawe yaliyo hai. Watu wengi wanajitahidi kuchongwa, kusawazishwa na kufanywa wazuri kwa uwezo wao wenyewe; lakini hawawezi kuwa "mawe yaliyo hai," kwa sababu hawakuunganishwa na Kristo. Pasipo mwunganiko huu, hakuna mwanadamu anayeweza kuokolewa. Bila kuwa na maisha ya Kristo ndani yetu, hatuwezi kustahimili dhoruba za majaribu. Usalama wetu wa kudumu unategemea hali yetu ya kujenga kwenye mwamba wa uhakika. Makutano wengi leo wanajenga kwenye msingi ambao haujajaribiwa. Mvua inaponyesha, na pepo zikavuma, na mafuriko jakaja, **(600)** nyumba yao itaanguka, kwa sababu haikujengwa kwenye Msingi wa milele, Yesu Kristo aliye jiwe kuu la pembeni.

Kwa wale wanojikwaza kwa neno, Kristo ni mwamba wa kuangusha. Lakini "jiwe walilolikataa waashi, Hilo limekuwa jiwe kuu la pembeni." Kama lilivyo jiwe lile lililokataliwa, Kristo katika kazi yake ya duniani alikuwa amebeba kupuuzwa na kutendewa mabaya. "Alidharauliwa na kukataliwa na watu; Mtu wa huzuni nyingi, ajuaye sikitiko; . . . Alidharauliwa wala hatukumhesabu kuwa kitu." Isaya 53:3. Lakini muda wake wa kutukuzwa ulikuwa karibu. Kwa kule kufufuka kutoka katika wafu angetangazwa "kwa uweza kuwa Mwana wa Mungu." Warumi 1:4. Wakati ajapo mara ya pili angedhihirishwa kama Bwana wa mbinguni na duniani. Wale ambao kwa sasa walitaka kumsulibisha wangetambua ukuu wake. Lile jiwe lililokataliwa lingekuwa jiwe kuu mbele ya malimwengu.

Na kwa "yeyote ambaye litamwangukia, litamsaga tikitiki." Watu wale waliomkataa Kristo muda si mrefu wangeona mji wao na taifa lao vikiharibiwa. Utukufu wake ungevunjwa, na kutawanywa kama mavumbi ya upepo. Lakini kilichowaharibu Wayahudi ni nini? Ilikuwa ni mwamba ambao, ikiwa wangejenga juu yake, ungekuwa salama yao. Ilikuwa ni wema wa Mungu uliodharauliwa, haki iliyokataliwa, rehema iliyopuuzwa. Wanadamu walijipanga kuwa kinyume na Mungu, na yote ambayo yangekuwa wokovu wao yaligeuka na kuwa uharibifu. Walikuta yale yote yaliyotolewa na Mungu kuleta uzima yakiwapeleka katika mauti. Katika kitendo cha Wayahudi kumsulibisha Kristo kulikuwa na uangamivu wa Yerusalemu. Damu ile iliyomwagwa Kalvari ilikuwa ni uzito uliowazamisha katika uangamivu kwa ulimwengu huu na ule ujao. Hivyo ndivyo itakavyokuwa siku kuu ya mwisho, wakati hukumu itakapowaangukia wale walioikataa neema ya Mungu. Kristo, aliye jiwe la kuangusha, ndipo atakapoonekana kwao akiwa kama mlima wa hukumu. Utukufu wa mwonekano wake, ambao kwa wenye haki ni uzima, kwa waovu utakuwa moto ulao. Kwa sababu ya upendo uliokataliwa, neema iliyodharauliwa, mwenye dhambi ataharibiwa.

Kwa kutumia vielelezo vingi na maonyo yaliyorudiwa-rudiwa, Yesu alionyesha kile ambacho kwa Wayahudi kingekuwa matokeo ya kumkataa Mwana wa Mungu. Katika maneno haya alikuwa akiwaambia watu wote wa kila kizazi wanaokataa kumpokea kama Mkombozi wao. Kila onyo limewekwa kwa ajili yao. Hekalu takatifu lililoharibiwa, yule mwana asiye mtiifu, wakulima wa shamba wakaidi, wajenzi wakorofi, vinajitokeza katika uzoefu wa kila mdhambi. Ikiwa hafanyi toba, yale maangamizi ambayo yalisemwa kuwa matokeo ya vitendo hivyo itakuwa sehemu ya mtu huyo.

## Sura ya 66

# Makabiliano

[Sura hii imejengwa katika Mathayo 22:15-46; Marko 12:13-40; Luka 20:20-47.]

Makuhani na wakuu walikuwa wamesikiliza kwa ukimya makemeo ya Kristo. Hawakuweza kukana maneno yake. Lakini walikuwa wale watu walioazimia zaidi kumtega ili kumnasa, na kwa lengo hilo walituma kwake wapelelezi, "waliojifanya kuwa watu wa haki, ili wamnase katika maneno yake, wapate kumtia katika enzi na mamlaka ya liwali." Hawakupeleka Mafarisayo wale wa zamani ambao Yesu alikuwa ameshakutana nao mara nyingi, bali walituma vijana, waliokuwa wanaonekana wenye hamasa na hamu, na ambao waliwadhania kwamba hawafahamiki kwa Kristo. Hawa waliambatana pamoja na Maherodi kadhaa, ambao wangesikia maneno ya Kristo, ili ya kwamba wawe mashahidi dhidi yake katika mashtaka yake. Mafarisayo na Maherodi walikuwa maadui wakubwa sana, lakini walikuwa kitu kimoja katika kufanya uadui dhidi ya Kristo.

Daima Mafarisayo walikuwa wamekerwa na hali ya kuelemewa na kodi ambayo Warumi waliwatoza. Walichukulia kwamba kulipa kodi ile ilikuwa kinyume na sheria ya Mungu. Sasa walipaona mahali penye fursa ya kumtega Yesu. Wale wapelelezi walimjia, huku wakijifanya kuwa wema, kama vile ni watu wenye hamu ya kufahamu wajibu wao, wakasema, "Mwalimu, twajua ya kwamba wasema na kufundisha yaliyo ya haki, wala hujali cheo cha mtu, bali unafundisha njia ya Mungu kwa kweli. Je! Ni halali tumpe Kaisari kodi, au sivyo?"

**(602)** Yale maneno kwamba, "twajua ya kwamba wasema na kufundisha yaliyo ya haki," ikiwa yangekuwa ya dhati, yangekuwa ni ya kukiri kwa ajabu. Lakini yalisemwa ili kudanganya; wala ushuhuda wao haukuwa wa kweli. Mafarisayo walijua kwamba Kristo alisema na kufundisha kwa usahihi, na kwa ushuhuda wao huo watahukumiwa.

Wale waliouliza swali hilo kwa Yesu walidhani kwamba walikuwa wameficha kikamilifu kusudi lao; lakini Yesu alisoma mioyo yao kama asomaye kitabu kilicho wazi, na akaona unafiki wao. "Mbona mnanijaribu?" alisema; kwa njia hiyo akiwapa ishara ambayo hawakuwa wameuliza, kwa kuwaonyesha kwamba alisoma kusudi lao lililofichwa. Walikuwa bado wamechanganyikiwa wakati aliposema, "Nionyesheni dinari." Waliileta, naye akawauliza, "Ni ya nani sanamu hii na anwani hii? Wakamwambia, Ni ya Kaisari." Akionyesha kwenye anwani ile ambayo iko kwenye sarafu, Yesu alisema, "Basi, mlipeni Kaisari yaliyo ya Kaisari, na Mungu yaliyo ya Mungu."

Wale wapelelezi walikuwa wametarajia kwamba Yesu angejibu swali lao moja kwa moja, kwa kukubali upande mmoja au mwingine. Ikiwa angesema, Si halali kumpa Kaisari kodi, angeshtakiwa kwa mamlaka za Kirumi na kutiwa nguvuni kwa kuhamasisha uasi. Lakini ikiwa angesema kwamba ni halali kulipa kodi hiyo, walikusudia kumshtaki kwa watu kwamba anapingana na sheria ya Mungu. Sasa walijihisi kutatizwa na kushindwa. Mipango yao ilipanguka. Namna swali lao lilivyomalizwa kwa ufupi iliwaacha bila neno zaidi la kusema.

Jibu la Kristo halikuwa na kukwepa, bali lilikuwa jibu sahihi la dhati kwa swali lile. Akiwa ameshika sarafu ya Warumi mkononi mwake, ambayo ilikuwa na sura na jina la Kaisari, alitangaza kwamba kwa kuwa walikuwa wanaishi chini ya ulinzi wa mamlaka ya Warumi, iliwapasa kuipatia mamlaka hiyo kitu kile cha kuitegemeza ilichotaka, kwa kadiri ambavyo jambo hilo lisingepingana na kiwango cha juu cha wajibu wao. Lakini wakati wakitakiwa kuheshimu kwa amani sheria za nchi, iliwapasa wakati wote kutoa heshima yao ya kwanza kwa Mungu.

Yale maneno ya Mwokozi kwamba, "Mlipeni . . . Mungu yaliyo ya Mungu," yalikuwa ni kemeo kali kwa Wayahudi wale wenye njama. Ikiwa wangekuwa wametimiza kwa uaminifu wajibu wao kwa Mungu, wasingekuwa taifa lililovunjika, likitawaliwa na mamlaka ya kigeni. Hakuna bendera ya Kirumi ambayo ingepepea juu ya Yerusalemu, hakuna ulinzi wa Kirumi ambao ungekaa malangoni mwa mji huo, hakuna liwali wa Kirumi ambaye angetawala ndani ya kuta zake. Wakati huo taifa la Wayahudi lilikuwa linalipa adhabu ya uasi wao kwa Mungu.

Wale Mafarisayo waliposikia jibu la Kristo, "walistaajabu, wakamwacha, wakaenda zao." Alikuwa amekemea unafiki na ufidhuli wao, **(603)** na katika kufanya hili alikuwa ametamka kanuni kuu, kanuni inayobainisha mipaka ya wajibu wa mwanadamu kwa serikali ya kidunia na wajibu wake kwa Mungu. Katika akili za wengi

swali linalosumbua lilikuwa limejibiwa. Baada ya pale wangeishikilia kanuni hiyo sahihi. Na ingawa wengi waliondoka zao bila kuridhika, waliona kwamba msingi wa swali lile ulikuwa umewekwa vizuri, na walistaajabishwa na uwezo wa Yesu kuona mbali.

Haukupita muda baada ya Mafarisayo kunyamazishwa Masadukayo walijitokeza na maswali ya mitego. Hayo makundi mawili yalikuwa na uadui mkubwa. Mafarisayo walifuata sana mila za mapokeo. Walikuwa wafuatiliaji wa kutimiza maadhimisho ya nje na taratibu zake, wakiwa na bidii katika kutawadha, kufunga, na sala ndefu, na sadaka za kujionyesha. Lakini Kristo alisema kwamba waliiacha sheria ya Mungu kwa kufundisha maagizo ya wanadamu kama ndiyo mafundisho ya kidini. Wao walikuwa kama tabaka la watu mafidhuli na wanafiki; lakini walikuwemo miongoni mwao watu wenye upendo halisi, ambao waliyapokea mafundisho ya Kristo na wakawa wanafunzi wake. Masadukayo waliyakataa mapokeo ya Mafarisayo. Walidai kwamba wanaamini sehemu kubwa ya Maandiko, na kuyachukulia kwamba ni mwongozo wa maisha; lakini kivitendo walikuwa na mashaka na tamaa ya mali.

Masadukayo walikataa habari ya uwepo wa malaika, ufufuo wa waliokufa, na mafundisho kuhusu maisha ya baadaye, pamoja na thawabu na adhabu zake. Katika mambo haya yote walitofautiana na Mafarisayo. Katika mambo hayo yote suala la ufufuko au kiyama lilikuwa ndilo somo lenye ubishani mkubwa. Mafarisayo walikuwa waumini wakubwa kuhusu ufufuo, lakini katika majadiliano haya **(604)** mtazamo wao kuhusu hali ya maisha ya baadaye ulikuwa unaleta hali ya kuchanganyikiwa. Kwao kifo kilikuwa fumbo lisiloelezeka. Hali yao ya kukosa uwezo wa kukabili hoja za Masadukayo kuhusu kifo ilileta usumbufu wa kudumu. Majadiliano kati ya pande hizo mbili mara kwa mara yalisababisha mabishano ya hasira, yakizidi kuongeza pengo kati yao kuliko ilivyokuwa kabla.

Kuhusu wingi wa watu Masadukayo walikuwa nyuma sana kwa mbali kuliko wapinzani wao hao, na hawakuwa na nguvu ya kuungwa mkono sana miongoni mwa watu wa kawaida; lakini wengi wao walikuwa na utajiri, na walikuwa na ushawishi unaosababishwa na mali. Miongoni mwao walikuwemo makuhani walio wengi, na mara kwa mara kuhani mkuu alichaguliwa kutoka miongoni mwao. Hata hivyo, hilo lilifanywa kwa masharti ya wazi kwamba itikadi yao ya kuwa na wasiwasi na baadhi ya mafundisho isitawale. Kwa sababu ya idadi na umaarufu wa Mafarisayo, ilikuwa lazima kwa Masadukayo kukubaliana na mafundisho ya Mafarisayo kwa nje tu wakati walipokuwa wakishikilia utumishi wowote wa kikuhani; lakini ile hali yenyewe ya kwamba walikuwa na sifa za kuwa katika utumishi ule ilileta ushawishi wa kueneza makosa yao.

Masadukayo walikataa mafundisho ya Yesu; alikuwa anasukumwa na roho ambayo hawakuweza kuikiri vile ilivyojidhihirisha; na mafundisho yake kuhusu Mungu na maisha yajayo yalipingana na nadharia zao. Waliamini kwamba Mungu ndiye kitu hai pekee ambacho kiko juu kuliko mwanadamu; lakini walitoa hoja kwamba uwezo wa juu na usimamizi wa kimungu ungemnyang'anya mwanadamu uwezo wa kuwa huru kimaadili, na kumshusha hadi kuwa kama mtumwa. Imani yao ilikuwa kwamba, akisha kumwumba mwanadamu, Mungu alikuwa amemwacha yeye peke yake, akiwa huru pasipo kutawaliwa na mamlaka nyingine ya juu kuliko yeye. Walishikilia imani kwamba mwanadamu alikuwa huru kuendesha maisha yake mwenyewe na kuelekeza matukio ya ulimwengu huu; kwamba hatima yake ilikuwa mikononi mwake mwenyewe. Walikataa dhana ya kwamba Roho wa Mungu hufanya kazi kupitia jitihada za mwanadamu au njia za asili. Lakini bado walisema kwamba, kwa njia ya kutumia vizuri uwezo wake wa asili, mwanadamu angeweza kuinuliwa na kuangaziwa ufahamu zaidi; kwamba maisha yake yangefanywa safi kwa kufanya mambo sawasawa na kwa usahihi.

Mawazo yao kuhusu Mungu ndiyo yaliyoumba tabia yao. Kwa mujibu wa mtazamo wao Mungu hakuwa na jambo la kufanya kwa wanadamu, kwa hiyo walikuwa na hali ndogo sana ya mtu kujali mtu mwingine; kulikuwa na mwunganiko kidogo sana wa kimahusiano miongoni mwao. Wakiwa wanakataa kutambua kazi ya Roho Mtakatifu katika matendo ya mtu, walikosa nguvu zake maishani mwao. Kama walivyokuwa Wayahudi wengine, hawa nao walijidaia haki yao ya kuzaliwa kama watoto wa Ibrahimu, na ya bidii yao ya kutii kweli-kweli matakwa ya sheria; lakini walikosa roho ya kweli ya sheria na imani na ukarimu vilivyokuwa kwa Ibrahimu. Hisia zao za asili za huruma zilifanywa kuwa finyu. Waliamini kwamba inawezekana kwa watu wote kupata **(605)** raha na baraka za maisha; kwa hiyo mioyo yao haikuguswa na mahitaji na shida za watu wengine. Waliishi kwa ajili ya maisha yao wenyewe.

Kwa maneno yake na matendo yake, Kristo alifanya ushuhuda kuhusu nguvu ya Mungu iletayo matokeo yaliyo juu kuliko ya mwanadamu, kuhusu maisha ya mbele yaliyo ng'ambo ya haya ya sasa, kuhusu Mungu aliye Baba wa watoto wa wanadamu, akiangalia daima haja zao halisi, alifunua utendaji kazi wa nguvu ile ya Mungu iliyo katika ukarimu na huruma iliyokemea hali ya upekee wa ubinafsi wa Masadukayo. Alifundisha kwamba Mungu huusukuma moyo kwa njia ya Roho Mtakatifu kwa ajili ya mahitaji ya mwanadamu ya ulimwengu huu na yale ya maisha ya milele. Alionyesha makosa ya kutumainia uwezo wa mwanadamu kupata badiliko lile la tabia ambalo linaweza kutendwa na Roho wa Mungu pekee.

Hili ni fundisho ambalo Masadukayo walikuwa wameamua kulikataa. Kwa kule kutafuta kupambana na Kristo, walijisikia kuwa na uwezo wa kumfikisha mahali pa kutoheshimika, hata kama wasingeweza kufanikiwa kumhukumu. Ufufuo ndiyo mada waliyochagua kuitumia kumwuliza. Ikiwa angekubaliana nao, bado angekuwa amewakwaza Mafarisayo. Ikiwa atatofautiana nao, walikuwa wamepanga kuonyesha kwamba mafundisho yake hayafai.

Masadukayo walikuwa na hoja kwamba ikiwa mwili wa hali ya kutokufa unaundwa na viini vya mada ambavyo ni kama vile vya mwili unaokufa, basi utakapofufuliwa kutoka katika wafu lazima uwe na nyama na damu, na lazima katika ulimwengu ule wa milele mwili huo urejee katika maisha yale yale yaliyokatizwa duniani. Kwa hali hiyo walihitimisha kwamba mahusiano ya duniani yataendelezwa, mume na mke wataunganishwa tena, ndoa zitarejeshwa, na vitu vyote vitaendelea kama vile vilivyokuwa kabla ya kufa, madhaifu na maumivu ya maisha haya yakidumishwa hata katika maisha yajayo.

Katika jibu la maswali yao, Yesu alifunua pazia linalofunika maisha yajayo. Alisema, "Katika kiyama hawaoi wala hawaolewi, bali huwa kama malaika mbinguni." Alionyesha kwamba Masadukayo hawakuwa sahihi katika imani yao. Vigezo vyao vya hoja havikuwa sahihi. "Mwapotea, kwa kuwa hamyajui maandiko wala uweza wa Mungu," aliongeza. Hakuwalaumu kama alivyolaumu Mafarisayo, wenye unafiki, bali kwa kuwa hawa walikuwa na kosa katika imani yao.

Masadukayo walikuwa wamejigamba kwamba katika wanadamu wote wao ndio waliokuwa wakiyashika kweli kweli Maandiko. Lakini Yesu alionyesha kwamba walikuwa hawajui maana ya kweli ya Maandiko. Kwamba lazima maarifa yaletwe mahali pake moyoni kwa kuangaziwa na Roho Mtakatifu. Alitangaza kwamba hali yao ya kutojua Maandiko na uweza wa Mungu ndiyo sababu ya **(606)** kuchanganya imani na giza akilini. Walikuwa wanatafuta kuzileta siri za Mungu ndani ya mipaka ya mawazo yao finyu. Kristo aliwapa wito wa kuzifungulia mawazo yao zile kweli takatifu ambazo zingepanua na kuimarisha uelewa wao. Maelfu ya watu wanakuwa wasioamini kwa kuwa mawazo yao finyu hayawezi kuzielewa siri za Mungu. Hawawezi kueleza udhihirisho wa ajabu wa uweza wa Mungu katika ukuu wake, kwa hiyo wanakana ushahidi wa uweza huo, wakiuhusianisha na nguvu za asili ambazo nazo pia bado wanazielewa kwa kiasi kidogo sana. Ufunguo pekee wa kufungulia siri zinazotuzunguka ni kukiri kuwepo kwa uweza wa Mungu ndani ya hizo. Wanadamu wanahitaji kumtambua Mungu kama Mwumbaji wa malimwengu, Yeye anayeamrisha na kuendesha vitu vyote. Wanahitaji muono mpana wa tabia yake, na wa siri ya nguvu zake.

Kristo aliwaambia wasikilizaji wake kwamba ikiwa kusingekuwa na ufufuo wa wafu, Maandiko waliyodai kuyaamini yasingekuwa na maana. Alisema hivi, "Tena kwa habari ya kiyama ya wafu, hamjalisoma neno lililonenwa na Mungu, akisema, Mimi ni Mungu wa Ibrahimu, na Mungu wa Isaka, na Mungu wa Yakobo? Mungu si Mungu wa wafu, bali wa walio hai." Mungu huviona vitu visivyokuwepo kwa namna ile ambavyo vingekuwa kama vingekuwepo. Anaona mwisho tokea mwanzo, na huona matokeo ya kazi yake kama ile iliyokwisha kukamilika. Wenye thamani waliokufa, tangu Adamu mpaka mtakatifu wa mwisho anayekufa, wataisikia sauti ya Mwana wa Mungu, nao watatoka makaburini kwenda katika maisha ya kutokufa. Mungu atakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu wake. Kutakuwa na uhusiano wa karibu na wa upendo kati ya Mungu na watakatifu watakaokuwa wamefufuliwa. Mungu anaiona hali hii, inayotazamiwa katika kusudi lake, kama vile tayari sasa ipo. Waliokufa wanaishi katika Yeye.

Wale Masadukayo walinyamazishwa na maneno hayo ya Kristo. Hawakuweza kumjibu. Hakuna hata neno moja ambalo hata fursa ndogo ingepatikana ya kulitumia kumshtaki. Wapinzani wake wale hawakuwa wamefaidiwa kitu isipokuwa kulaumiwa na watu.

Hata hivyo, Mafarisayo wao hawakupoteza tumaini la kupata uwezekano wa kumsukuma kusema maneno ambayo wangeyatumia dhidi yake. Walimtumia mwandishi mmoja msomi ili amwulize Yesu kuhusu amri iliyo na umuhimu mkubwa kuliko zote katika sheria.

Mafarisayo walikuwa wametukuza sana amri nne za kwanza, ambazo zinaonyesha wajibu wa mwanadamu kwa Muumba wake, wakionyesha kwamba zina matokeo makubwa kwa mbali kuliko zile sita nyingine, ambazo zinabainisha wajibu wa mwanadamu kwa mwanadamu mwenzake. Kama matokeo yake, **(607)** walishindwa kwa kiwango kikubwa kutenda matendo ya utauwa. Yesu alikuwa amewaonyesha watu kuhusu mapungufu yao makubwa, na alikuwa amefundisha umuhimu wa matendo mema, akisema kwamba mti hujulikana kwa matunda yake. Kwa sababu hii alikuwa amelaumiwa kwamba anatukuza amri sita za mwisho na kuziweka juu ya zile nne za kwanza.

Mwanasheria yule akamkabili Yesu kwa swali la moja kwa moja, "Katika amri zote ni ipi iliyo ya kwanza?" Jibu la Kristo ni la moja kwa moja na lenye nguvu: "Ya kwanza ndiyo hii, Sikia, Israeli, Bwana Mungu wetu ni Bwana mmoja; nawe mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote, na kwa nguvu zako zote." Kristo akasema kwamba amri ya pili iko kama ya kwanza, maana inatoka ndani ya hiyo, inasema, "Mpende jirani yako kama nafsi yako. Hakuna amri nyingine iliyo kuu kuliko hizi." "Katika amri hizi mbili hutegemea torati yote na manabii."

Amri nne za kwanza katika amri kumi zinajumuishwa katika amri moja kwamba, "Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote." Zile sita za mwisho zinajumuishwa katika ile nyingine isemayo, "Mpende jirani yako kama nafsi yako." Amri zote hizi mbili ni udhihirisho wa upendo. Ya kwanza haiwezi kushikwa na nyingine ikavunjwa, wala ya pili haiwezi kushikwa wakati ile ya kwanza inavunjwa. Mungu anapokuwa katika nafasi yake sahihi katika kiti cha enzi cha moyoni, nafasi sahihi itatolewa kwa jirani yetu. Tutampenda kama tunavyojipenda. Na kadiri tu tunavyompenda Mungu kwa upendo wa juu ndipo inawezekana kumpenda jirani yetu kwa upendo usiogawanyika.

Na kwa kuwa amri zote zinajumuishwa pamoja kama upendo kwa Mungu na kwa mwanadamu, maana yake ni kwamba amri moja haiwezi kuvunjwa pasipo kukiuka msingi huu wa upendo. Kwa hiyo Kristo aliwafundisha wasikilizaji wake kwamba sheria ya Mungu si amri nyingi zilizotengana-tengana, nyingine zikiwa na umuhimu mkubwa, huku nyingine zikiwa na umuhimu mdogo na wakati mwingine zikawa za kupuuzwa. Bwana wetu anaonyesha amri nne za kwanza na amri sita za mwisho kama kitu kizima kimoja chenye asili ya mbinguni, na anafundisha kwamba upendo kwa Mungu utaonyeshwa kwa kutii amri zake zote.

Yule mwandishi aliyekuwa amemwuliza Yesu aliongozwa vema katika sheria, naye alishangazwa na maneno yake. Hakutarajia kwamba Yesu angedhihirisha ufahamu wa Maandiko kwa kina na ukweli wa namna ile. Alikuwa ameelewa mtazamo mpana wa misingi inayoshikilia amri takatifu. Alikiri kwa dhati pale pale mbele ya hadhara ya makuhani na wakuu kwamba Kristo alikuwa ametoa tafsiri sahihi ya sheria, kwa kusema: "Hakika, Mwalimu, umesema vema ya kwamba Mungu ni mmoja, wala hakuna mwingine ila yeye; na kumpenda yeye kwa moyo wote, na **(608)** kwa ufahamu wote, na kwa nguvu zote, na kumpenda jirani kama nafsi yako, kwafaa kuliko sadaka nzima za kuteketezwa na dhahibu zote pia."

Hekima ya jibu la Kristo ilikuwa imemsadikisha yule mwandishi. Alijua kwamba dini ya Wayhudi ilikuwa ya maonyesho ya nje badala ya upendo wa ndani. Alikuwa na ufahamu fulani wa kutostahili kwa sadaka za kimaadhimisho tu, na uchinjaji wa wanyama kwa ajili ya ondoleo la dhambi bila kuwa na imani. Upendo na utii kwa Mungu, na kumjali mwanadamu bila ubinafsi, vilionekana kwake vikiwa na thamani zaidi ya kaida zote hizo za kidini. Ule utayari wa mtu huyu kukubali usahihi wa hoja ya Kristo, na mwitikio wake mbele za watu wa kuazimia kwake na kusukumwa kutokea ndani yake, vilidhihirisha roho ambayo kwa kiasi kikubwa ni tofauti na ile ya makuhani na wakuu. Kwa upendo moyo wa Yesu ulimwendea yule mwandishi mwaminifu aliyekuwa amediriki kusimama mbele ya macho ya chuki ya makuhani na mbele ya vitisho vya wakuu akasema maneno ya kuonyesha usadikisho wa moyo wake. "Naye Yesu, alipoona kwamba amejibu kwa busara, alimwambia, Wewe hu mbali na ufalme wa Mungu."

Yule mwandishi alikuwa karibu na ufalme wa Mungu, kwa namna ya kwamba alitambua kwamba matendo ya haki yanakubalika kwa Mungu zaidi kuliko sadaka za kuteketezwa na dhabihu. Lakini alihitaji kutambua tabia ya

kimbingu ya Kristo, na kwa njia ya imani katika Yeye apokee nguvu ya kufanya matendo ya haki. Ibada ya maadhimisho ya kaida haikuwa na thamani yoyote, isipokuwa kama imeunganishwa na Kristo kwa imani iliyo hai. Hata sheria yenyewe ya maadili inaweza kushindwa kufikia makusudi sahihi, isipokuwa mpaka ieleweke kwa kuhusianishwa na Mwokozi. Kristo alikuwa ameonyesha tena na tena kwamba sheria ya Baba yake ilikuwa na kitu fulani cha kina kuliko amri tu ya kimamlaka. Katika sheria kumewekwa kanuni ile ile inayofunuliwa katika injili. Sheria inaonyesha wajibu wa mwnadamu na humwonyesha hatia yake. Lazima atafute kwa Kristo msamaha na nguvu ya kutenda kile kinachotakiwa na sheria.

Mafarisayo walikuwa wamemkusanyikia Yesu kwa karibu wakati alipokuwa anajibu swali lile la mwandishi. Sasa akiwageukia wao aliwauliza swali: "Mwaonaje katika habari za Kristo? Ni mwana wa nani?" Swali hili liliulizwa ili kuijaribu imani yao kumhusu Masihi, - kutaka kuonyesha ikiwa wanamchukulia kama mwanadamu wa kawaida au kama Mwana wa Mungu. Kibwagizo cha sauti nyingi kilijibu swali hilo kwamba, "Ni wa Daudi." Hili lilikuwa jina ambalo unabii ulilitoa kwa Masihi. Yesu alipodhihirisha uungu wake kwa miujiza yake mikuu, wakati alipowaponya wagonjwa na kufufua waliokufa, watu walikuwa wameulizana wao kwa wao, "Huyu siye mwana wa Daudi?" Yule mwanamke Msirofoinike, yule Bartimayo kipofu, na wengine wengi walikuwa wamemlilia kutaka msaada wakisema, "Unirehemu, Bwana, Mwana wa Daudi." Mathayo 15:22. Wakati akiwa amepanda mwanapunda kuingia Yerusalemu alikuwa amepambwa kwa **(609)** sauti za shangwe kwamba, "Hosana, Mwana wa Daudi; ndiye mbarikiwa, yeye ajaye kwa jina la Bwana." Mathayo 21:9. Na wale watoto wadogo kule hekaluni walikuwa wameimba siku ile nyimbo za shangwe za jina hilo. Lakini wengi waliomwita Yesu kwa jina hilo hawakutambua uungu wake. Hawakuelewa kwamba Mwana wa Daudi alikuwa pia Mwana wa Mungu.

Katika kujibu kauli ile kwamba Kristo alikuwa Mwana wa Daudi, Yesu alisema, "Imekuwaje basi Daudi katika Roho (Roho ya uvuvio kutoka kwa Mungu) kumwita Bwana, akisema, Bwana alimwambia Bwana wangu, Uketi mkono wa kuume, hata niwawekapo adui zako kuwa chini ya miguu yako? Basi, Daudi akimwita Bwana, amekuwaje ni mwanawe? Wala hakuweza mtu kumjibu neno; wala hakuthubutu mtu yeyote tangu siku ile kumwuliza neno tena."

## Sura ya 67

# Ole kwa Mafarisayo

[Sura hii imejengwa katika Mathayo. 23; Marko 12:41-44; Luka 20:45-47; 21:1-4.]

Ilikuwa ni siku ya mwisho ya Kristo kufundisha hekaluni. Usikivu wa makutano waliokuwa wamekusanyika Yerusalemu ulikuwa umevutwa kwake; watu walikuwa wamejazana katika viwanja vya hekalu, wakitazama pambano lililokuwa limeendelea, na kwa hamu walikamata kila neno lililotoka kinywani mwake. Kamwe mwonekano kama ule haukupata kushuhudiwa. Pale alisimama kijana wa Galilaya, akiwa haheshimiwi heshima ya kidunia wala alama ya ufalme. Waliokuwa wakimzunguka pande zote walikuwa makuhani waliokuwa katika nguo za kitajiri, wakuu wakiwa katika majoho na nembo zinazoonyesha ukuu wa vyeo vyao, na waandishi waliokuwa na magombo mikononi mwao, ambao walifanya rejea mara kwa mara. Yesu alisimama mbele yao kwa utulivu, akiwa kama mfalme. Akiwa kama ambaye amekabidhiwa mamlaka ya mbinguni, aliwatazama bila hofu wapinzani wake, ambao walikuwa wamekataa na kudharau mafundisho, na ambao walikuwa na kiu ya maisha yake. Walikuwa wamemshambulia kwa maswali wakiwa wengi; lakini mipango yao ya kumtega na kumhukumu ilikuwa kazi bure. Alikuwa amekutana na changamoto baada ya changamoto, akiwasilisha ukweli ulio safi na angavu ulio tofauti na giza na makosa ya makuhani na Mafarisayo. Alikuwa ameonyesha mbele ya viongozi hawa hali yao halisi, na hukumu ambayo hakika ingeifuata tabia ya kung'ang'ania matendo maovu. Onyo lilikuwa limetolewa kwa uaminifu. Lakini bado **(611)** kazi nyingine ilikuwa imebaki kwa ajili yake kufanya. Kusudi jingine lilikuwa bado likamilishwe.

Hamu ya watu katika kazi ya Kristo ilikuwa imeongezeka. Walishikwa na mafundisho yake, lakini walikuwa wameogopeshwa pia. Walikuwa wamewaheshimu makuhani na marabi kwa kuamini katika ufahamu wao na wema wao. Katika mambo yote ya dini wao waliishia kupata heshima na mamlaka. Sasa waliona watu wanaondoa wasiwasi waliokuwa nao juu ya Yesu, mwalimu ambaye wema wake na ufahamu wake viling'aa sana. Waliangalia mwonekano wa makuhani na wazee, waliona kwao kuaibika na kuchanganyikiwa. Walishangaa kuona wakuu wale hawamwamini Yesu, wakati mafundisho yake yalikuwa ya wazi na mepesi sana. Wao wenyewe hawakujua wafuate njia gani. Kwa hamu ya huzuni waliangalia waone mwelekeo wa wale wenye mashauri ambayo walikuwa wamefuata wakati wote.

Katika mifano ambayo Kristo alikuwa amesema, lengo lake lilikuwa ni kuwaonya wakuu na kufundisha watu ambao walikuwa radhi kufundishwa. Lakini kulikuwa na haja ya kusema kwa uwazi zaidi. Kupitia heshima yao kwa mapokeo na upofu wao katika ukuhani potofu, watu walikuwa **(612)** wamefanywa watumwa. Lazima Kristo avunje minyororo hii. Lazima tabia ya makuhani, wakuu, na Mafarisayo iwekwe wazi zaidi.

"Waandishi na Mafarisayo 'wameketi katika kiti cha Musa'; basi, yoyote watakayowaambia, myashike na kuyatenda; lakini kwa mfano wa matendo yao, msitende; maana wao hunena lakini hawatendi." Waandishi na Mafarisayo walidai kupewa mamlaka ya kimbingu sawa na ile ya Musa. Walijifanya kukalia nafasi yake kama watafsiri wa sheria na waamuzi wa watu. Kwa hiyo walidai kwa watu heshima na utii. Yesu aliwataka watu wafanye yale ambayo marabi walifundisha kwa mujibu wa sheria, lakini wasifuate kielelezo chao. Wao wenyewe hawakutenda mafundisho yao.

Na walifundisha mengi ambayo yalikuwa kinyume na Maandiko. Yesu alisema, "Wao hufunga mizigo mizito na kuwatwika watu mabegani mwao; wasitake wenyewe kuigusa kwa kidole chao." Mafarisayo walilundika lundo la kanuni, ambazo zilikuwa na msingi wake katika mapokeo, na pasipo sababu zilidhibiti uhuru wa mtu. Na sehemu fulani za sheria zile walizieleza kwa namna ambayo zinaagiza kwa watu maadhimisho ambayo hata wao wenyewe waliyapuuza kisirisiri, na ambayo, walipotakiwa wao kuyafuata, walidai kwamba haziwahusu.

Kufanya maonyesho ya wema wao lilikuwa kusudi lao la wakati wote. Hakuna kitu kilichokuwa kitakatifu zaidi kiasi cha kuondoa lengo hili. Kuhusu amri Mungu alikuwa amemwambia Musa, "Yafunge yawe dalili juu ya mkono wako, nayo yatakuwa kama utepe katikati ya macho yako." Kumbukumbu 6:8. Maneno haya yana maana ya kina. Kadiri neno la Mungu linavyotafakariwa na kutendwa, mwanadamu atainuliwa kwa ujumla. Katika kutenda kwa haki na rehema, mikono itafunua, kama muhuri, kanuni ya sheria ya Mungu. Itahifadhiwa safi mbali

na rushwa, na mbali na vyote vilivyo vibaya na vya udanganyifu. Itakuwa myepesi katika matendo ya upendo na huruma. Macho, yakiwa yameelekezwa katika kusudi jema, yatakuwa wazi na ya kweli. Mwonekano wa mwili, kuongea kwa macho, vitadhihirisha tabia isiyolaumiwa kitu kwa mtu apendaye na kuheshimu neno la Mungu. Lakini yote haya hayakuzingatiwa na Wayahudi wa siku za Kristo. Amri iliyotolewa kwa Musa ilitafsiriwa katika uelekeo kwamba kanuni za Maandiko zivaliwe na mtu. Ziliandikwa hivyo pia kwenye kipande cha karatasi ya ngozi, na kufungwa kichwani au mkononi kwa namna ambayo zinaweza kusomeka. Lakini hali hii haikufanya sheria ya Mungu kuwa imara katika akili na moyo. Vikaratasi vya ngozi hivyo vilivaliwa tu kama nembo, **(613)** kuvuta usikivu. Vilifikiriwa kumpa mvaaji hali ya kuwa mtu wa dini ambapo ingevuta hali ya kuheshimiwa na watu. Yesu alipiga katika hali hii ya kuigiza:

"Tena matendo yao yote huyatenda ili kutazamwa na watu; kwa kuwa hupanua hirizi zao, huongeza matamvua yao; hupenda viti vya mbele katika karamu, na kuketi mbele katika masinagogi, na kusalimiwa masokoni, na kuitwa na watu, Rabi. Bali ninyi msiitwe Rabi, maana mwalimu wenu ni mmoja, nanyi nyote ni ndugu. Wala msimwite mtu baba duniani; maana Baba yenu ni mmoja, aliye wa mbinguni. Wala msiitwe viongozi; maana kiongozi wenu ni mmoja, naye ndiye Kristo." Katika maneno ya wazi kiasi hicho Mwokozi alifunua dhamira ya ubinafsi iliyofika mbali, ikionyesha unyenyekevu wa unafiki, wakati moyo ulikuwa umejawa na ulafi na husuda. Wakati watu walipoalikwa karamuni, wageni walikuwa wanakaa kulingana na hadhi yao, na wale waliopewa nafasi ya heshima kubwa kuliko zote walihudumiwa kwanza na kupata upendeleo. Daima Mafarisayo walikuwa wanajitahidi kupata heshima hizi. Yesu alikemea vitendo hivi.

Alikemea pia kiburi kilichoonyeshwa katika kutafuta cheo cha rabi, au bwana. Cheo kile, alisema, si cha mwanadamu, bali cha Kristo. Makuhani, waandishi, na wakuu, watafsiri na wasimamizi wa sheria, wote walikuwa ndugu, watoto wa Baba mmoja. Yesu aliwafundisha watu kwamba wasimpe mwanadamu yeyote cheo cha heshima kinachoashiria uwezo wake wa kudhibiti dhamiri zao na imani yao.

Yesu angelikuwa duniani leo, akizungukwa na wale wanaoitwa "Mchungaji" au "Askofu," Je, asingerudia maneno yake kwamba, "Wala msiitwe viongozi; maana kiongozi wenu ni mmoja, naye ndiye Kristo"? Maandiko yanasema hivi kuhusu Mungu, "Jina lake ni takatifu la kuogopwa." Zaburi 111:9. Ni mwanadamu gani anayestahili jina hilo? Mwanadamu anadhihirisha hali ya chini kiasi gani kinyume cha hekima na haki inayoonyeshwa na jina hilo! Ni wangapi kati ya hao wanaokalia cheo hiki ambao wanawakilisha vibaya jina na tabia ya Mungu! Jamani, ni mara nyingi kiasi gani tamaa ya makuu ya ulimwengu, udhalimu, na dhambi mbaya zaidi vimefichwa chini ya mavazi ya vyeo vya juu na vitakatifu! Mwokozi aliendelea:

"Naye aliye mkubwa wenu atakuwa mtumishi wenu. Na yeyote atakayejikweza, atadhiliwa; na yeyote atakayejidhili, atakwezwa." Tena na tena Kristo alikuwa amefundisha kwamba ukuu wa kweli unapimwa na maadili. Katika kipimo cha mbinguni, ukuu wa tabia unahusisha kuishi kwa ajili ya ustawi wa wanadamu wenzetu, katika **(614)** kufanya matendo ya upendo na rehema. Kristo Mfalme wa utukufu alikuwa mtumishi wa mwanadamu aliyeanguka.

Alisema, "Ole wenu waandishi na Mafarisayo, wanafiki! Kwa kuwa mnawafungia watu ufalme wa mbinguni; ninyi wenyewe hamwingii, wala wanaoingia hamwaachi waingie." Kwa kupotosha Maandiko, makuhani na wanasheria walipofusha akili za wale ambao vinginevyo wangekuwa wamepokea kuujua ufalme wa Kristo, na yale maisha ya ndani, ya kimbingu ambayo ni ya muhimu kwa utakatifu wa kweli.

"Ole wenu waandishi na Mafarisayo, wanafiki! Kwa kuwa mnakula nyumba za wajane, na kwa unafiki mnasali sala ndefu; kwa hiyo mtapata hukumu iliyo kubwa zaidi." Mafarisayo walikuwa na ushawishi mkubwa kwa watu, na hivyo walitumia hali hii kutafuta maslahi yao. Waliaminiwa na wajane, na halafu wakajionyesha kwamba wana wajibu kwa mali zao katika mambo ya dini. Wakishapata udhibiti wa pesa zao, wajanja hawa walizitumia kwa faida yao wenyewe. Ili kufunika udanganyifu wao, walifanya sala ndefu za hadhara, na walitenda matendo ya kujionyesha kuwa wema. Yesu alitangaza kwamba unafiki huu ungewaletea hukumu kuu. Kemeo lile lile linawaangukia wengi katika siku zetu wanaojidai kuwa wema sana. Maisha yao yamefungwa na ubinafsi na uchoyo, na bado wanatupia juu ya hayo yote vazi la kujionyesha kuwa safi, na kwa namna hiyo kwa muda huo wanawadanganya wanadamu wenzao. Lakini hawawezi kumdanganya Mungu. Anasoma kila kusudi la moyo, naye atamhukumu kila mtu kwa kadiri ya matendo yake.

Yesu anahukumu dhuluma bila huruma, lakini alikuwa makini asishushe chini uwajibikaji. Alikemea ubinafsi ule ulioharibu na kutumia vibaya mali ya mjane. Wakati huo huo alimpongeza mjane aliyeleta sadaka yake kwa ajili ya hazina ya Mungu. Matumizi mabaya ya mwanadamu ya sadaka hayakuweza kuzuia mbaraka wa Mungu kwa mtoaji.

Yesu alikuwa katika sehemu ambapo kulikuwa na chombo cha hazina, na aliangalia wale walioleta sadaka zao. Wengi miongoni mwa matajiri walileta pesa nyingi, ambazo walitoa kwa madaha ya kujionyesha. Yesu aliwatazama kwa huzuni, lakini hakusema neno juu ya kutoa kwao kwa uhuru. Mwonekano wake ulionekana kuwaka alipomwona maskini mjane akisogea kwa kusita-sita, kama vile akiogopa kuonekana. Kadiri matajiri na wenye madaha walivyokwisha kupita, kutoa sadaka zao, alirudi nyuma kama vile kutaka kupata ujasiri zaidi. Lakini alitamani kufanya jambo fulani, ingawa kidogo kama kilivyokuwa, kwa ajili ya kazi aliyopenda. Aliiangalia sadaka yake mkononi mwake. Ilikuwa ndogo sana ikilinganishwa na sadaka za wale waliokuwa karibu naye, lakini ilikuwa ndiyo yake yote. **(615)** Akiangalia fursa yake, aliharakisha kutupa mle senti mbili zake, na akageuka na kuharakisha kuondoka. Lakini katika kufanya hili alivutia jicho la Yesu, ambalo lilikuwa limekazwa kwake.

Yesu aliwaita wanafunzi wake kwake, na kuwataka waone umakini wa mwanamke yule mjane. Halafu maneno yake ya kumsifu yakamfuata: "Amin, nawaambia, Huyu mjane maskini ametia zaidi kuliko wote." Machozi ya furaha yalijaza macho ya yule mama kadiri alivyohisi kwamba tendo lake lilithaminiwa na kueleweka. Wengi wangekuwa wamemshauri abaki na senti zake kwa ajili ya matumizi yake; kwamba ikipelekwa katika mikono ya makuhani ambao wanalishwa vizuri, ingepotea kuonekana katika sadaka kubwa zilizoletwa katika hazina. Lakini Yesu alielewa msukumo aliokuwa nao. Mwanamke yule aliamini kwamba huduma ya hekalu ilikuwa imeamriwa na Mungu, na alikuwa na hamu ya kufanya kubwa awezalo kuliwezesha. Alifanya awezalo, na tendo lake lilikuwa kumbukumbu yake wakati wote, na furaha yake milele. Moyo wake uliienda na sadaka yake; thamani yake ilikadiriwa, si kwa thamani ya sarafu, bali kwa upendo wake kwa Mungu na shauku katika kazi ya Mungu iliyosukuma kitendo hiki.

Yesu alisema kuhusu maskini yule mjane, "Ametia zaidi kuliko wote." Matajiri walikuwa wametoa kutoka katika vingi, wengi ili kuonekana na kusifiwa na watu. Matoleo yao makubwa hayajawanyang'anya raha, au starehe; hayakudai kafara, na hayakuweza kulinganishwa na senti ya mjane.

Msukumo ndio unaoleta tabia ya matendo yetu, ukiyatia muhuri kuonyesha kutokufaa kwake au kustahili kwake kwa viwango vya uadilifu mkubwa. Mungu hahesabu thamani kwa kuangalia ukubwa wa vitu ambavyo kila jicho linaona na kila ulimi kusifia. Majukumu madogo ambayo hufanywa kwa moyo wa kupenda, sadaka ndogo zisizo za maonyesho, na ambazo kwa macho ya mwanadamu zinaweza kuonekana zisizostahili, ndizo zinazoonekana za kiwango cha juu machoni pake. Moyo wenye imani na upendo ndio unaopendwa zaidi na Mungu kuliko sadaka za gharama kubwa mno. Yule maskini mjane alitoa maisha yake katika tendo lile dogo alilolifanya. Alijinyang'anya chakula ili apate kutoa zile senti mbili kwa ajili ya kazi aliyopenda. Naye alifanya vile kwa imani, akiamini kwamba Baba yake wa mbinguni asingepuuza kuona uhitaji wake mkubwa. Hii roho isiyo ya ubinafsi na imani kama ya mtoto ndivyo vilivyovuta ukubali kutoka kwa Mwokozi.

Miongoni mwa maskini kuna watu wengi wanaotamani kuonyesha shukrani zao kwa Mungu kwa ajili ya neema na ukweli wake. Wanatamani sana kushirikiana na ndugu zao waliojaliwa mali zaidi katika kuipeleka mbele kazi yake. Roho hizi zisizimishwe. Hebu na watoe senti zao katika benki ya mbinguni. Ikiwa zinatolewa kwa moyo uliojawa na upendo kwa Mungu, hizi zinazoonekana ndogo zinakuwa sadaka zilizobarikiwa, dhabihu isiyokadirika gharama yake, ambayo inamfanya Mungu kutabasamu na kubariki.

**(616)** Yesu aliposema kuhusu mjane yule kwamba, alikuwa "ametia zaidi kuliko wote," maneno yake yalikuwa ya kweli, si tu kwa msukumo, bali pia hata matokeo ya sadaka yake. Zile "senti mbili, kiasi cha nusu pesa" zimeleta katika hazina ya Mungu kiasi kikubwa cha pesa kwa mbali kuliko michango ya Wayahudi wale matajiri. Matokeo ya sadaka ile ndogo yamekuwa kama mto, ambao huwa mdogo unakoanzia, lakini ukipanuka na kuongezeka kina kadiri unavyotiririka kupita katika vizazi. Kwa njia maelfu imechangia kuwapa ahueni maskini na kuineza injili. Kielelezo chake cha kujitoa kimefanya kazi na kuleta mabadiliko katika mioyo ya maelfu walioko katika kila nchi na katika kila kizazi. Imewagusa wote wawili, yaani, matajiri na maskini, na sadaka zao zimetanua thamani ya sadaka yake. Mbaraka wa Mungu kwa senti ya mjane umeifanya kuwa chanzo cha

matokeo makubwa. Hivyo ndivyo ilivyo kwa kila sadaka inayotolewa na kila tendo linalotendwa kwa moyo wa dhati kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Inaunganishwa na makusudi yake Aliye Juu. Hakuna mwanadamu anayeweza kupima matokeo ya sadaka hiyo kwa ajili ya mema.

Mwokozi aliendelea na makemeo yake kwa waandishi na Mafarisayo: "Ole wenu viongozi vipofu, ninyi msemao, Mtu atakayeapa kwa hekalu, si kitu; bali mtu atakayeapa kwa dhahabu ya hekalu, amejifunga! Wapumbavu ninyi na vipofu; maana ni ipi iliyo kubwa, ile dhahabu, au lile hekalu liitakasayo dhahabu?" Makuhani walitafsiri matakwa ya Mungu kulingana na viwango vyao wenyewe vilivyo finyu na visivyo sahihi. Walijifanya kutambulika kama watu wanaoweza kubainisha mambo mema dhidi ya mambo yaletayo hatia ya dhambi za namna mbalimbali, wakiyapita baadhi ya mambo mepesi, na kuyaona mengine ambayo huenda hayana umuhimu mkubwa kama vile ni makosa yasiyosameheka. Kwa kuangalia pesa waliwasamehe watu viapo vyao. Na kwa kulipwa fedha nyingi walijifanya hawaoni uhalifu uliokuwa mkubwa. Wakati huo huo makuhani hawa na wakuu walitoa adhabu kali kwa makosa madogo.

"Ole wenu waandishi na Mafarisayo, wanafiki! Kwa kuwa mnalipa zaka za mnanaa na bizari na jira, lakini mmeacha mambo makuu ya sheria, yaani, adili, na rehema, na imani; hayo imewapasa kuyafanya, wala yale mengine msiyaache." Katika maneno haya Kristo anakemea tena matumizi mabaya ya majukumu matakatifu. Jukumu lenyewe hili haliweki kando. Mfumo wa kutoa zaka ulianzishwa na Mungu, na ulifuatwa tangu nyakati za kale zaidi. Ibrahimu, aliye baba wa waaminifu alilipa zaka ya vyote alivyokuwa navyo. Watawala wa Kiyahudi walitambua jukumu hilo la zaka, na hilo lilikuwa sahihi; lakini hawakuwaacha watu wavutwe wenyewe kufanya **(617)** wajibu wao huo. Kanuni zisizo maana ziliwekwa katika kila jambo. Matakwa yalikuwa na utata mchangamano mkubwa kiasi kwamba ilikuwa jambo lisilowezekana kwao kuzifuata. Hakuna aliyejua kwamba ni katika hatua ipi alikuwa ametekeleza wajibu wake. Kama Mungu alivyoutoa, mfumo huo ulikuwa wa haki na mzuri; lakini makuhani na marabi walikuwa wameufanya kuwa mzigo wa kuchosha.

Yote ambayo Mungu huagiza yana matokeo. Kristo alitambua ulipaji wa zaka kama wajibu; lakini alionyesha kwamba hili lisingefanya kisingizio cha kuacha majukumu mengine. Mafarisayo walikuwa wanakazania na kutekeleza sana kutoa zaka za mboga za majani ya bustani, kama vile mnanaa, bizari, na jira; hili haliwagharimu sana, liliwapa kutambuliwa kwa utoaji na utakatifu. Wakati huo huo vizuizi visivyo na maana viliwakandamiza watu na kuharibu heshima ya mfumo huo mtakatifu wa watu walioteuliwa na Mungu. Walijaza mawazo ya watu kwa taratibu za kutofautisha, na wakageuza hamu yao kutoka katika ukweli muhimu. Yale mambo yenye uzito zaidi ya sheria, yalipuuzwa. Kristo alisema, "Hayo imewapasa kuyafanya, wala yale mengine msiyaache."

Sheria nyingine pia zilikuwa zimepotoshwa na marabi kwa namna hiyo hiyo. Katika maelekezo yaliyotolewa kupitia Musa ilikataliwa kula kitu chochote kilicho kichafu. Ulaji wa nyama ya nguruwe, na nyama za wanyama wengine kadhaa, ulikatazwa, ili wasijaze uchafu katika damu yao na kufupisha maisha yao. Lakini Mafarisayo hawakuyaacha makatazo hayo kama Mungu alivyokuwa amewapa. Walienda mbele katika misimamo mikali ambayo haikuruhusiwa. Miongoni mwa mambo mengine waliyotakiwa kufanya, watu walitakiwa kuchuja maji yote ya kutumia, ili yasije yakabakiwa na mdudu hata aliye mdogo, ambaye angeweza kuangukia katika kundi la wanyama wasio safi. Yesu akionyesha mkinzano uliokuwepo kati taratibu hizi ndogo na ukubwa wa dhambi walizokuwa wanafanya, aliwaambia Mafarisayo, Ninyi "viongozi vipofu, wenye kuchuja mbu na kumeza ngamia."

"Ole wenu, waandishi na Mafarisayo, wanafiki! Kwa kuwa mmefanana na makaburi yaliyopakwa chokaa, nayo kwa nje yaonekana kuwa mazuri, bali ndani yamejaa mifupa ya wafu, na uchafu wote." Kama vile kaburi lililopakwa chokaa na kupambwa kwa uzuri linavyoficha masalia ya miili iliyooza, ndivyo utakatifu wa nje wa makuhani na wakuu ulivykuwa umeficha uovu. Yesu aliendelea hivi:

"Ole wenu, waandishi na Mafarisayo, wanafiki! Kwa kuwa mnayajenga makaburi ya manabii, na kuyapamba maziara ya wenye haki, na kusema, Kama sisi tungalikuwako zamani za baba zetu, hatungalishirikiana nao katika damu ya manabii. Hivi mwajishuhudia wenyewe, ya kwamba ninyi ni wana wao **(618)** waliowaua manabii." Kuonyesha kuthamini manabii waliokufa, Wayahudi walikuwa na bidii sana katika kuyasafisha makaburi yao; lakini hawakunufaika na mafundisho yao, wala hawakusikiza maonyo yao.

Mnamo nyakati za Kristo hali ya kishirikina ilikuwa inafanywa kwa ajili ya sehemu walipolala waliokufa, na kiasi kikubwa cha pesa kilitumika katika kuyapamba makaburi. Machoni pa Mungu hii ilikuwa ibada ya sanamu.

Katika hali hii ya kuwajali waliokufa, watu walionyesha kwamba hawakumpenda Mungu zaidi, wala hawakumpenda jirani kama wanavyojipenda. Ibada ya sanamu kama hiyo hufanywa kwa kiwango kikubwa leo. Wengi wana hatia ya kupuuza kuhudumia wajane na yatima, wagonjwa na maskini, huku wakijenga minara ya gharama kubwa ya kumbukumbu kwa ajili ya waliokufa. Muda, fedha na nguvu zinatumiwa kwa uhuru kabisa katika kusudi hili, wakati wajibu kwa walio hai – wajibu ambao Kristo ameagiza wazi wazi – unaachwa bila kutimizwa.

Mafarisayo walijengea makaburi ya manabii, na waliyapamba, nao waliambiana wao kwa wao kwamba, Ikiwa tungeishi mnamo kipindi kile cha baba zetu, tusingeungana nao katika kumwaga damu ya watumishi wa Mungu. Lakini wakati huo huo walikuwa wanapanga kuyaondoa maisha ya Mwana wa Mungu. Hebu hali hii iwe somo kwetu. Inaweza kufungua macho yetu tukaona nguvu za Shetani katika kudanganya akili zinazogeuka kuiacha nuru ya ukweli. Watu wengi wanafuata katika njia ile ya Mafarisayo. Wanaheshimu watu wale ambao wamekufa kwa sababu ya imani yao. Wanaushangaa upofu wa Wayahudi kwa kitendo chao cha kumkataa Kristo. Wanasema kwamba, Ikiwa tungeishi wakati ule Kristo alipokuwepo, tungepokea mafundisho yake kwa furaha; kamwe tusingeshiriki katika hatia ya wale waliomkataa Mwokozi. Lakini wakati utii kwa Mungu unapodai hali ya kujikana nafsi na kujinyenyekeza, watu hawa hawa wanakataa wito wao, na kukataa kutii. Kwa njia hiyo wanadhihirisha roho ile ile iliyodhihirishwa na Mafarisayo ambao walikemewa na Yesu.

Wayahudi walijua kidogo sana kuhusu namna watakavyowajibishwa vibaya kwa kumkataa Kristo. Kuanzia wakati ule damu isiyo na hatia ilipomwagwa kwa mara ya kwanza, wakati Habili mwenye haki alipokufa kwa mkono wa Kaini, historia hiyo ilikuwa imerudiwa-rudiwa, pamoja na kuongezeka kwa hatia. Katika kila kizazi manabii walikuwa wameinua sauti zao dhidi ya dhambi za wafalme, wakuu na watu, wakisema maneno waliyopewa na Mungu, na wakitii mapenzi yake hata kwa hatari ya kupoteza maisha yao. Kutoka kizazi hata kizazi adhabu ya watu waliokataa nuru na ukweli inakusanyika kama lundo. Maadui hawa wa Kristo walikuwa sasa wanajibebesha lundo hili vichwani mwao. Dhambi ya makuhani na wakuu ilikuwa kubwa zaidi kuliko ilivyokuwa katika vizazi vilivyotangulia. Kwa kumkataa kwao Mwokozi, walikuwa wamejifanya kuwajibika **(619)** kwa ajili ya damu ya wote wenye haki waliouawa tangu Habili hadi Kristo. Walikuwa wanakaribia kukijaza kikombe cha uovu hadi kiasi cha kufurika. Na muda si mrefu kilikuwa kimwagwe vichwani mwao katika kupatilizwa kwa haki. Kuhusu habari hii, Yesu aliwaonya hivi:

"Hivyo ije juu yenu damu yote ya haki iliyomwagika juu ya nchi, tangu damu ya Habili, yule mwenye haki, hata damu ya Zakaria bin Barakia, mliyemwua kati ya patakatifu na madhabahu. Amin, nawaambieni, Mambo hayo yote yatakuja juu ya kizazi hiki."

Waandishi na Mafarisayo waliomsikiliza Yesu walijua kwamba maneno yake yalikuwa ya kweli. Walijua jinsi nabii Zakaria alivyouawa. Wakati maneno ya maonyo yalipokuwa yanatoka midomoni mwake, ghadhabu ya kishetani ilimjaa mfalme mwasi, na kwa amri yake nabii huyo aliuawa. Damu yake ilijipakaza kwenye mawe yale ya viwanja vya hekalu, wala haikuwezekana kuipangusa kutoka pale; ilisalia pale ikiwa kama ushuhuda dhidi ya Israeli aliyeasi. Kwa muda wote ambao hekalu lile lingesimama, kungekuwa na doa la damu ile ya mwenye haki, ikimlilia Mungu ili alipize kisasi. Kadiri Yesu alivyowarejesha katika matukio haya ya kuogofya, dalili ya hofu ilionekana miongoni mwa makutano.

Akitazama mbele, Yesu alisema kwamba kutotubu kwa Wayahudi na tabia yao ya kushindwa kuonyesha uvumilivu kwa watumishi wa Mungu vingekuwa jinsi ile ile katika siku za usoni kama ilivyokuwa huko nyuma:

"Kwa sababu hiyo, angalieni, mimi natuma kwenu manabii na wenye hekima na waandishi; na wengine wao ninyi mtawaua na kuwasulibisha, na wengine wao mtawapiga katika masinagogi yenu, na kuwafukuza mji kwa mji." Manabii na wenye hekima, wakijawa imani na Roho Mtakatifu, - Stefano, Yakobo, na wengine wengi, - wangehukumiwa na kuuawa. Kwa mkono ulioinuliwa juu mbinguni, na nuru ya kimbingu ikizunguka mwili wake, Kristo aliwaambia wale waliokuwa mbele yake akiwa kama hakimu. Sauti yake, ambayo ilikuwa imesikika mara nyingi ikiwa ya upole na kujali, sasa ilisikika ikikemea na kuhukumu. Wasikilizaji walitetemeka. Msukumo uliofanywa na maneno na matendo yake usingewezekana kuepukwa.

Makemeo ya Yesu yalikuwa dhidi ya unafiki, dhambi pana, ambazo kwa hizo watu walikuwa wakiziharibu roho zao wenyewe, wakiwadanganya watu na kutokumheshimu Mungu. Katika hoja za uongo za makuhani na wakuu

zilizoonekana kama za ukweli Yesu aliona nguvu za kishetani zikifanya kazi. Alikuwa ameikemea dhambi kwa maumivu na uchungu; lakini hakunena neno lolote la kisasi. Alikuwa na hasira takatifu dhidi ya mfalme wa giza; lakini hakujaribu kufanya hasira za kulipiza. Hivyo ndivyo Mkristo anayeishi kwa kupatana na Mungu, akiwa na tabia tamu za upendo na huruma, atakavyohisi kuwa na **(620)** hasira ya haki dhidi ya dhambi; wala hatakuwa na hisia za hasira ya kudhuru wale wanaomdhuru. Hata anapokutana na wale wanaosukumwa na nguvu itokayo kuzimu ili kuendeleza uongo, bado atahifadhi utulivu na kujitawala katika Kristo.

Upendo wa mbinguni ulikuwa katika sura ya Mwana wa Mungu alipolitazama hekalu na halafu kuwaangalia wasikilizaji wake. Kwa sauti yenye kusongwa na maumivu mazito ya moyo na machozi machungu alisema, "Ee Yerusalemu, Yerusalemu, uwauaye manabii, na kuwapiga kwa mawe wale waliotumwa kwako! Ni mara ngapi nimetaka kuwakusanya pamoja watoto wako, kama vile kuku avikusanyavyo pamoja vifaranga vyake chini ya mabawa yake, lakini hamkutaka!" Haya ni mapambano ya mwisho-mwisho wakati wa kutengana. Katika maombolezo haya ya Kristo moyo wenyewe wa Mungu ulimwagika. Hilo lilikuwa fumbo la kwa heri la uvumilivu wa upendo wa Mungu kwao.

Kwa namna inayofanana Mafarisayo na Masadukayo walinyamazishwa. Yesu aliwahutubia wanafunzi wake, na alijiandaa kuondoka, si kama mtu aliyeshindwa na kulazimishwa kuondoka kwa adui zake, bali kama mtu ambaye kazi yake imekamilika. Alipumzika akiwa mshindi katika mapambano.

Lulu ya ukweli iliyotoka katika midomo ya Kristo katika siku ile ya matukio mengi iliwekwa kama hazina katika mioyo ya watu wengi. Kwao mawazo mapya yalihuishwa na kuwa hai, matarajio mapya yaliamshwa, na historia mpya ilianza. Baada ya kusulibiwa na kufufuka kwa Kristo, watu hawa walikuja katika mstari wa mbele, na walilitimiza agizo la mbingu kwa kutumia hekima na juhudi iliyoendana na ukubwa wa kazi. Waliupeleka ujumbe uliogusa mioyo ya watu, ukidhoofisha ushirikina wa zamani ambao ulikuwa umeleta hali ya ubandia katika maisha ya maelfu ya watu. Mbele ya ushuhuda wao nadharia na falsafa za wanadamu zilikuwa kama hadithi za kubuni. Matokeo yaliyotiririka kutoka katika maneno ya Kristo yalikuwa ya uweza mkuu kwa umati ule uliokuwa unashangaa na kutekewa mle ndani ya hekalu la Yerusalemu.

Lakini Israeli kama taifa lilikuwa limejiachanisha na Mungu. Matawi ya asili ya mti wa mtende yalivunjika. Akiangalia kwa mara ya mwisho kule ndani ya hekalu, Yesu alisema kwa sauti ya huruma, "Angalieni, nyumba yenu mmeachiwa hali ya ukiwa. Kwa maana nawaambia, Hamtaniona kamwe tangu sasa, hata mtakaposema, Amebarikiwa ajaye kwa jina la Bwana." Mpaka wakati huu Kristo alikuwa ameliita hekalu lile nyumba ya Babab yake; lakini sasa pindi Mwana wa Mungu alipokuwa anatoka katika viwanja vya kuta zile, uwepo wa Mungu ungeondolewa milele kutoka katika hekalu lile lililojengwa kwa ajili ya utukufu wake. Kuanzia wakati huo maadhimisho ya humo ndani yasingekuwa na maana, na huduma zake zingekuwa ni dhihaka.

## Sura ya 68

# Katika Uwanja wa Nje

[Sura hii imejengwa katika Yohana 12:20-43.]

“Palikuwa na Wayunani kadha wa kadha miongoni mwa watu waliokwea kwenda kuabudu kwenye sikukuu. Basi hao walimwendea Filipo, mtu wa Bethsaida ya Galilaya, wakamwomba, wakisema, Bwana, sisi tunataka kumwona Yesu. Filipo akaenda, akamwambia Andrea; kisha Andrea na Filipo wakamwambia Yesu."

Wakati huu kazi ya Kristo ilikuwa imepata kushinda sana. Alikuwa amekuwa mshindi katika pambano lake dhidi ya makuhani na Mafarisayo. Kutengana kwa mwisho kulikuwa kumefika. Hali hii ilionekana kutokuwa na matumaini kwa wanafunzi. Lakini Yesu alikuwa anakaribia kumaliza kazi yake. Tukio kuu ambalo halikuhusu taifa la Wayahudi pekee bali ulimwengu lilikuwa linakaribia kutokea. Yesu aliposikia ombi la shauku kwamba, "Tunataka kumwona Yesu," likitoa mwangwi wa kilio cha wenye njaa walioko ulimwenguni, sura yake iliwaka, naye akasema, "Saa imefika atukuzwe Mwana wa Adamu." Katika lile ombi la Wayunani kulikuwa na matokeo ya kafara yake kuu.

Watu hawa walikuja kumtafuta Mwokozi wakati wa mwisho wa maisha yake wakitokea Magharibi, kama vile ambavyo mamajusi wale wa awali walitokea Mashariki. Mnamo wakati wa kuzaliwa kwa Kristo Wayahudi walikuwa wamezungushiwa mambo ya fikira zao wenyewe kiasi kwamba hawakujua kuhusu kuja kwake. Mamajusi wale **(622)** waliotoka katika nchi ya kipagani walikuja penye hori la ng’ombe wakiwa na zawadi zao, ili kumwabudu Mwokozi. Vivyo hivyo Wayunani hawa, wanaowakilisha mataifa, kabila, na watu wa ulimwengu, walikuja kumwona Yesu. Hivyo ndivyo ambavyo watu wa nchi zote na vizazi vyote wangevutwa na msalaba wa Mwokozi. Hivyo ndivyo ambavyo "watakuja kutoka mashariki na magharibi, nao wataketi pamoja na Ibrahimu, na Isaka, na Yakobo katika ufalme wa mbinguni." Mathayo 8:11.

Wayunani wale walikuwa wamesikia habari za Yesu kuingia Yerusalemu kwa ushindi. Baadhi walisambaza habari kwamba alikuwa amefukuza kutoka hekaluni makuhani na wakuu, na kwamba alikuwa achukue mamlaka ya kiti cha enzi cha Daudi, na kutawala kama mfalme wa Israeli. Wayunani wale walitafuta kujua ukweli kuhusu kazi yake. Walisema, "Tunataka kumwona Yesu." Ombi lao liliruhusiwa. Ombi lile lilipoletwa kwa Yesu, alikuwa katika sehemu ya hekalu ambayo watu wote walikuwa wametengwa naye isipokuwa Wayahudi, lakini alienda nje kwa Wayunani wale waliokuwa katika viwanja vya nje, naye alifanya nao mazungumzo.

Saa ya kutukuzwa kwa Kristo ilikuwa imekuja. Alikuwa amesimama katika kivuli cha msalaba, na swali lile la Wayunani lilikuwa limemwonyesha kwamba kafara ambayo alikuwa anaelekea kuifanya ingewaleta kwa Mungu wana na binti wengi. Alijua kwamba muda si mrefu Wayunani wale ambao hawakupata kuota wangemwona. Wangemwona akiwa amewekwa karibu na Baraba, yule mnyang’anyi na mwuaji, ambaye angechaguliwa kwamba awekwe huru kabla ya Mwana wa Mungu. Wangewasikia watu, wanaohimizwa na makuhani na wakuu, wakifanya chaguo lao. Na kuhusu lile swali lililoulizwa kwamba, "Nimtendeje Yesu aitwaye Kristo?" jibu lingetolewa kwamba, "Asulibishwe." Mathayo 27:22. Kwa kufanya huu upatanisho kwa ajili ya dhambi za wanadamu, Kristo alijua kwamba ufalme wake ungekamilishwa, nao ungetawanyika katika ulimwengu wote. Angefanya kazi ya Mrejeshaji, na Roho wake angeshinda. Kwa muda fulani alitazama kipindi kichacho, akazisikia sauti zikitoka katika sehemu zote za dunia zikisema, "Tazama Mwanakondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu." Yohana 1:29. Ndani ya watu hawa wageni aliyaona mavuno makubwa, wakati ukuta unaotenganisha kati ya Wayahudi na Mataifa utakapovunjwa na kuangushwa, na mataifa yote, lugha, na watu watakaposikia ujumbe wa wokovu. Udhihirisho wa hili, ukamilishaji wa matumaini yake, umeonyeshwa katika maneno haya, "Saa imefika atukuzwe Mwana wa Adamu." Lakini njia ambayo lazima itumike kutekeleza utukufu huu haikuwa mbali na mawazo ya Kristo. Kuwakusanyia ndani Mataifa kulikuwa kunafuata njia yake ya kifo iliyokuwa karibu. Ni kwa njia ya kifo chake tu ndipo ulimwengu ungeokolewa. Kama ilivyo kwa punje ya ngano **(623)** lazima Mwana wa Adamu atupwe katika ardhi na kufa, na azikwe asionekane; lakini angeishi tena.

Kristo alionyesha wakati wake wa mbele, akiueleza kwa vielelezo vya vitu vya asili, ili ya kwamba wanafunzi waelewe. Matokeo ya kweli ya kazi yake yangefikiwa kwa kifo chake. Alisema, "Amin, amin, nawaambia, Chembe

ya ngano isipoanguka katika nchi, ikafa, hukaa hali iyo hiyo peke yake; bali ikifa, hutoa mazao mengi." Punje ya ngano inapoanguka udongoni na kufa, inachipuka, na kuzaa matunda. Vivyo hivyo kifo cha Kristo kingeleta matokeo ya tunda la ufalme wa Mungu. Kama ilivyo kwa sheria inayotawala mimea, uhai ulikuwa uwe matokeo ya kifo chake.

Wale wanaolima ardhi wanacho kielelezo cha daima mbele yao. Kila mwaka mtu hufanya kazi ya kupata nafaka ya kutosha kwa njia inayoonekana kama ni kutupa sehemu ya nafaka iliyochaguliwa, kwa muda fulani inafichwa chini ya udongo, ili iangaliwe na Bwana. Halafu ndipo jani changa hutokea, halafu suke, na halafu ngano pevu katika suke. Lakini maendeleo haya hayawezi kufanyika ikiwa mbegu haikuzikwa, ikafichwa, isionekane, na ikawa kwa ujumla kama vile imepotea.

Mbegu iliyozikwa ardhini inazaa tunda, halafu hilo hupandwa tena. Kwa njia hiyo mavuno huzidishwa. Hivyo ndivyo ambavyo kifo cha Yesu msalabani kitazaa matunda ya uzima wa milele. Tafakari ya kafara hii itakuwa utukufu wa wale ambao, kama tunda lake, wataishi maisha ya milele.

Mbegu ya ngano inayosalia na uhai wake haiwezi kuzaa tunda. Inakaa hivyo peke yake. Kristo angeweza, kama angependa, kujiokoa na mauti yake. Lakini ikiwa angefanya hivyo, lazima asalie kuwa peke yake. Asingewaleta kwa Mungu wana na binti. Kwa kuyatoa maisha yake tu ndipo angewapa wanadamu uhai. Ni kwa kuanguka ardhini na kufa tu ndipo angekuwa mbegu ya mavuno yale mengi, - umati ule mkubwa ambao umekombolewa kwa Mungu kutoka katika kila taifa, na kabila, na lugha, na jamaa.

Yesu anaunganisha ukweli huu pamoja na somo la kujikana nafsi ambalo wote wanapaswa kujifunza: "Yeye aipendaye nafsi yake ataiangamiza; naye aichukiaye nafsi yake katika ulimwengu huu ataisalimisha hata uzima wa milele." Lazima wote wanaotaka kuzaa matunda kama watenda kazi pamoja na Kristo waanguke udongoni na kufa. Lazima maisha yatupwe katika udongo wa mahitaji ya ulimwengu. Lazima kujipenda binafsi, kujipendeza mwenyewe vipotee. Na sheria ya kujikana nafsi ni sheria ya kujihifadhi. Mkulima huhifadhi nafaka yake kwa njia ya kuitupa ardhini. Hivyo ndivyo ilivyo katika maisha ya mwanadamu. Kutoa ni kuishi. Maisha yatakayohifadhiwa ni yale yanayotolewa bure kumtumikia Mungu na mwanadamu. Wale ambao **(624)** wanayatoa maisha yao katika ulimwengu huu kwa ajili ya Kristo watayahifadhi mpaka kufika katika uzima wa milele.

Maisha yanayotumiwa kibinafsi ni kama chembe ambayo imeliwa. Inatoweka, wala hakuna kinachoongezeka. Mwanadamu anaweza akajikusanyia kwa ajili yake binafsi; anaweza kuishi na kufikiri na kupanga kwa ajili yake binafsi; lakini maisha yake hupita, naye hana kitu. Sheria ya kujihudumia mwenyewe ni sheria ya kujiangamiza mwenyewe.

Yesu alisema, "Mtu akinitumikia, na anifuate; nami nilipo, ndipo na mtumishi wangu atakapokuwapo. Tena mtu akinitumikia, Baba atamheshimu." Wote ambao wamebeba pamoja na Yesu msalaba wa kujitoa kafara watakuwa washirika wa utukufu wake pamoja naye. Furaha ya Kristo katika kujishusha kwake na kupata maumivu ilikuwa ni kwamba wanafunzi wake wapate kutukuzwa pamoja naye. Wao ni tunda la kujitoa kwake kafara. Utendaji kazi wa tabia na roho yake ndani yao ni zawadi yake, na itakuwa furaha yake milele zote. Raha hii wanayoshiriki pamoja naye kama tunda la kazi na kafara yao inaonekana katika mioyo mingine na kuishi. Wao ni watenda kazi pamoja na Kristo, naye Baba atawaheshimu kama anavyomheshimu Mwana wake.

Ule ujumbe wa Wayunani, uliokuwa ukitabiria kukusanywa ndani kwa Mataifa, ulileta katika mawazo ya Yesu kazi yake yote. Kazi ya ukombozi ilipita mbele yake, kuanzia wakati ule mpango huo ulipowekwa mbinguni, mpaka kwenye kifo chake ambacho sasa kilikuwa karibu. Wingu la kigeni lilionekana kama kumfunika Mwana wa Mungu. Mwangaza wa wingu hilo ulionekana kwa wale waliokuwa karibu yake. Alifungiwa katika mawazo. Hatimaye ukimya ulivunjwa na sauti yake ya kuomboleza akisema, "Sasa roho yangu imefadhaika; nami nisemeje? Baba, uniokoe katika saa hii?" ni kama vile Kristo alikuwa tayari anakinywea kikombe cha uchungu. Ubinadamu wake uliiogopa saa ile ya kuachwa peke yake, wakati ambapo kwa namna zote angeachwa hata na Mungu mwenyewe, wakati ambapo wote wangemwona kama amepigwa, amepigwa na Mungu, na kuteswa. Aliogopa kwa vile ambavyo umma ungemwona, akitendewa kama mhalifu mbaya kuliko wote, na kile kifo cha aibu na cha kudhalilisha. Utabiri wa pambano lake dhidi ya nguvu za giza, kujua habari ya mzigo wa kutisha, na

ghadhabu ya Baba kwa sababu ya dhambi vilisababisha roho ya Yesu kunyong'onyea, na picha ya kifo ikaitawala sura yake.

Halafu ulikuja wakati wa kujisalimisha katika mapenzi ya Baba yake. Alisema "Lakini ni kwa ajili ya hayo nilivyoifikia saa hii. Baba, ulitukuze jina lako." Ni kwa njia ya kifo cha Kristo tu ndipo ufalme wa Shetani ungepinduliwa. Ni kwa njia hiyo tu ndipo mwanadamu angekombolewa, na Mungu akatukuzwa. Yesu alikubali kupitia katika maumivu, alikubali kutoa kafara. Mtukufu wa mbinguni alikubali kuumia akiwa Mbeba Dhambi. Alisema, "Baba, ulitukuze jina lako." Pindi **(625)** Kristo aliposema maneno haya, mwitio ulikuja ukitoka katika wingu lililokuwa juu ya kichwa chake ukisema: "Nimelitukuza, nami nitalitukuza tena." Maisha yote ya Kristo, tangu horini pa ng'ombe mpaka wakati maneno haya yaliposemwa, alikuwa amemtukuza Mungu; na katika majaribu yaliyokuwa yanakuja maumivu yake ya uungu na ubinadamu yangelilitukuza kweli kweli jina la Baba yake.

Sauti ile iliposikika, nuru ilimlika kutoka katika wingu lile, ikamzunguka Kristo, kama vile mikono ya Mweza wa Yote ilirushwa kwake na kumzunguka kama ukuta wa moto. Watu waliloona tukio hili kwa hofu na mshangao. Hakuna aliyethubutu kuzungumza. Wote walisimama wakiwa kimya na macho yao yakiwa yamekazwa kwa Yesu. Baada ya ushuhuda wa Baba kuwa umetolewa, wingu lile lilinyenyuka, na kutawanyika mawinguni. Kwa muda ule ushirika uonekanao kati ya Baba na Mwana ulikoma.

"Basi mkutano uliosimama karibu wakasikia, walisema ya kwamba kumekuwa ngurumo; wengine walisema, Malaika amesema naye." Lakini wale Wayaunani waliokuja kuulizia waliliona wingu lile, waliisikia ile sauti, waliilewa maana yake, na walimwona Kristo kweli kweli; kwao alifunuliwa kama ni Aliyetumwa na Mungu.

Sauti ya Mungu ilikuwa imesikika wakati wa ubatizo wa Yesu mnamo mwanzo wa kazi yake, na kwa mara nyingine kule mlimani alipobadilika sura. Na sasa mnamo wakati wa kuifunga kazi yake ilisikika kwa mara ya tatu, ikisikiwa na watu wengi zaidi, tena katika mazingira ya pekee. Yesu alikuwa ametoa ukweli mahsusi unaohusu hali ya Wayahudi. Alikuwa ametoa wito wake wa mwisho, na kutangaza hatima yao ya kuangamia. Na sasa Mungu anatia muhuri tena kwenye kazi hii ya Mwana wake. Alimtambua Yeye ambaye amekataliwa na Israeli. Yesu alisema, "Sauti hiyo haikuwako kwa ajili yangu, bali kwa ajili yenu." Ilikuwa ni ushahidi wa kuvikwa taji ya Umasihi wake, kiashirio kutoka kwa Baba kwamba Yesu alikuwa amesema ukweli, na alikuwa Mwana wa Mungu.

Kristo aliendelea hivi, "Sasa hukumu ya ulimwengu huu ipo; sasa mkuu wa ulimwengu huu atatupwa nje. Nami nikiinuliwa juu ya nchi, nitawavuta wote kwangu. Aliyanena hayo akionyesha ni mauti gani atakayokufa." Hii ni hali ya hatari kwa ulimwengu. Ikiwa mimi nakuwa mpatanishi kwa dhambi za wanadamu, ulimwengu utaangaziwa. Ngome ya Shetani katika mioyo ya wanadamu itavunjwa. Sura ya Mungu iliyoharibiwa itarejeshwa kwa wanadamu, na hatimaye jamaa ya watakatifu waaminio watairithi nyumba ya mbinguni. Haya ni matokeo ya kifo cha Kristo. Mwokozi inaingia katika kutafakari tukio la ushindi lililo mbele yake. Anaouona msalaba, msalaba wenye ukatili na aibu, pamoja na kutisha kunakoambatana nao, uking'aa kwa utukufu.

**(626)** Lakini si kwamba msalaba unakamilisha kazi ya ukombozi wa mwanadamu tu. Unayadhihirishia malimwengu yote upendo wa Mungu. Mfalme wa ulimwengu huu anatupwa nje. Shutuma ambazo Shetani ameleta dhidi ya Mungu zinafutwa. Upinzani ambao ameufanya dhidi ya mbingu unaondolewa milele. Malaika na wanadamu wanavutwa kwa Mkombozi. Yeye alisema, "Nami nikiinuliwa juu ya nchi, nitawavuta wote kwangu."

Watu wengi walikuwa karibu na Kristo aliposema maneno haya, na mmoja wao akasema, "Sisi tumesikia katika torati ya kwamba Kristo adumu hata milele; nawe wasemaje ya kwamba imempasa Mwana wa Adamu kuinuliwa? Huyu Mwana wa Adamu ni nani? Basi Yesu akawaambia, Nuru ingaliko pamoja nanyi muda kidogo. Enendeni maadamu mnayo nuru hiyo, giza lisije likawaweza; maana aendaye gizani hajui aendako. Maadamu mnayo nuru, iaminini nuru hiyo, ili mpate kuwa wana wa nuru."

"Walakini ajapokuwa amefanya ishara nyingi namna hiyo mbele yao, hawakumwamini." Wakati fulani walikuwa wamemwuliza Mwokozi hivi, "Unafanya ishara gani basi, ili tuione tukakuamini?" Yohana 6:30. Ishara zisizohesabika zilikuwa zimetolewa; lakini walikuwa wamefumba macho yao na kuifanya migumu mioyo yao. Sasa kwa kuwa Baba mwenyewe alikuwa amenena, nao wasingedai ishara nyingine zaidi, ila bado walikataa kuamini.

"Walakini hata katika wakuu walikuwamo wengi waliomwamini; lakini kwa sababu ya Mafarisayo hawakumkiri, wasije wakatengwa na sinagogi." Walipenda sifa za watu kuliko kukubaliwa na Mungu. Ili kupona kejeli na aibu, walimkana Kristo, na waliikataa zawadi ya uzima wa milele. Ni wangapi ambao wamekuwa wakifanya jambo kama hilo katika karne zote tangu pale. Wote hao wanaambiwa na Mwokozi maneno haya: "Yeye apendaye maisha yake atayapoteza." Anasema pia kwamba, "Yeye anikataaye mimi, asiyeyakubali maneno yangu, anaye amhukumuye; neno hilo nililolinena ndilo litakalomhukumu siku ya mwisho." Yohana 12:48.

Ole ni kwa wale ambao hawakujua muda wa kujiliwa kwao! Pole pole na kwa maumivu Kristo aliliacha hekalu lile milele.

## Sura ya 69

# Kwenye Mlima wa Mizeituni

[Sura hii imejengwa katika Mathayo 24; Marko 13; Luka 21:5-38.]

Maneno ambayo Kristo aliwaambia wazee na makuhani kwamba, "Nyumba yenu mmeachiwa hali ya ukiwa" (Mathayo 23:38), yalitia woga mioyoni mwao. Yalileta chuki, lakini swali liliendelea kuinuka mawazoni mwao kuhusu umuhimu wa maneno haya. Hatari ilikuwa kama inawatisha. Je, ingewezekana kwamba hekalu lile la fahari, lililokuwa utukufu wa taifa, baadaye liwe lundo la uharibifu? Utabiri ule wa uovu ulijadiliwa na wanafunzi, na wakasubiri kwa hamu kupata kauli mahsusi kutoka kwa Yesu. Kadiri walivyoenda naye nje ya hekalu, walimvuta mawazo kuelekea katika uimara na uzuri wa jengo lile. Mawe ya hekalu ya marumaru safi, meupe, na baadhi yakiwa na ukubwa unaovutia yalilipendezesha. Sehemu ya ukuta wake ilikuwa imestahimili uvamizi wa jeshi la Nebukadneza. Katika ukamilifu wa ujenzi wake ukuta ule ulionekana kama jiwe moja gumu lililochimbwa zima-zima na kuwekwa pale. Wanafunzi wasingeelewa kwamba ni kwa jinsi gani hizo kuta za fahari zingeweza kubomoshwa.

Usikivu wa Yesu ulipovutwa kuelekea katika fahari ya hekalu lile, je, ni maneno gani ambayo hakusema lakini lazima yalikuwa ndiyo mawazo yake Yeye Aliyekataliwa! Mandhari ile iliyokuwa machoni pake ilikuwa ya kupendeza hasa, lakini akasema kwa huzuni kwamba, Nayaona yote. Majengo hayo ni ya kushangaza kabisa. Mnanionyesha hizi kuta kama vile haziwezi kuharibiwa kabisa; lakini sikilizeni maneno yangu, nawaambia: “Siku zitakuja ambapo halitasalia jiwe juu ya jiwe ambalo halitabomoshwa."

**(628)** Maneno aliyosema Kristo yalisikiwa na watu wengi; lakini wakati alipokuwa peke yake, Petro, Yohana, Yakobo na Andrea walikuja kwake akiwa amekaa kwenye Mlima wa Mizeituni. Wakasema, "Tuambie, mambo hayo yatakuwa lini? Nayo ni nini dalili ya kuja kwako, na ya mwisho wa dunia?" Yesu aliwajibu wanafunzi wale pasipo kutenganisha kati ya uharibifu wa Yerusalemu na siku kuu ya kuja kwake. Alichanganya maelezo ya matukio hayo mawili. Ikiwa angeweka wazi kwa wanafunzi wake matukio yajayo kama alivyoyaona Yeye, wasingeweza kustahimili hali ambayo wangeona. Kwa huruma yake kwao alichanganya maelezo ya zahama kuu mbili, akiwaacha wanafunzi wajifunze maana ya mambo hayo wao wenyewe. Wakati alipoongelea uharibifu wa Yerusalemu, maneno yake ya unabii yalivuka tukio lile hadi wakati wa mlipuko wa mwisho katika siku ile ambayo Bwana atainuka kutoka mahali pake ili kuwaadhibu walimwengu kwa maovu yao, wakati dunia itakapofichua damu iliyomo ndani yake, na wakati ambapo haitaendelea tena kuwafunika wale iliowaua. Maelezo yote haya yalitolewa, si kwa ajili ya wanafunzi wale tu, bali kwa ajili ya wote ambao wangeishi wakati wa matukio ya mwisho ya historia ya dunia.

Akiwageukia wanafunzi wake, Kristo alisema, "Angalieni mtu asiwadanganye. Kwa sababu wengi watakuja kwa jina langu, wakisema, Mimi ni Kristo; nao watadanganya wengi.” Akina masihi wengi wa bandia watatokea, wakidai kufanya miujiza, na kutangaza kwamba wakati wa kulikomboa taifa la Wayahudi umewadia. Hawa watapotosha wengi. Maneno ya Yesu yalitimia. Katika kipindi kilicho kati ya kifo chake na kuvamiwa kwa Yerusalemu mamasihi wengi wa uongo walitokea. Lakini onyo hili lilitolewa pia kwa wale wanaoishi katika zama hizi za ulimwengu. Udanganyifu ule ule uliofanywa kabla ya kuangamizwa kwa Yerusalemu umekuwa ukifanywa katika zama zote, na utafanywa tena.

"Nanyi mtasikia habari za vita na matetesi ya vita; angalieni, msitishwe; maana hayo hayana budi kutukia; lakini ule mwisho bado." Kabla ya kuharibiwa kwa Yerusalemu, watu walipambana kutafuta ukuu. Watawala waliuawa. Wale walioonekana kutaka kushika zamu ya kukalia kiti cha enzi walichinjwa. Kulikuwa na vita na tetesi za vita. "Hayo hayana budi kutukia," Kristo alisema, "lakini ule mwisho [wa taifa la Wayahudi kama taifa] bado. Kwa maana taifa litaondoka kupigana na taifa, na ufalme kupigana na ufalme; kutakuwa na njaa, na matetemeko ya nchi mahali mahali. Hayo yote ndiyo mwanzo wa utungu." Kristo alisema, Kadiri marabi wanavyoona dalili hizi, watatangaza kwamba hizo ni hukumu za Mungu za mwisho kwa mataifa kuwashikilia utumwani wateule wake. Watatangaza kwamba dalili hizi ni uwakilishi wa ujio wa **(629)** Masihi. Msidanganyike; hizo ni mwanzo wa hukumu zake. Watu wamejiangalia wao wenyewe. Hawakutubu na kuongoka ili niwaponye. Dalili wanazofikiri ni ishara ya kuwekwa huru kutoka katika utumwa ni dalili za kuharibiwa kwao.

"Wakati huo watawasaliti ninyi mpate dhiki, nao watawaua; nanyi mtakuwa watu wa kuchukiwa na mataifa yote kwa ajili ya jina langu. Ndipo wengi watakapojikwaa, nao watasalitiana, na kuchukiana." Wakristo walipatwa na yote haya. Kina baba na kina mama walisaliti watoto wao. Watoto waliwasaliti wazazi wao. Watu wenye uhusiano na urafiki wa karibu walipelekana hadi mbele ya Sanhedrin ili wahukumiwe. Watesaji walitekeleza makusudi yao kwa kumwua Stefano, Yakobo, na Wakristo wengine.

**(630)** Kupitia kwa watumishi wake, Mungu aliwapa Wayahudi nafasi ya mwisho ya kutubu. Alijidhihirisha mwenyewe kwa ushuhuda wake wakati wa kuwakamata hao, katika kuwahoji, na katika vifungo magerezani. Lakini bado mahakimu wao waliwatamkia hukumu ya kifo. Walikuwa watu ambao ulimwengu haukustahili kuwa nao, na kwa kuwaua Wayahudi walimsulibisha upya Mwana wa Mungu. Itakuwa hivyo tena. Mamlaka zitatunga sheria za kubana uhuru wa dini. Watajipa haki ambayo ni ya Mungu peke yake. Watadhani kwamba wanaweza kulazimisha dhamiri, wakati yenyewe inaweza kudhibitiwa na Mungu tu. Hata sasa wako wanatengeneza mwanzo wa hayo; wataendelea na kazi hii mpaka watakapofikia mwisho ambao hawawezi kuuvuka. Mungu ataingilia kati kwa ajili ya watu walio watiifu kwake, watu wazishikao amri.

Katika kila tukio la mateso, wale wanaoyashuhudia hukata shauri kwenda upande wa Kristo au kuwa dhidi ya Kristo. Wale wanaoonyesha huruma kwa watu ambao wamehukumiwa isivyo haki wanaonyesha kuuungana na Kristo. Wengine wanasutwa kwa sababu kanuni za ukweli zinakata katikati katika kitendo chao. Wengi hujikwaa na kuanguka, wakiiasi imani ambayo waliitetea hapo kabla. Wale wanaoasi wakati huu wa kujaribiwa, kwa lengo la kupata usalama wao wenyewe, hutoa ushahidi wa uongo, na kuwasaliti ndugu zao. Kristo ametuonya kuhusu hili, ili ya kwamba tusishangazwe na jambo hilo lisilo la kawaida, yaani, mwenendo wa kikatili wa wale wanaoikataa nuru.

Kristo aliwapa wanafunzi wake dalili ya maangamizi yaliyokuwa yanaujia Yerusalemu, na aliwaambia namna ya kuyaepuka: "Hapo mtakapoona mji wa Yerusalemu umezungukwa na majeshi, ndipo jueni ya kwamba uharibifu wake umekaribia. Ndipo walio katika Uyahudi na wakimbilie milimani, na walio katikati yake wakimbilie nje, na walio katika mashamba wasiuingie. Kwa kuwa siku hizo ndizo za mapatilizo, ili yatimizwe yote yaliyoandikwa." Onyo hili lilitolewa ili litiiwe miaka arobaini baadaye, wakati wa kuharibiwa kwa Yerusalemu. Wakristo walitii amri hiyo, na hakuna Mkristo aliyeangamia wakati wa kuanguka kwa mji huo.

Yesu alisema, "Ombeni, ili kukimbia kwenu kusiwe wakati wa baridi, wala siku ya sabato." Yeye aliyeifanya Sabato hakuikomesha, kwa kuigongomelea msalabani. Sabato haikufutwa wala kukomeshwa wakati wa kifo chake. Ingeendelea kutunzwa kama siku takatifu hata miaka arobaini baadaye. Kwa miaka arobaini wanafunzi wangeendelea kuomba kwamba kukimbia kwao kusiwe siku ya Sabato.

Yesu alitoka katika habari ya kuharibiwa kwa Yerusalemu na kwenda ghafla katika tukio kuu, kipande cha mwisho katika mnyororo wa historia ya dunia hii, - kuja kwa Mwana wa Mungu katika ukuu na utukufu. Katikati ya matukio haya mawili, mtazamo wa Yesu unaziona karne nyingi za giza, karne ambazo **(631)** kanisa lake linakuwa na alama ya damu, machozi na dhiki. Wakati ule wanafunzi wake wasingeweza kustahimili kutazama matukio haya, kwa hiyo Yesu aliyapita kwa kutaja kwa ufupi. "Wakati huo kutakuwapo dhiki kubwa, ambayo haijatokea namna yake tangu mwanzo wa ulimwengu hata sasa, wala haitakuwapo kamwe. Na kama siku hizo zisingalifupizwa, asingeokoka mtu yeyote; lakini kwa ajili ya wateule zitafupizwa siku hizo." Kwa miaka zaidi ya elfu moja mateso yale ambayo ulimwengu haukupata kuona mfano wake yalikuwa yawajilie wafuasi wa Kristo. Mamilioni na mamilioni ya mashahidi wa Kristo waaminifu wangeuawa. Ikiwa mkono wa Mungu usingenyooshwa na kuwahifadhi watu wake, wote wangeangamia. "Lakini kwa ajili ya wateule," alisema, "zitafupizwa siku hizo."

Sasa, kwa lugha isiyoweza kukosewa, Bwana wetu anaongea kuhusu kuja kwake, na anatoa onyo kuhusu hatari zitakazotangulia kuja kwake ulimwenguni. "Wakati huo mtu akiwaambia, Tazama, Kristo yupo hapa, au yuko kule msisadiki. Kwa maana watatokea makristo wa uongo, na manabii wa uongo, nao watatoa ishara kubwa na maajabu; wapate kuwapoteza, kama yamkini, hata walio wateule. Tazama, nimekwisha kuwaonya mbele. Basi wakiwaambia, Yuko jangwani, msitoke; yumo nyumbani, msisadiki. Kwa maana kama vile umeme utokavyo mashariki ukaonekana hata magharibi, hivyo ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu." Ikiwa moja kati ya dalili za maangamizi ya Yerusalemu, Kristo alikuwa amesema kwamba, "Manabii wengi wa uongo watatokea, nao watadanganya wengi." Manabii wa uongo waliibuka, wakiwadanganya watu, na wakiwaongoza

watu wengi sana kuwapeleka jangwani. Watenda maajabu na wachawi, wakidai kuwa na nguvu ya miujiza, waliwaongoza watu walio wafuasi wao kwenda katika sehemu za maficho milimani. Lakini unabii huu ulisemwa pia kwa ajili ya siku za mwisho. Dalili hii imetolewa kama dalili ya kuja kwake mara ya pili. Hata sasa akina kristo wa uongo na manabii wa uongo wanafanya ishara na maajabu ili kuwagilibu wanafunzi wa Yesu. Je, hatusikii sauti ya kilio isemayo, "Tazama, yuko jangwani"? Je, maelfu si wamekwenda jangwani, wakitumaini kumwona Kristo? Na je, hatusikii wito wa sauti isemayo "Tazama, yumo nyumbani" ikitoka miongoni mwa maelfu ya makusanyiko ya watu wanaojigamba kwamba wanawasiliana na roho za waliotengana nao kwa mauti? Haya ndiyo madai yenyewe ya imani ya umizimu. Lakini Kristo anasemaje? "Msisadiki. Kwa maana kama vile umeme utokavyo mashariki ukaonekana hata magharibi, hivyo ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu."

Mwokozi anatoa dalili za kuja kwake, na zaidi ya hilo, anaonyesha muda ambapo dalili za kwanza miongoni mwa hizo zitatokea: "Mara, baada ya dhiki ya siku zile, jua litatiwa giza, na mwezi **(632)** hautatoa mwanga wake, na nyota zitaanguka mbinguni, na nguvu za mbinguni zitatikisika; ndipo itakapoonekana ishara yake Mwana wa Adamu mbinguni; ndipo mataifa yote ya ulimwengu watakapoomboleza, nao watamwona Mwana wa Adamu akija juu ya mawingu ya mbinguni pamoja na nguvu na utukufu mwingi. Naye atawatuma malaika zake pamoja na sauti kuu ya parapanda, nao watawakusanya wateule wake toka pepo nne, toka mwisho huu wa mbingu mpaka mwisho huu."

Mwishoni mwa kipindi cha mateso makubwa ya upapa, Kristo alisema, jua lingetiwa giza, na mwezi usingetoa mwanga wake. Kinachofuata, nyota zingeanguka kutoka mbinguni. Na anasema, "Kwa mtini jifunzeni mfano; tawi lake likiisha kuchipuka na kuchanua majani, mwatambua ya kuwa wakati wa mavuno u karibu; nanyi kadhalika, myaonapo hayo yote, tambueni ya kuwa yu karibu, mlangoni." Mathayo 24:32, 33.

Kristo ametoa dalili za kuja kwake. Alitangaza kwamba tunaweza kujua wakati atakapokuwa amekaribia, hata akiwa mlangoni. Anasema kuhusu wale wazionao dalili hizi, "Kizazi hiki hakitapita, hata hayo yote yatakapotimia." Dalili hizi zimetokea. Sasa tunajua kwa hakika kwamba kuja kwa Bwana kumewadia. Alisema, "Mbingu na nchi zitapita; lakini maneno yangu hayatapita kamwe."

Kristo anakuja na mawingu na utukufu mkuu. Anakuja na kundi kubwa la malaika wenye kung'aa. Atakuja kuwafufua waliokufa, na kuwabadilisha watakatifu walio hai kutoka utukufu hadi utukufu. Atakuja kuwatukuza wale ambao wamempenda, na kuzishika amri zake, na kuwapeleka kwake mwenyewe. Hajawasahau wao wala ahadi yake. Kutakuwa na kuunganisha tena mnyororo wa familia. Tunapowaangalia wapendwa wetu wanaokufa, tunaweza kufikiria kuhusu asubuhi ile wakati parapanda ya Mungu itakapolia, wakati ambapo "wafu watafufuliwa, wasiwe na uharibifu, nasi tutabadilika." 1 Wakorintho 15:52. Kitambo kidogo, tutamwona Mfalme katika uzuri wake. Kitambo kidogo, atafuta machozi yote kutoka machoni petu. Kitambo kidogo, atatusimamisha "mbele ya utukufu wake bila mawaa katika furaha kuu." Yuda 24. Kwa sababu hiyo, wakati alipotoa dalili za kuja kwake alisema, "Basi mambo hayo yaanzapo kutokea, changamkeni, mkaviinue vichwa vyenu, kwa kuwa ukombozi wenu umekaribia."

Lakini Kristo hakuifunua siku na saa ya kuja kwake. Alitamka wazi wazi kwa wanafunzi wake kwamba hata Yeye mwenyewe hakuweza kuifanya siku na saa ya kuja kwake kujulikana. Ikiwa angekuwa na uhuru wa kufunua jambo hili, kwa nini basi ahitaji kuwahimiza kudumu katika kukesha? Wapo wale wanaodai kujua siku na saa halisi ya kuja kwa Bwana wetu. Wanakazana kwa bidii kuweka ramani ya **(633)** wakati ujao. Lakini Bwana amewaonya ili kuondoka katika habari hiyo. Muda hasa wa kuja kwa Mwana wa Adamu mara ya pili ni siri ya Mungu.

Kristo anaendelea, akionyesha hali ya ulimwengu mnamo wakati wa kuja kwake: "Kwa maana kama vile ilivyokuwa siku za Nuhu, ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu. Kwa kuwa kama vile siku zile zilizokuwa kabla ya Gharika watu walivyokuwa wakila, na kunywa, wakioa na kuolewa, hata siku ile aliyoingia Nuhu katika safina, wasitambue, hata Gharika ikaja, ikawachukua wote, ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu." Hapa Kristo haleti habari ya milenia ya ulimwenguni hapa, miaka elfu moja ambayo watu wote wataitumia kujitayarisha kwa ajili ya umilele. Anatuambia kwamba kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa wakati Mwana wa Adamu ajapo.

Wakati wa siku za Nuhu ilikuwaje? "Bwana akaona ya kuwa maovu ya mwanadamu ni makubwa duniani na kwamba kila kusudi analowaza moyoni mwake ni baya tu sikuzote." Mwanzo 6:5. Wakazi wa ulimwengu wa kabla ya Gharika waligeukia mbali na Yehova, wakikataa kuyafanya mapenzi yake matakatifu. Walifuata makusudi yao wenyewe yasiyo matakatifu na mawazo yaliyopotoka. Waliharibiwa kwa sababu ya uovu wao; na leo ulimwengu unafuata njia ile ile. Hii haionyeshi dalili za kufariji kwa uongo za utukufu wa milenia. Wavunjaji wa sheria ya Mungu wanajaza upotofu duniani. Kupingana kwao, mashindano yao ya mbio za farasi, michezo yao ya kamari, tabia yao ya kutapanya mali, vitendo vyao viashiriavyo hali ya kuwa na tamaa ya mwili, hisia zao zisizodhibitika, vinajaza vurugu ulimwenguni.

Katika unabii wa uharibifu wa Yerusalemu Kristo alisema, "Kwa sababu ya kuongezeka maasi, upendo wa wengi utapoa. Lakini mwenye kuvumilia hata mwisho, ndiye atakayeokoka. Tena habari njema ya ufalme itahubiriwa katika ulimwengu wote, kuwa ushuhuda kwa mataifa yote; hapo ndipo ule mwisho utakapokuja." Unabii huu utatimizwa kwa mara nyingine. Ongezeko la uovu wa wakati ule litapata mfano wake katika kizazi hiki. Vivyo hivyo pia kuhusu kuihubiri injili. Kabla ya kuanguka kwa Yerusalemu, Paulo, akiandika kwa kuwezeshwa na Roho Mtakatifu, alisema kwamba injili ilihubiriwa kwa "viumbe vyote chini ya mbingu." Wakolosai 1:23. Vivyo hivyo leo, kabla ya kuja kwa Mwana wa Adamu, injili ya milele itahubiriwa "kwa kila taifa, na kabila, na lugha, na jamaa." Ufunuo 14:6, 14. Mungu "ameweka siku atakayowahukumu walimwengu." Matendo 17:31. Kristo anatwambia ni lini siku hiyo itakapokuja. Hasemi kwamba ulimwengu wote utaongolewa, bali kwamba "habari njema ya ufalme itahubiriwa katika ulimwengu wote, kuwa ushuhuda kwa mataifa yote; hapo ndipo ule mwisho utakapokuja." Kukuhimiza kurudi kwa Bwana wetu kuko ndani ya uwezo wetu kwa sisi kuupatia ulimwengu injili. Haitupasi kutarajia tu kuja kwa siku ya Mungu bali pia kuiharakisha. 2 Petro 3:12. Ikiwa **(634)** kanisa lingekuwa limefanya kazi yake liliyopewa kama Bwana alivyoagiza, ulimwengu wote ungekuwa umeshaonywa kabla ya sasa, na Bwana Yesu angekuwa ameshakuja duniani kwa nguvu na utukufu mkuu.

Baada ya kuonyesha dalili za kuja kwake, Kristo alisema, "Mwonapo mambo hayo yanaanza kutokea, tambueni ya kwamba ufalme wa Mungu u karibu." "Angalieni, kesheni, (ombeni)." Mungu amekuwa akiwapa wanadamu maonyo ya kuja kwa hukumu zake. Wale ambao wana imani katika ujumbe wake wa wakati wao, na ambao walitendea kazi imani yao, katika kuzitii amri zake, waliepuka hukumu zilizowaangukia wale wasiotii na wasioamini. Neno lilimjia Nuhu, likisema, "Ingia wewe na jamaa yako yote katika safina; kwa maana nimekuona wewe u mwenye haki mbele zangu katika kizazi hiki." Nuhu alitii na aliokolewa. Ujumbe ulikuja kwa Lutu, "Ondokeni mtoke katika mahali hapa kwa sababu Bwana atauharibu mji huu." Mwanzo 7:1; 19:14. Lutu alijiweka chini ya uongozi wa wajumbe kutoka mbinguni, naye aliokolewa. Ndivyo ilivyokuwa kwa wanafunzi wa Kristo walipewa onyo la kuharibiwa kwa Yerusalemu. Wale waliokesha kuzitazama ishara za kuja kwa uharibifu, waliondoka kutoka katika mji, wakaepuka maangamizi. Vivyo hivyo sasa tunapewa onyo kuhusu kuja kwa Kristo mara ya pili na kuhusu maangamizi yatakayouangukia ulimwengu. Wale wanaolizingatia onyo hilo wataokoka.

Kwa kuwa hatujui muda hasa wa kuja kwake, tumetakiwa kukesha. "Heri watumwa wale, ambao bwana wao ajapo atawakuta wanakesha." Luka 12:37. Wale wanaokesha wakisubiri kuja kwa Bwana hawaubiri tu bila kazi. Matarajio ya kuja kwa Kristo ni kuwafanya watu wamche Bwana, na waogope hukumu zake zinazosababishwa na uasi. Ni kuwaamsha ili waone dhambi kuu ya kukataa neema yake iliyotolewa. Wale wanaokesha wakimngoja Bwana wanasafisha nafsi zao kwa kuutii ukweli. Wanachanganya bidii ya kazi katika kule kudumu kukesha. Kwa sababu wanajua kwamba Bwana yu mlangoni, hamu yao inaharakishwa kushirikiana na ufahamu wa kimbingu katika kushughulikia wokovu wa roho. Hawa ndio watumwa waaminifu na wenye hekima ambao wanawapatia watu wa nyumba ya Bwana "posho kwa wakati wake." Luka 12:42. Wanautangaza ukweli unaohusika kwa wakati huu. Kama vile ambavyo Henoko, Nuhu, Ibrahimu, au Musa alivyotangaza ukweli uliokuwa kwa ajili ya wakati wake, ndivyo watumwa wa Kristo sasa wanavyotoa maonyo maalum kwa ajili ya kizazi hiki.

Lakini Yesu analeta picha ya kundi jingine: "Lakini, mtumwa yule akisema moyoni mwake, Bwana wangu anakawia kuja, akaanza kuwapiga wajoli wake, wanaume kwa wanawake, akila na kunywa na kulewa; bwana wake mtumwa huyo atakuja siku asiyodhani na saa asiyojua." **(635)** Mtumwa mwovu anasema moyoni mwake, "Bwana wangu anakawia kuja." Hasemi kwamba Kristo hatakuja. Hapuuzi wazo la kuja kwa Kristo mara ya pili. Lakini katika moyo wake na kwa matendo yake anaonyesha kwamba kuja kwa Bwana kumekawia. Anaondosha mawazoni mwa wengine usadikisho kwamba Bwana anakuja haraka. Ushawishi wake unawaweka watu katika imani isiyo sahihi na hali ya kuchelewa katika kutokujali. Wanathibitika katika mambo ya kiulimwengu. Mali za

dunia, mawazo potofu, vinatawala akili yao. Mtumwa mwovu hula na kunywa na walevi, anaungana na ulimwengu katika kutafuta anasa. Anawaua watumwa wenzake, akishtaki na kutuhumu wale ambao ni waaminifu kwa Bwana wao. Anajichanganya na ulimwengu. Matakwa yanaongeza matakwa mengine katika uasi. Ni usimilishaji wa kuogofya. Anawekwa katika mtego pamoja na ulimwengu. "Bwana wake mtumwa huyo atakuja siku asiyodhani na saa asiyojua, atamkata vipande viwili, na kumwekea fungu lake pamoja na wasioamini."

"Walakini usipokesha, nitakuja kama mwivi, wala hutaijua saa nitakayokuja kwako." Ufunuo 3:3. Kurejea kwa Kristo kutashtukiza walimu wa uongo. Wanasema, "Kuna amani na salama." Kama wale makuhani na walimu waliokuwepo kabla ya kuanguka kwa Yerusalemu, wanatafuta namna ya kanisa kufurahia ustawi na utukufu wa kidunia. Wanatafsiri dalili za nyakati kama kivuli cha mambo haya. Lakini neno la uvuvio linasemaje? "Ndipo uharibifu uwajiapo kwa ghafla." 1 Wathesalonike 5:3. Kwa wote wakaao kwenye uso wa nchi, kwa wote wanaoifanya dunia hii kuwa nyumbani kwao, siku ya Mungu itakuja kama mtego. Inakuja kama mwizi aviziaye.

Ulimwengu, ukiwa umejawa na vurugu, ukiwa umejawa na anasa zilizo kinyume na Mungu, ukiwa umelala usingizi, usingizi katika usalama wa bandia, watu wanakuona kuja kwa Bwana kukiwa mbali. Wanayacheka maonyo. Wanajivuna kwa kiburi kwamba, "Vitu vyote vinakaa hali iyo hiyo, tangu mwanzo wa kuumbwa." "Na kesho itakuwa kama leo, sikukuu kupita kiasi." 2 Petro 3:4; Isaya 56:12. Tutaendelea kuzama zaidi katika kupenda raha. Lakini Kristo anasema, "Tazama, naja kama mwivi." Ufunuo 16:15. Katika wakati ule ule ulimwengu unapouliza kwa kubeza kwamba, "Iko wapi ahadi ile ya kuja kwake?" dalili ziko zinatimia. Wakati wanapolia wakisema, "Kuna amani na salama," ndipo uharibifu unapokuja. Wakati mwenye kubeza, mwenye kukataa ukweli, anapokuwa amekuwa na imani potofu; wakati kazi za kila siku katika njia mbalimbali za kupata pesa zinapoendelea kufanywa pasipo kujali; wakati mwanafunzi msomi anapokuwa katika juhudi ya kutafuta kufahamu kila kitu isipokuwa Biblia yake, Kristo anakuja kama mwivi.

**(636)** Kila kitu ulimwenguni kiko katika hali ya kuvutia. Dalili za nyakati zinaashiria hatari. Matukio yajayo yako yanavitupa vivuli vyake kabla. Roho wa Mungu anaondoka duniani, na janga hufuata janga baharini na nchi kavu. Kuna machafuko, matetemeko, moto, mafuriko, mauaji ya kila aina. Nani awezaye kuona mambo yajayo? Usalama uko wapi? Hakuna uhakika katika kitu chochote cha mwanadamu au cha dunia. Watu wanajikusanya kwa haraka chini ya beramu ambazo wamejichagulia. Pasipo kupumzika wanaangalia mienendo ya viongozi wao. Kuna watu ambao wanasubiri na kukesha na kufanya kazi kwa ajili ya kuja kwa Bwana. Watu wa kundi jingine wanaangukia katika kufuata uongozi wa mwasi mkuu wa kwanza. Wachache wanaamini kwa moyo na kwa roho kwamba kuna kuzimu inayopaswa kuepukwa na mbingu inayopaswa kupatikana.

Hatari inatuvizia. Jua huangaza mbinguni, likipita katika mzunguko wake wa kawaida, na mbingu bado zinautangaza utukufu wa Mungu. Watu bado wanakula na kunywa, wakipanda mimea na kujenga nyumba, wakioa, na kuolewa. Wachuuzi bado wananunua na kuuza. Watu wanapambana mmoja dhidi ya mwingine, wakishindania nafasi za juu kuliko. Wapenda anasa bado wanajikusanya katika majumba ya maonyesho, maonyesho ya kushindanisha farasi, na kumbi za michezo ya kamari. Msisimko wa hali ya juu upo, lakini saa ya rehema inafungwa haraka, na kila shauri linakaribia kukatwa milele. Shetani anaona kwamba muda wake ni mfupi. Ameweka mawakala wake wote kazini ili ya kwamba watu wadanganywe, waaminishwe isivyo sahihi, wazingwe na mambo na kushikiliwa humo, mpaka wakati wa rehema uishe, na mlango wa rehema ufungwe milele.

Kwa muda wa karne nyingi maneno ya onyo ya Bwana wetu yanakuja kwetu kutoka pale kwenye Mlima wa Mizeituni, yakisema: "Jiangalieni, mioyo yenu isije ikalemewa na ulafi, na ulevi, na masumbufu ya maisha haya; siku ile ikawajia ghafla." "Basi, kesheni ninyi kila wakati, mkiomba, ili mpate kuokoka katika haya yote yatakayotokea, na kusimama mbele za Mwana wa Adamu."

## Sura ya 70

# "Hao Ndugu Zangu Walio Wadogo"

[Sura hii imejengwa katika Mathayo 25:31-46.]

“Hapo atakapokuja Mwana wa Adamu katika utukufu wake, na malaika watakatifu wote pamoja naye, ndipo atakapoketi katika kiti cha utukufu wake; na mataifa yote watakusanyika mbele zake; naye atawabagua." Hivyo ndivyo ambavyo Kristo alipokuwa kwenye Mlima wa Mizeituni aliwaonyesha wanafunzi wake picha ya tukio la siku kuu ya hukumu. Na alionyesha kwamba uamuzi wa hukumu unageukia kwenye jambo moja. Wakati mataifa yote yatakapokuwa yamekusanywa mbele zake, kutakuwa na makundi mawili tu, na hatima yao ya milele itaamuliwa na kile ambacho wamemfanyia au ambacho wamepuuza kumfanyia alipokuwa katika nafsi za maskini na wenye shida.

Katika siku hii Yesu hawaonyeshi watu kazi kuu aliyowafanyia ya kuutoa uhai wake kwa ajili ya ukombozi wao. Anaonyesha kazi ya uaminifu waliyofanya kwa ajili yake. Atawaambia wale atakaowaweka mkono wake wa kuume kwamba, "Njoni, mliobarikiwa na Baba yangu, urithini ufalme mliowekewa tayari tangu kuumbwa ulimwengu; kwa maana nalikuwa na njaa, mkanipa chakula; nalikuwa na kiu, mkaninywesha; nalikuwa mgeni, mkanikaribisha; nalikuwa uchi, mkanivika nalikuwa mgonjwa, mkaja kunitazama; nalikuwa kifungoni, mkanijia." Lakini hawa watu wanaopongezwa na Kristo hawajui kwamba walikuwa wanamhudumia Yeye. Anajibu maulizo yao ya mshangao kwamba, "Kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hao ndugu zangu walio wadogo, mlinitendea mimi."

Yesu alikuwa amewaambia wanafunzi wake kwamba wangechukiwa na watu wote, wangeteswa na kuudhiwa. Wengi wangefukuzwa kutoka majumbani mwao, na kuletwa katika hali ya umaskini. Wengi wangekuwa katika msongo kwa sababu ya maradhi na **(638)** upweke. Wengi wangetupwa gerezani. Alikuwa amewaahidi wale wote ambao waliwaacha marafiki na nyumba zao kwa ajili yake baraka mara mia katika maisha haya. Sasa aliwahakikishia baraka maalum wote ambao wangewahudumia ndugu zao. Alisema, Yawapasa kuniona mimi ndani ya wote wanaoumia kwa ajili ya jina langu. Vile ambavyo mngenihudumia mimi, ndivyo mnavyotakiwa kuwahudumia hao. Huo ndio ushahidi kwamba ninyi ni wanafunzi wangu.

Wote ambao wamezaliwa katika jamaa ya mbinguni kwa namna ya pekee ni ndugu wa Bwana wetu. Upendo wa Kristo unawafunga pamoja washiriki wa familia yake, na popote upendo huo unapodhihirishwa mahusiano ya kimbingu yanadhihirishwa hapo. "Kila apendaye amezaliwa na Mungu, naye anamjua Mungu." 1 Yohana 4:7.

Wale ambao Kristo anawakubali katika hukumu huenda walijua kidogo sana mambo ya thiolojia, lakini wamekuwa wakitenda kanuni za Kristo. Kwa njia ya ushawishi wa Roho wa mbinguni wamekuwa baraka kwa watu wanaowazunguka. Hata miongoni mwa wapagani wamo watu ambao wamekuwa na roho ya ukarimu; kabla ya maneno ya uzima kuangukia masikioni mwao wameonyesha urafiki wa ukarimu kwa wamishenari, kiasi hata cha kuwahudumia kwa gharama ya kuhatarisha maisha yao. Miongoni mwa wapagani kuna watu wanaomwabudu Mungu bila kujua, wale ambao kamwe hawajawahi kuletewa nuru na wahubiri walio wanadamu, lakini hawataangamia. Ingawa hawaijui sheria ya Mungu iliyoandikwa, wameisikia sauti yake ikinena kupitia vitu vya asili, nao wamefanya mambo yanayotakiwa na sheria. Matendo yao ni ushuhuda kwamba Roho Mtakatifu amegusa mioyo yao, nao wanatambuliwa kama watoto wa Mungu.

Ni mshangao na furaha kiasi gani kwa wale walio wadogo miongoni mwa mataifa, na miongoni mwa wapagani, watakaposikia sauti kutoka midomoni mwa Mwokozi ikisema, "Kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hao ndugu zangu walio wadogo, mlinitendea mimi"! Ni furaha kiasi gani itakayokuwa moyoni mwa Mwenye Upendo usio mwisho wakati wafuasi wake wanapoyatazama kwa mshangao na furaha maneno yake ya kuwakubali!

Lakini upendo wa Kristo hautendi kwa kufungiwa kwa kundi moja tu. Yeye anajitambulisha kuwa pamoja na kila mtoto wa mwanadamu. Ili tupate kuwa watu wa familia ya mbinguni, Yeye alikuja kuwa mmoja wa wanafamilia ya duniani. Yeye ni mwana wa Adamu, na kwa njia hiyo ni kaka wa kila mwana na binti wa Adamu. Wafuasi wake hawapaswi kujihisi kwamba wametenganishwa na ulimwengu uwazungukao unaoangamia. Wao ni sehemu ya mtandao mkubwa wa jamii ya wanadamu; na Mbingu inawaona kama kina kaka wa wadhambi na wa watakatifu.

Upendo wa Yesu unawakumbatia wale walioanguka, walio katika upotovu, na watenda dhambi; na kila tendo la ukarimu linalotendwa ili kuiinua nafsi iliyoanguka, kila tendo la huruma, linakubalika kwamba aliyefanyiwa hilo ni Kristo.

**(639)** Malaika wa mbinguni wanatumwa kuwahudumia wale watakaokuwa warithi wa wokovu. Kwa sasa hatuwajui ni wepi; bado haijadhihirishwa kwamba ni wepi watakaoshinda, na kushiriki urithi wa watakatifu katika nuru; lakini malaika wa mbinguni wanapita katika marefu na mapana yote ya dunia, wakitafuta kuwafariji wanaohuzunika, kuwalinda walio hatarini, kuiongoa kwa Kristo mioyo ya watu. Hakuna mtu hata mmoja anayepuuzwa wala kupitwa. Mungu haheshimu sifa za kibinadamu, Yeye anawatunza watu wote aliowaumba.

Kadiri unavyowafungulia mlango watu wa Kristo walio wahitaji na wenye shida, unawakaribisha malaika wasioonekana. Unakuwa umealika ushirikiano pamoja na viumbe wa mbinguni. Wanakuwa wameleta mazingira matakatifu ya raha na amani. Wao wanatoka na shangwe za sifa midomoni mwao, na sauti kuu ya kujibu tendo hili husikika mbinguni. Kila tendo la huruma huleta muziki mtamu kule. Baba akiwa katika kiti chake cha enzi huwaingiza watenda kazi wasio wabinafsi miongoni mwa watu ambao ni hazina ya thamani kuu.

Wale waliokuwa mkono wake wa kushoto, wale waliompuuza akiwa katika umbo la maskini na wenye shida, hawakujua hatia yao. Shetani amewapofusha; hawakuwa wametafakari kile walichodaiwa kufanya kwa ndugu zao. Walikuwa wamezama katika ubinafsi, na wala hawakujali mahitaji ya wengine.

Mungu amewapa mali wale walio matajiri kusudi wawasaidie na kuwafariji watoto wake wenye shida; lakini mara nyingi hawajali mahitaji ya wengine. Wao wanajiona wenye hadhi ya juu zaidi kwa ndugu zao walio maskini. Hawajiweki katika nafasi ya mtu maskini. Hawajui majaribu na mapambano ya mtu aliye maskini, na huruma hutoweka mioyoni mwao. Matajiri hujifungia katika majumba mazuri na makanisa ya kifahari mbali na maskini; mali ambayo wamepewa na Mungu ili kuwabariki wenye kuhitaji inatumiwa katika kuimarisha kiburi na ubinafsi. Kila siku maskini wanapokonywa ufahamu ambao wangeupata kuhusu huruma na upendo wa Mungu. Maana ametoa kwa wingi ili wapate kufarijiwa kwa kupewa mahitaji ya maisha. Wanalazimishwa kusikia hali ya umaskini ambao unayafanya maisha kuwa finyu, nao mara nyngi hujaribiwa kuwa na kijicho, wivu, na kufanya maamuzi yasiyo sahihi. Mara nyingi wale ambao hawakupitia katika msongo wa kukosa mahitaji wanawatendea maskini kwa jeuri, na huwafanya wajisikie kwamba wanaonekana kama maskini ombaomba.

Lakini Kristo anatazama yote hayo, na anasema, mimi ndiye niliyekuwa na njaa na kiu. Mimi ndiye nilikuwa mgeni. Mimi ndiye niliyekuwa naumwa. Mimi ndiye niliyekuwa kifungoni. Wakati ulipokuwa unakula kwa karamu kwenye meza yako iliyofurika, nilikuwa naumwa njaa katika kijumba cha kimaskini au katika mtaa ulio tupu. Ulipokuwa umestarehe katika nyumba yako ya fahari, Mimi sikuwa na mahali pa kulaza kichwa changu. Ulipokuwa **(640)** umejivisha nguo nzuri za fahari mahali pako, nilikuwa mtupu. Wakati wewe unafanya starehe zako, nilikuwa nasumbuka gerezani.

Je! Mlipowasaidia maskini wenye njaa kwa kipande cha mkate, mlipowapa nguo chakavu ili kuwakinga na baridi, mlikumbuka kama mlikuwa mnampatia Bwana wa utukufu? Katika maisha yenu yote nilikuwa karibu yenu nikiwa katika umbo la wanaoteseka. Hamkupenda kuingia katika kushirikiana nami. Siwajui.

Wengi wanahisi kwamba ungekuwa upendeleo mkubwa kutembelea sehemu za makumbusho ya matukio ya maisha ya Kristo duniani, kukanyaga mahali alipokanyaga, kulitazama ziwe lile ambalo alipenda kufundisha kando yake, na vilima na mabonde ambavyo mara kwa mara vilionwa na macho yake. Lakini kumbe hatuhitaji kwenda Nazareti, Kapernaumu, au Bethania, eti ili kutembea katika nyayo za Yesu. Hebu tuzitafute nyayo zake kando ya kitanda cha mgonjwa, katika vijumba vya kimaskini, katika mitaa yenye msongamano mkubwa katika miji mikubwa, na kila mahali ambapo kuna mioyo ya wanadamu inayohitaji faraja. Katika kufanya vile Yesu alivyofanya akiwa duniani, tutakuwa tunatembea katika nyayo zake.

Watu wote wanaweza kupata jambo la kutenda. Yesu alisema kwamba, "Maskini mnao siku zote pamoja nanyi," (Yohana 12:8), kwa hiyo hakuna mtu anayehitaji kuona kwamba hana mahali pa kutenda kazi. Mamilioni ya roho za watu walio karibu ya kupotea, wakiwa wamefungiwa katika minyororo ya kutojua na ya dhambi, hawajasikia upendo wa Kristo kwao kwa kiasi kinachostahili. Je! Ikiwa hali yao na yetu zingebadilishanwa, tungetamani watufanyie nini sisi? Tuna wajibu mkubwa wa kuwatendea mambo haya yote, kwa kadiri ya namna yalivyo ndani ya uwezo wetu. Kanuni ya maisha ya Kikristo, ambayo lazima iwe ndicho kigezo ambacho kitamwezesha

kila mmoja wetu ama kusimama au kuanguka wakati wa hukumu, ni, "Yoyote myatakayo mtendewe na watu, nanyi watendeeni vivyo hivyo." Mathayo 7:12.

Mwokozi ametoa maisha yake ya thamani ili kuanzisha kanisa ambalo lina uwezo wa kutunza roho za wenye huzuni na waojaribiwa. Kundi la waamini lililo mahali fulani linaweza kuwa maskini, lisilo na kisomo, na lisilo maarufu; lakini katika Kristo wanaweza kufanya kazi majumbani, kwa majirani, kanisani, na hata "nchi zilizo mbele kupita nchi zetu," ambayo matokeo yake yatafika mbali kama ulivyo umilele.

Kwa sababu ya kupuuza kazi hii wanafunzi wapya wengi hawakui kiroho zaidi tu ya kuongeza alfabeti za uzoefu wa Kikristo. Walitakiwa kuifanya hai ile nuru iliyoangaza mioyoni mwao wakati Kristo alipowaambia, "Mmesamehewa dhambi zenu" kwa njia ya kuwasaidia wale walio katika uhitaji. Nguvu kubwa ya wakati wote ambayo mara nyingi inakuwa chanzo cha hatari kwa wachanga hao ingepaswa kuelekezwa katika mifereji ambayo ndani yake **(641)** vinatirirka vijito vya baraka. Katika kazi hii ya kufanya wema kwa wengine, umimi ungesahulika kabisa.

Wale wanaowahudumia wengine watahudumiwa na Mchungaji Mkuu. Wao wenyewe watakunywa katika yale maji yaliyo hai, nao watatosheka. Hawatatafuta kufanya mambo ya maburudisho ya kusisimua, kutafuta badiliko katika maisha yao. Mada kuu ya hamu yao itakuwa ni, Ni jinsi gani tunaweza kuponya roho zinazokaribia kupotea! Mashirikiano ya kijamii yatakuwa na manufaa kwao. Upendo wa Mkombozi utaivuta mioyo na kuileta katika umoja.

Tunapotambua kwamba sisi ni watenda kazi pamoja na Mungu, ahadi zake hazitatamkwa kwa dharau. Zitachoma mioyoni mwetu, na zitaangaza katika midomo yetu. Katika tukio la Mungu kumpa Musa ahadi, wakati alipoitwa kuhudumia watu wasiojua, wasio na nidhamu, na waasi, alisema, "Uso wangu utakwenda pamoja nawe, nami nitakupa raha." Na alisema, "Bila shaka mimi nitakuwa pamoja nawe." Kutoka 33:14; 3:12. Ahadi hii inatolewa kwa wote wanaofanya mahali pa Kristo kazi kwa ajili ya watu wake wanaoteseka na kuwa na shida.

Upendo kwa mwanadamu ni udhihirisho wa duniani wa upendo wa Mungu. Mfalme wa utukufu alifanyika kuwa mmoja wetu ili kupandikiza upendo huu, kutufanya kuwa watoto wa familia moja. Na pindi maneno aliyosema wakati wa kuondoka kwake yanapotimizwa, kwamba, "Mpendane ninyi kwa ninyi, kama nilivyowapenda ninyi" (Yohana 15:12); pindi tunapowapenda walimwengu kama alivyowapenda, kazi yake inatimizwa kwa ajili yetu. Tunastahilishwa kwa ajili ya kuishi mbinguni; maana tunayo mbingu ndani ya mioyo yetu wenyewe.

Lakini "uwaokoe wanaochukuliwa ili wauawe; Nao walio tayari kuchinjwa uwaopoe. Ukisema, Sisi hatukujua hayo; Je! Yeye aipimaye mioyo siye afahamuye? Naye ailindaye nafsi yako siye ajuaye? Je! Hatamlipa kila mtu sawasawa na kazi yake?" Mithali 24:11, 12. Katika siku kuu ya hukumu, wale ambao hawakufanya kazi kwa ajili ya Kristo, ambao wamesukumwa kuelekea katika kujifikiria wao wenyewe, wakijihudumia wenyewe, watawekwa na Hakimu wa dunia yote katika kundi la wale waliotenda maovu. Wanapata hukumu ile ile moja.

Kila mtu amekabidhiwa dhamana. Kutoka kwa kila mmoja Mchungaji Mkuu atadai hivi, "Liko wapi kundi lako ulilopewa, kundi lile zuri?" Na "Utasema nini wewe, atakapowaweka rafiki zako kuwa kichwa juu yako?" Yeremia 13:20, 21.

## Sura ya 71

# Mtumishi wa Watumishi

[Sura hii imejengwa katika Luka 22:7-18, 24; Yohana 13:1-17.]

Katika chumba cha juu cha nyumba ya makazi kule Yerusalemu, Kristo alikuwa amekaa mezani pamoja na wanafunzi wake. Walikuwa wamekusanyika ili kusherehekea sikukuu ya Pasaka. Mwokozi alipanga kwamba sikukuu hii isherehekewe na Yeye pamoja na wale kumi na wawili tu. Alijua kwamba saa yake ilikuwa imekaribia; Yeye mwenyewe alikuwa ndiye mwana-kondoo wa pasaka wa kweli, na siku Pasaka ilipoliwa ndiyo siku ambayo angesulibiwa. Alikuwa anakaribia kukinywea kikombe cha ghadhabu, muda si mrefu alikuwa apokee ubatizo wa mwisho wa mateso. Lakini saa chache za ukimya zilikuwa bado zipo kwake, nazo zingetumika kuwanufaisha wanafunzi wake wapendwa.

Maisha yote ya Yesu yalikuwa maisha ya huduma isiyo na ubinafsi. Kauli kwamba Mwana wa Adamu hakuja "kutumikiwa, bali kutumika," (Mathayo 20:28), ilikuwa amekuwa somo katika kila tendo alilotenda. Katika chakula hiki cha Pasaka ya mwisho, Yesu alirudia somo lake kwa kutumia kielelezo lililodumu mawazoni na mioyoni mwao milele kuhusu tendo hili.

Mazungumzo kati ya Yesu na wanafunzi wake mara nyingi yalifanyika wakati wa furaha yenye utulivu, ambayo ilithaminiwa sana na wao wote. Chakula cha Pasaka kilikuwa ni tukio la kupendeza kwa namna ya pekee; lakini katika tukio hili Yesu alifadhaika. Moyo wale ulikuwa na mzigo, na kivuli kilikuwa kimefunika sura yake. **(643)** Alipokutana na wanafunzi katika chumba cha ghorofani, walidhani kwamba jambo fulani lilikuwa mzigo katika mawazo yake, na ingawa hawakujua sababu yake, walipatwa na hisia ya huruma kwa ajili ya huzuni yake.

Walipokuwa wamekusanyika mezani, alisema kwa sauti ya huzuni yenye mguso, "Nimetamani sana kuila pasaka hii pamoja nanyi kabla ya kuteswa kwangu; kwa maana nawaambia ya kwamba siili tena hata itakapotimizwa katika ufalme wa Mungu. Akapokea kikombe, akashukuru, akasema, Twaeni hiki, mgawanye ninyi kwa ninyi; Maana nawaambia ya kwamba tangu sasa sinywi mazao ya mzabibu hata ufalme wa Mungu utakapokuja."

Kristo alijua kwamba muda wa Yeye kuondoka ulimwenguni ulikuwa umefika, apate kwenda kwa Baba yake. Na akiwa amewapenda walio wake waliokuwa ulimwenguni, aliwapenda upeo. Sasa alikuwa katika kivuli cha msalaba, na uchungu ulikuwa unatesa moyo wake. Alijua kwamba ataachwa katika hali ya upweke katika saa yake ya kusalitiwa. Alijua kwamba angeuawa kwa kifo kama cha mhalifu mkubwa kuliko wote. Alijua jinsi wale aliokuja kuwaokoa wasivyo na shukrani na walivyo wakatili. Alijua ukubwa wa kafara aliyopaswa kufanya, na akajua kwamba ni kwa wangapi ambao kwao kafara hiyo ingekuwa bure. Akiyajua yote hayo yaliyokuwa mbele yake, kwa asili angetiwa hofu na mawazo hayo ya kudhalilishwa na kuteswa. Lakini aliwatazama wale kumi na wawili, waliokuwa wamekuwa pamoja naye kama walio wake, na ambao, baada ya aibu na huzuni na maovu, wangeachwa ili wapambane ulimwenguni. Mawazo yake kuhusu atakavyoteseka yaliunganishwa daima na wanafunzi wake. Hakujifikiria Yeye mwenyewe. Kuwajali wao lilikuwa ndilo jambo la juu mawazoni mwake.

Katika jioni hii ya mwisho ya kuwa na wanafunzi wake, Yesu alikuwa na mambo mengi ya kuwaambia. Ikiwa wangekuwa wamejiandaa kupokea kile alichotaka kuwajulisha, wangeepuka huzuni za kuvunja moyo, kutokana na mfadhaiko na kutokuamini. Lakini Yesu aliona kwamba wasingestahimili kubeba yote ambayo angesema. Alipowaangalia nyusoni mwao, maneno ya maonyo na faraja yalizuiwa midomoni mwake. Vipindi fulani vilipita kukiwa na ukimya. Yesu alionekana kama anayesubiri. Wanafunzi wao walikuwa wametulia. Huruma na huzuni zilizoamshwa na Kristo zilionekama kama zimetoweka. Maneno yake ya huzuni, yanayoonyesha mateso yake, yaliwapatia mguso kidogo sana. Hali ya jinsi walivyotazamana wao kwa wao iliashiria wivu na mashindano.

Kulikuwa na "mashindano kati yao, kwamba ni nani anayehesabiwa kuwa mkubwa." Kushindana huku, kulikofanyika mbele yake, kulimhuzunisha na kumwumiza. Wale wanafunzi waling'ang'ania wazo walilopendelea kwamba Kristo angetawazwa madarakani, na kukalia nafasi yake katika kiti cha enzi cha Daudi. Na kimoyo-moyo kila mmoja alitamani kupata nafasi ya juu katika **(644)** ufalme ule. Walikuwa wamejipangia nafasi wao wenyewe na kila mmoja wao, na, badala ya kuwachukulia ndugu kuwa ndio wanaostahili zaidi, walikuwa wamejifanya kuwa wa kwanza. Ombi la Yakobo na Yohana kwamba wakae upande wa kulia na wa

kushoto wa kiti cha enzi cha Kristo lilikuwa limeamsha hasira za wale wengine. Habari ya kwamba wale ndugu wawili wangediriki kuomba nafasi ya juu iliwavuruga wale wengine kumi ambao waliona tishio la kutengwa. Walihisi kwamba wamehukumiwa isivyo sahihi, kwamba juhudi na talanta zao hazikuthaminiwa. Yuda ndiye aliyekuwa mkali zaidi kwa Yakobo na Yohana.

Wakati wanafunzi walipoingia katika chumba cha chakula, mioyo yao ilikuwa imejawa na hisia mbaya za namna hiyo. Yuda aliendа moja kwa moja karibu na Kristo upande wa kushoto; Yohana alikuwa upande wa kulia. Ikiwa kungekuwa na cheo cha juu, Yuda alikuwa ameazimia kukipata, na cheo kile kingekuwa kinachofuata baada ya kile cha Kristo. Na Yuda alikuwa msaliti.

Sababu nyingine ya kupingana ilikuwa imeibuka. Wakati wa sikukuu ilikuwa desturi kwa mtumishi kuosha miguu ya wageni, na katika tukio hili maandalizi yalikuwa yamefanywa kwa ajili ya huduma hiyo. Chombo cha maji, beseni, na taulo vilikuwepo pale, tayari kwa uoshaji wa miguu; lakini hakuna mtumishi ambaye alikuwa pale, na ilikuwa ni wajibu wa wanafunzi kufanya kazi ile. Lakini kila mmoja wa wanafunzi, akisukumwa na kiburi, alijitahidi asifanye kazi ya mtumishi. Wote walionyesha hali ya kutohusika, wakionekana kutojua kwamba kulikuwa na kitu cha kufanywa na wao. Kwa ukimya wao ule walikataa kujishusha.

Je! Kristo angeziletaje nafsi hizi maskini mahali ambapo Shetani asingepata ushindi wa uhakika dhidi yao? Angewezaje kuwaonyesha kwamba kudai tu kuwa ni wanafunzi hakukuwafanya kuwa wanafunzi, au kuwahakikishia mahali katika ufalme wake? Ni jinsi gani ambavyo angewaonyesha kwamba huduma ya upendo, kujishusha kwa kweli, ndivyo vinavyoleta ukuu halisi? Angewashaje moto wa upendo mioyoni mwao, na kuwawezesha kuelewa kile alichotaka kuwaambia?

Wale wanafunzi hawakufanya lolote la kuhudumiana. Yesu alisubiri kwa muda kidogo ili aone kwamba wangefanya nini. Halafu Yeye, aliye Mwalimu wa kimbingu, aliinuka kutoka mezani. Akiweka kando vazi lake la juu ambalo lingekwamisha kujongea kwake, alichukua taulo, akajifunga. Wanafunzi waliangalia kwa hamu ya mshangao, na wakiwa kimya walisubiri kuona jambo ambalo lingefuata. "Kisha akatia maji katika bakuli, akaanza kuwatawadha wanafunzi miguu, na kuifuta kwa kile kitambaa alichojifunga." Kitendo hiki kilifungua macho ya wanafunzi. Aibu chungu na hali ya kudhalilika vilijaza mioyo yao. Walilielewa kemeo ambalo halikusemwa kwa mdomo, na walijiona kwa ujumla katika nuru mpya.

Hivyo ndivyo ambavyo Kristo alionyesha upendo wake kwa wanafunzi wake. Roho yao ya ubinafsi ilimjaza huzuni, lakini hakuingia katika kupambana nao **(645)** kuhusu ugumu wao. Badala yake aliwapa mfano ambao wasingeusahau kamwe. Upendo wake kwao usingeyumbishwa au kuzimwa kwa urahisi. Alijua kwamba Baba amempa vitu vyote mikononi mwake, na ya kwamba alikuja kutoka kwa Mungu, na alienda kwa Mungu. Alikuwa na ufahamu kamili wa uungu wake; lakini alikuwa ameweka kando taji yake ya kifalme na joho la kifalme, naye alikuwa amechukua namna ya mtumishi. Moja kati ya matendo yake ya mwisho ya maisha yake duniani ilikuwa ni kujifunga kama mtumishi, na kufanya kazi mahali pa mtumishi.

Kabla ya Pasaka Yuda alikuwa amekutana na makuhani na waandishi kwa mara ya pili, na alikuwa amefunga nao mkataba kumfikisha Yesu mikononi mwao. Lakini baada ya pale alijichanganya na wanafunzi wengine kama vile hana hatia ya baya lolote, na akaonyesha hamu katika kazi ya kuandaa sikukuu ile. Wanafunzi hawakujua chochote kuhusu kusudi la Yuda. Yesu peke yake ndiye aliweza kusoma siri yake. Lakini hakupenda kumweka wazi. Yesu alikuwa na njaa ya roho yake. Alihisi mzigo mkubwa kwa ajili yake kama ule wa Yerusalemu alipoulilia mji huo uliokuwa unaelekea kuangamia. Moyo wake ulikuwa unalia ukisema, Nawezaje kukuacha? Nguvu zizuiazo za upendo ule zilihisiwa na Yuda. Wakati mikono ya Mwokozi ilipokuwa inaosha miguu yake ile yenye mavumbi, na kuifuta kwa taulo, moyo wa Yuda ulisisimka tena na tena kwa hisia ambazo zingemfanya wakati ule na pale pale aungame dhambi. Lakini hakujishusha. Aliufanya moyo wake kuwa mgumu dhidi ya toba; na misukumo ya nyuma, ambayo kwa muda ilikuwa imewekwa kando, ilimtawala tena. Sasa Yuda alichukizwa na kitendo cha Kristo kuosha miguu ya wanafunzi wake. Alifikiri hivi, Ikiwa Yesu anajishusha kiasi hiki, hawezi kuwa mfalme wa Israeli. Matumaini yote ya heshima za kidunia na ufalme wa kidunia yaliharibika. Yuda aliridhika kwamba hakukuwa na kitu cha manufaa ambacho kingepatikana kwa kumfuata Kristo. Baada ya kumwona akijidhili, kama alivyodhani, alipata uhakika wa kusudi lake la kumwacha, alikiri kwamba alidanganyika. Alikuwa amepagawa na pepo, na aliazimia kukamilisha kazi aliyokuwa amekubali kuifanya ya kumsaliti Bwana wake.

Katika kule kuchagua nafasi yake pale mezani, Yuda alikuwa amejaribu kujiweka wa kwanza, na Kristo aliyekuwa kama mtumishi alimhudumia yeye kwanza. Yohana, ambaye alikuwa amekasirikiwa sana na Yuda, aliachwa na kuwa wa mwisho. Lakini Yohana hakulichukulia jambo hilo kama kemeo au jambo la kuzingatia. Kadiri wanafunzi walivyotazama tendo hilo la Kristo, waliguswa sana. Ilipokuja zamu ya Petro, alihamaki kwa mshangao, akisema, "Bwana! Wewe wanitawadha miguu mimi?" Kujishusha kwa Kristo kuliuvunja moyo wake. Alijawa na aibu kwa kule kufikiri kwamba hakuna mmoja wa wanafunzi aliyefanya huduma hii. Kristo alisema, "Nifanyalo wewe hujui sasa; lakini utalifahamu baadaye." Petro hakuweza kuvumilia kumwona Bwana wake, aliyemwamini kuwa ni Mwana wa Mungu, akifanya mahali pa mtumishi. Moyo wake wote uliinuka dhidi ya hali hii ya kujishusha. **(646)** Hakugundua kwamba Kristo alikuja ulimwenguni kwa ajili ya hilo. Kwa msisitizo mkubwa alisema, "Wewe hutanitawadha miguu kamwe."

Kwa upole Kristo alimwambia Petro, "Kama nisipokutawadha, huna shirika nami." Huduma ambayo ilikataliwa na Petro ilikuwa ni ishara ya utakaso wa hali ya juu. Kristo alikuwa amekuja kuuosha moyo dhidi ya doa la dhambi. Kwa kukataa kumruhusu Kristo kuosha miguu yake, Petro alikuwa anakataa utakaso huo wa juu uliokuwa ndani ya kujishusha. Alikuwa anamkataa Bwana wake. Kumruhusu Bwana kufanya kazi ya utakaso wetu si udhalilishaji. Unyenyekevu wa kweli mno ni kupokea kwa moyo wa shukrani jambo lolote linalofanyika kwa ajili yetu, na kufanya huduma ya Kristo kwa dhati.

Kwa maneno yale kwamba, "Kama nisipokutawadha, huna shirika name," Petro alisalimisha kiburi chake na matakwa binafsi. Hakuweza kuvumilia habari ya kutengwa na Kristo; kwake hicho kingekuwa kifo. Akasema, "Si miguu yangu tu, hata na mikono yangu na kichwa changu pia. Yesu akamwambia, Yeye aliyekwisha kuoga hana haja ila ya kutawadha miguu, bali yu safi mwili wote; nanyi mmekuwa safi, lakini si nyote."

Maana ya maneno haya ni ya zaidi ya usafi wa mwili. Bado Kristo anaongea kuhusu usafi ule wa juu kwa kutumia kielelezo cha chini. Yeye aliyetoka kuoga alikuwa safi, lakini miguu yenye malapa ilipata mavumbi muda si mrefu, na kwa hiyo ilihitaji kuoshwa tena. Hivyo Petro na wenzake walikuwa wameoshwa katika chemchemi kuu iliyofunguliwa kwa ajili ya dhambi na unajisi. Kristo aliwakiri kwamba ni wake. Lakini majaribu yalikuwa yamewaingiza katika uovu, kwa hiyo bado walihitaji neema yake itakasayo. Yesu alipojifunga taulo ili kuosha mavumbi ya miguu yao, kwa tendo lile alipanga kuosha kutengwa kwao, wivu wao, na kiburi chao kutoka mioyoni mwao. Hili lilikuwa na matokeo makubwa ya mbali zaidi kuliko kuosha mavumbi ya miguu tu. Kwa roho waliyokuwa nayo wakati ule, hakuna hata mmoja wao aliyekuwa amejiandaa kushiriki na Yesu. Wasipoletwa katika hali ya kujishusha na kuwa na upendo, hawakuwa wamejiandaa kushiriki katika chakula cha pasaka, au kushiriki katika tendo la kumbukumbu ambayo Kristo alitaka kuanzisha. Lazima mioyo isafishwe. Kiburi na kujitafutia manufaa binafsi hujenga mashindano na chuki, lakini Yesu aliosha yote haya katika kule kuwaosha miguu. Badiliko la hisia lililetwa. Alipowatazama, Yesu alisema, "Mmekuwa safi." Sasa kulikuwa na kuungana kwa mioyo, upendo kwa mtu na mwenzake. Walikuwa wamekuwa wanyenyekevu na wenye kufundishika. Ukimwacha Yuda, kila mmoja alikuwa tayari kumpa mwingine haki ya kukalia nafasi ya juu. Sasa wakiwa na mioyo iliyonyenyekezwa na ya shukrani walikuwa tayari kupokea maneno ya Kristo.

Kama Petro na wenzake, sisi pia tumeoshwa katika damu ya Kristo, lakini mara kwa mara usafi wa moyo unatiwa mavumbi kwa njia ya kukutana na uovu. Lazima tuje kwa Kristo kwa ajili ya neema yake itakasayo. Petro alisita kuleta miguu yake iliyochafuliwa na mavumbi ili igusane na mikono ya Bwana na Mwalimu wake; **(649)** lakini ni mara ngapi tunaleta mioyo yetu ya dhambi na iliyochafuka ili igusane na moyo wa Kristo! Kucheza kwetu na maovu, kutojali kwetu na kiburi chetu vinamhuzunisha kiasi gani! Lakini lazima tulete kwake madhaifu yetu yote na uchafu wetu wote. Yeye peke yake ndiye anayeweza kutuosha tukawa safi. Tunakuwa hatujajiandaa kushiriki pamoja naye mpaka tusafishwe na uweza wake.

Yesu aliwaambia wanafunzi wale kwamba, "Mmekuwa safi, lakini si nyote." Alikuwa ameosha miguu ya Yuda, lakini moyo wake haukuwa umejitoa kwake. Haukuwa umesafishwa. Yuda hakuwa amejisalimisha kwa Kristo.

Baada ya Kristo kuosha miguu ya wanafunzi, na kuvaa mavazi yake na kukaa tena, aliwaambia, "Je! Mmeelewa na hayo niliyowatendea? Ninyi mwaniita, Mwalimu, na, Bwana; nanyi mwanena vema, maana ndivyo nilivyo. Basi ikiwa mimi, niliye Bwana na Mwalimu, nimewatawadha miguu, imewapasa vivyo kutawadhana miguu ninyi kwa ninyi. Kwa kuwa nimewapa kielelezo; ili kama mimi nilivyowatendea, nanyi mtende vivyo. Amin, amin, nawaambia ninyi, Mtumwa si mkuu kuliko bwana wake; wala mtume si mkuu kuliko yeye aliyempeleka."

Kristo alitaka wanafunzi wake waelewe kwamba ingawa alikuwa amewaosha miguu, tendo hilo halikumwondolea heshima yake. "Ninyi mwaniita, Mwalimu, na, Bwana; nanyi mwanena vema, maana ndivyo nilivyo." Na akiwa mkuu wa zama zote hivyo, aliweka neema na umuhimu katika huduma hiyo. Hakuna aliyekuwa ameinuliwa juu kama Kristo, lakini alishuka mpaka katika wajibu wa hali ya chini mno. Kristo mwenyewe aliweka kielelezo hicho cha kujishusha ili kwamba watu wake wasipotoshwe na ubinafsi ukaao katika moyo wa asili, ambao unajiimarisha katika kujihudumia wenyewe. Hakuacha somo hili kuu katika mamlaka ya mwanadamu. Aliliona kama lenye matokeo makubwa, kiasi kwamba Yeye mwenyewe, aliye sawa na Mungu, alifanya kazi ya mtumishi kwa wanafunzi wake. Walipokuwa wanashindana kwa ajili ya cheo cha juu, Yeye ambaye kwake kila goti litapigwa, Yeye ambaye malaika wanaona wameheshimiwa kwa kumhudumia, aliinama ili kuosha miguu ya wale waliomwita Bwana. Aliosha miguu ya mwenye kumsaliti pia.

Katika maisha yake na masomo yake, Kristo ametoa mfano mkamilifu wa huduma isiyo na ubinafsi ambayo chanzo chake kiko ndani ya Mungu. Mungu haishi kwa ajili yake mwenyewe. Kwa kuumba ulimwengu, na kwa kuvishikilia vitu vyote, anatumika kwa ajili ya wengine muda wote. "Huwaangazia jua lake waovu na wema, huwanyeshea mvua wenye haki na wasio haki." Mathayo 5:45. Mungu amekabidhi huduma hii itakiwayo kwa Mwana wake. Yesu alipewa kusimama kwenye kichwa cha wanadamu, ili kwamba kwa kielelezo chake afundishe maana ya huduma. Maisha yake yote yalikuwa chini ya sheria ya kutumika. Aliwatumikia wote, aliwahudumia wote. Kwa njia hiyo aliiishi sheria ya Mungu, na kwa mfano wake alionyesha jinsi tunavyopaswa kuitii.

**(650)** Tena na tena Yesu alikuwa amejaribu kuweka kanuni hii ndani ya wanafunzi wake. Wakati Yakobo na Yohana walipoomba nafasi ya upendeleo, alikuwa amesema, "Mtu yeyote anayetaka kuwa mkubwa kwenu, na awe mtumishi wenu." Mathayo 20:26. Katika ufalme wangu kanuni ya upendeleo na ukuu haina nafasi. Ukuu pekee uliopo ni ukubwa wa kujishusha. Sifa pekee inapatikana katika kujitoa kwa ajili ya kuwatumikia wengine.

Sasa, akisha kuwaosha wanafunzi miguu, alisema, "Kwa kuwa nimewapa kielelezo; ili kama mimi nilivyowatendea, nanyi mtende vivyo." Katika maneno haya Kristo hakuwa anaagiza kuhusu tendo la ukarimu tu. Kulikuwa na maana zaidi kuliko kuosha miguu ya wageni ili kuondoa mavumbi ya safari. Hapa Yesu alikuwa anaweka huduma ya kidini. Kwa tendo lile la Bwana wetu maadhimisho haya ya kujishusha yalifanywa kuwa kaida iliyotengwa rasmi. Ilipaswa iadhimishwe na wanafunzi, ili ya kwamba wadumu kukumbuka masomo yake ya unyenyekevu na utumishi. Kaida hii ni maandalizi ya Kristo yaliyoamuliwa kwa ajili ya huduma ya sakramenti. Wakati kiburi, kutofautiana, kugombania ukubwa vinaendelezwa, moyo hauwezi kuingia katika ushirika na Kristo. Hatuko tayari kupokea ushirika wa mwili wake na damu yake. Kwa hiyo Yesu aliweka kumbukumbu ya mateso yake ili kuanza kuadhimishwa.

Pindi wanapokuja katika maadhimisho haya, watoto wa Mungu wanapaswa waweze kukumbuka maneno ya Bwana wa uzima na utukufu kwamba, "Je! Mmeelewa na hayo niliyowatendea? Ninyi mwaniita, Mwalimu, na, Bwana; nanyi mwanena vema, maana ndivyo nilivyo. Basi ikiwa mimi, niliye Bwana na Mwalimu, nimewatawadha miguu, imewapasa vivyo kutawadhana miguu ninyi kwa ninyi. Kwa kuwa nimewapa kielelezo; ili kama mimi nilivyowatendea, nanyi mtende vivyo. Amin, amin, nawaambia ninyi, Mtumwa si mkuu kuliko bwana wake; wala mtume si mkuu kuliko yeye aliyempeleka. Mkiyajua hayo, heri ninyi mkiyatenda." Ndani ya mwanadamu kuna mwelekeo wa kujiinua juu zaidi kuliko mwenzake, kufanya kazi kwa ajili ya mahitaji binafsi, kutafuta nafasi ya juu zaidi; na mara nyingi hali hii husababisha fikira ovu na uchungu wa moyo. Kaida hii inayotangulia Chakula cha Bwana inapaswa kusafisha kutokuelewana kote huku, kumleta mtu nje ya ubinafsi wake, kumshusha chini kutoka kwenye mironjo aliyoitumia kujiinua, hadi katika unyenyekevu wa moyo ambao utamfanya amhudumie ndugu yake.

Yeye aliye Mtazamaji mtakatifu wa mbinguni yupo katika kipindi hiki ili kukifanya kiwe cha kupeleleza moyo, cha kusadikisha dhambi, na cha tumaini la baraka la kusamehewa dhambi. Kristo akiwa katika ukamilifu wa neema yake yupo pale ili kubadili mkondo wa mawazo ambayo yamekuwa yakipita katika mifereji ya ubinafsi. Roho Mtakatifu huharakisha fahamu za wale wanaofuata kielelezo cha Bwana wao. Kadiri kujishusha kwa Mwokozi kwa ajili yetu kunavyokumbukwa, mawazo **(651)** huunganishwa na mawazo; mnyororo wa kumbukumbu unaletwa, kumbukumbu za wema mkuu wa Mungu na za wema na upendo wa marafiki wa duniani. Baraka zilizosahaulika, huruma zilizotumiwa vibaya, ukarimu uliopuuzwa, vinaletwa katika kumbukumbu. Mizizi ya uchungu ambayo imeuzinga mmea wa thamani wa upendo inawekwa wazi. Mapungufu

ya tabia, kupuuzia wajibu, kukosa shukrani kwa Mungu, kutopenda wenzetu, vinaletwa katika kumbukumbu. Dhambi inaonekana katika nuru ya namna Mungu anavyoiona. Mawazo yetu si mawazo ya kuridhika, bali ya upinzani mkali na ya kujishusha. Akili inahamasika kuvunjilia mbali kila kizuizi ambacho kimesababisha utengo. Mawazo maovu na maneno maovu yanaachwa. Dhambi zinaungamwa, zinasamehewa. Neema ya Kristo itiishayo huja moyoni, na upendo wa Kristo huivuta mioyo pamoja katika umoja uliobarikiwa.

Kadiri somo la huduma hii ya maandalizi linapojifunzwa hivyo, hamu ya kiwango cha juu cha maisha ya kiroho huwashwa. Naye Shahidi wa kimbingu ataiitikia hamu hii. Moyo utainuliwa. Tunaweza kushiriki Ushirika tukiwa na ufahamu wa kusamehewa kwa dhambi. Mwangaza wa jua la haki ya Kristo utajaza vyumba vya akili zetu na vya hekalu la moyo. Tunamwona "Mwana-kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu." Yohana 1:29.

Kwa wale wanaopokea roho ya huduma hii, haiwezi kuwa kama maadhimisho tu. Somo lake la wakati wote litakuwa ni, "Tumikianeni kwa upendo." Wagalatia 5:13. Katika kule kuosha miguu ya wanafunzi wake, Kristo alitoa ushahidi kwamba angefanya huduma yoyote, hata iwe ya kujishusha kiasi gani, ambayo ingewafanya kuwa warithi pamoja naye wa utajiri wa milele wa hazina ya mbinguni. Katika kutenda desturi hiyo ya kidini, wanafunzi wake wanaahidi kwa namna hiyo hiyo kuwahudumia wengine. Kila mahali kaida hii inapoadhimishwa kwa usahihi, watoto wa Mungu wanaletwa katika uhusiano mtakatifu, kusaidiana na kubarikiana. Wanaweka agano kwamba maisha yatatumiwa kwa huduma isiyo ya ubinafsi. Na hii, si tu kwa mtu na mwenzake. Uwanja wao wa kazi ni mpana kama ulivyokuwa wa Bwana wao. Ulimwengu umejaa watu wanaohitaji huduma yetu. Maskini, wasio na msaada, wasiojua kitu, wako kila upande. Wale ambao wameshiriki na Kristo katika chumba cha juu wataondoka kwenda kutoa huduma kama Yeye alivyofanya.

Yesu, aliyetumikiwa kuliko wote, alikuja kuwa mtumishi wa wote. Na kwa sababu alihudumia wote, atatumikiwa na kuheshimiwa na wote tena. Na wale wanaotaka kushiriki sifa zake za kiungu, na kushiriki naye raha ya kuziona roho zilizokombolewa, lazima wafuate mfano wake wa utumishi usio wa ubinafsi.

Yote haya yalieleweka katika maneno ya Yesu kwamba, "Nimewapa kielelezo; ili kama mimi nilivyowatendea, nanyi mtende vivyo." Hii ndiyo ilikuwa nia ya huduma hii aliyoanzisha. Na akasema, "Mkiyajua hayo," mkijua kusudi la masomo haya, "heri ninyi mkiyatenda."

## Sura ya 72

# "Kwa Ukumbusho Wangu"

[Sura hii imejengwa katika Mathayo 26:20-29; Marko 14:17-25; Luka 22:14-23; Yohana 13:18-30.]

"Bwana Yesu usiku ule aliotolewa alitwaa mkate, naye akiisha kushukuru akaumega, akasema, Huu ndio mwili wangu ulio kwa ajili yenu; fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu. Na vivi hivi baada ya kula akakitwaa kikombe, akisema, Kikombe hiki ni agano jipya katika damu yangu; fanyeni hivi kila mnywapo, kwa ukumbusho wangu. Maana kila mwulapo mkate huu na kukinywea kikombe hiki, mwaitangaza mauti ya Bwana hata ajapo." 1 Wakarintho 11:23-26.

Kristo alikuwa amesimama kwenye eneo la mpito kati ya mifumo miwili ya desturi na kati ya sikukuu mbili za mifumo hiyo. Yeye, aliye Mwana-kondoo wa Mungu asiye na waa, alikuwa anakaribia kujitoa kama sadaka ya dhambi, ili ya kwamba kwa njia hiyo aufikishe kwenye mwisho mfumo wa ibada za vivuli na maadhimisho ambayo kwa miaka elfu nne yalikuwa yamesonda kidole kwa kifo chake. Alipokula Pasaka na wanafunzi wake, mahali palipokuwa pa sikukuu ile, alianzisha huduma ambayo ingekuwa kumbukumbu ya kafara yake kuu. Maadhimisho hayo ya kitaifa ya Wayahudi yalikuwa yaachwe milele. Ibada ambayo ilianzishwa na Kristo ingefanywa na wafuasi wake katika nchi zote na vizazi vyote.

Pasaka ilianzishwa kama maadhimisho ya ukumbusho wa ukombozi wa Israeli kutoka katika utumwa wa Misri. Mungu alikuwa ameelekeza kwamba, mwaka hadi mwaka, watoto watakapouliza maana ya kaida hii, historia ile inapaswa kurudiwa. Kwa njia hiyo ukombozi ule wa ajabu ungekuwa kama mpya katika akili ya watu wote. Kaida ya Chakula cha Bwana ilitolewa **(653)** ili kuwa ukumbusho wa ukombozi mkuu ulioletwa kama matokeo ya kifo cha Kristo. Kumbukumbu hii itaendelea kusherehekewa mpaka atakapokuja mara ya pili katika uweza na utukufu. Hii ni njia ambayo kwayo kazi kubwa kwa ajili yetu itapaswa kuendelea kuwa mpya akilini mwetu.

Wakati wa ukombozi wao kutoka Misri, wana wa Israeli walikula chakula cha Pasaka wakiwa wamesimama, wakiwa wamejifunga viuno vyao, na wakiwa na fimbo zao mikononi, wakiwa tayari kwa safari. Ile namna walivyosherehekea kaida hii iliendana na hali yao; maana walikuwa wanakaribia kuondoka kwenda mbali na nchi ya Misri, na walikuwa waanze safari ngumu na ya maumivu ya kupitia jangwani. Lakini mnamo siku za Kristo hali ya mambo ilikuwa imebadilika. Kwa sasa si kwamba walitaka kuondoka katika nchi ya ugeni, bali walikuwa wakazi katika nchi yao. Kulingana na upatanifu wa pumziko walilokuwa wamepewa, wakati huu watu walishiriki chakula cha Bwana katika mkao wa kujinyoosha kwa kuegamea nyuma. Makochi yalipangwa kuzunguka meza, na wageni waliyalalia, wakijiegemeza kwenye mkono wa kushoto, na kuuacha mkono wa kuume ukiwa huru ili kutumika katika kula. Katika mkao huu mgeni angeweza kulaza kichwa chake kwenye kifua cha mtu aliyeko juu upande wa nyuma yake. Na miguu, ikiwa kwenye mwisho wa nje wa kochi lile, ingeweza kuoshwa na mtu anayepita kwenye mzunguko wa nje wa mduara.

Bado Kristo yuko penye meza iliyotandazwa chakula cha pasaka. Keki zisizo na chachu zilizokuwa kwa kawaida zinatumika katika kipindi cha pasaka zilikuwa mbele yake. Divai ya pasaka, isiyoguswa na uchachu, iko mezani. Kristo anatumia alama hizi kueleza kafara yake isiyo na dosari. Hakuna kitu chenye kuharibiwa na chachu, ishara ya dhambi na kifo, ambacho kingemwakilisha "Mwana-kondoo asiye na ila, asiye na waa." 1 Peter 1:19.

"Nao walipokuwa wakila Yesu alitwaa mkate, akabariki, akaumega, akawapa wanafunzi wake, akasema, Twaeni, mle; huu ndio mwili wangu. Akakitwaa kikombe, akashukuru, akawapa, akisema, Nyweni nyote katika hiki; kwa maana hii ndiyo damu yangu ya agano, imwagikayo kwa ajili ya wengi kwa ondoleo la dhambi. Lakini nawaambieni, Sitakunywa kabisa tangu sasa uzao huu wa mzabibu, hata siku ile nitakapokunywa mpya pamoja nanyi katika ufalme wa Baba yangu."

Yuda yule mwenye kumsaliti alikuwepo katika huduma hii ya sakramenti. Alipokea kwa Yesu ile ishara ya mwili wake uliovunjwa na ya damu yake iliyotiririshwa. Aliyasikia yale maneno kwamba, "Fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu." Na akiwa amekaa pale mbele ya Mwana-kondoo wa Mungu, msaliti huyu alisumbuliwa na makusudi yake yale ya giza, na akaendelea kushikilia mawazo yale ya kisasi na uovu wa chini-chini.

Wakati wa kuosha miguu, Kristo alikuwa ametoa kemeo la wazi la kuthibitisha kwamba alifahamu tabia ya Yuda. Alisema, "Si nyote mlio safi" (Yohana 13:11). **(654)** Maneno haya yalimthibitishia yule mwanafunzi asiye wa kweli kwamba Kristo aliyasoma makusudi yake. Sasa Kristo alisema wazi wazi zaidi. Walipokuwa wamekaa mezani alisema, huku akiwatazama wanafunzi wake, "Sisemi habari za ninyi nyote; nawajua wale niliowachagua; lakini andiko lipate kutimizwa, Aliyekula chakula changu Ameniinulia kisigino chake."

Hata sasa bado wanafunzi hawakumshuku Yuda. Lakini waliona kwamba Kristo alionekana kusumbuka sana. Wingu zito liliwakalia wote, hisia ya mambo yajayo ya janga la kutisha, ambalo hawakulijua ni la namna gani. Walipokuwa wanakula wakiwa kimya, Yesu alisema, "Amin, amin, nawaambieni, Mmoja wenu atanisaliti." Kwa maneno haya walitekwa na mshangao na wasiwasi. Hawakuweza kupambanukiwa kwamba ni jinsi gani mmoja wao angemtendea usaliti Mwalimu wao wa kimbingu. Kwa sababu ipi wamsaliti? Na wamsaliti kwa nani? Ni moyo wa mtu yupi ambao ungefikia hali ya kupanga hivyo? Hakika si mmoja wa wale kumi na wawili waliopendelewa zaidi ya watu wengine katika kusikia mafundisho ya Yesu, ambao waliokuwa wameshiriki upendo wake wa ajabu, na ambao kwa ajili yao alikuwa ameonyesha kuwajali kwa kuwaleta katika ushirika wa karibu na Yeye!

Kadiri walivyogundua umuhimu wa maneno yake, na kugundua jinsi maneno yake yalivyokuwa ya kweli, woga na kutojiamini viliwahusuru. Walianza kupeleleza mioyo yao wenyewe kuona ikiwa kulikuwa na wazo lolote lililokuwa dhidi ya Bwana wao. Kwa maumivu makubwa sana ya hisia, mmoja baada ya mwingine aliuliza akisema, "Je! Ni mimi?" Lakini Yuda alikaa kimya. Hatimaye kwa kuguswa kwa kina Yohana aliuliza, "Bwana, ni nani?" Yesu akajibu, "Yeye aliyetia mkono wake pamoja nami katika kombe, ndiye atakayenisaliti. Mwana wa Adamu aenda zake, kama alivyoandikiwa; lakini ole wake mtu yule ambaye amsaliti Mwana wa Adamu! Ingekuwa heri kwake mtu yule kama asingalizaliwa." Wale wanafunzi walikuwa wamechunguzana nyuso kwa ukaribu walipokuwa wanauliza kwamba, "Je! Ni mimi?" na sasa ukimya wa Yuda uliyavuta macho yao wote kwake. Katikati ya zile kelele na kuchanganyikiwa, Yuda hakuwa amesikia maneno ya Yesu alivyojibu swali la Yohana. Lakini sasa, ili kukwepa kuchunguzwa na wanafunzi, aliuliza kama walivyokuwa wamefanya, "Ni mimi, Rabi?" Yesu akasema kwa uthabiti, "Wewe umesema."

Akiwa katika mshangao na kuchaganyikiwa kwa makusudi yake kuwekwa wazi, Yuda aliinuka haraka ili kuondoka mle chumbani. "Basi Yesu akamwambia, Uyatendayo yatende upesi. . . . Basi huyo, akiisha kulipokea lile tonge, akatoka mara hiyo. Nako kulikuwa ni usiku." Ilikuwa usiku pia kwa msaliti huyo kadiri alivyogeukia mbali akiondoka kwa Kristo kwenda katika giza la nje.

Mpaka wakati hatua hii ilipofikiwa, Yuda hakuwa amevuka mpaka wa uwezekano wa kutubu. Lakini wakati huu alipoondoka mbele ya uwepo wa Bwana wake na mbele ya **(655)** wanafunzi wenzake, uamuzi wa mwisho ulikuwa umefanywa. Alikuwa amevuka mstari wa mpaka.

Uvumilivu wa Yesu ulikuwa umekuwa wa ajabu katika kushughulika na nafsi hii iliyokuwa ikijaribiwa. Hakuna jambo ambalo lingepaswa kufanywa ili kumwokoa Yuda ambalo halikufanywa. Baada ya kuwa amefanya makubaliano mara mbili ya kumsaliti Bwana wake, bado Yesu alimpa nafasi ya kutubu. Kwa kusoma makusudi ya siri ya moyo wa msaliti yule, Kristo alimpa Yuda ushuhuda wa mwisho wa uungu wake. Kwa mwanafunzi huyu asiye wa kweli huu ulikuwa wito wa mwisho wa kutubu. Hakuna wito ambao moyo wa Kristo wa uungu ulikuwa umebakiza. Mawimbi ya rehema, ambayo yalisukumizwa kwa kiburi cha usumbufu kurudishwa yalikotoka, yalirudi katika upendo wa kujishusha. Lakini ingawa alishangazwa na kugutushwa kwa kugunduliwa kwa hatia yake, Yuda alikuwa mtu anayedhamiria zaidi. Alitoka katika chakula kile cha sakramenti na kuondoka zake kwenda kutekeleza kazi yake ya kumsaliti.

Katika kumtamkia ole Yuda, Kristo alikuwa pia na kusudi jema kwa wanafunzi wake. Kwa njia hiyo aliwapa uthibitisho wa juu wa Umasihi wake. Alisema, "Nawaambia kabla hayajatukia, ili yatakapotukia mpate kuamini ya kuwa mimi ndiye." Ikiwa Yesu angebaki kimya, katika hali kama ile ya kutojua yaliyokuwa yanamjia, wanafunzi wangedhani kwamba Bwana wao hana maono ya kiungu, na kwamba ameshtushwa pasipo kujua na kusalitiwa katika mikono ya genge la wauaji. Mwaka mmoja kabla, Yesu alikuwa amewaambia wanafunzi wale kwamba alikuwa amechagua kumi na wawili, na kwamba mmoja alikuwa ni mwovu. Sasa maneno aliyomwambia Yuda, yakionyesha kwamba mipango yake ya usaliti ilikuwa inajulikana na Bwana wake kwa

ukamilifu, ingeimarisha imani ya wafuasi wa kweli wa Kristo wakati wa kuteseka kwake. Na wakati ambapo Yuda angekuja katika hatima yake ya kutisha, wangekumbuka ole ile ambayo Yesu alimtamkia msaliti yule.

Mwokozi alikuwa bado ana kusudi jingine. Hakuwa ameificha huduma yake mbali na yeye aliyemjua kama msaliti. Wanafunzi hawakuelewa maneno yake wakati wa uoshaji wa miguu aliposema, "Si nyote mlio safi," wala wakati walipokuwa mezani aliposema, "Aliyekula chakula changu ameniinulia kisigino chake." Yohana 13:11, 18. Lakini baada ya pale, wakati maana ya Yesu ilipokuwa wazi, walikuwa na kitu cha kuzingatia kuhusu uvumilivu na wema wa Mungu kwa yeye aliyekuwa anapotea kwa kiburi.

Ingawa Yesu alimjua Yuda tangu mwanzo, alimwosha miguu. Na msaliti huyu alipendelewa kuungana na Kristo katika kushiriki ile sakramenti. Mwokozi mwenye uvumilivu aliondoa kila kiashirio cha mtazamo mbaya ili kwamba mwenye dhambi ampokee, atubu, na kutakaswa kutokana na uchafu wa dhambi. Kielelezo hiki ni kwa ajili yetu. Tunapoona kwamba mtu yuko katika makosa na dhambi, hatupaswi kujitenga naye. Hatupaswi **(656)** kutengana naye bila kujali na kumwacha kuwa mawindo ya majaribu, au kumsukumia kwenye uwanja wa mapigano wa Shetani. Hii si njia ya Kristo. Kule kuwaosha wanafunzi miguu kulikuwa ni kwa sababu wao pia walikuwa watu wenye makosa na wenye mapungufu, na wote isipokuwa mmoja wao waliletwa katika toba kwa njia hiyo.

Kielelezo cha Kristo kinakataza hali ya kujiona bora kuliko wengine wakati wa Chakula cha Bwana. Ni kweli kwamba dhambi ya wazi humtenga mtu aliyeitenda. Roho Mtakatifu ndiye anayeweza kufundisha kuhusu hilo. 1 Wakorintho 5:11. Lakini zaidi ya hapo hakuna awezaye kuweka hukumu. Mungu hakuwaachia wanadamu mamlaka ya kusema ni wepi wanaopaswa kujihudhurisha katika matukio haya. Maana ni nani awezaye kuusoma moyo? Nani awezaye kutofautisha magugu kutoka katika ngano? "Mtu ajihoji mwenyewe, na hivyo aule mkate, na kukinywea kikombe." Maana "kila aulaye mkate huo, au kukinywea kikombe hicho cha Bwana isivyostahili, atakuwa amejipatia hatia ya mwili na damu ya Bwana." 1 Wakorintho 11:28, 27, 29.

Wakati waumini wakusanyikapo ili kuadhimisha kaida hizi, wapo wajumbe wasioonekana kwa macho ya kibinadamu. Kunaweza kukawa na mtu ambaye ni Yuda katika kundi hilo, na kama ni hivyo, wajumbe kutoka kwa mfalme wa giza wapo hapo, maana wanawatembelea wote wanaokataa kuongozwa na Roho wa Mungu. Malaika wa mbinguni wanakuwepo pia. Watembezi hawa wasioonekana wapo katika kila tukio kama hilo. Wanaweza wakaja kundini watu ambao si watumishi wa moyo wa ukweli na utakatifu, lakini ambao wanapenda kushiriki katika huduma hii. Hawa wasizuiliwe. Kuna mashuhuda waliopo ambao walikuwepo wakati ule Yesu alipoosha miguu ya wanafunzi na ya Yuda. Macho ambayo ni zaidi ya yale ya mwanadamu yaliona tukio lile.

Kwa njia ya Roho Mtakatifu Kristo yupo ili kutia muhuri kwenye kaida yake. Yupo ili kuusadikisha na kuulanisha moyo. Hakuna mtupo wa jicho, hakuna wazo la toba, ambalo linakwepa kuonwa naye. Maana anamsubiri mtu mwenye moyo uliopondeka atubuye. Vitu vyote viko tayari kwa ajili ya kumpokea mtu huyo. Yeye aliyeiosha miguu ya Yuda anatamani kuosha kila moyo kutoka katika doa la dhambi.

Kusiwe na mtu wa kujitenga na Ushirika eti kwa sababu huenda watu wasiostahili wakawemo. Kila mwanafunzi anaitwa kushiriki hadharani, na kwa njia hiyo kushuhudia ya kwamba anamkubali Kristo kama Mwokozi wake. Katika nyakati zake hizi zilizoamuliwa ndipo Kristo hukutana na watu wake, na kuwatia nguvu kwa kuwepo kwake. Hata kama huduma hii inaweza kusimamiwa na mioyo na mikono isiyostahili, lakini bado Kristo yupo hapo ili kuwahudumia watoto wake. Wote wanaokuja na imani yao ikiwa imekazwa kwake watabarikiwa sana. Wote wanaopuuza vipindi hivi vya upendeleo wa kimbingu watapata hasara. Kuhusu hawa inaweza kuwa sahihi kusema, "Si nyote mlio safi."

Katika kushiriki mkate na divai pamoja na wanafunzi wake, Kristo alijitoa **(659)** kwao kama Mkombozi. Aliwakabidhi agano jipya, ambayo kupitia hiyo wote wanaompokea huwa watoto wa Mungu, na warithi pamoja na Kristo. Kwa njia ya agano hili kila mbaraka ambao mbingu iliweza kutoa kwa ajili ya maisha haya na yale yajayo ulikuwa wao. Kitendo hiki cha agano kingesajiliwa kwa damu ya Kristo. Na ufanyaji wa sakramenti hii ungeendelea kuwaonyesha wanafunzi kafara ya daima iliyofanywa kwa ajili ya kila mmoja wao kama sehemu ya jamii yote kubwa ya wanadamu walioanguka.

Lakini ibada ya Ushirika haikupaswa kuwa wakati wa huzuni. Hili halikuwa kusudi lake. Wakati wanafunzi wa Bwana wanapokuwa wamekusanyika mezani, hawapaswi kukumbuka na kuombolezea mapungufu yao.

Hawapaswi kuzama katika uzoefu wao wa kidini uliopita, iwe uzoefu ule ulikuwa unaoinua juu au unaoshusha. Hawatakiwi kukumbuka tofauti zilizopo kati yao na ndugu zao. Huduma ya maandalizi imeshamaliza yote haya. Kujichunguza, kuungama dhambi, kumaliza tofauti, vyote vimefanywa. Sasa wanakuja kukutana na Kristo. Hawapaswi kusimama katika kivuli cha huzuni ya msalaba, bali katika nuru yake iokoayo. Wanapaswa kufungua mioyo ili kupokea miale ya nguvu ya Jua la Haki, ingawa haionekani, wanatakiwa wasikie maneno yake kwamba, "Amani nawaachieni; amani yangu nawapa; niwapavyo mimi sivyo kama ulimwengu utoavyo." Yohana 14:27.

Bwana wetu anasema kwamba, Chini ya usadikisho wa dhambi, kumbukeni kwamba nilikufa kwa ajili yenu. Mnapoonewa na kuteswa kwa ajili yangu na injili, kumbukeni upendo wangu, ulio mkubwa sana kiasi kwamba niliyatoa maisha yangu kwa ajili yenu. Majukumu yanapoonekana kuwa magumu na makali, na mizigo yenu kuwa mizito msiyoweza kubeba, kumbukeni kwamba kwa ajili yenu niliustahimili msalaba, nikiidharau aibu. Pindi mioyo itakapozimia kwa ugumu wa majaribu, kumbukeni kwamba Mkombozi wenu anaishi akiomba kwa ajili yenu.

Huduma ya Ushirika inasonda kidole katika kuja kwa Kristo mara ya pili. Iliwekwa ili kudumisha tumaini hili katika mawazo ya wanafunzi wale. Kila mara walipokutana pamoja ili kukumbuka kufa kwake, walikumbuka jinsi ambavyo alitwaa "kikombe, akashukuru, akawapa, akisema, Nyweni nyote katika hiki; kwa maana hii ndiyo damu yangu ya agano, imwagikayo kwa ajili ya wengi kwa ondoleo la dhambi. Lakini nawaambieni, Sitakunywa kabisa tangu sasa uzao huu wa mzabibu, hata siku ile nitakapokunywa mpya pamoja nanyi katika ufalme wa Baba yangu." Katika mateso yao walipata faraja katika tumaini la kurudi kwa Bwana. Thamani isiyosemekana kwao ilikuwa ni wazo kwamba, "Kila mwulapo mkate huu na kukinywea kikombe hiki, mwaitangaza mauti ya Bwana hata ajapo." 1 Wakorintho 11:26.

**(660)** Hivi ni vitu ambavyo hatupaswi kusahau. Upendo wa Yesu, pamoja na uwezo wake, vinapaswa vihifadhiwe vikiwa kama vipya katika kumbukumbu zetu. Kristo ameanzisha huduma hii ili kwamba ipate kunena na fahamu zetu kuhusu upendo wa Mungu ambao umeonyeshwa kwa ajili yetu. Haiwezekani kuwa na mwungano kati ya mioyo yetu na Mungu isipokuwa kupitia Kristo. Lazima mwungano na upendo kati ya ndugu na ndugu ushikamanishwe na kutiwa mafuta ya milele na upendo wa Yesu. Na hakuna kitu kilicho chini zaidi kuliko kifo cha Kristo ambacho kingeweza kuufanya upendo wake ufanye kazi kwa ajili yetu. Ni kwa sababu ya kifo chake tu kwamba tunaweza kutazamia kwa furaha kuja kwake mara ya pili. Kafara yake ndiyo kitovu cha tumaini letu. Lazima tukaze imani yetu kwenye kafara hii.

Kaida zinazoashiria maumivu na mateso ya Bwana wetu zinachukuliwa zaidi kama desturi. Zilianzishwa kwa kusudi. Fahamu zetu zinahitaji kuhimizwa katika kushikilia siri za utauwa. Ni jambo muhimu kwa wote kuelewa, kwa kiasi kikubwa kwa mbali kuliko tujuavyo, mateso ya fidia ya Kristo. "Kama vile Musa alivyomwinua nyoka jangwani," ndivyo hivyo Mwana wa Adamu alivyoinuliwa juu, "ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele." Yohana 3:14, 15. Lazima tutazame msalaba wa Kalvari, mahali alipo Mwokozi anayekufa. Hamu zetu za ndani zinadai kwamba tuonyeshe imani yetu katika Kristo.

Bwana wetu alisema, "Msipoula mwili wake Mwana wa Adamu na kuinywa damu yake, hamna uzima ndani yenu. . . . Kwa maana mwili wangu ni chakula cha kweli, na damu yangu ni kinywaji cha kweli." Yohana 6:53-55. Hili ni la kweli kuhusu maumbile yetu ya asili. Tunapata hata maisha haya ya kidunia kwa kifo cha Yesu. Mkate tunaokula unapatikana kwa kununuliwa kwa njia ya mwili wake uliovunjwa. Maji tunayokunywa yananunuliwa kwa michirizi ya damu yake. Kamwe mtu, mtakatifu au mwenye dhambi, hali mkate wake wa kila siku, asiponawirishwa na mwili na damu ya Kristo. Msalaba wa Kalvari ni kama chapa ambayo imetiwa kwenye kila mkate. Unaakisiwa katika kila maji ya chemchemi. Kristo amefundisha yote haya katika kuchagua ishara za kafara yake. Nuru iangazayo kutoka katika ibada ile ya Ushirika katika chumba cha ghorofani inatakasa vyakula vya maisha yetu ya kila siku. Meza ya familia inakuwa kama meza ya Bwana, na kila mlo katika familia unakuwa kama sakramenti.

Na maneno ya Kristo ni ya ukweli mkubwa kiasi gani kuhusu hali yetu ya kiroho. Anasema, "Aulaye mwili wangu na kuinywa damu yangu anao uzima wa milele." Tunaweza kuishi maisha ya utakatifu kwa kupokea maisha yaliyomwagwa kwa ajili yetu kutoka kwenye msalaba wa Kalvari. Na tunapata maisha haya kwa kulipokea neno lake, kwa kufanya vitu vile ambavyo ameagiza. Kwa njia hiyo tunakuwa wamoja pamoja naye. Anasema, "Aulaye mwili wangu na kuinywa damu yangu hukaa ndani yangu, nami hukaa ndani yake. Kama vile Baba **(661)** aliye

hai alivyonituma mimi, nami ni hai kwa Baba; kadhalika naye mwenye kunila atakuwa hai kwa mimi." Yohana 6:54, 56, 57. Kwa namna ya pekee andiko hili lina uhusiano na Ushirika mtakatifu. Kadiri imani inavyotafakari kafara kuu ya Bwana wetu, moyo unageuka na kuwa kama maisha ya kiroho ya Kristo. Moyo huo utapokea nguvu ya kiroho kutoka katika kila tendo la Ushirika. Ibada hiyo hufanya mwunganiko ulio hai ambao kwa huo muumini anafungamanishwa na Kristo, na hivyo kufungamanishwa na Baba. Kwa namna ya pekee inafanya mwunganiko kati ya mwanadamu mwenye utegemezi na Mungu.

Kadiri tunavyopokea mkate na divai vinavyoashiria mwili uliovunjwa na damu iliyochuruzika, tunajiunga kwa mawazo katika lile tukio la Ushirika lililofanyika katika chumba cha juu. Tunaonekana kupita katika bustani iliyotengwa na mateso ya Yeye aliyebeba dhambi za ulimwengu. Tunashuhudia pambano ambalo kwa hilo upatanisho wetu na Mungu ulipatikana. Kristo anawekwa wazi akiwa amesulibiwa katikati yetu.

Kwa kumwangalia Mkombozi aliyesulibiwa, tunaelewa kwa utimilifu ukubwa na maana ya kafara iliyofanywa na Mwenye uweza wa mbinguni. Mpango wa wokovu unatukuzwa mbele yetu, na wazo la Kalvari linaamsha hisia zilizo hai na takatifu mioyoni mwetu. Sifa kwa Mungu na kwa Mwana-kondoo zitakuwa mioyoni mwetu na midomoni mwetu; maana kiburi na kujiabudu haviwezi kutoka katika moyo unaokumbuka matukio ya Kalvari.

Yeye atazamaye upendo wa Mwokozi usiolinganishwa na kitu atainuliwa katika mawazo yake, atasafishwa moyoni, atabadilishwa kitabia. Ataondoka kwenda kuwa nuru kwa ulimwengu, kuakisi kwa kiasi fulani upendo huu wa ajabu. Kadiri tunavyotafakari zaidi msalaba wa Kristo, ndivyo tutakavyozoea zaidi lugha ya mtume aliposema, "Lakini mimi, hasha, nisione fahari juu ya kitu chochote ila msalaba wa Bwana wetu Yesu Kristo, ambao kwa huo ulimwengu umesulibishwa kwangu, na mimi kwa ulimwengu." Wagalatia 6:14.

# Sura ya 73

## "Msifadhaike Mioyoni Mwenu"

[Sura hii imejengwa katika Yohana 13:31-38; 14-17.]

Akiwatazama wanafunzi wake kwa upendo wa kimbingu, na kwa huruma ya upendo, Kristo alisema, "Sasa ametukuzwa Mwana wa Adamu, naye Mungu ametukuzwa ndani yake." Yuda alikuwa ameondoka zake kutoka katika chumba kile cha ghorofani, na Kristo alikuwa peke yake akiwa pamoja na wale kumi na mmoja. Alikuwa anakaribia kuwaambia habari za utengano kati yake na wao uliokuwa unakuja; lakini kabla ya kufanya hilo alionyesha lengo kuu la kazi yake. Hili ndilo ambalo daima aliwaonyesha. Ilikuwa furaha yake kwamba masumbuko na mateso yake yote yangelitukuza jina la Baba. Anayaelekeza mawazo ya wanafunzi wake katika hili kwanza.

Halafu akiwaambia kwa neno la kuonyesha ukaribu, "Watoto wadogo," alisema, "bado kitambo kidogo nipo pamoja nanyi; mtanitafuta; na kama vile nilivyowaambia Wayahudi ya kwamba, Mimi niendako ninyi hamwezi kuja; kadhalika sasa nawaambia ninyi."

Wale wanafunzi hawakuweza kufurahi waliposikia hayo. Hofu iliwaangukia. Walimsogelea zaidi Mwokozi. Kiongozi wao na Bwana, Mwalimu wao mpendwa na Rafiki, alikuwa kipenzi kwao kuliko maisha. Walikuwa wamemtazama Yeye ili kupata msaada wakati wa mambo magumu, kupata faraja wakati wa huzuni na kufadhaika. Sasa alikuwa awaache, wakiwa kundi tegemezi lenye upweke. Giza lilijaza mioyo yao.

Lakini maneno ya Mwokozi kwao yalikuwa yamejaa tumaini. Alijua kwamba wangeyumbishwa na adui, na kwamba mbinu za Shetani zanafanikiwa zaidi dhidi ya wale wanaosongwa na ugumu wa mambo. Kwa hiyo aliwaelekeza mbali na "vinavyoonekana," ili waelekee katika "visivyoonekana." 2 Wakorintho 4:18. Aliyageuza mawazo yao kutoka katika maisha ya ugenini ya duniani na kuyaelekeza nyumbani mbinguni.

**(663)** "Msifadhaike mioyoni mwenu;" alisema; "mnamwamini Mungu, niaminini na mimi. Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi; kama sivyo, ningaliwaambia; maana naenda kuwaandalia mahali. Basi mimi nikienda na kuwaandalia mahali, nitakuja tena niwakaribishe kwangu; ili nilipo mimi, nanyi mwepo. Nami niendako mwaijua njia." Nilikuja ulimwenguni kwa ajili yenu. Nafanya kazi kwa ajili yenu. Ninapoondoka zangu bado nitafanya kazi kwa ajili yenu. Nilikuja ulimwenguni kujifunua kwenu, ili ya kwamba mpate kuamini. Naenda kwa Baba kushirikiana naye kwa ajili yenu. Lengo la kuondoka kwa Kristo lilikuwa kinyume cha kile kilichohofiwa na wanafunzi. Haikumaanisha utengano wa mwisho kabisa. Alikuwa anaenda kuandaa mahali kwa ajili yao, ili ya kwamba arudi tena, na kuwapeleka kwake. Wakati alipokuwa anajenga makao kwa ajili yao walipaswa kujenga tabia ili ifanane na hali ya kimbingu.

Bado wanafunzi walitatanishwa. Tomaso, ambaye mara nyingi alisumbuliwa na mashaka, alisema, "Bwana, sisi hatujui uendako; nasi twaijuaje njia? Yesu akamwambia, Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi. Kama mngalinijua mimi, mngalimjua na Baba; tangu sasa mnamjua, tena mmemwona."

Hakuna njia nyingi za kwenda mbinguni. Kila mmoja hawezi kuchagua njia yake. Kristo anasema, "Mimi ndimi njia, . . . mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi." Tangu hubiri lile la kwanza la injili lilipohubiriwa, wakati lilipotangazwa mle Edeni kwamba uzao wa mwanamke utaponda kichwa cha nyoka, Kristo alikuwa ameinuliwa kama njia, kweli, na uzima. Alikuwa njia wakati Adamu alipokuwa anaishi, wakati Habili alipomtolea Mungu damu ya mwana-kondoo aliyechinjwa, ikiwakilisha damu ya Mkombozi. Kristo alikuwa njia ambayo kwayo wazee na manabii waliokolewa. Yeye ni njia ambayo kwa hiyo tu tunaweza kumfikia Mungu.

Kristo alisema, "Kama mngalinijua mimi, mngalimjua na Baba; tangu sasa mnamjua, tena mmemwona." Lakini bado wanafunzi hawakuelewa. Filipo akasema, "Bwana, utuonyeshe Baba, yatutosha."

Akiwa ameshangazwa na ugumu wa Filipo kuelewa, Kristo aliuliza kwa mshangao wa uchungu, "Mimi nimekuwapo pamoja nanyi siku hizi zote, wewe usinijue, Filipo?" Je! Inawezekana kwamba humwoni Baba katika kazi anazofanya kupitia Mimi? Hauamini kwamba nilikuja kushuhudia kuhusu Baba? "Basi wewe wasemaje, Utuonyeshe Baba?" "Aliyeniona mimi amemwona Baba." Kristo hakuwa amekoma kuwa **(664)** Mungu

wakati alipofanyika mwanadamu. Ingawa alikuwa amejishusha mpaka hali ya ubinadamu, Uungu ulikuwa bado wake. Kristo pekee ndiye angeweza kumwakilisha Baba kwa wanadamu, na wanafunzi walikuwa wamejaliwa kuuona uwakilishi huu kwa zaidi ya miaka mitatu.

"Mnisadiki ya kwamba mimi ni ndani ya Baba, na Baba yu ndani yangu; la! Hamsadiki hivyo, sadikini kwa sababu ya kazi zenyewe." Imani yao ilipaswa ijengwe salama kwenye ushahidi uliotolewa katika kazi za Kristo, kazi ambazo hakuna mwanadamu ambaye, kwa yeye mwenyewe, alikuwa amepata kuzifanya, au hata kuweza kuzifanya. Kazi za Kristo zilishuhudia uungu wake. Baba alikuwa amefunuliwa ndani yake.

Ikiwa wanafunzi wangeamini huu mwunganiko muhimu kati ya Baba na Mwana, imani yao isingewaacha wakati walipoona mateso ya Kristo na kifo chake kwa ajili ya kuwokoa ulimwengu unaoangamia. Kristo alikuwa anatafuta kuwatoa katika hali yao ya chini ya imani kuwapeleka katika uzoefu ambao wangepata wakitambua kweli kweli kwamba Yeye ni nani, - Mungu aliye katika mwili wa mwanadamu. Alitaka waone kwamba lazima imani yao iwaongoze juu kwenda kwa Mungu, na kutiwa nanga pale. Ni jinsi gani Mwokozi wetu mwenye huruma alivyotafuta kuwaandaa wanafunzi wake kwa uvumilivu na ustahimilivu kwa ajili ya dhoruba ya majaribu ambayo muda si mrefu ingewapiga. Angewafanya wafichwe pamoja naye ndani ya Mungu.

Wakati Kristo alipokuwa akinena maneno haya, utukufu wa Mungu ulikuwa unaangaza katika uso wake, na wote waliokuwepo walihisi mshangao mtakatifu kadiri walivyosikiliza maneno yake kwa hamu. Mioyo yao ilivutwa zaidi kwake; na kadiri walivyovutwa kwa Kristo kwa upendo mkuu zaidi, walivutwa mtu mmoja kwa mwingine. Waliona kwamba mbingu ilikuwa karibu sana, na kwamba maneno waliyosikia yalikuwa ujumbe wao kutoka kwa Baba wa mbinguni.

Yesu aliendelea kwamba, "Amin, amin, nawaambieni, Yeye aniaminiye mimi, kazi nizifanyazo mimi, yeye naye atazifanya." Yesu alikuwa na hamu sana kwamba wanafunzi wake waelewe kusudi la uungu wake kuungana na ubinadamu. Alikuja ulimwenguni kuuonyesha utukufu wa Mungu, ili kwamba mwanadamu ainuliwe na nguvu irejeshayo. Mungu alidhihirishwa ndani yake ili kwamba Yeye naye adhihirishwe ndani yao. Yesu hakufunua viwango, au kuonyesha uweza, ambao wanadamu hawawezi kuwa nao kwa njia ya imani ndani yake. Ubinadamu wake mkamilifu ni ule ambao wafuasi wake wote wanaweza kuwa nao, ikiwa watakuwa watiifu kwa Mungu kama alivyokuwa.

"Naam, na kubwa kuliko hizo atafanya, kwa kuwa mimi naenda kwa Baba." Kwa maneno haya Kristo hakuwa na maana kwamba kazi za wanafunzi zingekuwa za namna ya kutukuzwa zaidi kuliko zake, bali kwamba zingekuwa na mapana makubwa zaidi. Hakuwa anaongelea hasa ufanyaji wa miujiza, bali alikuwa anaongea kuhusu kazi zote ambazo zingefanyika chini ya utendaji wa Roho Mtakatifu. **(667)** Baada ya kupaa kwa Bwana, wanafunzi waligundua utimilifu wa ahadi yake. Matukio ya kusulibiwa, kufufuka, na kupaa kwa Kristo yalikuwa uhalisia ulio hai kwao. Waliona kwamba unabii ulikuwa umetimia kama ulivyo. Waliyasoma Maandiko, na wakayakubali mafundisho yao kwa imani na uhakika ambao haukujulikana kabla. Walijua kwamba yule Mwalimu wa kimbingu alikuwa vile vyote alivyojisema kuwa. Kadiri walivyoeleza uzoefu wao, na kuinua upendo wa Mungu, mioyo ya watu iliyeyushwa na kutiishwa, na makutano ya watu walimwamini Yesu.

Ahadi ya Mwokozi kwa wanafunzi wake ni ahadi kwa kanisa lake mpaka mwisho wa wakati. Mungu hakupanga kwamba mpango wake wa kuwakomboa wanadamu ufikie matokeo yasiyo na umuhimu mkubwa. Wote watakoenda kufanya kazi, wakiwa hawatumaini katika mambo wanayoweza kufanya wao wenyewe, bali katika yale ambayo Mungu anaweza akafanya kwa ajili yao na kupitia kwao, kwa hakika wataiona ahadi yake ikitimia. "Naam, na kubwa kuliko hizo atafanya," alisema, "kwa kuwa mimi naenda kwa Baba."

Mpaka hapo bado wanafunzi walikuwa hawajapambanukiwa na hali ya Mwokozi kuwa na rasilimali na nguvu zisizo na mpaka. Aliwaambia, "Hata sasa hamkuomba neno kwa jina langu." Yohana 16:24. Alielezea kwamba siri ya mafanikio yao ingekuwa katika kuomba kwa ajili ya nguvu na neema kwa jina lake. Yeye angekuwa mbele ya Baba ili kuomba kwa ajili yao. Anawasilisha sala ya mwombaji mnyenyekevu kama vile ndilo hitaji lake mwenyewe badala ya nafsi ile iombayo. Kila ombi la dhati husikiwa mbinguni. Inawezekana lisiwasilishwe kwa ufundi; lakini ikiwa moyo uko ndani yake, litapaa kwenda katika mahali patakatifu Yesu anapohudumia, naye ataliwasilisha kwa Baba bila neno lolote la kusita, likiwa zuri na la kunukia uvumba wa ukamilifu wake Yeye.

Njia ya wema na uaminifu si njia ambayo haina vikwazo, bali katika kila jambo gumu tunapaswa tuone wito wa kuomba. Hakuna yeyote aishiye ambaye ana nguvu asizopata kwa Mungu, na chanzo hicho cha nguvu kiko wazi hata kwa mwanadamu mdhaifu mno kuliko wote. "Mkiomba lolote kwa jina langu, hilo nitalifanya, ili Baba atukuzwe ndani ya Mwana. Mkiniomba neno lolote kwa jina langu, nitalifanya."

"Kwa jina langu," ndivyo Kristo alivyowataka wanafunzi wake waombe. Katika jina la Kristo wanafunzi wake wanatakiwa kusimama mbele za Mungu. Kupitia katika thamani ya kafara iliyofanywa kwa ajili yao, wanakuwa wenye thamani mbele za Mungu. Kwa sababu ya kuharibiwa kwa haki ya Kristo wanahesabiwa wenye thamani. Kwa ajili ya Kristo Bwana huwasamehe wamchao. Ndani yao haoni uchafu wa dhambi. Anatambua ndani yao hali ya kufanana na Mwana wake, wamwaminiye.

**(668)** Bwana hufadhaishwa pindi watu wake wanapojiona wenye thamani ya chini. Anatamani warithi wake walioteuliwa wajithamini sawa sawa na gharama aliyowalipia. Mungu aliwataka, la sivyo asingemtuma Mwana wake kwa gharama kubwa vile ili kuwakomboa. Ana kazi nao, na anapendezwa sana wanapopeleka matakwa makubwa kwake, ili kwamba wapate kulitukuza jina lake. Wanaweza kutarajia mambo makubwa ikiwa wanaamini katika ahadi zake.

Lakini kuomba kwa jina la Yesu kuna maana kubwa zaidi. Kuna maana kwamba tunatakiwa kukubali tabia yake, kudhihirisha roho yake, na kufanya matendo yake. Ahadi ya Mwokozi inatolewa kwa masharti. Anasema, "Mkinipenda, mtazishika amri zangu." Haokoi watu dhambini, bali kutoka dhambini; na wale wampendao wataonyesha pendo lao kwa kutii.

Utii wote wa kweli hutoka moyoni. Kwa Kristo kazi ilikuwa ya moyo. Na ikiwa tunakubaliana, Yeye atajitambulisha hivyo katika mawazo yetu na makusudi yetu, akichanganya mioyo na mawazo yetu katika hali ya kupatana na mapenzi yake, kiasi kwamba wakati wa kumtii tutakuwa tunatenda kulingana na misukumo yetu wenyewe maana inapatana na mapenzi yake. Nia, iliyosafishwa na kutakaswa, itakuta hitaji lake la juu ni kufanya kazi yake. Tunapomjua Mungu kama tunavyojaliwa kumjua, maisha yetu yanakuwa maisha ya utii endelevu. Kupitia katika kuikubali tabia ya Kristo, kupitia ushirika pamoja na Mungu, dhambi itakuwa kitu cha kuchukiwa kwetu.

Vile Kristo alivyoiishi sheria akiwa katika ubinadamu, ndivyo tunavyoweza kufanya ikiwa tutaishikilia Nguvu ile kwa ajili ya kupata nguvu. Lakini hatutakiwi kuutwika wajibu wa majukumu yetu juu ya watu wengine, na kuwasubiri wao ndio watwambie la kufanya. Hatuwezi kutegemea mashauri ya mwanadamu. Bwana atatufundisha jukumu letu kwa kupenda kama ambavyo atamfundisha na mtu mwingine. Ikiwa tutakuja kwake kwa imani, atazinena siri zake kwetu tukiwa mtu binafsi. Mara nyingi mioyo yetu itawaka ndani yetu kadiri Yeye anavyotuvuta karibu ili kufanya ushirika pamoja nasi kama alivyofanya kwa Henoko. Wale wanaoamua kutofanya lolote katika njia yoyote wanayodhani haitampendeza Mungu, watajua ni njia ipi ya kufuata baada ya kupeleka shauri lao kwake. Nao watapokea si hekima tu, bali pia nguvu. Uwezo wa kutii, wa kutumika, utatolewa kwao, kama vile Kristo alivyoahidi. Vitu vyovyote vilivyotolewa kwa Kristo – vile “vitu vyote” vya kutosheleza mahitaji ya wanadamu walioanguka – vilitolewa kwake Yeye kama kichwa na kiwakilishi cha wanadamu. Na “lolote tuombalo, twalipokea kwake, kwa kuwa twazishika amri zake, na kuyatenda yapendezayo machoni pake.” 1 Yohana 3:22.

Kabla ya kujitoa mwenyewe kama mhanga wa kafara, Kristo alitafuta zawadi muhimu na kamilifu kuliko zote ili awape wafuasi wake, zawadi ile ambayo **(669)** ingezileta rasilimali za neema zisizo na ukomo mahali wanapoweza kuzifikia. Akasema, "Nami nitamwomba Baba, naye atawapa Msaidizi mwingine, ili akae nanyi hata milele; ndiye Roho wa kweli; ambaye ulimwengu hauwezi kumpokea, kwa kuwa haumwoni wala haumtambui; bali ninyi mnamtambua, maana anakaa kwenu, naye atakuwa ndani yenu. Sitawaacha ninyi yatima; naja kwenu." Yohana 14:16-18.

Kabla ya hapa Roho alikuwepo ulimwenguni; tangu mwanzo kabisa wa kazi ya ukombozi alikuwa akisukuma katika mioyo ya watu. Lakini wakati Kristo alipokuwa duniani, wanafunzi hawakuhitaji msaidizi mwingine. Ni mpaka waliponyang’anywa uwepo wake ndipo wangehisi kumhitaji Roho, na hapo ndipo angekuja.

Roho Mtakatifu ni mwakilishi wa Kristo, lakini akiwa hana umbo la kibinadamu, yu huru. Akiwa amefunikwa na mwili, Kristo asingeweza kuwa kila mahali katika mwili. Kwa hiyo ilikuwa ni kwa faida yao kwamba aende kwa

Baba, na amtume Roho ili achukue nafasi yake duniani. Tangu wakati huo hakuna mtu ambaye angenufaishwa kuliko wengine kwa sababu ya kuwa mahali alipo Kristo au kuwa na bahati ya kukutana na Kristo uso kwa uso kuliko inavyowezekana kwa wengine. Kwa Roho Mtakatifu Mwokozi angepatikana kwa wote. Kwa namna hii Kristo angekuwa karibu nao zaidi kuliko kama asingepaa kwenda juu.

"Naye anipendaye atapendwa na Baba yangu; nami nitampenda na kujidhihirisha kwake." Yesu alisoma wakati wa mbele wa wanafunzi wake. Alimwona mmoja akiletwa kwenye jukwaa la kunyongewa, mwingine akiletwa kwenye msalaba, mwingine kizuizini katikati ya miamba ya upweke ya bahari, wengine wakiletwa katika mateso na vifo. Aliwatia moyo kwamba katika kila majaribu atakuwa pamoja nao. Ahadi ile haijapoteza sehemu yoyote ya nguvu zake. Bwana anajua mambo yote yahusuyo watumishi wake waaminifu ambao kwa ajili yake wanayaweka maisha yao gerezani au ambao wanafukuziwa katika visiwa vya upweke. Anawafariji kwa uwepo wake mwenyewe. Mtu aaminiye anaposimama kwa ajili ya ukweli katika kizimba cha mahakama ya wasio haki, Kristo husimama karibu naye. Kristo anateswa tena na tena katika kiwiliwili cha mwanafunzi wake. Pindi mtu anapofungwa ndani ya kuta za gereza, Kristo anajaza upendo wake moyoni mwa mtu huyo. Mtu anapoteswa hadi kufa kwa ajili ya Kristo, Kristo husema, Mimi ni yeye "aliye hai; nami nalikuwa nimekufa, na tazama, ni hai hata milele na milele. Nami ninazo funguo za mauti, na za kuzimu." Ufunuo 1:18. Maisha yanayotolewa kafara kwa ajili yangu yamehifadhiwa hadi katika utukufu wa milele.

Wakati wowote na mahali popote, katika huzuni zote na mateso yote, wakati mwonekano unapoonekana kuwa giza na nyakati za usoni kutatanisha, nasi tunapojisikia tusio na msaada na wapweke, Mfariji atatumwa kama jibu la ombi la **(670)** imani. Hali halisi inaweza kututenga mbali na kila rafiki wa duniani; lakini hakuna hali, hakuna umbali, vinavyoweza kututenga na Mfariji wa kimbingu. Popote tulipo, popote tuwezapo kwenda, daima yuko upande wetu wa kuume ili kutusaidia, kutuwezesha, kutushikilia, na kutufurahisha.

Bado wanafunzi walishindwa kuelewa maneno ya Kristo katika uhalisia wake wa kiroho, naye akafafanua tena maana yake. Alisema, angejidhihirisha kwao kwa Roho. "Lakini huyo Msaidizi, huyo Roho Mtakatifu, ambaye Baba atampeleka kwa jina langu, atawafundisha yote." Hamtaweza tena kusema kwamba, Hatuwezi kuelewa. Hamtaweza tena kuona kupitia katika kioo cha giza-giza. Mtaweza "kufahamu pamoja na watakatifu wote jinsi ulivyo upana, na urefu, na kimo, na kina; na kuujua upendo wake Kristo, upitao ufahamu kwa jinsi ulivyo mwingi, mpate kutimilika kwa utimilifu wote wa Mungu." Waefeso 3:18, 19.

Wanafunzi wale walikuwa wabebe ushuhuda wa maisha na kazi za Yesu. Kupitia neno lao angesema na watu wote walio kwenye uso wa dunia. Lakini katika mateso na kifo cha Yesu wangesumbuliwa na jaribu kuu na mfadhaiko mkuu. Ili baada ya uzoefu huu neno lao liwe lenye usahihi, Yesu aliahidi kwamba "atawafundisha yote, na kuwakumbusha yote niliyowaambia."

Aliendelea kwamba, "Hata bado nikali ninayo mengi ya kuwaambia, lakini hamwezi kuyastahimili hivi sasa. Lakini yeye atakapokuja, huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote; kwa maana hatanena kwa shauri lake mwenyewe, lakini yote atakayoyasikia atayanena, na mambo yajayo atawapasha habari yake. Yeye atanitukuza mimi, kwa kuwa atatwaa katika yaliyo yangu na kuwapasha habari." Yesu alikuwa amewafunulia wanafunzi wake njia pana ya ukweli. Lakini ilikuwa vigumu sana kwao kuhifadhi masomo yake kwa usahihi wake mbali na hali ya kuingiliwa na mafundisho ya mapokeo na kanuni za waandishi na Mafarisayo. Walikuwa wamefundishwa kuyapokea mafundisho ya marabi kama ndiyo sauti ya Mungu, na hili lilikuwa bado lina nguvu katika akili zao, na liliathiri mwelekeo wa mwenendo wao. Mawazo ya kidunia, vitu vya ulimwengu huu, bado vilikuwa na nafasi kubwa katika mawazo yao. Hawakuelewa hali ya kiroho ya ufalme wa Kristo, ingawa alikuwa amewaeleza mara kwa mara. Mawazo yao yalikuwa yamechanganyikiwa. Hawakupambanukiwa na thamani ya maandiko ambayo Kristo alifundisha. Mengi ya mafundisho yalionekana karibu ya kupotea kwao. Kristo aliona kwamba hawakushikilia maana halisi ya maneno yake. Kwa huruma aliahidi kwamba Roho Mtakatifu atawakumbusha maneno haya katika akili yao. Na alikuwa ameacha kusema mambo mengi ambayo yasingeeleweka kwa wanafunzi. Haya nayo pia wangefunuliliwa na Roho Mtakatifu. Roho angeharakisha **(671)** uelewa wao, ili kwamba wapate kugundua mambo ya mbinguni. Yesu alisema, "Lakini yeye atakapokuja, huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote."

Mfariji huyo anaitwa "Roho wa kweli." Kazi yake ni kubainisha na kuhifadhi ukweli. Kwanza Yeye hukaa moyoni akiwa kama Roho wa kweli, na kwa njia hiyo huwa Mfariji. Kuna faraja na amani katika ukweli, lakini hakuna

amani ya kweli wala faraja ya kweli inayoweza kupatikana katika uongo. Shetani hupata nguvu dhidi ya akili za watu katika nadharia za uongo na mapokeo ya uongo. Kwa kuwaelekeza watu katika viwango vya uongo, anabadilisha na kuharibu tabia. Kupitia Maandiko Roho Mtakatifu ananena na akili ya mtu, na kuuweka ukweli moyoni. Kwa njia hiyo analiweka wazi kosa, na kulifukuza kutoka moyoni. Kristo anawatiisha watu wake kwa njia ya Roho wa ukweli, atendaye kazi kwa kutumia neno la Mungu.

Katika kule kuwaelezea wanafunzi wake kazi ya Roho Mtakatifu, Kristo alitaka kuwajaza furaha na tumaini vilivyoujaza moyo wake mwenyewe. Alifurahia kwa sababu ya msaada mkubwa aliokuwa amelipatia kanisa. Roho Mtakatifu alikuwa ndiye zawadi kubwa kuliko zote ambazo angeweza kuzipata kutoka kwa Baba yake kwa ajili ya kuwatukuza watu wake. Roho angetolewa kama chanzo cha kutia nguvu, na bila huyu kafara ya Kristo isingekuwa na kazi kwa watu. Nguvu ya uovu imekuwa ikijiimarisha kwa kare nyingi, na kujisalimisha kwa watu katika utumwa huu wa kishetani kulikuwa kwa hali ya kushangaza. Dhambi ingeweza kupingwa na kushindwa kwa uwezo pekee wa Nafsi ya Tatu ya Uungu, ambaye asingekuja na nguvu iliyorekebishwa, bali katika utimilifu wa uweza wa uungu. Roho ndiye anayekifanya kile kilicholetwa na Mkombozi wa ulimwengu kipate kufanya kazi. Moyo hufanywa upya na Roho. Kupitia Roho mtu aaminiye anakuwa mshirika wa hali ya uungu. Kristo alikuwa amemtoa Roho wake kama nguvu ya kimbingu ili kushinda mienendo yote ya kurithi na kufundishwa ya uovu, na kuingiza tabia yake kwa kanisa.

Kuhusu Roho Yesu alisema, "Yeye atanitukuza mimi." Mwokozi alikuja kumtukuza Baba kwa kuonyesha pendo lake; hivyo ndivyo ambavyo Roho angemtukuza Kristo kwa kufunua neema yake kwa ulimwengu. Sura ile ile ya Mungu inapaswa kuonyeshwa tena ndani ya wanadamu. Heshima kwa Mungu, heshima kwa Kristo, inajumuishwa katika kuzikamilisha tabia za watu wake.

"Naye [Roho wa ukweli] akiisha kuja, huyo atauhakikisha ulimwengu kwa habari ya dhambi, na haki, na hukumu." Kulihubiri neno hakutakuwa na kazi kama hakutakuwa na uwepo wa wakati wote wa Roho Mtakatifu. Huyu ndiye mwalimu mwezeshaji pekee wa ukweli wa kimbingu. Pale tu **(672)** ukweli unapoenda moyoni ukiambatana na Roho ndipo unapohimiza dhamira au kubadilisha maisha. Mtu anaweza kuwasilisha herufi za neno la Mungu vizuri, anaweza kuwa mtu anayejua amri zake zote na ahadi zake; lakini ikiwa Roho Mtakatifu haufikishi ukweli mahali pake nyumbani, hakuna nafsi itakayoanguka juu ya Mwamba na kuvunjika. Hakuna kiwango cha elimu, hakuna kujaliwa, hata kuwe kukubwa kiasi gani, kunakoweza kumfanya mtu kuwa mfereji wa nuru bila kushirikiana na Roho wa Mungu. Kuipanda mbegu ya injili hakuwezi kufanikiwa isipokuwa mbegu imehimizwa katika uhai kwa umande wa mbinguni. Kabla hata ya kitabu kimoja cha Agano Jipya kuandikwa, kabla hata ya hubiri moja kutolewa baada ya Kristo kupaa, Roho Mtakatifu aliwajilia wale mitume waliokuwa wakiomba. Hapo ndipo ushuhuda wa adui zao ulipokuwa huu, "Mmeijaza Yerusalemu mafundisho yenu." Matendo 5:28.

Kristo ameahidi zawadi ya Roho Mtakatifu kwa kanisa lake, na ahadi hiyo ni yetu kama ilivyokuwa ya wanafunzi wale wa kwanza. Lakini kama ilivyo kwa kila ahadi nyingine, inatolewa kwa masharti. Wapo wengi wanaoamini na kuonyesha kudai ahadi hiyo ya Bwana; wanasema kuhusu Kristo na kuhusu Roho Mtakatifu, lakini hawapati manufaa yoyote. Hawasalimishi moyo ili waongozwe na kutawaliwa na nguvu za mbinguni. Hatuwezi kumtumia Roho Mtakatifu. Roho ndiye wa kututumia sisi. Kupitia Roho wake Mungu anafanya kazi ndani ya watu wake katika "kutaka kwenu na kutenda kwenu, kwa kulitimiza kusudi lake jema." Wafilipi 2:13. Lakini wengi hawatajisalimisha kwa hili. Wanataka kujiongoza wenyewe. Hii ndiyo sababu kwamba hawapokei zawadi ya mbinguni. Roho hutolewa kwa wale tu wanaomsubiri Mungu kwa unyenyekevu, wanaotegemea maongozi yake na neema yake. Nguvu za Mungu zinasubiri watu hao wazidai na kuzipokea. Baraka hii iliyoahidiwa, ikidaiwa kwa imani, inaleta baraka nyingine zote mahali pake katika mnyororo. Inatolewa kulingana na wingi wa utajiri wa neema ya Kristo, naye yu tayari kumpatia kila mtu sawasawa na uwezo wa kupokea wa mtu huyo.

Katika mazungumzo yake kwa wanafunzi, Yesu hakuashiria maombolezo yoyote kuhusu mateso yake na kifo chake. Jambo lake la mwisho alilowaachia lilikuwa ni lile la amani. Alisema, "Amani nawaachieni; amani yangu nawapa; niwapavyo mimi sivyo kama ulimwengu utoavyo. Msifadhaike mioyoni mwenu, wala msiwe na woga."

Kabla ya kuondoka katika chumba kile cha ghorofani, Mwokozi aliwaongoza wanafunzi wake kuimba wimbo wa sifa. Sauti yake ilisikika, si sauti kama ya aliaye kwa maombolezo, bali kama zauti za furaha ya Pasaka:

"Haleluya.

Enyi mataifa yote, msifuni Bwana,
Enyi watu wote, mhimidini.
Maana fadhili zake kwetu sisi ni kuu,
Na uaminifu wa Bwana ni wa milele." Psalm 117.

**(673)** Baada ya wimbo huo, waliondoka. Walipita katika mitaa yenye misongamano ya watu, wakipita na kutoka nje nje ya lango la mji kuelekea Mlima wa Mizeituni. Waliendelea pole pole, kila mmoja akiwa ametekwa na mawazo yake mwenyewe. Walipoanza kutelemka kuelekea penye mlima, Yesu alisema, kwa sauti ya huzuni ya kina, "Ninyi nyote mtachukizwa kwa ajili yangu usiku huu kwa kuwa imeandikwa, Nitampiga mchungaji, na kondoo wa kundi watatawanyika." Mathayo 26:31. Wanafunzi walisikiliza kwa huzuni na mshangao. Walikumbuka jinsi watu walivyokuwa wamechukizwa na kuondoka kule Kapernaumu wakati Yesu aliposema kwamba Yeye ni mkate wa uzima. Lakini hawa kumi na wawili hawakuwa wamejionyesha kwamba hawana imani. Petro, akiongea kwa niaba ya wenzake, alikuwa ametangaza utiifu wake kwa Kristo. Halafu Mwokozi alikuwa amesema kwamba, "Je! Mimi sikuwachagua ninyi Thenashara, na mmoja wenu ni shetani?" Yohana 6:70. Mle katika chumba cha ghorofani Yesu alisema kwamba mmoja wa wale kumi na wawili angemsaliti, na kwamba Petro angemkana. Lakini sasa maneno yake yanawajumuisha wote.

Sasa sauti ya Petro inasikika kwa nguvu ikipinga na kusema, "Wajapochukizwa wote kwa ajili yako, mimi sitachukizwa kamwe." Mle katika chumba cha juu alikuwa amesema hivi, "Mimi nitautoa uhai wangu kwa ajili yako." Yesu alikuwa amemwonya kwamba usiku ule ule angemkana Mwokozi wake. Sasa Kristo anarudia onyo lake: "Amin, amin, nakuambia, Jimbi hatawika hata wewe utakapokuwa umenikana mara tatu." Lakini Petro pekee "akazidi sana kusema, Ijaponipasa kufa nawe, hata hivyo sitakukana kamwe. Na wote wakasema vile vile." Marko 14:29, 30, 31. Katika kule kujiaminia binafsi waliikana kauli iliyokuwa inarudiwa ya Yeye ajuaye. Hawakuwa wamejiandaa kwa jaribio; wakati ambapo jaribu lingewazingira, wangeelewa udhaifu wao.

Wakati Petro aliposema angemfuata Bwana wake hata gerezani na katika kifo, alikuwa na maana hiyo, kila neno katika hayo; lakini hakujijua. Moyoni mwake kulikuwa kumefichwa chembechembe za uovu ambazo zingeibuliwa maishani kulingana na mazingira. Ikiwa asingewezeshwa kuzifahamu hizo, zingemsababishia maangamivu ya milele. Mwokozi aliona ndani yake hali ya kujipenda na kuwa na uhakika ambavyo vingeupita na kuushinda upendo wake kwa Kristo. Tabia isiyo na ustahimilivu, dhambi isiyofishwa, roho ya kutojali, hasira isiyo takatifu, kutochukua tahadhari katika kuingia majaribuni, vilikuwa vimeonyeshwa katika uzoefu wa maisha yake. Onyo la dhati la Kristo lilikuwa ni wito wa kujipeleleza moyo. Petro alihitaji kuacha kujiamini yeye binafsi, na kuwa na imani ya kina katika Kristo. Ikiwa angepokea onyo hilo kwa unyenyekevu, angemhakikishia Mchungaji wa kondoo kwamba angechunga kondoo wake. Alipotaka kuzama katika Bahari ya Galilaya, alilia akisema, "Bwana, niokoe." Mathayo 14:30. Hapo ndipo mkono wa Kristo uliponyoshwa **(674)** na kumshika mkono. Vivyo hivyo sasa, ikiwa angemlilia Yesu akisema, Niokoe kutokana na kujitumainia kwangu, angehifadhiwa. Lakini Petro alijisikia kwamba alikuwa amefanywa asijiamini, na aliona kitendo hicho kama ni ukatili. Alikuwa amechukizwa tayari, na akazidi kuwa wa kujitumainia binafsi.

Yesu anawatazama wanafunzi wake kwa huruma. Hawezi kuwaokoa na jaribu, lakini hawaachi bila faraja. Anawahakikishia kwamba angezivunja nguvu za kaburi, na kwamba upendo wake kwao usingekwisha. Anasema, "Baada ya kufufuka kwangu, nitawatangulia kwenda Galilaya." Mathayo 26:32. Kabla ya kumkana wana uhakika wa kusamehewa. Baada ya kifo chake na ufufuko, walijua kwamba walikuwa wamesamehewa, na walikuwa wapendwa moyoni mwa Kristo.

Yesu na wanafunzi wake walikuwa njiani kwenda Gethsemane, wakiwa sehemu ya chini ya Mlima wa Mizeituni, mahali pa kupumzikia ambapo mara kwa mara Yesu alipatembelea kwa ajili ya kuomba na kutafakari. Mwokozi alikuwa amewafafanulia wanafunzi wake kazi yake kwa ulimwengu, na uhusiano wa kiroho uliokuwepo kati yake na yule ambaye wangemtegemea. Sasa alieleza somo hilo kwa kielelezo. Mbalamwezi ilikuwa inatoa mwangaza wake, na kulionyesha shamba la mizabibu lililostawi. Akivuta usikivu wa wanafunzi kulielekea shamba lile, analitumia kama lugha ya mfano.

"Mimi ndimi mzabibu wa kweli," alisema. Badala ya kuchagua mtende ulio mzuri, mwerezi uliopanda na kuwa mrefu, au mwaloni ulio mgumu, Yesu anachukua mzabibu pamoja na vikonyo vyake vinavyoning'inia vikijisokota kwenye mti mwingine wa kuvitegemeza akijiwakilisha Yeye. Mitende, mierezi, na mialoni inasimama yenyewe

peke yake. Haihitaji kutegemezwa. Lakini mzabibu hujisokota kwenye ufito uliosimikwa ili kuutegemeza, na hukua ukipanda kuelekea mbinguni. Vivyo hivyo Kristo katika ubinadamu wake alikuwa **(675)** tegemezi kwa nguvu za mbinguni. Alisema, "Mimi siwezi kufanya neno mwenyewe." Yohana 5:30.

"Mimi ndimi mzabibu wa kweli." Wayahudi walikuwa wakati wote wanauchukulia mzabibu kama mmea wa fahari, na mfano wa kitu chenye nguvu sana, kizuri sana, na chenye kuzaa matunda. Israeli ilikuwa imewakilishwa kama mzabibu uliopandwa na Mungu katika Nchi ya Ahadi. Wayahudi walijenga tumaini lao la wakovu kwenye uhalisia wa mwunganiko wao na Israeli. Lakini Yesu anasema, Mimi ndimi mzabibu halisi. Msidhani kwamba kwa kule kuwa na mwunganiko na Israeli mnaweza kuwa washirika wa maisha ya Mungu, na warithi wa ahadi zake. Maisha ya kiroho yanapatikana kupitia mimi tu.

"Mimi ndimi mzabibu wa kweli, na Baba yangu ndiye mkulima." Katika vilima vya Palestina Baba yetu wa mbinguni alikuwa ameupanda huu Mzabibu mzuri, na Yeye mwenyewe ndiye alikuwa mkulima. Watu wengi walivutiwa na uzuri wa Mzabibu huu, na walitangaza kwamba una asili ya mbinguni. Lakini kwa viongozi wa Israeli ulionekana kama mzizi katika nchi kavu. Waliuchukua ule mmea, wakauchubua, na kuukanya-kanyaka chini ya miguu yao isiyo na utakatifu. Mawazo yao yalikuwa ni kuuharibu milele. Lakini Mkulima wa mbinguni hakukoma kuutazama mmea wake. Baada ya watu kudhani kwamba wameuua, aliuchukua na kuupanda tena upande wa pili wa ukuta. Shina la mzabibu huo lisingeonekana tena. Lilifichwa mbali na ghasia za ufidhuli za wanadamu. Lakini matawi ya Mzabibu huo yalining'inia mpaka juu ya ukuta ule. Hayo yalikuwa yauwakilishe Mzabibu. Kupitia hayo matawi mengine yasiyo kwenye mzibibu huo bado yangeoteshwa kwenye Mzabibu huu kwa kufungamanishwa na kuunganishwa. Kutokana na matawi hayo matunda yamepatikana. Kumekuwa na mazao ambayo yanachumwa na wapita-njia.

"Mimi ni mzabibu; ninyi ni matawi," Kristo aliwaambia wanafunzi wake. Ingawa alikuwa anakaribia kuondolewa kutoka kwao, mwunganiko wa kiroho kati yake na wao ungekuwa usiobadilika. Yeye aliwaambia kwamba, Mwunganiko uliopo kati ya tawi na mzabibu huwakilisha mahusiano mnayotakiwa kuendeleza na mimi. Kile kitawishina kinapandikizwa kwenye mzabibu ulio hai, nacho hukua kwenye shina la mzabibu kikishikana nao nyuzinyuzi kwa nyuzinyuzi, vishipajani kwa vishipajani. Ule uhai wa mzabibu unakuwa ndio uhai wa tawi lile. Vivyo hivyo nafsi iliyokufa katika makosa na dhambi hupokea uhai kupitia mwunganiko wake na Kristo. Mwunganiko unafanywa kwa imani ya mtu ndani ya Kristo kama Mwokozi wake binafsi. Udhaifu wa mwenye dhambi huunganishwa na nguvu za Kristo, hali yake ya kuwa mtupu huunganishwa na ile hali ya ujazo ya Kristo, unyonge wake huunganishwa na uweza udumuo wa Kristo. Hapo anapata mawazo ya Kristo. Ubinadamu wa Kristo umegusa ubinadamu wetu, na ubinadamu wetu umegusa uungu. Hivyo kwa nguvu ya Roho Mtakatifu mwanadamu anakuwa mshirika wa hali ya uungu. Anapokelewa ndani ya yeye aliye Mpendwa.

**(676)** Mwungano huu na Kristo, pindi unapofanyika, lazima udumishwe. Kristo alisema, "Kaeni ndani yangu, nami ndani yenu. Kama vile tawi lisivyoweza kuzaa peke yake, lisipokaa ndani ya mzabibu; kadhalika nanyi, msipokaa ndani yangu." Huu si mguso wa juu tu, si mwunganiko wa kukatika-katika. Lile tawi lililounganishwa hugeuka na kuwa sehemu ya mzabibu ule. Mawasiliano katika hali ya uhai, nguvu, na uzaaji wa matunda kati ya mzizi na matawi ni ya wakati wote na yasiyozuiwa. Likishakutenganishwa na mzabibu, tawi haliwezi kuishi. Yesu naye alisema, Hamwezi kuendelea kuwa hai mkiwa kando yangu. Uzima ambao mmeupata kwangu unaweza kudumishwa kwa kuwa na ushirika wa kudumu pamoja nami. Pasipo mimi hamwezi kushinda hata dhambi moja, au kupingana na jaribu hata moja.

"Kaeni ndani yangu, nami ndani yenu." Maana ya kukaa ndani ya Kristo ni kuendelea kupokea kutoka kwa Roho wake, maisha ya kujisalimisha kwa utumishi wake kikamilifu bila kuacha sehemu. Lazima njia ya mawasiliano kati ya mtu na Mungu wake iwe wazi wakati wote. Kama vile tawi la mzabibu linavyodumu kufyonza maji ya madini kutoka kwa mzabibu ulio hai, ndivyo sisi tunavyopaswa kumng'ang'ania Yesu, na kupokea kutoka kwake nguvu na ukamilifu wa tabia kwa njia ya imani.

Mzizi hupeleka lishe yake kupitia kwa matawi mpaka kwenye tawi dogo la juu kabisa. Ndivyo Kristo anavyopitisha mkondo wa nguvu za kiroho kwenda kwa kila aaminiye. Kwa muda ambao nafsi inakuwa imeunganishwa na Kristo, hakuna shaka kwamba itapatwa na hatari ya kunyauka au kuoza.

Uhai wa mzabibu utadhihirika katika kupamba kwa matunda kwenye matawi. Yesu alisema, "Akaaye ndani yangu nami ndani yake, huyo huzaa sana; maana pasipo mimi ninyi hamwezi kufanya neno lolote." Tunapoishi kwa imani kwa Mwana wa Mungu, matunda ya Roho yataonekana maishani mwetu; hakuna hata mmoja atakayeyakosa.

"Baba yangu ndiye mkulima. Kila tawi ndani yangu lisilozaa huliondoa." Wakati kitawishina kinapounganishwa na mzabibu kwa nje, kunaweza kusiwe na mwunganiko halisi. Hapo kutakuwa hakuna kukua wala kuzaa. Kwa mtu huyo kunaweza kukawa na hali inayoonekana kama mwunganiko na Kristo pasipo mwungano halisi wa imani. Kuikiri imani huwaweka watu kanisani, lakini tabia na mwenendo ndivyo vinavyoonyesha kama wameunganishwa kweli na Kristo. Ikiwa hawazai matunda, hao ni matawi ya uongo. Kutengana kwao na Kristo kunajumuisha maangamivu ambayo ni kamili kama ilivyowakilishwa na tawi lililokufa. Kristo alisema, "Mtu asipokaa ndani yangu, hutupwa nje kama tawi na kunyauka; watu huyakusanya na kuyatupa motoni yakateketea."

"Na kila tawi lizaalo hulisafisha (hulipogolea), ili lizidi kuzaa." Miongoni mwa wale kumi na wawili waliokuwa wamemfuata **(677)** Yesu, mmoja wao aliyekuwa kama tawi lililonyauka alikuwa anakaribia kuondolewa; waliobaki wangepitishwa chini ya upanga unaopogolea wa jaribu lenye uchungu. Kwa huruma ya upendo Yesu alifafanua makusudi ya mkulima. Kule kupogoa kutasababisha maumivu, lakini anayepiga upanga ni Baba. Hafanyi kazi kwa mkono wenye hasira ya kuharibu wala moyo usio wa kupenda. Kuna matawi ambayo yanaranda-randa ardhini; haya lazima yalegezwe kutoka kwenye ardhi na kufungwa kwenye fito. Yanapaswa yakue kuelekea juu mbinguni, na kupata utegemezi wake ndani ya Mungu. Lazima yale majani yaliyozidi yanayofyonza na kuondosha mkondo wa uzima ambao ungesalia katika matunda yapunguzwe na kuondolewa. Yanayokua zaidi kuliko inavyotakiwa lazima yakatwe, ili kutoa nafasi ya kupitisha miale iponyayo ya Jua la Haki. Mkulima huondoa mimea yenye athari, ili ya kwamba matunda yawe bora na ya kutosha.

Yesu alisema, "Hivyo hutukuzwa Baba yangu, kwa vile mzaavyo sana." Mungu anatamani kupitia kwenu kudhihirisha utakatifu, ukarimu, huruma, ambavyo ni tabia yake. Lakini Mwokozi hawafanyi wanafunzi wake kujishughulisha ili kuzaa matunda. Yeye anawaambia wakae ndani yake. Anasema, "Ninyi mkikaa ndani yangu, na maneno yangu yakikaa ndani yenu, ombeni mtakalo lote nanyi mtatendewa." Kristo anakaa ndani ya wafuasi wake kwa njia ya neno. Hii ni sawa na ule mwunganiko muhimu unaowakilishwa na kuula mwili wake na kuinywa damu yake. Maneno ya Kristo ni roho na uzima. Ukiyapokea unapokea uzima wa Mzabibu. Unaishi "kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu." Mathayo 4:4. Uzima wa Kristo ulio ndani yenu huzaa matunda kama yale yale anayozaa Yeye. Kuishi katika Kristo, kumtii Kristo, kutegemezwa na Kristo, kufyonza viini-lishe kutoka kwa Kristo, kunasababisha kuzaa matunda yanayofanana na Kristo.

Katika mkutano wake huu wa mwisho na wanafunzi wake, hamu kubwa ya Kristo kwa wanafunzi wake ilikuwa ni kwmba wapendane kama Yeye alivyowapenda. Alisema kuhusu hili tena na tena. Alisema kwa kurudia-rudia kwamba, "Haya nawaamuru ninyi, mpate kupendana." Amri yake ya kwanza kabisa alipokuwa nao peke yao katika kile chumba cha ghorofani ilikuwa ni, "Amri mpya nawapa, Mpendane. Kama vile nilivyowapenda ninyi, nanyi mpendane vivyo hivyo." Amri hii ilikuwa mpya kwa wanafunzi wale; maana hawakuwa wamependana kama Kristo alivyokuwa amewapenda. Aliona kwamba lazima mawazo mapya na mivuto mipya itawatawala; kwamba lazima watatekeleza kanuni nyingine zilizo tofauti na hiyo; kupitia maisha na kifo chake walikuwa wapokee dhana mpya ya upendo. Amri ya kupendana ilikuwa na maana mpya katika kafara yake aliyojitoa. Kazi **(678)** yote ya neema ni mwendelezo mmoja wa utumishi wa upendo, wa kujikana, na wa jitihada ya kujitoa kafara. Katika kila saa ya maisha ya Kristo katika dunia hii ya ugenini, upendo wa Mungu ulikuwa unatiririka kutoka kwake katika vijito visivyozibika. Wote wanaojazwa Roho wake watapenda kama alivyopenda. Kanuni ile ile iliyomhimiza Kristo itawahimiza katika kushughulika kwao kote miongoni mwa wao kwa wao.

Upendo huu ndio ushahidi wa uanafunzi wao. Yesu alisema, "Hivyo watu wote watatambua ya kuwa ninyi mmekuwa wanafunzi wangu, mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi." Watu wanapofungwa pamoja, pasipo kulazimishwa wala kutafuta manufaa binafsi, bali kwa upendo, wanaonyesha utendaji wa ushawishi ambao uko juu kuliko ushawishi wowote wa kibinadamu. Mahali panapokuwa na umoja huu, kuna ushahidi kwamba sura ya Mungu inarejeshwa katika uanadamu, kwamba kanuni mpya ya maisha imepandikizwa. Panaonyesha kwamba

pana nguvu ya hali ya uungu inayoweza kuzistahimili nguvu zisizo za kibinadamu za uovu, na ya kwamba neema ya Mungu inatiisha ubinafsi ulio ndani ya moyo wa asili.

Upendo huu, ukidhihirishwa kanisani, hakika utachochea ghadhabu ya Shetani. Kristo hakuwawekea wanafunzi wake njia rahisi. Alisema, "Iwapo ulimwengu ukiwachukia, mwajua ya kuwa umenichukia mimi kabla ya kuwachukia ninyi. Kama mngekuwa wa ulimwengu, ulimwengu ungewapenda walio wake; lakini kwa kuwa ninyi si wa ulimwengu, bali mimi naliwachagua katika ulimwengu, kwa sababu hiyo ulimwengu huwachukia. Likumbukeni lile neno nililowaambia, Mtumwa si mkubwa kuliko bwana wake. Ikiwa waliniudhi mimi, watawaudhi ninyi; ikiwa walilishika neno langu watalishika na lenu. Lakini haya yote watawatenda kwa ajili ya jina langu, kwa kuwa hawamjui yeye aliyenipeleka." Injili inapelekwa mbele kwa vita vikali, katikati ya upinzani, hatari, na mateso. Lakini wale wanaofanya kazi hii wanafuata tu nyayo za Bwana wao.

Kama Mkombozi wa ulimwengu, Kristo alikuwa wakati wote anakabiliwa na hali iliyoonekana kama ni kushindwa. Yeye, aliye mjumbe wa huruma kwa ulimwengu wetu, alionekana kufanya kidogo katika kazi aliyotaka kufanya katika kuinua na kuokoa. Nguvu za kishetani zilikuwa kazini wakati wote zikiipinga njia yake. Lakini hakukatishwa tamaa. Kupitia unabii wa Isaya alitangaza, "Nimejitaabisha bure, nimetumia nguvu zangu bure bila faida; lakini hakika hukumu yangu ina Bwana, na thawabu yangu ina Mungu wangu." Ahadi hii inatolewa kwa Kristo kwamba, "Bwana, mkombozi wa Israeli, Mtakatifu wake, amwambia hivi yeye anayedharauliwa na wanadamu; yeye anayechukiwa na **(679)** taifa hili; . . . Bwana asema hivi: . . . Nitakuhifadhi, nitakutoa uwe agano la watu hawa, ili kuiinua nchi hii, na kuwarithisha urithi uliokuwa ukiwa; kuwaambia waliofungwa, Haya, tokeni; na hao walio katika giza, Jionyesheni. . . . Hawataona njaa, wala hawataona kiu; hari haitawapiga, wala jua; kwa maana yeye aliyewarehemu atawatangulia, naam, karibu na chemchemi za maji atawaongoza." Isaya 49:4, 5, 7-10.

Yesu alishikilia neno hili, naye hakumpatia Shetani nafasi. Wakati hatua za mwisho za mateso ya Yesu zilipokuwa zinakaribia, wakati huzuni ya kina ilipokuwa imeifunika nafsi yake, aliwaambia wanafunzi wake, "Yuaja mkuu wa ulimwengu huu, wala hana kitu kwangu." "Mkuu wa ulimwengu huu amekwisha kuhukumiwa." Sasa atatupwa nje. Yohana 14:30; 16:11; 12:31. Kwa kutumia jicho la kinabii Kristo alifuatilia matukio ambayo yangetokea mnamo wakati wa pambano lake la mwisho. Alijua kwamba wakati atakapolia akisema, "Imekwisha," mbingu yote ingeshangilia ushindi. Masikio yake yalinasa kwa mbali muziki na sauti za shangwe za ushindi zilizokuwa katika viwanja vya mbinguni. Alijua kwamba kengere ya mwisho ya utawala wa Shetani ingelia, na jina la Kristo lingetukuzwa kutoka ulimwengu hadi ulimwengu katika malimwengu yote.

Kristo alifurahia kwamba angewafanyia wafuasi wake mambo mengi zaidi ya vile ambavyo wangeomba au kudhani. Alinena kwa uhakika, akijua kwamba tamko lenye uweza lilishatolewa kabla ya ulimwengu kuumbwa. Alijua kwamba ukweli, ukiwa na silaha ya nguvu isiyo na kikomo ya Roho Mtakatifu, ungeshinda katika vita dhidi ya uovu; na kwamba bendera yenye michirizi ya damu ingepepea kwa ushindi juu ya wafuasi wake. Alijua kwamba maisha ya wanafunzi wake wenye matumaini yangekuwa kama yake, yakiwa mfululizo wa ushindi usiopingwa, hapa ukiwa hauonekani kuwa hivyo, lakini ukigundulika kuwa hivyo baada ya wakati huu.

Alisema, "Hayo nimewaambieni mpate kuwa na amani ndani yangu. Ulimwenguni mnayo dhiki; lakini jipeni moyo; mimi nimeushinda ulimwengu." Kristo hakushindwa, wala hakukata tamaa, na wanafunzi wake wanatakiwa kudhihirisha imani ya hali kama hiyo hiyo. Wanatakiwa kuishi vile alivyoishi, na kufanya kazi vile alivyofanya kazi, maana wanamtegemea Yeye kama Kiongozi wa Kazi mkuu. Lazima wawe na ujasiri, nguvu na ustahimilivu. Ingawa vitu vinavyoonekana kama kutowezekana vinazuia njia yao, kwa neema yake wanatakiwa kusonga mbele. Badala ya kuhofia mambo magumu, wanaalikwa kushinda juu ya yote hayo. Hawapaswi kukatishwa tamaa na chochote, na wanapaswa wawe na tumaini kwa kila kitu. Kwa kutumia mnyororo wa dhahabu wa upendo wake usiolinganishwa na kitu, Kristo amewafunga akiwaunganisha na kiti cha enzi cha Mungu. Kusudi lake ni kwamba ushawishi wa juu kabisa katika malimwengu, unaochimbuka kutoka katika chanzo cha nguvu zote, uwe wao. Wanatakiwa kuwa na nguvu **(680)** ya kuupinga uovu, nguvu ile ambayo haiwezi kuhimiliwa na dunia, wala kuzimu, nguvu itakayowawezesha kushinda kama Kristo alivyoshinda.

Kristo anataka kwamba mpango wa mbinguni, mpangilio wa serikali ya mbinguni, upatanifu wa kiungu wa mbinguni, uwakilishwe katika kanisa lake duniani. Kwa njia hiyo anatukuzwa ndani ya watu. Kupitia kwao Jua la Haki litaangaza kwa ulimwengu. Kristo amelipatia kanisa vitu vya kutosha, ili kwamba apokee mapato mengi ya

utukufu kutoka kwa watu wake waliokombolewa, mali yake iliyonunuliwa. Amewekeza kwa watu wake uwezo na baraka ili kwamba wawakilishe wingi wake wa vitu. Kanisa, likiwa limejaliwa haki ya Kristo, ndilo hazina yake, ambamo utajiri wa huruma yake, neema yake, na upendo wake, vinapaswa kuonekana kwa utimilifu na mwonekano wa kiwango cha juu mno. Kristo anawatazama watu wake katika usafi na ukamilifu wao, wakiwa kama zawadi ya mateso yake, na matokeo ya ombi la dhati la utukufu wake, - Kristo, Kitovu kikuu, ambaye kutoka kwake utukufu wote hutokea na kutawanyika.

Kwa maneno mazito na ya tumaini Mwokozi alimaliza mafundisho yake. Halafu aliubwaga mzigo mzito wa nafsi yake kwa sala ya kuwaombea wanafunzi wake. Akiwa ameinua macho yake mbinguni, alisema, "Baba, saa imekwisha kufika. Mtukuze Mwanao, ili Mwana wako naye akutukuze wewe; kama vile ulivyompa mamlaka juu ya wote wenye mwili, ili kwamba wote uliompa awape uzima wa milele. Na uzima wa milele ndio huu, Wakujue wewe, Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma."

Kristo alikuwa ameimaliza kazi aliyopewa kufanya. Alikuwa amemtukuza Mungu duniani. Alikuwa amelidhihirisha jina la Baba. Alikuwa amekusanya watu wale ambao wangeendelea na kazi yake miongoni mwa wanadamu. Na alisema, "Nami nimetukuzwa ndani yao. Wala mimi simo tena ulimwenguni, lakini hawa wamo ulimwenguni, nami naja kwako. Baba mtakatifu, kwa jina lako ulilonipa uwalinde hawa, ili wawe na umoja kama sisi tulivyo." "Wala si hao tu ninaowaombea; lakini na wale watakaoniamini kwa sababu ya neno lao. Wote wawe na umoja; . . . Mimi ndani yao, nawe ndani yangu, ili wawe wamekamilika katika umoja; ili ulimwengu ujue ya kuwa ndiwe uliyenituma, ukawapenda wao kama ulivyonipenda mimi."

Kwa namna hiyo, katika lugha ya mwenye mamlaka ya kimbingu, Kristo analiweka kanisa aliloteua mikononi mwa Baba. Akiwa kama kuhani mkuu aliyewekwa wakfu anawaombea watu wake. Akiwa kama mchungangaji mwaminifu anawakusanya kondoo wake chini ya kivuli chake Mwenyezi, mahali pa kimbilio la uhakika na lenye nguvu. Kinachomsubiri sasa ni pambano la mwisho dhidi ya Shetani, naye anaondoka kwenda kukabiliana nalo.

# Sura ya 74

## Gethsemane

[Sura hii imejengwa katika Mathayo 26:36-56; Marko 14:32-50; Luka 22:39-53; Yohana 18:1-12.]

Akiwa pamoja na wanafunzi wake, Mwokozi alipita taratibu kuelekea katika bustani ya Gethsemane. Mbalamwezi ya msimu wa Pasaka, mbalamwezi kubwa na iliyojaa, ilimlika kupitia katika anga lisilo na mawingu. Mji ule wenye mahema ya mahujaji ulikuwa uko kimya.

Yesu alikuwa amezungumza sana na wanafunzi wake na kuwafundisha; lakini alipokaribia Gethsemane, alikuwa na ukimya usio wa kawaida. Mara kwa mara alikuwa amekuja mahali hapa kwa ajili ya kupata utulivu na kuomba; lakini hakuwa na moyo uliojaa huzuni kama huu wa usiku wake wa mateso ya mwisho. Katika maisha yake yote ya duniani alitembea katika uwepo wa Mungu. Alipokuwa katika kukabiliana na watu waliopagawa na roho wa Shetani, alisema kwamba, "Naye aliyenipeleka yu pamoja nami, hakuniacha peke yangu; kwa sababu nafanya siku zote yale yampendezayo." Yohana 8:29. Lakini sasa alionekana kama amefungiwa mbali na nuru ya uwepo wa Mungu iwezeshayo. Sasa alihesabiwa pamoja na waharifu. Lazima abebe hatia ya wanadamu walioanguka. Lazima uovu wetu sote utwishwe juu yake Yeye asiyejua dhambi. Dhambi inaonekana ya kutisha sana kwake, uzito wa hatia ambao lazima aubebe ni mkubwa sana, kiasi kwamba anajaribiwa kuogopa kwamba utamfungia mbali na upendo wa Baba yake milele. Akisikia jinsi hasira ya Mungu dhidi ya uasi ilivyo ya kutisha, alilia akisema, "Roho yangu ina huzuni nyingi kiasi cha kufa."

Walipokaribia bustanini, wanafunzi wake walikuwa wamegundua badiliko lililomjia Bwana wao. Kamwe hawakuwahi kumwona akiwa na **(686)** ukimya kiasi kile. Kadiri alivyoendelea, hali hii mpya ya ukimya ilizidi kuwa kubwa; lakini hawakudiriki kumwuliza sababu ya hali ile. Mwili wake uliwayawaya kama vile alikuwa karibu na kuanguka. Walipofika bustanini, wanafunzi walimtafutia mahali pake pa kawaida pa kupumzika, ili kwamba Bwana wao apate kupumzika. Kila hatua ambayo alipiga sasa ilihitaji nguvu nyingi. Aligumia kwa sauti kubwa, kama mtu aliyekuwa anaumia sana kwa sababu ya uzito wa mzigo wa kutisha. Wenzake walimsaidia mara mbili, la sivyo angeanguka chini.

Karibu na mahali pa kuingilia bustanini, Yesu aliwaacha wanafunzi pale isipokuwa watatu, akiwataka wajiombee na kumwombea na Yeye. Aliingia katika faragha za bustani ile akiwa pamoja na Petro, Yakobo na Yohana. Hawa watatu walikuwa watu wa karibu sana wa Kristo. Walikuwa wameuona utukufu wake kwenye mlima alipobadilika sura; walikuwa wamemwona Musa na Eliya wakizungumza naye; walikuwa wameisikia sauti kutoka mbinguni; na sasa katika pambano lake kuu, Yesu alitaka wawe karibu yake. Mara nyingi walikuwa naye usiku mzima mahali hapa. Katika nyakati hizo, baada ya mida ya kukesha na kuomba, huwa wanalala pasipo usumbufu wakiwa mbali kidogo na Bwana wao, mpaka wakati alipokuwa anawaamsha asubuhi ili waingie katika kazi mpya. Lakini sasa alitaka watumie usiku wote wakiomba pamoja naye. Lakini hakudhani kwamba wangeweza hata kushuhudia shida ambayo angeipitia.

"Kaeni hapa, mkeshe pamoja nami," aliwaambia.

Alienda mbele kidogo kutoka mahali walipokuwa – si mbali sana bali mahali pa karibu ambapo wote walimwona na kumsikia – na kuanguka kifudifudi chini. Alihisi kwamba dhambi ilikuwa imemtenganisha na Baba yake. Pengo lililokuwa katikati lilikuwa pana sana, jeusi sana, lenye kina kirefu sana, kiasi kwamba roho yake ilitetemeshwa nalo. Asingeweza kutumia nguvu yake ya kiungu kukwepa maumivu haya. Lazima apate maumivu ya matokeo ya dhambi ya mwanadamu akiwa kama mwanadamu. Lazima akiwa kama mwanadamu ndipo akutane na ghadhabu ya Mungu dhidi ya uasi.

Yesu alikuwa amesimama katika kimo kilicho tofauti na pale alipowahi kusimama kabla. Mateso yake yanaweza kuelezwa kwa uzuri zaidi kwa kutumia maneno ya nabii, "Amka, Ee upanga, juu ya mchungaji wangu, na juu ya mtu aliye mwenzangu, asema Bwana wa majeshi." Zekaria 13:7. Akiwa kama mbadala na mdhamini wa mwanadamu mwenye dhambi, Kristo alikuwa anateseka chini ya haki ya kimbingu. Aliona maana ya haki. Mpaka wakati huu alikuwa amekuwa mpatanishi wa wengine; lakini sasa Yeye mwenyewe alitamani kuwa na mpatanishi.

Yesu alipohisi kuvunjika kwa mwungano wake na Baba, aliogopa kwamba katika hali ya ubinadamu asingeweza kustahimili pambano lililokuwa linakuja dhidi ya nguvu za giza. Katika jangwa la majaribu hatima ya jamii ya wanadamu ilikuwa hatarini. Kristo alikuwa mshindi. Sasa **(687)** mjaribu alikuwa amekuja kwa ajili ya pambano lake la mwisho la kuogofya. Alikuwa amejiandaa kwa pambano hili kwa miaka mitatu ya huduma ya Kristo. Kila kitu kwake mwovu kilikuwa kama kiko hatarini. Ikiwa angeshindwa hapa, tumaini lake la ukuu lingepotea; hatimaye falme za ulimwengu zingekuwa za Kristo; yeye angepinduliwa na kutupwa nje. Lakini ikiwa Kristo angeshindwa, dunia ingekuwa ufalme wa Shetani, na jamii ya wanadamu ingekuwa chini ya mamlaka yake milele. Akiwa na masuala hayo ya pambano mbele yake, nafsi ya Kristo ilijawa na utisho wa kutengwa na Mungu. Shetani alimwambia kwamba kama alikuwa amekuwa mdhamini wa ulimwengu wenye dhambi, ile hali ya kutenganishwa ingekuwa ya milele. Angekuwa na fungu lake katika ufalme wa Shetani, na kamwe asingekuwa na umoja na Mungu tena.

Na ni nini kingepatikana kwa kafara hii? Ni jinsi gani wanadamu wenye hatia na wasio na shukrani walivyoonekana wasio na tumaini! Shetani alileta mbele ya Mkombozi hali iliyo katika namna zilizo ngumu sana kwamba: Watu wanaodai kuwa walio juu ya wengine wote kwa mafanikio ya mali na hali njema ya kiroho wamekukataa. Wanatafuta kukuua, wewe uliye msingi, kitovu, na muhuri wa ahadi zilizotolewa kwao kama watu walioteuliwa. Mmoja wa wanafunzi wako mwenyewe, ambaye amesikiliza mafundisho yako, na ambaye amekuwa mbele sana katika shughuli za kanisa, atakusaliti. Mmojawapo wa wafuasi wako shupavu atakukana. Wote watakuacha. Hali yote ya Kristo ilisumbuliwa na wazo hilo. Kwamba wale ambao ameshughulika ili kuwaokoa, wale aliowapenda sana, wataungana katika njama za Shetani, hali hii iliuchoma moyo wake. Pambano lilikuwa la kutisha. Kipimo chake kilikuwa ni hatia ya taifa lake, ya washtaki wake na mwenye kumkana, hatia ya ulimwengu ulio katika uovu. Dhambi za wanadamu zilikuwa nzito sana juu ya Kristo, na hali ya kuijua ghadhabu ya Mungu dhidi ya dhambi vilikuwa vinayakandamiza maisha yake.

Mtazame anapotafakari kuhusu gharama ya kulipa kwa ajili ya nafsi ya mwanadamu. Katika masumbuko yake anaishikilia ardhi yenye baridi, kama vile kuzuia asisukumiwe mbali zaidi na Mungu. Umande unaoanguka usiku unashuka kwenye mwili ule uliolala kifudifudi, lakini hausikii. Sauti inatoka katika midomo yake iliyochoka ikisema, "Baba yangu, ikiwezekana, kikombe hiki kiniepuke." Hata hivyo anaongeza kwamba, "Walakini si kama nitakavyo mimi, bali kama utakavyo wewe."

Moyo wa mwanadamu huhitaji faraja wakati wa mateso. Kristo alihisi hitaji hili kwa vina virefu vya utu wake. Katika masumbuko yake haya ya hali ya juu alikuja kwa wanafunzi wake akiwa na hamu ya kusikia maneno ya faraja kutoka kwa wale ambao mara nyingi alikuwa amewabariki na kuwafariji, akaishia katika huzuni na maumivu. Yeye ambaye mara kwa mara alikuwa na maneno ya faraja kwao sasa alikuwa anateseka kwa maumivu yaliyo juu ya yale ya kibinadamu, naye alitamani kujua kwamba walikuwa wanamwombea na kujiombea wenyewe. **(688)** Ni jinsi gani ukubwa wa dhambi ulivyoonekana kuwa wa giza! Kuiacha jamii ya wanadamu ibebe matokeo ya hatia ya dhambi yake yenyewe lilikuwa ndilo jaribu la kutisha mno lililomjia, ili Yeye asimame mbele za Mungu bila hatia. Ikiwa lau angejua kwamba wanafunzi wake walielewa na kutambua hilo, angepata nguvu.

Akiinuka kwa jitihada za maumivu, alijivuta mpaka mahali pale alipowaacha wenzake. Lakini "akawakuta wamelala." Ikiwa angewakuta wanaomba, angepata ahueni. Ingekuwa kwamba walikuwa wanatafuta kimbilio kwa Mungu, ili kwamba nguvu za kishetani zisiwashinde, angefarijiwa na imani yao iliyo imara. Lakini hawakuwa wamelisikiliza onyo lililorudiwa-rudiwa kwamba, "Kesheni, mwombe." Mwanzoni walikuwa wamepata shida sana kumwona Bwana wao, ambaye mara nyingi alikuwa mpole na mwenye utukufu, akipambana na huzuni iliyozidi uwezo wa kutafakari. Walikuwa wameomba wakati waliposikia vilio vikubwa vya mtu atesekaye. Hawakutarajia kumwacha Bwana wao, lakini walionekana kupoozeshwa na hali ya kuwa na usingizi ambayo wangeweza kuifukuzia mbali ikiwa wangeendelea kumlilia Mungu. Hawakuwa wameonyesha umuhimu wa kukesha na kuomba kwa dhati ili kustahimili majaribu.

Muda mfupi tu kabla ya kuelekeza miguu yake kwenda bustanini, Yesu alikuwa amewaambia wanafunzi wake kwamba, "Mtakunguwazwa ninyi nyote kwa ajili yangu usiku huu." Walikuwa wamempatia hakikisho la nguvu kwamba wangeenda pamoja naye hata gerezani au hata katika kifo. Na maskini, Petro, mwenye kujitumainia, alikuwa ameongeza kwamba, "Hata wajapokunguwazwa wote, lakini siyo mimi." Marko 14:27, 29. Lakini wale

**(689)** walijitumainia wenyewe. Hawakumtazama Msaidizi mwenye nguvu kama ambavyo Kristo alikuwa amewashauri. Kwa hiyo wakati Mwokozi alipokuwa katika wakati wenyewe wa kuhitaji faraja na maombi yao, walikutwa wamesinzia. Hata Petro alikuwa amelala.

Na Yohana, yule mwanafunzi aliyependwa sana aliyekuwa ameegemea kifuani pa Yesu, alikuwa amelala. Kwa kweli, upendo wa Yohana kwa Bwana wake ulipaswa kumweka macho wakati wote. Maombi yake ya dhati yalitakiwa kuchanganyika na yale ya Mwokozi wake mpendwa katika wakati huu wa huzuni kubwa. Mkombozi huyu alikuwa ametumia mida ya usiku akiwaombea wanafunzi wake, ili kwamba imani yao isishindwe. Ikiwa sasa Yesu angemwuliza Yakobo na Yohana swali ambalo alipata kuwauliza kwamba, "Je! Mwaweza kunywea kikombe nitakachonywea mimi, na kubatizwa katika ubatizo nitakaobatizwa?" wasingediriki kujibu kwamba, "Twaweza." Mathayo 20:22.

Wale wanafunzi waliamshwa na sauti ya Yesu, lakini walimfahamu kwa shida, sura yake ilikuwa imebadilishwa sana na masumbuko. Akimwambia Petro, Yesu alisema, "Simoni, umelala? Hukuweza kukesha saa moja? Kesheni mwombe, msije mkaingia majaribuni, roho i radhi ila mwili ni dhaifu." Udhaifu wa wanafunzi wake uliamsha huruma ya Yesu. Alihofu kwamba wasingeweza kustahimili jaribio ambalo lingewajia wakati wa kusalitiwa kwake na wakati wa kifo chake. Hakuwakemea, lakini alisema, "Kesheni mwombe, msije mkaingia majaribuni." Hata katika maumivu yake makubwa, alikuwa bado anatafuta kusamehe madhaifu yao. Alisema, "Roho i radhi ila mwili ni dhaifu."

Kwa mara nyingine tena Mwana wa Mungu alizongwa na mahangaiko yapitayo yale ya kibinadamu, akiwa amenyong'onyea na kuzimia moyo, alijikokota tena na kurudi mahali pa pambano lake la kwanza. Mateso yake yalikuwa makubwa kuliko hata yale ya kwanza. Kadiri maumivu ya moyo yalivyozidi kwake, jasho lake likawa "kama matone ya damu yakidondoka nchini." Miti ya mivinje na mitende ilikuwa ndiyo mashahidi wa kimya wa masumbuko yake yale. Kutoka katika matawi yenye majani ya miti hii ulidondoka umande mzito kwenye mwili wake uliopigwa, kama vile hali ya asili ilikuwa inatoa machozi ikilia kwa ajili ya Mwumbaji wake aliyekuwa akipambana na nguvu za giza akiwa peke yake.

Muda mfupi kabla, Yesu alikuwa amesimama kama mti wa mwerezi wenye nguvu, akistahimili dhoruba ya upinzani iliyokuwa ikimkabili. Mielekeo yenye usumbufu, mioyo iliyojawa na uovu na kiburi, ilikuwa imejitahidi kumchanganya na kutaka kumshinda pasipo mafanikio. Alisimama imara kama katika hali ya uweza wa kimbingu akiwa Mwana wa Mungu. Sasa alikuwa kama mwanzi uliopigwa na kuinamishwa na dhoruba kali. Alikuwa amekaribia kukamilisha kazi yake kama mshindi, katika kila hatua akiwa amejipatia ushindi dhidi ya nguvu za giza. Akiwa kama **(690)** yeye ambaye ametukuzwa tayari, alikuwa amedai kuwa na umoja na Mungu. Kwa sauti ya ujasiri alikuwa ameziimba nyimbo zake za sifa. Alikuwa amewaambia wanafunzi wake kwa maneno ya kutia moyo na ya upendo. Sasa saa ya nguvu ya giza ilikuwa imekuja. Sasa sauti yake ilisikika katika anga tulivu la jioni, si katika sauti ya shangwe za ushindi, bali ikiwa imejawa na maumivu ya mwanadamu. Yale maneno ya Mwokozi yalisikiwa na masikio ya wanafunzi waliokuwa wanasinzia yakisema, "Baba yangu, ikiwa haiwezekani kikombe hiki kiniepuke nisipokunywa, mapenzi yako yatimizwe."

Mwitikio wa kwanza wa hisia wa wanafunzi ulikuwa ni kwenda kwake; lakini alikuwa amewataka wabaki pale, wakikesha na kuomba. Wakati Yesu alipokuja pale walipokuwa, alikuta wakiwa bado wamelala. Kwa mara nyingine tena alikuwa ametamani faraja ya kuwa pamoja nao, kwa maneno kadhaa ya wanafunzi wake ambayo yangempunguzia maumivu, na kuvunja giza lililokuwa limemzingira. Lakini macho yao yalikuwa mazito; "wala hawakujua la kumjibu." Uwepo wake uliwaamsha. Waliuona uso wake ukionyesha mwonekano wa jasho la damu kwa sababu ya masumbuko, na walijawa na hofu. Hawakuweza kuelewa yale maumivu yake ya akili. "Uso wake ulikuwa umeharibiwa sana zaidi ya mtu yeyote, na umbo lake zaidi ya wanadamu." Isaya 52:14.

Alipogeuka na kuondoka, Yesu alipatafuta pahali pake pale pa faragha, na kuanguka kifudifudi, akiwa amegubikwa na utisho wa giza kuu. Ubinadamu wa Mwana wa Mungu ulitetemeka katika saa ile ya kujaribiwa. Kwa sasa hakuomba kwa ajili ya wanafunzi wake kwamba imani yao isishindwe, bali kwa ajili ya nafsi yake mwenyewe iliyokuwa majaribuni na katika maumivu. Wakati mgumu ulikuwa umekuja – wakati ambao ungeiamua hatima ya ulimwengu. Hatima ya wanadamu ilikuwa inatetema kwenye mizani. Hata sasa Kristo angeweza kukataa kunywea kikombe kilicho halali ya mwanadamu mwenye hatia. Alikuwa bado hachachelewa. Angeweza kufuta jasho la damu kutoka usoni mwake, na kumwacha mwanadamu aangamie katika uovu wake.

Angeweza kusema hivi, Hebu mwenye kuasi apokee adhabu ya dhambi yake, nami nitarudi kwa Baba yangu. Je! Mwana wa Mungu atakinywea kikombe cha maumivu machungu? Je! Asiye na hatia atakabiliwa na matokeo ya laana ya dhambi, ili kumwokoa mwenye hatia? Maneno yenye mtetemo yanatoka katika midomo iliyokauka ya Yesu yakisema, "Baba yangu, ikiwa haiwezekani kikombe hiki kiniepuke nisipokunywa, mapenzi yako yatimizwe."

Alikuwa ametamka ombi hilo mara tatu. Kafara ile kuu ya mwisho ilikuwa imeutia hofu ubinadamu wake mara tatu. Lakini sasa historia ya jamii ya wanadamu inakuja mbele ya Mkombozi wa ulimwengu. Anaona kwamba waasi wa sheria, ikiwa wataachwa wenyewe, lazima waangamie. Anaona hali ya mwanadamu ya kutojiwezea lolote. Anaiona nguvu ya dhambi. Ole na vilio vya ulimwengu unaopotea vinainuka mbele yake. Anaona hatima **(693)** yake mbaya, na anafanya uamuzi wake. Anaamua kumwokoa mwanadamu kwa gharama yoyote juu yake. Anakubali ubatizo wake wa damu, ili ya kwamba kupitia kwake mamilioni wanaoangamia wapate uzima wa milele. Ameviacha viwanja vya mbinguni, mahali ambapo mambo yote ni safi, furaha, na utukufu, kuja kumwokoa kondoo mmoja aliyepotea, ulimwengu mmoja ulioanguka kwa kuasi. Na hataweza kugeukia mbali kutoka kwenye kusudi hilo. Atakuwa neema kwa jamii iliyochagua kutenda dhambi. Sasa ombi lake linaonyesha hali ya kujisalimisha anaposema: "Ikiwa haiwezekani kikombe hiki kiniepuke nisipokunywa, mapenzi yako yatimizwe."

Akishakufanya uamuzi huo, alianguka chini kama aliyekufa mahali pale ambapo kabla alikuwa kama ameinuka kidogo. Wakati huu wanafunzi wake walikuwa wapi, ili waiweke mikono yao ya upendo chini ya kichwa cha Bwana wao anayezimia ili kukitegemeza, na kuuosha ule uso, uliokuwa umeharibika kweli kweli kuliko wa wana wa wanadamu? Mwokozi alitembea kwenye shinikizo akiwa peke yake, na hakukuwa na mtu aliyekuwa pamoja naye.

Lakini Mungu aliteseka pamoja na Mwana wake. Malaika waliyatazama maumivu ya Mwokozi. Walimwona Bwana wao akiwa amezongwa na majeshi ya nguvu za kishetani, hali yake ikiwa imekandamizwa na utisho wa fumbo. Kulikuwa na ukimya mbinguni. Hakuna kinubi kilichoguswa. Laiti kama wenye mwili wa kufa wangeona mshangao wa majeshi ya malaika wakati yalipokuwa katika ukimya wa huzuni yakimtazama Baba alivyokuwa anaondoa miale yake ya nuru, upendo, na utukufu kutoka kwa Mwana wake mpendwa, wangeelewa vizuri zaidi jinsi dhambi ilivyo ya kuchukiza machoni pake.

Malimwengu ambayo hayakuanguka na malaika wa mbinguni walikuwa wametazama kwa hamu kubwa kadiri pambano lilivyoelekea mwisho. Shetani na nguvu zake zote za uovu, majeshi ya uasi, walilitazama kwa tashwishwi pambano hili la kazi ya ukombozi. Nguvu za wema na za uovu zilisubiri kuona kwamba ni jibu gani ambalo lingekuja kwa ajili ya ombi la mara ya tatu la Kristo lililokuwa lile lile likirudiwa-rudiwa. Malaika walikuwa wametafuta kuleta faraja kwa mwenye masumbuko huyu wa mbinguni, lakini hilo lisingekuwa hivyo. Hakukuwa na njia ya Mwana wa Mungu kupona. Katika pambano hili la kutisha, wakati ambapo kila kitu kilikuwa hatarini, wakati kikombe cha fumbo kilipokuwa kinatetema mkononi mwa mwenye kuteseka huyu, mbingu zilifunguka, nuru ilimlika katika giza la dhoruba katika saa ile ya zahama, na malaika mwenye nguvu asimamaye katika uwepo wa Mungu, anayekalia nafasi iliyoachwa na Shetani alipoanguka, alikuja karibu na Kristo. Malaika hakuja kuchukua kikombe kile kutoka mkononi mwa Kristo, bali kumtia nguvu ili akinywee, akipewa pia uhakika wa upendo wa Baba. Alikuja kumpa nguvu huyu mwombaji mwenye asili ya uungu na ubinadamu. Alimwonyesha mbingu zilizofunguka, akimwambia kuhusu watu watakaookolewa kama matokeo ya mateso yake. Alimhakikishia kwamba Baba yake ni mkuu zaidi na mwenye uweza zaidi kuliko Shetani, kwamba kifo chake kingeleta matokeo ya kumhafifisha Shetani, na ya kwamba ufalme wa ulimwengu huu ungepewa kwa watakatifu wake Aliye Juu. Alimwambia kwamba **(694)** angeiona kazi ya nafsi yake, na kuridhishwa, maana angeona umati mkubwa wa jamii ya wanadamu waliookoka, waliookoka milele.

Maumivu ya Kristo hayakukoma, lakini huzuni zake na hali ya kukata tamaa vilimwacha. Dhoruba haikupungua kwa namna yoyote, lakini Yeye aliyekuwa mhanga wa dhoruba hiyo alitiwa nguvu ili kukutana na ghadhabu ya dhoruba hiyo. Aliijia akiwa mtulivu na asiye na papara. Amani ya mbinguni ilitulia kwenye uso wake wenye michirizi ya damu. Alikuwa amebeba kile ambacho hakiwezi kamwe kubebwa na mwanadamu yeyote; maana alikuwa ameonja mateso ya kifo ya kila mwanadamu.

Wale wanafunzi waliokuwa wamelala walikuwa wameamshwa na nuru iliyokuwa imemzunguka Mwokozi. Walimwona malaika akiinama kwa Bwana wao aliyelala kifudifudi. Walimwona akiinua kifuani pake kichwa cha Mwokozi, na kumwonyesha mbinguni. Waliisikia sauti yake, kama sauti ya muziki mtamu, akinena maneno ya faraja na tumaini. Wanafunzi wale walikumbuka tukio la kubadilika sura kule mlimani. Walikumbuka ule utukufu uliomzunguka Yesu kule hekaluni, na ile sauti ya Mungu iliyonena kutoka katika wingu. Sasa utukufu kama ule ule ulionyeshwa, na hawakuwa na woga tena kuhusu Bwana wao. Alikuwa chini ya uangalizi wa Mungu; malaika mwenye nguvu alikuwa ametumwa ili kumlinda. Kwa mara nyingine tena wanafunzi wakiwa katika uchovu wao wanatingwa na usingizi wa ajabu uliokuwa umewazinga. Kwa mara nyingine tena Yesu anawakuta wamelala usingizi.

Akiwatazama kwa huzuni aliwaambia, "Laleni sasa, mpumzike; tazama, saa imekaribia, na Mwana wa Adamu anatiwa katika mikono ya wenye dhambi."

Hata alipokuwa amenena maneno haya, alisikia vishindo vya miguu ya kundi la watu wenye fujo wakimtafuta, na akasema, "Ondokeni, twendeni zetu; tazama, yule anayenisaliti amekaribia."

Hazikuonekana dalili za masumbuko aliyokuwa amepata Yesu wakati huu alipotembea ili kukutana na mwenye kumsaliti. Akiwa amesimama mbele zaidi ya wanafunzi wake alisema, "Ni nani mnayemtafuta?" Wakajibu, "Ni Yesu Mnazareti." Yesu akajibu, "Ni mimi." Wakati maneno haya yalipokuwa yanasemwa, yule malaika ambaye kabla alikuwa amemhudumia alikuja katikati ya Yesu na lile kundi. Nuru ya kimbingu iliangaza usoni pa Yesu, na umbo kama la hua lilimtia kivuli pande zote. Lile kundi la wauaji halikustahimili wakati huu kusimama mbele ya utukufu huu wa kimbingu. Waliweweseka kurudi nyuma. Makuhani, wazee, askari, na hata Yuda mwenyewe, walianguka chini kama watu waliokufa.

Malaika aliondoka, na nuru ikatoweka. Yesu alikuwa na fursa ya kutoroka, lakini alibaki pale, akiwa mtulivu na mwenye staha. Akiwa kama aliyetukuzwa alisimama katikati ya kundi hili gumu, sasa akiwa amedhoofu na pasipo msaada. Wanafunzi waliangalia, wakiwa kimya na wakiwa wamepigwa butwaa.

**(695)** Lakini mambo yalibadilika haraka. Lile kundi lilijikusanya tena. Askari wale wa Kirumi, makuhani na Yuda, walimkusanyikia Kristo. Walionekana kama walioona aibu ya udhaifu wao, na wakiogopa kwamba bado angeweza kuwakwepa. Mkombozi aliuliza tena swali lake, "Mnamtafuta nani?" Walikuwa wamepata ushahidi kwamba Yeye aliyekuwa amesimama mbele yao alikuwa Mwana wa Mungu, lakini hawakusadikishwa. Walilijibu swali lile kwamba, "Mnamtafuta nani?" Walijibu tena kwamba, "Yesu Mnazareti." Mwokozi akasema, "Nimekwisha kuwaambieni ya kwamba ni mimi; basi ikiwa mnanitafuta mimi, waacheni hawa waende zao" – huku akielekeza kwa wanafunzi wake. Alijua jinsi imani yao ilivyokuwa dhaifu, na alitaka kuwakinga na majaribu na mateso. Alikuwa tayari kuwa kafara kwa ajili yao.

Yuda mwenye kumsaliti hakusahau jukumu lake la kufanya. Wakati kundi lile lilipoingia bustanini, alikuwa anaongoza njia, akifuatiwa kwa karibu na kuhani mkuu. Alikuwa amewapa ishara watu wale waliotaka kumkabili Yesu, akisema, "Nitakayembusu, huyo ndiye; mkamateni." Mathayo 26:48. Sasa alijifanya kama hayuko pamoja nao. Akija karibu na **(696)** Yesu, aliushika mkono wake kama rafiki ambaye wanafahamiana. Kwa maneno kwamba, "Salamu, Rabi" akambusu kwa kurudiarudia, huku akionekana kulia kama anayemwonea huruma katika hatari aliyokuwa nayo.

Yesu akamwambia, "Rafiki, fanya ulilolijia." Sauti yake ilitetema kwa huzuni kadiri alivyoongeza maneno kwamba, "Yuda, wamsaliti Mwana wa Adamu kwa kumbusu?" Maneno haya ya kusihi yalipaswa kuamsha dhamiri ya msaliti huyu, na kuugusa moyo wake wenye usumbufu; lakini heshima, uaminifu, na huruma ya kibinadamu vilikuwa vimemwacha. Alisimama kwa ujasiri na upinzani, pasipo kuonyesha mwelekeo wa kulainika. Alikuwa amejitoa kwa Shetani, na hakuwa na nguvu za kumpinga. Yesu hakulikataa busu la msaliti.

Lile kundi lenye fujo lilipata nguvu lilipoona Yuda amegusa mwili wake Yeye ambaye muda mfupi tu alikuwa ametukuzwa machoni pao. Sasa walimkamata Yesu, wakamfunga mikono yake ile ya thamani ambayo wakati wote ilitumika kutenda mema.

Wanafunzi walikuwa wamedhani kwamba Bwana wao hawezi kuruhusu achukuliwe. Kwa kutumia nguvu ile ile iliyokuwa imewafanya watu wa kundi lile kuanguka kama waliokufa angewafanya kukosa nguvu, mpaka Yesu na

wenzake watoroke. Walifadhaika na kuumia walipoona kamba zikiletwa ili kuifunga mikono yake Yeye waliyempenda. Kwa hasira Petro alichomoa upanga wake na kujaribu kumpigania Bwana wake, lakini aliishia tu kukata sikio la mtumishi wa kuhani mkuu. Yesu alipoona hicho kilichofanyika, alijifungua mikono yake, ingawa ilikuwa imebanwa barabara na askari wa Kirumi, akasema, "Mwe radhi kwa hili," akaligusa sikio lililojeruhiwa, nalo likapona wakati huo huo. Halafu akamwambia Petro, "Rudisha upanga wako mahali pake, maana wote waushikao upanga, wataangamia kwa upanga. Ama wadhani ya kuwa mimi siwezi kumsihi Baba yangu, naye ataniletea sasa hivi zaidi ya majeshi kumi na mawili ya malaika?" – jeshi moja mahali pa kila mmoja wa wanafunzi wake. Wanafunzi wale walifikiri hivi, Kwa nini asijiokoe na kutuokoa na sisi? Akijibu mawazo yao hayo ambayo hayakutamkwa, aliongeza hivi, "Yatatimizwaje basi maandiko, ya kwamba hivyo ndivyo vilivyopasa kujiri?" "Je! Kikombe alichonipa Baba, mimi nisikinywee?"

Maafisa wakubwa wa wazee wa Wayahudi hawakujiepusha kuungana katika kumkabili Yesu. Kukamatwa kwake kulikuwa jambo muhimu sana kiasi kwamba wasingeliacha mikononi mwa watumishi wadogo tu; wale makuhani na wazee werevu walikuwa wameungana na askari wa hekalu na genge la watu wenye fujo katika kumfuata Yuda kwenda Gethsemane. Je! Ni kundi gani hili ambalo waheshimiwa wale wenye cheo wanaungana nalo – genge la watu wenye hasira, wakiwa na silaha za aina zote, kama watu wanaowinda mnyama wa mwitu!

**(697)** Akiwageukia wale makuhani na wazee, Kristo aliwakazia macho yake yapelelezayo ndani. Maneno aliyotamka wasingeyasahau katika muda wa maisha yao yote. Yalikuwa kama mishale mikali ya Mwenyezi. Kwa mamlaka alisema: Je! Mmekuja wenye panga na marungu kama kukamata mnyang'anyi? Kila siku naliketi hekaluni nikifundisha. Mlikuwa na kila nafasi ya kuninyoshea mikono yenu na kunikamata, lakini hamkufanya hivyo. Usiku ndio unaofaa zaidi kwa kazi yenu. “Hii ndiyo saa yenu, na mamlaka ya giza.”

Wanafunzi walitiwa hofu walipoona Yesu akiruhusu kuchukuliwa na kufungwa. Walichukizwa kwa sababu aliruhusu mateso haya kwake na kwao. Hawakuweza kuelewa mwelekeo wake, na walimlaumu kwa kujisalimisha mikononi mwa kundi lile baya. Katika woga na huzuni zao, Petro alipendekeza kwamba wajiokoe wenyewe. Kwa kufuata pendekezo hili, "wote wakamwacha, wakakimbia." Lakini Kristo alikuwa ameshatabiri hali hii ya kumwacha aliposema, "Tazama, saa yaja, naam, imekwisha kuja, ambapo mtatawanyika kila mmoja kwao kwao, na kuniacha mimi peke yangu; walakini mimi si peke yangu, kwa kuwa Baba yupo pamoja nami." Yohana 16:32.

## Sura ya 75

# Mbele ya Anasi na Behewani kwa Kayafa

[Sura hii imejengwa katika Mathayo 26:57-75; 27:1; Marko 14:53-72; 15:1; Luka 22:54-71; Yohana 18:13-27.]

Yesu aliharakishwa kuvuka kijito cha Kedroni na kupita katika miti mingi ya mizeituni, na kupitia katika mitaa ya mji iliyokuwa kimya usingizini. Muda ulikuwa umevuka usiku wa manane, na makelele ya fujo za kikundi kile kilichomfuata yalipenya katika anga lile tulivu. Mwokozi alikuwa amefungwa na kulindwa barabara, na alijongea kwa maumivu. Lakini kwa haraka ya shauku waliomkamata waliharakisha kwenda naye kwenye kasri ya Anasi, kuhani mkuu aliyekuwa amemaliza muda wake.

Anasi alikuwa mkuu wa familia ya kikuhani iliyokuwa inahudumu, na kwa hali iliyo tofauti na umri wake alikuwa anatambuliwa kama kuhani mkuu. Mashauri yake yalitafutwa na yalitekelezwa kama vile ni sauti ya Mungu. Lazima amwone kwanza Yesu aliye mfungwa wa mamlaka ya kikuhani. Lazima awepo wakati mfungwa huyu anapohojiwa, kwa hofu kwamba Kayafa ambaye alikuwa ndiye kuhani mkuu asiyekuwa na uzoefu sana angeshindwa kufikia lengo walilokuwa wanatafuta kulifikia. Lazima ujanja wake, werevu wake wa hila, na ustadi wake wa kupambanua mambo utumike katika tukio hili; maana, katika matukio yote, lazima kuhukumiwa kwa Kristo kupatikane.

Kristo alikuwa ahojiwe kwa njia rasmi mbele ya Sanhedrin; lakini kule mbele ya Anasi alihojiwa kwa mahojiano ya awali kwanza. Chini ya utawala wa Kirumi uliokuwepo baraza la Sanhedrin halikuwa na uwezo wa kutekeleza hukumu ya kifo. Wangeweza tu kumchunguza mshtakiwa, na kupitisha hukumu, ambayo ilipaswa kuidhinishwa na mamlaka za Kirumi. Kwa hiyo ilikuwa ni lazima kuleta mashtaka dhidi ya Kristo **(699)** yanayohusu jinai dhidi ya Warumi. Lazima pia yapatikane mashtaka ambayo yatamtia hukumuni kwa mtazamo wa macho ya Wayahudi. Si wachache miongoni mwa makuhani na wakuu ambao walikuwa wamesadikishwa na mafundisho yake Kristo, na ni hofu tu ya kutengwa na sinagogi iliyosababisha wasimkiri. Makuhani walikumbuka vema swali la Nikodemo kwamba, "Je! Torati yetu humhukumu mtu kabla ya kumsikia kwanza, na kujua atendavyo?" Yohana 7:51. Swali hili lilikuwa kwa muda fulani limelisambaratisha baraza na kutibua mipango yao. Yusufu wa Arimathaya na Nikodemo sasa hawakutakiwa kuarifiwa kuhusu baraza hili, lakini walikuwepo wengine ambao wangethubutu kuzungumza kwa kutaka kufuatwa kwa haki. Uchunguzi wa mashtaka lazima ufanywe kwa namna ambayo ungewaleta pamoja wajumbe wote wa baraza la Sanhedrin kuwa kitu kimoja dhidi ya Kristo. Kulikuwa na mashtaka mawili ambayo makuhani walitamani kuyashikilia. Ikiwa ingethibitika kwamba Yesu ni mwenye kukufuru, angehukumiwa na Wayahudi. Ikiwa angepatikana na hatia ya kuchochea uasi dhidi ya serikali, hukumu yake toka kwa Warumi ingepatikana. Anasi alijaribu kuyaweka mashtaka hayo ya pili. Alimwuliza Yesu kuhusu wanafunzi wake na mafundisho yake, akitumaini kwamba mshtakiwa yule angempa maelezo ambayo angeyafanyia kazi. Alitafuta kushawishi kauli ambayo ingeonyesha kwamba Kristo alikuwa anatafuta kuanzisha kundi la siri, kwa nia ya kuanzisha ufalme mpya. Hapo ndipo makuhani wangempeleka kwa Warumi wakimshtaki kama mtu anayevunja amani na mtu anayechochea maasi.

Kristo alisoma makusudi ya kuhani kama kitabu kilicho wazi. Kama anayesoma moyo wa ndani wa mtu aliyemwuliza, alikana kwamba kulikuwa na mafungamano ya siri kati yake na wafuasi wake, au kwamba aliwakusanya kwa siri au gizani ili kuficha mipango yake. Hakuwa na siri katika mipango yake au mafundisho yake. Alisema, "Mimi nimesema na ulimwengu waziwazi; siku zote nalifundisha katika sinagogi na katika hekalu, wakusanyikapo Wayahudi wote; wala kwa siri mimi sikusema neno lolote."

Mwokozi alionyesha tofauti kati ya vile alivyofanya kazi na njia zile zilizotumiwa na washtaki wake. Kwa miezi kadhaa walikuwa wamemwinda, wakitafuta kumnasa na kumleta mbele ya mahakama ya siri, mahali ambapo kwa njia ya kiapo cha uongo wangepata kile ambacho kilikuwa hakiwezekani kupatikana kwa njia za haki. Sasa walikuwa wanatekeleza azma yao hiyo. Kule kuhusuriwa na kundi lenye fujo usiku wa manane, dhihaka na matusi aliyofanyiwa kabla ya kuhukumiwa, au hata kabla ya kushtakiwa, ilikuwa ndiyo namna yao ya kufanya kazi, si namna yake Yeye. Vitendo vyao vilikuwa vya uvunjaji wa sheria. Kanuni zao wenyewe zilisema kwamba kila mtu anapaswa atendewe kama asiye na hatia mpaka anapothibitishwa kuwa na hatia. Kwa kanuni zao hizo wale makuhani walikuwa katika nafasi ya kuhukumiwa.

Akimgeukia yule aliyemwuliza, Yesu alisema, " Ya nini kuniuliza mimi?" Je! Makuhani na wakuu hawakutuma wapelelezi kuchunguza mienendo yake, na kuleta taarifa ya kila neno? Je! Hawa hawakuwepo katika kila mkusanyiko **(700)** wa watu, na kuwapelekea makuhani taarifa ya maneno na matendo yake? Alisema, "Waulize wale waliosikia ni nini niliyowaambia; wao wanajua niliyoyanena."

Anasi alinyamazishwa na uamuzi wa jibu lile. Akihofu Yesu asiseme jambo kuhusu njia zake ambazo alitamani ziendelee kufunikwa, hakusema kitu zaidi kwake katika wakati huu. Mmoja wa maafisa wake, akiwa amejawa na ghadhabu kwa kuona Anasi amenyemazishwa, alimpiga Yesu kofi usoni, akisema, "Wamjibu hivi Kuhani Mkuu?" Kristo alijibu kwa upole kwamba, "Kama nimesema vibaya, ushuhudie ule ubaya; bali kama nimesema vema, wanipigia nini?" Hakutamka maneno ya kuumiza. Jibu lake la upole lilitoka katika moyo likiwa halina dhambi, la upole, ambalo lisingeshtakiwa neno.

Kristo aliumizwa sana na hali ya kutendewa jeuri na matusi. Akiwa mikononi mwa viumbe aliowaumba, na wale aliokuwa anatoa kafara ya kudumu kwa ajili yao, alipokea kila aina ya ufidhuli. Na aliumia kwa kiasi kinachoshabihiana na ukamilifu wa utakatifu wake na chuki yake dhidi ya dhambi. Kushtakiwa na watu waliojifanya kuwa waovu na katili kuliendelea kuwa kafara ya kudumu kwake. Kuzungukwa na wanadamu wanaoongozwa na Shetani ilikuwa ni chukizo kwake. Na alijua kwamba kwa wakati mfupi tu, kwa kumlika kwa nguvu yake ya uungu, angeweza kuwaangusha mavumbini wale watesi wake waliokuwa katili. Hali hii iliyafanya mateso kuwa magumu kustahimili.

Wayahudi walikuwa wanamtafuta Masihi ambaye angedhihirishwa kwa mwonekano wake. Walimtarajia, kwa nguvu ya kushinda ya ghafla, abadilishe mkondo wa mawazo ya watu, na kuwalazimisha kukiri ukuu wake. Kwa hiyo, waliamini, angeweza kupata kujitukuza mwenyewe, na kutimiza matumaini ya matakwa yao. Kwa hiyo wakati Kristo alipotendewa kwa jeuri, lilikuja kwake jaribu kubwa la nguvu kwamba adhihirishe sifa yake ya uungu. Kwa neno, kwa jinsi ya kuangalia, angewalazimisha watesi wake kukiri kwamba alikuwa Bwana aliye juu ya wafalme na wakuu, na makuhani na hekalu. Lakini ilikuwa ndiyo kazi yake ngumu kubaki katika nafasi aliyokuwa amechagua ya kuwa mmoja pamoja na wanadamu.

Malaika wa mbinguni walishuhudia kila hatua aliyofanyiwa kamanda wao. Walitamani kumwokoa Kristo. Chini ya Mungu malaika wana uwezo wote. Katika tukio moja, katika kutii agizo la Kristo, waliwaua watu wa vita mia na themanini na tano elfu wa jeshi la Ashuru katika usiku mmoja. Ingekuwa rahisi kiasi gani kwa malaika, waonao tukio la aibu la kushtakiwa kwa Kristo, kudhihirisha kuchukizwa kwao kwa kuwaua maadui hawa wa Mungu! Lakini hawakuagizwa kufanya jambo hili. Yeye ambaye angeweza kuwaangamiza adui zake na kuwaua alistahimili **(703)** ukatili wao. Upendo wake kwa Baba yake, na ahadi yake, vilivyofanywa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu, kuwa Mbeba Dhambi, vilimfanya kuyastahimili pasipo kulalamika magumu aliyotendewa na wale aliokuja kuwaokoa. Ilikuwa ni sehemu ya kazi yake kustahimili, katika ubinadamu wake, mabezo na matusi yote ambayo wanadamu walilundika juu yake. Tumaini pekee la wanadamu lilikuwa katika kukubali huku kwa Kristo kwa mambo yote aliyovumilia kutoka katika mikono na mioyo ya wanadamu.

Kristo hakuwa amesema jambo lolote ambalo linaweza kuwanufaisha washtaki wake; lakini bado alifungwa, kuashiria kwamba alikuwa mhalifu. Hata hivyo lazima wajifanye kuwa wanafuata haki. Ilikuwa lazima kuwe na kitu mfano wa utaratibu rasmi wa kuendesha mashtaka kisheria. Mamlaka zile ziliharakisha kitu hicho. Walijua jinsi watu walivyomchukulia Yesu, na waliogopa kwamba ikiwa kitendo kile cha kumtia nguvuni kingevuma mpaka mbali, kungekuwa na jitihada za kumwokoa. Pia, kama mchakato wa mashtaka na kutoa hukumu visingefanyika haraka, kungekuwa na kukawia kwa muda wa juma moja la kusherehekea sikukuu ya Pasaka. Hali hii ingefanya mipango yao kushindwa. Ili kupata hukumu juu ya Yesu walitegemea sana ghasia za kundi la watu, wengi wao wakiwa watu wa kawaida wa fujo kutoka pale pale Yerusalemu. Ikiwa kutakuwa na juma zima la kucheleweshа, hamasa ya watu ingepungua, na mambo yangetulia. Sehemu kubwa ya watu wangeunga mkono upande wa Kristo; wengi wangejitokeza na ushuhuda wa kumtetea, wakiweka wazi matendo makuu aliyokuwa ameyafanya. Hali hii ingeibua chuki ya umma dhidi ya baraza la Sanhedrin. Mwenendo wao katika kesi ungebatilishwa, na Yesu angewekwa huru, ili kupata heshima mpya kutoka kwa makutano. Kwa hiyo makuhani na wakuu waliazimia kwamba kabla ya makusudi yao kujulikana, lazima Yesu afikishwe mikononi mwa Warumi.

Lakini kabla ya yote, lazima tuhuma ipatikane. Bado walikuwa hawajapata tuhuma yoyote. Anasi aliagiza kwamba Yesu apelekwe kwa Kayafa. Kayafa alikuwa mtu wa jamii ya Masadukayo, ambao miongoni mwao

wakati huu walikuwemo adui wakubwa wa Yesu. Yeye mwenyewe, ingawa alikuwa na mapungufu ya nguvu ya ushawishi, alikuwa mkali, asiye na huruma, na asiye na maadili, kama alivyokuwa Anasi. Hakusaza mbinu yoyote katika kuhakikisha Yesu anaangamizwa. Sasa ilikuwa mapema asubuhi, na kukiwa na giza kubwa; likitumia kurunzi na mienge lile kundi lenye silaha lilisonga mbele pamoja na mshtakiwa wao kwenda kwenye kasri la kuhani mkuu. Mahali hapa, wakati wajumbe wa Sanhedrin walikuwa wanakusanyika kujadiliana, Anasi and Kayafa walimwuliza Yesu tena, lakini bila mafanikio.

Baraza lilipokwisha kukusanyika katika ukumbi wa hukumu, Kayafa alikalia kiti chake kama mwenyekiti. Kila upande kulikuwa na waamuzi, na wale waliovutiwa sana na kesi ile. Askari wa Kirumi walikuwa wamepangwa **(704)** jukwaani chini ya kiti kikuu kile. Chini ya kiti kile cha heshima ndipo Yesu aliposimama. Macho yote ya umati yalikuwa yamekazwa kwake. Msisimko ulikuwa mkubwa sana. Katika umati wote Yeye peke yake ndiye aliyekuwa mtulivu na mpole. Mazingira yenyewe yaliyomzunguka pale alipo yalionekana kujawa na ushawishi wa utakatifu.

Kayafa alikuwa amemchukulia Yesu kama mpinzani wake. Hamu ya watu kumsikia Mwokozi, na mwonekano wa jumla kama wa kutaka kukubali mafundisho yake, vilikuwa vimeamsha wivu mbaya wa kuhani mkuu huyu. Lakini kadiri sasa Kayafa alivyomwangalia mshtakiwa huyu, alipigwa na mshangao mkubwa kwa mwonekano wake wa wema na unyenyekevu. Usadikisho ulimjia kwamba mtu huyu alitoka kwa Mungu. Kilichofuata aliondosha kwa dhihaka wazo hilo. Ghafla **(705)** sauti yake ilisikika kwa dharau, sauti ya kuonyesha ukuu ikidai kwamba Yesu afanye moja ya miujiza yake mbele yao. Lakini maneno yake yalipita masikioni mwa Mwokozi kama vile hakuyasikia. Watu walilinganisha ukuu na uheshimiwa wa Anasi na Kayafa na mwonekano wa upole na mvuto wa Yesu. Hata katika mawazo ya umati ule wenye moyo mgumu swali liliibuka kwamba, Je! Mtu huyu mwenye mwonekano wa utauwa atahukumiwa kama mhalifu?

Kayafa, akihisi ushawishi uliokuwa unapatikana, aliiharakisha kesi. Maadui wa Yesu walikuwa katika utata mkubwa. Waliazimia kupata kumhukumu, lakini hawakujua namna ya kufanikisha hili. Wajumbe wa baraza lile waligawanyika kati ya Mafarisayo na Masadukayo. Kulikuwa na kutoelewana kukubwa na mapambano baina yao; hawakudiriki kusogelea baadhi ya masuala waliyokuwa hawakubaliani kwa kuogopa kugombana. Kwa maneno machache Yesu angeweza kuamsha chuki zao wao kwa wao, na hivyo kuondosha ghadhabu yao kutoka kwake. Kayafa alijua jambo hili, na alitamani kuepusha kuibua mapambano. Kulikuwa na mashahidi wengi wa kuthibitisha kwamba Kristo alikuwa amewadharau makuhani na waandishi, kwamba alikuwa amewaita wanafiki na wauaji; lakini ushahidi huu kaukuonekana kufaa kuletwa pale. Masadukayo katika mapambano yao makali dhidi ya Mafarisayo walikuwa wametumia lugha hiyo hiyo. Na ushahidi huo usingekuwa na nguvu mbele ya Warumi, ambao wao wenyewe walikuwa hawakupendezwa na unafiki wa Mafarisayo. Kulikuwa na ushahidi wa kutosha kwamba Yesu alikuwa hajali mapokeo ya Wayahudi, na alikuwa amesema maneno yasiyoheshimu maadhimisho ya kaida zao; lakini kuhusu mapokeo Mafarisayo na Masadukayo walikuwa katika makali ya upanga; na ushahidi huu pia usingekuwa na uzito kwa Warumi. Adui wa Kristo hawakudiriki kumshtaki kuhusiana na utunzaji wa Sabato, ili uchunguzi wa hilo usije ukadhihirisha tabia ya kazi yake. Ikiwa miujiza yake ya kuponya ingewekwa wazi, kusudi lenyewe la makuhani lingeshindwa.

Mashahidi wa uongo walikuwa wamepewa rushwa ili wamshtaki Yesu kwa kuchochea uasi na kupanga kuanzisha serikali nyingine. Lakini ushahidi wao ulithibitika kuwa usiopangiliwa na unaopingana. Walipohojiwa na kupimwa walipinga kauli zao wenyewe.

Mapema katika huduma yake Kristo alikuwa amesema, "Livunjeni hekalu hili, nami katika siku tatu nitalisimamisha." Katika lugha ya kistiari ya unabii, hapo alikuwa ametabiri kuhusu kifo chake na ufufuko wake. "Alinena habari za hekalu la mwili wake." Yohana 2:19, 21. Wayahudi walikuwa wameelewa maneno haya kwa maana yake ya kawaida, kwamba yanahusu hekalu la Yerusalemu. Katika yote ambayo Kristo alikuwa amesema, makuhani hawakupata kitu cha kumshtaki Yesu **(706)** isipokuwa hili. Kwa kuyasema isivyo sahihi maneno haya walitarajia kunufaika nayo. Warumi walikuwa wameshiriki kulijenga upya na kulipamba hekalu hili, na walikuwa na fahari kubwa kuhusu jengo hili; dharau yoyote ambayo ingefanywa kwa hilo hakika ingewachukiza. Hapa Warumi na Wayahudi, Mafarisayo na Masadukayo, walikutana kwa pamoja; maana wote walilichukulia hekalu hili kwa heshima kubwa. Mashahidi wawili kuhusu jambo hili walipatikana ambao ushahidi wao haukupingana kama ilivyokuwa kwa wengine waliokuwa wametangulia. Mmoja wa hao aliyekuwa amehongwa

ili kumshtaki Yesu, alisema, "Huyu alisema, Naweza kulivunja hekalu la Mungu, na kulijenga kwa siku tatu." Kwa njia hiyo maneno ya Kristo yalisemwa isivyo sahihi. Ikiwa yangesemwa kwa usahihi kama alivyoyatamka, yasingeweza kufanikisha hukumu hata mbele ya Sanhedrin. Ikiwa Yesu angekuwa mwanadamu tu, kama Wayahudi walivyodai, tamko lake hilo lingeonyesha tu kuwa la mtu ambaye hakutumia akili, la roho ya kujivuna, lakini lisingechukuliwa kama makufuru. Hata vile lilivyowasilishwa na mashahidi isivyo sahihi, maneno yale hayakuwa na kitu ambacho Warumi wangekiona kama uhalifu unaostahili kifo.

Kwa ustahimilivu Yesu alisikiliza ushahidi ule uliokuwa unapingana. Hakutoa neno lolote la kujitetea. Hatimaye washtaki wake walitatizika, wakachanganyikiwa, na kuumia vichwa. Mashtaka yale yalikuwa hayaendi mbele; ilionekana kama vile njama zao zitashindwa. Kayafa alikata tamaa. Njia moja ya mwisho ilikuwa bado ipo; lazima Kristo alazimishwe kujitia hukumuni Yeye mwenyewe. Kutokea kwenye kiti cha hukumu, kuhani mkuu alianza, uso wake ukifanywa kuwa na hasira, sauti yake na mwonekano wake wa nje ukionyesha wazi kwamba ikiwa angekuwa na mamlaka angemwangamiza mshtakiwa yule pale pale. Akasema, "Hujibu neno? Hawa wanakushuhudia nini?"

Yesu akatulia. "Alionewa, lakini alinyenyekea, Wala hakufunua kinywa chake; Kama mwana-kondoo apelekwaye machinjoni, Na kama vile kondoo anyamazavyo Mbele yao wakatao manyoya yake; Naam, hakufunua kinywa chake." Isaya 53:7.

Hatimaye, Kayafa, akiinua mkono wake wa kuume kuelekea mbinguni, aliongea na Yesu katika mfano wa kiapo: "Nakuapisha kwa Mungu aliye hai, utuambie kama wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu."

Katika habari hii Kristo hakubaki kimya. Kulikuwa na wakati wa kukaa kimya, na wakati wa kunena. Hakuwa amesema kitu mpaka alipoulizwa moja kwa moja. Alijua kwamba kujibu swali sasa ilikuwa ni kukifanya kifo chake kuwa cha hakika. Lakini swali lile lilikuwa limeulizwa na mamlaka ya juu iliyotambuliwa katika taifa, tena kwa jina la Aliye Juu. Kristo asingeshindwa kuonyesha heshima sahihi kwa sheria. Zaidi ya hili, uhusiano wake na Baba ulikuwa unahojiwa. Lazima atamke sifa yake na kazi yake. **(707)** Yesu aliwaambia wanafunzi wake kabla kwamba, "Kila mtu atakayenikiri mbele ya watu, nami nitamkiri mbele za Baba yangu aliye mbinguni." Mathayo 10:32. Sasa kwa mfano wake mwenyewe alilirudia somo lile.

Kila sikio lilikuwa limetegwa kusikia, na kila jicho lilikuwa limekazwa usoni mwake wakati alipojibu kwamba, "Wewe umesema." Nuru ya mbinguni ilikuwa kama inamlika kwenye mwili wake uliochoka alipokuwa anaongezea kwamba, "Lakini nawaambieni, Tangu sasa mtamwona Mwana wa Adamu ameketi mkono wa kuume wa nguvu, akija juu ya mawingu ya mbinguni."

Kwa muda uungu wa Kristo ulimlika kupitia katika ubinadamu aliokuwa amevaa. Kuhani mkuu aliogopa akiwa pale mbele ya macho yanayopenya ya Mwokozi. Jinsi alivyomwangalia ni kama vile alikuwa akiyasoma mawazo yake yaliyofichwa, na kuchoma moyoni mwake. Kamwe katika maisha yake ya baadaye hakusahau macho yale yaliyomtazama ya Mwana wa Mungu aliyekuwa katika mateso.

"Tangu sasa mtamwona Mwana wa Adamu ameketi **(708)** mkono wa kuume wa nguvu, akija juu ya mawingu ya mbinguni." Katika maneno haya Kristo alionyesha kinyume cha tukio hili lililokuwa linaendelea. Yeye, aliye Bwana wa uzima na utukufu, angeketi katika mkono wa kuume wa Mungu. Angekuwa mhukumu wa dunia yote, na uamuzi wake usingekuwa na kukata rufaa. Halafu kila jambo la siri lingewekwa wazi mbele za Mungu, na hukumu ingefanywa kwa kila mtu sawasawa na matendo yake.

Maneno ya Kristo yalimshtusha kuhani mkuu. Wazo kwamba kungekuwa na ufufuo wa waliokufa, wakati ambapo watu wote wangesimama katika kizimba cha Mungu, ili kulipwa sawasawa na matendo yao, lilikuwa la kutisha kwa Kayafa. Hakupenda kusikia kwamba siku za usoni angehukumiwa kulingana na matendo yake. Mbele yake kilipita haraka kitu kama senema kikionyesha matukio ya hukumu ya mwisho. Kwa muda aliona jambo la kuogofya la makaburi kuwatoa wafu waliokuwemo, pamoja na siri ambazo alitamani kwamba bora zingefichwa. Kwa muda alihisi kama amesimama mbele ya Hakimu wa milele, ambaye jicho lake, lionalo mambo yote, lilikuwa linausoma moyo wake, likiweka wazi siri zilizotamaniwa kufichwa pamoja na waliokufa.

Tukio lile lilipita katika maono ya kuhani yule. Maneno ya Kristo yalimkata hasa, huyu Sadukayo. Kayafa alikuwa amekana fundisho la ufufuko, hukumu, na maisha yajayo. Sasa alipagawa na hasira ya kishetani. Je! Mtu huyu,

mfungwa aliyekuwa mbele yake, asumbue nadharia zake nzuri alizoshikilia? Akilirarua joho lake, ili kwamba watu waone utisho aliojifanya kuwa nao, alidai kwamba mshtakiwa yule atiwe hukumuni kwa kukufuru bila hata kuhojiwa zaidi. "Tuna haja gani tena ya mashahidi? Mmesikia kufuru yake; mwaonaje ninyi?" Wote wakamhukumu.

Usadikisho uliochanganyika na hasira ulimfanya Kayafa kufanya vile alivyofanya. Alijichukia yeye mwenyewe kwa kuamini maneno ya Kristo, na badala ya kurarua moyo wake katika kina cha ukweli, na kukiri kwamba Yesu alikuwa Masihi, alirarua majoho yake ya kikuhani akiazimia kuendelea kupinga. Kitendo hiki kilikuwa na umuhimu. Kayafa alitambua kidogo mno maana yake. Katika kitendo hiki, kilichofanywa ili kuwashawishi waamuzi na kumfanya Kristo kuhukumiwa, kuhani mkuu yule alikuwa amejihukumu mwenyewe. Kwa mujibu wa sheria ya Mungu alikuwa amepoteza sifa ya ukuhani. Alikuwa amejitamkia mwenyewe hukumu ya kifo.

Kuhani mkuu hakutakiwa kurarua vazi lake. Kwa mujibu wa sheria ya Kilawi, jambo hili lilikatazwa na adhabu yake ilikuwa ni kifo. Hakuna mazingira yoyote, wala tukio lolote, ambapo kuhani angerarua joho lake. Ilikuwa desturi miongoni mwa Wayahudi kwa mavazi kuraruliwa wakati wa kifo cha marafiki, lakini **(709)** makuhani hawakuruhusiwa kufanya desturi hii. Agizo la wazi lilikuwa limetolewa na Mungu kupitia Musa kuhusu jambo hili. Mambo ya Walawi 10:6.

Kila kitu kilichovaliwa na kuhani kilikuwa kamili na pasipo na waa. Tabia ya kitu halisi, Yesu Kristo, ndiyo iliyowakilishwa na yale mavazi rasmi mazuri. Hakuna kitu ambacho kingekubalika kwa Mungu isipokuwa kikamilifu, katika mavazi na mtazamo, katika maneno na moyo. Yeye ni mtakatifu, na lazima utukufu na ukamilifu wake uwakilishwe na ibada ya duniani. Hakuna kitu ambacho kingewakilisha kwa usahihi utakatifu wa ibada ya mbinguni isipokuwa ukamilifu. Mwanadamu mwenye mawazo mafupi lazima ararue moyo wake kwa kuonyesha roho ya unyenyekevu na toba. Hili ndilo ambalo Mungu angeangalia. Lakini hakuna kurarua majoho ya kikuhani ambako kungefanywa, maana hilo lingehalifu uwakilishi wa mambo ya mbinguni. Kuhani mkuu aliyethubutu kutokea katika utumishi mtakatifu, na kujihusisha na utumishi wa patakatifu, akiwa na vazi lililoraruliwa, aliangaliwa kama ambaye amejitenga mbali na Mungu. Kwa kurarua vazi lake alikuwa amejikatilia mbali na hali ya kuwa na sifa ya uwakilishi. Hakukubaliwa tena na Mungu kuwa kuhani mwenye kuhudumu. Njia hii ya matendo, kama ilivyoonyeshwa na Kayafa, ilionyesha hasira ya mwanadamu, kutokamilika kwa mwanadamu.

Kwa kurarua mavazi yake, Kayafa hakutekeleza sheria ya Mungu, akafuata mapokeo ya wanadamu. Sheria iliyowekwa na mwanadamu iliruhusu kwamba kwa hali ya kukufuru kuhani angeweza kurarua mavazi yake kwa kuchukizwa na dhambi hiyo, na asiwe na hatia. Kwa njia hiyo nafasi ya sheria ya Mungu ilichukuliwa na sheria za wanadamu.

Kila kitendo kilichotendwa na kuhani mkuu kilikuwa kinafuatiliwa na watu kwa hamu; na Kayafa alidhani kwamba kwa jambo lile alikuwa ameonyesha kuumia. Lakini katika kitendo hiki, kilichopangwa kutumika kama mashtaka dhidi ya Kristo, alikuwa anambeza Yeye ambaye Mungu alimwambia, "Jina langu limo ndani yake." Kutoka 23:21. Yeye mwenyewe alikuwa anakufuru. Akisimama chini ya hukumu ya Mungu, alitamka hukumu kwa Kristo kwamba ni mtu mwenye kukufuru.

Wakati Kayafa aliporarua vazi lake, kitendo chake kilikuwa na maana kuhusu nafasi ambayo taifa la Wayahudi kama taifa lingechukua mbele za Mungu. Wale watu waliopata kupendelewa na Mungu walikuwa wanajitenga naye, na walikuwa wanaelekea kwa haraka kuwa watu walioachwa na Yehova. Wakati Kristo akiwa msalabani alipolia kwamba, "Imekwisha" (Yohana 19:30), na pazia la hekalu likapasuka vipande viwili, Mlinzi Mtakatifu alitangaza kwamba Wayahudi walikuwa wamemkataa Yeye aliyekuwa uhalisia wa mifano ya ibada walizofanya, kitu halisi cha vivuli vyao vyote. Israeli aliachwa na Mungu. Ilikuwa sawa kwamba Kayafa alirarua majoho yake ya utumishi, yaliyoashiria kwamba alikuwa mwakilishi wa Kuhani Mkuu aliye mkuu; maana hayakuwa na maana tena kwake wala kwa watu wake. Ilikuwa sawa kwamba kuhani mkuu ararue majoho yake kwa kutopendezwa na yeye mwenyewe na taifa lake.

**(710)** Baraza la Sanhedrin lilikuwa limetamka kwamba Yesu anastahili kufa; lakini ilikuwa kinyume cha sheria ya Wayahudi kumshtaki na kumhukumu mshtakiwa wakati wa usiku. Katika maamuzi halali hakuna kitu ambacho kingefanyika isipokuwa wakati wa mwanga wa mchana na katika kikao kamili cha baraza. Licha ya hilo,

Mwokozi sasa alitendewa kama mhalifu aliyekwisha kuhukumiwa, na akatolewa ili atendewe mabaya na watu wa hali ya chini na wanadamu waovu. Kasiri ile ya kuhani mkuu ilizunguka viwanja vilivyo wazi mahali ambapo askari na makutano walikuwa wamekusanyikia. Kupitia katika kiwanja hiki, Yesu alipelekwa katika chumba cha uangalizi, kila upande akikutana na dhihaka ya madai yake kwamba ni Mwana wa Mungu. Maneno yake ya kuketi "upande wa kuume wa nguvu," na kuja, "juu ya mawingu ya mbinguni," yalirudiwa-rudiwa kwa kejeli. Akiwa katika chumba cha uangalizi akisubiri mashtaka ya kisheria, hakuwa amelindwa. Makundi ya watu wa kawaida walikuwa wameona ukatili aliokuwa ametendewa mbele ya baraza, kutokana na hali hiyo na wao walipata uhalali wa kuonyesha hali yao ya mambo ya kishetani. Wema wenyewe na utauwa wa Kristo uliwafanya kuwa kama wamepagawa. Upole wake, kutokuwa na hatia kwake, uvumilivu wake, viliwajaza chuki itokato kwa Shetani. Huruma na haki vilikanyagwa. Kamwe hakuna mhalifu aliyetendewa kwa namna isiyo ya ubinadamu kama alivyotendewa Mwana wa Mungu.

Lakini yapo maumivu makubwa yaliyourarua moyo wa Yesu; pigo lililosababisha maumivu ya kina ambayo hakuna mkono wowote wa adui ambao ungeweza kuyasababisha. Wakati alipokuwa akiendelea kushtakiwa kwa dhihaka mbele ya Kayafa, Kristo alikuwa amekanwa na mmoja wa wanafunzi wake.

Baada ya kumwacha Bwana wao peke yake kule bustanini, wawili kati ya wanafunzi wake walikuwa wameamua kulifuata, kwa mbali, lile kundi lililokuwa limemchukua Yesu. Wanafunzi hawa walikuwa ni Petro na Yohana. Makuhani walimtambua Yohana kama mwanafunzi wa Yesu aliyejulikana sana, nao walimpeleka ukumbini, wakitumaini kwamba kwa kushuhudia manyanyaso ambayo Kiongozi wake angefanyiwa, angeachana na wazo kwamba Yule alikuwa Mwana wa Mungu. Yohana alimtetea Petro, na kupata kibali cha yeye pia kuingia mle.

Mle ukumbini moto ulikuwa umewashwa; maana ilikuwa saa ya baridi sana ya usiku, kabla tu ya mapambazuko. Kundi lilikusanyika pale penye moto, na Petro kwa kujiamini bila kujali aliungana nao. Hakutaka kutambuliwa kama mwanafunzi wa Yesu. Kwa kuchanganyika na kundi lile bila kuchukua tahadhari, alitumaini kuchukuliwa kama mmoja wa wale waliokuwa wamemleta Yesu ukumbini.

Lakini pindi mwanga ulipomlika usoni pa Petro, mwanamke aliyekuwa anangoja mlangoni alimtazama. Alikuwa amegundua kwamba aliingia pamoja na Yohana, alitambua mwonekano wa huzuni usoni mwake, na alifikiri **(711)** kwamba atakuwa ni mwanafunzi wa Yesu. Yule mwanamke alikuwa mmoja wa watumishi katika nyumba ya Kayafa, na alikuwa na hamu ya kujua. Alimwambia Petro, "Wewe nawe, je! Hu mwanafunzi mmojawapo wa mtu huyu?" Petro alishtushwa na kuchanganyikiwa; macho ya watu wale waliokuwa pale yalimtazama. Alijifanya kama hakuelewa alichosema yule mwanamke; lakini mwanamke yule aling'ang'aniza, na kuwaambia wale waliokuwa pembeni yake kwamba huyu mtu alikuwa pamoja na Yesu. Petro alihisi kulazimishwa kujibu, na akasema kwa hasira, "Ee mwanamke, simjui." Hii ilikuwa ni mara ya kwanza kwake kukana, na mara jogoo aliwika. Ee Petro, uone aibu kuhusu Bwana wako! Bado kidogo umkane Bwana wako!

Mwanafunzi Yohana, alipoingia katika ukumbi wa hukumu, hakujaribu kuficha ukweli kwamba alikuwa mfuasi wa Yesu. Hakujichanganya na kundi lile baya lililokuwa linamshutumu Bwana wake. Hakuulizwa, maana hakutaka kujipa tabia isiyo yake, na kujiweka katika hatari ya kutiliwa shaka. Alitafuta kona iliyo salama ya kupumzikia isiyoonekana sana kwa lile **(712)** kundi la fujo, lakini karibu na Yesu kwa kadiri ilivyowezekana kwake. Hapa aliweza kuona na kusikia yote yaliyofanyika katika mashtaka ya Bwana wake.

Petro hakutaka kwamba tabia yake halisi ijulikane. Kwa kutaka kuonekana tofauti na alivyo alikuwa amejiweka katika uwanja wa adui, na alikuja kuwa mawindo rahisi ya majaribu. Ikiwa angekuwa ameitwa kupigana kwa ajili ya Bwana wake, angeweza kuwa askari mwenye ujasiri; lakini kidole cha kumbaini kilipoelekezwa kwake, alijithibitisha kuwa mwoga. Wengi ambao hawaogopi kupigana vita moja kwa moja kwa ajili ya Bwana wanasukumwa na mabezo na kuikana imani yao. Kwa kushikamana na wale ambao wanapaswa kuwaepuka, wanajiweka katika njia ya majaribu. Wanamwalika adui kuja kuwajaribu, na wanaongozwa kusema na kutenda yale ambayo katika mazingira mengine wasingekuwa na hatia nayo kamwe. Mwanafunzi wa Kristo ambaye katika siku zetu hizi anaficha imani yake anapopita katika utisho wa mateso au mashutumu humkana Bwana wake vile vile alivyofanya Petro katika ukumbi wa hukumu.

Petro alijaribu kutoonyesha kuvutwa na kesi ya Bwana wake, lakini moyo wake ulisikia milio ya huzuni pindi aliposikia dhihaka za kikatili, na alipoona mabaya aliyokuwa akitendewa. Zaidi ya haya, alishangazwa na

kukasirishwa kwamba Yesu angejidhalilisha Yeye mwenyewe na wafuasi wake kwa kujiweka katika vitendo vile. Kwa nia ya kuficha hisia zake halisi, aliazimia kuungana na watesi wa Yesu katika matani yao katika muda huu usiofaa. Lakini mwonekano wake haukuwa wa asili. Alikuwa anaishi maisha ya uongo, na wakati akijaribu kuzungumza kama mtu asiyejali kuhusika hakuweza kuzuia mwonekano wa huzuni kwa sababu ya lundo la mabaya aliyokuwa anatendewa Bwana wake.

Usikivu wake uliitwa kwa mara ya pili, na alidaiwa tena kuwa ni mfuasi wa Yesu. Sasa alitangaza kwa kiapo akisema, "Simjui mtu huyu." Bado fursa nyingine ilitolewa kwake. Saa moja ilikuwa imepita, wakati mmoja wa watumishi wa kuhani mkuu, ambaye alikuwa na undugu na mtu yule ambaye alikatwa sikio na Petro, alipomwuliza, "Je! Mimi sikukuona wewe bustanini pamoja naye?" "Hakika u mmoja wao, kwa sababu u Mgalilaya wewe," "kwa sababu hata usemi wako wakutambulisha." Petro aliposikia hayo akaruka kwa hasira. Wanafunzi wa Yesu walijulikana kwa lugha yao safi, na ili kuwadanganya kikamilifu wale waliokuwa wanamwuliza, na kuthibitisha tabia aliyotaka kuonyesha, sasa Petro alimkana Bwana wake kwa kulaani na kuapa. Kwa mara nyingine tena jogoo aliwika. Wakati huo Petro alimsikia jogoo, na akakumbuka maneno ya Yesu kwamba, "Kabla ya kuwika jogoo mara mbili, utanikana mara tatu." Marko 14:30.

Wakati viapo vya kushusha hadhi vilipokuwa bado vibichi midomoni mwa Petro, na sauti **(713)** ya jogoo aliyewika ikiwa bado iko masikioni mwa Petro, Mwokozi aligeuka kutoka kwa waamuzi wale wa kesi, na kumwangalia kikamilifu huyu mwanafunzi maskini. Wakati huo huo macho ya Petro yalivutwa kwa Bwana wake. Katika mwonekano ule wa unyenyekevu Petro alisoma upendo wa kina na huzuni, lakini hakukuwa na hasira pale.

Mwonekano wa uso ule wenye mateso uliokuwa umechoka, ile midomo yenye kwikwi, iliyoonekana kuwa yenye uvumilivu na msamaha, ilichoma moyo wa Petro kama mshale. Dhamiri iliamshwa. Kumbukumbu ilifanya kazi. Petro alikumbuka ahadi yake ya saa chache tu zilizokuwa zimepita kwamba angeenda na Bwana wake gerezani na hata katika mauti. Alikumbuka majonzi yake wakati Mwokozi alipomwambia kule katika chumba cha ghorofani kwamba angemkana Bwana wake mara tatu katika usiku ule ule. Petro alikuwa ndipo tu ametangaza kwamba hamjui Yesu, lakini sasa alitambua kwa majonzi ya uchungu jinsi Bwana wake alivyomjua vema, na jinsi alivyokuwa ameusoma moyo wake kwa usahihi, akaona uongo ambao ulikuwa haujulikani hata kwake yeye mwenyewe.

Wimbi la kumbukumbu nyingi lilimjia. Huruma ya Mwokozi, wema na uvumilivu wake, unyenyekevu wake na subira yake kwa wanafunzi wake wenye makosa, - yote hayo yalikumbukwa. Alikumbuka onyo lile kwamba, "Simoni, Simoni, tazama, Shetani amewataka ninyi apate kuwapepeta kama vile ngano; lakini nimekuombea wewe ili imani yako isitindike." Luka 22:31, 32. Alitafakari kwa hofu hali yake ya kutokuwa na shukrani, uongo wake, na uongo wake wa viapo. Kwa mara nyingine zaidi alimtazama Bwana wake, akauona mkono usioheshimu utakatifu ukiwa umeinuliwa ili kumpiga Bwana wake usoni. Akiwa hana uwezo tena wa kustahimili tukio lile, aliondoka ukumbini haraka, moyo wake ukiwa umepasuka.

Aliendelea hadi katika sehemu ya faragha gizani, hakujua na wala hakujali ni wapi. Hatimaye alijikuta yuko ndani ya Gethsemane. Tukio la saa chache zilizopita lilikuja kwa uwazi wake akilini mwake. Uso unaoteseka wa Bwana wake, ukiwa na michirizi ya jasho la damu ukitetemeka kwa masumbuko, ulimjia. Alikumbuka kwa uchungu kwamba Yesu alikuwa amelia na kuhangaika katika kuomba akiwa peke yake, wakati wale ambao wangeungana naye katika saa ile ya kujaribiwa walikuwa wamelala usingizi. Alikumbuka maneno ya Kristo ya kuwaagiza kwamba, "Kesheni, mwombe, msije mkaingia majaribuni." Mathayo 26:41. Alishuhudia tena tukio la ndani ya ukumbi wa hukumu. Ilikuwa ni mateso katika moyo wake uliokuwa unavuja damu kujua kwamba alikuwa ameongeza uzito wa mzigo wa mateso na majonzi ya Bwana wake. Katika eneo la mahali pale pale Yesu alipokuwa ameimwaga nafsi yake kwa mahangaiko akimwomba Baba yake, Petro naye alianguka kwenye uso wake, na kutamani kwamba angekufa.

Katika kusinzia wakati Yesu alipomtaka kukesha na kuomba ndipo Petro alipokuwa ameandaa njia ya dhambi yake kubwa. Kwa kule kulala wakati wa saa ile nyeti, wanafunzi **(714)** walitengeza hasara kubwa. Kristo alijua ukali wa uzoefu mgumu ambao wangepitia. Alijua jinsi ambavyo Shetani angefanya kazi ya kudhoofisha fahamu zao ili kwamba wasiwe tayari kwa ajili ya kujaribiwa. Kwa hiyo ndiyo maana aliwapa onyo. Ikiwa zile saa za bustanini zingetumika kwa kukesha na kuomba, Petro asingeachwa ategemee nguvu zake mwenyewe.

Asingekuwa amemkana Bwana wake. Ikiwa wanafunzi wale wangekesha pamoja na Kristo katika masumbuko yake, wangeandaliwa kuyaona mateso yake msalabani. Wangeelewa kwa kiasi fulani hali ya mahangaiko aliyokuwa nayo. Wangeweza kukumbuka maneno yake yaliyotabiri kuhusu mateso, kifo, na kufufuka kwake. Katikati ya majonzi ya wakati wa saa ya kujaribiwa, miale fulani ya matumaini ingeweza kuangaza katika giza na kuitegemeza imani yao.

Wakati kulipopambazuka, baraza la Sanhedrin lilikutana tena, na kwa mara nyingine Yesu aliletwa katika ukumbi wa baraza. Alikuwa amejitangaza kwamba ni Mwana wa Mungu, na walikuwa wametafsiri maneno yake kwa namna ambayo ingekuwa mashtaka dhidi yake. Lakini hawakuweza kumhukumu kwa hayo, maana wengi wao hawakuwepo katika shauri lile lililofanyika usiku, na hawakuwa wamesikia maneno yake. Na walijua kwamba mahakama ya Kirumi isingeona jambo humo linalostahili kifo. Lakini ikiwa wote wangesikia maneno yale yakirudiwa kutoka midomoni mwake mwenyewe, lengo lao lingefanikiwa. Wangeweza kutafsiri madai yake ya Umasihi kama madai ya kutaka kuasi kisiasa.

Walisema, "Kama wewe ndiwe Kristo, tuambie." Lakini Kristo alibaki kimya. Waliendelea kumwuliza maswali. Hatimaye kwa sauti ya kilio alijibu, "Nijapowaambia, hamtasadiki kabisa. Tena, nikiwauliza, hamtajibu." Lakini ili kwamba waachwe bila kisingizio aliongeza onyo la dhati kwamba, "Lakini tangu sasa Mwana wa Adamu atakuwa ameketi upande wa kuume wa Mungu Mwenyezi."

"Basi, wewe ndiwe Mwana wa Mungu?" waliuliza kwa sauti moja. Akawaambia, "Ninyi mwasema kwamba mimi ndiye." Wakapaza sauti wakisema, "Basi, tuna haja gani tena ya ushuhuda? Maana, sisi wenyewe tumesikia maneno ya kinywa chake."

Na kwa hiyo hukumu ya mara ya tatu ya mamlaka za Kiyahudi ni kwamba Yesu alipaswa afe. Kilichokuwa muhimu sasa, walifikiri, ilikuwa ni Warumi kuidhinisha hukumu hii, na kumtoa mikononi mwao.

Sasa ilikuja awamu ya tatu ya tukio la kumtendea jeuri na dhihaka, mbaya zaidi kuliko hata yale yaliyofanywa na watu wa kawaida. Pale pale mbele ya makuhani na wakuu, tena kwa ruhusa yao hali hii ilifanyika. Kila hisia ya huruma au ubinadamu ilikuwa imetoweka mioyoni mwao. Wakati hoja zao **(715)** zilipokuwa dhaifu, na kushindwa kunyamazisha sauti yake, walikuwa na silaha nyinginezo, kama ambavyo imetumika katika zama zote kuwanyamazisha wazushi, - mateso, matumizi ya mabavu, na kifo.

Wakati hukumu ya Yesu ilipotamkwa na waamuzi, ghadhabu ya kishetani iliwapagaa watu. Mwungurumo wa sauti zao ulikuwa kama ule wa wanyama wa mwitu. Umati ulimrukia Yesu, ukipiga makelele kwamba, Ana hatia, auawe! Isingekuwa askari wa Kirumi, Yesu asingesalia hai mpaka kufikia hatua ya kuangikwa msalabani. Angechanwa vipande-vipande mbele ya waamuzi wale, ikiwa mamlaka ya Kirumi isingeingilia kati, na kutumia silaha kuzuia matumizi ya nguvu ya kundi lile lenye hasira.

Wapagani walikuwa na hasira dhidi ya yule ambaye hakuna shtaka juu yake lililokuwa limethibitishwa. Maafisa wa Kirumi walitangaza kwamba kitendo cha Wayahudi kutamka hukumu juu ya Yesu walikuwa wanaingilia mamlaka ya Warumi, na kwamba ilikuwa hata kinyume cha sheria ya Kiyahudi kumhukumu mtu kifo kwa ushuhuda wake mwenyewe. Kuingilia kati huku kulileta ahueni ya muda katika mwenendo wa jambo lile; lakini viongozi wa Wayahudi walikuwa wote kama wamekufa kwa kukosa upendo na aibu.

Makuhani na wakuu walisahau heshima ya huduma yao, nao wakamtendea mabaya Mwana wa Mungu kwa matusi machafu. Walimdhihaki kuhusu jinsi kuzaliwa kwake kulivyotokea. Walitangaza kwamba kitendo chake cha kujifanya kuwa Masihi kilimfanya astahili kifo kibaya zaidi. Watu waovu kabisa walijihusisha katika kumtendea mabaya Mwokozi. Vazi kuu kuu lilitumiwa kufunika kichwa chake, na watesi wake wakampiga usoni, wakisema, "Ewe Kristo, tufumbulie; ni nani aliyekupiga?" Nguo ile ilipoondolewa, mtu mmoja alimtemea mate usoni mwake.

Malaika wa Mungu waliandika kwa uaminifu kila mtazamo wa jicho la kutusi, kila eneo la kutusi, na kila tendo la kutusi dhidi ya kamanda wao mpendwa. Siku moja watu wale waovu waliomkejeli na kumtemea mate Kristo katika uso wake wenye upole na uchovu watautazama uso ule ukiwa katika utukufu wake, uking’aa sana zaidi ya jua.

## Sura ya 76

# Yuda

Historia ya Yuda inaonyesha mwisho wa huzuni wa maisha ambayo yangeheshimiwa katika mambo ya Mungu. Ikiwa Yuda angekufa kabla ya safari yake ya mwisho kwenda Yerusalemu angechukuliwa kama mtu astahiliye kuwa na nafasi miongoni mwa wale kumi na wawili, na angekuwa mtu ambaye angekumbukwa sana kwa umuhimu wake. Kukataliwa ambako kumemfuata katika karne nyingi hizi kusingekuwepo ikiwa si kwa tabia zilizodhihirika mnamo mwishoni mwa historia yake. Lakini kule kuanikwa ulimwenguni kwa tabia yake ni kwa kusudi maalum. Ni onyo kwa wote ambao, kama yeye, wangesaliti dhamana takatifu.

Muda mfupi kabla ya Pasaka, Yuda alikuwa amerejea tena kufunga mkataba upya na makuhani ili kumkabidhi Yesu mikononi mwao. Halafu ilipangwa kwamba Mwokozi achukuliwe na kupelekwa katika sehemu mojawapo ya faragha kwenda kukesha na kuomba. Tangu ile karamu ya nyumbani kwa Simoni, Yuda alikuwa na fursa ya kutafakari juu ya tendo alilokuwa amefanya makubaliano ya kulitekeleza, lakini kusudi lake lilikuwa lisilobadilika. Kwa vipande thelathini vya fedha – bei ya mtumwa – alimuuza Bwana wa utukufu kwenda katika kudharauliwa na kifo.

Kwa asili Yuda alikuwa anapenda sana fedha; lakini hakuwa ameharibika kiasi cha kutenda tendo kama hili alilotenda. Alikuwa ameendekeza roho ovu ya tamaa ya mali mpaka ikawa ndiyo inayotawala msukumo wa maisha yake. Kupenda mali na utajiri kuliharibu mlinganyo wa upendo wake kwa Kristo. Kwa njia ya kuwa mtumwa wa uovu mmoja alijipeleka kwa Shetani, kwenda kusukumiwa katika marefu ya dhambi.

Yuda alikuwa ameungana na wanafunzi wakati makutano walipokuwa wanamfuata Kristo. Mafundisho ya Mwokozi yaliisukuma mioyo yao wakati walipokawia-kawia njia wakisikiliza maneno yake, yaliyotamkwa katika sinagogi, kando ya bahari, mlimani. **(717)** Yuda aliona wagonjwa, viwete, vipofu, wakimiminika kutoka mijini na katika miji mikubwa kwenda kwa Yesu. Aliona wanaokufa wakilazwa miguuni pake. Alishuhudia matendo makuu ya Mwokozi katika kuwaponya wagonjwa, akifukuza pepo, na kufufua waliokufa. Alihisi ndani yake binafsi ule uwezo wa Kristo. Aligundua kwamba mafundisho ya Kristo ni ya kiwango cha juu kuliko yote aliyokuwa amepata kusikia. Alimpenda yule Mwalimu Mkuu, naye akatamani kuwa pamoja naye. Alihisi hamu ya kubadilishwa tabia yake na maisha yake, na alitumaini kupata jambo hilo kwa kujiunganisha na Yesu. Mwokozi hakumkataa Yuda. Alimpa nafasi miongoni mwa wale kumi na wawili. Alimwamini kufanya kazi ya uinjilisti. Alimjalia uwezo wa kuponya wagonjwa na kufukuza pepo. Lakini Yuda hakufika mahali pa kujisalimisha kikamilifu kwa Kristo. Hakuachana na tamaa za mambo ya ulimwengu au ile hali yake ya kupenda pesa. Wakati alikubali nafasi ya kuwa mtenda kazi wa Kristo, hakujileta mahali pa kuumbwa upya na mbingu. Alihisi kwamba anaweza kusalia na maoni na mtazamo wake, naye alipalilia mwelekeo wa kukosoa na kulaumu.

Yuda aliheshimika sana miongoni mwa wanafunzi, na alikuwa na ushawishi mkubwa kwao. Yeye mwenyewe alijiona wa hali ya juu kwa sababu ya uwezo wake, na aliwaona wenzake kama watu wa hali ya chini sana kwake kwa uwezo na katika kufanya maamuzi. Alidhani kwamba, Walikuwa hawaoni fursa na kutumia manufaa ya mazingira yaliyokuwepo. Aliona kwamba kamwe kanisa lisingestawi ikiwa watu hawa wasioona mbali ndio viongozi humo. Petro alikuwa na ushupavu; angefanya jambo bila tahadhari ya kujali. Yohana, aliyekuwa ndiye mwenye hazina ya ile kweli iliyotoka midomoni mwa Kristo, alitazamwa na Yuda kama mtu asiyejua mambo ya uhasibu. Mathayo, ambaye mafunzo aliyosomea yalimfundisha kuwa sahihi katika mambo yote, alikuwa makini mno katika mambo ya uaminifu, na wakati wote alikuwa anatafakari maneno ya Kristo, na hivyo akazama katika hayo kiasi kwamba, kwa mujibu wa mawazo ya Yuda, hakuwa na uwezo wa kuaminiwa kufanya shughuli za haraka zinazohitaji mtu anayeona mbali. Hivyo ndivyo Yuda alivyowajumuisha wanafunzi wote, na kujigamba kwamba ikiwa si uwezo wake kama msimamizi mara nyingi kanisa lingeingia katika utata na kutokuwa na hali nzuri. Yuda alijiona kama mtu anayeweza, ambaye asingepitwa na mtu. Katika kujikadiria kwake mwenyewe alikuwa ndiye heshima ya kazi, na kwa namna hiyo alijionyesha yeye mwenyewe.

Yuda alikuwa kipofu asiyeona udhaifu wa tabia yake, na Kristo alimweka mahali ambapo angepata fursa ya kuona hali hiyo na kuisahihisha. Akiwa kama mtunza hazina wa wanafunzi, aliitwa ili kulipatia kundi lile dogo la wenzake mahitaji yao, na kuwapatia ahueni maskini kwa kukidhi mahitaji yao. Walipokuwa katika chumba cha

Pasaka Yesu alimwambia, "Uyatendayo yatende upesi" (Yohana 13:27), wanafunzi wakadhani kwamba amemtaka **(718)** akanunue mahitaji kwa ajili ya karamu ile, awapatie maskini mahitaji fulani. Katika kuwahudumia wengine, Yuda angeweza kukuza roho isiyo ya ubinafsi. Lakini wakati anasikiliza mafundisho ya Kristo kila siku na kushuhudia maisha yake yasiyo ya ubinafsi, Yuda aliendelea na mwenendo wa kujipendelea binafsi. Kiasi kidogo kilichokuwa kinakuja mikononi mwake kiliendelea kuwa jaribu endelevu kwake. Mara nyingi alipofanya huduma ndogo kwa Kristo, au kutumia muda kwa ajili ya utumishi wa kidini, alijilipa kutoka katika fedha hii ndogo isiyotosha. Machoni pake sababu hizi zisizo sahihi zilimpa kisingizio cha kitendo chake hicho; lakini machoni pa Mungu alikuwa mwizi.

Kauli ya Kristo iliyokuwa inarudiwa-rudiwa kwamba ufalme wake si wa ulimwengu huu ilimchukiza Yuda. Alikuwa amechora mstari mahali ambapo alitarajia kwamba Kristo angefanya kazi kwa kuufuata huo. Alikuwa amepanga kwamba Yohana Mbatizaji aokolewe kutoka gerezani. Lakini tazama, Yohana aliachwa kule gerezani mpaka akakatwa kichwa. Na Yesu, badala ya kuonyesha haki yake ya kifalme na kulipiza kisasi kwa ajili ya kifo cha Yohana, alielekea huko maeneo ya pembezoni. Yuda alitaka vita ya moja kwa moja. Alifikiri kwamba ikiwa Yesu asingewazuia wanafunzi kutekeleza mipango yao, kazi ingefanikiwa zaidi. Aliona hali ya kuongezeka kwa uadui kutoka kwa viongozi wa Wayahudi, na akaona upinzani wao haukufanyiwa kazi ipasavyo wakati walipotaka kwa Kristo ishara kutoka mbinguni. Moyo wake ulikuwa wazi katika kutokuamini, na yule adui alimpatia mawazo ya kuwa na maswali na kuasi. Aliwaza hivi, Kwa nini Yesu alikuwa anazungumzia sana mambo yanayokatisha tamaa? Kwa nini alitabiri majaribu na mateso kwa ajili yake na kwa wanafunzi wake? Matarajio ya kupata nafasi ya juu katika ufalme mpya yalimfanya Yuda kuipanga njia ya kazi ya Kristo. Je! Matumaini yake yangefadhaishwa? Yuda hakuwa amekubali kwamba Yesu si Mwana wa Mungu; lakini alikuwa anahoji, na kutafuta kupata ufafanuzi kuhusu matendo yake makuu.

Licha ya mafundisho yale ya Mwokozi, Yuda alikuwa anaendeleza wazo kwamba Kristo angetawala kama mfalme katika Yerusalemu. Wakati wa kuwalisha wale elfu tano alijaribu kulileta hili. Katika tukio hili Yuda alisaidia kugawa chakula kwa makutano wale wenye njaa. Alikuwa na fursa ya kuona manufaa aliyokuwa na uwezo nayo kuwapatia wengine. Alihisi hali ya kuridhishwa ambayo wakati wote hupatikana katika kumtumikia Mungu. Alisaidia kuwaleta wagonjwa kwa Yesu kutoka katikati ya makutano. Aliona kwamba ni nafuu gani, raha na furaha gani, inayokuja katika moyo wa mwanadamu kupitia nguvu ya uponyaji ya Mponyaji Mkuu. Alipaswa kuwa ameelewa njia za Kristo. Lakini alipofushwa na tamaa zake mwenyewe za ubinafsi. Yuda ndiye aliyepaswa kunufaika na ufahamu ulioletwa na mwujiza wa mikate. Lakini yeye ndiye aliyeanzisha **(719)** mkakati wa kumchukua Kristo kwa nguvu na kumfanya kuwa mfalme. Matarajio yake yalikuwa makubwa mno. Mfadhaiko wake ulikuwa mchungu.

Mazungumzo ya Kristo katika sinagogi kuhusu mkate wa uzima yalikuwa ndiyo hatima iliyogeuza historia ya Yuda. Alisikia maneno haya: "Msipoula mwili wake Mwana wa Adamu na kuinywa damu yake, hamna uzima ndani yenu." Yohana 6:53. Aliona kwamba Kristo alikuwa anatoa mali ya kiroho kuliko ya kiulimwengu. Alijiona kama mtu anayeona mbali, na alifikiri kwamba aliweza kuona kuwa Kristo asingekuwa na heshima, na ya kwamba asingetoa vyeo vya juu kwa wafuasi wake. Aliazimia kutojifungamanisha na Kristo kwa karibu bali kwamba afikirie kujitenga. Angekuwa mtazamaji. Na kweli akawa mtazamaji.

Tangu wakati huo alionyesha mashaka ambayo yaliwachanganya wanafunzi. Alianzisha hoja za upinzani na upotoshaji, akirudia hoja zilizosisitizwa na waandishi na Mafarisayo dhidi ya madai ya Kristo. Yuda alitafsiri matatizo yote na misalaba midogo na mikubwa, ugumu na vikwazo vilivyoonekana kuzuia kazi ya injili kama ushahidi dhidi ya ukweli. Alikuwa analeta maneno ya Maandiko ambayo yalikuwa hayahusiani na ukweli uliokuwa unafundishwa na Kristo. Maandiko haya, ambayo yametenganishwa na muktadha wake sahihi, yaliwatatanisha wanafunzi, na yaliongeza hali ya mfadhaiko iliyokuwa imewasonga wakati wote. Lakini haya yote yalifanywa na Yuda katika hali ya kuonekana kwamba alikuwa makini. Na wakati wanafunzi walikuwa wanajifunza kutafuta ushahidi wa kuthibitisha maneno ya Mwalimu Mkuu, Yuda yeye aliwaongoza kama wasiojitambua katika mwelekeo mwingine. Hivyo kwa njia ya kidini, na mwonekano wa hekima, alikuwa anaonyesha mada katika nuru tofauti na ile aliyowapa Yesu, na kuunganisha kwenye maneno ya Yesu maana ambayo siyo aliyoonyesha. Wakati wote mapendekezo yake yaliamsha hamu ya matakwa ya ulimwengu huu, na kwa njia hiyo akawageuza wanafunzi kutoka katika mambo muhimu ambayo walipaswa kutafakari. Kwa ujumla, yale mashindano kwamba ni yupi kati yao atakuwa mkubwa kuliko wote yalikuwa yanaamshwa na Yuda.

Wakati Yesu alipomwambia yule kijana tajiri na mtu mkubwa sharti la kuwa mwanafunzi, Yuda alihuzunishwa. Alidhani kwamba kuna kosa lilikuwa limefanyika. Ikiwa watu kama huyu mtu mkubwa wangeweza kuunganishwa na kundi la wanaoamini, wangesaidia kuipeleka mbele kazi ya Kristo. Alifikiri hivi, Ikiwa Yuda angewekwa kuwa mshauri, angependekeza mambo mengi ya manufaa kwa ajili ya kanisa hili dogo. Kanuni zake na njia zake zingetofautiana kwa namna fulani na hizi za Kristo, katika mambo haya alifikiri kwamba yeye ni mwerevu kuliko Kristo.

**(720)** Katika yote yale Kristo aliwaambia wanafunzi wake kwamba kulikuwa na kitu ambacho, moyoni, Yuda hakukubaliana nacho. Katika ushawishi wake chachu ya kutoridhika ilikuwa inafanya kazi yake haraka. Wanafunzi wale hawakuona nguvu halisi iliyokuwa ndani ya hali hii; lakini Yesu aliona kwamba Shetani alikuwa anasafirisha tabia zake kwenda kwa Yuda, na hivyo kufungua mfereji wa kuutumia kuwashawishi na wanafunzi wengine. Mwaka mmoja kabla ya kusalitiwa, Kristo alilisema hili, kwamba, "Je! Mimi sikuwachagua ninyi Thenashara, na mmoja wenu ni shetani?" Yohana 6:70.

Lakini Yuda hakufanya upinzani wa wazi, wala hakuonekana kama kuhoji mafundisho ya Mwokozi. Hakufanya manung'uniko ya wazi mpaka wakati wa karamu nyumbani kwa Simoni. Mariamu alipoitia mafuta miguu ya Mwokozi, Yuda alidhihirisha mwelekeo wake mbaya. Alipokemewa na Yesu moyo wake ulionekana kama umerudi katika kuwa na hasira. Kiburi kilichojeruhiwa na hamu ya kulipiza kisasi vilivuka vizuizi, na tamaa iliyomshikilia kwa muda mrefu ilimkalia. Huu utakuwa ndio uzoefu wa kila mmoja anayeng'ang'ania kucheza na dhambi. Chembechembe za ufidhuli ambazo hazipingwi na kushindwa, huleta mwitikio kwa majaribu ya Shetani, na moyo hushikiliwa mateka katika matakwa yake.

Lakini Yuda alikuwa hajawa na moyo mgumu kikamilifu. Hata alipokuwa ameahidi mara mbili kumsaliti Mwokozi, kulikuwa bado na fursa ya kutubu. Katika chakula cha Pasaka Yesu alithibitisha uungu wake kwa kufunua makusudi ya msaliti. Kwa upendo alimjumuisha Yuda katika huduma aliyoifanya kwa wanafunzi wake. Lakini wito huo wa mwisho wa upendo haukusikiwa. Halafu hatima ya Yuda ikaamuliwa, na miguu ile ambayo Yesu alikuwa ameiosha iliondoka na kwenda kufanya kazi ya usaliti.

Yuda alifikiri kwamba ikiwa Yesu angesulibishwa, tukio hilo lingepita bure. Kitendo chake cha kumsaliti Mwokozi kisingebadilisha matokeo. Ikiwa Yesu asingekuwa wa kufa, kitendo kile kingemlazimisha tu kujiokoa. Katika matukio yote, Yuda yeye angenufaika na mpango ule wa werevu. Alihesabu kwamba alikuwa amefanya ujanja mkali kwa mapatano yale ya kumsaliti Bwana.

Hata hivyo Yuda hakuamini kwamba Kristo angejiruhusu kutiwa nguvuni. Katika kule kumsaliti, kusudi la Yuda lilikuwa ni kumfundisha Kristo somo. Alitaka kufanya kazi ambayo ingemfanya Mwokozi tangu pale awe mwangalifu na kumchukulia kwa heshima anayostahili. Lakini Yuda hakujua kwamba alikuwa anamtoa Yesu ili afe. Ni mara ngapi, kadiri Mwokozi alivyofundisha kwa mifano, waandishi na Mafarisayo walivyochukuliwa na vielelezo vyake kwenda mbali! Ni mara ngapi walikuwa wamejitamkia hukumu wao wenyewe! Mara nyingi wakati ukweli ulipoletwa mahali pake mioyoni mwao, walikuwa wamejazwa na ghadhabu, na walikuwa wameokota mawe ili kumpiga; **(721)** lakini mara kwa mara alikuwa anawatoroka. Kwa kuwa alikuwa amekwepa mitego mingi, Yuda alidhani, kwa hakika asingejiruhusu kuchukuliwa.

Yuda aliamua kuliweka suala hilo kwenye jaribio. Ikiwa Kristo alikuwa Masihi kweli, watu ambao alikuwa amewatendea mengi, wangemkusanyikia, na wangemtangaza kuwa mfalme. Hili lingetuliza daima mawazo ya watu wengi ambayo yalikuwa katika utata. Yuda angejipatia sifa ya kumweka mfalme kwenye kiti cha enzi cha Daudi. Na kitendo hiki kingempatia nafasi ya cheo cha kwanza, baada tu ya kile cha Kristo, katika ufalme mpya.

Mwanafunzi huyu wa uongo alitekeleza sehemu yake ya kumsaliti Yesu. Kule bustanini, alipowaambia viongozi wa lile kundi lenye fujo kwamba, "Nitakayembusu, huyo ndiye; mkamateni." (Mathayo 26:48), aliamini kabisa kwamba Kristo angewatoka mikononi. Halafu sasa kama wangemlaumu, angesema kwamba, Kwani sikuwaambia mmkamate?

Yuda aliwaona wakamataji wa Kristo, kwa kutekeleza maneno yake, wakimfunga barabara. Kwa mshangao alimwona Mwokozi akijiruhusu kuchukuliwa na kupelekwa. Akiwa na wasiwasi alimfuata kutoka bustanini kwenda kwenye mashtaka mbele ya wakuu wa Wayahudi. Kila wakati alitarajia kwamba angewashangaza adui zake, kwa kuonekana mbele yao akiwa kama Mwana wa Mungu, na kuangusha njama zao na nguvu zao zote.

Lakini kadiri saa moja baada ya nyingine ilivyopita, na Yesu akijisalimisha katika matendo mabaya yote aliyotendewa, woga wa kutisha ulimjia msaliti huyu kwamba alikuwa amemwuza Bwana wake katika kifo.

Kadiri mwenendo wa mashtaka na mateso ya Kristo ulivyokaribia mwisho, Yuda hakuweza tena kuvumilia maumivu ya hatia ya nafsi yake. Ghafla sauti kubwa ilivuma katika ukumbi, ikipeleka miale ya hofu katika mioyo ya watu wote, ikisema: Hana hatia; mwachie huru, Ee Kayafa!

Umbile refu la Yuda lilionekana likipenya katikati ya watu waliokuwemo mle. Uso wake ulikuwa umefura, na matone makubwa ya jasho yalikuwa usoni pake. Akikimbia penye kiti cha hukumu, alitupa chini **(722)** mbele ya kuhani mkuu vile vipande thelathini vya fedha vilivyokuwa malipo ya kumsaliti Bwana wake. Akilishikilia joho la Kayafa kwa shauku, alimsihi amwachie Yesu awe huru, akitangaza kwamba hakufanya lolote linalostahili kifo. Kwa hasiri Kayafa alijitikisa na kumsukumia mbali, lakini alikuwa amechanganyikiwa, na hakujua la kusema. Udanganyifu wa makuhani uliwekwa wazi. Ilibainika kwamba walikuwa wamemhonga mwanafunzi yule ili amsaliti Bwana wake.

Yuda akalia tena akisema, "Nalikosa nilipoisaliti damu isiyo na hatia." Lakini kuhani mkuu aliyekuwa amerejesha ujasiri, alijibu kwa kiburi, "Basi, haya yatupasani sisi? Yaangalie haya wewe mwenyewe." Mathayo 27:4. Wale makuhani walikuwa na ya nia kumfanya Yuda kuwa nyenzo yao; lakini walidharau udhaifu wake. Wakati alipowarudia akiungama, walimkataa kwa dharau.

Sasa Yuda alijitupa miguuni pa Yesu, akimkiri kuwa Mwana wa Mungu, na akimwomba ajiokoe. Mwokozi hakumkaripia msaliti wake. Alijua kwamba Yuda hakutubu; ungamo lake lililazimishwa na moyo wake wa hatia kwa hofu ya kujua habari ya hukumu iliyokuwa inamjia, lakini hakuhisi majonzi ya kina yanayovunja moyo kwamba alikuwa amemsaliti Mwana wa Mungu asiye na waa, na kumkana Aliye Mtakatifu wa Israeli. Lakini Yesu hakutamka neno lolote la kumhukumu. Alimtazama Yuda kwa huruma, na kusema, Nalikuja ulimwenguni kwa ajili ya saa hii.

Minong'ono ya mshangao ilisikika katika ukumbi wote. Kwa kushangazwa walimwona Kristo akimvumilia aliyemsaliti. Kwa mara nyingine walipitiwa na roho ya usadikisho kwamba mtu huyu alikuwa zaidi ya mwenye mwili wa kufa. Ila waliuliza kwamba, Lakini ikiwa ni Mwana wa Mungu, kwa nini hakujiokoa mwenyewe kutoka katika vifungo vyake na kuonyesha ushindi juu ya hao wanaomshtaki?

Yuda aliona kwamba maombi yake hayana mafanikio, na aliondoka haraka katika ukumbi ule akilalama kwamba, Nimechelewa! Nimechelewa! Alihisi kwamba asingesalia kuwa hai amshuhudie Yesu akisulibiwa, na kwa uchungu aliondoka akajinyonga.

Baadaye siku ile ile, katika njia itokayo katika ukumbi wa Pilato kwenda Kalvari, kulikuwa na sauti nyingi na makelele ya kundi la waovu waliokuwa wakimpeleka Yesu mahali pa kusulibiwa. Walipopita sehemu ya pambeni kidogo, chini ya mti uliokauka, waliona mwili wa Yuda. Lilikuwa tukio la kusikitisha kuona. Uzito wake ulikuwa umekata kamba aliyokuwa amejinyongea kwenye mti. Katika kule kuanguka, mwili wake ulifumuka vibaya, na sasa mbwa walikuwa wanautafuna. Mabaki ya mwili wake yalizikwa mara ili yasiendelee kuonekana; lakini katika kundi lile dhihaka zilipungua, na wengi walionyesha nyuso zenye huzuni ndani yao. Ilionekana kama mapatilizo yalikuwa yameanza kuwajilia tayari wale waliokuwa na hatia ya damu ya Yesu.

## Sura ya 77

# Katika Ukumbi wa Hukumu wa Pilato

[Sura hii imejengwa katika Mathayo 27:2 , 11-31; Marko 15:1-20; Luka 23:1-25; Yohana 18:28-40; 19:1-16.]

Ndani ya ukumbi wa Pilato, liwali wa Kirumi, Kristo anasimama akiwa amefungwa kama mfungwa. Pande zake zote kuna askari walinzi, na ukumbi unajaa haraka watazamaji. Nje tu ya lango kuna waamuzi wale wa Sanhedrin, makuhani, wakuu, na makundi ya watu wa fujo.

Baada ya kumtangaza Yesu kuwa na hatia, baraza la Sanhedrini limekuja kwa Pilato kupata idhini ya hukumu ile na kuitekeleza. Lakini hawa maafisa wa Kiyahudi hawakuweza kuingia katika ukumbi wa hukumu wa Warumi. Kulingana na sheria zao wangenajisika, na hivyo kuzuiwa kushiriki sherehe za Pasaka. Katika upofu wao hawakuona kwamba chuki ya kuua ilikuwa imeinajisi mioyo yao. Hawakuona kwamba Kristo alikuwa mwana-kondoo halisi wa Pasaka, na ya kwamba, kwa kuwa walikuwa wamemkataa, sikukuu ile kubwa ilikuwa imekosa maana kwao.

Mwokozi alipoletwa katika ukumbi wa hukumu, Pilato hakumwangalia kwa macho ya kirafiki. Gavana huyu wa Kirumi alikuwa ameitwa kwa haraka kutoka katika chumba chake cha kulala, na aliazimia kufanya kazi yake haraka iwezekanavyo. Alikuwa amejiandaa kushughulika na mtuhumiwa huyu kwa **(724)** ukali wa kihakimu. Akijionyesha kuwa na mwonekano wa ukali, aligeuka ili kuona aina ya mtu ambaye alipaswa kumhukumu, kiasi kwamba alikuwa amelazimika kuitwa kutoka katika hali ya kupumzika wakati ule wa mapema vile. Alijua kwamba lazima awe mtu fulani ambaye mamlaka za Kiyahudi zilikuwa na hamu kwamba achunguzwe na kuhukumiwa haraka.

Pilato aliwatazama wale watu waliomleta Yesu kumshtaki, na halafu macho yake ya kiupelelezi yalielekea kwa Yesu. Alikuwa na wajibu wa kushughulikia aina zote za uhalifu; lakini hapo kabla haikuwahi kutokea kuletwa kwake mtu mwenye mwonekano wa wema na utauwa kama huyu. Usoni mwake hakuona dalili yoyote ya hatia, hakuna mwonekano wa hofu, hakuna kiburi wala ukaidi. Alimwona mtu aliye mtulivu na mwenye mwonekano wa heshima, ambaye sura yake haikuonyesha dalili zozote za uhalifu, bali muhuri ya mbinguni.

Mwonekano wa Kristo ulivuta hisia za Pilato. Hali yake ya asili iliamshwa. Alikuwa amesikia habari za Yesu na kazi zake. Mke wake alikuwa amemwambia jambo fulani kuhusu matendo ya ajabu yaliyofanywa na nabii yule wa Galilaya, aliyeponya wagonjwa na kufufua waliokufa. Sasa hili lilirejea kama ndoto katika mawazo ya Pilato. Alikumbuka tetesi alizokuwa amesikia kutoka kwa vyanzo kadhaa. Aliamua kudai Wayahudi waeleze mashtaka yao dhidi ya mfungwa yule.

Alisema, Mtu huyu ni nani, na kwa nini mmemleta? Mna tuhuma gani dhidi yake? Wayahudi wale waliteteleka. Wakijua kwamba wasingeweza kuchanganua mashtaka yao dhidi ya Kristo, hawakupenda mwenendo wa kesi uwe wa hadhara. Walijibu kwamba alikuwa mdanganyifu aitwaye Yesu wa Nazareti.

Pilato aliuliza tena, "Ni mashtaka gani mnayoleta juu ya mtu huyu?" Makuhani hawakujibu swali lake, lakini katika maneno ambayo yalionyesha kutopendezwa, walisema, "Kama huyu asingekuwa mtenda mabaya, tusingemleta kwako." Wakati watu wanaounda Sanhedrin, watu wa juu wa taifa, wanapokuletea mtu wanayesema kwamba anastahili kifo, kuna hitaji tena la kutaka walete mashtaka dhidi yake? Walitumaini kumshawishi Pilato kwa kutumia hali ya umuhimu wao, na hivyo kumfanya akubali ombi lao bila kufanya uchunguzi mwingi. Walikuwa na hamu ya kupata idhini ya hukumu yao; maana walijua kwamba watu ambao walikuwa wameshuhudia matendo ya ajabu ya Kristo wangesimulia habari inayotofautiana na yale ya kwao ya kutengeneza.

Wale makuhani walidhani kwamba kwa kumtumia Pilato aliyekuwa dhaifu na anayeyumba katika maamuzi wangeendelea na mipango yao bila shida. Kabla ya hapa alikuwa ametia sahihi idhini ya kifo kwa haraka, akiwahukumu kifo watu ambao waliwajua kwamba hawakustahili kifo. Katika mtazamo wake maisha ya mshtakiwa hayakuwa **(725)** na thamani kubwa; iwe alikuwa sahihi au akiwa na hatia hakukuwa na madhara.

Wale makuhani walidhani kwamba Pilato angeidhinisha adhabu ya kifo kwa Yesu bila kumpa nafasi ya kusikilizwa. Walitafuta nafasi hiyo kwa kutegea fursa ya tukio la sikukuu kubwa ya kitaifa.

Lakini kulikuwa na kitu ndani ya mshtakiwa yule kilichomzuia Pilato kufanya hivyo. Hakuthubutu kufanya jambo hilo. Aligundua makusudi ya makuhani. Alikumbuka jinsi ambavyo, muda si mrefu, Yesu alikuwa amemfufua Lazaro, mtu aliyekuwa amekufa kwa siku nne; na aliazimu kujua, kabla ya kutia sahihi hukumu ile, mashtaka yake yalikuwa ni nini, na ikiwa yangewezekana kuthibitishwa.

Ikiwa hukumu yenu inajitosheleza, kwa nini mmemleta kwangu? Aliuliza. "Haya! Mtwaeni ninyi, mkamhukumu kwa ile torati yenu!" Walipobanwa hivyo makuhani wakasema kwamba walikuwa wameshaipitisha hukumu ile, lakini bado tu kupata hukumu ya Pilato ya kuhalalisha hukumu yao. Pilato aliuliza, Hukumu yenu ni ipi? Wakajibu kwamba, Hukumu ya kifo; lakini ni kinyume cha sheria kwa sisi kumwua mtu. Walimwomba Pilato azingatie neno lao kuhusu hatia ya Kristo, na atekeleze hukumu yao. Walikuwa tayari kuwajibika kwa matokeo yoyote.

Pilato hakuwa hakimu wa haki wala mwenye utambuzi; lakini ingawa alikuwa dhaifu wa mambo ya uadilifu, alikataa kukubali ombi lao hili. Hakuwa tayari kumhukumu Kristo mpaka mashtaka yaletwe dhidi yake.

Makuhani walikuwa katika utata. Waliona kwamba lazima wafiche unafiki wao chini ya siri nzito. Lazima wasiruhusu ionekane kwamba Kristo amekamatwa kwa sababu za kidini. Ikiwa hili lingesemwa kama sababu, mashtaka yao yasingekuwa na uzito kwa Pilato. Lazima wafanye ionekane kwamba Yesu alikuwa anatenda kinyume cha sheria ya nchi; hapo ndipo angeadhibiwa kama mhalifu wa kisiasa. Ghasia na upinzani dhidi ya serikali ya Kirumi vilikuwa vikiibuka mara kwa mara miongoni mwa Wayahudi. Warumi walikuwa wameshughulika na upinzani huu kwa ukali, walikuwa wanafuatilia wakati wote kwa lengo la kukomesha kila kitu ambacho kingeonekana kutaka kusababisha vurugu za upinzani.

Siku chache tu kabla ya hii Mafarisayo walikuwa wamejaribu kumtega Kristo kwa swali kwamba, "Ni halali tumpe Kaisari kodi?" Lakini Yesu alikuwa amefunua unafiki wao. Warumi waliokuwepo walikuwa wameona jinsi wenye njama wale walivyoshindwa vibaya, na mfadhaiko wao alipowajibu kwamba, "Vya Kaisari mpeni Kaisari, na vya Mungu mpeni Mungu." Luka 20:22-25.

Sasa makuhani walifikiri wafanye ionekane kwamba kwenye tukio lile Kristo **(726)** alikuwa amefundisha kile walichotamani afundishe. Katika msimamo wao huo mkali waliwaitisha mashahidi wa uongo kuja kuwasaidia, "Wakaanza kumshtaki, wakisema, Tumemwona huyu akipotosha taifa letu, na kuwazuia watu wasimpe Kaisari kodi, akisema kwamba yeye mwenyewe ni Kristo, mfalme." Shutuma tatu hizi, kila moja ikiwa haina msingi. Makuhani walijua hili, lakini walitaka kusema uongo alimradi tu wafikie lengo walilolitaka.

Pilato aliligundua kusudi lao. Hakuamini kwamba mshtakiwa yule alikuwa amefanya njama dhidi ya serikali. Mwonekano wake wa upole na unyenyekevu ulikuwa haukubaliani kabisa na mashtaka yale. Pilato alishawishika kuamini kwamba njama kubwa zilikuwa zimefanywa ili kumwangamiza mtu asiye na hatia aliyesimama kama kikwazo kwa wenye heshima wa Kiyahudi. Akimgeukia Yesu alimwuliza, "Je! Wewe ni Mfalme wa Wayahudi?" Mwokozi alijibu, "Wewe wasema." Na aliposema tu, wapinzani wake waliinuka kama vile walikuwa wamemlikiwa na mwale wa jua.

Waliposikia jibu lake, Kayafa na wale waliokuwa pamoja naye walimwita Pilato ashuhudie kwamba Yesu alikuwa amekiri kutenda uhalifu ule aliokuwa anashtakiwa. Kwa vilio vya makelele, makuhani, waandishi, na wakuu walidai kwamba ahukumiwe kufa. Makelele yale yalipokelewa na kundi la watu wa fujo, na makelele yakawa makubwa sana. Pilato alichanganyikiwa. Kwa kuona kwamba Yesu hakuwajibu lolote washtaki wake, Pilato alimwambia, "Hujibu neno? Tazama ni mambo mangapi wanayokushtaki! Wala Yesu hakujibu neno tena."

Akiwa amesimama nyuma ya Pilato, mahali anapoonwa na wote walio katika ukumbi wa mahakama, Kristo alisikia mabaya yote; lakini hakujibu neno lolote kuhusu mashtaka yote ya uongo waliyotoa dhidi yake. Mwonekano wake wote ulionyesha ushahidi wa kutokuwa na hatia. Alisimama bila kutishwa na ghadhabu ya mawimbi yaliyokuwa yanampiga. Ilikuwa kama vile mawimbi ya ghadhabu yao, yaliyokuwa yakipanda juu zaidi na zaidi, yakiwa kama mawimbi ya bahari iliyochafuka, yalipiga, lakini hayakumgusa. Alisimama akiwa kimya,

lakini ukimya wake ulikuwa unaongea kitu. Ulikuwa kama nuru ing'aayo kutoka katika utu wa ndani kwenda nje ya mtu.

Pilato alishangazwa na mwonekano wake. Aliuliza, Je! Huyu mtu hatishwi na mwenendo wa kesi hii kwa kuwa hajali kuokoa maisha yake? Kadiri alivyomtazama Yesu, akistahimili matusi na dhihaka pasipo kurudisha neno, alifikiri kwamba huyu hawezi kuwa asiye na haki kama vile makuhani walivyokuwa wanalazimisha. Akitarajia kupata ukweli halisi kutoka kwa Yesu mwenyewe na kuepuka ghasia za umati wa watu, Pilato aliienda pamoja naye pembeni, na akamwuliza tena, "Wewe ni Mfalme wa Wayahudi?"

Yesu hakujibu swali hili moja kwa moja. Alijua kwamba Roho **(727)** Mtakatifu alikuwa anashughulika na Pilato, na alimpatia fursa ya kukiri usadikisho wake. Yesu alimwuliza, "Wewe wasema hivi kwa nafsi yako, au watu wengine walikuambia habari zangu?" maana yake ni kwamba, kilichosukuma swali lile la Pilato kilikuwa ni mashtaka ya makuhani, au nia ya kupokea nuru kutoka kwa Kristo? Pilato alielewa maana ya swali la Kristo, lakini kiburi kilipanda moyoni mwake. Hakuwa tayari kukiri usadikisho uliokuwa ukimsukuma. Akasema, "Ama! Ni Myahudi mimi! Taifa lako na wakuu wa makuhani ndio waliokuleta kwangu. Umefanya nini?"

Fursa ya dhahabu ya Pilato ilikuwa imepita. Lakini bado Yesu hakumwacha bila nuru zaidi. Wakati akiwa hakujibu swali la Pilato moja kwa moja, alitamka kwa uwazi kazi yake ya utume. Alimpa Pilato kuelewa kwamba Yeye hakuwa anatafuta kiti cha enzi cha duniani.

Kristo alisema, "Ufalme wangu sio wa ulimwengu huu. Kama ufalme wangu ungekuwa wa ulimwengu huu, watumishi wangu wangenipigania, nisije nikatiwa mikononi mwa Wayahudi. Lakini ufalme wangu sio wa hapa. Basi Pilato akamwambia, Wewe u mfalme basi? Yesu akajibu, Wewe wasema, kwa kuwa mimi ni mfalme. Mimi nimezaliwa kwa ajili ya haya, na kwa ajili ya haya mimi nalikuja ulimwenguni, ili niishuhudie kweli. Kila aliye wa hiyo kweli hunisikia sauti yangu."

Kristo alithibitisha kwamba neno lake lilikuwa ndani yake ni ufunguo ambao ungewafungulia siri wale waliojiandaa kuyapokea. Lilikuwa na nguvu ndani yake, na hii ndiyo iliyokuwa siri ya kuenea kwa ufalme wake wa ukweli. Alitamani kwamba Pilato aelewe kwamba hali yake ya kuangamia ingejengwa upya kwa kuupokea na kuutumia ukweli.

Pilato alikuwa na hamu ya kujua ukweli. Akili yake ilichanganyikiwa. Kwa hamu aliyakamata maneno ya Mwokozi, na moyo wake ulihamasishwa na hamu kubwa ya kutaka kujua ukweli ulikuwa upi, na jinsi gani angeweza kuupata. Akauliza, "Kweli ni nini?" Lakini hakusubiri jibu. Ghasia iliyokuwa nje ilimkumbusha kile kilichokuwa kinaendelea wakati ule; maana makuhani walikuwa wanadai hatua za haraka zichukuliwe. Alienda nje kwa Wayahudi, akatangaza kwa msisitizo kwamba, "Mimi sioni hatia yoyote kwake."

Maneno haya yatokayo kwa hakimu mpagani yalikuwa ya kemeo kwa udanganyifu na uongo wa wakuu wa Israeli ambao walikuwa wanamshtaki Mwokozi. Pindi makuhani na wazee waliposikia maneno haya ya Pilato, kufadhaishwa kwao na ghadhabu yao havikujua mpaka. Walikuwa wametafuta na kusubiri fursa hii. Sasa walipoona dalili za Yesu kuachiwa huru, walionekana kuwa tayari kumchana vipande-vipande. Kwa sauti walimpinga Pilato, na walimtishia kwamba angepingana na serikali ya Kirumi. Walimshutumu **(728)** kwa kukataa kumhukumu Yesu, ambaye, walithibitisha, kwamba alikuwa amejiweka kuwa kinyume cha Kaisari.

Sasa sauti za hasira zilisikika, zikitangaza kwamba ushawishi wa Yesu wa kuhamasisha uasi ulikuwa unajulikana katika nchi yote. Makuhani walisema, "Huwataharakisha watu, akifundisha katika Uyahudi yote, tokea Galilaya mpaka huku."

Wakati huu Pilato hakuwa na wazo la kumhukumu Yesu. Alijua kwamba Wayahudi walikuwa wamemshtaki kwa chuki na upotofu. Alijua kwamba jukumu lake lilikuwa lipi. Haki ilidai kwamba Kristo anapaswa aachiwe huru haraka. Lakini Pilato alitishwa na matakwa maovu ya watu. Ikiwa angekataa kumtia Yesu mikononi mwoa, ghasia ingeongezeka, na yeye aliogopa kukutwa na hali hii. Aliposikia kwamba Kristo alikuwa mtu wa Galilaya, aliamua kumpeleka kwa Herode, mtawala wa jimbo lile, ambaye wakati huu alikuwa Yerusalemu. Pilato aliona kwamba atumie njia hii kusukumia kwa Herode wajibu uliokuwa kwake wa kuendesha shauri lile. Alifikiri pia kwamba atumie fursa hii kutibu upinzani wa muda mrefu uliokuwepo kati yake na Herode. Na ilithibitisha hivyo. Wale mahakimu wawili walitengeneza urafiki wao kwa kutumia kesi ya Mwokozi.

Pilato alimleta tena Yesu mikononi mwa askari, na katikati ya makelele na matusi yale ya kundi la fujo aliharakishwa kupelekwa katika ukumbi wa hukumu wa Herode. "Herode alipomwona Yesu alifurahi sana." Alikuwa hajawahi kukutana na Mwokozi kabla, lakini "alikuwa akitaka sana kumwona tangu siku nyingi, maana amesikia habari zake, akataraji kuona ishara iliyofanywa na yeye." Herode huyu ndiye yule ambaye alikuwa na mikono yenye madoa ya damu ya Yohana Mbatizaji. Herode aliposikia kuhusu Yesu kwa mara ya kwanza, aliogopa sana, na akasema, "Yohana, niliyemkata kichwa, **(729)** amefufuka;" "na kwa hiyo nguvu hizo zinatenda kazi ndani yake. Marko 6:16; Mathayo 14:2. Lakini bado Herode alitamani kumwona Yesu. Sasa kulikuwa na fursa ya kuokoa maisha ya nabii huyu, na mfalme huyu alitumaini kusahau milele kumbukumbu ya kile kichwa chenye damu kilicholetwa kwake kikiwa katika kombe. Alitamani pia kufurahisha udadisi wake, akafikiri kwamba ikiwa Kristo angeonyeshwa matarajio ya kuachwa huru, angefanya kitu chochote ambacho angetakiwa kufanya.

Kundi kubwa la makuhani na wazee lilikuwa limemsindikiza Kristo kwenda kwa Herode. Na Mwokozi alipoletwa mle ndani, waheshimiwa hawa, wote wakiongea kwa msisimko, walitoa mashtaka yao kwake. Lakini Herode alijali kidogo sana yale mashtaka yao. Aliamuru pawe na ukimya, akitaka apate fursa ya kumwuliza Kristo. Aliagiza kwamba minyororo aliyofungwa Kristo ilegezwe, wakati huo huo akiwalaumu adui za Kristo kwa kumtendea ukatili. Akiutazama kwa huruma uso wa Mwokozi wa ulimwengu, alichosoma katika uso ule ni hekima na usafi. Yeye kama alivyokuwa Pilato aliridhika kwamba Kristo alikuwa ameshtakiwa kwa hila na husuda.

Herode alimhoji Kristo kwa maneno mengi, lakini katika yote Kristo alidumu katika ukimya mkubwa. Kwa agizo la mfalme yule, wenye udhaifu na vilema waliletwa ndani, na Kristo alitakiwa kuthibitisha madai yake ya kutenda miujiza. Watu husema kwamba unaweza kuponya wagonjwa, Herode alisema. Nina hamu ya kuona kwamba umaarufu huo ambao umeenea sana si uongo. Yesu hakuwa na mwitikio wowote; na Herode akaendelea kusisitiza akisema: Ikiwa uliweza kufanya miujiza kwa ajili ya wengine, ifanye sasa kwa ajili ya manufaa yako mwenyewe, nayo itakuwa na msaada kwako. Akaamuru tena akisema, Tuonyeshe ishara kwamba unao uweza ambao tetesi zimeonyesha kwamba unao. Lakini Kristo alikuwa kama mtu ambaye hakusikia wala kuona. Mwana wa Mungu alikuwa amechukua hali ya ubinadamu. Lazima afanye vile ambavyo mwanadamu angefanya katika mazingira ya namna ile. Kwa hiyo asingefanya mwujiza ili kujiokoa na maumivu na mateso ambayo lazima yastahimiliwe na mwanadamu pindi anapowekwa katika nafasi kama ile.

Herode aliahidi kwamba ikiwa Kristo angetenda mwujiza fulani pale mbele yake, angefunguliwa na kuachwa huru. Washtaki wa Kristo walikuwa wamepata kuona kwa macho yao matendo makuu yaliyofanywa na uweza wake. Walishasikia amri yake ikiliagiza kaburi kumtoa mfu aliyekuwemo ndani yake. Walishamsikia mfu akitii sauti ya Kristo na kutoka kaburini. Hofu iliwajaa kwamba anaweza akatenda mwujiza sasa. Kitu ambacho hawakupenda kuliko vyote ni Yeye kuthibitisha uweza wake. Udhihirisho kama huo ungethibitisha kwamba mipango yao ni **(730)** ya uharibifu, na huenda ungegharimu maisha yao. Kwa mara nyingine tena makuhani na wakuu, kwa wasiwasi, walisisitiza mashtaka yao kwake. Wakizipandisha juu sauti zao, walisema, Huyu ni msaliti, mwenye kukufuru. Anafanya miujiza kwa kutumia nguvu alizopewa na Beelzebuli, mkuu wa pepo. Ukumbi uligeuka na kuwa na mwonekano wa kuchanganyikwa, wengine wakipiga kelele kuhusu jambo moja na wengine jambo jingine.

Sasa dhamiri ya Herode ikawa isiyojitambua kwa mbali kuliko wakati alipotetemeka kwa hofu pindi Herodia alipoomba kichwa cha Yohana Mbatizaji. Kwa muda alikuwa amehisi kuchomwa sana kwa sababu ya hatia ya kitendo chake kile kibaya; lakini fahamu zake za kimaadili zilikuwa zimeshushwa zaidi na zaidi kwa sababu ya maisha ya kujipenda na ubinafsi. Sasa moyo wake ulikuwa umefanywa kuwa mgumu kiasi kwamba aliweza hata kujivunia adhabu aliyokuwa ametoa kwa Yohana kwa sababu ya kuthubutu kumwonya. Na sasa alimtisha Yesu, akitangaza kwa kurudia-rudia kwamba alikuwa na mamlaka ya kumwacha huru au kumhukumu. Lakini hakuna ushahidi uliotoka kwa Yesu kuashiria kwamba amesikia neno hilo.

Herode alikerwa na ukimya huu. Ilionekana kuonyesha kudharauliwa kwa mamlaka yake. Kwa mfalme huyu mwenye kujiona na kiburi kilichopitiliza, kemeo la wazi lingeonekana lisilochukiza sana kuliko kupuuzwa hivi. Kwa hasira alimtisha Yesu tena, ambaye aliendelea kuwa mtulivu na kimya.

Kazi ya Kristo katika ulimwengu huu haikuwa ya kufurahisha udadisi usio maana. Alikuja kuwaponya waliovunjika mioyo. Ikiwa Kristo angetakiwa kusema neno ili kuponya majeraha ya nafsi inayoumwa dhambi, asingeweza kukaa kimya. Lakini hakuwa na maneno kwa ajili ya wale ambao wangeishia tu katika kuukanyaga ukweli chini ya miguu yao isiyo mitakatifu.

Kristo angeweza kumwambia Herode maneno ambayo yangeweza kupenya masikioni mwa mfalme huyo mwenye moyo mgumu. Angeweza kumpiga kwa hofu na kutetemeka kwa njia ya kuonyesha mbele yake uovu wote wa maisha yake, na utisho wa uangamivu uliokuwa unakaribia. Lakini ukimya wa Kristo ulikuwa ni kemeo kali zaidi ambalo angeweza kutoa. Herode alikuwa amekataa ukweli alioambiwa na yule aliye mkuu miongoni mwa manabii, na hakukuwa na ujumbe mwingine ambao angepokea. Mwenye nguvu wa mbinguni hakuwa na neno kwa ajili yake. Sikio lile ambalo lilikuwa limefunguliwa kusikia shida za wanadamu, halikuwa na nafasi kwa ajili ya amri za Herode. Macho yale yaliyokuwa yametulia daima juu ya mwenye dhambi ajutaye, upendo usameheo, hayakuwa na hali ya kumtazama Herode. Midomo ile iliyokuwa imetamka ukweli ugusao sana, ambayo ilikuwa imewasihi kwa sauti ya upendo wale wenye dhambi wakubwa na walioshushwa chini, ilifungwa kwa mfalme huyu mwenye majivuno ambaye hakuhisi kumhitaji Mwokozi.

Uso wa Herode uliongezeka kuwa na giza la hasira. Akiugeukia umati ule, **(731)** alimtangaza Yesu kwa hasira kuwa ni laghai. Halafu alimwabia Kristo, Ikiwa hautatoa ushahidi wa madai yako, nitakutia mikononi mwa askari na watu. Labda wanaweza kufanikiwa kukufanya uongee. Ikiwa wewe ni laghai, kinachokustahili ni kifo katika mikono yao; ikiwa wewe ni Mwana wa Mungu, jiokoe mwenyewe kwa kutenda mwujiza.

Muda si muda baada ya maneno hayo kutamkwa uvamizi ulifanywa kwa Kristo. Kama walivyo wanyama wa mwitu, umati huu ulimrukia Yeye aliyekuwa kama mawindo kwao. Yesu aliburutwa huku na huko, Herode akiungana na kundi hilo la fujo katika kumdhalilisha Mwana wa Mungu. Ikiwa askari wa Kirumi wasingeingilia, na kuurudisha nyuma ule umati, Mwokozi angechanwa vipande-vipande pale.

"Basi Herode akamfanya duni, pamoja na askari zake, akamdhihaki, na kumvika mavazi mazuri." Askari wa Kirumi waliungana katika kumdhalilisha. Yote yale ambayo askari hawa waovu na dhalimu, wakisaidiwa na Herode na wakuu wa dini wa Kiyahudi, waliweza kuchochea yalilundikwa juu ya Mwokozi. Lakini bado uvumilivu wake wa kimbingu haukushindwa.

Watesi wa Kristo walikuwa wamejaribu kuipima tabia ya Kristo kwa kulinganisha na zile za kwao; walikuwa wamemwonyesha kuwa ni mwenye kuchukiza kama wao. Lakini nyuma ya mwonekano wa mambo yote yaliyopo tukio jingine lilijiingiza, - tukio ambalo wote wangeliona siku moja likiwa katika utukufu wake. Kulikuwa na baadhi waliotetemeka mbele ya uwepo wa Kristo. Wakati umati ule wa watu wabaya ulipokuwa ukimsujudia kwa dhihaka, baadhi ya watu waliokuja kwa kusudi hilo walirudi nyuma. Wakiogopa na wakiwa wamenyamazishwa. Herode alisadikishwa. Miale ya mwisho ya rehema ilikuwa inaumlikia moyo ule uliofanywa na dhambi kuwa mgumu. Alifikiri kwamba huyu hakuwa mtu wa kawaida; maana uungu ulimlika katika ubinadamu. Katika muda ule Kristo alipokuwa amezungukwa na wenye dhihaka, wafedhuli, na wauaji, Herode alihisi kama alikuwa anamwona Mungu aliyekuwa kwenye kiti chake cha enzi.

Akiwa na moyo mgumu vile, Herode hakudiriki kuidhinisha ile hukumu ya Kristo. Alitamani kujiepusha na jukumu lile la kutisha, na akamrudisha Yesu kule kwenye ukumbi wa hukumu wa Kirumi.

Pilato alihuzunishwa na kusikitishwa sana. Wayahudi waliporudi kwake wakiwa na mshtakiwa wao aliwauliza kwamba walitaka yeye afanye nini. Aliwakumbusha kwamba alishamchunguza Yesu, na kuona hakuna hatia kwake; aliwaambia kwamba walikuwa wameleta malalamiko dhidi ya Yesu, lakini hawakuwa wameweza kuthibitisha hata shtaka moja. Alikuwa amempeleka Yesu kwa Herode, mtawala wa sehemu ya Galilaya, na mtu wa taifa lao wenyewe, lakini yeye pia hakuwa ameona hatia inayompasa kufa. Akasema, "Kwa hiyo nitamrudi, kisha nitamfungua."

Pilato alionyesha udhaifu wake hapa. Alikuwa ametangaza kwamba Yesu hakuwa na **(732)** hatia, lakini bado alitaka Yesu apigwe ili kuwaridhisha waliomshtaki. Alikuwa tayari kuitoa kafara haki na kanuni ili kupata muafaka wa kundi lile lenye fujo. Hali hii ilimweka katika nafasi mbaya. Umati ule walitumia vibaya ukosefu wake wa uwezo wa kufanya uamuzi, na wakadai kwa nguvu zaidi uhai wa mshtakiwa. Ikiwa tangu mwanzoni Pilato angesimama imara, akikataa kumhukumu mtu ambaye hakuona hatia kwake, angekuwa amevunja

mnyororo wa kifo ambao ungemfunga katika kosa na hatia kwa muda wote wa maisha yake. Ikiwa angetenda kulingana na kusadikishwa kwake kuhusu haki, Wayahudi wasingejielekeza katika kumshinikiza. Kristo angepata kuuawa, lakini hatia isingekuwa juu ya Pilato. Lakini sasa Pilato alikuwa amefuata hatua kwa hatua katika kukiuka haki ya dhamiri yake. Alikuwa ametafuta udhuru wa kuacha kuhukumu kwa haki na usahihi, na sasa alijikuta kama hana msaada mikononi mwa makuhani na wakuu. Hali yake ya kuyumbayumba na kutokuwa na uamuzi fasaha ilimhakikishia uangamivu wake.

Hata sasa Pilato hakuachwa atende kwa upofu. Ujumbe kutoka kwa Mungu ulimwonya dhidi ya kitendo alichotaka kufanya. Kama jibu la ombi la Kristo, mke wa Pilato alikuwa ametembelewa na malaika kutoka mbinguni, na yule mwanamke alimwona Mwokozi katika ndoto na kuongea naye. Mke wa Pilato hakuwa Myahudi, lakini pindi alipomwona Yesu ndotoni, hakuwa na mashaka na tabia yake au kazi yake. Alimjua kuwa ni Mwana wa kifalme wa Mungu. Alimwona akishtakiwa katika shauri lile lililofanyika katika ukumbi wa hukumu. Aliiona mikono ikiwa imefungwa kama mikono ya mhalifu. Alimwona Herode na askari wake wakifanya kazi ya kutisha. Aliwasikia makuhani na wakuu, wakiwa wamejawa na husuda na ubaya, wakimshtaki sana. Alisikia maneno kwamba, "Sisi tunayo sheria, na kwa sheria hiyo amestahili kufa." Alimwona Pilato akimtoa Yesu ili apigwe, baada ya kuwa ametangaza kwamba, "Mimi sioni hatia yoyote kwake." Aliisikia hukumu ikitamkwa na Pilato, na kumwona akimtoa Yesu kwa wauaji wake. Aliuona msalaba ukiinuliwa kule Kalvari. Aliiona dunia ikifunikwa na giza, na kukisikia kilio kisicho cha kawaida kwamba, "Imekwisha." Bado tukio jingine lilionekana kwa mwanamke huyu. Alimwona Kristo akiwa ameketi kwenye wingu jeupe, huku dunia ikipepesuka angani, na wauaji wake wale wakikimbia kutoka mbele ya utukufu wake. Kwa kilio cha hofu yule mama aliamka, na mara moja alimwandikia Pilato maneno ya onyo.

Wakati Pilato alipokuwa anasitasita kwamba afanye nini, mjumbe alipenya katika umati, na kumpatia Pilato barua kutoka kwa mke wake, iliyosomeka hivi:

"Usiwe na neno na yule mwenye haki; kwa sababu nimeteswa mengi leo katika ndoto kwa ajili yake." **(733)** Uso wa Pilato ulibadilika. Alichanganyikiwa na hisia zake mwenyewe. Lakini wakati alipokuwa akiendelea kukawia kuteda, makuhani na wakuu walikuwa wakiendelea kuhamasisha zaidi mawazo ya watu. Pilato alilazimishwa kutenda. Sasa alijikumbusha desturi ambayo ingeweza kusaidia kumweka huru Kristo. Ilikuwa ni desturi kwamba katika sikukuu hii mtu mmoja ambaye amechaguliwa na watu hufunguliwa. Desturi hii ilianzishwa na wapagani; hakukuwa na kivuli cha haki katika desturi hii; lakini ilikuwa inathaminiwa sana na Wayahudi. Wakati huu mamlaka za Kirumi zilikuwa zimemshikilia mfungwa mmoja aitwaye Baraba, ambaye alikuwa amehukumiwa adhabu ya kifo. Mtu huyu alikuwa amedai kuwa ni Masihi. Alidai kuwa na mamlaka ya kuanzisha utaratibu mwingine wa mambo, ili kuuweka ulimwengu katika usahihi. Akiwa chini ya imani potofu ya kishetani alidai kwamba chochote ambacho angeweza kupata kwa njia ya wizi na unyang'anyi kilikuwa cha kwake. Alikuwa amefanya mambo ya ajabu kwa nguvu za kishetani, alikuwa amejipatia ufuasi miongoni mwa watu, na alikuwa ameshawishi upinzani dhidi ya serikali ya Kirumi. Chini ya kifuniko cha udadisi wa kidini alikuwa mtu mwovu sana na mwenye nguvu, akiwa amejikita katika uasi na ukatili. Kwa kuwapa watu wachague kati ya mtu huyu na Mwokozi asiye na hatia, Pilato alidhani kwamba angeamsha kwao hamu ya kutenda haki. Alitumaini kwamba angepata huruma yao kwa Yesu kinyume na upinzani wa makuhani na wakuu. Hivyo, akiugeukia umati, alisema kwa dhati sana, "Mnataka niwafungulie yupi? Yule Baraba, au Yesu aitwaye Kristo??"

Jibu lilitoka kwa lile kundi la fujo kama mwungurumo wa wanyama wa mwitu kwamba, "Utufungulie Baraba!" Makelele yale yaliongezeka zaidi na zaidi, Baraba! Baraba! Akidhani kwamba watu hawakuwa wameelewa swali lake, Pilato aliuliza, "Mwapenda niwafungulie Mfalme wa Wayahudi?" Lakini walipiga kelele sana wakisema, "Mwondoe huyu, utufungulie Baraba."! "Basi, nimtendeje Yesu aitwaye Kristo?" Pilato aliuliza. Kwa mara nyingine tena umati ule uliunguruma kama mapepo. Mapepo yenyewe, katika maumbo ya wanadamu, yalikuwa katika umati ule, na kwa hiyo ni jibu gani lingetolewa tofauti na kusema, "Asulibiwe"?

Pilato alipata shida. Hakuwa amedhani kwamba ingekuwa hivyo. Alisita kumtoa mtu asiye na hatia afe kifo kibaya na cha kikatili. Baada ya sauti za miungurumo kukoma, aliwageukia watu, akisema, "Kwani? Ni ubaya gani alioutenda?" Lakini jambo lile lilikuwa limeshaenda mbali sana kiasi kwamba kusingekuwa na hoja tena. Wao walichotaka sio ushahidi wa kutokuwa na hatia kwa Kristo, bali Yeye kuhukumiwa.

Bado Pilato aliazimia kumwokoa Yesu. "Akawaambia mara ya tatu, Kwa sababu gani? Huyu ametenda uovu gani? Sikuona kwake hata neno **(734)** lipasalo kufa. Basi nikiisha kumrudi nitamfungua." Lakini kule kutaja kuhusu kumfungua kuliwakoroga watu wakakosa kujizuia mara kumi zaidi. Wakasema, "Msulibishe, msulibishe." Kitendo cha Pilato kukosa maamuzi kuliongeza dhoruba ya sauti kubwa zaidi na zaidi.

Yesu alichukuliwa, akiwa amedhoofu kwa uchovu na akiwa amefunikwa majeraha, na akiwa amepigwa mbele ya umati. "Nao askari wakamchukua ndani ya behewa, ndiyo Praitorio (yaani, nyumba ya uliwali), wakakusanya pamoja kikosi kizima. Wakamvika vazi la rangi ya zambarau, wakasokota taji ya miiba, wakamtia kichwani; wakaanza kumsalimu, Salamu, Mfalme wa Wayahudi! . . . Wakamtemea mate, wakapiga magoti, wakamsujudia." Ghafla tu mkono mmoja wa mtu mwovu ulinyakuwa mwanzi uliokuwa umewekwa mkononi mwa Yesu, na kumpiga nao kichwani penye ile taji, na kuisukuma miiba ya taji ile kumchoma kichwani, na kuifanya damu itiririke katika uso na kidevu chake.

Shangaeni, enyi mbingu! Na ushangazwe, Ee dunia! Tazama mtesaji na yeye mwenye kuteswa. Umati wenye hasira unamzingira Mwokozi wa ulimwengu. Dhihaka na kuzomea vimechanganyika na viapo vya kukufuru. Kuzaliwa kwake kwa hali duni na maisha yake ya unyenyekevu yanazawadiwa hivi na kikundi cha fujo kisicho na huruma. Madai yake ya kuwa Mwana wa Mungu yanakejeliwa, na utani wa kishenzi na matusi vinatolewa kutoka mdomo mmoja hadi mwingine.

Shetani aliliongoza lile kundi katili kumtenda mabaya Mwokozi. Kusudi la Shetani lilikuwa ni kumsukuma Yesu alipize kama ingewezekana, au kumsukuma atende mwujiza ili kujiokoa, na kwa njia hiyo awe amevunja mpango wa wokovu. Doa moja la maisha yake ya kibinadamu, anguko moja la ubinadamu wake kushindwa kustahimili majaribu yale, ingemfanya Mwana-kondoo wa Mungu asiwe dhabihu kamilifu, na kufanya ukombozi wa mwanadamu kushindwa. Lakini Yeye ambaye kwa amri angeweza kuleta jeshi la mbinguni kuja kumsaidia – Yeye ambaye angeweza kulisambaratisha lile kundi ovu likatawanyika kutoka kwake kwa hofu ya mwako wa nuru ya ukuu wake wa kimbingu – alijisalimisha kwenye matukano na ukatili akiwa katika utulivu mkamilifu.

Adui za Kristo walikuwa wamedai mwujiza kama uthibitisho wa uungu wake. Walikuwa na ushahidi mkubwa kwa mbali kuliko wowote waliokuwa wanatafuta. Kadiri ukatili wao ulivyomdhalilisha anayeteswa hadi katika hali ya chini kuliko binadamu anavyoweza kutendewa katika sura ya Shetani, ndivyo upole na uvumilivu wake ulivyoongezeka na kumwinua Yesu juu zaidi kuliko kiwango cha mwanadamu, na kuthibitisha uasili wake wa familia ya Mungu. Kudhiliwa kwake kulikuwa ndiyo udhihirisho wake wa kukwezwa. Matone ya damu ya maumivu yaliyotiririka usoni na kidevuni kutoka katika majeraha ya kichwani pake yalikuwa uthibitisho wa kupakwa kwake "mafuta ya shangwe" (Waebrania 1:9.) kama kuhani mkuu wetu. **(735)** Ghadhabu ya Shetani ilikuwa kubwa kadiri ilivyoona kwamba mabaya yote yaliyotendwa kwa Mwokozi hayakuwa yamelazimisha hata manung'uniko midomoni mwa Yesu. Ingawa alikuwa amechukua namna ya mwanadamu, alihimizwa na nguvu za kimungu, na hakuachana kwa namna yoyote na mapenzi ya Baba yake.

Wakati Pilato alipokuwa amemtoa Yesu apigwe na kudhihakiwa, alidhani kwamba atachochea huruma ya makutano. Alifikiri kwamba wataamua kwamba adhabu ile imetosha. Alidhani kwamba hata chuki ya makuhani ingekuwa imeridhika sasa na kutulia. Lakini kwa ufahamu makini Wayahudi waliona udhaifu wa kumwadhibu vile mtu ambaye ametangazwa kuwa hana hatia. Walijua kwamba Pilato alikuwa anajaribu kumwokoa mshtakiwa yule, na waliazimia kwamba Yesu asiachiwe huru. Walifikiri kwamba, Pilato amempiga ili kuturidhisha, na ikiwa tutashinikiza jambo hili kwa dhati, tutapata kile tunachotaka.

Sasa Pilato aliagiza kwamba Baraba aletwe katika ukumbi wa mahakama. Sasa alionyesha mbele ya watu wale wafungwa wawili wakiwa wamesimama pamoja, na akielekeza kwa Mwokozi alisema kwa sauti ya kubembeleza, "Tazama, mtu huyu!" "Mtu huyu namleta nje kwenu, mpate kufahamu ya kuwa mimi sioni hatia yoyote kwake."

Mwana wa Mungu alisimama pale, akiwa amevaa kanzu ya dhihaka na taji ya miiba. Mgongo wake ulionyesha michirizi mirefu ya damu kutokana na mapigo ya kikatili. Uso wake ulikuwa na madoa ya damu, na ulionyesha dalili za uchovu na maumivu; lakini hakuna wakati uso ule ulipoonekana mzuri zaidi kuliko wakati huu. Uso wa Mwokozi haukuharibiwa na adui wale. Kila mwonekano wake ulionyesha upole na kukubaliana na hali na huruma ya upendo kwa adui zake wakatili. Kwake hakukuwa na udhaifu wa woga, bali nguvu na wema wa uvumilivu. Katika hali yenye mwonekano tofauti kulikuwa na mfungwa mwingine pembeni yake. Kila

mwonekano wa Baraba ulitangaza vile alivyokuwa mtu mbaya. Tofauti iliyokuwepo kati ya hao wawili ilionekana kwa kila aliyetazama. Baadhi ya watazamaji walikuwa wanalia. Pindi walipomtazama Yesu, mioyo yao ilijawa na huruma. Hata makuhani na wakuu walisadikishwa kwamba Yeye alikuwa vile alivyodai kuwa.

Wale askari wa Kirumi waliokuwa wamemzunguka Kristo hawakuwa na mioyo migumu wote; baadhi walikuwa wanamwangalia kwa umakini usoni pake ili kuona ushahidi wowote wa kuonyesha kwamba alikuwa mhalifu au mtu hatari. Mara kwa mara waligeuka na kumwangalia Baraba kwa mtazamo wa kuchukizwa naye. Haikuhitaji kuangalia sana ili kumgundua alivyokuwa. Kwa mara nyingine walimgeukia Yeye aliye katika kuhukumiwa. Walimwangalia kwa hisia za huruma mteswaji yule wa kimbingu. Ukimya wa kujisalimisha wa Kristo ulilipiga muhuri mawazoni mwao **(736)** tukio lile, kamwe lisifutike mpaka ama wakati ambapo wangemkiri kama Kristo, au kumkataa na kuamua hatima yao.

Pilato alijawa na mshangao kwa ile hali ya kutolalamika ya Kristo. Hakuwa na mashaka kwamba mwonekano wa Mtu huyu, unaotofautiana na wa Baraba, ungewafanya Wayahudi kumwonea huruma. Lakini hakuelewa chuki iliyopitiliza ya makuhani dhidi ya Yesu, ambaye, kama Nuru ya ulimwengu, alikuwa amefanya giza lao na makosa yao kudhihirika. Walikuwa wameufanya umati ule wa fujo kuwa kama vichaa, na kwa mara nyingine tena makuhani, wakuu, na watu walipaza sauti zao za kutisha wakisema, "Msulibishe! Msulibishe!" Hatimaye, akiwa amepoteza subira yote kwa makelele yale yasiyo na sababu, Pilato alilia kwa sauti bila kujizuia, akisema, "Mtwaeni ninyi basi, mkamsulibishe; kwa maana mimi sioni hatia kwake."

Liwali huyu wa Kirumi, ingawa anayafahamu matukio ya kikatili, alisukumwa na huruma kwa mfungwa huyu anayeteseka, ambaye, akiwa amehukumiwa na kupigwa, na kichwa kinachotoa damu na mgongo uliochanika-chanika, alikuwa bado ana wadhifa wa ufalme kwenye kiti chake. Lakini makuhani walitangaza kwamba, "Sisi tunayo sheria, na kwa sheria hiyo amestahili kufa, kwa sababu alijifanya kuwa Mwana wa Mungu."

Pilato alitatizwa. Hakuwa na dhana sahihi kuhusu Kristo na kazi yake; lakini alikuwa na imani hai kwa Mungu na katika vitu vyenye uhai vilivyo vikuu kuliko wanadamu. Wazo lililokuwa limekuja wakati fulani mawazoni mwake sasa lilijijenga zaidi. Alijiuliza ikiwa haiyumkini kwamba huyu ni wa mbinguni aliyekuwa amesimama mbele yake, akiwa amevikwa kanzu ya kifalme ya dhihaka, na akiwa amevikwa taji ya miiba.

Aliendа tena katika ukumbi wa hukumu na kumwambia Yesu, "Wewe umetokapi?" Lakini Yesu hakumpa jibu lolote. Mwokozi alikuwa ameongea na Pilato kwa uhuru, akifafanua kazi yake kama shahidi wa ukweli. Pilato hakuwa amejali nuru ile. Alikuwa ametumia vibaya mamlaka yake ya hakimu kwa kutelekeza kanuni na mamlaka ili kukidhi madai ya kundi la fujo. Yesu hakuwa na nuru zaidi kwa ajili yake. Akighadhibika kwa kudhalilishwa na ukimya ule, alisema kwa kuhamaki: "Husemi nami? Hujui ya kuwa mimi nina mamlaka ya kukufungua, nami nina mamlaka ya kukusulibisha?" Yesu alimjibu, "Wewe hungekuwa na mamlaka yoyote juu yangu, kama usingepewa kutoka juu; kwa hiyo yeye aliyenitia mikononi mwako yuna dhambi iliyo kubwa zaidi."

Kwa njia hiyo Mwokozi mwenye huruma, akiwa katikati ya mateso yake makali na huzuni, alisamehe kwa kiasi kiwezekanacho kitendo cha liwali yule wa Kirumi aliyemtoa ili asulibiwe. Lilikuwa ni tukio gani hili la kuendeleza ulimwenguni wakati wote! Ni nuru kiasi gani inayoangazwa na tukio hili lenye tabia yake Yeye aliye Hakimu wa dunia yote!

**(737)** "Yeye aliyenitia mikononi mwako yuna dhambi iliyo kubwa zaidi," Yesu alisema. Kwa habari hii Kristo alikuwa na maana ya Kayafa, ambaye, kama kuhani mkuu, aliwakilisha taifa la Wayahudi. Walijua kanuni iliyotawala mamlaka za Kirumi. Walikuwa na nuru katika unabii iliyomshuhudia Kristo, na katika mafundisho yake yenyewe na miujiza. Waamuzi wa Kiyahudi walikuwa wamepokea ushahidi usio na makosa kuhusu uungu wa Yeye ambaye walimhukumu kufa. Kwa mujibu wa nuru yao wangeweza kuhukumiwa.

Hatia kubwa zaidi na kuwajibika kukubwa zaidi vilikuwa juu ya wale waliokuwa katika nafasi za juu zaidi katika taifa, wale waliokabidhiwa ule ukweli mtakatifu waliokuwa wanausaliti. Pilato, Herode, na askari wa Kirumi walikuwa hawamjui Yesu ukilinganisha na hao wengine. Walifikiria kuwafurahisha makuhani na wakuu kwa kumtendea jeuri Yesu. Hawakuwa na nuru ambayo Wayahudi walikuwa wameipata kwa wingi sana. Ikiwa nuru ingekuwa imetolewa kwa wale askari, wasingekuwa wamemtendea Kristo kwa ukatili kama walivyofanya.

Kwa mara nyingine tena Pilato alipendekeza kumwachia huru Mwokozi. "Lakini Wayahudi wakapiga makelele wakisema, Ukimfungua huyu, wewe si rafiki yake Kaisari." Hivyo ndivyo hawa wanafiki walivyojifanya kuwa na wivu kwa ajili ya mamlaka ya Kaisari. Miongoni mwa wapinzani wote dhidi ya utawala wa Kirumi, Wayahudi ndio waliokuwa wapinzani wakubwa. Wakati ilipokuwa salama kwao kutenda, walikuwa madikteta wakubwa katika kulazimisha utekelezaji wa matakwa yao ya kitaifa na ya kidini; lakini wakati walipotaka kufikia kusudi fulani la kikatili, waliutukuza utawala wa Kaisari. Ili kutekeleza kusudi la kumwangamiza Kristo, walikuwa tayari kukiri kuutambua utawala wa kigeni waliouchukia.

Waliendelea kwamba, "Kila mtu ajifanyaye kuwa mfalme humfitini Kaisari." Hili lilikuwa linamgusa Pilato katika udhaifu wake. Aliangaliwa na serikali ya Kirumi kwa mashaka, na alijua kwamba taarifa kama hiyo ingekuwa ni uangamivu kwake. Alijua kwamba ikiwa Wayahudi wangezuiwa, hasira yao ingegeuziwa kwake. Wasingeacha kutumia kila mbinu kuhakikisha kwamba wanalipiza kisasi. Alikuwa na mfano mahsusi mbele yake jinsi walivyokuwa wanang'ang'ana wakiutafuta uhai wake Yeye waliyekuwa wanamchukia bila sababu.

Ndipo Pilato akakaa mahali pake kwenye kiti cha hukumu, akamleta tena Yesu mbele ya watu, akisema, "Tazama, Mfalme wenu!" Makelele kama ya watu wenye wazimu yalisikika tena, "Mwondoshe! Mwondoshe! Msulibishe." Kwa sauti iliyosikika mbali na karibu, Pilato aliuliza, "Je! Nimsulibishe mfalme wenu?" Lakini maneno yalitoka katika midomo ya makufuru kama isiyo ya kidini yakisema, "Sisi hatuna mfalme ila Kaisari."

Kwa njia hiyo ya kumchagua mtawala mpagani, taifa la Wayahudi lilikuwa limejiondoa **(738)** katika mfumo wa kutawaliwa na Mungu. Walikuwa wamemkataa Mungu kama mfalme wao. Kuanzia hapo hawakuwa na Mwokozi. Hawakuwa na mfalme tena isipokuwa Kaisari. Makuhani na waalimu walikuwa wamewafikisha watu mahali hapo. Walikuwa na hali ya kuwajibika kwa hili, na kwa matokeo ya kuogofya ambayo yangefuata. Dhambi ya taifa na uangamivu wa taifa lote vilisababishwa na viongozi wa dini.

"Basi Pilato alipoona ya kuwa hafai lolote, bali ghasia inazidi tu, akatwaa maji, akanawa mikono yake mbele ya mkutano, akasema, Mimi sina hatia katika damu ya mtu huyu mwenye haki; yaangalieni haya ninyi wenyewe." Pilato alimtazama Mwokozi kwa hofu na katika hali ya kuhukumiwa mwenyewe. Katika kundi kubwa la nyuso zilizogeuka, uso wa Kristo tu ndio uliokuwa na amani. Nuru nyororo ilionekana iking'aa kuzunguka kichwa chake. Pilato akasema moyoni mwake, Huyu ni Mungu. Akiwageukia makutano alitangaza kwamba, Sina hatia na damu yake. Mchukueni ninyi wenyewe mkamsulibishe. Lakini zingatieni, enyi makuhani na wakuu, namtangaza mtu huyu kuwa ni mwenye haki. Kwa kazi hii ya leo hebu huyo anayedaiwa na mtu huyu kuwa ni Baba yake awahukumu ninyi wala si mimi. Halafu akamwambia Yesu, Nisamehe kwa kitendo hiki; siwezi kukuokoa. Na alipokuwa amempiga Yesu tena, alimtoa ili asulibiwe.

Pilato alitafuta kumponya Yesu. Lakini aliona kwamba hawezi kufanya hilo, na bado akabaki na cheo chake na heshima yake. Kuliko apoteze mamlaka yake ya duniani, alichagua kuutoa kafara uhai usio na hatia. Ni wangapi ambao, kwa kutaka kuepuka hasara au maumivu, wanatoa kafara kanuni kwa namna ile ile. Dhamiri na wajibu unaelekeza katika njia moja, na matakwa binafsi yanaelekeza katika njia nyingine. Mkondo unaelekea kwa nguvu katika uelekeo usio sahihi, na yule anayeafikiana na uovu hufagiliwa mbali katika giza nene la hatia.

Pilato alijisalimisha chini ya matakwa ya kundi la wenye hasira. Badala ya kuhatarisha cheo chake, alimtoa Yesu ili asulibiwe. Lakini licha ya tahadhari nyingi, kitu kile kile alichohofia kilimjia. Heshima zake ziliondolewa kwake, alitupwa chini kutoka katika cheo chake kile cha juu, na akiwa ameathiriwa na hatia na kiburi kilichojeruhiwa, aliyafikisha mwisho maisha yake muda ambao si mrefu baada ya kusulibishwa kwa Yesu. Hivyo ndivyo ambavyo wote wanaoafikiana na dhambi watakavyoishia kuambulia huzuni na uangamivu. "Iko njia ionekanayo kuwa sawa machoni pa mtu, Lakini mwisho wake ni njia za mauti." Mithali 14:12.

Wakati Pilato alipojitangaza kuwa hana hatia ya damu ya Kristo, Kayafa alijibu kwa ufidhuli, "Damu yake na iwe juu yetu, na juu ya watoto wetu." Maneno hayo mabaya yalidakwa na makuhani na wakuu, na yakarudiwa na umati katika mwungurumo wa sauti zisizo za kibinadamu. Umati wote ukajibu ukisema, "Damu yake na iwe juu yetu, na juu ya watoto wetu."

Watu wa Israeli walikuwa wamefanya uchaguzi wao. Wakielekeza vidole kwa Yesu walikuwa **(739)** wamesema, "Si huyu, bali Baraba." Baraba, mnyang'anyi na mwuaji, alikuwa mwakilishi wa Shetani. Kristo alikuwa mwakilishi wa Mungu. Kristo alikuwa amekataliwa; Baraba alikuwa amechaguliwa. Kwa hiyo wangekuwa na

Baraba. Kwa kufanya uchaguzi huu walimchagua yeye ambaye alikuwa mwongo na mwuaji tangu mwanzo. Shetani alikuwa kiongozi wao. Wakiwa kama taifa wangetekeleza udikteta wake. Wangefanya kazi zake. Lazima wastahimili utawala wake. Watu wale wale waliomchagua Baraba mahali pa Kristo walikuwa wanaenda kukutana na ukatili wa Baraba wakati wote.

Wakimtazama Mwana-kondoo wa Mungu aliyepigwa, Wayahudi walikuwa wamepaza sauti wakisema, "Damu yake na iwe juu yetu, na juu ya watoto wetu." Sauti zile mbaya sana zilipanda juu hadi kwenye kiti cha enzi cha Mungu. Hukumu ile, ambayo ilikuwa imetamkwa juu yao wenyewe, iliandikwa mbinguni. Ombi lile lilisikiwa. Damu ya Mwana wa Mungu ilikuwa juu ya watoto wao na watoto wa watoto wao, laana ya kudumu.

Kwa hali ya kutisha laana hiyo ilionekana wakati wa kuharibiwa kwa Yerusalemu. Kwa hali ya kutisha imeonekana pia katika hali ya taifa la Wayahudi kwa miaka elfu moja na mia nane, - tawi lililotupwa kutoka kwenye mzabibu, tawi lililokufa lisilozaa matunda, la kukusanywa na kuchomwa. Kutangatanga kutoka nchi moja hadi nyingine ulimwenguni kote, kutoka karne hadi karne, ni wafu, wafu katika makosa na dhambi!

Ombi lile litatimizwa kwa namna ya kutisha mnamo siku kuu ya hukumu. Ni wakati Kristo atakapokuja duniani tena. Watu watamwona akiwa siyo kama mfungwa azungukwaye na kundi la watu wenye hasira. Wakati huo watamwona akiwa kama mfalme wa mbinguni. Kristo atakuja katika utukufu wake, katika utukufu wa Baba yake, na utukufu wa malaika watakatifu. Elfu kumi mara elfu kumi, na maelfu kwa maelfu ya malaika, wana wa Mungu walio wazuri na wenye shangwe ya ushindi, wakiwa na wema na utukufu wa hali ya juu, watamsindikiza katika njia yake. Halafu atakaa kwenye kiti cha enzi cha utukufu wake, na mataifa yote watakusanywa mbele zake. Hapo ndipo kila jicho litakapomwona, hata na wale waliomchoma. Mahali pale pa taji ya miiba, atavaa taji ya utukufu, - taji ndani ya taji. Badala ya ile kanzu chakavu ya kifalme ya zambarau, atavikwa vazi jeupe kuliko weupe wote, "jinsi asivyoweza dobi duniani kuyafanya meupe." Marko 9:3. Na kwenye vazi lake na paja lake kutakuwa na jina limeandikwa, "Mfalme wa wafalme, na Bwana wa mabwana." Ufunuo 19:16. Wale waliomdhihaki na kumtemea mate watakuwepo pale. Wale makuhani na wakuu wataliona tena lile tukio lao la katika ukumbi wa hukumu. Kila hali iliyokuwepo itatokea tena mbele yao, kama vile imeandikwa kwa herufi za moto. Halafu wale walioomba kwamba, "Damu yake na iwe juu yetu, na juu ya watoto wetu," watapokea jibu la ombi lao. Hapo ndipo ulimwengu wote utakapojua **(740)** na kuelewa. Watu watabaini kwamba ni nani ambaye wao, walio maskini, wanyonge, viumbe dhaifu, wamekuwa wakipiga vita dhidi yake. Kwa hofu na maumivu makubwa watapaza sauti wakiililia milima na miamba kwamba, "Tuangukieni, tusitirini, mbele za uso wake yeye aketiye juu ya kiti cha enzi, na hasira ya Mwana-Kondoo. Kwa maana siku iliyo kuu, ya hasira yao, imekuja; naye ni nani awezaye kusimama?" Ufunuo 6:16, 17.

## Sura ya 78

# Kalvari

[Sura hii imejengwa katika Mathayo 27:31-53; Marko 15:20-38; Luka 23:26-46; Yohana 19:16-30.]

"Na walipofika mahali paitwapo Fuvu la Kichwa, ndipo walipomsulibisha."

"Ili awatakase watu kwa damu yake mwenyewe," Kristo "aliteswa nje ya lango." Waebrania 13:12. Kwa sababu ya kuikiuka sheria ya Mungu, Adamu na Hawa walifukuzwa kutoka Edeni. Kristo, aliye mbadala wetu, alipaswa kuteswa akiwa nje ya Yerusalemu. Alifia nje ya lango, mahali ambako wahalifu na wauaji waliadhibiwa. Maneno yafuatayo yanakuwa na maana halisi, "Kristo alitukomboa katika laana ya torati, kwa kuwa alifanywa laana kwa ajili yetu." Wagalatia 3:13.

Umati mkubwa ulimfuata Yesu kutoka katika ukumbi wa hukumu kwenda Kalvari. Habari za kuhukumiwa kwake zilikuwa zimesambaa kote katika Yerusalemu, na watu wa matabaka yote na hadhi zote walimiminika kuelekea mahali pa kusulibishiwa. Makuhani na wakuu walikuwa wamefungwa na ahadi kwamba wasiwasumbue wafuasi wa Kristo ikiwa atatiwa mikononi mwao, na wanafunzi na waamini kutoka katika mji ule na eneo linalouzunguka waliungana na msafara uliokuwa unamfuata Mwokozi.

Pindi Yesu alipolipita lango la mahakama ya Pilato, msalaba uliokuwa umeandaliwa kwa ajili ya Baraba ulitwishwa kwenye mabega yake yaliyokuwa yamechubuliwa yakitoka damu. Marafiki wawili wa Baraba walikuwa wasulibishwe kwa wakati mmoja pamoja na Yesu, nao pia walitwishwa misalaba. Mzigo wa Mwokozi **(742)** ulikuwa mzito sana kwake kwa namna alivyokuwa amechoka na kuteseka. Tangu alipokula chakula cha Pasaka pamoja na wanafunzi wake, alikuwa hajala wala kunywa tena kitu chochote. Alikuwa amesumbuka bustanini Gethsemane akipambana na nguvu za kishetani. Alikuwa amestahimili maumivu ya kusalitiwa, na alikuwa amewaona wanafunzi wake wakimwacha na kukimbia. Alikuwa amepelekwa kwa Anasi, halafu kwa Kayafa, na baadaye kwa Pilato. Kutoka kwa Pilato alikuwa amepelekwa kwa Herode, na kurudishwa tena kwa Pilato. Kutoka kwenye matukano mpaka matukano tena, kutoka katika dhihaka hadi dhihaka nyingine, akiwa ameteswa kwa mapigo mara mbili, - usiku wote ule kulikuwa na matukio ya hali ya kumtesa mtu kwa kiwango cha juu kabisa. Kristo hakuwa ameshindwa. Hakuwa ametamka neno isipokuwa lile lenye mwelekeo wa kumtukuza Mungu. Katika njia yote hiyo ya mateso mabaya na kejeli alikuwa amesalia kuwa imara na mwenye heshima. Lakini wakati msalaba ulipowekwa juu yake baada ya mapigo ya mara ya pili, hali ya mwanadamu haikuweza kustahimili zaidi. Alianguka chini ya mzigo ule akiwa amenyong'onyea.

Umati uliokuwa unamfuata Mwokozi uliziona hatua zake zilizokuwa dhaifu, lakini hawakuonyesha huruma yoyote. Walimkejeli na kumshambulia kwa maneno kwa kule kushindwa kubeba msalaba ule mzito. Ule mzigo ulitwishwa juu yake tena, na akaanguka tena chini. Watesi wake wakaona kwamba ni jambo lisilowezekana kwake kuubeba mzigo wake ule kwenda mbali zaidi ya pale. Walipata hali ya kukanganyikiwa kwamba wangepataje mtu wa kukubali kubeba mzigo ule wa kudhalilisha. Wayahudi wenyewe wasingeweza kufanya jambo hili, maana unajisi huu ungewazuia kuisherehekea Pasaka. Wala hakuna mtu miongoni mwa kundi lile la wenye fujo lililokuwa linamfuata Yesu ambaye angekubali kujishusha hadi kubeba msalaba.

Wakati huu mgeni, Simoni Mkirene, akiwa anaingia mjini kutoka vijijini, alikutana na msafara huo. Anasikia maneno ya umati ya dhihaka na kejeli; anayasikia maneno yale mabaya yakirudiwa-rudiwa kwamba, Toa njia kwa ajili ya Mfalme wa Wayahudi! Anasimama kwa kushangazwa na tukio lile; na pindi anapoonyesha hali ya kuwa na huruma, wanamhusuru na kuutwika msalaba mabegani pake.

Simoni alikuwa ameshasikia habari za Yesu. Wana wake walikuwa watu wanaomwamini Mwokozi, lakini yeye hakuwa mwanafunzi wake. Kule kuubeba msalaba kwenda Kalvari kulikuwa mbaraka kwa Simoni, na daima baada ya pale alikuwa na shukrani sana kwa ajili ya tukio hili. Lilimsababisha aubebe msalaba wa Kristo kwa kutaka, na daima kwa furaha apate kusimama chini ya msalaba huo.

Si wanawake wachache ambao wako miongoni mwa umati uliokuwa unamfuata Yeye ambaye hakupatikana na hatia yoyote kwenda kwenye kifo chake cha kikatili. Macho yao yamekazwa kwa Yesu. Baadhi yao walikuwa

wameshamwona kabla. Baadhi wamewahi kumpelekea wagonjwa wao na wenye shida. Baadhi wamepata kuponywa wao wenyewe. Kisa cha mambo ambayo yamefanyika kinasimuliwa. Wanaishangaa chuki ya umati ule kwake Yeye ambaye kwa ajili yake mioyo yao ilikuwa inayeyuka na ikiwa tayari kupasuka. **(743)** Na licha tu ya kitendo cha umati ule wenye wazimu, na maneno ya hasira ya makuhani na wakuu, wanawake hawa wanaonyesha hali ya huruma. Wakati Yesu anapoanguka akizimia chini ya msalaba, wanaangua kilio cha huzuni kubwa.

Hiki ndicho kitu pekee kilichomvutia Kristo. Ingawa alikuwa amejawa na maumivu, akiwa amebeba dhambi za ulimwengu, hakuacha kujali mwonekano wa majonzi ya watu. Aliwatazama wanawake hawa kwa huruma ya upendo. Walikuwa si watu wanaomwamini; alijua kwamba hawakuwa wanamlilia kama Yeye aliyetumwa kutoka kwa Mungu, bali walikuwa wanasukumwa na hisia za huruma za kibinadamu. Hakudharau huruma yao, bali iliamsha moyoni mwake huruma ya kina kwa ajili yao. Akasema, "Enyi binti za Yerusalemu, msinililie mimi, bali jililieni nafsi zenu na watoto wenu." Kutoka katika tukio lile lililokuwa mbele yake, Yesu alitazama mbele katika tukio la kuharibiwa kwa Yerusalemu. Katika tukio lile la kutisha, wengi wa wale waliokuwa wanamwombolezea sasa wangeangamia na watoto wao.

Kutoka katika anguko la Yerusalemu mawazo ya Yesu yalipitiliza mpaka kwenye hukumu kuu zaidi. Katika uharibifu wa mji huu usiotubu aliona alama ya uharibifu wa mwisho utakaoujia ulimwengu. Alisema, "Ndipo watakapoanza kuiambia milima, Tuangukieni, na vilima, Tufunikeni. Kwa kuwa kama wakitenda mambo haya katika mti mbichi, itakuwaje katika mkavu?" Yesu alijiwakilisha kwa mti mbichi, Mkombozi asiye na hatia. Mungu aliruhusu ghadhabu yake dhidi ya uasi imwangukie Mwana wake mpendwa. Yesu alikuwa asulibishwe kwa ajili ya dhambi za wanadamu. Ni maumivu gani, basi, ambayo mdhambi ambaye angeendelea na dhambi angekabiliwa nayo? Wote wasioamini na wasiotubu wangejua huzuni na maumivu ambayo lugha isingeweza kuyaeleza.

Miongoni mwa makutano waliomfuata Mwokozi kwenda Kalvari walikuwemo wengi ambao walikuwa pamoja naye wakiimba hosanna kwa furaha na kupeperusha matawi ya mitende wakati alipoingia Yerusalemu kwa shangwe. Lakin si wachache ambao waliimba sifa wakati ule, kwa kuwa ilikuwa shangwe ya wengi kufanya hivyo, ambao sasa walipanua sauti zilizosema "Msulibishe! Msulibishe!" Wakati Kristo alipoingia Yerusalemu kwa shangwe, matumaini ya wanafunzi yalikuwa yamepanda hadi juu kabisa. Walikuwa wanamkaribia sana Bwana wao, wakihisi kwamba ilikuwa heshima ya juu kuunganishwa naye. Sasa katika mateso yake walimfuata kwa mbali. Walikuwa wamejawa na majonzi, na waliinama kwa mfadhaiko mkubwa. Ni jinsi gani ambavyo maneno ya Yesu yalithibitika: "Ninyi nyote mtachukizwa kwa ajili yangu usiku huu kwa kuwa imeandikwa, Nitampiga mchungaji, na kondoo wa kundi watatawanyika." Mathayo 26:31.

**(744)** Walipofika mahali pa kusulibishwa, wafungwa wale walifungwa kwenye kifaa kile cha kutesea. Wale wanyang'anyi wawili walipambana pale mikononi mwa wale waliokuwa wanawaweka kwenye misalaba; lakini Yesu hakufanya ubishi wowote. Mama wa Yesu, akitegemezwa na Yohana yule mwanafunzi mpendwa, alikuwa amefuata nyayo za Mwana wake kwenda Kalvari. Alikuwa amemwona Yesu akinyong'onyea chini ya uzito wa msalaba, na alikuwa ametamani kuweka mkono wake chini ya kichwa kile kilichojeruhiwa ili kumsaidia, na kuosha uso ule ambao wakati fulani uliegemezwa kifuani pake. Lakini hakuruhusiwa kupata nafasi hiyo. Yeye, pamoja na wanafunzi, alikuwa bado anatumaini kwamba Yesu angeonyesha uwezo wake, na kujiokoa kutoka mikononi mwa adui zake. Kwa mara nyingine tena moyo ulizama chini pindi alipokumbuka maneno ambayo Yesu alisema akitabiri matukio yale yale ambayo yalikuwa yanatokea wakati huu. Kadiri wale wanyang'anyi walivyokuwa wakifungwa msalabani, mama huyu alitazama kwa maumivu makali. Je! Yeye aliyerejesha uhai kwa waliokufa angejiruhusu asulibishwe? Je! Mwana wa Mungu angejiruhusu auawe kikatili kiasi hiki? Je! Mama huyu aachane na imani yake kwamba Yesu ni Masihi? Je! Ashuhudie tu aibu ya Yesu na huzuni zake, bila hata kumhudumia katika shida yake hii? Aliona mikono ya Yesu ikinyoshwa kwenye msalaba; nyundo na misumari vilileta, na kadiri ambavyo misumari ile ilipigiliwa na kuingia katika misuli, wale wanafunzi waliofadhaishwa walimwondoa mama wa Yesu aliyekuwa katika hali ya kuzimia wakamwondoa mahali pa tukio lile la kikatili.

Mwokozi hakufanya manung'uniko yoyote ya kulalamika. Uso wake ulibaki wenye utulivu, lakini matone makubwa ya jasho yalikuwa usoni mwake. Hakukuwa na mkono wowote wa upendo wa kupangusa jasho lile la kifo kutoka usoni mwake, wala hakukuwa na maneno yoyote ya kufariji na kumtia shime ili kuupa moyo ule wa

mwanadamu faraja. Wakati askari walipokuwa wanafanya kazi yao hiyo ya kuogofya, Yesu aliwaombea adui zake, akisema, "Baba, uwasamehe, kwa kuwa hawajui watendalo." Mawazo yake yalipita kutoka katika maumivu yake Yeye na kwenda kwenye dhambi ya watesi wake, na mapatilizo ya kutisha ambayo yangewajilia. Hakuna laana ambazo ziliitishwa ziwashukie wale askari waliokuwa wakimtendea mabaya. Hakuna kisasi kilichoelekezwa kwa makuhani na wakuu, waliokuwa wakikazania kutekelezwa kwa kusudi lao. Yesu aliwahurumia kwa kutojua kwao na hatia yao. Alipumua dua tu ya kuwaombea msamaha, - "kwa kuwa hawajui watendalo."

Ikiwa wangejua kwamba walikuwa wanamtesa Yeye aliyekuwa amekuja kuiokoa jamii ya wanadamu kutoka katika uangamivu wa milele, wangetekewa kwa woga na hofu. Lakini kutokujua kwao hakukuondoa hatia yao; maana walikuwa na fursa ya kujua na kumkubali Yesu kama **(745)** Mwokozi wao. Baadhi yao wangeweza kuona hata dhambi yao, na kutubu, wakaongoka. Wengine kwa ukaidi wao wangefanya isiwezekane ombi la Kristo kujibiwa kwa ajili yao. Lakini, kwa njia hiyo, kusudi la Mungu lilikuwa linafikia utimilifu wake. Yesu alikuwa anapata haki ya kuwa mtetezi wa wanadamu mbele za Baba.

Ombi lile la Kristo kwa ajili ya adui zake liliuhusu ulimwengu. Lilimjumuisha kila mdhambi ambaye alikuwa amepata kuishi au ambaye angeishi, tangu mwanzo wa ulimwengu mpaka mwisho wa wakati. Hatia ya kumsulibisha Mwana wa Mungu iko juu ya wote. Msamaha umetolewa kwa wote bure. "Yeyote atakaye" aweza kuwa na amani na Mungu, na kuurithi uzima wa milele.

Mara tu baada ya Yesu kupigiliwa msalabani, msalaba uliinuliwa na watu wenye nguvu, na kwa kutumia nguvu nyingi za kikatili waliushindilia mahali palipoandaliwa kwa ajili yake. Tendo hili lilisababisha maumivu makali mno kwa Mwana wa Mungu. Halafu Pilato aliandika maelezo kwa Kiebrania, Kiyunani, na Kilatini, na kuyaweka kwenye msalaba, juu ya kichwa cha Yesu. Yalisomeka hivi, "Yesu Mnazareti, Mfalme wa Wayahudi." Maandishi haya ya anwani yaliwakera Wayahudi. Katika mahakama ya Pilato walikuwa wamepaza sauti wakisema, "Msulibishe." "Sisi hatuna mfalme ila Kaisari." Yohana 19:15. Walikuwa wametangaza kwamba yeyote ambaye angetambua mfalme mwingine yeyote alikuwa ni msaliti. Pilato aliandika maneno ya mwelekeo waliokuwa wameonyesha. Hakuna jinai iliyokuwa imetajwa, isipokuwa kwamba Yesu alikuwa Mfalme wa Wayahudi. Maelezo yale ya anwani yalikuwa ni ishara ya kutambua hali ya Wayahudi kujikabidhi chini ya utawala wa Kirumi. Anwani ile ilitangaza kwamba yeyote ambaye angedai kuwa Mfalme wa Wayahudi wangemhukumu stahili ya kifo. Makuhani walikuwa wamejikweza. Wakati walipokuwa wakifanya njama za kifo cha Yesu, Kayafa alikuwa ametangaza kuwa ni muhimu mtu mmoja afe ili kuliokoa taifa. Sasa unafiki wao ulifunuliwa. Ili kumwangamiza Kristo, walikuwa tayari kutoa kafara hata uwepo wa taifa lao.

Makuhani waliona kile walichokuwa wamefanya, na wakamwomba Pilato abadili anwani ile. Walisema kwamba, "Usiandike, Mfalme wa Wayahudi; bali ya kwamba yule alisema, Mimi ni mfalme wa Wayahudi." Lakini Pilato alikuwa na hasira dhidi yake mwenyewe kwa sababu ya udhaifu wake aliokuwa ameonyesha kabla, na aliwadharau wale makuhani na wakuu wenye wivu na ujanja. Aliwajibu kwa kutopendezwa, "Niliyoandika nimeyaandika."

Mamlaka iliyo juu kuliko Pilato na kuliko Wayahudi ilikuwa imeelekeza kwamba anwani ile iwekwe juu ya kichwa cha Yesu. Kwa uwezo wa Mungu anwani ile ingeamsha mawazo, na hali ya kuyachunguza Maandiko. Mahali pale Kristo aliposulibishiwa palikuwa karibu na mji. Maelfu ya watu kutoka nchi zote walikuwa Yerusalemu wakati ule, na maelezo yale yanayomtangaza Yesu wa **(746)** Nazareti kuwa Masihi yangeonekana kwao. Ilikuwa ni ukweli ulio hai, ulionukuliwa na mkono ulioongozwa na Mungu.

Katika kule kuteseka kwa Kristo msalabani unabii ulitimizwa. Karne kadhaa kabla ya kusulibishwa, Mwokozi alikuwa ametabiri mambo ambayo angetendewa. Alisema, "Kwa maana mbwa wamenizunguka; Kusanyiko la waovu wamenisonga; Wamenizua mikono na miguu. Naweza kuihesabu mifupa yangu yote; Wao wananitazama na kunikodolea macho. Wanagawanya nguo zangu, Na vazi langu wanalipigia kura." Zaburi 22:16-18. Unabii unaohusu mavazi yake ulitekelezwa bila kushauriwa wala kuingiliwa na marafiki au maadui wa Yeye aliyesulibiwa. Nguo zake zilitolewa kwa askari waliokuwa wamemweka msalabani. Kristo alisikia majadiliano ya watu wale wakati walipokuwa wanagawana mavazi yake. Kanzu yake ilifumwa yote haikushonwa, nao wakasema, "Tusiipasue, lakini tuipigie kura, iwe ya nani."

Katika unabii mwingine Mwokozi alitangaza kwamba, "Laumu imenivunja moyo, Nami ninaugua sana. Nikangoja aje wa kunihurumia, wala hakuna; Na wa kunifariji, wala sikumwona mtu. Wakanipa uchungu kuwa chakula changu; Nami nilipokuwa na kiu wakaninywesha siki." Zaburi 69:20, 21. Kwa kawaida iliruhusiwa kuwapa dawa ya kunywa wale wanaoteseka msalabani karibu na kufa ili kupunguza hisia ya maumivu kwao. Yesu alipewa kitu kama hicho; lakini alipokionja, alikikataa. Asingekubali kitu kinachopumbaza akili yake. Lazima imani yake isimame imara kwa Mungu. Hapo ndipo mahali kulipokuwa na nguvu zake. Kuhafifisha hisia zake kungemnufaisha Shetani.

Adui za Yesu walipata nafasi ya kumaliza hasira zao kwake walipomwona akining'inia kwenye msalaba. Makuhani, wakuu na waandishi waliungana na kundi la watu wa fujo kumdhihaki Mwokozi aliyekuwa katika kufa. Wakati wa kubatizwa na wakati wa kubadilika sura sauti ya Mungu ilikuwa imesikika ikimtangaza Kristo kwamba ni Mwana wake. Tena, muda tu kabla ya kusalitiwa kwa Kristo, Baba alikuwa amenena, akishuhudia uungu wa Kristo. Lakini sasa sauti kutoka mbinguni ilikuwa kimya. Hakuna ushuhuda uliosikika wa kumtetea Kristo. Aliteseka kwa matukano na dhihaka toka kwa waovu akiwa peke yake.

Walisema, "Ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu, shuka msalabani." "Na ajiokoe mwenyewe, kama ndiye Kristo wa Mungu, mteule wake." Kule katika jangwa la majaribu Shetani alikuwa amesema, "Ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu, amuru kwamba mawe haya yawe mikate." "Ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu jitupe chini" kutoka kwenye kinara cha hekalu. Mathayo 4:3, 6. Na Shetani pamoja na malaika zake, wakiwa katika miili ya wanadamu, walikuwepo mahali pa **(749)** msalaba. Mwovu mkuu na majeshi yake walikuwa wanashirikiana na makuhani na wakuu. Waalimu wa watu walikuwa wamehamasisha makundi ya fujo yasiyojua ili yatamke hukumu dhidi ya Yeye ambaye wengi wao walikuwa hata hawajapata kumwona, hadi wakati huo walipotakiwa kutoa ushahidi dhidi yake. Makuhani, wakuu, Mafarisayo, na makundi ya watu wa kawaida waliofanywa kuwa na mioyo migumu waliunganishwa pamoja katika nguvu za kishetani. Wakuu wa dini waliungana na Shetani na malaika zake. Walikuwa wanafanya matakwa yake.

Yesu, akiteseka na kufa, alisikia kila neno wakati makuhani walipokuwa wakisema, "Aliokoa wengine, hawezi kujiokoa mwenyewe. Yeye ni mfalme wa Israeli; na ashuke sasa msalabani, nasi tutamwamini." Yesu angeweza kushuka chini kutoka msalabani. Lakini hakufanya hivyo kwa sababu asingeweza kujiokoa mwenyewe na bado mdhambi akapata tumaini la msamaha na kukubaliwa na Mungu.

Katika kumdhihaki kwao Mwokozi, watu waliojidai kuwa ndio werevu wa unabii walikuwa wanarudia maneno yale yale ambayo Uvuvio ulikuwa umetabiri kwamba wangeyatamka wakati wa tukio hili. Lakini katika upofu wao hawakuona kwamba wanatimiza unabii ule. Wale ambao walisema kwamba, "Amemtegemea Mungu; na amwokoe sasa, kama anamtaka; kwa maana alisema, Mimi ni Mwana wa Mungu," walijua kidogo sana kama ushuhuda wao ungesikika kwa vizazi ambavyo vingefuata. Lakini ingawa yalisemwa kwa dhihaka, maneno haya yaliwafanya watu wachunguze Maandiko kwa namna ambayo hawakupata kufanya kabla. Wenye hekima walisikia, wakachunguza, wakatafakari, na wakaomba. Wapo wale ambao hawakupumzika mpaka, kwa kulinganisha andiko na andiko, walipoona maana ya kazi ya Kristo. Kamwe hakukupata kuwepo kabla ufahamu wa jumla kuhusu Yesu kama wakati aliponing'inia kwenye msalaba. Nuru ya ukweli ilikuwa inamlika ndani ya mioyo ya wengi walioona tukio la kusulibishwa, na ambao walisikia maneno ya Kristo.

Katika mateso yake Yesu mwale mmoja wa nuru ya faraja ulitokeza. Huo ulikuwa ni ombi la mnyang'anyi atubuye. Mwanzoni wale wanyang'anyi wote wawili waliosulibishwa pamoja naye walikuwa wamemshutumu; na mmoja akiwa katika mateso yake alizidi tu kuwa mbaya na mpotofu. Lakini mwenzake hakuwa hivyo. Mtu huyu hakuwa mhalifu mwenye moyo mgumu; alikuwa amepotoshwa na mashirikiano maovu, lakini alikuwa na hatia kidogo kuliko wengi wa wale waliokuwa wamesimama pale kando ya msalaba wakimtendea mabaya Mwokozi. Alikuwa amepata kumwona na kumsikiliza Yesu, na alikuwa amesadikishwa na mafundisho yake, lakini makuhani na wakuu walikuwa wamemgeuzia mbali na Yesu. Akitafuta kukatiza usadikisho, alikuwa amezama zaidi na zaidi katika dimbwi la dhambi, mpaka akatiwa nguvuni, akashtakiwa kama mhalifu, na kuhukumiwa kufa msalabani. Katika ukumbi wa hukumu na katika njia ya kwenda Kalvari alikuwa pamoja na Yesu. Alikuwa amemsikia Pilato akitangaza kwamba, "Mimi sioni hatia yoyote kwake." Yohana 19:4. Alikuwa amegundua **(750)** mwonekano wake wa wema, na huruma yake ya kuwasamehe watesi wake. Akiwa pale msalabani anawaona wakuu wa dini wengi wakirusha maneno ya kejeli, na kumkashfu Bwana Yesu. Anaviona

vichwa vinavyotikiswa-tikiswa. Anayasikia maneno mabaya ambayo yamedakwa na mwenzake mwenye hatia akisema: "Je! Wewe si Kristo? Jiokoe nafsi yako na sisi." Miongoni mwa wanaopita pale anawasikia wengi wakimtetea Yesu. Anawasikia wakirudia maneno ya Yesu, na kusimulia kazi zake. Usadikisho unamrudia kwamba huyu ni Kristo. Akimgeukia mhalifu mwenzake alisema, "Wewe humwogopi hata Mungu, nawe u katika hukumu iyo hiyo?" Wale wezi ambao wanakufa hawana cha kuogopa tena kwa watu. Lakini kwa mmoja wao kuna msukumo unaomshawishi kwamba yuko Mungu wa kumwogopa, na kuna siku za usoni za kumfanya atetemeke. Na sasa, akiwa amechafuliwa na dhambi kama alivyokuwa, historia ya maisha yake inakaribia kufungwa. Anaomboleza akisema, "Nayo ni haki kwetu sisi, kwa kuwa tunapokea malipo tuliyostahili kwa matendo yetu; bali huyu hakutenda lolote lisilofaa."

Sasa hakuna swali. Hakuna mashaka, hakuna lawama. Alipohukumiwa kwa uhalifu wake, mwizi yule alikuwa amekuwa asiye na matumaini na aliyekata tamaa; lakini mawazo mageni, ya upendo sasa yaliibuka. Anakumbuka yote aliyosikia kuhusu Yesu, jinsi alivyokuwa ameponya wagonjwa na kusamehe dhambi. Alikuwa amesikia maneno ya wale walioamini katika Yesu na kumfuata wakilia. Alikuwa ameona na kusoma yale maelezo pale juu ya kichwa cha Mwokozi. Alikuwa amewasikia wapita-njia wakiyarudia-rudia, baadhi wakiyasema kwa midomo ya kutetemeka kwa majonzi, na wengine kwa kejeli na dhihaka. Roho Mtakatifu anamlikia akili yake, na kidogo-kidogo mnyororo wa ushahidi unaungana pamoja. Katika Yesu, aliyechubuliwa, kudhihakiwa na anayening'inia msalabani, anamwona Mwana-kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu. Tumaini linachanganyika na maumivu ya mateso katika sauti yake kama mtu anayekufa asiye na tumaini anajikabidhi kwa Mwokozi. Analia akisema, "Bwana, nikumbuke utakapoingia katika ufalme wako" (KJV).

Jibu lilikuja haraka. Sauti nyororo na tamu, iliyojaa upendo, huruma na nguvu, ilitoka ikiwa na maneno: Amin, nakuambia leo hivi, utakuwa pamoja nami peponi.

Kwa saa ndefu za mateso ya Yesu, matukano na dhihaka vilikuwa vimeingia katika masikio yake. Kadiri alivyoning'inia msalabani, bado sauti ya kejeli na laana zinaelea-elea. Kwa moyo wenye hamu ametafuta kusikia sauti kutoka kwa wanafunzi wake za kuonyesha imani yao. Amesikia maneno ya kuomboleza tu yasemayo, "Tulikuwa tukitumaini ya kuwa yeye ndiye atakayewakomboa Israeli." Ilikuwa furaha kiasi gani sasa kwa Mwokozi kusikia maneno ya imani na upendo yatokayo kwa mnyang'anyi anayekufa! Wakati Wayahudi walioko mbele wanamkana, na hata wanafunzi wanakuwa na mashaka kuhusu uungu wake, maskini mnyang'anyi, ambaye yuko kwenye **(751)** ukingo wa umilele, anamwita Yesu "Bwana." Wengi walikuwa tayari kumwita Bwana wakati alipotenda miujiza, na baada ya kuwa amefufuka kutoka kaburini; lakini hakuna mtu aliyemkiri wakati alipokuwa ananing'inia na kufa msalabani isipokuwa mwizi anayetubu ambaye aliokolewa katika saa ya mwisho.

Watu waliokuwa pale waliyasikia maneno yale wakati mwizi alipomwita Yesu kuwa ni Bwana. Sauti ya mtu huyu aliyekuwa anatubu ilivuta hisia zao. Wale waliokuwa chini ya msalaba wakibishana katika kugawana mavazi ya Kristo, na kuyapigia kura, waliacha kwanza wakasikiliza. Sauti zao za mahasira zilinyamazishwa. Kwa kupigwa butwaa walimtazama Kristo, na wakasubiria jibu ambalo lingetoka katika midomo yake anayekufa.

Aliposema maneno yale ya ahadi, wingu la giza lililoonekana kuuzunguka msalaba lilipenywa na nuru angavu iliyo hai. Amani kamili ya kukubaliwa na Mungu ilimjia yule mwizi aliyetubu. Yesu aliyekuwa katika mateso alitukuzwa. Yeye ambaye alionekana kushindwa kwa mujibu wa macho ya wengine wote alikuwa ndiye Mshindi. Alitambuliwa kwamba ndiye Mbebaji wa Dhambi. Watu wanaweza wakaonyesha nguvu zao kwenye mwili wake. Wanaweza kulichoma hekalu lile takatifu kwa taji ya miiba. Wanaweza kumnyang'anya mavazi yake, na kugombana kuhusu namna ya kuyagawa. Lakini hawawezi kumnyang'anya uwezo wake wa kusamehe dhambi. Katika kufa anaonyesha ushuhuda wa uungu wake na wa utukufu wa Baba. Sikio lake si zito hata lisisikie, wala mkono wake si mfupi hata usiweze kuokoa. Ni haki yake ya kifalme kuwaokoa kabisa wote wajao kwa Mungu kupitia kwake.

Nakwambia leo hivi, utakuwa pamoja nami peponi. Kristo hakuahidi kwamba mwizi yule angekuwa pamoja na Yeye peponi siku ile ile. Yeye mwenyewe hakwenda peponi siku ile. Alilala kaburini, na asubuhi ya kufufuka kwake alisema, "Sijapaa kwenda kwa Baba." Yohana 20:17. Lakini mnamo siku ya kusulibishwa, siku inayoonekana kama vile ni ya kushindwa na ya giza, ndipo ahadi hiyo ilipotolewa. "Leo" wakati akiwa anakufa msalabani kama mhalifu, Kristo anamhakikishia maskini huyu mdhambi kwamba, Utakuwa pamoja nami peponi.

Wale wezi waliosulibishwa pamoja na Yesu waliwekwa "mmoja huku na mmoja huku, na Yesu katikati." Jambo hili lilifanywa kwa maelekezo ya makuhani na wakuu. Nafasi ya Kristo ya katikati ya wezi ilikuwa inaashiria kwamba Yeye alikuwa mhalifu mkuu kuliko wote wale. Hivyo maandiko haya yalitimia, "Akahesabiwa pamoja na hao wakosao." Isaya 53:12. Lakini mahuhani hawakuona maana kamili ya kitendo chao kile. Kama vile ambavyo Yesu, aliyesulibiwa pamoja na wezi, alivyowekwa "katikati," ndivyo msalaba wake ulivyowekwa katikati ya ulimwengu ulio dhambini. Na maneno ya msamaha aliyoambiwa yule mwizi yaliwasha nuru ambayo itayaangazia maeneo yasiyofikika ya dunia.

**(752)** Kwa mshangao malaika waliangalia upendo mkuu wa Yesu, ambaye, akiwa anateseka kwa maumivu makali ya akili na mwili, aliwafikiria wengine tu, na akaitia moyo nafsi itubuyo kuamini. Katika mateso yake Yeye kama nabiinalikuwa amenena kwa binti za Yerusalemu; kama kuhani na mtetezi alikuwa amemwomba Baba kuwasamehe wauaji wake; kama Mwokozi mwenye upendo alikuwa amesamehe dhambi za za mwizi yule aliyetubu.

Kadiri macho ya Yesu yalivyokuwa yakipita kwa umati wa watu waliokuwa karibu naye, mtu mmoja alivuta hisia zake. Chini ya msalaba alikuwepo mama yake, akiwa anategemezwa na mwanafunzi Yohana. Hakuweza kuvumilia kusalia mbali na Mwana wake; naye Yohana, akijua kuwa mwisho ulikuwa karibu, alikuwa amemrudisha tena mahali pa msalaba. Katika saa yake ya kufa, Kristo alimkumbuka mama yake. Akiuangalia uso wa mama yake uliokuwa umejawa na majonzi na akamwangalia Yohana, alimwambia mama, "Mama, tazama, mwanao!" halafu akamwambia Yohana, "Tazama, mama yako!" Yohana alielewa maneno ya Kristo, na alikubali dhamana ile. Mara ile ile alimchukua Mariamu na kumpeleka nyumbani kwake yeye, na tangu pale alimtunza kwa upendo. Mwokozi mwenye upendo na huruma; katikati ya maumivu ya mwili na mateso ya akili, alifikiria kumjali mama yake! Hakuwa na pesa ya kumpa ili kumfariji; lakini aliiamini dhamana ya moyo wa Yohana, na alimkabidhi kwa Yohana mama yake kama kumbukumbu yake ya thamani. Kwa njia hiyo alimpatia mama kile alichohitaji zaidi, - huruma ya upendo ya mtu ampendaye kwa sababu mama yule alimpenda Yesu. Na katika kumpokea mama yule kama amana takatifu, Yohana alikuwa anapokea mbaraka mkubwa. Yule mama alikuwa ni kumbukumbu ya Yohana ya wakati wote kuhusu Bwana wake mpendwa.

Mfano kamili wa upendo wa Yesu kwa mzazi unaangaza katika ukungu wa vizazi kwa mnga’ao usiozimika. Kwa karibu miaka thelathini Yesu alikuwa amesaidia kubeba mizigo ya nyumbani kwa mahangaiko yake ya kazi za kila siku. Na sasa, hata katika mateso yake ya mwisho, anakumbuka kukidhi mahitaji ya mama yake mjane aliye katika huzuni. Roho kama hiyo itaonekana ndani ya kila mwanafunzi wa Bwana wetu. Wale wanaomfuata Kristo wanaona kwamba kuwaheshimu na kukidhi mahitaji ya wazazi wao ni sehemu ya dini yao. Baba na mama hawatakosa kamwe kupokea hali ya kujali na huruma ya upendo kutoka kwa mtu mwenye moyo wenye upendo wa Kristo.

Na sasa Bwana wa utukufu alikuwa anakufa, akiwa fidia kwa ajili ya wanadamu. Katika kuutoa uhai wake wa thamani, Kristo hakuhimizwa na furaha ya ushindi. Mambo yote yalikuwa ni majonzi tu. Si hofu ya kifo iliyomwelemea. Si maumivu wala kupoteza heshima kwa sababu ya msalaba vilivyomsababishia maumivu yasiyoelezeka. Kristo alikuwa mkuu wa wanaoteseka; lakini mateso yake yalisababishwa na kujua ukubwa wa mweleko wa dhambi, kujua kwamba **(753)** kwa njia ya kufahamiana na uovu, mwanadamu amepofushwa katika matendo ya dhambi. Kristo aliona jinsi mzizi wa dhambi ulivyo na kina kirefu katika moyo wa mwanadamu, jinsi ambavyo wachache tu ndio wangependa kubomoa ngome ya dhambi na kutoroka kutoka humo. Alijua kwamba pasipo msaada kutoka kwa Mungu, lazima mwanadamu apotee, na aliona watu wengi wakipotea huku wakiwa mahali ambapo wanaweza kuufikia msaada mwingi wa kutosha.

Uovu wetu wote uliwekwa juu ya Kristo aliyekuwa mbadala na mdhamini wetu. Alihesabiwa kama mkosaji, ili ya kwamba apate kutukomboa kutoka katika hukumu ya sheria. Hatia ya kila mzao wa Adamu ilikuwa inatia uzito katika moyo wa mwanadamu. Ghadhabu ya Mungu dhidi ya dhambi, udhihirisho wa kutisha wa kuchukizwa kwake kwa sababu ya uovu, viliujaza moyo wa Mwana wake kwa ukali. Maisha ya Kristo yote yalikuwa yanautangazia ulimwengu ulioanguka habari njema ya neema ya Baba na upendo wake usameheo. Wokovu kwa mwenye dhambi mkuu ilikuwa ndiyo mada yake. Lakini sasa akiwa na uzito wa kutisha aliokuwa amebeba, hawezi kuuona uso wa Baba wa upatanisho. Kuondolewa kwa sura ya kimbingu kutoka kwa Mwokozi mnamo saa hii ya maumivu makali kuliuchoma moyo wake kwa huzuni ambayo kamwe haiwezi kueleweka kwa

mwanadamu. Machungu haya yalikuwa makubwa mno kiasi kwamba maumivu ya mwili hayakusikika kwa urahisi.

Kwa kutumia majaribu makali sana Shetani aliufinya moyo wa Yesu. Yesu hakuweza kuona kupitia katika milango ya kaburi. Tumaini halikumwonyesha kufufuka kwake kutoka kaburini kama mshindi, au kumwambia kuhusu kukubalika kwa kafara yake kwa Baba. Aliogopa kwamba dhambi ilikuwa ni chukizo kubwa sana kwa Mungu kiasi kwamba kutengana kwao kungekuwa kwa milele. Kristo alihisi maumivu ambayo mdhambi atakuwa nayo wakati rehema itakapokuwa haipo tena ili kumbembeleza mwenye hatia. Ilikuwa ni hisia ya dhambi, ile iletayo ghadhabu ya Baba juu yake Kristo aliye mbadala wa mwanadamu, iliyofanya kile kikombe alichokinywea kuwa kichungu sana, na kuuvunja moyo wa Mwana wa Mungu.

Kwa mshangao malaika walishuhudia maumivu yale ya Mwokozi. Majeshi ya mbinguni yalifunika nyuso zao ili yasione jambo lile la kuogofya. Vitu vya asili visivyo hai vilionyesha huruma kwa Mwasisi wake aliyekuwa akitukanwa na kufa. Jua lilikataa kutazama tukio lile la kutisha. Mionzi yake kamili na angavu ilikuwa inaangazia dunia wakati wa katikati ya mchana, wakati ambapo ghafla lilionekana kama vile limeondoshwa. Giza kamili, lililo kama guo jeusi la msiba, liliufunika msalaba. "Palikuwa na giza juu ya nchi yote hata saa tisa." Hakukuwa na kupatwa kwa jua wala sababu nyingine ya asili ya giza hili, ambalo lilikuwa nene kama la usiku wa manane bila mwezi wala nyota. Ilikuwa ni ushuhuda wa kimwujiza uliotolewa na Mungu ili kwamba imani ya vizazi vya baada ya wakati huo ithibitike.

Uwepo wa Mungu ulifichwa katika giza lile nene. Yeye hulifanya giza kuwa hema lake, na huustiri utukufu wake mbali na macho ya wanadamu. Mungu na **(754)** malaika zake watakatifu walikuwa kando ya ule msalaba. Baba alikuwa pamoja na Mwana wake. Lakini uwepo wake haukufunuliwa. Ikiwa utukufu wake ungemlika kutoka katika wingu lile, kila mwanadamu ambaye angeona angeangamia. Na katika saa ile ya kutisha Kristo hakupaswa kufarijiwa kwa uwepo wa Baba yake. Alitembea katika shinikizo akiwa peke yake, na miongoni mwa wanadamu hakuwepo aliyekuwa pamoja naye.

Katika giza lile nene, Mungu aliyafunika mateso ya mwisho-mwisho ya Mwana wake. Wote waliokuwa wamemwona Kristo katika mateso yake walikuwa wamesadikishwa kuhusu uungu wake. Uso ule, ambao wakati fulani ulikuwa unaonwa na wanadamu, haukusahauliwa kamwe. Kama vile uso wa Kaini ulivyomdhihirisha kwamba ni mwuaji, vivyo hivyo uso wa Kristo ulidhihirisha kutokuwa na hatia, usafi, ukarimu, - sura ya Mungu. Lakini washtaki wake hawakuweza kuusikiza muhuri huu wa mbinguni. Kwa saa nyingi za mateso Kristo alikuwa ametazamwa na umati mkubwa wa watu wenye mizaha. Sasa kwa rehema alikuwa amefichwa na kifuniko cha Mungu.

Ukimya kama wa kaburi ulionekana kukifunika kilima cha Kalvari. Hofu isiyo na jina iliwashika makutano waliokuwa wamekusanyika karibu na msalaba. Maneno ya kulaani na kukashfu yalikomea katikati ya sentensi zilizotamkwa nusu-nusu. Wanaume, wanawake, na watoto walianguka chini kifudifudi. Umeme wa radi zilizo bayana ulimlika kutoka katika wingu, na kuuonyesha msalaba na Mkombozi aliyeangikwa hapo. Makuhani, wakuu, waandishi, watu wanaotekeleza mateso, na kundi la watu wenye fujo, wote walifikiri kwamba wakati wao wa kupatilizwa umekuja. Baada ya muda baadhi ya watu walinong'onezana kwamba huenda Yesu akashuka sasa kutoka msalabani. Baadhi walijaribu kushika njia ya kurudi mjini, huku wakijipiga-piga vifua vyao na kulia kwa hofu.

Saa tisa giza liliondoka kwa watu, lakini likaendelea kumzunguka Mwokozi. Lilikuwa ni ishara ya maumivu na utisho vilivyokuwa moyoni mwake. Hakuna jicho lililoweza kupenya kiza kilichozunguka msalaba, na hakuna mtu aliyeweza kupenya katika kiza kile kilichoizunguka nafsi ya Kristo inayoteseka. Radi zenye hasira zilionekana kama zikivurumishwa kwake alipokuwa akining'inia msalabani. Ndipo "Yesu akapaza sauti yake kwa nguvu akisema, Eloi, Eloi, lama sabakthani? Yaani, Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?" Pindi kiza kile kilivyotulia kumzunguka Mwokozi, sauti nyingi zilisikika zikisema: Kisasi cha Mungu ki juu yake. Radi za hasira ya Mungu zinavurumishwa kwake, kwa kuwa alijidai kuwa Mwana wa Mungu. Wengi waliomwamini walisikia kilio chake cha uchungu. Matumaini yaliwaacha. Ikiwa Mungu amemwacha Yesu, wafuasi wake wangetumainia nini tena?

Giza lilipoondoka na kuiacha roho ya Kristo iliyofinywa, alirejea katika hali ya kusikia maumivu ya kimwili, na akasema, "Naona kiu." Mmoja wa **(755)** askari wale wa Kirumi, aliyeguswa na huruma kadiri alivyoona midomo ile iliyokauka, alichukua sifongo kwenye ufito wa hisopo, na akiichovya ndani ya chombo chenye siki, alimpa Yesu. Lakini makuhani walimdhihaki katika mateso yake. Wakati giza lilipokuwa limeifunika dunia walikuwa wamepatwa na hofu; hofu yao ilipotoweka, hofu ilikuja kwamba huenda Yesu bado akawaponyoka. Walikuwa wametafsiri vibaya maneno yake kwamba, "Eloi, Eloi, lama sabakthani?" Kwa kuchukizwa na kupinga walisema, "Huyu anamwita Eliya." Walikatalia fursa ya mwisho ya kumwondoa Yesu matesoni. Walisema, "Acha; na tuone kama Eliya anakuja kumwokoa."

Mwana wa Mungu asiye na kosa alining'inia msalabani, nyama ya mwili wake ikiwa imetobolewa kwa misumari; mikono ile ambayo mara kwa mara iliwafikia watu kuwabariki, ilikuwa imepigiliwa misumari kwenye mbao za mti; miguu ile ambayo ilikuwa haichoki katika kuhudumia kwa upendo, ilikuwa imepigiliwa misumari kwenye mti; kile kichwa cha kifalme kilikuwa kimechomwa na taji ya miiba; midomo ile iliyokuwa ikitetema ilifanywa kuwa katika mwonekano wa kilio cha taabu. Na hayo yote aliyostahimili, - matone ya damu yaliyotiririka kutoka kichwani mwake, mikononi mwake, miguuni mwake, maumivu yaliyoharibu umbo lake, na maumivu yasiyotamkika yaliyoujaza moyo wake wakati uso wa Baba yake ulipofichwa kutoka kwake – yanazungumza na kila mtoto wa mwanadamu, na kutangaza kwamba, Mwana wa Mungu anahiari kubeba mzigo huu wa hatia kwa ajili yako; ameharibu nguvu ya kifo kwa ajili yako, na kufungua malango ya Paradiso. Yeye aliyetuliza mawimbi yenye hasira na akatembea juu ya mapovu ya maji, aliyeyafanya mapepo kutetemeka na magonjwa kutoweka, aliyeyafungua macho ya waliopofuka na kuwaita wafu warejee kuishi, - anajitoa kama kafara msalabani, na hii ni kwa sababu ya upendo kwako. **(756)** Yeye, Mbeba Dhambi, alistahimili ghadhabu ya haki ya kimbingu, na kwa ajili yako anakuwa dhambi yenyewe.

Wakiwa kimya watu waliokuwa wanaangalia walitazama wakisubiri kuuona mwisho wa tukio lile la kutisha. Jua liliangaza; lakini msalaba ulikuwa bado umefunikwa na giza. Makuhani na wakuu waligeuka kuungalia mji wa Yerusalemu; na tazama, wingu zito lilikuwa juu ya mji na nyanda za tambarare za Uyahudi. Jua la Haki, Nuru ya ulimwengu, lilikuwa linaondoa miale yake kutoka kwenye mji wa Yerusalemu ambao ulipata kupendwa. Zile radi kali za hasira ya Mungu zilielekezwa kuwa dhidi ya mji huo ulio katika hatima mbaya.

Ghafla giza liliondoka kwenye msalaba, na kwa sauti ya kusikika, kama ya tarumbeta, iliyoonekana kufika katika uumbaji wote, Yesu alipaza sauti akisema, "Imekwisha." "Ee Baba, mikononi mwako naiweka roho yangu." Nuru iliuzunguka msalaba, na uso wa Mwokozi uling'aa kwa utukufu kama wa jua. Halafu aliinamisha kichwa chake kifuani mwake, akafa.

Katikati ya giza lile la kuogofya, akionekana kama ameachwa na Mungu, Kristo alikuwa anamalizia kunywa machicha ya mwisho katika kikombe cha ole wa mwanadamu. Katika saa hizo za kutisha alikuwa ametegemea ushuhuda wa kukubaliwa na Baba yake ambao ulitolewa kwake baadaye. Alikuwa anajua vema tabia ya Baba yake; alielewa haki yake, rehema yake, na upendo wake mkuu. Kwa imani alipumzika ndani ya Yeye ambaye daima imekuwa furaha yake kumtii. Na kama katika kujisalimisha kwake alivyojikabidhi kwa Mungu, ile hisia ya kupotelewa na upendo wa Baba yake iliondolewa. Kwa imani Kristo alikuwa mshindi.

Kamwe dunia haikupata kushuhudia tukio kama lile kabla. Umati ule ulibaki umepooza, na ukiwa unashangaa kumwangalia Mwokozi. Kwa mara nyingine tena jua liliifunika dunia, na sauti kubwa kama ya radi ilisikika. Kulikuwa na tetemeko kubwa. Watu walitetemeshwa na kusukwasukwa wakikusanywa pamoja katika malundo. Kulikuwa na hali ngeni ya kuchanganyikiwa na kushangaza. Katika milima iliyo jirani, miamba ilipasuka, na kuporomokea katika tambarare. Makaburi yalivunjika yakafunguka, na wafu walitupwa nje ya makaburi yao. Ilionekana kama uumbaji wote ulikuwa unavunjika kuwa vichembe vidogo. Makuhani, wakuu, askari, wale watekelezaji wa mateso, na watu, wakiwa kimya kwa hofu, walikuwa wamelala chini kifudifudi.

Wakati ile sauti kuu kwamba, "Imekwisha" ilipotoka katika midomo ya Kristo, makuhani walikuwa wakihudumu hekaluni. Ilikuwa ni saa ya dhabihu ya jioni. Mwana-kondoo anayemwakilisha Kristo alikuwa ameletwa ili kuchinjwa. Akiwa amevalia mavazi yake muhimu na mazuri, kuhani alisimama akiwa ameinua kisu juu, kama Ibrahimu alivyofanya wakati alipotaka kumchinja mwana wake. Kwa hamu kubwa watu walikuwa wanatazama. Lakini sasa ardhi inatikisika na kutetemeka; **(757)** kwa kuwa Bwana mwenyewe alikuja karibu. Kwa sauti kama ya kelele pazia la ndani ya hekalu likachanwa na mkono usioonekana tangu juu mpaka chini, likipaacha mahali

ambapo kabla palijawa na uwepo wa Mungu pakiwa wazi na kuonwa na umati wa watu. Mahali hapa ndipo palipokuwa na Shekina. Hapa ndipo mahali ambapo Mungu alikuwa amedhihirisha utukufu wake juu ya kiti cha rehema. Hakuna mtu aliyepata kunyenyua pazia hili linalotenganisha kati ya chumba hiki na sehemu nyingine ya hekalu isipokuwa kuhani mkuu tu. Aliingia humu mara moja tu kwa mwaka kwa ajili ya kufanya upatanisho kwa dhambi za watu. Lakini sasa, tazama, pazia hili limepasuka vipande viwili. Patakatifu pa patakatifu pa duniani si patakatifu tena.

Mambo yote yanatisha na ni kuchanganyikiwa. Kuhani anakaribia kumchinja kondoo wa kafara; lakini kisu kinadondoka kutoka katika mikono yake iliyoishiwa nguvu, na kondoo anakimbia. Mfano wa kivuli wa kafara umekutana na kafara halisi katika kifo cha Mwana wa Mungu. Dhabihu kuu imefanywa. Njia ya kwenda patakatifu pa patakatifu imefunguliwa. Njia mpya iliyo hai imeandaliwa kwa ajili ya wote. Mwanadamu mwenye dhambi anayehuzunika hahitaji tena kumsubiri kuhani mkuu. Tangu hapo Mwokozi alikuwa ndiye wa kuhudumu kama kuhani na mtetezi mbinguni pa mbingu zote. Ilitokea kama vile sauti ya moja kwa moja ilikuwa imenena na watu wanaoabudu pale ikisema: Sasa ni mwisho wa kafara zote na dhabihu zote kwa ajili ya dhambi. Mwana wa Mungu amekuja kwa mujibu wa neno lake, "Tazama, nimekuja (katika gombo la chuo nimeandikiwa) Niyafanye mapenzi yako, Mungu." "Wala si kwa damu ya mbuzi na ndama, bali kwa damu yake mwenyewe aliingia mara moja tu katika Patakatifu, akiisha kupata ukombozi wa milele." Waebrania 10:7; 9:12.

# Sura ya 79

## "Imekwisha"

Kristo hakuyatoa maisha yake isipokuwa mpaka alipokuwa amekamilisha kazi aliyokuja kufanya, na kwa roho iliyokuwa inamtoka alipaza sauti akisema, "Imekwisha." Yohana 19:30. Ushindi wa vita ulikuwa umepatikana. Mkono wake wa kuume na mkono wake mtakatifu ilikuwa imempatia ushindi. Akiwa kama Mshindi alisimika bendera yake kwenye vilele vya milele. Je! Hakukuwa na furaha miongoni mwa malaika? Mbingu yote ilishangilia kwa ushindi wa Mwokozi, shetani alishindwa, na alijua kwamba ufalme wake ulikuwa umepotea.

Kwa malaika na kwa malimwengu ambayo hayakuanguka kilio kile kwamba "Imekwisha" kilikuwa na maana ya kina. Kazi kuu ya ukombozi ilifanywa kwa ajili yao na kwa ajili yetu. Wao na sisi tunashiriki matunda ya ushindi wa Kristo.

Tabia ya Shetani haikufunuliwa wazi kwa malaika au kwa malimwengu yasiyoanguka isipokuwa hadi wakati wa kifo cha Kristo. Muasi mkuu huyu alikuwa amejivika mwonekano wa uongo kiasi kwamba hata viumbe watakatifu hawakuelewa kanuni yake. Walikuwa hawajaona kwa uwazi hali halisi ya uasi wake.

Kilichokuwa kimemfanya kuwa dhidi ya Mungu kilikuwa ni ile hali ya kuwa na uwezo na utukufu wa ajabu. Kuhusu Lusifa Bwana anasema, "Wewe wakitia muhuri kipimo, umejaa hekima, na ukamilifu wa uzuri." Ezekieli 28:12. Lusifa alikuwa kerubi afunikaye. Kabla alikuwa anasimama katika nuru ya uwepo wa Mungu. Alikuwa wa hali ya juu kuliko viumbe wote walioumbwa, na alikuwa wa nafasi ya juu katika kufunua makusudi ya Mungu kwa malimwengu. Baada ya kuwa ametenda dhambi, uwezo wake wa kudanganya **(759)** ulikuwa wa udanganyifu mkubwa, na ilikuwa vigumu zaidi kupata namna ya kufunua tabia yake halisi, kwa sababu ya nafasi ya juu pamoja na Baba aliyokuwa nayo kabla.

Mungu angeweza kumwangamiza Shetani na wale waliomuunga mkono kwa urahisi kama mtu anavyoweza kutupa chini jiwe dogo; lakini hakufanya hivyo. Uasi haukutakiwa kushindwa kwa mabavu. Nguvu ya kulazimisha inapatikana katika serikali ya Shetani tu. Kanuni za Bwana si za utaratibu huo. Mamlaka yake iko katika wema, rehema, na upendo; na udhihirishaji wa kanuni hizi ndio mbinu za kutumia. Serikali ya Mungu ni ya uadilifu, na ukweli na upendo ndiyo nguvu inayopaswa kuendelezwa.

Kusudi la Mungu lilikuwa ni kuweka mambo katika msingi wa usalama wa milele, na katika mabaraza ya mbinguni iliamuliwa kwamba lazima Shetani apewe muda wa kuendeleza kanuni zilizounda msingi wa serikali yake. Alikuwa amedai kwamba kanuni zake zilikuwa nzuri zaidi kuliko zile za Mungu. Muda ulitolewa ili kanuni za Shetani zifanye kazi, ili kwamba zipate kuonwa na malimwengu ya mbinguni.

Shetani aliwaongoza watu kuingia katika dhambi, na mpango wa wokovu uliwekwa ukaanza kufanya kazi. Kwa miaka elfu nne, Kristo alikuwa anashughulikia kazi ya kumwinua mwanadamu, na Shetani alikuwa akishughulika kwa ajili ya kumwangamiza na kumshusha mwanadamu. Na malimwengu ya mbinguni yaliyaona yote hayo.

Yesu alipokuja katika ulimwengu huu, nguvu za Shetani ziligeuzwa na kusimamishwa dhidi yake. Tangu wakati ule alipojitokeza kule Bethlehemu akiwa kama mtoto, mnyang'anyi huyo alijitahidi sana kwa nyakati tofauti-tofauti kumwangamiza. Kwa kila njia iliyowezekana alijitahidi kuzuia Yesu asikue vema akiwa mtoto aliye mkamilifu, mtu mzima asiye na mapungufu, mwenye huduma takatifu, na aliye dhabihu isiyo na kasoro. Lakini alishindwa. Hakuweza kumwingiza Yesu katika dhambi. Hakuweza kumkatisha tamaa, au kumsukumia kando kutoka katika kazi aliyokuja duniani kuifanya. Tangu kule jangwani mpaka Kalvari, dhoruba ya ghadhabu ya Shetani ilimpiga, lakini kwa kadiri ilivyomwangukia zaidi pasipo huruma, ndivyo Mwana wa Mungu alivyoung'ang'ania kwa nguvu zaidi mkono wa Baba yake, na kusonga mbele kuipita njia ya matone ya damu. Jitihada zote za Shetani za kutaka kumkandamiza na kumshinda ziliishia katika kuleta nuru safi zaidi katika tabia yake njema isiyo na waa.

Mbingu yote na malimwengu yote ambayo hayakuanguka vilikuwa mashuhuda wa pambano hili. Ni kwa hamu kubwa kiasi gani walivyofuatilia mwisho wa matukio ya pambano hili. Walimwona Mwokozi akiingia katika bustani ya Gethsemane, nafsi yake ikiinama chini ikiwa na hali ya kutishwa na giza kuu. Walikisikia kile kilio

chake cha uchungu kwamba, "Baba yangu, ikiwezekana, kikombe hiki kiniepuke." Mathayo 26:39. Kadiri uwepo wa Baba ulivyoondolewa, walimwona akiwa na huzuni pamoja na uchungu wa huzuni ulio zaidi ya ule wa hatua ya mwisho ya kupambana na kifo. Jasho la damu lilisukumwa kupenya katika vinyweleo vyake, na **(760)** lilidondoka chini. Ombi la kutaka kuponywa lilitoka katika midogo yake mara tatu. Mbingu haikuweza tena kuvumilia kuona, na mjumbe wa faraja alitumwa kwa Mwana wa Mungu.

Mbingu ilimwona Mhanga huyu akisalitiwa mikononi mwa kundi la wauaji, na kwa dhihaka na mabavu akaharakishwa kutoka mahakama moja hadi nyingine. Ilizisikia kejeli za watesi wake kuhusu kuzaliwa kwake katika hali duni. Ilisikia maneno ya kumkana yaliyoendana na kulaani na kuapa yakitolewa na mmoja wa wanafunzi wake wapendwa. Iliona kazi mbaya isiyo na mipaka ya Shetani, na nguvu zake juu ya mioyo ya wanadamu. Lo, tukio la kuogofya! Mwokozi anahusuriwa wakati wa usiku wa manane mle Gethsemane, akiburutwa kutoka katika kasiri kwenda katika ukumbi wa hukumu na kurudishwa tena, akiletwa mara mbili kushtakiwa mbele ya makuhani, mara mbili mbele ya Sanhedrin, mara mbili mbele ya Pilato, na mara moja mbele ya Herode, akidhihakiwa, akipigwa, akihukumiwa, na kupelekwa kwenda kusulibiwa, akibeba mzigo mzito wa msalaba, akiwa katikati ya binti za Yerusalemu wanaoomboleza na umati wa watu wenye kejeli.

Mbingu ilimwangalia Kristo kwa majonzi na mshangao akining'inia kwenye msalaba, damu ikitiririka kutoka katika sehemu za mwili zilizojeruhiwa, na jasho lililochanganyika na damu likiwa usoni mwake. Damu ilidondoka kutoka kwenye mikono yake na miguu yake, tone baada ya tone, ikidondokea kwenye mwamba uliochimbiwa shimo kwa ajili ya kushindiliwa msalaba. Majeraha yaliyosababishwa na misumari yalipanuka kadiri uzito wa mwili wake ulivyoivuta mikono yake. Kupumua kwake kwa shida kuliongezeka kasi na kina, kadiri moyo wake ulivyotweta chini ya uzito wa mzigo wa dhambi za ulimwengu. Mbingu yote ilijazwa na mshangao wakati ombi la Yesu lilipotolewa katikati ya mateso makali, akisema, "Baba, uwasamehe; maana hawajui watendalo." Luka 23:34. Lakini bado walisimama pale watu, walioumbwa kwa mfano wa Mungu, wakiungana katika kuuangamiza uhai wa Mwana wake wa pekee. Ni mwonekano gani huu mbele ya malimwengu ya mbinguni!

Mamlaka na nguvu za giza zilikusanywa pamoja kuuzunguka msalaba, zikikitia kivuli cha kuzimu cha kutokuamini katika mioyo ya watu. Wakati Bwana alipowaumba viumbe hawa ili kusimama mbele ya kiti chake cha enzi, walikuwa wazuri na wenye utukufu. Kupendeza kwao na utakatifu wao vilikuwa vinalingana na nafasi za kuinuliwa kwao. Walikuwa wamepewa hekima kubwa ya Mungu, na kuvishwa umaridadi wa mbinguni. Walikuwa wahudumu wa Yehova. Lakini ni nani ambaye angetambua utukufu wa maserafi ndani ya malaika hawa walioanguka ambao wakati fulani walihudumu katika kumbi za mbinguni?

Nguvu za kishetani ziliungana na watu waovu katika kuwaongoza watu kuamini kwamba Kristo ni Mdhambi mkuu, na kumfanya kuwa wa kuchukiwa. Wale waliomdhihaki Kristo alipokuwa ametundikwa msalabani walikuwa wamevuviwa roho ya muasi mkuu wa kwanza. Aliwajaza udhalimu **(761)** na kauli za kuchukiza. Aliwajaza mioyo ya shutuma. Lakini kwa yote haya Shetani hakufanikiwa lolote.

Ikiwa dhambi moja ingeweza kuonekana ndani ya Kristo, ikiwa wakati fulani angejisalimisha kwa Shetani ili kuepuka mateso yale ya kutisha, adui wa Mungu na wanadamu angekuwa ameshinda. Kristo aliinamisha kichwa chake akafa, lakini aliishikilia imani yake na kujikabidhi kwa Mungu. "Nikasikia sauti kuu mbinguni, ikisema, Sasa kumekuwa wokovu, na nguvu, na ufalme wa Mungu wetu, na mamlaka ya Kristo wake; kwa maana ametupwa chini mshtaki wa ndugu zetu, yeye awashtakiye mbele za Mungu wetu, mchana na usiku." Ufunuo 12:10.

Shetani aliona kwamba vazi lake la bandia lilikuwa limechanwa na kutupiliwa mbali. Utawala wake ulifunuliwa wazi mbele ya malaika ambao hawakuanguka na mbele ya malimwengu ya mbinguni. Alikuwa amejifunua kwamba ni mwuaji. Kwa kumwaga damu ya Mwana wa Mungu, alikuwa amejing'oa kutoka katika hali ya kuhurumiwa na viumbe vya mbinguni. Tangu wakati ule kazi yake iliwekewa mipaka. Hata ajifanye kuwa na mtazamo gani, hakuweza tena kuwavizia malaika watokapo katika viunga vya mbinguni, na kuwashtaki ndugu zake Kristo kwamba wamevishwa mavazi meusi na yenye uchafu wa dhambi. Kiunganishi cha mwisho cha huruma kati ya Shetani na ulimwengu wa mbinguni kilivunjwa.

Lakini bado Shetani hakuangamizwa wakati ule. Hata wakati huo bado malaika hawakuelewa mambo yote yaliyohusishwa katika pambano kuu. Kanuni zilizokuwa hatarini zilikuwa zifunuliwe zaidi. Na kwa faida ya mwanadamu, lazima uwepo wa Shetani uendelezwe. Lazima mwanadamu pamoja na malaika waone ukinzani uliopo kati ya Mfalme wa nuru na mfalme wa giza. Lazima mwanadamu achague ambaye atamtumikia.

Wakati wa kuanza kwa pambano kuu, Shetani alikuwa ametangaza kwamba sheria ya Mungu ilikuwa haiwezekani kutiiwa, kwamba haki ilikuwa haipatani na rehema, na kwamba, ikiwa sheria ingevunjwa, ingekuwa vigumu kwa mdhambi kusamehewa. Shetani alisisitiza kwamba, Lazima kila dhambi ikutane na adhabu yake; na ikiwa Mungu ataondoa adhabu ya dhambi, asingekuwa Mungu wa ukweli na haki. Wanadamu walipovunja sheria ya Mungu, na kukiuka mapenzi yake, Shetani alishangilia. Alitangaza kuwa ilikuwa imethibitika kwamba sheria haiwezekani kutiiwa; mwanadamu asingeweza kusamehewa. Kwa sababu alikuwa amefukuzwa mbinguni baada ya kuasi kwake, Shetani alidai kwamba lazima jamii ya wanadamu ifungiwe mbali na upendo wa Mungu milele. Alisisitiza kwamba, Haiwezekani Mungu afuate haki, na bado aonyeshe rehema kwa mdhambi.

Lakini hata akiwa mdhambi, mwanadamu alikuwa katika nafasi iliyo tofauti na ile ya Shetani. Kule mbinguni Lusifa alitenda dhambi akiwa katika nuru ya utukufu wa Mungu. Yeye alipewa ufunuo mkubwa zaidi wa upendo wa Mungu kuliko ilivyofanyika kwa kiumbe mwingine yeyote. **(762)** Akielewa tabia ya Mungu, akifahamu wema wa Mungu, Shetani alichagua ubinafsi wake mwenyewe, utashi wake ulio huru. Uchaguzi huu ulikuwa hitimishi. Hakukuwa na jambo zaidi ambalo Mungu angefanya ili kumwokoa. Lakini mwanadamu alidanganywa; ujanja wa werevu wa Shetani uliitia akili ya mwanadamu giza. Alikuwa hajui kimo na kina cha upendo wa Mungu. Kwa ajili yake kulikuwa na tumaini la kuhitaji kuujua upendo wa Mungu. Kwa kuiona tabia ya Mungu huenda angevutwa kumrudia Mungu.

Kupitia Yesu, rehema ya Mungu ilifunuliwa kwa wanadamu; lakini rehema haiiweki haki kando. Sheria hufunua sifa za tabia ya Mungu, na yodi moja wala nukta moja ya torati haiwezi kubadilishwa ili kukubaliana na hali ya mwanadamu aliyeanguka. Mungu hakubadilisha sheria yake, bali alijitoa kafara Yeye mwenyewe, ndani ya Kristo, kwa ajili ya ukombozi wa mwanadamu. "Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake." 2 Wakorintho 5:19.

Sheria inataka haki, - maisha ya kuwa mwenye haki, tabia kamilifu; na mwanadamu hawezi kutoa jambo hili. Hawezi kukidhi madai ya sheria takatifu ya Mungu. Lakini Kristo, akija duniani kama mwanadamu, aliishi maisha matakatifu, na alidhihirisha tabia kamilifu. Anatoa mambo haya kama zawadi ya bure kwa wote wanaohiari kuyapokea. Maisha yake yanasimama kwa ajili ya maisha ya wanadamu. Kwa njia hiyo wana ondoleo la dhambi zilizopita, kwa njia ya uvumilivu wa Mungu. Zaidi ya hili, Kristo anawajaza wanadamu sifa za tabia ya Mungu. Anaijenga tabia ya wanadamu kwa kuifananisha na tabia ya kimbingu, vazi la nguvu na uzuri wa kiroho. Kwa njia hiyo ile haki inayotakiwa na sheria inatimizwa ndani ya mtu aaminiye katika Kristo. Mungu anaweza kuwa "mwenye haki na mwenye kumhesabu haki yeye amwaminiye Yesu." Warumi 3:26.

Upendo wa Mungu umeonyeshwa katika utendaji wake wa haki ambao haupungui zaidi kuliko rehema yake. Kutenda kwa haki ndio msingi wa kiti chake cha enzi, na ndilo tunda la upendo wake. Kusudi la Shetani lilikuwa ni kuondosha rehema kutoka katika ukweli na haki. Alitafuta kuthibitisha kwamba haki ya sheria ya Mungu ni adui wa amani. Lakini Kristo anaonyesha kwamba katika mpango wa Mungu vitu hivyo hivyo vimefungamanishwa pamoja kwa namna isiyotenganishika; kimoja hakiwezi kuwepo bila kingine. "Fadhili na kweli zimekutana, Haki na amani zimehusiana." Zaburi 85:10.

Kwa njia ya maisha yake na kifo chake, Kristo alithibitisha kwamba utendaji wa Mungu kwa haki haukuharibu fadhili zake, bali kwamba dhambi iliweza kusamehewa, na kwamba sheria ni ya haki, na ya kwamba inawezekana kutiiwa kwa ukamilifu. Mashtaka ya Shetani yalifutika. Mungu alikuwa amempatia mwanadamu ushahidi usioweza kukosewa wa upendo wake.

Sasa uongo mwingine ulikuwa uletwe. Shetani alitangaza kwamba neema ilivunja haki, kwamba kifo cha Kristo kiliikomesha sheria ya Baba. Ikiwa ingewezekana kwa sheria kubadilishwa au kukomeshwa, basi Yesu asingehitajika kufa. Lakini kuikomesha sheria kungekuwa **(763)** ni kuhuisha uasi, na kuuweka ulimwengu chini ya utawala wa Shetani. Yesu aliinuliwa msalabani kwa sababu sheria ilikuwa haibadiliki, kwa sababu mwanadamu angeokolewa kwa njia ya kutii maagizo ya sheria tu. Lakini bado Shetani anaonyesha kwamba

makusudi yale ambayo kwayo Kristo aliimarisha sheria yanaivunja. Hapa ndipo litakapotoka pambano kuu la mwisho kati ya Kristo na Shetani.

Kwamba sheria iliyotamkwa kwa sauti ya Mungu mwenyewe ina mapungufu, kwamba baadhi ya maagizo yake yamewekwa kando, ndiyo madai ambayo Shetani anafanya sasa. Huo ndio uongo mkuu wa mwisho ambao atauletea ulimwengu. Haihitaji kushambulia sheria yote; ikiwa anaweza kuwafanya watu kuacha kujali amri moja; kusudi lake linakuwa limetimia. Maana "mtu awaye yote atakayeishika sheria yote, ila akajikwaa katika neno moja, amekosa juu ya yote." Yakobo 2:10. Kwa kuhiari kuvunja amri moja, watu wanaletwa chini ya nguvu za Shetani. Shetani atatafuta kuutawala ulimwengu kwa kuweka sheria ya mwanadamu mahali pa sheria ya Mungu. Kazi hii imetabiriwa katika unabii. Kuhusu nguvu za uasi mkuu ambazo zinamwakilisha Shetani, imesemwa kwamba, "Naye atanena maneno kinyume chake Aliye juu, naye atawadhoofisha watakatifu wake Aliye juu; naye ataazimu kubadili majira na sheria; nao watatiwa mikononi mwake." Danieli 7:25.

Hakika watu wataweka sheria zao ili kuzipiku sheria za Mungu. Watatafuta namna ya kuzishurutisha dhamiri za wengine, na katika ushupavu wao wa kuzisimamia sheria hizo watawakandamiza wanadamu wenzao.

Vita dhidi ya sheria ya Mungu, iliyoanzishwa mbinguni, itaendelezwa mpaka mwisho wa wakati. Kila mwanadamu atajaribiwa. Kutii au kutotii ndilo jambo ambalo ni lazima liamuliwe na ulimwengu wote. Watu wote wataitwa ili wachague kati ya sheria ya Mungu na sheria za wanadamu. Hapa ndipo mstari unaogawanya utakapochorwa. Kutakuwa na makundi mawili tu. Kila tabia itaendelezwa kikamilifu; na wote wataonyesha kama watakuwa wamechagua upande wa utiifu au wa uasi.

Halafu ule mwisho utakuja. Mungu ataithibitisha sheria yake na kuwaokoa watu wake. Shetani na wale wote walioungana naye katika uasi watakatiliwa mbali. Dhambi na wenye dhambi vitaangaamia, shina na tawi, (Mal. 4:1), - Shetani aliye shina, na wafuasi wake walio matawi. Neno litakalotimia kwa mfalme wa uovu ni hili, "Kwa kuwa umeweka moyo wako kama moyo wa Mungu; . . . nami nimekuangamiza, Ewe kerubi ufunikaye, utoke katika mawe hayo ya moto. . . . Umekuwa kitu cha kutisha, wala hutakuwapo tena hata milele." Halafu "asiye haki hatakuwapo, utapaangalia mahali pake wala hatakuwapo;" "nao watakuwa kana kwamba hawakuwa kamwe." Ezekieli 28:6-19; Zaburi 37:10; Obadia 1:16.

**(764)** Hiki hakitakuwa kitendo cha mabavu kwa upande wa Mungu. Waliokataa rehema yake wanavuna walichokipanda. Mungu ni chemchemi ya uzima; na pindi mtu achaguapo utumishi wa dhambi, anajitenga na Mungu, na kwa jinsi hiyo hujikatilia mbali na uzima. Watu kama hao wanakuwa "wamefarikishwa na uzima wa Mungu." Kristo anasema, "Na wao wanichukiao hupenda mauti." Waefeso 4:18; Mithali 8:36. Mungu huwapatia kuwepo kwa muda ili ya kwamba waendeleze na kuthibitisha tabia yao na kufunua kanuni zao. Haya yakishafanyika, wanapokea matokeo ya uchaguzi wao. Kwa maisha ya uasi, Shetani na wote wanaoungana naye hujiweka nje sana ya upatanifu na Mungu kiasi kwamba uwepo wake tu ni moto ulao kwao. Utukufu wake Yeye aliye pendo utawaangamiza.

Mwanzoni mwa pambano kuu, malaika hawakujua hayo. Ikiwa Shetani na jeshi lake wangeachwa wakati ule ule wavune matokeo kamili ya dhambi yao, wangekuwa wameshaangamia; lakini isingekuwa wazi kwa viumbe wa mbinguni kwamba haya yalikuwa ndiyo matokeo yasiyoepukika ya dhambi. Yangesalia mashaka kuhusu wema wa Mungu yakiwa kama mbegu za uovu mawazoni mwao, ili kuzaa matunda ya kufisha ya dhambi na ole.

Lakini pindi pambano kuu litakapokwisha haitakuwa hivyo. Wakati huo, mpango wa ukombozi ukiwa umekamilika, tabia ya Mungu inafunuliwa kwa viumbe wote wa mbinguni. Amri zilizo katika sheria yake zinaonekana kuwa kamilifu na zisizoondosheka. Wakati huo dhambi itakuwa imefanywa kudhihirisha hali yake halisi, na Shetani kudhihirisha tabia yake. Halafu ukomeshaji wa dhambi utauthibitisha upendo wa Mungu na kuithibitisha heshima yake mbele ya malimwengu yenye viumbe wanaofurahia kufanya mapenzi yake, na ambao sheria yake i mioyoni mwao.

Naam, ndiposa malaika walipaswa kushangilia wakati walipomtazama Mwokozi akiwa msalabani; maana ingawa wakati ule hawakuelewa mambo yote, walijua kwamba uangamivu wa dhambi na Shetani ulikuwa umefanywa kuwa hakika milele, kwamba ukombozi wa mwanadamu ulikuwa umehakikishwa, na ya kwamba malimwengu yalikuwa yamewekwa katika hali iliyo salama. Kristo mwenyewe alielewa kwa ukamilifu matokeo ya kafara iliyofanywa Kalvari. Aliyatarajia yote haya wakati alipolia msalabani akisema, “Imekwisha.”

# Sura ya 80

## Katika Kaburi la Yusufu

Hatimaye Yesu alipumzika. Siku ndefu ya aibu na mateso ilikuwa imekwisha, kadiri miale ya mwisho ya jua linalotua ilivyoangaza na kuikaribisha Sabato, Mwana wa Mungu analala katika ukimya katika kaburi la Yusufu. Kazi yake ikiwa imekamilishwa, mikono yake ikiwa imekunjwa kwa amani, alipumzika kwa masaa yote matakatifu ya siku ya Sabato.

Hapo mwanzo Baba na Mwana walipumzika siku ya Sabato baada ya kazi yake ya uumbaji. Wakati ule inaposemwa kwamba "mbingu na nchi zikamalizika, na jeshi lake lote" (Mwanzo 2:1), Mwumbaji na viumbe wote wa mbinguni walishangilia kulitafakari tukio lile la utukufu. "Hapo nyota za asubuhi zilipoimba pamoja, na wana wote wa Mungu walipopiga kelele kwa furaha." Ayubu 38:7. Sasa Yesu alipumzika kutokana na kazi ya ukombozi; na ingawa kulikuwa na majonzi miongoni mwa wale waliokuwa wanampenda duniani, mbinguni kulikuwa na furaha. Utukufu wa machoni pa viumbe wa mbinguni ulikuwa ni ahadi ya wakati ujao. Mungu na malaika waliona huu uumbaji uliorejeshwa, jamii ya wanadamu iliyokombolewa, ambayo ikishaishinda dhambi kamwe isingeanguka tena, mambo ambayo ni matokeo ya kutiririka kutoka katika kazi ya Kristo iliyokuwa imekamilika. Siku ile ambayo Yesu alipumzika inaunganishwa na tukio hili milele. Maana "kazi yake ni kamilifu;"na "kila kazi aifanyayo Mungu itadumu milele." Kumbukumbu 32:4; Mhubiri 3:14. Wakati kutakapokuwa na "zamani za kufanywa upya vitu vyote, zilizonenwa na Mungu kwa kinywa cha manabii wake watakatifu tokea mwanzo wa ulimwengu" (Matendo 3:21), Sabato ya uumbaji, ile **(770)** siku ambapo Yesu alilala ili kupumzika katika kaburi la Yusufu, bado itaendelea kuwa siku ya kupumzika na kufurahi. Mbingu na dunia zitaungana kwa shangwe za sifa, kadiri ambavyo "Sabato hata Sabato" (Isaya 66:23) mataifa ya waliokombolewa watasujudu kwa furaha wakimwabudu Mungu na Mwana-kondoo.

Katika matukio ya mwisha ya siku ya kusulibiwa, ushahidi halisi wa utimilifu wa unabii ulitolewa, na ushuhuda mpya ulitolewa kuhusu uungu wa Kristo. Wakati giza lilipokuwa limetoweka kwenye msalaba, na kilio cha Mwokozi cha kukata roho kikishatolewa, mara sauti nyingine ilisikika, ikisema, "Hakika huyu alikuwa Mwana wa Mungu." Mathayo 27:54.

Maneno haya hayakusemwa kwa sauti ya kunong'ona. Macho yote yaligeuka ili kuona yalikotoka maneno yale. Ni nani aliyeyasema? Alikuwa akida, askari wa Kirumi. Uvumilivu wa kimbingu wa Mwokozi, na kifo chake cha ghafla, pamoja na kilio kile cha ushindi kilichotoka midomoni mwake, vilikuwa vimemgusa mpagani huyu. Akida aligundua umbo la Mwana wa Mungu ndani ya ule mwili wenye kuchubuliwa na kuvunjika uliokuwa unaning'inia msalabani. Hakuweza kujizuia kukiri imani yake. Kwa njia hiyo ushahidi ulitolewa tena ya kwamba Mwokozi wetu angeona matokeo ya kazi ya nafsi yake. Katika siku ile ile tu ya kifo chake, watu watatu, waliotofautiana sana kwa mbali, walikuwa wameikiri imani yao, - huyu mkuu wa kikosi cha walinzi wa Kirumi, yule aliyeubeba msalaba wa Mwokozi, na yule aliyekufa msalabani akiwa pembeni karibu na Kristo.

Wakati jioni ilipokaribia, utulivu usio wa kawaida duniani ulikuwa juu ya Kalvari. Umati wa watu ulitawanyika, na wengi walirudi Yerusalemu wakiwa wamebadilishwa rohoni kwa kiasi kikubwa kuliko walivyokuwa wakati wa asubuhi ya siku hiyo. Wengi walikuwa wamefurika kuelekea mahali pa kusulibiwa kwa sababu ya udaku, na wala si kwa sababu walikuwa wanamchukia Kristo. Lakini bado waliamini mashtaka ya makuhani, na walimwona Kristo kama laghai. Wakiwa na msisimko usio wa asili yao walikuwa wameungana na kundi lile lenye hasira katika kumchukia Kristo. Lakini pindi dunia ilipofunikwa na weusi, nao wakawa wamesimama wakishtakiwa na dhamiri zao wenyewe, walijisikia hatia ya makosa yao makubwa. Hakuna kejeli au kicheko cha dhihaka kilichosikika katikati ya hofu ile ya kuogofya; na wakati weusi ule ulipoondolewa walishika njia kwenda majumbani kwao wakiwa na ukimya wa huzuni. Walikuwa wameshawishika kwamba mashtaka ya makuhani yalikuwa ya uongo, kwamba Yesu hakuwa laghai; na majuma machache baadaye, Petro alipohubiri mnamo siku ya Pentekoste, hawa walikuwa miongoni mwa maelfu walioongoka kuja kwa Kristo.

Lakini viongozi wa Wayahudi hawakubadilishwa na matukio yale yaliyokuwa yameshuhudiwa. Chuki yao kwa Yesu haikuwa imepoa. Giza lile lililoifunika dunia siku ile ya kusulibiwa halikuwa nene zaidi ya lile lililoendelea kufunika mawazo ya makuhani na wakuu. Wakati wa kuzaliwa kwake nyota **(771)** ilikuwa imemjua Kristo, na

ilikuwa imewaongoza wale wenye hekima kuelekea kwenye hori mahali alipokuwa amelala. Majeshi ya mbinguni yalikuwa yamemjua, na yalikuwa yameimba sifa katika nyanda za tambarare za Bethlehemu. Bahari ilikuwa imeijua sauti yake, na ilikuwa imetii amri yake. Maradhi na kifo vilikuwa vimetambua mamlaka yake, na vilikuwa vimemrejeshea wahanga waliokuwa wameathiriwa. Jua lilikuwa limemjua, na katika mwonekano wake wa kifo cha maumivu, lilikuwa limeuficha uso wake wa nuru. Miamba ilikuwa imemjua, nayo ilikuwa imetetema na kuvunjika vipande vipande wakati alipolia. Viumbe vya asili visivyo hai vilikuwa vimemjua Kristo, navyo vilikuwa vimetoa ushuhuda wa uungu wake. Lakini makuhani na wakuu wa Israeli hawakumjua Mwana wa Mungu.

Hata hivyo wale makuhani na wakuu hawakutulia kwa amani. Walikuwa wametekeleza kusudi lao la kumwua Kristo; lakini hawakupata hisia ya ushindi kama walivyotarajia. Hata mnamo katika saa ya kile kilichoonekana kama kushinda kwao, walisumbuliwa na mashaka kuhusu kitu kingine ambacho kingefuata. Walikuwa wamesikia sauti ya kilio ikisema, "Imekwisha." "Baba, mikononi mwako naiweka roho yangu." Yohana 19:30; Luka 23:46. Walikuwa wameiona miamba ikipasuka, na walikuwa wameshuhudia tetemeko lenye nguvu, na walihangaika wala hawakutulia.

Walikuwa wameonyesha wivu dhidi ya ushawishi wa Kristo kwa watu alipokuwa yu hai; walikuwa na wivu kwake hata alipokuwa amekufa. Walimhofu Kristo aliyekufa kwa mbali zaidi kuliko walivyopata kumwogopa Kristo alipokuwa hai. Waliogopa kuona watu wakielekeza zaidi mawazo yao kwenye matukio yanayohusu kusulibiwa kwake. Waliyaogopa matokeo ya kazi ya siku ile. Kusingekuwa na sababu yoyote ya kuwafanya waendelee kuwa na mwili wowote msalabani mnamo siku ya Sabato. Sabato ilikuwa sasa inakaribia, na ingekuwa ni ukiukaji wa utakatifu wa Sabato kwa miili kuning'inia msalabani. Hivyo, kwa kutumia hili kama sababu ya uongo, viongozi hawa wa Wayahudi walimwomba Pilato kwamba vifo vya wahanga wale viharakishwe, na miili yao iondolewe kabla ya jua kuzama.

Pilato alikuwa hapendi mwili wa Yesu uendelee kuwa msalabani kama vile ambavyo na wao hawakupenda. Wakishapata ukubali wake, miguu ya wale wezi wawili ilivunjwa ili kuharakisha vifo vyao; lakini Yesu alikutwa akiwa amekwisha kufa. Wale askari katili walikuwa wamelainishwa na kile walichokuwa wamesikia na kuona kwa Kristo, na walijizuia kuivunja miguu yake. Kwa njia hiyo katika dhabihu ya Mwana-kondoo wa Mungu sheria ya Pasaka ilitimizwa, "Wasisaze kitu chake chochote hata asubuhi, wala wasimvunje mfupa wake; kama hiyo sheria yote ya Pasaka ilivyo ndivyo watakavyoishika." Hesabu 9:12.

Makuhani na wakuu walishangazwa kwa kuona kwamba Kristo alikuwa amekufa. Kifo cha msalaba kilikuwa ni mchakato wa taratibu; ilikuwa vigumu kugundua **(772)** kwamba ni wakati upi uhai ulikoma. Kilikuwa kitu ambacho hakijawahi kusikika kwamba mtu amekufa kwa kusulibishwa ndani ya saa sita. Makuhani walitamani kuwa na hakika na kifo cha Yesu, na kwa mapendekezo yao askari alichoma mkuki katika ubavu wa Mwokozi, kutoka katika jeraha hilo la mkuki, vilitiririka vijito viwili tofauti, kimoja cha damu, na kingine cha maji. Jambo hili lilionwa na wote waliokuwa wakitazama, na Yohana analieleza tukio hilo kwa uwazi sana. Anasema, "Askari mmojawapo alimchoma ubavu kwa mkuki; na mara ikatoka damu na maji. Naye aliyeona ameshuhudia, na ushuhuda wake ni kweli; naye anajua ya kuwa anasema kweli ili ninyi nanyi mpate kusadiki. Kwa maana hayo yalitukia ili andiko litimie, Hapana mfupa wake utakaovunjwa. Na tena andiko lingine lanena, Watamtazama Yeye waliyemchoma." Yohana 19:34-37.

Baada ya kufufuka kwake makuhani na wakuu walieneza taarifa kwamba Kristo hakufa msalabani, kwamba alizimia tu, na baadaye alipata fahamu. Habari nyingine zilisema kwamba haukuwa mwili halisi wa nyama na mifupa, bali mfano wa mwili, ndio uliowekwa kaburini. Kitendo cha yule askari wa Kirumi kinapinga uongo huu. Hawakumvunja miguu yake, kwa sababu alikuwa amekwisha kufa. Ili kuwaridhisha makuhani, walimchoma ubavuni. Ingekuwa uhai bado haujakoma, jeraha hili lingesababisha kifo mara ile.

Lakini kilichosababisha kifo cha Yesu si kule kuchomwa kwa mkuki, wala maumivu ya msalabani. Kile kilio kilichotolewa "kwa sauti kuu" (Mathayo 27:50; Luka 23:46), wakati wa kukata roho, kijito cha damu na maji kilichotiririka kutoka ubavuni mwake, vilitangaza kwamba alikufa kwa mpasuko wa moyo. Moyo ulipasuliwa na mahangaiko. Aliuawa na dhambi ya ulimwengu.

Kwa kifo kile cha Kristo matumaini ya wanafunzi wake yalitoweka. Waliziangalia kope za macho yake zilizofumbwa na kichwa kilichoinama, nywele zake zikiwa zimelowa damu, mikono na miguu yake iliyotobolewa, na majonzi yao yakawa yasiyoelezeka. Mpaka hatua ya mwisho walikuwa hawaamini kwamba angekufa; ilikuwa vigumu sana kwao kuamini kwamba alikuwa amekufa kweli. Wakiwa wamegubikwa na huzuni, hawakukumbuka maneno yake yaliyotabiri tukio hili. Hakuna chochote alichokuwa amesema ambacho kiliwapa faraja sasa. Waliona msalaba tu na Yeye aliyesulibiwa anayechuruzikwa na damu. Siku za usoni zilionekana kuwa giza na za kukatisha tamaa. Imani yao kwa Yesu ilikuwa imetoweka; lakini hawakupata kumpenda huyu Bwana wao kama walivyompenda sasa. Kamwe walikuwa hawajapata kuhisi thamani yake kabla, na hitaji lao la kutaka uwepo wake, kama ilivyokuwa sasa.

Hata ukiwa uliokufa, mwili wa Kristo ulikuwa na thamani kwa wanafunzi wake. Walitafuta kumfanyia mazishi ya heshima, lakini hawakujua namna ya kutekeleza **(773)** jambo hilo. Usaliti dhidi ya serikali ya Kirumi ndio uhalifu ambao ulisababisha Yesu kuhukumiwa, na watu wanaouawa kwa makosa haya walikuwa wanapelekwa mahali pa viwanja vya kuzikia hasa vilivyotengwa kwa ajili ya wahalifu. Yule Yohana mwanafunzi pamoja na wanawake kutoka Galilaya walikuwa wamebaki mahali pale pa msalaba. Hawakuweza kuuacha mwili wa Bwana wao mikononi mwa askari wale wasio na hisia njema, na kuzikwa katika kaburi lisilo na heshima. Lakini bado hawakuweza kuepuka hilo. Wasingepata upendeleo huo kutoka kwa mamlaka za Wayahudi, na hawakuwa na ushawishi kwa Pilato.

Wakiwa katika hali hii, Yusufu wa Arimathaya na Nikodemo walikuja kuwasaidia wanafunzi hawa. Wote hawa wawili walikuwa wajumbe wa baraza la Sanhedrin, na walikuwa wanafahamiana na Pilato. Wote wawili walikuwa watu wenye utajiri na ushawishi. Walikuwa wameazimia kwamba mwili wa Yesu unapaswa uzikwe kwa heshima.

Yusufu alienda kwa ujasiri kwa Pilato, na akauomba kwake mwili wa Yesu. Kwa mara ya kwanza Pilato alihakikisha kwamba Yesu alikuwa amekufa kweli. Zile taarifa zinazopingana zilikuwa zimemfikia kuhusu matukio yaliyoandamana na kusulibiwa kwake, lakini alikuwa amefichwa kwa makusudi habari ya kufa kwa Kristo. Pilato alikuwa ameonywa na makuhani na wakuu dhidi ya uongo wa wanafunzi wa Kristo kuhusu mwili wa Yesu. Kwa hiyo aliposikia ombi la Yusufu, alituma ujumbe kwa akida aliyesimamia shughuli ile ya msalabani, ili apate kujua hakika ya kifo cha Yesu. Alipata kwake pia maelezo ya matukio yaliyotokea Kalvari, kuthibitisha ushuhuda wa Yusufu.

Ombi la Yusufu lilikubaliwa. Wakati Yohana akisumbuka kuhusu mazishi ya Bwana wake, Yusufu alirudi na kibali cha Pilato kuhusu mazishi ya mwili wa Kristo; na Nikodemo alikuja na michanganyiko ya manemane na uudi ya gharama kubwa, ya thamani ipatayo uzito wa ratli mia moja, ili kuuhifadhi mwili. Mwenye heshima kuzidi wote mle Yerusalemu asingeweza kuonyeshwa heshima zaidi ya hiyo pindi afapo. Wanafunzi walishangazwa kuwaona hawa wakuu wenye mali wakiwa wanavutwa katika mazishi ya Bwana wao.

Si Yusufu wala Nikodemo aliyekuwa amempokea Mwokozi wazi wazi wakati alipokuwa hai. Walijua kwamba hatua kama hiyo ingewatenga na Sanhedrin, na walitumaini kumlinda kwa ushawishi wao katika baraza. Kwa muda fulani walionekana kama wamefanikiwa; lakini wale makuhani wabaya, walipoona kama wana mwelekeo wa kumpenda Kristo, walizuia mipango yao. Wakiwa hawapo, Yesu alikuwa amehukumiwa na kutolewa ili kuasulibiwa. Sasa kwa kuwa alikuwa amekufa, hawakuficha tena uhusiano wao na Yeye. Wakati wanafunzi waliogopa kujionyesha wazi wazi kama wafuasi wake, **(774)** Yusufu na Nikodemo walikuja kuwasaidia kwa ujasiri. Msaada wa watu hawa matajiri na wenye kuheshimiwa ulikuwa unahitajika mno wakati huu. Waliweza kumfanyia Bwana wao aliyekufa kile ambacho kisingewezekana kwa wanafunzi wale maskini kukifanya; na utajiri na ushawishi wao uliwalinda wale wanafunzi, kwa kiasi kikubwa, dhidi ya kudhuriwa na makuhani na wakuu.

Taratibu na kwa heshima waliuondoa msalani mwili wa Yesu kwa mikono yao. Machozi yao ya huruma yalidondoka haraka pindi walipoyatazama majeraha na mwili ulivyoharibiwa. Yusufu alikuwa anamiliki kaburi jipya, lililochongwa katika mwamba. Alikuwa amelihifadhi hili kwa ajili yake mwenyewe; lakini lilikuwa jirani na Kalvari, na sasa aliliandaa kwa ajili ya Yesu. Mwili ule, ukiwa na mafuta yale yaliyoletwa na Nikodemo, ulifungwa katika sanda kwa uangalifu, na Mkombozi alibebwa na kuwekwa kaburini. Pale wale wanafunzi watatu waliinyosha miguu ile iliyoharibiwa, na waliikunja kifuani mikono ile iliyochubuliwa. Wale wanawake wa

Galilaya walikuja kuona yote yaliyokuwa yamefanywa ambayo yaliwezekana kufanywa kwa mwili usio na uhai wa Mwalimu wao mpendwa. Halafu waliliona jiwe zito linasukumwa kuletwa katika mlango wa kaburi, na Mwokozi aliachwa apumzike. Wale wanawake ndio waliokuwa wa mwisho msalabani, na ndio waliokuwa wa mwisho penye kaburi la Kristo. Wakati vivuli vya jioni vinakusanyika, Mariamu Magdalene na kina Mariamu wale wengine walikawia-kawia pale penye kaburi la Bwana wao, wakimwaga machozi ya huzuni kwa sababu ya hatima ya Yeye waliyempenda. "Wakarudi, . . . . Na siku ya sabato walistarehe kama ilivyoamriwa." Luka 23:56.

Ile ilikuwa ni Sabato ambayo kamwe isingesahauliwa kwa wanafunzi wale waliokuwa na huzuni, na pia kwa makuhani, wakuu, waandishi, na watu. Wakati wa jua kutua jioni ya siku ya maandalio baragumu zililia, zikiashiria kwamba Sabato ilikuwa imeanza. Pasaka ilikuwa imesherehekewa kama ilivyokuwa imefanywa kwa karne nyingi, wakati Yeye iliyeelekeza kwake alikuwa ameuawa na mikono ya waovu, na akiwa amelala katika kaburi la Yusufu. Siku ya Sabato viwanja vya hekalu vilijaa waliokuja kuabudu. Kuhani mkuu aliyetoka Golgotha alikuwa pale, akiwa amevalia kwa fahari mavazi ya utakatifu. Makuhani waliovalia kofia nyeupe, wakiwa na shughuli nyingi, walifanya shughuli zao. Lakini baadhi ya waliokuwepo walikuwa hawatulii maana damu za mafahali na mbuzi zilikuwa zinatolewa kwa ajili ya dhambi. Walikuwa hawajui kama mfano wa kivuli ulikuwa umekutana na kitu halisi kilichoashiriwa, kwamba kafara ya daima ilikuwa imefanywa kwa ajili ya dhambi za ulimwengu. Hawakujua kwamba hakukuwa na thamani tena katika kutekeleza taratibu zile za kiibada. Lakini kabla haikupata kutokea kwa ibada kama ile kuwa na hisia za kuchanganyikiwa kama ilivyokuwa hii. Tarumbeta na sauti za vyombo vya muziki na sauti za waimbaji zilisikika kama kawaida. Lakini hali kama ngeni-ngeni iliharibu kila kitu. **(775)** Mmoja baada ya mwingine aliiulizia kuhusu tukio geni liililokuwa limetokea. Tangu zamani mpaka wakati huu patakatifu pa patakatifu palikuwa pamelindwa pasiingiwe na wasiohusika. Lakini sasa palikuwa wazi macho yte yakipaona. Pazia zito lililofumwa, lililofanyizwa kwa kitani safi, na kupakwa kwa uzuri dhahabu, rangi nyekundu, na zambarau, lilikuwa limepasuka kuanzia juu hadi chini. Mahali ambapo Yehova alikuwa anakutana na kuhani mkuu, ili kuleta utukufu wake, mahali ambapo palikuwa chumba kitakatifu cha Mungu, palikuwa wazi kwa ajili ya kila jicho kuona, - mahali ambapo hapatambuliwi tena na Bwana. Makuhani walihudumu mbele ya madhabahu kwa huzuni. Kufunuliwa kwa siri takatifu za patakatifu pa patakatifu kuliwajaza hofu ya janga lililokuwa linakuja.

Mawazo ya watu wengi yalikuwa na kazi nyingi kwa mawazo yaliyosababishwa na matukio ya Kalvari. Tangu tukio la kusulibiwa mpaka lile la kufufuka kulikuwa na macho mengi ambayo hayajasinzia yakiuchunguza unabii wakati wote, baadhi wakijifunza maana halisi ya sikukuu ile waliyokuwa wakiadhimisha wakati ule, baadhi wakitafuta ushahidi kwamba Yesu hakuwa vile alivyodai kuwa; na wengine wakiwa na mioyo ya huzuni walikuwa wakiyachunguza ili kuthibitisha kwamba alikuwa Masihi wa kweli. Ingawa walikuwa wanayachunguza kwa mitazamo tofauti, wote walisadikishwa na ukweli ule ule, - kwamba unabii ulikuwa umetimia katika matukio ya siku chache zilizokuwa zimepita, na kwamba Yeye aliyesulibiwa alikuwa Mkombozi wa ulimwengu. Wengi ambao wakati ule waliungana katika ibada ile kamwe hawakushiriki tena katika kaida ile ya Pasaka. Wengi hata miongoni mwa makuhani walisadikishwa kuhusu tabia ya kweli ya Yesu. Kuchunguza kwao unabii hakukuwa bure, na baada ya kufufuka kwake walimkiri kama Mwana wa Mungu.

Pindi Nikodemo alipoona Yesu ameinuliwa juu msalabani, alikumbuka maneno ya Yesu yaliyosemwa usiku ule kwenye Mlima wa Mizeituni: "Na kama vile Musa alivyomwinua yule nyoka jangwani, vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa; ili kila mtu aaminiye awe na uzima wa milele katika yeye." Yohana 3:14, 15. Katika Sabato ile, wakati Kristo alipokuwa amelala kaburini, Nikodemu alipata nafasi ya kutafakari. Nuru angavu zaidi iliangazia akili yake, na maneno yale ambayo Yesu alimwambia hayakuwa ya fumbo tena. Alijihisi kwamba alikuwa amepoteza mengi kwa kutojiunga na Mwokozi wakati alipokuwa bado hai. Sasa alikumbuka matukio ya Kalvari. Ombi la Kristo kwa wauaji wake na jibu lake kwa ombi la yule mwizi aliyetubu yaliongea na moyo wa mwana-baraza huyu msomi. Kwa mara nyingine tena alimtazama Mwokozi katika mateso yake; kwa mara nyingine aliyasikia maneno ya kile kilio kwamba, "Imekwisha," yakitamkwa kama maneno ya mshindi. Kwa mara nyingine tena aliiona dunia inayowayawaya, mbingu zenye giza, pazia lililopasuka, miamba inayotetema, na imani yake ikasimikwa milele. Tukio lile lile lililoharibu **(776)** matumaini ya wanafunzi liliwashawishi Yusufu na Nikodemo kuhusu uungu wa Yesu. Hofu zao zilishindwa na ujasiri wa imani imara isiyoyumba.

Kamwe Kristo hakupata kuvuta usikivu wa makutano kama wakati huu alipokuwa amelazwa kaburini. Kwa mujibu wa vitendo vyao, watu walileta pale katika viwanja vya hekalu wagonjwa wao na wanaoteseka,

wakiulizia hivi, Nani anaweza kutueleza habari za Yesu wa Nazareti? Wengi walikuwa wamekuja kutoka mbali wakimtafuta Yeye aliyekuwa ameponya wagonjwa na kufufua wafu. Sauti zilisikika kila upande zikisema, Tunamtaka Kristo Mponyaji! Katika wakati huu wale waliofikiriwa kuwa na dalili za ukoma walichunguzwa na makuhani. Wengi walilazimishwa kusikia waume zao, wake zao, au watoto wao wakitangzwa rasmi kuwa na ukoma, na kuhesabiwa kuwa na hatima mbaya ya kuondoka katika makazi ya kawaida ya nyumbani na ya kutunzwa na wenzao, kwenda kuwa kama mgeni aliyetengwa apazaye sauti ya uchungu akisema, "Ni najisi, ni najisi!" Mikono rafiki ya Yesu wa Nazareti, ambayo haikukataa kamwe kumgusa na kumponya mwenye ukoma anayekataliwa, ilikuwa imekunjwa kifuani mwake wakati huu. Midomo ile iliyokuwa imejibu ombi la mwenye ukoma kwa maneno ya faraja kwamba, "Nataka; takasika" (Mathayo 8:3), ilikuwa kimya sasa. Wengi waliwaendea wakuu wa makuhani na watawala ili kuonewa huruma na kuponywa, lakini ilikuwa kazi bure. Walionekana kama vile walitamani kuwa na Kristo akiwa hai miongoni mwao. Kwa kung'ang'aniza waliulizia wakimtaka Kristo. Wala hawakutaka kurudishwa nyuma. Lakini walifukuzwa kutoka katika viwanja vya hekalu, na walinzi waliwekwa penye malango ili kuwazuia makutano waliokuja na wagonjwa wao na watu waliokuwa mahututi, wakitaka kuingia.

Wale wenye shida waliokuwa wamekuja ili kuponywa na Mwokozi walifadhaika sana. Mitaa ilikuwa imejawa na vilio. Wagonjwa walikuwa wanakufa kwa kukosa mguso ule wa uponyaji kutoka kwa Yesu. Matabibu waliendewa lakini kawakuweza kusaidia kitu; hakukuwa na utaalam kama wa Yule aliyekuwa amelala katika kaburi la Yusufu.

Maombolezo ya vilio vya wenye shida yalileta katika mawazo ya maelfu mguso kwamba nuru kuu ilikuwa imeondoka ulimwenguni. Bila Kristo ulimwengu ulikuwa mweusi na wa giza. Wengi ambao sauti zao zilikuwa zimeshiriki kupiga kelele kwamba "Msulibishe, msulibishe," sasa waligundua janga lililokuwa limewaangukia, na, ikiwa Yesu angekuwa bado hai, walitamani kwamba wangepiga kelele wakisema, Tupatie Yesu!

Wakati watu walipotambua kwamba Yesu alikuwa ameuawa na makuhani, walihoji kuhusu kifo chake. Taarifa za mashtaka yake ziliwekwa kuwa siri sana kwa kadiri ilivyowezekana; lakini wakati alipokuwa kaburini, jina lake lilikuwa katika midomo ya maelfu, na taarifa za **(777)** mchakato wa kesi yake uliokuwa wenye dhihaka kwake, na za hali ya makuhani na wakuu kukosa kuonyesha ubinadamu, zilisambazwa kila mahali. Watu wenye uelewa wa akili waliwaita makuhani na wakuu na kuwataka wafafanue unabii wa Agano la Kale kuhusu Masihi, na wakati wakijaribu kutengeneza majibu ya uongo, wakawa kama watu waliorukwa na akili. Hawakuweza kufafanua unabii ulioelekeza kwa mateso na kifo cha Kristo, na wengi wa wale waliouliza wakashawishika kwamba Maandiko yalikuwa yametimia.

Kile kisasi ambacho makuhani walikuwa wamedhani kwamba kitakuwa kitamu kilikuwa tayari kimeleta uchungu kwao. Walijua kwamba walikuwa wanakabiliwa na ukali wa kupingwa na watu; walijua kwamba watu wale wale waliokuwa wameshawishiwa nao kuwa kinyume cha Yesu walikuwa sasa wakitishwa na kazi yao ile ya aibu. Makuhani hawa walikuwa wamejaribu kuamini kwamba Yesu ni mdanganyifu; lakini ilikuwa kazi bure. Baadhi yao walipata kusimama kando ya kaburi la Lazaro, na walikuwa wamemwona aliyekufa akirejeshwa kuwa hai tena. Walitetemeka kwa kuogopa kwamba Yesu angeweza kufufuka kutoka katika wafu, na kutokea mbele yao tena. Walipata kumsikia akitangaza kwamba alikuwa na uwezo wa kuuondoa uhai wake na kuutwaa tena. Walikumbuka kwamba alikuwa amesema, "Livunjeni hekalu hili, nami katika siku tatu nitalisimamisha." Yohana 2:19. Yuda alikuwa amewaambia maneno yaliyosemwa na Yesu akiwaambia wanafunzi wakati alipokuwa katika safari yake ya mwisho kwenda Yerusalemu, akisema: "Angalieni, tunapanda kwenda Yerusalemu; na Mwana wa Adamu atatiwa mikononi mwa wakuu wa makuhani na waandishi; nao watamhukumu afe; kisha watampeleka kwa Mataifa wapate kumdhihaki, na kumpiga mijeledi, na kumsulibisha; na siku ya tatu atafufuka." Mathayo 20:18, 19. Wakati waliposikia maneno haya, walikuwa wamedhihaki na kufanya mizaha. Lakini sasa walikumbuka kwamba utabiri wa Kristo ulikuwa umetimia kiasi kile. Alikuwa amesema kwamba angefufuka tena siku ya tatu, naye ni nani ambaye angeweza kusema kwamba hili nalo lisingetokea? Walitamani kuzuilia mbali mawazo haya, lakini hawakuweza. Kama alivyo baba yao, mwovu, waliamini na kutetemeka.

Sasa kwa kuwa kichaa cha msisimko kilikuwa kimepita, sura ya Kristo ilikuwa iingie akilini mwao. Walimwona kama alivyokuwa amesimama akiwa mtulivu na pasipo malalamiko mbele ya adui zake, akiumizwa na dhihaka

na matusi yao bila manung'uniko. Matukio yote ya uendeshaji wa kesi yake na kusulibishwa kwake yalirejea mawazoni mwao yakiwa na uwezo wa kusadikisha kwamba alikuwa Mwana wa Mungu. Walihisi kwamba huenda wakati wowote ule angesimama mbele yao, aliyeshtakiwa awe ndiye mshtaki, aliyehukumiwa ahukumu, aliyeuawa adai haki ya kifo cha wauaji wake.

Waliweza kupumzika kidogo mnamo siku ile ya Sabato. Ingawa wasingeweza kuingia **(778)** katika eneo la Mataifa kwa kuogopa kunajisika, lakini bado walifanya kikao cha baraza kuhusu mwili wa Kristo. Lazima kifo na kaburi vimshikilie Yeye waliyekuwa wamemsulibisha. "Wakuu wa makuhani, na Mafarisayo wakamkusanyikia Pilato, wakasema, Bwana, tumekumbuka kwamba yule mjanja alisema, alipokuwa akali hai, Baada ya siku tatu nitafufuka. Basi amuru kwamba kaburi lilindwe salama hata siku ya tatu; wasije wanafunzi wake wakamwiba, na kuwaambia watu, Amefufuka katika wafu; na udanganyifu wa mwisho utapita ule wa kwanza. Pilato akawaambia, Mna askari; nendeni mkalilinde salama kadiri mjuavyo." Mathayo 27:62-65.

Makuhani walitoa maelekezo ya namna ya kuhakikisha usalama wa lile kaburi. Jiwe kubwa lilikuwa limewekwa mlangoni mwa kaburi. Wao wakalifunga lile jiwe kwa kamba, wakizifungia kwenye mwamba mgumu, na kuzitia lakiri kwa chapa ya Kirumi. Jiwe lile lisingeweza kuondolewa bila kuvunja lakiri ile. Halafu kikosi cha askari mia moja kiliwekwa pale kulizunguka kaburi ili kuzuia kitendo chochote cha kujaribu kufungua. Makuhani walifanya yote waliyoweza kuhakikisha mwili wa Kristo unabaki mahali ulipokuwa umelazwa. Alizibiwa kweli kweli katika kaburi lake kama vile ilikuwa abaki mle wakati wote.

Mashauri na mipango ya wanadamu ni dhaifu. Wauaji hawa hawakujua kabisa kwamba jitihada zao hazikuwa na kazi yoyote. Lakini kwa kazi yao hiyo Mungu alitukuzwa. Jitihada zile zile zilizotumika kuzuia kufufuka kwa Kristo ndizo hoja zenye ushawishi wa nguvu za kuthibitisha kufufuka kwake. Kadiri idadi ya askari waliowekwa kulizunguka kaburi inavyozidi kuwa kubwa, ndivyo ambavyo ushuhuda ya kwamba alikuwa amefufuka ungekuwa na nguvu zaidi. Mamia ya miaka kabla ya kifo cha Kristo, Roho Mtakatifu alikuwa amenena kupitia kwa mwimbaji wa zaburi, akisema, "Mbona mataifa wanafanya ghasia, na makabila wanatafakari ubatili? Wafalme wa dunia wanajipanga, na wakuu wanafanya shauri pamoja, juu ya Bwana, na juu ya Masihi. . . . Yeye aketiye mbinguni anacheka, Bwana anawafanyia dhihaka." Zaburi 2:1-4. Walinzi wa Kirumi na silaha za Kirumi havikuwa na nguvu ya kumzuilia Bwana wa uzima mle ndani ya kaburi. Saa ya kuwekwa huru kwake ilikuwa inakaribia.

## Sura ya 81

# "Bwana Amefufuka"

[Sura hii imejengwa katika Mathayo 28:2-4, 11-15.]

Usiku wa siku ya kwanza ya juma ulikuwa unapita taratibu. Saa ya giza kuu, kabla ya kupambazuka, ilikuwa imefika. Kristo alikuwa bado ni mfungwa mle katika kaburi lake jembamba. Jiwe kubwa lilikuwa bado liko mahali pake pale; lakiri ya Kirumi ilikuwa haijavunjwa; walinzi wa Kirumi walikuwa wanalinda lindo lao. Na walikuwepo walinzi wengine wasioonekana. Majeshi ya malaika waovu yalikuwa yamekusanyika pale. Ikiwa ingewezekana, mfalme wa giza pamoja na jeshi lake lililoasi wangeendelea kulifanya kaburi lililokuwa na Mwana wa Mungu lifungwe kwa lakiri milele. Lakini jeshi la mbinguni lililizunguka kaburi. Malaika wale wenye nguvu zaidi walikuwa wanalilinda kaburi, na wakisubiri kumkaribisha Mfalme wa uzima.

"Na tazama, palikuwa na tetemeko kubwa la nchi; kwa sababu malaika wa Bwana alishuka kutoka mbinguni." Akiwa amevishwa mavazi maridadi ya Mungu, malaika huyu aliondoka katika viwanja vya mbinguni. Miale yenye mwanga mkali ya utukufu wa Mungu ilitangulia mbele yake, na kuangazia njia yake. "Na sura yake ilikuwa kama umeme, na mavazi yake meupe kama theluji. Na kwa kumwogopa, wale walinzi wakatetemeka, wakawa kama wafu."

Sasa, enyi makuhani na wakuu, nguvu za ulinzi wenu zi wapi? Askari werevu ambao hawajawahi kamwe kuogopa nguvu za mwanadamu sasa wako kama mateka waliochukuliwa pasipo upanga wala mkuki. Uso wanaouona si uso **(780)** wa mpiganaji mwenye mwili wa kufa; ni uso wa mwenye uwezo mkuu kuliko wote miongoni mwa jeshi la Bwana. Mjumbe huyu ndiye anayekalia nafasi iliyoachwa na Shetani wakati alipoanguka. Huyu ndiye yule aliyetangaza katika vilima vya Bethlehemu kuhusu kuzaliwa kwa Kristo. Dunia inatetemeka wakati anapokaribia, majeshi ya giza yanakimbia, na wakati anapolivingirisha jiwe, mbingu inaonekana kama imeshuka duniani. Wale askari wanamwona akiliondoa jiwe kama vile anaondoa kijiwe kidogo, na wanamsikia akilia kwa sauti kuu na kusema, Mwana wa Mungu, njoo huku; Baba yako anakuita. Wanamwona Yesu akitoka kaburini, na kumsikia akilitangazia kaburi lililopasuka kwamba, "Mimi ndimi huo ufufuo, na uzima." Kadiri anavyotoka kaburini akiwa na nguvu na utukufu, jeshi la malaika linainama na kumsujudia Mkombozi, na kumkaribisha kwa nyimbo za sifa.

Tetemeko liliashiria saa ambayo Kristo aliyatoa maisha yake, na tetemeko jingine liliushuhudia wakati ule alipoyatwaa kwa ushindi. Yeye aliyekuwa ameshinda mauti na kaburi alikuja kutoka kaburini akiwa na utisho wa ushindi, katikati ya nchi inayotetemeka, kuangaza kwa umeme wa radi, na kuunguruma kwa radi. Wakati atakapokuja duniani tena, atatetemesha "si nchi tu, bali na mbingu pia." "Dunia inalewa-lewa kama mlevi, nayo inawaya-waya kama machela." "Mbingu zitakunjwa kama karatasi;" "na viumbe vya asili vitaunguzwa, na kufumuliwa, na nchi na kazi zilizomo ndani yake zitateketea." Lakini "Bwana atakuwa kimbilio la watu wake, na ngome ya wana wa Israeli." Waebrania 12:26; Isaya 24:20; 34:4; 2 Petro 3:10; Yoeli 3:16.

Wakati wa kifo cha Yesu askari wale walikuwa wameiona dunia ikifunikwa na giza wakati wa mchana kati; lakini wakati wa kufufuka waliona mwanga wa malaika ukiangaza wakati wa usiku, na waliwasikia wakazi wa mbinguni wakiimba kwa sauti kuu na ushindi wakisema: Umemshinda Shetani na nguvu za giza; Umekimeza kifo katika kushinda!

Kristo alitoka kaburini akiwa ametukuzwa, na walinzi wa Kirumi walimwona. Macho yao yalikazwa kwenye uso wake Yeye ambaye muda mfupi tu uliokuwa umepita walikuwa wamemdhihaki na kumtendea jeuri. Katika Huyu aliyetukuzwa waliona mfungwa yule waliyekuwa wamemwona kule katika ukumbi wa hukumu, yule amabye walikuwa wamesokota taji ya miiba kwa ajili yake. Huyu ndiye Yule aliyekuwa amesimama mbele ya Pilato na Herode pasipo ubishi, mwili wake ukiwa umeharibiwa kwa mapigo. Huyu alikuwa Yule aliyekuwa amepigiliwa misumari msalabani, Yule ambaye makuhani na wakuu walimtikisia vichwa vyao, kwa madaha na kuridhika, wakisema, "Aliokoa wengine; hawezi kujiokoa mwenyewe." Mathayo 27:42. Huyu ndiye Yule aliyekuwa amelazwa katika kaburi jipya la Yusufu. Amri ya mbinguni ilikuwa **(781)** imemfungulia mateka huyu. Hata milima ikilundikwa juu ya milima kwenye kaburi lake asingezuiliwa kutoka mle.

Kwa kuwaona malaika wale na Mwokozi aliyetukuzwa walinzi wa Kirumi walikuwa wamezimia na kuwa kama wafu. Wakati msafara huo wa mbinguni ulipofichwa kutoka machoni pao, walisimama kwa miguu yao, na kwa haraka kadiri ambavyo miguu yao inayotetemeka iliweza kuwakimbiza, walishika njia kuelekea katika lango la bustani. Wakiyumbayumba kama walevi, waliharakisha kwenda mjini, wakiwaambia watu waliokutana nao habari za ajabu zilizotokea. Walikuwa wanaenda kwa Pilato, lakini habari zilishazifikia mamlaka za Wayahudi, na wakuu wa makuhani na watawala wakatuma ujumbe kwa wale askari kwamba waje kwao kwanza. Wale askari walieleza kitu chenye mwonekano wa ajabu sana. Wakitetemeka kwa woga, uso wao ukiwa umepoteza rangi, walitoa ushuhuda wa kufufuka kwa Kristo. Wale askari walisimulia mkasa mzima, vile vile kama walivyouona; hawakuwa wamepata muda wa kufikiria au kusema kitu kingine chochote tofauti na ukweli. Kwa maneno ya maumivu walisema, aliyesulibiwa alikuwa Mwana wa Mungu; tumemsikia malaika akimtangaza kwamba ni mwenye Mamlaka wa mbinguni, Mfalme wa utukufu.

Nyuso za wale makuhani zilikuwa kama za waliokufa. Kayafa alijaribu kuongea. Midomo yake ilitikisika kuonyesha kwamba anaongea lakini haikutoa sauti. Wale askari walitaka kuondoka katika chumba cha baraza, wakati sauti fulani ilipowataka wasubiri. Hatimaye Kayafa alipata uwezo wa kunena. Subirini, subirini, alisema. Msimwambie mtu yeyote vitu hivyo mlivyoona.

Taarifa za kudanganyia zilitolewa wakapewa askari wale. Makuhani wakasema, "Semeni ya kwamba wanafunzi wake walikuja usiku, wakamwiba, sisi tulipokuwa **(782)** tumelala." Hapa makuhani walijishinda wenyewe. Inawezekanaje askari waseme kwamba wanafunzi walikuwa wameuiba mwili wakati wakiwa wamesinzia? Ikiwa walikuwa wamesinzia, walijuaje? Na ikiwa wanafunzi walikuwa wamethibitishwa kuwa na hatia ya kuuiba mwili wa Kristo, je, makuhani si wangekuwa wa kwanza kuwahukumu? Au ikiwa kikosi kizima cha lindo kilikuwa kimelala pale pale mahali pa kaburi, je, makuhani si wangekuwa wakali kuwashtaki kwa Pilato?

Wale askari walitishwa na wazo lile la kujiletea juu yao wenyewe shtaka la kulala kwenye lindo. Hii ilikuwa jinai ambayo ingewasababishia hata adhabu ya kifo. Je, watoe ushuhuda wa uongo, wadanganye watu, na kuweka maisha yao hatarini? Je, si walikuwa wamekesha usiku kucha wakilinda? Wangestahilije kusimama hukumunu, hata kama ni kwa kutaka pesa, wakati waliapa kusema ukweli?

Ili kuunyamazisha ushuhuda ule walioogopa, makuhani waliahidi kuwahakikishia wale walinzi usalama, wakisema kwamba Pilato asingependa taarifa zile zisambae zaidi ya pale zilipokuwa zimefika. Wale askari wa Kirumi wakauza uaminifu wao kwa Wayahudi kwa pesa. Walikuja mbele ya makuhani wakiwa na mzigo wa ujumbe wa kweli wa kushtua; waliondoka pale wakiwa na mzigo wa pesa, na kwenye ndimi zao kukiwa na taarifa za uongo walizokuwa wametungiwa na makuhani.

Wakati huo huo taarifa ya kufufuka kwa Kristo zilikuwa zimeshapelekwa kwa Pilato. Ingawa Pilato alikuwa anawajibika kwa kumtoa Kristo auawe, alikuwa kama vile hahusiki. Wakati akiwa amemhukumu Mwokozi bila kupenda, na akiwa na huruma, hakuwa amehisi aibu mpaka wakati huu. Kwa hofu sasa alijifungia ndani ya nyumba yake, akitaka asionane na mtu yeyote. Lakini makuhani walienda mpaka mahali alipo, wakamsimulia habari waliyokuwa wamebuni, na wakamsisitiza asione kwamba wale askari walinzi walizembea wajibu wao. Kabla ya kuwakubalia hili, aliwauliza wale walinzi yeye mwenyewe kwa faragha. Wakihofia usalama wao, hawakudiriki kuficha jambo lolote, na kutoka kwao Pilato alipata habari ya yote yaliyotokea. Hakushughulikia jambo lile zaidi, lakini tangu wakati ule kwake hakukuwa na amani tena.

Wakati Yesu alipolazwa kaburini, Shetani alishinda. Alidiriki kutumaini kwamba Mwokozi asingerejea katika maisha yake tena. Aliudai mwili wa Bwana, na kuweka walinzi wake penye kaburi, akitafuta kuendelea kumshikilia mfungwa wake. Wakati wajumbe wa mbinguni walipokaribia pale malaika zake wakakimbia alipatwa na hasira kubwa sana. Alipomwona Kristo akitoka kaburini kwa ushindi, alijua kwamba ufalme wake ungefikia mwisho, na ya kwamba lazima hatimaye atakufa.

**(785)** Makuhani walikuwa wamekuwa nyenzo za Shetani kwa kule kumwua Kristo. Sasa kwa ujumla walikuwa katika himaya yake. Walikuwa wamenaswa katika mtego mahali ambamo hawakupata namna ya kuepuka isipokuwa kuendeleza vita yao dhidi ya Kristo. Waliposikia habari za kufufuka kwake, waliogopa ghadhabu za watu. Walihisi kwamba maisha yao yalikuwa hatarini. Tumaini pekee kwao lilikuwa ni kuthibitisha kwamba Kristo alikuwa laghai kwa kusema kwamba hakuwa amefufuka. Waliwahonga wale askari, na kufanikiwa kuipata

hali ya Pilato kukaa kimya. Walisambaza taarifa zao za uongo mbali na karibu. Lakini walikuwepo mashuhuda ambao wasingewezekana kunyamazishwa. Watu wengi walikuwa wamesikia ushuhuda wa wale askari kuhusu kufufuka kwa Kristo. Na baadhi ya waliokuwa wamekufa waliofufuka pamoja na Kristo walikuwa wamewatokea wengi, na kutangaza kwamba amefufuka. Taarifa za watu waliokuwa wamewaona watu hao waliofufuka na kusikia ushuhuda wao zililetwa kwa makuhani. Makuhani na wakuu walikuwa katika hofu ya kudumu, wakiogopa kwamba huenda wakakutana na Kristo wakati wakitembea-tembea mitaani, au mahali pa faragha majumbani kwao. Walihisi kwamba hakukuwa na usalama kwao. Makomeo na vizuizi vya milango yao vilionekana kuwa ulinzi hafifu kuweza kumzuia Mwana wa Mungu. Usiku na mchana walijiliwa na lile tukio baya lililotukia katika ukumbi wa hukumu, wakati walipopaza sauti zao wakisema, "Damu yake na iwe juu yetu, na juu ya watoto wetu." Mathayo 27:25. Kamwe kumbukumbu ya tukio lile isingefutika kutoka mawazoni mwao. Kamwe usingizi wa amani usingekuja wakati walalapo.

Wakati sauti ya malaika mwenye nguvu iliposikika mahali pa kaburi la Kristo, ikisema, Baba yako anakuita, Mwokozi alitoka kaburini kwa uhai uliokuwa ndani yake. Sasa maneno yake yalithibitika kwamba, "Nautoa uhai wangu ili niutwae tena. . . . Nami ninao uweza wa kuutoa, ninao na uweza wa kuutwaa tena." Sasa ulikuwa umetimia unabi aliokuwa amewaambia makuhani na wakuu kwamba, "Livunjeni hekalu hili, nami katika siku tatu nitalisimamisha." Yohana 10:17, 18; 2:19.

Pale penye kaburi lile la Yusufu ambalo limepasuka, Yesu alikuwa ametangaza maneno ya ushindi akisema, "Mimi ndimi huo ufufuo na uzima." Maneno haya yangeweza kutamkwa na Mungu tu. Viumbe hai vyote vilivyoumbwa vinaishi kwa mapenzi na nguvu za Mungu. Ni vitegemezi vinavyopokea uzima wa Mungu. Tangu serafi wa juu kabisa mpaka kiumbe hai cha hali ya chini kabisa, vyote vinahuishwa kutoka kwa Chanzo cha uhai. Yeye tu aliye umoja na Mungu ndiye aliyekuwa na uwezo wa kusema, Nina uwezo wa kuutoa uhai wangu, na ninao uwezo wa kuutwaa tena. Katika uungu wake, Kristo alikuwa na nguvu ya kuvunja vifungo vya mauti.

Kristo alifufuka kutoka kwa wafu akiwa kama malimbuko ya wale waliolala. Alikuwa kitu halisi badala ya mganda wa malimbuko utikiswao, na kufufuka kwake kulitokea mnamo **(786)** siku ile ile ambapo mganda wa kutikisa ungetolewa mbele za Bwana. Kwa zaidi ya miaka elfu moja maadhimisho haya ya ishara yalifanyika. Ngano ya kwanza kukomaa katika mavuno ya mashamba ilikusanywa, na wakati watu walipopanda kwenda Yerusalemu kwa ajili ya Pasaka, mganda wa malimbuko haya ulitikiswa kama sadaka ya shukrani mbele za Mungu. Kabla ya kutoa sehemu hii, mundu usingewekwa katika shamba la nafaka na kukusanywa ghalani. Ule mganda uliowekwa wakfu kwa Mungu uliwakilisha mavuno yote. Vivyo hivyo Kristo aliye malimbuko aliwakilisha mavuno makubwa ya kiroho yatakayokusanywa kwa ajili ya ufalme wa Mungu. Kufufuka kwake ni mfano wa kivuli na ahadi ya kufufuka kwa wenye haki wote waliokufa. "Maana, ikiwa twaamini ya kwamba Yesu alikufa akafufuka, vivyo hivyo na hao waliolala katika Yesu, Mungu atawaleta pamoja naye." 1 Wathesalonike 4:14.

Pindi Kristo alipofufuka, alileta kutoka kaburini kundi kubwa la mateka. Lile tetemeko la wakati wa kufa kwake lilikuwa limepasua makaburi yao, na wakati alipofufuka, walitoka humo pamoja naye. Hawa ni wale waliokuwa watenda kazi pamoja na Mungu, na ambao kwa gharama ya maisha yao walikuwa wameushuhudia ukweli. Sasa walikuwa wawe mashahidi wake Yeye aliyekuwa amewafufua kutoka katika wafu.

Wakati wa huduma yake, Yesu alikuwa amewafufua wafu wakarejea kuwa hai. Alikuwa amemfufua kijana wa mjane wa kule Naini, na binti wa mkuu wa sinagogi, na Lazaro. Lakini hawa hawakuvikwa kutokufa. Baada ya kufufuliwa, bado wangekufa wakati mwingine. Lakini wale waliotoka kaburini wakati wa kufufuka kwa Kristo walifufuliwa kwa ajili ya uzima wa milele. Walipaa pamoja naye wakiwa nyara za ushindi wake juu ya mauti na kaburi. Yesu alisema, Hawa si mateka wa Shetani tena; nimewakomboa. Nimewaleta kutoka kaburini kama malimbuko ya mamlaka yangu, wawe pamoja nami mahali nilipo, wasione mauti tena wala kupata huzuni.

Hawa walienda mjini, wakawatokea wengi, wakitangaza kwamba, Kristo amefufuka kutoka katika wafu, nasi tumefufuliwa pamoja naye. Kwa njia hiyo ukweli mtakatifu wa kufufuka kwake kulifanywa kuwa hai milele. Watakatifu waliofufuliwa walitoa ushuhuda kuonyesha ukweli wa maneno haya, "Wafu wako wataishi, maiti zangu zitafufuka." Kufufuka kwao kulikuwa kielelezo cha kutimia kwa unabii kwamba, "Amkeni, kaimbeni, ninyi mnaokaa mavumbini, kwa maana umande wako ni kama umande wa mimea, nayo ardhi itawatoa waliokufa." Isaya 26:19.

Kwa mtu aaminiye, Kristo ni ufufuo na uzima. Ndani ya Mwokozi wetu uzima uliopotea kwa sababu ya dhambi unarejeshwa; maana ana uzima ndani yake mwenyewe **(787)** wa kumhuisha ampendaye. Amekabidhiwa haki ya kutoa hali ya kutokufa. Ule uzima alioutoa katika ubinadamu, anautwaa tena, na kuugawa kwa wanadamu. Alisema, "Mimi nalikuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele." "Yeyote atakayekunywa maji yale nitakayompa mimi hataona kiu milele; bali yale maji nitakayompa yatakuwa ndani yake chemchemi ya maji, yakibubujikia uzima wa milele." "Aulaye mwili wangu na kuinywa damu yangu anao uzima wa milele; nami nitamfufua siku ya mwisho." Yohana 10:10; 4:14; 6:54.

Kwa mtu aaminiye, kifo ni jambo dogo mno. Kristo anakisema kama vile ni cha wakati mfupi sana. "Mtu akilishika neno langu, hataona mauti milele," "hataonja mauti milele." Kwa Mkristo, kifo si kitu bali usingizi, muda mfupi sana wa ukimya na giza. Uzima unafichwa pamoja na Kristo ndani ya Mungu, na wakati "Kristo atakapofunuliwa, aliye uhai wetu, ndipo na ninyi mtafunuliwa pamoja naye katika utukufu." Yohana 8:51, 52; Wakolosai 3:4.

Sauti ile iliyolia msalabani kwamba, "Imekwisha," ilisikika miongoni mwa waliokufa. Ilipenya kuta za makaburi, na kuwaamuru waliolala kuinuka. Hivyo ndivyo itakavyokuwa wakati sauti ya Kristo itakaposikika kutoka mawinguni. Sauti ile itapenya makaburi na kuyafungua, na waliokufa katika Kristo watafufuka. Wakati wa kufufuka kwa Kristo makaburi machache tu ndiyo yaliyofunguliwa, lakini wakati wa kuja kwake mara ya pili watakatifu wote waliokufa wataisikia sauti yake, nao watatoka makaburini na kuwa na maisha matukufu yasiyo ya kufa. Nguvu ile ile iliyomfufua Kristo kutoka kwa wafu italifufua kanisa lake, na kulitukuza pamoja naye, juu ya mamlaka zote, juu ya nguvu zote, juu ya kila jina liitwalo, si katika ulimwengu huu tu, bali pia katika ulimwengu ujao.

## Sura ya 82

# "Unalilia Nini?"

[Sura hii imejengwa katika Mathayo 28:1, 5-8; Marko 16:1-8; Luka 24:1-12; Yohana 20:1-18.]

Wanawake waliokuwa wamesimama karibu na msalaba wa Kristo walitazama na kusubiri saa za Sabato zipite. Mnamo siku ya kwanza ya juma, asubuhi na mapema, walishika njia kwenda kaburini, wakiyachukua manukao ya thamani ili kuupaka mwili wa Mwokozi. Hawakufikiri kuhusu kufufuka kwake. Jua la tumaini lao lilikuwa limezama, na usiku ulikuwa umekaa mioyoni mwao. Kadiri walivyotembea walisimuliana kazi za Kristo za wema na maneno yake ya faraja. Lakini hawakukumbuka maneno yake kwamba, "mimi nitawaona tena." Yohana 16:22.

Wakiwa hawajui hata kilichokuwa kinatokea, walifika karibu na bustani, wakisema kadiri walivyoendelea kwenda, "Ni nani atakayetuvingirishia lile jiwe mlangoni pa kaburi?" Walijua kwamba wasingeweza kuliondoa lile jiwe, lakini bado waliendelea kwenda. Na tazama, mbingu ziliangaza ghafla kwa utukufu ambao haukuletwa na jua lililokuwa linatokeza. Dunia ilitetemeka. Waliona kwamba lile jiwe lilikuwa limevingirishiwa pembeni. Kaburi lilikuwa tupu.

Wale wanawake hawakuwa wamekuja kaburini wakitoka wote katika uelekeo mmoja. Mariamu Magdalena alikuwa wa kwanza kufika pale; na kwa kuona kwamba jiwe lilikuwa limeondolewa, aliharakisha kwenda kuwaambia wanafunzi. Wakati hayo yanatokea wale wanawake wengine walifika pale. Nuru ilikuwa inaangaza mahali pale pa kaburi, lakini mwili wa Yesu haukuwemo mle. Kadiri walivyokawia-kawia pale, ghafla waliona kwamba hawakuwa peke yao. Kijana mmoja wa kiume aliyekuwa amevikwa mavazi yang'aayo alikuwa amekaa kando ya kaburi. Huyu alikuwa yule malaika aliyekuwa amelivingirisha jiwe. Alikuwa amechukua mwonekano wa mwanadamu ili kwamba **(789)** asiwashitue hawa rafiki za Yesu. Lakini nuru ya mbinguni ilikuwa bado inaangaza pande zake zote, na wanawake wale waliogopa. Waligeuka ili kukimbia, lakini maneno ya malaika yule yaliwabakiza pale. Alisema, "Msiogope ninyi; kwa maana najua ya kuwa mnamtafuta Yesu aliyesulibiwa. Hayupo hapa; kwani amefufuka kama alivyosema. Njoni, mpatazame mahali alipolazwa. Nanyi nendeni upesi, mkawaambie wanafunzi wake, Amefufuka katika wafu. Tazama, awatangulia kwenda Galilaya; ndiko mtakakomwona. Haya, nimekwisha waambia." Kwa mara nyingine wanaangalia ndani ya kaburi, na wanasikia tena habari zile za kushangaza. Malaika mwingine ambaye yuko katika umbo la mwanadamu yupo pale, na anasema, "Kwa nini mnamtafuta aliye hai katika wafu? Hayupo hapa, amefufuka. Kumbukeni alivyosema nanyi alipokuwa akaliko Galilaya, akisema, Imempasa Mwana wa Adamu kutiwa mikononi mwa wenye dhambi, na kusulibiwa, na kufufuka siku ya tatu."

Amefufuka, amefufuka! Wanawake wale wanayarudia maneno hayo tena na tena. Hakuna uhitaji wa manukato ya kumpaka tena. Mwokozi yu hai, si mfu. Sasa wanakumbuka kwamba alipokuwa anaongea kuhusu kifo chake alisema kwamba angefufuka. Hii ni siku njema kiasi gani kwa ulimwengu! Wanawake wale waliondoka haraka pale kaburini "kwa hofu na furaha nyingi, wakaenda mbio kuwapasha wanafunzi wake habari."

Mariamu hakuwa amesikia hizo habari njema. Alienda kwa Petro na Yohana akiwa na ujumbe wa huzuni kwamba, "Wamemwondoa Bwana kaburini, wala hatujui walikomweka." Wale wanafunzi waliharakisha kwenda kaburini, na kukuta hali iko vile Mariamu alivyosema. Waliona sanda na kitambaa, lakini hawakumwona Bwana wao. Lakini bado hata hapa kulikuwa na ushahidi kwamba amefufuka. Nguo za kuzikiwa hazikutupwa pembeni hivi hivi tu, bali zilikunjwa kwa uangalifu, kila moja mahali pake. Yohana "akaona na kuamini." Bado alikuwa hajaelewa Maandiko kwamba lazima Kristo afufuke kutoka katika wafu; lakini sasa alikumbuka maneno ya Mwokozi yaliyotabiria kufufuka kwake.

Kristo mwenyewe ndiye aliyekuwa ameziweka vizuri sana zile nguo za kaburini. Wakati malaika mwenye nguvu aliposhuka pale penye kaburi, aliungana pale na mwingine, ambaye alikuwa amekuwa na wenzake wakiulinda mwili wa Bwana. Kadiri yule malaika kutoka mbinguni alivyolivingirisha jiwe, huyo mwingine aliingia ndani ya kaburi, na akafungua nguo ambazo mwili wa Yesu ulikuwa umezungushiwa. Lakini mkono wa Mwokozi ndio uliokunja kila nguo, na kuiweka vizuri mahali pake. Machoni pake Yeye anayeongoza nyota na atomu, hakuna kitu ambacho si cha muhimu. Mpangilio mzuri na ukamilifu unaonekana katika kazi yake yote.

Mariamu alikuwa amemfuata Yohana na Petro kwenda kaburini; waliporudi Yerusalemu, yeye alibaki. Alipoangalia ndani ya kaburi lililo wazi, majonzi yaliujaza moyo wake. Alipochungulia ndani, aliwaona wale malaika wawili, mmoja akiwa sehemu ya kichwani na **(790)** mwingine sehemu ya miguuni mahali hapo ulipokuwa umelazwa mwili wa Yesu. Wakamwuliza, "Mama, unalilia nini?" Akajibu kwamba, "Kwa sababu wamemwondoa Bwana wangu, wala mimi sijui walikomweka."

Halafu aligeuka, kwenda mbali na wale malaika, akidhani kwamba angeweza kupata mtu wa kumwambia kitu kilichokuwa kimefanyika kuhusu mwili wa Yesu. Sauti nyingine ikamwambia, "Mama, unalilia nini? Unamtafuta nani?" Kwa macho yale yanayolengalenga machozi, Mariamu aliona umbo la mwandamu, naye akidhani kwamba ni mtunzaji wa bustani ile, alimwambia, "Bwana, ikiwa umemchukua wewe, uniambie ulipomweka, nami nitamwondoa." Ikiwa kaburi hili la mtu tajiri lilionekana la kuheshimika mno kiasi kwamba lisingefaa kwa ajili ya Yesu, yule mama alikuwa atoe nafasi nyingine kwa ajili ya kumzikia. Kulikuwa na kaburi mahali ambalo maneno ya Yesu mwenyewe yalikuwa yameliacha likiwa tupu, kaburi lile alimokuwa amelazwa Lazaro. Je! Kule asingepata mahali pa kumlaza Bwana wake? Aliona kwamba kuujali mwili ule wa Yesu wa thamani kungekuwa faraja kubwa katika majonzi yake.

Lakini sasa kwa sauti yake halisi iliyokuwa inajulikana Yesu alisema, "Mariamu." Sasa alijua kwamba yule aliyekuwa anazungumza naye si mtu mgeni kwake, na alipogeuka alimwona Kristo aliye hai akiwa mbele yake. Kwa furaha alisahau kwamba Kristo alikuwa amesulibiwa. Alipomkimbilia kwa shangwe, kama anayetaka kukumbatia miguu yake, alisema, "Raboni." Lakini Kristo alinyosha mkono wake, akisema, "Usinishike; kwa maana sijapaa kwenda kwa Baba. Lakini enenda kwa ndugu zangu ukawaambie, Ninapaa kwenda kwa Baba yangu naye ni Baba yenu, kwa Mungu wangu naye ni Mungu wenu." Naye Mariamu akaondoka zake kwenda kwa wanafunzi akiwa na ujumbe wa furaha.

Yesu alikataa kupokea heshima ya watu wake mpaka alipokuwa na uhakika kwamba dhabihu yake ilikuwa imepokelewa na Baba. Alipaa kwenda mbinguni, na alilisikia hakikisho kutoka kwa Mungu mwenyewe kwamba upatanisho wake kwa ajili ya dhambi za wanadamu ulikuwa umetosha na kuzidi, kwamba kwa damu yake wote wangepata uzima wa milele. Baba aliidhinisha agano lililofanywa kwa njia ya Kristo, kwamba angewapokea wanadamu watubuo na watiio, na kwamba angewapenda kama anavyompenda Mwana wake. Kristo alikuwa akamilishe kazi yake, na kutimiza ahadi yake ya kumfanya mwandamu kuwa na thamani "kuliko dhahabu safi, na watu kuliko dhahabu ya Ofiri." Isaya 13:12. Mamlaka yote mbinguni na duniani ilitolewa kwa Mfalme wa Uzima huyu, na alirudi kwa wafuasi wake katika ulimwengu wa dhambi, ili ya kwamba aingize nguvu zake na utukufu wake ndani yao.

Wakati Mwokozi alipokuwa mbele ya Mungu, akipokea vipawa kwa ajili ya kanisa lake, wanafunzi walikuwa wanafikiri kuhusu kaburi lililo wazi, na walilia na kuomboleza. Siku iliyokuwa ya furaha kwa mbingu yote, kwa wanafunzi ilikuwa ya mashaka, kuchanganyikiwa na kutatanishwa. Hali yao ya kutoamini **(793)** ushuhuda wa wanawake wale inaonyesha ushahidi wa jinsi imani yao ilivyokuwa imeshuka na kuwa haba. Habari za kufufuka kwa Kristo zilikuwa tofauti na vile walivyotarajia kiasi kwamba hawakuweza kuziamini. Walifikiri kwamba, Habari zile zilikuwa nzuri mno kiasi kwamba zisingekuwa za kweli. Walikuwa wamesikia habari nyingi za mafundisho ya dini na kile kinachoitwa nadharia za kisayansi za Masadukayo kiasi kwamba mawazo waliyokuwa nayo akilini kuhusu ufufuo yalikuwa yasiyo wazi. Hawakujua vizuri maana ya kufufuka kutoka katika wafu. Hawakuwa na uwezo wa kuhimili mada hiyo.

Malaika walikuwa wamesema kwamba, "Enendeni zenu, mkawaambie wanafunzi wake, na Petro, ya kwamba awatangulia kwenda Galilaya; huko mtamwona, kama alivyowaambia." Malaika hawa walikuwa wamekuwa na Kristo kama malaika walinzi katika maisha yake yote ya duniani. Walikuwa wameshuhudia kushtakiwa na kusulibiwa kwake. Walikuwa wamesikia maneno yake kwa wanafunzi wake. Hili lilionyeshwa na ujumbe wao kwenda kwa wanafunzi wale, na ujumbe ule ulipaswa kuwashawishi wao kwamba ni wa kweli. Maneno kama yale yangetoka tu kwa wajumbe wa Bwana wao aliyefufuka.

"Mkawaambie wanafunzi wake, na Petro," ndivyo walivyosema wale malaika. Tangu Kristo alipokufa, Petro alikuwa ameinama chini kwa kujisikia hatia. Kumkana Bwana kwa aibu vile, na kitendo cha Mwokozi kumtazama kwa upendo na maumivu, vilidumu kuwepo mbele yake. Yeye alikuwa ameumia sana zaidi ya wanafunzi wote. Uhakika unatolewa kwake kwamba toba yake imekubaliwa na msamaha umetolewa kwake. Ametajwa kwa jina.

"Mkawaambie wanafunzi wake, na Petro, ya kwamba awatangulia kwenda Galilaya; huko mtamwona." Wanafunzi wote walikuwa wamemwacha, na wito wa kukutana nao tena unawajumuisha wote. Hajawatupilia mbali. Wakati Mariamu Magdalena alipowaambia kwamba amemwona Bwana, alirudia wito wa kukutana naye Galilaya. Na kwa mara ya tatu ujumbe ulitumwa kwao tena. Baada ya kuwa amepaa kwenda kwa Baba, Yesu alijitokeza kwa wale wanawake wengine, akisema, "Salamu! Wakakaribia wakamshika miguu, wakamsujudia. Kisha Yesu akawaambia, Msiogope; enendeni, mkawaambie ndugu zangu waende Galilaya, ndiko watakakoniona."

Kazi ya kwanza ya Kristo duniani baada ya kufufuka kwake ilikuwa ni kuwaaminisha wanafunzi wake kuhusu upendo wake usioondosheka, na hali yake ya kuwajali. Kuwapa uthibitisho kwamba alikuwa Mwokozi wao aliye hai, kwamba alikuwa amevunja vifungo vya kaburi, na kwamba asingeweza tena kushikiliwa na adui kifo; kufunua kwamba alikuwa na moyo ule ule wa upendo aliokuwa nao wakati alipokuwa pamoja nao akiwa Mwalimu wao mpendwa, alijitokeza kwao tena na tena. Bado angeweza kuvuta vifungo vya upendo zaidi kwao. Alisema, Enendeni, mkawaambie ndugu zangu kwamba wakakutane na mimi kule Galilaya. **(794)** Waliposikia ahadi hii ya kukutana, ikiwa imetolewa bayana hivyo, wale wanafunzi walianza kutafakari kuhusu maneno ya Kristo aliyowaambia akitabiri habari ya kufufuka kwake. Lakini hata wakati huu hawakufurahishwa. Hawakuweza kutupilia mbali mashaka yao na kutatanishwa kwao. Hata wakati wale wanawake walipotangaza kwamba wamemwona Bwana, wale wanafunzi hawakuamini. Waliwadhania kwamba wamekutana na ndoto za uongo.

Shida ilionekana kukusanyika juu ya shida. Mnamo siku ya sita ya juma walikuwa wamemwona Bwana wao akifa; mnamo siku ya kwanza ya juma lililofuata walijikuta wakiwa wamenyang'anywa mwili wake, na walishutumiwa kwamba wameuiba mwili huo na kuuondoa pale ili kuwadanganya watu. Walipoteza matumaini hata ya kusahihisha mawazo ya uongo yaliyokuwa yanaongezeka kusambaa dhidi yao. Waliogopa uadui wa makuhani na ghadhabu ya watu. Walitamani kuwepo kwa Yesu, ambaye alikuwa msaada wao kila wakati kulipokuwa na hali ya kuchanganyikiwa.

Mara nyingi waliyarudia yale maneno kwamba, "Tulikuwa tukitumaini ya kuwa yeye ndiye atakayewakomboa Israeli." Wakiwa na upweke na ugonjwa wa moyo walikumbuka maneno yake kwamba, "Kama wakitenda mambo haya katika mti mbichi, itakuwaje katika mkavu?" Luka 24:21; 23:31. Walikutana pamoja katika chumba cha ghorofani, na wakafunga milango na kuikaza, wakijua kwamba huenda hatima iliyompata Mwalimu wao mpendwa ikawapata wao pia.

Wakati wote huu walipaswa kufurahia kujua habari za kufufuka kwa Mwokozi. Kule bustanini, alikuwa amesimama akilia, wakati Yesu alipokuwa karibu kabisa na yeye. Macho yake yalikuwa yamepofushwa na machozi kiasi kwamba hakuweza kumtambua. Na mioyo ya wanafunzi ilikuwa imejawa na majonzi kiasi kwamba hawakuamini ujumbe wa malaika wala maneno ya Kristo mwenyewe.

Wangapi ambao bado wanafanya yale yaliyofanywa na wanafunzi hawa! Wangapi ambao wanarudia kilio cha Mariamu kisicho na matumaini kwamba, "Wamemwondoa Bwana wangu, wala mimi sijui walikomweka"! Ni wangapi ambao wanapaswa kuambiwa maneno ya Mwokozi kwamba, "Unalilia nini? Unamtafuta nani?" Yeye yu karibu nao kabisa, lakini macho yao yaliyopofushwa kwa sababu ya kujawa na machozi hayamwoni. Anaongea nao, lakini hawaelewi.

Laiti vichwa vilivyoinamishwa vingeinuliwa, macho yakafumbuliwa ili kumwona, masikio yakaisikiliza sauti yake! "Nendeni upesi, mkawaambie wanafunzi wake, Amefufuka." Wasisitizeni wasiangalie katika kaburi jipya la Yusufu, lililokuwa limefunikwa kwa jiwe kubwa, na kutiwa lakiri kwa muhuri ya Kirumi. Kristo hayuko mle. Msitazame katika kaburi lililobaki tupu. Msiomboleze kama wale wasio na tumaini wala msaada. Yesu yu hai, na kwa sababu yu hai, nasi tutakuwa hai pia. Kutoka katika mioyo ya shukrani, kutoka katika midomo iliyoguswa na moto mtakatifu, hebu wimbo wa furaha usikike ukisema, Kristo amefufuka! Yu hai apate kutuombea. Chukua tumaini hili, nalo litaishikilia nafsi kama nanga ya uhakika iliyojaribiwa. Amini, nawe utauona utukufu wa Mungu.

## Sura ya 83

# Njiani Kwenda Emau

[Sura hii imejengwa katika Luka 24:13-33.]

Baadaye jioni sana mnamo siku ile ya kufufuka, wawili miongoni mwa wanafunzi walikuwa njiani wakienda Emau, mji mdogo ulio umbali wa maili nane kutoka Yerusalemu. Wanafunzi hawa hawakuwa na nafasi yoyote muhimu katika kazi ya Kristo, lakini walikuwa waamini wake wa dhati. Walikuwa wamekuja mjini ili kuadhimisha Pasaka, na walikuwa wametatanishwa sana na matukio yaliyokuwa yametukia muda kitambo. Walikuwa wamesikia habari za asubuhi kuhusu kuondolewa kwa mwili wa Kristo kutoka katika kaburi, na taarifa ya wanawake waliokuwa wameona malaika na kukutana na Yesu. Sasa walikuwa wanarejea majumbani mwao kutafakari na kuomba. Wakiwa na huzuni walitembea jioni ile, wakizungumza kuhusu matukio ya kushtakiwa na kusulibishwa kwake. Kamwe walikuwa hawajawahi kuvunjika moyo kiasi kile. Wakiwa hawana matumaini wala imani, walikuwa wanatembea katika kivuli cha msalaba.

Wakiwa hawajafika mbali katika safari yao mtu mgeni kwao aliungana nao, lakini walikuwa wamemezwa na mfadhaiko wao na kukata tamaa kiasi kwamba hawakumzingatia sana. Waliendelea na mazungumzo yao, wakieleza mawazo ya mioyo yao. Walikuwa wakitoa hoja kuhusu mafundisho ambayo Kristo alikuwa ametoa, ambayo ilionekana kama hawakuweza kuyaelewa. Kadiri walivyoongea habari zilizokuwa zimetokea, Yesu alitamani kuwafariji. Alikuwa ameona huzuni yao; alielewa mawazo yao yaliyokuwa yanawasumbua na kuwatatanisha kiasi cha kuleta akilini mwao mawazo kwamba, **(796)** Je! Mtu huyu, aliyejiruhusu mwenyewe kuteswa, aweza kuwa Kristo? Majonzi yao hayakuweza kuzuilika, nao wakalia machozi. Yesu alijua kwamba mioyo yao ilikuwa imefungwa pamoja naye kwa upendo, naye alitamani kuwapangusa machozi yao, na kuwajaza raha na furaha. Lakini lazima kwanza awape mafundisho ambayo wasingeyasahau kamwe.

"Akawaambia, Ni maneno gani haya mnayosemezana hivi mnapotembea? Wakasimama wamekunja nyuso zao. Akajibu mmoja wao, jina lake Kleopa, akamwambia, Je! Wewe peke yako u mgeni katika Yerusalemu, hata huyajui yaliyotukia humo siku hizi?" Walimweleza kuhusu kufadhaika kwao kwa ajili ya Bwana wao, "aliyekuwa mtu nabii, mwenye uwezo katika kutenda na kunena mbele za Mungu na watu wote;" lakini "wakuu wa makuhani na wakubwa wetu walivyomtia katika hukumu ya kufa, wakamsulibisha." Wakiwa na mioyo inayoumizwa na fadhaa, na wakiwa na midomo yenye kwikwi, wakaongeza kwamba, "Nasi tulikuwa tukitumaini ya kuwa yeye ndiye atakayewakomboa Israeli. Zaidi ya hayo yote, leo ni siku ya tatu tangu yalipotendeka mambo hayo."

Ni ajabu kwamba wanafunzi wale hawakukumbuka maneno ya Kristo, na kutambua kwamba alikuwa ametabiri matukio yale yaliyokuwa yametokea! Hawakutambua kwamba sehemu ya mwisho ya kuonekana kwake ingekuwa ya hakika kama ilivyokuwa ile sehemu ya kwanza, kwamba siku ya tatu angefufuka tena. Hii ilikuwa sehemu ambayo walipaswa kukumbuka. Makuhani na wakuu hawakusahau hili. Mnamo siku "iliyo baada ya Maandalio, wakuu wa makuhani, na Mafarisayo wakamkusanyikia Pilato, wakasema, Bwana, tumekumbuka kwamba yule mjanja alisema, alipokuwa akali hai, Baada ya siku tatu nitafufuka." Mathayo 27:62, 63. Lakini wanafunzi hawakukumbuka maneno haya.

"Akawaambia, Enyi msiofahamu, wenye mioyo mizito ya kuamini yote waliyoyasema manabii! Je! Haikumpasa Kristo kupata mateso haya na kuingia katika utukufu wake?" Wale wanafunzi walishanga kwamba huyu mtu mgeni kwao anaweza kuwa nani, kwamba amepenya hadi katika mioyo yao, na kuzungumza kwa ujasiri, upole, na huruma, na kwa matumaini vile. Kwa mara ya kwanza tangu Kristo aliposalitiwa, walianza kuhisi matumaini. Mara nyingi walimtazama mwenzao yule, na kufikiri kwamba maneno yake yale yalikuwa maneno ambayo Kristo angesema. Walijawa na mshangao, na mioyo yao ilianza kudunda kwa matarajio ya furaha.

Akianzia kwa Musa, aliye Alfa wa historia ya Biblia, Kristo alifafanua katika Maandiko yote mambo yaliyomhusu yeye mwenyewe. Ikiwa **(799)** angejitambulisha kwao kwanza, mioyo yao ingetosheka. Katika kujawa na furha wasingekuwa na njaa ya kitu kingine zaidi. Lakini ilikuwa lazima kwao kuelewa ushuhuda ambao mifano ya kivuli na unabii wa Agano la Kale vilihusisha kwake. Lazima imani yao ijengwe katika shuhuda hizo. Kristo

hakutenda mwujiza wowote kuwashawishi, lakini kazi yake ya kwanza ilikuwa ni kuyafafanua Maandiko. Walikuwa wamekichukulia kifo chake kama uharibifu wa matumaini yao yote. Sasa alionyesha kutoka katika manabii kwamba hii ilikuwa ndio ushahidi wa nguvu zaidi kwa ajili ya imani yao.

Katika kuwafundisha wanafunzi hawa, Yesu alionyesha umuhimu wa Agano la Kale kama ushuhuda wa kazi yake. Watu wengi wanaojitambulisha kuwa Wakristo sasa wanakataa Agano la Kale, wakidai kwamba haina matumizi tena. Lakini hayo si mafundisho ya Kristo. Aliithamini kwa kiwango kikubwa sana kiasi kwamba, "Wasipowasikia Musa na manabii, hawatashawishiwa hata mtu akifufuka katika wafu." Luka 16:31.

Sauti ya Kristo ndiyo inayonena kupitia kwa wazee na manabii, tangu mnamo siku za Adamu hadi wakati wa matukio ya mwisho wa wakati. Mwokozi anafunuliwa katika Agano la Kale kwa uwazi kama ilivyo katika Agano Jipya. Nuru kutoka katika unabii wa wakati uliopita ndiyo inayofanya maisha ya Kristo na mafundisho ya Agano Jipya kuwa na uwazi na uzuri. Miujiza ya Kristo ni uthibitisho wa uungu wake; lakini uthibitisho wenye nguvu zaidi kwamba Yeye ni Mkombozi wa ulimwengu unapatikana kwa kulinganisha nabii za Agano la Kale pamoja na historia ya Agano Jipya.

Akitoa hoja kutoka katika unabii, Kristo aliwapatia wanafunzi wake wazo sahihi la vile ambavyo angekuwa katika ubinadamu. Matarajio yao ya Masihi ambaye alikuwa achukue kiti chake cha enzi na nguvu za kifalme kulingana na matakwa ya wanadamu yalikuwa ya upotofu. Yangeingiliana na mawazo sahihi ya kushuka kwake kutoka nafasi ya juu sana hadi ya chini sana ambayo ingewezekana kuchukuliwa na mtu. Kristo alitamani kwamba wanafunzi wake wawe safi na wa kweli katika kila hali. Lazima waelewe hadi mbali iwezekanavyo kuhusu kikombe cha mateso kilichokuwa kimewekwa kama sehemu yake. Aliwaonyesha kwamba pambano la kutisha ambalo hawakuweza kulielewa lilikuwa ni utimilifu wa agano lililofanywa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Lazima Kristo afe, maana lazima kila mvunjaji wa sheria afe ikiwa anaendelea na dhambi. Haya yote yalikuwa yafanyike, lakini yasingeishia katika kushindwa, bali katika ushindi wa milele wa utukufu. Yesu aliwaambia kwamba lazima kila jitihada ifanywe ili kuuokoa ulimwengu kutoka dhambini. Lazima wafuasi wake waishi kama alivyoishi, na kutenda kama alivyotenda, kwa jitihana kubwa na uvumilivu.

**(800)** Hayo ndiyo mambo ambayo Kristo aliongea na wanafunzi wake, akiyafungua mawazo yao ili kwamba wayaelewe Maandiko. Wanafunzi wale walikuwa wamechoka, lakini mazungumzo yale hayakuwachosha. Maneno ya upendo na uhakikisho yalitoka midomoni mwa Mwokozi. Lakini bado macho yao yaliendelea kufumbwa. Pindi alipowaambia kuhusu kupinduliwa kwa Yerusalemu, waliutazama kwa kilio mji ule unaosubiri kuangamia. Lakini bado hawakuhisi kwamba huyu wanayesafiri naye ni nani. Hawakujua kwamba mhusika wa mada ya mazungumzo yao ndiye aliyekuwa anatembea kando yao; maana Kristo aliongea kuhusu Yeye mwenyewe kama anayeongea kuhusu mtu mwingine. Walidhani kwamba alikuwa mmoja wa wale waliokuwa katika kuadhimisha sikukuu ile, ambaye alikuwa anarudi nyumbani kwake. Alitembea kwa uangalifu kama wao pale katika ile njia mbaya ya mawe, akisimama mara kwa mara pamoja nao ili kupumzika. Waliendelea hivyo katika barabara ile ya milima wakiwa pamoja na Yeye ambaye muda si mrefu alikuwa achukue nafasi yake katika mkono wa kuume wa Mungu, na ambaye angesema kwamba, "Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani," alipotembea pamoja nao. Mathayo 28:18.

Wakati wa safari yao jua lilikuwa limezama, na kabla wasafiri hawa hawajafika mahali pao pa kupumzikia, wakulima mashambani walikuwa wameondoka. Na pindi wale wanafunzi walipotaka kuingia nyumbani kwao, yule mtu mgeni alionekana kama alikuwa aendelee na safari yake. Lakini wanafunzi walihisi kuvutwa naye sana. Mioyo yao ilikuwa na njaa ya kusikia zaidi maneno yake. Wakasema, "Kaa pamoja nasi." Hakuonekana kukubali mwaliko ule, lakini walimsisitiza, wakisema, "Kwa kuwa kumekuchwa, na mchana unakwisha." Kristo alikubaliana na kule kusihi kwao. "Akaingia ndani kukaa nao."

Ikiwa wanafunzi wale wangeshindwa kusisitiza mwaliko wao, wasingejua kwamba msafiri mwenzao alikuwa Bwana aliyefufuka. Kristo halazimishi kamwe ushirikiano na mtu yeyote. Anapendelea kushirikiana na wale wanaomhitaji. Kwa furaha anaingia katika nyumba inayojishusha, na huufurahisha moyo wa hali ya chini sana. Lakini ikiwa watu hawajali kufikiri kuhusu huyu Mgeni kutoka mbinguni, au kumwomba akae pamoja nao, anapita na kwenda zake. Kwa njia hiyo wengi hupata hasara kubwa. Hawamjui Kristo zaidi ya vile wanafunzi walivyokuwa wanamjua alipotembea nao njiani.

Muda si mrefu chakula chepesi cha jioni kinaandaliwa. Kinawekwa mbele ya mgeni, ambaye amekaa kwenye kiti kikubwa cha mezani. Ananyosha mikono yake kukibariki chakula kile. Wale wanafunzi wanaanza kushangaa tena. Rafiki yao yule anainyosha mikono yake sawasawa kabisa na vile Bwana wao alivyofanya mara kwa mara. Wanatazama tena, na tazama, wanaona alama za misumari mikononi mwake. Wote wawili wanasema kwa msahangao kwamba, Ni Bwana Yesu! Amefufuka kutoka katika wafu! **(801)** Wanainuka ili kujitupa miguuni pake na kumsujudia, lakini anatoweka kutoka machoni pao. Wanapaangalia mahali alipokuwa ameketi Yeye ambaye mwili wake ulikuwa umelazwa kaburini muda si mrefu, na kuambiana wao kwa wao, "Je! Mioyo yetu haikuwaka ndani yetu hapo alipokuwa akisema nasi njiani, na kutufunulia maandiko?"

Lakini hawawezi kukaa na kuongea wakiwa na habari hizi za kuwaambia watu. Uchovu wao na njaa yao vimeondoka. Wanaacha mlo wao bila hata kuuonja, na mara wanashika njia tena kwa furaha wakirudi kwa njia ile ile waliyokuwa wamepita, wakiharakisha kwenda kuwapasha habari wanafunzi walioko mjini. Katika baadhi ya maeneo ya njia ile hakuna usalama, lakini wanapanda kupitia miinuko mikali, huku wakiteleza kwenye miamba iliyo laini. Hawaoni, hawajui, kwamba wana ulinzi wake Yeye aliyekuwa amesafiri pamoja nao katika njia ile. Wakiwa na fimbo ya msafiri mkononi mwao, waliendelea na safari, wakitamani kwenda haraka kuliko walivyoweza. Mara wanapotea njia na kuipata tena. Wakati mwingine wanakimbia, wakati mwingine wanajikwaa, wanasonga mbele, Yule Mwenzao asiyeonekana akiwa karibu yao njia yote.

Usiku ni wa giza, lakini Jua la Haki linawaangazia. Mioyo yao inaruka kwa furaha. Wanaonekana kama walio katika ulimwengu mpya. Kristo ni Mwokozi aliye hai. Hawamwombolezei tena kwamba amekufa. Kristo amefufuka – wanarudia tena na tena. Huu ndio ujumbe ambao wanawapelekea watu wale wanaohuzunika. Lazima wawaambie kisa cha ajabu cha safari yao ya kwenda Emau. Lazima wawasimulie kuhusu Yeye aliyeungana nao njiani. Wanapeleka ujumbe mkuu mno ambao haujapata kutolewa kwa ulimwengu, ujumbe wa habari za furaha ambao kwa huo matumaini ya jamaa ya wanadamu hutegeme kwa wakati na milele.

## Sura ya 84

# "Amani Iwe Kwenu"

[Sura hii imejengwa katika Luka 24:33-48; Yohana 20:19-29.]

Walipofika Yerusalemu wale wanafunzi wawili waliingilia katika lango la mashariki, ambalo linakuwa wazi usiku nyakati za sikukuu. Majumba yako gizani na katika ukimya, lakini wasafiri wale wanashika njia ya kupita katika mtaa mwembamba wakimulikiwa na mbalamwezi iliyokuwa inatokeza. Wanaenda katika kile chumba cha ghorofani mahali Yesu alipokuwa kwa saa za jioni ile ya mwisho kabla ya kifo chake. Wanajua kwamba watawakuta ndugu zao pale. Hata kama muda ulikuwa emeenda sana, wanajua kwamba wanafunzi wale hawatalala mpaka wajue kwa hakika kilichotokea kuhusu mwili wa Bwana wao. Wanakuta mlango wa chumba kile ukiwa umefungwa barabara. Wanabisha hodi, lakini hakuna anayeitika. Mambo yote yamekwisha. Wanajitaja majina yao. Mlango unafunguliwa kwa uangalifu, wanaingia, na Mwingine, bila kuonekana, anaingia pamoja nao. Halafu mlango unafungwa tena na kukazwa, kuzuia wapelelezi wasiingie.

Wale wasafiri wanawakuta hawa katika mshangao. Sauti za wale waliomo katika chumba zinapaa kwa shukrani na nyimbo za sifa, zikisema, "Bwana amefufuka kweli kweli, naye amemtokea Simoni." Halafu wale wasafiri wawili, wakipumua haraka haraka vile walivyokuwa katika safari, wanasimualia kisa cha ajabu cha jinsi Yesu alivyowatokea. Ndipo wakiwa wamemaliza tu, na baadhi wakisema kwamba hawawezi kuamini, maana ni habari nzuri mno kiasi kwamba haziwezi kuwa za kweli, ndipo, tazama, Nafsi nyingine inasimama mbele yao. Kila jicho linakazwa kwa mgeni yule. Hakuna mtu ambaye amebisha hodi mlangoni kutaka kuingia. Hakuna **(803)** sauti za vishindo vya nyayo za miguu zitembeazo ambazo zimesikika. Wanafunzi wanashtushwa, na kushangaa maana yake nini. Ndipo wanasikia sauti ya Bwana wao. Kwa sauti bayana na ya wazi maneno yanatoka midomoni mwake, yakisema, "Amani iwe kwenu."

"Wakashituka, wakaogopa sana, wakidhani ya kwamba wanaona roho. Akawaambia, Mbona mnafadhaika? Na kwa nini mnaona shaka mioyoni mwenu? Tazameni mikono yangu na miguu yangu, ya kuwa ni mimi mwenyewe. Nishikenishikeni, mwone; kwa kuwa roho haina mwili na mifupa kama mnavyoniona mimi kuwa nayo. Na baada ya kusema hayo aliwaonyesha mikono yake na miguu yake."

Waliitazama ile mikono na miguu iliyoharibiwa na misumari ile ya kikatili. Waliitambua sauti yake, iliyokuwa tofauti na nyingine yoyote waliyopata kusikia. "Basi walipokuwa hawajaamini kwa furaha, huku wakistaajabu, aliwaambia, Mna chakula chochote hapa? Wakampa kipande cha samaki wa kuokwa. Akakitwaa, akala mbele yao." "Basi wale wanafunzi wakafurahi walipomwona Bwana." Imani na furaha vilichukua nafasi ya kutoamini, nao wakamkiri Mwokozi wao aliyefufuka kwa hisia ambayo haina maneno ya kuieleza.

Wakati wa kuzaliwa kwa Yesu malaika alitangaza kwamba, Amani iwe duniani, kwa watu wote aliowaridhia. Na sasa wakati wa kutokea kwake kwa wanafunzi wake kwa mara ya kwanza baada ya kufufuka, Mwokozi aliwaambia maneno hayo hayo ya baraka kwamba, "Amani **(804)** iwe kwenu." Daima Yesu yuko tayari kutamka amani kwa watu ambao wamelemewa na mashaka na hofu. Hutusubiri tumfungulie mlango wa moyo, na kumwambia, Kaa nasi. Yeye husema, "Tazama, nasimama mlangoni, nabisha; mtu akiisikia sauti yangu, na kuufungua mlango, nitaingia kwake, nami nitakula pamoja naye, na yeye pamoja nami." Ufunuo 3:20.

Kufufuka kwa Yesu kulikuwa ni mfano wa ufufuo wa wote walalao ndani yake. Mwonekano wa Mwokozi aliyefufuka, jinsi alivyo, kuongea kwake, vilijulikana vyote kwa wanafunzi wake. Vile Yesu alivyofufuka kutoka katika wafu, ndivyo wale wanaolala katika Yeye watakavyofufuka. Tutawajua rafiki zetu, kama vile wanafunzi walivyomjua Yesu. Yawezekana, katika maisha haya ya kufa, wakawa wamebadilika kwa miili kuharibika, kudhoofu, au kubadilika umbo, wakati huo wakafufuka wakiwa na afya iliyo kamilifu na sawasawa; lakini bado katika mwili wenye utukufu utambulisho wao utaendelea kuwepo. Wakati huo tutajua kama tunavyojuliwa. 1 Wakorintho 13:12. Katika uso unaong'aa kwa nuru iangazayo kutoka katika uso wa Yesu, tutatambua alama za utambulisho za sura za wale tuwapendao.

Wakati Yesu alipokutana na wanafunzi wake, aliwakumbusha kuhusu maneno aliyowaambia kabla ya kifo chake, kwamba lazima yatimizwe mambo yote yaliyoandikwa katika sheria ya Musa, na katika manabii, na katika

Zaburi kumhusu Yeye. "Ndipo akawafunulia akili zao wapate kuelewa na maandiko. Akawaambia, Ndivyo **(805)** ilivyoandikwa, kwamba Kristo atateswa na kufufuka siku ya tatu; na kwamba mataifa yote watahubiriwa kwa jina lake habari ya toba na ondoleo la dhambi, kuanza Yerusalemu. Nanyi ndinyi mashahidi wa mambo haya."

Wanafunzi walianza kutambua hali ya kazi yao na mapana yake. Walikuwa wauhubirie ulimwengu kweli za ajabu ambazo Kristo alikuwa amekabidhi kwao. Matukio ya maisha yao, kufa na kufufuka kwake, unabii ulioelekeza kwa matukio haya, utakatifu wa sheria ya Mungu, siri ya mpango wa ukombozi, uwezo wa Yesu wa kuondoa dhambi, - walikuwa mashahidi wa mambo yote haya, na walikuwa wayafanye yajulikane kwa ulimwengu wote. Walikuwa waihubiri injili ya amani na wokovu kwa njia ya toba na nguvu za Mwokozi.

"Naye akiisha kusema hayo, akawavuvia, akawaambia, Pokeeni Roho Mtakatifu. Wowote mtakaowaondolea dhambi, wameondolewa; na wowote mtakaowafungia dhambi, wamefungiwa." Roho Mtakatifu alikuwa hajadhihirishwa kikamilifu; maana Kristo alikuwa hajatukuzwa. Kujazwa kwa Roho kwa wingi hakukufanyika hadi baada ya kupaa kwa Kristo. Kabla ya kumpokea huyo, wanafunzi wale wasingeweza kutekeleza agizo la kuihubiri injili ulimwenguni mwote. Lakini kwa sasa Roho alitolewa kwa kusudi maalum. Kabla ya wanafunzi kuweza kutekeleza wajibu wao rasmi unaohusiana na kanisa, Kristo aliwapulizia Roho Mtakatifu. Alikuwa anakabidhi kwao amana takatifu mno, na alitamani kuwaonyesha kwamba bila Roho Mtakatifu kazi hii isingewezekana kufanywa.

Roho Mtakatifu ni pumzi ya uhai wa kiroho ndani ya mtu. Kumjaza mtu Roho ni kumjaza mtu uhai wa Kristo. Kunamhuisha mpokeaji kwa kumpa kuwa na sifa za Kristo. Wale tu wanaofundishwa hivyo na Mungu, ambao wana utendaji wa ndani wa Roho, na wenye maisha ambayo ndani yake kunadhihirishwa maisha ya Kristo, ndio wanaopaswa kusimama kama watu wawakilishi, wakihudumu kwa niaba ya kanisa.

Kristo alisema, "Wowote mtakaowaondolea dhambi, wameondolewa; na wowote mtakaowafungia dhambi, wamefungiwa." Hapa Kristo hakutoa uhuru kwa mtu yeyote kutoa hukumu kwa wengine. Katika hubiri lake la Mlimani alikataza jambo hili. Hiyo ni haki ya Mungu. Lakini ameweka wajibu kwa waamini mmoja-mmoja walio katika kanisa lenye utaratibu. Kanisa linao wajibu kwa wale wanaoangukia dhambini, kuonya, kufundisha, na ikiwezekana kurejesha. Bwana anasema, "karipia, kemea, na kuonya kwa uvumilivu wote na mafundisho." 2 Timotheo 4:2. Shughulika **(806)** na watenda mabaya kwa uaminifu. Okoa kila nafsi iliyo hatarini. Msiwaache watu wajidanganye. Iite dhambi kwa jina lake halisi. Tangaza kile ambacho Mungu amesema kuhusu kudanganya, kutunza Sabato, kuiba, kuabudu sanamu, na kila uovu mwingine wowote. "Wafanyao mambo kama hayo hawataurithi ufalme wa Mungu." Wagalatia 5:21. Ikiwa wanadumu kuwa dhambini, hukumu uliyotangaza kutoka katika neno la Mungu inakuwa imetamkwa juu yao huko mbinguni. Katika kule kuchagua kutenda dhambi, wanamwacha Krsto; lazima kanisa lionyeshe kwamba haliungi mkono vitendo vyao, la sivyo nalo pia litakuwa halimheshimu Bwana wake. Lazima liiseme dhambi vile Mungu anavyoisema. Lazima lishughulike na dhambi kwa namna ambavyo Mungu anaelekeza, na hatua yake hiyo inaidhinishwa mbinguni. Yeye anayedharau mamlaka ya kanisa anadharau mamlaka ya Kristo mwenyewe.

Lakini upo upande wenye kunga'aa wa jambo hilo. "Wowote mtakaowafungia dhambi, wamefungiwa." Hebu wazo hili liinue zaidi wakati wote. Katika kutumika kwa ajili ya walio makosani, hebu kila jicho lielekezwe kwa Kristo. Hebu wachungaji wa kondoo wawe na wema kwa kondoo wa malisho ya Bwana. Hebu wawaeleze wenye makosa kuhusu rehema ya Mwokozi yenye kusamehe. Hebu wamtie moyo mwenye dhambi ili atubu, na kumwamini Yeye anayeweza kusamehe. Hebu na watangaze, kwa mamlaka ya neno la Mungu, kwamba, "Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote." 1 Yohana 1:9. Wote wanaotubu wamehakikishiwa kwamba, "Atarejea na kutuhurumia; atayakanyaga maovu yetu; nawe utazitupa dhambi zao zote katika vilindi vya bahari." Mika 7:19.

Hebu toba ya mwenye dhambi na ikubaliwe na kanisa kwa moyo wa dhati. Hebu anayetubu aongozwe kutoka katika giza la kutokuamini kwenda katika nuru ya imani na haki. Hebu mkono wake unaotetemeka uwekwe katika mkono wa upendo wa Kristo. Ondoleo la dhambi kama hilo linaidhinishwa mbinguni.

Ni katika mwelekeo huu tu ndipo kanisa lina mamlaka ya kuondoa dhambi. Ondoleo la dhambi linaweza kupatikana kwa wema wa Kristo tu. Hakuna mtu yeyote, wala mmoja wa wanadamu yeyote, aliyepewa uwezo wa kumwondoa mtu hatiani. Kristo aliwataka wanafunzi wake kuhubiri ondoleo la dhambi katika jina lake katika

mataifa; lakini wao wenyewe hawakuwezeshwa kuondoa hata doa moja la dhambi. Jina la Yesu ndilo jina pekee “chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo." Matendo 4:12.

Wakati Yesu alipokutana na wanafunzi wake kwa mara ya kwanza kule katika chumba cha ghorofani, Tomaso hakuwepo pamoja nao. Alisikia taarifa za watu wengine, na kupokea ushahidi mwingi kwamba Yesu alikuwa amefufuka; lakini mfadhaiko na kutoamini vilikuwa vimeujaza moyo wake. Alipowasikia wanafunzi wakisimulia habari za kutokea kwa ajabu kwa Mwokozi aliyefufuka, habari hizo zilimwingiza tu katika lindi la mfadhaiko wa kina. Ikiwa Yesu alikuwa **(807)** amefufuka kweli kutoka kwa wafu, basi kusingekuwa na tumaini tena la kupata ufalme wa kawaida wa kidunia. Na ile hali ya kufikiri kwamba Bwana wake angejidhihirisha kwa wanafunzi wote isipokuwa yeye tu ilijeruhi kiburi chake. Aliazimia kutoamini, na kwa juma zima alisumbuliwa na mashaka ya kutoamini kwake, ambayo yalionekana kama giza tofauti na tumaini na imani iliyokuwa kwa ndugu zake.

Mnamo wakati huu alisema kwa kurudiarudia kwamba, “Mimi nisipoziona mikononi mwake kovu za misumari, na kutia kidole changu katika mahali pa misumari, na kutia mkono wangu katika ubavu wake, sisadiki hata kidogo." Hakuweza kuona kupitia macho ya ndugu zake, au kufanyia kazi imani iliyotegemea ushuhuda wao. Alimpenda Bwana wake, lakini alikuwa ameruhusu wivu na kutokuamini kujaza akili zake na moyo wake.

Idadi kadhaa ya wanafunzi walikifanya kile chumba cha juu kuwa nyumbani pao kwa muda, na wakati wa jioni wote isipokuwa Tomaso walikusanyika mahali hapa. Jioni moja Tomaso aliazimu kukutana na wengine. Licha ya kutokuamini kwake, alikuwa na imani hafifu kwamba zile habari njema ni za kweli. Wakati wanafunzi walipokuwa wakila chakula cha jioni, waliongea kuhusu ushahidi ambao Kristo alikuwa amewapatia katika unabii. "Akaja Yesu, na milango imefungwa, akasimama katikati, akasema, Amani iwe kwenu."

Akimgeukia Tomaso alimwambia, "Lete hapa kidole chako; uitazame mikono yangu; ulete na mkono wako uutie ubavuni mwangu, wala usiwe asiyeamini, bali aaminiye." Maneno haya yanaonyesha kwamba alifahamu vema mawazo na maneno ya Tomaso. Yule mwanafunzi mwenye mashaka alijua kwamba hakuna hata mmoja wa wenzake wale aliyekuwa amemwona Yesu kwa juma zima. Haiwezekani kwamba walikuwa wamemwambia Bwana kuhusu kutokuamini kwake. Alimtambua Huyu aliyekuwa mbele yake kwamba ni Bwana. Hakuwa na hamu ya uthibitisho zaidi. Moyo wake uliruka kwa shangwe, na alijitupa miguuni pa Yesu akilia kwamba, "Bwana wangu na Mungu wangu."

Yesu alikubali kukiri huko kwa Tomaso, lakini kwa upole alikemea kutokuamini kwake: "Wewe, kwa kuwa umeniona, umesadiki; wa heri wale wasioona, wakasadiki." Imani ya Tomaso ingeweza kuwa ya kumpendeza Kristo zaidi ikiwa angekuwa radhi kuamini ushuhuda wa ndugu zake. Ikiwa ulimwengu sasa ungefuata mfano wa Tomaso, hakuna hata mmoja ambaye angeuamini wokovu; maana wote wampokeao Kristo lazima wafanye hivyo kwa sababu ya ushuhuda wa wengine.

Wengi wanaoona mashaka wanatoa udhuru kwa kusema kwamba ikiwa wangekuwa tu na ushahidi ule ambao Tomaso alikuwa nao kutoka kwa ndugu zake, wangeamini. Hawatambui kwamba si tu kwamba wanao ushahidi ule, bali **(808)** pia kwamba wanao mwingi zaidi ya ule. Wengi ambao, kama Tomaso, husubiri mpaka mashaka yote yaondolewe, kamwe hawatapata wanachotamani kupata. Pole pole wanazoea kukubali hali ya kutoamini. Wale wanaojifunza kutazama upande wa giza, na kunung’unika na kulaumu, hawajui wafanyalo. Wako wanapanda mbegu za mashaka, na watavuna mashaka kama mavuno yao. Mnamo wakati ambapo imani na ujasiri vinahitajika sana, wengi watajikuta hawana uwezo wa kuamini na kutumaini.

Katika namna ile alivyotenda kwa Tomaso, Yesu aliwapa somo wafuasi wake. Mfano wake unaonyesha jinsi ambavyo tunapaswa kuwashughulikia wale ambao wana imani dhaifu, na wanaotanguliza mashaka yao. Yesu hakumjazia Tomaso makemeo, wala hakuingia katika mapambano na yeye. Alijifunua kwa mwenye mashaka huyu. Tomaso hakutumia busara katika kulazimisha hali ya imani yake, lakini Yesu, kwa upendo wake mwingi na kujali kwingi, aliangusha vizuizi vyote. Ni kwa nadra sana kuondoa hali ya kutoamini kwa kutumia mapambano. Badala yake hali hiyo inaleta njia ya kujitetea, na kupata kuungwa mkono na udhuru. Lakini hebu Yesu, katika upendo na wema wake, na afunuliwe kama Mwokozi aliyesulibiwa, na kutoka katika midomo ya wengi ambao walikuwa hawaamini kabla yatasikika maneno ya kukiri ya Tomaso kwamba, "Bwana wangu na Mungu wangu."

## Sura 85

# Kando ya Bahari Tena

[Sura hii imejengwa katika Yohana 21:1-22.]

Yesu alikuwa ameahidi kukutana na wanafunzi wake kule Galilaya; na mara tu baada ya Pasaka kuhitimishwa walielekea katika eneo hilo. Kutokuwepo kwao Yerusalemu mnamo wakati wa maadhimisho ya sikukuu kungeeleweka kama hali ya kutoridhika na kwamba ni upinzani wa uasi, kwa hiyo walibaki pale mpaka ilipoisha; baada ya hapo, walirejea kwa furaha maeneo ya nyumbani kukutana na Mwokozi kama alivyokuwa ameelekeza.

Miongoni mwa wanafunzi wale, saba walikuwa kundi moja. Walikuwa wamevaa nguo za hali duni za kivuvi; walikuwa maskini katika mali za dunia, lakini matajiri katika maarifa na matendo ya ukweli, ambavyo machoni pa Mbingu viliwapatia nafasi ya juu kama waalimu. Walikuwa watu ambao hawakupata kuwa wanafunzi katika shule za manabii, lakini kwa miaka mitatu walikuwa wamefundishwa na Mkufunzi aliye mkuu kuliko wote waliopata kujulikana duniani. Chini ya mafunzo yake walikuwa wamekuwa watu walioinuliwa, wenye ufahamu, na waliochujwa, mawakala ambao kupitia kwao wanadamu wangeongozwa kuujua ukweli.

Muda mwingi wa huduma ya Yesu ulikuwa umetumiwa karibu na Bahari ya Galilaya. Wakati wanafunzi walipokusanyika mahali hapa palipoonekana kama patulivu pasipo na usumbufu, walijikuta wamezungukwa na vitu vya kuwakumbusha kuhusu Yesu na matendo yake makuu. Mle baharini, wakati ule mioyo yao ilipojawa na hofu, wakati tufani kali ilipotaka kuwaangamiza, Yesu alikuwa ametembea kwenye maji kuja kuwaokoa. Hapa ndipo dhoruba ilipotulizwa kwa neno lake. Machoni pao kulikuwa na ufukwe mahali ambapo zaidi ya watu elfu kumi walikuwa wamelishwa kwa mikate na samaki vilivyokuwa vichache na vidogo. Mahali ambapo si mbali ulikuwepo mji wa Kapernaumu, mahali pa matukio ya miujiza mingi. Kadiri wanafunzi **(810)** walivyoutazama ule mwonekano, akili zao zilijawa na maneno na matendo ya Mwokozi wao.

Jioni ile ilikuwa ya kupendeza, na Petro, ambaye alikuwa bado ana upendo wa zamani wa kazi za mashua na uvuvi, alipendekeza kwamba waende baharini wakazishushe nyavu. Wote walikuwa tayari kuungana na mpango huu; walikuwa na uhitaji wa chakula na mavazi, vitu ambavyo vingepatikana kwa mafanikio ya kazi za uvuvi wa usiku. Kwa hiyo walitoka wakaenda mashuani kuvua, lakini hawakupata kitu. Walisumbuka na kazi ya usiku mzima, pasipo na mafanikio. Katika saa hizo za kuchosha waliongea kuhusu Bwana wao ambaye hakuwepo, na kukumbuka matukio ya ajabu waliyokuwa wameshuhudia katika kazi yake kando ya baari ile. Walijihoji kuhusu hatima yao ya siku za usoni, huzuni ikawajaa kwa sababu ya kufikiri kuhusu hatima yao.

Wakati wote mwangalizi pekee aliyekuwa pwani aliwafuata kwa jicho lake, wakati Yeye mwenyewe alikuwa haonekani. Baada ya muda mrefu kulipambazuka. Mashua ilikuwa umbali mfupi tu kutoka ufukweni, na wanafunzi wale wakaona mtu mgeni akiwa amesimama ufukweni, ambaye aliwadakiza kwa swali, "Wanangu, mna kitoweo?" Walipojibu kwamba, "La," "Akawaambia, Litupeni jarife upande wa kuume wa chombo, nanyi mtapata. Basi wakatupa; wala sasa hawakuweza kulivuta tena kwa sababu ya wingi wa samaki."

Yohana alimtambua yule mgeni, na akasema kwa mshangao, "Ndiye Bwana." Petro alijawa na furaha na hamasa kiasi kwamba kwa hamu yake alijitupa majini na muda si mrefu alikuwa tayari amesimama karibu na Bwana wake. Wale wanafunzi wengine walikuja ndani ya mashua, wakizikokota nyavu zenye samaki. "Basi waliposhuka pwani, wakaona huko moto wa makaa, na juu yake pametiwa samaki, na mkate."

Walikuwa wameshikwa na mshangao mno kiasi kwamba hawakuuliza mahali moto na chakula kile vilikotoka. "Yesu akawaambia, Leteni hapa baadhi ya samaki mliowavua sasa hivi." Petro aliharakisha kwenda penye wavu, aliokuwa amedondosha, akawasaidia ndugu zake kuuvuta hadi ufukweni. Baada ya kazi kukamilika, na maandalizi kufanywa, Yesu aliwataka wanafunzi wale waje wale. Alikimega kile chakula, na kuwagawia, na akafahamika na kutambuliwa na wale wanafunzi wote saba. Ule mwujiza wa kulisha watu elfu tano ubavuni mwa mlima ulirejea mawazoni mwao; lakini butwaa isiyo ya kawaida ilikuwa imewashika, na wakiwa kimya walimtazama Mwokozi aliyefufuka.

Walikumbuka wazi wazi tukio la kando ya bahari wakati Yesu alipokuwa amewataka wamfuate. Walikumbuka jinsi ambavyo, kwa amri yake, walikuwa wameondoka kwenda kutupa nyavu katika sehemu ya kina, wakanasa samaki wengi wa kujaza nyavu, hata kiasi cha kutoboa nyavu. Halafu Yesu akawaita na kuwataka waache vyombo vyao vya kuvulia, na akawaahidi kuwafanya kuwa **(811)** wavuvi wa watu. Kwa lengo la kuwarejeshea akilini mwao matukio haya, na kuzamisha kwa kina mguso wa matukio hayo, alitenda mwujiza huu tena. Kitendo chake kilikuwa cha kufanya upya agizo lake la utume kwa wanafunzi wale. Kiliwaonyesha kwamba kifo cha Bwana wao hakikuwa kimepunguza wajibu wao wa kuifanya kazi aliyokuwa amewapatia. Ingawa wangeondolelewa uwepo wake pamoja nao kimwili, na kuondolelewa njia za kuwategemeza katika ajira zao za awali, bado Mwokozi aliyefufuka angewatunza. Wakiwa wanafanya kazi yake, angewapatia mahitaji yao. Na Yesu alikuwa na kusudi katika kuwataka washushe nyavu zao upande wa kuume wa chombo. Akiwa ufukweni alikuwa amesimama upande huo. Huu ulikuwa upande wa imani. Ikiwa wangefanya kazi kwa kuunganishwa naye, - uwezo wake wa kiungu ukiungana na jitihada zao za kibinadamu, - wasingeshindwa kufanikiwa.

Kristo alikuwa atoe fundisho jingine, hasa likimhusu Petro. Kitendo cha Petro kumkana Bwana wake kilikuwa kimekuwa cha aibu kikikinzana na tamko lake la ahadi ya kumfuata Bwana. Hakuwa amemheshimu Kristo, na alikuwa amesababisha mzigo wa kutoamini kwa ndugu zake. Walidhani kwamba asingeruhusiwa kurudi katika nafasi yake ya awali miongoni mwao, na yeye mwenyewe alihisi kwamba alikuwa amehafifisha uaminifu wake. Kabla ya kuitwa kuibeba tena kazi yake ya kitume, lazima atoe ushahidi wa ungamo lake mbele yao wote. Tofauti na hivi, dhambi yake, ingawa ingekuwa imeungamwa, ingekuwa imeharibu mvuto wake kama mtumishi wa Kristo. Mwokozi alimpatia fursa ya kujipatia hali ya kuaminika tena miongoni mwa ndugu zake, na, kwa kiasi kikubwa iwezekanavyo, kuondoa hali ya fedheha aliyokuwa ameleta katika injili.

Anapewa fundisho kwa ajili ya wafuasi wote wa Kristo. Injili haifanyi maafikiano na uovu. Haiwezi kuwa na udhuru na dhambi. Dhambi za siri zapaswa kuungamwa kwa Mungu kwa siri; lakini, kwa dhambi za wazi, ungamo la wazi linahitajika. Fedheha ya dhambi ya mwanafunzi inakuwa fedheha ya Kristo. Inamfanya Shetani kushangilia ushindi, na kuziyumbisha nafsi za watu ili kuzifanya zijikwae. Kwa kutoa uthibitisho wa toba, mwanafunzi huyo anapaswa kuondosha fedheha hii na kuipeleka mbali kwa kadiri uwezo wake uwezavyo.

Wakati Kristo na wanafunzi wale walipokuwa wanakula pamoja pale kando ya bahari, Mwokozi alimwambia Petro, "Je! Simoni wa Yohana, wewe wanipenda kuliko hawa?" akiongea kuhusu wale wenzake. Wakati fulani Petro alikuwa ametangaza kwamba, "Wajapochukizwa wote kwa ajili yako, mimi sitachukizwa kamwe." Mathayo 26:33. Lakini sasa alifanya makadirio ya kweli zaidi juu yake. Akasema, "Ndiyo, Bwana, wewe wajua kuwa nakupenda." Hakuna hakikisho la nguvu kwamba upendo wake ni mkubwa zaidi ya ule wa wenzake. Hatoi maoni yake binafsi kuhusu kujitoa kwake. Anamwachia Yeye anayeweza kusoma hisia za moyo ili ahukumu udhati wake wa moyo, - "Wewe wajua kwamba nakupenda." Yesu akamwambia, "Lisha wana-kondoo wangu."

**(812)** Yesu alimwuliza tena Petro swali lile la kipimo, kwa maneno yale yale ya awali: "Simoni wa Yohana, wanipenda?" Awamu hii hakumwuliza Petro ikiwa anampenda zaidi kuliko wenzake walivyompenda. Jibu la pili lilikuwa kama lile la kwanza, likiwa halina uhakika wa kujidai binafsi: "Ndiyo, Bwana, wewe wajua kuwa nakupenda." Yesu akamwambia, "Lisha kondoo zangu." Kwa mara nyingine zaidi Mwokozi aliuliza swali lile lile la kupima: "Simoni wa Yohana, wanipenda?" Petro akahuzunika; alidhani kwamba Yesu alikuwa na wasiwasi na upendo wake. Alijua kwamba Bwana wake anayo sababu ya kukosa imani kwake, na akiwa na maumivu ya moyo alijibu kwamba, "Bwana, wewe wajua yote; wewe umetambua ya kuwa nakupenda." Yesu akamwambia tena kwamba, "Lisha kondoo zangu."

Petro alikuwa amemkana Bwana wake mara tatu wazi wazi, na kutoka kwake Yesu alipata hakikisho la upendo na utii mara tatu, akilikandamizia mahali pake swali lile kali, likiwa kama mshale wenye chembe katika moyo wake ule uliokuwa umejeruhiwa. Yesu alidhihirisha kina cha toba ya Petro mbele ya kusanyiko la wanafunzi, na alionyesha jinsi mwanafunzi yule mshupavu alivyokuwa amenyenyekeshwa.

Kwa kawaida Petro alikuwa mwenye kimbelembele na mshupavu, na Shetani alikuwa ametumia sifa hizi kumpindua. Muda mfupi tu kabla ya kuanguka kwa Petro, Yesu alikuwa amemwambia kwamba, "Shetani amewataka ninyi apate kuwapepeta kama vile ngano; lakini nimekuombea wewe ili imani yako isitindike; nawe utakapoongoka waimarishe ndugu zako." Luka 22:31, 32. Sasa wakati huo ulikuwa umefika, na badiliko la ndani ya Petro lilikuwa dhahiri. Maswali yale ya mwisho ya Bwana ya kupima hayakumwalika kuwa mbele, na kujibu

kwa ujasiri binafsi; na kwa sababu ya maumivu na toba yake, Petro alikuwa ameandaliwa vema zaidi kuliko kabla kufanya kazi ya kuchunga kondoo.

Kazi ya kwanza ambayo Kristo alikabidhi kwa Petro wakati wa kumrejesha ni kulisha wana-kondoo. Petro alikuwa na uzoefu kidogo sana katika kazi hii. Ingehitaji uangalizi mkubwa na upole, uvumilivu na ustahimilivu mwingi. Ilimwita kuhudumu kwa wale waliokuwa wachanga katika imani, kufundisha wasiojua, kuwafungulia Maandiko, na kuwaelimisha kwa ajili ya kutumika katika huduma ya Kristo. Kabla ya wakati huu Petro alikuwa hajafaa kufanya kazi hii, au hata kuelewa umuhimu wake. Lakini hii ilikuwa ndiyo kazi ambayo Bwana alimwita kuifanya. Uzoefu wake wa mateso yale aliyopitia na toba ile aliyofanya vilikuwa vimemwandaa kwa kazi hii.

Kabla ya kuanguka kwake, Petro alikuwa mara kwa mara anaongea pasipo uangalifu, kutokana na hisia za mvuto wa wakati husika. Kila wakati alikuwa tayari kuwakosoa wengine, na kuonyesha mawazo yake, kabla ya kuwa na hali ya kujifahamu kwa uwazi au kuelewa kitu cha kusema. Lakini Petro aliyekuwa ameongoka alikuwa tofauti sana. Aliendelea kuwa na ari ile ile ya awali, lakini neema ya Kristo ilitawala ari hiyo. Hakuwa tena mtu wa ushupavu wa msisimko, wa kujiamini binafsi, na wa kujiinua, bali mtulivu, **(815)** mwenye kujitawala, na anayefundishika. Hapo alikuwa na uwezo wa kuwalisha wana-kondoo pamoja na kondoo wa kundi la Kristo.

Ile namna Mwokozi alivyoshughulika na Petro ilikuwa na fundisho kwa Petro na wale wenzake. Iliwafundisha namna ya kukutana na mkosaji kwa njia ya uvumilivu, huruma, na upendo wenye kusamehe. Ingawa Petro alikuwa amemkana Bwana wake, upendo ambao alipewa na Yesu usingemwangusha kamwe. Upendo huo ndio ambao mchungaji huyu wa kondoo wa kiwango cha chini alipaswa kuwa nao kwa ajili ya kondoo na wana-kondoo waliokabidhiwa chini ya uangalizi wake. Akikumbuka udhaifu wake na kushindwa kwake, Petro alikuwa ashughulike na kundi lake la kondoo kwa upole kama vile Kristo alivyokuwa ameshughulika naye.

Swali lile ambalo Kristo alikuwa amemwuliza Petro lilikuwa muhimu. Alitaja sharti moja tu la uanafunzi na huduma. Alisema, "Wanipenda?" Hii ndiyo sifa muhimu ya kustahilisha. Ingawa huenda Petro alikuwa na sifa nyinginezo zote, lakini bado bila kuwa na upendo wa Kristo asingeweza kuwa mchungaji wa kondoo mwaminifu achungaye kundi la Bwana. Kujua mambo, ukarimu, umahiri wa kunena, shukrani, na bidii vyote ni vitu vya kusaidia tu katika kazi njema; lakini pasipokuwa na upendo wa Yesu moyoni, kazi ya mtumishi wa Kikristo ni ya kushindwa.

Yesu alitembea peke yake pamoja na Petro, maana kulikuwa na jambo fulani alilotaka kumjulisha yeye peke yake. Kabla ya kifo chake, Yesu alikuwa amemwambia kwamba, "Niendako huwezi kunifuata sasa; lakini utanifuata baadaye." Petro alikuwa amelijibu hilo hivi, "Bwana, kwa nini mimi nisiweze kukufuata sasa? Mimi nitautoa uhai wangu kwa ajili yako." Yohana 13:36, 37. Aliposema haya, alijua kidogo sana kuhusu vimo na vina ambako miguu ya Yesu angeelekea katika kuongoza njia. Petro alikuwa ameanguka pindi jaribu lile lilipokuja, lakini alikuwa apate fursa tena ya kuthibitisha upendo wake kwa Kristo. Ili kumfanya atiwe nguvu kwa ajili ya jaribio la mwisho la imani yake, Mwokozi alimfunulia siku zake za usoni. Alimwambia kwamba baada ya kuishi maisha ya kutumika, wakati ambapo umri wake ulikuwa unasimulia kuhusu nguvu zake, angemfuata kweli Bwana wake. Yesu alisema, "Wakati ulipokuwa kijana, ulikuwa ukijifunga mwenyewe na kwenda utakako; lakini utakapokuwa mzee, utainyosha mikono yako, na mwingine atakufunga na kukuchukua usikotaka. Akasema neno hilo kwa kuonyesha ni kwa mauti gani atakayomtukuza Mungu."

Kwa njia hiyo Yesu alimfanya Petro ajue jinsi kifo chake kitakavyokuwa; alimwambia hata kuhusu kuinyosha mikono yake kwenye msalaba. Kwa mara nyingine tena alimsisitiza mwanafunzi yule akisema, "Nifuate." Petro hakuvunjika moyo kwa kufunuliwa hilo. Alihisi kuwa radhi kuteseka na kufa kwa ajili ya Bwana wake.

Kabla ya wakati huu Petro alikuwa amemfahamu Kristo kwa mwili, kama wengi wamjuavyo sasa; lakini sasa alikuwa asifungiwe katika hali hiyo tena. Hakumjua tena kama alivyokuwa amemjua kabla katika kujumuika naye katika ubinadamu. **(816)** Alikuwa amempenda kama mwanadamu, kama mwalimu aliyetumwa na mbingu; sasa alimpenda kama Mungu. Alikuwa amejifunza somo kwamba kwake Kristo alikuwa ni yote katika yote. Sasa alikuwa ameandaliwa kushiriki katika utume wa Bwana wa kujitoa kafara. Wakati alipoletwa msalabani hatimaye, alisulibishwa kichwa kikielekea chini kwa kuomba hivyo yeye mwenyewe. Alifikiria kwamba ni heshima kubwa iliyopitiliza kusulibishwa vile alivyosulibishwa Bwana wake.

Kwa Petro yale maneno kwamba "Nifuate" yalikuwa yamejawa na mafundisho. Somo hili halikutolewa kwa ajili ya kifo chake tu, bali pia kwa ajili ya kila hatua ya maisha yake. Muda wote kabla ya hapa Petro alikuwa amejengeka katika kutenda kwa kujitegemea. Alikuwa amejaribu kupanga mipango kwa ajili ya kazi ya Mungu, badala ya kusubiri kufuata mpango wa Mungu. Lakini hakufaidiwa chochote kwa kukimbia kutangulia mbele ya Bwana. Yesu anamsisitiza kwamba, "Nifuate." Usikimbie mbele yangu. Hapo hautaweza kukabiliana na majeshi ya Shetani ukiwa peke yako. Niache nitangulie mbele yako, nawe hutashindwa na adui.

Kadiri Petro alivyotembea pamoja na Yesu, aliona kwamba Yohana alikuwa anafuata. Hamu ya kutaka kujua hatima ya yule ya siku zijazo ilimjia, na "akamwambia Yesu, Bwana, na huyu je? Yesu akamwambia, Ikiwa nataka huyu akae hata nijapo, imekupasaje wewe? Wewe unifuate mimi." Petro alipaswa kuzingatia kwamba Bwana wake angemfunulia yote ambayo yalikuwa mema sana kwa ajili yake kujua. Ni jukumu la kila mmoja kumfuata Kristo, pasipokuwa na udadisi usio wa lazima wa kutaka kujua kazi iliyokabidhiwa kwa wengine. Katika kule kusema kuhusu Yohana kwamba, "Ikiwa nataka huyu akae hata nijapo," Yesu hakutoa hakikisho kwamba mwanafunzi huyu aishi mpaka wakati wa kuja kwa Bwana mara ya pili. Alichofanya tu ni kutangaza uweza wake wa hali ya juu, kwamba hata kama angependa iwe hivyo, isingeathiri kazi ya Petro kwa namna yoyote. Hatima ya wote wawili, Yohana na Petro, ilikuwa mikononi mwa Bwana. Utii katika kumfuata ulikuwa ndilo jukumu lililotakiwa kwa kila mmoja wao.

Ni wangapi ambao wako kama Petro leo! Wanakuwa na hamu ya kufuatilia mambo ya wengine, na wakiwa na hamu ya kutaka kujua majukumu ya wengine, huku wakiwa katika hatari ya kutelekeza yale ya kwao. Kazi yetu ni kumtazama Kristo na kumfuata. Tutaona makosa katika maisha ya wengine, na dosari katika tabia zao. Ubinadamu umezungukwa na kasoro. Lakini katika Kristo tutapata ukamilifu. Tukimtazama, tutabadilishwa.

Yohana aliishi na kuwa na uzee wa umri mkubwa. Alishuhudia maangamizi ya Yerusalemu, na uharibifu wa hekalu lile kuu, - ishara ya maangamizi ya mwisho ya ulimwengu. Akielekea katika siku zake za mwisho mwisho Yohana alimfuata Bwana wake kwa karibu zaidi. Mzigo wa ushuhuda wake kwa makanisa ulikuwa ni, "Wapenzi, na mpendane;" "naye akaaye katika pendo, hukaa ndani ya Mungu, na Mungu hukaa ndani yake." 1 Yohana 4:7, 16.

**(817)** Petro alikuwa amehifadhiwa kwa kazi yake ya utume, lakini heshima na mamlaka aliyopokea kwa Kristo haikuwa imempatia mamlaka ya ukuu juu ya ndugu zake. Yesu alilifanya jambo hili wazi wakati alipojibu swali la Petro kwamba, "Na huyu je?" Alikuwa amesema kwamba, "Imekupasaje wewe? Wewe nifuate mimi." Petro hakuheshimiwa kuwa mkuu wa kanisa. Upendeleo ambao Kristo alikuwa amemwonyesha katika kumsamehe uovu wake, na kumkabidhi kazi ya kulisha kundi, na uaminifu wa Petro mwenyewe katika kumfuata Kristo, ulimpatia ujasiri wa kuaminiwa na wenzake. Alikuwa na mvuto mkubwa kanisani. Lakini alilibeba katika maisha yake yote somo lile ambalo Kristo alikuwa amemfundisha pale kando ya Bahari ya Galilaya. Akiyaandikia makanisa kwa kuongozwa na Roho Mtakatifu, alisema:

"Nawasihi wazee walio kwenu, mimi niliye mzee, mwenzi wao, na shahidi wa mateso ya Kristo, na mshirika wa utukufu utakaofunuliwa baadaye; lichungeni kundi la Mungu lililo kwenu, na kulisimamia, si kwa kulazimishwa, bali kwa hiari kama Mungu atakavyo; si kwa kutaka fedha ya aibu, bali kwa moyo. Wala si kama wajifanyao mabwana juu ya mitaa yao, bali kwa kujifanya vielelezo kwa lile kundi. Na Mchungaji mkuu atakapodhihirishwa, mtaipokea taji ya utukufu, ile isiyokauka." 1 Petro 5:1-4.

## Sura ya 86

# Mkawafanye Mataifa Yote Kuwa Wanafunzi

[Sura hii imejengwa katika Mathayo 28:16-20.]

Akisimama hatua moja tu kutoka kwenye kiti chake cha enzi cha Mbinguni, Kristo aliwakabidhi wanafunzi wake kazi. Alisema, "Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi." "Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe." Marko 16:15. Maneno hayo yalirudiwa tena na tena, ili kwamba wanafunzi wapate kuelewa umuhimu wake. Nuru ya mbinguni ilitakiwa iangaze kwa uwazi, ikiwa na miale yenye nguvu, kwa wakazi wote wa dunia, wa tabaka la juu na la chini, matajiri na maskini. Wanafunzi hawa walikuwa wawe watenda-kazi pamoja na Mkombozi wao katika kazi ya kuuokoa ulimwengu.

Kazi hiyo ilikuwa imetolewa kwa wale kumi na wawili wakati Kristo alipokutana nao katika chumba cha ghorofani; lakini ilikuwa sasa itolewe kwa idadi kubwa zaidi. Katika mkutano ule wa mlimani kule Galilaya, waamini wote ambao waliwezekana kuitwa kuja pamoja walikuwa wamekusanyika. Kristo mwenyewe, kabla ya kufa kwake, alikuwa ameonyesha muda na mahali pa mkutano huu. Wale malaika mahali pa kaburi waliwakumbusha wanafunzi kuhusu ahadi yake ya kukutana nao Galilaya. Ahadi hiyo ilirudiwa kwa waamini waliokuwa wamekusanyika Yerusalemu mnamo wakati wa juma la Pasaka, na kupitia kwao iliwafikia watu wengi waliokuwa katika hali ya upweke wakiombolezea kifo cha Bwana wao. Kwa hamu kubwa watu wote walijielekeza katika mazungumzo hayo. Walishika njia kwenda mahali pa kukutania kwa kupitia njia ndefu za mzunguko, wakifika kutokea pande tofauti-tofauti, wakikwepa kuamsha hisia za wivu wa Wayahudi. Walikuja wakiwa na mioyo ya mshangao, wakizungumza pamoja habari zilizokuwa zimewafikia kumhusu Kristo.

Katika wakati uliomuliwa, kadiri ya watu mia tano walikuwa wamekusanywa kama kundi pale kando kando ya mlima, wakiwa na hamu ya kujifunza mambo yote ambayo yangewezekana kujifunzwa **(819)** kutoka kwa wale waliokuwa wamemwona Kristo tangu kufufuka kwake. Wanafunzi hao walipita wakiwa vikundi kwa vikundi, wakisimulia yote waliyokuwa wameona na kusikia kuhusu Yesu, na kutoa hoja kwa kutumia Maandiko kama alivyokuwa amefanya pamoja nao. Tomaso alieleza kisa cha kutokuamini kwake, na alisimulia jinsi mashaka yake yalivyokuwa yamefagililiwa mbali. Ghafla Yesu alisimama katikati yao. Hakuna yeyote aliyeweza kueleza kwamba alikuwa ametoka wapi na amekujaje. Wengi waliokuwa pale walikuwa hawajamwona kamwe; lakini waliona alama za kusulibishwa katika mikono na miguu yake; mwonekano wake ulikuwa kama uso wa Mungu, na walipomwona, walimsujudia.

Lakini baadhi walikuwa na mashaka. Hivyo ndivyo itakavyoendelea kuwa wakati wote. Wapo wale wanaoshindwa kuitendea kazi imani, na wanajiweka katika upande wa mashaka. Hawa wanapata hasara kubwa kwa sababu ya kutokuamini kwao.

Haya ndiyo mazungumzo pekee ambayo Yesu alifanya na waamini wengi baada ya kufufuka kwake. Alikuja na kuongea nao akisema, "Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani." Wanafunzi walikuwa wamemsujudia kabla hajaongea, lakini maneno yake, yaliyokuwa yakishuka kutoka katika midomo iliyokuwa imefungwa katika kifo, yaliwavuvia nguvu ya pekee. Sasa alikuwa Mwokozi aliyefufuka. Wengi wao walikuwa wamepata kumwona akionyesha uweza wake katika kuwaponya wagonjwa na kudhibiti nguvu za mashetani. Waliamini kwamba alikuwa na nguvu za kusimika ufalme wake Yerusalemu, nguvu za kusambaratisha upinzani wote, nguvu juu ya vitu vya asili. Alikuwa ametuliza maji yenye hasira; alikuwa ametembea kwenye uso mweupe wa maji; alikuwa amewafufua waliokufa wakaishi tena. Alitangaza kwamba alikuwa amepewa "mamlaka yote." Maneno yake yalichukua mawazo ya wasilizaji wake na kuyapandisha juu kutoka katika vitu vya kidunia na vya muda kwenda kwa vitu vya mbinguni vya kudumu. Waliinuliwa na kupata uelewa wa juu mno wa heshima na utukufu wake.

Maneno ya Kristo pale ubavuni mwa mlima yalikuwa ni tangazo kwamba kafara yake kwa niaba ya mwanadamu ilikuwa imejaa na kukamilika. Masharti ya upatanisho yalikuwa yametimizwa; kazi ile aliyojia ulimwenguni ilikuwa imekamilika. Alikuwa njiani kuelekea kwenye kiti cha enzi cha Mungu, kwenda kuheshimiwa na malaika, falme, na mamlaka. Alikuwa ameingia katika kazi ya uombezi. Akiwa amevikwa mamlaka isiyo na mpaka,

aliwapa wanafunzi kazi: "Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari." Mathayo 28:19, 20.

Waisraeli walikuwa wamefanywa kuwa watunzaji wa ukweli mtakatifu; lakini Ufarisayo ulikuwa umewafanya kuwa watu wa kujikweza, watu wa kujiona kuliko **(820)** wanadamu wote. Kila kitu kinachohusu makuhani na wakuu – mavazi yao, desturi, maadhimisho, mapokeo – viliwafanya kutokustahili kuwa nuru ya ulimwengu. Walijiangalia wenyewe, taifa la Kiyahudi, kama ndilo ulimwengu. Lakini Kristo aliwaagiza wanafunzi wake kuihubiri imani na ibada ambayo ndani yake isingekuwa na kitu cha tabaka rasmi la watu au nchi, imani ambayo ingetekelezeka miongoni mwa watu wote, mataifa yote, na matabaka yote ya watu.

Kabla ya kuwaacha wanafunzi wake, Kristo alitamka wazi wazi uhalisia wa ufalme wake. Alikumbusha akilini mwao kile alichokuwa amewaambia kuhusu ufalme huo. Alisema kwamba kusudi lake halikuwa kuanzisha ufalme katika dunia hii inayopita, bali ufalme wa kiroho. Hakuwa wa kutawala kama mfalme wa kidunia kwenye kiti cha enzi cha Daudi. Kwa mara nyingine tena aliwafunulia Maandiko, akionyesha kwamba yote aliyopita ndani yake yalikuwa yamepangwa mbinguni, katika mashauri kati ya Baba na Yeye. Yote yalikuwa yametabiriwa na watu waliovuviwa na Roho Mtakatifu. Alisema hivi, Mnaona kwamba yote niliyowafunulia kuhusu kukataliwa kwangu kama Masihi yametimia. Yote niliyosema kuhusu mateso ambayo yangenipata na kifo ambacho ningekufa, yamethibitika. Siku ya tatu nilifufuka. Fuatilieni Maandiko kwa dhati zaidi, nanyi mtaona kwamba katika mambo yote haya maelezo ya unabii kuhusu Mimi yametimizwa.

Kristo aliwapatia wanafunzi wake kufanya kazi aliyokuwa ameacha mikononi mwao, kuanzia Yerusalemu. Yerusalemu ulikuwa kitovu cha matendo yake ya ajabu ya kujidhili kwa ajili ya jamii ya wanadamu. Alikuwa ameteswa pale, kukataliwa na kuhukumiwa. Nchi ya Uyahudi ilikuwa ndiyo mahali pake pa kuzaliwa. Pale, akiwa amevaa ubinadamu, alikuwa ametembea pamoja na watu, na wachache walikuwa wameona jinsi mbingu ilivyokuwa imekuja karibu na dunia wakati Yesu alipokuwa pamoja nao. Lazima kazi ya wanafunzi ianzie Yerusalemu.

Katika mtazamo wa yale mateso yote yaliyokuwa yamempata Kristo, na kazi yake isiyotambuliwa ambayo alikuwa ameanzisha pale, wanafunzi wale wangependa wapangiwe eneo jingine la kazi linalotia matumaini; lakini hawakuomba ombi hilo. Mahali pale pale alipokuwa ametawanya mbengu za ukweli ndipo palitakiwa papaliliwe na wanafunzi, na mbengu ingechipuka na kuzaa mazao mengi. Katika kazi yao wanafunzi wale wangekutana na mateso kwa sababu ya wivu na chuki za Wayahudi; lakini Bwana wao alikuwa amestahimili hali hii, na wao wasingeikimbia. Lazima rehema ya kwanza itolewe kwa wale waliomwua Mwokozi.

Na mle Yerusalemu walikuwepo wengi waliokuwa wamemwamini Yesu kwa siri, na wengi ambao walikuwa wamedanganywa na makuhani na wakuu. Injili ilipaswa iwasilishwe kwa hawa pia. Wangeitwa ili **(821)** watubu. Ilikuwa ukweli wa ajabu uwekwe wazi kwamba kupitia Kristo ondoleo la dhambi lingeweza kupatikana. Wakati Yerusalemu yote ilikuwa imesisimshwa na matukio ya majuma machache yaliyokuwa yamepita, kuihubiri injili kungeleta mguso wa kina sana.

Lakini kazi isingekomea hapa. Ingepanuka hadi maeneo ya mbali ya dunia. Kristo aliwaambia wanafunzi wake kwamba, Mmekuwa mashahidi wa maisha yangu ya kujikana kwa niaba ya ulimwengu. Mmeshuhudia kazi zangu kwa ajili ya Israeli. Ingawa hawakuweza kuja kwangu ili kwamba wapate uzima, ingawa makuhani na wakuu wamenifanyia vile walivyoazimia, ingawa wamenikataa kama Maandiko yalivyotabiri, bado watakuwa na fursa nyingine ya kumkubali Mwana wa Mungu. Mmeona kwamba wote wajao kwangu, wakiungama dhambi zao, nawapokea bure. Yeye ajaye kwangu sitamtupa kamwe. Wote wanaotaka, wanaweza kupatanishwa na Mungu, na kuupokea uzima wa milele. Kwenu ninyi, wanafunzi wangu, nakabidhi ujumbe huu wa rehema. Unatakiwa utolewe kwa Israeli kwanza, na baada ya hapo kwa mataifa yote, lugha, na jamaa. Unatakiwa utolewe kwa Wayahudi na Mataifa. Wote waaminio na wakusanywe katika kanisa moja.

Kwa njia ya zawadi ya Roho Mtakatifu wanafunzi wale wangepata nguvu ya ajabu. Ushuhuda wao ungethibitishwa na ishara na maajabu. Miujiza ingetendwa, si tu na wanafunzi wale, bali pia na wale ambao wangepokea ujumbe wao. Yesu alisema, "Kwa jina langu watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya; watashika

nyoka; hata wakinywa kitu cha kufisha, hakitawadhuru kabisa; wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya." Marko 16:17, 18.

Mnamo wakati ule kulikuwa na vitendo vya kupeana sumu. Watu wasio wema hawakusita kutumia mbinu hii kuwaondosha wale walioonekana kuzuia maslahi yao. Yesu alijua kwamba maisha ya wanafunzi wake yangehatarishwa kwa namna hiyo. Wengi wangedhani kwamba wanamtumikia Mungu kwa kufanya vitendo vya kuwaua mashahidi hawa. Kwa hiyo aliwaahidi kuwalinda dhidi ya hatari hii.

Wanafunzi hawa walikuwa wawe na uweza ule ule ambao Yesu alikuwa nao wa kuponya "ugonjwa na udhaifu wa kila namna katika watu." Kwa kuponya magonjwa ya mwili katika jina lake, wangethibitisha nguvu zake kwa ajili ya kuponya moyo. Mathayo 4:23; 9:6. Na kipawa kipya kiliahidiwa kwao. Wanafunzi wale ilikuwa wahubiri miongoni mwa mataifa mengine, na wangepokea uwezo wa kuzungumza lugha nyingine. Mitume na wenzao walikuwa watu ambao hawana kisomo, lakini kwa njia ya kumwagwa kwa Roho Mtakatifu mnamo siku ya Pentekoste, hotuba yao, iwe katika lugha yao au lugha ya kigeni, ilikuwa safi, nyepesi, na sahihi, katika maeneo yote mawili, yaani, maneno na lafudhi.

**(822)** Hivyo ndivyo Kristo alivyowapatia wanafunzi wake kazi ya utume. Alitoa kwa ukamilifu mahitaji kwa ajili ya kutenda kazi hiyo, na alibeba mwenyewe wajibu kwa ajili ya mafanikio ya kazi hiyo. Kwa kadiri ambavyo wangetii neno lake, na kufanya kazi kwa kuunganika naye, wasingeshindwa. Enendeni kwa mataifa yote, aliwaambia. Enendeni sehemu za mbali zinazokaliwa na watu duniani, lakini mjue kwamba uwepo wangu uko kule. Fanyeni kazi kwa imani na ujasiri, maana hautakuja kamwe muda ambao nitawaacha.

Agizo la Mwokozi kwa wanafunzi wale liliwajumuisha waamini wote. Linahusisha wote wanaomwamini Kristo mpaka mwisho wa wakati. Ni kosa baya mno kudhani kwamba kazi ya kuokoa roho inategemea watumishi waliowekwa wakfu peke yao. Wote ambao wamejiwa na uvuvio wa mbinguni wanakabidhiwa kazi ya injili. Wote wanaopata uzima wa Kristo wamewekwa rasmi kufanya kazi kwa ajili ya wokovu wa wanadamu wenzao. Kazi ilianzishwa kwa ajili ya kazi hii, na wote wanaochukua viapo vitakatifu vya kazi hiyo wanaahidi hivyo kuwa watenda-kazi pamoja na Kristo.

"Roho na Bibi-arusi wasema, Njoo! Naye asikiaye na aseme, Njoo!" Ufunuo 22:17. Kila mmoja anayesikia anatakiwa kurudia mwaliko huo. Vyovyote wito wa mtu uwavyo maishani, hamu yake ya kwanza inapaswa kuwa ya kuongoa roho kwa Kristo. Anaweza akawa hana uwezo wa kunena mbele ya makutano, lakini anaweza akafanya kazi kwa mtu mmoja mmoja. Anaweza akawasiliana nao kuhusu mafundisho yaliyopokelewa kutoka kwa Bwana wake. Huduma ya neno la Mungu haiko katika kuhubiri peke yake. Wanaoitenda kazi ni pamoja na wale wanaosaidia kuponya wagonjwa na wenye shida, kusaidia wahitaji, kusema maneno ya faraja kwa waliopoteza tumaini na kwa wale wenye imani ndogo. Katika maeneo ya mbali na karibu zipo roho ambazo zimelemewa na hisia ya kuwa na hatia. Si ugumu wa maisha, masumbuko, au umaskini unaoshusha utu wa mwanadamu. Ni hatia, kutenda mabaya. Hali hii huleta kutokuwa na amani na kukosa kuridhika. Kristo anatamani kuona watumishi wake wakihudumia mioyo yenye magonjwa ya dhambi.

Wanafunzi walitakiwa waanzie kazi mahali walipokuwa. Eneo lililo gumu na lisilovutia halikupaswa kupitwa. Hivyo ndivyo kila mmoja wa watenda-kazi wa Kristo anavyotakiwa kuanzia mahali alipo. Katika familia zetu kwenyewe kunaweza kukawa na roho zenye hitaji la kuhurumiwa, zikiwa zina njaa ya mkate wa uzima. Kunaweza kukawa na watoto wanaotakiwa kufundishwa kumjua Kristo. Wapo wapagani ndani ya malango yetu. Hebu na tufanye kwa uaminifu kazi iliyo karibu yetu zaidi. Halafu ndipo jitihada zetu zipanuke hadi mbali kwa kiasi ambacho mkono wa Mungu unaweza kuongoza njia. Kazi ya watu wengi inaweza kuonekana kama inazingwa na mazingira fulani; lakini, popote ilipo, ikiwa inatendwa kwa imani na kwa dhati itaonekana katika sehemu muhimu za dunia. Kazi ya Kristo alipokuwa duniani ilionekana kujibana katika eneo dogo, lakini watu wengi kutoka katika nchi zote walisikia ujumbe wake. Mara nyingi Mungu hutumia mbinu nyepesi mno kutenda kazi inayoleta matokeo makubwa mno. Ni **(823)** mpango wake kwamba kila sehemu ya kazi yake itategemea kila sehemu nyingine, kama gurudumu ndani ya gurudumu, yote yakifanya kazi kwa kupatana. Mtenda kazi mwenye unyenyekevu mno, anayesukumwa na Roho Mtakatifu, atagusa nyuzi zisizoonekana, na sauti ya mtetemo wa nyuzi hizo italia mpaka miisho ya dunia, na kutoa sauti ya muziki kwa vizazi vyote.

Lakini agizo lile kwamba, "Enendni ulimwenguni kote," lisiangaliwe kwa makosa. Tunaitwa ili kuinua macho yetu kuona "nchi zilizo mbali." Kristo anavunjilia mbali ukuta utenganishao, fahari ya utaifa igawanyayo, naye hufundisha upendo kwa jamaa yote ya wanadamu. Anawainua watu kutoka katika duara finyu linalotawaliwa na ubinafsi wao; anapiga marufuku mistari yote ya mipaka ya nchi na tofauti za kubuni za jamii. Hafanyi tofauti kati ya majirani na wageni, marafiki na maadui. Anatufundisha kumwona kila mtu mwenye kuhitaji kama ndugu yetu, na ulimwengu kama eneo letu la kazi.

Wakati Mwokozi aliposema, "Enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi," alisema pia kwamba, "Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; kwa jina langu watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya; watashika nyoka; hata wakinywa kitu cha kufisha, hakitawadhuru kabisa; wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya." Ahadi hiyo inafika mbali kama lilivyo agizo hilo la utume. Si kwamba karama zote hizo zinatolewa kwa kila aaminiye. Roho hugawa "kwa kila mtu kama apendavyo." 1 Wakorintho 12:11. Lakini vipawa vya Roho vimeahidiwa kwa kila mtu kulingana na mahitaji yake kwa ajili ya kazi ya Bwana. Ahadi hiyo ni yenye nguvu na ya kuaminika sasa kama ilivyokuwa mnamo siku za mitume. "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Huu ni upendeleo kwa watoto wa Mungu, na imani inapaswa kuyashikilia yote yanayowezekana kupatikana kama uidhinishaji wa imani.

"Wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya." Ulimwengu huu ni jumba kubwa la wagonjwa, lakini Kristo alikuja kuponya wagonjwa, kutangaza kuokolewa kutoka katika utumwa wa Shetani. Alikuwa na afya na nguvu ndani yake mwenyewe. Aliweka uzima wake ndani ya wagonjwa, wenye shida, waliopagawa na mapepo. Hakumfukuza yeyote aliyekuja kupata nguvu yake ya kuponya. Alijua kwamba wale waliomwomba msaada walikuwa wamekuja na magonjwa; lakini hakukataa kuwaponya. Na pindi uweza wa Kristo ulipoingia ndani ya mioyo ya maskini hawa, walisadikishwa dhambi zao, na wengi waliponywa magonjwa yao ya kiroho, pamoja na maradhi ya mwili. Bado injili ina nguvu ile ile, na kwa nini sisi leo tusishuhudie matokeo kama yale?

Kristo anasikia maumivu ya kila mwenye shida aumiaye. Wakati roho wachafu wanapochana mwili wa mwanadamu, Kristo anahisi laana hiyo. Wakati homa inapokuwa ikiwaka katika mkondo wa maisha, Yeye anayasikia maumivu hayo. Na yuko tayari kuponya sasa kama wakati ule alipokuwa duniani katika mwili. Watumishi wa Kristo ndio **(824)** wawakilishi wake, mifereji ya kazi zake. Anatamani kuonyesha uweza wake wa kuponya kupitia hao.

Namna Mwokozi alivyoponya magonjwa mna fundisho kwa wanafunzi wake. Katika tukio moja alipaka macho ya mtu kipofu kwa matope, na akamwambia, "Nenda kanawe katika birika ya Siloamu, . . . Basi akaenda na kunawa; akarudi anaona." Yohana 9:7. Uponyaji ule ungefanywa tu kwa uweza wa Mponyaji Mkuu yule, lakini Kristo alitumia njia nyepesi ya asili. Wakati hakuonekana akitumia tiba ya vidoge, aliruhusu matumizi ya tiba za asili nyepesi.

Kwa wagonjwa wengi waliopokea uponyaji, Yesu alisema, "Usitende dhambi tena, lisije likakupata jambo lililo baya zaidi." Yohana 5:14. Hivyo alifundisha kwamba ugonjwa ni matokeo ya kukiuka sheria za Mungu, zote mbili, yaani, za asili na za kiroho. Maumivu makubwa duniani yasingekuwepo ikiwa watu wangedumu kuishi kulingana na mpango wa Mwumbaji.

Kristo alikuwa mwongozi na mwalimu wa Israeli ya kale, na aliwafundisha kwamba afya ni zawadi ya kutii sheria za Mungu. Tabibu Mkuu huyu aliyeponya wagonjwa kule Palestina alikuwa amenena na watu kutokea katika nguzo ya wingu, akiwaambia wanachopaswa kufanya, na kile ambacho Mungu angewafanyia. Alisema, "Kwamba utaisikiza kwa bidii sauti ya Bwana, Mungu wako, na kuyafanya yaliyoelekea mbele zake, na kutega masikio usikie maagizo yake, na kuzishika amri zake, mimi sitatia juu yako maradhi yoyote niliyowatia Wamisri; kwa kuwa Mimi ndimi Bwana nikuponyaye." Kutoka 15:26. Kristo aliwapatia Waisraeli maelekezo bayana kuhusu mwenendo wao wa maisha, na aliwahakikishia kwamba, "Bwana atakuondolea ugonjwa wote." Kumbukumbu 7:15. Walipotekeleza masharti hayo, ahadi hiyo ilithibitika kwao. "Katika kabila zao asiwepo mwenye kukwaa." Zaburi 105:37.

Mafundisho haya ni kwa ajili yetu. Kuna masharti ya kuzingatiwa na wote wanaotaka kuhifadhi afya. Lazima wote wajifunze masharti haya. Bwana hapendezwi na ujinga unaohusu sheria zake, ziwe za asili au za kiroho. Tunapaswa tuwe watenda-kazi pamoja na Mungu kwa ajili ya kurejesha afya ya mwili na ya roho.

Na tunapaswa tufundishe wengine namna ya kuhifadhi na kurejesha afya. Kwa wagonjwa tunapaswa kutumia tiba ambayo Mungu ametoa katika vitu vya asili, na tunapaswa tuwaelekeze kwake Yeye pekee awezaye kurejesha. Ni kazi yetu kuwapeleka wagonjwa na wenye mateso kwa Kristo katika mikono ya imani yetu. Tunapaswa tuwafundishe kumwamini Mponyaji Mkuu. Tunapaswa tushikilie ahadi zake, na kuomba udhihirisho wa nguvu zake. Kiini chenyewe cha injili ni urejeshaji, na Mwokozi anatutaka tuwafanye **(825)** wagonjwa, wasio na tumaini, na wenye shida washikilie nguvu zake.

Nguvu ya upendo ilikuwa katika kuponya kote kwa Kristo, na ni katika kushiriki upendo ule tu, kwa imani, ndipo tunapoweza kuwa nyezo za kazi yake. Ikiwa tunapuuza kujiunganisha na Kristo kwa mwunganiko wa kimbingu, mkondo wa nguvu iletayo uzima hauwezi kutiririka katika vijito vilivyojaa kutoka kwetu kwenda kwa watu. Kuna mahali ambapo hata Mwokozi hakuweza matendo mengi makuu kwa sababu ya kutokuamini kwao. Vivyo hivyo sasa kutokuamini kunalitenganisha kanisa na Msaidizi wake wa kimbingu. Lina udhaifu wa kushindwa kushikilia ukweli wa milele. Kwa kanisa kukosa imani, Mungu anafadhaishwa, na kupokonywa utukufu wake.

Ni katika kufanya kazi ya Kristo kwamba kanisa linakuwa na ahadi ya uwepo wa Kristo. Alisema, Enendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi; "na, tazama, mimi niko pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari." Kujitia nira yake ni moja kati ya masharti ya kwanza ya kupokea uwezo wake. Maisha yenyewe ya kanisa hutegemea uaminifu wake katika kutimiza agizo la Bwana la utume. Kupuuza kazi hii kwa hakika ni kukaribisha uharibifu na uozo wa kiroho. Mahali ambapo hakuna kazi ya moja kwa moja kwa watu wengine, upendo hupungua, na imani hufifia.

Kristo anapenda kwamba watumishi wake wawe waelimishaji wa kanisa katika kazi ya injili. Wanatakiwa wafundishe watu namna ya kutafuta na kuokoa wapotevu. Lakini, je, hii ndiyo kazi ambayo wako wanafanya? Naam, ni wangapi wanaohangaika kupuliza cheche za uhai katika kanisa lililo tayari kufa! Ni makanisa mangapi ambayo, kama wana-kondoo wagonjwa, yanatunzwa na wale ambao walipaswa kuwa wanatafuta kondoo waliopotea! Na wakati wote mamilioni kwa mamilioni wanaangamia bila Kristo.

Upendo wa Mungu umechochewa hadi katika vina visivyo na kipimo kwa ajili ya wanadamu, na malaika wanashangaa kuona shukrani za juu juu tu kwa watu wanaopokea upendo mkubwa kiasi hicho. Malaika wanaishangaa hali ya mwanadamu kuutambua kwa kina kidogo upendo wa Mungu. Mbingu inasimama kwa hasira pale wanadamu wanapopuuza upendo huo. Laiti tungejua jinsi Kristo anavyoichukulia hali hiyo? Baba na mama wangejisiaje, ikiwa wangejua kwamba mtoto wao, aliyepotelea katika baridi na theluji, amepitwa na wale ambao wangemwokoa, na kuachwa aangamie? Je! Wasingeudhika kwa kiwango cha kutisha, na kuchukizwa sana? Je! Wasingewalaumu hao wauaji kwa ghadhabu iliyochemka sawa na kiwango cha machozi yao, na kali kama upendo wao? Maumivu ya kila mwanadamu ni maumivu ya mtoto wa Mungu, na wale ambao hawanyoshi mkono wa msaada kwa wenzao wanaopotea wanahamasisha hasira yake ya haki. Hii ni hasira ya Mwana-kondoo. Mnamo siku kuu ya Hukumu, Kristo atawatangazia wale wanaodai kuwa pamoja na Kristo, lakini bado wamekuwa hawajali mahitaji ya wanadamu wenzao, "Nawaambia, Siwajui mtokako; ondokeni kwangu ninyi nyote mlio wafanyaji wa udhalimu." Luka 13:27.

**(826)** Katika agizo lile la utume kwa wanafunzi wake, Kristo si tu kwamba aliilezea kazi yao, bali pia aliwapatia ujumbe wao. Alisema, Mwafundishe watu "kuyashika yote niliyowaamuru ninyi." Wale wanafunzi walipaswa kufundisha kile ambacho Yesu alikuwa amefundisha. Kinajumuishwa kile alichokuwa amesema, si tu katika umbo lake Yeye mwenyewe, bali pia kupitia manabii na walimu wote wa Agano la Kale. Mafundisho ya mwanadamu yanafungiwa nje. Hakuna nafasi kwa mapokeo, kwa nadharia za mwanadamu na mahitimisho yake, au kwa sheria zilizotungwa na kanisa. Katika agizo lile la Yesu hakuna nafasi ya sheria zilizopitishwa na mamlaka za uongozi wa kanisa. Watumishi wa Kristo hawapaswi kufundisha lolote katika hayo. "Torati na manabii," pamoja na maandiko ya maneno na matendo yake mwenyewe, ni hazina iliyokabidhiwa kwa wanafunzi wale kwamba itolewe kwa ulimwengu. Jina la Kristo ndiyo kauli mbiu yao, ndiyo nembo ya utambulisho wao, ndicho kifungo cha mwunganiko wao, ndiyo mamlaka yao ya kufanya kazi hiyo, na ndicho chanzo cha mafanikio yao. Hakuna kitu ambacho hakina nembo hiyo kitakachotambuliwa katika ufalme wake.

Injili inatakiwa iwasilishwe, si kama nadharia isiyo hai, bali kama nguvu iliyo hai ya kubadilisha maisha. Mungu anatamani kwamba mtu anayepokea neema yake awe shuhuda wa uweza wake. Anawapokea bure wale ambao njia zao zimekuwa za kumchukiza mno; wanapotubu, anawajaza Roho wa kimbingu, kuwaweka katika nafasi ya

juu sana ya kuaminiwa, na kuwapeleka katika kambi ya wasio waaminifu ili wakauhubiri wema wake usio na mipaka. Anapenda watumishi wake wapeleke ushuhuda ya kwamba kupitia neema yake wanadamu wanaweza kuwa na kufanana na Kristo katika tabia, na wanaweza kufurahia katika uhakika wa upendo wake mkuu. Anapenda tupeleke ushuhuda kwamba hawezi kutosheka mpaka jamii ya wanadamu wamerejeshwa na kurudishiwa utakatifu wao kama wana na binti zake.

Ndani ya Kristo kuna upole wa mchungaji, hisia ya upendo ya mzazi, na neema isiyo na kifani ya Mwokozi mwema. Anaonyesha baraka zake kwa namna ya kuvutia. Hatosheki kwa kutangaza tu baraka hizi; anaziweka kwa namna ya kuvutia, ili kuhamasisha hamu ya kuwa nazo. Kwa hiyo watumishi wake wanapaswa kuwasilisha utajiri wa utukufu wa Zawadi isiyosemeka. Upendo wa ajabu wa Kristo utayeyusha na kutiisha mioyo, wakati ambapo mafundisho yale yale ya kurudiarudia hayatafanya jambo lolote. "Watulizeni mioyo, watulizeni mioyo, watu wangu, asema Mungu wenu." "Wewe uuhubiriye Sayuni habari njema, Panda juu ya mlima mrefu; Wewe uuhubiriye Yerusalemu habari njema, Paza sauti kwa nguvu; Paza sauti yako, usiogope; Iambie miji ya Yuda, Tazameni, Mungu wenu! . . . Atalilisha kundi lake kama mchungaji, Atawakusanya wana-kondoo mikononi mwake; Na kuwachukua kifuani mwake, Nao wanyonyeshao atawaongoza polepole." Isaya 40:1, 9-11. **(827)** Waambieni watu habari zake Yeye aliye "Mashuhuri miongoni mwa elfu kumi;" na Yeye ambaye "ndiye mzuri sana pia." Wimbo Ulio Bora 5:10, 16. Maneno pekee hayawezi kueleza hayo. Hebu na yaonekane katika tabia na kudhihirika katika maisha. Kristo amekaa ndani ya kila mwanafunzi ili kuonekana. Mungu ameshampangia kila mmoja ili wote "wafananishwe na mfano wa Mwana wake." Warumi 8:29. Ndani ya kila mmoja kunapaswa kuwa na hali ya kuudhihirishia ulimwengu upendo wa Kristo wa subira, na utakatifu, unyenyekevu, wema, na ukweli wake.

Wanafunzi wale wa kwanza walitoka kwenda kulihubiri neno. Walimdhihirisha Kristo katika maisha yao. Na Mungu alifanya kazi pamoja nao, "na kulithibitisha lile neno kwa ishara zilizofuatana nalo." Marko 16:20. Wanafunzi hawa walijiandaa kwa ajili ya kazi yao. Kabla ya siku ya Pentekoste walikutana pamoja, na kuondoa tofauti zao zote. Walikuwa na nia moja. Waliamini ahadi ya Kristo kwamba baraka ingetolewa, na waliomba kwa imani. Hawakuomba kupewa baraka hiyo kwa ajili yao wenyewe tu; walikuwa wamelemewa na mzigo kwa ajili ya wokovu wa roho. Injili ilikuwa ipelekwe mbali mipakani mwa dunia, na walidai kipawa cha nguvu iliyoahidiwa na Kristo. Halafu ilikuwa kwamba Roho Mtakatifu alimwagwa, na maelfu waliongoka katika siku moja.

Hivyo ndivyo ambavyo ingekuwa sasa. Badala ya mwanadamu kukisia kwa kubahatisha jambo la kuhubiri, hebu neno la Mungu ndilo lihubiriwe. Hebu Wakristo na waachane na upinzani, wajitoe kwa Mungu kwa ajili ya kuokoa waliopotea. Hebu kwa imani na waombe baraka ile, nayo itakuja. Kumwagwa kwa Roho mnamo siku za mitume kulikuwa ni "mvua ya vuli," na matokeo yake yalikuwa ya utukufu. Lakini "mvua ya masika" itakuwa nyingi zaidi. Yoeli 2:23.

Wote wanaotoa nafsi, mwili, na roho kwa Mungu watakuwa wanapokea wakati wote kipawa cha nguvu za mwili na akili. Utoaji wa mbingu usiokoma utakuwa kwao. Kristo anawapatia pumzi ya roho yake mwenyewe, uzima wa maisha yake mwenyewe. Roho Mtakatifu huweka nguvu zake kufanya kazi moyoni na akilini. Neema ya Mungu hupanuka na kuzidisha uwezo wao wa akili, na kila ukamilifu wa hali ya uungu huja kuwasaidia katika kazi ya kuokoa roho. Kupitia ushirikiano pamoja na Kristo wamekamilishwa ndani yao, na katika ubinadamu wao wanawezeshwa kufanya matendo ya Mwenyezi.

Mwokozi anatamani kudhihirisha neema yake na kutia chapa ya tabia yake katika ulimwengu wote. Ulimwengu ni mali yake aliyonunua, na anatamani kuwafanya wanadamu kuwa huru, na safi, na watakatifu. Ingawa Shetani anajitahidi kukwamisha kusudi hili, bado kupitia damu iliyomwagika kwa ajili ya ulimwengu kuna ushindi ambao utapatikana ambao utaleta utukufu kwa Mungu na Mwana-kondoo. Kristo hatatosheka mpaka ushindi umekamilika, na "ataona mazao ya taabu **(828)** ya nafsi yake, na kuridhika." Isaya 53:11. Mataifa yote ya dunia yatasikia injili ya neema yake. Si wote watakaopokea neema yake; lakini "wazao wake watamtumikia. Zitasimuliwa habari za Bwana, Kwa kizazi kitakachokuja." Zaburi 22:30. "Na ufalme, na mamlaka, na ukuu wa ufalme, chini ya mbingu zote, watapewa watu wa watakatifu wake Aliye juu," na "dunia itajawa na kumjua Bwana, kama vile maji yanavyoifunika bahari." "Basi, wataliogopa jina la Bwana toka magharibi, na utukufu wake toka maawio ya jua." Danieli 7:27; Isaya 11:9; 59:19.

"Jinsi ilivyo mizuri juu ya milima miguu yake aletaye habari njema, Yeye aitangazaye amani, Aletaye habari njema ya mambo mema, Yeye autangazaye wokovu, Auambiaye Sayuni, Mungu wako anamiliki! . . . Pigeni kelele za furaha, imbeni pamoja, Enyi mahali pa Yerusalemu palipokuwa ukiwa; Kwa kuwa Bwana amewafariji watu wake. . . . Bwana ameweka wazi mkono wake mtakatifu Machoni pa mataifa yote; Na ncha zote za dunia Zitauona wokovu wa Mungu wetu." Isaya 52:7-10.

## Sura ya 87

# "Kwa Baba Yangu, Naye Ni Baba Yenu"

[Sura hii imejengwa katika Luka 24:50-53; Matendo 1:9-12.]

Wakati ulikuwa umewadia wa Kristo kupaa kwenda kwenye kiti cha enzi cha Baba yake. Kama mshindi wa kimbingu alikuwa anataka kurudi katika viwanja vya mbinguni akiwa pamoja na nyara za ushindi. Kabla ya kifo chake alikuwa amemtangazia Baba yake kwamba, "nimeimaliza kazi ile uliyonipa niifanye." Yohana 17:4. Baada ya kufufuka kwake alikawia duniani kwa kipindi fulani, ili kwamba wanafunzi wamfahamu akiwa katika mwili wake uliofufuka na kutukuzwa. Sasa alikuwa tayari kwa ajili ya kuagana nao. Alikuwa amethibitisha uhalisia kwamba alikuwa Mwokozi aliye hai. Wanafunzi wake hawahitaji tena kumhusianisha na kaburi. Waliweza kumfikiria kama aliyetukuzwa mbele ya mbingu.

Yesu alichagua sehemu aliyopenda kwenda mara kwa mara wakati alipokuwa akikaa pamoja na wanadamu na alipafanya kuwa mahali pake pa kutokea wakati wa kupaa. Mahali palipoheshimiwa kwa ajili ya tukio hilo si Mlima Sayuni, mahali pa mji wa Daudi, wala si Mlima Moria, mahali penye hekalu. Pale ndipo Kristo alipokuwa amedhihakiwa na kukataliwa. Mahali pale ndipo ambapo mioyo ya watu ilikuwa imeyasukumia mbali na kuyarudisha nyuma kwa nguvu mawimbi ya rehema, ambayo bado yanarudirudi yakiwa na ongezeko kubwa la upendo. Tangu wakati huo, akiwa amechoka na kulemewa moyoni, Yesu alikuwa akitoka na kwenda kutafuta mahali pa kupumzikia kwenye huo Mlima wa Mizeituni. Ile Shekina takatifu, wakati ilipokuwa inaondoka katika hekalu lile la kwanza, ilisimama kwenye mlima wa mashariki, kama vile linasita kuachana na mji ule mteule; vivyo hivyo Kristo alisimama kwenye Mlima wa Mizeituni, akiuangalia Yerusalemu kwa moyo wenye huruma. Vichaka vya miti na vibonde vya **(830)** mlimani pale vilikuwa vimetakaswa kwa maombi na machozi yake. Mitelemko mikali ya mlima huo ilikuwa imetoa mwangwi wa sauti za shangwe za watu wengi waliokuwa wakimtangaza kuwa mfalme. Kwenye mtelemko wa mlima ndipo nyumbani mwa Lazaro, Bethania, alipopata hifadhi. Chini kabisa ya mlima huo ndipo palipokuwa na bustani ya Gethsemane mahali ambapo alikuwa ameomba na kupata masumbuko akiwa peke yake. Alikuwa apae kwenda mbinguni kutokea kwenye mlima huu. Wakati atakapokuja tena miguu yake itatua kwenye kilele cha mlima huu. Akiwa si kama mtu mwenye huzuni, bali kama mfalme mwenye utukufu na shangwe za ushindi. Atasimama kwenye Mlima wa Mizeituni, wakati ambapo haleluya za Kiebrania zitakuwa zikichanganyika na hosana za Mataifa, na sauti za waliokombolewa zikiwa kama za jeshi lenye nguvu zitapaa zikiimba kwamba, "Mvikeni taji Bwana wa wote!"

Sasa akiwa pamoja na wale wanafunzi wake kumi na mmoja Yesu alishika njia kwenda kwenye mlima huo. Walipopita katika lango la Yerusalemu, macho mengi ya watu wanaoshangaa yalikiangalia kile kikundi kidogo, kilichokuwa kinaongozwa na Yeye ambaye majuma machache tu yaliyokuwa yamepita alikuwa amehukumiwa na wakuu na kusulibishwa. Wale wanafunzi hawakujua kwamba hii ingekuwa mara yao ya mwisho kuzungumza na Bwana wao. Yesu alitumia muda ule katika kuzungumza nao, akirudia mafundisho yake ya kabla. Pindi walipokaribia Gethsemane, alisita akasimama, ili kwamba wapate kutafakari mafundisho aliyowapa wakati wa usiku ule wa mateso yake. Aliutazama tena mzabibu ule ambao wakati ule alikuwa ameufananisha na umoja uliopo kati ya kanisa lake na Yeye mwenyewe pamoja na Baba yake; akarudia tena ukweli ule aliokuwa ameufunua kabla. Pande zote zilizomzunguka kulikuwa na vitu vya kukumbusha upendo wake usiotafuta faida binafsi. Hata wanafunzi wale ambao walipendwa sana na moyo wake, wakati wa mateso yake, walikuwa wamempinga na kumwacha.

Kristo alikuwa ameishi katika hali ya ugenini ulimwenguni kwa miaka thelathini na mitatu; alikuwa amevumilia kejeli za ulimwengu, matusi, na dhihaka zake; alikuwa amekataliwa na kusulibishwa. Sasa, akiwa anataka kupaa kwenda kwenye kiti chake cha enzi chenye utukufu, – anapotafakari hali ya utovu wa shukrani ya watu aliokuja kuwaokoa, - hatawaondolea huruma yake na upendo wake? Je! Upendo wake hautaelekezwa katika eneo lile anapokubalika, mahali ambapo malaika wasio na dhambi wanamsubiri ili wafanye mapenzi yake? La! Ahadi yake kwa wapendwa wake wale anaowaacha duniani ni: "Nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari." Mathayo 28:20.

Walipofika kwenye Mlima wa Mizeituni, Yesu aliongoza njia na kukipita kilele cha mlima ule, mpaka maeneo yaliyo karibu na Bethania. Hapo alisimama kidogo, na wanafunzi wakakusanyika kwake. Miale ya nuru ilionekana kuangaza kutoka kwake kadiri alivyowatazama kwa upendo. Hakuwalaumu kwa sababu ya makosa yao na kushindwa kwao; maneno ya upendo wa kina yalikuwa ndiyo ya mwisho kusikika masikioni mwao yakitoka midomoni mwa Bwana wao. Kwa mikono iliyonyoshwa **(831)** kuwabariki, na kama vile ni namna ya kuwahakikishia utunzaji na ulinzi wake, aliinuliwa taratibu kutoka miongoni mwao, akivutwa kwenda mbinguni kwa nguvu kubwa zaidi kuliko kani yoyote ya mvutano ya duniani. Kadiri alivyoondoka kwenda juu, wale wanafunzi waliopigwa butwaa walitazama kwa macho yaliyokazwa ili kuona hatua ya mwisho ya Bwana wao anayepaa. Wingu la utukufu lilimficha kutoka katika upeo wa macho yao; na maneno yakarudi kwao yakiwa kama wingu lenye jeshi la malaika waliompokea yakisema, "Tazama, niko pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari." Wakati huo huo muziki mtamu na wa furaha kuu wa wimbo wa kwaya ya malaika ulielea angani ukiwashukia mahali walipo.

Wakati ambapo wanafunzi wale walikuwa bado wamekaza macho juu, sauti zilizosikika kama wimbo mtamu zilizungumza nao. Waligeuka, wakaona malaika wawili wakiwa katika mwonekano wa wanadamu, ambao walizungumza nao, wakisema, "Enyi watu wa Galilaya, mbona mmesimama mkitazama mbinguni? Huyu Yesu aliyechukuliwa kutoka **(832)** kwenu kwenda juu mbinguni, atakuja jinsi iyo hiyo mlivyomwona akienda zake mbinguni."

Malaika hawa walikuwa wa kundi lile lililokuwa linasubiri katika wingu ling'aalo ili kumsindikiza Yesu kwenda nyumbani kule mbinguni. Ni malaika walioinuliwa zaidi kuliko jeshi lote la malaika, na ni wale wawili waliokuwa wamekuja mahali pa kaburi wakati wa kufufuka kwa Kristo, na walikuwa pamoja naye katika maisha yake yote ya duniani. Kwa hamu kubwa mbingu yote ilikuwa imesubiri mwisho wa kukawia kwake ulimwenguni akiathiriwa na laana ya dhambi. Sasa wakati ulikuwa umefika wa wakazi wa mbinguni kumpokea mfalme wao. Je! Malaika wale wawili hawakutamani kuungana na kundi lile kubwa kumkaribisha Yesu mbinguni? Lakini kwa kuwahurumia na kuwapenda hawa ambao amewaacha, walisubiri kuwapatia faraja. "Je! Hao wote si roho watumikao, wakitumwa kuwahudumu wale watakaourithi wokovu?" Waebrania 1:14.

Kristo alikuwa amepaa mbinguni akiwa katika umbo la mwanadamu. Wanafunzi wale walikuwa wameliona wingu likimpokea. Yesu yule yule aliyekuwa ametembea na kuongea na kuomba pamoja nao; aliyekuwa ameumega mkate pamoja nao; aliyekuwa pamoja nao katika vyombo ziwani; na ambaye siku ile alikuwa amehangaika pamoja nao kuupanda Mlima wa Mizeituni, - Yesu yule yule sasa alikuwa ameenda kushiriki katika kiti cha enzi cha Baba yake. Na malaika wale walikuwa wamewahakikishia kwamba Yule Yule waliyekuwa wamemwona akipanda kwenda mbinguni, angekuja tena akiwa vile vile alivyopaa. Atakuja "na mawingu; na kila jicho litamwona." "Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu; nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza." "Hapo atakapokuja Mwana wa Adamu katika utukufu wake, na malaika watakatifu wote pamoja naye, ndipo atakapoketi katika kiti cha utukufu wake." Ufunuo 1:7; 1 Wathesalonike 4:16; Mathayo 25:31. Hivyo ndivyo itakavyotimizwa ahadi ya Bwana mwenyewe aliyoitoa kwa wanafunzi wake: "Basi nikienda na kuwaandalia mahali, nitakuja tena, niwakaribishe kwangu, ili nilipo mimi, nanyi mwepo." Yohana 14:3. Kwa hayo wanafunzi wangefurahia katika tumaini la kurudi kwa Bwana wao.

Wale wanafunzi waliporudi Yerusalemu, watu waliwatazama kwa mshangao. Baada ya mateso na kusulibiwa kwa Kristo, ilifikiriwa kwamba hawa wangeonekana wakiwa wameteteleka na kuaibika. Adui zao walitarajia kuona nyusoni mwao mwonekano wa huzuni na kushindwa. Badala ya mambo hayo waliona furaha na shangwe za ushindi. Nyuso zao zilikuwa zinametameta kwa furaha isiyo ya kidunia. Hawakuombolezea kufadhaishwa kwa matarajio yao, bali walikuwa wamejaa hali ya kumsifu na kumshukuru Mungu. Wakiwa na furaha walisimulia kisa cha ajabu cha kufufuka kwa Kristo na kupaa kwake kwenda mbinguni, na ushuhuda wao ulipokelewa na wengi.

**(833)** Wale wanafunzi hawakuwa tena watu wasio na matumaini ya siku za usoni. Walijua kwamba Yesu alikuwa mbinguni, na kwamba huruma zake zilikuwa bado pamoja nao. Walijua kwamba walikuwa na rafiki aliye kwenye kiti cha enzi cha Mungu, na walikuwa na hamu ya kumwomba Baba katika jina la Yesu. Kwa kicho cha dhati walipiga magoti na kuomba, wakirudia ahadi ile kwamba, "Mkimwomba Baba neno lolote atawapa kwa

jina langu. Hata sasa hamkuomba neno kwa jina langu; ombeni, nanyi mtapata; furaha yenu iwe timilifu." Yohana 16:23, 24. Waliunyosha mkono wa imani juu zaidi na zaidi, wakiwa na hoja yenye nguvu kwamba, "Kristo Yesu ndiye aliyekufa; naam, na zaidi ya hayo, amefufuka katika wafu, naye yuko mkono wa kuume wa Mungu; tena ndiye anayetuombea." Warumi 8:34. Na Pentekoste iliwaletea utimilifu wa furaha mbele ya uwepo wa Mfariji, kama Kristo alivyokuwa ameahidi.

Mbingu yote ilikuwa inasubiri kumkaribisha Mwokozi katika viwanja vya mbinguni juu. Pindi alipopaa, aliongoza njia, na mateka wengi waliokuwa wamewekwa huru wakati wa kufufuka kwake walifuata. Jeshi la mbinguni, wakiwa na shangwe na sifa na wimbo wa mbinguni, waliusindikiza msafara huo wa furaha.

Kadiri walivyokaribia mji wa Mungu, hamasa inachangizwa na wale malaika wanaosindikiza, wakiimba -

" Inueni vichwa vyenu, enyi malango,
Inukeni, enyi malango ya milele,
Mfalme wa utukufu apate kuingia."

Kwa furaha walinzi wa malango wanaitikia, wakisema, -

"Ni nani Mfalme wa utukufu?"

Wanasema hivi, si kwa sababu hawamjui ni nani, bali kwa kuwa wanapenda kusikia jibu linaloinua sifa kwamba, -

"Bwana mwenye nguvu, hodari, Bwana hodari wa vita.
Inueni vichwa vyenu, enyi malango,
Naam, viinueni, enyi malango ya milele,
Mfalme wa utukufu apate kuingia."

Kwa mara nyingine tena sauti ya kuchangiza inasema, "Ni nani Mfal,e wa utukufu?" maana malaika hawachoki kamwe kusikia jina lake likiinuliwa. Wale malaika wanaosindikiza wanajibu, -

"Bwana wa majeshi,
Yeye ndiye Mfalme wa utukufu." Zaburi 24:7-10.

Ndipo malango ya mji wa Mungu yanafunguliwa wazi, na msafara wa malaika unapita na kuingia kwa kwa shangwe za muziki wa furaha.

**(834)** Mle pana kiti cha enzi, nacho kinazungukwa na upinde wa mvua wa ahadi. Kuna makerubi na maserafi. Makamanda wa majeshi ya malaika, wana wa Mungu, wawakilishi wa malimwengu ambayo hayakukosea, wamekusanyika pamoja. Baraza lile la mbinguni ambalo mbele yake Lusifa alimshtaki Mungu na Mwana wake, wawakilishi wa malimwengu yale ambayo hayakuanguka ambako Shetaki alifikiria kuanzisha mamlaka yake, - wako pale wote ili kumkaribisha Mkombozi. Wana hamu ya kusherehekea ushindi wake na kumtukuza Mfalme wao.

Lakini Kristo anawapungia mkono wa kuwazuia. Wakati bado; kwa sasa hawezi kupokea taji ya utukufu na joho la kifalme. Anaingia mbele ya Baba yake. Anaonyesha kichwa chake kilichojeruhiwa, ubavu ule uliotobolewa, miguu ile iliyoharibiwa; anainua mikono yake, inayoonyesha alama za misumari. Anaonyesha kwenye zile alama za ushindi wake; anawasilisha kwa Mungu ule mganda wa kutikiswa; wale waliofufuliwa pamoja naye kama wawakilishi wa watu wengi watakaotoka makaburini wakati arudipo mara ya pili. Anamkaribia Baba, Yeye ambaye anakuwa na furaha kwa mwenye dhambi mmoja anayetubu; anayefurahi pamoja na mtu huyo kwa kuimba. Kabla ya kuwekwa misingi ya dunia, Baba na Mwana waliungana na kufanya agano la kumkomboa mwanadamu ikiwa atashindwa na Shetani. Walikuwa wameshikiliana mikono yao kwa ahadi ya dhati kwamba Kristo awe dhamana ya jamii ya wanadamu. Yesu ametimiza ahadi hii. Wakati alipolia akiwa msalabani kwamba, "Imekwisha," alikuwa anamwambia Baba. Uzito wa mzigo ulikuwa umebebwa kikamilifu. Sasa anatangaza: Baba, imekwisha. Nimefanya mapenzi yako, Ee Mungu wangu. Nimekamilisha kazi ya ukombozi. Ikiwa haki yako imetoshelezwa, "hao ulionipa nataka wawe pamoja nami popote nilipo." Yohana 19:30; 17:24.

Sauti ya Mungu inasikika ikitangaza kwamba haki imetoshelezwa. Shetani ameshindwa. Kwa maumivu ya Kristo, wale wanaohangaika duniani wameneemeshwa "katika huyo Mpendwa." Waefeso 1:6. Mbele ya malaika wa mbinguni na wale wawakilishi wa malimwengu ambayo hayakuanguka, hawa wanatangaziwa kuhesabiwa haki. Pale alipo Yeye, ndipo kanisa lake litakapokuwa. "Fadhili na kweli zimekutana, haki na amani zimehusiana." Zaburi 85:10. Mikono ya Baba inamkumbatia Mwana wake, na neno hili linasemwa, "Na wamsujudu malaika wote wa Mungu." Waebrania 1:6.

Kwa furaha isiyotamkika, watawala na falme na mamlaka vinakiri ukuu wa Mfalme wa uzima. Malaika wa jeshi la mbinguni wanaanguka kifudifudi mbele zake, huku shangwe za furaha zikivijaza viwanja vya mbinguni, "Astahili Mwana-Kondoo aliyechinjwa, kuupokea uweza na utajiri na hekima na nguvu na heshima na utukufu na baraka." Ufunuo 5:12. **(835)** Nyimbo za ushindi zinachanganyika na muziki unaotoka katika vinubi vya malaika, mpaka mbingu zinaonekana kufurikishwa na furaha na sifa. Upendo umeshinda. Kilichopotea kimepatikana. Mbingu inatoa sauti ya nyuzi laini ikisema, "Baraka na heshima na utukufu na uweza una yeye aketiye juu ya kiti cha enzi, na yeye Mwana-Kondoo, hata milele na milele." Ufunuo 5:13.

Kutoka katika tukio lile la furaha ya mbinguni, unarudi kwetu duniani mwangwi wa maneno ya ajabu ya Kristo kwamba, "Ninapaa kwenda kwa Baba yangu naye ni Baba yenu, kwa Mungu wangu naye ni Mungu wenu." Yohana 20:17. Jamaa ya mbinguni na jamaa ya duniani zimekuwa moja. Bwana wetu amepaa kwa ajili yetu, na kwa ajili yetu yu hai. "Naye, kwa sababu hii, aweza kuwaokoa kabisa wao wamjiao Mungu kwa yeye; maana yu hai sikuzote ili awaombee." Waebrania 7:25.